# FASIRI HURU YA BIBLIA

## ***U*NAWEZA KUIELEWA BIBLIA!**

***Injili kama ilivyoandikwa na Petro:***
***Marko na 1 & 2 Petro***

NA BOB UTLEY,
PROFESA MSTAAFU WA KANUNI ZA UFASIRI
(UTAFASILI WA BIBLIA)

MWONGOZO WA USOMAJI WA FASIRI MFUATANO
AGANO LA KALE, VOL.02

BIBLE LESSONS INTERNATIONAL, MARSHAL, TEXAS
2012

# ORODHA YA YALIYOMO

Neno Toka kwa Mwandishi:Ni kwa namna gani fasiri hii inaweza kukusaidia! ..... i

Mwongozo Mzuri wa Usomaji wa Biblia: Utafiti Binafsi kwa Ukweli Uliothibitika ..... iii

Fasiri

Mtu aitwaye Petro ..... 01

Utangulizi wa Marko ..... 03

Marko 1 ..... 08

Marko 2 ..... 39

Marko 3 ..... 52

Marko 4 ..... 70

Marko 5 ..... 84

Marko 6 ..... 93

Marko 7 ..... 104

Marko 8 ..... 116

Marko 9 ..... 128

Marko 10 ..... 142

Marko 11 ..... 168

Marko 12 ..... 180

Marko 13 ..... 203

Marko 14 ..... 229

Marko 15 ..... 255

Marko 16 ..... 272

Utangulizi kwa 1 Petro 1 ..... 278

1 Petro 1 ..... 283

1 Petro 2 ..... 305

1 Petro 3 ..... 320

1 Petro 4 ..... 338

1 Petro 5 ..... 350

Utangulizi wa 2 Petro ..... 360

2 Petro 1 ..... 364

2 Petro 2 ..... 384

2 Petro 3 ..... 400

Viambatisho

Maelezo mafupi ya muundo wa Visarufi vya Kiyunani .......... 413
Uhakiki wa Tofauti za Kiuandishi .......... 422
Kauli ya Mafundisho .......... 426

# MADA MAALUM: ORODHA YA YALIYOMO

Arche, 1:1 ..... 09
Toba katika Agano la Kale, 1:4 ..... 13
Ukiri, 1:5 ..... 14
Uasilishaji, 1:10 ..... 17
Ujuzi wa Pekee, 1:10 ..... 18
Utatu, 1:11 ..... 18
Uwakilishi wa Namba katika Maandiko, 1:13 ..... 20
Maneno ya Kiyunani kwa ajili ya Majaribu na vidokezo vyake, 1:13 ..... 21
Shetani, 1:13 ..... 22
Familia ya Herode Mkuu, 1:14 ..... 24
Ufalme wa Mungu, 1:15 ..... 26
Imani, 1:15 ..... 27
Sabato, 1:21 ..... 29
Waandishi, 1:22 ..... 30
Mapepo (pepo wachafu), 1:23 ..... 31
Aliye Mtakatifu, 1:24 ..... 33
Upungaji Pepo, 1:25 ..... 34
Moyo, 1:26 ..... 42
Mafarisayo, 2:16 ..... 46
Kufunga, 2:18 ..... 48
Maherodi, 3:6 ..... 54
Uharibifu (Apollumi), 3:6 ..... 55
Mwana wa Mungu, 3:11 ..... 56
Namba Kumi na Mbili, 3:14 ..... 59
Jedwali la Majina ya Mitume, 3:16 ..... 60
Ameni, 3:28 ..... 65
Utu wa Roho, 3:29 ..... 66
Milele, 3:29 ..... 67
Utaratibu wa Ufafanuzi wa kimaandiko kwa dhambi zisizosameheka, 3:29 ..... 68
Utafsiri wa mifano, 4 ..... 72
Siri katika Injili,4:11 ..... 76
Hitaji la Ustahimiivu, 4:17 ..... 78

Wokovu (Njeo za Kitenzi cha Kiyunani), 4:17 .......... 80
Kutiwa Mafuta katika Biblia, 6:13 .......... 97
Wanafiki, 7:6 .......... 107
Lugha ya kibinadamu, 7:20 .......... 110
Kuwekewa Mikono, 7:13 .......... 114
Ufufuo, 8:31 .......... 123
Kupelekwa (Apostello), 9:37 .......... 137
Wafu wako wapi, 9:43 .......... 139
Ktisis, 10:6 .......... 146
Amri Kumi, 10:19 .......... 150
Wingi wa Mali, 10:23 .......... 153
Utukufu, 10:37 .......... 159
Fidia/Ukombozi, 10: 45 .......... 162
Yesu Mnazareti, 10:47 .......... 165
Milele, 11:14 .......... 172
Maombi ya Kusihi, 11:23 .......... 176
Jiwe kuu la Pembeni, 12:10 .......... 183
Baraza Kuu la Wazee wa Sinagogi, 12:13 .......... 185
Masadukayo, 12:18 .......... 188
Uandishi wa Torati Ya Mussa, 12:26 .......... 190
Majina ya Uungu, 12:35 .......... 195
Viwango vya Thawabu na Adhabu, 12:40 .......... 199
Sarafu zitumikazo katika Palestina Nyakati za Yesu, 12:42 .......... 200
Utabiri wa Agano la Kale Juu ya Nyakati zijazo dhidi ya Utabiri wa Agano Jipya, 13 .......... 205
Fasihi ya Matukio ya Siku za Mwisho, 13 .......... 210
Majibu ya Maswali Mawili ya Wanafunzi ya Mathayo, 13:4 .......... 212
Enzi Hizi na Enzi Zijazo, 13:8 .......... 214
Chukizo la Uharibifu, 13:14 .......... 216
Uchaguzi/Kuamriwa na Hitaji la uwiano wa kithiolojia, 13:20 .......... 218
Maombi ya Kusihi, 13:20 .......... 219
Miezi Arobaini na miwili, 13:20 .......... 221
Ujio wa Mawinguni, 13:26 .......... 223
Uwakilishi wa Namba katika Maandiko, 13:26 .......... 223
Baba, 13:32 .......... 226

Msaada kwa Wahitaji, 14:5 ........ 233
Pasaka, 14:22 ........ 238
Karamu ya Bwana katika Yohana, 14:22 ........ 240
Agano, 14:24 ........ 241
Kumiminwa, 14:24 ........ 242
Saa, 14:35 ........ 245
Laana, 14:71 ........ 253
Pontio Pilato, 15:1 ........ 257
Wanawake katika Biblia, 15:40 ........ 267
Wanawake waliomfuata Yesu, 16:1 ........ 273
Manukato ya Maziko, 16:1 ........ 274
Uchaguzi/ Kuamriwa kwanza na hitaji la uwiano wa Kithiolojia, 1:2 ........ 285
Urithi wa Waamini, 1:4 ........ 288
Wokovu, 1:5 ........ 289
Yesu na Roho, 1:11 ........ 293
Mafundisho ya kanisa la kwanza, 1:11 ........ 294
Maoni ya Paulo juu ya Sheria ya Musa, 1:12 ........ 295
Utakatifu wa Agano Jipya, 1:15 ........ 297
Takatifu, 1:16 ........ 298
Adilisha, 2:5 ........ 307
Ukristo ni Ushirika, 2:5 ........ 307
Unyenyekevu, 2:13 ........ 312
Serikali ya Kibinadamu, 2:13 ........ 313
Mapenzi ya Mungu, 2:15 ........ 314
Maonyo ya Paulo kwa Watumwa, ........ 316
Haki, 3:14 ........ 326
Tumaini, 3:15 ........ 329
Wafu wako wapi?, 3:18 ........ 332
Ujuzi wa kipekee, 3:22 ........ 335
Uovu na Wema katika Agano Jipya, 4:3 ........ 340
Mtazamo wa Kibiblia juu ya Pombe na unywaji wa Pombe, 4:3 ........ 340
Kwanini Wakristo wanateseka, 4:12 ........ 347
Koinonia, 4:13 ........ 347
Uovu binafsi, 5:8 ........ 354

Ustahimilivu, 5:8 ..... 355
Silasi/Silvano, 5:8 ..... 358
Ukuaji wa Mkristo, 1:5 ..... 370
Dhamana, 1:10 ..... 372
Waitwao, 1:10 ..... 374
Utume, 1:10 ..... 375
Ukweli katika Maandiko ya Yohana, 1:12 ..... 377
Kweli katika Maandiko ya Yohana, ..... 378
Kuja Mara ya Pili, 1:16 ..... 380
Wana Mungu katika Mwanzo, 2 ..... 389
Kuaharibu, Kuangamiza, Kuchafuka, 2:12 ..... 396
Moto, 3:7 ..... 403
Mpango wa Ukombozi wa YHWH, 3:7 ..... 406

# NENO TOKA KWA MWANDISHI
# NI KWA NAMNA GANI FASIRI HII ITAKUSAIDIA?

Kutafasiri Biblia ni uwiano wa wastani na wa kiroho ambao unajaribu kumwelewa mwandishi wa kale aliyevuviwa kuandika ili kuwezesha ujumbe wa Mungu uweze kueleweka na kutumiwa katika zama hizi.

Mchakato wa kiroho ni muhimu sana lakini mugumu sana kuelezea. Unahusisha kujitoa na kuwa wazi kwa Mungu. Lazima pawepo na njaa (1) kwa ajili yake (2) ya kumjua yeye na (3) kumtumkia yeye. Mchakato huu unahusisha maombi, ukiri na kuwa tayari kubadili mfumo wa kuishi. Roho Mtakatifu ni wa muhimu sana katika mchakato wa utafasiri, lakini kwa nini wakristo waaminifu, wanaompenda Mungu wanaielewa Biblia tofauti kabisa na kuitafasiri visivyo.

Mchakato wa uwiano huu ni rahisi kuuelezea. Lazima tuwe na msimamo na haki kwa maandiko badala ya kuathiriwa na hali ya upendeleo binafsi au wa ki-madhehebu. Sote tumefungamanishwa ki-historia. Hakuna yeyote mtafasiri miongoni mwetu awezae kubisha. Fahiri hii inatoa kwa uangalifu uwiano ulio sahihi wenye kanuni tatu za tafasiri zilizoundwa kusaidia kudhibiti hali zetu za upendeleo.

## KANUNI YA KWANZA

Kanuni ya kwanza ni kuona muundo wa kihistoria ambao kwayo Biblia iliandikwa na tukio zima la kihistoria katika uandishi wake. Mwandishi wa mwanzo alikuwa na kusudi, ujumbe wa kuwakilisha. Andiko haliwezi kumaanisha kitu kwetu ambacho hakikumaanishwa na ile asili, na mwandishi aliyevuviwa wa zama hizo. Kusudi lake na wala sio mahitaji yetu ki-historia, ki-musisimko, ki-tamaduni na mapokeo ya ki-madhehebu yetu ni— ufunguo.

Matumizi ni mbia mkubwa wa tafasiri, lakini tafasiri sahihi lazima ipate kipaumbele kwa matumizi. Lazima isisitizwe kwamba, kila andiko la Biblia lina tafasiri moja tu, na si vinginevyo. Maana hii ndiyo mwandishi wa mwanzo wa Biblia alivyokusudia akiongozwa na roho kuiwasilisha katika enzi zake. Maana hii moja yaweza kuwa na matumizi anwai, katika tamaduni na mazingira tofauti. Matumizi haya lazima yaambatane na ukweli halisi wa mwandishi wa awali. Kwa sababu hii, mwongozo wa fasiri hii imetayalishwa kwa namna ya kutoa utangulizi kwa kila kitabu cha Biblia.

## KANUNI YA PILI

Kanuni ya pili ni kuibainisha fasihi moja. Kila kitabu cha Biblia ni hati ya kumbukumbu iliyounganishwa. Wafasiri hawana haki ya kutenganisha hoja moja ya ukweli kwa nyingine. Kwa hiyo hatuna budi kujaribu kuelewa kusudi la kitabu kizima cha Biblia kabla ya kutafasiri fasihi ya kitabu kimoja kimoja. Sehemu moja—sura, aya, au mistari haiwezi kumaanisha ambacho kitabu kizima hakimaanishi. Tafsiri sharti iwiane na mtizamo mzima kuelekea mtimzamo wa sehemu ya vifungu vya Biblia. Kwa hiyo mwongozo huu wa fasiri ya mafunzo haya umelenga kuwasaidia wanafunzi kuchambua muundo wa kila andiko ki-aya. Mgawanyo wa ibara na sura havikuvuviwa bali ni kutusaidia tu ili kubaini mawazo.

Kutafasiri katika ngazi ya aya na sio sentesi, ibara,kifungu au ngazi ya neno ndio ufunguo katika kufuata maana ya mwandishi aliyokusudia. Aya zimejengwa kwenye mada iliyounganishwa pamoja, mara nyingi huitwa sentesi yenye dhamira au mada. Kila neno, kifungu, ibara na sentesi katika aya kwa kiasi fulani vinahusiana na dhamira iliyo pamoja. Aidha haya huweka ukomo, inapanua , kuieleza na/ au kuihoji. Maelekezo sahihi (ufunguo) kwa tafsiri sahihi ni kufuata wazo la mwandishi wa awali aya kwa aya kufuatana na fasihi binafsi ambayo inatengeneza Biblia nzima..Tafsiri hizi zimechaguliwa kwa sababu zinatumia nadharia mbalimbali za tafsiri.

1. Andiko la Kiyunani la United Bible Society ni rekebisho la chapisho la Nne la (UBS$^4$). Andiko hili liliandikwa ki-aya na wasomi wa maandiko ya kisasa.

2. Toleo la New King James Version (NKJV) ni utafsiri wa fasihi wa neno kwa neno uliosimamia kwenye mapokeo ya machapisho ya Kiyunani yaliyojulikana kama "Upokeaji wa Maandishi". Mgawanyo wa aya zake ni mrefu kuliko tafasiri zinginezo. Urefu wa aya hizi unamwezesha wasomi kuona mada zilizo pamoja.
3. Toleo la New Revised English Version(NRSV) ni tafsiri ya neno kwa neno lililoboreshwa. Inatengeneza pointi ya kati baina ya matoleo mawili ya kisasa yanayofuata. Mgawanyo wa aya zake ni wa msaada mkubwa katika kubainisha masomo.
4. Toleo Today's English Version(TEV) ni utafsiri sawia wenye nguvu uliyochapishwa na muungano wa vyama vya Biblia. Unajaribu kutafasiri Biblia kwa njia ya kumwezesha msomaji au mnenaji wa kiingereza cha kisasa kuelewa maana iliyomo katika andiko la Kigiriki. Mara nyingi, hasa hasa katika injili, inagawanya aya kufuatana na mnenaji hata kuliko somo lenyewe, sawa na NIV. Kwa kusudi la mtafasiri, hili halina msaada. Inapendeza kuona kuwa vitabu vya UBS[4] na TEV vimechapishwa na mtu yule yule lakini aya zake zinatofautiana.
5. The Jerusalem Bible(JB) ni tafsiri sawia yenye mlinganyo wa nguvu iliyosimamia kwenye tafasiri ya Katoliki ya Ufaransa. Ni nzuri mno katika kufanya ulinganifu wa aya kutoka katika mtizamo wa ki-Ulaya.
6. Chapisho la andiko ni uboreshaji wa mwaka 1995 wa toleo la Biblia New American Standard Bible (NASB) ambalo ni tafasili ya neno kwa neno. Pia maoni ya mstari kwa mstari yanafuata aya hizi.

## KANUNI YA TATU

Kanuni ya tatu ni kusoma Biblia tofauti tofauti ili kupata uwezekano mpana wa maana (somo la maana ya maneno) kwamba maneno ya Kibiblia au vifungu yanaweza kuwa nayo. Daima, neno au fungu la maneno katika Kiyunani yanaweza kueleweka kwa njia mbalimbali. Tafsiri hizi tofauti husaidia kubaini na kuelezea utofauti uliopo katika maandiko ya awali ya Kiyunani. Lakini haya hayaathiri mafundisho, bali husaidia katika kujaribu kurejelea maandiko asili yaliyoandikwa na mwandishi wa kwanza aliyevuviwa.

Fasiri hii humpa mwanafunzi njia ya haraka ya kuchunguza fasiri zake. Hii haina maana kuwa ni ya kumalizia, bali ni ya utoaji taarifa na udadisi kimawazo. Mara nyingi tafsiri nyingine hutusaidia tusiwe ving'ang'anizi na wafinyu wa mawazo na mapokeo ya kimadhehebu. Watafasili wanapaswa kuwa na upana mkubwa wa kuelewa tafsiri tofauti tofauti na kuweza kubaini ni kwa ugumu upi maandiko ya kale yanaweza kuwa. Inashangaza kuona ni kwa kiasi kidogo kilioje cha makubaliano yaliopo kati ya Wakristo ambao wanadai kuamini biblia kama chanzo chao pekee cha ukweli. Kanuni hizi zimenisaidia kushinda hali yangu ya kufungwa kihistoria na kunifanya nipambane na maandiko ya zama hizo. Ni matumaini yangu kuwa kanuni hizi zitakuwa za Baraka kwako.

Bob Utley
Juni 27, 1996
Haki Miliki © 2013 Bible Lessons International

# MWONGOZO KWA USOMAJI MZURI WA BIBLIA:

# UTAFITI BINAFSI KWA UKWELI ULIOTHIBITIKA

Kinachofuata ni maelezo mafupi ya Dr. Bob Utley mwana falsafa wa kanuni za ufasili na njia alizotumia katika fasihi yake.

Tunaweza kuufahamu ukweli? Unapatikana wapi? Tunaweza kuuthibitisha kimantiki? Kweli, kuna mamlaka ya kimsingi? Kuna imani kamili inayoweza kulinda maisha yetu, na ulimwengu wetu tuliomo? Kuna maana yeyote katika maisha? Kwa nini tuko hapa? Tunakwenda wapi? Maswali haya yanauliza kwa watu wote wenye tafakuri zenye uwiano—wameyatawala maarifa ya binadamu tangu mwanzoni mwa nyakati (Mhu. 1:13-18; 3:9-11). Naweza kukumbuka utafiti wangu binafsi kwa ajili ya ungamanisho la maisha yangu. Nimekuwa mwamini katika Kristo kwenye umri mdogo, awali kabisa nikizingatia juu ya ushahidi wa watu wengine muhimu kwenye familia yangu. Nilivyokuwa kufikia utu uzima, maswali juu yangu na ulimwengu ninamoishi ulivyokuwa.Tamaduni za kawaida na dini hazikuleta maana yeyote kwenye uzoefu niliousoma au kukutana nao. Ulikuwa ni muda wa kuchanganyikiwa, kutafuta, kutamani, na mara nyingi fikra zisizokuwa na tumaini katika uso wa ulimwengu mgumu, usiojali nilimoishi.

Wengi walidai kuwa na majibu kwa maswali haya ya msingi, lakini baada ya utafiti na kufikiri nikapata majibu yao yamelenga juu ya (1) falsafa binafsi, (2) hadithi za kubuniwa za kale, (3) uzoefu binafsi, au (4) Saikolojia zilizojichomoza. Nilihitaji digrii fulani ya uthibitisho, baadhi ya vielelezo, kiasi cha busara ambamo ningelenga mtazamo wangu wa kidunia, kiini cha uzima wangu, sababu yangu ya kuishi.
Niliyapata haya katika usomaji wangu wa biblia. Nilianza kutafuta ushahidi wa udhamini nilioupata katika (1) utegemezi wa historia ya biblia kama ulivyothibitishwa na elimu kale, (2) usahihi wa Nabii za Agano la Kale, (3) umoja wa jumbe za Biblia zaidi ya miaka 1600 ya kutolewa kwake na (4) shuhuda binafsi za watu ambao maisha yao yalibadilika moja kwa moja baada ya kusoma biblia. Ukristo, kama mfumo wa imani na kuamini uliounganishwa, una uweo wa kukabiliana na maswali magumu ya maisha ya mwanadamu. Siyo haya tu yanaweza kutoa muundo kazi, lakini mwelekeo unaotokana na uzoefu wa imani za kibiblia uliniletea furaha zenye hisia na ustahimili.

Nilijiridhisha ya kuwa nimepata kiini cha uzima wa maisha yangu—Kristo, kama ninavyoelewa kupitia maandiko.Ulikuwa ni uzoefu mgumu, msukumo wenye kuweka huru. Ingawa, naweza kukumbuka mshituko na maumivu yalipoanza kunifahamisha juu ya tafasiri ngapi tofauti ya kitabu hiki zimetetewa, wakati mwingine hata ndani ya makanisa hayo ya aina moja. Nikithibitisha mwongozo wa Ki-Mungu na uaminifu wa biblia haukuwa mwisho, lakini ni mwanzo pekee. Ni kwa vipi naweza kuthibitisha au kukataa tafsiri zinazotofautiana na kugongana za kurasa nyingi ngumu ndani ya maandiko kwa wale waliokuwa wakidai mamlaka yake na uaminifu?
Kazi hii imekuwa lengo la maisha yangu na hija ya imani. Nilifahamu ya kuwa imani katika Kristo imeniletea furaha na amani kubwa. Mawazo yangu yametamani baadhi ya imani kamili katikati ya nadharia ya utamaduni wangu na mfumo wa imani gonganishi wa dini na majivuno ya kimadhehebu. Katika utafiti wangu wa mitazamo halali kwenye utafsiri wa fasihi ya kale, nilishangaa kuvumbua historia yangu, ya kitamaduni, ya kimadhehebu na uzoefu wa kipendeleo. Kwa kawaida kabisa, mara nyingi, nimesoma Biblia ili kuimarisha mtizamo wangu. Nimeutumia kama chanzo cha mfumo wa imani kuvamia imani nyingine wakati nikijihakikishia usalama wangu na utoshelevu. Ni kwa namna gani utambuzi wa maumivu haya yalikuwa kwangu!

Ingawa siwezi kuwa kipingamizi moja kwa moja, naweza kuwa msomaji mzuri wa biblia. Naweza kuweka ukomo wa upendeleo kwa kutambua na kukubali uwepo wao. Sijawaweka huru,lakini nimeukabiri udhaifu wangu. Mtafsiri mara nyingi ndio adui mbaya wa usomaji mzuri wa biblia! Ngoja

nitaje baadhi ya dhanio nilizoleta kwenye usomaji wa biblia ili, msomaji, aweze kuzichunguza pamoja nami:

## DHANIO


1. Ninaamini biblia ni uvuvio wa ki-pekee wa ufunuo binafsi wa Mungu mmoja na aliye wa kweli. Kwa hiyo, ni lazima itafsiriwe katika mwanga wa kusudi la Ki-Ungu la mwandishi wa mwanzo (yaani Roho) kupitia mwandishi wa kibinadamu katika muundo wa historia uliokusudiwa.
   - Wapokeaji wa mwanzo
   - Ujumbe ulioandikwa
   - Kusudi la mwandishi wa mwanzo
2. Ninaamini biblia iliandikwa kwa ajili ya mtu wa kawaida—kwa watu wote! Mungu alilazimika mwenyewe kuongea kwetu waziwazi kupitia historia na tamaduni zilizomo. Mungu hakuuficha ukweli, anatutaka sisi kuelewa! Kwa hiyo, inalazimika kutafsiriwa katika (uwazi) katika siku hizo, na siku hizi tulizomo. Biblia haitakiwi kumaanisha kwetu yale ambayo hayakumaanisha kwa wale wa mwanzo walioisoma au kuisikia. Inaeleweka kwa wastani wa mawazo ya kibinadamu na kutumia aina ya njeo mbadala za kawaida za mawasiliano ya ki-binadamu.
3. Ninaamini Biblia inakusudi na ujumbe uliowekwa pamoja. Haina mkanganyiko ndani yake, ingawa inajumuisha (njia ngumu na zinazokinzana). Hivyo basi, mtafsiri mzuri wa biblia ni biblia yenyewe.
4. Ninaamini kwa kila kurasa (pasipo kujumuisha unabii) ina maana moja iliyosimama kwenye kusudi la mwanzo la mwaandishi aliyevuviwa. Ingawa hatuwezi kutia shaka kutambua kusudi la mwandishi wa mwanzo, viashirio vingi daima vimeelekeza katika uelekeo wake;
   a. Aina ya fasihi tanzu uliochaguliwa kuelezea ujumbe
   b. Mtindo wa kihistoria na/au muda maalumu ulioshawishi maandiko kuandikwa
   c. Muundo wa fasihi wa kitabu husika pamoja na kila fasihi moja
   d. Muundo wa maandishi (elezewa kwa fasaha) wa fasihi moja kama zinavyo husiana na ujumbe
   e. Umbo la kisarufi husika lililowekwa kuwasilisha ujumbe
   f. Maana zilizochaguliwa kuwakilisha ujumbe

Mafunzo ya kila eneo hili liwe chanzo cha mafunzo yetu katika aya. Kabla sijaelezea njia zangu za usomaji mzuri wa biblia, hebu nielezee angalau njia zisizosahihi zinazotumiwa siku hizi zilizopelekea kuwepo kwa tafsiri tofauti nyingi na hivyo basi zinatakiwa kuepukika.


## II. Mbinu zisizofaa

1. Kutojali mazingira ya fasihi ya vitabu vya Biblia na kutumia kila sentesi, ibara, au maneno binafsi kama maelezo ya kweli yasiyohusiana na kusudi la mwandishi wa mwanzo au mtindo mpana. Hii mara nyingi huitwa "uhakiki wa andiko"
2. Kutoujali muundo wa ki-hisoria wa vitabu kwa kubadilisha muundo wa ki-historia unaodhaniwa kuwa ni mdogo au usiosaidika kutoka kwenye andiko lenyewe.
3. Kutojali muundo wa kihistoria wa vitabu na kusoma kama gazeti la mtaani lililoandikwa asili kwa wakristo binafsi wa kisasa.
4. Kuupa muundo wa kihistoria wa vitabu kwa kuliistiari andiko ndani ya ujumbe wa falsafa/theolojia isioendana na wasikiaji wa kwanza na kusudi la mwandishi wa mwanzo.
5. Kutojali muundo wa mwanzo kwa kubadilisha mtindo wa theolojia ya mtu, mafundisho yanayopendeka, au mambo ya kisasa yasiyoendana na kusudi la mwandishi wa mwanzo na ujumbe uliotolewa. Tabia hii mara nyingi hufuata usomaji wa mwanzo wa biblia kama kigezo cha kuanzisha mamlaka ya mnenaji. Hii mara nyingi hurejewa kama "mwitikio wa msomaji"

(utafsiri wa-andiko-lililomaanisha-kwangu). Kwa wastani, vitu vitatu vinavyoendana vinaweza kupatikana katika mawasiliano ya binadamu yalioandikwa.




Siku za nyuma, mbinu tofauti za usomaji zimenitazamisha juu ya moja kati ya vitu vitatu. Lakini kweli tunatamka kwa dhati uhuisho wa Biblia wa kipekee na mchora uliofanyiwa mabadiliko unaofaa zaidi:




Kwa kweli vitu hivi nyote vitatu lazima vijumulishwe katika mchakato wa ufasiri. Kwa kusudi la uthibitisho, ufasiri wangu unalenga juu ya moja kati ya vitu viwili: mwandishi wa mwanzo na maandiko. Ninayamkinika kujibu matusi mabaya niliyoyachunguza (1) shutumu au kutakasa maandiko na (2) tafasili ya "mwitikio wa msomaji" (unamaanishwa nini kwangu).Matusi yanaweza kutokea katika kila hatua. Ni lazima kila mara tuchunguze mienendo yetu, upendeleo wetu, mbinu na matumizi. Lakini ni kwa jinsi gani tunaweza kuyachunguza kama hapatakuwepo na mipaka ya ufasihi, ukomo au kigezo? Hapa ni pale kusudi la mwandishi na muundo wa maandiko yaliponipa baadhi ya vigezo kuzuia maeneo ya fasiri zilizo halali. Katika kuangazia hizi mbinu za usomaji zisizofaa, zipi ni baadhi ya mitazamo mizuri ya usomaji mzuri wa biblia ambao unatoa digri ya uthibitisho na misimamo?

## III. Mitazamo inayofaa katika usomaji mzuri wa Biblia

Katika hatua hii sijadili mbinu pekee za ufasiri wa namna mahususi lakini kwa pamoja kanuni halali kwa aina yote ya maandiko ya kibiblia. Kitabu kizuri kwa namna ya mitazamo mahususi ni *How To Read The Bible For All Its Worth*, ya Gordon Fee na Douglas Stuart, kilichochapishwa na Zondervan.

Utaratibu wangu mwanzoni ulinitizamisha juu ya msomaji aliyemruhusu Roho Mtakatifu kuangaza biblia kupitia kwa miduara minne ya usomaji binafsi. Hii inamfanya Roho, andiko na msomaji wawe kiwango cha mwanzo, na siyo cha juu. Vile vile hii inamlinda msomaji kutokuwa na mwanya wa kushawishiwa na mtoa maoni. Nimesikia ikisemwa: "Biblia inaangazia zaidi katika fasihi". Hii haimaanishi kukashifu maoni juu ya msaada wa usomaji lakini ni ombi kwa muda unaofaa kwa matumizi yao. Tunalazimika kuusaidia ufasiri wetu kutoka katika andiko lenyewe. Maeneo matatu yanatoa angalau ukomo wa uthibitisho:

1. muundo wa kihistoria
2. mazingira ya fasihi
3. muundo wa kisarufi (vipashio)
4. matumizi ya maneno ya kisasa
5. milango muhimu iliyo sambamba
6. namna tanzu ya uwasilishaji

Tunahitajika kuweza kutoa sababu na mantiki zilizo nyuma ya ufasii wetu. Biblia ndiyo chanzo pekee cha imani yetu na mazoezi. Kwa huzuni, mara nyingi wakristo hawakubali juu ya kile

kinachofundishwa au kukiri. Ni kushindwa kudai uhuisho juu ya Biblia na kupelekea waamini washindwe kukubali juu ya kile kinachofundishwa na kutakiwa! Miduara mine ya usomaji imeundwa kutupatia utambuzi wa ufasili ufuatao:

1. **Mzunguko wa kwanza wa usomaji**
    a. Soma kitabu katika mkao mmoja. Soma tena katika fasili tofauti , kwa matumaini kutoka katika fasili tofauti za nadharia
        1) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
        2) Mlinganyo wenye nguvu (TEV, JB)
        3) Ufafanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
    b. Angalia kiini cha kusudi la uandishi mzima. Tambua dhamira yake.
    c. Tenga (ikiwezekana) fasihi moja, sura, ibara au sentesi inayoelezea waziwazi Kiini cha kusudi au dhamira
    d. Tambua fasihi tanzu yenye nguvu
        1) Agano la kale
            a) Simulizi za waebrania
            b) Mashairi ya waebrania (fasihi za hekima, zaburi)
            c) Unabii wa ki-Ebrania (lugha ya mjazo, shairi)
            d) Alama za siri za ki-sheria
        2) Agano jipya
            a) Simulizi (Injili, matendo)
            b) Hadithi za mafumbo (Injili)
            c) Barua/nyaraka
            d) Fasihi za mafunuo
2. **Mzunguko pili wa usomaji**
    a. Soma kitabu kizima tena, ukitafuta kufahamu mada muhimu au masomo.
    b. Elezea kwa muhtasari wa mada muhimu na elezea kwa kifupi yaliomo kwa maelezo rahisi
    c. Angalia kusudi la maelezo yako na eleza kwa mapana kwa msaada wa usomaji.
3. **Mzunguko wa tatu wa usomaji**.
    a. Soma tena kitabu kizima, ukitafuta kutambua muundo wa ki-historia na Matukio lengwa kwa ajili ya uandishi kutoka katika kitabu cha Biblia yenyewe.
    b. Taja vipengele vya ki-historia ambavyo vinatajwa katika kitabu cha Biblia.
        1) Mwandishi
        2) Tarehe
        3) Wapokeaji
        4) Kusudu mahsusi la uandishi
        5) Mwelekeo muundo wa kitamaduni unaorandana na kusudi la mwandishi
        6) Marejeo toka kwenye matukio na watu wa kihistoria/ kale
    c. Panua maelezo yako kwa kiwango cha aya kutoka katika sehemu ya kitabu cha biblia unayotafasiri. Mara nyingi tambua na kuelezea fasihi. Inaweza kuwa na vifungu na aya nyingi. Hii inakuwezesha wewe kufuata wazo na muundo wa maandiko ya mwandishi wa mwanzo.
    d. Angalia muundo wako wa kihistoria kwa kutumia msaada wa usomaji
4. **Mzunguko wa nne wa usomaji**
    a. Soma tena bayana fasihi moja katika tafasiri nyinginezo nyingi
        1) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
        2) Mwenendo linganifu (TEV, JB)
        3) Ufafanuzi (Living Bible, Amplified Bible)

b. Angalia fasihi au muundo wa kisarufi
    1) Misemo ya kujirudia Waefeso.1:6, 12, 14
    2) Muundo wa kisarufi unaojirudia Warumi 8:31
    3) Mbinyo wa mawazo (dhana zinazoafikiana)
c. Taja vipengele vifuatavyo:-
    1) Istilahi muhimu
    2) Istahili zisizo za kawaida
    3) Muundo muhimu wa kisarufi
    4) Maneno magumu, ibara, na sentesi
d. Angalia njia muhimu zilizosambamba
    1) Angalia njia za wazi za ufundishaji kwenye somo lako kwa kutumia
        a) Vitabu vya thiolojia
        b) Biblia za marejeo
        c) Itifaki
    2) Angalia maneno mawili yanayokinzana katika somo lako. Kweli nyingi za ki-Biblia zinatolewa katika rahaja mbili zinazofanana. Migongano mingi ya ki-madhehebu hutokea kutokana nauthibitisho nusu wa maandiko ya Biblia. Biblia zote zimevuviwa. Ni lazima tutafute ujumbe mzima ili kutoa mlinganyo wa ki-maandiko katika tafasiri zetu.
    3) Angalia milinganisho ndani ya kitabu, kilekile, mwandishi Yule Yule, au namna ileile, Biblia ina mfasiri wake mzuri kwa sababu ina mwandishi mmoja ambaye ni Roho Mtakatifu.
e. Tumia misaada ya kusoma kuangalia uchunguzi wako wa muundo wa kihistoria na tukio.
    1) Soma biblia
    2) Ensaikolopidia za biblia, vitabu vya mkononi na kamusi
    3) Tangulizi za biblia
    4) Fasihi za biblia (katika hatua hii kwenye usomaji wako ruhusu jamii ya waamini, waliopita na waliopo, kusaidia na kusahihisha usomaji wako binafsi)

## IV. Matumizi ya utafasiri wa Biblia.

Katika hatua hii tunageukia matumizi, umechukua muda kuelewa andiko katika muundo wake, sasa lazima utumie katika maisha yako, utamaduni wako, na elezea mamlaka ya Ki-biblia kama "uelewa ule mwandishi wa ki-biblia wa mwanzo alivyosema katika zama zake na kutumia ukweli huo katika zama hizi". Matumizi lazima yafuate utafasiri wa kusudi la mwandishi wa mwanzo katika muda na mantiki.

Hatuwezi kutumia njia ya Biblia katika zama zetu mpaka pale tutakapo fahamu kile alichokuwa akikisema katika zama hizo. Njia ya Biblia isimaanishe kile asicho kimaanisha!
Maelezo yako kwa kirefu, kwa kiwango cha aya (mzunguko wa usomaji #3) yatakuwa mwongozo wako. Matumizi lazima yafanyike katika kiwango cha aya, na sio kiwango cha neno, maneno yana maana pekee katika mazingira, ibara zina maana pekee katika mazingira na sentensi zina maana pekee katika mazingira. Mtu pekee aliyevuviwa ambaye amejumuishwa katika mchakato wa utafsiri ni mwandishi wa mwanzo. Kipekee unafuata utangulizi wake kwa mwanga wa Roho Mtakatifu. Lakini nuru sio uvuvio. Kusema "asema Bwana"lazima, tufungamane na kusudi la mwandishi wa mwanzo. Matumizi lazima yaendane bayana na kusudi lote la uandishi mzima, maandishi bayana, na muendelezo wa kiwango cha aya.

Usiruhusu mambo ya zama hizi yatafasiri Biblia, iruhusu Biblia ijiongee yenyewe. Hii itatuhitaji kuvuta kanuni kutoka kwenye andiko. Hii itakubalika kama andiko litaiwezesha kanuni. Bahati mbaya wakati mwingi kanuni zetu ni "zetu" na si kanuni za ki-maandiko.

Katika kutumia Bibilia, ni muhimu kukumbuka kuwa (isipokuwa katika unabii) maana moja na moja pekee itakubalika kwa andiko la Kibiblia pekee. Maana hiyo iendane na kusudi la mwandishi wa mwanzo kama alivyo eleza tatizo au hitaji katika zama zake. Mengi ya matumizi yanayowezekana yanaweza kutolewa kutoka katika maana hii moja. Matumizi yatategemea mahitaji ya wapokeaji lakini ni lazima yaendane na maana ya mwandishi wa mwanzo.

## V. Sura ya utafasiri wa kiroho.

Zaidi ya hapo nimejadili mantiki na mchakato wa ki-maandiko uliojumuishwa kwenye utafasiri na matumizi. Sasa ngoja nijadili kwa kinaga ubaga mwelekeo wa kiroho wa utafasiri. Mfuatano ufuatao umekuwa wa msaada sana kwangu.

1. Omba kwa ajili ya msaada wa Roho (kama vile 1Kor. 1:26-2:16)
2. Omba kwa ajili ya msaada binafsi na kusafishwa kutoka katika dhambi inayojulikana (kama vile 1 Yohana 1:9)
3. Omba kwa ajili ya hamu kubwa ya kumjua Mungu (kama vile Zab. 19:7-14, 42:1, 119:1)
4. Tumia utambuzi wowote mpya mara moja katika maisha yako.
5. Baki mnyenyekevu na anayefundishika.

Ni vigumu kuweka mlinganyo kati ya mchakato wa kimantiki na uongozi wa kiroho wa Roho Mtakatifu. Dondoo zifuatazo zimesaidia kulinganisha hizi mbili:

1. Kutoka kwa mwandishi James W.Sire, *scripture twisting*,kr. 17-18
   "Nuru huja kwenye mawazo ya watu wa Mungu na sio tabaka la watu wa kiroho. Hakuna daraja la ualimu katika ukristo wa kibiblia. Hakuna kuongoza, hapana mtu awaye yote ambaye tafsiri zote nzuri zitoke kwake. Na hivyo, wakati roho mtakatifu anatoa karama maalumu ya hekima, maarifa na utambuzi wa kiroho huwa pamoja. Hakutoa hizi kwa wakristo waliokirimiwa kuwa wao ndo pekee watafsiri wenye mamlaka ya Neno lake. Ni juu ya kila watu wake kujifunza, kuamua na kutambua kwa kufanya marejeo kwenye Biblia ambayo inasimama kama yenye mamlaka hata kwa wale ambao Mungu amewapa uwezo pekee. Kwa kufupisha, wazo mnalofanya kupitia kitabu kizima ni kuwa Biblia ni ufunuo wa kweli wa Mungu kwa watu wote, ya kuwa ni mamlaka yetu ya mwisho katika mambo yote ambayo inayaongelea, kuwa sio fumbo lote lakini inaweza kueleweka vya kutosha na watu wa kawaida kwa kila tamaduni."
2. Juu ya Kierkegaard, inayopatikana toka kwa Benard Ramm,*Protestant Biblical Interpretation(tafsiri ya biblia ya ki-protestanti*) Uk.75:
   Kutokana na Kierkegaard, kisarufi, misamiati na usomaji wa kihistoria wa Biblia ulikuwa ni muhimu lakini utangulizi wa usomaji wa kweli wa Biblia na kusoma Biblia kama neno la Mungu mmoja lazima alisome kwa moyo wake wote mdomoni mwake, kutoka ncha ya kidole, na shauku ya matarajio katika mazungumzo na Mungu. Usomaji wa Biblia pasipo tafakari, kutojali au kielimu, au weledi sio usomaji wa Biblia kama neno la Mungu, kama mmojawapo asomavyo barua ya mapenzi isemavyo, tena mmoja asoma kama neno la Mungu.
3. H.H Rawley katika *The Relevance of the Bible*, Uk.19:
   Hakuna uelewa mdogo wa kisomi wa Biblia, ingawa yote, inaweza kumiliki hazina yote. Haidharau uelewa huo, kwa kuwa ni muhimu kwa uelewa wote. Lakini ni lazima iongeze uelewa wa kiroho wa hazina ya kiroho ya kitabu hiki kwa ujumla. Kwa huo uelewa wa kiroho kitu fulani ambacho ni zaidi ya hadhari ya kiroho ni muhimu. Mambo ya kiroho ni utambuzi wa kiroho, na wanafunzi wa Biblia wanahitaji fikra za upokeaji wa kiroho. Ile hamu ya kumtafuta Mungu ambayo inaweza kumsababisha ajitoe kwake. Ni kama kupita zaidi ya usomaji wa kisayansi kuingia kwenye urithi wa utajiri wa hiki kitabu kikubwa kuliko vyote.

## VI. Njia hizi za Fasiri

*Study Guide Commentary (Mwongozo wa usomaji) wa* fasihi umeundwa kusaidia njia zako za utafsiri katika njia zifuatazo:

1. Maelezo fasaha ya kihistoria yanayotambulisha kila kitabu baada ya kufanya "mduara wa usomaji #3" angalia taarifa hizi.
2. Utambuzi wa ki-mazingira unapatikana katika kila kurasa. Hii itakusaidia kuona jinsi gani maandishi/fasihi imeundwa.
3. Katika kila mwanzo wa kifungu au fasihi kubwa inaunganisha mgawawanyo wa aya na maelezo ya kichwa cha makala yanatolewa kutoka katika tafsiri za kisasa.
   a. United Bible Society Greek Text.Toleo la nne lililobadilishwa (UBC)
   b. The New American Standard Bible 1995 ya kisasa (NASB)
   c. The New King James Version (NKJV)
   d. The New Revised Standard Version (NRSV)
   e. Today's English Version (TEV)
   f. The Jerusalem Bible (JB)

Aya zilizogawanywa hazikuvuviwa. Lazima ziyakinishwe kutoka katika mazingira fulani. Kwa kulinganisha tafsiri nyingi za kisasa kutoka tafsiri nyingi za ki-nadharia na mitizamo ya kitheolojia, tunaweza kuchanganua muundo unaokusudiwa wa mawazo ya mwandishi wa mwanzo, kwani kila aya ina ukweli mmoja mkubwa. Huu uliitwa "mada ya sentensi" au wazo la kati la andiko, hilo wazo lililounganishwa ni ufunguo kwa tafsiri nzuri ya kihistoria na kisarufi. Mmojawapo asitafsiri, kuhubiri au kufundisha chini ya aya, vilevile ukumbuke ya kuwa kila aya inahusiana na aya zingine. Hii ndo maana kiwango cha aya kinachoelezea kitabu kizima ni muhimu. Ni lazima tuweze kufuata mtiririko wa kimantiki wa somo lililotolewa na mwandishi wa mwanzo aliyevuviwa.

4. Muhtasari wa Bob unafuata mtazamo wa kifungu kwa kifungu kwa utafsiri wake. Hii inatulazimisha kufuata mawazo ya mwandishi wa mwanzo. Muhtasari unatoa habari kutoka sehemu nyingi.
   a. Mazingira ya fasihi
   b. Utambuzi wa kihistoria na tamaduni
   c. Habari za kisarufi
   d. Usomaji wa neno
   e. Njia muhimu zilizo sambamba
5. Mahali fulani katika fasihi, andiko lililochapishwa toka toleo jipya la Marekani (1995 mpaka sasa hivi) litaongezewa na tafsiri za matoleo mbalimbali ya kisasa.
   a. New King James Version (NKJV) ambayo unafuata mswaada wa "Upokeaji wa Maandiko halisi".
   b. The New Revised Standard Version (NRSV) ambayo ni rudio la neno-kwa-neno Kutoka katika Umoja makanisa asili ya Revised Standard Version
   c. The Today's English Version (TEV) ambayo ni tafsiri ya mlinganyo wa nguvu Kutoka American Bible Society.
   d. The Jerusalem Bible (JB) ambayo ni tafsiri ya Kiingereza inayotegemea kutoka tafsiri ya Mlinganyo wa nguvu wa Katoriki ya Ufaransa.
6. Kwa wale wote ambao hawasomi ki-giriki, ukilinganisha na tafsiri za kiingereza inaweza kusaidia kutambua matatizo katika andiko:
   a. Tofauti za mswada
   b. Maana ya maneno mbadala
   c. Muundo na maandiko magumu ya kisarufi Ingawa tafsiri za kiingereza haziwezi kuleta suluhu kwenye matatizo hayo yanayalenga kama sehemu ya ndani na usomaji kamili.
   d. Karibia kila kifungu, maswali muhimu ya majadiliano yanatolewa ambayo yanajaribu kulenga maswala muhimu ya utafsiri wa kifungu hicho

# MTU AITWAYE, PETRO

## FAMILIA YAKE

A. Familia ya Petro iliishi huko Galilaya sehemu ya watu wa mataifa katika mji wa Bethsaida uliokuwa Kaskazini mwa mwambao wa ziwa Galilaya (au ziwa Tiberia kama vile Yohana 1:44), lakini inavyoonekana alisogea sehemu za Kapernaumu (kama vile Marko 1:21,29).

B. Jina la baba yake aliitwa Yona (kama vile Mt. 16:17) au Yohana (kama vile Yohana 1:42; 21:15-17).

C. Jina alilopewa lilikuwa Simion (kama vile Marko 1:16,29,30,36), ambalo lilikuwa likijulikana huko Palestina kwenye karne ya kwanza. Ilikuwa ni namna ya Wayahudi kuita simeoni (kama vile Mdo. 15:14; 2 Pet. 1:1), ambalo lilikuwa ni jina la moja ya makabila kumi na mawili ya Israeli (kama vile Mwa. 29:33; Kut. 1:1). Yesu alimwita jina Petro (*Petros*, likimaanisha "mwamba," lilimaanisha kuelezea nguvu zake za baadaye na uthabiti) katika Mt. 16:18; Mk. 3:16; Lk. 6:14; na Yohana 1:42. Muundo wa Kiaramu ni *Cephas* (kama vile Yohana 1:42; 1 Kor. 1:12; 3:22; 9:5; 15:5; Gal. 1:18; 2:9,11,14). Mara nyingi katika Agano Jipya haya majina mawili hutolewa pamoja (kama vile Mt. 16:16; Lk 5:8; Yn. 1:40; 6:8,68; 13:6,9,24,36; 18:10,15,25; 20:2,6;21:2-3,7,11,15).

D. Jina la nduguye Petro aliitwa Andrea (kama vile Mk 1:16). Alikuwa mwanafunzi wa Yohana Mbatizaji (kama vile Yn.1:35,40) na baadaye akawa mwamini na mfuasi wa Yesu (kama vile Yn. 1:36-37). Alimleta Simoni kwa Yesu (kama vile Yn. 1:41). Baada ya miezi kadhaa Yesu akakutana nao huko ziwa Galilaya na kuwaita kuwa wanafunzi kamili (kama vile Mt. 4:18-20; Mk. 1:16-18; na Lk. 5:1-11).

E. Alikuwa na mke (kama vile Mk. 1:30; 1 Kor. 9:5), lakini hapakutaja idadi ya watoto aliokuwa nao.

## KAZI YAKE

A. Familia ya Petro ilimiliki boti za uvuvi na hata kuweza kuwa na watumishi.

B. Familia ya Petro yawezakuwa ilikuwa na uhusiano na Yakobo, Yohana, na babaye, Zebedayo (kama vile Lk 5:10).

C. Petro alirudi kwenye kazi yake ya uvuvi baada ya kifo cha Yesu (kama vile Yohana 21).

## MWONEKANO WAKE

A. Nguvu za Petro
   1. Alikuwa ni mfuasi aliyejitoa, lakini mwenye maamuzi ya ghafla (kama vile Mk. 9:5; Yn. 13:4-11).
   2. Alijaribu kutenda kwa imani, lakini mara zote alishindwa (mf. Kutembea juu ya maji, kama vile Mt. 14:28-31).
   3. Alikuwa jasiri hata tayari kufa (kama vile Mt. 26:51-52; Mk. 14:47; Lk. 22:49-51; Yohana 18:10-11).
   4. Baada ya kufufuka kwake, Yesu akamwelezea yeye binafsi kama kiongozi mwenye kufedhehesha kati ya wale kumi na wawili katika Yohana 21 na kutoa nafasi ya kutubu na kurejeshwa kwenye uongozi.

B. udhaifu wa Petro
   1. Alikuwa na tabia zake za mwanzo dhidi ya ushikiliaji wa sheria za Kiyahudi
      a. akila na watu wa mataifa (Gal. 2:11-21)
      b. sheria za chakula (Matendo 10:9-16)
   2. Aliwapenda Mitume wote, hakuelewa kikamilifu mafundisho mapya muhimu ya Yesu na matokeo yake
      a. Marko 9:5-6
      b. Yohana 13:6-11; 18:10-11
   3. Binafsi aliweza kukemewa vikali na Yesu (Mk. 8:33; Mt. 16:23)
   4. Alikutwa amelala badala ya kuomba kwenye wakati mgumu wa hitaji la Yesu pale Gethsemani (Mk.14:32-42; Mt. 26:36-46; Lk. 22:40-60)
   5. Mara kadhaa alirudia kumkana Yesu kuwa hamjui (Mk. 14:66-72; Mt. 26:69-75; Lk. 22:56-62; Yhana 18:16-18,25-27)

## UONGOZI WAKE WA KUNDI LA KITUME

A. Kuna orodha nne za Mitume (kama vile Mt. 10:2-4; Mk. 3:16-19; Lk. 6:14-16; Mdo. 1:13). Mara nyingi Petro huandikwa wa kwanza. Wale kumi na wawili waligawiwa katika makundi matatu ya watu wanne. Naamini hili liliwasaidia kufanya mzunguko wa kwenda kuziona familia zao.
B. mara nyingi Petro alitumika kama msemaji mkuu kwa ajili ya kundi la Kitume (kama vile Mt. 16:13-20; Mk. 8:27-30; Lk. 9:18-21). Sura hizi pia zimetumika kutetea mamlaka ya Petro ndani ya kundi (kama vile Mt. 16:18). Hata hivyo, ndani ya muktadha huu alikemewa na Yesu yeye kutumika kama chombo cha shetani (kama vile Mt.16:23; Mk. 8:33). pia, kipindi wanafunzi wanabishana ni nani aliye mkubwa kati yao, Petro hakufikiliwa kuchukua nafasi hiyo (kama vile Mt. 20:20-28, hasa mst. 24; Mk. 9:33-37; 10:35-45).
C. Petro hakuwa kiongozi wa kanisa la Yerusalemu. Hili liliangukia kwa Yakobo, nduguye Yesu (kama vile Mdo.12:17; 15:13; 21:18; 1 Kor. 15:7; Gal. 1:19; 2:9,12).

## HUDUMA YAKE BAADA YA YESU KUFUFUKA

A. Nafasi ya uongozi wa Petro kwa wazi inaonekana mwanzoni mwa sura za Matendo ya Mitume
   1. Aliwaongoza kwenye uchaguzi wa kumrithi Yuda (kama vile Matendo 1:15-26).
   2. Alihubiri hotuba ya mwanzo siku ile ya Pentekoste (kama vile Matendo 2).
   3. Alimponya Yule kiwete na kuhubiri mafundisho yake ya mara ya pili yaliyoandikwa (kama vile Matendo 3:1-10; 3:11-26).
   4. Alizungumza kwa ujasiri kwenye baraza la wakuu wa sinagogi katika Matendo 4.
   5. Alisimamia nidhamu ya kanisa kwa Anania na Safira katika Matendo 5.
   6. Alizungumza kwenye baraza la Yerusalemu katika Matendo 15:7-11.
   7. Matukio mengine mbalimbali na miujiza inaelezewa juu yake katika Matendo.
B. Petro, hata hivyo, hakuwakilisha matokeo ya injili
   1. Alishikilia mtazamo wa Agano la Kale (kama vile Gal. 2:11-14).
   2. Alipaswa kuwa na mafunuo maalum akimjumuisha Kornelio (kama vile Matendo 10) na watu wengine wa mataifa.

## MWAKA WAKE WA UTULIVU

A. Pana habari ndogo kumhusu Petro baada ya Baraza la Yerusalemu katika Matendo 15
   1. Wagalatia 1:18
   2. Wagalatia 2:7-21
   3. 1 Wakorintho 1:12; 3:22; 9:5; 15:5
B. tamaduni za mwanzo za kanisa
   1. Kuuwawa kwa Petro huko Rumi kumetajwa kwenye waraka wa Clement kwenye kanisa la Korintho katika mwaka wa 95b.k.
   2. Tertullian (150-222 B.K) pia alikumbuka kuuwawa kwa Petro huko Rumi na Nero (mwaka wa 54-68 b.k).
   3. Clementi wa huko Iskanderia (mwaka wa 200 ) anasema Petro aliuwawa huko Rumi.

# UTANGULIZI WA MARKO

## MAELEZO YA UFUNGUZI

A. Kanisa la mwanzo mara nyingi liliepuka kunakiri, kusoma na kufundisha kitabu cha Marko kama rejeo kwa Mathayo na Luka kwa sababu waliona Marko kama toleo la "muhtasari wa kiongozi" (yaani., injili iliyojengeka), mtizamo ambao hasa baadae ulielezewa na Augustino.
B. Kitabu cha Marko mara nyingi hakirejerewi na makasisi wa Kiyunani wa kanisa la mwanzo au watetezi wa karne ya pili (watetezi wa imani).
C. tangu kuinuka kwa mtizamo wa kisasa wa historia ya visarufi kwenye utafasiri wa Kibiblia, injili ya Marko imechukua umuhimu mpya kwa sababu inatazamwa kama injili ya kwanza kuandikwa. Wote Mathayo na Luka hutumia maelezo yake kuwasilisha maisha ya Yesu na umuhimu wake. Hivyo basi kitabu cha Marko kimekuwa ni nyaraka ya kimsingi kwenye kanisa, cha kwanza kuandika habari za maisha ya Yesu.

## UWASILISHAJI

A. Injili sio wasifu wa kisasa au historia. Ni maandiko yenye kuchaguliwa kithiolojia yakitumika kumtambulisha Yesu kwenye hadhira mbalimbali na kuwaleta kwenye imani katika Yeye. Ni "habari njema"kuhusu maisha ya Yesu kwa ajili ya kusudi la uinjilisti (kama vile Yohana 20:30-31).
B. Marko anaelezea miundo minne tofauti ya kihistoria na makusudi manne ya kithiolojia
   1. Maisha na mafundisho ya Yesu
   2. Maisha na huduma ya Petro
   3. Hitaji la kanisa la mwanzo
   4. Kusudi la uinjilisti wa Yohana aitwaye Marko
C. Injili zote nne ni za kipekee huko Mashariki ya Karibu fasihi za Wayunani-Warumi. Waandishi waliovuviwa walikuwa na Roho ya kuongoza shughuli ya kuchambua mafundisho ya Yesu na matendo ambayo kwa uwazi yalithibitisha tabia na/ au kusudi lake.

   Waliyapanga haya maneno na matendo kwa njia tofauti. Mfano mmoja ungalikuwa ni kulinganisha ujumbe wa Mathayo kule mlimani (Mathayo 5-7) kukiwa na ujumbe wa Luka juu ya uwanda (kama vile Lk. 6:20-49). Ikajakuwa dhahiri kuwa Mathayo alijaribu kuyakusanya mafundisho yote ya Yesu kuwa ujumbe mmoja mrefu, wakati Luka akieneza mafundisho yale yale kwenye injili yake yote. Kitu kile kile kingaliweza kuzungumza kuhusu Mathayo kuiweka miujiza ya Yesu pamoja, wakati Luka akieneza kwenye injili yake yote.

   Hii inadokeza uwezo wa mwandishi wa injili sio tu kwa kuchagua na kupanga mafundisho ya Yesu, bali pia kwendana nayo kwa ajili ya makusudio yao wenyewe (soma Fee and Stuart's *Howto Read the Bible For All Its Worth*, kur. 113-134). Ukiwa unaisoma injili mtu lazima aendelee kuuliza ni hoja gani ya kithiolojia mwandishi anajaribu kuitengeneza. Kwa nini ajumuishe haswa hili tukio, muujiza, somo kwenye hoja hii kwenye uwasilisho huu wa Yesu?
D. Injili ya Marko ni mfano mzuri wa lugha ya Koine ya huko Uyunani kama lugha ya pili ya watu wa ulimwengu wa Kimediterania. Lugha ya mama ya Marko ilikuwa ni Kiaramu (kama ilivyokuwa kwa Yesu na Wayahudi wote wa karne ya kwanza wa huko Palestina). Kionjo hiki cha Kisemiti mara nyingi ni cha dhahiri katika injili ya Marko.

## UANDISHI

A. Yohana aitwaye Marko kitamaduni amekuwa akitambulika na Mtume Petro kwenye uandishi wa injili hii. Kazi yenyewe (kama zilizo injili zingine) ni yenye kushabihiana.
B. Ushuhuda mwangine wa macho wa habari za Petro ni ukweli kwamba Marko hakuandika matukio matatu makuu ambayo Petro mwenyewe alihusika.
   1. Kutembea kwake juu ya maji (kama vile Mt. 14:28-33)
   2. Akiwa msemaji mkuu huko Kaisaria Filipi kwa ajili imani ya wale kumi na wawili (kama vile Mt. 16:13-20), katika Marko ni sura ya 8:27-30 tu ndiyo inazungumzia na kifungu "juu ya mwamba huu" na "maelezo ya ufalme wa Mungu" vimeondolewa.

3. Uwakala wake wa kodi za hekalu kwa ajili yake mwenyewe na Yesu (kama vile Mt. 17:24-27) huenda unyenyekevu wa Petro ulimpelekea mwenyewe kutolisisitiza hili kwenye hotuba yake akiwa huko Rumi.

C. Tamaduni za mwanzo za kanisa
1. zikiandikwa toka huko Rumi mwaka wa 95 b.k, zikimdokeza Marko (kama iivyokuwa kwa *Shepherd of Hermes*).
2. Papias, askofu wa Hierapolis (yapata mwaka wa 130 b.k), akaandika *Interpretation of the Lord's Sayings*, kilichorejewa na Eusebius (mwaka wa 275-339 b.k) kwenye *Ecclesiastical History* 3:39:15 yake. Anadai kuwa Marko alikuwa mtafasiri wa Petro aliyeandika kwa usahihi, lakini hakuyaweka katika mpangilio wa kimatukio, kumbukumbu za Petro kumhusu Yesu. Inavyoonekana Marko alichukua na kufuatisha mahubiri ya Petro na kuyaweka pamoja kwa ajili ya uwasilishi wa injili. Papias anadai kuwa alipata habari hizi toka kwa "wazee," ambao yawezekana kumrejerea Mtume Yohana.
3. Justin Martyr (mwaka 150 b.k), anarejea Marko 3:17, akiongeza kuwa linatoka kwenye kumbukumbu za Petro.
4. Utangulizi wa imani ya Marcion kwa Marko, ulioandikwa yapata mwaka wa 180 b.k, unamtambua Petro kama shuhuda wa macho wa injili ya Mrko. Pia inaelezea kuwa Marko aliandika injili toka Italia baada ya kifo cha Petro (kidesturi akiwa Rumi yapata mwaka wa 65 b.k).
5. Irenaeus, akiandika yapata mwaka wa 180 b.k, akimtaja Yohana aitwaye Marko kama mtafasiri wa Petro na mwenye kuweka pamoja kumbukumbu zote baada ya kifo cha Petro (kama vile *Contra Haereses* 3:1:2).
6. Clement wa Iskanderia (mwaka wa 195 b.k) anadai kuwa wale wote waliosikia mahubiri ya Petro walimwomba Marko ayaandike haya mahubiri.
7. The Muratorian Fragment (yaani., orodha ya vitabu vilivyokubaliwa), ikiandikwa yapata mwaka wa 200 b.k toka Rumi, ingawa andiko halikuwa kamili, lakini inaonekana kumthibitisha Marko kama mwandishi wa jumbe za Petro.
8. Tertullian (mwaka wa 200 b.k) kwenye chapisho *Against Marcion* (4:5) anasema Marko alichapisha kumbukumbu zote za Petro.
9. Kwenye chapisho la *The Expositor's Bible Commentary* juzuu ya 8, uk. 606, Walter Wessel anatengeneza hoja yenye kusisimua kuwa tamaduni za makanisa ya mwanzo hapo juu yanatokana na makanisa mbalimbali ya kimazingira
   a. Papias toka Asia Ndogo
   b. Anti-Marcion Prologue na Muratorian Fragment yote toka Rumi
   c. Irenaeus (cf. *Adv. Haer.* 3:1:1) toka Lyons huko Ufaransa. Desturi za Irenaeus pia zinapatikana katika Tertullian (kama vile *Adv. Marc.* 4:5) toka Afrika Kaskazini na Clement wa Iskanderia huko Misri (kama vile *Hypotyposeis* 6, akirejewa na Eusebius, *Eccl. His.* 2:15:1-2; 3:24:5-8; 6:14:6-7). Haya mazingira mbalimbali yalileta ukubarifu kwenye kuyaamini kwa sababu ya ukubarifu mpana wa desturi za Ukristo wa mwanzo.
10. Kutokana na Eusebius' *Eccl. His.* 4:25, Origen (230 B.K) katika *Commentary on Matthew* (hapana fasiri inayofahamika juu ya Marko na mtu yeyote mpaka karne ya tano) inasema Marko aliandika injili kama Petro alivyoielezea kwake.
11. Eusebius mwenyewe aliijadili injili ya Marko katika *Eccl. His.* 2:15 na kusema Marko aliandika mahubiri ya Petro kwa maombi ya wale walioisikia ili kwamba yapate kusomwa katika makanisa yote. Eusebius alizisimamia hizi desturi juu ya maandiko ya Clement wa Iskanderia.

D. Ni ni tunachokifahamu juu ya Yohana aitwaye Marko
1. Mama yake alikuwa ni mwamini aliyejulikana sana huko Yerusalemu ambaye nyumbani kwake kanisa lilikutanika (yumkini siku ile ya Karamu ya Bwana, kama vile Marko 14:14-15; Mdo. 1:13-14; Matendo 12:12). Huenda alikuwa ni mtu asiye na jina ambaye alikimbia "uchi" toka kwenye bustani ya Gethsamane (Marko 14:51-52).
2. Alifuatana na mjomba wake aitwae Barnabas (kama vile Kol. 4:10) na Paulo pindi wakirudi Antiokia kutoka Yerusalemu (Matendo 12:25).
3. Alikuwa mwenza wa Paulo na Barnaba kwenye safari ya kwanza ya Umishionari (Matendo 13:5), lakini akarudi nyumbani ghafla (Matendo 13:13).

4. Baadaye Barnabas akahitaji kumchukua Marko kwenye safari yake ya pili ya Umishionari, lakini ikasababisha kutokuwepo maelewano kati ya Barnaba na Paulo (Matendo 15:37-40).
5. Baadaye waliweza kuungana tena na Paulo na kuwa marafiki na mtenda kazi mwenza (Kol. 4:10; 2 Tim. 4:11;Filemoni 2:4).
6. Alikuwa mshirika na mtenda kazi mwenza wa Petro (1 Pet. 5:13), yumkini huko Rumi.

E. maarifa binafsi ya Marko kuhusu maisha ya Yesu yanaonekana kuthibitishwa na Marko 14:51-52, pale mtu alipokimbia uchi toka kwenye bustani ya Gethsemane mara tu baada ya Yesu kukamatwa. Haya maelezo yasiyo ya kawaida yanaonekana kuaksi uzoefu binafsi wa Marko.

## TAREHE

A. Injili ndio shuhuda wa macho kuhusu habari na tafasiri za maisha ya Yesu, matendo, na mafundisho yake, inavyoonekana yalichukuliwa toka kwenye jumbe za Petro. Ziliwekwa pamoja na kusambazwa baada ya kifo chake, kusema hivyo wale Anti-Marcionite Prologue and Irenaeus (ambao pia waliongezea baada ya kifo cha Paulo). Wote Paulo na Petro waliuwawa chini ya utawala wa Nero (mwaka wa 54-68 b.k) huko Rumi (desturi za kanisa). Tarehe kamili haijulikani, lakini ni kweli, baadaye yumkini tarehe ya Marko ilikuwa katikati ya karne ya sita.
B. yawezekana kuwa Anti-Marcionite Prologue na Irenaeus haurejerei kwenye kifo cha Petro, lakini kuondoka kwake (yaani., safari ya kuondoka kwake) toka Rumi. Kuna baadhi ya shuhuda za kidesturi (yaani., Justin na Hippolytus) kuwa Petro alizuru huko Rumi wakati wa utawala wa Claudio (41- 54 b.k), (Eusebius' *Eccl. His.* 2:14:6).
C. Inaonekana kuwa Luka alihitimisha kitabu cha Matendo wakati Paulo akiwa gerezani mwanzoni mwa karne ya sita. Ikiwa hili ni kweli kwamba Luka alimtumia Marko kwenye injili yake, hivyo lazima yawezakuwa imeandikwa kabla ya kitabu cha Matendo na, kwa hiyo, mapema zaidi mwanzoni mwa karne ya sita.
D. Uandishi na tarehe za Marko haziwezi kwa namna yeyote kuathiri ukweli wa kihistoria/kithiolojia/kiinjilisti wa hii injili. Yesu, na sio mwandishi aliye mwanadamu, ndiye mlengwa mwenyewe!
E. inashangaza kuwa hakuna injili (hata Yohana, iliyoandikwa kati ya mwaka 95-96 b.k) inayorejelea au kudokeza uharibifu wa Yerusalemu (kama vile Mt. 24; Marko 13; Luka 21) katika mwaka wa 70 b.k na generali wa Kirumi, baadaye mfalme mkuu, Titus. Marko yumkini alikwisha andika kabla ya hili tukio. Hata yawezekana kuwa injili ya Mathayo na Luka iliandikwa kabla ya hukumu kuu juu ya dini ya Kiyahudi. Lazima ielezewe kuwa tarehe kamili kwa ajili ya uwekaji pamoja wa mihitasari ya injili haijulikani kwa muda huu (kama inavyohusiana kifasihi injili moja na nyingine).

## WAPOKEAJI

A. Marko anahusianishwa na Rumi waandishi mbalimbali wa makanisa ya mwanzo
   1. 1 Petro 5:13
   2. Viambishi awali vya Marko, Luka na Yohana (Italia)
   3. Irenaeus (Rumi, kama vile *Adv. Haer.* 3:1:2)
   4. Clement wa Iskanderia (Rumi kama vile Eusebius *Eccl. Hist*. 4:14:6-7; 6:14:5-7)

B. Marko haelezei hasa kusudi lake la kuiandika injili. Pamekuwepo na nadharia mbalimbali.
   1. Vijarida vya kiinjilisti (kama vile Marko 1:1) vilivyoandikwa mahususi kwa Warumi (kama vile Marko 1:15; 10:45)
      a. vipengele vya Kiyahudi vilivyotafasiriwa (kama vile Marko 7:3-4; 14:12; 15:42)
      b. maneno ya Kiarama yaliyotafasiriwa (kama vile Marko 3:17; 5:41; 7:1,34; 10:46; 14:36; 15:22,34)
      c. utumiaji wa maneno mengi ya Kilatini (kama vile executioner (muuaji), Marko 6:27; sextanus, Marko 7:4; census, Marko 12:14; quadrans (sarafu ya shaba ya Rumi ya kale), Marko 12:42; praetorium(ukumbi wa kutolea hukumu), Marko 15:16; centurion(jemedari wa jeshi la Kirumi mwenye umri mkubwa), Marko 15:39; flagellare,Marko 15:42)
      d. lugha jumuishi yenye kuhusiana na Yesu

1) lugha jumuishi yenye kuhusiana na wale walioko Palestina (kama vile Marko 1:5,28,33,39; 2:13; 4:1;6:33,39,41,55)
2) lugha jumuishi yenye kuhusiana na watu wote (kama vile Marko 13:10)
2. Mateso yaliyoambatana na moto huko Rumi katika mwaka wa 64 b.k, pale Nero alipowalaumu Wakristo, na kuanzisha mateso makali kwa waamini. Mara nyingi Marko aliyataja haya mateso (kama vile mateso ya Yesu 8:31; 9:39; 10:33-34,45 na mateso ya wafuasi wake 8:34-38; 10:21,30,35-44).
3. Kuchelewa kwa ujio wa pili
4. Kifo cha mashuhuda wa Yesu, hasa wale Mitume
5. Kuinuka kwa makundi ndani ya makanisa yaliyotawanyika sehemu kubwa
   a. Wakristo waliobadili itikadi (Galatians)
   b. wenye ujuzi (1 Yohana)
   c. muunganikano wa a na b (yaani., Wakolosai na Waefeso; 2 Pet. 2)

## MAELEZO YA KIMUUNDO

A. Marko anaandaliwa kiasi kwamba wiki ya mwisho ya maisha ya Yesu ndiyo mpango wa zaidi ya theruthi moja ya kitabu.umuhimu wa kithiolojia wa wiki ya mateso ni dhahiri.

B. tangu Marko, kutokana na desturi za kanisa la mwanzo, zilizochukuliwa toka jumbe za Petro, (yaani., yumkini huko Rumi) ikajakuwa wazi ni kwa nini simulizi za kuzaliwa kwake zilijumuishwa. Marko alianzia pale uzoefu wa Petro ulipoanzia, akiwa na Yesu kama mtu wa umri, na kithiolojia akihusianishwa na jumbe za toba za Yohana Mbatizaji na imani katika maandalizi kwa ajili ya kazi ya Masihi. jumbe za Petro zilitumia dhana ya "Mwana wa Adamu" na "Mwana wa Mungu." Injili inaaksi thiolojia yake Petro juu ya ubinadamu wa Yesu. Mwanzoni alikuwa mwalimu mkubwa na mponyaji, lakini ikajakuwa wazi kuwa alikuwa Masihi! huyu Masihi hakuwa generali wa kushinda vita, lakini mtumishi mwenye mateso (kama vile Isaiah 53).

C. Maelezo ya msingi ya Marko ya muundo wa kimazingira yanatumika kwa pamoja na mihitasari mingine ya injili (yaani., Mathayo na Luka)
   1. Huduma ya Wagalilaya (Marko 1:14-6:13)
   2. Huduma nje ya Galilaya (Marko 6:14-8:30)
   3. Safari ya kwenda Yerusalemu (Marko 8:31-10:52)
   4. Wiki ya mwisho maeneo ya Yerusalemu (Marko 11:1-16:8)

D. hata yawezekana kuwa muundo wa Marko unaigiza vipengere muhimu vya mahubiri ya Kitume ya mwanzo (yaani., Mdo. 10:37-43, kama vile C. H. Dodd's *NewTestament Studies* kur. 1-11). Ikiwa hili ni kweli hivyo injili zilizoandikwa ni utimilisho wa kipindi cha desturi za kimasimulizi (yaani., *kerygma*). Dini ya Kiyahudi waliamini mafundisho ya kusimulia yalikuwa bora kuliko yale yaliyoandikwa.

E. Marko anaainishwa na habari za utokaji haraka (yaani., "pasipo kuchelewa," kama vile Marko 1:10) ya maisha ya Yesu. Marko hakuweka kumbukumbu ya vipindi vya mafundisho marefu, lakini aliendа haraka toka tukio moja hadi jingine (yaani., utumiaji wake wa kurudia wa neno "pasipo kuchelewa"). Injili ya Marko inamdhihirisha Yesu kwa matendo yake. Hata hivyo, habari za kasi hii zinasambazwa kwa maelezo dhahiri ya mashuhuda wa macho (yaani., Petro).

## MZUNGUKO WA KWANZA WA USOMAJI (Kutoka"Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.
Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Dhamira ya kitabu kizima
2. Aina ya fasihi iliyotumika (uwasilishaji)

## MZUNGUKO WA PILI WA USOMAJI (Kutoka"Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Mada ya sehemu ya kwanza ya fasihi
2. Mada ya sehemu ya pili ya fasihi
3. Mada ya sehemu ya tatu ya fasihi
4. Mada ya sehemu ya nne ya fasihi
5. N.k.

# MARKO 1

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA* | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Mahubiri ya Yohana Mbatizaji<br>1:1-8 | Yohana Mbatizaji anaandaa Njia<br>1:1-8 | Shughuli za Yohana Mbatizaji<br>1:1-8 | Mahubiri ya Yohana Mbatizaji<br>1:1-3<br>1:4-5<br>1:6-8 | Tangazo la Yohana Mbatizaji<br>1:1-8 |
| Ubatizo wa Yesu<br>1:9-11 | Yohana anambatiza Yesu<br>1:9-11 | Ubatizo wa Yesu<br>1:9-11 | Ubatizo na Majaribu Yesu<br>1:9-11 | Yesu anabatizwa<br>1:9-11 |
| Majaribu ya Yesu<br>1:12-13 | Shetani anamjaribu Yesu<br>1:12-13 | Majaribu ya Yesu<br>1:12-13 | 1:12-13 | Kujaribiwa Jangwani<br>1:12-13 |
| Mwanzo wa Huduma ya Galilaya<br>1:14-15 | Yesu anaanza Huduma yake ya Galilaya<br>1:14-15 | Mwanzo wa shughuli ya Yesu Galilaya<br>1:14-15 | Yesu anaita wavuvi wanne<br>1:14-15 | Yesu anaanza kutangaza ujumbe<br>1:14-15 |
| Kuitwa kwa Wavuvi wane<br>1:16-20 | Wavuvi wanne wanaitwa kama Wanafunzi<br>1:16-20 | 1:16-20 | 1:16-18<br>1:19-20 | Wanafunzi Wanne wanaitwa<br>1:16-18<br>1:19-20 |
| Mtu mwenye Pepo wachafu<br>1:21-28 | Yesu anatoa pepo wachafu<br>1:21-28 | 1:21-28 | Mtu mwenye roho mchafu<br>1:21-22<br>1:23-24<br>1:25<br>1:26-27<br>1:28 | Yesu anafundisha Kapernaumu na kutoa Pepo<br>1:21-22<br>1:23-28 |
| Uponyaji wa Watu wengi<br>1:29-34 | Mama Mkwe wa Petro anaponywa<br>1:29-31<br>Wengi wanaponywa Baada ya machweo Ya Sabato<br>1:32-34 | 1:29-31<br>1:32-34 | Yesu anaponya wengi<br>1:29-31<br>1:32-34 | Matibabu ya mama mkwe wa Petro<br>1:29-31<br>Uponyaji kadhaa<br>1:32-34 |
| Safari ya Mahubiri<br>1:35-39 | Mahubiri Galilaya<br>1:35-39 | 1:35-39 | Yesu anahubiri Galilaya<br>1:35-37<br>1:38<br>1:39 | Yesu anaondoka kimya kimya Karpenaumu na Kusafiri kupitia Galilaya<br>1:35-39 |
| Kutakaswa Kwa Mkoma<br>1:40-45 | Yesu anatakasa Mkoma<br>1:40-45 | 1:40-45 | Yesu anaponya mtu<br>1:40<br>1:41-44 | uponyaji wa mtu aumwaye ugonjwa wa ngozi<br>1:40-45 |

| 1:45 |
|---|

* Ingawa hazijavuviwa, migawanyo ya aya ndiyo ufunguo wa kuelewa na kufuatilia kusudio la asili la mwandishi. Kila tafsiri ya kisasa imegawanya na kufanya muhtasari wa aya. Kila aya ina mada kuu, kweli au wazo. Kila toleo limebeba hiyo mada kwa namna yake ya pekee. Unaposoma maandiko ya mwandishi jiulize ni tafsiri ipi inawiana na uelewa wako wa somo na mgawanyo wa mistari.

Katika kila sura lazima tusome Biblia kwanza na kujaribu kutambua somo (aya), kisha tulinganishe na matoleo ya kisasa. Ni pale tunapoelewa kusudi la asili la mwandishi kwa kufuata mantiki yake na jinsi alivyojieleza tunaielewa kwa Biblia kiukweli. Ni mwandishi wa asili tu aliyevuviwa — wasomaji hawana haki ya kurekebisha ujumbe. Wasomaji wa biblia wana wajibu wa kutumia ukweli uliovuviwa kwenye siku na maisha yao.

Fahamu kwamba maneno yote ya kiufundi na vifupisho vimefafanuliwa kwa kirefu kwenye nyaraka zifuatazo: Maelezo Fasaha Ya Muundo Wa Sarufi Za Kiyunani (Brief Definitions of Greek Grammatical Structure), Uhakiki Wa Tofauti Za Kiandishi (Textual Criticism), Ufafanuzi na Maelezo ya Kimaandiko (Glossary).

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka "Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 1:1**
***1* Mwanzo wa Injili ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.**

**1:1 "Mwanzo"** Je tungo hii ya utangulizi inarejerea

1. mwanzo kabisa wa Mwanzo. 1:1 na Yohana 1:1
2. mwanzo wa Yesu kuvaa mwili kama ilivyo katika 1 Yohana 1:1
3. mwanzo wa huduma ya Yesu ya Wazi (yaani uzoefu binafsi wa Petro)

Aya ya kwanza kibayana inarejerea unabii wa Agano la Kale juu ya Masihi kutoka kwa Isaya. Hadithi ya Injili inaanza katika desturi ya kinabii ya Israeli. Nukuu katika Marko 1:2 na 3 ni muunganiko wa Mal. 3:1 na Isa. 40:3.

## MADA MAALUMU: *ARCHĒ*

Neno la Kiyunani archē linamaanisha "mwanzo" au "asili" ya kitu.

1. mwanzo wa mpangilio ulioumbwa (kama vile. Yohana 1:1; Ebr. 1:10)
2. mwanzoni mwa injili (kama vile Mk. 1:1; Flp. 4:15; 2 The. 2:13; Ebr. 2:3; 1 Yohana 1:1)
3. mwanzo wa jicho la kwanza la ushahidi (kama vile Luka 1:2)
4. mwanzo wa dhambi (miujiza, kama vile. Yohana 2:11)
5. mwanzo wa mafundisho (kama vile Ebr. 5:12)
6. mwanzo wa udhihirisho uliojikita katika kweli ya injili (kama vile. Ebr. 3:14)
7. mwanzo, Kol. 1:18; Ufu. 3:14

Ilikuja kutumika juu ya "utawala" au "mamlaka"

1. juu ya wanadamu rasmi watawalao
   a. Luka 12:11
   b. Luka 20:20

c. Warumi 13:3; Tito 3:1
2. juu ya mpangilio wa mamlaka
    a. Warumi 8:38
    b. 1 Kor. 15:24
    c. Efe. 1:21; 3:10; 6:12
    d. Kol. 1:16; 2:10,15

◙**"wa Injili"** Pamoja na Marko yawezekana ni injili ya kanza kuandikwa, haya ni matumizi ya kwanza ya neno *euangelion* (kama vile Marko 1:14,15; 8:35; 10:29; 13:10; 14:9) na mwandishi wa Injili (Matumizi ya Paulo katika Gal. 2:2 na 1 The. 2:9 ingefuata mtiririko mapema). IKibayana ni "habari njema" au "ujumbe mwema." Hii kibayana inaaksi Isa. 61:1 na yawezekana 40:9 na 52:7. Toleo la *Jerome Biblical Commentary* inasema "matumizi ya Marko ya neno 'injili' ni sawasawa na ile ya Paulo inayoweza kumaanisha aidha tendo la kutangaza au maudhui ya kile kinachotangazwa" (ukurasa wa 24).

◙**"ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu"** Muundo wake wa kisarufi unaweza ukaeleweka kama (1) ujumbe uliotolewa na Yesu au (2) ujumbe juu ya Yesu. Hii ya 2 inawezekana kuwa maana iliyokusudiwa. Hatahivyo, the *Dictionary of Jesus and the Gospels*, kilichochapishwa na IVP, kinasema "Kishamirisho cha ('ya') yawezekana ni vyote viwili ya umilikishi binafsi na yenye lengo kusudiwa: Yesu natangaza injili na injili yake inaelezea maisha yake" (ukurasa wa 285).

Mstari wa 1 si sentensi iliyokamilika. Inawezekana ni kichwa cha habari cha kitabu. Maandiko ya kale ya Kiyunani א, A, B, D, L, na W yanaongeza tungo "Mwana wa Mungu" Inayofuatiwa na matoleo ya NKJV na NRSV, TEV, na NIV, wakati linakosekana katika (1) 2) ;*א) toleo la kishamu la Kipalestina; (3) au toleo moja la Koptiki; (4) Toleo la ki-Georgia; sawasawa pia kutoka (5) Tafsiri ya ki-Armeni na (6) nukuu ya andiko hili kutoka katika fasiri ya Origen juu ya Yohana. Toleo la UBS[4] linatoa mjumuisho wa alama "C" (ngumu kuamua). Angalia Mada maalum juu ya "Mwana wa Mungu" katika Marko 3:11.

Ni ngumu kwa wakristo wa kisasa wanaopenda na kuiamini Biblia kuuzipa umaana tafsiri hizi mabali mabali za maandiko ya Kiyunani, lakini ni ngumu kama itakavyoonekana kwa madhanio yetu juu ya uvuvio na utunzaji wa ufunuo binafsi wa Mungu, ni halisia. Nyongeza hii hata inaonekana ni ya kimakusudi, wala si kwa bahati mbaya. Waandishi wa kwanza wa ki-Orthordox walikuwa makini juu ya maoni ya kiuvumi juu ya Yesu, kama vile uasilishaji ambao ulielezea kwamba Yesu alifanyika Mwana wa Mungu. Waandishi hawa wa kale mara kwa amara walirekebisha maandiko ya Kiyunani kwa kuyanakili ili kuyafanya yawe ya ki-orthordox kithiolojia (kama vile 1 Yohana 5:7-8). Kwa ajili ya kusoma na kujifunza zaidi juu ya marekebisho haya ya kimakusudi yanayosumbua ya maandiko ya Kiyunani angalia Bart D. Ehrmans' *The Orthodox Corruption of Scripture*. Kibayana anajadili Marko 1:1 katika kurasa za 72-75.

◙**"ya Yesu"** Siku zote katika Uyahudi wa karne ya kwanza baba alitoa jina kwa mtoto. Katika namna hiyo hiyo Baba wa Mbinguni, kupitia malaika, alitoa jina kwa mtoto. Majina yote ya Kiyahudi yalibeba maana ya uwakilishi; hili halikuwa tofauti na mengine. Yesu ni muunganiko wa nomino mbili za Kiebrania: (1) YHWH na (2) wokovu. Maana inapatikana katika Mt. 1:21. Yesu ni fasiri ya Kiyunani ya jina la Kiebrania Yoshua. Alithibitisha kuwa Musa mpya, Yoshua mpya na Kuhani Mkuu mpya.

◙**"Kristo"** Hii ni fasiri ya Kiyunani ya jina la Kiebrania "Masihi," ambalo linamaanisha "mpakwa mafuta." Katika Agano la Kale Mungu aliwapaka mafuta viongozi (yaani manabii, makuhani na wafalme) iliashiria wito wake na kuwezeshwa kwa ajili ya jukumu alililopewa. Neno "Masihi" halitumiki mara kwa mara katika Agano la Kale (kama vile Dan. 9:25,26 kwa ajili ya mfalme wa matukio ya siku za mwisho), lakini dhana kwa hakika ipo. Inafanana na ya Mt. 1:1, "Mwana wa Daudi," ambayo inarejerea uzao wa kifalme wa mfalme mteule wa Israeli "Daudi." Mungu alimuahidi Daudi katika 2 Samweli 7 kwamba mmoja wa uzao wake siku zote atatawala katika Israeli. Ahadi hii ilionekana kuvunjwa na uharibifu wa Kibabeli

wa Yerusalemu na kuchukuliwa kwa wakazi wake (yaani mnamo 586 k.k.). Hatahivyo, manabii walianza kuona uzao wa baadaye wa ki-Daudi (yaani Isaya, Mika, Malaki). Yesu ni "mwana wa Daudi," aliyehaidiwa "mwana wa adamu" (kama vile Dan. 7:13), na "mwana wa Mungu" (imetumika mara tano katika Marko).

Inashangaza kwamba sehemu pekee katika injili yote ambapo maelezo ya "Yesu Kristo" inatumika katika mstari wa ufunguzi (ni mara mbili tu katika Mt. na Yohana  haipo kabisa katika Luka). Mara nyingi, Marko anatumia "Yesu." Matumizi haya yanashabihiana na msisitizo wa kithiolojia wa Marko juu ya ubinadamu wa Yesu, wakati uungu wa wake unafichwa (yaani siri ya Kimasihi) mpaka ukamilishaji Wake wa misheni ya Kimasihi (yaani Mtumishi Atesekaye). Haipo mapaka kitabu cha Matendo ya Mitume ambapo "Yesu Kristo" linakuwa jina linalojirudia rudia.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 1:2-8**
**[2] Kama ilivyoandikwa katika nabii Isaya, Tazama, namtuma mjumbe wangu Mbele ya uso wako, Atakayeitengeneza njia yako. [3] Sauti ya mtu aliaye nyikani, Itengenezeni njia ya Bwana, Yanyosheni mapito yake. [4] Yohana alitokea, akibatiza nyikani, na kuuhubiri ubatizo wa toba liletalo ondoleo la dhambi. [5] Wakamwendea nchi yote ya Uyahudi, nao wa Yerusalemu wote, wakabatizwa katika mto wa Yordani, wakiziungama dhambi zao. [6] Na Yohana alikuwa amevaa singa za ngamia na mshipi wa ngozi kiunoni mwake, akala nzige na asali ya mwitu. [7] Akahubiri akisema, Yuaja nyuma yangu aliye na nguvu kuliko mimi, ambaye mimi sistahili kuinama na kuilegeza gidamu ya viatu vyake. [8] Mimi niliwabatiza kwa maji; bali yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu.**

**1:2 "Kama ilivyoandikwa"** Neno "imeandikwa" ni njeo ya wakati mtimilifu, ambayo ilikuwa ni nahau iliyotumika kuashiria ufunuo wa milele wa Mungu (yaani maandiko).

◙ **"katika nabii Isaya"** Nukuu hii ni muunganiko wa Mal. 3:1 na Isa. 40:3. Haitokani na Maandiko ya Kimasoreti au Tafsiri ya Agano la Kale ya Kiyunani ya Isa. 40:3. Kwasababu ya hii baadhi ya waandishi walibadili maadishi kuwa "ilivyoandikwa katika manabii" (yaani katika kipengele cha Manabii cha Kanoni ya Agano la Kale). Umoja unapatikana katika maandiko ya Kiyunani א, B, L na D, lakini wingi upo katika MSS A, na W. Isaya 40-66 zina msisitizo mkubwa katika matukio ya siku za mwisho: (1) Mtumishi atesekaye (yaani haswa Isa. 52:13-53:12) na (2) zama mpya za Roho (haswa Isaya 56-66). Katika ufunguzi unaofuata wa Marko kuna maelezo kadhaa kwa Isaya.

◙ **"namtuma mjumbe wangu Mbele ya uso wako"** Neno "mjumbe" linaweza kurejerea kwa malaika (kama vile Kutoka. 23:20a, ambayo yangekuwa maelezo mengine kwa Kutoka), lakini hapa inarejerea kwa "mjumbe" (kama vile Mal. 3:1). Hii linaweza kuwa mzaha juu ya jina la Injili (yaani habari njema). Hii ni moja ya nukuu chache za Agano la Kale katika Marko ambalo liliandikwa kimsingi. Inarejerea kwa huduma ya Yohana (kama vile Marko 1:4). Inaonesha kwamba desturi ya kinabii ya Agano la Kale inatimilizwa (Hii pia inaaksiwa pia katika uponyaji wa Yesu na upungaji pepo,ambayo pia ni unabii wa kimasihi katika Isaya). Huduma ya Yohana Mbatizaji unatajwa katika Injili zote nne.

**1:3 "'Sauti ya mtu aliaye nyikani '"** Hii ni nukuu ya Isa. 40:3 kutoka katika vyanzo visivyojulikana. Neno "jangwa" inamaanisha sehemu ya ardhi ya malisho isiyokaliwa na watu kuliko sehemu kavu, uvumo wa upepo, jangwa la mchanga.

◙ **"'Itengenezeni njia ya Bwana'"** Hii ni kauli tendaji shurutishi isiyo timilifu, ambayo inaashiria uharaka. Katika Toleo la MT, Bwana (yaani, *adon*) inasomwa, lakini YHWH (Bwana) katika mandiko ya kiebrania. Tungo kiasili inarejerea maandalizi ya kimwili kwa utembeleo wa kifalme (kama vile Isa. 57:14; 62:10). Ilikuja kurejerea kisitiari kwa huduma ya Yohana Mbatizaji kiroho akiandaa njia kwa ajili ya Yesu Masihi ambaye pia anaitwa "Bwana" (iyaani, *kurios*).

◙ **"'Yanyosheni mapito yake'"** Toleo la MT na LXX yana "yanyosheni mapito ya Mungu wetu." Marko (au Petro) lilirekebisha andiko (au inanukuu kutoka muundo wa andiko usiojulikana) kufanya kibayana ifanane na Yesu, sio YHWH.

**1:4 "Yohana Mbatizaji"** Kwanini Yohana abatize na maji?

1. Agano la Kale linaweka mfano wa kuashiria ufunguzi wa "agano jipya" (kama vile Kutoka. 19:10,14; Isa. 1:16; Yer. 31:34; Ezek. 36:25)
2. tendo la kutakasa kutoka katika kutiwa unajisi wa kisherehe (kama vile Mambo ya Walawi 15).
3. sitiari ya kinabii ya matukio ya siku za mwisho yay a utoaji wa maji ya uhai kutoka kwa Mungu (mfano, Isa. 12:2-3; Yer. 2:13; 17:13; Ezek. 47:1; Zek. 13:1; 14:8; Ufunuo. 22:1)
4. uigilizaji wa ubatizo wa kilawi kama ibada ya uingizwaji kufanyika sehemu ya watu wa Mungu
5. Njia ya kiualimu wa kiyahudi ya kuandaa mahujaji wote kukabili YHWH katika Hekalu (yawezekana kwa kuzamishwa, kama vile Miqvaot tractate katika *Mishnah*). Ibada ya uogaji bado inafanyiwa kazi na Waislamu kabla ya kuingia msikitini.

◙ **"alitokea"** Hii inaweza ikawa njia ya Marko ya kuelezea kwa unabii ya kutokea kwa kushangaza kwa Eliya kabla "kutokea ghafla" kwa Masihi (kama vile Mal. 3:1).

◙ **"akihubiri"** Hili ni neno "kufanyika ishara" (*kērussō*), ambayo inamaanisha "kutangaza ujumbe kwa upana wa au kwa uwazi" (kama vile Marko 1:4,7,14,38,39,45). Marko haitumii muundo wa kitenzi cha injili (*euaggelizō).* Yohana alikuja kuhubiri ubatizo wa toba (angalia Mada Maalum). Ujumbe huu uliendelea na Yesu, lakini kwa msisitizo wa nyongeza wa "imani" (angalia Mada Maalum katika Marko 1:15). Agano pacha linahitaji toba na imani inayoonyeshwa na ubatizo kufanyika kitu cha mahubiri ya kitume (yaani *kerygma*)

1. Petro
   a. mahubiri ya kwanza ya kanisa (Mdo. 2:37-39)
      (1) tubu
      (2) kubatizwa
   b. mahubiri ya pili ya kanisa (Mdo. 3:16,19)
      (1) imani
      (2) kutubu
2. Philipo (Mdo. 8:12)
   a. amini
   b. kubatizwa
3. Paulo
   a. mfungwa kwa kifilipi (Mdo. 16:31,33)
      (1) kuamini
      (2) kubatizwa
   b. kwaheri kwa ajili ya wazee wa Waefeso (Mdo. 20:21)
      (1) toba kumuelekea Mungu
      (2) imani katika Kristo
   c. ushuhuda wa Agrippa (Mdo. 26:18)
      (1) kugeuka kutoka gizani (Shetani), yaani kutubu
      (2) kuelekea nuru (Mungu)

Kwangu mimi mahitaji ya Agano Jipya ni

1. tubu
2. amini
3. tii
4. shindania

Lengo la Agano Jipya katika kufanana na Kristo sasa ili kwamba wengine wataona mabadiliko na kuvutwa kwa imani katika Kristo!

◙ **"ubatizo wa toba"** Ubatizo sio kigezo cha msamaha, lakini fursa kwa ukiri wa wazi wa waamini. Hili si tendo la kisakramenti, lakini mtazamo mpya kuelekea dhambi na uhusiano mpya pamoja na Mungu. Ni ishara ya nje ya mabadiliko ya ndani.

## MADA MAALUM: TOBA (AGANO LA KALE)

Dhana hii ni ya muhimu sana lakini ni vigumu kuitolea ufafanuzi. Wengi wetu tunao ufafanuzi ambao unatokana na ushirikishwaji wa kimadhehebu. Hata hivyo, mara nyingi huu "mwelekeo" wa ufafanuzi wa kithiolojia unalazimisha maneno kadhaa ya Kiebrania (na Kiyunani) ambayo kwa upekee wake hayamaanishi "elekea" ufafanuzi huu. Lazima ikumbukwe kwamba waandishi wa kitabu cha Agano la Kale (isipokuwa Luka) walikuwa wanafikra wa Kiebrania waliotumia maneno ya lugha ya Koine ya Kiyunani, hivyo sehemu ya kuanzia ni ile ya maneno yenyewe ya Kiebrania, ambayo kimsingi ni mawili.

1. *nacham* ( BDB 636, KB 688)
2. *shub* ( BDB 996, KB 1427)

Neno la kwanza, *nacham*, kiuhalisia linaonekana kumaanisha "kueleza pumzi ya ndani" linatumika katika maana kadhaa.

a. "kupumzika" au "kufariji" (m.f. Mwa. 5:29; 24:67; 27:42; 37:35; 38:12; 50:21; mara nyingi linatumika katika majina, kama vile 2 Fal. 15:14; 1 Nya. 4:19; Neh. 1:1; 7:7; Nahumu 1:1)
b. "kuhuzuka" (m.f. Mwa. 6:6,7)
c. "kughairi" (m.f. Kut. 13:17; 32:12,14; Hes. 23:19; Ayubu 42:5-6)
d. "huruma" (m.f. Kut. 32:36)

Tambua kwamba haya yote yanahusisha hisia za ndani! Hapa ndipo palipo na ufubuzi: hisia za ndani ambazo huelekea katika tendo. Badiliko hili la tendo mara kwa mara huelekezwa kwa watu wengine, lakini pia kuelekea kwa Mungu. Ni hili badiliko la mtazamo na tendo kumwelekea Mungu ambalo hukazia neno hili kwa umuhimu huu wa kithiolojia. Lakini hapa ungalifu lazima ufanyiwe kazi. Mungu anasemekana "kutubu" (kama vile Mwa. 6:6, 7; Kut. 32:14; Amu. 2:18; 1 Sam. 15:11, 35; Zab. 106:45), lakini hili si matokeo ya sononeko juu ya dhambi au makosa, bali ni njia ya kiaandiko ya kuonyesha huruma ya Mungu na uangalifu (kama vile Hes. 23:19; 1 Sam. 15:29; Zab. 110:4; Yer. 4:27-28; Eze.24:14). Adhabu istahiliyo dhambi na uasi inasamehewa ikiwa mtenda dhambi ameamua kwa usahihi kuongoka kutoka dhambini kwake/kwao na kurudi kwa Mungu. Huu ni uthamanisho mpya wa maisha.

Neno la pili, *shub*, linamaanisha "kurudi" (kurudi kutoka, kurejea, kurudi kwa). KITENZI *shub* (BDB 996, KB 1427) kimsingi kinamaanisha "kugeuka" au "kurejea tena" Kitenzi hiki kinaweza kutumika kwa

1. kumuelekea Mungu, Hes. 14:43; Yos. 22:16,18,23,29; Amu. 2:19; 8:33; 1 Sam. 15:11; 1 Fal. 9:6; Yer. 3:19; 8:4
2. kumrudia Mungu, 1 Fal. 8:33,48; 2 Nya. 7:14; 15:4; 30:9; Zab. 51:13; 116:7; Isa. 6:10; 10:21,22; 31:6; Yn. 4:6,8-11 (tambua hasa Yeremia 7 na Amosi 4)
3. YHWH anamwambia Isaya hapo awali kwamba Yuda haitaweza/isingeweza kutubu (kamavile Isa. 6:10), lakini si mara ya kwanza katika kitabu hiki, Yeye anawahita warudi Kwake.

Toba si hisia nyingi sana kama ulivyo mtazamo kumwelekea Mungu. Huu uthamani mpya wa maisha kutoka upekee kuelekea Kwake. Hii inadokeza utayari wa kubadilika na kubadilishwa. Si ukomavu kamili kuihusu dhambi, bali ukomavu wa uasi unaojulikana! Huu ni ukinyume wa matokeo yaliyo kitovu Anguko la Mwanzo 3. Hiii inadokeza kwamba sura na ufanano wa Mungu (Mwa. 1:26-27), ingawa iliharibika, umerejeshwa! Ushirika pamojana Mungu kupitia mwanadamu aliyeanguka inawezakana kurejeshwa tena.

Toba katika Agano la Kale kimsingi inamaanisha "badiliko la tendo," ambapo "toba" katika Agano Jipya inamaanisha "badiliko la fikra" (tazama Mada Maalum: Toba [Agano Jipya]). Yote haya ni muhimu kwa ajili ya toba ya kweli ya kibiblia. Pia ni muhimu kutambua kwamba toba ni vyote tendo la awali na hatua endelevu. Tendo la awali linawezakuonekana katika Marko 1:15; Matendo ya Mitume 3:16 na 19; 20:21, ambapo hatua endelevu inaweza

kuonekana katika 1 Yohana 1:9; Ufunuo 2 na 3. Toba si uchaguzi (kama vile Luka 13:3,5)!

Ikiwa ni kweli kwamba mahitaji ya maagano mawili ni "toba" na "imani" (m.f. Mt. 3:2; 4:17; Marko 1:4,15; 2:17; Luka 3:3,8; 5:32; 13:3,5; 15:7; 17:3), kisha neno *nacham* linarejea juu ya hisia zenye nguvu za kutambaua dhambi ya mtu na kugeuka kutoka ndani ya hiyo dhambi, ambapo neno *shub* lingaliweza kurejea juu ya kurudi toka dhambini na kumwelekea Mungu (moja ya mfano wa haya matendo ya kiroho uko katika Amosi 4:6-11, "hamkunirudia mimi" [mara tano] ana Amosi 5:4,6,14, "Nitafuteni mimi. . .Mtafuteni Bwana. . .Tafuteni mema, wala si mabaya").

Mfano wa kwanza ulio mkuu wa nguvu ya toba ni ile dhambi ya Daudi Bathsheba (kama vile 2 Samweli 12; Zaburi 32,51). Kulikuwa na matokeo endelevu kwa Daudi, familia yake, na Israeli, lakini Daudi alirejeshwa katika ushirika pamoja na Mungu! Hata Manase aliyekuwa dhalimu aliweza kutubu na kusamehewa (kama vile 2 Nya. 33:12-13).

Maneno yote haya yanatumika kwa usawa katika Zab. 90:13. Lazima kuwepo na utambuzi wa dhambi na nia iliyokusudiwa, kurudi kwa mtu binafsi kuto dhambini, pamoja na shauku ya kumtafuta Mungu na haki Yake (kama vile Isa. 1:16-20). Toba ni hatua tambuzi, hatua binafsi, na hatua ya kimaadili. Haya yote yanahiajika, yote ni kwa ajili ya kuanza uhusiano mpya pamoja na Mungu na kuushikilia uhusiano huo mpya. Hisia za ndani za majuto hurejesha ndani ya utele wa uaminifu kwa Mungu na kwa ajili ya Mungu!

◙ **"kwa ajili ya ondoleo la dhambi"** Neno "msamaha" kibayana inamaanisha "kuondoa. Hii ni moja ya maneno ya Kibiblia kwa msamaha. Lina muunganiko wa kisitiari Siku ya Upatanisho wa Agano la Kale (kama vile Mambo ya Walawi 16) ambapo moja ya mbuzi maalumu wawili inaondolewa kutoka katika kambi ya Israeli, kiishara kuchukua dhambi (kama vile Law. 16:21-22; Ebr. 9:28; 1 Pet. 2:24). Tungo "ya dhambi" ni kishamirisho milikishi.

**1:5 "Wakamwendea nchi yote ya Uyahudi, nao wa Yerusalemu wote"** Huu ni utiaji chumvi kulikopitiliza (yaani utiaji chumvi), lakini inaonesha athari kubwa kwa mahubiri ya Yohana. Alikuwa sauti ya kwanza ya kinabii kutokea Malaki kama miaka 400 kabla. Hii ni njeo ya wakati usio timilifu ambao unamaanisha kwamba watu waliendelea kuja kwasababu walitambua Yohana kama nabii.

◙ **"wakibatizwa"** Hii pia ni njeo ya wakati usio timilifu ambayo inazungumzia kitendo endelevu kwa wakati uliopita. Wayahudi wengi walihisi siku mpya siku mpya wa shughuli za Mungu na walikuwa wakijiandaa kwa ajili ya hilo.

◙ **"wakitubu dhambi zao"** Hii ni kauli ya kati wakati uliopo endelevu, ambayo kibayana inamaanisha “kusema kilekile." Hii ilikuwa ukiri wao wa umma wa hitaji kwa ajili ya msamaha wa kiroho. Kuna maana kwamba ikiwa Wayahudi hawa wangetubu na kubadili mitindo yao ya maisha, YHWH angewasamehe dhambi zao (kama vile Marko 1:4; Mt. 3:6; Luka 3:3). Hii hakika ni utaratibu wa Agano la Kale. Inajumuisha msamaha kamili kupitia toba, imani, mabadiliko ya mtindo wa maisha na sasa ubatizo kama uwakilishi wa nje! Huu utaratibu wa Agano la Kale inarekebishwa na huduma ya Kimasihi ya Yesu. Vitu hivi bado vina mantiki, lakini sasa imani ya kibinafsi katika Yesu kama Kristo ni jambo kuu (kama vile 2:38; 3:16,19; 20:21). Injili nne zinatengeneza kipindi cha mpito. Marko 1:14-15 kiko katika Yohana Mbatizaji, lakini kithiolojia inatabiri kwa mbele ujumbe wa injili uliokamilika (yaani, kutubu, kuamini na kuishi maisha mapya). Jambo kubwa ni vile Yesu ni nani! Yeye ni mwakilishi wa YHWH, mfunuaji, na wakala wa ukombozi na hukumu. Hii ni sababu kwa Siri ya Ki-Masihi katika Marko. Yesu ni Mungu kamili kutoka mwanzoni kabisa (yaani kutungwa kwa bikra), lakini hii haikudhihirishwa kamili mpaka baada ya ufufuo na kupaa.

## MADA MAALUMU: KUTUBU (AGANO JIPYA)

Toba (sambamba na imani) ni hitaji la pande zote mbili yaani Agano la Kale (Nacham, BDB 636, KB 688, mf., Kut.

13:17; 32:12,14; Shuv, BDB 996, KB 1427, m.f. 1 Flm. 8:47; Eze. 14:6; 18:30; tazama Mada Maalumu: Toba [Agano la Kale]) na Agano Jipya.

1. Yohana Mbatizaji (Mt. 3:2; Marko 1:4; Luka 3:3,8)
2. Yesu (Mt. 4:17; Marko 1:15; Luka 5:32; 13:3,5; 15:7; 17:3)
3. Petro (Matendo 2:38; 3:19; 8:22; 11:18; 2 Petro. 3:9)
4. Paulo (Matendo 13:24; 17:30; 20:21; 26:20; Rum. 2:4; 2 Kor. 2:9-10)

Lakini Toba ni nini? Ni huzuni ya kiroho? Ni kumaanisha kuacha dhambi? Eneo zuri katika Agano la Jipya katika kuelewa maana tofauti ya dhana hii ni 2 Wakorintho 7:8-11, ambapo hizo tatu zinanahusiana, lakini ni tofauti, maneno ya Kiyunani yanatumiika.

1. "huzuni" (*lupeō*, kama vile. mst. 8 [mara mbili], 9 [mara tatu], 10 [mara mbili], 11). Inamaanisha kupata maumivu au kutambua na ina maana ya kitheolojia isiyofungamana na upande wo wote.
2. "toba" (*metanoeō*, kama vile mst. 9,10). Ni muunganiko wa neno "baada ya" na "kumbukumbu," ambayo inadokeza akili mpya, njia mpya ya kufikiri, mtazamo mpya kuhusu maisha na Mungu. Hii ni toba ya kweli.
3. "majuto" (*metamelomai*, kama vile mst. 8 [mara mbili], 10). Ni muungano wa "baada ya" na "uangalifu." Linatumika juu ya Yuda katika Mt. 27:3 na Esau katika Ebr. 12:16-17. Linadokeza sikitiko juu ya matokeo, si juu ya matendo. Toba na imani ni matendo ya kimaagano yanayohitajika (kama vile Marko 1:15; Matendo 2:38,41; 3:16,19; 20:21). Kuna baadhi ya maandiko ambayo yanadokeza kwamba Mungu hutoa toba (kama vile Matendo 5:31; 11:18; 2 Tim. 2:25). Lakini maandiko mengi yanalitazama hili kama mwitikio muhimu wa agano la mwanadamu kwa majitoleo ya Mungu ya wokovu huru.

Maelezo ya maneno yote ya Kiebrania na Kiyunani yanahitajika ili kuelewa maana kamili ya toba. Neno la Kiebrania linadai "mabadiliko ya tendo," ambapo neno la Kiyunani linadai "mabadiliko ya akili." Mtu aliyeokolewa anapokea akili na moyo mpya (kama vile Eze. 36:26-27). Anafikiri tofauti na kuishi tofauti. Badala ya "Kilicho ndani ni kwa ajili yangu?" sasa swali ni "Mapenzi ya Mungu ni nini?" Toba si hisia ambazo hufifia au dhambi ya moja kwa moja, bali uhusiano mpya na Aliye Mtakatifu ambaye humbadilisha mwamini kwa uendelevu na kuwa ndni ya utakatifu. Si rahisi mtu akasitisha kufanya kitu au kuachana nacho, bali ni kwa mtazamo na uelekeo mpya katika maisha. Anguko linatusabisha sisi kujitazama wenyewe lakini injili inaturuhusu sisi kumtazama Mungu. Toba ni tendo la kugeuka na imani ni tendo la kugeukia kitu/kifikra!

**1:6 "Yohana alikuwa amevaa mavazi ya Singa za ngamia"** Haya yalikuwa mavazi yake ya kawaida ya kila siku (yaani kauli ya kati endelevu ya wakati kamilifu). Hii haikuwa ngozi ya ngamia, lakini iliyoungwa kutokana na manyoya yake (kama vile 2 Wafalme. 1:8; Mt. 3:4). Alikuwa mtu tu wa jangwa na nabii (kama Zek. 13:4). Yohana alivaa kama Eliya, ambaye Mal. 3:1 na 4:5 alisema angekuwa mtangulizi wa Masihi.

◙ **"nzige na asali"** Hiki kilikuwa chakula halisi cha watu wa jangwani. Nzige walikuwa kilawi wasafi na chakula kinachokubalika (kama vile Law. 11:22). Alikula ambacho kwa asili kilikuwa kinapatikana.

**1:7** Mstari huu na Marko 1:8 inaonesha maudhui ya maandalizi ya ujumbe wa Yohana. Alitambua kazi yake na nafasi yake kuhusiana wa Mungu Ajaye (kama vile Yohana 3:30). Alijiskia yeye mwenyewe kuwa mtumwa, mtumishi (yaani watumwa tu waliowavua wengine). Kushuka kwa Yohana binafsi inaandikwa katika injili zote nne (kama vile Mt. 3:11; Luka 3:16; na Yohana 1:27; pia katika mahubiri ya Paulo 13:25). Yawezekana hii ilijumuisha na waandishi wa injili kwasababu ya uvumi uliofuatia baadaye kwa Yohana Mbatizaji (kama vile Mdo. 18:24-19:7).

**1:8 "naliwabatiza ninyi kwa maji"** Kumbuka, ubatizo wa Yohana ulikuwa umeandaliwa. Hii hairejerei ubatizo wa Kikristo. Yohana alikuwa nabii wa mwisho wa Agano la Kale (kama vile Luka 16:16), muhubiri wa kupita sio muhubiri wa kwanza wa injili (kama vile Luka 16:16; Mdo. 19:17). Yeye kama nukuu kutoka Isaya anaunganisha agano la kale na agano Jipya.

◙ **"Atawabatiza ninyi kwa Roho Mtakatifu"** Hii inatofautiana na ubatizo wa Yohana. Masihi ataanzisha zama mpya za Roho. His baptism will be withUbatizo wake utakuwa na (au "ndani ya" au "kwa") Roho. Kumekuwepo na mjadala mkubwa kati ya madhehebu kuwa inamaanisha nini katika uzoefu wa Kikristo. Baadhi wanalichukulia kumaanisha hali ya

kutiwa nguvu baada ya wokovu, namna fulani ya Baraka ya pili. Kibinafsi nafikiria inarejerea kufanyika mkristo (kama vile 1 Kor. 12:13). Sikatai kujazwa kwa baadaye na uwezesho lakini ninaamini kuna ubatizo mmoja wa kuanzia wa kiroho katika Kristo ambamo waamini wanajitanabaisha na kifo cha Yesu na ufufuo (kama vile Rum. 6:3-4; Efe. 4:5; Kol. 2:12). Hii kazi ya kuanzia ya Roho inaelezwa katika Yohana 16:8-11. Kwa uelewa wangu kazi za Roho Mtakatifu ni:

1. kushihudia juu ya dhambi
2. kufunua ukweli kuhusu Kristo
3. kupelekea kukubalika kwa Injili
4. kubatizwa katika Kristo
5. kumshuhudia mwamini juu ya dhambi inayoendelea
6. kutengeneza kufanana na Kristo ndani ya mwamini

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 1:9-11**
**9 Ikawa siku zile, Yesu alikuja kutoka Nazareti ya Galilaya, akabatizwa na Yohana katika Yordani. 10 Mara alipopanda kutoka majini, akaona mbingu zinapasuka, na Roho, kama hua, akishuka juu yake; 11 na sauti ikatoka mbinguni, Wewe ndiwe Mwanangu, mpendwa wangu; nimependezwa nawe.**

**1:9 "Yesu alikuja kutoka Nazareti ya Galilaya"** Yesu alizaliwa katika Bethlehemu ya Yudea, akaisha miaka michache katika Misri, na baadaye akakaa katika Nazareti, mji wa Yusufu na Maria ambao ulikuwa mdogo, makazi mapya ya Wayudea kaskazini. Huduma ya mwanzo ya Yesu ilikuwa katika eneo hili la kaskazini kuzunguka Bahari ya Galilaya, ambayo inatimiza unabii wa Isa. 9:1.

◙ **"Yesu. . .akabatizwa"** Injili zinatofautiana katika masimulizi yake ya awali ya huduma za Yesu katika Galilaya na Yudea. Inaonekana kwamba kulikuwa na huduma ya mapema ya wayudea na baadaye ingine, lakini mtiririko wa injili zote nne lazima uwekwe sawa ili uweze kuona maono haya ya mwanzo ya Wayudea (yaani Yohana 2:13-4:3). Kwanini Yesu alibatizwa siku zote imekuwa ni jambo linalofukuta kwa waamini kwasababu ubatizo wa Yohana ulikuwa ni ubatizo wa toba. Yesu hakuhitaji msamaha kwakuwa hakuwa na dhambi (kama vile 2 Kor. 5:21; Heb. 4:15; 7:26; 1 Pet. 2:22; 1 Yohana 3:5).
Nadharia hizi zimekuwa:

1. ilikuwa ni mfano kwa waamini kufuata
2. ulikuwa ni utambulisho Wake kwa hitaji la waamini
3. ilikuwa nikuwekwa wakfu na kuwezeshwa kwa ajili ya huduma
4. ilikuwa ni ishara kwa ajili ya jukumu lake la ki-ukombozi
5. ilikuwa ni uthibitishaji wake wa huduma na ujumbe wa Yohana mbatizaji
6. Ilikuwa ni utabiri wa kinabii wa kifo chake, maziko na ufufuo (kama vile Rum. 6:4; Kol. 2:12).

Haijalishi sababu, huu ulikuwa ni wakati mzuri wa maisha ya Yesu. Ingawa haimaanishi kwamba Yesu alifanyika Masihi katika wakati huu, jambo ambalo ni uvumi wa mwanzo wa uasilishaji (kama vile *The Orthodox Corruption of Scripture* by Bart D. Ehrman, kurasa za 47-118), ilikuwa na umuhimu mkubwa kwake Yeye.

**1:10**
**NASB, NKJV, "mara"**
**NRSV "punde"**
**TEV "mara moja"**
**NJB "ghafla"**

Hili ni neno linalozoeleka kuonekana katika Marko. Linaweka alama ya Injili yake. Hapa *euthus* inafasiriwa "kwa haraka" au "moja kwa moja" (kama vile Marko 1:10,12,18,20,21,20,28,42; 2:2,8,12; 3:6; 4:5,15,16,17,29;5:5,29,42; 6:25,27,45, 50,54; 7:35; 8:10; 9:15,20,24; 10:52; 11:3; 14:43,45; 15:1). Hili ni neno ambalo linatoa Injili ya Marko hisia ya haraka na kuwa ya kimatendo, jambo ambalo lingewapendezesha na kuwavutia Warumi. Kifungu hiki cha maneno kinatokea mara

47 katika Marko (kama vile *A Translator's Handbook on the Gospel of Mark* kilichoandikwa na Robert Bratcher na Eugene Nida, ukurasa wa 29).

◙ **"alipopanda kutoka majini"** Hii inaweza kuwa maelezo kwa Isa. 63:11, ambapo kwa asili ingerejerea Bahari ya Shamu (yaani safari mpya katika Yesu ambaye kwa muda mfupi angejaribiwa kwa siku arobaini kama Israeli kwa miaka arobaini). Mstari huu hauwezi ukatumiwa kama uhakikiwa andiko kwa ajili ya kuzamishwa. Katika muktadha inaweza kumaanisha kutoka ndani ya mto, na sio kutoka chini ya maji.

◙**"Akaona"** Hii inaweza kumaanisha kwamba ni Yesu tu aliyeona na kusikia ukiri wa ki-Masihi. Ikiwa ndivyo, hii ingeshabihiana katika maudhui ya sasa ya Siri za ki-Masihi za Marko inayojirudia rudia. Hatahivyo, injili zingine (kama vile Mt. 3:13-17; Luka 3:21-22).

◙ **"mbingu zikifunguka"** Haya yanaweza kuwa maelezo kwa Isa. 64:1. Neno hili linamaana ya kuachia wazi, ambayo ingekuwa sitiari kwa ajili ya kuchana wazi kizuizi cha juu cha nchi (kama vile Mwa. 1:6).

◙ **"Roho kama hua"** Asili ya sitiari hii inaweza kuwa

1. Roho ikitanda juu ya maji katika Mwanzo. 1:2
2. ndege waliotumwa na Nuhu nje ya Safina katika Mwa. 8:6-12
3. Matumizi ya walimu wa Kiyahudi kama ishara ya taifa la Israeli (kama vile Zab. 68:13; 74:19)
4. uwakilishi wa unyenyekevu na amani (kama vile Mt. 10:16)

Sababu moja ambayo binafsi nimejizatiti nayo kwa mbinu za historia ya kisarufi ya fasiri ya kibiblia ambayo inaweka shabaha juu ya kusudio la kiuandishi kama inavyoelezewa katika muktadha wa kifasihi, ni ujanja ujanja au njia za kiakili za wafasiri wa kale (na pia kisasa) walicheza na maandiko ili kulenga kushabihiana na muundo wao wa kithiolojia wa sasa. Kwa kuongeza thamani ya kimahesabu ya barua za neno la Kiyunani "hua" (*peristera*), ambayo ni sawasawa na 801, mtu anapata thamani ileile ya kimahesabu ya maneno ya Kiyunani *alpha* (sawasawa na 1) na *omega* (sawasawa na 800), hivyo hua ni sawasawa na Roho ya Kristo ya milele.Hili ni jambo lenye akili sana, lakini ni utambuzi wa maandiko, sio ufafanuzi wa maandiko!

◙ **"juu Yake"** Hiki ni kielezi *eis* ambacho kinamaanisha "ndani ya." Hailengi kumaanisha kwamba Yesu hakuwa ytayari na Roho Mtakatifu, lakini ilikuwa ni ishara maalumu inayoonekana ya uwezeshwaji wa Roho katika majukumu ya ki-Masihi aliyopewa. Hii inaweza pia kuwa maelezo kwa kutimilizwa kwake kwa unabii (kama vile Isa. 63:11). Marko anatumia kielezi "ndani ya" *(eis),* lakini Mathayo na Luka wanatumia "juu ya" (*epi*). Hii ni kwasababu Injili ya Marko ambayo haina simulizi za kuzaliwa wala kutembelewa, inaanza na huduma ya Yesu pamoja na tukio la ubatizo. Huu ufupisho wa uharaka ulitumika na makundi ya uvumishaji, wawasilishaji na wenye ujuzi kuelezea kwamba Yesu, mwanadamu wa kawaida alikuwa amewezeshwa pamoja na "Roho ya Kristo" kwa wakati huu na baadaye alikuwa na uwezo wa kufanya miujiza. Baadaye waandishi, hivyo kubadilisha kielezi kuwa "kuelekea" (*pros*).

## MADA MAALUM: UASILISHAJI (kufuru ya mwanzo)

Hii ilikuwa moja ya maoni ya kwanza ya uhusiano wa Yesu na Uungu kama Mungu kamili na wakati huo huo mwanadamu kamili (kama vile 1 Yohana 4:1-3). Kimsingi ilielezea kwamba Yesu alikuwa mwanadamu wa kawaida katika kila namna na alikuwa " ame asilishwa," "amechukuliwa" katika nmna maalumu na Mungu wakati wa ubatizo wake (kama vile Mt. 3:17; Marko 1:11) au wakati wa ufufuo wake (kama vile Rum. 1:4). Yesu aliishi maisha ya kipekee ambayo Mungu wakati fulani (ubatizo, ufufuo), [1] alimtwaa kama "Mwanawe" (kama vile Rum. 1:4; Flp. 2:9) au [2] "kutwaliwa," kama vile Zab. 2:7, ikinukuu katika Ebr. 1:5; 5:5, ikimrejerea Yesu. Hili lilikuwa kanisa la mwanzo na kufuru ya karne ya nane. Badala ya Mungu kufanyika mwanadamu (kuvaa mwili), kufuru inarudisha hili na sasa mwanadamu amefanyika Mungu! Inakataa Kuwepo kabla kwa Yesu (kama vile Yohana 1:1-2; 8:56-59; 16:28; 17:5; 2

Kor. 8:9; Flp. 2:6-7; Kol. 1:17; Ebr. 1:3; 10:5-8).
Ni ngumu kuelezea kwa vitendo namna gani Yesu, Mungu Mwana, alikuwa Mungu kabla, ulithawabiwa au kunakshiwa kwa maisha ya aina yake. Ikiwa alikuwa tayari ni Mungu? Ikiwa alikuwa na utukufu wa Kimungu tayari hapo mwanzo (yaani Yohana 1:1-2; Flp. 2:6) Kwa namna gani angetakiwa aheshimiwe zaidi? Ingawa ni ngumu kwetu kuelewa, Baba kwa namna fulani alimuheshimu Yesu kwa namna maalumu kwa utimilizwaji wake mkamilifu wa mapenzi ya Baba.

## MADA MAALUM: UJUZI WA KIPEKEE

Walimu wenye mafunuo ya uongo waliamini kwamba viumbwavyo, ulimwengu (maada) ni ovu, na kwahiyo katika upinzani wa ulimwengu wa roho, na kwamba roho tu ndiyo njema. Walijenga Mungu muovu na viumbe ya Agano la Kale kuelezea uumbaji wa ulimwengu (maada) na kumfanya Yesu Kristo kama Mungu kamili wa kiroho.

Imani za Walimu wajuzi wa uongo zinapingana kiukubwa na mafundisho yanayokubaliwa na mkristo. Ukristo unatufundisha kwamba wokovu unapatikana kwa kila mtu, sio wateule wachache na kwamba inakuja kutoka neema kupitia imani katika Yesu Kristo (Waefeso 2:8-9), na kutoka katika masomo au kazi. Chanzo cha ukweli ni Biblia tu, Ukristo unaelezea.

Walimu wa uongo walimngawanya kwa Yesu. Mtazamo mmoja ni kwamba alitokea tu kuwa na umbo lake la kibinadamu lakini kwamba alikuwa katika roho tu. Mtazamo mwingine uliweka wazi kwamba roho yake ya kiungu ilikuja juu ya mwili wake katika Ubatizo na kuondoka kabla ya kusulubiwa. Ukristo, kwa upande mwingine unashikilia kuwa Yesu alikuwa mwanadamu kamili na Mungu kamili na asili hizi zote zilikuwepo na muhimu kutoa sadaka ya kupendeza kwa dhambi ya ubinadamu.

**1:11 "sauti ikatoka mbinguni"** Walimu wa kiyahudi wanaita sauti ya kimbingu a *Bath Kol* (kama vile Marko 9:7), ambayo ilikuwa ni mbinu ya kuthibitisha mapenzi ya Mungu wakati wa kipindi cha kati ya Agano la Kale na Jipya ambapo hapakuwa na nabii. Hii ingeweza kuwa ni ukiri wenye nguvu sana wa kiungu kwa wale wote wenye kufahamu Uyahudi wa walimu wa kiyahudi.

◙ **"'Wewe ni Mwanangu Mpendwa'"** Majina haya mawili yanaunganisha vipengele vya Masihi (Zab. 2:7) kwa Mtumishi Atesekaye wa Isaya (Isa. 42:1). Neno "mwana" katika Agano la Kale lingerejerea (1) taifa la Israeli; (2) Mfalme wa Israeli; au (3) kuja kwa Mfalme Masihi kutoka kwa Daudi. Angalia Mada Maalum katika Marko 3:16. Tazama nafsi tatu za Utatu katika Marko 1:11: Roho, sauti kutoka mbinguni, na Mwana, mpokeaji wa vyote viwili.

## MADA MAALUMU: UTATU

Angalia kazi za watu hawa wote watatu katika mazingira ya pamoja. Neno "utatu," kwanza lilibuniwa na Tertallian, sio neno la Kibiblia, lakini dhana yake imesambaa sana.

A. Injili
   1. Mt. 3:16-17; 28:19 (na nyingine zinazoendana nazo)
   2. Yohana 14:26
B. Matendo-Mdo. 2:32-33, 38-39
C. Paulo
   1. Rum. 1:4-5; 5:1,5; 8:1-4,8-10
   2. 1 Kor. 2:8-10; 12:4-6
   3. 2 Kor. 1:21-22; 13:14
   4. Gal. 4:4-6
   5. Efe. 1:3-14,17; 2:18; 3:14-17; 4:4-6
   6. 1 The. 1:2-5
   7. 2 The. 2:13
   8. Tit. 3:4-6

D. Petro – 1 Pet. 1:2
E. Yuda-kur. 20-21

Uwingi wa Mungu umedokezwa katika Agano la Kale

A. Matumizi ya uwingi kumhusu Mungu
   1. Jina Elohim liko katika wingi (angalia mada maalumu: majina ya Uungu), lakini linapotumika kumhusu Mungu mara zote unakuta lina kitenzi kilichoko katika umoja.
   2. "Sisi" katika Mwa. 1:26-27; 3:22; 11:7
A. "Malaika wa Bwana" (angalia mada maalumu: Malaika wa Bwana) alikuwa mwakilishi wa Uungu aliyeonekana
   1. Mwanzo 16:7-13; 22:11-15; 31:11,13; 48:15-16
   2. Kutoka 3:2,4; 13:21; 14:19
   3. Waamuzi 2:1; 6:22-23; 13:3-22
   4. Zakaria 3:1-2
B. Mungu na Roho wake ni nafsi tofauti, Mwa. 1:1-2; Zab. 104:30; Isa. 63:9-11; Ezek. 37:13-14
C. Mungu (YHWH) na Masiha (Adonai) nao ni nafsi tofauti, Zab. 45:6-7; 110:1; Zak. 2:8-11; 10:9-12
D. Masiha na Roho Mtakatifu ni nafsi tofauti, Zak. 12:10
E. Wote watatu wametajwa katika Isa. 48:16; 61:1

Uungu wa Yesu na nafsi/haiba ya Roho vimesababisha matatizo kwa uhalisia, kwa wale wanaamini uwepo wa Mungu mmoja (angalia mada maalumu: wanaoamini uwepo wa Mungu mmoja), kwa waumini wa awali

1. Tertellian-ilimshusha Mwana kwa Babaye
2. Origin-aliishusha nafsi ya Uungu wa Mwana na Roho
3. Arius-anaukana Uungu wa Mwana na Roho
4. Watawa-waliamini katika ufanisi wa udhihilisho wa matukio ya Mungu mmoja kama Baba, Mwana, na Roho

Utatu ni kanuni anzilishi ya kihistoria iliyoelezewa na maneno ya Kibiblia.

1. Uungu kamili wa Yesu, ambao ni sawa na wa Baba, ulithibitishwa katika mwaka wa 325 B.K na baraza la Nicea (kama vile Yoh.1:1; Fil. 2:6; Tit. 2:13)
2. Nafsi kamili na Uungu wa Roho ambao ni sawa na wa Baba na Mwana ulithibitishwa katika mwaka 381 B.K na baraza la Constantino
3. Mafundisho ya Uungu yameelezewa kiundani katika kazi ya Augustine De Trinitate

Hakika kuna muujiza hapa. Lakini Agano Jipya linathibitisha nafsi moja ya Kiuungu (wanaoamini uwepo wa Mungu mmoja) ikiwa na udhihirisho wa nafsi tatu za umilele (Baba, Mwana, na Roho)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 1:12-13**
**12 Mara Roho akamtoa aende nyikani. 13 Akawako huko jangwani siku arobaini, hali akijaribiwa na Shetani; naye alikuwa pamoja na wanyama wa mwitu, na malaika walikuwa wakimhudumia.**

**1:12-13** Habari hii ya majaribu ya Yesu yanafupishwa sana ukilinganisha na Mt. 4:1-11 na Luka 4:1-13. Katika simulizi hizi kusudi la majaribu liko wazi: Namna gani Yesu angetumia nguvu Zake za Kimasihi kukamilisha jukumu lake la Ukombozi (kama vile James Stewart, *The Life and Teaching of Jesus Christ*, ukurasa wa. 39-46)? Lakini hadithi hii ya fupi ya Marko inaweza kuwa ilikuwa na maana gani? Inawezekana kwamba Petro aliona tukio hili kama uwakilishi wa Yesu kushindwa na uovu (yaani kuwezeshwa na Roho), kutabiriwa kwa Juma la Upendo. Lakini haya ni madhanio tu. Andiko lenyewe halitoi habari isipokuwa juu ya muda wa tukio—mara tu baada ya Yesu' (1) kuwezeshwa na Roho na (2) Ukiri unaofanywa na Baba, lakini mbele ya huduma ya wazi. Hii ni moja ya matukio matatu yanayotajwa kabla ya huduma ya wazi ya Yesu ([1] huduma ya Yohana; [2] ubatizo wa Yohana; na [3] majaribu ya Shetani).

**1:12 "Mara"** Angalia dokezo katika Marko 1:10.

◙ **"Mara Roho akamtoa aende nyikani"** Neno "impelled akamtoa" ni neno zito "kumtoa nje" (mara kwa mara ikitumika juu ya kupunga pepo, kama vile Marko 1:34,39; 3:15,22,23; 6:13; 7:26; 9:18,28,38). Kujaribiwa kwa mwana

kulisababishwa na yule muovu, lakini kwa kushamirishwa na Roho (kama vile Mt. 4:1-11; Luka 4:1-13). Ilikuwa mapenzi ya Mungu kwamba Yesu ajaribiwe! Ningependekeza vitabu viwili vizuri juu ya mada hii, *The Life and Teaching of Jesus* kilichoandikwa na James S. Stewart and *Between God and Satan* kilichoandikwa na Helmut Thielicke.

Katika Agano la Kale jangwa ilikuwa ni muda wa kuteswa kwa Israeli, lakini pia muda wa mahusiano ya upendo ya karibu. Walimu wa Kiyahudi waliita jangwa na kipindi cha kutangatanga kama fungate kati ya YHWH na Israeli. Eliya na Yohana Mbatizaji walikua katika Jangwa. Ilikuwa ni sehemu iliyojitenga kwa ajili ya mafunzo, tafakari na maandalizi kwa ajili ya huduma ya kiutendaji. Hiki kipindi kilikuwa muhimu kwa ajili ya maandalizi ya Yesu (kama vile Ebr. 5:8).

**1:13 "siku arobaini"** Hii inatumika kivyote vyote kibayana na kimafumbo katika Biblia. Inaashiria kipindi kirefu cha muda usio julikana (yaani, refu zaidi ya mzunguko wa mwezi, lakini fupi kuliko mabadiliko ya kimajira).

## MADA MAALUM: UWAKILISHI WA NAMBA KATIKA MAANDIKO

A. Namba fulani zilitenda kazi maeneo yote kama tarakimu na ishara.
   1. Moja – Mungu (yaani, Kumb. 6:4; Efe. 4:4-6)
   2. Nne – dunia nzima (yaani, pembe nne, nchi nne za dunia, yaani, Isa. 11:12; Yer. 49:36; Dan. 7:2; 11:4; Zek. 2:6; Mt. 24:31; Marko 13:27; Ufu. 7:1)
   3. Sita – kutokamilika kwa mwanadamu (moja chini ya 7, m.f, Ufu. 13:18)
   4. Saba – itimilifu wa Kiungu (siku saba za uumbaji). Tambua matumizi ya kiishara katika Ufunuo:
      a. vinara vya taa saba, Ufu. 1:12,20; 2:1
      b. nyota saba, Ufu. 1:16,20; 2:1
      c. makanisa saba, Ufu. 1:20
      d. Roho saba za Mungu, Ufu. 3:1; 4:5; 5:6
      e. taa saba, Ufu. 4:5
      f. Mihuri saba, Ufu. 5:1,5
      g. pembe saba na macho saba, Ufu. 5:6
      h. malaika saba, Ufu. 8:2,6; 15:1,6,7,8; 16:1; 17:1
      i. baragumu saba, Ufu. 8:2,6
      j. nghurumo saba, Ufu. 10:3,4
      k. elfu saba, Ufu. 11:13
      l. vichwa saba, Ufu. 13:1; 17:3,7,9
      m. mapigo saba, Ufu. 15:1,6,8; 21:9
      n. vitasa saba, Ufu. 15:7; 21:9
      o. wafalme saba, Ufu. 17:10

   5. Kumi– ukamilifu
      a. matumizi katika Injili
         1) Mt. 20:24; 25:1,28
         2) Marko 10:41
         3) Luka 14:31; 15:8; 17:12,17; 19:13,16,17,24,25
      b. matumizi katika Ufunuo
         1) Ufu. 2:10, siku kumi dhiki
         2) Ufu. 12:3; 17:3,7,12,16, pembe kumi
         3) Ufu. 13:1, vilemba kumi
      c. Vigawe vya kumi katika Ufunuo
         1) 144,000 = 12x12x1000, kama vile Ufu. 7:4; 14:1,3
         2) 1,000 = 10x10x10, kama vile Ufu. 20:2,3,6
   6. Kumi na Mbili – ushirika wa mwanadamu
      a. Wana kumi na wawili wa Yakobo (yaani, makabila kumi na mbili ya Israeli, Mwa. 35:22; 49:28)
      b. nguzo kumi na mbili, Kut. 24:4

c. mawe kumi mawili katika juu ya kifua cha Kuhani Mkuu, Kut. 28:21; 39:14
d. mikate kumi na miwili, juu ya meza Mahali Patakatifu (ishara ya utoaji wa Mungu wa kwa makabila kumi na mawili), Law. 24:5; Kut. 25:30
e. Watu kumi na wawili, Kumb. 1:23;
f. mawe kumi na mawili, Jos. 4:2,3,4,8,9,20
g. mitume kumi na wawili, Mt. 10:1

matumizi katika Ufunuo

1) makabila kumi na mbili elfu waliotiwa mhuri, Ufu. 7:5-8
2) nyota kumi na mbili, Ufu. 12:1
3) milango kumi na miwili, malaika kumi na wawili, makabila kumi na mawili, Ufu. 21:12
4) misingi ya mawe kumi na mawili, majina ya Mitume kumi na mawili, Ufu. 21:14
5) Yerusalemu mpya ilikuwa Yerusalemu ilikuwa vipimo vya mraba elfu kumi na mbili, Ufunuo 21:16
6) milango kumi na miwili ilitotengenezwa kwa lulu kumi na mbili Ufu. 21:21
7) mti wa uzima uzaao matunda, aima kumi na mbili, Ufu. 22:2

7. Arobaini –namba za nyakati
   a. wakati mwingine ni halisi (kuhamishwa na kutangatanga nyikani, m.f. Kut. 16:35); Kumb. 2:7; 8:2
   b. inaweza kuwa halisi au ya kiishara
      1) mafuriko, Mwa. 7:4,17; 8:6
      2) Musa juu ya Mlima Sinai, Kut. 24:18; 34:28; Kumb. 9:9,11,18,25
      3) mgawanyo wa maisha ya Musa:
      a) miaka arobaini ndani ya Misri
      b) miaka arobaini jangwani
      c) miaka arobaini ya kuiongoza Israeli
      4) Yesu alifunga siku arobaini, Mt. 4:2; Marko 1:13; Luka 4:2
   c. Tambua (kwa maana ya Upatanisho) tarakimu za wakati hii tarakimu inajitokeza katika wakati wa uteuzi ndani ya Bibia!
8. Sabini – namba ya jumla ya watu
   a. Israeli, Kut. 1:5
   b. wazee sabini, Kut. 24:1,9
   c. matukio ya siku za mwisho, Dan. 9:2,24
   d. kundi la huduma, Luka 10:1,17
   e. msamaha (70x7), Mt. 18:22

B. Marejeo mazuri
   1. John J. Davis, *Biblical Numerology*
   2. D. Brent Sandy, *Plowshares and Pruning Hooks*

◙ **"akijaribiwa"** Hiki ni kifungu cha maneno tendwa ya wakati usio timilifu inayounganishwa na tendaji ya wakati usio timilifu ya kitenzi "kisaidizi". Neno "jaribu" (*peirazō*) lina visawe vya "kujaribu kwa lengo na mtazamo wa kuelekea uharibifu." Kutoka katika sentensi ya daraja la kwanza yenye masharti katika Mt. 4 (kama vile Marko 4:3,6) tunajifunza kwamba majaribu yalikuwa juu ya namna ya kutumia nguvu yake ya ki-Masihi kuweza kukamilisha mapenzi ya Mungu ya ki-ukombozi.

## MADA MAALUMU: MANENO YA KIYUNANI YAHUSUYO KUPIMA NA VIDOKEZO VYAKE

Kuna manaeno mawili ya Kiyunani ambayo yana kidokezo kwa ajili ya kumpima mtu kwa kusudi fulani.

1. *Dokimazō, Dokimion, Dokimasia*

Neno hili *ni* neno la mtu yule afuaye vyuma kwa ajili ya kujaribu uhalisia wa kitu fulani (yaani, kistiari mtu fulani) kwa moto (tazana Mada Maalumu: Moto). Moto hudhihilisha chuma halisi na huteketeza (yaani, husafisha) dongo la

chuma. Kitendo hiki cha kifizikia kinakuwa nahau yenye nguvu kwa Mungu na/au Ibilisi na/au binadamu kuwajaribu wengine. Neno hili linatumika tu katika maana chanya ya kujaribu kwa kuangalia hadi kuufikia ukubalifu (tazama Mada Maalumu: Mungu Huwajaribu Watu Wake [Agano la Kale).

Linatumika katika Agano la Kale kwa ajili ya

a. Madume ya ng'ombe – Luka 14:19
b. sisi wenyewe – 1 Kor. 11:28
c. imani yetu – Yakobo 1:3
d. hata Mungu –Ebr. 3:9

Matokeo ya majaribu hayajafikiriwa kuwa chanya (kama vile. Rum. 2:18; 14:22; 16:10; 2 Kor. 10:18; 13:3,7; Flp. 2:27; 1 Pet. 1:7), hivyo, neno husilisha wazo la mtu aliyepimwa na kuhakikishwa

a. kuwa wa thamani
b. kuwa wazuri
c. kuwa halisi
d. kuwa wa maana
e. kuwa wa kuheshimiwa

2. *Peirazō, Peirasmus*

Neno hili mara nyingi lina maana nyingine ya kupimwa kwa kusudi la utafutaji au ukataaji. Linatumika katika maana nyingine kwa majaribu ya Yesu nyikani.

a. Linabeba jaribio la kumtega Yesu (kama vile Mt. 4:1; 16:1; 19:3; 22:18, 35; Marko 1:13; Luka 4:2; Ebr. 2:18).
b. Neno hili (*peirazōn*) linatumika kama wadhifa kwa Ibilisi katika Mt. 4:3; 1 The. 3:5 (yaani, "mjaribu").
c. Matumizi
   1) Lilitumiwa na Yesu alipokuwa akiwaonya wanadamu kutomjaribu Mungu (kama vile Mat. 4:7; Luka 4:12, [au Kristo kama vile 1 Kor 10:9]).
   2) Pia linamaanisha jaribio la kufanya kitu fulani ambacho kimeshindikana (kama vile Ebr.11:29).

Linatumika katika maana nyingine kwa majaribu na masumbufu ya waamini (kama vile 1 Kor. 7:5; 10:9, 13; Gal. 6:1; 1 The. 3:5; Ebr. 2:18; Yakobo. 1:2, 13, 14; 1 Pet. 4:12; 2 Pet 2:9).

◙**"na shetani"** Biblia kwa kurudia rudia inaelezea nguvu binafsi ipitayo kawaida ya uovu.

## MADA MAALUM: SHETANI

Hili suala gumu sana kutokana na sababu kadhaa.

1. Kitabu cha Agano la Kale hakimfunui adui mkuu apingaye mema, bali mtumishi wa YHWH (angaliA. B. Davidson, OT Theology, kr. 300-306), ambaye anampa mwanadamu uchaguzi wa bure na pia kumlaumu mwanadamu juu ya kutokuwa kwake mwenye haki. Kuna Mungu mmoja pekee (angalia Mada Maalum: Mungu aliye mmoja, uweza wa aina moja, sababu moja iliyo ndani ya Agano la Kale—YHWH (kama vile Isa. 45:7; Amosi 3:6).
2. Hii dhana ya huyu adui mkuu wa Mungu wa kipekee ilikuwa katika kipindi cha ukimya wa fasihi ya Agano la Kale na Agano Jipya (pasipo sheria za kikanisa) chini ya ushawishi wa pande mbili za dini za Kiajemi (Dhana ya Zoroaster). Hii, katika kurudia, kwa kiwango kikubwa hizi ziliwashawishi viongozi wa dini za Kiyahudi na jamii ya Essene (yaani, Magombo ya Kale ya Bahari ya Chumvi).
3. Kitabu cha Agano Jipya kiliikuza dhana ya Agano la Kale katika namna yaugumu wa kushangaza, lakini wa kipekee, wa aina nyingi.

Ikiwa moja ya mitazamo ya somo la uovu kutokana na kipengele cha thiolojia ya kibiblia (kila kitabu au mwandishi au aina ya somo lililofundishwa na maelezo ya kimuhtasari yaliotengwa), tena ni mawazo tofauti sana ya uovu unaofunuliwa. Ikiwa, kwa vyo vyote, moja ya mitazamo ya somo la uovu kutoka mtazamo usio wa kibiblia au mtazamo wa ziada wa kibiblia wa dini za ulimwengu au dini za mashariki, tena maendeleo mengi ya kitabu cha Aagano Jipya

yanatabiriwa katika ule uwili wa Kiajemi na ukiroho wa utawala wa Wagiriki-Waroma.

Ikiwa wazo la awali lilijikita juu ya Andiko la mamlaka ya Kiungu (kama Mimi Niko!), kasha ukuaji wa kitabu cha Agano Jipya lazima uonekane kama ufunuo endelevu. Yawapasa Wakristo kujilinda dhidi ya kuyaruhusu mafunzo ya mila na desturi za Kiyahudi au fasihi ya mashariki (Dante, Milton) kwa ajili ya ushawishi wa dhana ya baadaye. Kuna siri fulani na utata katika eneo hili la ufunuo. Mungu amechagua kutovifunua vipengele vyote vya uovu, chimbuko lake (angalia Mada Maalum: Lusfa), uendelevu wake, sababu yake, lakini Yeye amelifunua ondoleo lake!

Katika neno la Agano la Kale "shetani" au "mshtaki" (BDB 966, KB 1317) anaweza kuhusiana na makundi matatu yaliyojitenga.

1. washtaki wa mwanadamu (kama vile 1 Sam. 29:4; 2 Sam. 19:22; 1 Fal. 11:14,23,25; Zab. 109:6)
2. washtaki wa kimalaika (kama vile Hes. 22:22-23; Ayubu 1-2; Zek. 3:1)
3. washtaki wa kimapepo (kama vile 1 Nyak. 21:1; 1 Fal. 22:21; Zek. 13:2)

Baadaye katika kipindi cha ukimya wa Agano la Kale na Agano Jipya tu ndipo yule nyoka wa Mwanzo 3 alipotambujlishwa kama Shetani (kama vile Book of Wisdom 2.23-24; II Enoch 31:3), na baadaye hili lilikuja kuwa uchagujzi wa sheria za Kiyahudi. Sot 9b na Sanh. 29a). Wale "wana wa Mungu" wa Mwanzo 6 walikuja kuwa malaika katika I Enoch 54:6. Nalitaja hili, si usahihi wa kitheolojia, bali hili linaonyesha maendeleo yake. Katika Kitabu cha Agano Jipya kazi hizi linapewa kundi la kimalaika, uovu wa kibinadamu (kama vile 2 Kor. 11:3; Ufu. 12:9). Chimbuko la uovu wa kibinadamu ni gumu au haliwezekani (linategemeana na hoja ya mtazamo wako) kuibainisha kutokana na kitabu cha Agano la Kale. Moja ya sababu ya hili ni kuwepo kwa Mungu wa Israeli Aliye mmoja (angalia Mada Maalum: Mungu Aliye Mmoja; pia nukuu 1 Fal. 22:20-22; Mhu. 7:14; Isa. 45:7; Amosi 3:6). Usababishi wote (kama vile Isa. 45:7; Amosi 3:6) alipewa YHWH ili kuonyesha upekee na ubora Wake (kama vile Isa. 43:11; 44:6,8,24; 45:5-6,14,18,21,22). Chimbuko la uhakika wa habari ni (1) Ayubu 1-2, ambapo Shetani ni mmoja wa "wana wa Mungu" (yaani, malaika) au (2) Isaya 14 na Ezekieli 28, ambapo wafalme wenye majivuno waliokuwa karibu na mashariki (Babeli na Tiro) kwa hakika wanatumika kueleza juu ya majivuno ya Shetani (kama vile 1 Tim. 3:6). Nimechanganywa kihisia kuhusu mtazamo huu. Ezekieli anatumia stiari za Bustani ya Edeni, si kwa mfalme wa Tiro pekee kama Shetani (kama vile Eze. 28:12-16), bali pia kwa mfalme wa Misri kama Mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya (Ezekieli 31). Hata hivyo, Isaya 14, hasa mist. ya. 12-14, anaonekana kuufafanua uasi wa kimalaika kupitia majivuno. Ikiwa Mungu alitaka kuifunua kwetuj ile asili ya kipekee na chimbuko la Shetani, hii ni njia isiyo wazi na ni sehemu ya kulifanya hili. Yatupasa kujilinda dhidi ya uelekeo wa thiolojia ya mfululizo wa kuchukulia mambo madogo madogo, sehemu za utata wa semi mbalimbali, waandishi, vitabu, aina na kuziunganisha kama vipande vya mafumbo ya Uungu.

Nakubaliana na Alfred Edersheim (The Life and Times of Jesus the Messiah, juzuu. 2, viambatisho XIII [kr. 748-763] na XVI [kr.770-776]) kwamba Sheria za Dini ya Kiyahudi kwa kiasi kikubwa zimepewa ushawishi na zile pande mbili za Kiajemi na sikiko la kimapepo. Hawa Walimu wa sheria za Kikyahudi si chimbuko zuri la ukweli ndani ya eneo hili. Kimsingi Yesu anaachana na mafundisho ya Masinagogi ndani ya eneo hili. Nafikiri kwamba ile dhana ya adui wa YHWH aliyekuwa katika umbo la kimalaika iliendelezwa kutokana na miungu mikuu miwili ya pande mbili za ki-Irani, Ahkiman na Ormaza, ambapo iliendelezwa tena na Walimu wa Sheria katika pande mbili za YHWH na Shetani.

Kuna uhakika wa ufunuo endelevu katika kitabu cha Agano Jipya kama sifa ya, lakini si kama wanavyoeleza Walimu wa Sheria za Kiyahudi. M fano mzuri wa utofauti huu ni "vita ya mbinguni." Anguko la Shetani kimantiki lina umuhimu, lakini ubatana haokutolewa (angalia Mada Maalum: Anguko la Shetani na Malaika Zake). Hata kile kilichotolewa kinafunikwa katika aina ya ukiyama (kama vile Ufu. 12:4,7,12-13). Ingawa Shetani anaondolea kwa Yesu na kutupwa duniani, bado anafanya kazi kama mtumishi wa YHWH (kama vile Mt. 4:1; Luka 22:31-32; 1 Kor. 5:5; 1 Tim. 1:20). Katika eneo hili yatupasa kuzuia uchunguzi. Kuna nguvu binafsi ya ushawishi na uovo, lakini bado kuna Mungu mmoja pekee na bado tunawajibika kwa ajili ya chaguzi zetu. Kuna mapambano ya kiroho, wakati wote kabla na baada ya wokovu. Ushindi unaweza kuja tu na kubaki pale pale kupitia Mungu wa Utatu. Uovu umeshindwa na utaondoshwa kama vile Ufu. 20:10)!

◙ **"wanyama wa porini"** Hii inawezekana ilikuwa ni rejea ya kawaida ya eneo lisilokaliwa. Hatahivyo, kwasababu ya wanyama wa mwituni wanatumika kama sitiari kwa ajili au majina ya mapepo katika Agano la Kale (kama vile NEB) hii pia ingeweza kurejerea mahali pa shughuli za kimapepo (kama vile Zab. 22:12-13,16,21; Isa. 13:21-22; 34:11-15).

Wanyama wa porini hawa pia kunaweza kuwa ni mwendelezo wa maelezo wa safari mpya, zama mpya ya ushirika uliorejeshwa kati ya mwanadamu na wanyama (kama vile Isa. 11:6-9; 65:25; Hos. 2:18). Biblia mara kwa mara inaelezea zama mpya kama urejesho wa Bustani ya Edeni (kama vile Mwanzo 2; Ufunuo. 21-22). Taswira ya asili ya Mungu ndani ya mwanadamu (kama vile Mwanzo. 1:26-27) inarejeshwa kupitia kifo cha kidhabihu cha Yesu. Ushirika kamili ambao ulikuwepo kabla ya anguko (kama vile Mwanzo 3), unawezekana tena.

◙ **"malaika walikuwa wakimuhudumia"** Hii ni njeo isiyo kamilifu ambayo inamaansha (1) kitendo kinachoendelea kwa wakati uliopita au (2) mwanzo wa shughuli wa wakati uliopita. Malaika walimtumikia (1) Eliya katika Jagwa kwa namna ile ile (yaani wakileta chakula, kama vile 1 Wafalme 18:7-8). Hii inamaanisha kwamba Yesu kama sauti ya kinabii mpya (kama vile Kumb. 18:18-22) na (2) Israeli katika Jangwa hivyo pia. Hii inaweza kuwa ilimaanisha Yesu kama Musa mpya anayerandana na ubatizo wake na majaribu (kama vile 1 Kor. 10:1-13).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 1:14-15**
**14 Hata baada ya Yohana kutiwa gerezani, Yesu akaenda Galilaya, akiihubiri Habari Njema ya Mungu, 15 akisema, Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni, na kuiamini Injili.**

**1:14-15** Mistari hii miwili ni madokezo. Marko anatumia mara kwa mara mbinu hii (kama vile Marko 1:14-15,21-22,39; 2:13; 3:7b-9; 6:7,12-13). Muhtasari huu unaelezea kweli za kithiolojia
1. Yesu alikuwa maarufu na wengi walikuja kumsikiliza akihubiri
2. Yesu alikuwa mwenye nguvu, akipunga pepo na kuponya watu
3. alihamisha nguvu zake kwenda kwa wanafunzi Wake (yaani safari za kimisheni za Kumi na Mbili na za Sabini)
4. kusudi la tangazo la Yesu lilikuwa toba na imani

**1:14 "Yohana kutiwa gerezani"** Yohana alikuwa kifungoni (yaani, *paradidōmi*, ambalo limetumika mara ishirini katika Marko kwa ajili ya "kugeukia mwenye mamlaka") na Herode Antipas kwasababu aliendelea hadharani kushutumu ndoa ya Herode kwa mke wa zamani wa kaka yake (kama vile Marko 6:16-17).

## MADA MAALUM: FAMILIA YA HERODE MKUU

A. Herode Mkuu
   1. Mfalme wa Yudea (37-4 k.k.), Idumean (kutoka Edom), ambao kupitia ujanja wa kisiasa na msaada wa Marko Antoni, waliweza kuteuliwa mtawala wa sehemu kubwa ya Palestina (Kanaani) kwa seneti ya kirumi katika 40 k.k.
   2. Anatajwa katika Mt. 2:1-19 na Luka 1:5
   3. Watoto wake
      a. Herode Filipo (mwana wa Mariamne wa Simoni)
         (1) mume wa Herodia (4 k.k. – 34 b.k)
         (2) Anatajwa katika Mt. 14:3; Marko 6:17
      b. Herode Filipo I (mwana wa Cleopatra)
         (1) Mtawala wa eneo kaskazini na Magharibi ya bahari ya Galilaya (4 k.k. – 34B. k)
         (2) anatajwa katika Luka 3:1
      c. Herode Antipa
         (1) Mtawala wa Galilaya na Perea (4 k.k. – 39 b.k)
         (2) Anatajwa katika Mt. 14:1-12; Marko 6:14,29; Luka 3:1,19; 9:7-9; 13:31; 23:6-12,15; Mdo. 4:27;

13:1

d. Archelaus, Herode wa Ethnarch
    (1) Mtawala wa Yudea, Samaria, na Idumaya (4 k.k. – 6b.k)
    (2) anatajwa katika Mt. 2:22

e. Aristobulus (mwana wa Mariamne)
    (1) ametajwa kama Baba wa Herode Agrippa I aliyekuwa
        (a) Mfalme wa Yudea (37-44 B.K)
        (b) anatajwa katika Mdo. 12:1-24; 23:35
            (i) mwana wa Herode wa Agrippa II
                – Mtawala ngome ya kaskazini (50-70 B.K)
            (ii) mtoto wake wakike aliitwa Bernice
                – mwenza wa kaka yake
                – anatajwa katika Mdo. 25:13-26:32
            (iii) mtoto wake Drucilla
                – mke wa Felix
                –anatajwa katika Mdo.24:24

B. Rejea za kibiblia kuhusu Herode

1. Herode Mtawala, inatajwa katika Mathayo 14:1 na kuendelea; Luka 3:1; 9:7; 13:31, na 23:7, alikuwa mtoto wa Herode Mkuu. Wakati wa kifo cha Herode Mkuu, ufalme wake uligawanywa kwa watoto wake wa kiume. Neno "Tetrarch (mtawala)" lilimaanisha"kiongozi wa sehemu ya nne." Herode huyu alijulikana kama Herode Antipa, ambalo limefupishwa kutoka katika Antipater. Alikuwa akitawala Galilaya na Perea. Hii ilimaanisha kiasi hiki katika huduma ya Yesu iliyokuwa katika mipaka ya kizazi hiki cha pili cha Mtawala Idumean.

2. Herodia alikuwa mtoto wa kike wa kaka wa Herode Antipa aliyeitwa Aristobulus. Lakini kabla alikuwa ameolewa na Filipo ambaye ni ndugu ayekuwa wa ukoo wa Herode Antipa. Huyu hakuwa Filipo Mtawala aliyeongoza eneo tu la kaskazini ya Galilaya, lakini ndugu mwingine alikuwa Filipo, aliyeishi katika Rumi. Herodia alikuwa na binti mmoja na Filipo. Katika safari ya Herode Antipa kutembelea Rumi alikutana na alitongozwa na Herodita, aliyekuwa akitafta kutanuka kisiasa. Hivyo, Herode Antipa alimtaliki mkewe aliyekuwa Malkia wa Nabatean, na Herodia alimtaliki Filipo ili kwamba Herode Antipa aweze kuolewa. Yeye alikuwa pia ni dada wa Herode Agrippa I (kama vile Mdo. 12).
3. Tunajifunza juu ya jina la mtoto wa kike wa Herodia, Salome, kutoka katika kitabu cha Flavius Josephus, Mambo ya Kale ya Wayahudi 8:5:4. Yawezekana lazima alikuwa na umri kati ya kumi na mbili na kumi na saba kwa wakati huu. Kwa dhahiri alikuwa akiongozwa na kurubuniwa vibaya na mama yake. Baadaye aliolewa na Filipo Mtawala, lakini muda kidogo akabaki mjane.
4. Kama miaka kumi baada ya kukamatwa kwa Yohana Mbatizaji, Herod Antipa alikwenda Rumi katika sherehe ya mke wake Herodia, kutafuta cheo cha mfalme kwakuwa Agripa I kaka yake alikuwa hapo mwanzo amepewa cheo hicho. Lakini Agrippa I aliwaandikia Rumi na kuwashutumu Antipa kwa kushirikiana na Wa-Parthi, adui wa Rumi mwenye kuchukiwa kutoka katika utawala wa kisiasa (Mesopotamia). Mtawala kidhahiri aliamini Agrippa I na Herode Antipa, pamoja na mkewe Herodia, walikuwa wameenda uhamishoni Uhispania
5. Inaweza ikawa rahisi kukumbuka hawa wakina Herode tofauti tofauti kama wanavyowasilishwa katika Agano Jipya kwa kukumbuka kwamba Herode Mkuu aliuwa watoto katika Betlehemu; Herod Antipa aliuwa Yohana Mbatizaji; Herode Agrippa I aliuwa Mtume Yakobo; na Herode Agrippa II alisikia kukata rufaa juu ya Paulo iliyowekwa katika kumbukumbu katika kitabu cha Matendo ya Mitume.

Kwa ajili ya usuli wa taarifa juu ya familia ya Herode Mkuu, tazama kielezo cha Flavius Josephus in Kumbukumbu ya Kale ya Wayahudi.

◙ **"Yesu alikuja kutoka Galilaya"** Injili inaandika kwamba huduma ya Yesu kijiografia ni Galilaya, katika Yudea, Galilaya. Yesu aliondoka Palestina ya kusini wakati Yohana alipokamatwa (kama vile Mt. 4:12; Luka 4:14-15; Yohana 1:43).

Huduma kwa ukubwa ilitawala mataifa ya kaskazini mwa Palestina na ulikuwa ni utimilizwaji wa unabii wa Isa.9. Hakuna aliyetegemea chochote cha muhimu kiroho kuanzia katika jimbo hili, ikiondolewa mbali kutoka hekaluni (kama vile Yohana 1:46) na ya Kwanza kushindwa na kupeleka uhamishoni na mamlaka za Mesopotamia (yaani Ashuru na Babeli mpya).

◙ **"akihubiri Injili ya Mungu"** Kutumika kwa neno hili "injili" lazima kuwe kuna sifa. Mara ya kwanza ujumbe wa Yesu ulikua sawasawa na Yohana. Injili kamili ya Yesu haiwezi kukamilika mpaka baada ya maisha yake, kifo, maziko, ufufuo na kupaa. Mstari wa 15 unatoa maudhui ya mahubiri ya mwanzo kabisa. Kile ambacho Yohana alikihubiri kilidhihirishwa na kufanywa hai ndani ya Yesu wa Nazareth (kama vile Yohana 14:6).

**1:15 "'saa imefika'"** Tungo hii ilitambulishwa na neno *hoti*, ambalo siku zote linaashiria nukuu inayoonekana dhahiri katika Marko. Hii inaaksi kumbukumbu ya maneno ya Yesu yanavyokumbukwa na Petro. Hii ni kauli tendwa elekezi ya wakati timilifu ambayo ni umuhimu wa umasihi na unabii (kama vile Efe. 1:10; Gal. 4:4; 1 Tim. 2:6; Tito 1:3). Sauti irabu tendwa inaksi shughuli za Mungu katika na kudhibiti muda na historia.

◙ **"'ufalme wa Mungu'"** Hii inarejerea utawala wa Mungu. Ni vyote uhalisia wa sasa na hitimisho la baadaye. Katika Injili ya Mathayo hii mara nyingi inarejerewa kama "ufalme wa mbinguni." Tungo hizi ni sambamba (linganisha na Mt. 13:11 pamoja na Marko 4:11 na Luka 8:10). Ufalme ulifika wakati Yesu alipozaliwa. Inaelezewa na kudhihirishwa katka maisha ya Yesu na mafundisho. Itahitimishwa katika kurejea Kwake. Lilikuwa ni somo la mahubiri ya Yesu na mifano. Ilikuwa ni maudhui lengwa ya jumbe zake alizozungumza.

## MADA MAALUMU: UFALME WA MUNGU

Katika Agano la Kale Mungu alifikiriwa kama mfalme wa Israeli (kama vile 1 Sam. 8:7; Zab. 10:16; 24:7-9; 29:10; 44:4; 89:18; 95:3; Isa. 43:15; 44:6) na Masiha akawepo kama mfalme aliyedhaniwa/kutegemewa (kama vile Zab. 2:6; Isa. 9:6-7; 11:1-5). Na kuzaliwa kwa Yesu pale Betlehemu (mwaka wa 6-4 K.K) ufalme wa Mungu ukavunjiliwa ndani ya historia ya mwanadamu kwa nguvu mpya na ukombozi (“Agano Jipya,” kama vile Yer. 31:31-34; Ezek. 36:27-36).

1. Yohana Mbatizaji akatangaza kukaribia kwa ufalme (kama vile Mt. 3:2; Mk. 1:15).
2. Yesu wazi wazi akafundisha kwamba ufalme ulikuwa tayari ndani yake mwenyewe na mafundisho yake (kama vile Mt. 4:17,23; 10:7; 12:28; Luka 10:9,11; 11:20; 17:21; 21:31-32). Na bado ufalme unakuja (kama vile Mt. 16:28; 24:14; 26:29; Marko 9:1; Luka 21:31; 22:16,18).

Katika ufanano wa madokezo kwenye Marko na Luka tunakipata kifungu, “ufalme wa Mungu.” Hii ilikuwa mada ya kawaida katika mafundisho ya Yesu yakijumisha utawala wa Mungu uliopo kiatika mioyo wa watu, ambao siku moja utakamilishwa katika ulimwengu wote. Huu unaakisishwa kwenye maombi ya Yesu katika Mt.6:10. Mathayo, akiwaandikia Wayahudi, alipendelea kifungu kile ambacho hakitumii jina la Mungu (yaani Ufalme wa Mbinguni), wakati Marko na Luka, akiwaandikia watu wa mataifa, anatumia usanifu wa kawaida, akiweka jina la Uungu.

Hiki ni kile kifungu cha mfano katika mihitasari ya injili. Hotuba za kwanza na za mwisho za Yesu, na zaidi mafumbo yake, yanashughulika na mada. Zinarejerea utawala wa Mungu katika mioyo ya wanadamu sasa! Inashangaza kuona kwamba Yohana anatumia kifungu hiki mara mbili tu (na kamwe sio kwenye mafumbo ya Yesu). Katika injili ya Yohana “uzima wa milele” ni sitiari muhimu.

Mvutano na kifungu hiki unasababishwa na ujio mara mbili wa Kristo, Agano la Kale linatazamisha kwenye ujio mmoja wa Masihi wa Mungu kama afisa wa kijeshi, ujio wa kitukufu-lakini Agano Jipya linaonyesha kuwa alikuja kwanza kama mtumishi mwenye mateso katika Isaya 53 na mfalme mnyenyekevu katika Zak. 9:9. Enzi mbili za Kiyahudi (angalia mada maalumu: Enzi hii na Enzi inayokuja), enzi ya uovu na enzi mpya ya haki, zimeingiliana. Kwa sasa Yesu anatawala ndani ya mioyo ya waumini, lakini siku moja atatawala juu ya uumbaji wote. Atakuja kama Agano la Kale lilivyotabiri (kama vile Ufunuo 19)! Waamini wanaishi ndani ya ulimwengu wa Mungu “uliotayari” dhidi

ya “ule ambao bado” (kama vile Gordon D. Fee na Douglas Stuart's *How to Read The Bible For All Its Worth*, kurasa za. 131-134).

**NASB, NKJV** **“uko karibu”**
**NRSV** **“umekaribia”**
**TEV** **“uko karibu**
**NJB** **“umekaribia sana”**

Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati timilifu ambayo inamaanisha kwamba ufalme wa Mungu ulikuwa umepita uhalisia (kama vile Marko 1:1-3) na kama pia uhalisia wa sasa (kama vile Mt. 12:28; Luka 11:20; 17:21). Tungo "saa imefika" inafanana na tungo hii na kusisitiza uhalisia wa neno la Mungu la kinabii sasa kufanyika tukio la kihistoria. Ile "Zama mpya ya Haki" ilianzishwa katika kuzaliwa kwa Yesu, lakini haikujulikana kamili mpaka Juma la Upendo na haikutiwa nguzu kamili mpaka Pentekoste
Ingawa Ufalme hakika umekuja, lakini pia kuna maandiko ya Agano Jipya ambayo yanamaanisha kwamba udhihirisho wake kamili ni ubaadaye (kama vile Marko 9:1; 14:25; Mt. 26:29; Luka 22:18; Mdo. 1:11; 1 The. 4:13-18). Tunachoweza kufanya sasa pamoja na Kristo kiaamua tumaini letu la matukio yajayo ya siku za mwisho (kama vile Marko 8:38).

◙ **"'tubu'"** Angalia Mada Maalum juu ya toba katika Marko 1:4.

◙ **"'na iamini injili"** mfanano katika Mt. 4:17 na Luka 4:14-15 havina muhtasari unaofanana.

## MADA MAALUM : Imani, Amini, au Sadiki – (*Pistis* [nomino], *Pisteuō,* [kitenzi], *Pistos* [kivumishi])

A. Hili ni aina ya neno muhimu katika Biblia (kama vile. Ebr. 11:1,6). Lilikuwa ni somo la Yesu katika mahubiri ya awali (kama vile Mk. 1:15). Kiwastani kuna mahitaji mapya mawili ya agano: toba na imani (Mk. 1:15; Mdo. 3:16, 19; 20:21)
B. Asili na historia yake ya maneno haya
   1. Neno “imani” katika Agano la Kale lilimaanisha mtiifu, mwaminifu au mwaminifu wa kutumainiwa na yalikuwa ni maelezo ya asili ya Mungu na si yetu.
   2. Linatokana na neno la Kiebrania (*emun, emunah*, BDB 53, yaani., Hab. 2:4), ambalo mwanzo kabisa lilimaanisha “kuwa na uhakika au imara.” Kuitumikia imani ni
      a. Kumkaribisha mtu (yaani imani binafsi, sadiki, kama vile. E.1.hapo chini)
      b. Kuamini imani kuhusu mtu (yaani maandiko, kama vile E.5.hapo chini)
      c. Kuishi maisha kama ya mtu huyo (yaani., mfano wa Kristo)
C. Matumizi yake katika Agano la Kale

Lazima isisitiziwe kuwa imani ya Ibrahim ilikuwa si kwa ajili ya Masiha ajaye, lakini ni kwa ahadi ya Mungu ya kwamba atapata mtoto na uzao (kama vile Mwa. 12:2-5; 17:4-8; Rum. 4:1-5). Ibrahim aliikubali ahadi hii kwa kumwamini Mungu (angalia Mada Maalumu: kuamini, amini, imani na uaminifu katika Agano la Kale) na neno lake. Bado anamashaka na kuhusika juu ya ahadi hii, ambayo ilimchukua miaka kumi na mitano kutimizwa. Imani yake isiyo kamili, hata hivyo, alikubaliwa na Mungu. Mungu anapenda kufanya kazi na mwanadamu mwenye mapungufu anayejongea kwake na katika ahadi zake kwa imani, hata kama kwa kipimo cha chembe ya haradari (kama vile. Mt. 17:20) au imani mchanganyiko (kama vile. Marko 9:22-24)

D. Matumizi yake katika Agano Jipya

Neno “kuamini” linatoka katika neno la Kiyunani *pisteuō* au nomino *pistis,* ambayo yanatafasiliwa kwa Kiingereza “kuamini” “amini” au “imani.” Kwa mfano, nomino haijitokezi katika injili ya Yohana, lakini kitenzi kinatumika mara nyingi. Katika Yohana 2:23-25 kuna uwalakini katika uhalisia wa uwajibikaji wa kundi kwa Yesu wa Nazareti kama Masiha. Mifano mwingine wa matumizi ya kubabiya ya neno hili “kuamini” ni katika Yohana 8:31-59 na Matendo 8:13, 18-24. Imani ya kweli ya Kibiblia ni zaidi ya uwajibikaji wa awali. Lazima ifuatishwe na mchakato wa uwanafunzi (kama

vile Mt. 13:20-23, 31-32; 28:19-20)

E. Matumizi yake ikiwa na vivumishi
1. *eis* inamaanisha "ndani ya." Muundo huu wa kipekee unasisitizia waumini kuweka imani zao kwa Yesu
   a) ndani ya jina lake (Yohana 1:12; 2:23; 3:18; 1 Yohana 5:13)
   b) ndani yake (Yohana 2:11; 3:15,18; 4:39; 6:40; 7:5,31,39,48; 8:30; 9:36; 10:42; 11:45,48; 12:37,42; Mt. 18:6; Mdo. 10:43; Fil. 1:29; 1 Petro. 1:8)
   c) ndani yangu (Yohana 6:35; 7:38; 11:25,26; 12:44,46; 14:1,12; 16:9; 17:20)
   d) ndani ya mwanaye (Yohana 3:36; 9:35; 1 Yohana 5:10)
   e) ndani ya Yesu (Yohana 12:11; Mdo. 19:4; Gal. 2:16)
   f) ndani ya nuru (Yohana 12:36)
   g) ndani ya Mungu (Yohana 14:1)
2. *ev* inamaanisha "katika" kama ilivyo katika Yohana 3:15; Marko 1:15; Mdo. 5:14
3. *epi* ikimaanisha "katika" au "juu ya" kama ilivyo katika Mt. 27:42; Mdo. 9:42; 11:17; 16:31; 22:19; Rum. 4:5,24; 9:33; 10:11; 1 Tim. 1:16; 1 Petr. 2:6
4. uhusika wa mahali usio na kivumishi kama ilivyo katika Yohana 4:50; Gal.3:6; Mdo. 18:8; 27:25; 1Yoh. 3:23; 5:10
5. *hoti* likimaanisha "kuamini kwamba," inatoa kilichomo kama kile kinachotakiwa kuaminiwa
   a) Yesu ni Mtakatifu wa Mungu (Yohana 6:69)
   b) Yesu ni Mimi ndiye (Yohana 8:24)
   c) Yesu katika Baba na Baba ndani yake (Yohana 10:38)
   d) Yesu ni Masiha ( Yohana 11:27; 20:31)
   e) Yesu ni mwana wa Mungu (Yohana 11:27; 20:31)
   f) Yesu alitumwa na Babaye (Yohana 11:42; 17:8,12)
   g) Yesu ni wamoja na Babaye (Yohana 14:10-11)
   h) Yesu alikuja toka kwa Babaye (Yohana 16:27,30
   i) Yesu anajitambulisha mwenyewe katika jina la Agano la Babaye "Mimi ndiye" (Yohana 8:24; 13:19)
   j) Tutaishi naye (Rum. 6:8)
   k) Yesu alikufa na kufufuka tena (1The. 4:14)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 1: 16-20**
**[16] Naye alipokuwa akipita kando ya bahari ya Galilaya, akamwona Simoni na Andrea nduguye, wakitupa jarife baharini; kwa maana walikuwa wavuvi. [17] Yesu akawaambia, Njoni mnifuate, nami nitawafanya kuwa wavuvi wa watu. [18] Mara wakaziacha nyavu zao, wakamfuata. [19] Akaendelea mbele kidogo, akamwona Yakobo wa Zebedayo, na Yohana nduguye, nao pia walikuwa chomboni, wakizitengeneza nyavu zao. [20] Mara akawaita, wakamwacha baba yao Zebedayo ndani ya chombo pamoja na watu wa mshahara, wakaenda, wakamfuata.**

**1:16 "bahari ya Galilaya"** Bahari hii inajulikana kwa majina kadhaa katika Biblia .
1. bahari ya Chinnereth (kama vile Hes. 34:11; Yos. 12:3; 13:27)
2. ziwa la Gennesareti (kama vile Luka 5:1)
3. Bahari ya Tiberias (kama vile Yohana 6:1; 21:1)
4. bahari ya Galilaya (ikijulikana zaidi, kama vile Marko 1:16; 7:31; Mt. 4:18; 15:29; Yohana 6:1)

◙ **"Simono na Andrea. . .wakarusha nyavu"** Tazama kwa mara ya kwanza rasmi Petro anaitwa Marko, wakati katika Yohana 1:35-42 ilikuwa ni Andrea. Bahari ya Galilaya ilitoa samaki zote kwa ajili ya Palestina. Nyavu hizi zinajulikana kama nyavu za mkono, ambazo zilikuwa karibia futi 10 kwa upana wa futi 15. Samaki kilikuwa chakula kikuu kwa milo ya Wayahudi.

**1:17 "'Nifuate'"** Hiki ni kihisishi kinachofanya kazi kama kauli shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu. Hii lazima kuwa haikuwa kukutana kwa mara ya kwanza kati ya Yesu na wavuvi hawa (kama vile Yohana 1:35 na kuendelea). Hii ilifuatia

kufanyika wito wao kuwa rasmi, na wafuasi wa kudumu wa mwalimu wa Kiyahudi (kama vile Marko 1:17 na 20).

◙ **"'nitawafanya kuwa wavuvi wa watu'"** Huu ni mzaha juu ya kazi yao. Kuvua katika Agano la Kale kulikuwa mara kwa mara kama sitiari kwa ajili ya hukumu (kama vile Yer. 16:16. Ezek. 29:4-5; 38:4; Amosi 4:2; Hab.1:14-17). Hapa ni sitiari kwa ajili ya wokovu.

**1:18** Hii inarudiwa katika Mt. 4:18-22, lakini ikiwa na utofauti kidogo kihadithi katika Luka 5:1-11.

**1:19-20 "mashua"** Hizi zilikuwa mashua kubwa za uvuvi. Yohana na Yakobo, wana wa Zebedayo walikuwa wenye kufanikiwa katikati ya wavuvi wengine (yaani walikuwa wafanyakazi walioajiliwa). Yohana kibayana inavyoonekana walikuwa na mikataba ya kibiashara mara kwa mara ya kuuza samaki kwa familia ya kikuhani Yerusalemu (yaani, Yohana alikuwa akijulikana na wao, kama vile Yohana 18:15-16).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 1: 21-28**
**21 Wakashika njia mpaka Kapernaumu, na mara siku ya sabato akaingia katika sinagogi, akafundisha. 22 Wakashangaa mno kwa mafundisho yake; kwa maana alikuwa akiwafundisha kama mtu mwenye amri, wala si kama waandishi. 23 Na mara palikuwapo ndani ya sinagogi lao mtu mwenye pepo mchafu; akapaza sauti, 24 akisema, Tuna nini nawe, Yesu wa Nazareti? Je! Umekuja kutuangamiza? 25 Nakutambua u nani, Mtakatifu wa Mungu. Yesu akamkemea, akisema, Fumba kinywa, umtoke. 26 Yule pepo mchafu akamtia kifafa, akalia kwa sauti kuu, akamtoka. 27 Wakashangaa wote, hata wakaulizana, wakisema, Nini hii? Ni elimu mpya! Maana kwa uweza awaamuru hata pepo wachafu, nao wamtii! 28 Habari zake zikaenea mara kotekote katika nchi zote kandokando ya Galilaya.**

**1:21 "Kapernaumu"** Yesu kwasababu ya jiji la Nazareti kukosa imani (kama vile Luka 4:16-30) na kama utimitifu wa unabii (kama vile Mt. 4:13-16), aliuchukulia mji huu kama makao makuu (kama vile Marko 2:1). Huduma katika jiji la Karprnaumu (kama vile Marko 1:21-3:6) inatumika kuelezea shughuli halisia za Yesu. Matukio haya yanafunua kiuhalisia mamlaka Yake, nguvu na U-Masihi. Hii ni kama kionjo kwenye maisha yake ya kila siku na shughuli za Yesu wakati wote wa huduma yake ya wazi kwa watu.

◙ **"mara"** Angalia dokezo katika Marko 1:10.

◙ **"Sabato"** Angalia Mada Maalumu inayofuata

## MADA MAALUM: SABATO

Hili linatokana na maana ya kiebrania "pumziko" au "kuacha kwa muda" (BDB 992). Linahusiana na siku ya saba ya uumbaji ambapo Mungu aliacha kazi zake baada ya kumaliza uumbaji wake wa mwanzo (kama vile Mwa. 2:1-3). Mungu hakupumzika kwa sababu alikuwa amechoka, lakini ni kwa sababu (1) uumbaji ulikuwa umekamilika na kuonekana unapendeza machoni pake (kama vile Mwa. 1:31) na (2) kumpa mwanadamu mwongozo kwa ajili ya ibada na pumziko. Utaratibu kama ilivyo siku ya kuabudu ulianzia Mwa. 2:2-3, ambapo YHWH alitumia pumziko lake kama utaratibu kwa ajili ya wanyama (kama vile Kut. 23:12) na mwanadamu (binadamu huhitaji utaratibu wa kila mara wa kazi, pumziko, na ibada). Sabato ilianza kama ilivyo siku zote za mwanzo 1, jioni; kwa hiyo, Ijumaa jioni mpaka Jumamosi jioni ulikuwa ni muda rasmi kwa ajili ya sabato. Maelezo yote juu ya kuishika sabato yametolewa katika kitabu cha Kutoka (hasa katika sura 16; 20; 31; na 35) na Mambo ya Walawi (hasa sura ya 23-26). Hasa utumiaji wa kwanza wa siku hii kwa Waisraeli ilikuwa ni katika Kut. 16:25-26 kwenye kusanyiko la manna. Baadaye ikajakuwa sehemu ya "amri kumi" (kama vile Kut. 20:8-11; Kumb. 5:12-15). Huu ni mfano mojawapo ambapo Amri Kumi katika Kutoka 20 kwa kiasi kidogo zimetofautiana na zile zilizoko katika Kumbukumbu la Torati 5. Zile za Kumbukumbu la Torati lilimwandaa Mwisraeli kwa ajili ya makazi, maisha ya kilimo huko Kanaani.

Mafarisayo walizichukua hizi taratibu na, kwa majadiliano yao ya kusimuliana, wakazitafasiri kwa namna ya kuzitumia kwenye sheria nyingi. Yesu mara nyingi alitenda miujiza, akijua wazi anakwenda kinyume na sheria zao ili

kwamba waweze kuingia kwenye mjadala. Ilikuwa sio sabato aliyoikataa Yesu, bali kujihesabia kwao haki na kukosekana kwa upendo.

Hii inatoka katika neno la Kiebrania likiwa na maana ya "pumziko" au "mwisho/kituo." Imeunganishwa na siku ya saba ya uumbaji pale ambapo Mungu aliacha kazi zake zote baada ya kumaliza uumbaji wake wa awali (kama vile Mwanzo. 2:1-3). Mungu hakupumzika kwasababu alikuwa amechoka lakini kwasababu (1) uumbaji ulikuwa umekamilika na mwema (kama vile Mwa. 1:31) na (2) kumpa mwanadamu utaratibu wa mara kwamara kwa ajili ya kuabudu na kupumzika. Sabato inaanza kama siku zote katikaza Mwanzo 1, mara baada ya machweo; hivyo, machweo ya Ijumaa kuelekea machweo ya siku ya Jumamosi ilikuwa muda rasmi. Maelezo yote ya yale yanayotakiwa kufanywa yanatolewa katika Kutoka (haswa sura za 16,20,31, na 35) na Mambo ya Walawi (haswa sura za 23-26). Mafarisayo walikuwa wamechukua sheria hizi na kwa mijadala yao ya vinywa, wakifasiri kujumuisha sheria nyingi. Yesu mara kwa mara alifanya miujiza, akijua kuwa anavunja sheria zao ili aingie kwenya mijadala ya kimazungumzo pamoja nao. Haikuwa Sabato ambayo Yesu aliikataa au kuishusha uthamani lakini kujihesabia kwao haki kisheria na kukosa kwao upendo.

◙ **"hekalu"** Hili ni neno ambatani ambalo linamaanisha kibayana "kuja kwa pamoja." Ilikuwa ni desturi ya Yesu kuhudhuria ibada mara kwa mara. Hekalu lilikuza katika Mesopotamia wakati wa uhamisho wa Kibabeli. Ilikuwa sehemu yao ya kuabudu, elimu na utunzaji wa kidesturi. Ilikuwa ni namna yao ya kuelezea imani yao ya Kiyahudi, Kama ambavyo Hekalu lilikuwa utambulisho wao wa kitaifa. Kulikuwa na angalau hekalu moja katika kila mji ikiwa na angalau wayahudi kumi.

◙ **"akaanza kuhubiri"** Ilikuwa kawaida kwa mtu kutoka katika kusanyiko au wageni rasmi kuchagua kuongoza sehemu ya mafundisho ya huduma ya ibada. Siku zote kifungu cha habari kutoka katika Torati (yaani Mwanzo – Kumbukumbu la Torati) lilisomwa na kifungu kutoka katika Manabii (yaani Yoshua – Wafalme na Isaya – Malaki).

**1:22,27 "wakashangazwa"** Kidhahiri hii ilimaanisha "kupewa usikivu." Aina ya ufundishaji ya Yesu na maudhui yalikuwa kiasili ni tofauti na yale ya Wayahudi. Walinukuliana wao kwa wao kama mamlaka, lakini alizungumza akiwa na malaka ya Kimungu (kama vile Mt. 5:17-48). Mafundisho ya Yesu na matendo yalisababisha mshangao, mshtuko na hata hofu (kama vile Marko 1:22,27; 2:12; 5:42; 6:2,51; 7:37; 9:6,15; 10:26,32; 11:18; 14:33).

**1:22 "sio kama waandishi"** Yesu hakunukuu masimulizi ya mdomo (yaani, Kitabu cha sheria za kiyahudi). Wayahudi walijali kutovunja amri za Mungu, hivyo kila mstari wa Torati (maandiko ya Musa, Mwanzo-Kumbu kumbu la Torati) ilifasiriwa na majadiliano ya ualimu wa kiyahudi. Baadaye haya yalikuzwa katika shule, huru (yaani, Hillel) na nyigine yenye kuzingatia mambo yote ya Kiyahudi (yaani, Shammai). Walimu wa Kiyahudi waongozao shule hizi walikuwa mara kwa mara wakinukuliwa kama mamlaka. Waandishi walikuwa walimu stadi wenye taaluma wafundishao Uyahudi waliofasiri desturi za kinywa kwa hali za maeneo yao na mahitaji. Waandishi wengi katika siku za Yesu walikuwa Mafarisayo.

## MADA MAALUM: WAANDISHI

Hili jina linatokana na nomino ya Kiebrania (BDB 706, KB 767) ambayo inamaanisha "ujumbe uliozungumzwa," "kumbukumbu iliyoandikwa/amri" (KB 766). Tafsiri ya Kiyunani grammateus (Agano la Kale la Kiebrania-LXX) mara nyingi hurejelea ujumbe ulioandikwa. Jina hili linaweza kudokeza

1. mwelimishaji (Nehemia 8)
2. mtawala wa kiserikali (2 Fal 22:3-13)
3. mchukua kumbukumbu/mhazili (1 Nya. 24:6; 2 Nya. 34:13; Yer. 36:22)
4. mkuu wa majeshi (kama vile Amu. 5:14)
5. kiongozi wa kidini (yaani, Ezra, Ezra 7:6; Neh. 12:12-13)

Katika Agano Jipya mara nyingi hawa wanahusiana na Mafarisayo (tazama Mada Maalum: Mafarisayo). Katika

maana iliyo dhahiri hawa walikuwa watu waliokuwa wameelimishwa katika Agano la Kale na katika ustadi wa Masimlizi (yaani, Buku la Sheria za Kiyahudi). Hawa walisaidia kufasiri na kutumia desturi za Kiyahudi kila siku (kama vile Sira 39:6). Kwa uwazi kabisa waandishi pia waliitwa "wanasheria" (kama vile Marko 12:28; Luka 7:30; 10:25; 11:45; 14:3). Hata hivyo, haki yao (yaani, ushikiliaji sana wa sheria za Kiyahudi na taratibu) kusikngeleta amani kwa Mungu (kama vile Mt. 5:20; Rum. 3:19-20; 9:1-5,30-32; 10:1-6; Kol. 2:20-22).

Mara nyingi hawa walikuwa wakitabiri katika injili za ki-Muhtasari (Yohana hawataji kamwe, Yohana 8:3 si halisi), kama walivyompinga Yesu, na kwa uwazi kabisa kuja kama wakuu toka Yerusalem (kama vile Marko 3:22; 7:1). Wengine, hata hivyo, walimtii (kama vile Mt. 8:19).

1. mgogoro kuhusu kula pamoja na watenda dhambi na watoza ushuru, Marko 2:16; Mt. 9:9-13
2. mgogoro kuhusu chimbuko la mamlaka ya Yesu katika upungaji pepo, Marko 3:22
3. mgogoro kuhusu kusamehe dhambi, Mt. 9:3; Luka 5:21
4. dai la ishara zishangazazo Mt. 12:38
5. mgogoro kuhusu kunawia mikono (yaani, taratibu za unawaji), Mt. 15:1-2; Marko 7:1-5
6. mgogoro kuhusu kukubaliwa kwake na umati katika kuingia kwa shangwe humo Yerusalemu, Mt. 21:15
7. sababu mashtaka ya Yesu (yaani, kutafuta heshima na ukuu), Marko 12:38-40
8. shutuma za Yesu kuhusu wao kuwa na miongozo ya kinafiki na ya kiupofu katika kiti cha Musa, Mt. 23:1-36

Kwa sababu ya ufahamu wao wa Maandiko, kwanza wangetakiwa kuwa wamekwisha mgundua na kumshikilia Yesu, lakini desturi zao (kama vile Isa. 29:13; 6:9-10) zilikuwa zimewapofusha! Nuru ilipogeuka kuwa giza, tazama jinsi giza lilivyo kuu!

**1:23 "mtu. . .mwenye pepo mchafu"** Hii ilikuwa tukio la kupagawa na pepo (kama vile Marko 1:34). Tazama namna alivyokuwa katika kuabudu, kuendeleza uonekano. Agano jipya linatenga utofauti katika udhaifu wa kimwili na kupagawa na pepo, ingawa mara kwa mara inakuwa na dalili zinazofanana. Katika tukio hili pepo ndiye anayemshurutisha mtu. Mtu huyu alipoteza utashi wake mwenyewe. Mtazamo wa Kiyahudi ulidhania na uwepo wa viumbe vyema vya Kiroho (kama vile Marko 1:13; Mt. 18:10; Mdo. 12:15; 2 Wafalme. 6:17) na uovu (kama vile Marko 1:23,26,27; 3:11,20; 5:2,8,13; 6:7; 7:25), walioathiri maisha ya watu.

## MADA MAALUMU: MALAIKA NA MAPEPO

A. Watu wa kale waliamini kwamba viumbe vyote vina uhai. Walifikiri kwamba sifa za mwanadamu ni sawa na nguvu ya asili, wanyama, na viumbe vya asili. Maisha yalielezeka kupitia mwingiliano wa uwepo wa vitu/viumbe hivi na wanadamu.
B. Mifano hii wakati mwingine ilileta matokeo ya kuabudu miungu mingi (miungu wengi). Kwa kawaida mapepo (*genii*) ilikuwa miungu midogo au nusu miungu (mizuri au miovu) ambao ilileta matokeo kadha wa kadha katika maisha ya watu binafsi.
   1. Machufuko na migogoro huko Mesopotamia,
   2. Mpangilio na kazi huko Misri,
   3. Kanaani, tazama W. F. Albright's *Archaeology and the Religion of Israel,* Toleo la Tano, kur. 67-9
C. Agano la Kale halielezi sana au kukuza jambo la miungu wadogo, malaika, au pepo, huenda ni kwa sababu ya msistizo wake mkali unaozungumzia Imani ya Mungu mmoja (tazama Mada Maalumu : Mungu mmoja Imani ya Mungu mmoja kama vile Kut. 8:10; 9:14; 15:11; Kumb. 4:35,39; 6:4; 33:26; Zab. 35:10; 71:19; 86:8; Isa. 46:9;Yer. 10:6-7; Mik. 7:18). Haliizungumzii miungu ya uongo ya mataifa ya wapagani (*Shedim*, BDB 993, kama vile Kumb. 32:17; Zab. 106:37) na halitaji majina au kufananisha baadhi yao.
   1. *Se'im* (mazimwi au majitu yenye manyoya, BDB 972 III, KB 1341 III, kama vile Law. 17:7; 2 Nya. 11:15; Isa. 13:21; 34:14)
   2. *Lilith* (jike, pepo apotoshaye kizinifu nyakati za usiku, BDB 539, KB 528, kama vile Isa. 34:14)
   3. *Mavet* (neno la Kiebrania liliotumika kumtaja mungu mwovu wa Wakanani, Mot, BDB 560, KB560, kama vile Isa. 28:15,18; Yer. 9:21; na kwa kadri iwezekavyo Kumb. 28:22)
   4. *Resheph* ( mahali, moto, au mawe yenye kutiririsha mvua ya mawe, BDB 958, KB 958, kama vile Kumb.

32:24; Zab. 78:48; Hab. 3:5)

5. *Dever* (uharibifu, BDB 184, kama vile Zab. 91:5-6; Hab. 3:5)
6. *Az'aze*l (jina halina uhakika, lakini huenda akawa pepo wa jangwani au jina la mahali, BDB 736, KB 736, kama vile Law. 16:8,10,26)

(Mifano hii inachukuliwa kutoka *Encyclopedia Judaica*, juzuu l. 5, uk. 1523.).Hata hivyo, hakuna imani ya Mungu wawili au uhuru wa malaika kutoka kwa YHWH katika Agano la Kale. Ibilisi chini ya YHWH (kama vile Ayubu 1-2; Zekaria 3), hayuko huru, ni adui anayejiongoza (kama vile A. B. Davidson, *A Theology of the Old Testament*, kr. 300-306).

D. Dini ya Kiyahudi iliendelezwa kipindi cha uhamisho wa Babeli (586-538 b.k). Kithiolojia iliathiriwa aina mbili za Kiajemi zilizochukua nafasi kwa wafuasi wa Zoroaster, mungu mkuu na mzuri aliitwa Mazda au Ormazd na mpinga uovu aitwaye Ahriman. Huyu aliruhusiwa ndani ya dini ya Kiyahudi baada ya uamisho na kuwa mfano wa aina mbili kati ya YHWH na malaika Zake na Ibilisi malaika zake au pepo.

Thiolojia ya dini ya Kiyahudi yenye kutoa mfano wa uovu inaelezwa na kunakiliwa vema katika Edersheim ya Alfred *The Life and Times of Jesus the Messiah,* juzuu. 2, kiambatisho XIII (kur. 749-863) na XVI (kur. 770-776). Dini ya Kiyahudi ilitoa mifano ya uovu katika njia tatu.

1. Ibilisi au Malaika wa maangamizi
2. kusudi la uovu (yetzer hara) ndani ya mwandamu
3. Malaika wa Mauti

Edersheim anayabainisha haya kama

1. Mshitaki
2. Mjaribu
3. Mwadhibishaji (juzuu. 2, uk. 756)

Kuna tofauti zinazodhihirika kitheolojia kati ya dini ya Kiyahudi iliyokuwepo baada ya uhamisho na nanma uwaslilishaji na maelezo ya uovu inavyofanyika ndani ya Agano Jipya.

E. Agano Jipya, haswaa Injili, linadai uwepo na upinzani wa uovu wa viumbe vya kiroho kwa mwanadamu na kwa YHWH (katika dini ya Kiyahudi, Ibilisi alikuwa adui wa mwanadamu, lakini si kwa Mungu). Hawa wanayapinga mapenzi ya Mungu, amri, na ufalme.

Yesu alikabiliana na kuvifukuza hivi viumbe vya kimapepo, pia viliitwa (1) roho chafu (kama vile. Luka 4:36; 6:18) au (2) roho za uovu kama vile. Luka 7:21; 8:2), kutoka kwa wanadamu. Yesu kwa udhihilisho alitengeneza tofauti kati ya maradhi (kimwonekano na kiakili) na hali ya kimapepo. Aliithibitisha nguvu Yake na mtazamo wa ndani wa kiroho kwa kuwatambua na kuwafahamu hawa pepo wabaya. Mara nyingi walimtambua na kumwita, lakini Yesu aliukataa ushuhuda wao, alihitaji wawe kimya, na kuyafukuzia mbali. Utambuzi wa pepo hawa ni ishara ya kuvunja ufalme wa Ibilisi.

Kuna upungufu wa ajabu wa habari ndani ya barua za Kitume za Agano Jipya kuhusiana na somo hili. Utambuzi huu kamwe haukuorodhesha karama za kiroho, wala methodolojia au hatua yake iliyotolewa kwa ajili ya vizazi vijavyo vya huduma au waamini.

F. Mwovu yu dhahiri; mwovu ni mtu binafsi; mwovu yupo. Si asili yake wala kusudi lake linalofunuliwa. Biblia inatetea ukweli wake na kwa ukali inapinga ushawishi wake yule mwovu. Ndani ya ukweli hakuna hatima yenye mitazamo yenye uwili ndani yake. Mungu yu ndani ya utawala wake mwenyewe ; mwovu anaangamizwa na kuhukumiwa na ataondolewa kutoka katika uumbaji.

G. Watu wa Mungu yawapasa kumpinga mwovu (kama vile Yakobo 4:7). Hawawezi kutawaliwa na naye (kama vile 1 Yohana 5:18), bali wanaweza kujaribiwa na ushuhuda na ushawishi wake kuangamizwa (kama vile Efe. 6:10-18). Mwovu ni sehemu ya mtazamo wa ulimwengu kwa wakristo uliofunuliwa. Wakristo wa sasa hawana haki ya kueleza wazi kwa mara nyingine (kutafasiri upya maandishi ya Rudolf Baltmann); kuyaua maovu (miundo ya kijamii ya Paul Tillich), wala kujaribu kuelezea kwa ukamilifu katika namna ya kisaikolojia (Sigmund Freud). Ushawishi wake umeenea kote, lakini umeangamizwa. Waamini wanahitaji kuenenda ndani ya ushindi wa Kristo!

**1:24**

**NASB** **"tuna vitu gani vya kufanya pamoja"**

**NKJV** **"unataka tufanyeje na wewe"**
**NRSV** **"unataka utufanye nini"**
**TEV, NJB** **"unatutaka nini"**

Hii kibayana "kile kinachofanyika kwetu na kwenu." Katika *A Translator's Handbook on the Gospel of Mark* Bratcher na Nida utagundua kwamba "Katika Uyunani wa zamani tungo ingemaanisha 'tuna nini cha kufanana mimi na wewe?' Hapa, hatahivyo, inashabihiana na Waebrania 'Kwanini kuingilia shughuli zangu'" (ukurasa 49). Nahau hii inaelezwa katika Waamuzi 11:12; 2 Sam. 16:10; 19:22; 1 Wafalme. 17:18; 2 Nyakati. 35:12.

◙ **"Yesu wa Nazareti"** Angalia angalizo katika Marko 10:47.

◙ **"'Je umekuja kutuharibu '"** Kisarufi hii inaweza kuwa aidha swali au kauli. Hii ilikuwa nahau ya Agano la Kale ya uadui (kama vile Waaamuzi.11:12; 2 Sam. 16:10; 19:22; 1 Wafalme. 17:18; 2 Wafalme. 3:13; 2 Nyakati. 35:21). Uovu unajua kwamba siku moja utahukumiwa!

◙ **"'Aliye Mtakatifu wa Mungu'"** Hii lilikuwa ni jina la ki-Masihi la Agano la Kale. Hii Itakuwa ukiri wa kujitoa lakini jaribio lililopigiwa hesabu kusababisha usumbufu kwa Yesu. Yesu baadaye alishutumiwa kwa kupokea nguvu kutoka kwa Shetani (kama vile Mt. 9:34; 12:24; Marko 3:22; Luka 11:15).

## MADA MAALUM : ALIYE MTAKATIFU

I. "Aliye Mtakatifu wa Israeli" ni jina la Uungu lililoshamiri katika Isaya (kama vile Isa. 1:4; 5:19; 10:17,20; 12:6; 17:7; 29:19,23; 30:11,12,15; 31:1; 37:23; 40:25; 41:14,16,20; 43:3,14,15; 45:11; 47:4; 48:17; 49:7; 54:5; 55:5; 60:9,14). Kwa sababu Yeye ni "mtakatifu," watu Wake yawapasa kuwa watakatifu (kama vile Law. 19:2; Mt. 5:48; 1 Pet. 1:16).

Jina hili, katika maana, linaeleza mvutano usiowezekana wa wenye dhambi, watu walioanguka kutii na kuingia katika kiwango cha utakatifu. Agano la Musa halikuwa na uwezekano wa kuutunza (kama vile Yos. 24:19; Matendo 15; Wagalatia 3; kitabu cha Waebrania). Agano la kale lilikuwa ni njia ya kuonyesha kutowezekana kwa wanadamu kukitii kiwango cha Mungu (Wagalatia 3), bado alikuwa pamoja nao, kuwaandaa kwa ajili ya jibu Lake katika hali ya kuanguka kwao (yaani, "Agano Jipya katika Yesu"). Akishusha kiwaango Chake, bali alikitoa kupitia Masihi Wake. Agano Jipya (kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:22-38) ni agano la imani na toba, na si utendaji wa mwanadamu, ingawa linatoa Ufanano wa Kristo (kama vile Yakobo 2:14-26). Mungu anamtaka mtu anaeangaza tabia yake kwa mataifa (kama vile Mt. 5:48).

II. "alivyo mtakatifu" inaweza kurejea juu ya
1. Mungu Baba (kama vile vifungu vingi vya Agano la Kale juu ya "aliye Mtakatifu wa Israeli")
2. Mungu Mwana (kama vile Mk 1:24; Luk. 4:34; Yohana 6:69; Matendo 3:14; 1 Yohana 2:20)
3. Mungu Roho (jina Lake, "Roho Mtakatifut" kama vile Yohana 1:33; 14:26; 20:22).

Matendo 10:38 ni mstari ambapo watu wote wa asili ya Mungu wanahusishwa katika kupakwa mafuta. Yesu alipakwa mafuta (kama vile Luka 4:18; Matendo 4:27; 10:38). Dhana imepanuka ili kuwajumuisha waamini wote (kama vile 1 Yohana 2:27). Aliyepakwa mafuta amekuwa mpakwa mafuta! Hii inaweza kuwa sambamba na Mpinga Kristo au wapinga Kristo (kama vile 1 Yohana 2:18). Katika Agano la Kalelilikuwa ni tendo la kiishara la kimwali la kumiminia mafuta (kama vile Kut. 29:7; 30:25; 37:29) inahusiana na wale ambao waliitwa na kuandaliwa na Mungu kwa ajili ya kuifanya kazi yake maalumu (yaani, manabii, makuhani, na wafalme). Neno "Kristo" ni tafsiri ya neno la Kiebrania "aliye pakwa mafuta" au Masihi.

**1:25 "Yesu akamkemea"** Marko anatumia kitenzi hiki mara kwa mara: (1) mara nyingi kwa ajili ya pepo (kama vile Marko 1:25; 3:2; 9:25); (2) wa upepo na bahari (kama vile Marko 4:39); na (3) kwa Wanafunzi Wake (kama vile Marko 8:30,33; 10:13).

◙ **"'nyamaza'"** Hii ni kauli tendwa shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu "kufunga kinywa" (kama vile Marko 4:39). Amri mbili za Yesu zikielekezwa kwa pepo ni maneno yenye nguvu ikiwa na mfanano hasi.

◙ **"mtoke"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu.

## MADA MAALUM : UPUNGAJI PEPO

Upungaji Pepo yalikuwa mambo ya kawaida katika siku za Yesu, lakini njia za Yesu zilikuwa tofauti sana (kama vile Mt. 8:16; Marko 1:27). Upungaji Pepo Wake ilikuwa ishara ya Zama Mpya (kama vile Luka 9:1). Walimu wa Sheria za Kiyahudi (kama vile Mt. 12:27; Matendo ya Mitume 19:13) walitumia njia za nguvu za giza (tazama Alfred Edersheim, *The Life and Times of Jesus, The Messiah*, juzuu. 2, kiambatisho XIII, uk. 748-763; XVI, kur. 770 -776), lakini Yesu alitumia mamlaka yake Mwenyewe. Kuna mkanganyiko mkubwa na habari mbaya zinazoenea kwa sasa kuhusu upungaji pepo na pepo wachafu. Sehemu ya tatizo hili ni kwamba Agano Jipya haijadili juu ya mambo haya. Kama mchungaji natumaini ninayo habari zaidi kuhusu jambo hili. Hapa kuna baadhi ya vitabu ninavyoviamini.

1. Christian Counseling and the Occult, Kurt E. Koch
2. Demons in the World Today, Merrill F. Unger
3. Biblical Demonology, Merrill F. Unger
4. Principalities and Powers, John Warwick Montgomery
5. Christ and the Powers, Hendrik Berkhof
6. Three Crucial Questions About Spiritual Warfare cha Clinton Anton

Hii inanishangaza kwamba upungaji pepo haukuorodheshwa kama moja ya karama za kiroho na suala hilo halielezwi ndani ya barua za ki-Utume. Naamini katika mtazamo wa kiulimwengu kibiblia unahusisha ufalme wa kiroho (yaani, mema na mabaya), wakati uliopo na tendaji katika ufalme wa kiroho (yaani, Ayubu 1-2; Danieli 10; Efe. 6:10-18). Hata hivyo, Mungu amechagua kutofunua ule ubaya. Sisi kama waamini habari zote, tunahitaji kuishi ki-Ungu, maisha yenye manufaa Kwake! Lakini mambo mengine hayajafunuliwa kwa ukamilifu au kuimarishwa. Waamini wanahitaji kukumbuka kwamba upungaji pepo ni ushahidi unaonekana juu ya ushindi wa Yesu dhidi ya uovu (kama vile Luka 10:17-20). Kitabu cha Agano Jipya kinaunda tofauti iliyo wazi kati ya upungaji pepo na uponyaji (kama vile Mt. 8:16; Marko 1:32; Luka 4:40-41).

Tazama Mada Maalum:

1. Mada Malum: Shetani
2. Mada Maalum: Uovu Binafsi
3. Mada Maalum: Pepo Wachafu katika Agano la Kale

Mada Maalum: Pepo Wachafu katika Agano Jipya

**1:26** Udhihirisho kadhaa wa kimwili wa mapepo wachafu kumuacha mtu unaandikwa (kama vile Marko 1:26; 9:26; na Luka 9:39). Hii inaweza kuwa ni njia ya kuthibitisha kwamba pepo kweli lilikuwa limetoka. Hii ni ishara ya kwanza ya nguvu inaonesha wazi maana ya kimasihi ya Yesu. Jina la Agano la Kale (kama vile Zab. 16:10) ambayo mapepo yalimtambua Yeye na nguvu Zake kudhibiti na kuhukumu sawasawa kunaksi mamlaka ya kiroho ya Yesu wa Nazareti (kama vile Marko 1:27c). Habari hii inafanana na Luka 4:31-37.

**1:27 "'Mafundisho mapya yenye mamlaka'"** Hili ni neno la Kiyunani kwa "mpya" (yaani, *kainos*) yenye maana "jambo jipya lenye ubora," sio "jipya katika kipengele cha muda." Tungo "kwa mamlaka" inaweza kurejerea mafundisho ya Yesu (kama vile Mt. 7:29; NASB, NRSV, NJB) au kwa amri za Yesu (kama vile Luka 4:36; NKJV, TEV). Tokea Luka 4:36 ni ufanano wa moja kwa moja, mbadala wa pili unaonekana kuwa bora. Chanzo cha mamlaka ya Yesu ingefanyika jambo kuu kati ya Yesu na viongozi wa kiyahudi (kama vile Marko 11:28; Mt. 21:23; Luka 20:2). Walishindwa kukataa nguvu zake hivyo walianza kuhoji chanzo chake. Hii ni dhambi isiyosameheka!

**1:28 "mara"** Angalia Angalizo katika Marko 1:10.

◙ **"habari zake zikaenea kila mahali"** Upungaji pepo wa wazi ungetakiwa usemwe na kutajwa tena na tena kwa kurudia rudia.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 1:29-31**
**[29] Na mara walipotoka katika sinagogi, walifika nyumbani kwa Simoni na Andrea, pamoja na Yakobo na Yohana. [30] Naye mkwewe Simoni, mamaye mkewe, alikuwa kitandani, hawezi homa; na mara wakamwambia habari zake. [31] Akamkaribia, akamwinua kwa kumshika mkono, homa ikamwacha, akawatumikia.**

**1:30 "Naye mkwewe Simoni"** Hii inaonesha kuwa Petro alikuwa ameoa. Mkewe hakuwahi kutajwa katika Agano Jipya. Angeweza kuwa amekufa lakini 1 Kor. 9:5 inamaanisha alisafiri na Petro. Habari hii inafanana katika Luka 4:31-37 na Mt. 8:14-17.

◙ **"alikuwa amelele hawezi"** Hii ni njeo ya wakati usio timilifu inayoonesha tendo linaloendelea wakati uliopita. Alikuwa mgonjwa kwa muda fulani.

◙ **"mwenye homa"** Hii kibayana inamaanisha "kushikwa na homa." Hii ni njeo ya wakati uliopo, yenye kumaanisha tatizo linaloendelea. Tambua ugonjwa huu haukuhusianishwa na kupagawa na pepo (kama vile Marko 1:32). Nguvu ya Yesu dhidi ya magonjwa ni ishara ingine ya Utu wake na makusudi yake ya Ki-Masihi. Kama ilivyo mara kwa mara katika Injili miujiza ya Yesu ilikuwa mingi kwa ajili ya wanafunzi kama ilivyo kwa wapokeaji wengine. Yesu anajifunua mwenyewe kwa mitume wake wapya aliowachagua. Hapa anatenda kazi kwa huruma siku ya Sabato. Hii lazima iliwashangaza sana watu hawa wayahudi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 1: 32-34**
**[32] Hata kulipokuwa jioni, na jua limekwisha kuchwa, walikuwa wakimletea wote waliokuwa hawawezi, na wenye pepo. [33] Na mji wote ulikuwa umekusanyika mlangoni. [34] Akaponya wengi waliokuwa na maradhi mbalimbali, akatoa pepo wengi, wala hakuwaacha pepo kunena, kwa sababu walimjua.**

**1:32 "kulipokuwa jioni"** Inavyoonekana hii ilikuwa baada ya machweo, hivyo Sabato ilikuwa imekwisha na uponyaji wa mwili ulikuwa unaruhusiwa kwa taratibu za kiyahudi.

◙ **"wakimletea"** Hii ni njeo ya wakati usio timilifu unaomaanisha "kuendelea kubeba." Yesu hakutaka kujulikana kama mtengeneza miujiza lakini mtangazaji wa ukweli (kama vile Luka 4:43), lakini habari zilikuwa zishasambaa (kama vile Marko 1:28).

◙ **"waliokuwa hawawezi"** Mstari wa 32 unamaanisha kwamba "wote" waliokuwa wakiumwa au kupagawa na pepo katika mji mzima waliletwa kwa Yesu. Mstari wa 34 unasema kwamba aliwaponya na kuwaokoa "wengi" wao, lakini si kila mtu. Inashangaza kwamba maneno "wote" na "wengi" mara kwa mara inatumika kwa ufanano katika Biblia (kama vile Isaya 53:6 dhidi ya 53:11,12 na Rumi. 5:18. dhidi ya 19). Haijulikani ikiwa ikiwa Yesu aliwaponya wote walioletwa kwake au aliponya wengi wao tu. Katika bwawa la Bethsaida Yerusalemu, inaandikwa kwamba Yesu alimponya mmoja katika wagonjwa wote waliokuwepo. Yesu hakutoka katika njia yake ili kuponya lakini pale hali ilipokuwa njema alijidhihirisha (yaani muda wa kuponya kwa wanafunzi na ukiongeza huruma ya Yesu kwa walioumizwa na wenye mahitaji) Alitenda kazi kwa nguvu. Hakutoka katika kusudi lake akizunguka na kufanya uinjilishaji (yaani Mwanamke Msamaria, kama vile Yohana 4, haswa Marko 1:4). Uponyaji ulikuwa ishara lakini uinjilisti ulikuwa na makusudi na shabaha ya huduma Yake. Kuna baadhi ya mkanganyiko kuhusu mbinu ya Yesu katika uponyaji; wakati mwingine inategemea mwitikio wa imani wa watu wanaoumwa, wakati mwingine juu ya imani ya mtu au ndugu na marafiki wa wapendwa na mara kwa mara kwa ajili ya kusudi la kuonesha nguvu Zake, isiyohusiana na sehemu ya mpokeaji. Wokovu hakuambatana moja kwa moja na ukombozi wa mwili na uponyaji.

◙ **"wengi waliokuwa wamepagawa na pepo"** Tazama tofauti kati ya ugongwa na kupagawa na pepo.

**1:33** Hawa watu wa mjini walikuwa na shauku na wengine walitamani kuwa na afya zao za mwili na uzima wa kiroho.

**1:34 "akawaponya wengi"** Mstari huu ni wa kwanza kati ya mistari mingi ya kitabu cha Marko (kama vile Marko 1:34,43-44; 3:12; 4:11; 5:43; 7:24,36; 8:26,30; 9:9) ambayo mara nyingi imekuwa ikirejerewa kama "Siri ya Ki-Masihi ya Marko." Yesu anawaambia wanafunzi na wale aliowaponya kutosema juu ya tendo la uponyaji. Yesu hakutaka kujulikana kama tu mponyaji au mtenda miujiza. Hizi zilikuwa ni ishara tu zilizokuwa zikionesha U-Masihi Wake, ambao katika hatua hii katika maisha yake ulikuwa haujafunuliwa kikamilifu. Yesu alikuja ili (1) Kumfunua baba; (2) kujitoa Yeye mwenyewe kama dhabihu kwa ajili ya dhambi; na (3) kuwapa waamini mfano wa kufuata. Uponyaji na ukombozi ulikuwa ni ishara tu za huruma Yake kwa ajili ya wadhaifu, wagonjwa na wakuja. Hii ilikuwa pia ishara ya Agano la Kale iliyotabiriwa ya huduma ya Masihi (kama vile Isa. 61:1).

▣ **"hakuruhusu mapepo wazungumze"** Hii ni njeo ya wakati usio timilifu, ikiashiria kupunga pepo kadhaa (kama vile Marko 1:24). Angalia Mada Maalum juu ya mapepo katika Marko 1:24.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 1:35-39**
**35 Hata alfajiri na mapema sana akaondoka, akatoka akaenda zake mahali pasipokuwa na watu, akaomba huko. 36**
**Simoni na wenziwe wakamfuata; 37 nao walipomwona wakamwambia, Watu wote wanakutafuta. 38 Akawaambia,**
**Twendeni mahali pengine, mpaka vijiji vilivyo karibu, nipate kuhubiri huko nako; maana kwa hiyo nalitokea. 39**
**Akaenda akihubiri katika masinagogi yao, katika nchi yote ya Galilaya, na kutoa pepo.**

**1:35 "Hata alfajiri na mapema sana wakati bado giza"** Hii inarejerea majira ya usiku, wakati mwingine ni kati ya saa 9:00 na 12:00 alfajiri.

◙ **"akaomba huko"** Hii ni njeo ya wakati usio timilifu ambao unaonesha maisha ya mara kwa mara ya kimaombi ya Yesu. Katika Injili ya Luka msisitizo huu unarudiwa mara kwa mara. Katika Marko, kuna mifano mitatu tu ya Yesu akiomba: hapa, kulishwa kwa watu elfu tano (kama vile Marko 8:6), katika Gethsemane (kama vile Marko 14:32-42).

**1:37-39** Watu walikuwa wakimtafuta Yesu kwasababu alikuwa amewaponya, si kwasababu ya mafundisho Yake (kama vile Luka 4:43). Yesu muda wote alikuwa katika kazi kwasababu (1) Alitaka wote wasikie ujumbe Wake na (2) kusudi Lake lilieleweka vibaya.

**1:38**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"hicho ndicho nilichokuja kufanya"** |
| **NKJV** | **"kwasababu hiyo nalikuja"** |
| **NRSV** | **"kwakuwa hicho ndicho nilichokuja kufanya"** |
| **TEV, NJB** | **"kwasababu hiyo ndiyo sababu nalikuja"** |

Yesu alijua kwa ndani kabisa kwamba ametumwa (kama vile Luka 4:43) kutangaza injili ya Mungu (kama vile Marko 1:14-15). Alijua kwamba hakutumwa awe mtenda miujiza au mponyaji lakini kama muanzishaji wa siku mpya, uhusiano mpya na baba, uanzishaji rasmi na ufunguzi wa ufalme wa Mungu! Umuhimu wake Yeye kama mtu, maudhui ya ujumbe Wake, matendo Yake ya kiukombozi na Ufufuo wake wa utukufu na kupaa kulikuwa shabaha ya Ujumbe wake. Siri ya Ki-Masihi ya Marko ni njia ya kisarufi ya kuelezea kwamba vitu hivi visingeeleweka kwa ukamilifu au kufunuliwa mpaka miaka ya baadaye.

**1:39** Kuna utofauti wa kimaandiko katika Marko 1:39. Baadhi ya maandiko ya kale ya Kiyunani yana "akaondoka" (kama vile א, B, L, toleo la Kishamu ya Palestina, na fasiri za koptiki, pia NASB, NRSV, TEV, NJB), wakati maandiko ya Kiyunani yana A, C, D, W, matoleo ya Vulgate, na Peshitta pia fasiri za maandiko ya kiyunani yaliyotumika na Augustine yana "alikuwa" (kama vile NKJV). Toleo la *Textual Commentary on the Greek NewTestament* lililoandikwa na Bruce Metzger, kurasa za 75-76, zinaelezea kwamba wanakili walibadili "aliondoka" ili kuwe na ufanano wa Luka 4:44. Huu ni mfano mzuri wa ukweli kwamba tofauti zilizoko katika maandiko mengi ya Kiyunani hayana athari yoyote kithiolojia au kutengeneza utofauti wa kihistoria juu ya maana nzima ya hadithi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 1:40-45**
**40 Akaja kwake mtu mwenye ukoma, akamsihi na kumpigia magoti, na kumwambia, Ukitaka, waweza kunitakasa. 41 Naye akamhurumia, akanyosha mkono wake, akamgusa, akamwambia, Nataka, takasika. 42 Na mara ukoma wake ukamtoka, akatakasika. 43 Akamkataza kwa nguvu, akamwondoa mara, 44 akamwambia, Angalia, usimwambie mtu neno lolote, ila enenda zako ukajionyeshe kwa kuhani, ukatoe alivyoamuru Musa kwa kutakasika kwako, iwe ushuhuda kwao. 45 Lakini akatoka, akaanza kuhubiri maneno mengi, na kulitangaza lile neno, hata Yesu asiweze tena kuingia mjini kwa wazi; bali alikuwako nje mahali pasipokuwa na watu, wakamwendea kutoka kila mahali.**

**1:40 "mkoma"** Hii inafanana na ile katika Mt. 8:2-4 na Luka 5:12-16. Uyahudi ulichukulia ukoma kama ugonjwa uliotolewa kama adhabu na Mungu (kama vile 2 Nyakati 26:16-21). Kugusana na mkoma kungesababisha mtu kuwa najisi mbele ya wengine. Ugonjwa huu ulimaanisha kutengwa kabisa kijamii! Inashangaza sana kidesturi kwamba mtu huyu anayetengwa alimsogelea Yesu na kwamba Yesu alimgusa (kama vile Marko 1:41). Magonjwa ya Agano la Kale kaa ukoma yanajadiliwa katika Law. 13-14, inaelezea aina nyingi za magonjwa ya ngozi, yote ambayo yangeweza kumfanya mtu atengwe katika ibada.

◙ **"kumpigia magoti"** Katika Luka 5:12 inasema kwamba alianguka kifudifudi mbele za Yesu. Yesu hakuwa kama walimu wengine wa Sheria. Alichukua muda wa kuwajali watu wa kuja na waliotengwa wakihesabiwa kuwa wasiofaa.

◙ **"'Ukitaka, waweza kunitakasa '"** Hii ni sentensi ya daraja la tatu yenye masharti ambayo inamaanisha tendo halisia. Hakuwa anatilia mashaka uweza wa Yesu (yaani mkoma alimuita Yesu "Bwana" katika Mt. 8:2), lakini shauku Yake ya yeye kutenda.

**1:41 "Naye akamhurumia"** Yesu alijali wanadamu walioumbwa katika mfano wa Mungu. Andiko la Kimagharibi, MS D, lina "akachukizwa," lakini toleo la MSS א, A, B, na C lina "huruma." Maneno yanafanana katika Kiaramu. Ingawa maandiko ya zamani kabisa na bora kabisa yana "huruma" andiko lisilo la kawaida kabisa lingesomeka kama "akachukizwa" au "akapatwa na hasira." Angalia kiambatisho cha Pili katika Uhakiki wa Kimaandiko. Kuna maeneo mengine kadhaa katika Marko ambapo hasira ya Yesu inaandikwa katika muktadha usiotegemewa (kama vile Marko 1:43; 3:5 na 10:14; pia moja katika Yohana 11:33, 38). Hasira Yake ingeweza kuelekezwa kwenye magonjwa au uovu wa kizazi hiki. Marko anaonesha Yesu kama mwanadamu mkamilifu, mwenye hisia na akionesha hisia za kibinadamu juu yake mwenyewe na kwa wengine.

1. huruma au hasira (Marko 1:41; 3:5)
2. njaa ya kimwili (Marko 2:25)
3. kuhuzunishwa/kusononoshwa sana (Marko 7:34, 8:12)
4. kuchukizwa na kukaza uso (Marko 10:14)
5. upendo (Marko 10:21)
6. kuomboleza na kuwa katika tatizo (Marko 10:33-34)
7. kuachwa (Marko 15:34)
8. kiu (Marko 15:36)

◙ **"akamgusa"** Hii kidesturi ilikuwa ni "hapana! hapana!" Yesu kuwagusa watu ni jambo linalotokea na kuwa kawaida katika Injili (kama vile Marko 7:33; 8:22; 10:13; pia mara kadhaa watu walimgusa Yesu, mfano Marko 3:10; 5:22-28,30,31; 6:56) kama ishara ya kujali kwake binafsi na kujihusisha na mambo ya wengine.

◙ **"'takasika'"** Hii ni kauli tendwa shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu. Yesu anaponya kwa mamlaka yale yale ya binafsi kama ambavyo anavyofanya akifukuza mapepo.

**1:43 "Akamkataza kwa nguvu"** Hii kibayana ni "kupumua kwa kutoa hewa kwa nguvu," ambayo inamaanisha kilio kisichotoa sauti. Hii inaaksi Siri ya Kimasihi ya Marko. Injili ilikuwa bado haijakamilika, na ujumbe ulikuwa bado haujakamilishwa. Yesu hakutaka kujulikana kama mtenda miujiza.

◙ **"akamwondoa mara"** Hili ni neno la nguvu lililotumika na Roho kumpeleka Yesu nyikani (kama vile Marko 1:12).

**1:44 "'ukatoe alivyoamuru Musa'"** Hitaji hili lilifanana na kuhusiana na kuponywa kwa ukoma (kama vile Law 13, 14; Kumb. 24:8). Yesu hakukataa Agano la Kale (kama vile Mt. 5:17-19), lakini masimulizi ya mdomo ambayo yalikuwa yamekuzwa ndani ya dini ya Kiyahudi (kama vile Mt. 5:21-48). Yawezekana hii pia ilikuwa kwa ajili ya makuhani.

**1:45 "kulitangaza"** Hii ni tungo jina ya wakati uliopo. Huu ulikuwa ni ukaidi wa moja kwa moja kwa ombi ambalo alikuwa amepewa na Yesu (kama vile Marko 1:43-44).

◙ **"pasipokuwa na watu"** Hii inamaanisha eneo la malisho lisilokaliwa na makazi ya watu kama Marko 1:3.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini Marko inaanza na huduma ya Yohana Mbatizaji? Yeye anamwakilisha nani?
2. Je ubatizo unawekeza au kuwakilisha msamaha?
3. Je Yesu alibatizwa? Je alikuwa mwenye dhambi na mwenye kuhitajika kufanya toba?
4. Sehemu gani ya kipengele hiki ambayo ni ushahidi kwa umaanishwaji wa Utatu?
5. Kwanini Yesu alijaribiwa? Ni katika maeneo gani ya maisha Yake majaribu yalitokea?
6. Je ufalme wa Mungu upo hapa au utakuja baadaye?
7. Je Marko 1 inaeleza Yesu kukutana na wavuvi kwa mara ya kwanza?
8. Kwanini watu wa hekaluni katika Karpernaumu walishangazwa na mafundisho ya Yesu?
9. Je kupagawa na mapepo ni halisia au ni ushirikina wa kimila?
10. Kwanini mapepo yalifunua Yesu ni nani?
11. Kwanini utakasaji wa mkoma ulionekana kuwa jambo kubwa sana?
12. Kwanini Yesu alimwamuru mkoma asimwambie mtu kile kilichofanyika kwake?

# MARKO 2

| MIGAWANYO YA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Uponyaji wa Mtu aliyepooza | Yesu anamsamehe na kumponya Aliyepooza | Kumponya Aliyepooza | Yesu anamponya Mtu Aliyepooza | Tiba ya Aliyepooza |
| 2:1-12 | 2:1-12 | 2:1-1 | 2 2:1-5 | 2:1-12 |
| | | | 2:6-7 | |
| | | | 2:8-11 | |
| | | | 2:12 | |
| Kuitwa kwa Lawi | Mathayo Mtoza Ushuru | Kuitwa kwa Lawi | Kuitwa kwa Lawi | Kuitwa kwa Lawi |
| 2:13-17 | 2:13-17 | 2:13-14 | 2:13-14 | 2:13-14 |
| | | | | Kula pamoja na Watenda dhambi |
| | | 2:15-17 | 2:15-16 | 2:15-17 |
| | | | 2:17 | |
| Maswali kuhusu Kufunga | Yesua anaulizwa Kuhusu kufunga | Kufunga | Mjadala kuhusu Kufunga | |
| 2:18-20 | 2:18-22 | 2:18-20 | 2:18 | 2:18-22 |
| | | | 2:19-20 | |
| 2:21-22 | | 2:21-22 | 2:21-22 | |
| Kuvunja Masuke wa Sabato | Yesu ni Bwana za Sabato | Yesu na Sheria Sabato | Swali kuhusu siku ya Sabato | Kuchambua Masuke Siku ya Sabato |
| 2:23-28 | 2:23-28 | 2:23-28 | 2:23-24 | 2:23-26 |
| | | | 2:25-26 | |
| | | | 2:27-28 | 2:27-28 |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (<u>kutoka " Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia"</u>)**

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo wa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Marko 2:1-3:6 inahusiana na matukio manne yaliyotukia wakati wa ziara inayozungumziwa katika Marko 1:38-39.
   1. kusikia (Marko 2:1-12)
   2. kulifikia kundi lililokataliwa (Marko 2:13-17)
   3. swali kuhusu kufunga (Marko 2:18-20)
   4. mkanganyiko kuhusu desturi (Marko 2:23-38)

B. Marko 2:1-3:6 ni mkusanyiko wa kifasihi ambao unaonyesha kupanuka kwa upinzani juu ya Yesu kutokana na mtiririko wa kimamlaka. Yesu mwenyewe alitenda kinyume na Desturi zao (yaani., Buku la sheria na maadili ya Kiyahudi) ili kuibua mjadala wa kithiolojia kwa viongozi wa kidini. Tazama marudio ya neno "mbona" (Marko 2:7,16,18,24).

C. Ufanano
   1. Marko 2:1-12 — Mt. 9:1-8; Luka 5:12-26
   2. Marko 2:13-17 — Mt. 9:9-13; Luka 5:27-32
   3. Marko 2:18-22 — Mt. 9:14-17; Luka 5:33-39
   4. Marko 2:23-25 — Mt. 12:1-8; Luka 6:1-5

D. Yesu alikuja kumfunua Baba. Dini ya Kiyahudi imemficha katika taratibu na sheria. Yesu inaifunua chuki ya viongozi wa Kiyahudi na mipango yao ya migogoro kumhusu iliyoandikwa katika Marko. Mambo haya yanatoa ufafanuzi kuhusu tofauti kati ya Sheria za Dini ya Kiyahudi na uhuru wa agano jipya la Yesu na dini ya kweli .
   1. mamlaka ya Yesu kusamehe dhambi (Marko 2:1-12)
   2. umuhimu wa kufunga (Marko 2:18-22)
   3. umuhimu wa kuitunza sheria za Sabato (Marko 2:23-28)
   4. umuhimu wa kuzitunza desturi (Marko 7:1-8)
   5. suala la talaka (Marko 10:2-9)
   6. kutoa ushuru huko Rumi (Marko 12:13-17)
   7. asili ya ufufuo (Marko 12:18-27)
   8. amri (Marko 12:28-34)

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 2:1-12**
**[1] Akaingia Kapernaumu tena, baada ya siku kadha wa kadha, ikasikiwa ya kwamba yumo nyumbani.**
**[2] Wakakusanyika watu wengi, isibaki nafasi hata mlangoni; akawa akisema nao neno lake. [3] Wakaja watu**
**wakimletea mtu mwenye kupooza, anachukuliwa na watu wanne. [4] Na walipokuwa hawawezi kumkaribia kwa**
**sababu ya makutano, waliitoboa dari pale alipokuwapo; na wakiisha kuivunja wakalitelemsha godoro alilolilalia**

**yule mwenye kupooza. [5] Naye Yesu, alipoiona imani yao, akamwambia yule mwenye kupooza, Mwanangu, umesamehewa dhambi zako. [6] Na baadhi ya waandishi walikuwako huko, wameketi, wakifikiri mioyoni mwao, [7] Mbona huyu anasema hivi? Anakufuru. Ni nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa mmoja, ndiye Mungu? [8] Mara Yesu akafahamu rohoni mwake kwamba wanafikiri hivyo nafsini mwao, akawaambia, Mbona mnafikiri hivi mioyoni mwenu? [9] Vyepesi ni vipi, kumwambia mwenye kupooza, Umesamehewa dhambi zako, au kusema, Ondoka, ujitwike godoro lako, uende? [10] Lakini mpate kujua ya kwamba Mwana wa Adamu anayo amri duniani ya kusamehe dhambi, (hapo amwambia yule mwenye kupooza), [11] Nakuambia, Ondoka, ujitwike godoro lako uende nyumbani kwako. [12] Mara akaondoka, akajitwika godoro lake, akatoka mbele yao wote; hata wakastaajabu wote, wakamtukuza Mungu, wakisema, Namna hii hatujapata kuiona kamwe.**

**2:1 "Kapernaumu"** Hili jina linamaanisha "kijiji cha Nahumu." Kwa sababu ya kutokuamini kwa watu wa huko Nazareti, Yesu aliuchagua mji huu ulio ndani ya Galilaya (kama vile Mt. 4:13) kama makazi yake makuu. Mji huu ulikuwa kandokando ya njia kuu itokayo Dameski hadi Misri. Kwa mjadala zaidi tazama *Cities of the Biblical World* na Moine F. DeVries, kr. 269-275.

◙ **"ikasikiwa"** Sifa njema za Yesu zilisababaisha watu kuja kumuona (yaani, wagonjwa, wadadisi, wenye mahitaji ya kweli, na viongozi wa kidini). Maneno ya Yesu yanaelezwa mara kwa mara kwa makundi tofautitofauti katika hadhira, lakini kwa kundi lile ambalo halikuandikwa mara kwa mara.

◙ **"yumo nyumbani"** Kwa vyo vyote vile hapa ni nyumbani kwa Petro ama numbani kwa Mariamu au nyumba ya kukodi haijulikani.

**2:2 "Wakakusanyika watu wengi"** Katika jamii za mashariki mlango ulio wazi unamaanisha "kuingia moja kwa moja," na walifanya hivyo.

◙**"isibaki nafasi hata mlangoni"** Pengine kulikuwa na uwanja mdogo, lakini hata hivyo, nyumba hii isingetosha kuwahifadhi watu wengi.

◙**"akawa akisema nao neno lake"** Hii ni Kauli tendaji elekezi ya wakati usio timilifu, ambayo inaweza kueleweka kama (1) mwanzo wa tendo au (2) kujirudia kwa tendo. Hili "neno" linaurejelea ujumbe wa Yesu wa mara kwa mara ulioelezwa katika Marko 1:14-15. Ishara zake na matendo yake vilibadilika, lakini kiini cha ujumbe wake kilibakia vile vile.

**2:3 "mtu mwenye kupooza"** Huu ni muungano wa kifungu "kupoteza "na"kandokando ya." Bila shaka huyu alikuwa mhanga wa ugonjwa wa kiharusi, mwenye kupooza kupooza upande mmoja. Matendo ya Yesu yalikuwa na sababaua pacha: (1) kutimiza unabii wa ki-Masihi wa Isa. 61:6 na (2) kuutangaza Uungu wake na mamlaka yake kwa kusamehe dhambi. Kwa wale waliokuwa na macho ya kiroho jambo hili lilikuwa sahihi, dhambi isiyo na utata!

**2:4 "waliitoboa dari"** Kiuhalisia "waliezua paa." Dari zilikuwa wazi mtaani na sehemu ambazo ni mahali pa kusanyiko la kijamii. Mara nyingi dari hizi zilikuwa tambarare na zilitengenezwa kwa tope na matawi yenye kufunikwa kwa majani. Luka 5:19 ina neno "matofali" ambapo inaweza kumaanisha uwanja. Hebu fikiri Yesu anaendelea kufundisha huku vipande vya dari vikiwaangukia.

◙ **"godoro"** Hili lilikuwa jamvi dogo lililotengenezwa kwa majani ambapo lilitumika kulalia.

**2:5 "imani yao"** Yesu aliiona imani ya marafiki waliokuwa wameambatana na yule mwenye kupooza na imani yake mtu huyo na kutenda kwa niaba ya imani yao.

◙ **"umesamehewa dhambi zako "** Huenda au bila shaka huu ulikuwa uchokozi wa makusudi kwa viongozi wao wa kidini waliokuwa eneoe lile. Pia Yetu alikuwa akiimarisha imani ya mtu huyu. Wayahudi waliamini kuwa kulikuwa na uhusianao kati ya yule mgonjwa na dhambi (kama vile Ayubu; Yohana 9:2; Yakobo 5:15-16). Mtu huyu alikuwa na hofu kwamba kwa namna fulani dhambi yake ilikuwa sambamba na kupooza kwake. Toleo la UBS[4] lina kauli tendwa elekezi ya wakati uliopo. Baadhi ya mandiko mengine ya Kiyunani yana kauli tendwa elekezi ya wakati timilifu (kama vile P[88], א,A, C, D, L, W), ambayo ni sawa na Luka 5:20. Hata hivyo, Mt. 9:2 na MS B zina kauli tendwa elekezi ya wakati uliopo. Ni vigumu kuchagua upi uchagauzi halisi kati ya chaguzi hizi.

**2:6 " waandishi"** Hawa walikuwa wataalamu wa Sheria za mazungumzo na zilizoandikwa. Kwa vyo vyote vile hawa walikuwa (1) walitumwa kutoka Yerusalemu kwa ajili ya kazi maalum ya kumchunga Yesu au (2) walikuwa wafasri maalum wa tamaduni za Kiyahudi kwa ajili ya watu wa mji. Hawa iliwapasa kufika mapema kwa ajili ya kuingaia ndani ya nyumba au walitarajiwa kupewa ruhusa ya kukaa mbele kwa sababu ya hadhi zao za kijamii. Tazama
MADA MAALUM: WAANDISHI katika Marko 1:22.

**NASB, NKJV** **" wakifikiri mioyoni mwao"**
**NRSV** **"wakijiuliza ndani ya mioyo yao"**
**TEV, NJB** **"awakajifikiria"**

Swali la kithiolojia ni Je! Yesu alizisoma fikra zao, na hivyo kuonyesha ushahidi mwingine wa Uungu wake (kama vile 1 Sam. 16:7; Zab. 7:9; 139:1-4; Mit. 16:2; 21:2; 24:12; Yer. 11:20; 17:10; 20:12; Luka 16:15; Matendo 15:8; Ebr. 4:12), au alizijua tamaduni zao na kutazama nyuso zao?

Hii yenyewe (kama vile Marko 2:8) inaweza kuwa ishara nyingine. Walimu wa Sheria za Kiyahudi Isa. 11:3 kama Masihi mwenye uwezo wa kuzibaini fikra za watu.

## MADA MAALUM : MOYO

Neno la Kiyunani *kardia* limetumika katika maandiko ya kale ya Kiyunani na Agano Jipya kuashiria neno la Kiebrania lēb (BDB 523, KB 513). Limetumika kwa njia tofauti kadhaa (kama vile. Bauer, Arndt, Gingrich na Danker, *A Greek-English Lexicon*,, 2nd ed. kur. 403-404).

1. Kitovu/Kituo cha maisha ya kimwili, neno mbadala kwa mtu (kama vile. Matendo 14:17; 2 Kor. 3:2-3; Yakobo 5:5)
2. Kitovu cha maisha ya kiroho (yaani, adilifu)
    a. Mungu anatujua mioyo (kama vile. Luka 16:15; Rum. 8:27; 1 Kor. 14:25; 1 The. 2:4; Ufu. 2:23)
    b. Imetumika kwa maisha ya kiroho ya mwanadamu (kama vile. Mt. 15:18-19; 18:35; Rum. 6:17; 1 Tim. 1:5; 2 Tim. 2:22; 1 Pet. 1:22)
3. Kitovu cha maisha ya kifikra (yaani,uwezo wa kufikiri, kama vile. Mt. 13:15; 24:48; Matendo 7:23; 16:14; 28:27; Rum. 1:21; 10:6; 16:18; 2 Kor. 4:6; Efe. 1:18; 4:18; Yakobo 1:26; 2 Pet. 1:19; Ufu. 18:7; moyo ni sawa na mawazo katika 2 Kor. 3:14-15 na Flp. 4:7)
4. kitovu cha maamuzi binafsi (yaani, matakwa,kama vile.Matendo 5:4; 11:23; 1 Kor. 4:5; 7:37; 2 Kor. 9:7)
5. Kitovu cha hisia za ndani (kama vile Mt. 5:28; Matendo 2:26,37; 7:54; 21:13; Rum. 1:24; 2 Kor. 2:4; 7:3; Efe. 6:22; Flp. 1:7)
1. Mahali pa pekee kwa shughuli za kiroho (kama vile. Rum. 5:5; 2 Kor. 1:22; Gal. 4:6 [yaani,Kristo katika mioyo yetu, Efe. 3:17])
7. Moyo ni njia mbadala ya ki-sitiari ya kumrejerea mtu (kama vile. Mt. 22:37, kwa kunukuu Kumb. 6:5). Mawazo, sababu, na matendo vikichangia kikamilifu kwenye moyo kubainisha kikamilifu mtu alivyo. Agano la Kale lina baadhi ya matumizi ya maneno ya kushangaza.
    a. Mwa. 6:6; 8:21, "Mungu alihuzunishwa katika moyo," pia tazama Hosea 11:8-9
    b. Kumb. 4:29; 6:5; 10:12, "kwa moyo wako wote na nafsi yako yote"
    c. Kumb. 10:16; Yer. 9:26, "Roho zisizo na tohara" na Rum. 2:29
    d. Ezek. 18:31-32, "moyo mpya"
    e. Ezek. 36:26, "moyo mpya" dhidi ya "moyo wa jiwe" (kama vile Ezek. 11:19; Zak. 7:12)

**2:7 "Anakufuru"** Adhabu ya kukufuru ilikuwa ni kupigwa mawe hadi kufa (kama vile Law. 24:16). Yesu alikabiliwa na shitaka hili isipokuwa alikuwa na Uungu. Yesu kusamahe dhambi pia ni dai la kutouelewa Uungu au ya kuwa mwakilishi wa nguvu na mamlaka ya kiungu.

◙ **"Ni nani awezaye kusamehe dhambi isipokuwa mmoja, ndiye Mungu"** Ujumbe wa Yesu uhusuo toba na imani (kama vile Marko 1:14-15) ulitabirikwa katika dhahanio la dhambi za wanadamu wote (hata watu wa agano la Agano la Kale, kama vile Rum. 3:9-18). Dhambi ni mbaya na tabia za mtiririko wa mahusiano tu, bali kipengele cha matukio ya milele. Dhambi, na nguvu yake na matokeo yake, ndizo sababu zilizomfanya Yesu kuja (kama vile Marko 10:45; 2 Kor. 5:21). Ni Mungu pekee awezaye kusamehe dhambi kwa sababu kimsingi dhambi iko kinyume naye (kama vile Mwa. 20:6; 39:9; 2 Sam. 12:13; Za. 41:4; 51:4). Kwa kuwa kitabu cha Isaya ni rejea ya mara kwa mara (au dokezo) katika Injili ya Marko kuna baadhi ya mistari katika Isaya ambayo inahusika na zama mpya na msamaha: Isa. 1:18; 33:24; 38:17; 43:25; 44:22. Hii ni ishara nyingine ya ki-Masihi.

**2:8,12 "Mara"** Tazama maelezo katika Marko 1:10.

◙ **"Yesu akafahamu"** Tazama maelezo katika Marko 2:7.

◙ **"rohoni mwake" herufi kubwa z**a machapisho ya Kiyunani ya Agano Jipya haikuwa na

1. nafasi kati ya maneno
2. alama za kiuandishi
3. herufi kubwa na ndogo (herufi zote zilikuwa kubwa)
4. migawanyo ya mistari na sura

Hivyo, ni andiko pekee ambalo linaweza kubainisha uhitaji wa herufi kubwa. Mara nyingi herufi kubwa zinatumika kwa ajili ya

1. majina ya Uungu
2. majina ya mahari
3. majina ya watu

Hili neno "rohoni" linaweza kurejelea:

1. Roho Mtakatifu (kama vile Marko 1:5)
2. utambuzi binafsi wa tabia ya mwanadamu (kama vile Marko 8:12; 14:38)
3. baadhi ya viumbe wa ulimwengu wa roho (yaani, roho chafu, kama vile Marko 1:23)

Katika muktadha huu kipengele hiki kinamrejelea Yesu kama mtu.
Mimi binafsi nakanusha dhana ya kithiolojia ya wanadamu kuwa na sehemu tatu (mwili, nafsi, na roho iliyojikita katika 1 The. 5:23). Mara nyingi wale wanaitetea dhana hii wanalibadili dhahanio hili la kithiolojia katika mtiririko wa tafsiri ya kibiblia ambapo maandiko yote ya kibiblia yanatafsriwa. Hivi vipengele vinakuwa sehemu ya kidhibiti ambapo Mungu uhusiana na mwanadamu. Wanadamu ni wamoja (kama vile Mwa. 2:7). Kwa muhtasari mzuri wa nadharia za mwanadamu kama mwenye sehemu tatu, sehemu mbili za mwanadamu, ama mwenye sehemu moja tazama Frank Stagg's Polarities of Man's Existence in a Biblical Perspective na Millard J. Erickson's Christian Theology (toleo la pili) kr. 538-557.

**2:9,11 "'Ondoka, ujitwike godoro lako, uende'"** Hizi ni kauli mbili shurutishi zenye kufuatiwa na kauli shurutishi ya wakati uliopo. Hii ilikuwa tiba ya ghafla na ya mwisho. Hii ilifanyika kwa sababu tatu.

1. kwa sababu Yesu alimjali mtu aliyekuwa muhitaji na alimpa zawadi ya imani yake
2. kuendelea kuwafundisha injili wanafunzi kama inavyohusiana na nafsi yake na wito wake
3. kuendelea kukabiliana na majibizano ya viongozi wa kidini

Hawa viongozi wa kidini wana uchaguzi wa aina mbili tu: kuamini katika yeye au kueleza juu ya nguvu zake na

mamlaka yake.

**2:10 "'Mwana wa Adamu'"** Hiki ni kirai vumishi kinachotokana na Agano la Kale. Hiki kilitumika katika Eze. 2:1 na Zab. 8:4 katika asili ya maana yake ya kweli ya "mwanadamu." Hata hivyo, kilitumika katika Dan. 7:13 katika andiko la kipekee ambalo linamaanisha yote mawili ubinadamu na Uungu wa mtu anayeelezwa na ufalme huu mdogo wa siku za mwisho (kama vile Marko 8:38; 9:9; 13:26; 14:26). Kwa kuwa ufalme huu mdogo haukutumiwa na walimu wa Kiyahudi na hivyo hakuwa mzalendo, alikuwa amejitenga, maana za kijeshi, Yesu aliuchagua huu kama kamilisho la udogo wa aina zote za kuficha na kuifunua asili yake ya uwili, mwanadamu kamili na Uungu kamili (kama vile 1 Yohana 4:1-3). Huu ulikuwa upendeleo wake binafsi wa kujifafanua.Neno hili limetumika mara kumi na tatu katika Marko (mara mara katika uhusiano na mateso ya Yesu, kama Marko 8:31;9:12,31; 10:33,45; 14:21,41).

◙ **"'anayo amri duniani ya kusamehe dhambi'"** Yesu alitenda muujiza huu kwa makusudi ya kuwathibitishia waandishi hawa. Suala hili la mamlaka (yaani, *exousia*) litakuwa la muhimu. Hawa hawezi kuukana uweza wake, hivyo watadai kwamba uweza wake na mamlaka yake ni asili ya kimapepo au ya ki- Shetani (kama vile Mt. 10:25; 12:24-29; Luka11:14-22).

**2:12 "wakastaajabu wote"** Hii haikuwa kwa sababu ya uponyaji; walikuwa wamekwisha muona akifanya hivyo hapo awali, bali suala la kusamehe dhambi! Hawa (waandishi na Mafarisayo) walikuwa na dhambi zao. Kwa uwazi kabisa Yesu aliuonyesha uweza wake na mamlaka yake. Nastaajabu ikiwa viongozi hawa "walimtukuza Mungu" juu ya tukio hili pia.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 2:13-14**
***13*** **Akatoka tena, akaenda kando ya bahari, mkutano wote ukamwendea, akawafundisha.** ***14*** **Hata alipokuwa akipita, akamwona Lawi wa Alfayo, ameketi forodhani, akamwambia, Nifuate. Akaondoka akamfuata.**

**2:13 "mkutano wote ukamwendea, akawafundisha"** Hizi ni kauli mbili za vitenzi vya wakati usio timilifu. Mara nyingi Yesu alitumia muda katika kuihubiri injili na kuwajali watu. Ndio maana watu wa kawaida walimpenda sana. Yeye alikuwa tofauti na kutoa hukumu, utengano, na viongozi wa kidini.

**2:14 "Lawi"** Jina hili katika Kiebrania linamaanisha "mwenzi." Hili ni jina la kabila la kuhani wa Israeli. Yesu alilibadilisha jina la mtu huyu na kumwita"Mathayo" jina ambalo linamaanisha "zawadi ya YHWH" (kama vile Marko 3:18; Mt. 9:9) au, kama Paulo, wazazi wake walimpa majina mawili wakatai wa kuzaliwa kwake.

◙ **"ameketi forodhani"** Ukusanyaji wa kodi ulikuwa mfumo maarufu uliochukiwa na watu wengi wa Kiyahudi kwa sababu mfumo huu uliwekwa na mamlaka za Kirumi. Wakusanya kodi waliwalazimisha watu kutoa kiasi fulani cha mazao yote kwa ajili ya Rumi. Herode Antipas naye alikuwa akipata sehemu fulani ya kodi zilizokusanywa. Cho chote walichokikusanya nje ya kiwango kilichowekwa, watu hawa walikitunza kama ujira wao. Ukusanyajai kodi ulifahamika sana kwa ulaghai wake wa hali ya juu. Huenda Lawi alikuwa akikusanya kodi itokanayo na usafirishaji wa samaki.

◙**"'Nifuate'"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Huu ulikuwa wito maalum wa kiuanafunzi (kama vile Marko 1:17,20). Lazima ikumbukwe kwamba walimu wa Sheria za Kiyahudi waliitwa wanafunzi kwa ajili ya kujifungamanisha na Sheria, lakini Yesu aliwaita watu hawa kwa ajili ya kuwafungamanisha naye. Yesu, kutokuwa mtu wa kuzitenda sheria za Musa (yaani., Buku la Sheria na Maadili ya Kiyahudi), ni njia ya wokovu. Tendo la toba si tendo la kuirudia Sheria ya Musa, bali kumrudia Yesu, Masihi wa YHWH. Yesu hakuipinga Sheria, bali alijiweka katika nafasi ya utamaduni na kama fasiri kamili (kama vile Mt. 5:17-48). Wokovu ni wa mtu, si kanuni au utendaji mwingine wa mfumo maalum. Suala hili ndiyo sababu ya msingi iliyomfanya Yesu kuwa katika mgogoro wa makusudi na viongozi wa kidini.

Katika kitabu chake *The Method and Message of Jesus' Teachings*, Robert H. Stein anatengeza hoja nzuri kuhusu usemi huu:

> "Ingawa neno 'chama kisichopingwa' lina maana nyingi kanushi, za matumizi ya Archibald M. Hunter ya neno hili ni sahihi na yanafafanua vema msimamo wa moja kwa moja ambao Yesu aliuhitaji toka kwa wafuasi wake. Kinywani mwa kila mtu madai kumhusu Yesu yataonekana kuwa ushahidi kamili wa wale wenye kujipenda wenyewe, kwa Yesu, kwa namna iliyo dhahiri anamaanisha kwamba ulimwengu wote unamzunguka Yeye, na ni kwamba hatma ya wanadamu wote inategemea katika kumkubali kwao au kumkataa kwao . Kwa mujibu wa Yesu, hatima ya mwanadamu inamzunguka.Kumkataa yeye kunamaanisha hukumu ya milele; kumkubali kunamaanishakukubaliwa na Mungu. Hoja ya msingi ya historia na wokovu, Yesu anadai kuwa, ni Yeye Mwenyewe. Kumtii Yeye ni kuwa na hekima na kuiepuka hukumu, bali kuyakataa maneno yake ni kuwa mpumbavu na kupotea, kwa maana manenoyake ndiyo yenye msingi wa kweli wa kujenga (Mt. 7:24-27)" (uk. 118).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 2:15-17**
[15] **Hata alipokuwa ameketi chakulani nyumbani mwake, watoza ushuru wengi na waliketi pamoja na Yesu na wanafunzi wake; kwa maana walikuwa wengi wakimfuata.** [16] **Na waandishi na Mafarisayo walipomwona anakula pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi, waliwaambia wanafunzi wake, Mbona anakula pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi?** [17] **Yesu aliposikia aliwaambia, Wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio hawawezi; sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi**.

**2:15 "alipokuwa ameketi chakulani nyumbani mwake"** Hapa ni nyumbani kwa Lawi (kama vile Luka 5:29). Yesu alikuwa akila na watu waliotengwa kijamii na kidini kama njia ya kuanzisha majadiliano ya kidini pamoja nao. Hawa walikusanyika kwake kwa sababu alikuwa akifanya mambo kwa utofauti sana na viongozi wa Kiyahudi waliojihesabia haki. Tendo la kula lilikuwa tukio muhimu katika Mashariki ya Karibu ya Kale ambapo tendo hili lilimaanisha ushirika na ukubalifu. Hawa walikuwa wamejinyoosha juu ya meza iliyokuwa upande wa iliyokuwa na umbo dogo la kiatu cha farasi kushoto kwake yenye miguu nyuma yake (hili limepingwa na J. Jeremias katika kitabu chake cha *The Eucharistic Words of Jesus*, kr. 20-21. Yeye anadai kwamba Wayahudi hawakuzifuata desturi za Mediterranea zinazohusu pumziko kwa usahihi, isipokuwa siku za siku kuu). Katika Mashariki ya Karibu wengine ambao hawakualikwa kushiriki mlo wangekuja katika eneo la kulia chakula na kusimama karibu na kuta au karibu na mlango au madirishani na kusikiliza mazungumzo.

Mtu anashangaa namna ishara za matukio ya siku za mwisho zinavyopaswa kutambuliwa katika muktadha huu. Je! Hii siku kuu inatabiri juu ya karamu ya ki-Masihi ambayo itawahusisha wale waliotengwa (kama vile Mt. 8:11; Luka 13:29 huenda tendo hili linaiakisi Isa. 59:15b-21)? Ikiwa ni hivyo, kuna utambuzi wa kithiolojia kwamba ushirika pamoja na Kristo unaakisi ushirika wa ufalme wa siku za mwisho. Watenda dhambi wanapatanishwa sasa na hata milele! Watenda dhambi wote wanakaribishwa (na wote wametenda dhambi, hata watu wa Agano la Kale, kama vile Rum. 3:9-18).

◙ **"wenye dhambi"** Kifungu hiki kinawarejelea watu ambao hawakuwashika maagizo yote ya Mapokeo ya Fasihi simulizi (yaani, Sheria na Maadili ya Kiyahudi). Mara nyingi watu hawa walirejelewa katika maana ya kushushwa hadhi kama "watu walioishiwa." Hawa hawakukamilishwa ndani ya masinagogi kwa ukamilifu.

◙ **"na wanafunzi wake"** watu hawa wenye kuchambua walikuwa na umakini sana wa maneno na matendo yote ya Yesu. Kiukweli hapo awali walimaanisha watu hawa. Hawa walikuwa na uwezo wa kuchukua kumbukumbu na kumfafanua Yesu ulimwenguni.

◙ **"kwa maana walikuwa wengi wakimfuata "**Sarufi ni ngumu, lakini inaonekana kuwarejelea "wenye dhambi"

na si wanafaunzi wake.

**2:16 "waandishi na Mafarisayo"** Waandishi hawakuwa kwa ajili dini moja/chama cha siasa, ingawa wengi wao katika siku za Yesu walikuwa Mafarisayo. Mafarisayo walikuwa walikuwa wa dhehebu la thiolojia fulani ya Dini ya Kiyahudi iliyoshamiri wakatai wa kipindi cha Mkabayo. Hawa walikuwa na msimamo sana na walikuwa wanadini watiifu waliozifuata Mapokeo ya Fasihi Simulizi (yaani., Buku la Sheria na Maadili ya Kiyahudi).

## MADA MAALUM : MAFARISAYO

I. Neno lilikuwa na uwezekana wa kuwa na asili moja kati ya hizi zifuatazo:
   A. "Kujitenga." Kundi hili lilianza wakati wa ufuasi wa kiongozi wa Kiyahudi Yuda wa karne ya pili ( huu ni mtizamo mpana sana unaokubalika), na kujitenga wao wenyewe toka kwenye umma wa watu ili kutunza tamaduni simulizi za sheria ya Musa (yaani., mienendo ya kichini chini ya Kiyahudi iliyopatikana karne ya 18).
   B. "Kugawa" Hii ni maana nyingine toka kwenye kiini kile kile cha lugha ya Kiebrania (BDB 827, BDB 831 I, KB 976); yoye yakimaanisha "kugawanya." Baadhi ya wasomi wanasema linamaanisha mfasili (kama vile Neh. 8:8; 2 Tim. 2:15).
   C. "Uajemi." Hii ni maana nyingine toka kwenye kiini kile kile cha lugha ya Kiarama (BDB 828, KB 970). Baadhi ya mafundisho ya mafarisayo yanaingiliana na wafuasi wa dini za Kiislamu za awali toka Uajemi zilizoanzishwa na Zoroaster (angalia maada maalumu Uovu).

II. Pamekuwepo na nadharia nyingi nani alianzisha Ufarisayo.
   A. Kikundi cha kithiolojia cha dini ya mwanzo ya Kiyahudi (angali., Yusufu)
   B. Kikundi cha kisiasa toka kipindi kile cha Herode
   C. Kikundi cha kisomi cha wafasiri wa sheria za musa ambao walitaka kuwasaidia watu wa kawaida kuelewa Agano la Musa na tamaduni simulizi zilizowazunguka.
   D. Mienendo ya chini kwa chini ya waandishi, kama vile Ezra na Sinagogi kuu, wakigombea uongozi wa ukuhani mkuu katika hekalu.

Yaliundwa nje ya misigishano na
   1. Makabila wasiokuwa Wayahudi (hasa Antiokia IV).
   2. jamii ya watu wakuu dhidi ya watu wa kawaida
   3. wale waliojifungamanisha kwenye maisha ya agano dhidi ya Wayahudi wa kawaida toka Palestina

III. Habari zetu kuwahusu wao zinatoka
   A. Yusufu, aliyekuwa mfarisayo
      1. Vitu vya kale vya Kiyahudi
      2. Vita vya Wayahudi
   B. Agano Jipya
   C. Asili ya awali ya Kiyahudi

IV. Mafundisho yao makuu
   A. Imani ya kuja kwa Masihi, iliyoshawishiwa na waandishi wa Kibiblia wa Kiyahudi wenye fasihi ya kimaono kama vile Enock.
   B. Imani ya kwamba Mungu yu hai katika maisha yetu ya kila siku. Hii moja kwa moja ilikuwa kinyume na Masadukayo (kama vile Mdo 23:8). Mafundisho mengi ya Kifarisayo yalikuwa ni kijazilizo cha yale ya Masadukayo.
   C. Imani katika maelekezo ya kimwili baada ya maisha yaliyolenga maisha ya duniani, yaliyojumuisha zawadi na adhabu (kama vile Dan.12:2)
   D. Imani katika mamlaka ya Agano la Kale vile vile simulizi za kitamaduni (Talmud). Walitambua kuwa watiifu kwa amri za Mungu za Agano la Kale kama zilivyo tafasiliwa na shule za wasomi wa sheria za Kiyahudi (Shammai, asiyependa mabadiliko na Hillel, anayependa mabadiliko). Watafasiri wa sheria za Kiyahudi walisimamia juu ya mazungumzo kati ya wanasheria/walimu wa falsafa mbili zinazokinzana, mmoja asiyependa mabadiliko na mwingine anayependa mabadiliko. Mazungumzo haya ya kisimulizi juu ya maana

ya andiko hatimaye likaandikwa kwa miundo miwili: sheria za kiibada za Wababel na sheria za kiibada zisizo kamili za Wapalestina. Waliamini kuwa Musa alipokea hizi sheria za mdomo kwenye Mlima Sinai. Mwanzo wa haya mazungumzo ya kihistoria yalianzishwa na Ezra na watu wa "Sinagogi kuu" (baadaye wakaitwa Wakuu wa Sinagogi)

E. Imani ilioanzishwa juu ya mafundisho ya kithiolojia ya kimalaika. Haya yalijumuisha viumbe wazuri na wabaya. Hili lilianzia huko Uajemi yenye pande mbili na fasihi za Kiyahudi zenye mwingiliano na Biblia.

F. Imani juu ya mamlaka ya kifalme ya Mungu, lakini pia mazoezi ya utashi huru wa binadamu (*yetzer)*.

V. Nguvu ya mabadilko ya Kifarisayo.

A. Walipenda , waliheshimu, kuamini mafunuo ya Mungu (yaani., yote, yakijumuisha sheria, Manabii, Maandiko, na simulizi za kitamaduni)

B. Walijitolea kuwa wafuasi wenye haki (yaani., maisha ya kila siku na imani) wa mafunuo ya Mungu. Walitaka "Israel yenye haki" kutimiza ahadi ya kinabii ya siku mpya yenye mafanikio.

C. Walitetea kuwepo usawa na jamii za Kiyuda, ambao unajuisha ngazi zote za watu, kwa maana kuwa, walikataa uongozi wa kikuhani (yaani., masadukayo) na thiolojia (kama vile Mdo 23:8).

D. Walipigania kitu halisi cha mtu kwenye agano la sheria za Musa. Walitetea au kudai mamlaka ya Mungu, lakini pia wakashikilia kwenye hitaji la utendaji huru wa mwanadamu

E. Agano Jipya linataja mafarisayo mbali mbali walioheshimika (yaani., Nikodemu, Mtawala tajili kijana, Yusufu wa Alimataya).

Walikuwa ni kundi hilo tu la dini ya Kiyahudi ya karne ya kwanza kuhimili uharibifu wa Yerusalem na hekalu toka kwa Warumi mwaka wa 70 B.k. wakawa ni dini ya Kiyahudi ya kisasa.

**2:16 "anakula pamoja na watoza ushuru na wenye dhambi"** Hili lazima liwe tukio la kawaida, si tarajio (kama vile Luka 5:29; 7:34; 15:1-2). Hili lilikuwa la kutisha sana kwa wale waliojihesabia haki, wasomi wa kidini!

**2:17 "' bali walio hawawezi '"** Hawa walikuwa na hisia za uhitaji wa imani (kama vile Mt. 5:3-4) na Yesu alikuwa mponyaji na rafiki yao (kama vile Luka 7:34; 19:10).

◙ **"'sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi'"** Hii ni kebehi, huenda huu ni usemi wa kubeza kama ilivyo 7:19. Usemi huu haukumaanisha kwamba viongozi wa kidini walikuwa na haki (kama vile Mt. 5:20) na hivyo haikuwapasa kutubu, bali ujumbe wa Yesu (kama vile Marko 1:14-15) ulikuwa wa kufaa kwa wale walijisikia kuwa na hitaji la kiroho. Mara nyingi Yesu alitumia semi za methali katika Mafundisho yake (kama vile Marko 2:17,21,22,27; 3:27; 4:21,22,25; 7:15; 8:35,36,37; 9:40,50; 10:25,27,31,43-44). Hakuna aliye kipofu zaidi kuliko wanaodhani ya kuwa wanaona!
Toleo la Textus Receptus linaongeza kifungu "kwa toba" mwishoni mwa mstari huu unauofuatia ufanano wa maandishi ya Luka (kama vile Marko 5:32) na Byzantine, bali tofauti hii haikuwekwa katika toleo la UBS[4] kama kitu hatarishi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 2:18-20**
**[18] Nao wanafunzi wake Yohana na Mafarisayo walikuwa wakifunga; basi wakamwambia, Kwani wanafunzi wa Yohana na wanafunzi wa Mafarisayo hufunga, bali wanafunzi wako hawafungi? [19] Yesu akawaambia, Walioalikwa arusini wawezaje kufunga maadamu bwana-arusi yupo pamoja nao? Muda wote walipo na bwana-arusi pamoja nao hawawezi kufunga. [20] Lakini siku zitakuja watakapoondolewa bwana-arusi, ndipo watakapofunga siku ile.**

**2:18-20 "wakifunga"** Mafarisayo na wanafunzi wa Yohana walikuwa wanaamrishwa kitamaduni kufunga mara mbili kwa juma, kila Jumatatu, na kila Alhamisi (kama vile Luka 18:12). Sheria ya Musa ilikuwa na agizo la kufunga mara moja kwa mwaka, Siku ya Upatanisho (kama vile Mambo ya Walawi 16). Huku kufunga mara mbili kwa Juma ni mfano mzuri wa kudumisha mapokeo (kama vile Zekaria 7-8). Tendo la kufunga hupoteza thamani yake pale linapokuwa la lazima na

kuwa la kiushawishi (kama vile Mt. 6:16-18).

## MADA MAALUM: KUFUNGA

Kufunga, ingawa hakujaamriwa katika Agano Jipya, kulitarajiwa katika wakati muafaka kwa ajili ya wanafunzi wa Yesu (kama vile Mt. 6:16,17; 9:15; Marko 2:19; Luka 5:35). Kufunga kunakostahili kunapatikana katika Isaya 58. Yesu alijiweka mwenyewe kuwa wa mfano (kama vile Mt. 4:2). Kanisa la mwanzo lilifunga (kama vile Mdo. 13:2-3; 14:23; 2 Kor. 6:5; 11:27). Mienendo na tabia ni vya muhimu; kwenda na wakati; umbali na jambo kutokea ni la kiuchaguzi. Kufunga katika agano la kale sio sharti la waamini wa Agano Jipya (kama vile Mdo. 15:19-29). Kufunga sio njia ya ya kuonyesha u-kiroho cha mtu (kama vile Isaya 58; Mt. 6:16-18), lakini ni njia ya kumsogeza mtu karibu na Mungu na kuhitaji mwongozo wake (yaani., Yesu, Mt. 4:2). Yaweza kuwa ni msaada wa kiroho.
Tabia ya kanisa la mwanzo dhidi ya uwazi ulisababishwa na waandishi walioingiza neno"kufunga" katika sura mbali mbali (yaani., Mt. 17:21; Marko 9:29; Mdo. 10:30; 1 Kor. 7:5). Kwa ajili ya maelezo zaidi juu ya ya maandiko haya yenye maswali mwone Bruce Metzger's *A Textual Commentary on the Greek New Testament*, kilichochapishwa na United Bible Societies.

**NASAB, NKJV "walikuja"**
**NRSV "watu walikuja"**
**TEV, NJB "baadhi ya watu walikuja"**

Mstari wa 18 unaanza kwamba wanafunzi wake Yohana na Mafarisayo walikuwa wakifunga. Wengine wana unukuu mstari huu na kumuuliza Yesu kuhusu sababu inayowafanya wanafunzi wake wasiwe wanafunga.

**2:19** Kisarufi swali hili linatarajia jibu hasi.

◙ **"'bwana-arusi'"** Kuna taswira nyingi za Agano la Kale zilizowekwa katika dhana ya "harusi." Katika Agano la Kale YHWH bwana- arusi au mume wa Israeli. Katika muktadha huu Yesu ndiye bwana–arusi na kanisa ni bibi-arusi (kama vile Efe. 5:23-32). Katika Marko 2:20 kifungu "watakapoondolewa bwana-arusi" kinarejelea pindi utengano utakapotokea.

Na sasa, sisi kama wafasiri tunao uchaguzi wa aina mbili. Wa kwanza, tunaweza kuliona hili kama sitiari ya kitamaduni inayohusu wakati wa furaha unaohusiana na harusi. Hakuna anayefunga wakati wa harusi! Wa pili, tunaweza kuliona hili kama fumbo la wakati Yesu alipokuwa duniani na ujio wa kusulibiwa kwake. Marko (mfasiri wa Petro) alikuwa amekwisha kufahamu maana kamili ya maneno haya yenye uzito kistiari (katika Dini ya Kiyahudi neno bwana-arusi ilkuwa stiari, si la Masihi, bali Ufalme wa Mungu Ujao). Je! Hili ni tendo la kutabiri juu ya kifo cha Yesu? Yeye ameufunua wazi u-Masihi wake na Uungu wake kupitia maneno yake na amri zake (yaani, kupunga pepo, uponyaji, kusamehe dhambi). Hata hivyo, Siri ya Masihi ya Marko inamsababisha mtu kustaajabu! Lakini lugha ya kimafumbo na maana yake ya Marko 2:21-22 inanifanya niuone muktadha mzima katika mbadala, matukio ya siku za siku za mwisho, mazingira (yaani, bwana- arusi apoteaye, bali Mwana wa Mungu anarudi na kubakia pale pale). Kati ya mauti na kurudi (yaani., karamu ya ki- Masihi), Wafuasi wake watafunga katika namna ipasayo na katika wakati upasao.

**2:20 "'watakapoondolewa'"**Hili linaweza kuwa dokezo la Isa. 53:8 katika Agano la Kale la Kiebrania. Baada ya kusulibiwa, ufufuo, na kupaa ndipo Petro alipoelewa zaidi umuhimu wa Isaya 53.

◙ "**watakapofunga'"** Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati ujao (usemi wa ndani), si kauli shurutishi (amri).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 2:21-22**
**[21] Hakuna mtu ashonaye kiraka cha nguo mpya katika vazi kuukuu; ikiwa ashona, kile kipya kilichotiwa huliharibu lile vazi kuukuu, na pale palipotatuka huzidi. [22] Wala hakuna mtu atiaye divai mpya katika viriba vikuukuu; ikiwa atia, ile divai mpya itavipasua viriba vile, divai ikamwagika, vile viriba vikaharibika. Bali hutia divai mpya katika viriba vipya.**

**2:21** Mstari huu unaiakisi kweli ya kitamaduni, iliyobadilishwa katika mithali.

**2:22 "viriba vikuukuu"** neno hili liliwarejelea mbuzi waliokuwa wakichunwa kwa kutumia njia hii kama kuzipa mwanya ngozi kutumika kama chombo cha kubebea vimiminika. Hizi ngozi mpya zilizotiwa rangi ya shaba zingekuwa na uwezo wa kupanuka zenyewe. Hizi ngozi zilibadilika na kuwa kuu kuu, tendo la kuzianika na kuzipanua lilizisababisha kugawanyika. Dini ya Kiyahudi haikuwa na uwezo wa kuzipokea tambuzi za Yesu na usahihishaji wake, hivyo, jambo hili lilifanywa kuwa la kiubatili na utupu. Agano Jipya (kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:22-38) limetimia katika Yesu! Hakuja jambo liwezalo kubaki kama lilivyo.

Kuna tofauti kadhaa za Kiyunani zinazohusianishwa na mstari huu. Nyingine zinatokana na ufanano ulio katika Mt. 9:17 na Luka 5:37-38. Njia ya Marko ya kuyanakili matukio haya katika muhtasari iliwasababisha waandishi kuweka bidii ya kuisanifisha lugha yake. Yatambue majina ya Yesu yaliyo tumia muundo wa kistiari katika muktadha huu: (1) tabibu, Marko 2:17; (2) bwana-arusi, Marko 2:19; (3) divai mpya, Marko 2:21-22; na (4) Bwana wa Sabato, Marko 2:28.

◙ **"ikamwagika"** Tazama Mada Maalum: *Apollumi* katika Marko 3:6.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 2:23-28**
**23 Ikawa alipokuwa akipita mashambani siku ya sabato, wanafunzi wake walianza kuendelea njiani wakivunjamasuke. 24 Mafarisayo wakamwambia, Tazama, mbona wanafanya lisilokuwa halali siku ya sabato? 25 Akawaambia, Hamkusoma popote alivyofanya Daudi, alipokuwa ana haja, na kuona njaa, yeye na wenziwe? 26 Jinsi alivyoingia katika nyumba ya Mungu, zamani za kuhani mkuu Abiathari, akaila mikate ile ya Wonyesho, ambayo si halali kuliwa ila na makuhani, akawapa na wenziwe? 27 Akawaambia, Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, si mwanadamu kwa ajili ya sabato. 28 Basi Mwana wa Adamu ndiye Bwana wa sabato pia.**

**2:23 " alipokuwa akipita mashambani siku ya sabato**" Hiki kifungu kinarejelea kuenenda kwa miguu kupita katika mashamba ya masuke ambayo yalikuwa yakivizunguka vijiji na miji. Haya "mashamba ya masuke" yangeweza kurejelea aina yo yote nafaka (yaani., shayiri, ngano).

**2:24 "'mbona wanafanya lisilokuwa halali siku ya sabato'"** Mafarisayo waliyachukulia matendo ya wanafunzi kama (1) uvunaji; (2) kupura; na (3) kuandaa chakula siku ya Sabato, kitu ambacho ni mwiko kulingana na taratibu za mapokeo zilizojikita katika Kut. 34:21. Wanafunzi wa Yesu hawakufanya jambo lo lote lililo kinyume na sheria kulingana na sheria za Agano la Kale zinazohusu kusanyiko (kama vile Kumb. 23:25); tatizo lilikuwa siku (kama avile Mwa. 2:1-3; Kut. 20:8-11; 23:12; 31:15; Kumb. 5:12-15) ambayo waliitumia kufanya jambo hili! Inaonekana kwamba waandishi wa Injili waliichukua kumbukumbu ya matendo ya Yesu siku ya Sabato ili kuonyesha (1) mkanganyiko waliousababisha au (2) kwamba Yesu aliyafanya mambo haya kila siku na hakuitunza siku ya Sabato.

**2:25-28** Huu usemi ulio maarufu (kama vile Marko 2:27) uliotolewa na Yesu ni wa kipekee kwa Marko. Huu unaeleza mamlaka yake ya kuufasiri tena uelewa wa tamaduni za Agano la Kale na miongozo yake (kama vile Mt. 5:17-48). Katika ukweli hii ni ishara nyingine kwamba Yesu alikuwa akidai kuwa yeye ni Masihi wa Mungu.

**2:25** Kisarufi swali hili linatarajia jibu hasi. Kifungu hiki kinayarejelea maelezo ya maisha ya Daudi yaliyoandikwa katika 1 Samueli 21. Mara nyingi Yesu alilitumia Agano la Kale kutoa ufafanuzi wa mafundisho yake (kama vileMarko 2:25-26; 4:12; 10:6-8,19; 12:26,29-30,36).

**2:26 ' "nyumba ya Mungu'"** Kifungu hiki kinalirejelea Hema la muda lilijengwa huko Nodi.

◙ **"'Abiathari'"** Kuna tatizo la kihistoria kati ya 1 Sam. 21:1 na kuendelea, pale inapolinganishwa na 2 Sam. 8:17 na 1 Nya. 18:16 kuhusu jina Abiathari au Abimeleki: (1) wote baba na mwana wanaitwa Kuhani Mkuu na (2) Yesu alitumia kihusishi, *epi*, chenye kimilikishi katika maana ya "katika siku za" ambacho kilimaanisha "wakati wa kipindi chake" (kama vile Matendo 11:28; Heb. 1:2). Tunafahamu kwamba punde tu baada ya tukio hili Mfalme Sauli alimuua Abimeleki na Abiathari kumkimbilia Daudi (kama vile 1 Sam. 22:11-23) na kuwa mmoja wa makuhani wakuu wawili waliotambuliwa (yaani, Abiathari na Zadoki).

Huu ni moja ya mfano wa aina ya matatizo ambayo kimsingi hayawezi kuelezewa vinginevyo. Hii si tofauti ya machapisho ya Kiyunani. Ikiwa kulikuwa na mtu mwenye kufikiri juu ya uandishi wa kale kabla ya machapisho ya mafunjo, ulikuwa uandishi wa kuandika kwa mkono (ambapo ni madhaanio). Hili liliwasumbua walimu wote wa Biblia kwamba Yesu aliinukuu tofauti historia ya Agano la Kale, hasa katika muktadha huu Yesu anawakaripia Mafarisayo na si kusoma Maandiko.

Kuna baadhi ya vitabu ambavyo vinajaribu kushughulikia chaguzi za kitamaduni katika kufasiri maandiko magumu.

1. *Hard Sayings of the Bible* by Walter C. Kaiser, Jr., Peter H. Davids, F. F. Bruce na Manfred T. Branch.
2. *Encyclopedia of Bible Difficulties* na Gleason L. Archer.
3. *Answers to Questions* na F. F. Bruce.

◙ **"'mikate ile ya Wonyesho'"** Hii mikate ilikuwa na thamani ipatayo paundi 6 kila mmoja! Kulikuwa na mikate 12 iliyoondolewa kwa kila juma na mikate ya kale yenye kuashiria utoaji wa YHWH kwa makabila kumi na mawili ya Israeli ambayo ilitakiwa kuliwa na makuhani pekee (kama vile Kut. 25:23-28; Lawi 24:5-9). Mungu alifanya utengefu huu kwa ajili ya kutawala kwa njia hii. Yesu anadai kuwa na mamlaka kama ya Kuhani Mkuu na haki ile ilekwa kuwa anakaribia kuwa mfalme, Dauidi!

**2:27** Amri za Sabato zilikuwa zimewekwa kipaumbele. Mapokeo haya yakawa suala la kidini, si upendo wanadamu walioumbwa kwa sura ya Mungu. Kipaumbele cha sheria kiliondoa kipaumbele cha uhusiano. Faida hizi zimeondoa upendo. Mapokeo ya kidini (yaani., Mapokeo ya Sheria) yameiondoa dhamira ya Mungu (kama vile. Isa. 29:13; Kol. 2:16-23). Ni kwa namna gani mtu humtosheleza Mungu? Ufanano mzuri wa Agano la Kale unaweza kuwa tendo la utoaji wa dhabihu. Mungu alilidhamiria hili kama njia kwa watenda dhambi, wanadamu wenye uhitaji wa kumjia yeye na kuurejesha uhusiano uliovunjika, lakini jambo hili lilibadilishwa na kuwa kama taratibu, tendo la kiruturjia. Hivyo hivyo, sheria za Sabato! Mwanadamu amekuwa mtumishi badala ya kusudi lenyewe (yaani., kusudi la sheria).

Semi tatu za Marko 2:27-28 ni, kataika maana moja, ufanano (yaani., matumizi ya moja kwa moja ya maneno ya mwanadamu). Hili neno "Mwana wa Adamu" katika Marko 2:28 ni nahau ya ki-Semiti ya kifungu mwanadamu" (kama vile Zaburi 8:4; Eze. 2:1). Yakaja kuwa maelezo binafsi ya Yesu. Yesu, Adamu, anaifunua hatima ya utu na upendeleo wa mwanadamu! Mungu anakuwa mmoja wetu, kwetu! Mwanadamu anahitaji kuzitawala desturi. Mungu yu kwa ajili yetu kwa namna ya kipekee na kwa ujumla.

**2:28 "Mwana wa Adamu"** Tazama Maelezo katika Marko 2:10.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe zaBiblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Orodhesha stiari ambazo Yesu alizitumia kujieleza mwenyewe katika 17, 19, 21-22, 28.
2. Kwa nini viongozi wa kidini waliyashambulia sana mafundisho ya Yesu?

3. Kwa nini Yesu alimwita mtu ambaye alikuwa anachukiwa na kutengwa kama Lawi kuwa mwanafaunzi wake?
4. Ni kwa namna gani mafundisho ya Yesu yalihusiana na mapokeo ya Wayahudi?
5. Kwa nini tendo la kufunga halikuwa sehemu ya lazima sana kwetu katika kumwabudu Mungu?
6. Nini kiini cha kweli ya fumbo la Yesu katika Marko 2:19-22?
7. Je! Yesu hakuhusika na sherehe za Kitamadauni au ni uwezekano mwingine wa matendo yake katika Marko 2:23-28?
8. Unafikiri nini kuhusu tatizo la kihistoria katika Marko 2:26?
9. Ni kwa nmana gani Marko 2:27 inahusiana na siku za leo?

# MARKO 3

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Mtu mwenye mkono Uliopooza | Kuponywa siku ya sabato | Yesu na sheria za sabato (2:23-3:6) | Mtu mwenye mkono uliopooza | Kuponywa mkono uliopooza |
| 3:1-6 | 3:1-6 | | 3:1-4a<br>3:4b-6 | 3:1-6 |
| Makutano kando Ya bahari | Makutano makubwa yamfuata Yesu | Kazi ya uponyaji | Makutano kando ya bahari | Makutano wamfuata Yesu |
| 3:7-12 | 3:7-12 | 3:7-12 | 3:7-11<br>3:12 | 3:7-12 |
| Kuchaguliwa kwa Wanafunzi kumi na wawili | Mitume kumi na wawili | Wanafunzi kumi na wawili wachaguliwa | Yesu achagua mitume kumi na wawili | Kuwateua Mitume kumi na wawili |
| 3:13-19 | 3:13-19 | 3:13-19a | 3:13-15<br>3:16-19 | 3:13-19 |
| Yesu na Belzebuli | Nyumbailiogawanyika Haiwezi simama | Maswali juu ya nguvu za Yesu<br>3:19b-27 | Yesu na Belzebuli | Familia yake yamsikitikia Yesu |
| 3:20-30 | 3:20-27 | | 3:20-21 | 3:20-21 |
| | | | | Madai ya waandishi Wa habari |
| | | | 3:22<br>3:23-26<br>3:27 | 3:22-27 |
| | Dhambi isiyosamehewa | | | |
| | 3:28-30 | 3:28-30 | 3:28-30 | 3:28-30 |
| Mama na ndugu Wa Yesu | Mama yake Yesu na ndugu zake wanatumwa Kwake | | Mama yake Yesu na ndugu zake | Ukoo wa kweli wa Yesu |
| 3:31-35 | 3:31-35 | 3:31-35 | 3:31-32<br>:33-35 | 3:31-35 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka "Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu

4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 3:1-6**
**[1] Akaingia tena katika sinagogi; na palikuwako huko mtu mwenye mkono uliopooza; [2] wakamvizia ili kuona kama atamponya siku ya sabato; wapate kumshitaki. [3] Akamwambia yule mtu mwenye mkono uliopooza, Simama katikati. [4] Akawauliza, Ni halali siku ya sabato kutenda mema, au kutenda mabaya? Kuponya roho au kuiua? Wakanyamaza. [5] Akawakazia macho pande zote kwa hasira, akiona huzuni kwa ajili ya ugumu wa mioyo yao, akamwambia yule mtu, Nyosha mkono wako. Naye akaunyosha; mkono wake ukawa mzima tena. [6] Mara wakatoka wale Mafarisayo, wakawa wakifanya shauri juu yake pamoja na Maherodi, jinsi ya kumwangamiza.**

**3:1 "katika Sinagogi" jambo** hili linafanana na lile lililoko katika Mt. 12:9-14 na Luka 6:6-11. Sinagogi lilianza kipindi cha uhamisho wa Babeli. Palikuwa ni mahali pa msingi wa elimu, maombi, kuabudu, na ushirika. Palikuwa ni mahali maalumu pa kuuelezea Uyahudi kama ilivyokuwa Hekalu kuwa kitovu cha kitaifa. Yesu alitembelea kwenye masinagogi mara kwa mara. Alijifunza maandiko yake na utamaduni katika Shule za Sinagogi huko Nazareti. Alifanikiwa kuabudu kama Myahudi katika karne ya kwanza.

Pia inafurahisha kuona kuwa, inavyoonekana kimakusudi kabisa, alitenda kwa namna ya uchokozi siku ya Sabato na ndani ya Sinagogi. Kwa makusudi alikiuka mapokeo ya fasihi simulizi (yaani., kitabu cha sheria na maadili ya Kiyahudi) ya wazee ili kuingia kwenye majibishano ya kithiolojia /majadiliano na wakuu wa kidini (wote wa mahali na kitaifa; wote Mafarisayo na Masadukayo ). Majadiliano yaliyoendelea ya thiolojia yake ni kama yalivyopotosha toka kwenye desturi za kawaida ni mahubiri ya mlimani (kama vile Mathayo 5-7, hasa 5:17-48).

◙**"mkono uliopooza"** Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati timifu. Luka 6:6 inasema ulikuwa ni mkono wake wa kulia, ambao ungaliathiri utendaji wake wa kazi.

**3:2 "wakamvizia ili kuona"** Hii ni njeo ya wakati usio timilifu. Inarejelea mahudhurio ambayo hayajawahi kuonekana ya wakuu wa kidini.

◙ **"kama"** Hii ni sentensi yenye masharti daraja la kwanza,ambayo inadhaniwa kuwa kweli. Yesu aliponya siku ya sabato ndani ya Sinagogi mbele za macho yao!

◙ **"wapate kumshitaki"** Hii ni *hina*, au kusudi, kishazi. Wao hawakuwa na nia na yule mtu kilema. Walitaka kumkamata Yesu kwa kuvunja sheria hivyo kama kumvunjia heshima na kumkataa. Huruma ya Yesu ilikuwa kwa ajili ya mtu, kuendelea kuwafundisha wanafunzi, na kukabiliana na utawala uliozoeleka, waliofungamana na mila, viongozi wa kidini wenye kujihesabia haki.

**3:3**
**NASB "Inuka na uje mbele"**
**NKJV "njoo mbele"**
**NRSV "sogea mbele"**
**TEV "njoo hapa mbele"**
**NJB "inuka na usimame katikati"**

Hii kwa maana iliyowazi ni "kusimama katikati ya". Hii ni Kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Hili lilikuwa kwamba kila mmoja apate kuona.

**3:4** Waalimu wa sheria ya kiyahudi walianzisha mapokeo ya fasihi simulizi kwa kiwango cha juu (kitabu cha sheria na maadili ya kiyahudi) kilichotafsiri sheria za Musa (kama vile Marko 2:24). Walifanya matamko mazito juu ya kile kinachoweza kufanyika kisheria au kutofanyika siku ya sabato. Mtu anaweza kumusaidia aliyejeruhiwa kwa dharula, lakini sio kuimarisha hali yake. Swali la Yesu lilifunua matatizo ya vipaumbele juu ya tamaduni zao juu ya mahitaji ya

mwanadamu. Hii mara zote ndio kweli ya wale wenye kushika sheria sana!

◙ **"kuponya"** Hili ni neno la Kigiriki *sōzō*. Limetumika kwa namna mbili tofauti katika Agano jipya: (1) linafuatisha matumizi ya Agano la kale ya ukombozi wa matatizo ya kimwili na (2) limetumika kwa ukombozi wa kiroho. Kwenye Injili mara nyingi lina maana ya ile ya kwanza (kama vile Marko 3:4; 8:35a; 15:30-31; hata uponyaji, kama vile Marko 5:23,28,34; 6:56; 10:52), lakini katika Marko 8:35b; 10:26; 13:13 laweza kurejelea maana ya pili. Utumiaji mara mbili wa aina ile ile upo katika Yakobo (#1 kwenye Marko 5:15,20, lakini #2 kwenye Marko 1:21;
2:14; 4:12).

◙ **"roho"** Hili ni neno la Kigiriki *psuchē*. Ni vigumu sana kulielezea. Laweza kuongelea

1. Maisha yetu ya kimwili Duniani (kama vile Marko 3:4; 8:35; 10:45)
2. Hisia zetu na utambuzi binafsi (kama vile Marko 12:30; 14:34)
3. Roho zetu, ufahamu wa milele (kama vile Marko 8:36,37)

Ugumu wa kulitafasiri neno hili unatokana na utumiaji wake wa falfasa za Kiyunani, wanadamu wana nafsi, kinyume cha dhana ya Kiebrania ya wanadamu ni nafsi (kama vile Mwa. 2:7).

**3:5 "Akawakazia macho pande zote kwa hasira "** Injili ya Marko iko wazi zaidi kuandika hisia za Yesu (kama vile. Marko 1:40-42,43; 3:1-5; 10:13-16,17-22; 14:33-34; 15:34). Ukimya usioweza kusikika na kujiona bora kwa wakuu wa kidini wenye kijihesabia haki walimkasilisha Yesu! Jambo hili linaendelea kubainishwa katika 2:27-28.

◙ **"huzuni kwa ajili ya ugumu wa mioyo yao"** Huu ni muundo wenye kutiliwa mkazo wa neno huzuni (*lupē*) na kihusishi *jua*. Umetumika hapa pekee katika Agano jipya. Yesu alitambulishwa na tatizo la mtu huyu na akaonyesha tofauti dhidi ya misimamo isiyobadilika ya viongozi wa kidini. Hawakupenda kuona ukweli kwa sababu walikuwa wamejitoa kwenye mapokeo (kama vile Isa. 29:13; Kol. 2:16-23). Ni kwa namna gani hili linatokea kwetu mara kwa mara?

Neno "ugumu" linamaanisha kugeuka kuwa jiwe (kama vile Rum. 11:25; Efe. 4:18). Tazama Mada Maalumu katika: Moyo katika Marko 2:6.

◙ **"mzima tena"** Neno hili (yaani.,kurejesha kwenye hali yake ya mwanzo) linadokeza kwamba mkono uliopooza ni ajali, sio tatizo la kuzaliwa nalo. Toleo la *Gospel of Hebrews* lisilokuwa la sheria za kanisa lina kumbukumbu za utamaduni kwamba alikuwa mwashi aliyekuja kwa Yesu kumuuliza ili kuurejesha mkono wake na hivyo anaweza kurudi na kuendelea na kazi.

**3:6 "wakatoka wale Mafarisayo"** Luka 6:11 inasema "kwa ghadhabu." Kwa maana iliyo wazi "ni kuwa nje ya ufahamu" (kama vile 2 Tim. 3:9). Tazama muhtasri kwenye Mafarisayo katika Marko 2:16.

◙ **"upesi"** tazama muhtasari katika Marko 1:10.

◙ **"wakifanya shauri"** Hii ni Kauli tendaji elekezi ya wakati usio timilifu ikitumika katika maana ya mwanzo wa tendo wakati uliopita. Katika Marko 3:11 kauli tatu za wakati usio timilifu zimetumika kuonyesha matendo yaliyorudiwa kwenye wakati uliopita. Matumizi haya mawili ni maana ya lugha kuu katika hii njeo.

◙ **"pamoja na Maherodi"** kwa kawaida Mafarisayo wasiopenda mabadiliko na wazalendo wasingaliweza kufanya lolote mbele ya Maherodi waliobobea kisiasa waliounga mkono utawala wa Herode na umiliki wa Kirumi.

## MADA MAALUM: MAHERODI

Maherodi lilikuwa kundi maalum katika karne ya kwanza katika Palestina na walitoa mahusiano yao na familia tawala ya Herodi (angalia Josephus, Antiq. 14.15.6).

Maherodi walikuwa familia ya watawala wa Edomu (Edom) kwa kuanza na Herode Mkuu. Wakati wa kifo chake vijana wake kadhaa waligawana ufalme wake. Maherodi wote walikuwa waunga mkono serikali ya Kirumi. Wafuasi wao walitaka kulinda heshima yao ya kisiasa. Walipendelea utawala wa Maherodi kuliko utawala wa moja kwa moja

wa Kirumi. Kikundi hiki kilikuwa ni cha kisiasa pekee. Hawakutambua rasmi thiolojia ya Mafarisayo au Masadukayo.

◙ **"jinsi ya kumwangamiza"** Viongozi hawa walichukizwa na uponyaji siku ya Sabato, lakini angalia mtu aliyepanga mauaji hakuwa na shida! Ni wazi msingi wa maamuzi yao ulikuwa katika kitabu cha Kutoka. 31:13-17. Mambo mabaya yalifanywa kwa jina la Mungu. Kwa hakika hiki ni kivuli cha kifo cha Yesu katika mikono ya uongozi wa kiyahudi.

## MADA MAALLUM: UHARIBIFU *(APOLLUMI)*

Neno hili lina elimu-maana pana, ambayo imesababisha mkanganyiko mkubwa katika kuhusianisha na dhana ya kithiolojia juu ya hukumu ya milele dhidi ya maangamizo. Maana halisi ya msingi inatoka kwenye neno apo pamoja na ollumi, likimaanisha kuharibu/angamiza.

Tatizo linalokuja kwenye matumizi ya neno hili kitamathari. Hili laweza kuonekana wazi katika toleo la Louw na Nida's *Greek-English Lexicon of the New Testament, Based On Semantic Domains*, juzuu. 2, uk. 30. Inaorodhesha maana nyingi za neno.

1. Angamiza (mfano Mt. 10:28; Luka 5:37; Yohana 10:10; 17:12; Mdo. 5:37; Rum. 9:22 toka juzuu. 1, uk. 232)
2. Kushindwa kupata (mfano Mt. 10:42, juzuu. 1, uk. 566)
3. kupoteza (mfano., Luka 15:8, juzuu. 1, uk. 566)
4. Kutokufahamu eneo (mfano., Luka 15:4, juzuu. 1, uk. 330)
5. kufa (mfano., Mt. 10:39, juzuu. 1, uk. 266)

Gerhard Kittel, *Theological Dictionary of the New Testament, vol. 1,* ukurasa 394, anajaribu kuonyesha matumizi tofauti kwa kuorodhesha maana Nne:

1. kuangamiza au kuuwa (mfano Mt. 2:13; 27:20; Marko 3:6; 9:22; Luka 6:9; 1 Kor. 1:19)
2. Kupoteza au kupata hasara (mfano., Marko 9:41; Luk. 15:4,8)
3. kuangamia (mfano., Mt. 26:52; Marko 4:38; Luka 11:51; 13:3,5,33; 15:17; Yohana 6:12,27; 1 Kor. 10:9-10)
4. kupotea (mfano., Mt. 5:29-30; Marko 2:22; Luka 15: 4,6,24,32; 21:18; Mdo. 27:34)

Kittle baadaye alisema, "kwa ujumla tunaweza kusema kuwa mstari wa #2 na #4 inayaweka chini maelezo yanayohusiana na ulumwengu huu katika mihitasari ya injili, wakati mstari wa #1 na #3 inayashusha chini maelezo yanayohusiana na ulimwengu ujao, kama ilivyo katika kitabu cha Paulo na Yohana" (uk. 394).

Ukiangalia ndani humu kuna mkanganyiko. Neno lina elimu-maana pana ya utumiaji ambayo waandishi tofauti wa Agano Jipya wanaitumia katika maana tofauti. Nampenda Robert B. Girdlestone, *Synonyms of the Old Testament,* kur 275-277. Alihusianisha neno kwa watu wale kimaadili walikuwa wamekwisha haribika na wakisubiri utengano wa milele toka kwa Mungu dhidi ya wale watu wanaomjua Kristo na wana uzima wa milele ndani yao. Kundi la awali ni lile "lililookolewa" na kundi la kwanza ni lile "lililoangamizwa."

Robert B. Girdlestone, katika maaandishi yake yenye maneno yaliyokaribiana maana ya Agano la Kale, uk. 276, anaelekeza kuwa kuna sehemu nyingi ambazo neno hili laweza lisitafasiliwe kama maangamizi, "maumivu kama hayo yanakifanya kitu kiutendaji kionekana kutokuwa na maana kwa kusudi lake la awali."

1. Upotevu wa marhamu, Mt. 26:8
2. Uharibifu wa kutia divai katika viriba vikuukuu, Mt. 9:17
3. Uharibifu wa nywele, Luka 21:18
4. Uharibifu wa chakula, Yohana 6:27
5. Uharibifu wa dhahabu ipoteayo, 1 Pet. 1:7
6. Uharibifu wa ulimwengu, 2 Pet. 3:6
7. Uharibifu wa kimwili, Mt. 2:13; 8:25; 12:14; 21:41; 22:7; 26:52; 27:20; Rum. 2:12; 14:15; na 1 Kor. 8:11

Neno hili kamwe halirejerei maangamizi ya mtu, lakini mwisho wa uwepo wa kimwili. Pia mara nyingi linatumika katika maana iliyo sawa. "watu wote wanahesabika kuharibika kimaadili, yaani, wameshindwa kuchukuliana na kusudi ambalo kizazi kilifanywa kuwa viumbe hai" (uk.276). Ukubarifu wa Mungu kwenye tatizo ya dhambi hii alikuwa ni Yesu Kristo (kama vile Yohana 3:15-16 na 2 Pet. 3:9). Wale wote walioikataa injili sasa wametizamishwa kwenye uharibifu mwingine, unaojumuisha mwili na roho (kama vile 1 Kor. 1:18; 2 Kor. 2:15; 4:3; 2 The. 2:10). kwa

hoja nyingine iliyokinyume angalia Fudge, *the fire that consumes*.

Binafsi (kama vile R. B. Girdlestone, *Synonyms of the Old Testament*, uk. 276) hafikirii kuwa neno hili linadokeza maangamizi (kama vile E. Fudge, *The Fire That Consumes*). Neno "milele" linatumika pote kwa adhabu ya milele na uzima wa milele katika Mt. 25:46. Kulishusha thamani moja ni kuyashusha yote!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 3:7-12**
[7] **Naye Yesu akajitenga, yeye na wanafunzi wake, akaenda baharini. Mkutano mkuu ukamfuata, kutoka Galilaya, na Uyahudi,** [8] **na Yerusalemu, na Idumaya, na ng'ambo ya Yordani, na pande za Tiro na Sidoni, mkutano mkuu, waliposikia habari za mambo yote aliyokuwa akiyatenda, wakamwendea.** [9] **Akawaambia wanafunzi wake ya kwamba chombo kidogo kikae karibu naye, kwa sababu ya mkutano, wasije wakamsonga.** [10] **Maana aliponya wengi, hata wote waliokuwa na misiba wakamrukia wapate kumgusa.** [11] **Na pepo wachafu, kila walipomwona, walianguka mbele yake, wakalia wakisema, Wewe ndiwe Mwana wa Mungu.** [12] **Akawakataza sana, wasimdhihirishe.**

**3:7-8** Ongezeko kubwa la watu waliokuwa wakimfata Yesu ni sababu mojawapo ya upinzani kutoka kwa viongozi wa kidini (kama vile Mt.12:15 -16; Luka 6:17-19).

**3:8 "Idumaya"** Hii inarejelea nchi ya kale ya Edomu ambapo palikuwa ni nyumbani mwa Herodi.

◙ **"ng'ambo ya Yordani"** hii inarejelea eneo lililokuwa linaitwa Perea katika mkoa wa ng'ambo ya Yordani. Huu ni mmojawapo wa mikoa mitatu iliyofahamika kama miji ya makimbilio kulingana na sheria ya Musa (yaani Yuda, Galilaya, na nchi nyingine upande wa Yordani [yaani., Perea, kama vile. *Baba Bathra* 3:2]). Ki uhalali unatajwa kama nchi iliyoko kati ya mito Yaboki na Arnoni (katika Agano la kale , Ammoni na Moab).

◙ **"pande za Tiro na Sidoni"** Hii inarejelea ufalme wa kale wa Foinike.

◙ **"mkutano mkuu" ni** dhahiri hapa kuna mchanganyiko wa Wayahudi na Watu wa mataifa.

**3:9 "chombo"** Hii inarejerea mtumbwi mdogo wa makasia.

◙ **"ukiwa tayari kwa ajili yake muda wote"** Mtumbwi huu wakati wote ulipatikana na kwa kuhofia kuzidiwa na makutano waliusukuma ndani ya bahari (kama vile. Marko 1:45).

**3:10 "waliokuwa na misiba wakamrukia"** Hii ni dhahiri kuwa "kuanguka mbele zake." Kila aliyekuwa mgonjwa alitamani kumgusa (kama vile. Marko 5:25-34). Makutano haya walionekana kama chumba cha dharula cha kusubiria daktari hospitalini.

**3:11** kuna mfuatano wa vitenzi vya wakati usio timilifu katika mstari huu ambavyo vinaonyesha majibizano ya Yesu yanayoendelea na pepo wabaya tazama MADA MAALUM: UPUNGAJI PEPO katika Marko 1:25.

◙ **"mwana wa Mungu"** Hawa pepo wabaya hawakuwa mashahidi kwa ajili ya manufaa ya Yesu, lakini kutilia mkazo matarajio ya makutano. Hii ilipelekea kushutumiwa katika Marko 3:22 kwamba nguvu za Yesu zimetoka kwa Shetani (kama vile Mt. 9:34; 10:25; 11:18). Viongozi wa Kiyahudi hawakuweza kushindana na nguvu za Yesu, hivyo basi walitilia mashaka chanzo cha mamlaka yake.

## MADA MAALUM:MWANA WA MUNGU

A. Kuna mkanganyiko mkubwa juu ya utambuzi wa kifungu "wana wa Mungu." Pamekuwepo na tafasiri tatu kuu
   1. Kifungu kinarejea juu ya uzao wa ki-Mungu wa Sethi (kama vile Mwanzo 5, soma maelezo kwenye 4:14

2. Kifungu kinarejea juu ya kikundi cha viumbe wa kimalaika
3. Kifungu kinarejea juu ya wafalme, wadhalimu au uzao wa Kaini (kama vile Mwanzo 4)

B. Ushahidi kwa ajili ya kifungu hiki unarejea juu ya uzao wa Sethi
1. Muktadha wa haraka wa fasihi wa Mwanzo 4 na 5 unaonyesha maendeleo ya uzao wa uasi wa Kaini na uzao wa Sethi uliochaguliwa. Kwa hiyo, ushahidi wa kimuktadha unaonekana kuupendelea uzao wa ki-Mungu wa Sethi
2. Walimu wa dini ya Kiyahudi wamekuwa wakitofautiana juu ya uelewa wa kifungu hiki. Baadhi wanadai kuwa kinamrejelea Sethi (lakini wengi wanadai malaika)
3. Kifungu cha umoja "wana wa Mungu," ingawa mara nyingi kinatumika kwa viumbe vya kimalaika, mara chache kinarejelea wanadamu.
   a. Kumb. 14:1 – "wana wa YHWH Mungu wako"
   b. Kumb. 32:5 – "Wana wake"
   c. Kut. 22:8-9; 21:6 (yumkini mwamuzi wa Kilawi)
   d. Zaburi 73:15 – "wana wenu"
   e. Hosea 1:10 – "wana wa Mungu aliye hai"

C. Ushahidi wa kifungu unaorejelea viumbe vya kimalaika
1. Huu umekuwa ni uelewa wa kawaida wa kimapokeao wa kifungu hiki. Muktadha mpana wa kitabu cha Mwanzo ungaliunga mkono huu mtizamo kama mfano mwingine wa uovu wa kimiujiza wa kuyazuia mapenzi ya Mungu kwa mwanadamu (walimu wa dini waliyasema haya kwa kinyongo)
2. Wingi wa kifungu(wana wa Mungu) unatumika kwa wingi kabisa katika Agano la Kale kwa ajili ya malaika
   a. Ayubu 1:6
   b. Ayubu 2:1
   c. Ayubu 38:7
   d. Zaburi 29:1
   e. Zaburi 89:6,7
   f. Danieli 89:6
3. Kitabu cha 1 Henoko kipindi kati ya Agano la Kale na Agano Jipya (kama vile I Enoch 6:1-8:4; 12:4-6; 19:1-3; 21:1-10) na Yubileyi (kama vile Ayubu 5:1), ambacho kilikuwa kikifahamika kati ya waamini kipindi cha Agano Jipya , kikiwa na *Genesis Apocryphon* toka kwenye magombo ya Bahari ya Chumvi, vinayafasiri haya kama malaika wale walioasi
4. Muktadha wa haraka wa sura ya 6 unaonekana kudokeza kuwa "watu wale wenye nguvu ambao walikuwa ni watu wa kale waliojulikana" walitokana na mchanganyiko huu usio sawa wa utaratibu wa uumbaji.
5. Maandiko ya kale ya Kiyunani yanalitafasiri hili "wana wa Mungu" kama "malaika wa Mungu"
6. 1 Henoko hata anadai kuwa gharika ya Nuhu ilikuwa kuangamiza huu muunganikano wa malaika/mwanadamu ambao haukuwa wa kirafiki dhidi yake na YHWH na mpango wake wa uumbaji (kama vile I Enoch 7:1na kuendelea; 15:1na kuendelea; 86:1na kuendelea)
7. Katika fasihi ya Ugariti "wana wa Mungu" inarejele kwa washirika wa hekalu la miungu wengi (yaani., wale viumbe wa chini wa kiroho)

D. Ushahidi wa kifungu unarejelea kwa wafalme au wadhalimu wa uzao wa Kaini
1. Kuna tafasiri mbali mbali za kale ambazo zinaunga mkono huu mtizamo
   a. Targum wa Onkelo (karne ya pili B.K) inatafasiri "wana wa Mungu" kama "wana wa watu wenye uwezo"
   b. Symmachus (karne ya pili B.K) tafasiri ya Kiyunani, inaritafasiri "wana wa Mungu" kama "wana wa wafalme"
   c. Neno *"elohim"* linatumika kwa viongozi wa Israel (kama vile Kut. 21:6; 22:8; Zab. 82:1,6), kumbuka Biblia ya NIV na NET
   d. *Nephilim* lililounganishwa na *Gibborim* katika Mwa. 6:4, *Gibborim* ni kutoka *Gibbor* likimaanisha "mwanaume mwenye nguvu jasiri; utajiri au nguvu
   e. Ufasiri huu na ushahidi umechukuliwa toka maneno magumu ya Biblia kur. 106-108.

E. Ushahidi wa kihistoria wa watetezi wa matumizi yote

1. Kifungu kinarejelea kwa Sethi
   a. Cyril wa Iskanda
   b. Theodoret
   c. Augustine
   d. Jerome
   e. Calvin
   f. Kyle
   g. Gleason Archer
   h. Watts
2. Kifungu kinarejelea kwa viumbe wa kimalaika
   a. Waandishi wa tafasiri ya maandiko ya kale
   b. b. Philo
   c. Josephus (*Antiquities* 1:3:1)
   d. Justin Martyr
   e. Irenaeus
   f. Clement wa Isakanderia
   g. Tertullian
   h. Origen
   i. Luther
   j. Ewald
   k. Delitzsch
   l. Hengstenberg
   m. Olford
   n. Westermann
   o. Wenham
   p. NET Bible

F. Ni kwa namna gani "Manefili" wa Mwanzo 6:4 wanahusiana na "wana wa Mungu" na "binti za wanadamu" wa Mwanzo 6:1-2? Kumbuka hizi nadharia:
   1. Wao ni matokeo ya majitu makubwa (kama vile Hesabu 13:33) ya muunganikano kati ya malaika na binadamu wa kike.
   2. Havihusiani kabisa. Vimetajwa tu kama viliwahi kuwepo kwenye uso wa dunia kwenye nyakati za matukio ya Mwanzo 6:1-2 na pia baadaye
   3. R. K. Harrison katika *Introduction to the Old Testament*, uk. 557, ana nukuu yenye kutatiza, "kukoswa moja kwa moja thamani ya utambuzi wa ndani juu ya elimu ya binadamu na maendeleo yake kuelekea kwenye mwingiliano wa mahusiano ya *homo sapiens* na viumbe wa mwanzo waliotokana na Adamu ambamo sura nzima imehusika, na ambayo imekubalika kwa wale wasomi ambao wameweza kuwafatilia." Hili linanijulisha kuwa aliyaona haya makundi mawili kama yenye kuwakilisha makundi tofauti ya tabia za kibinadamu. Hili lingalidokeza uumbaji maalum wa baadae wa Adamu na Hawa, lakini pia maendeleo ya kimabadiliko ya viumbe *Homo erectus*

G. Ni haki kuweka wazi uelewa wangu wa mkanganyiko wa andiko hili. Kwanza, ngoja tukumbushane sisi sote kuwa andiko kwenye Mwanzo ni fupi na ni gumu. Msikiaji wa mwanzo ambaye ni Musa alikuwa amekwisha kuwa na utambuzi wa ndani zaidi wa kihistoria au Musa alitumia utaribu wa simulizi au kuandikwa toka kipindi cha utawala wa kiume kwamba yeye mwenyewe hakuelewa kwa ukamilifu. Hili suala sio mada muhimu ya kithiolojia. Mara nyingi tunakuwa wadadisi kuhusu vitu ambavyo maandiko yanavigusia lakini ni vigumu kueleweka. Itakuwa bahati mbaya kufanya thiolojia kiundani nje ya hili na sehemu zenye kufanana za habari ya kibiblia. Kama tungetaka habari hizi Mungu angaliweza kuzitoa kwa uwazi na ukamilifu. Mimi pekee naamini walikuwa malaika na wanadamu kwa sababu:
   1. Ni mwendelezo, ingawa haikukatazwa, kukitumia kifungu "wana wa Mungu" kwa ajili ya malaika katika Agano la Kale
   2. Mtafasiri wa maandiko ya kale ya Kiebrania (Iskanderia) analitafasiri (karne ya kwanza K.K) "wana wa Mungu" kama "malaika wa Mungu"
   3. Kitabu cha maandiko ya uongo chenye matukio ya mwisho cha 1 Henoko (yumkini yaliandikwa miaka ya 200 K.K) ni halisia kuwa yanarejelea kwa malaika (kama vile sura ya 6-7)
   4. Kithiolojia inaunganisha na 2 Petro 2 na Yuda juu ya malaika waliotenda dhambi na hawakutunza mazingira yao vizuri, ninajua kuwa kwa kiasi Fulani hili linaleta mkanganyiko kwa Mathayo 22:30, lakini hawa malaika maalum hawako mbinguni wala duniani bali wako katika gereza maalum(Tartarus)
   5. Nafikiria kuwa sababu mojawapo ya matukio mengi ya Mwanzo 1-11 yanapatikana katika tamaduni (yaani., habari za uumbaji wenye kufanana , habari za kufanana za gharika, habari mfanano za malaika kuwachukua malaika) ni kwa sababu wanadamu wote walikuwa pamoja na walikuwa na maarifa juu ya YHWH wakati wa kipindi hiki, lakini baada ya kutawanyika kwenye mnara wa Babel maarifa haya yakapotoshwa na kubadilishwa kwenye imani ya miungu wengi.

      Mfano mzuri wa hadithi za kubuniwa zilikuwa ni watu wenye maumbo makubwa nusu wanadamu wenye uwezo mkubwa wa kufikiri yaliyoitwa majitu (titans) yaliyokuwa yamewekwa gerezani kwenye *Tartarus*, hili ni jina lililotumika mara moja kwenye Biblia (kama vile 2 Petro 2) kwa ajili ya sehemu ya

kuwaweka malaika wasiotunza vizuri ukazi wao. Katika thiolojia ya sheria za dini ya Kiyahudi kuzimu kuligawanywa katika sehemu mbili kwa ajili ya watakatifu paliitwa Paradiso na kwa ajili ya waovu paliitwa (*Tartarus*).

**3:12** Hili bado linaendelea kutiliwa mkazo katika "siri za Masihi" kwenye Marko. Yesu , kwa neno na matendo, ni ufunuo kamili wa Yeye kama Masihi mwanzoni mwa kitabu cha Marko, lakini kwa kutokufahamu kwa (1) viongozi wa kiyahudi (yaani., Masihi kama shujaa wa taifa anairejesha Israeli ijulikane Duniani) na (2) makutano (yaani ., Masihi kama mtenda miujiza), Yesu aliwaonya watu kadhaa tofauti kwamba wasimdhihirishe. Injili pekee ndiyo itakayokamilisha maisha yake baada ya kifo, kufufuka, na kupaa mbinguni.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 3:13-19**
**[13] Akapanda mlimani, akawaita aliowataka mwenyewe; wakamwendea. [14] Akaweka watu kumi na wawili, wapate kuwa pamoja naye, na kwamba awatume kuhubiri, [15] tena wawe na amri ya kutoa pepo. [16] Akawaweka wale Thenashara; na Simoni akampa jina la Petro; [17] na Yakobo, mwana wa Zebedayo, na Yohana nduguye Yakobo, akawapa jina la Boanerge, maana yake, wana wa ngurumo; [18] na Andrea, na Filipo, na Bartholomayo, na Mathayo, na Tomaso, na Yakobo wa Alfayo, na Thadayo, na Simoni Mkananayo, [19] na Yuda Iskariote, ndiye aliyemsaliti. Kisha akaingia nyumbani.**

**3:13 "akapanda mlimani"** Hili linaweza kufahamika kwa njia mbili: (1) Yesu aliondoka eneo lililokuwa jirani na bahari ya Galilaya na akaenda juu ya kilele cha mlima au (2) huu ni utambulisho wa mpangilio wa mahubiri ya mlimani (kama vile Mt. 5-7), ambayo Marko hakuweka kumbukumbu.

**3:14 "akaweka watu kumi na wawili"** Hii inafanana na mahubiri ya wazi katika Luka 6:12-16. Marko hakuweka kumbukumbu ya mahubiri ya Mathayo kule mlimani (yaani., Mt. 5-7).

## MADA MAALUMU: NAMBA KUMI NA MBILI

Kumi na mbili mara nyingi imekuwa kiishara (angalia Mada Maalumu: Namba za Kiishara katika Andiko namba ya shirika

A. Nje ya biblia
   1. Ishara kumi na mbli za ukanda
   2. Miezi kumi na miwili ya mwaka
B. Katika Agano la Kale (BDB 1040 kuongeza 797)
   1. wana wa Yakobo (Makabila ya Kiyunani)
   2. waliotazamishwa kwenye
      a. Nguzo kumi na mbili za madhabahu katika Kut. 24:
      b. Vito kumi na viwili juu ya kifua cha kuhani mkuu (ambayo vinasimama kwa niaba ya makabila) katika Kut. 28:21
      c. unga mwembamba wa mkate kimi na miwili katika sehemu takatifu ya kibanda katika Law. 24:5
      d. wapelelezi kumi na wawili waliotumwa huko Kanaani katika idadi ya kabila (mmoja kutoka katika kila kabila)
      e. fimbo kumi na mblili (viwango vya kikabila) katika uhasi wa Kora katika Hes. 17:2
      f. mawe kumi na mawili ya Yoshua katika Yos. 4:3,9,20
      g. majimbo kumi na mawili ya kiutawala katika utawala wa Suleimani katika 1 Fal. 4:7
      h. mawe kumi na mawili ya madhabahu yaYHWH katika 1 Fal. 18:31
C. Katika Agano Jipya
   1. Mitume kumi na wawili waliochaguliwa
   2. Vikapu kumi na iwili vya mikate (kimoja kwa kila Mtume) katika Mt. 14:20
   3. Viti kumi na viwili vya enzi ambapo Wanafunzi wa Agano Jipyala wamekaa (vinayorejea juu ya makabila

12 ya Israeli) katika Mt. 19:28

4. Majeshi kumi na mmawili ya malaika wa kumsaidia Yesu katika Mt. 26:53
5. Ishara ya Ufunuo
    a. Wazee 24 juu ya viti 24 4:4
    b. 144,000 (12x12,000) katika 7:4; 14:1,3
    c. nyota kumi na mbili juu ya taji la mwanamke katika 12:1
    d. malango kumi na mawili, malaika kumi na wawili wakiakisi makabila kumi na mawili katika 21:12
    e. Mawe kumi na mawili ya misingi ya Yerusalemu mpya na juu yao majina ya mitume kumi na mawili katika 21:14
    f. Mianzi kumi na mbili elfu katika 21:16 (kipimo cha mji mpya, Yerusalemu Mpya)
    g. kuta ni dhiraa 144 katika 21:17
    h. malango kumi na mawili ya lulu katika 21:21

miti mipya katika Yerusalemu yenye aina aina kumi na bili za tunda (moja kwa kila mwezi) katika 22:2

**3:14** Kuna baadhi ya tungo zimeongezwa katika mstari huu na waandishi wa kale wa Kigiriki, א, B, na ina mabadiliko kidogo, katika C. Tungo iliyoongezwa ni "yeye yule aliyeitwa mtume" (tazama tanbihi katika NRSV). Maandiko mengi yana uhakika kwamba nyongeza hii imechukuliwa kutoka katika Luka 6:13.

◙ **"wapate kuwa pamoja naye"** Yesu alihusika kwa undani zaidi kuwafundisha hawa kumi na mbili. Robert Coleman ameandika vitabu viwili vya kusaidia kuelewa mbinu za Yesu: *The Master Plan of Evangelism* na *The Master Plan of Discipleship*,vyote ambavyo vinahusika na ukuaji wa kanisa la awali wakitumia kanuni sawa na za Yesu.

◙ **"na kwamba awatume kuhubiri"** Yesu alikuja kuhubiri habari njema za ufalme. Aliwafundisha wanafunzi wafanye kama yeye: (1) kumi na mbili (kama vile. Marko 6:7-13; Mt. 10:1,9-14; Luka 9:1-6) na (2) baadae ,wanafunzi sabini (kama vile Luka 10:1-20).

**3:15 "pepo"** Hii inawezekana inarejelea kwa malaika walioasi, wakitenda kwa niaba ya shetani. Hata hivyo, Biblia imenyamaza juu ya pepo wabaya. Mamlaka ya Yesu juu yao yanaimarisha nguvu zake na huduma ya Kimasihi.Tazama mada maalumu katika Marko 1:24.

**3:16 "Akawaweka wale Thenashara"** Hawa kumi na mbili wametajwa mara nne kwenye Agano jipya (kama vile. Mt. 10:2-4; Marko 3:16-19; Luka 6:14-16; na Matendo 1:13 [utambulisho kwa Mt. 10:2-4]). Orodha mara zote inajitokeza katika makundi manne yenye watu watatu. Amri mara nyingi inabadilika kwenye makundi (lakini Petro mara zote ni wa kwanza na Yuda Iskarioti mara zote ni wa mwisho). Inawezekana kwamba makundi haya yaliaksi namna ya mzunguko ili kuwaruhusu hawa wanaume kurudi nyumbani muda baada ya muda kuangalia mahitaji ya familia zao. Inashangaza ni kwa kiasi gani kidogo tunaelewa juu ya mitume wa mwanzo kabisa. Mara nyingi tunatumaini katika Utamaduni wa kanisa la awali.

## MADA MAALUMU: CHATI YA MAJINA YA MITUME

| | **Mathayo 10:2-4** | **Marko 3:16-19** | **Luka 6:14-16** | **Mdo. 1:12-18** |
|---|---|---|---|---|
| **Kundi la kwanza** | Simoni (Petro)<br>Andrea (Petro nduguye)<br>Yakobo (mwana wa Zebedayo)<br>Yohana (nduguye Yakobo) | Simoni (Petro)<br>Yakobo (mwana wa `Zebedayo)<br>Yohana (nduguye Yakobo)<br>Andrea | Simoni (Petro)<br>Andrea (Petro nduguye)<br>Yakobo<br>Yohana | Petro<br>Yohana<br>Yakobo<br>Andrea |
| **Kundi la** | Filipo | Filipo | Filipo | Filipo |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **pili** | Bartholomayo<br>Thomaso<br>Mathayo (mtunza ushuru) | Bartholomayo<br>Mathayo<br>Thomaso | Bartholomayo<br>Mathayo<br>Thomaso | Thomaso<br>Bartholomayo<br>Mathayo |
| **Kundi la tatu** | Yakobo (mwana wa Alfayo)<br>Thadayo<br>Simoni (Mkananayo)<br>Yuda (Iskariote) | Yakobo (mwana wa Alfayo)<br>Thadayo<br>Simoni (Mkananayo)<br>Yuda (Iskariote) | Yakobo (mwana wa Alfayo)<br>Simoni (Zelote)<br>Yuda (wa Yakobo)<br>Yuda (Iskariote) | Yakobo (mwana wa Alfayo)<br>Simoni (Zelote)<br>Yuda (wa Yakobo) |

Kutoka katika muhtasari wa Luka 6:14:

◙ **"Simoni, aliyemwita jina la pili Petro"** Kuna orodha nyingine tatu za mitume kumi na wawili. Kwa kawaida Petro ni wa kwanza; Yuda Iskariote ni wa mwisho daima. Kuna makundi matatu kati ya manne ambayo yamebaki kwa usawa, hata kama mtiririko wa majina ndani ya makundi unageuzwa mara kwa mara (kama vile Mathayo. 10:2-4; Marko 3:16-19; Mdo. 1:13).

◙ **"Andrea"** Neno la Kiyunani linamaanisha "mwenye sifa za kiume." Kutoka Yohana 1:29-42 tunajifunza kwamba Andrea alikuwa mwanafunzi wa Yohana Mbatizaji na kwamba alimtambulisha nduguye, Petro, kwa Yesu.

◙ **"Yakobo"** Hili ni jina la Kiebrania "Jacob" (BDB 784), ambalo linamaanisha "chukua nafasi ya," kama vile Mwa. 25:26). Kuna wanaume wawili wanaitwa Yakobo katika katika orodha ya wale Kumi na wawili. Ni nduguye Yohana (kama vile Marko 3:17) na sehemu ya mzunguko wa ndani (yaani, petro, yakobo, na yohana). Huyu ni nduguye Yohana.

◙ **"Yohana"** Huyu alikuwa nduguye Yakobo na moja wa mzunguko wa ndani wa wanafunzi. Aliandika vitabu vitano katika Agano Jipya na aliishi kipindi kirefu kuliko mtume ye yote yule.

◙ **"Filipo"** Jina la Kiyunani linamaanisha "mpenda farasi" Wito wake umeandikwa katika Yohana 1:43-51.

◙ **"Bartolomayo"** Jina linamaanisha "mwana wa mtawala wa Misri" Anaweza kuwa Nathanaeli wa Injili ya Yohana (kama vile Yohana 1:45-49; 21:20).

◙ **"Mathayo"** Jina la Kiebrania (kutoka *Mattithiah*, kama vile 1 Nya. 9:31; 15:18,21; 16:5; 25:3,21; Neh. 8:4) linamaanisha "karama ya YHWH." Hii inarejea katika Lawi (kama vile Marko. 2:13-17).

◙ **"Tomaso"** Jina la Kiebrania linamaanisha "pacha" au Didimus (kama vile Yohana 11:16; 20:24; 21:2).

◙ " **Yakobo wa Alfayo "** Hili ni jina la Kiebrania "Jacob." Kuna wanaume wawili walioitwa kwa jina la Yakobo katika wale Kumi na wawili. Mmoja ni nduguye Yohana (kama vile Luka 6:17) na sehemu ya mzunguko wa ndani (yaani, Petro, Yakobo, na Yohana). Huyu anajulikana kama "Yakobo aliye mdogo" (kama vile Marko 3:17).

◙ "**Simoni aitwaye Zelote**" Maandishi ya Kiyunani ya Marko yana "Mkananayo" (pia Mathayo. 10:4). Marko, ambaye Injili iliandikwa kwa Warumi, asingetakiwa kutumia "maneno makali" ya kisiasa, Zelote, ambalo linarejea juu ya Wapigania Mabadiliko wa Kiyahudi Waishio mstuni walio kinyume na utawala wa Kirumi. Luka anamtaja kwa istilahi hii `(kama vile Mdo. 1:13). Istilahi ya Mkananayo ina minyumbuo mbali mbali.

1. kutoka eneo la Galilaya lijulikanalo kama Kana
2. kutoka matumizi ya Agano la Kale ya Wakanaani kama mfanyabiashara
3. kutoka jina la jumla kama mwenyeji wa Kanaani.

Kama jina la jumla alilolitumia Luka ni sahihi, basi Zelote linatokana na neno la Kiaramu "*enthusiast*" (kama vile Mdo.

1:17). Uchaguzi wa Yesu wa wanafunzi kumi na wawili walikuwa wametoka makundi shindani tofauti na mbalimbali. Simoni alikuwa mmoja wa kundi la kizalendo ambalo lilipigania kupinduliwa kwa ghasia za mamlaka ya Kirumi. Mara nyingi Simoni na Lawi (yaani, Mathayo, mtoza ushuru) na kila mmoja .wasingekuwa katika chumba kile kile

◙ "Yuda wa Yakobo" Pia aliitwa "Lebbeus" (kama vile Mt. 10:3) au "Yuda" (kama vile Yohana 14:22). Yote Thadayo na Lebbeus inamaanisha "mtoto apendwaye.

◙ "Yuda Iskariote," Kuna Simoni wawili, Yakobo wawili, na Yuda wawili. Jina Iskariote lina uwezekano wa minyumbuo miwili:

1. mtu wa Kerioth (mji) katika (kama vile Yos. 15:23, ambapo ingemaanisha yeye alikuwa wa Yudea pekee)
2. jina la baba yake (kama vile Yohana 6:71; 13:2,26)
3. "mtu wa uadui" au mwuaji, ambapo ingemaanisha yeye pia alikuwa Zelote, kama Simoni

◙ **" Simoni akampa jina la Petro "** Wayahudi wengi wa Galilaya walikuwa na majina mawili ya Kiyahudi (yaani Simoni au Simeoni, lenye maana "kusikia") na jina la Kigiriki (ambalo kamwe hakupewa). Yesu alimpatia jina la "mwamba". Kwa Kigiriki ni *petros* na kwa Kiaramu ni *cephas* (kama vile Yn. 1:42; Mt. 16:16). Petro ni shahidi, chanzo cha utume nyuma ya Injili ya Marko. Tazama utangulizi kwa ajili ya muhtasari kamili.

**3:17 "Boanerge. . .wana wa ngurumo"** Marko anatafsiri jina kwa Kiaramu kwa ajili ya viongozi wa (yumkini kwa Warumi) mataifa. Hawa ndugu (yaani Yakobo na Yohana) walikuwa na majina mengine katika Luka 9:54.

**3:18 "Andrea"** Hili ni neno la Kigiriki lenye maana "mwanaume." Kutoka Yohana 1:29-42 tunajifunza kwamba Andrea alikuwa mwanafunzi wa Yohana Mbatizaji na akamtambulisha kaka yake, Petro, kwa Yesu.

◙ **"Filipo"** Hili ni neno la Kigiriki lenye maana ya “mpenda Farasi." Jina hili limechanganuliwa katika Yohana 1:43-51.

◙ **"Bartholomayo"** Hili neno lina maana ya "mwana wa Ptolemy aliyekuwa mtawala wa Wagiriki na Wamisri." yumkini akawa ni Nathanieli katika Injili ya Yohana (kama vile Yohana 1:45-49; 21:20).

◙ **"Mathayo" H**ili ni neno la Kiebrania lenye maana ya “zawadi ya YHWH." Hili jina linamrejelea Lawi (kama vile. Marko 2:13-17).

◙ **"Tomaso”** Hili ni neno la Kiebrania lenye maana ya “pacha" au Didimasi (kama vile Yn. 11:16; 20:24; 21:2).

◙ **"Yakobo"** Hili ni jina la Kiebrania “Yakobo." Kuna watu wawili wametajwa kwa jina la Yakobo kwenye orodha ya wanafunzi kumi na mbili. Mmoja ni ndugu yake Yohana (kama vile Marko 3:17) na sehemu ya ndani (yaani, Petro, Yakobo, na Yohana). Huyu mwingine Yakobo hafahamiki sana.

◙ **"Thadayo"** pia aliitwa "Lebeusi" (kama vile Mt. 10:3) au "Yuda" (kama vile. Yohana 14:22). Majina Yote ya Thadayo na Lebbeus yanamaanisha "mwana mpendwa."

**NASB "Simoni Zelote"**
**NKJV "Simoni mkanaani"**
**NRSV "Simoni mkanaani"**
**TEV "Simoni shujaa"**

Andiko la Kigiriki la Marko lina neno "mkanaani" (pia Mt. 10:4). Marko, ambaye Injili yake iliandikwa kwa Warumi, yumkini hakupenda kuitumia neno "la uchochezi/kuwagawa" "zelote," ambalo linarejelea Myahudi anaepinga utawala wa Kirumi. Luka alimuita kwa neno hili (kama vile. Luka 6:15 na Mdo. 1:13). Neno mkanaani yumkini linatokana na asili kadhaa.

1. Ya eneo la Galilaya linalofahamika kama Kana

2. Kutoka kwenye Agano la kale limetumia mkanaani kama mfanyabiashara
3. Kutokana na jumla ya jina kama mkanaani asili (pia iliitwa Palestina)

Kama jina la Luka ni sahihi, basi, “Zelote” linatokana na neno la Kiaramu “shauku” (kama vile Luka 6:15; Mdo 1:17). Wanafunzi wa Yesu wale kumi na wawili waliochaguliwa walitoka maeneo tofauti na makundi yanayopingana. Simoni alikuwa mtu wa kundi la kitaifa ambaye alitetea vurugu za kuiondoa mamlaka ya Kirumi. Kwa kawaida hawa Simoni na Lawi (yaani., Mathayo mtoza ushuru) hawakuwa katika chumba kimoja kila mmoja.

**3:19 "Yuda Iskarioti"** Kuna Simoni wawili, Yakobo wawili na Yuda wawili. "Iskarioti" inawezekana yana asili mbili: (1) mtu wa Keriothi katika Yuda (kama vile Yos. 15:23) au (2) "mtu wa panga" au muuaji, ambaye inamaanisha pia kuwa ni Zelote, kama Simoni.

◙ **"ndiye aliyemsaliti"** Kitenzi hiki kimepambwa na maelezo ya Injili ya Yohana juu ya Yuda (kama vile Yn. 6:71; 12:4; 13:2,26-27; 18:2-5). Kwa asili linamaanisha "kuwa juu ya mamlaka" (kama vile Marko 1:14). Uhalisia wa Yuda na / au shauku ya theolojia katika kumsaliti Yesu ni siri.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 3:20-27**
**[20] Mkutano wakakusanyika tena, hata wao wenyewe wasiweze hata kula mkate. [21] Jamaa zake walipopata habari wakatoka kwenda kumkamata; maana walisema, Amerukwa na akili. [22] Nao waandishi walioshuka kutoka Yerusalemu wakasema, Ana Beelzebuli, na, Kwa mkuu wa pepo huwatoa pepo. [23] Akawaita, akawaambia kwa mifano, Awezaje Shetani kumtoa Shetani? [24] Na ufalme ukifitinika juu ya nafsi yake, ufalme huo hauwezi kusimama; [25] na nyumba ikifitinika juu ya nafsi yake, nyumba hiyo haiwezi kusimama. [26] Na kama Shetani ameondoka juu ya nafsi yake, akafitinika, hawezi kusimama, bali huwa na kikomo. [27] Hawezi mtu kuingia ndani ya nyumba ya mtu mwenye nguvu, na kuviteka vitu vyake, asipomfunga kwanza yule mwenye nguvu; ndipo atakapoiteka nyumba yake.**

**3:20 "kisha akaingia nyumbani"** Hii inarejelea nyumba moja kama Marko 2:1 na yumkini Marko 7:17; 9:38.

◙ **"mkutano"** Haya ni matokeo ya huduma ya uponyaji na ukombozi wa Yesu (kama vile. Marko 1:45; 2:2,13; 3:7,20).

◙ **"hata wao wenyewe wasiweze hata kula mkate”** Hiki ndicho kichohusisha familia yake sana. Yesu mara zote alikuwa na muda kwa ajili ya watu wahitaji. Alijitolea kwa ajili yao.

**3:21**
**NASB, NKJV "jamaa zake"**
**NRSV, TEV "familia yake"**
**NJB "ndugu zake"**

Kwa maana iliyo wazi hii ni “waliotoka upande wake." Toleo la KJV lina “marafiki," lakini ni wazi hawa walikuwa ni Mama yake na Umbu lake.

**NASB "kumkamata"**
**NKJV "kumshikilia"**
**NRSV "kumzuia"**
**TEV, NJB "kumshitaki"**

Hiki ni kitenzi imara kwenye Mathayo (kama vile Mt. 14:3; 18:28), lakini kwa kawaida hakuna vurugu katika Marko. Mara nyingi kinarejelea kwa wagonjwa wanaohitaji msaada kwa kuwainua kwa mikono. Ndugu zake walijaribu kumpeleka nyumbani kwa nguvu kwa sababu walifikiria kuwa anatenda mambo ya kipumbavu (kama vile. Marko 3:31-35).

**NASB** **"amerukwa na akili"**
**NKJV, NJB** **"amepoteza ufahamu"**
**NRSV** **"hana ufahamu"**
**TEV** **"amechanganyikiwa"**

Andiko la Kiyunani lina utata kama ni kwa nani maelezo haya yalimhusu. Ni kwa ndugu (yaani., NASB, NKJV, NJB,NIV) au ni kitu ambacho ndugu walisikia wengine wakisema (yaani., NRSV, TEV)?

Neno katika muktadha huu linamaanisha "kutenganishwa kutoka katika msawazo wa akili" (kama vile 2 Kor. 5:13). Mara nyingi limetumika katika Marko kwa ajili ya "mshangao" wa watu (kama vile Marko 2:12; 5:42).

Hii inaonyesha kwamba ingawa Yesu alikuwa na umati mkubwa wa makutano, hakuelewa kwa (1) wanafunzi wake; (2) viongozi wa kidini; (3) kwa ndugu zake; na (4) hao makutano.

**3:22 Nao waandishi walioshuka kutoka Yerusalemu "** Hii inarejelea wale waliotajwa katika Marko 2:6,16, ambao ni dhahili walikuwa ni kundi lililotoka kwa Wakuu wa Sinagogi waliotumwa kukusanya taarifa za mafundisho na matendo ya Yesu.

◙ **"ana"** Hii inamaanisha ana milikiwa na pepo wabaya na nguvu zake zinatoka kwa shetani (kama vile Mt. 9:34; Yn. 7:20; 8:48-52; 10:20). Jambo sawa na alilolizungumza Yohana mbatizaji (kama vile Mt. 11:18). Hawakuikana miujiza ya Yesu hivyo walitilia mashaka chanzo cha nguvu zake na mamlaka.

◙ **"Beelzebuli"** Hii ni nomino isiyonyambulika inatamkwa Beelzebub katika toleo la KJV, lakini Beelzebuli katika tafsiri za kisasa. Neno "beel" linaakisi neno la semeti ba'al, ambalo linamaanisha "bwana," "mmiliki," "mwajiri,"au "mme." Ni jina kwa ajili ya miungu ya kanaani inayohusika na ustawi.

Neno "zebul" linaweza kumaanisha (1) urefu (yaani.,mlima au mbingu); (2) mwana wa mfalme (yaani Zabul); au (3) mavi ya mnyama. Mara nyingi Wayahudi hubadilisha herufi za miungu ya kigeni ili kuishusha heshima.

Kama "zebub"inaweza kurejelea

1. Baali wa Ekroni (kama vile. 2 Fal. 1:2,3,6)
2. miungu ya Wafilisti, Zebaba
3. mchezo wa neno la Kiaramu au utani wa "bwana wa uadui" (yaani., *be'el debaba*)
4. "bwana wa nzi" (Kiaramu "nzi" *dibaba*)

Kutamka, *Beelzebub*, hakufahamiki kwa utaalamu wa dini na sheria za Kiyahudi. kwa habari zaidi juu majina ya uovu binafsi tazama *The NewInternational Dictionary of New Testament Theology*, juzuu. 3,uk. 468-473.

◙ **"kwa mkuu wa pepo"** Jina Beelzebuli kwa kawaida sio jina la shetani katika Uyahudi. Yesu alilitumia kama lenye maana sawa na shetani katika Marko 3:23.

**3:23-26** Yesu alionyesha mantiki ya tabia ya nguvu zake juu ya pepo wabaya kwa shetani. Ni wazi kuwa kiongozi kwenda kinyume na mtumishi wake ni maafa!

**3:23 "akawaita"** Hii ni kuwaonyesha wao (yaani., waandishi katika Marko 3:22) kwamba aliweza kuyasoma mawazo yao (tazama muhtasari katika Marko 2:6b). na pia aliwapa nafasi zaidi ya kuusikiliza ujumbe wake sawasawa.

◙ **"mifano"** maana ya wazi kwa neno hili (*parabolē*, limetumika mara 13 katika Marko) ni "tupa pembeni ." kwa kawaida ni tukio la maisha imetumika kuelezea kwa mfano wa ukweli wa kiroho.

**3:24 "kama"** Hii ni sentensi ya hali ya tatu yenye maana ya matendo yanayowezekana.

**3:27 " asipomfunga kwanza yule mwenye nguvu "** Huu ni utaji wa Kimasihi uliorejelewa katika Isa. 49:24-25. Na hii pia inaonyesha kwamba ufahamu wa Yesu una nguvu zaidi kuliko shetani. Katika Uyahudi matendo ya upungaji pepo ni ya kawaida (kama vile Marko 9:38; Mdo 19:14). Ni nini kilichokuwa si cha kawaida katika nguvu na mamlaka zilizotolewa na

Yesu dhidi ya nguvu za pepo wabaya na utaratibu uliotumiwa na waalimu wa sheria wa Kiyahudi. Yesu alionyesha wazi kwamba kwa kuja kwake shetani ameshashindwa tayari! Hata Augustine anaweka dondoo katika Marko 3:24 kama ushahidi kwamba ahadi za miaka elfu moja tayari ziko sasa (yaani.,miaka elfu moja).

Mstari huu unatumika leo kama ushahidi wa andiko kwa ajili ya "kumshurutisha" shetani kutoka kwenye mikutano ya Wakristo. Andiko hili haliwezi kuwa na maana kama kigezo kwa ajili ya Wakristo kuomba dhidi ya shetani. Waaminio hawakufundishwa kamwe kumwelezea shetani. Mstari huu umegeuzwa kuwa wimbo wa ushirikina ambao kwa ujumla ni nje ya tabia ya Agano jipya.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 3:28-30**
**[28] Amin, nawaambia, Dhambi zote; watasamehewa wanadamu, na kufuru zao watakazokufuru zote; [29] bali mtu atakayemkufuru Roho Mtakatifu hana msamaha hata milele; ila atakuwa ana dhambi ya milele, [30] kwa vile walivyosema, Ana pepo mchafu. zote watasamehewa wanadamu, na kufuru zao watakazokufuru**

**3:28 "amin"** Hili kwa maana iliyo wazi ni "amina." Mwanzoni Yesu alitumia "kweli" ambalo ni neno la pekee. Kwa kawaida ni maelezo ya maana sana yaliyotangulia.

## MADA MAALUM: AMINA

I. AGANO LA KALE
   A. Neno "Amina" linatoka kwenye neno la Kiebrania lenye maana ya
      1. "ukweli" (emun, emunah, BDB 53)
      2. "Uaminifu" (emun, emunah, BDB 53)
      3. "imani" au "uaminifu"
      4. "amini" (dmn, BDB 52)
   B. Asili yake ya neno inadokeza mkao wa mwili wa mtu ulivyo imara. Kinyume cha hili kinaonyesha mwili wa mtu Yule asio imara, unaotereza (kama vile Zab. 35:6; 40:2; 73:18; Yeremia 23:12) au kizuizi (kama vile Zab. 73:2). Kutokana na utumiaji huu wa fasihi unatengeneza upanuzi wa kiisitiari wa imani, uaminifu, utiifu na wa kutegemewa (kama vile Hab. 2:4)
   C. Utumiaji maalumu (angalia mada maalumu: kuamini, amini, imani na uaminifu katika agano la kale)
      1. Nguzo, 2 Fal. 18:16 (1 Tim. 3:15)
      2. Kuthibitika, Kut 17:12
      3. Uimalifu, Kut. 17:12
      4. Uthabiti, Isa. 33:6
      5. Ukweli, 1 Fal. 10:6; 17:24; 22:16; Mith. 12:22
      6. Thabiti, 2 Nya. 20:20; Isa. 7:9
      7. Stahili (sheria alizopewa Musa), Zab. 119:43,142,151,160

   D. Katika Agano la Kale maneno mawili ya Kiebrania yanatumika kwa ajili ya imani thabiti
      1. Bathach(BDB 105), imani
      2. Yra(BDB 431), hofu, heshima, abudu (kama vile Mwa. 22:12)
   E. Kwa maana ya kuamini au uaminifu ulioanzishwa kwa matumizi ya liturujia ambao ulitumika kuthibitisha maelezo ya kweli ya mtu mwingine (kama vile. Hes. 5:22; Kumb. 27:15-26; 1 Fal. 1:36; 1 Nya. 16:36; Neh. 5:13; 8:6; Zab. 41:13; 72:19; 89:52; 106:48; Yer. 11:5; 28:6).
   F. Kiongozi cha kithiolojia kwenye neno hili sio uaminifu wa mwanadamu, bali ni wa Mungu mwenyewe (kama vile Kut. 34:6; Kumb. 32:4; Zab. 108:4; 115:1; 117:2; 138:2). Tumaini la mwanadamu aliyeanguka ni neema, uaminifu, kutii Agano la Mungu na ahadi zake. Wale wanaomfahamu Mungu wanahitajika kufanana naye (kama vile. Hab. 2:4). Biblia ni historia na kumbu kumbu ya Mungu kurejesha taswira yake (kama vile Mwa. 1:26-27) kwa mwanadamu. Wokovu unarejesha uwezo wa mwanadamu kuwa na ushirika wa ndani na Mungu. Hii ndio sababu ya kuumbwa kwetu.

II. AGANO JIPYA

A. Utumiaji wa neno “amina” kama hitimisho la kiliturujia kwa minajili ya kuthibitisha ukweli wa maelezo/taarifa ni la kawaida katika Agano Jipya (kama vile. 1 Kor. 14:16; Ufu. 1:7; 5:14; 7:12).
B. Utumiaji wa neno kama kifungio cha maombi ni wa kawaida kwenye Agano Jipya (kama vile. Rum. 1:25; 9:5; 11:36; 16:27; Gal. 1:5; 6:18; Efe. 3:21; Flp. 4:20; 2 Thess. 3:18; 1 Tim. 1:17; 6:16; 2 Tim. 4:18).
C. Yesu ndiye yeye aliyelitumia hili neno (limezidishwa mara 25 katika Yohana, yaani., Yohana 1:51; 3:3,5,11; n.k.) kuyatambulisha maelezo muhimu (kama vile Luka 4:24; 12:37; 18:17,29; 21:32; 23:43).
D. Linatumika kama cheo kwa Yesu katika Ufu 3:14 (pia angalia 2 Kor 1:20, yamkini jina la heshima la Mungu kutoka Isa. 65:16)
E. Dhana ya kusadiki au sadiki, au kuamini au amini inaelezewa katika neno la Kiyunani *pistos* au *pistis*, ambalo linatafasiliwa katika Kiingereza kama “imani”,“sadiki”,“kuamini”(angalia mada maalumu: Sadiki, Kuamini au Imani).

◙ **" Dhambi zote; watasamehewa wanadamu, na kufuru zao watakazokufuru zote "** Hii inaonyesha ukubwa wa Rehema za Mungu katika Kristo. Tungo “wana wa wanadamu" ni Lahaja ya kawaida ya semiti inayorejelea mahitaji ya mwanadamu (kama vile Zab. 8:4; Ezek. 2:1).

**3:29 “bali mtu atakayemkufuru Roho Mtakatifu”** Hii lazima ifahamike kuwa ni kabla ya historia ya Upentekosti. Na imetumika kwa maana ya ukweli wa Mungu uliokataliwa. Mafundisho ya mstari huu kwa kawaida yanaitwa “dhambi isiyosamehewa”. Na lazima imetafsiriwa katika mwanga wa vigezo vifuatavyo:

1. Tofauti katika Agano la kale kati ya “makusudi” na “dhambi isiyo ya makusudi”, (kama vile. Hes. 15:27-31)
2. Ndugu zake Yesu wasiomwamini wanatofautiana na wanaowaamini Mafarisayo katika muktadha huu.
3. Maelezo ya msamaha katika Marko 3:28
4. Tofauti kati ya injili zinazofanana, zaidi hubadili “mwana wa Adamu” (kama vile Mt.12:32; Luka 12:10) kwenda “wana wa wanadamu ," (kama vile Mt. 12:31; Marko 3:28).

Katika mwanga wa hapo juu, dhambi hii imefanywa na wale ambao, katika uwepo wa nuru kubwa na ufahamu, bado wanamkataa Yesu kwa maana ya Mungu juu ya ufunuo na wokovu. Wamebadili nuru ya injili kuwa giza la shetani (kama vile Marko 3:30). Wameikataa taswira ya roho na yenye kutumainiwa (kama vile Yn. 6:44,65). Dhambi ya kutokusamehewa haijakataliwa na Mungu kwa sababu ya tendo lake moja au neno, lakini kwa mwendelezo, wasio na imani kuendelea kumkataa Mungu katika kristo (yaani waandishi na Mafarisayo).

Dhambi hii imefanywa pekee na wale ambao wamewekwa wazi na injili. Wale waliosikia ujumbe juu ya Yesu kwa uwazi ndio haswa wanahusika kwa ajili ya kukataliwa. Huu ni ukweli maalum wa tamaduni za kisasa kwamba wanaendelea kuielekea injili, lakini wakimkataa Yesu (yaani ., Marekani, utamaduni wa magharibi).

Kwa ajili ya utatu wa Roho mtakatifu tazama mada maalum ifuatayo.

## MADA MAALUM: UTU WA ROHO

Kwenye Agano la Kale “Roho wa Mungu” (yaani *ruach*) ilikuwa nguvu iliyotimiza kusudi la YHWH, lakini kuna kidokezo kwamba alikuwa mtu binafsi (yaani Mungu mmoja, tazama Mada Maalumu: U-Mungu mmoja). Hata hivyo kwenye Agano Jipya ukamilifu wa nafsi ya ubinadamu na utu wa Roho umefunuliwa:

1. Anaweza kufanyiwa kufuru (kama vile Mt. 12:31; Marko 3:29)
2. Hufundisha (kama vile Luka 12:12; Yohana 14:26)
3. Hushuhudia (kama vile Yohana 15:26)
4. Ana hukumu, anaongoza (kama vile Yohana 16:7-15)
5. Anaitwa “ambaye" (yaani, *hos*, kama vile Efe 1:14)
6. Anaweza kuhuzunishwa (kama vile Efe. 4:30)
7. Anaweza kuzimishwa (kama vile 1 The. 5:19)
8. Anaweza kupingwa (kama vile Mdo. 7:51)
9. Anawatetea waaminio (kama vile Yohana 14:26; 15:26; 16:7)

10. Humtukuza Mwana (kama vile Yohana 16:14)

Maandiko ya utatu (hapa yapo matatu mioongoni mwa mengi, tazama Mada Maalumu: Utatu) pia anazungumza juu ya watu watatu.

1. Mt. 28:19
2. 2 Kor. 13:14
3. 1 Pet. 1:2

Ingawa neno la Kiyunani "roho" (*pneuma*) ni sio na jinsi wakati linapohusika Roho, Agano Jipya kila mara hutumia KIVUMISHI KIONYESHI CHA JINSIA YA KIKE (kama vile Yohana 16:8,13-14).

Roho anahusishwa na shughuli za binadamu.

1. Mdo. 15:28
2. Rum. 8:26
3. 1 Kor. 12:11
4. Efe. 4:30

Mwanzoni kabisa mwa matendo, jukumu la roho lina sisitizwa (kama katika injili ya Yohana). Pentekoste haikuwa mwanzo wa kazi ya Roho bali, sura mpya. Yesu kila wakati alikuwa na Roho. Ubatizo wake haukuwa mwanzo wa kazi ya Roho bali mwanzo wa sura mpya. Roho ndio njia yenye nguvu ya makusudi ya Baba kwa sura yake (tazama Mada Maalumu: Mpango wa Ukombozi wa Milele wa YHWH)!

◙ **"hana msamaha milele"** maelezo haya lazima yatafsiriwe katika mwanga wa Marko 3:28.

◙ **" ila atakuwa ana dhambi ya milele "** huku ni kuikataa injili (yaani.,mtu na kazi ya Yesu) katka uwepo wa nuru kuu! kuna simulizi mbalimbali zinazoelezea tungo "dhambi ya milele." Baadhi ya maandiko ya kale ya Uyunani

1. yamebadilishwa kwenda tungo milikishi (yaani, *hamartias*) – C*, D, W
2. Yameongeza "hukumu" (yaani., *kriseōs*) – A na $C^2$ (kama vile KJV)
3. Yameongeza "mateso" (yaani., *kolaseōs*), ndogo sana 1234

Inashangaza waandishi wa mwanzoni kuongelea juu ya "dhambi ya milele."

Toleo la $UBS^4$ linatupatia "dhambi ya milele" daraja B (mara zote haina mashaka).

## MADA MAALUM : MILELE (*aiōnios*)

Robert B. Girdlestone, katika kitabu chake cha *Synonyms of the Old Testament*,, anayo maoni yenye kuvutia kuhusiana na neno "milele":

"Kivumishi aiōnios kinatumika zaidi ya mara arobaini katika Agano Jipya sambamba na maisha ya milele, ambayo yanachukuliwa kama sehemu ya thawabu iliyopo, kwa namna Fulani ni kama ahadi ya wakati ujao. Pia linatumika kuueleza uwepo wa Mungu wa milele katika Rum. 16.26; kwa thamani ya upatanisho wa Kristo wa milele katika Ebr. 9.12; 13.20; na enzi zilizopita katika Rum. 16.25; 2 Tim. 1.9; Tito 1.2. content

Hili neno linatumika sambamba na rejea ya moto wa milele, Mt. 18.8; 25.41; Yuda 1:7; adhabu ya milele, Mt. 25.46; hukumu ya milele au shitaka, Marko 3.29; Ebr. 6.2; maangamizi ya milele, 2 The. 1:9. Hili neno katika vifungu hivi linamaanisha hatima, na inavyoonekana linaashiria kwamba wakati hukumu hizi zitakapotekelezwa, wakati wa matazamio, mabadiliko, au nafasi ya kuirejesha bahati ya mtu, utakuwa umetimia kwa usahihi na milele daima. Yatupasa kuelewa kwa uchache sana kuhusu wakati ujao, kuhusu uhusiano wa maisha ya mwandamu na kuishi kwake kulikobaki, na kuhusu uzito wa mwenendo wa wale wasiamini, kama ilivyotazamwa katika nuru ya umilele. Ikiwa, kwa upande mwingine, ni kosa kuongeza kwenye neno la Mungu, kwa namna nyingine yatupasa kuliepuka kosa hili; na ikiwa tutafadhaishwa chini ya mafundisho yahusuyo adhabu ya milele kama ilivyokwisha wekwa kwenye maandiko, yatupasa turidhike na subira, tukijikita kwenye Injili ya upendo wa Mungu katika Kristo, huku tukitambua ya kuwa kuna mazingira ya kuwepo giza ambalo hatuwezi kulikabiri" (kr. 318-319).

**MADA MAALUM: Taratibu za Ufafanuzi wa kimaandiko katika kufasiri "Dhambi Isiyosameheka"**

Kumbuka kwamba Injili inaaksi mazingira ya Kiyahudi

1. Aina mbili za dhambi (angalia Mada Maalum: dhambi zisizo za kukusudia [Agano la Kale], kama vile Law. 4:2,22,27; 5:15,17-19; Hes. 15:27-31; Kumb. 1:43; 17:12-13)
   a. isiyo ya kukusudia
   b. ya kukusudia
2. Mazingira ya Kiyahudi kabla ya Upentekoste (yaani kutimilizwa kwa injili [yaani kifo, ufufuo, kupaa] na kipawa maalumu cha Roho bado hakijaja)

A. Tazama muktadha wa kifasihi wa Marko 3:22-30
   1. Kutoamini kwa familia yake mwenyewe Yesu (kama vile Marko 3:31-32)
   2. kutoamini kwa Mafarisayo (kama vile Marko 2:24; 3:1,6,22)

B. Linganisha ufanano wa Injili ambapo jina "Mwana wa Adamu" inabadilika kuwa "wana wa wanadamu"
   1. Mt. 12:22-37 (yaani, 12:32, "neno dhidi ya Mwana wa Adamu")
   2. Luka 11:14-26; 12:8-12 (yaani, 12:10, "neno dhidi ya Mwana wa Adamu")
   3. Marko 3:28 (yaani, "dhambi zoteza wana wa wanadamu zitasamehewa")

Dhambi isiyosameheka ni kukataliwa kunakoendelea kwa Yesu katika uwepo wa nuru kuu. Mafarisayo walielewa vizuri kwa usahihi lakini walikataa kuamini. Kwa namna hii inahusiana na kufanana na "dhambi mpaka mauti" katika 1 Yohana (Angalia Mada Maalum: Dhambi mpaka mauti).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 3:31-35**

***31*** **Wakaja mamaye na nduguze; wakasimama nje, wakatuma mtu kumwita.** ***32*** **Na makutano walikuwa wameketi, wakimzunguka, wakamwambia, Tazama, mama yako na ndugu zako wako nje, wanakutafuta.** ***33*** **Akawajibu, akisema, Mama yangu na ndugu zangu ni akina nani?** ***34*** **Akawatazama wale walioketi wakimzunguka pande zote, akasema, Tazama, mama yangu na ndugu zangu!** ***35*** **Kwa maana mtu ye yote atakayeyafanya mapenzi ya Mungu, huyo ndiye ndugu yangu, na umbu langu, na mama yangu.**

**3:31-35** Mistari hii inasimuliwa katika Marko 3:21. Kuna taswira ya wazi kati ya ujinga, lakini huruma, ya wasio kuwa na imani na familia ya Yesu (kama vile Yn. 7:5) na wakaidi, uadui wa viongozi wa kidini wasiokuwa na imani. Yesu kwa upekee zaidi anaelezea kwamba mapenzi ya Mungu ni kumtumaini Yeye (kama vile Yn 6:40; 14:6).

**3:33 "Mama yangu na ndugu zangu ni akina nani"** swali hili la kushangaza linaonyesha kujitambua kwa Yesu na misingi ya asili ya imani kibiblia kwamba anaweza kuelezewa kipekee katika maneno ya uzao mpya,familia mpya. maisha ya kifamilia yalikuwa ya muhimu sana katika sura ya maisha ya kiyahudi kwamba walitumia maneno ya familia kwa ajili ya ushirika wa muhimu wa waaminio. Waaminio wanaelezewa kama miungu kwa wanajumuia katika familia;Mungu ni Baba, Yesu ni mwana wa pekee na mwokozi ,lakini hata sisi pia ni watoto wa Mungu.

**3:35 "' Kwa maana mtu ye yote atakayeyafanya mapenzi ya Mungu '"** imani katika kristo ni mapenzi ya Mungu kwa ajili ya wanadamu wote (kama vile Yn. 1:12; 3:16; 6:40; 14:6; 1 Yn. 5:12,13). Tazama mada maalum: mapenzi ya Mungu katika 1 Pet. 2:15. Tambuwa kwa upana zaidi, ulimwengu unaitikia wito wa imani ya Yesu na ujumbe wake.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni <u>mwongozo</u> wa kujifunza wa fasiri inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyeweza Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Mjadala huu wa maswali unawekwa ili kukusaidia wewe kufikiri maana ya chapisho kupitia sehemu ya kitabu. Wanamaanisha kuchochea sio kumalizia.

1. Kwa nini mpangilio wa Luka ni tofauti na wa Marko? (Marko 3:22-30)
   ni masimulizi gani kutoka kwa Mathayo yameongezwa kwa Marko?
2. Kwa nini viongozi wa kidini walifanya mashitaka haya dhidi ya Yesu katika sura hii? Je wao walikuwa na ufahamu zaidi?
3. Kwa nini Yesu alijaribu kuangalia sababu na wao?
4. "dhambi isiyosamehewa" ni ipi?
5. Ni katika muktadha upi dhambi isiyoweza kusameheka inaweza kutubiwa leo? Je mmojawapo anaweza kuitubia?
6. Katika kifungu hiki dhambi isiyosameheka inasimuliwa katika 1 Yn. 5:16 au Ebr. 6 na 10?
7. Ni kwa namna gani dhambi hii inasimuliwa katika wokovu? Kwa namana gani dhambi hii inasimuliwa kwa wasioamini katika familia ya Yesu?
8. Ni kwa jinsi gani maneno ya kumtukana Yesu yanasameheka lakini sio kumkufuru Roho mtakatifu?
9. Tofauti yake ni nini (linganisha Mt. 12:31-32 na Luka 12:10 na Marko 3:28)?

# MARKO 4

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Mfano wa mpanzi<br>4:1-9 | Mfano wa mpanzi<br>4:1-9 | Kufundisha kwa mafunzo<br>4:1-9 | Mfano wa mpanzi<br>4:1-2<br>4:3-8<br>4:9 | Mfano wa mpanzi<br>4:1-9 |
| Kusudi la mifano Inayofamika<br>4:10-12 | Kusudi la mifano<br>4:10-12 | 4:10-12 | Kusudi la mifano<br>4:10-12 | Kwa nini Yesu aliongea kwa Mifano<br>4:10-12 |
| Ule mfano wa mpanzi Unaelezewa<br>4:13-20 | Ule mfano wa mpanzi unaelezewa<br>4:13-20 | 4:13-20 | Yesu anaelezea mfano wa mpanzi<br>4:13-20 | Ule mfano wa mpanzi Unaelezewa<br>4:13-20 |
| Taa chini ya pishi<br>4:21-23 | Taa chini mvunguni<br>4:21-25 | 4:21-25 | Taa chini ya kiango<br>4:21-23 | Kuyapokea na Kuyashika Mafundisho ya Yesu<br>4:21-23 |
| 4:24-25 | | | 4:24-25 | Mifano ya vipimo<br>4:24-25 |
| Mfano wa mbegu<br>4:26-29 | Mfano wa mbegu<br>4:26-29 | Mbegu ichipukayo Kwa siri<br>4:26-29 | Mfano wa mbegu<br>4:26-29 | Mifano ya mbegu ikuwayo yenyewe<br>4:26-29 |
| Mfano wa mbegu Ya haradari<br>4:30-32 | Mfano wa mbegu ya haradari<br>4:30-32 | Mbegu ya haradari<br>4:30-32 | Mfano wa mbegu ya haradari<br>4:30-32 | Mfano wa mbegu ya haradari<br>4:30-32 |
| Utumiaji wa mifano<br>4:33-34 | Matumizi ya mifano Ya Yesu<br>4:33-34 | 4:33-34 | 4:33-34 | Utumiaji wa mifano<br>4:33-34 |
| Kuituliza dhoruba<br>4:35-41 | Upepo na mawimbi vinatii<br>4:35-41 | Upepo na bahari vinatulia<br>4:35-41 | Yesu anatuliza dhoruba<br>4:35-38<br>4:39-40<br>4:41 | Kuituliza dhoruba<br>4:35-41 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka "Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Sura mbali mbali zinazofuata katika kitabu cha Marko zinaaksi ukuaji wa upinzani wa viongozi wa kidini. Marko anaonyesha tofauti kati ya kujulikana kwa Yesu mbele za watu na kutojulikana kwake kwenye uongozi wa kidini.

B. Yesu aliamua kuondoka toka kwenye mahubiri ya kwenye masinagogi hadi mikutano ya wazi. Hii ilikuwa mojawapo ya kupunguza nguvu ya uongozi wa kidini na kutoa nafasi ya umati wa watu kuweza kusikia neno lake.

C. Kuielewa mifano ilikuwa na ilihusiana na ahadi ya imani ya mwanzo. Hata Mitume mwanzoni hawakuweza kufahamu mafundisho ya kimafumbo ya Yesu. Kwa namna nyingine kuyaelewa mafundisho kulitegemea juu ya
   1. Uchaguzi
   2. Kuangaziwa na nguvu ya Roho
   3. Utashi wa kutubu na kuamini

   Uelewa unajumuisha uwezesho wa Kiungu na mwitikio wa imani ya mwanadamu!

D. Neno "mifano" ni neno la pamoja katika Kiyunani lenye kumaanisha "kutupa pamoja na." Utokeaji wa kawaida ulitumika kuelezea ukweli wa kiroho. Ingawa sharti ikumbukwe kuwa kwa waandishi wa injili hili neno la Kiyunani liliaksi neno la Kiebrania *mashal* (BDB 605), lenye kumaanisha "kitendawili" au "mithali," neno la hekima. Lazima mtu apende kufikiri tena kuhusu masuala na kutarajia matokeo katika mtizamo wa kushangaza wa asili ya ufalme wa Mungu ambao sasa upo ndani ya Yesu. Kwa baadhi ya wale waliosikia mifano walificha ukweli (kama vile Marko 4:10-12).

E. Mifano ya Marko 4 inafanana na ile ya Mathayo na Luka

| Marko | Mathayo | Luka |
|---|---|---|
| Mifano minne ya udongo 4:3-20 | | |
| Taa iliyoficha | 13:3-23 | 8:5-15 |
| 4:21-25 | | |
| Mbegu zenye kumea na kukua | | 8:16-18 |
| 4:26-29 | | |
| Mbegu ya haradari | | |
| 4:30-32 | 13:31-32 | |
| Utumiaji wa mifano | | |
| 4:33-34 | 13:33-35 | |
| (kama vile Marko 4:10-12) | | |

F. Mifano ya kwenye udongo au mfano wa mpanzi ambayo hupatikana katika injili zote, ni aina ya ufasiri yenye kuleta suluhisho kwa wengine. Yesu alichukua muda kuielezea mifano kwa wanafunzi. Hata mpaka hapo hawakuielewa, ni nafasi gani wengine waliweza kuipata? Hii mifano ina dhana ya kiuainishi na/au kiistiari, ambayo yapaswa kutambuliwa au maana ya kusudio imepotea

G. Marko 4:21-25 imerudiwa katika Mathayo kwa muktadha tofauti:
Marko 4:21 – Mathayo 5:15
Marko 4:22 – Mathayo 10:26
Marko 4:24 – Mathayo 7:2
Marko 4:25 – Mathayo 13:12; 25:29
Panaweza pakawepo na maelezo aina mbili
1. Yesu alirudia na kuyatumia tena mafundisho yake na mifano kwa makundi tofauti na wakati tofauti
2. Waandishi wa injili wanachagua, wanapanga, na kuendana na maneno ya Yesu kwa ajili ya fasihi yao wenyewe na makusudi ya kithiolojia (kama vile *How to Read the Bible for All Its Worth* na Gordon Fee and Doug Stuart, kur. 113-134).

H. Marko anaweka kumbukumbu ya mtiririko wa miujiza ambayo hudhihirisha nguvu ya Yesu na mamlaka katika Marko 4:35-8:26. Miujiza ilimaanisha kuthibitisha ukweli wa mafundisho mapya yaliyo muhimu ya Yesu. Alijifanya mwenyewe kuwa mada ya kujadiliwa

## MADA MAALUM:UFASIRI WA MIFANO

Madokezo ya injili yaliandikwa miaka mingi baada ya maisha ya Yesu. Wandishi wa injili (kwa kusaidiwa na Roho) kimaadili walijizoeza kwenye fasihi simulizi. Walimu wa sheria walifundisha kwa mpangalio wa simulizi. Yesu aliiga huu utaratibu wa simulizi kwenye mafundisho. Kwa ufahamu wetu kamwe hakuandika mafundisho au hotuba zake. Kuongezea katika kumbukumbu, uwasilishaji wa mafundisho ulikuwa wa kujirudia,kufupishwa, na kuelezewa kwa mifano. Wandishi wa injili walizitunza hizi kumbukumbu. Mifano, iliyokuwa migumu kuielezea, ni moja ya hizi mbinu.

"Mifano kwa uzuri zimeelezewa kama hadithi zenye kuwa na maana mbili zinazolingana; kiwango cha habari hutoa taswira ambapo ukweli hudhaniwa na kueleweka," *Dictionary of Jesus and the Gospels,* (uk. 594).
"mfano ni msemo au hadithi ambayo hutafuta kupeleka hoja ambayo mnenaji hupenda kuisisitizia kwa kuielezea kwa mifano kwenye mazingira ya maisha ya kawaida," *The Zondervan Pictorial Bible Encyclopedia* (uk. 590).
Ni vigumu kuelezea kiusahihi ni nini kilichoeleweka kwa neno "mifano" katika siku za Yesu
1. Baadhi wanasema liliaksi neno l;a Kiebrania *mashal* ambalo lilimaanisha kitendawili cha aina yeyote (Marko 3:23), msemo wa kiujanja (Mithali, Luka 4:23), miseemo mifupi (Marko 7:15), msemo wa kimafumbo ("msemo usioeleweka").
2. Wengine wanashikilia zaidi kwenye maelezo yasio kamili ya hadithi fupi.

Kulingana na kila mtu anavyojaribu kulielezea neno, zaidi ya theruthi moja ya mafundisho ya Yesu yaliyoandikwa yako katika muundo wa mafumbo. Huu ulikuwa ni uwasilishaji mkuu wa fasihi ya Agano Jipya. Hakika mifano ya Yesu ilikuwa ni ya ukweli. Ikiwa mtu atakubaliana na maelezo ya pili, bado pana aina nyingine mbalimbali ya hadithi fupi fupi:
1. hadithi rahisi za kueleweka (Luka 13:6-9)
2. hadithi ngumu zisizoeleweka (Luka 15:11-32)
3. hadithi kinzani (Luka 16:1-8; 18:1-8)
4. za uainishaji/kiistiari (Mt. 13:24-30, 47-50; Luka 8:4-8, 11-15; 10:25-37; 14:16-24; 20:9-19; Yohana. 10; 15:1-8)

Katika kushughulika na suala hili la aina ya mafumbo mtu lazima atafasiri misemo hii kwa hoja mbalimbali. Hoja ya kwanza ingalikuwa ni kanuni za ufasiri wa pamoja zenye kutumika kote kwenye uwasilishaji wa kibiblia. Baadhi ya miongozo:
1. kutambua kusudi la kitabu kizima au kwa kiasi Fulani sehemu ya fasihi

2. kuwatambua wasikilizaji wa mwanzo. Ni muhimu kuwa mara nyingi mfano wa aina ile ile unatolewa kwenye makundi tofauti, mfano:
    a. kondoo aliyepotea katika Luka 15 uliowalenga wenye dhambi
    b. kondoo aliyepotea katika Mt. 18 uliolenga kwenye kanuni
3. uwe na uhakika wa kuandika kwa uharaka muktadha wa huo mfano. Mara nyingi Yesu au wandishi wa injili huzungumzia hoja kuu (mara nyingi mwishoni mwa mfano au haraka baada ya kuuzema).
4. kuelezea kiini cha kusudi la mfano katika sentensi yenye habari moja. Mifano huwa na wahusika wawili au watatu. Mara nyingi ni ukweli uliodokezwa, kusudi, au hoja (mpango) kwa kila mhusika (Luka 15:11-22 ina wahusika 3 lakini sio mfano wa msamaria Mwema, Luka 10:25-37).
5. angalia sura zinazofanana katika injili zingine, baadaye tena viatabu vingine vya Agano Jipya na Agano la Kale

Hatua nyingine ya kanuni za utafasiri ni zile zenye kuhusiana hasa na suala la kimafumbo

1. Soma (usikilize ikiwezekana) mfano tena na teana. Hizi zilitolewa kwa ulazima wa kusimuliwa, na sio uchunguzi ulioandikwa.
2. Mingi ya mifano ina kweli kuu moja ambacho huhusiana na muktadha wa kihistoria na kifasihi wa wote Yesu na/ au wainjilisti.
3. Uwe mwangalifu kuyatafasiri maelezo. Mara nyingi huwa tu ni sehemu ya mazingira ya hadithi.
4. Kumbuka kuwa mifano sio kweli yenyewe. Ni mfanano wa maisha halisi, lakini mara nyingi wenye kukuzwa, ili kulazimisha hoja (ukweli).
5. Tambua hoja kuu ya hadhithi ambayo umati wa Wayahudi wa karne ya kwanza wangaliweza kuitambua (Kenneth E. Bailey, *Jesus Through Middle Eastern Eyes*). Baadaye angalia angalia mpindisho wa hadithi au mshangao. Mara nyingi huja mwishoni mwa hadithi (kama vile A. Berkeley Mickelsen, *Interpreting the Bible*, kur. 221-224).
6. mifano yote ilitolewa ili kupata mwitikio. Mwitikio huo mara nyingi ulihusiana na dhana ya "ufalme wa Mungu." Yesu ndiye mwanzilishi wa ufalme mpya wa Kimasihi (Mt. 21:31; Luka 17:21). Wale wote waliomsikia lazima wajongee kwake sasa!

Ufalme pia ulihusu mambo yajayo (Mathayo25). Hatma ya mbele ya mtu ilitegemea namna alivyojongea kwa Yesu kwa wakati. Mifano ya ufalme ilielezea ufalme mpya uliojiri ndani ya Yesu. Waliielezea kwa hitaji la kimaadili na maana kuu ya uanafunzi. Hakuna chochote chawezakuwa kama kilivyokuwa. Kwa umuhimu yote ni mapya na yanamlenga Yesu!

7. Mifano mara nyingi haielezei hoja au kiini cha ukweli. Mfasiri sharti atafute majibu ya kimuktadha yanayodhihilisha kweli kuu halisi yenye kufundisha kwa wapokeaji wa mwanzo lakini sasa ambayo ni tata kwetu.

Hoja ya tatu ambayo mara nyingi ni yenye mkanganyiko ni ile yenye kuwa na uficho wa ukweli wa kimafumbo. Yesu mara nyingi alizungumza mifano yenye hali isioeleweka (kama vile. Mt. 13:9-15; Marko 4:9-13; Luko 8:8-10; Yohana. 10:6; 16:25). Hili lilihusiana na unabii katika Isa. 6:9-10. Moyo wa wasikiaji unaamua kiwango cha uelewa (kama vile Mt. 11:15; 13:9,15,16,43; Marko 4:9,23,33-34; 7:16; 8:18; Luka 8:8; 9:44; 14:35).

Hata hivyo, lazima ielezewe kuwa uati wa watu (Mt. 15:10; Marko 7:14) na Mafarisayo (Mt. 21:45; Marko 12:12; Luka 20:19) walielewa kile Yesu alichokuwa akizungumza lakini wakakataa kuitikia kiusahihi kwa imani na toba. Kwa maana moja huu ndio ukweli wa mfano wa udongo (Mathayo 13; Marko 4; Luka 8). Mifano ilikuwa na maana ya kudhihilisha ukweli (Mt. 13:16-17; 16:12; 17:13; Luka 8:10; 10:23-24).

Grant Osborne, katika kitabu chake cha *Hermeneutical Spiral,* uk. 239, analeta hoja kuwa "mifano ni chombo chenye kuleta mkabala na hufanya kazi tofauti kutegemeana na wasikilizaji...kila kundi (viongozi, umati wa watu, wanafunzi) linakabiliwa kitofauti na mifano." Mara nyingi wanafunzi hawakuielewa mifano au mafundisho Yake (kama vile Mt. 15:16; Marko 6:52; 8:17-18,21; 9:32; Luka 9:45; 18:34; Yohana. 12:16).

Hoja ya nne pia ni yenye mkanganyiko. Inashughulika na kweli kuu ya mifano. Wengi wa watafasiri wa sasa wametenda ufasiri wa mifano kiistiari. Istiari ilibadili maelezo ya muundo wa ukweli kuwa wenye kufafanuliwa kiundani. Njia hii ya utafasiri hailengi kwenye muundo wa kihistoria, muundo wa kifasihi, au kusudi la kiuandishi, bali

kuwasilisha mawazo ya mfasiri, na sio andiko.
Hata hivyo, lazima ikubalike kuwa mifano ambayo Yesu aliitafasiri iko karibu na ile ya kiistiari au uainishaji. Yesu alitumia maelezo kuupeleka ujumbe (mpanzi, Mathayo 13; Marko 4; Luka 8 na watumwa waovu, Mathayo 21; Marko 12, Luka 20).
Baadhi ya mifano mingine ina kweli kuu mbalimbali. Mfano mzuri ni ule wa Mwana Mpendwa wa pekee (Luka 15:11-32). Sio tu upendo wa Baba na uasi wa mwana lakini ni mwenendo wa kijana mkubwa ambaye ndiye kiini cha maana kamili ya mfano.

Nukuu ya kukusaidia ni kutoka *Linguistics and Biblical Interpretation* by Peter Cotterell na Max Turner:

"Alikuwa ni Adulf Julicher zaidi ya wengine ambaye alielekeza usomaji wa Agano Jipya dhidi ya jaribio lenye maamuzi kuelewa wajibu wa mfano katika mafundisho ya Yesu. Umuhimu wa kuiweka kiistiari mifano iliachwa na utafiti ukaanza kwa ajili ya suluhisho lenye kutuwezesha kupenye kwenye maana ya kweli yao. Lakini kama Yeremia alivyoweka sawa, 'bidii zake za kuiweka huru mifano toka kwenye utafasiri usioaminika na usio na mantiki wa kila maelezo ulimsababishia kuangukia kwenye makosa makubwa.' Kosa lilikuwa ni lenye kusisitiza na sio tu huo mfano uweze eleweka kama wenye kupeleka wazo moja, bali kuwa wazo liweze kuwa la pamoja" (uk. 308).

Nukuu nyingine inayoweza kukusaidia *The Hermeneutical Spiral* by Grant Osborne:

"Mpaka sasa nimeweza kutambua viashilia vingi kuwa mifano hakika ni istiari, ingawa inadhibitiwa na kusudio la mwandishi. Blomberg (1990) kiukweli hakubaliani kuwa kuna hoja nyingi kama ilivyo wahusika katika mifano na hakika ni istiari. Wakati hili kwa kiasi Fulani limekuzwa, liko karibu na ukweli kuliko mkabiliano wa 'hoja moja'" (uk. 240).

Je mifano inapaswa kutumika kufundisha kweli ya maandiko au kuiangaza kweli ya maandiko? Wengi wa watafasiri wameweza kushawishiwa na utumiaji mbaya wa njia za kiistiari za kuitafasiri mifano iliyowaruhusu kuitumia kuanzisha mafundisho yasiyo na uhusiano na kusudi la mwanzo la Yesu wala lile la mwandishi wa injili. Maana lazima iendane na kusudio la uandishi. Yesu na wandishi wa injili walikuwa katika hali ya uvuvio, lakini wafasiri sio. Hata hivyo, mifano imetumika vibaya nab ado inafanya kazi kama chombo cha kufundishia ukweli, ukweli wa kimafundisho. Msikilize Bernard Ramm juu ya hoja yake.

"Mifano haifundishi mafundisho na madai ya kuwa isitumike kabisa katika uandishi wa kimafundisho sio sahihi. . .lazima tuangalie matokeo kwa uwazi, mafundisho dhahili ya Bwana wetu , nay ale ya Agano Jipya yaliyobaki. Mifano yenye maangalizo sahihi yaweza kutumika kuelezea kwa mifano mafundisho, kuangaza maarifa ya Kikristo na kufundishia masomo kwa vitendo." *Protestant Biblical Interpretation* (uk. 285).
Katika kuhitimisha ngoja nitoe nukuu tatu ambazo zinaaksi maonyo kwenye utafasiri wa mifano:

1. Zilizochukuliwa toka *How to Read the Bible For All Its Worth* by Gordon Fee and Doug Stuart,

"Mifano zimepatwa na matokeo ya kutotafasiriwa kiusahihi katika nafasi ya pili ndani ya kanisa baada ya ufunuo" (uk. 135).

2. Ikichukuliwa toka *Understanding and Applying the Bible* by J. Robertson McQuilkin,

"Mifano imekuwa ni chanzo cha baraka zisizo ambilika katika kuwafumbua watu wa Mungu kuhusu ukweli wa kiroho. Kwa wakati ule ule, mifano imekuwa chanzo cha machafuko yasioambilika katika yote mafundisho na utendaji ndani ya kanisa" (uk. 164).

3. Ikichukuliwa toka T*he Hermeneutical Spiral* by Grant Osborne,

"Mifano imekuwa kati ya maandiko yaliyoandikwa sana lakini mpaka sasa kikanuni za ufasri yametumia vibaya kwenye sehemu za maandiko. . .utendaji wake bado ni mgumu kueleweka kwenye uwasilishaji wa kibiblia. Umuhimu wa mifano kwa ajili ya mawasiliano ni mkubwa, pale ambapo huleta ulinganifu au msingi wa hadithi juu ya kila maarifa ya kila siku. Hata hivyo, hadithi yenyewe ina uwezo wa kuwa na maana nyingi, na wasomaji wa sasa wanapata shida ya kuitafasiri kama walivyokuwa wasikilizaji wa kale" (uk. 235).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 4:1-9**
**1 Akaanza kufundisha tena kando ya bahari. Wakamkusanyikia mkutano mkubwa mno, hata yeye akapanda chomboni, akakaa baharini, mkutano wote ulikuwako juu ya nchi kavu kando ya bahari. 2 Akawafundisha mambo mengi kwa mifano, akawaambia katika mafundisho yake, 3 Sikilizeni; Tazama, mpanzi alitoka kwenda kupanda; 4 ikawa alipokuwa akipanda, mbegu nyingine ilianguka kando ya njia, wakaja ndege wakaila. 5 Nyingine ikaanguka penye mwamba, pasipokuwa na udongo mwingi; mara ikaota kwa kuwa na udongo haba; 6 hata jua lilipozuka iliungua, na kwa kuwa haina mizizi ikanyauka. 7 Nyingine ikaanguka penye miiba; ile miiba ikamea ikaisonga, isizae matunda. 8 Nyingine zikaanguka penye udongo ulio mzuri, zikazaa matunda, zikimea na kukua, na kuzaa, moja thelathini, moja sitini, na moja mia. 9 Akasema, Aliye na masikio ya kusikilia, na asikie.**

**4:1 "Akaanza tena kufundisha kando ya bahari"** Hiki hakikuwa kitu kipya (kama vile Marko 2:13; 3:7) lakini sasa ni kwamba masuala ya sinagogi yakajakuwa yakiongezeka karibu naye, akaendelea na huduma ya mafundisho sehemu za wazi. Yesu alihitaji watu wa kawaida kuweza kuwa naye karibu na mafundisho yake

◙ **"wakamkusanyikia mkutano mkubwa mno"** Palikuwepo na umati mkubwa wa watu, lakini ile mifano inaonyesha kuwa wachache waliitikia. Uwepo wa kusanyiko kubwa ni mada inayojirudia katika Marko (kama vile Marko 2:13; 3:9; 4:1,36; 5:31; 7:33; 8:1,2; 9:14,17; 14:43; 15:8).

◙ **"akapanda chomboni"** Hili neno la Kiyunani linarejerea mashua. Katika Marko 3:9 Yesu akaulizia mashua zingine za kuweza kusubilia iwapo kusanyiko la watu litakuwa kubwa. Baadaye lingalikuwa ni jukwaa la kuhubiria. Kila aliyekuwa mgonjwa alitaka kumgusa. Ni msongamano wa aina gani alitaka kuusababisha.

◙ **"akakaa"** Mtu atashangaa ikiwa kukaa kwa Yesu (yaani., dhidi ya kusimama) kungeaksi aina ya kitamaduni ya walimu wa Kiyahudi (yaani., walimu wa dini ya Kiyahudi walikaa pindi walipofundisha) au ikiwa hili lilisababishwa na myumbo wa mashua.

◙**"juu ya nchi kavu"** Yesu angeweza kutumia ongezeko la sauti asili ya maji kuweza kuongea na umati mkubwa wa watu.

**4:2 "akawafundishwa"** Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati usio timilifu ikimaanisha akawafundisha tena na tena (yaani., "mambo mengi").

◙ **"mifano"** Angalia Mada Maaalum: Kuitafasiri Mifano katika Marko 4.

**4:3 "'Sikilizeni hili'"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Kumbuka, mifano ilitolewa kwa kusimuliwa. Walimu wa dini ya Kiyahudi wangalifundisha, alafu wakafupisha, alafu wakaionyesha. Yesu alifuata utaratibu huu (kama vile William L. Blevins' *Birth of a NewTestament*, kur. 1-13).

◙ **"mpanzi"** Huu ulikuwa ni mtizamo wa kawaida huko Galilaya. Huu mfano ulileta maana kubwa pale mtu alipotambua ni namna gani hawa wakulima walivyoilima ardhi yote iliyozunguka vijiji vyao. Hii mifeleji ilikatiza njia. Baadaye waliweza kupanda shamba lote kwa mikono. Yesu alitumia huu utendaji wa kawaida kuweza kuelezea upokeaji wa kiroho (yaani., aina nne za udongo).

**4:4 "kando ya barabara"** Hii inarejerea njia ya watu wote ipitayo kwenye mashamba ya vijiji. Pindi mashamba haya yalipolimwa njia hizi zilipotea lakini kwa haraka waliweza kuzirejeza kwa ajili ya kuzitumia.

**4:5 "penye mwamba"** Hili linarejerea kwenye uwepo wa mwanzo, uliopo chini ukiwa na kiasi Fulani cha udongo juu yake, na sio miamba ya kumomonyoka. kina cha udongo hakikufahamika machoni pa watazamaji.

**4:7 "penye miba"** Hili linarejerea kwenye eneo la miiba lililoandaliwa vizuri kiasi kwamba haikuweza kuonekana baada ya kulimwa.

**4:8 " zikazaa matunda, zikimea na kukua, na kuzaa, moja thelathini, moja sitini, na moja mia"** Aina tofauti za udongo na eneo ziliwezesha kupatikana mazao mengi. Kuna machapisho mbalimbali yanayohusiana na kihusishi *en*. Hata hivyo, tofauti ya aina ya machapisho ya Kiyunani kiukweli hayabadili maana ya andiko. Yumkini yote matatu yanapaswa kuwa *en*, ambayo yangelifuatisha ushawishi wa lugha ya Kiarama

**4:9, 23 "'Mwenye masikio, na asikie'"** Hii ni nahau ya Kisemiti. Inaonyesha hitaji la kuwa mwangalifu kifikra na matumizi yake binafsi (kama vile Mt. 11:15; 13:9,43; Luka 8:8; 14:35; Ufu. 2:7,11,17,29; 3:6,13,22;13:9). Hili yumkini linaaksi maombi ya Kiebrania, neno *Shema* (kama vile Kumb. 6:4), lenye kumaanisha "kusikia ili kutenda." Kusikia lazima kusababishe kitendo (kama vile Yakobo 2:14-26).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 4:10-12**
**10 Naye alipokuwa peke yake, wale watu waliomzunguka, na wale Thenashara, walimwuliza habari za ile mifano. 11 Akawaambia, Ninyi mmejaliwa kuijua siri ya ufalme wa Mungu, bali kwa wale walio nje yote hufanywa kwa mifano,**
**12 ili wakitazama watazame, wasione; Na wakisikia wasikie, wasielewe; Wasije wakaongoka, na kusamehewa.**

**4:10 "Naye alipokuwa peke yake"** Hili linamaanisha kujitenga na wanafunzi wake. Inavyoonekana hawakufurahia kuuliza maswali kwenye hadhira ya watu. Dhahiri inaonyesha hawakuielewa mifano.

**4:11 "'Ninyi mmejaliwa'"** Hii ni kauli tendwa timilifu elekezi. Sisi ni watumishi wenye kuwajibika juu ya kweli za kiroho tulizonazo. " Na kila aliyepewa vingi, kwake huyo vitatakwa vingi" (kama vile Luka 12:48). Haya mafundisho ya faragha, ambayo yanaonekana kuwepo mara kwa mara, yaweza kuelezea tofauti kati ya vidokezo vya injili na injili ya Yohana. Yesu alizungumza kitofauti katika Yohana. Yawezekana kuwa ni mafundisho ya kimafumbo, ambayo ni ya kawaida katika mihitasari ya injili, iliyofanyika mbele za umati wa watu na kuwa ya aina tofauti kabisa (yaani., maelezo ya"Mimi ndiye") yalifanyika faragha akiwa na wanafunzi na hiki ndicho injili ya Yohana ilikiandika. Yawezekana kuwa hili suala zima la maelekezo maalum kwa ajili ya wale kumi na wawili lingeweza kutenda kwenye kanisa la mwanzo kama njia ya kusisitiza mamlaka ya Kitume. Wao, na yeye, waliifahamu kuitafasiri "kweli" ya maneno ya Yesu. Mafunuo yote huja kupitia wanafunzi hawa waliochaguliwa na kuvuviwa.

◙ **"'siri'"** Hili ni neno la Kiyunani *mustērion*. Limetumika katika Agano Jipya katika maana mbalimbali tofauti. Katika muktadha huu linafunua kweli ambayo viongozi nz umati wa watu walishindwa kuuelewa (kama vile Isa. 6:9-10).

## MADA MAALUM: SIRI KATIKA INJILI

A. Katika vidokezo vya injili "muujiza" unatumika kwenye mitizamo ya kiroho iliyokusanywa toka kwenye mifano ya Yesu.
   1. Marko 4:11
   2. Mathayo 13:11
   3. Luka 8:10

B. Paulo anaitumia kwa namna tofauti mbalimbali.
   1. Kusita kwa Israeli kuwaruhusu watu wa mataifa ili kujumuishwa. Uvamizi huu wa watu wa mataifa utatenda kazi kama chombo kwa ajili ya Wayahudi kumkubali Kristo Yule wa unabii (kama vile Rum. 11:25-32).
   2. Injili ilijulikana kwa mataifa, ikisema kuwa wote wamejumuishwa katika Kristo na kupitia Kristo (kama vile Rum. 16:25-27; Kol. 2:2).
   3. Miili mipya ya waamini kwenye ujio wa mara ya pili (kama vile 1 Kor. 15:5-57; 1 The. 4:13-18).

4. Kuhitimisha mambo yote katika Kristo (kama vile Efe. 1:8-11).
5. Wamataifa na Wayahudi kama warithi wenza (kama vile Efe. 2:11-3:13).
6. Ushirika wa ndani kati ya Kristo na kanisa ulioelezewa kwa namna ya maneno ya ndoa (kama vile Efe. 5:22-33).
7. Wamataifa wakajumuishwa ndani ya watu wa agano na Roho wa Kristo kuishi ndani yao ili kuleta ukomavu unaomfanana Kristo, yaani, kurejesha taswira ya Mungu iliyoharibika ndani ya mwanadamu (kama vile Mwa. 1:26-27; 5:1; 6:5,11-13; 8:21; 9:6; Kol. 1:26-28).
8. Mpinga Kristo wa siku ya mwisho (kama vile 2 The. 2:1-11).
9. Wimbo wa kanisa la mwanzo kuhusu muujiza wa injili unaopatikana katika 1 Tim. 3:16.

C. Katika ufunuo wa Yohana unatumika kumaanisha alama za Yohana za matukio ya siku ya mwisho.
1. 1:20
2. 10:7
3. 17:5,6

Hizi ni kweli ambazo mwanadamu hawezi kuzigundua; lazima zifunuliwe na Mungu. Hii mitizamo ni ya muhimu kwa ajili ya uelewa wa kweli wa mpango wa Mungu wa milele kwa ajili ya ukombozi wa watu wote (kama vile Mwa. 3:15). Angalia MADA MAALUM: MPANGO WA YHWH WA UKOMBOZI WA MILELE

◙ **"ufalme wa Mungu"** Angalia kumbukumbu katika Marko 1:15.

◙**"bali kwa ale walio nje"** Roho Mtakatifu na upokeaji binafsi vyote vinahitajika ili kuielewa kweli ya kiroho. Wale wote wanaomkataa Roho hutenda dhambi iliyoandikwa katika Marko 3:29. Mifano ilikuwa makusudi mawili ya kuuficha ukweli (kama vile Mt. 11:25-27) na uwazi kuudhihilisha ukweli (kama vile Luka 10:29 na mifano inayofuata). Moyo wa wale wenye kusikia ndiyo suluhisho.

**4:12** Rejeo hili linatoka kwenye toleo la Kiaramu la Targum la Isa. 6:9. Ufanano wa ukoo wa Mathayo toka kwenye tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania yananukuu zote Isa. 6:9 na 10. Mahubiri ya Isaya yalikataliwa na waisareli wenye vichwa vigumu aliowahubiri kwenye karne ya nane k.k. waliomsikiliza Yesu katika karne b.k vile vile waliyakataa mafundisho yake. Vitenzi tegemezi vinamiliki nukuu hii, ambapo vinaonyesha tukio la hiari juu ya sehemu ya wasikilizaji. Ingawa Marko anaandika kwa watu wa mataifa, yumkini Warumi, mara nyingi alidokeza kwenye maandiko ya Agano la Kale (kama vile Marko 1:2-3; 2:25-26; 4:12; 10:6-8,19; 12:26,29-31,36).

◙ **"wasije wakaongoka"** Hili lilikuwa neno la Agano la Kale (yaani., *shub*, BDB 996) kwa ajili ya toba.

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA) MARKO 4:13-20**
**[13] Akawaambia, Hamjui mfano huu? Basi mifano yote mtaitambuaje? [14] Mpanzi huyo hulipanda neno. [15] Hawa ndio walio kando ya njia lipandwapo neno; nao, wakiisha kusikia, mara huja Shetani, akaliondoa lile neno lililopandwa mioyoni mwao. [16] Kadhalika na hawa ndio wapandwao penye miamba, ambao kwamba wakiisha kulisikia lile neno, mara hulipokea kwa furaha; [17] ila hawana mizizi ndani yao, bali hudumu muda mchache; kisha ikitokea dhiki au udhia kwa ajili ya lile neno, mara hujikwaa. [18] Na hawa ndio wale wapandwao penye miiba; ni watu walisikiao lile neno, [19] na shughuli za dunia, na udanganyifu wa mali, na tamaa za mambo mengine zikiingia, hulisonga lile neno, likawa halizai. [20] Na hawa ndio waliopandwa penye udongo ulio mzuri; ni watu walisikiao lile neno na kulipokea, na kuzaa matunda, mmoja thelathini, mmoja sitini, na mmoja mia.**

**4:13 "'Hamjui mfano huu? Basi mifano yote mtaitambuaje'"** Maelezo haya ni ya kipekee kwa Marko, lakini inaonyesha kuwa Yesu alitarajia wanafunzi kuielewa. Familia yake haikuelewa, bila umakini na maelezo ya kina, wasingelifahamu. Mfano huu ni kielelezo kwa ajili ya wengine. Hapa pana kanuni mbalimbali muhimu kwa ajili ya kuitafasiri mifano:
1. jaribu kukumbuka muktadha wa kihistoria na kifasihi
2. tambua kiini cha ukweli
3. Usiyapuuzie maelezo

4. angalia ufanano wa injili
5. angalia mpinduo usitarajiwa au maelezo ya kushangaza ambayo yatakuwa ndio mwito wa kitendo chenye kusimamia juu ya ufalme mpya wa kimaadili

**4:14** Hizi mbegu zinarejerea kwenye tangazo la injili. Mfano wa Mathayo (kama vile Marko 13:19) huiita "neno la ufalme."

**4:15 "Shetani"** Huu unyang'anyi wa ile kweli umeelezewa kiusahihi katika 2 Kor. 4:4. Mfano wa Mathayo (kama vile Mt.13:19) unaongeza kuwa "hawajui," baadaye huja shetani na kuliondoa lile neno mioyoni mwao ili wasije wakalitafakari tena. Angalia Mada Maalum katika Marko 1:13.

◙**"huliondoa"** Hili neno la Kiyunani *airō* laweza kumaanisha (1) kuangamiza (kama vile Yohana 11:48) au (2) kuondoa uhai wa mtu (kama vile Luka 23:18; Mdo. 12:19); pasipo neno, hakuna maisha!

**4:16 "wakisha kulisikia neno, mara hulipokea kwa furaha"** Ukubalifu wa mwanzo wa ile kweli sio sababu pekee (kama vile Marko 4:17 na 19). Imani ya Kibiblia haiangalii maamuzi yaliyopita, bali ni katika ushirika wenye kukua. Wokovu sio sera ya bima ya moto au tiketi ya mbinguni, bali ni urejesho wa "taswira ya Mungu," wenye kuruhusu ushirika wa karibu na Mungu. Kumea vizuri sio mbadala wenye mahusiano ya kuzaa matunda mengi (kama vile Marko 4:20).

**4:17 "ila hawana mizizi ndani yao"** Hii mifano hutumiwa na Yohana kwenye kuamini katika Marko 8:30 na kuendelea.

◙**"ikitokea dhiki au udhia"** Ustahimilifu ni ushuhuda wa imani ya kweli.

## MADA MAALUM: HITAJI LA USTAHIMILIVU

Mafundisho ya Kibiblia yenye kuhusiana na maisha ya Kikristo ni magumu kuyaelezea kwa sababu yanawasilishwa katika jozi halisi ya upembuzi wa kimashariki (angalia Mada Maalum: Fasihi ya Mashariki [mafumbo ya Kibiblia]). Jozi hizi zinakinzana, ingawa bado zote ni za Kibiblia. Wakristo wa Kimagharibi yamejaribu kuchagua ukweli mmoja na kuachana na ukweli wa pili. Ngoja nielezee kwa mifano.

A. je wokovu ni maamuzi ya mwanzo kumwamini Kristo au ni kuyatoa maisha yako yote kwenye uanafunzi?
B. je wokovu ni uchaguzi kwa neema itokayo kwa Mungu Mkuu au kuamini kwa mwanadamu na mwitikio wa toba kwenye ahadi ya Kiungu?
C. je wokovu, mara unapoupata, ni vigumu kuupoteza, au kunahitajika kwa ajili ya kuongeza jitihada?

Suala la ustahimilivu limekuwa lenye mkanganyo kwa muda wote wa historia ya kanisa. Tatizo lilianza inavyoonekana na mgongano wa sura za agano Jipya:

A. maandiko juu ya ahadi
   1. maelezo ya Yesu (Yohana 6:37; 10:28-29)
   2. maelezo ya Paulo (Rum. 8:35-39; Efe. 1:13; 2:5,8-9; Fil. 1:6; 2:13; 2 The. 3:3; 2 Tim. 1:12; 4:18)
   3. maelezo ya Petro ( 1 Pet. 1:4-5)
B. maandiko juu ya hitaji la ustahimilivu
   1. maelezo ya Yesu (Mt. 10:22; 13:1-9,24-30; 24:13; Marko 13:13; Yohana 8:31; 15:4-10; Ufu. 2:7,17,26; 3:5,12,21)
   2. maelezo ya Paulo (Rum. 11:22; 1 Kor. 15:2; 2 Kor. 13:5; Gal. 1:6; 3:4; 5:4; 6:9; Fil. 2:12; 3:18-20; Kol. 1:23; 2 Tim. 3:2)
   3. maelezo ya mwandishi wa Waebrania (2:1; 3:6,14; 4:14; 6:11)
   4. maelezo ya Yohana (1 Yohana 2:6; 2 Yohana 9)
   5. maelezo ya Baba (Ufu. 21:7)

Masuala ya wokovu wa Kibiblia toka kwa pendo, rehema, na neema ya Mungu Mkuu wa Utatu. Hakuna mwanadamu atakaye okolewa pasipo kuanzishwa na Roho (kama vile Yohana 6:44,65).Uungu huja kwanza na kuweka ajenda, lakini huhitaji kwamba lazima wachukue hatua katika imani na toba, kwa hali zote mwanzoni na kuendelea. Mungu hutenda na wanadamu katika ushirika wa agano.kuna faida na uwajibikaji! Wokovu hutolewa kwa wanadamu wote.

Kifo cha Yesu kinashughulika na tatizo la dhambi ya uumbaji la mwanadamu aliyeanguka. Mungu amekwisha kutoa njia na kuwataka wale wote walioumbwa kwa sura yake kuitikia kwenye pendo lake katika Yesu.
Kama ukihitaji kusoma zaidi juu ya somo hili toka kwenye mtizamo wa wale wasio wafuasi wa Calvin, angalia

1. Dale Moody, *The Word of Truth,* Eerdmans, 1981 (kur. 348-365)
2. Howard Marshall, *Kept by the Power of God*, Bethany Fellowship, 1969
3. Robert Shank, *Life in the Son*, Westcott, 1961

Biblia inayaainisha matatizo mawili tofauti katika eneo hili: (1) kuzichukulia ahadi kama kibali cha kuishi pasipo mafanikio, maisha ya ubinafsi na (2) kuwatia moyo wale wote wanaojitahidi na huduma na dhambi binafsi. Tatizo ni kuwa makundi potofu yanachukua jumbe zisizo sahihi na kujenga miundo ya kithiolojia juu ya sura za Kibiblia .baadhi ya Wakristo huhitaji ujumbe wa ahadi, wakati wengine huhitaji onyo kali! Ni kundi lipi ulilopo wewe?

◙ **"kwa ajili ya lile neno"** Tambua kuwa dhiki inahusiana na injili (kama vile Mt. 5:10-12; 1 Pet. 2:11-12,21; 3:14-17; 4:12-16). Mwana wa Mungu, neno la Mungu, na watu wa Mungu ndio kusudio la ulimwengu ulioanguka.

**4:18** Aina ya tatu ya udongo inarejerea kwa wale wanaolisikia neno, lakini matatizo ya nje (kama vile Marko 4:19) husababisha (yaani., mbegu – neno) kufa. Tambua tofauti ya wazi kati ya uotaji na uzaaji wa matunda! Mwanzo mzuri haumaanishi kushinda mbio, bali ni umaliziaji mzuri (kama vile Yohana 15; Waebrania 11).

**4:19 "shughuli za dunia na udanganyifu wa mali"** Haya yanarejerea majaribu kwenye huu ulimwengu ulioanguka (au zama).

**4:20 "mmoja thelathini, mmoja sitini, na mmoja mia"** Wingi sio muhimu kama uzaaji wa matunda!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 4:21-25**
**21 Akawaambia, Mwaonaje? Taa huja ili kuwekwa chini ya pishi, au mvunguni? Si kuwekwa juu ya kiango? 22 Kwa maana hakuna neno lililositirika, ila makusudi lije likadhihirika; wala hakuna lililofichwa, ila makusudi lije likatokea wazi. 23 Mtu akiwa na masikio ya kusikilia, na asikie. 24 Akawaambia, Angalieni msikialo; kipimo kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa, na tena mtazidishiwa. 25 Kwa maana mwenye kitu atapewa, naye asiye na kitu, hata kile alicho nacho atanyang'anywa.**

**4:21 "taa"** Maswali mawili ya kwanza kwa Marko 4:21 kisarufi yanategemea jibu la "hapana." Nuru humaanisha kuangaza. Imani humaanisha kuzaa matunda. Aya hii inaelezea ni kwa nini wengi hawakuielewa mifano ya Yesu. Mifano humaanisha kuangaza, mioyo miovu ya wanadamu na mienendo, na sio Mungu, huzuia nuru. Mungu anahitaji kuwasiliana (kama vile Marko 4:22).Yesu, katika mtizamo wa haraka kwenye muktadha, lazima atakuwa akizungumza tangazo lijalo la injili kamili ya ya ufufuo na kupalizwa. Kujirudia kwa siri za Kimasihi kwa Marko, kuuficha ukweli kulisababishwa na utumiaji wa mifano, ni ukosefu wa uelewa juu ya sehemu ya ndani ya mzunguko wa wanafunzi wakihitaji hili liweze kuonekana kwenye muktadha wa mbeleni (yaani., baada ya Pentekoste).

◙ **"pishi"** Hiki kilikuwa chombo chenye kuhifadhi kipimo cha vitu vikavu. Neno hili ni la Kilatini, yumkini likithibitisha kuwa injili ya Marko iliandikwa kwa ajili ya Warumi.

◙ **"uvunguni"** Kwa maana iliyo wazi huu ni "mkeka." Huu ulitumiwa sio tu kwa ajili ya kulalia (kama vile Marko 7:30), bali kwa ajili ya kukalia wakati wa kula mtu akiwa ameinama.

◙**"kiango"** Hili laweza kurejerewa kwa njia mbalimbali tofauti ambapo taa ziliwekwa ili kwamba kuifanya ile nuru: (1) iweze kuchomoza ukutani; (2) iweze kumulika juu ya ukuta; au (3) baadhi ya aina ya msingi.

**4:23 "ikiwa"** Hii ni sentensi yenye masharti daraja la kwanza. Yesu anadhani kuwa baadhi (hatimaye wote) watafahamu ubinadamu wake, lengo, na ahadi zake.

**4:24-25** Hili linazungumza kuhusu kanuni za kiroho. Ujumbe wa injili umeenea ng'ambo; maelezo ya kukua ni aina ya udongo mbegu ilipoangukia. Kuwa wazi kwa mwanadamu kwa ajili ya kweli ya kiroho ni muhimu. Hili halirejelei tu kwenye mwitikio wa mwanzo lakini kuendelea kuitikia. Mwitikio dhaifu utakataliwa

**4:24 "'Angalieni mlisikialo'"** Hili linarejerea kwenye ukubarifu binafsi wa Yesu au kukataliwa. Walimu wa dini ya Kiyahudi wanaamini kuwa mawazo yalikuwa ni bustani iliyolimwa tayari kwa kupandwa mbegu. Kile tunachoruhusu macho yetu kuona na masikio kusikia (kama vile Marko 4:9,23) huweka mizizi. Tunakuwa vile tuishivyo, tunavitizama, au kuweka vipaumbele!

◙**"' kipimo kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa'"** Huu mstari hauna mahusiano na utoaji wa fedha, bali ni utambuzi wa mambo ya rohoni. Huu ukweli vile vile unaelezewa katika Mt. 5:7; 6:14-15; 18:21-35; Marko 11:25; Luka 6:36-37; Yakobo 2:13; 5:9. Hii sio kazi ya wenye haki, bali ni kweli ile atendayo mtu ndiyo yenye kudhihirisha moyo wake. Waamini wana moyo mpya na familia mpya.

**4:25** Linapokuja suala la injili, huendelea kutoa na kuwapa wale wapokeao, lakini wale wanaoikataa,haifanyi chochote! Yesu anatumia mithali za kimafumbo (kama vile Marko 4:22,25;6:4; 8:35; 10:43-44). Hili lilikuwa mfano hasa wa waalimu wa Mashariki ya Karibu. Hii sura inatumia muundo TENDAJI, ambao yumkini ni maneno mengi kwa ajili ya Mungu. Mungu ni mwakilishi asiyeelezeka wa tendo lenyewe.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 4:26-29**
**26 Akasema, Ufalme wa Mungu, mfano wake ni kama mtu aliyemwaga mbegu juu ya nchi; 27 akawa akilala na kuondoka, usiku na mchana, nayo mbegu ikamea na kukua, asivyojua yeye. 28 Maana nchi huzaa yenyewe; kwanza jani, tena suke, kisha ngano pevu katika suke. 29 Hata matunda yakiiva, mara atapeleka mundu, kwa kuwa mavuno yamefika.**

**4:26 "mbegu"** Mfano huu ni wa kipekee kwa Marko. Kwa sababu ya mstari wa 14 tunalifahamu hili linarejelea kwenye ujumbe wa injili. Ukuaji ni matokeo ya mbegu nzuri na udongo mzuri. Hii ni dhana ya Kiungu na kibinadamu ya agano.

**4:27-29** Hili laweza kuaksi wokovu kama mchakato (kama vile 1 Kor. 1:18; 15:2; 2 Kor. 2:15; 2 Pet. 3:18). Huu mfano unaelezea ukuaji wa ajabu na kushangaza wa imani kwenye maisha ya wana wa Adamu walioanguka. Lengo ni kuzaa matunda!

## MADA MAALUM: WOKOVU (NJEO ZA VITENZI VYA KIYUNANI

Wokovu siyo kitu, bali ni uhusiano. Haiishii hapo mtu anapomwamini Kristo; ndiyo safari imeanza! Siyo Sera ya bima ya moto, wala tiketi ya kwenda mbinguni, bali ni kukua kumfanana Kristo. Tunao usemi katika Amerikaunaosema, kadiri wawili katika ndoa wanavyoendelea kuishi, ndiyo wanaendelea kufanana. Hili ndilo lengo la wokovu!

**WOKOVU KAMA KITENDO KILICHO KAMILISHWA (WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU)**

- Matendo 15:11
- Warumi 8:24
- 2 Timotheo 1:9
- Tito 3:5
- Warumi 13:11(inajumuisha WAKATI ULIOPITA USIOTIMILIFU ukiwa na mazingira ya WAKATI UJAO )

**WOKOVU KAMA HALI YA KUWA (WAKATI TIMILIFU)**

- Waefeso 2:5,8

**WOKOVU KAMA MCHAKATO UNAOENDELEA (WAKATI ULIOPO)**

- 1 Wakorintho 1:18; 15:2
- 2 Wakorintho 2:15
- 1 Petro 3:21

**WOKOVU KAMA UKAMILISHO WA WAKATI UJAO (WAKATI UJAO KATIKA NJEO YA KITENZI au MAZINGIRA)**
- Warumi 5:9, 10; 10:9,13
- 1 Wakoritho 3:15; 5:5
- Wafilipi 1:28;
- 1 Wathesalonike 5:8-9
- Waebrania 1:14; 9:28
- 1 Petro 1:5,9

Kwa hivyo, wokovu unaanza na uamuzi wa imani ya awali (kama vile Yohana 1:12; 3:16; Rum 10:9-13),lakini hili lazima liendane na mchakato wa imani katika mtindo ya maisha (kama vile Rum. 8:29; Gal. 3:19; Efe.1:4; 2:10), ambao siku moja utakuja kukamilishwa kwa kuonekana (kama vile 1 Yoh. 3:2). Hatua hii ya mwisho inaitwa utukufu.Hili linaweza kuelezwa kama.

1. Utukufu wa awali – udhihirisho (kukombolewa kutoka katika adhabu ya dhambi)
2. Wokovu endelevu–utakaso (kuokolewa toka katika nguvu ya dhambi)
3. Wokovu wa mwisho – utukufu (kuokolewa kutoka katika uwepo wa dhambi)

**4:29 "atapeleka mundu"** Hii ni stiari kwa ajili ya mavuno ya siku ya mwisho. Inarejelea kwenye siku ya hukumu (kama vile Yoeli 3:13; Mt. 3:12; 13:30).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 4:30-32**
**30 Akasema, Tuulinganishe na nini ufalme wa Mungu? Au tuutie katika mfano gani? 31 Ni kama punje ya haradali, ambayo ipandwapo katika nchi, ingawa ni ndogo kuliko mbegu zote zilizo katika nchi, 32 lakini ikiisha kupandwa hukua, ikawa kubwa kuliko miti yote ya mboga, ikafanya matawi makubwa; hata ndege wa angani waweza kukaa chini ya uvuli wake.**

**4:30** Hili linafanana na lile la kwenye Mt. 13:31-32.

**4:31 "mbegu ye haradari"** Walimu wa dini ya Kiyahudi wanasema zilikuwa ni mbegu ndogo. Lakini bado vichaka hukua zaidi ya urefu wa futi kumi na mbili. Huu mfano na ule uliopo juu. Ukuaji wa kiroho waweza kuanza kidogo, lakini matokeo ni makubwa! Kama mbegu ya injili inavyokuwa ndani ya moyo wa mtu katika ufanano wa Kristo, vivyo hivyo kwetu, ufalme wa Mungu hukua ndani ya ufalme wa ulimwengu (kama vile Mt. 13:33).

**4:32** Mwisho wa mstari huu wawezakuwa ni dokezo kwenye miti mikubwa kwenye andiko la Agano Jipya la Ezek. 17:22-24 na Dan.4:11-12 linalowakilisha ufalme.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 4:33-34**
**33 Kwa mifano mingi ya namna hii alikuwa akisema nao neno lake, kwa kadiri walivyoweza kulisikia; 34 wala pasipo mfano hakusema nao; lakini akawaeleza wanafunzi wake mwenyewe mambo yote kwa faragha.**

**4:33 " Kwa mifano mingi ya namna hii alikuwa akisema nao neno lake"** Tumeweza kuandika sehemu ndogo ya huduma ya Yesu aliyoifanya kwa njia ya maongezi (kama vile Yohana 21:25). Wengi wetu tunapenda kuwa tungeyapata mafundisho zaidi ya Yesu na matendo yake (kama vile Yohana 20:30), lakini tunapaswa kutambua kuwa tuna kila kitu tunachokihitaji kuhusu Mungu, dhambi, uhai, kifo, nakadhalika (kama vile Yohana 20:31). Lazima tuchukue hatua juu ya kile tulichopewa. Mistari hii miwili inafanana na ile ya Mt.13:33-35.

◙**"kwa kadri walivyoweza kulisikia"** Hii inarejelea kwenye upokeaji wa mambo ya kiroho (kama vile Marko 4:9,23). Waamini wa leo wana faida ya Roho Mtakatifu aishie ndani yetu ili kutusaidia kuyaelewa maneno ya Yesu.

**4:34** Hili linaaksi maelezo ya mwanzo ya Marko 4:10-12 na 13.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 4:35-41**
**[35] Siku ile kulipokuwa jioni, akawaambia, Na tuvuke mpaka ng'ambo. [36] Wakauacha mkutano, wakamchukua vile vile alivyo katika chombo. Na vyombo vingine vilikuwako pamoja naye. [37] Ikatokea dhoruba kuu ya upepo, mawimbi yakakipiga chombo hata kikaanza kujaa maji. [38] Naye mwenyewe alikuwapo katika shetri, amelala juu ya mto; wakamwamsha, wakamwambia, Mwalimu, si kitu kwako kuwa tunaangamia? [39] Akaamka, akaukemea upepo, akaiambia bahari, Nyamaza, utulie. Upepo ukakoma, kukawa shwari kuu. [40] Akawaambia, Mbona mmekuwa waoga? Hamna imani bado? 41 Wakaingiwa na hofu kuu, wakaambiana, Ni nani huyu, basi, hata upepo na bahari humtii?**

**4:35-41** Huu unaanzisha muktadha mpana wa miujiza, Marko 4:35-8:26.Yesu aauthibitisha ujumbe wake kwa kuionyesha miujiza. Hili tukio muhimu linafanana na lile la Mt. 8:18,23-27 na Luka 8:22-25.

**4:36** Mstari huu unazo tabia zisizo za kawaida ambazo hazipatikani katika mfanano.

1. Inamaana gani kusema "wakamchukua vile vile katika chombo"? Toleo la TEV linakitafasiri kama "wanafunzi wakaingia chomboni mle alimokwisha kaa Yesu." Huu unaonekana ni uchaguzi wenye kufaa.
2. Inamaana gani kusema "na vyombo vilikuwepo pamoja nao"? je lilikuwa ni kundi la Kitume lililokuwa kwenye boti zingine ndogo au boti zingine nazo zilikubwa na dhoruba? Haya ni maelezo dhahili ya ushuhuda wa macho (yaani., wa Petro), lakini kusudi na madokezo yake hayajulikani.

**4:37 "Ikatokea dhoruba kuu ya upepo"** Dhoruba kuu za ghafla ilikuwa ya kawaida kwenye ziwa Galilaya kwa sababu ya milima iliyokuwa imezunguka na kuwa chini ya usawa wa bahari. Hii yawezakuwa ni dhoruba mbaya kuwahi kutokea kwa sababu hata wale wavuvi wazoefu walipatwa na hofu kati yao.

**4:38** Hili tukio dhahili lilitumika kuuonyesha utulivu wa Yesu na hofu ya wanafunzi ya matukio ya muda huo. Swali kuhusu uhusika wa Yesu ni kwa watu wote. Ikiwa Mungu ni wa upendo, ni kwa nini waamini wanapatwa na majaribu ya kutisha katika maisha?

◙ "**Tunaangamia"** Angalia Mada Maalum: *Apollumi* katika Marko 3:6.

**4:39** Hili kwa nguvu limeonyesha uweza na mamlaka ya Yesu—hata upepo wa bahari unamtii.

◙**"Nyamaza, na utulie "** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo ikifuatiwa na kauli tendwa timilifu yenye kushurutisha. Yesu, kama Mungu, mwakilishi wa Baba wa uumbaji (kama vile Yohana 1:3,10; 1 Kor. 8:6; Kol. 1:16; Ebr. 1:2), alikuwa, na anazo, nguvu juu yake (kama vile Zab. 33:7; 65:2; 147:18).

**4:40** Hili ni swali zuri kwa ajili ya waamini wote katika kila hali. Yesu anawafundisha wanafunzi Wake kwa maneno na vitendo.

**4:41** Mstari huu kwa uwazi unaonyesha uchanga wa kithiolojia wa Mitume. Muktadha unatofautisha aina mbalimbali za kutokuamini: (1) familia zao; (2) viongozi wa kidini; na (3) wanafunzi. Namba 1 na 3 ni ukuaji wa kiroho. Kutokuamini kwao kuliegamia juu ya kukosa maarifa, lakini namba 2 ni wenye usumbufu. Wamepewa ishara baada ya ishara, kweli baada ya kweli, lakini kuwepo kwa upendeleo kabla viongozi wa kidini hawakukataa tu kuamini, bali waliyaona matendo ya Yesu na mafundisho ni ya nguvu za shetani! Hii ni dhambi isiyo sameheka!

## MASWALI YA MJADALA.

Huu ni <u>mwongozo</u> wa kujifunza wa fasiri. Inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Mjadala huu wa maswali unawekwa ili kukusaidia wewe kufikiri maana ya chapisho kupitia sehemu ya kitabu. Wanamaanisha kuchochea sio kumalizia.

1. Kwa nini huu mfano (Marko 4:3-5) ni wa muhimu katika kuitafasiri mingine yote?
2. Ni kwa namna gani uhusiano kati ya Ukuu wa Mungu na mapenzi huru ya Mwanadamu vinashughulika katika kifungu hiki?
3. Toa kiini cha ukweli kwenye haya:
    a. Marko 4:21-23
    b. Marko 4:24-25
    c. Marko 4:28-29
    d. Marko 4:30-32
4. Ni upi ukweli wenyewe wa hii mifano yote? (Kumbuka muktadha)
5. Orodhesha makundi matatu katika muktadha huu yale yasiyo amini.

# MARKO 5

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Uponyaji wa mtu Mwenye mapepo Wa Wagerasi | mtu mwenye mapepo aponywa | mwenye pepo wa wagerasi | Yesu anaponya mtu mwenye roho waovu | mwenye kujaa pepo wa Wagerasi |
| 5:1-10 | 5:1-20 | 5:1-13 | 5:1-5 | 5:1-20 |
| | | | 5:6-8 | |
| | | | 5:9a | |
| | | | 5:9b-10 | |
| 5:11-20 | | | 5:11-13 | |
| | | 5:14-20 | 5:14-16 | |
| | | | 5:17 | |
| | | | 5:18 | |
| | | | 5:19 | |
| | | | 5:20 | |
| Binti wa Yairo na Mwanamke Anayegusa mavazi Ya Yesu | Binti anarejeshwa na mwanamke anaponywa | binti wa Yairo anafufuka | Binti wa Yairo na mwanamke anayegusa mavazi ya Yesu | uponyaji wa mwanamke atokwaye na damu na binti wa Yairo anarejeshewa uhai |
| 5:21-24a | 5:21-43 | 5:21-24a | 5:21-23 | 5:21-24 |
| | | | 5:24 | |
| 5:24b-34 | | 5:4b-34 | | |
| | | | 5:25-28 | 5:25-34 |
| | | | 5:29-30 | |
| | | | 5:31 | |
| | | | 5:32-34 | |
| 5:35-43 | | 5:35-43 | 5:35 | 5:35-43 |
| | | | 5:36-39 | |
| | | | 5:40-41 | |
| | | | 5:42-43 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka ”Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia”)

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA 5:1-43

Sura hii imekusudiwa kuonesha maisha ya kila siku ya Yesu katika siku zenyewe za Yesu wakati wa kipindi chake cha huduma yake kwa watu. Nguvu ya Yesu na mamlaka yanadhihirishwa kwa

A. mpagawa pepo Mgerasi inafanana katika Mt. 8:28-34 na Luka 8:26-39 Mistari ya 1-20 (inaonesha nguvu ya Yesu juu ya ulimwengu wa roho)

B. Binti wa Yairo inafanana na ya Mt. 9:18-19,23-26 na Luka 8:40-42,49-56 Mistari 21-24, 35-43 (inaonesha nguvu ya Yesu juu ya mauti)

C. Mama mwenye kutoka damu inafanana na Mt. 9:20-22 na Luka 8:43-48 Mistari 25-34 (inaonesha nguvu ya Yesu juu ya magonjwa)

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 5:1-13**
**1 Wakafika ng'ambo ya bahari mpaka nchi ya Wagerasi. 2 Na alipokwisha kushuka chomboni, mara alikutana na mtu, ambaye ametoka makaburini, mwenye pepo mchafu; 3 makao yake yalikuwa pale makaburini; wala hakuna mtu ye yote aliyeweza kumfunga tena, hata kwa minyororo; 4 kwa sababu alikuwa amefungwa mara nyingi kwa pingu na minyororo, akaikata ile minyororo, na kuzivunja-vunja zile pingu; wala hakuna mtu aliyekuwa na nguvu za kumshinda. 5 Na sikuzote, usiku na mchana, alikuwako makaburini na milimani, akipiga kelele na kujikata-kata kwa mawe. 6 Na alipomwona Yesu kwa mbali, alipiga mbio, akamsujudia; 7 akapiga kelele kwa sauti kuu, akasema, Nina nini nawe, Yesu, Mwana wa Mungu aliye juu? Nakuapisha kwa Mungu usinitese. 8 Kwa sababu amemwambia, Ewe pepo mchafu, mtoke mtu huyu. 9 Akamwuliza, Jina lako nani? Akamjibu, Jina langu ni Legioni, kwa kuwa tu wengi. 10 Akamsihi sana asiwapeleke nje ya nchi ile.**
**11 Na hapo milimani palikuwa na kundi kubwa la nguruwe, wakilisha. 12 Pepo wote wakamsihi, wakisema, Tupeleke katika nguruwe, tupate kuwaingia wao. 13 Akawapa ruhusa. Wale pepo wachafu wakatoka, wakaingia katika wale nguruwe; nalo kundi lote likatelemka kwa kasi gengeni, wakaingia baharini, wapata elfu mbili; wakafa baharini.**

**5:1 "Wakafika ng'ambo ya bahari"** Yawezekana ilikua bado usiku (kama vile Marko 4:35). Wanafunzi walitakiwa kuendesha mashua kwa kuwa Yesu alikuwa amekwisha tuliza dhoruba.

◙**"mpaka nchi ya Wagerasi"** Huu ni upande wa pembezoni mwa kaskazini mashariki mwa bahari ya Galilaya, paitwapo Dekapoli. Eneo hili zaidi sana llikuwa la Mataifa na wageni wenye kushika tamaduni na mila za Kiyahudi. Vitabu vinne vya Injili vinatofautiana katika herufi: Gerasa (MSS א*, B, D, na Luka 8:26), Gergesa (MSS אi[2], L), Gergusta (MS W), au Gadara (MSS A, C, na Mt. 8:28). Yote hii ilikuwa miji katika eneo hili.

**5:2 "Na alipokwisha kushuka chomboni"** Labda wanafunzi walisikia kilio (Marko 5:5) na walikuwa na furaha kumruhusu Yesu aende kwanza!

◙**"mara"** Angalia angalizo katika Marko 1:10.

◙**"mtu"** Mt. 8:28 na kuendelea ina watu wawili. Mathayo pia alikuwa na watu wawili vipofu nje ya Yeriko (kama vile Mt. 20:29; Marko 10:46; Luka 18:35). Hii ni sifa ya Injili ya Mathayo. Marko na Luka wanakubali kwamba kulikuwa na mwenye kupagawa na pepo mmoja tu (kama vile Luka 8:26na kuendelea). Kwa ajili ya mjadala zaidi soma *Hard Sayings of the Bible* kurasa za 321-322.

◙**"mwenye pepo mchafu makao yake yalikuwa pale makaburini"** Hii ni hadithi ya dhahiri juu ya mtu aliyekuwa amepagawa na pepo. Agano Jipya halijadili chanzo cha kupagawa na pepo au maelezo ya ndani ya mpangilio juu ya naamna ya kushughulikia. Upungaji pepo haujawahi kutajwa kaka karama ya Roho. Angalia Mada Maalumu: Mapepo na Upungaji pepo katika Marko 1:25.

**5:3 "akikaa makaburini"** Walikuwa wamefika maeneo ya makaburi ya eneo la mahali. Watu wa eneo hilo walikuwa wamemfukuza huyu mwehu aliyepagawa na mapepo aende eneo hilo. Alikuwa amepafanya kama eneo lake.

◙**"wala hakuna mtu aliyekuwa na nguvu za kumshinda"** Alikuwa na nguvu zisizo za kawaida.

**5:4 "alikuwa amefungwa mara nyingi kwa pingu na minyororo"** Hii ni kauli ya kitenzi jina tendwa ya wakati timilifu. Inavyoonekana watu wa mjini walikuwa wamejaribu kumfunga kwa minyororo. Alikuwa anajulikana vizuri kama tatito la mahali hapa.

◙**"akaikata ile minyororo, na kuzivunja-vunja zile pingu"** Hii pia inaonesha nguvu zake zisizokuwa za kawaida.

**5:5 "akipiga kelele na kujikata-kata kwa mawe"** Tabia hii inahusianishwa na kutaka kujidhuru binafsi au shughuli za ibada za kipagani za Agano la Kale (kama vile 1 Wafalme. 18:28). Taarifa za kutosha za hali ya tabia za mara kwa mara za mtu huyu lazima zilitokana na watu wa kijiji hiki.

**5:6 "alipiga mbio, akamsujudia"** Neno la kwanza linaashiria uadui. Neno la pili linaashiria heshima na kutambuliwa kwa nafasi na mamlaka ya Yesu (kama vile Marko 5:4b).

**5:7 "akapiga kelele kwa sauti kuu, akasema, Nina nini nawe, Yesu, Mwana wa Mungu aliye juu?"** Moja ya pepo lilianza kuzungumza na Yesu. Yalijua kuwa yeye ni nani (kama vile Marko 1:23; Yakobo 2:19). Hata walizungumza nae kwa tungo ya ki-Masihi. Kwa namna hii, kilichowasumbua ni hofu (tofauti na 1:23).

◙**"Nakuapisha kwa Mungu"** Hii ilikuwa ni nahau ya kiebrania ambayo ilimaanisha "kuapia kwa Mungu."

◙**"usinitese"** Hii kisarufi aidha ni kauli tendaji saidizi ya wakati uliopita usiokamilifu "usije ukaanzisha kitendo" (kama vile Barbara na Timotheo Friberg's *Analytical Greek NewTestament*, ukurasa 120). Mapepo yalijua kwamba hukumu inakuja (kama vile Marko 1:23-24; Mt. 25:41; Ufu. 12:9; 20:10). Ufanano katika Mt. 8:29 na Luka 8:28 na 31 pia inamaanisha matukio ya siku za mwisho. Mapepo haya inavyoonekana hayakujua juu ya kuja mara mbili kwa Masihi. Hata "pepo" zinaweza kutaabisha!

**5:8,9 "amemwambia"** Njeo ya wakati usio timilifu: (1) kitendo kinachorudiwa katika wakati uliopita (2) mwanzo wa kitendo kwa muda uliopita #2 unaonekana kushabihiana. Hatahivyo, ikiwa mpangilio wa kauli za Yesu kwa mapepo upo nje ya mpangilio, hivyo #1 inaweza kuwa sahihi. Marko anaweza kuwa anatumia njeo katika hali ya urafiki kwasababu ya njeo pia ambayo ipo katika Marko 5:10.

**5:9 "Jina lako nani?”** Swali hili linaweza kuwa nahau ya kiebrania na kurejerea sifa zao.

◙**"Legioni"** Katika Jeshi la Kirumi kiasi cha watu 6,000 ndiyo lilitengeneza kikosi. Hili ni moja ya maneno ya Kilatini yatumikayo katika Marko. Hii inaweza kuwa ilikuwa sitiari na kiwango cha udhibiti juu ya mtu. Hata hivyo kwasababu ya Marko 5:13, ambayo inaelezea mapepo yasababishayo kifo cha nguruwe 2,000 inaweza kuwa dhahiri.

**5:10 "nje ya nchi ile"** Hii inaweza kurejerea (1) eneo la makaburini; (2) the wilaya ya Dekapoli; au (3) yawezekana kuzimu ambayo inaandikwa katika mfano wa Luka 8:31. Mathayo inafanana "kabla ya wakati uliokusudiwa" (kama vile Mt. 8:29).

**5:11** Kundi la nguruwe linaonesha kuwa hili lilikuwa ni eneo la Mataifa.

**5:12 "tuache tuwaingie nguruwe"** Angalia utaona kwamba mapepo yalikuwa na ombi kwa Yesu. Andiko halitwambii kwanini Yesu aliruhusu haya mapepo kuwaingia nguruwe au kwanini yenyewe yalitaka hivyo. Yawezekana mapepo kumtoka mtu na kuingia katika nguruwe ilikuwa ni njia nyepesi ya kutia moyo mtu huyu kuamini kwamba amefunguliwa (yaani kisaidizi cha imani, sawasawa na kutema mate katika ardhi kutengeneza tope kwa ajili ya macho ya kipofu). Mapepo yanaweza kuwa yaliomba kwasababu (1) walipendelea nguruwe kuliko kwenda kuzima au (2) tendo hili lingesababisha watu wa mjini kumuomba Yesu aondoke. Mapepo hayafanyi ili kumsaidia Yesu!

**5:13 "walizama"** Hii ni kauli tendwa elekezi ya wakati usio timilifu. Walikimbilia shimoni mmoja baada ya mwingine!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 5:14-20**
**[14] Wachungaji wao wakakimbia, wakaieneza habari mjini na mashambani. Watu wakatoka walione lililotokea. [15] Wakamwendea Yesu, wakamwona yule mwenye pepo, ameketi, amevaa nguo, ana akili zake, naye ndiye aliyekuwa na lile jeshi; wakaogopa. [16] Na wale waliokuwa wameona waliwaeleza ni mambo gani yaliyompata yule mwenye pepo, na habari za nguruwe. [17] Wakaanza kumsihi aondoke mipakani mwao. [18] Naye alipokuwa akipanda chomboni, yule aliyekuwa na pepo akamsihi kwamba awe pamoja naye; [19] lakini hakumruhusu, bali alimwambia, Enenda zako nyumbani kwako, kwa watu wa kwenu, kawahubiri ni mambo gani makuu aliyokutendea Bwana, na jinsi alivyokurehemu. [20] Akaenda zake, akaanza kuhubiri katika Dekapoli, ni mambo gani makuu Yesu aliyomtendea; watu wote wakastaajabu.**

**5:14 "Watu wakatoka walione lililotokea"** Kutamani kujua na hofu vilipelekea watu wa mjini kuja hata wakati wa usiku.

**5:15 "ameketi"** Hii ni ya kwanza katika mfuatano wa hali zinazoelezea amani mpya ya huyu mtu na kutulia kwake.

◙**"amevaa nguo"** Hii ina maanisha siku zote hakuwa amezoea kuvaa nguo (kama vile Luka 8:27).

◙**"ana akili zake"** Kupagawa na pepo kunajidhihirisha kwenyewe katika njia nyingi
1. kutoongea (Marko 9:17,25; Mt. 9:32)
2. kutoongea wala kuona (Mt. 12:22)
3. kifafa (Mt. 17:15,18)
4. kuwa na nguvu nyingi (Marko 5:3-4)
5. kujig'ata g'ata (Marko 1:26; 9:20)
6. kupooza (Mdo. 8:17)

Hatahivyo, sio matatizo yote ya kimwili yana asili au kwamba chanzo chake ni mapepo. Katika Injili ugonjwa na kupagawa mara kwa mara kunatofautishwa (kama vile Marko 1:32,34; 6:13; Mt. 4:24; 10:8; Luka 4:40-41; 9:1; 13:32).

**5:17 "Wakaanza kumsihi aondoke mipakani mwao"** Hii ni kauli ya kali elekezi ya wakati uliopita usio timilifu na kitenzi jina tendaji cha wakati uliopo. Kukataliwa huku ndio sababu ambayo mapepo yaliitumia kutaka kuingia kwa nguruwe! Watu wa mjini walimtaka Yule aliyemtuliza ambaye hakuwahi kuwa na mtu kabla ya kumtuliza aondoke. Tofauti kubwa iliyoje na kijiji cha Yohana 4. Inavyoonekana sababu za kiuchumi zilikuzwa ziakawa nzito kuliko urejesho wa mtu huyu.

**5:19 "Enenda zako nyumbani kwako, kwa watu wa kwenu"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Yesu alikuwa anamwambia arudi nyumbani. Yesu alijua uwepo wa inavyoonekana mfuasi ambaye ni mataifa ungesababisha matengano ya baadhi ya watu wa Kiyahudi. Kwa kukaa sasa Yesu alikuwa shuhuda katika eneo hili la Mataifa. Bado alionesha kuwajali watu hawa hata kama walikuwa wenye kujali na wenye kupenda mali!

◙**"kawahubiri"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu. Shirikisha wenzako kile ambacho Mungu amekufanyia. Inavyoonekana alifanya jambo hili vyema kabisa (kama vile Marko 5:20). Hii inaonesha Yesu anawapenda mataifa.

**5:20 "Dekapoli"** Neno hili la Kiyunani linamaanisha "miji kumi." Ilikuwa shirikisho lilikuwa la Iskanda Mkuu. Jimbo hili lilikuwa kaskazini mwa Perea na mashariki mwa bahari ya Galilaya. Lilikuwa kimbilio la desturi za watu wa kuja walioshikilia desturi na mila za kiyahudi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 5: 21-24**
**[21] Hata Yesu alipokwisha kuvuka kurudia ng'ambo katika kile chombo, wakamkusanyikia mkutano mkuu; naye alikuwa kando ya bahari. [22] Akaja mtu mmoja katika wakuu wa sinagogi, jina lake Yairo; hata alipomwona, akaanguka miguuni pake, [23] akimsihi sana, akisema, Binti yangu mdogo yu katika kufa; nakuomba uje, uweke mkono wako juu yake, apate kupona, na kuishi. [24] Akaenda pamoja naye; mkutano mkuu wakamfuata, wakimsonga-songa.**

**5:22 "mtu mmoja katika wakuu wa sinagogi, jina lake Yairo"** Jina lake linamaanisha "YHWH amenitia nuru." Huyu alikuwa mtu mwenye majukumu ya kiutawala kama kusimamia majengo ya hekalu. Alikuwa mtu mwenye asili ya kidini katika jamii.

◙**"akaanguka miguuni pake"** Hii ilikuwa ishara ya heshima na vile vile ibada (kama vile Marko 5:6,22,33 ambapo maneno tofauti yanatumika, lakini tendo lile lile). Kiongozi mwenye mbobezi wa kidini kuinama kifudi fudi mtaani mbele ya mwalimu wa kiyahudi asiye rasmi lilikuwa ni jambo lisilotegemewa!

◙**"Binti yangu mdogo yu katika kufa"** Mathayo 9:18 inasema kwamba alikuwa amekwisha kufa. Mtu huyu aliamini kwamba uwepo wa Yesu na mguso wake ungemponya na kurejesha binti yake.

**5:23**

| | |
|---|---|
| **NASB, TEV** | **"atakuwa mzima"** |
| **NKJV** | **"ataponywa"** |
| **NRSV** | **"anaweza akaponywa"** |
| **NJB** | **"anaweza kuokolewa"** |

Hili ni neno la kauli tendwa ya wakati uliopita usio timilifu *sōzō*, lililotumika katika namna ya Agano la Kale kuashiria ukombozi wa kimwili (kama vile Yakobo 5:15). Katika Agano Jipya inachukua namna ya wokovu wa kiroho. Haijulikani kithiolojia ikiwa wale wote ambao Yesu aliwaponya waliokolewa pia kiroho. Matendo yake lazima yalianzisha mchakato ambao ungepelekea baadaye maisha ya mtu wa kiroho haijaandikwa katika maandiko.
Kama vile mfano angalia katika sura hii ambapo imani ya mwenye kupagawa na pepo inaonekana baada ya kuponywa na sio kabla. Binti anasaidiwa kwasababu ya imani ya baba yake na mwanamke anayetokwa na damu alikuwa tayari kumfanya Yesu najisi kwa tendo la kumgusa mwalimu katika ubinafsi (hata kiushirikina). Ni mahali gani ukomo wa faida binafsi inakoma na imani kuanza?

**5:24 "wakimsonga-songa"** Luka 8:42 inaongeza kwamba shinikizo la umati wa watu lilikuwa kubwa sana mpaka kiasi cha kufanya kuwa ngumu kupumua.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 5:25-34**
**[25] Na mwanamke mmoja mwenye kutoka damu muda wa miaka kumi na miwili, [26] na kuteswa mengi kwa mikono ya matabibu wengi, amegharimiwa vitu vyote alivyo navyo, kusimfae hata kidogo, bali hali yake ilizidi kuwa mbaya [27] aliposikia habari za Yesu, alipita katika mkutano kwa nyuma, akaligusa vazi lake; [28] maana alisema, Nikiyagusa mavazi yake tu, nitapona. [29] Mara chemchemi ya damu yake ikakauka, naye akafahamu mwilini mwake kwamba amepona msiba ule. [30] Mara Yesu, hali akifahamu nafsini mwake kwamba nguvu zimemtoka, akageuka kati ya**

**mkutano, akasema, Ni nani aliyenigusa mavazi yangu? [31] Wanafunzi wake wakamwambia, Je! Wawaona makutano wanavyokusonga-songa, nawe wasema, Ni nani aliyenigusa? [32] Akatazama pande zote ili amwone yule aliyelitenda neno hilo. [33] Na yule mwanamke akaingiwa na hofu na kutetemeka, akijua lililompata, akaja akamwangukia, akamweleza kweli yote. [34] Akamwambia, Binti, imani yako imekuponya, enenda zako kwa amani, uwe mzima, usiwe na msiba wako tena.**

**5:25 "mwenye kutoka damu muda wa miaka kumi na miwili"** Hii ingemfanya awe najisi mbele za watu (kama vile Law. 15:25-27) na, hivyo kumtenga mbali na miundo yote ya ibada za kiyahudi (yaani hekalu na sinagogi).

**5:26 "na kuteswa mengi kwa mikono ya matabibu wengi"** Luka, tabibu anaacha maoni haya nje katika Luka 8:43 na kuendelea.

◙**"amegharimiwa vitu vyote alivyo navyo, kusimfae hata kidogo"** Tiba ya Kiyahudi kwa hili tatizo inaorodheshwa katika Talmud kama (1) kubeba majivu ya yai la mbuni katika kifundo cha kitambaa kwa kuzunguka shingo wakati wa msimu wa jua na katika kifundo cha kitambaa cha pamba wakati wa kipupwe (2) kubeba nywele za mahindi kutoka katika kinyesi cha punda wa kike mweupe (kama vile Shabb. 110 A & B).

**5:27 "akaligusa vazi lake"** Yawezekana alichokigusa kilikuwa ni kitambaa chake cha maombi, kilitumika na wanaume kujifunika kichwa wakati wa ibada. Kilikuwa kikiitwa Tallith (kama vile Hes. 15:38-40; Kumb. 22:12). Kwa mwanamke ambaye ni najisi kumgusa mwalimu wa  lilikuwa ni tendo lisilokubalika. Mwanamke huyu kutapatapa akihitaji msamaha sana!

**5:30 "mara"** Angalia angalizo katika Marko 1:10.

◙**"hali akifahamu nafsini mwake kwamba nguvu zimemtoka"** Asili hasa ya nguvu hii au aina gani ya nguvu anayoizungumzia haijulikani uhakika wake bado. Kidhahiri ilikuwa inatoka kwa Mungu (kama vile Luka 5:17). Yesu alihisi athari yake. Yesu alikuwa na uwezo wa kuiweka juu ya wengine katika kuwatuma Kumi na Mbili na Sabini kimisheni.

◙**"kwamba nguvu zimemtoka"** Mathayo 8:17 inanukuu Isa. 53:4 kwamba Masihi angetuponya kwasababu alichukua madhaifu yetu.

◙**"Nani aliyegusa mavazi Yangu"** Kulikuwa na kusanyiko kubwa (kama vile Marko 5:31). Mathayo 9:20 ina "kifundo cha urembo/ncha." Taulo la maombi lilikuwa na vifundo vya urembo vya bluu kumi na tatu, kama kuisifu sheria ya Musa.

**5:32 "kaangaza huko na huko"** Hii njeo ya wakati usio mkamilifu ilimaanisha kuangalia umati wa watu. Katika tukio hili Yesu hakuwa amepewa taarifa kiungu juu ya nani au nini kilikuwa kimetokea. Yawezekana swali lilikuwa limeulizwa kwa mwanamke (yaani fursa ili akiri wazi imani yake).

**5:33 "akihofu na kutetemeka"** Wanawake walikuwa na nafasi ya chini sana katika jamii. Hakuwa tayari kuzungumza mbele ya hadhara ya watu. Pia alijua kwamba kwakuwa alikuwa najisi basi hakuwa na ruhusa ya kumgusa mwalimu.

**5:34 "'binti'"** Mafundisho ya Yesu yanafunua ukweli kwamba wanadamu kupitia imani katika Yesu wanaweza kufanyika watu wa familia ya Mungu. Wokovu unaelezwa katika kuzaliwa au kwa maneno ya kisheria kuashiria uhusiano wa kifamilia. Sitiari zenye nguvu kiasi gani kwa ajili ya utajiriba ya Mkristo!

◙**"'imani yako imekuponya'"** Sio mguso bali kutendea kazi imani yake katika Yeye ndiyo ulikuwa msingi. Imani yenyewe sio jambo kubwa sana lakini lengo lililo katika imani (yaani Yesu). Hakukuwa na chochote kama miujiza hapa, wala haikuwa nguvu ya fikra chanya bali nguvu ya Yesu. Haya ni matumizi mengine ya Kiyunani *sōzō* na katika namna yake ya Agano la Kale (kama vile Marko 5:23). Hii hapa ni kauli tendaji elekezi ya wakati timilifu ambayo ilimaanisha kwamba aliponywa na kubaki ameponywa tatizo lake la mwili.

◙**"'nenda kwa amani umeponya mateso yako'"** Zote mbili ni kauli tendaji shurutishi za wakati uliopo. Neno amani (*eirēnē*) lina ufanano kamili wa ukamilifu mzima na ustawi, sio tu ukosefu wa matatizo. Neno "mateso" inatoka katika mzizi "kupiga/kuswaga."

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 5:35-43**
**35 Hata alipokuwa katika kunena, wakaja watu kutoka kwa yule mkuu wa sinagogi, wakisema, Binti yako amekwisha kufa; kwani kuzidi kumsumbua mwalimu? 36 Lakini Yesu, alipolisikia lile neno likinenwa, akamwambia mkuu wa sinagogi, Usiogope, amini tu. 37 Wala hakumruhusu mtu afuatane naye, ila Petro, na Yakobo, na Yohana nduguye Yakobo. 38 Wakafika nyumbani kwa yule mkuu wa sinagogi, akaona ghasia, na watu wakilia, wakifanya maombolezo makuu. 39 Alipokwisha kuingia, akawaambia, Mbona mnafanya ghasia na kulia? Kijana hakufa, bali amelala tu. 40 Wakamcheka sana. Naye alipokwisha kuwatoa nje wote, akamtwaa babaye yule kijana na mamaye, na wale walio pamoja naye, akaingia ndani alimokuwamo yule kijana. 41 Akamshika mkono kijana, akamwambia, Talitha, kumi; tafsiri yake, Msichana, nakuambia, Inuka. 42 Mara akasimama yule kijana, akaenda; maana alikuwa amepata umri wa miaka kumi na miwili. Mara wakashangaa mshangao mkuu. 43 Akawaonya sana, mtu asijue habari ile; akaamuru apewe chakula.**

**5:35 "'amekufa'"** Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati uliopita usiotimilifu. Nina uhakika Yairo hakuweza kusubiri kabisa! Hii inaonekana kuwa jaribu la imani yake au mfano mwingine wa nguvu za Yesu na mamlaka.

**5:36**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"akasikia kle kilichokuwa kikizungumzwa"** |
| **NKJV** | **"mara baada ya kusikia lile neno lililokuwa likizungumzwa"** |
| **NRSV, NJB** | **"akisiakia kile walichokuwa wakizungumza"** |
| **TEV** | **"Yesu hakujali kile walichokuwa wakikizungumza"** |
| **NIV** | **"akipuuzia kile walichokuwa wakimeza mate"** |

Mzizi wa Kiyunani unamaanisha "kusikia bila kujali." Inaweza kueleweka kama "kupuuzia" au "kusikia vibaya." Neno hili ni tata kiasi kwamba mapema sana waandishi walilibadili kuelekea neno "kusikia" (kama vile MSS א[a], A, C, D, na K), ambalo linapatikana katika ufanano la Luka, 8:50.

◙**"'Usiogope *tena*'"** Hii ni kauli shurutishi ya wakati uliopo yenye kiambata hasi ambayo siku zote inamaanisha kusimamisha tendo wakati liko katika mchakato. Kinyume cha hofu ni imani!

◙**"'amini tu'"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Kauli rahisi lakini iliyo ya muhimu (kama vile Mdo. 16:31).

**5:37 "hakumruhusu mtu afuatane naye"** Kwanini Yesu alikuwa na kikundi cha ndani cha wanafunzi (kama vile Marko 1:29; 5:37; 9:2; 13:3; 14:33) haijulikani. Injili ya Marko ni ushuhuda wa macho wa Petro. Huku kuwa ndani hakukuwapa upendeleo maalumu kwasababu Yakobo aliuwawa mapema sana. Yesu hakutaka umaarufu wake kama mponyaji ana hata yeye aliyemfufua kutoka katika wafu afanye kujulikana. Hii ni moja kati ya kadhaa ya aina ya kauli katika Marko ambayo wanathiolojia wanaita"Siri ya Kimasihi" (kama vile Marko 5:43). Tayari alikuwa na matatizo makubwa ya kimahitaji kwa kuwa na kundi kubwa.

◙**"ila Petro, na Yakobo, na Yohana nduguye Yakobo "** Hiki kilikuwa kikundi cha ndani cha karibu cha wanafunzi (kama vile Marko 9:2; 14:33; Mt. 17:1; 26:37; Luka 9:28).

**5:38 "watu wakilia, wakifanya maombolezo makuu"** Hizi zilikuwa shughuli za mazishi za Kiyahudi zilizo zoeleka na hata zilizokuwa zikitegemewa. Ilionesha kwamba watu wa familia walikuwa wakitegemea kifo cha binti mdogo na walikuwa wameshafanya maandalizi.

**5:39 "mtoto hajafa, lakini amelala'"** Kulala ilikuwa ni sitiari ya Agano la Kale ya Kifo. Yesu analitumia juu ya Lazaro katika Yohana 11:11. Hapa inahusianishwa na kifo. Mtu anaweza kushangaa ikiwa Marko 5:37 inafikiriwa kuwa rejea ya "Siri ya

Marko ya Kimasihi" sasa kwanini aliuwaambia hili mkutano wa watu, mpaka Anajaribu kupunguza athari (yaani kupunguza uvumi) wa binti kufufuliwa?

**5:40 "wakaanza kumcheka"** Hii ni njeo ya wakati usio timilifu ambao inamaanisha wapiti njia waliendelea kucheka muda ulio ongezwa au kwamba walianza kumcheka katika wakati huu.

◙**"na wale walio pamoja naye"** Hii inarejerea Petro, Yakobo na Yohana. Katika namna nyingi miujiza ya Yesu ilikuwa kwa ajili ya mafunzo ya wanafunzi na imani kuliko kwa watu aliokuwa akiwasaidia!

**5:41 "'Talitha, kumi'"** Hii ni tungo ya Kiaramu. Wayahudi wa siku za Yesu walizungumza kiaramu na wala sio kiebrania. Hii ilikuwa lugha mama ya Yesu. Ziko tungo kadhaa za Kiaramu zilizo andikwa katika Injili (kama vile *Sabbata*, Marko 3:4; *Boanerges,* Marko 3:17; Shetani, Marko 3:23,26; 8:33; *Talitha cumi*, Marko 5:41; *Ephphatha*, Marko 7:35; *Gehanna*, Marko 9:43,45,47; *pascha*, Marko 14:14; *Abba*, Marko 14:36; *Eloi, Eloi, lama sabachthani*, Marko 15:34). Ukweli kwamba Marko anafasiri ili inaonesha hadhira yake iliyokusudiwa kwamba ilikuwa ni mataifa.

**5:42 "ghafla . .ghafla"** Angalia angalizo katika Marko 1:10.

◙**"alikuwa miaka kumi na mbili"** Hii ingemaanisha kwamba alikuwa na jukumu la kutunza sheria (yaani *bath mitzvah*) na ilikuwa umri wa kuolewa. Wavulana walianza kubeba najukumu kwa sheria na kuoa katika umri wa miaka kumi na tatu (yaani *bar mitzvah*). Umri wa kuishi ulikuwa mfupi zaidi na vizazi vya familia iliishi pamoja; hivyo walioa katika umri mdogo zaidi kuliko leo.

**5:43 "Akawaonya sana, mtu asijue habari ile"** Yesu hakutaka kujulikana kama mponyaji au mtenda miujiza. Alifanya shughuli zake kufunua huruma ya Mungu na kuthibitisha ujumbe Wake na mamlaka (kama vile Marko 1:44; 3:12; 5:43; 7:36;8:26,30; 9:30; Mt. 8:4; 9:30; 12:16; 17:9).

◙**"akaamuru apewe chakula"** Haya ni maelezo ya ushuhuda mwingine. Yesu anaonesha kujali juu ya binti mdogo. Hii pia inathibitisha kuwa kweli amerejeshewa maisha yake ya kimwili.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni nini maana ya kupagawa na pepo? Je yaweza kutokea leo? Je Wakristo waweza kuathiriwa?
2. Kwanini Yesu aliruhusu nguruwe kuharibiwa?
3. Kwanini watu wa mjini wa mahali wamfukuze Yesu?
4. Kwanini mwenye pepo alilazimika kubaki?
5. Inamaanisha nini "nguvu zilikuwa zimemtoka?"
6. Kwanini Yesu anaita wafu, "wamelala?"
7. Kwaniini Yesu anataka suala la kumfufua binti wa Yairo kuendelea kuwa siri?
8. kwanini Yesu alikuwa na kikundi cha ndani cha karibu cha wanafunzi?

# MARKO 6

| MIGAWANYO YA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJV** |
| Kukataliwa kwa Yesu huko Nazareti | Yesu anakataliwa huko Nazareti | Kukataliwa huko Nyumbani | Yesu Anakataliwa huko Nazareti | Kuitembelea Nazareti |
| 6:1-6a | 6:1-6 | 6:1-6a | 6:1-3 | 6:1-6a |
| | | | 6:4 | |
| | | | 6:5-6a | |
| Agizo la wale Kumi na wawili | Kuwatuma Kumi Na Wawili | Kuamrisha na Maelekezo kwa wale Kumi na Wawili | Yesu Anawatuma Wanafunzi Kumi na Wawili | Agizo la Wale Kumi na Wawili |
| 6:6b-13 | | 6:6b-13 | 6:6b-11 | 6:6b-13 |
| | 6:7-13 | | | |
| | | | 6:12-13 | |
| Kifo cha Yohana Mbatizaji | Yohana Mbatizaji Anakatwa Kichwa | Kifo cha Yohana Mbatizaji | Kifo cha Yohana Mbatizaji | Herodi na Yesu |
| 6:14-29 | 6:14-29 | 6:14-16 | 6:14 | 6:14-16 |
| | | | 6:15a | |
| | | | 6:15b | |
| | | | 6:16-18 | Yohana Mbatizaji Anakatwa Kichwa |
| | | 6:17-29 | | |
| | | | | 6:17-20 |
| | | | 6:19-20 | |
| | | | 6:21-23 | |
| | | | | 6:21-29 |
| | | | 6:24a | |
| | | | 6:24b | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | 6:25 | |
| | | | 6:26-29 | |
| Kulisha watu Elfu Tano | Kulisha watu Elfu Tano | Watu Elfu Tano Wanalishwa | Yesu Anawalisha Watu Elfu Tano | Muujiza wa Kwanza wa Mikate |
| 6:30-44 | 6:30-44 | 6:30-44 | 6:30-32 | 6:30-44 |
| | | | 6:33-36 | |
| | | | 6:37a | |
| | | | 6:37b | |
| | | | 6:38a | |
| | | | 6:38b | |
| | | | 6:39-44 | |
| Kutembea juu ya Maji | Yesu Anatembea Juu ya Bahari | Yesu Anatembea Juu ya Maji | Yesu Anatembea Juu ya Maji | Yesu Anatembea Juu ya Maji |
| 6:45-52 | 6:45-52 | 6:45-46 | 6:45-50a | 6:45-52 |
| | | 6:47-52 | | |
| | | | 6:50b-52 | |
| Kuponya Wagonjwa Humo Gineresati | Wengi Wanamgusa na kuwa vema | Kuamini katika katika Yesu na kuamini | Yesu awaponya Wagonjwa humo Ginerasati | Tiba huko Gineresati |
| 6:5356 | 6:53-56 | 6:53-56 | 6:53-56 | 6:53-56 |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka "Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia")**

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo wa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## ULINGANIFU WA UFANANO WA VITABU VYA KIINJILI

A. Mistari ya 1-6 inafananishwa katika Mt. 13:54-58.
B. Mistari ya 6b-13 inafananishwa katika Mt. 9:35-11:1 na Luka 9:1-6.
C. Mistari ya 14-29 inafananishwa katika Mt. 14:1-12 na Marko 6:14-16 na katika Luka 9:7-9.
D. Mistari ya 30-44, ambayao inazungumzia tendo la kulisha watu eltano, inapatikana katika Injili nne (Marko 6:30-44; Mt. 14:13-21; Luka 9:10-17; Yohana 6:1-13).
E. Mistari ya 45-52 inafananishwa katika Mt. 14:22-23 na Yohana 6:14-21.
F. Mistari ya 53-56 inafananishwa katika Mt. 14:34-36

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 6:1-6a**
**1 Akatoka huko, akafika mpaka nchi ya kwao; wanafunzi wake wakamfuata. 2 Na ilipokuwa sabato, alianza kufundisha katika sinagogi; wengi waliposikia wakashangaa, wakisema, Huyu ameyapata wapi haya? Na, Ni hekima gani hii aliyopewa huyu? Na, Ni nini miujiza hii mikubwa inayotendeka kwa mikono yake? 3 Huyu si yule seremala, mwana wa Mariamu, na ndugu yao Yakobo, na Yose, na Yuda, na Simoni? Na maumbu yake hawapo hapa petu? Wakajikwaa kwake. 4 Yesu akawaambia, Nabii hakosi heshima, isipokuwa katika nchi yake mwenyewe, na kwa jamaa zake, na nyumbani mwake. 5 Wala hakuweza kufanya mwujiza wo wote huko, isipokuwa aliweka mikono yake juu ya wagonjwa wachache, akawaponya. 6 Akastaajabu kwa sababu ya kutokuamini kwao.**

**6:1 "Akatoka huko"** Kifungu hiki kinairejelea Kaprenaumu, ambayo ilikuwa makao yake makuu ni Galilaya.

◙ **"akafika mpaka nchi "** Kiuhalisia kifungu hiki ni "sehemu ya uenyeji wake" na kinairejelea Nazareti (kama vile Marko 1:9,24), alipokulia. Mahali hapa palikuwa maili ishirini kusini mwa Kapernaumu. Kwa namna iliyo dhahiri yalikuwa makazi mapya ya Wayudea.

◙ **"wanafunzi wake wakamfuata"** Yesu aliwapa mafunzo wanafunzi wake kwa kutembea nao muda wote (tazama Robert Coleman's The Master Plan of Evangelism). Mafundi mengi ya Yesu na miujiza yake ilikuwa ni kwa ajili ya faida yao.

**6:2 "kufundisha katika sinagogi"** Mara nyingi Yesu alijihudhurisha katika sinagogi. Alialikwa mara kwa mara kuzungumza kama mwalimu mgeni, tendo ambalo lilikuwa la kawaida.

◙ **"wengi waliposikia wakashangaa"** Hawa hawakuyakubali mafundisho yake, lakini waliulizana juu ya sifa zake na kiwango cha elimu yake. Suala holi ni sawa na tendo la Wafarisayo kuuliza juu ya mamlaka yake.

◙ **"'Huyu ameyapata wapi haya'"** Hekima ya Yesu, uweza, na mamlaka vilimshangaza kila mmoja. Yesu kama mtoto alikuwa kama watoto wengine wa vijijini. Makundi tofautitofauti yaliendelea kuulizana juu ya chimbuko la maarifa haya nini chanzo cha maarifa haya? Ni dhahiri kuwa Yesu alikuwa na hekima kubwa na mamlaka kuu!

◙ **"nini miujiza hii mikubwa inayotendeka kwa mikono yake"** Kapernaumu ilikuwa maili 20 tu kutoka Nazareti hivyo habari zilizohusu miujiza yake zilienea.

**6:3 "'Huyu si yule seremala'"** Hili neno seremala linamaanisha "mhunzi" ambao unaweza kumaanisha mtengenezaji wa mbao, chuma,au jiwe. Justin anasema neno hili lilimrejelea mtu alikuwa akitengeneza plau na kamba (yaani, Dial. 88:8). Kwa namna iliyo dhahiri Yesu alikuwa seremala maarufu wa mji baada ya kifo cha Yusufu.

◙ **"'mwana wa Mariamu'"** Kama alivyo "mtu huyu" wa Marko 6:2, pengine jambo hili lilizungumzwa ili kuonyesha dharau. Watu wa mji waliifahamu habari ya mimba ya Mariamu. Origen anasema andiko halisi linasomwa "mwana wa seremala na Mariumu" kwa sababu haikuwa kawaida hata kidogo kumtaja mama. Kwa sababu ya Yohana 8:41 wengine

wanaona kuwa kifungu hiki kilihusiana na habarai zilizoenea kwa haraka kwamba Yesu alikuwa mtoto haramu wa askari wa Kirumi. Tofauti nyingi za MSS zinajikita katika mtazamo wa kithiolojia wa wakopsti ambao wangeogopa kwamba mafundisho ya Uzao wa Kibikra ulihusishwa na ufanano wa kifungu cha Mathayo "mwana wa seremala na Mariamu" (kama vile Mt. 13:55).

◙ **"'ndugu yao'"** Kifungu hiki kinaonyesha utoto wa kawaida wa Yesu (kama vile Luka 2:40,52). Pia kinaonyesha kuwa Mariamu alikuwa na watoto wengine. Kutokana na hili ndugu wa kike na kiume wanaorodheshwa (kama vile Mt. 13:55-56), wawili, Yakobo na Yuda, ni waandishi wa Agano Jipya.

**NASB "Wakajikwaa kwake"**
**NKJV "walimfedhehesha"**
**NRSV "walimwahibisha"**
**TEV "walimkataa"**
**NJB "wasingemkubali"**

Hili ni neno *skandalon*,ambalo linalomaanisha fimbo ya kunasia. Tunalipata neno la Kiingereza "aibu" kutokana na neno la Kiyunani.

Hii dhana ina umuhimu mkubwa wa Ki-masihi (kama vile Zab. 118:22; Isa. 8:14; 28:16). Kama walivyo viongozi wa kidini watu wa mji wasioushinda mtazamo wao (kama vile Marko 6:4).

**6:4 "Nabii"** Mstari wa 4 ilikuwa methali maarufu katika siku za Yesu. Kwa hakika Yesu alikuwa na zaidi ya nabii, lakini alikuwa moja ya majina yaliyotumiwa na Musa kama Mtu wa pekee wa Mungu ajaye (kama vile Kumb. 18:15,18).

**6:5 "hakuweza kufanya mwujiza wo wote huko"** Kifungu hakimaanishi kuwa Yesu alikuwa na udhaifu mahali fulani, bali kwa mapenzi yake mwenyewe aliweka mipaka ya huduma yake. Ufanano wa Mt. 13:58 una kifungu "haku" badala ya "asingeweza." Yesu hakuwa mheshimu watu; Hakuwa na nia. Luka 7:11-14 inaonyesha kwamba mara nyingi Yesu alidai mwitikio wa imani, lakini lilikuwa hitaji la awali la kawaida. Imani katika Mungu na katika Yesu hufungua milango ya ulimwengu wa roho. Ni kwa nmna gani imani si muhimu kama ilivyo kwa yule aliyeondolewa imani hiyo!

◙ **"aliweka mikono yake juu ya wagonjwa wachache"** Tazama Mada Maalum katika Marko 7:32.6:6a

**6:6a**
**NASB " Akastaajabu kwa sababu ya kutokuamini kwao"**
**NKJV "alishangaa kwa sababu ya kutokuamini kwao"**
**NRSV "alishangazwa na kutoamini kwao"**
**TEV "alishangaa sana, kwa sababu watu hawakuwa na imani"**
**NJB "alishangazwa na upungufu wao wa imani"**

Hii ni kauli tendaji elekezi isito timilifu, udiwa. Yesu alishangazwa na upofu na ugumu wa watu (Yesu alikataliwa mara mbili humo Nazareti, kama vile Luka 4:16-31). Katika uwepo wa kweli kuu, hata ishara za kimiujiza (kama vile Marko 6:2), alikataa kuamini (kama vile. Isa. 6:9-10)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 6: 6b-13**
**6b Akazunguka-zunguka katika vile vijiji, akifundisha. 7 Akawaita wale Thenashara, akaanza kuwatuma wawili wawili, akawapa amri juu ya pepo wachafu; 8 akawakataza wasichukue kitu cha njiani isipokuwa fimbo tu; wala mkate, wala mkoba, wala pesa za bindoni; 9 lakini wajifungie viatu; akasema, Msivae kanzu mbili. 10 Akawaambia, Mahali po pote mtakapoingia katika nyumba, kaeni humo hata mtakapotoka mahali pale. 11 Na mahali po pote wasipowakaribisha ninyi wala kuwasikia, mtokapo huko, yakung'uteni mavumbi yaliyo chini ya miguu yenu, kuwa ushuhuda kwao. 12 Wakatoka, wakahubiri kwamba watu watubu. 13 Wakatoa pepo wengi, wakapaka mafuta watu wengi waliokuwa wagonjwa, wakawapoza.**

**6:7 "akaanza kuwatuma wawili wawili"** Neno hili linaweza kuakisi agizo maalum na si jukumu la kiulimwengu.

◙ **"wawili wawili"** Kifungu hiki kinaweza kuwarejelea mashahidi mbili waliohitajika kuthibitisha juu ya jambo fulani (kama vile Kumb. 19:15).Pia kinaweza kuwa kipengele cha kijamii utiaji moyo katika namna ya idadi fulani. Hawa mashahidi wawili walikumbana na machafuko ya kiroho na tamaduni za kiulimwengu.

◙ **"akawapa amri juu ya pepo wachafu"** Ufanano ulio katika Luka 9:1 unaongeza "na kuponya magonjwa."Ufanano ulio katika Mt. 10:8 unaongeza "kuwaponya wagonjwa, kuwafufua wafu, kuwatakasa wakoma, kuwafukuza pepo." Matendo haya yote ni ishara za Masihi wa Agano la Kale, ishara za utunzaji wa Mungu, ishara za uweza wa Mungu na ufalme wake ujao. Tazama Mada Maalum katika Marko 1:25.

Uweza wa Yesus na mamlaka yake wanaweza kupewa wafuasi wake. Hakika kuna nguvu inayowashirikisha wale Kumi na Wawili na Yesu ambayo haiwezi kuigwa, bali nguvu ya Mungu inayopatikana katika katika kanisa lake. Katika siku zetu nguvu hii iko wapi? Inaonekana kwamba hizi nguvu zinatumika kuuthibitisha ujumbe wa injili na kumpa ubora muhubiri wa injili. Hili bado ni la kweli katika siku zetu. Hata hivyo, katika tamaduni ujumbe wa ijili umechukua asili, alafu waamini yawapasa kutembea kwa imani, si kwa kuona; kumwamini Mungu, si kudai miujiza (kama vile Yoahna 4:48). Miujiza si jibu la tatizo la imani! Pia inawezekana sana kwamba hukumu ya Mungu juu ya kanisa lililo vuguvugu ni hisia za mafanikio, lakini ukweli wa mambo yasiyo sahihi.

Ishara na miujiza pamoja na kazi za pepo na malaika ziliongezeka kwa Mitume wa wakati wa Yesu. Kazi ya kiroho hakika inawasilishwa katika kila zama, lakini ilichochewa katika ujio wa kwanza wa Yesu na ilichochewa tena kutokana na kukaribia kwa kuja kwake mara ya pili.

Nafurahi katika kudhihirisha kwa ishara za upendo na nguvu za Mungu (yaani, vipawa badao vinatenda kazi), bali kweli za injili, si uwepo au kutokuwepo kwa uthibitisho wa kimwili. Miujiza na ishara inaweza kuigwa (kama vile Mt. 24:24; 2 The. 2:9; Ufu. 13:13; 16:14; 19:20). Haiwapasi waamini kudai uthibitisho! Imani kama ya watoto ni ukuu wa kiroho kwa ishara ya nguvu ya asili na maajabu.

**6:8 "akawakataza wasichukue kitu cha njiani isipokuwa fimbo tu"** Injili za Kimuhtasari zote zinaliandika hili, lakini katika tofauti ya namna fulani. Mathayo 10:9-11 inamaanisha "wasichukue fimbo nyingine ya kutembea nayo." Luka 9:3 ni sawa na Mt. 10:10, lakini inaondoa kifungu "wasipate" cha Mt.

**10:9**. Wasafiri wote hubeba fimbo kwa ajili ya ulinzi. Hoja ya semi hizi ni kwamba hawa wamishionari iliwapasa kumtegemea moja kwa moja utoaji wa Mungu moja kwa moja (katika namna zote kimwili na kiroho) na si mali zao. Kwa mjadala kamili unaohusu tofauti kati ya Mathayo, Marko, na Luka kuhusu kitu cha kuchukuliwa na wanafunzi na kisichopaswa kuchukuliwa na wanafunzi katika umisheni wao tazama Hard Sayings of the Bible, kr. 422-24.

◙ **"mkoba"** Bila shaka hii ni shanta.

◙ **"wala pesa za bindoni"** Bila shaka inamaanisha kibindo cha pesa.

**6:9 "'Msivae kanzu mbili'"** Hii ni rejea ya joho ambalo pia lilikuwa likitumika kujifunika wakati wa kulala. Hii inamaanisha kuchukua nguo za ziada (yaani, kutokujaribu kujiandaa kwa lo lote).

**6:10 "'kaeni humo hata mtakapotoka mahali pale'"** Haikuwapasa kutafuta malazi mazuri na bora. Sehemu ya kwanza ambayo kwa imani ilifungua milango ya malazi yao ilikuwa ni eneo la kushi.

**6:11** "**mahali po pote wasipowakaribisha ninyi wala kuwasikia**" Kifungu "Mahali po pote" kinaweza kurejelea mji au sinagogi. Kiuhalisia hili neno ni "kupokea," lakini kwa maana ya kukaribisha.

◙ " **yakung'uteni mavumbi yaliyo chini ya miguu yenu kuwa ushuhuda kwao** " Hii inahusisha ishara ya sura ya mwonekano wa hukumu na utengano (kama vile Matendo 13:51; na tendo hilo hilo katika Marko 18:6). Hii ilikuwa desturi ya Kiyahudi ya kawaida wakati walipoingia Yuda kwa mara nyingine toka Samaria.

Kuna sentensi ya nyongeza katika Marko 6:11, NKJV, "Amini, amin nawaambia, itakuwa bora kwa Sodoma na Gomora katika siku ya hukumu kwa ajili ya mji" Hiki kinapatikana katika machapisho A na machapisho mengine ya Kiyunani madogo sana yaliyofuatia. Hii si halisi kwa Marko, lakini inaonekana kuwafananao kutokana na Mt.10:15.

**6:12 ". . . wakahubiri kwamba watu watubu"** Toba ni muhimu kwa ajili ya imani ya uhusiano na Mungu (kama vile Mt. 3:2; 4:17; Marko 1:15; 6:12; Luka 13:3,5; Matendo 2:38; 3:19; 20:21). Hili neno lilimaanisha mabadiliko ya matendo, ambapo katika lugha ya Kiyunani lilimaanisha mabadiliko ya kifikra. Toba ni hiari ya kubadilika kutoka maisha binafsi aliyozoea mtu hadi maisha mapya na yenye kuongozwa na Mungu. Ni wito toka katika hali ya upendeleo na utumwa wa mtu binafsi. Kimsingi huu ni mtazamo mpya, oni jipya, ukuu mpya. Toba ni mapenzi ya Mungu kwa kila mwanadamu, aliteyefanywa kwa sura yake (kama vile Eze. 18:21,23,32; Luka 13:1-5; na 2 Pet. 3:9). Kifungu cha Agano Jipya ambacho kinaakisi maneno tofautitofauti ya Kiyunani yanayohusu toba ni 2 Kor. 7:8-12

1. *lupe*, "huzuni" au "machungu" Marko 6:8 (mara mbili), 9 (mara tatu), 10 (mara mbili), 11
2. *metamelomai*, "kujali," Marko 6:8 (mara mbili), 9
3. *metanoeō*, "kutubu," "akilini," Marko 6:9, 10

Tofauti ni toba isiyo ya kweli [*metamelomai*], kama vile Yuda, Mt. 27:3 na Esau, Heb. 12:16-17 dhidi ya imani ya kweli [*metanoeō*].

Imani ya kweli kithiolojia inahusianishwa na

1. Yesu kuhubiri juu ya amri za Agano Jipya (kama vile Mt. 4:17; Marko 1:15; Luka 13:3,5)
2. hotuba za kimitume katika Matendo (yaani, *kerygma*, kama vile Matendo 3:16,19; 20:21)
3. uweza wa karama za Mungu (kama vile Matendo 5:31; 11:18 na 2 Tim. 2:25)
4. kupotea (kama vile 2 Pet. 3:9). Toba si ya hiari

Tazama MADA MAALUM: TOBA KATIKA AGANO LA KALE katika Marko 1:4d.

**6:13 "Wakatoa pepo wengi, wakapaka mafuta watu wengi waliokuwa wagonjwa"**
Tambua kuwa Agano Jipya inatengeneza tofauti kati ya magonjwa na umiliki wa mapepo. Tazama maelezo katika Marko 1:25c.

◙ "**wakapaka mafuta**" Mafuta yalikuwa yakitumika katika maana tofautitofauti: (1) kama mafuta (kama vile Yakobo 5:14); (2) kama vile ishara ya Roho Mtakatifu, hasa kwa wafalme wa Agano la Kale, makuhani, na manabii; na (3) kama msaada wa kisaikolojia wa kuutambua msaada wa uwepo wa Mungu. Yesu aliitumia aina za kimwili kadhaa na tofautitofauti katika uponyaji.

## MADA MAALUMU: KUTIWA MAFUTA KATIKA BIBLIA

(Kitenzi cha Kiebrania, BDB 602, KB 643 I; nomino, BDB 603)

A. Yalitumika kwa ajili ya urembeshaji (BDB 691 I. kama vile Kumb. 28:40; Ruthu 3:3; 2 Sam. 12:20; 14:2; 2 Nya. 28:15; Dan. 10:3; Mik. 6:15)
B. Yalitumika kwa ajili ya wageni (BDB 206, kama vile Zab. 23:5; Luka 7:38,46; Yohana 11:2)
C. Yalitumika kwa ajili ya uponyaji (BDB 602, kama vile Isa. 61:1; Marko 6:13; Luka 10:34; Yakobo 5:14) [yalitumika kwa maana ya tiba na kinga katika Eze. 16:9]
D. Yalitumika katika maandalizi ya mazishi (kama vile Marko 16:1; Yohana 12:3,7; 19:39-40; 2 Nya. 16:14, lakini likiwa bila kitenzi "kutiwa mafuta")
E. Yalitumika katika maana ya kidini (ya jambo, BDB 602, kama vile Mwa. 28:18; 31:13 [nguzo]; Kut. 29:36 [madhabahu]; Kut. 30:26; 40:9-16; Law. 8:10-13; Hes. 7:1 [hema])
F. Yalitumika kuwasimika viongozi
   1. Makuhani
      a. Haruni (Kut. 28:41; 29:7; 30:30)
      b. Wana wa Haruni (Kut. 40:15; Law. 7:36)
      c. waliowekwa wakfu (Hes. 3:3; Law. 16:32

2. Wafalme
    a. Na Mungu (kama vile 1 Sam. 2:10; 2 Sam. 12:7; 2 Fal. 9:3,6,12; Zab. 45:7; 89:20)
    b. Na manabii (kama vile 1 Sam. 9:16; 10:1; 15:1,17; 16:3,12-13; 1 Fal. 1:45; 19:15-16)
    c. Na makuhani (kama vile 1 Fal. 1:34,39; 2 Fal. 11:12)
    d. na wazee (kama vile Amu. 9:8,15; 2 Sam. 2:7; 5:3; 2 Fal. 23:30)
    e. juu ya Yesu kama mfalme wa Kimasihi
    (kama vile Zab. 2:2; Luka 4:18 [Isa. 61:1]; Matendo 4:27; 10:38; Heb. 1:9 [Zab. 45:7])
    f. wafuasi wa Yesu (kama vile 2 Kor. 1:21; 1 Yohana 2:20,27 [mafuta)
3. Juu ya manabii kadri iliyowezekana (kama vile 1 Fal. 19:16; Isa. 61:1)
4. Kuvikomboa vyombo visivyoaminika vya ki-Uungu
    a. Koreshi (kama vile Isa. 45:1)
    b. Mfalme wa Tiro (kama vile Eze. 28:14, ambapo alitumia stirahi za Bustani ya Edeni)
5. Neno au cheo "Masihi" maana yake ni "Mtiwa mafuta" (BDB 603), kama vile Zab. 2:2; 89:38; 132:10

Matendo 10:38 ni mstari ambapo nafsi tatu za Uungu zinazwekwa pamoja katika kutiwa mafuta.Yesu alipakwa mafuta (kama vile Luka 4:18; Matendo 4:27; 10:38). Dhana inapanuliwa ili kuwajumuisha waamini wote (kama vile 1 Yohana 2:27). Mpakwa mafuta anakuwa wapakwa mafuta! Hii inaweza kuwa sambamba na Mpinga Kristo na wapinga kristo (kama vile 1 Yohana 2:18). Tendo la ishara ya Agano la Kale la kumiminiwa mafuta mwilini (kama vile Kut. 29:7; 30:25; 37:29) linahusiana na wale walioitwa na kuandaliwa na Mungu kwa kazi maalumu (yaani, manabii, makuhani, na wafalme). Neno "Kristo" ni tafsiri ya neno la Kiebrania "mpakwa mafuta " au Masihi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 6:14-16**
**[14] Naye Mfalme Herode akasikia habari; kwa maana jina lake lilikuwa kutangaa, akasema, Yohana Mbatizaji amefufuka katika wafu, na kwa hiyo nguvu hizi zinatenda kazi ndani yake. [15] Wengine walisema , Ni Eliya. Wengine walisema, Huyu ni nabii, au ni kama mmoja wa manabii. [16] Lakini Herode aliposikia, alisema, Yohana, niliyemkata kichwa, amefufuka.**

**6:14 "**Mfalme Herode" Jina la "Mfalme" halikuwa jina maalum la Herode Antipasi. Huyu aliitwa Tetrarch, ambapo ilimaanisha "tawala mara nne." Huyu alikuwa mwana wa Herode Mkuu na mwanamke Msamaria. Aliitawala Perea na Galilaya kati ya 4 k.k. na b.k. 39 pale alipopelekwa uhamishoni baada ya kumuomba Kaizari kuwa Mfalme.Tazama Mada Maalum inayohusu Nuymba ya Herode Mkuu katika Marko 1:14.

◙ **"Mbatizaji amefufuka katika wafu"** Kifungu hiki kinaakisi imani ya Kifarao katika ufufuo wa kimwili (kama vile Matendo 23:6; 24:21; Ebr. 6:2). Hii ilikuwa juhudi na ya kueleza juu ya uweza na mamlaka ya Yesu (yaani., viongozi wa kidini kulihusianisha hili na Shetani au mapepo; wenyeji wa mji walilikataa hili kwa sababu ya kuufahamu sana utoto wa Yesu ; watu hawa walilihusianisha na Yohana Mbatizaji au manabii wengine wa Agano la Kale).

**6:15 "Eliya"** Hili lilionyesha maana za ki-Masihi za huduma ya Yesu. Hili linahusiana na utabiri wa Mal. 3:1-2 na 4:5-6.

◙ **"Huyu ni nabii, au ni kama mmoja wa manabii"** Jambo hili linaonyesha kuwa watu walikuwa na hisia za mamlaka mpya katika mafundisho yake ambayo hakuwa katika Israeli kwa mamia ya miaka, tangu Malaki (au mwandishi wa Mambo ya Nyakati). Pia lianaakisi unabii wa Sheria ya Musa wa Kumb. 18:15 na kuendelea kuhusu nabii ajaye kama Musa.

**6:16 "niliyemkata"** Kifungu hiki kinaonyesha hatia ya dhamiri ya Herode (kama vile Mt. 14:10; Luka 9:9) na uhaba wa taarifa kuhusu uhusiano kati ya Yohana na Yesu

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 6:17-29**
**[17] Kwa maana Herode mwenyewe alikuwa ametuma watu, akamkamata Yohana, akamfunga gerezani, kwa ajili ya Herodia, mkewe Filipo ndugu yake, kwa kuwa amemwoa; [18] kwa sababu Yohana alimwambia Herode, Si halali kwako kuwa na mke wa nduguyo. [19] Naye yule Herodia akawa akimvizia, akataka kumwua, asipate. [20] Maana**

**Herode alimwogopa Yohana; akimjua kuwa ni mtu wa haki, mtakatifu, akamlinda; na alipokwisha kumsikiliza alifadhaika sana; naye alikuwa akimsikiliza kwa furaha. [21] Hata ilipotokea siku ya kufaa, na Herode, sikukuu ya kuzaliwa kwake, alipowafanyia karamu wakubwa wake, na majemadari, na watu wenye cheo wa Galilaya; [22] ndipo binti yake yule Herodia alipoingia, akacheza, akampendeza Herode na wale walioketi pamoja naye karamuni. Mfalme akamwambia yule kijana, Niombe lo lote utakalo, nitakupa. [23] Akamwapia, Lo lote utakaloniomba nitakupa, hata nusu ya ufalme wangu. [24] Basi akatoka, akamwuliza mamaye, Niombe nini? Naye akasema, Kichwa cha Yohana Mbatizaji. [25] Mara akaingia kwa haraka mbele ya mfalme, akaomba akisema, Nataka unipe sasa hivi katika kombe kichwa cha Yohana Mbatizaji. [26] Mfalme akafanya huzuni sana, lakini kwa ajili ya viapo vyake, na kwa ajili ya hao walioketi karamuni, hakutaka kumkatalia. [27] Mara mfalme akatuma askari, akaamuru kuleta kichwa chake. Basi akaenda, akamkata kichwa mle gerezani, [28] Akakileta kichwa chake katika kombe, akampa yule kijana, naye yule kijana akampa mamaye. [29] Wanafunzi wake waliposikia habari, walikwenda, wakauchukua mwili wake, wakauzika kaburini.**

**6:17-29** Hili liko nje ya mtiririko wa mfululizo wa matukioe. Hili liliwekwa kwa ajili ya kutoa maelezo ya Marko 6:14.

**6:17 "Herodia"** Huyu alikuwa mke wa Filipi, ndugu yake Herode Antipasi (kama vile Mt. 14:3). Hawa waliishi Rumi. Huyu alikuwa mpwa wa Antipasi kupitia Aristobulus. Antipasi alimwacha na Filipandi akamuoa.

Kulingana na Josephus (yaani., moja ya watu kale wa Wayahudi 18.5.4), Herodia aliolewa na mwana wa Herode Mkuu, Herode (ambaye mama yake alikuwa Marianne, binti wa kuhani mkuu). Pia anasema binti wa Herodia, Salome, baadaye aliolewa na Filipi. Inawezekana kwamba Herode alijulikana kama Herode Filipi.

**6:18** Uhusiano huu ulienda kinyume na Law. 18:16; 20:21.

**6:19 "Herodia akawa akimvizia"** Hii ni kauli ya wakati uliopo usiyo timilifu. Huyu alizimika kurudiarudia suala lile lile kwa Herode Antipasi. Herode (kauli ya wakati uliopo usio timilifu) alimficha mbali naye (Marko 6:20).

**6:20 "Herode alimwogopa Yohana"** Hi ni kwa sababu Yohana alikuwa mtu mtakatifu. Mathayo 14:4 inasema kuwa huyu aliuogopa umaarufu wa Yohana kwa watu. Herode alikuwa mtu wa woga. Alimwogopa sana Yohana, Herodia, na wwageni lakini hakumwogopa Mungu!

**6:21** Kuna makundi matatu ya wageni: (1) mamlaka za kiraia; (2) mamlaka za kijeshi; na (3) matajiri wenyeji na viongozi maarufu.

◙ **"ilipotokea"** Kwa vyo vyote Herode alimwita Yohana au alikwenda gerezani huko Machaerus (yaani., upande wa mashariki mwa Bahari Tuli, kama vile Josephus' Antiquities 18.5.2).

◙ **"alifadhaika sana; naye alikuwa akimsikiliza kwa furaha"** Hili linaonyesha fumbo la kwenda tofauti na ukweli, ambao bado wanaendelea kuikataa nuru (kama vile Yohana 3:19-21).

Herodia alisubiri hadi wakati ulipofika—wa kusanyiko la hadhara, karamu ya kilevi, karamu isiyo halali, na ahadi ya aibu—kuulazimisha mkono wa Herode kufanya matakwa yake.

**6:22 "binti yake yule Herodia"** Josephus, alimwita Salome binti wa Filipi.

◙ **"akacheza"** Haikuwa kawaida kwa wanawake wa jamii yake kucheza katika kusanyiko la aina hii. Hizi taratibu hizi za kucheza mara nyingi zililikuwa zikifanywa na makahaba au wachezaji maarufu.

◙ **"'Niombe lo lote utakalo, nitakupa'"** Herode alilisema hili mbele ya wakuu wa utawala na asingeritengua (kama vile Marko 6:21,26).

**6:23 "Akamwapia"** Alilitumia jina la Mungu ili kuthibitisha uhakika wake.

**6:24** Mstari huu unathibitisha juu ya shauku na mpango wa mama yake uliyojificha (kama vile Marko 6:28b).

**6:26** Hitaji la Herode la kuwashangaza marafiki zake na nyumba yake lilitabiri woga wake (*perilupos*, ambao ni uchungu uliozidi kipimo, kama vile Mt. 26:38; Marko 14:34).

**6:27 "askari"** Hili ni neno la Kilatini la walinzi maalum. Kwa uhalisia wake linarejelea kuchunguza, lakini lilikuja kutumika kumaanisha mwuuaji (yaani, Seneca). Marko lina maneno na vifungu mengi va Kilatini kuliko Injili nyingine. Huenda liliandikwa maalum kwa Warumi.

◙ **"gerezani"** Katika Antiquities 18.5.2 Josephus anatwambia kuwa hii ilikuwa ngome ya Herode iliyoitwa Machaerus, ambayo ilikuwa karibu na Bahati ya Chumvi humo Moabu.

**6:29** Ni dhahiri kuwa Yohana Mbatizaji alikuwa katika mapenzi ya Mungu. Huduma yake ilidumu kwa miezi ipatayo kumi na nane. Ingawa sababu halisi ya kifo chake ilikuwa ni kumkemea mwanamke mwovu, Mungu alikuwa katika utawala wake wa historia kwa ajili ya makusudi yake. Mstari huu pia uliakisi hofu ya Kiyahudi juu ya mazishi sahihi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 6:30-44**
**30 Na mitume wakakusanyika mbele ya Yesu; wakampa habari za mambo yote waliyoyafanya, na mambo yote waliyoyafundisha. 31 Akawaambia, Njoni ninyi peke yenu kwa faragha, mahali pasipokuwa na watu, mkapumzike kidogo. Kwa sababu walikuwako watu wengi, wakija, wakienda, hata haikuwapo nafasi ya kula. 32 Wakaenda zao faragha mashuani, mahali pasipokuwa na watu. 33 Watu wakawaona wakienda zao, na wengi wakatambua, wakaenda huko mbio kwa miguu, toka miji yote, wakatangulia kufika. 34 Naye aliposhuka mashuani, akaona mkutano mkuu, akawahurumia; kwa sababu walikuwa kama kondoo wasio na mchungaji; akaanza kuwafundisha mambo mengi. 35 Hata zilipopita saa nyingi za mchana, wanafunzi wake walimwendea, wakasema, Mahali hapa ni nyika tupu, na sasa kunakuchwa; 36 uwaage watu hawa, ili waende zao mashambani na vijijini kandokando, wakajinunulie chakula. 37 Akajibu, akawaambia, Wapeni ninyi chakula. Wakamwambia, Je! Twende tukanunue mikate ya dinari mia mbili ili tuwape kula? 38 Akawaambia, Mnayo mikate mingapi? Nendeni mkatazame. Walipokwisha kujua wakasema, Mitano, na samaki wawili. 39 Akawaagiza wawaketishe wote, vikao vikao, penye majani mabichi. 40 Wakaketi safu safu, hapa mia hapa hamsini. 41 Akaitwaa ile mikate mitano na wale samaki wawili, akatazama mbinguni, akashukuru, akaimega ile mikate, akawapa wanafunzi wake wawaandikie; na wale samaki wawili akawagawia wote. 42 Wakala wote wakashiba. 43 Wakaokota vipande vilivyomegwa vya kuweza kujaza vikapu kumi na viwili; na vipande vya samaki pia. 44 Na walioila ile mikate wapata elfu tano wanaume.**

**6:30 "mitume"** Haya ni matumizi pekee ya neno hili katika Injili ya Marko. Mara nyingi aliwahita "wanafunzi." Neno "Mitume" linatokana na maana ya neno la Kiyunani "kutuma" (*apostellō*). Yesu aliwachagua wanafunzi wake kumi na wawili kuwa pamoja naye katika maana maalum na kuwaita mitume" (kama vile Luka 6:13). Hiki kitenzi mara nyingi kilitumiwa na Yesu kumaanisha kuwa alitumwa toka kwa Baba (kama vile Mt. 10:40; 15:24; Marko 9:37; Luka 9:48; Yohana 4:34;5:24,30,36,37,38;6:29,38,39,40,57; 7:29; 8:42; 10:36; 11:42; 17:3,8,18,21,23,25; 20:21). Katika nyenzo za Kiyahudi, hili neno lilitumika juu ya mtu aliyetumwa kama mwakilishi maaum wa mwingine, sawa na "barozi." Hawa walitenda kazi katika maagizo ya safari hii kama wawakilishi wa Yesu. Nguvu zao na mamlaka yao yalikuwa ya kupewa.

◙ **"wakakusanyika mbele ya Yesu"** Hii ni sehemu ya mafundisho ya Yesu. Aliwafundsha, aliwaonyeha namna, aliwatumat, na aliwauliza maswali. Hivi ndivyo walivyojifunza. Tazama Robert Coleman's The Master Plan of Evangelism, kitabu ambacho kinanukuu na kuonyesha utekelezaji wa mafundisho ya Yesu kwa wanafunzi / mitume wake .

**6:31** Kama Yesu alivyohitaji kujitenga na makutano (kama vile Marko 3:20), na sasa walifanya hivyo wanafunzi wake. Kwa masaa ishirini na nne kwa siku watu walikuja kwa ajili ya kupata msaada. Mafundisho yao hayakukamilika. Walihitaji muda wa ziada na wati maalum!

**6:32 "mashuani"** Hili neno mara nyingi linarejelea mtumbwi mkubwa wa uvuviu, ambao ungekuwa na uwezo wa kubeba watu kumi na tatu (kama vile Mt. 4:21-22; 823; Matendo 21:2-3), lakini pia linatumika kumaanisha mashua ndogo ndogo (kama vile Luka 5:2).

**6:33 "wakaenda huko mbio kwa miguu, toka miji yote"** Je! Unaweza kufikiri ni makutano makubwa kiasi gani ya wagonjwa, viwate, na watu waliodadisi waliokuwa wakitoka pembezoni? Watu hawa walikuwa na hofu.

**6:34 "akawahurumia"** Mara nyingi Yesu alikuwa na muda wa kukutana na watu wahitaji (kama vile Mt. 9:36).

◙ **"kama kondoo wasio na mchungaji"** Hii stiari ina msingi wa Agano la Kale (kama vile Hes. 27:17; Eze. 34:5; Zek.13). Hili linaweza kuwa dokezo la maneno ya Yesu yaliyoifichwa katka Yohana 10.

◙ "**akaanza kuwafundisha**" Mwitikio wa Yesu makutano ya wahitaji ulikuwa kwa ajili ya mafundisho. Walihiytaji utimilifu wa kiroho, si urejesho wa kimwili. Yesu alikutana na mahiotaji yote mawili (kama vile Mt. 14:14).

**6:35 "'Mahali hapa ni nyika tupu'"** Hapa ni "mahali palipojitenga" pa Marko 6:31.

**6:37 "'Wapeni ninyi chakula'"** Yesu alikuwa akiijaribu imani ya wanafunzi wake. Kwa namna iliyo dhahiri walikuwa wakilitafuta tatizo, na sasa wanakutana nalo!

◙ **"dinari mia mbili"** Dinari mara nyingi ilkuwa ujira wa vibarua wa kawaida (kama vile Mt. 20:2) au wanajeshi.

**6:38 "'Mitano, na samaki wawili'"** Hata wao wenyewe wasingetoshelezwa. Yesu aliitumia nafasi hii kuwaonyesha wanafunzi kwamba yale waliokuwa nayo yalikuwa yanatosha na kuzidi ikiwa angepewa yeye ikiwa wangemwamini!

**6:39 "wawaketishe wote, vikao vikao"** Hii ni nahau (yaani., kifasihi *sumpinō*, *sumpinō, company, company*) zilimaanisha "kuwa tayari kwa ajili ya kula!" Yesu anaonekana kuwaagiza wanafunzi kuyaweka tayari makutano kwa mgawanyo wa chakula katika muundo wa kawaida.

◙ **"penye majani mabichi"** Huu ni ushahidi wa macho wa maelezo ya Petro. Hii pia inaweza kumaanisha kipindi karibia na Sikukuu ya Pasaka katika majira ya kuchipua.

**6:41 "akatazama mbinguni"** Kawaida ya maombi ya Kiyahudi ilikuwa ilikuwa ni kusimama na kuinua mikono na kicha kuinuliwa juu huku macho yakiwa yamefunguliwa. Yesu alikuwa akionyesha kuwa chanzo cha mamlaka yake ni Baba wa mbinguni.

◙ **"akaimega. . . akawapa wanafunzi"** Hii ni kauli ya wakatai uliopo na kauli ya wakati usio timilifu. Muujiza wa mazidisho ulitokea katika mikono ya Yesu. Ufanano ulio katika Yohana 6 unatengeneza matarajio ya kithiolojia ya umati huu. Wayahudi wa siku za Yesu walimtarajia Masihi kwa ajili ya kuwapa chakula kama alivyofanya Musa kipindi cha kutangatanga jangwani (kama vile Yohana 6:30-40). Yesu anawapa ishara kuu waliyoihitaji, lakini hawakuwa na uwezo, au wasingeweza kuiona.

**6:42** Usemi huu unatumika katai Agano la Kale ya Kiebrania (yaani., tafsri ya Kiyunani ya Agano la Kale ) kwa watu wa Agano la Kale waliolishwa kwa manna na karamu (kama vile Zab. 78:29; 105:40). Huu ujumbe wa Agano la Kale linaendelezwa katika Yohana 6:30- 40, ambapo matarajio ya walimu wa sheria za Kiyunani ya kugawa chakula kama Musa alivyofanya. Yesu ni Musa mpya; Ukombozi wake ni uhamisho mpya; na unaleta zama mpya za wingi (kama vile Zab. 132:15; Isa. 49:10).

**6:43 " vipande vilivyomegwa vya kuweza kujaza vikapu kumi na viwili; na vipande vya samaki pia**" Kifungu hiki kinaonyesha kwamba Yesu hakufanya miujiza kwa ajiali ya chakula cha siku hiyo. Iliwapasa kukitunza kile walichokuwa nacho kwa ajili ya siku inayofuatia. Baadhi ya watoa maoni (William Barclay) wanakanusha suala la kimiujiza na kudai

kwamba mvulana huyo alishiriki chakula (kama vile Yohana 6:9) na kwamba wengine waliokuwa kataika umati waliliona hili na kuishiriki milo yao. Ikiwa ni hivyo, hivyo vikapu kumi na viwili vilitoka wapi? Upendeleo wetu unaathiri fasiri yetu katika namna inayofanana upendeleo wa watu wa siku za Yesu uliowaathiri!

**6:44 "elfu tano wanaume"** Hii ni sababu ya muda mrefu (kama vile Marko 6:33) na eneo lililojitenga (kama vile Marko 6:32). Huenda hapakuwepo wanawake na watoto wengi. Hatukijui kiwango kamili cha mkutano. Yalikuwa Makubwa!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 6:45-46**
**45 Mara akawalazimisha wanafunzi wake wapande mashuani, watangulie kwenda ng'ambo hata Bethsaida, wakati yeye alipokuwa akiwaaga mkutano. 46 Hata alipokwisha kuagana nao akaenda zake mlimani kuomba.**

**6:45 "Bethsaida"** Hili ni jina la mji lenye kumaanisha "nyumba ya nuru" Eneo hili lilikuwa upande wa masharaiki wa bahari.

◙ "**yeye alipokuwa akiwaaga mkutano**" Ufanano katika Yohana 6 una habari nyingi zaidi kuhusu mwitikio wa makutano haya. Hoja za Marko ni mafundisho ya wanafaunzi na huruma ya Yesu, ambapo maelezo ya Yohana yananukuu namna Yesu alivyokamilisha matarajio ya Kiyahudi kuhusu Masihi kuwalisha Wayahudi kama Musa alivyo fanya (yaani, manna). Hawa walijaribu kumfanya mfalme. Hili linaonyesha kutokuelewa kwao kuhusu maagizo ya Yesu (yaani., kama wanafunzi wake, Nyumba yake, na viongozi wa kidini).

**6:46 "akaenda zake mlimani kuomba"** Yesu alikuwa na muda wa ziada. Kifungu hiki kilikuwa dhahiri hasa katika Injili ya Luka. Yesu aliujua kuwa muujiza huu usingeeleweka kwao. Kadri alivyokwepa kuponya, Hakutaka kuwa kuwa mlishaji (kama vile Yohana 6:15). Alikuja kumfunua Baba, lakini makutano wasingeweza au wasingeona. Katika maana hii huu ni utimilifu wa jaribu la Shetani katika jangwa la watu kujaribiwa kwa mkate (yaani., ulishaji wa asili, kama vile Mt. 4:3-4)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 6:47-52**
**47 Na kulipokuwa jioni mashua ilikuwa katikati ya bahari, na yeye yu peke yake katika nchi kavu. 48 Akawaona**
**wakitaabika kwa kuvuta makasia, kwa maana upepo ulikuwa wa mbisho; hata ilipopata kama zamu ya nne ya usiku**
**akawaendea, akitembea juu ya bahari; akataka kuwapita. 49 Nao walipomwona anatembea juu ya bahari, walidhani**
**ya kuwa ni kivuli, wakapiga yowe, 50 kwa kuwa wote walimwona, wakafadhaika. Mara akasema nao, akawaambia,**
**Changamkeni; ni mimi, msiogope. 51 Akapanda mle chomboni walimo; upepo ukakoma; wakashangaa sana mioyoni**
**mwao; 52 kwa maana hawakufahamu habari za ile mikate, lakini mioyo yao ilikuwa mizito.**

**6:48 "Akawaona"** Haijulikani kama hili lilikuwa tendo (1) kuona kimwili au (2) maarifa ya asili.

◙ **"wakitaabika kwa kuvuta makasi"** Kifungu hiki kinatokana na Kiyunani kilicho katika Kiingereza kama "maumivu." Ni vigumu kugoa nanga dhidi ya upepo.

◙ **"zamu ya nne ya usiku"** Katika masaa ya Kirumi kifungu hiki kingeweza kuwa saa tatu 3:00 usiku hadi 6:00 saa sita.

◙ **"akawaendea, akitembea juu ya bahari"** Hii ni asili nyingine ya muujiza wa Yesu kwa kusudi la kuimarisha imani ya wanafunzi. Hawa waliushuhudia uweza na mamlaka katika njia nyingi na tofautitofauti. Lakini bado hakuendelea kuamini; bado waliendelea kutokuamini (kama vile Marko 6:49-50) na walishangazwa (kama vile Marko 6:51). Inawezekana kwamba muujiza huu ulimaanisha kukamilisha Yakobo 9:8; 38:16; Zab. 77:19; na Isa. 43:16. Yesu alitenda matendo ya ki-Ungu toka Agano la Kale (kama vile Marko 6:52).

◙ **"akataka kuwapita"** Kifungu hiki hakionekani kuendana na muktadha isipokuwa kinamaanisha kuunganishwa na Ayubu 9:8 na 11! Katika tambihi ya toleo la TEV kuna kifungu "alijiunga nao" Hiki kitenzi kinamaana nyingine katika Luka 12:32 na 17:7.

**6:49 "kivuli"** Kiuhalisia hili neno linamaanisha "zimwi" kama katika Mt. 14:26. Hili ni lenye mkazo linalotumika kumaanisha "hofu ya kiakili na kiroho vurugu" (kama vile The Greek-English Lexicon of Bauer, Arndt, Gingrich, na Danker, uk. 805).

**6:50 "'Changamkeni '"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakataia uliopo inayotumiwa na Yesu Mara nyingi (kama vile Mt. 9:2,22; 14:27; Marko 6:50; 10:49; Yohana 16:33; Matendo 23:11).

◙ **"msiogope'"** Hii kauli ya kati (yenye ushshidi) shurutishi ya wakatai timilifu pia inatumiwa na Yesu mara kwa mara (kama vile Mt. 14:27; 17:7; 28:10; Marko 6:50; Luka 5:10; 12:32; Yohana 6:20; Ufu. 1:17). Kwa mara nyingine neno hili linaweza kumuhusiana Yesu na Musa (kama vile Kut. 14:13; 20:20). Yesu alikuwa Musa au mnenaji wa ki-Uungu (kama vile Mwa. 15:1; Yos. 8:1).

**6:51** Kwa uthihirisho wa kutokuwepo ni ufafanuzi wa kutembea kwa Petro (na kuzama) juu ya maji (kama vile Mt. 14:28-31). A. T. Robertson's *Word Pictures in the New Testament*, juzuu 1, uk. 319, lina kifungu "Huenda Petro hakuwa mpenzi wa kusimulia simulizi hili."

**6:52 "maana hawakufahamu"** Hawa walikuwa na uwezo mdogo wa kujifunza. Yesu aliwavumilia. Hili linanitia moyo!

◙ "**mioyo yao ilikuwa mizito**" Hii ni kauli tendwaji endelevu ya wakati timilifu.Hii dhana ya kithiolojia ni ngumu . Je! Hili linamaanisha (kwa kauli tendaji) kwamba Mungu au Roho alikuwa karibu na fikra zao? Huenda hii ni asili ya upendeleo wao binafsi na desturi za Kiyahudi zilizowashangaza kueleka kweli ambayo ni dhahiri sana katika msingi wa maisha ya Yesu (kama vile Marko 8:17-18). Hili neno "mtu" halikuendana na kipengele cho chote walicho kifahamu (kama vile Marko 4:13,40; 7:18). Hii ni dhamira ya mara kwa mara katika Marko. Tazama MADA MAALUM: MOYO katika Marko 2 :6

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 6: 53-56**
[53] **Hata walipokwisha kuvuka, walifika nchi ya Genesareti, wakatia nanga.** [54] **Nao wakiisha kutoka mashuani, mara watu walimtambua,** [55] **wakaenda mbio, wakizunguka nchi ile yote, wakaanza kuwachukua vitandani walio hawawezi, kwenda kila mahali waliposikia kwamba yupo.** [56] **Na kila alikokwenda, akiingia vijijini, au mijini, au mashambani, wakawaweka wagonjwa sokoni, wakamsihi waguse ngaa pindo la vazi lake; nao wote waliomgusa wakapona.**

**6:55** Hili linaonyesha uhitaji, ghasia, na huruma na uweza wa Yesu. Pia huu ulikuwa mfano wa kipaumbele cha watu. Mara nyingi Yesu alitoa muda mwingi kwao.

**6:56 "pindo la vazi lake"** Kifungu hiki kinarejelea juu ya "maombi ya shara" (kama vile Hes. 15:38-40; Kumb. 22:12). Watu hawa walikuwa na hofu na hali ya kutofikiri na ubinafsi.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe zaBiblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni kwa namna gani mnaweka ulinganifu kati ya Injili tofauti tofauti?
2. Kwa nini kuna tofauti ya maoni kuhusu Yesu ni nani?
3. Je! Ufufuo ilikuwa dhana ya kawaida ya siku za Yesu?
4. Kwa nini Mugu alilihusu kuchukiwa, mwanamke mwovu kusababisha kifo cha mtu mkubwa kama Yohana?
5. Kwa nini Yesu aliyavutia makutano makubwa kiasi hiki?
6. Kwa nini Yesu alilisha 5,000?
7. Ni kwa namna gani huduma ya mafundisho ya Yesu yalihusiana na uponyaji wake

# MARKO 7

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Desturi za wazee | Unajisi huja toka ndani | Desturi za wazee | Mafundisho ya wazee | Desturi za Mafarisayo |
| 7:1-13 | 7:1-23 | 7:1-8 | 7:1-2 | 7:1-13 |
| | | | 7:3-4 | |
| | | | 7:5 | |
| | | | 7:6-7 | |
| | | | 7:8 | |
| | | 7:9-13 | 7:9-13 | |
| | | | Vitu vimfanyavyo Mtu Kuwa najisi | Juu ya najisi na visivyo najisi |
| 7:14-23 | | 7:14-16 | 7:14-16 | 7:14-16 |
| | | 7:17-23 | 7:17-19 | 7:17-23 |
| | | | 7:20-23 | |
| Mwanamke ni Msirofoinike | Yule Myunani alionyesha imani yake | Mwanamke ni Msirofoinike | Imani ya Yule mwanamke | Binti ya mwanamke Msirofoinike Aponywa |
| 7:24-30 | 7:24-30 | 7:24-30 | 7:24-27 | 7:24-30 |
| | | | 7:28 | |
| | | | 7:29 | |
| | | | 7:30 | |
| Mtu kiziwi na Mwenye utasi Aponywa | Yesu amponya kiziwi | Uponyaji | Yesu amponya kiziwi | Uponyaji wa mtu kiziwi |
| 7:31-37 | 7:31-37 | 7:31-37 | 7:31-34 | 7:31-37 |
| | | | 7:35-37 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka "mwongozo wa usomaji mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na RohoMtakatifu nivipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## UFANANO WA VIDOKEZO VYA INJILI

A. Marko 7:1-23 inafanana na Mt. 15:1-20
B. Marko 7:24-30 inafanana na Mt. 15:21-28
C. Marko 7:31-8:9 inafanana na Mt. 15:29-38

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 7:1-8**
[1]**Kisha Mafarisayo, na baadhi ya waandishi waliotoka Yerusalemu, wakakusanyika mbele yake,** [2]**wakaona wengine katika wanafunzi wake wakila vyakula kwa mikono najisi, yaani, isiyonawiwa.** [3]**Kwa maana Mafarisayo na Wayahudi wote wasiponawa mikono mpaka kiwiko, hawali, wakishika mapokeo ya wazee wao;** [4]**tena wakitoka sokoni, wasipotawadha, hawali; na yako mambo mengine waliyopokea kuyashika, kama kuosha vikombe, na midumu, na vyombo vya shaba.** [5]**Basi wale Mafarisayo na waandishi wakamwuliza, Mbona wanafunzi wako hawaendi kwa kuyafuata mapokeo ya wazee, bali hula chakula kwa mikono najisi?** [6]**Akawaambia, Isaya alitabiri vema juu yenu ninyi wanafiki, kama ilivyoandikwa, Watu hawa huniheshimu kwa midomo Ila mioyo yao iko mbali nami;** [7]**Nao waniabudu bure, Wakifundisha mafundisho Yaliyo maagizo ya wanadamu,** [8] **Ninyi mwaiacha amri ya Mungu, na kuyashika mapokeo ya wanadamu.**

**7:1 "Mafarisayo"** Hawa walikuwa ni viongozi wa kuaminika katika nyakati zao. Kiutamaduni walikuwa bora zaidi. Mazungumzo ya Yesu na wao mara nyingi yaliandikwa (kama vile Marko 7:5-8; 11:27-33; 12:13-17). Tazama muhtasari katika Marko 2:6.

◙**" baadhi ya waandishi waliotoka Yerusalemu"** mara zote viongozi wa kidini walimfuata ili kupata makosa (kama vile. Marko 3:22; Yn 1:19). Ni dhahili walikuwa ni watafuta makosa waliotoka katika baraza la kiyahudi (tazama mada maalumu katika Marko 12:13) la Yerusalem. Baraza hili liliundwa na watu 70 kutoka

1. Familia za kikuhani zinazoongoza (yaani., Masadukayo , tazama mada maalumu katika Marko 12:18)
2. Viongozi wa kidini wa mahali (yaani , Mafarisayo)
3. Matajiri wanaomiliki ardhi

**7:2 "kwa mikono najisi,yaani isiyonawiwa"** hii sio safi, lakini kidini (kama vile. Marko 7:4). Sherehe ya utakaso ilikuwa ni jambo la muhimu sana kwao (kama vile. Luka 11:38; Mat. 15:2). Limetamkwa kwa maneno ya kipekee sana katika kitabu cha sheria na maadili ya Kiyahudi. Mabishano yapo juu ya desturi ya fasihi simulizi, ambayo yametafsiriwa katika maandiko ya Agano la kale.

◙**"najisi"** hili ni neno la Kigiriki *koinos*,ambalo linamaanisha "kawaida" au "patikana kwa wote." Ni jina la kisasa ambalo lilitolewa na Wagiriki nyakati za Yesu. Neno la Kilatini "vulgate" lina vidokezo sawa (yaani patikana kwa wote). Katika muktadha huu linarejelea kwamba ni sherehe za utakaso kwa sababu ya kushika vitu vilivyo najisi.

**7:3**
**NASB** **" wasiponawa mikono mpaka kiwiko "**
**NKJV** **"wasiponawa mikono yao kwa njia maalumu**
**NRSV** **"wasiponawa kikamilifu mikono yao"**
**TEV** **"wasiponawa mikono yao kwa njia sahihi**
**NJB** **"wasipo osha mikono yao mpaka kiwiko"**

Kuna maandiko mbalimbali kwenye tungo hii. Andiko lisilo la kawaida linalosomwa ni *pugmē*, ambalo linamaana"kwanza" linapatikana kwenye maandiko ya kale A, B,na L, ambapo *pukna*, lenye maana ya "marudio," linapatikana kwenye, א W, na toleo la Vulgate na Peshitta.Baadhi ya maandiko ya kale yanaacha mabano katika Marko 7:3-4 (yaani., maandiko ya karne ya kumi na tisa 037, yanatambulika kwa herufi kubwa za za Kigiriki , na baadhi ya tafsiri za Koptiki na Ashuru na Diatesaroni). Toleo la UBS[4] linatupatia chaguo #1 kama jibu "A" daraja (la uhakika). inawezekana kwamba ni vigumu kwa neno la Kigiriki kuakisi tafsiri ya Kigiriki ya tungo ya Kiaramu "wasiponawa mikono yao kwa chombo (maalumu)" (kama vile. *Theological Dictionary of the NewTestament,* limehaririwana Gerhard Friedrich na Geoffrey W. Broomiley, juzuu. 6, uk. 916). Mafarisayo walichukua katika Agano la kale taratibu zinazohitajika hekaluni kwa ajili ya makuhani na kuzieleza kwa Wayahudi

wa “kweli” kila siku. Waliongeza kwenye sheria za Musa.

Chaguo lingine limechukuliwa kama njia za Waalimu wa sheria ya Kiyahudi kuosha mikono ya mtu mwingine kwa mkono uliokunja ngumi,lakini hili halithibitishwi na maandiko yoyote ya tamaduni za Waalimu wa sheria ya Kiyahudi, ingawa inarejelea dhana ya kuteka maji na kuyamimina juu ya kiwiko (na mikono ikiwa inaelekea chini) na mkono ulio wazi ambao unaweza kusugua kiwiko tena.

Neno hili “kuosha” (*niptō*, kama vile. Mat. 15:2) kwa kawaida limetumika kurejelea kuosha sehemu za mwili na sio kuoshs mwili wote (yaani., *louō,* kama vile. Yn 13:10).

◙**" wakishika mapokeo ya wazee wao”** Tamaduni hizi (kama vile. Gal. 1:14) zimeweka kanuni katika kitabu cha sheria na maadili ya Kiyahudi (yaani., Mishna). Kuna matoleo mawili ya desturi za waalimu wa sheria ya Kiyahudi. Toleo moja lililokamilika ni kutoka kitabu cha sheria na maadili ya Wahudi la Babeli na toleo ambalo bado halijakamilika linatoka Palestina. Usomaji wa kisasa wa fasihi hii umezuiwa kwa sababu hakuna hata mmoja mwenye uhakika ni lini majadiliano halisi yalizungumzwa au kuwekwa kumbukumbu. Baada ya shule mbili za kutafsiri sheria za waalimu wa Kiyahudi kuanzishwa , moja yenye kushikilia mambo ya kale (yaani., *Shammai*) na moja yenye kupenda mabadiliko (yaani.,*Hillel*). Majadiliano haya yote msingi wake ni mjadala huu wa waalimu wa sheria wa Kiyahudi. Waalimu wa sheria ya Kiyahudi wana dondoa kuwa watangulizi wao ni wenye mamlaka.

**7:4 "wasipotawadha"** Wayahudi wanaelezea sheria inayosimulia makuhani kuingia kwenye Hema ikihusisha wayahudi wote (kama vile. Kut.30:19). Kawaida hizi zinasimulia sherehe za utakaso. Waliendelea na taratibu hizi kwa muda mrefu zaidi kwa kufahamu mambo yaliyokwisha tabiriwa kutoka katika kitabu cha sheria za Walawi. kuna maandiko kadhaa ya Kigiriki kwenye hii tungo. Baadhi ya maandiko ya Kigiriki yana:

1. Kauli ya kati tegemezi ya wakati usio timilifu ya *baptizō* (yaani., MSS A, D, W kama vile toleo Vulgate na tafsiri ya Ashuru)
2. Kauli tendwa elekezi ya wakati uliopo ya *baptizō* (yaani., MSS F, L)
3. Kauli ya kati tegemezi ya wakati usio timilifu ya *rantizō* "kunyunyiza" (yaani., MSS, א B na tafsiri ya koptiki). Tafsiri za kisasa zina chaguo #1. Kila mwandishi wa habari yumkini aliingiza #3 kwa sababu *baptizō* limekuwa neno la kifungu kwa ajili ya ubatizo wa Wakristo.

Toleo la UBS[4] linatupatia #1 a "B" daraja (lenye uhakika)

**NASB** **“na vyombo vya shaba”**
**NKJV** **“vyombo vya shaba na samani”**
**NRSV** **“birika la shaba”**
**TEV** **“mabakuli ya shaba na vitanda”**
**NJB** **“sahani za shaba”**

Neno hili “vyombo” ni neno la kilatini. Marko ametumia maneno ya kilatini zaidi sana kuliko wengine kwenye Agano jipya. Hii yumkini iliakisi uandishi kwa Warumi akiwa Rumi. kuna maandiko mbalimbali ya Kigiriki yaliyoongeza *klinōn* (yaani , vitanda au samani) katika machapisho A, D, and W, ambapo $P^{45}$, א, B, na L limeachwa. Inawezekana waandishi wa habari, walifahamu Law. 15, wakaongeza tungo, au baadae waandishi wa habari, hawakufanana na andiko la Agano la kale, walifikilia hayana maana na wakayafuta. Kisio linatia
shauku,lakini teolojia ina umuhimu.

**7:5 "wakamwuliza"** hii ni njeo ya kauli ya wakati usio timilifu ambayo inadokeza kwamba walimwuliza zaidi na zaidi tena au walianza kumwuliza zaidi.

◙**"hawaendi kwa kuyafuata mapokeo ya wazee"** hili lilikuwa ni tatizo kwa ajili yao. Hata limewekwa kumbukumbu kwenye fasihi ya Kiyahudi ya Walimu wa sheria ya Kiyahudi kwa kushindwa kuosha mikono yao vizuri. Kitabu cha sheria na maadili ya kiyahudi, ambacho kina kumbukumbu ya majadiliano ya waalimu wa sheria ya Kiyahudi jinsi ya kuelewa chombo cha maandiko ya Agano la kale,linakuwa na “mamlaka”.

**7:6 " Isaya alitabiri vema juu yenu "** Yesu aliamini kwamba maandiko ya Agano la kale kihistoria toka siku za Isaya yalisimulia juu ya kizazi hiki cha Mafarisayo miaka mia saba baadae. Hii inaonyesha umuhuimu wa maandiko kwa kila kizazi kipya. Kweli ya Mungu huathiriwa na tamaduni, lakini pia huvuka nyakati na tamaduni ! Yesu ananukuu toka Isa. 29:13.

◙**"wanafiki"** huu ni mchanganyiko wa kutoka katika maneno mawili "chini"na "kuhukumu". Ni neno ambalo limetumika kuelezea muigizaji anaecheza nyuma ya barakoa.Yesu aliwalaumu kwa kuangalia baadhi ya mambo, lakini zaidi wakiwazuia wengine (kama vile. Isa. 29:13; Kol. 2:16-23). Sio kwa bahati mbaya kwamba "wanafiki" na waosha mikono wamejitokeza pamoja kwenye Zab. 26:4 na 6!

## MADA MAALUM: WANAFIKI (katika Mathayo)

Hili neno ambatani (*hupokritēs*) kwa maana iliyo wazi linatafasiriwa "kuhukumu chini ya." ingalimaanisha (1) kidokezo kwenye neno la kitamthilia kwa ajili ya kuzungumza toka nyuma ya pazia (yaani., kuigiza) au (2) matumizi yake ya mwanzo yalikuwa ni "kuhitimisha ufasiri."

Mafarisayo walitenda nje ya utaratibu wa kidini na ibada (mara nyingi hadharani) ili wapate kusifiwa na watu, na sio kumpendeza Mungu (ingawa nina uhakika kuwa ilikuwa ni moja ya sababu):

1. kutoa misaada, sio tu kuwasaidia wahitaji, bali ili wapate kusifiwa na watu, Mt. 6:2
2. wakiomba kwenye Masinagogi na kuomba hadharani ili waonekane mbele za watu, Mt. 6:5
3. walipofunga walionekana kuwa wasio nadhifu ili wengine wapate kuvutiwa na namna walivyo wa kiroho, Mt. 6:16
4. walisema kitu hiki lakini wakitenda kitu kingine (kama vile Mt. 15:7-9; Marko 7:1-7; Isa. 29:13)
5. walijaribu kumkamata Yesu kwa maswali ya mitego, na sio kutafuta hekima ya kweli, Mt. 22:15-22
6. waliwazuia wengine wasiweze kuingia kwenye ufalme, Mt. 23:13-15
7. hulipa zaka za bizari na jira na kuacha mambo makuu ya sheria, Mt. 23:23
8. walisafisha kikombe kwa nje, na sio ndani, Mt. 23:25
9. walikuwa ni makaburi matupu yasiyosafishwa, Mt. 23:27-28 (kama vile *Dictionary of Biblical Imagery,* uk. 415)
10. walikuwa wenye kujihesabia haki, Mt. 23:29-30
11. walikuwa na sehemu maalum huko jehanamu, Mt. 24:51

◙"kama ilivyoandikwa" njeo hii ni kauli ya wakati timilifu "imesimama kama ilivyoandikwa". Hii ni lahaja ya kati ya Kiyahudi kwa ajili ya kurejelea maandiko yaliyovuviwa (kama vile Marko 9:12-13; 11:17; Mt. 4:4,7,10). Dondoo ni kutoka katika tafsiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania ya Isa. 29:13, ambayo huelezea ubinafsi wa kujihesabia haki wa mwanadamu. Yesu anatupatia mfano huu kwenye Marko 7:9-19 na ule unaofanana kwenye Mt. 15:4-6.

◙"'mioyo'" kwa Wayahudi hili ni eneo la maamuzi, hata hivyo, msingi wa matendo. Walitumia utaratibu wa kidini kwa maana ya kupata kukubaliwa na Mungu. Utamaduni wao ulikuwa mkuu! Hii mara zote ilikuwa ni hatari kwa watu wa kidini. Tazama mada maalum katika Marko 2:6.

◙"'iko mbali'" hii ina maana "kushikilia katika mahali." Mazoea ya kidini mara zote yametumika kuzuia kabisa ibada kwa Mungu. Mara nyingi dini ni kizuizi, na sio daraja, kwenda kwa Mungu.

**7:7** ni shutuma za kushangaza za wanafiki wa kidini na urasimu.

**7:8 "mwaiacha"** hii inamaanisha "kutupilia mbali (yaani , Amri za Mungu) na kulenga taswira ya "shika", lenye maana "shikilia," "kukamata" au "kung'ang'ania" utamaduni.

◙ "**amri ya Mungu, na kuyashika mapokeo ya wanadamu"** jambo hili ni ufunuo (Agano la kale) dhidi ya tamaduni (kitabu cha sheria na maadili ya wayahudi). Hili ni jambo la kila mmoja katika kila desturi (au dhehebu). Mamlaka ya kidini ni jambo la muhimu sana!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 7:9-13**
**9Akawaambia, Vema! Mwaikataa amri ya Mungu mpate kuyashika mapokeo yenu. 10Maana Musa alisema, Waheshimu baba yako na mama yako, na, Amtukanaye babaye au mamaye kufa na afe. 11Bali ninyi husema, Mtu akimwambia babaye au mamaye, Ni Korbani, yaani, wakfu, kitu changu cho chote kikupasacho kufaidiwa nacho, huwa basi; 12wala hammruhusu baada ya hayo kumtendea neno babaye au mamaye; 13huku mkilitangua neno la Mungu kwa mapokeo yenu mliyopokeana; tena mwafanya mambo mengi yaliyo sawasawa na hayo.**

**7:9**
**NASB "una mamlaka ya kupangilia"**
**NKJV "vyote pia umevikataa"**
**NRSV "una njia nzuri ya kukataa"**
**TEV "una njia bora zaidi ya kukataa"**
**NJB "kwa namna gani imefanywa kwa werevu kwako"**

Dhihaka hizi zenye kuumiza, vile vile kama kwenye Yohana 3:10.

**7:10 "Musa alisema "**inafanana na Mt. 15:4 ina , "Mungu akasema." Hii inaonyesha uvuvio wa Mungu nyuma ya maneno ya Musa.

◙**"'waheshimu'"** hii ni dondoo kutoka katika amri kumi zilizoandikwa kwenye Kut. 20:12 na kurudiwa kwenye Kumb.5:16.linatoka kwenye neno lifaalo la Kiebrania "kulipa uzito" (BDB 457), ambalo linamaanisha kutambua thamani ya kitu.

**7:11 "bali"** hii ni kauli hali daraja la tatu, ambalo linaongelea matendo ya karibu.Yesu anarejelea njia za kisasa zinazozuia sheria za Mungu (kama vile. Marko 7:12).

◙**"'baba yako na mama yako'"** hii inaonyesha heshima inayohitajika kwa ajili ya wazazi wote.

◙**"Amtukanaye babaye au mamaye'"** hili ni dondoo kutoka katika kitabu cha Kut.21:17. Kutokuheshimu kulileta adhabu kali. Waalimu wa sheria za Kiyahudi walipangilia mstari huu kwa maana ya utamaduni wao.

◙**"'korbani'"** hii ni tafsiri ya Kigiriki ya kiebrania (sio kiaramu) "zawadi" itolewayo kwa Mungu (yaani, au kwa hekalu, kama vile. Toleo la NKJV). Yesu alionyesha katika siku zake mfano mmoja jinsi viongozi wa dini ya kiyahudi walivyokuwa na shauku ya kuzuia na kuelezea sheria za Agano la kale kwa mapokeo yao ya fasihi simulizi. Walishauri na kupitisha mengi kwenye mapokeo yao ya fasihi simulizi (kama vile. Mt. 5:33-34; 23:16-22).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 7:14-16**
**14Akawaita makutano tena, akawaambia, Nisikieni nyote na kufahamu. 15Hakuna kitu kilicho nje ya mtu ambacho kikimwingia chaweza kumtia unajisi, bali vile vimtokavyo, ndivyo vimtiavyo unajisi yule mtu. 16Mtu akiwa na masikio ya kusikilia, na asikie.]**

**7:14 "akawaita makutano tena"**Yesu aliwaelezea makutano unafiki wawaandishi na utamaduni zao. Toleo la NKJV lina neno *panta* (yaani, wote) badala ya *palin* (yaani, tena).

◙**"'nisikieni. . .kufahamu'"** hizi zote ni kauli tendaji shurutishi za wakati uliopita usiotimilifu. Tungo hii inatambulisha mfano wa kushangaza na wa muhimu.

**7:15** Huu ni mfano wa kiwango cha juu wa Yesu akilitafasiri tena Agano la Kale (kama vile Mt. 5:17-48). Anabatilisha muundo wa chakula wa Walawi 11. Hii ilikuwa namna ya nguvu ya kutetea mamlaka Yake (yaani.,anaweza kubadilisha au kulikanusha Agano la Kale, lakini wasiwe wao). Pia hili laweza kuwa ni neno la kuonya kwa wale wanaochukulia masuala

ya dini yaliyo nje ya taratibu ya chakula na vinywaji (kama vile Rum. 14:13-23; 1 Kor. 8:1-13; 10:23-33). Maneno ya Yesu yanadhihilisha uhuru wa kipekee wa Agano Jipya (kama vile Rum.14:1-15:13; 1 Kor. 8-10).

**7:16** Mstari huu ulijumuishwa ndani ya machapisho mengi ya Kiyuani ya herufi kubwa (A, D, K, W, θ), mkusanyiko wa injili nne katika simulizi moja, na maandiko ya Kiyuani yaliyotumiwa na Augustine (kama vile NKJV and NJB). Hata hivyo, umeondolewa katika matoleo ya MSS, א, B, na L. Yawezekana ilikuwa ni nyongeza ya kiuandishi toka Marko 4:9 au 23. Toleo la NASB (lililoboreshwa mwaka 1995) linaujumuisha katika mabano kuonyesha kuna baadhi ya mashaka yaliyomo kwenye lile la asili. Toleo la USB[4] linapima lile ondoleo kwa alama "A" (yenye uhakika).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 7:17-23**
**17 Hata alipoingia nyumbani, ameuacha mkutano, wanafunzi wake wakamwuliza habari za ule mfano.**
**18 Akawaambia, Hivi hata ninyi hamna akili? Hamfahamu ya kwamba kila kitu kilicho nje ya mtu, kikimwingia, hakiwezi kumtia unajisi; 19 kwa sababu hakimwingii moyoni, ila tumboni tu; kisha chatoka kwenda chooni? Kwa kusema hivi alivitakasa vyakula vyote. 20 Akasema, Kimtokacho mtu ndicho kimtiacho unajisi. 21 Kwa maana ndani ya mioyo ya watu hutoka mawazo mabaya, uasherati, 22 wivi, uuaji, uzinzi, tamaa mbaya, ukorofi, hila, ufisadi, kijicho, matukano, kiburi, upumbavu. 23 Haya yote yaliyo maovu yatoka ndani, nayo yamtia mtu unajisi.**

**7:17 "Wanafunzi wake wakamuuliza"** Mathayo 15:15 inamzungumzia Petro. Maneno ya Yesu yalikuwa ya kustaabisha kwa wote Wayahudi wa karne ya kwanza! Yesu alimwondoa Musa! Ambaye alikuwa ni mwalimu wa dini ya Kiyahudi asiye rasmi?

**7:18 "'Hivi ninyi nanyi hamna akili'"** Yesu aliushangaa ugoigoi wa wanafunzi waliokuwa nao. Ujumbe wake ulikuwa wa tofauti kwa kile walichowahi kukisikia katika maisha yao (yaani.,thiolojia ya Kifarisayo). Tamaduni ni ngumu kuzirekebisha (kama vile Marko 4:13,40; 6:52; 8:21). Kumwamini Yesu kama Masihi aliyeahidiwa kunamaanisha ni mgawanyo muhimu ukiwa na matarajio ya mila na tamaduni pendwa. "Neno la uzima" linalipita"neno lililoandikwa"! Waamini wanamwabudu Yesu, na sio Biblia. Mara nyingi watoa maoni wanasema kuwa Yesu aliyakataa mapokeo ya fasihi simulizi ya Wayahudi, lakini mara zote akithibitisha sheria za Agano la Kale.

Hata hivyo, kukataliwa kwa sheria za chakula na kukataliwa kwa mafundisho ya Musa juu ya talaka katika Mt. 5:31-32 (kama vile Marko 10:2-12) kwa uwazi kabisa kunaonyesha kuwa Yesu alijiona kama mfasiri sahihi na hata Bwana wa Agano la Kale (kama vile Mt. 5:38-39). Yeye ni hatma ya mafunuo ya Mungu. Kati yetu hakuna hata mmoja mwenye kuithamini Biblia alifurahie hili. Tunaiona Biblia kama yenye mamlaka na muhimu. Hata hivyo, ni maandiko mangapi ya Agano la Kale ambayo Yesu aliyaona kama yasiyodhihilisha kusudi la Baba? Hili sio tu kwamba liliwashangaza waandishi, kwa kiasi fulani hata mimi limenishangaza! Linanikumbusha mimi kuwa Agano la Kale sio la muhimu kwa waamini wa Agano Jipya (kama vile Matendo 15; Wagalatia 3). Hakika ni la kimaandiko na hakika linamdhihilisha Mungu, lakini mimi sifungwi na kaida za dini na taratibu (kama vile Mdo. 15:6-11,19). Ninafungwa na mtazamo wa kidunia na ufunuo wa Mungu na kusudi lake na ahadi (kama vile Mt. 5:17-20)!

**7:19**
**NASB, NRSV** "(alivitakasa vyakula vyote)"
**NKJV** "hivyo akavitakasa vyakula vyote"
**TEV** "(. . .Yesu akatamka vyakula vyote vyasitahili kuliwa)"
**NJB** "(hivyo akatamka vyakula vyote ni sawa)"

Mabano yanaaksi maoni ya mtafasiri kuwa ni hoja za kiuandishi (yumkini toka kwenye uzoefu wa Petro katika Matendo 10). Ni ukweli wa Agano Jipya (kama vile Rum. 14:13-23; 1 Kor. 8:1-13; 10:23-33). Mwanadamu hayuko sawa na Mungu akisimamia juu ya kipi wakile au wasikile! Agano Jipya haliegamii juu ya taratibu za Agano la Kale (yaani.,Walawi 11;

Matendo 15). Mungu anaangalia moyo, na sio tumbo!

**7:20** Walimu wa dini ya Kiyahudi wa Agano la Kale wanasema kuwa mawazo ni shamba lenye rutuba, kitalu cha mbegu kilichoandaliwa na kuwa macho na masikio ni madirisha ya nafsi. Chochote kile mtu anachoruhusu kuingiza, huotesha mizizi. Dhambi huanza katika fikra na kukuwa katika matendo. Lugha za kibinadamu huudhihirisha moyo!

## MADA MAALUM: LUGHA YA BINADAMU

I. MAWAZO YA UFUNGUZI TOKA MITHALI
  A. Lugha ni sehemu ya taswira ya Mungu kwa mwanadamu (yaani., uumbaji umezungumzwa katika kuweko na Mungu kuzungumza kwenye uumbaji wake wa mwanadamu). Ni sehemu muhimu ya hulka bayana.
  B. Kauli ya mwanadamu inatuwezesha kuwasiliana na wengine jinsi tunavyofikiria kuhusu maisha. Kwa hiyo, inadhihilisha jinsi tulivyo (Mith. 18:2; 4:23, 20-27). Kauli ni ladha chachu ya mtu (Mith. 23:7)
  C. Sisi ni viumbe jamii. Tunawajibika na ukubalifu na uthibitisho. Tunavihitaji kutoka kwa Mungu na kutoka wanadamu wenzetu. Maneno yana nguvu ya kuyakabili mahitaji haya katika hali chanya (Mith. 17:10) na hasi (Mith. 12:18).
  D. Kuna nguvu ya ajabu katika kauli ya mwanadamu (Mith. 18:20-21-nguvu ya kubariki na kuponya (Mith. 10:11,21) na nguvu ya kulaani na kuangamiza (Mith. 11:9)
  E. Tunavuna kiile tulichopanda katika eneo hili (Mith. 12:14)

II. KANUNI TOKA KWENYE MITHALI
  A. Kauli za mwanadamu zilizo kinyume na zenye uharibifu
    1. Maneno ya mtu mwovu (1:11-19; 10:6; 11:9,11; 12:2-6)
    2. Maneno ya mwasherati (5:2-5; 6:24-35; 7:5 na kuendelea; 9:13-18; 22:14)
    3. Maneno ya mtu mwongo (6:12-15,19; 10:18; 12:17-19,22; 14:5,25; 17:4; 19:5,9,28; 21:28; 24:28; 25:18; 26:23-28)
    4. Maneno ya mtu mjinga (10:10,14; 14:3; 15:14; 18:6-8)
    5. Maneno ya mtu mwenye kushuhudia uongo (6:19; 12:17; 19:5,9,28; 21:28; 24:28; 25:18)
    6. Maneno ya msengenyaji (6:14,19; 11:13; 16:27-28; 20:19; 25:23; 26:20)
    7. Maneno ya mlopokaji (6:1-5; 12:18; 20:25; 29:20)
    8. Maneno ya msingizaji (29:5)
    9. Mtu mwenye maneno mengi (10:14,19,23; 11:13; 13:3,16; 14:23; 15:2; 17:27-28; 18:2; 21:23; 29:20)
    10. Maneno ya upotoshaji (17:20; 19:1)
  B. Kauli ya mwanadamu iliyo dhahili, yenye kuponya na kujenga
    1. Maneno ya mwenye haki (10:11,20-21,31-32; 12:14; 13:2; 15:23; 16:13; 18:20)
    2. Maneno ya utambuzi (10:13; 11:12)
    3. Maneno ya maarifa (15:1,4,7,8; 20:15)
    4. Maneno yenye kuponya (15:4)
    5. Maneno yenye jibu la upole (15:1,4,18,23; 16:1; 25:15)
    6. Maneno yenye jibula kufurahisha (12:25; 15:26,30; 16:24)
    7. Maneno ya kisheria (22:17-21)

III. SEHEMU YA AGANO LA KALE INAYOENDELEA KATIKA AGANO JIPYA
  A. Kauli ya mwanadamu inatuwezesha kuwasiliana na wengine jinsi tunavyofikiria kuhusu maisha. Kwa hiyo, inadhihilisha jinsi tulivyo (Mt. 12:33-37; 15:1-20; Mk 7:2-23).
  B. Sisi ni viumbe jamii. Tunawajibika na ukubalifu na uthibitisho. Tunavihitaji kutoka kwa Mungu na kutoka wanadamu wenzetu. Maneno yana nguvu ya kuyakabili mahitaji haya katika hali chanya (2 Tim. 3:15-17) na hasi (Yak. 2:2-12).
  C. Kuna nguvu ya ajabu katika kauli ya mwanadamu ;nguvu ya kubariki (Efe. 4:29) na nguvu ya kulaani (Yakobo 3:9). Tunawajibika kwa kile tutakayoyasema (Mt. 12:36-37; Yak. 3:2-12)
  D. Tutahukumiwa kutokana na maneno yetu (Mt. 12:33-37; Lk. 6:39-45) vile vile na matendo yetu (Mt.

25:31-46). Tunavuna kile tupandacho (Gal. 6:7)

**7:21 "ndani ya mioyo yao"** Yesu aliorodhesha mlolongo wa mienendo na matendo ya uovu. Aina zile zile za dhambi zililaumiwa na walio wakakamavu. Paulo pia alikuwa na orodha ya dhambi kama hizi (kama vile Rum. 1:29-31; 1 Kor. 5:11; 6:9; 2 Kor. 12:20; Gal. 5:19-21; Efe. 4:31; 5:3-4; Kol. 3:5-9; 2 Tim. 3:2-5). Angalia MADA MAALUM: UOVU NA WEMA katika 1 Petro 4:2.

◙**"Uasherati"** Neno la Kiingereza "picha za utupu" zinachangia mzizi ule ule wa neno kama lilivyo neno hili la Kiyunani. Lilimaanisha tendo la kujamiana kusiko sahihi: kujamiiana kabla ya ndoa, ubasha, kumwingilia mnyama, na wajibu wa kumuoa mjane wa ndugu yako (ndugu kushindwa kuhusiana kwa maana ya kujamiana na mjane wa aliayeachwa na nduguye kwa minajiri ya kumpatia mrithi).katika Agano la Kale kulikuwepo na tofauti kati ya kutokuwa mwaminifu kwenye ndoa(uzinzi) na kujamiiana kabla ya ndoa (uasherati). Hata hivyo, utofauti huu umepotea kwenye kipindi hiki cha Agano Jipya.

◙**"uuaji. . .tamaa mbaya. . .hila. . .kiburi"** Maneno haya yenye kufanana yanauelezea ulimwengu wa kipagani kwenye Rum. 1:29-31. Walionyesha moyo wa kutokujizuia, moyo uliogeuka "zaidi kwa ajili yetu kwa gharama yeyote."

◙**"uzinzi"** Hili ni neno *moicheia*, lenye kurejelea uhusiano wa kujamiana nje ya ndoa (kama vile 1 Kor. 6:9-10). Likajaanza kutumika kiistiari kwa ajili ya ibada ya sanamu. Katika Agano la Kale YHWH alikuwa bwana na Israel alikuwa mke: kwa hiyo, kuitafuta miungu mingine ilikuwa ni aina ya kukosa uaminifu katika ndoa.

◙**"tama mbaya"** Hili linatumika katika Rum. 13:13 kuonyesha ni namna gani waumini hawapaswi kuishi. Katika *Greek-EnglishLexicon of the NewTestament Based on Semantic Domains,* juzuu ya 1, uk. 771, Louw and Nida analielezea hili neno kama"tabia ya moja kwa moja ya kutokuweza kujizuia kimaadili, mara nyingi kukiwa na maana ya uasherati." Tambua ni kiasi gani cha maneno haya yanadokeza kujamiiana kusikozuilika, ambayo ni tabia ya tamaduni za kipagani za karne ya kwanza.

**7:22** Utaratibu wa orodha hii ya dhambi hubadilika toka tafasiri moja hadi nyingine. Kwa ufupi, maisha mbali na Mungu ni Maisha yaliyo nje ya mipaka! Orodha ya Paulo katika Gal. 5:19-21 inaelezea kuhusu uovu na orodha katika Gal. 5:22-23 inaelezea maisha ya kiungu.

**NASB, NRSV**
**NJB "husuda"**
**NKJV "upumbavu"**
**TEV "wivu"**

Hii kwa maana iliyo wazi ni "kijicho" (kama vile kumbukumbu ndogo za toleo la NASB). Watu wa huko Mashariki ya Karibu walikuwa makini kwa mtu kuwaroga (yaani.,kuwachawia). Katika Kiebrania lina kidokezo cha kuwa mbinafsi mwenye wivu (kama vile Kumb. 15:9; Mith. 23:6).

**NASB, NRSV**
**NJB, TEV "ufisadi"**
**NKJV "matukano"**

Neno kwa maana iliyo wazi ni "matukano," ambalo humaanisha kumnenea mtu jambo ambalo si kweli. Laweza kutumika katika kashfa au ubaya kumhusu Mungu au mwanadamu (kama vile Mdo. 6:11; Rum. 2:24).

◙**"kiburi"** Hili linarejelea kujiinua, kudharauliwa, au mtu mwenye majivuno (kama vile Luka 1:51; Rum. 1:30; 2 Tim. 3:2;Yakobo 4:6; 1 Pet. 5:5).

**7:23** Ufanano ulioko katika Mt. 15:20 unafupisha mazungumzo yote (kama vile 1 Sam. 16:7).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 7:24-30**
**[24]Akaondoka huko, akaenda zake hata mipaka ya Tiro na Sidoni. Akaingia katika nyumba, akataka isijulikane na mtu; lakini hakuweza kusitirika. [25]Ila mara mwanamke, ambaye binti yake yuna pepo mchafu, alisikia habari zake, akaja akamwangukia miguuni pake. [26]Na yule mwanamke ni Myunani, kabila yake ni Msirofoinike. Akamwomba amtoe pepo katika binti yake. [27]Akamwambia, Waache watoto washibe kwanza; maana si vizuri kukitwaa chakula cha watoto, na kuwatupia mbwa. [28]Naye akajibu, akamwambia, Naam, Bwana, lakini hata mbwa walio chini ya meza hula makombo ya watoto. [29]Akamwambia, Kwa sababu ya neno hilo, enenda zako, pepo amemtoka binti yako. [30]Akaenda zake nyumbani kwake, akamkuta yule kijana amelazwa kitandani, na yule pepo amekwisha kumtoka.**

**7:24 "Tiro"** Hii ni sehemu ya Kaskazini Magharibi mwa Bahari ya Galilaya, nje ya mipaka za nchi ya ahadi. Ilikuwa ni sehemu maarufu ya watu wa mataifa. Kifungu "na Sidoni" hakimo katika machapisho machache ya Kiyunani, kama vile D, L,na W, lakini lipo katika Mt. 15:21 na Marko 7:31 na machapisho ,א, A, na B, vile vile kama ilivyo kwa matoleo ya Vulgate and Peshitta.

◙**"akataka asijulikane na mtu"** Haya yalikuwa ni matokeo ya miujiza yake (kama vile Marko 3:8). Hata maeneo aliyopita ya watu wa mataifa hakupata kupumzika wala muda wa faragha akiwa na wanafunzi wake.

**7:25 "binti yake mdogo alipagawa na pepo"** Namna binti alivyopagawa na pepo haielezewi hapa hata katika habari ya Marko 9:17-29. Wala kwa masuala haya haionekani kuwa ni pepo wa kawaida (yaani.,kupagawa na pepo toka kizazi kimoja hadi kingine ndani ya familia). Angalia Mada Maalum: Upungaji Pepo katika Marko 1:25.

◙**"akamwangukia miguuni pape"** Hii ilikuwa alama ya kitamaduni ya (1) hali ya kusihi kwa kumaanisha au (2) unyenyekevu. Yawezekana kuwa alikwisha sikia miujiza ya Yesu na, pasipo kukata tamaa, akamkabili huyu mwalimu wa Kiyahudi kwa hofu!

**7:26 "mwanamke Myunani, Msirofoenike"** Kumbuka,Yesu aliwasaidia watu wengine wasio Wayahudi (kama vile Marko 5:1;11:17; Mt. 8:5-13; Yohana 4), lakini ndani ya mipaka ya kijiografia ya nchi ya ahadi. Kama Yesu alikuwa tayari ameanza huduma ya uponyaji kwenye nchi ya wasio Wayahudi, angelikataliwa na makutano ya Wayahudi kwa sababu ya chuki zao. Kuna ufanano wenye kufurahisha kati ya huduma ya Yesu kwa Yule yule mama Msirofoenike na huduma ya Eliya kwa mwanamke Msirofoenike katika 1 Fal. 17. Kote kote upendo wa Mungu unahusika, na msaada upo kwa watu wa mataifa waliochukiwa. Huu ungewezakuwa ni ushuhuda usio wa moja kwa moja wa huduma yake ya Kimasihi. Ni lugha ipi ilitumika kati ya huyu mama na Yesu?
Dhahili, inavyoonekana ilikuwa ni Kiyunani. Kukua kwa Yesu pande za Kaskazini mwa Palestina kungalimfanya ajue lugha nyingi. Katika Luka 4:16-20 Yesu alisoma gombo la Isaya kwa Kiebrania.Angaliweza kufunua Biblia ya Kiebrania kwenye shule za Sinagogi. Mara nyingi aliongea Kiarama. Aliweza kuzungumza kwa lugha ya Koine, ya huko Uyunani (yaani.,mazungumzo ya faragha akiwa na Pilato).

◙**"akamwomba"** Hii ni njeo ya wakati usiotimilifu. Akamwomba mara nyingi!

◙**"amtoe pepo "**Hii ni kauli tendaji tegemezi ya wakati uliopita usiotimilifu. Alikuwa bado anamashaka kuhusu uwezo wa Yesu au ridhaa ya kutenda, ambayo imeelezewa kwa dhamira tegemezi.

**7:27 "binti yake"** Hili neno lililozoeleka linairejelea Israel (kama vile Mt. 15:24).

**7:27-28**

| | |
|---|---|
| **NASB, NRSV** | |
| **TEV** | **"mbwa"** |
| **NKJV, NJB** | **"mbwa wadogo"** |

Hili ni tumizi pekee la neno hili katika Agano Jipya. Ukali wake hupotea kwa vile ni mdogo kiumbo (yaani.,*kunarion*), "mbwa wachanga" (toleo la NJB lina "mbwa wa nyumbani"). Wayahudi waliwaita watu wasio Wayahudi "mbwa" kama neno la kuwadhihaki. Mazungumzo haya yalikusudia kuwasaidia wanafunzi kukabiliana na chuki dhidi ya watu wa mataifa (kama vile Mt. 15:23). Yesu alilitambua hili na mbele za watuakathibitisha kuwa imani yake ilikuwa kubwa (kama vile Mt. 15:28).

**7:28 "'Bwana'"** Hii yawezekana ilitumika kwa maana ya kitamaduni ya neno "Bwana" au "Bwana," kama lilivyo katika Yohana 4:11. Hii inashangaza kuona mfano uliotumia neno *kurios* lililonenwa kwa Yesu na injili ya Marko.

◙**"watoto"** Hii kwa maana iliyo wazi ni "watoto wadogo" (*paidion*). Kuna miundo midogo mbalimbali inayopatikana katika muktadha huu. Katika *Word Pictures in the NewTestament*, juzuu ya 1, uk. 326, A. T. Robertson anasema "watoto wadogo kwa makusudi hudondosha makombo ya chakula kwa ajili ya mbwa." Mtummoja alipenda mahadhi ya sauti ya Yesu, mwonekano wa usoni, na mwonekano wa mwili ungaliweza kuwekwa kwenye kumbukumbu. Nafikiria mkabiliano ulikuwa wa maana zaidi kuliko maneno matupu kuweza kuandikwa.

◙**"makombo ya watoto"** Tajiri alitumia mkate kujifuta mikono baada ya kula, kama taulo ya kujifutia.

**7:29 "'kwa sababu ya neno hili'"** Yesu alifurahishwa na mwenendo wa Yule mama alivyoendelea pamoja na imani (kama vile Mt. 15:28). Yesu aliwaponya/kuwaokoa watu kulingana na imani ya mwingine mara kadhaa (kama vile Marko 2:3-12; 9:14-29; Mt. 8:5-13).

◙**"enenda zako, pepo amemtoka binti yako"** Huyu mwanamke alimwamini Yesu kuwa angeweza kuyaondoa mapepo hata akiwa mbali pasipo miujiza.

**7:29,30 "amekwisha kumtoka"** Katika Marko 7:29 ni kauli tendaji timilifu elekezi na katika Marko 7:30 ni kauli tendaji timilifu yenye hali ya kuendelea, ambayo inaangazia kwenye matokeo yenye kushikamana na tendo lililopita. Mapepo yalimtoka na kukaa mbali.

**7:30 "akiwa amelala kitandani"** Hii ni kauli tendwa timilifu ya hali ya kuendelea ambayo ingaliweza kueleweka kwa namna mbili: (1) pepo walimtoka kwa vurugu (kama vile Marko 1:26; 9:26) na kumrusha binti kwenye kitanda au (2) hali yake ya kupagawa ilimsababisha kuwa wa kitandani.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 7:31-37**
**[31]Akatoka tena katika mipaka ya Tiro, akapita katikati ya Sidoni, akaenda mpaka bahari ya Galilaya, kati ya mipaka ya Dekapoli. [32]Wakamletea kiziwi, naye ni mwenye utasi, wakamsihi amwekee mikono. [33]Akamtenga na mkutano faraghani, akatia vidole vyake masikioni mwake, akatema mate, akamgusa ulimi, [34]akatazama juu mbinguni, akaugua, akamwambia, Efatha, maana yake, Funguka. [35]Mara masikio yake yakafunguka, kifungo cha ulimi wake kikalegea, akasema vizuri. [36]Akawaonya wasimwambie mtu; lakini kadiri ya alivyozidi kuwaagiza, ndivyo walivyozidi kutangaza habari; [37]wakashangaa mno kupita kiasi, wakinena, Ametenda mambo yote vema; viziwi awafanya wasikie, na bubu waseme.**

**7:31** Maelezo ya kijiografia ni mageni. Sidoni ilikuwa Kaskazini mwa Tiro juu ya uwanda wa bahari, Dekapoli ilikuwa Kusini Mashariki mwa bahari ya Galilaya. Toleo la NKJV lina neno "akatoka mipaka ya Tiro na Sidoni," lakini tafasiri hii haiungwi mkono na matoleo ya $P^{45}$, A, W, na Peshitta. Shutuma nyingi za kimaandiko zinaunga mkono lile neno gumu lililomsababisha Yesu aende Kaskazini na mashariki kabla ya kwenda Kusini.

◙**"Bahari ya Galilaya"** Mkusanyiko wa aina ile ile ya maji huitwa (1) Kenereti katika Agano la Kale; (2) Ziwa Genesareti katika Luka 5:1; na (3) Bahari ya Tiberia kwenye karne ya kwanza kipindi cha utawala wa Kirumi katika Yohana 6:1; 21:1.

◙**"mipaka ya Dekapoli"** Haya yalikuwa ni maeneo ya nchi ya Wagerasi (kama vile Marko 5:1-20). Pia lilikuwa ni eneo la watu wa mataifa mashariki na kusini mwa bahari ya Galilaya. Huduma ya Yesu katika maeneo haya inaonyesha upendo wake kwa ajili ya watu wa mataifa.

**7:32 "kiziwi, na mwenye utasi"** Neno hili limetumika hapa tu katika Agano Jipya na katika tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani katika Isa. 35:6. Mstari wa 37 waweza kuhusiana na Isa. 35:5-6, ambao huelezea huduma ya Masihi ya siku zijazo.

◙**"amwekee mkono"** angalia Mada Maalum ifuatayo.

## MADA MAALUM:KUWEKEWA MIKONO KATIKA BIBLIA

Hii ishara ya kujumuishwa inatumiwa sana katika njia mbalimbali katika Biblia.

1. kula kiapo (yaani mkono katika uvungu wa paja [kama vile Mwanzo 24:2,9; 47:29])
2. kuchukua uongozi wa familia (kama vile Mwanzo 48:14,17,18)
3. kutambua kifo cha dhabihu ya mnyama kama mbadala
    a. Makuhani (kama vile Kutoka 29:10,15,19; Law. 16:21; Hes. 8:12)
    b. kuwalaza watu (kama vile Law. 1:4; 3:2,8; 4:4,15,24; 2 Nyakati. 29:23)
4. mtu wa kukaa pembeni kumtumikia Mungu kwa ajili ya jukumu maalumu au huduma (kama vile Hes. 8:10; 27:18,23; Kumb. 34:9; Mdo. 6:6; 13:3; 1 Tim. 4:14; 5:22; 2 Tim. 1:6)
5. kushiriki katika kurusha mawe kwa kimahakama kwa kumpiga mwenye dhambi (kama vile Law. 24:14)
6. mkono katika mdomo wa mtu huashiria ukimya au tafakari (kama vile Waamuzi. 18:19; Ayubu 21:5; 29:9; 40:4; Mika 7:16)
7. Mkono wa mtu ukiwa katika kichwa chake humaanisha huzuni/ombolezo (2 Sam. 13:19)
8. kupokea Baraka za afya, furaha na utauwa (kama vile Mt. 19:13,15; Marko 10:16)
9. ikihusiana na uponyaji wa mwili (kama vile Mt. 8:3; 9:18,20; Marko 5:23; 6:5; 7:32; 8:23; 16:18; Luka 4:40; 13:13; Mdo. 9:17; 28:8)
10. kupokea Roho Mtakatifu (kama vile Mdo. 8:17-19; 9:17; 19:6, angalia Kumb. 34:9)

Kwa kushangaza kuna ukosefu wa mfanano katika vifungu ambavyo kihistoria vimekuwa vinatetea kuwekwa wakfu kwa viongozi kwa ajili ya kazi ya injili (yaani kuwekwa wakfu, angalia Mada Maalum: Kuwekwa Wakfu).

1. Katika Mdo. 6:6 Ni mitume wanaoweka mikono yao kwa ajili ya huduma ya watu saba ya kanisa la mahali pamoja.
2. Katika Mdo. 13:3 Ni Mitume na Walimu wanaoweka mikono juu ya Barnaba na Paulo kwa ajili ya huduma ya kimishenari.
3. Katika Mdo. 1 Tim. 4:14 Ni viongozi wa kanisa la nyumbani (wazee) waliojumuishwa katika wito wa kwanza na kuwekwa rasmi.
4. In Katika 2 Tim. 1:6 Ni Paulo anayeweka mikono yake juu ya Timotheo.

Mtawanyiko na utata unaonyesha kukosekana kwa mpangilio katika kanisa la karne ya kwanza. Kanisa la kwanza lilikuwa zaidi katika kuendelea na kubadilika badilika na mara zote likitumia karama na vipawa vya roho vya waamini (kama vile Wakorintho 12; 14). Agano Jipya kwa ufupi tu limeandikwa kutetea au kushusha mfano wa serikali (Angalia mtawanyiko huu katika Mdo. 15) au taratibu za kuwekwa wakfu. Mpangilio wa desturi za kikanisa ni muhimu lakini sio kibiblia. Uungu wa uongozi ni zaidi kiumuhimu kuliko mfumo ya uongozi (yaani dola).

**7:33 "akamtenga na makutano faraghani"** Hii kwa vyovyote ilikuwa ni kusitisha mazungumzo kuhusu uponyaji na kumfanya mtu ajisikie zaidi kuwa kawaida (kama vile Marko 8:23).

◙**"akatia vidole vyake masikioni mwake"** Yesu alikuwa akiwasiliana na Yule mtu kile alichojaribu kukifanya katika ishara za kimwili kiweze kukubalika kitamaduni (yaani.,kuweka kidole kwenye masikio na mate kwenye ulimi).

◙**"akatema mate, akagusa ulimi"** Mate yalitumika kama dawa katika karne ya kwanza ya ulimwengu wa Kimediterania. Ilimaanisha kuongeza imani ya mtu.

**7:34 "akatazama juu mbinguni"** Hiki kilikuwa ni kipimo cha mkao wa kimwili kwa ajili ya maombi ya Wayahudi kipindi cha siku za Yesu (yaani.,kusimama, macho yakiwa wazi, kichwa kikiwa kimetazama juu, mikono ikiwa imeinuliwa juu).

◙**"akaugua"** Hii inarejelea hali ya kunyamaza pasipo kuzungumza kuonyesha hisia kali (kama vile Rum. 4; 8:22-23; 2 Kor. 5:12). Ikiwa ni kweli (kama vile Marko 7:34; Rum. 8:26) au sio kweli (kama vile Mdo. 7:34; Yakobo 5:9) inategemeana na muktadha wa fasihi. Hili lingeweza kuonyesha machungu ya Yesu juu ya dhambi na maradhi yaliyoko duniani yakisababishwa na uasi. Muundo ambatani wa hili neno unaonekana katika Marko 8:12.

◙**"Efatha"** Hii ni kauli tendwa shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu ya lugha ya Kiarama, ikimaanisha "kuwa wazi" (na walikuwepo, kama vile Marko 7:35). Petro alikumbuka maneno ya Kiaramu ambayo Yesu aliyaongea na Marko kuyatafasiri kwa Kiyunani kwa ajili ya viongozi (yaani.,Warumi) wasio Wayahudi. Angalia Mada Maalum Katika Marko 5:41.

**7:36 "Aliwaonya wasimwambie mtu"** Sababu ya hili ni kwamba injili ilikuwa bado kukamilika. Yesu hakutaka kutambulika kama mtenda miujiza. Shauku ya makutano tayari ilikuwa tatizo."Siri ya Kimasihi" inaainishwa na Marko. Hata hivyo, inashangaza kwa sababuYesu alitenda mambo mengi na kwa kusema hivyo akayadhihilisha mambo mengi kwa ajili yake Mwenyewe katika Marko.Yesu kwa uwazi alijidhihirisha Mwenyewe kama Masihi na kutimiliza matarajio ya Wayahudi wa sasa walio na macho ya kuona!

**7:37** Kumponya kiziwi ilikuwa ni alama ya wazi ya Kimasihi (kama vile Isa. 35:5-6).

◙**"'Ametenda mambo yote vema'"** Hii ni kauli tendaji timilifu elekezi. Ni usemi ulioje uliofanywa na watu wa kaskazini mwa Palestina!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyeweza Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Mjadala huu wa maswali unawekwa ili kukusaidia wewe kufikiri maana ya chapisho kupitia sehemu ya kitabu. Wanamaanisha kuchochea sio kumalizia.

1. Tunawezaje kuhusiana kwenye utamaduni? Elezea maana ya utamaduni.
2. Je Yesu aliliweka kando Agano Jipya? Ikiwa ndivyo tunalichukuliaje Agano la Kale kama lenye uvuvio (Marko 7:19)
3. Elezea tofauti kati ya mtazamo wa Yesu kuhusu dini na ule wa Mafarisayo .
4. Kwa ni ni Yesu alikwenda kwenye maeneo ya watu wa mataifa yaliyojulikana? (Marko 7:24)
5. ni kwa namna gani Yule binti alipagawa na pepo? Je inatokea hivyo kwa siku za leo? (Marko 7:25)
6. Kwa nini Yesu aliwakanya wasimwambie mtu kuhusu kuponywa kwa Yule mtu? (Marko 7:36)

# MARKO 8

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| USB[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Kuwalisha watu Elfu nne | Kuwalisha watu elfu nne | Watu elfu nne walishwa | Yesu awalisha watu elfu nne | Muujiza wa pili wa mkate |
| 8:1-10 | 8:1-10 | 8:1-10 | 8:1-3 | 8:1-10 |
| | | | 8:4 | |
| | | | 8:5 | |
| | | | 8:6-10 | |
| Hitaji la ishara | Mafarisayo watafuta Ishara | Mithari juu ya ishara | Mafarisayo waomba miujiza | Mafarisayo waomba miujiza toka Mbinguni |
| 8:11-13 | 8:11-12 | 8:11-13 | 8:11-12 | 8:11-13 |
| | Jilindeni na chachu Ya mafarisayo | | | |
| | 8:13-21 | | 8:13 | |
| Chachu ya Mafarisayo na Maherodi | | Chachu ya mafarisayo | Chachu ya Mafarisayo na Maherodi | Chachu ya Mafarisayo na Maherodi |
| 8:14-21 | | 8:14-21 | 8:14-15 | 8:14-21 |
| | | | 8:16 | |
| | | | 8:17-19 | |
| | | | 8:20 | |
| | | | 8:21 | |
| Kuponywa kwa Mtu kipofu huko Bethaida | Kipofu aliyepooza aponywa huko Bethaida | Mtu kipofu aponywa | Yesu amuponya kipofu huko Bethaida | Uponyaji wa mtu kipofu huko Bethaida |
| 8:22-26 | 8:22-26 | 8:22-26 | 8:22-23 | 8:22-26 |
| | | | 8:24 | |
| | | | 8:25-26 | |
| Tamko la Petro Kumhusu Yesu | Petro anamkiri Yesu kama ndiye Kristo | Ukiri wa Petro | Tamko la Petro kumhusu Yesu | Ukiri wa imani ya Petro |
| 8:27-30 | 8:27-30 | 8:27-30 | 8:27 | 8:27-30 |
| | | | 8:28 | |
| | | | 8:29a | |
| | | | 8:29b | |
| | | | 8:30 | |
| Yesu abashiri Kifo chake na Ufufuko | Yesu atabiri kifo chake na ufufuko | | Yesu azungumzia kuhusu mateso yake na kifo | Unabii wa kwanza wa wiki ya mateso |
| 8:31-9:1 | 8:31-33 | 8:31-33 | 8:31-33 | 8:31-33 |
| | Jitwike msalaba | Kuhusu uanafunzi | | Masharti ya |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Na unifuate<br>8:34-9:1 | 8:34-9:1 | 8:34-9:1 | kumfuata Kristo<br>8:34-9:1 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka "Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo wa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## VIDOKEZO VYA UFANANO WA INJILI

A. Mtu atashangaa ikiwa Yesu alilisha umati wa watu mara kadhaa au kwa sababu fulani zisizo julikana kwa watafsiri wa kisasa wa Magharibi, hili tukio linajirudia (yaani., 6:34-44 na 8:1-10)
B. Marko 8:10-12 inafanana na Mt. 15:39-16:4.
C. Marko 8:13-26 inafanana na Mt. 16:5-12.
D. Marko 8:27-30 inafanana na Mt. 16:13-20 na Luka 9:18-21.
E. Marko 8:31-37 inafanana na Mt. 16:21-26 na Luka 9:22-25.
F. Marko 8:38-9:1 inafanana na Mt. 16:27-28 na Luka 9:26-27.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 8:1-10**
**1 Katika siku zile, kwa vile ulivyokuwa mkuu tena ule mkutano, nao wamekosa kitu cha kula, akawaita wanafunzi**
**wake, akawaambia, 2 Nawahurumia mkutano kwa sababu yapata siku tatu wamekaa nami, wala hawana kitu cha**
**kula; 3 nami nikiwaaga waende zao nyumbani kwao hali wanafunga, watazimia njiani; na baadhi yao wametoka**
**mbali. 4 Wanafunzi wake wakamjibu, Je! Ataweza wapi mtu kuwashibisha hawa mikate hapa nyikani? 5 Akawauliza,**
**Mnayo mikate mingapi? Wakasema, Saba, 6 Akawaagiza mkutano waketi chini; akaitwaa ile mikate saba,**
**akashukuru, akaimega, akawapa wanafunzi wake wawaandikie; wakawaandikia mkutano. 7 Walikuwa na visamaki**
**vichache; akavibarikia, akasema wawaandikie na hivyo pia. 8 Wakala, wakashiba, wakakusanya mabaki ya vipande**
**vya mikate makanda saba. 9 Na watu waliokula wapata elfu nne. Akawaaga. 10 Mara akapanda chomboni pamoja**
**na wanafunzi wake, akaenda pande za Dalmanutha.**

**8:1 "katika siku zile"** Habari hii inatokea hasa kwenye maeneo ya watu wa mataifa (kama vile Marko 7:31).

◙ **"tena palikuwepo na mkutano mkubwa"** Hii inaainisha huduma ya Yesu kwenye kipindi hiki.

**8:2 "nawahurumia mkutano"** Neno hili "kuhurumia" linatokana na neno la Kiyunani kwa ajili sehemu ya chini ya viungo vya mwili. (Ini, figo, matumbo). Katika Agano la Kale Wayahudi walitoa nafasi ya kumhurumia Yule aliyekuwa na hisia ya ndani. Yesu anawapenda watu (kama vile Marko 1:41; 6:34; 8:2; 9:22; Mt. 9:36; 14:41; 15:32; 18:27; 20:34; Luka 7:13; 10:33). Watu hawa walikwisha kataliwa na walimu wa dini ya Kiyahudi katika maisha yao yote. Walijikusanya chini ya uangalizi wa Yesu.

◙ **"yapata siku tatu wamekaa nami"** Huu ulikuwa ni muda wa ziada wa mafundisho. Wayahudi walianza kuhesabu siku toka jioni moja hadi nyingine. Sehemu yeyote ya siku ilihesabiwa; kwa hiyo, hii haimaanishi kurejelea kwenye siku tatu, za masaa 24. Hawakuruhusiwa kwenda mbali hata kununua chakula cha ziada. Walipaswa kula kile walicholeta.

**8:3 "ikiwa"** Hii ni sentensi yenye masharti daraja la kwanza, yenye kuzungumzia tendo muhimu. Yesu hadai kuwa wote wako katika hatua ya kuanguka, bali wengine ni wagonjwa na dhaifu wanaweza kuzimia.

◙ **"watazimia njiani"** Huku kuzimia kungalisababishwa na ukosefu wa chakula. Angalia Amu. 8:15 na Omb. 2:19 katika tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania. Walikwisha tumia chakula chote walichokileta na wamekuwa wakifunga.

◙ **"baadhi yao wametoka mbali"** Hii inaonyesha namna umaarufu wa Yesu ulivyokuwa kama mtenda miujiza. Watu wasio na tumaini huenda kokote, na kujaribu chochote kwa ajili ya kupata msaada!

**8:4 "'ataweza wapi mtu kuwashibisha mikate nyikani'"** Hata kama walikuwa na fedha hapakuwepo na mahali pa kununua chakula. Yesu alikuwa akiijaribu imani ya wanafunzi wake kwa kutoa kwake! Walishindwa (kama vile Marko 6:34-44).

**8:6 "kaeni chini"**Hili linarejelea sehemu ya kupumzika, yenye kumaanisha wawe tayari kwa ajili ya chakula.

**8:6-8 "mkate. . .samaki"** Huu ulikuwa ni mlo wa kawaida wa kila siku kwa watu wa Palestina. Hili linafanana na lile la 6:34-

◙ **"akavibariki"** Haya maombi ya baraka juu ya chakula ni ya kushukuru juu ya uangalizi na utoaji wa Mungu wa kila siku (kama vile Mt. 6:11). Wayahudi mara zote waliomba kabla ya kula.

◙ **"akamega. . .kuwapatia"** Huu ni wakati uliopita usio timilifu ukifuatiwa na njeo ya wakati usio timilifu. Hii miujiza ya kujiongeza ilitokea pindi mikate alipokwisha Marko 6:41.

**8:8 "mabaki ya vipande vya mikate makanda saba"** Hili ni neno la tofauti kwa ajili ya kikapu toka 6:43. Hivi vikapu vilikuwa ni vikubwa (kama vile Mdo. 9:25). Vipande vya mikate vilivyobaki vilikusanywa kwa ajili ya kutumika baadaye. Hata hivyo, toka Marko 8:14 tunajifunza namna wanafunzi walivyosahau na kuwaaga.

**8:9 "wapata elfu nne"** Mathayo 15:83 anaongeza "watu," ikimaanisha umati ulikuwa mkubwa. Yumkini hapakuwepo na idadi kuwa ya wanawake na watoto kwenye hili eneo lililojitenga, lakini hakika palikuwepo na baadhi.

**8:10 "mara akapanda"** Angalia kumbukumbu katika Marko 1:10.

◙ **"pande za Dalmanutha"** Kuna tofauti mbalimbali katika kifungu hiki. Tatizo ni kuwa hakuna sehemu iliyojulikana kwa jina hili huko Palestina katika siku za Yesu. Kwa hiyo, waandishi walibadali jina la sehemu hii ili kwendana na ile ya Mathayo "Magadan" (NKJV "Magdala").

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 8:11-12**
**11 Wakatokea Mafarisayo, wakaanza kuhojiana naye; wakitafuta kwake ishara itokayo mbinguni; wakimjaribu. 12 Akaugua rohoni mwake, akasema, Mbona kizazi hiki chatafuta ishara? Amin, nawaambieni, Hakitapewa ishara kizazi hiki.**

**8:11 "Mafarisayo. . .wakaanza kuhojiana nae"** Hili lilikuwa ni la kawaida kutokea. Wasingaliweza kuikana mamlaka yake, nguvu, au umaarufu, walijaribu kumtega kwa maswali ambayo yangalisababisha baadhi ya watu kujitenga. Angalia Mada Maalum juu ya Mafarisayo katika Marko 2:16.

◙ **"ishara toka mbinguni"** Katika injili ya Yohana neno "ishara" lilikuwa na maana maalum, lakini hapa linarejelea kwenye ombi la Mafarisayo kwa ajili ya kuwahakikishia mamlaka yake, yumkini (1) unabii (kama vile Kumb. 13:2-5; 18:18-22); (2) ishara ya Kimbingu (kama vile Isa. 7:11; 38:7-8); au (3) ishara ya matukio ya siku za mwisho (ushindi wa kivita juu ya maadui).

◙ **"ili kumjaribu"** Neno *peirazō* lina kidokezo cha kujaribu, kikiwa na mtazamo wa uharibifu." Hili linaweza lisiwe rejeo la moja kwa moja kwa kutokuamini kipindi cha kutangatanga nyikani (kama vile Kut. 17:7; Hes. 14:11-12,22; Kumb. 33:8). Angalia Mada Maalum juu ya maneno ya Kiyunani kwa ajili "kujaribu" katika Marko 1:13.

**8:12 "Akaugua "** Hili ni neno ambatani na kwa hivyo linapanua muundo wa neno "akaugua" (kama vile Marko 7:34). Yesu aliwaonyesha mamlaka yake aliyonayo kwa matendo na maneno, lakini bado upofu wao wa kiroho uliendelea.

◙ **"rohoni mwake"** Hili linarejea kwenye ubinadamu wa Yesu (kama vile Marko 2:8). Lina kidokezo kama kile kile cha Marko 14:38 kwa kumheshimu mwanadamu. Neno "roho" linatumika katika Marko kwa ajili ya

1. Roho Mtakatifu (Marko 1:10,12)
2. Roho wachafu (yaani mapepo, Marko 1:23,26,27; 3:11,30; 5:2,8,13; 6:7; 7:25; 9:17,20,25)
3. Roho wa mwanadamu (Marko 2:8; 8:12; 14:38)

◙ **"'kizazi hiki'"** Hili neno pia lina madokezo ya Agano la Kale yenye kuhusiana na kipindi cha kutangatanga nyikani (kama vile Hes. 32:13; Kumb. 1:35; 32:5,20).

◙**"Amini"** Hii kwa maana iliyo wazi ni "amina." Angalia Mada Maalum "Amina" katika Marko 3:28.

◙ **"'nawambieni, hakitapewa ishara kizazi hiki'"** Hii ni nahau ya Kiebrania yenye kukanushi kwa nguvu (na sio sentensi yenye masharti ya Kiyunani) yenye kuhusiana na kuelewa, ingawa ni kiapo kisichoelezeka. Ukilinganisha Mt. 16:4 dhahiri Yesu alimaanisha hakuna ishara zingine. Yesu alikwishawapa ishara nyingi (yaani., utimilifu wa nabii za Agano la Kale katika matendo yake na maneno), lakini walikataa kuwaamini au kumwamini kwa sababu alizipinga desturi zao, nafasi za kitamaduni, na umaarufu wao.

**8:13** Yesu kwa sehemu kubwa alitembea kwenda Kaskazini mwa Palestina kwa sababu alitaka wote wausikie ujumbe wake lakini pia ni kwa sababu ya kusanyiko la umati wa watu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 8:14-21**
**[14] Wakasahau kuchukua mikate, wala chomboni hawana ila mkate mmoja tu. [15] Akawaagiza, akasema, Angalieni, jihadharini na chachu ya Mafarisayo na chachu ya Herode. [16] Wakabishana wao kwa wao, kwa kuwa hawana mikate. [17] Naye Yesu akatambua, akawaambia, Mbona mnabishana kwa sababu hamna mikate? Hamfahamu bado, wala hamjaelewa? Je! Mioyo yenu ni mizito? [18] Mna macho, hamwoni; mna masikio, hamsikii? Wala hamkumbuki? [19] Nilipoivunja ile mikate mitano na kuwapa wale elfu tano, mlichukua vikapu vingapi vimejaa vipande? Wakamwambia, Kumi na viwili. [20] Na ile saba kuwapa wale elfu nne, mlichukua makanda mangapi yamejaa vipande? Wakamwambia, Saba. [21] Akawaambia, Hamjafahamu bado?**

**8:14** Dhahiri haya ni maelezo ya ushuhuda wa macho toka kwa Petro.

**8:15 "akawaagiza"** Hii ni kauli ya kati endelevu ya wakati usiotimilifu toka kwenye neno kuu "kuamuru kwa mamlaka" ( kama vile Marko 5:43; 7:36; 8:15; 9:9). Hili neno ni tabia ya Marko (yaani., mara nyingi likihusiana na "siri za Kimasihi").

**NASB, NRSV** **"tazama!"**
**NKJV** **"angalia"**
**TEV** **"kuwa mwangalifu"**
**NJB** **"Macho yako yakaone"**

Kwa maana iliyo wazi ni "angalia" (yaani., *horaō*). Ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo,yenye kudokeza kuendeleza uangalifu ili kuwapo na tahadhari nzuri.

**NASB, NKJV**
**NRSV "uwe mwangalifu"**
**TEV "uwe macho"**
**NJB "angalia"**

Hii pia ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Hizi amri kali zote ni kutoka kwenye maneno tofauti ya Kiyunani yakimaanisha "kuangalia" (yaani., *horaō* na *blepō*), ikimaanisha kuwa waamini wanapaswa kuwa macho saa zote (kama vile Marko 4:24; 12:38; 13:5,9,23,33) dhidi ya kujihesabia haki binafsi.

◙ **"'ya Herode'"** Wandishi wa mwanzo walijaribu kusanifisha misemo ya Yesu. Katika Marko 3:6 na 12:13 Yesu anasema "Maherodi"; kwa hiyo, machapisho ya Kiyunani P[45], G, na W, vile vile pia baadhi ya matoleo ya Vulgate, na tafasiri za Koptiki, yalibadilisha muundo wa chanzo milikishi. Machapisho makubwa ya Kiyunani yanashuhudia juu ya hiki chanzo milikishi (kama vile MSS ,א, A, B, C, D, na L). angalia Mada Maalum juu ya familia ya Herode katika Marko 1:14.

◙**"chachu"** Hii mara nyingi ilikuwa ni ishara ya machafuko, kama lilivyo kwenye andiko hili (kama vile 1 Kor. 5:6-8; Gal. 5:9). Hili laweza kuwa ni kulichezea neno katika Kiarama kwa sababu neno "chachu" na "neno" yanafanana. Tatizo la wanafunzi lilikuwa sawa na lile la Mafarisayo, ambao ni upofu wa kiroho. Lazima wawe macho muda wote. Maherode linawakilisha tatizo lingine— hali ilivyokuwa kwa gharama yeyote!

**8:16 "wakaanza kubishana wao kwa wao kwa kuwa hawana mikate"** Hii ni kauli isiotimilifu. Wanafunzi walikuwa bado hawajajifunza somo. Yesu atatoa mahitaji yote! Yesu anazungumza kuhusu namna ya kudhibiti upotofu na walifikiri anazungumza kuhusu chakula! Toleo la NKJV linaongeza neno "kubishana" ndani ya sentensi fupi (kama yafanyavyo machapisho madogo ya Kiyunani) ikifuatisha Mt. 16:7. Toleo la NASB linakamilisha kusudi lile lile kwa kuongeza maneno yenye mlazo (yaani., "kuanza"na "kweli").

**8:17 "Nae Yesu akatambua"** Sio kila mara kujua namna Yesu alivyotambua mambo. Wakati mwingine ni kwa maarifa yasiyo ya kawaida na wakati mwingine akizijua tabia na mienendo ya watu.

◙ **"'Mbona mnabishana kuhusu mikate'"** Hili ni la kwanza kati ya maswali sita au saba ambayo Yesu alielezea kuhusu sikitiko lake kwamba wanafunzi wake bado hawamwelewi! Huu muktadha wote wa Marko unadhihilisha ni namna gani ilikuwa ni ngumu kwa ajili ya "rafiki na adui" kuweza kuukabiri moja kwa moja ujumbe mpya wa Yesu. Wanafunzi wake, familia yake, watu wa nyumbani kwao, umati wa watu, na viongozi wa dini wote hawakuwa na macho au masikio ya kiroho!

◙ **"'Hamfahamu bado, wala kuelewa'"** Hii ni dhamira yenye kujirudia (kama vile Marko 8:21; 6:52). Familia ya nyumbani kwao Yesu, wanafunzi wake, watu wa miji, na viongozi wa dini hawakumwelewa Yesu. Yumkini hii ni njia ya kuonyesha hali ya kiroho kabla ya utimilisho kamili wa roho kuja siku ya Pentekoste (au siri ya Kimasihi inafunuliwa katika mateso, kufufuka kwake Bwana).

◙ **"'je? Mioyo yenu ni mizito'"** Hii ni kauli tendwa timilifu yenye hali ya kuendelea ikidokeza utulivu wa hali ya kiroho uletwao na mshauri toka nje (kama vile Marko 4:13,40; 6:52; 7:18; 8:17,21,33; 9:10,32). Hiki ndicho kitakachotokea kwa Yuda Iskarioti. Angalia MADA MAALUM: MOYO katika Marko 2:6.

**8:18** Hili ni rejeo la Agano la Kale toka Ezekiel 12:2 (kama vile Yer. 5:21), ambalo kithiolojia linafanana na Isa. 6:9-10 (kama vile Marko 4:12). Manabii wa Agano la Kale walizungumza neno la Mungu, lakini hawakuelekwa kwa sababu ya hali ya kiroho ya wale waliowasikiliza. Rejea hizi za Agano la Kale ziko katika muundo wa kisarufi wenye

kutarajia jibu la "ndiyo".

◙ **"'wala hamkumbuki'"** Yesu anawakemea kwa ajili ya kukoswa kwao uelewa wa kiroho wenye kuhusiana na muujiza wa kuwalisha chakula (kama vile Marko 8:17-21). Kifungu hiki pia kina mwongozo wa Agano la Kale (kama vile Kumb. 4:9-10; 8:11,19). Watu wa Mungu lazima washikilie na kutenda juu ya kweli ya Mungu.

**8:19 "vikapu"** Hili ni neno tofauti toka 8:8. Hili ni neno lililotumika katika Marko 6:43 (yaani., vikapu vidogo). Anawakumbushia juu ya muujiza wa kuwalisha uliopita. Hawakuwahi kufanya uhusiano wowote (kama vile Marko 8:32-33; 9:32-34; 10:35-37).

**8:20** Mstari wa 19 unarejelea kwenye kuwalisha watu katika Marko 6, lakini mstari wa 20 unarejea kwenye kuwalisha watu kulikopo katika Marko 8.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 8:22-26**
**22 Wakafika Bethsaida, wakamletea kipofu, wakamsihi amguse. 23 Akamshika mkono yule kipofu, akamchukua nje ya kijiji, akamtemea mate ya macho, akamwekea mikono yake, akamwuliza, Waona kitu? 24 Akatazama juu, akasema, Naona watu kama miti, inakwenda. 25 Ndipo akaweka tena mikono yake juu ya macho yake, naye akatazama sana; akawa mzima, akaona vyote waziwazi. 26 Akampeleka nyumbani kwake, akisema, Hata kijijini usiingie.**

**8:22 "kipofu"** Moja ya unabii wa Isaya kuhusu Masihi ulikuwa kwamba atamfanya aone Yule kipofu (kama vile Isa. 29:18-35:5; 42:7,16,18,19). Upofu wa kimwili ni stiari ya Agano la Kale kwa ajili ya upofu wa kiroho Yohana 9. Hili dhahili linahusiana na upofu wa kiroho wa wan (kama vile Isa. 56:10; 59:10). Mchezo wa aina ile ile juu ya upofu wa kiroho na kimwili waziwazi unaonekana katika afunzi katika Marko 8:15,18.

**8:23 "akamchukua nje ya kijiji"** Hili lilikuwa kwa ajili ya kusudi la kumweka mtu katika hali ya kawaida na kutunza siri ya uponyaji (kama vile Marko 7:33; 8:26).

◙ **"akamtemea mate katika uso na kuweka mikono juu yake"** Hizi zilikuwa ni njia za uponyaji kitamaduni, moja kiroho na nyingine kimwili. Ilikuwa ni namna ya kujenga imani ya mtu. Angalia MADA MAALUM: KUWEKA MIKONO katika Marko 7:32.

**8:24 "'Naona watu kama miti'"** Yesu hakuzuiliwa katika mamlaka, lakini alikuwa akitenda juu ya imani ya mtu huyu. Huu ulikuwa ni sehemu ya uponyaji au uponyaji uliokuwa ukifanyika kwa hatua ulioandikwa katika injili.

**8:25** Mstari huu unaanza na Yesu akiweka mikono juu ya macho ya mtu aliyekuwa kipofu. Baadaye kitendo kinahamia kwa mtu (kama vile toleo la NJB). Lazima atazame na kuangalia kwa makini (kama vile Mt. 7:5). Alipoonyesha ushirikiano, mara tu akaona.

**8:26** Hii ni rejea ya Marko kwa Yesu kimsisitizo akiwaambia watu aliowaponya wasisambaze habari za kupona kwao. Upokeaji wa maandiko (yaani., toleo la KJV au NKJV) hata huongeza kifungu na kuufanya kuwa muhimu zaidi. Yesu hakutaka kujulikana kama mponyaji. Alitumia uponyaji kuonyesha rehema ya Mungu, kuijenga imani ya wanafunzi, na kuthibitisha huduma yake ya ufundishaji.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 8:27-30**
**27 Akatoka Yesu na wanafunzi wake, wakaenda kwenye vijiji vya Kaisaria-Filipi; na njiani akawauliza wanafunzi wake, akasema, Watu huninena mimi kuwa ni nani? 28 Wakamjibu, Yohana Mbatizaji; wengine, Eliya; wengine, Mmojawapo wa manabii. 29 Naye akawauliza, Na ninyi mnasema ya kuwa mimi ni nani? Petro akamjibu, akamwambia, Wewe ndiwe Kristo. 30 Akawaonya wasimwambie mtu habari zake.**

**8:27-30** Hili tukio ni tukio la njia panda katika injili ya Marko. Simulizi za miujiza zinazothibitisha mamlaka, nguvu, na ukomo wa Uungu wa Yesu. Kutokana na hili baada ya msisitizo huu lililofuata ni kusulubiwa. Injili ya Marko inabadilika toka kwenye mtizamo wa nani aliyeko juu ya kitendo hiki cha ukombozi (yaani., kile alichofanya).

**8:27 "kwenye vijiji"** Mathayo 16:13 ina kifungu "kwenye vijiji vya." Yesu alitaka kufanya mambo mawili (1) kuondoka kutoka kwenye umati na (2) kuhubiri kwenye vijiji vyote. Kwa hali hiyo sababu ya #1 inashinda.

◙ **"Kaisaria-Filipi"** Huu mji upo yapata maili 25 Kaskazini mwa ziwa Galilaya kwenye eneo maarufu la watu wa mataifa. Lilikuwa likidhibitiwa na Herod Philip, na sio Herod Antipa.

◙ **"na njiani akawauliza"** Wakiwa njiani wakitembea Yesu akaanza (njeo ya wakati usiotimilifu) kuwauliza.

◙ **"'Watu huninena kuwa mimi ni nani'"** Mathayo 16:13 ina "Mwana wa Adamu," ambalo ni jina alilolichagua Yesu Mwenyewe. Hiki ndicho kiini cha swali la kidini.

**8:28 "Yohana Mbatizaji"** Huu ulikuwa ni ushauri wa Herod Antipas, vile vile pia baadhi ya ushauri wa watu (kama vile Marko 6:14,16; Luka 9:19).

◙ **"Eliya"** Hili lingedokeza kuwa Yesu alikuwa ni mtangulizi wa Masihi (kama vile Mal. 4:5).

◙ **"mmoja wa manabii"** Mathayo 16:14 ina "Yeremia." Chaguzi zote hizi zinahusisha urejeshaji na yalikuwa majina ya heshima, lakini yakiwa si ya Kimasihi.

**8:29 "'Ninyi mwasema Mimi ni nani'"** Huu ni wingi na ulielezewa kwa wanafunzi wote. Neno "wewe" ni la msisitizo kwenye Kiyunani kwa sababu kihisishi kimetangulizwa (yaani., kimewekwa kwanza kwenye sentensi).

◙ **"'Wewe ni Kristo'"** Petro, mcheshi wa kundi, alijibu kwanza. Huu ni unukuzi wa Kiebrania wa neno "Masihi" (BDB 603), lenye kumaanisha "Mpakwa Mafuta." Yesu alisita kukubali kuitwa mbele ya watu jina hili kwa sababu ya wanasiasa wabaya wa Kiyahudi, kijeshi, na tafasiri za kitaifa. Katika muundo huu binafsi, alikubali, hata kulitafuta jina hili. Ufanano wa Mt. 16:16 una jina kamili, "Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai." Marko (mwandishi wa Petro) anaondoa sifa za Petro alizompa Yesu (kama vile Mt. 16:17,19).

**8:30 "Akawaonya wasimwambie mtu habari zake"** Huu ni mfano mwingine wa siri za Kimasihi ambazo ni za kawaida katika Marko (kama vile Marko 1:33-34,43; 3:12; 4:11; 5:43; 7:24,36; 8:26,30). Walifahamu jina lakini sio lengo!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 8:31-33**
**[31] Akaanza kuwafundisha kwamba imempasa Mwana wa Adamu kupatikana na mateso mengi, na kukataliwa na wazee, na wakuu wa makuhani, na waandishi, na kuuawa, na baada ya siku tatu kufufuka. [32] Naye alikuwa akinena neno hilo waziwazi. Petro akamchukua, akaanza kumkemea. [33] Akageuka, akawatazama wanafunzi wake, akamkemea Petro, akasema, Nenda nyuma yangu, Shetani; maana huyawazi yaliyo ya Mungu, bali ya wanadamu.**

**8:31 "Akaanza kuwafundisha"** Njeo ya wakati usio timilifu yaweza kumaanisha (1) kukianza kitendo au (2) mwendelezo wa kitendo siku za nyuma. Hapa #1 unadokezwa na muktadha, lakini bado kuna kauli isio timilifu nyingine katika Marko 8:32 ambayo inadokeza #2. Huu ni utabiri wa kwanza wa Yesu wa mateso yake na kifo, lakini kuna mwingine (kama vile Marko 9:12,31; 10:33-34).

◙ **"Mwana wa Adamu imempasa"** Hii inaonyesha kuwa Yesu kwa wazi alifahamu lengo lake na gharama yake (kama vile Marko 10:45). Hili lilikuwa dhahili alama ya utabiri Mafarisayo waliokuwa wakiitafuta katika Marko 8:12 kumthibitisha nabii wa kweli (kama vile Kumb. 13:2-5; 18:18-22).

◙ **"kupatikana na mateso mengi"** Hii ilikuwa ni dhana ya huduma ya Kimasihi ambayo Wayahudi waliikosa (kama vile Mwa.3:15; Zaburi 22; Isa. 52:13-53:12; Zak. 9-14). Katika fikra za Wayahudi Masihi alionekana kama ni uzao wa Daudi, shujaa wa kivita wa Israeli. Lakini angalipaswa kuwa pia kuhani, kama ilivyo katika Zaburi 110 na Zakaria 3-4. Hii asili mara mbili inaaksiwa katika matarajio ya jamii ya Masihi wawili kwenye magombo ya bahari ya chumvi, moja ya kifalme (toka Yuda) na kuhani (toka Law.). Wajibu wa matarajio ya uongozi wa nguvu unaonekana moja kwa moja kujitenga toka kwenye mateso ya Masihi. Yesu alijaribu mara kadhaa kuwajulisha wanafunzi kuhusu mateso yake yaliyotabiriwa (kama vile Marko 8:31; 9:12,30-31; 10:33-34), lakinihawakumwelewa (kama vile Marko 8:32-33; 9:32-34; 10:35-37).

◙ **"kukataliwa"** Hii inamaanisha "kutokukubaliwa" kwa sababu Yesu hakutimiza vigezo vya Umasihi walivyovijua viongozi wa Kiyahudi. Hakukidhi matarajio.

◙ **"na wazee, na wakuu wa makuhani, na waandishi"** Hii ilikuwa ni njia ya kulirejelea baraza la wakuu wa Sinagogi, baraza la wazee sabini toka Yerusalemu lililofuatia baada ya Mahakama kuu. Angalia Mada Maalum katika Marko 12:13.

◙ **"atauwawa. . .na kufufuka"** Hiki ndicho kiini cha ujumbe wa injili: ni mbadala wa dhabihu, na uthibitisho wa Uungu uliotukuka wa kukubaliwa kwake.

## MADA MAALUM: UFUFUO

Katika Biblia hali ya kulejeshwa toka mautini ina maana tatu.

A. Wale wote ambao hawakufa lakini wakaenda kukaa pamoja na Mungu (yaani., Enoko, kama vile Mwa. 5:24; Eliya, kama vile 2 Fal.. 2:11), ambao huitwa "utafasiri."
B. Baadhi, kupitia nguvu ya Mungu, hurejeshwa toka kwenye lango la mauti hadi kuwa na uhai. Hii huitwa "kurudi uzimani." Watakufa kwa kiasi Fulani huko mbeleni.
C. pamekuwepo na ufufuo mmoja tu (yaani., Yesu). Alikufa lakini akafufuka toka katika wafu (yaani., *kuzimu*) na kupewa mwili mpya ulioandaliwa kwa ajili ya uzima wa milele wakiwa na Mungu (kama vile 1 Kor. 15:20,23; "mzaliwa wa kwanza katika wafu," kama vile Kol. 1:15,17). Kwa sababu ya Yeye, waamini watafufuliwa kwenye ujio wake wa pili (kama vile Zab. 49:15; 73:24; Isa. 26:19; Dan. 12:2; Mt. 22:31-32; Marko 12:26-27; Yohana 5:25,28-29; 6:39-40,44,54; Rum. 8:11; 1 Wakorintho 15; 1 The. 4:13-18; 1 Yohana 3:2).

Ushuhuda kwa ajili ya ufufuo

A. Baada ya siku (50) baadaye kwenye Pentekoste, ufufuko ukajakuwa ujumbe muhimu wa hotuba za Petro (kama vile Matendo 2). Maelfu walioishi kwenye maeneo tukio lilipotokea waliamini!
B. Maisha ya wanafunzi yalibadilika moja kwa moja toka kwenye kukatishwa tamaa (hawakutarajia ufufuko) kwa ujasiri, hata kifo.
C. Paulo anaorodhesha mashuhuda wa macho katika 1 Kor. 15:5-8, ikimjumuisha yeye mwenyewe (kama vile Matendo 9).

Umuhimu wa ufufuo

A. Inavyoonyesha Yesu alikuwa ni waliyedai ndiye (kama vile Mt. 12:38-40, utabiri wa kifo na ufufuo)
B. Mungu aliweka kibali chake juu ya maisha ya Yesu, mafundisho, na kifo mbadala! (kama vile Rum. 4:25)
C. Inatuonyesha ahadi kwa Wakristo wote (yaani., ufufuko wa miili, kama vile 1 Wakorintho 15)

Madai ya Yesu kuwa atafufuka kutoka katika wafu

A. Mt. 12:38-40; 16:21; 17:9,22, 23; 20:18-19; 26:32; 27:63
B. Marko 8:31; 9:1-10,31; 14:28,58
C. Luka 9:22-27
D. Yohana 2:19-22; 12:34; sura ya 14-16

Wote Petro na Paulo wanadai kuwa Zaburi 16 inamrejelea Yesu, Masihi

A. Petro katika Matendo 2:24-32
B. Paulo katika Matendo 13:32-37

Usomaji zaidi

A. *Evidence That Demands a Verdict* cha Josh McDowell
B. *Who Moved the Stone?* cha Frank Morrison

C. *The Zondervan Pictorial Encyclopedia of the Bible*, "Resurrection," "Resurrection of Jesus Christ"

◙ **"baada ya siku tatu atafuafuka tena"** Kifungu hiki kingerejelea kwa Hos. 6:1-2. Kimetafasiriwa kwa namna ile ile ya toleo la Aramaic Targum kwenye mstari huu. Hata hivyo, Yesu anaonekana kufanya dokezo kwenye Yona 1:17 (kama vile Mt. 12:39; 16:4). Hii aina ya alama za kiutabiri dhahili kilikuwa ni kile Mafarisayo walikuwa wakikiuliza katika Marko 8:12 (kama vile Mt. 16:4). Hii aina ya utabiri ulikuwa ni msingi wa kumwelezea nabii wa kweli kutokana na Kumb.13:2-5; 18:18-22. Yesu aliwaonyesha ishara baada ya ishara, lakini hawakuweza kutambua, wala kuona!

**8:32**
**NASB "Nae alikuwa akilinena neno hili waziwazi"**
**NKJV, TEV "alilizungumza neno hili waziwazi"**
**NRSV "aliyasema haya yote waziwazi"**
**NJB "akayaweka wazi mbele yao"**

Hii ni njeo nyingine ya wakati usiotimilifu kama ilivyo kwa Marko 8:31. Hapo inamaanisha "kuanza," lakini hapa yaweza kurejelea kitendo chenye kujirudia (yaani., Yesu akawaambia kuhusu mateso yake na kifo chake mara kadhaa). Akanena nao waziwazi—pasipo mifano, pasipo ishara, wala stiari (kama vile Yohana 10:24; 11:14; 16:25,29; 18:20).

◙ **"Petro akamchukua"** Hili lilifanyika kwa utiifu, lakini pasipo ufahamu wa kutosha, Petro anatenda kama msaidizi wa shetani kwa namna ya kuitumia nafasi ya Kimasihi ya kuwafikia watu na kuwaokoa (kama vile Marko 1:12-13; Mt. 4:1-11).

◙ **"akaanza kumkemea"** Hili ni neno zito la Kiyunani (kama vile toleo la LXX la Mwa. 37:10; Luka 4:41; 2 Tim.4:2). Lilitumiwa na Yesu katika Marko 1:25; 3:12; 4:39; na 9:25. Katika muktadha huu Petro "akamkemea" au "kumlaumu" Yesu kwa hoja zake. Kusudi lake haswa lilikuwa ni kumlinda Yesu, na sio kumlaumu. Petro hakuelewa uwakilishi na asili ya unabii wa mateso ya Yesu. Yesu alimkemea Petro katika Marko 8:33 kwa ajili ya kukoswa kwake mtazamo wa kiroho na kutoelewa haraka.

**8:33 "akawatazama wanafunzi wake"** Yesu alilizungumza neno hili kwa Petro, lakini katika maana iliyo wazi alikuwa akiwaelezea wanafunzi wote.

◙ **"Nenda nyuma yangu, shetani"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Yesu alimwamuru petro aondoke mbele yake. Hili lina vidokezo vya Agano la Kale vya kukataliwa (yaani., "rudi nyuma yangu," kama vile 1 Fal. 14:9; Ezek.23:35). Pasipo kutambua, Petro alikuwa akimjaribu Yesu kwa namna kama ile Shetani aliyoitumia akiwa nyikani (kama vile Marko 1:12-13; Mt. 4:1-11). Shetani alimtaka Yesu aushangilie utii wa kibinadamu kwa namna yeyote ile badala ya ule wa kalvari msalabani (yaani., juu ya kuwalisha, kuwaonyesha miujiza, kuujadili ujumbe wake). Petro hakutambua kuwa mateso na kifo cha Yesu ulikuwa ni mpango wa Mungu (kama vile Marko 10:45; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29; 2 Kor. 5:21). Angalia MADA MAALUM: SHETANI katika Marko 1:13.
Mara nyingi mateso makali na majaribu madogo madogo hutokana na marafiki na ndugu wa karibu! Ufalme wa Mungu, na sio upendeleo wa kibinadamu, manufaa binafsi, au malengo binafsi, ndio kipaumbele kikuu (kama vile Marko 8:34-38).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 8:34-9:1**
**34 Akawaita mkutano pamoja na wanafunzi wake, akawaambia, Mtu ye yote akitaka kunifuata na ajikane mwenyewe, ajitwike na msalaba wake, anifuate. 35 Kwa kuwa mtu atakaye kuiponya nafsi yake, ataiangamiza, na mtu atakayeiangamiza nafsi yake kwa ajili yangu na kwa ajili ya Injili, huyu ataisalimisha. 36 Kwa kuwa itamfaidia mtu nini kuupata ulimwengu wote, akipata hasara ya nafsi yake? 37 Ama mtu atoe nini badala ya nafsi yake? 38 Maana kila mtu atakayenionea haya mimi, na maneno yangu, katika kizazi hiki cha uzinzi na dhambi, Mwana wa Adamu atamwonea haya mtu huyo, atakapokuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika watakatifu. 9-1 Akawaambia, Amin, nawaambia, Pana watu katika hawa wasimamao hapa, ambao hawataonja mauti kabisa, hata**

**watakapouona ufalme wa Mungu umekuja kwa nguvu.**

**8:34 "akawaita mkutano pamoja na wanafunzi wake"** Marko ndio injili pekee iliyoandika uwepo wa umati mkubwa kuweko huko Kaisaria-Filipi. Mara nyingi hili tukio linaonekana kuwa ni mafundisho ya muda wa faragha, lakini dhahili na wengine nao walikuwepo. Huu umati ungaliweza kuwajumuisha hata wale wasio Wayahudi na yumkini hapakuwepo na Mafarisayo au viongozi wa dini kwa sababu kidesturi ulifanyikia nje ya nchi ya ahadi kwenye eneo la watu wa Mataifa. Inaonyesha kwenye umati huu kuwa Yesu alidhihirisha gharama ya kweli ya uanafunzi, umuhimu, na kujitoa kikwelikweli kwa ajili ya kumfuata Yeye. Aliwashauri kumfuata, lakini kwa wazi aliwaelezea gharama yake!

◙ **"ikiwa"** Hii ni sentensi yenye masharti daraja la kwanza, inayoonekana kuwa kweli kutokanana na mtazamo wa mwandishi au kusudio lake.

◙ **"mtu yeyote akitaka kunifuata"** Tambua mwaliko wa wote wa kuwa wanafunzi wa Yesu. Lakini kuna gharama (yaani., wokovu ni bure, lakini kuwa mwanafunzi ni lazima na ni gharama ambayo unayotakiwa kujikana mwenyewe). Inafurahisha kuona kuwa maneno aliyoyasema Yesu kwa Petro katika Marko 8:33 (*hupage opisō mou*) sasa yanatumika tena (*opisō mou*), lakini katika maana ya "atakae kunifuata" (yaani., kuwa mwanafunzi). Kuna ufuataji usio sahihi (Petro kama mwakilishi wa shetani) ufuataji usio sahihi (yaani., kutokuwa na huduma). Kile Petro alichomsababisha amkemee Yesu sasa kwa wazi kinaelezewa kuwa lengo kwa ajili ya wote, "jitwike msalaba wako"!

◙ **"ajikane"** Hii ni kauli ya kati shurutishi ya wakati uliopita yenye kudokeza "kujikana," "kujikataa," "kutangaza upya," au "kutojijali" (kama vile Mt. 16:24; 20:35,75; Marko 8:34; 14:30,32,72; Luka 9:23; 12:9; 23:34,61; Yohana 13:38). Anguko (kama vile Mwanzo 3) limefanya uhuru wa mwanadamu na ubinafsi kuwa lengo la maisha, lakini sasa waamini lazima wamurudie Mungu toka kwenye kujitegemea kwao wenyewe. Wokovu ni urejesho wa taswira ya Mungu ndani ya mwanadamu, uliyoharibika kwenye anguko. Hii inaruhusu ushirika wa ndani pamoja na Baba, ambao ndio lengo la uumbaji.

◙ **"ajitwike msalaba wake"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita. Kifungu hiki "jitwike msalaba wako" kinarejea kwa mkosaji mwenye hatia akitakiwa kuubeba msalaba wake mwenyewe kwenda mahali pa kusulubiwa. Hii ilikuwa ni stiari ya kitamaduni kwa ajili ya kifo cha aibu, na mateso. Katika muktadha huu kinarejelea kwenye "kifo cha dhambi zetu za asili." Injili ni wito muhimu kwa ajili ya ushirika, uanafunzi wa moja kwa moja (kama vile Mt. 10:38; 16:24; Luka 9:23; 14:27; 17:33; Yohana 12:25). Kama Yesu alivyoutoa uhai wake kwa ajili ya wengine, hivyo tunapaswa kuufuata mfano wake (kama vile 2 Kor. 5:14-15; Gal. 2:20; 1 Yohana 3:16). Hili linaonyesha wazi kuwa matokeo ya anguko yamekwisha ondolewa.

◙ **"na unifuate"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Hii ni lugha ya kiuanafunzi wa sheria za Kiyahudi. Ukristo ni maamuzi ya kumaanisha yakifuatiwa na mwendelezo wa uanafunzi (kama vile Mt. 28:19-20; Efe. 2:8).

**8:35-37 "kuiponya nafsi yake. . .ataiangamiza"** Huu ni mchezo kwenye neno la Kiyunani "mwenyewe," *psuchē*.katika muktadha huu kuna ukinzani kati ya kuishi kiroho (ukitazamia ufalme) na kuishi kibinafsi (maisha ya duniani, kibinafsi). Tafsiri ya Williams ya agano Jipya lina "maisha ya juu. . .maisha ya chini." Kama tukiishi kwa ajili ya Kristo tutaishi milele; tukiishi kwa namna yetu wenyewe tumekufa kiroho (kama vile Mwa. 3; Isa. 59:2; Rum. 5:18-19; 7:10-11; 8:1-8; Efe. 2:1,5; Kol.2:13; Yakobo 1:15) na siku moja tutakufa milele (kama vile Ufu. 2:11; 20:6,14; 21:8). Ukweli huu unafanana na mfano ule wa "tajiri mjinga" (kama vile Lk. 12:16-20).

**8:35 "injili"** Hii ni ambatani ya neno *eu* (nzuri) na *angelos* (ujumbe). Mwanzoni lilimaanisha kutangaza habari njema, lakini lilikuja kutumika kwa ajili ya ujumbe kumhusu Yesu kama Masihi alivyoleta wokovu (na linahusiana na mafundisho). Inasimama kwa ajili ya kweli ya Ukristo na kuitangaza ile kweli. Injili ya marko yawezakuwa ya kwanza kutumika katika maana hii (kama vile Marko 1:1,14-15; 8:35; 10:29; 14:9).

**8:36 "'kuupata ulimwengu wote'"** Hii pia ilikuwa ni moja ya jaribu la Yesu (kama vile Mt. 4:8-9).

◙**"'akapata hasara ya nafsi yake'"** Hii ni kauli tendwa isio na kikomo ya wakati uliopita ya neno lililotumika kuelezea hasara ya kitu ambacho mwanzoni alikuwa akikimiliki (kama vile Mt. 16:26; Mdo. 27:10).

**8:37** Hili ni swali la nguvu. Wapi penye umuhimu wa kwanza, maisha ya sasa au maisha ya milele? Maisha ya ubinafsi yanaondoa furaha ya maisha na zawadi ya maisha! Haya maisha kwa pamoja ni zawadi na utumishi.

**8:38 "'yeyote anioneaye aibu Mimi na maneno Yangu'"** Hili linarejelea kipindi cha wakati ule kila mmoja anakutana na injili. Ukweli huo huo unaelezewa katika namna tofauti katika Mt. 10:32-33 na Luka 12:8-9. Kile watu wanachokiamua siku za leo kuhusu injili ndicho kinaamua maisha yao ya baaadaye. Yesu ni injilil! Kifungu hiki ni sentensi yenye masharti daraja la tatu, inayotanguliza tahadhari (kama vile toleo la TEV na NJB).

◙ **"'katika kizazi hiki cha uzinzi na dhambi'"** Wayahudi katika kipindi cha utulivu walianzisha thiolojia ya zama mbili. Zama za sasa zinatawaliwa na dhambi, ubinafsi, na kutokuwa haki. Angalia Mada Maalum: zama mbili za Wayahudi katika Marko 13:8. Hata hivyo, Mungu alikuwa tayari kumtuma Masihi na kuanzisha enzi mpya ya haki. Yesu anaelezea kuwa Yeye Mwenyewe alikuwa anaianzisha hii siku mpya na kuwa hii haki mpya inategemea (kama vile., ni yenye tahadhari juu yake Yohana 1:12; 3:16) kwenye imani ya mtu na kuamini ndani yake, na sio utendaji wa mwanadamu (kama vile Yer. 31:31-34; Mt. 5:20).

◙ **"'Mwana wa Adamu'"** Huu ni usanifishaji binafsi wa Yesu; hauna masuala ya kitaifa, kijeshi, au ujumuishwaji kwenye karne ya kwanza ya dini ya Kiyahudi. Neno linatokana na matumizi yake katika Ezek. 2:1 na Zaburi. 8:4 ,ambapo lilimaanisha "mwanadamu" na Dan. 7:13, linamaanisha Masihi na Uungu (yaani., kupaa mawinguni, kumkaribia Mungu na kuupokea ufalme wa Mungu). Neno linajumuisha dhana mbili za ubinadamu wa Yesu, Mungu kamili na mwanadamu kamili (kama vile 1 Yohana 4:1-3).

◙ **"atakaporudi"** Agano la Kale kwa uwazi linadhihilisha ujio wa Masihi. Hata hivyo, maisha ya Yesu akiwa hapa duniani yalionyesha kuwa Mwa.3:15; Zaburi 22; Isaya 53; na Zakaria 9-14 zinarejelea mateso ya Masihi. Ujio wa utukufu wa mara ya pili wa Masihi kama Bwana na mwamuzi wa ulimwengu utakuwa ni namna kamili ya Wayahudi walivyokuwa wakimtarajia aje mara ya kwanza. Fikra zao zilizojifunga, mfumo wao wa imani ya kithiolojia ulisababisha wamkatae Yesu. Ujio wa mara ya pili ni kweli kuu na yenye kujirudia katika Agano Jipya (kama vile Mt. 10:23; 16:27-28; 24:3,27,30,37;26:64; Marko 8:38-39; 13:26; Luka 21:27; Yohana 21:22; Mdo. 1:11; 1 Kor. 1:7; 15:23; Flp.. 3:20; 1 The.1:10; 2:19; 3:13; 4:16; 2 The. 1:7,10; 2:1,8; Yakobo 5:;7-8; 2 Pet. 1:16; 3:4,12; 1 Yohana 2:28; Ufu. 1:7).

◙ **"'katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika watakatifu'"** Huu ni utabiri wa Agano la Kale toka kwa Dan. 7:10 (kama vile Mt.16:27; Marko 13:20; Luka 9:26; 2 The. 1:7). Hili linarejelea kwenye ujio wa mara ya pili. Hii ilikuwa ni njia nyingine ya kuutetea Uungu wa Yesu. Mara kadhaa katika injili ya Mathayo malaika ndio wenye kuwakusanya na kuwagawa wanadamu kwenye tukio la siku ile ya mwisho (kama vile Marko 13:39-41,49; 24:31).

◙ **"utukufu"** Katika Agano la Kale maneno ya Kiebrania yaliyozoeleka kwa ajili ya neno "utukufu" (*kabod*) mwanzoni yalikuwa ni maneno ya kibiashara (yenye kurejelea jozi ya mizani) likimaanisha "kitu kizito." Kile kilichokuwa kizito ndicho kilionekana cha thamani au kilikuwa na thamani muhimu. Mara nyingi dhana ya mng'aro iliongezwa kwenye neno kuelezea ukuu wa Mungu (kama vile Kut.15:16; 24:17; Isa. 60:1-2). Yeye peke yake ni wa thamani na kuheshimika. Anang'aa kiasi cha mwanadamu aliyeanguka kutoweza kustahimili (kama vile Kut. 33:17-23; Isa. 6:5). Mungu anaweza kujulikana vizuri kupitia Kristo (kama vile Yer. 1:14; Mt. 17:2; Yohana 14:8-9; Ebr. 1:3; Yakobo 2:1).

Neno "utukufu" kwa kiasi fulani ni lenye utata.

1. Laweza kufanana na lile "Mungu wa utukufu"
2. Laweza kurejea kwenye "utakatifu" au "ukamilifu" wa Mungu
3. Lingalirejea kwenye taswira ya Mungu ambayo mwanadamu aliumbwa kwayo (kama vile Mwa. 1:26-27; 5:1; 9:6), lakini ambao baadaye ulififia kupitia uasi (kama vile Mwa. 3:1-22)

mara ya kwanza limetumika kwa uwepo wa YHWH akiwa na watu wake katika wingu la utukufu kipindi cha kutangatanga nyikani (kama vile Kut. 16:7,10; Law. 9:23; Hes. 14:10).

**9:1** Pamekuwepo na nadharia nyingi kuelezea habari za Yesu. Zingeweza kurejelea kwenye

1. Kupaa kwa Yesu
2. Ufalme uliopo tayari ndani ya Yesu
3. Ujio wa Roho siku ya Pentekoste
4. Kuangamizwa kwa Yerusalemu katika mwaka wa 70 B.K
5. Matarajio ya kurudi haraka kwa Yesu
6. Kuenea haraka kwa Ukristo
7. kitendo cha kubadilika sura.

Hizi nadharia zinatizamisha juu ya vifungu tofauti katika andiko: (1) "baadhi ya watu waliosimama hapa"; (2) "ufalme wa Mungu"; au (3) "kuja kwa nguvu." Ubashiri mzuri ni ule wa #7 kwa sababu ya uharaka wa muktadha wa Marko. 9:2-13 na 2 Pet. 1:16-18. pia, hapana nadharia nyingine zaweza kuelezea hizi dhana zote tatu za andiko. Lakini tambua kama zinaweza, basi zinamrejelea Petro, Yakobo, na Yohana.

◙ **"Amini"** Hii kwa maana iliyo wazi ni "amina." Angalia Mada Maalum katika Marko 3:28.

◙ **"hawataonja mauti"** Hili ni kanusho mara mbili lililotumika kama kifungu cha kiistiari (yaani., ukomo wa maisha).

◙ **"ufalme wa Mungu"** angalia kumbukumbu katika 1:15.

◙ **"umekuja kwa nguvu"** Hii ni kauli tendaji timilifu yenye hali ya kuendelea, ambayo inadokeza ujio kamili wa ufalme wa Mungu. Huu ndio ukinzani uliopo kwa maana kuwa ufalme, kwa maana halisi, ulianzishwa na ujio wa Yesu (yaani.,kujivika umwili wa kibinadamu),lakini tukitarajia tukio la mbeleni (yaani., ujio wa mara ya pili).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana..

1. Je Yesu alilisha makundi makubwa mawili ya watu au palikuwepo na mtu mwingine aliyesaidia kulisha
2. Aina gani ya "ishara" Mafarisayo waliitaka?
3. Kwa nini Yesu aliwakemea wanafunzi?
4. Kwa nini Yesu alipendelea kumponya Yule kipofu kwanza?
5. Kwa nini habari za Mathayo zimejikamilisha zaidi kuliko zile ya Marko kuhusu ukiri wa Petro?
6. Ni nini hasa ukiri wa Petro unadokeza kumhusu Yesu?
7. Kwa nini wanafunzi walipata mshangao kwenye mafundisho ya Yesu kuhusu kifo chake huko Yerusalemu?
8. Elezea kwa maneno yako kile mistari ya 34-38 inamaanisha.

# MARKO 9

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Kugeuzwa kwa Yesu | Yesu anabadilika juu Ya mlima | Ugeukaji | Ugeukaji | Ugeukaji |
| 9:2-8 | 9:2-13 | 9:2-8 | 9:2-6 | 9:2-8 |
| | | Unabii juu ya Eliya | 9:7-8 | Swali juu ya Eliya |
| 9:9-13 | | 9:9-13 | 9:9 | 9:9-13 |
| | | | 9:10-11<br>9:12-13 | |
| Uponyaji wa kijana Mwenye pepo Mchafu | Kijana anaponywa | Mtoto mwenye kifafa anaponywa | Yesu anamponya kijana mwenye pepo mchafu | Pepo la kifafa |
| 9::14-29 | 9:14-29 | 9:14-29 | 9:14-16 | 9:14-29 |
| | | | 9:17-18<br>9:19-20a<br>9:21b-22<br>9:23<br>9:24<br>9:25<br>9:26-27<br>9:28<br>9:29 | |
| Yesu anatabiri kifo Chake na Ufufuo | Yesu tena anatabiri kifo Chake na ufufuo | Mateso yanatabiriwa | Yesu tena anaongea juu ya Kifo chake | Utabiri wa pili wa mateso |
| 9:30-32 | 9:30-32 | 9:30-32 | 9:30-31<br>9:32 | 9:30-32 |
| Nani mkubwa Zaidi? | Nani mkubwa zaidi? | Ukuu wa kweli | Nani mkubwa zaidi | Nani mkubwa? |
| 9:33-37<br>9:34-37 | 9:33-37 | 9:33-37 | 9:33 | 9:33-37 |
| Yeye asiye Kinyume chetu Yu upande wetu | Yesu anakataza udhehebu | mpunga pepo asiyejulikana | yeye asiye kinyume chetu yu upande wetu | Juu ya kutumia jina la Yesu |
| 9:38-41 | 9:38-41 | 9:38-41 | 9:38<br>9:39-41 | 9:38-42 |
| | | | | ukarimu unaoneshwa Kwa wanafunzi wa Kristo |
| 9:41 | | | | |
| Jaribu la dhambi | Yesu anaonya juu Ya makosa | Maonyo ya Kuzimu | Jaribu la dhambi | juu ya kuwapoteza wengine |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 9:42-50 | 9:42-48<br>Chumvi isiyokuwa<br>Na ladha haina<br>Thamani | 9:42-48<br>wanafunzi walio<br>kama chumvi | 9:42-48 | 9:42-50 |
| | 9:49-50 | 9:49-50 | 9:49 | |
| 9:50a | | | | |
| 9:50b | | | | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI(Kutoka"Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## ULINGANIFU WA UFANANO WA VITABU VYA INJILI

A. Marko 9:2-8 inafanana na Mt. 17:1-8 na Luka 9:28-36.
B. Marko 9:9-13 inafanana na Mt. 17:9-13 na Luka 9:36.
C. Marko 9:14-29 inafanana na Mt. 17:14-20 na Luka 9:37-43.
D. Marko 9:30-32 inafanana na Mt. 17:22-23 na Luka 9:43-45.
E. Marko 9:33-37 inafanana na Mt. 18:1-5 na Luka 9:46-48.
F. Marko 9:38-50 inafanana na Mt. 18:6-14 na Luka 9:49-50.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 9:2-8**
**[2]Hata baada ya siku sita Yesu akawatwaa Petro, na Yakobo, na Yohana, akawaleta juu ya mlima mrefu faraghani,**
**peke yao; akageuka sura yake mbele yao; [3]mavazi yake yakimeta-meta, meupe mno, jinsi asivyoweza dobi duniani**
**kuyafanya meupe. [4]Wakatokewa na Eliya pamoja na Musa, nao walikuwa wakizungumza na Yesu. [5]Petro akajibu,**
**akamwambia Yesu, Rabi, ni vizuri sisi kuwapo hapa; na tufanye vibanda vitatu, kimoja chako wewe, kimoja cha**
**Musa, na kimoja cha Eliya. [6]Maana, hakujua la kunena, kwa kuwa waliingiwa na hofu nyingi. [7]Kisha likatokea**
**wingu, likawatia uvuli; sauti ikatoka katika lile wingu, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, msikieni yeye. [8]Mara**
**hiyo walipotazama huku na huku, hawakuona mtu pamoja nao ila Yesu peke yake. atakapokuwa amefufuka katika wafu.**

**9:2 "siku sita"** Luka 9:28 ina "siku nane." Maelezo ya kama muda huo dhahiri sio ya kawaida katika Injili ya Marko.

◙**"Petro, na Yakobo, na Yohana"** Hili kundi la ndani la wanafunzi walikuwa marazote wapo katika matukio makubwa makubwa (kama vile Marko 5:37). Tukio hili lilikuwa na uzito kwo kama ilivyokuwa kwa Yesu.

◙**"juu ya mlima mrefu"** Desturi zinasema (yaani Injili ya Waebrania isiyokuwa ya ki-kanoni) inasema kwamba ilikuwa ni Mlima Tabor, lakini yawezekana ilikuwa moja vya mipando ya milima ya Mlima Hermon.

Mtu anaweza kushangaa ikiwa tajiriba hii ilikuwa namna ya kiuandishi ya kumuaksi tajiriba ya Mlima Sinai.

1. mlima mrefu
2. wingu
3. uso kutukuzwa (Kutoka 34:29)
4. kipindi cha siku sita (kama vile Kutoka 24:16)

Mada hii ya Kutoka (yaani Yesu kama Musa mpya, kutoa agano jipya, kuwatoa watu Wake katika utumwa wa dhambi) ni maelezo yanayojirudia rudia katika Marko. Katika Injili ya Luka, inasema Yesu, Musa na Eliya walijadili juu ya safari ya wokovu ya Yesu.

◙**"peke yao"** Luka 9:28 inataja kusudi la "kuomba."Yesu alitaka kukaa mbali na umati wa watu na ili awafundishe wanafunzi kwa faragha. Katika hali hii alikuwa na darasa la ndani la uongozi.

◙**"akageuka sura yake mbele yao"** Hii ni kauli tendwa elekezi ya wakati uliopita usio timilifu wa ambatani*meta* (yaani baada) na*morphoō* (yaani Muundo), ikiwa na matokeo ya kimaana ya "kubadili mwonekano wa mtu." Tunapata neno la Kiingereza "metamorphosis" kutoka katika neno la Kiyunani. Mg'ao wa Yesu unaonesha utukufu wa sasa udumuo kupitia mwili wake wa duniani. Mg'ao wa Uuungu wake wa kweli ulionekana kwa wanafunzi hawa (kama vile 2 Pet. 1:16-18). Neno*morphē* (kama vile Flp. 2:6-7) inaashiria hali ya kuhimu ya kutobadilika kwa kitu au mtu (kinyume cha *schēma*, kama vile Flp. 2:8, hali ya nje ibadilikayo).

Mageuzi haya haya yanawezekana kwa wafuasi wake (kama vile Rum. 12:2; 2 Kor. 3:18). Katika namna hii inarejerea urejesho wa taswira ya kimungu ndani ya mwanadamu, iliyoharibiwa katika Anguko la Mwanzo 3. Yesu anatuwezesha sisi kufanyika wanadamu wa kweli, tufananao na Kristo.

**9:3**
**NASB** **"mavazi yake yakimeta-meta, meupe mno"**
**NKJV** **"mavazi yake yakimeta-meta, meupe mno"**
**NRSV** **"mavazi yake yakimeta-meta, meupe mno"**
**TEV** **"mavazi yake yakimeta-meta, kwa mg'ao mweupe sana"**
**NJB** **"mavazi yake yakimeta-meta, kwa mg'ao mweupe wa ajabu"**

Mathayo 17:2 inaongeza kwamba"Sura yake ilig'aa kama Jua." Hii hakika ni kipengele cha utukufu wa Yesu ambao mara kwa mara una kiambata cha mg'ao (kama vile angalizo kamili katika Marko 8:38).

**NASB, NKJV** **"jinsi asivyoweza dobi duniani kuyafanya meupe"**
**NRSV** **"jinsi asivyoweza dobi duniani kuyafanya meupe"**
**TEV** **"meupe sana kiasi kwamba hakuna dobi duniani awezaye kuyafua"**
**NJB** **"nyeupe sana kiasi kwamba hakuna dobi duniani awezaye kuyafanya meupe"**

Hii inarejerea kwa mfanyakazi aliyefanya kazi ya kusafisha nguo.
Ni katika mistari kama hii vitabu vya historia vinakuwa vya msaada sana. Niruhusu nikutajie kadhaa ambavyo vimenisaidia mimi kuelewa desturi ya Mashariki ya Karibu ya Kale.

1. Roland de Vaux, *Ancient Israel*, two vols.
2. Fred H. Wright, *Manners and Customs of Bible Lands*
3. James M. Freeman, *Manners and Customs of the Bible*
4. Jack Finegan, *Light From the Ancient Past*, two vols.
5. James S. Jeffers, *The Greco-Roman World of the NewTestament Era*
6. K. A. Kitchen, *Ancient Orient and the Old Testament*
7. Edwin M. Yamauchi, *The Stones and the Scriptures*

**9:4 "Eliya. . .Musa. . .Yesu"** Hii inaonesha ufunuo wa Mungu unaoendelea.Tazama inavyoonekana tayari walikuwa na miili yao ya ufufuko jambo linashangaza kuhusiana na ufahamu wa 1 The. 4:13-18. Hawa wawili walikuwa watu mashuhuri katika Agano la Kale waliowahi kuwa na sehemu yaunabii wa matukio ya siku za mwisho (yaani Eliya mbele ya Masihi na Musa, nabii kama Yesu).

◙**"Wakatokewa"**Neno hili linatumika katika kutokea kwa malaika katika Luka 1:11 na 22:43, na Yesu katika Luka 24:34.

◙**"nao walikuwa wakizungumza na Yesu"** Hiki ni kifungu cha maneno cha wakati usio kamilifu, ambayo inamaanisha yalikuwa ni mazungumzo ya muda mrefu. Luka 9:31 inasema walikuwa wakizungumzia kuondoka kwa Yesu (yaani safari ya ukombozi) kutoka Yerusalemu. Kuna athari ya ajabu kati ya kifungu hiki cha habari na Kutoka 24:12-18.
1. kipengele cha muda "siku sita" (Marko 9:2)
2. sehemu, "juu ya mlima mrefu" (Marko 9:2)
3. uwepo wa wingu na Mungu akizungumza ndani yake (Marko 9:7 )
4. kutajwa kwa utukufu wa sura ya Musa na hapa sura ya Yesu (Luka 9:29; Kutoka 34:29-30)

**9:5 "Petro akamwambia Yesu"** Luka 9:32 inasema wanafunzi watatu walikuwa wamesinzia baada ya siku ndefu na mpando wa mlima mkali na Petro aliamka kwa muda kumuona Eliya na Musa wakiondoka.

◙**"'Mwalimu'"** Ile inayofanana ya Mathayo ina "Bwana" na ya Luka ina "Mkuu."

◙**"ni vizuri sisi kuwapo hapa"** Ni ufahamu na tajiriba nzuri kiasi gani ya kiroho na kimwili hii ilifanyika kuwa; ni uthibitisho wa namna gani wa Yesu kama Masihi aliyehaidiwa katika Agano la Kale.

◙**"vibanda"** Hii lazima lilikuwa nijengo lifananalo na vijumba vyenye kuezekwa kwa majani vitumikavyo wakati wa sherehe za Madhabahu. Maana ya kauli ya Petro ilikuwa kwamba ikiwa wageni wa Agano la Kale wenye utukufu wangeendelea kukaa zaidi, wao pia wangeendelea kukaa kwa muda mrefu zaidi!

**9:6** Wakati wote ambapo Petro hakuwa anajua nini cha kufanya, alizungumza!

**9:7 "wingu"** Huu ulikuwa ni uwakilishi wa uwepo wa YHWH katika safari ya ukombozi (kama vile Kutoka. 13-14). Walimu wa Kiyahudi waliita hii "wingu la Utukufu *Shekinah*," ikiwa na maana kwamba YHW amekaa waziwazi na kwa kudumu na Israeli..

◙**"likawafunika"** Neno hili linaaksi nama ya Agano la Kale la wingu maalumu la uwepo wa YHWH kutoa kivuli (yaani ulinzi) na uongozi kwa watu wa Mungu wakati wa kipindi cha kutanga tanga Jangwani (yaani miaka 38 ). Wingu hili lilitokea tena mara tatu likihusianishwa na Yesu.
1. wakati wa kutungiwa kwake mimba Mariamu alifunikwa na Roho (kama vile Luka 1:35)
2. wakati wa Ubatizo, Yesu anaaambiwa na sauti kutoka mbinguni (wingu lenyewe halitajwi kwa udhahiri, kama vile Mt. 3:17)
3. wakati wa Ubadilikaji wake sauti inasikika (kama vile Mt. 17:5; Luka 9:34)

Neno hili linatumika mara mbili katika Agano Jipya, mara moja juu ya kivuli cha Petro kuwaangukia watu na kusababisha uponyaji wao (kama vile Mdo. 5:15) miundo ya ambatani ya neno katika Ebr. 9:5, ikirejerea Kerubi kufunika kwa kivuli juu ya Kiti cha Rehema katika Sanduku la Agano.

◙**"sauti"** Hii ni aidha (1) inahusiana na YHWH kuzungumza kutokea katika wingu katika jangwa au (2) ile *Bath Kol* (yaani sauti kutoka mbinguni), ambayo ilikuwa njia ya Mungu ya kufunua mapenzi ya YHWH wakati wa kipindi cha ukimya kati ya Agano la Kale na Agano Jipya (kama vile Marko 1:11).

◙**"Mwanangu Mpendwa"** Neno "mwana" katika tungo hii ya Agano la Kale lilitumika (1) Israeli nzima; (2) Mfalme wa Israeli kama mwakilishi wa YHWH; na(3) Masihi ajaye aliyehaidiwa (kama vile Zaburi 2:7). Hii ni mara ya pili kwamba

Baba anamwambia mwanawe katika namna hii maalumu kwa cheo hiki maalumu (kama vile Mt. 3:17; 17:5). Angalia angalizo kamili katika Marko 1:11 na Mada Maalumu katika Marko 3:11.

◙**"Msikilizeni Yeye"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo ambayo inaaksi unabii wa Kumb. 18:15. Kilele cha ufunuo wa Baba ni mkutambuliwa na kupewa utii (kama vile Luka 6:46).

**9:8** Mstari huu unamaanisha aidha kwamba (1) jambo hili lilikuwa ni maono au (2) mabadiliko ya ghafla yaliyotokea katika ulimwengu unaoonekana.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 9:9-13**
**9Na walipokuwa wakishuka mlimani aliwakataza wasimweleze mtu waliyoyaona, hata Mwana wa Adamu atakapokuwa amefufuka katika wafu. 10Wakalishika neno lile, wakiulizana wao kwa wao, Huko kufufuka katika wafu maana yake nini? 11Wakamwuliza, wakisema, Mbona waandishi hunena ya kwamba imempasa Eliya kuja kwanza? 12Akajibu akawaambia, Ni kweli Eliya yuaja kwanza, na kurejeza upya yote; lakini, pamoja na haya, ameandikiwaje Mwana wa Adamu ya kwamba atateswa mengi na kudharauliwa? 13Lakini nawaambia, Eliya amekwisha kuja, nao wakamtenda yote waliyoyataka kama alivyoandikiwa.**

**9:9 "Na walipokuwa wakishuka mlimani aliwakataza wasimweleze mtu waliyoyaona, hata Mwana wa Adamu atakapokuwa amefufuka katika wafu"** Hapa palikuwa ni mahali pekee ambapo suala la muda linahusianishwa na maonyo ya kujirudia rudia juu ya ukimya wao (kama vile Marko 5:43; 7:36; 8:30). Katazo hili linatokana na ukweli kwambaa injili ilikuwa bado haijakamilika. Kwa wakati wa baadaye, kumbukumbu zao za tukio hili lingeweza kueleweka vizuri zaidi katika ufahamu wa matukio mengine ya injili (kama vile 2 Pet. 1:16-18).

**9:10 "wakiulizana wao kwa wao, Huko kufufuka katika wafu maana yake nini?"** Wanafunzi hawakuelewa utofauti kati ya "Kuja kwa Mara ya Pili" (8:38) na "Ufufuo" (9:9). Wayahudi siku za Yesu walitegemea kuja mara moja tu kwa Masihi katika Historian a kuja huku kulihusianishwa na ushindi wa kivita na utawala na ukuu wa taifa la Israeli juu ya mataifa yote duniani. Angalia MADA MAALUMU: UFUFUO katika Marko 8:31.

**9:11 "waandishi"** Hawa kiutamaduni walikuwa wafasiri wa Agano la Kale wanaoheshimika ambao walielezea namna inavyofananishwa na siku zao. Katika muda huu wengi wa Waandishi walikuwa Mafarisayo.Angalia Mada maalumu katika Marko 2:6.

**9:12-13 "Ni kweli Eliya yuaja kwanza. . .Eliya amekwisha kuja"** Yesu anaelezea kwamba Yohana Mbatizaji alikuwa ametimiliza jukumu lake la kiunabii la Eliya linalopatikana katika Mal. 3:1 na 4:5. Kumekuwako na mjadala sana juu ya jibu ambalo Yesu alitoa. Kibayana alitaja kwamba Eliya alikuwa tayari amekwisha kuja katika huduma ya Yohana Mbatizaji (kama vile Mt. 11:10, 14; Marko 9:11-13; Luka 1:17). Hata hivyo wakati Mafarisayo walipouliza Yohana Mbatizaji mwenyewe katika Injili ya Yohana (Yohana 1:20-25) ikiwa alikuwa ni Eliya, yeye alikataa waziwazi. Huku kutofautiana kunaweza kutatuliwa na ukweli kwamba Yohana kwamba alikuwa ni Eliya aliyefufuka, lakini Yesu alikiri kwamba Yohana kiuwakilishi alitimiliza maandalizi ya Eliya. Wote walivaa na kufanya kazi kwa kufanana, hivyo utambulisho wao ungekuwa wazi na dhahiri katika akili za Wayahudi waliokuwa wakijua juu ya Eliya na waliosikia kumuona Yohana Mbatizaji (Luka 1:17).

**9:12 "atateswa mengi na kudharauliwa"** Hili lilikuwa jambo la kushangaza kwa Wayahudi wa siku za Yesu waliotegemea mkombozi mwenye nguvu kama mahakimu wa Agano la Kale na hawakuwa wakitegemea mwokozi atesekekaye. Walikuwa wamekoswa utambuzi kadhaa wa Agano la Kale (yaani Mwa. 3:15; Zaburi 22; Isa. 52:13-53:12; Zekaria9-14). Iliwagharimu wanafunzi kumi na mbili miaka ya kuelewa; hata hawakuweza kuelewa kikamilifu mpaka huduma maalumu ya Roho ya Pentekoste (kama vile Yohana 16:13-14) ilivyowafunulia. Tambua kwamba Yesu anajaribu kujihusisha na wanafunzi kumi na mbili kwa namna ya mantiki ya kithiolojia. Analazimisha kuona uhusiano kati ya unabii tofauti mbili. Hawakuwa rasmi "waandishi," lakini punde lazima wafanye kazi kama wao. Yesu aliwashangaza kwa kutimilizwa kusikotarajiwa ambako kulikuwa dhahiri lakini kiuandishi (yaani Yohana Mbatizaji alifanya kazi kama utimilifu wa kuja kwa Eliya na kuandaa njia kwa ajili ya Masihi). Yesu alichukua muda wake wa faragha kufundisha wanafunzi wake. Hata

akiwa njiani kutoka mlimani anaanzisha jambo linalofanana (yaani utabiri wa Malaki juu ya Eliya). Hii ni kukamata kila fursa kwa ajili ya mafunzo ya kidini inayoaksiwa katika Kumb. 6:7 na 11:19.

**9:13 "kama alivyoandikiwa"** Eliya alikuwa anapitia mateso kutoka kwa Yezebeli (kama vile 1 Wafalme 19:2,10,14) kama ilivyokuwa Yohana kutoka kwa Herodia.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 9:14-29**
**[14]Hata walipowafikia wanafunzi, waliona mkutano mkuu wakiwazunguka, na waandishi wakijadiliana nao; [15]mara mkutano wote walipomwona walishangaa, wakamwendea mbio, wakamsalimu. [16]Akawauliza, Mnajadiliana nini nao? [17]Mtu mmoja katika mkutano akamjibu, Mwalimu, nimemleta mwanangu kwako, ana pepo bubu; [18]na kila ampagaapo, humbwaga chini, naye hutoka povu na kusaga meno na kukonda; nikasema na wanafunzi wako wamtoe pepo, wasiweze. [19]Akawajibu, akasema, Enyi kizazi kisichoamini, nikae nanyi hata lini? Nichukuliane nanyi hata lini? Mleteni kwangu. [20]Wakamleta kwake; hata alipomwona, mara yule pepo alimtia kifafa; naye akaanguka chini, akagaa-gaa, akitokwa na povu. [21]Akamwuliza babaye, Amepatwa na haya tangu lini? Akasema, Tangu utoto. [22]Na mara nyingi amemtupa katika moto, na katika maji, amwangamize; lakini ukiweza neno lo lote, utuhurumie, na kutusaidia. [23]Yesu akamwambia, Ukiweza! Yote yawezekana kwake aaminiye. [24]Mara babaye yule kijana akapaza sauti, akasema, Naamini, nisaidie kutokuamini kwangu.[25]Naye Yesu akiona ya kuwa mkutano unakusanyika mbio, akamkemea yule pepo mchafu, akamwambia, Ewe pepo bubu na kiziwi, mimi nakuamuru, mtoke huyu, wala usimwingie tena. [26]Akalia, akamtia kifafa sana, akamtoka; naye akawa kama amekufa; hata wengi wakasema, Amekufa. [27]Lakini Yesu akamshika mkono akamwinua naye akasimama. [28] Hata alipoingia nyumbani, wanafunzi wake wakamwuliza kwa faragha, Mbona sisi hatukuweza kumtoa? [29] Akawaambia, Namna hii haiwezi kutoka kwa neno lo lote, isipokuwa kwa kuomba.**

**9:14 "Hata walipowafikia wanafunzi"** Yesu alikuwa amewaacha wanafunzi waliosalia chini ya mlima. Luka 9:37 inasema walirudi siku inayofuata.

◙**"mkutano mkuu. . .waandishi wakijadiliana nao"** Vitu hivi vyote viwili vilitengeneza sifa ya huduma ya Yesu na sasa wanafunzi walikuwa wakipitia kivuli cha hali iliyokuwepo ya Yesu na pia kuja kwao katika huduma.Haya yalikuwa ni matatizo yanayojirudia rudia lakini pia fursa.

**9:15 "mara"** Angalia Angalizo katika Marko 1:10.

◙**"walishangaa"** Baadhi wanaona kama mshangao huu unahusiana na sura ya Yesu kuendelea kug'aa ikihusianishwa na Kutoka 34:29-30, lakini muktadha unaonekana kumaanisha kwamba mwonekano wa Yesu ulikuja wakati sahihi kwa ajili ya huduma na mafundisho

**NASB** **"wakamwendea mbio kumsalimu"**
**NKJV** **"wakamkimbilia kumsalimu"**
**NRSV** **"wakakimbia mbele kumwamkia"**
**TEV** **"wakamkimbilia na kumsalimia"**
**NJB** **"wakakimbia kumwamkia"**

Hii njeo ya wakati usio timilifu inaweza kumaanisha (1) mwanzo wa matendo (kama vile NASB) au (2) kurudiwa kwa kitendo kwa wakati uliopita. Umati huu wa watu ulikuwa na furaha kumuona Yesu na mmoja baada ya mwingine alikimbia na kumsalimia.

**9:16 "mnajadiliana nao nini"** Yesu alijadili swali hili pamoja na makutano ya watu. Waandishi hawakuwa na shida na kijana lakini kipengele cha kithiolojia cha wanafunzi kutoweza kumponya.

**9:17 "amepagawa na pepo"** Injili inaweka utofauti wa kiuhalisia kati ya kupagawa na pepo na ugonjwa wa mwili. Katika tukio hili kuna kiza katika kutoa tofauti. Dalili zinaelezwa na baba na maana ya maneno kadhaa ya Kiyunani katika

maandiko yanamaanisha kifafa, na hasa kujiuma uma.Kipengele hiki kilipelekewa au kuchochewa na kupagawa na pepo. Angalia Mada Maalumu: Mpagawa Mapepo katika Marko 1:23.

**9:18 "kukonda"** Haya ni maelezo ya kukamatwa na kubwagwa kwa kiwango cha juu.

◙**"nikasema na wanafunzi wako wamtoe pepo, wasiweze"** Wanafunzi walishangazwa pia. Yesu aliwapatia nguvu juu ya mapepo katika Marko 6:7,13, lakini kujaribu kwao katika tukio hili kulishindikana!

**9:19** Yesu anatumia maswali yasiyohitaji majibu katika Marko 9:19 kuelezea kukatishwa kwake tama juu ya kukosa imani kwa wanafunzi, makutano na waandishi.

**9:20 "pepo alimtia kifafa; naye akaanguka chini, akagaa-gaa, akitokwa na povu. "** Huku kulikuwa ni kupagawa na pepo kulikojidhihirisha kwenyewe katika namna ya kifafa.

**9:21** Kuna hadithi kadhaa katika Injili juu ya kupagawa na pepo kwa watoto. Namna gani na kwanini hili linatokea haitolewi maelezo.

**9:22** Asili ya uharibifu wa kipepo katika maisha ya huyu kijana unaonekana vizuri katika maelezo ya baba wa mtoto.

◙**"kuharibu"** Angalia Mada maalum: *Apollumi* katika Marko 3:6.

◙**"ikiwa"** Hii ni sentensi yenye masharti ya daraja la kwanza aambayo inadhaniwa kuwa kweli kulingana na mtazamo wa mwandishi kwa ajili ya makusudi ya kifasihi. Huu ulikuwa ni ukiri wa imani wa baba katika uweza wa Yesu wa kuponya.

◙**"'utuhurumie na utusaidie'"** Baba huyu alikuwa na imani. Kwa Yesu hata pale ambapo wanafunzi walishindwa kumkomboa mtoto wake.Katika*Word Studies in the NewTestament*, vol. 1. Ukurasa wa 113, M. R. Vincent anaweka wazo kwamba baba huyu alitambua kwa ukamilifu matatizo ya kijana wake, kama ilivyokuwa mwanamke mwenye asili ya syro-Foinike kwa binti yake (kama vile Mt.15:22).

**9:23 "'ukiweza'"** Huku ni kurudia kauli ya mtu huyu ya Marko 9:22. Ni sentensi nyingine yenye masharti ya daraja la kwanza. Mtu huyu alikiri uweza wa Yesu;sasa Yesu anajaribu imani yake.

◙**"'yote yawezekana kwake yeye aaminiye'"** Hii sio hundi wazi isiyojazwa chochote kwa wanadamu, hata wanadamu waaminio ili kumchezea Mungu bali ni ahadi kwamba Mungu atafanya mapenzi Yake kupitia imani ya kuamini (angalia GordonFee, *The Disease of the Health and Wealth Gospels*). Kuna masharti mawili: (1) mapenzi ya Mungu na (2) imani ya kuamini! Angalia Mada maalumu: Maombi yenye kumaanisha katika Marko 11:23.

**9:24 "naamini, nisaidie kutoamini kwangu'"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Kumbuka sio kusudio la imani wala kiasi kilicho cha muhimu (kama vile Mt. 17:20; Luka 17:6). Tazama kwamba Yesu alifanya kazi pamoja na mashaka ya mtu huyu kama ambavyo atafanya na kwetu.
Yesu anashughulikia imani ya baba na sio ya kijana kwasababu amekwisha pagawa tokea utotoni.Mtu anaweza kushangaa ikiwa moja ya sababu ya wanafunzi kutoweza kumtolea pepo kijana ilikuwa ni kwasababu ya baba kukosa imani kwao. Yesu mara kwa mara aliangalia imani ya wazazi au marafiki katika kusababisha matibabu na ukombozi. Maneno haya ya baba kukiri hitaji lake kusihi msaada wa Yesu kumsaidia katika imani yake. Haya ni maombi ambayo wengi wetu tulitakiwa tuombe! Toleo la Textus Receptus linaongeza *kurie* (yaani kazi ya Bwana), ambayo inaweza kuwa nyongeza ya kiuandishi kuonesha imani ya baba kwa kumtaja Yesu kama Bwana, lakini nyongeza hii haipo katika fasiri yoyote ya kisasa ya Kingereza kuachilia KJV na NKJV.

**9:25 "makutano wakakusanyika kwa haraka"** Haijulikani kwa namna gani hii inahusiana na upungaji pepo. Ni kinyume cha Siri ya ki-Masihi inayopatikana mara kwa mara katika Marko. Yesu anaonesha nguvu Yake na mamlaka katika hali ya

wanafunzi ambayo hawakuweza kushughulikia. Kusonga songa na shauku ya makutano siku zote ilikuwa tatizo lakini pia fursa.Hii inaweza kuwa makutano yaleyale katika Marko 9:14-15 au wengi zaidi ya wapya waliojiunga na makutano.

◙**"'wewe pepo bubu na kiziwi'"** Inavyoonekana hiki kilikuwa ni kipengele kingine wa matatizo ya kimwili ya kijana huyu (kama vile Marko 9:17) inayohusiana na kupagawa na pepo.

◙**"'mtoke na usimwingie tena'"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu na kauli tendaji tegemezi ya wakati uliopita usio timilifu "mtoke na usimwingie tena."

**9:26** Udhihirisho wa kimwili unaoendana na utokwaji wa kimapepo unaonekana kuwa jambo la kawaida lililozoeleka katika Agano Jipya wakati wa upungaji wa pepo.

◙**"kijana akawa mtu aliyekufa"** Hii ni dalili nyingine ya kubanwa, kubwagwa chini kwa kiwango cha juu.

**9:27 "Yesu akamshika kwa mkono na kumwinua"** Hatua hizi zilimwonesha kujali na huruma ya Yesu (kama vile Marko 1:31; 5:41). Hakuwa na hofu kugusa wagonjwa na waliopagawa na mapepo!

**9:28 "'Kwanini hatukuweza kumtoa'"** Walishangazwa sana! Mwanzoni walikuwa na uwezo wa kutoa pepo; kwanini sasa hawawezi? Mathayo 17:20 inasema ni kwasababu ya udogo wa imani yao .

**9:29 "Namna hii haiwezi kutoka kwa neno lo lote, isipokuwa kwa kuomba."** Maandiko mengine mengi ya Kiyunani yanaongeza "na kwa kufunga." Hatahivyo hii haipatikani katika אau B, wala maandiko ya Kiyunani yanayotumiwa na Klement. Nyongeza ya tungo ni ya kale na imesambaa, yawezekana kwa sababu ya uvuguvugu wa kanisa la kwanza kutoka katika dini ya Kiyahudi katika eneo hili. Inajumuishwa katika MSS $P^{45}$, $אi^{2}$, A, C, D, K, L, W, X, na Diatessaron. Angalia Mada Maalumu juu ya Kufunga katika Marko 2:18-20. Toleoo la $UBS^{4}$ linatoa usomaji mfupi alama ya "A" (hakika). Kithiolojia habari hii inamaanisha kwamba kuna aina nyingi za mapepo ambazo zinahitaji mbinu tofauti tofauti. Angalia Mada Maalum katika Marko 1:25.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 9:30-32**
**30 Wakatoka huko, wakapita katikati ya Galilaya; naye hakutaka mtu kujua. 31 Kwa sababu alikuwa akiwafundisha wanafunzi wake, akawaambia, Mwana wa Adamu yuaenda kutiwa katika mikono ya watu, nao watamwua; hata akiisha kuuawa, baada ya siku tatu atafufuka. 32 Lakini hawakulifahamu neno lile, wakaogopa kumwuliza.**

**9:30 "wakapita katikati ya Galilaya"** Haya bado ni mazingira ya kuacha Mlima wa Mgeuko na kuelekea kusini kupitia Galilaya. Yesu alitaka binafsi kuzungumza na watu wengi kadiri inavyowezekana.

◙**”naye hakutaka mtu kujua"** Hiki ni kipengele kingine cha shauku ya Yesu kutojulikana kama mponyaji au mtenda miujiza kwasababu ya kusongwa songwa na makutano kutafuta msaada wa kimwili kulikomsabaisha kushindikana kwake kufundisha na kuhubiri.

**9:31 "Mwana wa Adamu"** Angalia angalizo katika Marko 8:38c.

◙**"kutiwa katika mikono"** Hii ni kauli tendwa elekezi ya wakati uliopo. Neno linamaanisha "kuwaachia mamlaka." Hii ilikuwa mara ya tatu ambayo Yesu alijifunua vizuri kwa wanafunzi kile ambacho kingetokea katika Yerusalemu (kama vile Marko 8:31; 9:12).

◙**"'atafufuka'"** Angalia Mada Maalumu katika Marko 8:31.

◙**"siku tatu"** Katika kuandika muda kwa Kiyahudi, ilikuwa kama takribani masaa 30-38 (yaani muda kidogo wa Ijumaa kabla ya machweo, Jumamosi zote na sehemu ya Jumapili kabla ya jua kuzama). Kipindi cha Muda huu inaunganishwa na tajiriba ya Yona mara kadhaa (kama vile Mt. 12:39-40; 16:3; Luka 11:29-32).

**9:32 "hawakuelewa"** Hii ni mada inayojirudia rudia katika vitabu vya Injili. Injili ya Luka inafunua hali hii kiuhalisia.

1. wanafunzi hawakuelewa (Luka 2:50; 9:45; 18:34)
2. walitakiwa kuwa na maneno ya Yesu kwasababu maneno hayo yalifasiriwa kwa ajili yao (Luka 8:10)
3. Yesu alifungua akili za wanafunzi (Luka 24:45)

Walikuwa vipofu kama makutano mpaka maneno ya Yesu na ya Roho alipofungua fahamu mzao zilizofungwa na mioyo kuelekea katika kweli ya agano jipya. fahamu ya mwanadamu aliyeanguka haiwezi kuelezwa isipokuwa kwa msaada wa Roho na hata ni mchakato wa taratibu kutoka wokovu kuelekea kutakaswa.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 9:33-37**
**33 Wakafika Kapernaumu; hata alipokuwamo nyumbani, akawauliza, Mlishindania nini njiani? 34 Wakanyamaza; kwa maana njiani walikuwa wakibishana wao kwa wao, ni nani aliye mkubwa. 35 Akaketi chini, akawaita wale Thenashara akawaambia, Mtu atakaye kuwa wa kwanza atakuwa wa mwisho kuliko wote, na mtumishi wa wote.**
**36 Akatwaa kitoto, akamweka katikati yao, akamkumbatia, akawaambia, 37 Mtu akimpokea mtoto mmoja wa namna hii kwa jina langu, anipokea mimi; na mtu akinipokea mimi, humpokea, si mimi, bali yeye aliyenituma.**

**9:33 "Kapernaumu"** Mji huu, nyumbani kwa Petro na Andrea ilifanyika kuwa makao makuu ya Yesu baada ya kutoamini kwa Nazareti.

◙**"alipokuwamo nyumbani"** Hii yawezekana ilikuwa nyumbani kwa Petro (kama vile Marko 1:29) au nyumba ya kupanga iliyotumiwa na Yesu.

◙**"mlishindania nini njiani?"** Walikuwa wakibishana na sio tu kufanya majadiliano. Alikuwa maewaambia juu ya kifo Chake (mara tatu) na walitaka kujua nani kati yao angechukua nafasi ya kuwa kiongozi (kama vile Mt. 18:1-18; Luka 9:46-48; 22:24).

**9:34 "mkuu"** Hii inaonesha wivu wa makundi mengine ya wanafunzi dhidi ya kikundi cha ndani cha kina Petro, Yakobo na Yohana. inaweza kuaksi dhana yao ya kiyahudi ya ufalme wao wa duniani wa kitaifa.

**9:35 "akaketi"** Hii ingeashiria vipindi rasmi vya mafundisho (kama vile Marko 4:1; 9:35; Mt. 5:1;Luka 4:20).

◙**"atakaye kuwa wa kwanza"** Hii ni sentensi yenye masharti ya daraja la kwanza ambayo inadhaniwa kuwa kweli kutoka katika mtazamo wa mwandishi. Yesu hakushutumu malengo lakini katika namna ya maadili ya ufalme wa Mungu. Ukuu unahusianishwa na huduma (kama vile Marko 10:31,45; Mt. 20:26; 19:30; Yohana 13:5), si kwa ajili ya kutawala au nguvu! Ufalme wa mbinguni unatofautiana na jamii za wanadamu. Maneno haya ni mifano mizuri ya namna gani Yesu alirudia mafundisho yake katika mazingira tofauti tofauti na katika nyakati tofauti tofauti (kama vile Marko 10:43-44; Mt. 23:11; Luka 22:24-25).

◙**"mtumishi"** Yesu alizungumza Kiaramu. Msemo huu (yaani Marko 9:35-37) unaweza kuwa mzaha wa neno la Kiaramu*talya*, ambayo linamaanisha vyote "mtoto" namtumishi."

**9:36 "akamchukua mtoto"** Mathayo 18:1-18, Luka 9:46-49, hapa kwa ufasaha inaonesha kwamba Yesu anazungumza juu ya waamini wapya, sio watoto.

◙**"akambeba katika mikono yake"** Haya ni maelezo ya ushuhuda mwingine wa Petro. Inawezekana ikawa nyumba ya Petro na mtoto wa Petro!

**9:37 "'Mtu akimpokea mtoto mmoja wa namna hii kwa jina langu'"** "kwa Jina Langu" inamaanisha "katika sifa ya Yesu." Hakuna miujiza katika urudiaji wa maneno fulani. Nguvu inakuja kutokana na kumjua Yesu na kuiga matendo yake. Mwitikio wetu wa upendo kwa wengine kwasababu tu wafuasi wa Yesu ni njia ya kuelezea upendo wetu kwake (kama vile Mt. 25:31-45). Kutoka Mdo. 19:13-16 Tunajua kwamba wapunga pepo wa Kiyahudi walitumia jina la Yesu lakini kwa

matokeo yaliyoshangaza. Kutoka Mt. 7:21-23 tunajua kwamba ni uhusiano binafsi pamoja na Kristo ambacho ni muhimu, sio utani au hata kwa kurudia rudia kulitaja jina.

◙**"'na mtu akinipokea mimi, humpokea, si mimi, bali yeye aliyenituma'"** Kitabia Yesu anakiri nafasi ya kutukuzwa ya Baba. Hii imeandikwa katika Injili ya Yohana kwa kurudiwa rudiwa.Unyenyekevu huu kwa Baba sio kwa Yule ambaye hana cheo cha kulingana na mwingine bali kazi ndani ya Utatu.

## MADA MAALUMU: KUPELEKWA *(apostellō)*

Hili ni neno la kiyunani la kawaida kwa “kupelekwa” (yaani *apostellō*). Neno hili lina matumizi kadha ya kithiolojia:

1. Katika kiyunani cha sasa na kwa Wayahudi waliokuwa na elimu na viongozi wa dini, neno hili hutumiwa kama moja inayoitwa na kutumwa kama mwakilishi rasmi wa mwingine, kitu kama kiingereza chetu “Balozi”. (kama vile. 2 Kor. 5:20).
2. Injili daima zinatumia kitenzi hiki kwa Yesu kutumwa na baba yake, katika Yohana, linasikika zaidi kama Masihi (kama vile Mt. 10:40; 15:24; Marko 9:37; Luka 9:48 na hasa Yohana 5:36, 38; 6:29, 57; 7:26; 8:42; 10:36; 11:42; 17:3, 8, 18, 21,23 25; 20:21 (Yote “*apostellō*” na KISAWE CHAKE*pempō* inayotumika katika mst. 21). Inatumika kwa Yesu kutuma waumini (kama vile. Yn 17:18; 20:2121 [Yote "*apostellō*na KISAWE CHAKE ni "*pempō*" katika Yohana 20:21]).
3. Agano Jipya lilituma jina “Mtume” kwa wanafunzi
    a. Mitume kumi na wawili wa mwanzo kama mzunguko wa kwanza kati ya wanafunzi wake. (Marko 6:30; Luka 6;13; Matendo 1:2; 26)
    b. Kundi maalumu la msaada la Mitume na watumishi wenzie.
        1) Barnabasi (kama vile. Matendo 14:4, 14)
        2) Andronicus na Junias (KJV, Junia , kama vile. Rum. 16:7)
        3) Appollo (kama vile. 1 Kor. 4:6-9)
        4) Yakobo ndugu wa Bwana (kama vile. Gal. 1:19)
        5) Silvanus na Timotheo (kama vile. 1The. 2:6)
        6) Bila shaka Tito (kama vile 2 Kor. 8:23)
        7) Bila shaka Epafrodito (kama vile. Efe. 2:25)
    c. Zawadi inayoendelea katika kanisa (kama vile. 1 Kor. 12:28-29; Efe 4:11)
4. Paulo anatumia cheo hiki kwa ajili yake katika barua zake nyingi kama njia ya kuonesha mamlaka yake aliyopewa na Mungu kama mwakilishi wa Kristo. (kama vile. Rum. 1:1 1 Kor. 1:1; Gal. 1:1; Efe. 1:1; Kol. 1:1; Tim. 1:1 2Tim. 1:1; Tito 1:1).
5. Tatizo tunalokumbana nalo kama waamini wa leo ni kwamba Agano Jipya halitafasiri hii zawadi inayoendelea inahusu nini au vipi inabainishwa kwa waamini. Bila shaka mtu apaswa kutofautisha kati kumi nambaili ya awali (# 3b) na matumizi ya baadaye (# 3b). Tazama Mada Maalumu: Msukumo na Mada Maalumu: Mwangaza. Kama mitume wa leo hawakusukumwa kuandika maandiko mengi matakatifu (yaani, kitabu cha Wayunani kanoni kimefungwa, kama vile Yuda mst. 3; tazama. Mada Maalumu: kanuni ya kanisa) kisha kipi wanafanya tofauti na Manabii wa Agano Jipya na Wainjilisti (kama vile Efe. 4:11) hapa kuna uwezekano wa mambo.
    a. Waanzilishi wa kanisa la wamisionari huanza katika maeneo yasiyo ya uinjilisti (kutumika kama vile katika *Doache*)
    b. Viongozi wa Wachungaji katika eneo fulani au madhehebu.
    c. ? Napenda # 1.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 9:38-41**
**[38] Yohana akamjibu, akamwambia, Mwalimu, tulimwona mtu akitoa pepo kwa jina lako, ambaye hafuatani nasi; tukamkataza, kwa sababu hafuatani nasi. [39]Yesu akasema, Msimkataze, kwa kuwa hakuna mtu atakayefanya mwujiza kwa jina langu akaweza mara kuninenea mabaya; [40]kwa sababu asiye kinyume chetu, yu upande wetu. [41]Kwa kuwa ye yote atakayewanywesha ninyi kikombe cha maji, kwa kuwa ninyi ni watu wa Kristo, amin,**

**nawaambia, hatakosa thawabu yake.**

**9:38 "tukamkataza, kwa sababu hafuatani nasi "** Kuna utofautiano kadhaa katika maandiko ya Kiyunani.Mstari huu ni mgumu kuufasiri. Hii ilisababisha waandishi wa kale kuuurekebisha. Toleo lisomwalo zaidi la Kingereza cha kisasa linakubali (ikifuatiwa na toleo la UBS[4]) linapatikana katika MSS, א na B na fasiri ya kitamaduni ya Kiashamu.

**9:39 "'Msimkataze'"** Hii ni kauli shututishi ya wakati uliopo ikiwa na kiambata hasi ambayo mara nyingi inamaanisha kusitisha kitendo kilicho katika mchakato.

**9:40 "kwa sababu asiye kinyume chetu, yu upande wetu"** Yesu mara kwa mara alitumia mithali za kiutamaduni katika mafundisho Yake (kama vile Marko 2:17,21,22; 3:27; 4:21,22,25; 7:15; 8:35,36,37; 9:40,50; 10:25,27,31,43-44). Linganisha na Mt. 12:30 na Luka11:23. Kuna mjadala wa kuvutia sana juu ya kinachoonekana kuwa mvutano kati ya Marko 9:40 and na Luka 11:23 katika *Hard Sayings of the Bible* kilichochapishwa na IVP, kurasa za 466-467. Kitabu hiki ni raslimali yenye msaada kwa wanataaluma na wapeleka injili mashuhuri. Wanaelezea kwamba mazingira ya kimuktadha ya rejea yanaondoa kile kinachoonekana kuwa hali ya kutokukubaliana.

**9:41** Angalia vifungu vinavyofanana katika Mt. 10:42; 25:40. Kuna ulinganifu mkali sana kati ya Marko 9:38-41 na Marko 9:42-48.Wale ambao hawajaunganishwa rasmi kwa Yesu wanatambuliwa kwa matendo yao meme lakini wale ambao wanamfahamu Yeye wanaonywa kwa sitiari kali juu ya majukumu yao kwa waamini wapya. Mtawanyiko huu wa kushangaza unaelezea ukweli wa Marko 9:33-37. Pia katika mstari huu kunatajwa thawabu za ufalme kwa wale ambao wanamtumikia kwa uaminifu (kama vile Marko 9:41; 10:21,28-31 na mara kadhaa katika mahubiri ya Mlimani Mathayo 5:12,46; 6:5-6,16-18,19-21). Ni ngumu kuweka uwiano sawa wa wokovu huru katika kazi iliyomalizika ya Kristo na majukumu ya kiagano ya waaminio kwa kuiishi imani yao. Pia ni ngumu kuweka uwiano sawa dhana za viwango vya thawabu za Agano Jipya na adhabu (kama vile Mt. 10:45; 11:22;18:6; 25:21,23; Marko 12:40; Luka 12:47-48; 20:47).Angalia Mada Maalumu katika Marko 12:40.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 9:42-48**
**42Na ye yote atakayemkosesha mmojawapo wa wadogo hawa waniaminio, afadhali afungiwe jiwe la kusagia shingoni mwake, na kutupwa baharini. 43Na mkono wako ukikukosesha, ukate; ni afadhali kuingia katika uzima u kigutu, kuliko kuwa na mikono miwili, na kwenda zako jehanum, kwenye moto usiozimika;44 ambamo humo funza wao hafi, wala moto hauzimiki.45Na mguu wako ukikukosesha, ukate; ni afadhali kuingia katika uzima, u kiwete, kuliko kuwa na miguu miwili, na kutupwa katika jehanum; 46ambamo humo funza wao hafi, wala moto hauzimiki.**
**47Na jicho lako likikukosesha, ling'oe, ulitupe; ni afadhali kuingia katika ufalme wa Mungu, una chongo, kuliko kuwa na macho mawili, na kutupwa katika jehanum; 48ambamo humo funza wao hafi, wala moto hauzimiki.**

**9:42 "'Na ye yote atakayemkosesha mmojawapo wa wadogo hawa'"** Hii kithiolojia inarejerea kwa waamini wapya. Hatahivyo kunaweza na kuwa na uhusiano wa kimuktadha kwa somo lililofundishwa kutoka kwa kijana aliyepagawa na pepo. Mungu anawapenda watoto na hataki mtui yoyote kuwaonea.

◙**"'waniaminio'"** Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo ambayo inasisitiza imani kuendelea. Baadhi ya maandiko ya Kiyunani ya kale "in Me nadi yangu" (kama vile MSS A, B, C2, L, W, na Vulgate, Kiashamu, na fasiri ya Koptiki). Hii inaonekana kuwa na nyongeza ya kiuandishi kutoka kwa ufanano katika Mt. 18:6 kwasababu MSS א na C. Angalia Mada Maalumu katika Marko 1:15.

◙**"'kuwakosesha'"** Hii kifasihi inatumika wakati wa chambo cha mnyama aliyewekewa mtego.

◙**"'ikiwa'"** Hii ni sentensi ya daraja la kwanza yenye masharti. Haya ni maonyo makali kwa viongozi wa Kikristo. Mchungaji Mkuu hujali juu ya kondoo wote haswa wapya na wale walio hatarini, hivyo lazima na wao wafanye hivyo!
Hii ni utiaji chumvi (kama vile Mt. 5:29,30,38-46; 6:2-4; 7:3-5; 23:23-24; 10:24-25). Yesu anazungumza katika lugha ya kisitiari juu ya hukumu ya milele. Kauli za utiaji chumvi za kipindi hikli zimewachanganya waamini wa magharibi kwa

vizazi. Upendo wetu kwa Biblia na shauku yetu kumfuata Yesu kumesababisha waaminio wa Magharibi kukosa sitiari na aina ya uandishi wa mashariki wa Biblia.

◙**"'jiwe kubwa la kusagia'"** Hii inarejerea juu ya sehemu ya juu yenye duara ya jiwe kubwa la wanyama la kusagia. Hii ni utiaji chumvi mwingine wa Kimashariki uliotumika kuweka msisitizo juu ya ujumbe Wake.

◙**"'na kutupwa baharini'"** Hii ni kauli tendwa elekezi ya wakati timilifu ambayo inaashiria hali ya kudumu. Hii ilikuwa sitiari kali sana juu ya hukumu. Wakiwa watu wa jangwani, Wayahudi walikuwa waoga wa maji.

**9:43-47** Hii ni lugha ya ki-sitiari (yaani kutriwa chumvi) lakini inaonesha kujitoa kusikobadilika kunakodaiwa na Yesu (kama vile Robert H. Stein, *The Method and Message of Jesus' Teachings,* kurasa 8-11). Mistari hii ni mifano mizuri ya ushairi wa Waebrania yenye ufanano, iliyozoeleka katika Agano la Kale (kama vile Marko 2:21-22; 3:4,24-25,28; 4:22,30; 8:17,18; 9:43-47; 10:38,43-44; 13:24-25). Baadhi ya mifano katika Marko juu ufanano hasi ya Marko 2:19-20; 3:28-19; 4:25; 7:8,15; 8:35 (kama vile Stein, kurasa 27-29).

**9:43 "ikiwa"** Hii ni sentensi ya daraja la tatu leye masharti ambayo inazungumzia tendo linalotakikana.

◙**"'kuingia katika uzima'"** Kuna maneno mawili kwa ajili ya uhai/uzima katika Agano Jipya: (1) *bios* (yaani maisha ya duniani) na (2) *zoē* (yaani maisha ya kiroho). Yesu anazungumzia juu ya kuingia katika ulimwengu wa roho (yaani uzima wa milele). Hii inafanana na tungo" Ufalme wa Mungu" katika Marko 9:47. Waaminio wanaweza kuingia katika ufame sasa na kwa namna flani kupata ladha ya kimbingu kwa sasa (kama vile Efe. 2:5-6).
Kuna njia kadhaa zinazoelezwa katika Agano Jipya.

1. ulimwengu ujao, uzima wa milele (Marko 10:17,30)
2. kuokoa . .kupoteza uzima (Marko 8:35; Mt. 10:39; Luka 17:33)
3. kuingia katika uzima (Marko 9:43; Mt. 25:46)
4. kuingia katika furaha ya Bwana (Mt. 25:21,23)

◙**"'kuzimu'"** Hii ni*Gehenna* (kama vile Yer. 7:31). Hii ilikuwa ni eneo la kuabudia lamungu moto wa ustawi wa Foenike, Molech, katika bonde la wana wa Hinnon kusini tu mwa Yerusalemu. Hii ilikuwa ambapo watoto wa kwanza waliozaliwa walikuwa wakitolewa sadaka kwa mungu wa ustawi wa Wakanaani (kama vile Law. 18:21; 20:2-5; Kumb. 12:31; 18:10; 2 Wafalme.21:6; 2 Nyakati 28:3; 33:6; Yer. 2:23; 7:32; 32:35).Wayahudi walikuwa wanaona aibu juu ya ibada za sanamu za mababu zao kwamba waligeuza eneo hili kuwa sehemu ya kumwaga taka Yerusalemu. Sitiari za Yesu kwa ajili ya utengwaji wa milele kutoka katika upendo wa Baba (moto, minyoo, kunuka harufu mbaya) unawekwa mbali na utupaji wa taka hii. Neno hili linatumika na Yesu mara nyingi lakini mara moja tu kwa mwandishi mwingine wa Agano Jipya (Yakobo 3:6). Kuzimu ni halisi kama Mbingu ilivyo halisi kibiblia (kama vile Mt. 25:46). Angalia Mada Maalumu hapa chini, II., B.

## MADA MAALUM: Wafu Wako Wapi?

Paulo alilitumia neno hili mara nyingi kwa namna tofauti lakini katika maana zinazoshabihiana. Mara nyingi lilihusiana na utimilifu wa imani ya waamini (mfano 1 Tim. 1:1). Hili laweza kuellezewa kama utukufu, maisha ya milele, hatima ya wokovu, ujio wa mara ya pili, n.k. Utimilifu huu unajulikana, bali sula la muda ni mbeleni na halijulikani. Tumaini mara nyingi lilihusiana na “imani” na “upendo” (kama vile 1 Kor. 13:13; 1 The. 1:3; 2 The. 2:16).
Orodha ya muda ya baadhi ya matumizi ya Paulo ni:

1. Ujio wa mara ya pili, Gal. 5:5; Efe. 1:18; 4:4; Tit. 2:13
2. Yesu ni tumaini letu, 1 Tim. 1:1 (Mungu ni tumaini letu, 1 Tim. 5:5; 1 Pet. 3:5)
3. Waamini kuwasilishwa mbele ya Mungu, Kol. 1:22-23; 1 The. 2:19
4. Tumaini likewekwa mbinguni, Kol. 1:5
5. Imani katika injili, Kol. 1:23; 1 The. 2:19
6. Hatma ya wokovu, Kol. 1:5; 1 The. 4:13; 5:8

7. Utukufu wa Mungu, Rum. 5:2, 2 Kor. 3:12; Kol. 1:27
8. Wokovu wa watu wa mataifakupitia Kristo, Kol. 1:27
9. Uhakika wa wokovu, 1 The. 5:8
10. Maisha ya milele, Tit. 1:2; 3:7
11. matokeo ya ukomavu wa Mkristo, Rum. 5:2-5
12. ukombozi wa uumbaji wote, Rum. 8:20-22
13. kukubali utimilifu, Rum. 8:23-25
14. wadhifa wa Mungu, Rum. 15:13
15. shauku ya Paulo kwa waamini, 2 Kor. 1:7
16. agano la Kale kama mwongozo wa waamini wa Agano Jipya, Rum. 15:4

**9:44,46** Mistari 44 na 46 ni sawasawa katika Marko 9:48. Wala hayapatikani katika maandiko ya kale ya Kiyunani, א, B, CL, au W. Inaonekana kwamba mwandishi wa kale alichukua maneno kutoka Marko 9:48 na kuyaingiza katika Marko 9:44 na 46.

**9:48 "'ambamo humo funza wao hafi, wala moto hauzimiki.'"** Hii ni nukuu kutoka Isa. 66:24. Wayahudi walishangazwa kwamba mababu zao waliwachoma watoto wao (2 Wafalme. 21:6) kwamba walibadili eneo hili mpaka katika shimo la taka la Yerusalemu. Ni kutoka katika hili eneo ambalo Yesu alitoa lugha yake ya kisitiari kuhusu kutengwa milele kutoka kwa Mungu—Kuzimu. Neno lile lile milele linatumika juu ya mbingu katika Mt. 25:46, pia inatumika katika mstari ule ule wa hukumu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 9:49-50**
**[49]Kwa sababu kila mtu atatiwa chumvi kwa moto. [50]Chumvi ni njema; lakini chumvi ikiwa si chumvi tena, mtaitia nini ikolee? Mwe na chumvi ndani yenu, mkakae kwa amani ninyi kwa ninyi.**

**9:49 "'atatiwa chumvi kwa moto'"** Chumvi ilimaanisha kuponywa, kusafishwa na kuhifadhiwa. Pia ilitumika kuweka muhuri maagano (kama vile Hes. 18:19). Ilikuwa ni kipengele muhimu sana cha maisha kwa watu wa jangwani. Maneno chumvi na moto yanafanana katika muktadha huu kwa ajili ya kusafishwa. Mstari wa 49 una aina tofauti tofauti za maandiko mengi. Hizi zilikuwa kwasababu ya kutojulikana kwa (1) namna gani mstari unahusiana na Marko 9:48 au (2) mstari huu wenyewe ulihusu nini. Yawezekana mwandishi aliona rejea kwa Law. 2:13 na kujiweka katika pambizo wa andiko. Yesu mara kwa mara alitumia chumvi kama ulinganifu wa kuzungumza ukweli wa kiroho (kama vile Mt. 5:13; Luka 14:34-35).

**9:50** Mstari huu kama Marko 9:49, unaonekana kwa namna flani kutofanana na muktadha uliopita. Kama Marko 9:49 ilijumuishwa kwasababu ya neno "moto," mstari huu ulijumuishwa kwasababu ya neno "chumvi." Inaweza kurejerea kwa Marko 9:35. Ina kuwa na maana namna Wakristo wanavyoishi!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini Yesu "alibadilishwa?"
2. Namna gani tukio hili linahusiana na Agano la Kale?
3. Kwanini Wanafunzi walichanganyikiwa juu ya Eliya?
4. Kwanini wanafunzi bado hawakuelewa juu ya kifo cha Yesu na Ufufuo?
5. Je ni vibaya kwa Mkristo kuwa mwenye ndoto?
6. Namna gani Yesu anauangalia ukuu?

7. Je Yesu anazungumzia juu ya watoto katika Marko 9:35-37 na 42 au kuwatumia kama mifano kwa ajili ya watu wazima?
8. Je haya ni matamko juu ya hukumu?
9. Je tuichukue Marko 9:43-47 kama ilivyo?
10. Je chumvi huwakilisha nini?

# MARKO 10

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Mafundisho Kuhusu Talaka | Ndoa na Talaka | Kuhusu Ndoa | Yesu Anafundisha | Swali kuhusu Talaka |
| 10:1-12 | 10:1-12 | 10:1 | 10:1 | 10:1-12 |
| | | 10:2-9 | 10:2 | |
| | | | 10:3 | |
| | | | 10:4 | |
| | | | 10:5-9 | |
| | | 10:10-12 | 10:10-12 | |
| Watoto Wadogo Waliobarikiwa | Yesu Anawabariki Watoto wadogo | Kuwabariki Watoto Kuwabariki Watoto | Yesu Anawabariki Watoto | Yesu na Wadogo Watoto |
| 10:13-16 | 10:13-16 | 10:13-16 | 10:13-16 | 10:13-16 |
| Mtu Tajiri | Yesu Anamhasa Kijana Tajiri | Mtu Tajiri | Mtu Tajiri | Mtu Tajiri |
| 10:17-22 | 10:17-22 | 10:17-22 | 10:17 | 10:17-22 |
| | | | 10:18-19 | |
| | | | 10:20 | |
| | Kwa Mungu Mambo yote Yanawezekana | | 10:21-22 | Hatari ya Mali |
| 10:23-31 | 10:23-31 | 10:23-27 | 10:23 | 10:23-27 |
| | | | 10:24-25 | |
| | | | 10:26 | |
| | | | 10:27 | |
| | | | | Malipoya Kanusho |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 10:28-31 | 10:28<br>10:29-31 | 10:28-31 |
| Utabiri wa Kifo ya<br>Chake na Ufufuo wake | Kwa mara ya Tatu<br>Yesu anatabiri juu ya Kifo na Ufufuko wake | Kazi yay a Kutabiri<br>kwa mara ya Tatu | Yesu Anazungumzia<br>Kifo chake kwa Mara ya Tatu | Unabii wa Mara<br>Tatu wa kuhusu Huduma |
| 10:32-34 | 10:32-34 | 10:32-34 | 10:32-34 | 10:32-34 |
| Ombi la Yakoo na Zebedayo<br>Yohana | Ukuu ni Kutumika | Yakobo na Yohana<br>Wanataka Ukuu | Ombi la Yakobo na<br>Yohana | Wana wa<br>watoa ombi |
| 10:35-45 | 10:35-45 | 10:35-40 | 10:35<br>10:36<br>10:37<br>10:38<br>10:39-40 | 10:35-40<br><br><br><br>Uongozi na |
| Huduma | | | | |
| | | 10:41-45 | 10:41-45 | 10:41-45 |
| Uponyaji wa Anaponywa<br>Kipofu | Yesu Anamponya<br>Bartimayo Kipofu | Bartimayo Kipofu<br>Bartimayo Kipofu | Yesu Anamponya<br>huko Yeriko | Kipofu |
| 10:46-52 | 10:46-52 | 10:46-52 | 10:46-47<br>10:48<br>10:49<br>10:50<br>10:51a<br>10:51b<br>10:52 | 10:46-52 |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka"Mwongozo wa Usomaji  Mzuri wa Biblia")**
*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo wa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## UFANANO WA VITABU VYA INJILI

A. Talaka, Marko 10:2-12 (sawa na katika Mathayo 19:1-12)
B. Kuwabariki Watoto, Marko 10:13-16 (sawa na katika Mathayo 19:13-15; Luka 18:15-17)
C. Kijana Mdogo Mwenye Mali, Marko 10:17-31 (sawa na katika Mathayo 19:16-20:16; Luka 18:18-30)
D. Utabiri wa Kusulibiwa, Marko 10:32-34 (sawa na katika Mathayo 20:17-20; Luka 18:31-34)
E. Wana wa Zebedayo, Marko 10:35-45 (sawa na katika Mathayo 20:21-28)
F. Bathromayo Kipofu, Marko 10:46-52 (sawa na katika Mathayo 20:29-34; Luka 18:35-43)

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB ( LILILOBORESHWA) MARKO 10:1**
**[1] Akaondoka huko akafika mipakani mwa Uyahudi, na ng'ambo ya Yordani; makutano mengi wakakutanika tena wakamwendea; akawafundisha tena kama alivyozoea.**

**10:1 "Akaondoka huko akafika mipakani mwa Uyahudi, na ng'ambo ya Yordani "** Toleo la RSV na ASV lina kifungu "akaja katika maeneo ya Yudea na -Yordani." Huu muktadha unamaanisha kwamba Yesu alikuywa katika safarai yake ya mwisho ya kuelekea Yerusalemu. Kwamna iliyo dhahiri, alikwenda kaskazini kupitia Samaria, akakaribia katika Galilaya, na kuungana na umati wa wanahija waliokuwa wakielekea Yerusalemu. Wayahudi wengi walikataa kupitia Samaria wakatai wakiwa njiani kuelekea Yerusalemu, hivyo walipitia upande wa mashariki ya Yordani (yaani, kupitia Perea) na kisha wakatokea upande wa mashariki huko Yeriko. Ikiwa hili ndilo lililotokea basi linaeleza juu ya mstari huu wenye mkanganyiko (kama vile A. T. Robertson, *Word Pictures in the NewTestament*, juzuu 1, uk. 348, anadai kwamba robo tatau ya Injli ya Luka inajitokeza kati ya Marko 9 na 10 [yaani., 9:57-18:14]; pamoja na Mt. 18 na Yohana 7-11).

◙ **"makutano mengi wakakutanika tena wakamwendea"** Kipengele hiki kinaweza kurejerea (1) wanahija waliokuwa wakielekea Yerusalemu kwa ajili ya sikukuu au (2) wagonjwa, wachunguzi, viongozi wa Kiyahudi, na wa wanafunzi. Mara nyingi Yesu aliwahubiria makutano.

◙**" kama alivyozoea"** Kwa wakati wote Yesu alikuwa na nafasi ya kufundisha, Alifanya hivyo (kama vile Marko 1:21; 2:13; 4:2;6:2,6,34; 12:35; 14:49). Maudhui ya ujumbe wake yalikuwa

1. toba na kuamini (kama ulivyo ujumbe wa Yohana Mbatizaji)
2. ufalme wa Mungu unapatikana kwa kuwa na imani katika Yeye
3. ufalme wa Mungu hubadili namna ya kufikiri kwa mtu na maisha yake kwa ujumla.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 10:2-9**
**[2]Basi Mafarisayo wakamwendea, wakamwuliza, Je! Ni halali mtu kumwacha mkewe? Huku wakimjaribu. [3] Naye akajibu, akawaambia, Musa aliwaamuru nini? [4] Wakasema, Musa alitoa ruhusa kuandika hati ya talaka na kumwacha. [5] Yesu akawaambia, Kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu aliwaandikia amri hii. [6] Lakini tangu mwanzo wa kuumbwa ulimwengu, aliwafanya mume na mke. [7] Kwa sababu hiyo mtu atamwacha babaye na mamaye,**

**ataambatana na mkewe; [8] na hao wawili watakuwa mwili mmoja; hata wamekuwa si wawili tena, bali mwili mmoja. [9] Basi alichokiunganisha Mungu, mwanadamu asikitenganishe.**

**10:2 "**Mafarisayo" Tazama Mada Maalum : Mafarisayo katika Marko 2:16.

◙ **" wakimjaribu"** Hili neno *periazō* lina maana nyingine ya kujaribu kwa wazo la uharibifu (kama vile Marko 8:11; 10:2; 12:15; Mada Maalum kuhusu maneno ya "kujaribu" katika Marko 1:13). Swali hili lilimaanisha (1) kutofautisha kati ya maoni ya watu na walimu wa Sheri za Kiyahudi juu ya shule mbili za sheria za Kiyahudi za Shammai (zilizoshikilia ukale) na Hillel (yenye mabadialiko) au (2) kuiamsha hasira ya Herode Antipasi.

◙ **"Ni halali mtu kumwacha mkewe"** Tambua kwamba swali la Mafarisayo linahusu taraka, si ndoa. Pia, tambua kwamba Yessu anajibu swali la kipekee. Yesu analijadili suala hili katika muundo wa kawaida. Hawa Mafarisayo wanajaribu kumnasa katika kujitenga kwake na (1) wafuasi wa Hillel, Ambaye alikuwa na mtazamo wa kimabadiliko kuhusu taraka. Mathayo 19:3 inapanua swali ili kulijumuisha swali "Kwa nini" au taraka au (2) Herode Antipasi kwa sababau alikuwa ametarakisha (kama vile Marko 6:17-20). Hili neno "halali" lingeweza kuirejelea Sheria ya Musa au mila za walimu wa sheria za Kiyahudi (yaani, Buku la Sheria za Kiyahudi). Katika kujibu Yesu anakinukuu kifungu cha Kumbukumbu la Torati.

**10:4 " kuandika hati ya talaka"** Hii ni nukuu inayoka katika Kumb. 24:1-4. Musa aliweka utaratibu wa sheria kwa ajili ya kumlinda mwanamke (kama vile Kumb. 21:1-11). Huu utaratibu wa sheria ulikuwa na mahitaji kadha wa kadha.

1. ulichukua muda fulani
2. ulimchukua kuhani aua Mlawi kwa ajili yake
3. huenda ilihitaji kurudisha mahari

   Kwa hali hali ya matumaini, hatua hizi zingewapa wenza fursa ya kufanya mapatano.

Pia lazima ielezwe kwamba Kumb. 24 inatoa dhahanio la kuoa aua kuolewa tena kwa wote mwanamume na mwanamke. Hata hivyo, katika muktadha huu kifungu cha kitabu cha Kumbukumbu la Torati hakikutoa maelezo ya suala la utamaduni wa talaka pamoja na (1) kuhakikisha ubikra na uaminifu wa mwali na (2) kutoa muhtasari wa hatua muhimu na mipaka ya ndoa.

Tatizo halisi lilitokea katika mabadiliko ya fasiri ya kifungu hiki kwa shule za sheria za Kiyahudi ya Hillel (kama vile *The Christ of the Gospels* na J. W. Shepherd, kr. 451-457). Shule hii ililichagua neno "uovu" na kuipanua asili yake na maana yake. Mafarisayo walikuwa wakimnukuu Musa kwa ajili ya kumtega Yesu. Hawakuwa na haja ya kujifunza. Yesu alilihimarisha kusudi la Mungu katika ndoa kama mtu mmoja, mke mmoja maishani. Hakuna kilicho kamili. Talizo linakuja katika namna ya kuweka ulinganifu wa maneno ya Yesu katika muktadha huu panoja na maneno yake ya msamaha kataika muktadha mwingine. Kipimo cha Ufalme kwa waamini kiko juu, lakini, hivyo, ni neema ya Mungu! Katika eneo hili ukaribu wa kipengele kimoja hdi kingine ni bora zaidi kuliko miongozo ya kisheria yenye mkazo. Katika Agano la Kale YHWH alitumia talaka kueleza matendo ya watu wake juu ya Israeli kwa sababu ya wao kuabudu sanamu (kama vile Isa. 50:1; Yer. 3:1-8; Hos. 2:2). Kuna mifano kataika Agano la Kale ambapo taraka inahitajika (kama vile Mwa. 21:8-14; Kut. 21:10-11; Kum. 21:10-14; Ezra 9-10). Kuna wazo zuri sana lenye kuchokonoa makala katika "Journal of the Evangelical Theological Society" juzuu. 40 # 4, entitled "*Old Testament Perspectives on Divorce and Remarriage*" na Joe M. Sprinkle.

**10:5 "' Kwa sababu ya ugumu wa mioyo yenu'"** Yesu anawaeleza Waisraeli kama "wenye mioyo migumu" (kama vile Eze. 2:4; 3:7). Hili neno "kujitwalia mamlaka" ni kisawe cha sitiari (kama vile Kut. 32:9; 33:3,5,9; Kumb. 9:6,13). Mara nyingi hawa walitaka kufanya mambo katika namna yao. Mara nyingi hii ni shauku ya mwanadamu aliyeanguka! Mtazamo huu ulikuwa hata ndani ya wanafunza wake (kama vile Marko 3:5 na 6:52).
Suala la talaka ni mfano mzuri wa tatizo la kuyachunguza maandiko. Yatupasa kuiruhusu Biblia izungumze kila kitu. Hiki si kifungu pekee cha kibiblia kinachozungumzia talaka na ndoa.

Huu usemi wa Yesu unanitisha. Ni namna gani naweza kujua kwamba Kut. 24:1-4 halikuwa neno la la YHWH la mwisho kuhusiana na suala hili? Hili limo ndani ya Biblia. Ikiwa Yesu hakulipinga suala hili,huenda mimi kamwesiwezi kuhujua

uhusiano wa mipaka yake. Tatizo ni maandiko mangapi ya Agano la Kale yamehusishwa katika kifungu "ugumu wa miyo" na ni mara ngapi Mungu amekuwa na mapenzi kwetu? Faraja pekee inakuja katika mtazamo wa mfumo wa kweli wa masuala ya kithiolojia, kwa kuyachukulia maagano yote na hali za kihistoria (mfano, Marko 7:14-16,17-23). Wakristo wa Kiinjili ni wepesi kuyachunguza kweli ya maandiko, maadiko yenye dosari. Kithiolojia, Kupinga kwa Yesu juu ya Musa ni jambo linaloshangaza. Hii ilikuwa njia yenye nguvu ya kudai mamlaka yake. Hwa wanfunzi wa Kiyahudi wangekuwa wameshangazwa kwamba Yesu alifahamu kuwa kuna jambo alilolifanya Musa na alikuwa na uweza na mamlaka toka kwa YHWH kuyarudisha haya. Kipengekle hiki
kilicho katika Markoni ufanano wa kithiolojia wa Mt. 5:17-48.

**10:6 " mwanzo wa kuumbwa ulimwengu"** Tazama MADA MAALUM:*KTISIS* ifuatayo.

## MADA MAALUM: *KTISIS*

Neno hili, *ktisis*, lilitumika katika namna mbalimbali katika Agano Jipya. The lexicon kilichoandikwa na Louw na Nida kinaorodhesha uwezekano ufuatao.

1. uumbaji (tendo la uumbaji, kama vile Marko 13:19; Rum. 1:20-22; Efe. 3:9)
2. kiumbe (kile ambacho kimeiumbwa ili kiwe hai, kama vile Marko 10:6; Rum. 1:25; 8:39; Kol. 1:15;23)
3. ulimwengu (vyote vilivyoumbwa, kama vile Marko 13:19; Rum. 8:20; Ebr. 9:11)
4. taasisi (kama vile 1 Pet. 2:13, [#42.39])
5. mamlaka (kama vile 1 Pet. 2:13, [#37.47])

Paulo pia anaupa uhusika wa uhai uumbaji katika Rum. 8:18-25. Anaupa tabia uumbaji mpya wa Mungu, zama mpya na zama za Roho katika 2 Kor. 5:17 na Gal. 6:15. Waamini wanatakiwa waishi kama raia wa nyakati mpya (kama vile Rum. 6:4).

◙**"' aliwafanya mume na mke'"** Ndoa ilikuwa katika mpango wa uumbaji asilia wa Mungu asilia (kama vile Mwa. 1:27). Tendo la ndoa/ ni zawadi toka kwa Mungu ili kulikamilisha kusudi lake la kuijaza nchi (kama vile Mwa. 1:28).

**10:7 "'mtu atamwacha babaye na mamaye'"** Nukuu nyingine inayotoka katika kitabu cha Mwanzo (kama vile Marko 2:24). Hili linaonyesha thamani kubwa ya ndoa, hata juu ya mamlaka ya kizazi. Kulikuwa na utengano muhimu wa kifikra toka kwa wazazi hata kama si utengano wa kimwili (yaani., vizazi kadhaa vilivyoishi kwa pamoja).

**10:8 "' na hao wawili watakuwa mwili mmoja'"** Pia nukuu hii inatoka katika Mwa. 2:24. Katika ndoa,wawili huwa mwali mmoja —kimwili, kihisia, na katika kila namna. Hili linaonyesha kudumu kwa ndoa katika mpango wa Mungu. Musa aliishi miaka mingi tofauti na matukio yaliyoandikwa katika kitabu cha Mwanzo. Katika kipengele cha uumbaji wa Mwanzo anasema suala la kipaumbele cha ndoa kilichofuatia katika mrejeo wa mpangilio wa wale wawili wa mwanzo.

**10:9 "' alichokiunganisha Mungu'"** Kiuhalisia hili ni tendo la "kufungamanishwa pamoja." Taraka ni moja ya njia ya wanadamu aliyeanguka kuweka kando kile alichokihimarisha Mungu kama desturi za kijamii (yaani., ndoa ni nguzo ya jamii imara kama vile Kumb. 5:16,33; 4:40; 32:47, "siku zenu zipate kuongezeka na mpate kuenenda katika nchi ambyo Bwana wenu aliowajalia").Huu ni mfano mzuri wa agano la mwamini mwenye shauku ya/
kuyafanya mapenzi ya Mungu.

◙**"' mwanadamu asikitenganishe'"** Hii ni kauli tedaji shurutishi yenye kiambata hasi, ambacho mara nyingi kinamaanisha kustisha tendo ambalo tayari liko katika mchakato. Kwa mjadala ulio mzuri kuhusu ndoa, familia, na taraka tazama Frank Staff's *NewTestament Theology*, kr. 296-302

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 10: 10-12**
**[10] Hata nyumbani tena wanafunzi wakamwuliza habari ya neno hilo. [11] Akawaambia, Kila mtu atakayemwacha mkewe na kuoa mwingine azini juu yake; [12] na mke, akimwacha mumewe na kuolewa na mtu mwingine, azini.**

**10:10 " wanafunzi wakamwuliza habari ya neno hilo"** Mathayo 19:10 inaunukuu mshagao wa wanafunzi. Kulikuwa na udadisi kuhusu kile walichikuwa wamefundishwa kuhusu taraka nandoa. Kifungu hiki kinaonyesha muundo wa wa mafundisho ya Yesu ya hadhara na fasiri za kipekee. Muundo huu unaonyesha namna maneno ya Yesu yalivyo na wepesi wa kueleweka visivyo. Hii mikusanyiko ya binafsi ilikuwa fursa ya kuwapa mafaunzo wale Kumi na Wawili katika kuelewa vema na umuhimu wa kuwepo mtazamokuhusu Ufalme wa Mungu. Yesu alikuwa na tazamio, hatima ya mamlaka katika yeye si katika Agano la Kale (kama vile Mt. 5:17-19), japo aliliheshimu na mara nyingi alilikubali Agano la Kale.

**10:11-12** " **azini juu yake**. . . **azini**" Hivi vyte ni vitenzi vya kauli elekezi ya wakatai uliopo. Huu muundo (sarufi-muundo) wa neno "uzinzi" katika lugha ya Koine ya Kiyunani kwa vyo vyote unaweza kuwa kauli ya kati au irabu tendewa. Mathayo 5:32, ambayo inashughulika na suala hilo hilo, ina kitenzijina cha kauli tendwa ya wakatai usio timilifu. Hili linamaanisha kwamba miundo yote ni kauli tendewa. Ikiwa hili ni la kweli, alafu si taraka na kuoa tena huu ulikuwa uzinzi, lakini tendo la kisheria la kutomtenga wanamke, ambalo kiutamaduni lilimdharirisha kama kahaba. Kiuhalisia "huyu anasabibihwa kufanya uzinzi." Hili si andiko la moja kwa moja la kuzuia uzinzi katika ndoa. Hili linahusiana na kipengele cha kithiolojia cha fasiri ya Kiyahudi (yaani., Hillel dhidi ya Shammai).

Hata hivyo, mjadala wa agano la ndoa katai ya waamini (yaani., wanaokula kiapo katika jina la Kristo kudumu katika ndoa) ulikuwa, na ni, hakuna awezaye kuupinga mpango wa Mungu. Waamini wanahimizwa kuwa katika "kiwango cha juu cha ufalme." Mara nyingi taraka ina uovu wa aina mbili; si dhambi isyosameheka! Tazama maelezo kamili katika Marko 10:4.

**10:12 "na mke, akimwacha mumewe na kuolewa na mtu mwingine, azini"** Tafsiri hii inayafuatisha maandiko ya Iskanda Mkuu. Maandiko ya ki- Magharibi yanasoma "na mke akimwacha mumewe, na sipewe traka na kuolewa na mume mwingine, huyo, azini." Kifungu chenye ufanano kilicho katika Mt. 19: 1-12 kinauacha mstari huu, huenda ni kwa sababu ya Mathayo, alipowandikia Wayahudi, hakuona uhitaji wa kukiweka kifungu hiki. Katika lugha ya Kiyahudi wwanawake hawakuwa na haki ya kuomba taraka kwa waume zao. Marko, akiyaandikia Mataifa, analinukuu hili ili kuonyesha mtazamo wa kiulimwengu wa mafundisho ya Yesu. Hii mitazamo inayohusu kiwango cha kisheria cha mke na mume, iliiakisi sheria ya Kirumi. Huu ni ushahidi mwingine ambao Marko aliutumia kuwaandikia Warumi. Yesu ndiye mkuu wa familia (kama vile Marko 10:13-16)!

◙ "**akimwacha"** Hii ni sentensi shurutishi daraja la tatu yenye kumaanisha tendo lenye umuhimu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 10:13-16**
**13 Basi wakamletea watoto wadogo ili awaguse; wanafunzi wake wakawakemea. 14 Ila Yesu alipoona alichukizwa sana, akawaambia, Waacheni watoto wadogo waje kwangu, msiwazuie; kwa maana watoto kama hawa ufalme wa Mungu ni wao. 15 Amin, nawaambieni, Ye yote asiyeukubali ufalme wa Mungu kama mtoto mdogo hatauingia kabisa. 16 Akawakumbatia, akaweka mikono yake juu yao, akawabarikia.**

**10:13 "wakamletea"** Hii ni sentensi ya kauli ya wakati usio timilifu. Wazazi waliendela kuwaleta watoto wao kwake kwa ajili ya desturi za Kiyahudi zihusuzo baraka. Tendo hili halia maana yo yote kwa wokovu wa watoto hawa. Hawa walikuwa wamekwishakuzaniwa kama sehemu ya Israelikwa mana ya tohara na walikuwa wakisubiri mabadiliko yao ili kulikamilisha agano la ujana wa kuanzia umri wa mika kumi na miwali kwa wasicha na miaka kumi na mitatu kwa wavulana.

◙ **"watoto"** Luka 18:15 ana neno "iwachanga."Katika mzunguko wa Kiyahudi wasichana chini ya miaka 12 na wavulana chini ya miaka 13 walifikiriwa kama watoto.

◙ "**awaguse**" Mathayo 19:13 ana kifungu "aweke mikono juu yao" (kama vile Marko 10:16). Ilikuwa kawaida sana katika siku za Yesu kwa wazazi kuwaomba walimu wa sheria wawabariki watoto wao. Tendo hili hili linaonekana katika Mwa.48:8 na kuendelea. Mara nyingi hili lilifanywa siku ya kuzaliwa mtoto. Zaidi baraka hizi zilikuwa ni kwa ajili utulivuikra za wazazi kuliko "kuokolewa dhidi ya kupoteza" hadhi ya watoto!

◙ **" wanafunzi wake wakawakemea"** Hili neno "wake" ni la kiutata hivyo wandidhi wa kale waliongeza kifungu "wale waliowaleta" (kama vile NKJV). Hata hivyo, haya si machapisho ya kale ya kiyunani א , B, au C, bali hiki kimwekwa katika A, D, na W. Usomaji mfupi sana unapataikana pia katika Mt. 19:13 na Luka 18:15. Katika mashariki ya Karibu watoto hawakuwekwa kipaumbele kama inavyofanyika katika Magharibi. Wanafunzi wangefikiri kuwa walikuwa wakimlinda Yesu dhidi ya tendo mashambulizi, maangamizi. Hata hivyo, kwa Yesu mara kwa mara watu walikuwa na upendeleo

**10:14**
**NASB, NKJV**
**NJB "alikereka"**
**NKJV "alihuzunika sana"**
**TEV "alighadhabika"**

Hili ni neno lenye nguvu linalotumika katika Marko 10:41 kuonyesha hasira ya wanafaunzi kwa Yakobo na Yohana baada ya kuuliza nafasi za ukuu na katika Marko 14:4 kwa chuki ya Yuda ya Yesu kuwa mpakwa mafuta. Mathayo pia analitumia neno hili mara kadha (kama vile Marko 20:24; 21:15; 26:8).

Injili ya Marko inaufunua utu wa Yesu kwa kuziandika hisia zake (kama vile *Jesus and the Rise of Early Christianity* na Paul Barnett, uk. 156).

1. huruma kwa mwenye ukoma (Marko 1:40-42)
2. hasira juu ya ugumu wa mioyo ya Mafarisayo (Marko 3:1-5)
3. kuwaghadhabikia wanafunzi (Marko 10:13-16)
4. upendo kwa kijana mdogo tajiri (Marko 10:17-22)
5. huzuni kiasi cha kufa katika bustani ya Gethsemane (Marko 14:33-34)
6. kughairi tendo la msalabani (Marko 15:34)

Mara nyingi Yesu alionyesha vikwazo kwa wanafunzi (kama vile Marko 6:52; 8:17; 9:19). Aliwaona watoto kama uumbaji muhimu wa Mungu na kuwapenda. Mara kwa mara aliwatumia watoto kama chombo cha mafundisho ya imani ya kweli na uanafunzi.

◙ "'**watoto wadogo waje kwangu**'" Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati usio timilifu yenye kueleza uweza au umuhimu wa tendo.

◙ "'**msiwazuie**'" Hii ni kauli shurutishi ya wakati uliopo yenye kiambata hasi ambacho mara nyingi kinamaanisha kustisha tendo ambalo tayari liko kataika mchakatao.

◙ **"ufalme wa Mungu'"** Hiki ni kifungu injili cha kawaida kilichorejelea ukuu wa Mungu ndani ya mioyo ya wanadamu ambacho kitakamilishwa juu ya dunia yote kama ilivyo mbinguni. Tazama Mada maalum katika Marko 1:15.

**10:15 "'Amini'**" Tazama Mada Maalum: Amina katika Marko 3:28.

◙ **"'asiyeukubali'"** Hiki kinawarejelea vijana. Mara nyingi Yesu aliwatumia watoto kama mifanano ya kiroho (kama vile Mt. 18). Agano Jipya ni ufunuo kwa vijana. Huu si mjadala wa nafasi ya kiroho kwa watoto!
Hili neno la Kiyunani *dechomai* kwa asili yake lilimaanisha "kuwa na uangalizi wa jambo fulani."Katika maana hiyo huu ni ufanano wa neno *lambanō* . Hili lilikuja kutumika katika maana ya "kupokea " au "kuamini" au "kukaribisha." Kunaweza kuwa na tofauti isiyo ya moja kwa moja katika maana hii ambapo neno *dechomai* linasistiza juu ya mtoaji, ambapo neno *lambanō* linaakisi ushiriki halisi wa mtoaji (kama vile *Greek-English Lexicon of the New Testament Based on Semantic Domains* cha Louw na Nida, juzuu. 1, uk. 572, tambihi 31).

Ukweli ya kithiolojia ni kwamba wanadamu lazima "wampokee," "wamwamini," "wamkaribishe" Yesu. Wokovu unahusisha kumkaribisha mtu, kuziamini kweli inayomuhusu mtu huyo (yaani.,injili), na kuishi maisha yanayomwiga mtu huyo. Kulikuwa na kipengele halisi na mwendelezo wa wokovu.

◙ **"' hatauingia kabisa'"** Hii ni tungo ya ukanushi mara mbili wenye nguvu yenye kumaanisha "kamwe, hata kidogo."

Katika maana hii Yesu anautambulisha Ufalme wa Mungu kama watoto kwa kuwa na tumaini na imani katika yeye na kataika mafundisho yake. Hili linazungumzia hali ya kutokuwa wavumilivu katika siku zetu, lakini ni fundisho dhahiri la Agano Jipya. Mara nyingi hili linaitwa "sakata la utengefu wa injili." O ni kweli. Imani katika Yesu ndiyo njia pekee kwa Baba (kama vile Yohana 14:6)! Lazima suala hili liumbe maombi, ushahidi, na ubinadamu, si ujinga, hukumu na majivuno!

**10:16 "kawakumbatia, akaweka mikono yake**" Hapa kuna undani mwingine wa ushahidi wa Petro, kama ilivyo 9:36." akawabariki, akaweka mikono juu yao" Yesu alichukua muda kwa kuwa na kila mmoja wao. Tunaweza kuwatumainisha watoto wetu juu ya upendo wa Mungu aliofunua dhahiri katika Kristo. Kama Yesu alivyouamsha mtazamo na hadhi ya kijamii juu ya wanawake, ndivyo ilivyo, kwa watoto. Tazama MADA MAALUM : KUWEKA MIKONO katika Marko 7: 32.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 10:17-22**
**17 Hata alipokuwa akitoka kwenda njiani, mtu mmoja akaja mbio, akampigiamagoti, akamwuliza, Mwalimu mwema, nifanye nini nipate kuurithi uzima wa milele? 18 Yesu akamwambia, Kwa nini kuniita mwema? Hakuna aliye mwema ila mmoja, ndiye Mungu. 19 Wazijua amri, Usiue, Usizini, Usiibe, Usishuhudie uongo, Usidanganye, Waheshimu baba yako na mama yako. 20 Akamwambia, Mwalimu, haya yote nimeyashika tangu utoto wangu. 21 Yesu akamkazia macho, akampenda, akamwambia, Umepungukiwa na neno moja. Enenda, ukauze ulivyo navyo vyote, uwape maskini, nawe utakuwa na hazina mbinguni; kisha njoo unifuate. 22 Walakini yeye akakunja uso kwa neno hilo, akaenda zake kwa huzuni; kwa sababu alikuwa na mali nyingi.**

**10:17 " Hata alipokuwa akitoka kwenda njiani"** Injili ya Marko inabainishwa na ziara za Yesu. Hii ilikuwa mbinu ya Marko ya kifasihi ya kuumba uwasilishaji wake wa kumbukumbu za Petro (au hotuba).

◙ " **mtu** " Mathayo 19:20 anaongeza kivumishi "kijana"; Mt. 19:22 anaongeza "Huyu alikuwa mmoja wa wale waliokuwa wakimiliki mali nyingi (yaani., tajiri)"; ambapo Luka 18:18 anamuita "mtu mkubwa." Kwa uwazi kabisa mtu huyu alikuwa na mali nyingi, madili, mtu wa muhimu kiraia na mkuu wa kidini. Hili neno "mtu mkbwa" kinamaanisha kwamba huyu alikuwa kiongozi katika sinagogi la mahali pale. Tazama MADA MAALUM : HAKI katika 1 Petro 3:14. "kimbieni. . .na pigeni magoti" Tendo hili lilikuwa tendo lisilo la kawaida kwa mtu aliyebobea katika mali hadharani. Mtu huyu alionekana kuwa mtiifu katika swali lake na mwenye shauku ya kujua. Hii si juhudi ya kumjaribu au kumlia njama.

◙ **" Mwalimu mwema'"** Kifungu hiki kilifungua fursa kwa kuuchunguza mtazamo wa mtu huyu (kama vile Marko 10:18). Hili neno "mwema" (yaani., *agathos*) linaweza kueleweka katika mara kadhaa (mwema, mwenye manufaa, mkarimu, mwenye msdaa, mwenye heshima, au mwenye mwenendo mwema). Mtu huyu alimaanisha kwa nia moja, lakini Yesu alilitumia katika maana ya hitimisho.

◙ **"' nifanye nini'"** Uelewa wake wa maswala ya kiroho ulitazamia juu ya matendo yake. Mtu huyu amekuwa akijitweza katika kuyafuata mapokea ya sheria za Kiyahudi (kama vile Mt.19:16).

◙ **"' kuurithi uzima wa milele'"** Hili neno la kifamilia linamaanisha uhusiano binafsi pamoja na Mungu. Katika Agano la Kale makuhani walisemekana kuwa warithi wa Mungu na alikuwa wao kwa sababu hawakuwa na gawio la ardhi kama yalivyofanya makabila mengene. Hili swali halisi lilimaanisha kuwa mtu huyu aliamini kuwa alikuwa alikuwa akikubaliwa na Mungu kwa ukamilifu, lakini alitaka kuhakikisha.

◙ **"'uzima wa milele'"** Dhana ya maisha baada ya kifo (au ufalme wa siku za mwisho) lilitokana na vifungu kama Dan. 12:2 au Ayubu 14:14; 19:25-27. Mafarisayo walikuri juu ya maisha baada ya ufuko katika maneno ya kimwili. Hawa walijiamini kwamba YHWH angeliwazawadia maisha ya milele kwa sababu ya (1) upekee wao wa rangi (yaani., wana wa Ibrahimu) na (2) wao kuzifuata kwa ukamilifu desturi za Orad (yaani Sheria za Kiyahudi).

**10:18 " mwema "** Neno hili lilitumika kuonyesha kwamba kiwango cha huruma ya kweli ni haki ya Mungu. Hili neno "haki" linatokana na neno la tungo (yaani ., matete ya kwenye mto), yaliyotumika kama kipimo au rula.

◙ **"' Hakuna aliye mwema ila mmoja, ndiye Mungu'"** Yesu hakutengeneza usemi unaohusu wema wake mwenyewe, bali alitaka kumkumbusha mtu huyu kuhusu uelewa wake mdogo wa kufikiri juu ya Mungu na wema wa kweli (kama vile Mt. 5:48). Hili linaweza kuwa dokezo kwa 1 Kor. 16:34; 2 Kor. 5:13; 7:3; Zab. 25:8; 86:5; 100:5; 106:1; 107:1; 118:1; Ezra 3:11. Ufanano wa Mathayo unalibadili swali la mkuu huyu kuwa "Mwalimu, nifanye kitu gani kizuri ili niurithi uzima wa milele?" (Mt. 19:16). Badiliko hili linakuwa uthibitisho kwa dhana ya mtu huyu kuhusu wema na ukamilifu wa wema huu (kama vile Marko 19:20).

**10:19 "'Wazijua amri'"** Huu ni muhtasari wa mbili ya tatu ya Amri Kumi, ambazo ziliangalia nmna watu wa aganao walivyokuwa wakichukuliana.

◙ **"'Usidanganye'"** Hili linaweza kuwa kurejelea kuficha. Amri hii, kama inavyoelezwa, hakuwa sehemu ya Amri Kumi, wala haipatikanai katika mfumo huu po pote pale katika Agano la Kale. Pia huu ufanano ulio katika Mt. 19:18-19 na Luka 18:20 hauna kifungu hikiata hivyo, kwa uwazi,hii mihtasari yote inapingana na nukuu ya Yesu juu ya Amri. Tena hili ni tatizo la kawaida la ushuhuda wa ushahidi wa macho. Kwa hakika hili haliathiri uvuvio au uaminifu wa ufafanuzi wa Injili!

## MADA MAALUMU: AMRI KUMI (kama vile Kut. 20:1-17; Kumb. 5:6-21)

I. Maneno
   A. Kiuhalisia "Maneno Kumi" (kama vile. Kut. 34:28; Kumb. 4:13; 10:4).
   B. Clementi wa Alexandria aliziita "amri kumi za Mungu" (Deka Logous) na hii ilifuatwa na makasisis wa mwanzo.
   C. katika Biblia pia yaliitwa:
      1. "maagano" (yaani., uzao wa Kiebrania, kama vile. Kut. 34:28; Kumb. 4:13; 9:9; tazama mada maalum: Maagano)
         a. kutoka lugha ya Akkadia, *barah* – kula (yaani., chakula cha kawaida)
         b. kutoka lugha ya Akkadia, *biritu* – kubusu au nira (yaani., ahadi mshikamano kati ya watu)
         c. kutoka lugha ya Akkadia, *birit* – kati (yaani makubaliano kati ya pande mbili)
         d. baru – radha (yaani, uwajibikaji)
      1. "Ushuhuda" – kut. 16:34; 25:16 (yaani., mbao mbili)

II. Makusudi
   A. Yalifunua tabia ya Mungu (tazama Mada Maalum: Tabia za Mungu wa Israeli [Agano la kale])pekee na enye mamlaka (yaani., kuamini Mungu mmoja; tazama mada maalum: imani ya kuamini kuna Mungu mmoja)
      1. maadili, yanalenga jamii na kila mmoja mmoja
   B. Ni kwa ajili ya
      1. watu wote kwa sababu yamefunua mapenzi ya Mungu kwa ajili ya mwanaumme na wanadamu wote wameumbwa kwa sura ya Mungu.
      2. waaminio wa maagano pekee kwa sababu haiwezekani kuelewa na kutii bila msaada wa Mungu.
      3. C. S. Lewis – utashi wa ndani, hata katika makabila ya kale (Rum. 1:19-20; 2:14-15), inaakisi hapa.
   C. kama vile sheria za zamani zilikuwa
      1. kudhibiti na kuongoza mahusiano yaliyofanywa na watu wawili
      2. kudumisha na kuimarisha jamii
   D. walikuwa na uhakika na makundi mbalimbali ya watumwa na Wamisri waliotengwa katika jamii ya imani na sheria. B. S. watoto, makitaba ya Agano la kale, Kutoka—"mapigo nane ni vipengere vinavyokanusha vinavyoonyesha mipaka ya nje ya maagano. Hakuna kosa dogo lakini ni kukata kila kamba ambazo zina uhusiano wa kiroho na mwanadamu. Vipengere halisi viwili vinaonyesha ufafanuzi wa maagano ndani ya maisha. Amri kumi za Mungu zinaonyesha upande wa nje na upande wa ndani; inalinda kuzuia njia ya mauti na kuelekeza katika njia ya kuishi" (uk. 398).

III. Mifanano
   A. Kibiblia
      1. Amri kumi zimeandikwa mara mbili, kwenye Kutoka 20 na Kumbukumbu 5. Tofauti ndogo kwenye

amri ya 4, 5, na 10 amri zinaonyesha marekebisho ya hizi kanuni nzima kwa matukio tofauti.

2. hata hivyo, umoja wao unalenga kupelekwa kwenye usahihi.
3. ni dhahili wanasoma na kuthibitisha nyakati, kama kwenye Yoshua 24 inavyoonyeshwa.

B. Desturi

1. Baadhi ya mkusanyiko wa sheria zilizopangwa kwa mfumo maalum kutoka mashariki ya kale ya karib
   a. Ur-Nammu (ki-Sumeria, 2050 k.k.) kutoka mji wa Uri
   b. Lipit-Ishtar (ki-Sumeria, 1900 k.k.) kutoka mji wa Isini
   c. Eshnunna (ki-Akkadia, 1875 k.k.) kutoka mji wa Eshunna
   d. sheria ya Hammurabi (Babeli, 1690 k.k.) kutoka Babali lakini Stela ilipatikana ndani ya Susa
2. Muundo wa sheria kwenye Kut. 20:18-23:37 ni kawaida kabisa na mkusanyiko mwingine wa sheria zilizopangwa kwa mfumo maalumu na mashariki ya kale ya karibu. Hata hivyo, amri kumi zina mundo wa kipekee ambao unadokeza mamlaka yake (mamlaka ya mtu wa 2—lililoimarishwa zaidi).
3. Desturi bora zaidi zilizo dhahili ziliungana na mikataba ya wafalme wa Wahiti mwaka wa 1450-1200 k.k. baadhi ya mifano mizuri inayofanana na hii inaweza kuonekana katika
   a. Amri kumi
   b. Kitabu cha Kumbukumbu la Torati
   c. Yoshua 24

Misingi ya mikataba hii ni

   a. Utambulisho wa mfalme
   b. simulizi za matendo yake makuu
   c. uwajibikaji wa maagano
   d. ufundishwaji kwa ajili ya kuweka mkataba mahali patakatifu ili usomwe mbele za watu
   e. miungu ya ushirika inatajwa kama mashahidi
   f. Baraka kwa ajili ya waaminifu na laana kwa ajili ya wavunja sheria

4. Baadhi ya vyanzo vizuri kwenye mada hii
   a. George Mendenhall, sheria na maagano katika Israeli na mashariki ya karibu ya kale
   b. Dewey Beegle, Musa, mtumishi wa Yahweh
   c. W. Bezalin, asili na historia
   d. D. J. McCarthy, mkataba na maagano

IV. Umbile la Ndani

A. hasa, kwenye kitabu hiki, asili ya sheria za wana wa Israeli, ni wa kwanza kufanya tofauti kati ya walioimarishwa na walaghai.

1. Ulaghai ni muundo wa kawaida wa sheria ya mashariki ya karibu ya kale kwamba wana masharti – "kama" = "baadaye"
2. kuimarika kunakuwa na muundo mzuri zaidi kwamba unaelezewa kutoa maagizo, "wewe uta. . ." au "wewe hauta. . ."
3. Roland de Vaux kwenye Israeli ya kale: taasisi ya jamii, juzuu 1, uk. 146, anasema kwamba ulaghai ni hatua ya mwanzo inatumika kuweka usiri mahali na kuimarisha patakatifu.

B. amri kumi ni mwanzo wa kukana mwonekano wao – 8 hadi 10. Mtu wa pili ana muundo wa ajabu. Walikua labda na maana ya kuelezea jamii maagano yote, kila mshirika mmoja mmoja, au wote!

C. bamba mbili za mawe (Kut. 24:12; 31:18) mara nyingi zinatafsiriwa kama masimulizi ya vipengele vya wima na mlalo wa amri kumi. Uhusiano wa mtu kwa YHWH umetamkwa kwa amri nne na uhusiano wa mtu na mwenzake upo kwenye amri nyingine sita. Hata hivyo, kwenye nuru ya mkataba wa mfalme wa Wahiti, yumkini walikuwa na nakala mbili zilizotaja amri zote.

D. hesabu ya historia ya amri kumi

1. ni dhahili kwamba tuna marekebisho kumi. Hata hivyo,tofauti sahihi hatujapewa.
2. Orodha ya kisasa ya Kiyahudi inataja Kut. 20:2 kama amri ya kwanza ili kutunza hesabu hadi namba kumi walifanya Kut. 24:3-6 kuwa amri ya pili.
3. makanisa ya Romani Katholic na Lutherani, yanayomfuata Augostino, yanafanya Kut. 20:3-6 kuwa amri ya kwanza na kwa kusudi la kutunza hesabu hadi namba kumi, wakigawa mstari wa 17 kuwa amri mbili

tofauti.

4. makanisa ya marejeo, yanayomfuata Origen na makanisa ya awali ya mashariki na magharibi, yanadai kwamba Kut. 20:3 ni amri ya kwanza. Huu ni mtizamo wa kiyahudi wa kale uliowasilishwa na Philo na Josephus.

V. ni kwa namna gani wakristo wanasimulia anri kumi?

A. mtizamo wa juu wa Yesu wa maandiko umeandikwa katika mahubiri ya mlimani kwenye Mathayo 5-7 na hasa 5:17-48, ambao unatuonyesha maswali ya maana sana. Mahubiri yake mara zote yalionyesha msingi wa amri kumi na matumizi yake

B. nadharia ya uhusiano

1. kwa ajili ya waaminio

a. Roy Honeycutt, hizi amri kumi

1) "hatujawai kukuwa katika amri kumi kwa sababu hatujawai kukuwa katika Mungu" (uk. 7).

2) "kwa sababu amri ni mashahidi kwa Mungu, hata hivyo, kuna maana ambayo uhusiano wao na uhusiano wa Mungu umeshikamano kama ambavyo usivyo weka kutengana. Kwa hiyo, kama Mungu anahusika kwa ajili ya maisha yako, amri pia zitakuwa na uhusiano wa ndani zaidi kwa ajili madai na tabia ya Mungu iliyoandikwa" (uk. 8).

b. binafsi, ni lazima tuangalie mwongozo huu hoja kutoka kwenye simulizi ya imani iliyokwisha imarishwa. Kuwatenganisha kutoka kwenye imani na kuambatana na Mungu ni kuwaharibu wao. Hivyo basi, kwangu mimi, ni watu wote wenye maana kwamba Mungu anataka wamjue yeye. Wao pia wanasimuliwa kuwa mashahidi wa ndani wa uumbaji mwanadamu. Paulo analielezea hili kwenye Warumi 1:19-20; 2:14-15. Kwa maana hii amri zinaakisi nuru ya uangalizi kwamba mahusiano yanakaa kwa watu wote.

2. kwa ajili ya watu wote, kwenye jamii zote, kwa nyakati zote

a. Elton Trueblood,misingi kwa ajili ya ujenzi mpya. "dhana ya kitabu hiki kidogo ni kuvumbua sheria za maadili, kama zilizowakilishwa na amri kumi za Kiebrania, ni njia mojawapo ambapo kinga ya udhaifu inaweza kupatikana" (uk. 6).

b. George Rawlinson,fasiri ya madhabahu, "Kutoka"

"Nyakati zote walifanya muhtasari wa wajibu wa mwanadamu ambao ulizaa matunda ya kiroho kwenye uso wake, ambao unafaa kwa kila muundo wa mwanadamu katika jamii, na ambao,kwa kadri dunia itaendelea kuwepo, hauwezi kuachwa. Kushikilia amri kumi kama muhtasari bora wa sheria ya maadili kwa jamii za Wakristo limekubaliwa katika eneo hili, na lenyewe linatia ushuhuda mkazo ufupisho kamili mzuri zaidi" (uk. 130).

3. sio kwa maana kama ya wokovu, wala hawakuwai kuwa, maana ya Mungu kwa ajili ukombozi wa kiroho wa anguko la mwanadamu. Paulo anaeleza wazi hili katika Gal. 2:15-4:31 na Rum. 3:21-6:23. Anatumikia kama mwangalizi kwa ajili mwanadamu kwenye jamii. Wanalenga kwa Mungu na kisha kwa mwanadamu. Kukosa sehemu ya kwanza ni kukosa vyote! Maadili ya sheria, bila kubadilishwa, kukaa katika mioyo, ni taswira ya mwanadamu aliyeanguka asiye na matumaini! Amri kumi ni halali, lakini ni maandalizi pekee ya kukutana na Mungu katikati ya kushindwa kwetu. Kukataliwa kutoka kwenye wokovu wanajiongoza pasipo kiongozi!

**10:20** "'**haya yote nimeyashika**" Mtu huyu alikuwa akiyatimiza mahitaji yote ya kidini yaliyohusu tamaduni zake. Mtume Paulo pia alihisi kuwa ameyakamilisha mahitaji yote ya kidini (kama vile Matendo 23:1-2; Flp. 3:6). Mtu huyu hakusema uongo. Yeye aliamini kuwa hakuwa na hatia machoni pa Mungu.

◙ "**tangu utoto wangu**" Hili lilirejelea sherehe ya *Bar Mitzvah* katika umri wa miaka 13 ambapo mvulana alitambuliwa kama mtu mzima na kuwa mwenye wajibu wa kuishika Msheria.

**10:21** "**Yesu akamkazia macho, akampenda**" Hili ni la kipekee kwa Marko. Upendo wa Yesu, hata hivyo, hakuvidogoisha viwango vya Ufalme wa Mungu. Hapa kuna fumbo la upendo usio na masharti wenye kuhitaji mwitikio sahihi wa imani.

◙ **"'Umepungukiwa na neno moja'"** Oni hili linafanana na Marko 12:34. Yesu alitambua kwamba wanadamu walikuwa hatua ya ukaribu au zaidi ya Ufalme wa kweli, ambao haukutiliwa mkazo katika utendaji wa Musa au utambuzi wa rangi (kama vile Yohana 8:33), bali imani binafsi katika yeye. Huyu mkuu wa kidini alikuja katika haki ya kiroho, kwa mtu mwenye haki, aliuliza swali la haki, lakini kwa uwazi hakuwa na uwezo wa kuwa na uchaguzi sahihi! Yesu hakukidogoisha kiwango chake! Mtu huyu alienenda zake huku akihuzunika! Hivyo karibia na endelea!

◙ "' **ukauze ulivyo navyo vyote, uwape maskini**. . . **kisha njoo unifuate**'" Kifungu hiki kinaonyesha umuhimu wa imani ya Agano Jipya (kama vile Luka 14:33). Yesu alivifahamu vipaumbele vya mtu huyu vilipo. Ili kuwa Mkristo mtu anatakiwa kuviacha viyu vyote. Katika maana nyingine suala hili linaufanya Ukristo kuwa mgumu sana! Katika usemi huu Yesu alikuwa akiitazamia robo tatu ya Amri Kumi zinazohusiana na kipaumbele cha mtu kwa Mungu na Mungu pekee (kama vile Mt. 5:20).

Andiko hili haliwezi kugeuzwa na kuwa katika sheria kwa waamini wote (yaani., umaskini ndilo jambo zuri zaidi kwa Mungu). Lazima lionekane katika muktadha huu. Uhusiano wa kiroho katai ya Mungu na mwanadamu lazima uwe kipaumbele dhidi ya uhusiano wa kimwili (yaani, mali, utambuzi, kazi, familia, umiliki, hata maisha yenyewe). Ikiwa kumiliki ni uovu katika huo, kwa nini yatupasa kuwa maskini maskini mali zetu?

Hoja moja zaidi. Mara nyingi tunaweka tazamio katika hitaji la Yesu, lakini tunatambua kuwa Yesu alimpa mtu huyu agizo la kipekee. Alimwalika kujiunga na kundi lake la wanafunzi! fursa yake ilikuwa mbali sana kuliko gharama!

◙ **"' utakuwa na hazina mbinguni '"** Kwa sababu ya uasi wa mwanaadamu, baraka za Mungu zimetunzwa tena kwa ajili ya maisha baada ya kifo (kama vile Marko 10:30; Mt. 5-7). Wanadamu lazima wawe huru kuupuuzia utajiri wa kidunia kama ushahidi wa oungofu wa kiroho, si kama upendeleo.

**10:22 " kwa huzuni "** Neno hili linaweza kueleweka katika maana mbili (1) mshutuko au mshangao (2) huzuni inayotokana na kukatishwa tama au uso wa majonzi. Yote haya yanatengeneza maana katika muktadha huu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 10: 23-27**
**23 Yesu akatazama kotekote, akawaambia wanafunzi wake, Yesu akatazama kotekote! 24 Wanafunzi wakashangaa kwa maneno yake. Yesu akajibu tena, akawaambia, Watoto, jinsi ilivyo shida wenye kutegemea mali kuingia katika ufalme wa Mungu! 25 Ni rahisi ngamia kupenya katika tundu ya sindano kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu. 26 Nao wakashangaa mno, wakimwambia, Ni nani, basi, awezaye kuokoka? 27 Yesu akawakazia macho, akasema, Kwa wanadamu haiwezekani, bali kwa Mungu sivyo; maana yote yawezekana kwa Mungu.**

**10:23 " Yesu akatazama kotekote**" Mwonekano huu unatumika mara kadhaa kudokeza kwamba Yesu aliyatathmini mafundisho yake namna yalivyowabadilisha watu (kama vile Marko 3:5,34; 5:32; 10:23; 11:11). Luka pekee 6:10 ndiyo inayofanana. Hii ni kumbukumbu ya Petro ya kipekee.

◙ "' **jinsi ilivyo shida wenye kutegemea mali kuingia katika ufalme wa Mungu**'" Hili lingekuwa la kustaajabisha kwa wanafunzi (kama vile Marko 10:24). Mtazamo wa mapokeo ya Agano la Kale, uliojikita katika Kumb. 27-28, ulikuwa kwamba mali na afya ndiyo mambo yaliyohusiana na utimilifu wa agano la mtu na Baraka za Mungu. Hili ndilo jambo lililoelezwa na Ayubu na Zaburi 73. Wenye mali huamini katika rasilimali zao badala ya Mungu.

## MADA MAALUM: WINGI WA MALI

. Mtazamo wa kitabu cha Agano la Kale kwa ujumla
- A. Mungu ndiye mmiliki wa vitu vyote
  1. Mwanzo 1-2
  2. 1 Nyakati 29:11
  3. Zaburi 24:1; 50:12; 89:11
  4. Isaya 66:2
- B. Wanadamu ni wasimamizi wa mali kwa ajili ya makusudi ya Mungu

1. Kumbukumbu 8:11-20
2. Mambo ya Walawi 19:9-18
3. Ayubu 31:16-33
4. Isaya 58:6-10

C. Wingi wa mali ni sehemu ya ibada
   1. zaka za aina mbili
      a. Hesabu 18:21-29; Kumb. 12:6-7; 14:22-27
      b. Kumb. 14:28-29; 26:12-15
   2. Mithali 3:9
D. Wingi wa mali huonekana kama zawadi kutoka kwa Mungu kwa ajiri ya agano la uaminifu
   1. Kumbukumbu 27-28
   2. Mithali 3:10; 8:20-21; 10:22; 15:6
E. Onyo dhidi ya mali katika kuwagharimikia wengine
   1. Mithali 21:6
   2. Yeremia 5:26-29
   3. Hosea 12:6-8
   4. Mika 6:9-12
F. Wingi wa mali sio dhambi kuwa nayo isipokuwa ikiwekwa kama kipaumbele
   1. Zaburi 52:7; 62:10; 73:3-9
   2. Mithali 11:28; 23:4-5; 27:24; 28:20-22
   3. Ayubu 31:24-28

. Mtazamo wa kipekee wa kitabu cha Mithali

A. Mali imewekwa katika nafasi ya juhudi ya mtu binafsi
   1. uzembe na uvivu umelaaniwa – Mithali 6:6-11; 10:4-5,26; 12:24,27; 13:4; 15:19; 18:9; 19:15,24; 20:4, 13; 21:25; 22:13; 24:30-34; 26:13-16
   2. kufanya kazi kwa bidii kumeungwa mkono – Mithali 12:11,14; 13:11
B. Umaskini dhidi ya mali umetumika kueleza juu ya haki dhidi ya unyonge – Mithali 10:1na kuendelea; 11:27-28; 13:7; 15:16-17; 28:6,19-20
C. Hekima (kumjua Mungu na nenp lake na kuishi katika maarifa haya) ni bora kuliko utajiri- Mithali 3:13-15; 8:9-11,18-21; 13:18
D. Maonyo na makaripio
   1. Maonyo
      a. jihadhari na kudhamini deni la jirani yako (dhamana) –Mithali 6:1-5; 11:15; 17:18; 20:16; 22:26-27; 27:13
      b. jihadhari na kupata utajiri kwa njia ya uovu – Mithali 1:19; 10:2,15; 11:1; 13:11; 16:11; 20:10,23; 21:6; 22:16,22; 28:8
      c. jihadhari na mkopo – Mithali 22:7
      d. jihadhari na utajiri wa muda mfupi – Mithali 23:4-5
      e. mali hazifaidii kitu siku ya ghadhabu – Mithali 11:4
      f. utajiri una "marafiki" wengi– Mithali 14:20; 19:4
   2. makaripio
      a. ukarimu huungwa mkono – Mithali 11:24-26; 14:31; 17:5; 19:17; 22:9,22-23; 23:10-11; 28:27
      b. afadhali haki kuliko utajiri – Mithali 16:8; 28:6,8,20-22
      c. maombi kwa ajili ya uhitaji, na sio utosherevu – Mithali 30:7-9
      d. kumpa mhitaji ni kumpa Mungu – Mithali 14:31

. Mtazamo wa kitabu cha Agano Jipya

A. Yesu
   1. mali hutengeneza jaribu pekee la imani ndani yetu wenyewewe rasilimali na zetu badala ya Mungu na rasilimali Zake
      a. Mathayo 6:24; 13:22; 19:23

b. Marko 10:23-31
c. Luka 12:15-21,33-34
d. Ufunuo 3:17-19
2. Mungu atatupa mahitaji yetu ya kimwili
a. Matthayo 6:19-34
b. Luka 12:29-32
3. kupanda kunahusiana na kuvuna (kiroho pamoja na kimwili)
a. Marko 4:24
b. Luka 6:36-38
c. Mathayo 6:14; 18:35
4. toba huithiri mali
a. Luka 19:2-10
b. Mambo ya Walawi 5:16
5. unyanyasaji wa kiuchumi umelaaniwa
a. Mathayo 23:25
b. Marko 12:38-40
6. Humu ya nyakati za mwisho inahusiana na matumizi yetu ya mali – Mathayo 25:31-46

B. Paulo
1. Maoni ya kiutendaji kama ule wa Mithali (kazi)
a. Waefaso 4:28
b. 1 Wathesalonike 4:11-12
c. 2 Wathesalonike 3:8,11-12
d. 1 Timotheo 5:8
2. Maoni ya kiroho kama yale ya Yesu (mambo ni ya muda mfupi, iweni na utoshevu)
a. 1 Timotheo 6:6-10 (kuridhika)
b. Wafilipi 4:11-12 (kuridhika)
c. Waebrania 13:5 (kuridhika)
d. 1 Timotheo 6:17-19 (ukarimu na kuamini Mungu, si utajiri)
e. 1 Wakorintho 7:30-31 (kubadiklika badilika kwa mambo)

. Hitimisho

A. Hakuna theolojia ya kimfumo iliyo ya kibiblia kuhusiana na mali.
B. Hakuna kifungu cheye uhakika kuhusiana na suala hili, hivyo, mitazamo ya kiundani lazima ikusanywe kutokana na vifungu mbalimbali. Jihadhari na kutokutumia maoni yako katika maandiko haya yaliyojitenga.
C. Kitabu cha Mithali, ambacho kiliandikwa na watu wenye hekima (busara), wana mtazamo tofauti kuliko aina nyingine za miundo ya kibiblia. Kitabu cha Mithali ni cha kiutendaji na kina tazamio binafsi. Hiki kina ulinganifu na lazima kiwe na ulinganifu na Maandiko mengine (kama vile Yer. 18:18)
D. Katika hizi siku tulizonazo tunahitaji kuchambua maoni na utendji wake kuhusiana na mali katika nuru ya Biblia. Vipaumbele vyetu vimepotea ikiwa ubepari au ukomonisti ni mwongozo wetu wa pekee. Ni kwa nini na ni kwa namna gani kufanikiwa kwa mtu ni maswali muhimu sana kuliko kuliko kile mtu alichojilimbikizia.
E. Kujilimbikizia mali lazima kuwe na ulinganifu na ibada ya kweli na utumishi unaostahili kama vile 2 Wakorintho 8-9).

**10:24 "'Watoto'"**Yesu aliwaita wanafunzi kwa kutumia neno alilolitumia kataika mafundisho yake ya kipindi cha awali (kama vile Marko10:13-16). Hili linasistiza kwamba neno "watoto" linawarejelea waamini wachanga.

**◙ " jinsi ilivyo shida wenye kutegemea mali kuingia katika ufalme wa Mungu'"** Huu ni usemi wenye kushtua. Wokovu ni neema ya bure katika kazi ya Kristo iliyomalizika kwa mtu ye yote/kila mtu mwenye kuwa na mwitikio wa toba na imani. Tatizo linakuja pale tunapofikiri ya kuwa tunaafaidika au tuanapata thawabu! Imani ni ngumu kwa wenye majivuno, wenye kujitosheleza, mu walioanguka. Tungeipenda zaidi ikiwa uhusiano wetu na Mungu ulikuwa mgumu na

ni wa shida sana ili kwamba tuweze kuchukua gharama katika kuupata, lakini kama ilivyo, njia ya Mungu ya toba na imani ni kumwadhibu mwanadamu aliyeanguka, hasa kupitia mali, elimu, mwandamu mwenye hadhi.

Kwa kuwa mstari huu ni ufupisho wa waandishi kadhaa wa kale ambao walijaribu kuweka mipaka ya uchaguzi wao kwa kukiingiza kifungu bora (kama vile Bruce M. Metzger's *A Textual Commentary on the Greek New Testament*:

1. "wale wanaoitumainia mali" kipatikanacho katika MSS A, C, D, na katika Textus Receptus
2. "mwenye mali" katika MS W
3. "wale wenye kumiliki mali" katika minuscule 1241

**10:25 "' rahisi ngamia kupenya katika tundu ya sindano'"** Kama ilivyo Mt. 23:24, kifungu hiki ni ubobezi wa semi za kiufundi. Wandishi kadhaa na watoamaoni wengi wamejaribu kutoa maelezo ya usemi huu kama (1) kebehi kati ya "ngamia" (*kamēlos*) na "uzi" (*kamilus*), ambayo inatokaka katika karne ya tano au (2) kifungu kutumia "tundu ya sindano" hiki kinaurejelea mlango mmoja katika lango kuu la Yerusalemu, lakini kwa vyo vyote haya yana ushahidi wa kihistoria (kama vile Fee na Stuart's *How To Read the Bible For All Its Worth,* uk. 21). Mambo haya yanapungukiwa na hoja ya vichochezi (kama vile Mt. 19:24; Luka 18:25).

**10:26 " wakashangaa"** Mara nyingi Marko analitumia neno hili (*ekplēssomai*) kutoa ufafanuzi wa nmna watu walivyoyapokea mafundisho na matendo ya Yesu (kama vile Marko 1:22; 6:2; 7:37; 10:26; 11:18; na kisawe *thambeō* katika Marko 10:24). Ujumbe wa Yesu ulikuwa tofauti sana na ule wa walimu wa sheria za Kiyahudi, katika muundo mzima (yaani.,mamlaka yake) na ujumbe (yaani, chimbuko la Ufalme).

**NASAB " wakimwambia"**
**NKJV "wakasemezena"**
**NRSV "wakaambizana"**
**TEV "wakaulizana"**
**NJB "wakaambiana"**

Tafsiri hizi zenye kutofautiana zinahusiana na tofauti mbalimbali za Kiyunani.

1. NKJV, MSS A, D, W, na Textus Receptus
2. NRSV, TEV, NJB, MS M* na tasfiri ya Peshitta
3. NASB, MSS א, B, na C
4. Machapisho ya minuscule (yaani., 569) na baadhi ya tafsiri za ki-Koptiki zinakiondoa kifungu, kama Mt.19:25 na Luka 18:26

**10:27** Msistizo wa mstari huu kuhusu neema ya Mungu ni ulinganifu wa ukaribisho muhimu wa asili ya uanafunzi wa Agano Jipya. Wanadamu hawawezi kumkaribia Mungu mtakatifu, bali kweli yenye kushangazal, kustaajabisha ndiyo anayoiruhusu itukaribie!

Usemi huu unaweza kuwa dokezo la Agano la Kale la Mwa. 18:14 au Yer. 32:17,24. Tumaini la mwanadamu li katika tabia, ahadi, na matendo ya Mungu mmoja wa kweli.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 10 :28-31**
**[28] Petro akaanza kumwambia, Tazama, sisi tumeacha vyote tukakufuata wewe. [29] Yesu akasema, Amin, nawaambieni, Hakuna mtu aliyeacha nyumba, au ndugu waume, au ndugu wake, au mama, au baba, au watoto, au mashamba, kwa ajili yangu, na kwa ajili ya Injili, [30] ila atapewa mara mia sasa wakati huu, nyumba, na ndugu waume, na ndugu wake, na mama, na watoto, na mashamba, pamoja na udhia; na katika ulimwengu ujao uzima wa milele. [31] Lakini wengi walio wa kwanza watakuwa wa mwisho; na wa mwisho watakuwa wa kwanza.**

**10:28 "' tumeacha. . . tukakufuata wewe'"** Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati usio timilifu (yaani., waliviacha vyote mara moja), na kufuatiwa na kauli tendaji elekezi ya wakati timilifu (yaani., kuendelea katika hali ya uanafunzi). Katika maana moja Petro anamua tena kuwa mwanafunzi wa Yesu kuwa mfuasi wa Yesu. Petro anaweza kuwa anajaribu kulinganisha ahadi zao na hitaji la Yesu kwa tajiri, kijana mdogo.

**10:29** Mstari huu unaorodheshabaadhi ya vipengele vya kawaida vya jamii ya Kiyahudi ambapo wafuasi wake walihusishwa. Pia kwa uwazi mstari huu unaunganisha ahadi zake za kipekee (yaani.,"kwa ajili yangu") na kweli zake yaani., "kwa ajili ya injili").

Kanisa la mwanzo liliathiriwa na nadharia ya Kiyunani ya kujinyima mambo yahusuyo anasa, hasa useja. Inafurahisha kwamba wanawake hawatajwi katika orodha hii. Hii inamaanisha kwamba kuengana kindoa halikwa suala tarajiwa. Hata hivyo, husisho la neno "watoto" linaweza kumaanisha kwamba wake walijumuishwa kataika kifungu "aliyeacha nyumba." Kipaumbele cha ahadi ya mtu kwa Yesu lazima kisimame hata badala ya a familia (kama vile 1 Tim. 5:8). Hii haimaanishi useja, bali ni mahali ambapo hatima ya mtu inapotakiwa kakamilishwa.

**10:30** Yesu anaunyambulisha ufalme waMungu katika (1) namana za kidunia sana ambazo zinafananishwa na kile "walichokikosa" wanafaunzi katikamaisha haya na (2) uhusianao wa mpangilio huu wa ulimwengu. Baadhi ya baraka fungamanaoa mara mia zinafurahiwa sasa kwa kuwa mmoja wa Watu wa Mungu.

Haya maneno ya kawaida yanayozungumzia familia kimsingi yanatoa hakikisho kwamba maisha ya familia yaliyoathiriwa na uanafunzi yanarejeshwa kupitia familia kubwa—familia ya Mungu. Siamini kwamba kifungu hiki kinamaanisha kuahidi wingi wa mambo mema kataiaka maisha haya, kama ilivyofanyka katika Kumb. 27-28. Ukiziishi Baraka katika thawabu ya muundo wa huduma binafsi, na sasa kwa nini neema? Nyenzo za baraka si uzoefu wa waamini wote wanaomcha Mungu, bali ulivyo uzoefu wa furaha na wingi wa ukubwa wa familia ya Kikristo!

◙ **"pamoja na udhia"** Hili ni jumuisho lenye kuogofya, la kipekee kwa Marko. Wakristo watateswa katika ulimwengu huu ulioanguka (kama vile Mt. 5:10-12; Rum. 8:17; 2 Kor. 1:5,7; Flp. 3:10; 2 Tim. 2:9-12; 1 Pet. 4:12-16). Mateso haya yanafanya kazi kadhaa za makusudi ya ki-Ungu : (1) ushahidi kwamba tumeokolewa; (2) Maana ya maungu kutuumba sisi katika ufanano na Kristo; na (3) kuhakikisha kwamba ulimwengu utahukumiwa.

◙ **"ulimwengu ujao"** Dini ya Kiyahudi ya Kipindi cha Uwazi kati ya Agano la Kale na Aganao Jipya (waandishi wa walimu wa sheria za Kiyahudi na Magombo ya Bahari ya Chumvi) waliiona historia kaataka enzi mbili. Enzi za uovu wa sasa inayotawaliwana enzi ya kimalaika na uasi wa mwanadamu na enzi ambapo Mungu anakwenda kuivunja historia kupitia Masihi na kutengeneza enzi mpya, enzi ya haki na amani. Wakatai mwingine hili linafafanuliwa katiaka wingi wa kidunia kwa kufuata Kumb. 27-28 (kama vile Amosi 9:13-15) na wakatai mwingine katika "mbingu mpya na nchi mpya" (kama vile Isaya 56-66). Kutokana na Agano Jipya ni dhahiri kuwa enzi mpya (yaani., ufalme wa Mungu) ziliimarishwa katika kristo kuutwaa mwili huko Bethlehemu, lakini bado hazijakamilishwa. Agano Jipya inafunua ujiowa Masihi wa aina mbili, ya kwanza kama Mateso ya Mtumishi wa Isaya 53 na ya pili kama Mfalme wa Wafalme. Wakristo wanaishi katika "tayari, lakkini si katika bado" ya kukutana na enzi hizi za Kiyahudi. Sisi kamawafuasi wa Kristo tunabarikiwa kiroho katika enzi zote (kama vile Efe. 2:5-6). Tazama Mada Maalum: Enzi hizi na Enzi zijazo katika Marko 13:8.

◙ **" uzima wa milele"** Hili ndilo alililoliuliza yule kijana tajiri kuhusu—maisha na Mungu, aina ya maisha ya Mungu. Marko anakitumia kivumishi *(aiōnios* ) kuzungumzia dhambi ya milele katika Marko 3:29 na maisha ya milele hapa. Hili linatumika katika maisha (yaani., *zōa*) ya enzi mpya, maisha ya Ufalme wa Mungu. Yapo katika Katika, lakini yatakamilishwa katika kurudi kwake (yaani, *parousia*= kuwepo).

Hiki kifungu baiknishi ni adimu zaidi katika Injili za Kimuhtasari, lakini ni cha kawaida katika injili ya Yahana. Hiki ni kifungu cha msingi katika maandiko ya yote ya Yohana (kama vile Yohana 3:15; 4:36; 5:39; 6:54,68; 10:28; 12:25; 17:2,3; 1 Yohana 1:2; 2:25; 3:15; 5:11,13,20). Tazama MADA MAALUM : MILELE katika Marko 3: 29

**10:31** "**kwanza watakuwa wa mwisho**" Hii ilikuwa kweli ya kiroho yenye kustaajabisha (kama vile Mt. 19:30; 20:16). Mali na nafasi ya kweli haiangalii viwango vya utajiri (kama vile Isa. 55:8-9). Huu mkanganyiko kwa namna ya tofauti ulikuwa wa wanafaujnzi wa Aganao la Kale walikuwa na dhana kujihesabia haki (kama vile Mt. 19:30; Luka 13:30). Tazama Gordon Fee, *The Disease of the Health and Wealth Gospel.*

Hli linaweza kuelekezwa juu ya Petro kujitoa ghafla kama dhabihu za kuwa wanafunzi (kama vile Marko 10:28). Kifungu hiki kinaweka mpangilio wa hatua ya kithiolojia ya 10:41-45. Yesu, Mfalme wa Wafalme wa siku za mwisho, anakuwa Mtumishi Ateswaye wa Isa. 52:13-53:12! Waamini wawe na uamsho kuhusu maisha yake/kifo chake /huduma yake (kama vile 1 Yohana 3:16). Injili ni huduma, si nguvu; upendo si nguvu.

**ANDIKO LA NASAB (LILILOBORESHWA) MARKO 10:32-34**
**[31]Nao walikuwako njiani, huku wakipanda kwenda Yerusalemu; na Yesu alikuwa akiwatangulia, wakashangaa, nao katika kufuata wakaogopa. Akawatwaa tena wale Thenashara, akaanza kuwaambia habari za mambo yatakayompata, [33]akisema, Angalieni, tunapanda kwenda Yerusalemu; na Mwana wa Adamu atatiwa mikononi mwa wakuu wa makuhani na waandishi, nao watamhukumu afe, watamtia mikononi mwa Mataifa, [34] nao watamdhihaki, na kumtemea mate, na kumpiga mijeledi, na kumwua; na baada ya siku tatu atafufuka.**

**10:32 " njiani"** Katika Agano la Kale stiari ya njia au njia aua pitoilitumika kueleza maisha ya ki-Ungu (kama vile Zab. 23:3; 32:8; 50:23; 119:1; 139:3; Mit. 2:12-15; 4:18; 12:28; 15:24). Pia inaeleza juu ya huduma ya Yohana Mbatizaji ya "kutengeneza njia ya Bwana" (kama vile Isaya 40). Katika Matendo jina la kale la kanisa lilikuwa " Njia" (kama vile Marko 9:2; 19:9,23; 22:4,14,22).

Marko anaonekana kuiumba Injili yakekando na stiari ya kibiblia ya maisha ya imani (kama vile Marko 1:2,3; 8:27;9:33,34; 10:32,52). Yesu alikuwa katika uwelekeo wa hija ya msalabani (kama vile Marko 10:45).

◙ **" Yesu alikuwa akiwatangulia"** Kifungu hiki kinaweza kulirejelea kundi la ki-Utume au msafara wa wana-hija uliokuwa umetangulia kwa ajili ya sikukuu humo Yerusalemu.

◙ **" wakashangaa, nao katika kufuata wakaogopa"** Kifungu hiki lazima kihusiane na nabii tatu za Yesu za hapo awali kuhusu mateso na kifo chake humo Yerusalemu mikononi mwa wakuu wa Kiyahudi na KIrumi. Yesu alilijua litakalompata na bado aliendelea kutembea kwa kasi na kwa ujasiri. Hawa wanaweza kuwa walihofia kuhusu mateso na kifo chake kuwa na madhara kwao!

◙ **" Akawatwaa tena wale Thenashara"** Huu ni utabiri wa nne wa mateso na kifo cha Yesu (kama vile Marko 8:31; 9:12;31). Huu ni undani zaidi wa tabiri za Yesu. Yeye alijua fika kitakachotokea mbele yake (kama vile Marko 10:45). Bado wanafunzi wasingeweza kubaini kusudi na umuhimu wake (kama vile Marko 9:32; Luka 9:45; 18:34).

◙ **" akaanza kuwaambia habari za mambo yatakayompata"** Vitenzi vingi vilivyo katika Marko 10:32 ni vya kauli zisizo timilifu, zenye kurejelea tendo liliorudiwarudiwa. Nafikiri pia hili linaurejelea unabii wa Yesu uliorudiwa rudiwa kuhusu mateso yake ; hivyo, neno "akaanza" ni tafsiri iliyokosewa kauli hii isiyo timilifu (kama vile TEV). Katika maana moja Yesu alikuwa akiifunua nguvu na mamlaka yake kwa kuujua ubaadaye wake na kukitwala kifo na ufufuo wake (kama vile Yohana 10:17-18).

**10:33 "' Mwana wa Adamu'"** Tazama Maelezo katika Marko 8:38c.

◙ **" atatiwa mikononi mwa wakuu wa makuhani na waandishi"** Hiki ni kifungu bainishi cha Wakuu wa Sinagogi (kama vile Marko 14:43 na kuendelea) ambao walikuwa baraza kuu la Kiyahudi, ingawa katika karne ya kwanza hili lilikuwa na mamlaka yenye kuwekewa mipaka. Tazama Mada Maalum katika Marko 12:13. Yesu alitabiri juu ya mashambulizi ya Wakuu wa Sinagogi. Kuingia kwa Yesu katika Yerusalemu na kulisafisha Hekalu kulikazia chuki yake. Tendo la kwanza liliwakasirisha Mafarisayo na la pili liliwakasirisha Masadukayo.

◙ **" watamtia mikononi mwa Mataifa"** Kifungu hiki kiliirejelea kazi ya jeshi la Kirumi (kama vile Marko 15:1).
Wakuu wa Sinagogi hawakuwa na uwezo wa kutoa adhabu kubwa, ni sekali ya Kirumi pekee iliyofanya hivyo.

**10:34 " nao watamdhihaki"** Hili lilikamilishwa na askarai wa Kirumi katika Marko 15:16-20. Marko hakulinukuu jaribio la Yesu mbele ya Herode Antipasi (kama vile Luka 23).

◙ **" kumtemea mate"** Hii ilikuwa ishara ya Agano la Kale ya dharau (kama vile.Hes. 12:14; Kumb. 25:9; Ayubu 17:6; 30:10; Isa. 50:6). Askari wa Kirumi walizichukua chuki zote za Kiyahudina na mninu zote za kiutengano kisha wakamtwika Yesu (kama vile. Marko 14:65).

◙ **" kumpiga mijeledi"** Tendo la kupiga mijeredi ni tendo lililofanyika kabla ya kusulibiwa (kama vile Marko 15:15). Mikono ya mtu ilifungwa kwa kamba nyembamba. Askari walitumia mjeredi uliotengenezwa kwa vipande vya mimea fulani inayopatikana kwenye majabari, chuma, au mifupa iliyofungwa katika kingo za ngozi yenye urefu upatao hatua mbili kwa ajili ya kumpigia mfungwa nyuma ya mgongo. Tendo la kupiga kwa mijeredi liliharibu uti wa mgongo na liling'oa meno na hata macho. Wafungwa wengi walikufa kutokana na kipigo hiki. Hiki kilikuwa kipigo cha kikatili (kama vile Isa. 52:14).

◙ " **baada ya siku tatu** " Kuhalisia hii ni "baada ya siku tatu." Kipindi hiki cha wakati huenda kilihusiana na uzoefu wa Yona (kama vile Mt. 12:39-41; 16:4,21; Luka 11:39,32). Pia kinatajwa na Paulo katika muhtasari wake wa injili katika 1 Kor. 15:4. Yesu aliutumia unabii "siku ya tatu" katika uhusiano na matukio mawili: (1) Kufufuka kwake toka Wafu (kama vile Marko 8:31; 9:31; 10:34), lakini pia (2) Kujenga kwake hekalu jipya (kama vile Marko 14:58; 15:29; Yohana 2:19; Matendo 6:14).
Kuna tofauti ya machapisho ya Kiyunani iliyohusianishwa na kifungu hiki. Katika ufanano (Mt. 20:19 na Luka 18:33) kuna kifungu "siku ya tatu." Hiki kinapatikana hapa katika Marko katika MSS, A na W. Hata hivyo, Sifa bainifu ya uwekaji wa vifungu vya Marko inapatikana katika Marko na 8:31 na 9:31 ni "baada ya siku tatu," ambavyo vinajitokeza katika MSS, א, B, C, D, na L.

◙ **" atafufuka"** Hii ni kauli ya katai elekezi . Inatazamia juu ya kufufuka kwa Yesu (kama vile Yohana 10:17-18). Vifungu vingi vinavyozungumzia ufufuo wa Kristo ni vya kauali tendwa, zenye kutoa tazamio la Mungu Baba kama mwanzilishi wa ufufuo akionyesha kuikubali kwake dhabihu ya Kristo. Katika maana moja Utatu wote unahusishwa kataiaka ufufuo wa Yesu (yaani., Roho katika Rum. 8:11). Tazama Mada Maalum: Ufufuo katika Marko 8:31.

**ANDIKO LA NASAB (LILILOBORESHWA) MARKO 10:35-4O**
**[35] Na Yakobo na Yohana, wana wa Zebedayo, wakamwendea, wakamwambia, Mwalimu, twataka utufanyie lo lote tutakalokuomba. [36] Akawaambia, Mwataka niwafanyie nini? [37] Wakamwambia, Utujalie sisi tuketi, mmoja mkono wako wa kuume, na mmoja mkono wako wa kushoto, katika utukufu wako. [38] Yesu akawaambia, Hamjui mnaloliomba. Mwaweza kunywea kikombe ninyweacho mimi, au kubatizwa ubatizo nibatizwao mimi?**
**[39] Wakamwambia, Twaweza. Yesu akawaambia, Kikombe ninyweacho mimi mtakinywea, na ubatizo nibatizwao mimi mtabatizwa; [40] lakini habari ya kuketi mkono wangu wa kuume au mkono wangu wa kushoto si langu kuwapa, ila wao watapewa waliowekewa tayari.**

**10:35 " wana wa Zebedayo"** Mathayo 20:20 anasema kuwa mama yao ndiye aliyeuliza swali.

◙ "' **twataka utufanyie lo lote tutakalokuomba**'" Yesu aliyatabiri mateso na kifo chake kila wakati, Wanafunzi wake walikuwa wakipanga juu ya mtu atakeye chuhua nafasi yake kama kiongozi! Mtazamo wao wa kifikra bado ulikuwa wa ufalme wa kidunia na kuwa kwao watawala. Wanafunzi wake hawakuelewa hadi siku ya Pentekoste! Katika maana moja tukio hili limeandikwa ili kuonyesha namna gani wanafunzi hawa hawakuwa na uelewa juu ya mambo haya (kama vile Luka 18:34). Hii ni kebehi yenye kuhumiza!

**10:37 "kuume. . .kushoto'"** Hawa walihitaji sehemu za heshima na mamlaka. Tukio hili linaonyesha kwamba Petro hakukubalika kama kiongozi sahihi wa kundi la ki- Utume. Mwonekano wake ulimsababisha kuzungumza akiwa wa kwanza, lakini yeye hakujihisi kama kiongozi wao.

◙ **"' katika utukufu wako'"** Mathayo 20:21 ina kifungu "katika ufalme wako" Katika Marko hiki kinarejelea udhihirisho wa ufalme wa Mungu wa matukio ya siku za mwisho yanayoonekana (Marko 8:38; 10:37; 13:36).

## MADA MAALUM : UTUKUFU *(DOXA)*

I. Maana yake kubwa

Kuna maneno yapatayo ishirini yaliyo litafasiri neno "utukufu" (*doxa)* na agano la kale la Kiyunani, lakini neno la Kiebrania lililo muhimu sana ni *kabod* (BDB 458-459, 455-458). Maana yake ya msingi ni ile ambayo ni nzito. Lilikuwa

ni neno la kibiashara lililotumika kwenye ununuzi wa miamala (yaani .vipimo). likaja kuwa na elimu-maana kubwa ambapo dhana ya uzito ikajitokeza katika kilo, watu wenye nazo, mahali na vitu.

II. Utumiaji wa neno YHWH

A. ikajakuwa ndo njia ya kuelezea uwepo binafsi wa YHWH. Ilijumuisha nguvu zake, uweza (yaani, uliopita mipaka) akiwa na u-mtu wake na uwepo katika umbo la kirahisia.

B. Ilidokeza YHWH katika uumbaji, kama vile Zab. 19:1; 29:3,9; 104:31

C. Lilitumika katika udhihilisho wa wazi wa Mungu kwa mwanadamu likijiungamanisha na utengenezaji wa agano la watu wake. Yeye ni “utukufu wa Israel”,kama vile 1Sam. 15:29

1) Safari yao ya kutoka Misri kama vile Hes. 14:22 (ilitabiliwa katika Mwa. 15:12-21)

1) Katika wingu la utukufu lililowafunika na kuwaongoza kama vile Kut. 16:7,10

2) Utoaji wa sheria zake katika mlima Sinai

3) Matendo yake ya utoaji na hukumu wakati wa kutangatanga nyikani

a. Uwasi wa awali uliohusiana na taarifa ya wapelelezi kumi na mbili,kama vile Hes. 14:9-10

b. Uingiliaji kati wa Musa kwa niaba yao kama vile Hes. 14:20-21

c. Uasi wa Kola kama vile Hes. 16:19

d. Mgogora wa maji, kama vile Hes. 26:6

D. Ombi la Musa kutaka kumwona Mungu, kama vile Kut. 33:18-23

E. Lilitumika na YHWH mwenyewe

1) 1Nya. 29:11

2) Zab. 106:20; Yer. 2:11; Hos. 4:7; Rum. 1:23

3) Isa. 42:8; 45:7; 48:11; 58:8; 60:1-2,19 (Ufu. 21:23; 22:5)

4) Zak. 2:5,10

F. Lilitumika katika muunganikano wa uwepo wa YHWH na/ katika

1) Hema takatifu, kama vile Kut. 16:7,10; 29:43; 40:34-35; Law. 9:6,23

2) Hekalu, kama vile 1 Fal. 811; 2 Nya. 5:14; 7:1-3; Isa. 6:3; Hag. 2:3,9

3) Sanduku la agano, kama vile 1 Sam. 4:22; Zab. 63:2; 78:61

G. Lilitumika katika ufalme wa YHWH, kama vile 1 Nya 29:12-13; Zab. 24:7-10; 45:3

H. Lilitumika na YHWH katka hali ya kuadilisha (yaani, haki), kama vile Zab. 29:3; 97:6; Isa. 42:8; 48:11; 58:8; Hab. 2:14

III. Lilitumika kwa wanadamu na mataifa

A. Binadamu

1) Likiendana na “nafsi” (yaani, *nephesh)* kama vile Mwa. 49:6; Zab. 16:9; 108:1

2) Mali, kama vile Mwa. 31:1; Zab. 49:16,17; Isa. 10:3; 61:6; 66:11-12

3) Heshima, kama vile Mwa. 45:13; Zab. 8:6; Hag. 2:7

4) Sifa njema,kama vile Ayu 19:9; 29:20; Zab. 4:2; 49:17

5) Uzuri, kama vile 1 Nya. 29:12,28; 2 Nya. 17:5; 18:13; 32:27

B. Mataifa

1) Misri,

2) Ephrahim, kama vile Hos. 9:11

3) Samaria, kama vile Hos. 10:5

C. Wafalme

1) Ahausuero, kama vile Estha 1:4

2) Israel, kama vile Zab 21:6

3) Antiochus IV, kama vile Dan. 11:39

D. Majeshi ya mataifa

1) syria, kama vile Isa. 8:7

2) Israel, kama vile Isa. 17:4

3) Kedar, kama vile Isa. 21:16

IV. Lilitumika kwenye maelezo ya siku za mwisho

A. YEHOVA atarudi kwenye hekalu lake jipya, kama vile Eze. 43:2,4,5; 44:4

B. YHWH atauvutwa ulimwengu wote kwake, kama vile Isa. 40:5; 59:19; 60:1-3; 66:18-19
C. YHWH ataishusha Yerusalem “mpya” kama vile Isa. 66:10; Zak. 12:7

V. Kusudi la uumbaji ni kumtukuza YHWH
   A. Aliumba kwa ajili ya utukufu wake,kama vile Isa. 43:7
   B. Utukufu ni juu yake, kama vile 1 Nya. 16:29
   C. Imba/sifu utukufu wake, kama vile Zab. 66:2; 96:8; 115:1
   D. Yote tuyatendayo twayatenda katika yeye, kwa ajili ya utukufu wake, kama vile 1 Kor. 10:31; 2 Kor. 4:15; Efe. 5:22; 6:5; 1 Petr. 2:12
   E. Maelezo ya kwanza ya katekismu.

**10:38 "' Hamjui mnaloliomba'"** "Kuomba" ni kauli ya kati, ambayo inatazamia juu ya suala, "ninyi." Kifungu kinachofuata ni "mwaweza" pia ni kauli ya kati.

◙ **"kikombe"** Hili lilitumika katIka Agano la Kale kumaanisha hatima ya mtu, mara nyingi katika maana kanushi (kama vile Zab. 75:8; Isa. 51:17-23; Jer. 25:15-28; 49:12; 51:7; Omb. 4:21-22; Eze. 32:34; Hab. 2:16; Zek. 12:2). Hii ni stiari iliyotumiwa sana na Yesu katika Gethsemane (kama vile Marko 14:36) kuzungumzia kusulibiwa kwake.

◙ **"' kubatizwa ubatizo nibatizwao mimi'"** Hii ilikuwa stiari ya mateso, hata kifo (kama vile Luka 12:50). Utukufu wake ulihusisha maumivu (kama vile Ebr. 2:18; 5:8).

**10:39** Viongozi hawa wangehisishwa katika mateso yale yale na hawakuelewa kwamba Yesu alikuwa ana uzoefu wa kutosha (yaani., Yakobo katika Matendo 12:2 na Yohana katika Ufu. 1:9).

**10:40 "' wao watapewa waliowekewa tayari'"** Huu ni mfano mwingine wa kujidogoisha kwa Yesu kwa mpango na kusudi la Baba. Kuna mpango wa ki-Ungu (kama vile Matendo 2:3; 3:18; 4:28; 13:29). Andiko la kale la Iskanda (MS A*) linaongeza "na Baba yangu,"ambalo pia linapatikana katika Mt. 20:23.
Herufi machapisho ya Kiyunani zote zilikuwa zimeandikwa katika herufi kubwa pasipokutenganishwa kati ya maneno, pasipo alama za kiuandishi au kutengwa katai aya. Wakati mwingine waliamua kuzigawa tungo katika maneno yenye mkanganyiko. Tungo hii inaweza kugawanyika katika namna mbili (kama vile *Interpreting the New Testament* na Hans Conzelmann na Andreas Lindemann inafasiriwa na Siegfried S. Schotzmann, uk. 22)

1. "kwa yule anayemaanishwa"
2. "ilimaanisha wengine" (kama vile tafsri za Kishamu)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 10:41-45**
**[41] Hata wale kumi waliposikia wakaanza kuwakasirikia Yakobo na Yohana. [42] Yesu akawaita, akawaambia, Mwajua ya kuwa wale wanaohesabiwa kuwa wakuu wa Mataifa huwatawala kwa nguvu, na wakubwa wao huwatumikisha. [43] Lakini haitakuwa hivyo kwenu; bali mtu Lakini haitakuwa hivyo kwenu, atakuwa mtumishi wenu, [44] na mtu anayetaka kuwa wa kwanza wenu, atakuwa mtumwa wa wote. [45] Kwa maana Mwana wa Adamu naye hakuja kutumikiwa, bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi.**

**10:41 " waliposikia"** Hili linaonyesha kuwa Yakobo na Yohana walisubiri hadi wakati ule walipokuwa na Yesu pekee. Pia Iubinadamu wa Mitume. Hawa hawakuwa "watakataifu kamili," bali waliitwa watu, waliotengwa, na kutumiwa na Mungu. Wengine walighadhibika, si kwa saababu ya kutokuuliza kwa usahihi kwa Yakobo na Yohana, bali ni kwa sababu walikwenda kutoa ombi lao kwanza. Hawa mitume wateule bado waliendelea kuonyesha ubinafsi na dhambi.

**10:42** Kwa mara nyingine tena Yesu alieleza juu ya shauku na kutoelewa kwao kuhusu Ufalme .

**10 : 43**:
**NASB " Lakini haitakuwa hivyo kwenu"**
**NKJV "Bado haitakuwa hivyo kwenu"**

**NRSV** **"Bali si miongoni mwenu"**
**TEV** **"Hii, hata hivyo, si ilivyo miongoni mwenu"**
**NJB** **"Miongoni mwenu hili halitokei"**

Tafsiri hizi zinaakisi tofauti ya machapisho ya Kiyunani. Katika machapisho mengine (א, B, C*, D, L, W) kauli ya wakati uliopo inatumika (kama vile NASB, NRSV, TEV), ambayo pia inapatikana katika ufanano ulio katika Mt. 20:26. Hata hivyo, katika machapisho mengine (A na C 3) wakati ujao unapatikana (kama vile NKJV na inavyomaanishwa katika NJB).

◙ **"'anayetaka kuwa wa kwanza wenu'"** Yesu hatoi pingamizi kuhusiana na ukuu au shauku ya ukuu, bali anataoa ufafanuzi kuhusu ukuu ulio wa kweli kama huduma na ubunadamu (kama vile Mt. 20:26; Marko 9:35).

◙ **"mtumishi"** Hili ni neno *diakonos*, ambalo baadaye linakuwa rasmi/kazi ya shemasi. Waamini wote wanaitwa kutumika (kama vile Efe. 4:11-12).

**10:44** Hii inasaidia kutoa maelezo ya Marko 10:31.

◙ **"mtumwa"** Hili ni neno *doulos*, ambalo lilimrejelea mtumishi wa ndani.

**10:45** "'**Mwana wa Adamu**'" Tazama Maelezo katika Marko 8:38c.

◙ **"' hakuja kutumikiwa, bali kutumika'"** Huu ni ufafanuzi sahihi wa neno ukuu. Yesu aliyaumba maisha ya Ufalme kwa ajili yetu ili toa uhamsho (kama vile 1 Pet. 2:21). Kweli hii ilifundishwa kiishara katika Yesu kuwaosha miiguu wanafunzi wake huko ghorofani usiku ule aliposalitiwa (kama vile Yohana 13:14-15).
Ukweli huu mara nyingi ni mgumu kwa maongozi ya kanisa. Bali pasipo huu hakuna kanisa lenye utumishi.

◙ **" kutoa nafsi yake'"** Huu ni muhtasari wa mstari wa Injili ya Marko. Mara nyingi Yesu alikirejelea kifo chake kama thawabu yake au utukufu wake. Hii inamaanisha kuondolewa, upatanisho mbadala (yaani., kujitoa kwa ajili ya dhambi, kama vile. 2 Kor. 5:21) kwa Kristo (kama vile Mwa. 3:15; Isa. 52:13-53:12).

◙ **"' fidia"** Kiuhalisia hii ni "kulipa" au "kulipa gharama" (kama vile Mt. 20:28; Tito 2:14; 1 Pet. 1:18). Hiki kinaliakisi neno la Agano la Kale linalotumika kuwazungumzia watumwa na wafungwa wa vita wanaokuwa waliorejeshwa, mara nyingi na jamaa wa karibu (*go'el*). Yesu anajiunganisha katika upendo na haki ya Baba Mungu. Maisha ya gharama ya dhambi —aliyoyatoa Mungu!

## MADA MAALUM: FIDIA/KOMBOA

. AGANO LA KALE

A. Kuna maneno mawili ya kimsingi ya sheria ya Kiebrania yanayoeleza dhana hii.
   1. *Ga'al* (BDB 145 I, KB 169 I), ambalo kimsingi linamaanisha "kuwa huru kwa maana ya ile gharama iliyolipwa." Muundo wa neno *go'el* unaongeza dhana ya mpatanishi binafsi, mara nyingi huwa mmoja wa familia (yaani, mkombozi wa ndugu wa damu). Hiki kipengele cha kiutamaduni cha haki ya kununua vitu tena, wanyama, ardhi (kama vile Mambo ya Walawi 25,27), au ndugu na (kama vile Ruthu 4:14; Isa. 29:22) hili linaawilishwa kitheolojia hadi kwa ukombozi wa YHWH kwa Israeli kutoka Misri (kama vile Kut. 6:6; 15:13; Zab. 74:2; 77:15; Yer. 31:11). Huyu amekuwa "Mwokozi" (kama vile Ayubu 19:25; Zab. 19:14; 78:35; Mit. 23:11; Isa. 41:14; 43:14; 44:6,24; 47:4; 48:17; 49:7,26; 54:5,8; 59:20; 60:16; 63:16; Yer. 50:34).
   2. Neno *Padah* (BDB 804, KB 911), ambalo kimsingi linamaanisha "kuokoa" au "kusaidia."
      a. ukombozi wa mzaliwa wa kwanza (Kut. 13:13-15 na Hes. 18:15-17)
      b. ukombozi wa kimwili unatofautishwa na ukombozik wa kiroho (Zab. 49:7,8,15)

c. YHWH ataikomboa Israeli katoka katika dhambi na uhasi wao (Zab. 130:7-8)

B. Dhana ya kitheolojia inahusisha mambo kadhaa yanayohusiana.
   1. Kuna uhitaji, utumwa, unyanganywaji, kifungo.
      a. Kimaumbile
      b. Kijamii
      c. kiroho (kama vile Zab. 130:8)
   2. Gharama lazima ilipwe kwa ajili uya ukombozi, msamaha, na urejesho.
      a. Juu ya taifa la Israeli (kama vile Kut. 7:8)
      b. Juu ya mtu binafsi (kama vile Ayubu 19:25-27; 33:28; Isaya 53)
   3. Lazima mtu atende kama msuluishi na mtenda mema. Ndani ya *ga'al* mara nyingi huyu ni mmoja wa familia au ndugu wa karibu (i.e., *go'el*, BDB 145).
   4. Mara nyingi YHWH anajibainisha katika maneno ya kifamilia.
      a. Baba
      b. Mme
      c. Ndugu wa karibu kama Mkombozi/ Ukombozi wa Mlipa kisasi aliyesalimishwa kupitia nguvu binafsi ya YHWH; gharama ililipwa, na ukombozi ulikamilishwa!

. AGANO JIPYA

A. Kuna maneno kadhaa yaliyotumika kueleza dhana ya kitheolojia.
   1. *Agorazō* (kama vile 1 Kor. 6:20; 7:23; 2 Pet. 2:1; Ufu. 5:9; 14:3-4). Hili ni neno la kibiashara ambalo linaakisi juu ya ile gharama iliyolipwa kwa ajili ya kitu fulani. Sisi ni watu tulionunuliwa kwa damu tusioyandesha maisha yetu wenyewe. Sisis ni wa Kristo.
   2. *Exagorazō* (kama vile Gal. 3:13; 4:5; Efe. 5:16; Kol. 4:5). Hikli pia ni neno la kibiashara. Hili linaakisi juu ya kifo halisi cha Yesu kwa ajili yetu. Yesu aliiondoa ile "laanae" utedaji uliojikita ndani ya sheria yaani, Sheria ya Musa, kama vile Efe. 2:14-16; Kol. 2:14), ambayo wanadamu wenye dhambi wasingeitimiliza. Yeye aliiondoa laana (kama vile Kumb. 21:23) kwa ajili yetu sote (kama vile Marko 10:45; 2 Kor. 5:21)! Katika Yesu, Haki na pendo la Mungu huungana katika msamaha kamili, ukubalifu, na upenyo!
   3. *Luō,* "kuweka huru"
      a. *Lutron*, "gharama iliyolipwa" (kama vile Mt. 20:28; Marko 10:45). Haya ni maneno yenye nguvu kutoka ndani ya kinywa cha Yesu mwenyewe kuhusiana na kusudi la ujio Wake, kuwa Mwokozi wa ulimwengu kwa kulipa deni la dhambi isiyompasa (kama vile Yohana 1:29)
      b. *Lutroō*, "kuwekwa huru"
         1) kuikomboa Israeli (Luka 24:21)
         2) kujitoa mwenyewe kwa ajili ya kuwakomboa na kuwatakasa watu (Tito 2:14)
         3) Kuwa wasi na dhambi badala yake (1 Pet. 1:18-19)
      c. *Lutrōsis,* "ukombozi," "wokovu," au "uhuru"
         1) Unabii wa Zakaria kumhusu Yesu, Luka 1:68
         2) Sifa za Anna kwa Mungu kwa ajili ya Yesu, Luka 2:38
         3) Ubora wa Yesu, alipojitoa sadaka, Ebr. 9:12
   4. *Apolytrōsis*
      a. ukombozi katika Ujio wa Mara ya Pili (kama vile Matendo 3:19-21)
         1) Luka 21:28
         2) Warumi 8:23
         3) Waefeso 1:14; 4:30
         4) Waebrania 9:15
      b. Ukombozi katika kifo cha Kristo
         1) Warumi 3:24
         2) 1 Wakorintho 1:30
         3) Waefeso 1:7

4) Wakolosai 1:14

5. *Antilytron* (kama vile 1 Tim. 2:6). Hili ni andiko la maana sana (kama ilivyo Tito 2:14) ambayo linahusianisha kujitoa kwa Yesu kwa ajili ya kifo cha msalaba. Yeye ndiye mmoja na dhabihu pekee iliyokubaliwa, yeye aliyewafia "wote" (kama vile Yohana 1:29; 3:16-17; 4:42; 1 Tim. 2:4; 4:10; Tito 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 2:2; 4:14).

B. Dhana ya kitheolojia katika Agano Jipya.

1. Mwanadamu amefungwa na dhambi (kama vile Yohana 8:34; Rum. 3:10-18,23; 6:23).
2. Kifungo cha mwanadamu juu ya dhambia kimefunuliwa na Agano la Kale la Sheria ya Musa (kama vile Wagalatia 3) na Hotuba ya Yesu kule Mlimani (kama vile Mathayo 5-7). Matendo ya mwanadamu yamekuwa hati ya kifo (kama vile Kol. 2:14).
3. Yesu, Mwana-Kondoo asiye na dhambi, amekuja na kufa badala yetu (kama vile Marko 10:45; Yohana 1:29; 2 Kor. 5:21). Tumenunuliwa kutoka dhambini ili tumtumikie Mungu (kama vile Warumi 6).
4. Kwa maana hiyo wote YHWH na Yesu ni "ndugu wa karibu" wanaotenda kazi badala yetu. Hili linaendeleza zile stiari za kifamilia (yaani, baba, mume, mwana, kaka, ndugu wa karibu).
5. Ukombozi haukuwa gharama iliyolipwa kwa Shetani (yaani, theolojia ya Enzi za Kati), bali upatanisho wa neno la Mungu na haki ya Mungu pamoja na pendo la Mungu na kujitoa kwa ukamilifu ndani ya Kristo. Pale msalabani amani ilirejeshwa, uasi wa mwandamu ulisamehewa, sura na mfano wa Mungu ndani ya mwanadamu inatenda kazi kwa ukamilifu tena katika ushirika wa karibu!

Bado kuna kipengele kingine cha ukombozi kinachoendelea (kama vile Rum. 8:23; Efe. 1:14; 4:30), ambacho kinahusisha miili yetu ya ufufuo na uhusiano binafsi wa karibu sana pamoja na Mungu wa Utatu(tazama Mada Maalum: Utatu). Miili yetu iliyofufuliwa itakuwa kama mwili Wake (kama vile 1 Yohana 3:2). Yeye ana umbo-mwili, lakini mwenye sifa ya namna nyingine. Ni vigumu kutoa ufafanuzi wa fumbo la 1 Kor. 15:12-19 pamoja na 1 Kor. 15:35-58. Kwa uwazi umbo-mwili, mwili wa kidunia na kutakuwa na ule wa kimbingu, mwili wa kiroho. Yesu alikuwa na yote!

◙ **"ya"** Hiki ni kiunganishi cha Kiyunani *anti*. Wakati mwingine kinaunganishwa katika nomino

◙ **"fidia"** (*lutron* = *antilutron*, kama vile 1 Tim. 2:6). Inaweza kumaanisha "badala ya," "kwa niaba ya," au "katika nafasi ya." Uhusiano kati ya viunganishi *anti* na *huper* lizima utambuliwe kutokana na muktadha (kama vile 2 Kor. 5:14; Ebr. 10:12; 1 Pet. 2:21; 3:18; 1 Yohana 3:16). Yote haya yana maana nyingine ya la wa Yesu, upatanisho uliowakilishwa. Alikufa kwa ajili yetu, alizibeba dhambi zetu (kama vile Isa. 53:4-6).

◙ **"wengi"** Hili neno wengi limekuwa likitumiwa na baadhi ya watoamaoni kuweka mipaka ya upatanisho wa Kristo "mteule." Haya maneno "wengi" na "wote" ni ya kivisawe katika vifungu viwili ambavyo vinashughulika na ukombozi. Linganisha Isa. 53:11-12, "wengi" na Isa. 53:6, "wote." Ufanano huu unaonekana dhahiri katika Rum. 5:18, "wote" na Rum. 5: 19, neno "wengi." Yesu alilipa gharama kwa wote, bali wale wanaoitikia kwa toba na imani kwa yule Roho auguaye wanakombolewa. Marko 10:45 ni moyo wa kithiolojia wa Injili. Hilli lilikuja kuwa katika shauku ya mwitikio binafsi.Shauku ya wmanadamu lazima apewe Mungu kama zawadi (kama vile Rum. 12:1-2). Lazima wakristo wawe na uamsho juu ya kujitoa kwa Kristo (kama vile 1 Yohana 3:16.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 10:46-52**
**[46] Wakafika Yeriko; hata alipokuwa akishika njia kutoka Yeriko, pamoja na wanafunzi wake, na mkutano mkubwa, mwana wa Timayo, Bartimayo, yule mwombaji kipofu, alikuwa ameketi kando ya njia. [47] Naye aliposikia ya kwamba ni Yesu Mnazareti, alianza kupaza sauti yake, na kusema, Mwana wa Daudi, Yesu, Mwana wa Daudi. [48] Na wengi wakamkemea ili anyamaze, lakini alizidi kupaza sauti, Mwana wa Daudi, unirehemu. [49] Yesu akasimama akasema, Mwiteni. Wakamwita yule kipofu, wakamwambia, Jipe moyo; inuka, anakuita. [50] Akatupa vazi lake, akaruka, akamwendea Yesu. [51] Yesu akamjibu, akamwambia, Wataka nikufanyie nini? Yule kipofu akamwambia, Mwalimu wangu, nataka nipate kuona. [52] Yesu akamwambia, Enenda zako, imani yako imekuponya. Mara akapata kuona; akamfuata njiani.**

**10:46 "Yeriko"** Huu ni mojawapo ya miji ya lake ulimwenguni na mara nyingi uliitwa "Mji wa Mitende." Hili jina linamaanisha "yenye harufu nzuri." Eneo hili lilikuwa zuri sana lenye rutuba. Katika siku za Yesu kulikuwa Yeriko za aina mbili za Yeriko, mji wazamani na Rumi mpya yapata maili moja. Huu ulikuwa maili zipatazo 18 kaskazini mashariki mwa Yerusalemu ng'ambo yam to Yordani.

◙ **" hata alipokuwa akishika njia"** Mathayo 20:29 ina kifungu "walipokuwa wakiondoka"; Luka18:35 ina kifungu "apokaribia." Mkanganyiko huu ni ishara ya melezo ya ushahidi wa macho. Kumbuka kulikuwa na Yeriko za aina mbili katika siku za Yesu. Ahgeacha moja na kiendea nyingine.

◙ **"mkutano mkubwa,"** Hawa walikuwa wana-hija waliokuwa wakielekea Yerusalemu kwa ajili ya Pasaka, kandokando ya watu wa mji waliokuwa na shauku naye. Makuhani wengi wa Hekalu walikuwa wawakilishi wa Yeriko. Barabara ya kutoka Yeriko kuelekea Yerusalemu ilikuwa ya hatari sana kwa sababu ya wanyang'anyi (yaani., Mfano wa Msamaria Mwema); hivyo, watu walikuwa wakitembea katika makundi ya idadi kubwa ya watu.

◙ **"mwombaji kipofu. . . alikuwa ameketi kando ya njia"** Kuna tofauti ya machapisho ya Kiyunani katika kifungu hiki. Hii Nomino "mwombaji" ni neno adimu (kama vile Yohana 9:8). Mara nyingi dhana hii inaelezwa kupitia kauli endelevu (yaani., MSS A, K, W, א na Textus Receptus, kama vile NKJV). Hata hivyo, nomino (yaani., *prosaiteō*) ni katika MSS א, B, L (kama vile NASB, NRSV, TEV, na NJB). Machapisho D yana kisawe (yaani., *Epaiteō,* yote yameundwa kutoka kutokana na asili "kuuliza"), ambayao inapatikana katika ufanano wa Luka 18:35. Tofauti hizi hazina madhara katika kukifasiri kifungu hiki.

◙ **"Bartimayo"** Hili neno linamaanisha "mwana wa Timayo." Si kawaida kwa Marko kuandika maneno ya watu ambao Yesu aliwaponya au aliwatoa pepo wachafu. Kwa namna yenye kuvutia, Mathayo alikuwa na vipofu wawili (kama vile Mt. 20:30). Hasa ni kwa nini tukio hili lilitukia, halijulikani, lakini ni tofauti ya kawaida kati ya Mathayo na Marko/Luka.

◙ **"mwana wa Timayo"** Katika ligha ya Kiaramu neno hili lilimaanisha "chafu." Hii ilikuwa hatua ya kueleza maana ya jiana la Bartimayo kwa watawala wa Mataifa.

◙ **" alikuwa ameketi kando ya njia"** Huenda hii ilikuwa nafasi ya mwombaji kipofu ya kila siku ambapo alitegemea kupewa msaada (yaani ., Sadaka za Kiyahudi zilizohitajika kwa ajili ya maskini).

**10:47 "Yesu Mnazarethi"** Kwa namna ya kipekee Marko analiandika neno hili kama *Nazarēnos* (kama vile Marko 1:24; 10:47; 14:67; 16:6). Injili ya Mathayo inasema "Aliyeitwa Mnazarayo" (kama vile Mt. 2:23). Kijiji alichokulia Yesu kiliitwa Nazareti. Hiki hakitajwi katika Agano la Kale, katika Kitabu cha Sheria za Kiyahudi, au katika Josephus. Kwa uwazi haukuhalikutatuliwa kipindi cha John Hyrcanus (yaani., Hasmonaen), aliyetawala toka 134-104 k.k. Kuwepo kwa Yusufu na Mariamu waliotoka katika kijiji hiki kunamaanisha kwamba ukoo wa uzao Daudi uliishi hapa. Huenda kuna uhusiano wa sili ya historia kati ya jina Nazareti na jina la Mgawanyo wa jina la Kimasihi, ambalo ni *netser* katika Kiebrania (kama vile Isa. 11:1; Yer. 23:5; 33:15; Zek. 3:8; 6:12; Ufu. 5:5; 22:16). Kwa uwazi hili lilikuwa neno la kimakemeo kwa sababu ya umbali wa eneo lake toka Yerusalemu katika eneo la Mataifa (kama vile Yohana 1:46 na Matendo 24:5; hata kama hili, nalo, lilikuwa la kiunabii, Isa. 9:1). Hii inaweza kuwa sababu ya kuwekwa kataika maandishi yaliyoandikwa katika ubao uliotundikwa juu ya kichwa chake pale alipokuwa msalabani.

## MADA MAALUMU: YESU MNAZARETI

Kuna maneno mbalimbali ya Kiyunani ambayo Agano Jipya hutumia kumzungumzia Yesu.

A. Haya ni maneno ya Agano Jipya
   1. Nazarethi – mji katika Galilaya (kama vile Luka 1:26; 2:4,39,51; 4:16; Matendo 10:38). Mji huu hautajwi katika vyanzo vya wakati huu, bali umekutwa katika kumbukumbu ya maandishi ya baadaye. Kwa upande wa Yesu kuwa alitoka Nazarethi haikujitosheleza (kama vile Yohana 1:46). Alama ya msalaba wa

Yesu ambayo imeliweka jina la eneo hili ilikuwa alama ya aibu kwa Wayahudi.

2. Nazarēnos – pia inataja maeneo ya kijiografia (kama vile Luka 4:34; 24:19).
3. Nazōraios – inaweza kuurejea juu ya mji, lakini pia ingeweza kuwa mwaminifu na mtenda haki Masihi wa Kiebrania "Utanzu" (*netzer*, BDB 666, KB 718 II, kama vile Isa. 11:1; maana zinazokaribiana, BDB 855, Yer. 23:5; 33:15; Zek. 3:8; 6:12; iliyodokezwa katika Ufu. 22:16). Luka akilitumia hili kumhusu Yesu katika 18:37 na Matendo 2:22; 3:6; 4:10; 6:14; 22:8; 24:5; 26:9.
4. Iliyohusiana na #3 *nāzir* (BDB 634, KB 684), ambalo linamaanisha "aliyewakifishwa kwa maana ya nadhiri."

B. matumizi ya Kihistoria ya neno nje ya Agano Jipya.

1. Lilimaanisha kundi la ausi la Kiyahudi (Mkristo wa awali) (nāsōrayyā ya Kiaramu).
2. Lilitumika katika mzunguko wa Kiyahudi kuwatambulisha waamini katika Kristo (cf. Matendo 24:5,14; 28:22, nosri).
3. Lilikuja kuwa neno la kawaida katika kumaanisha waamini katika makanisa ya Kisiria (Kiaramu). "Mkisto" lilitumika katika makanisa ya Kyunani kumaanisha waamini.
4. Wakati mwingine baada ya kuanguka kwa Yerusalemu, Wafarisayo walikusanyika huko huko Jamnia na walichochea utengano rasmi kati ya sinagogi na kanisa. Mfano wa aina ya maapizo ya mazungumzo dhidi ya Wakristo unapatikana katika "*the Eighteen Benedictions" from Berakoth 28b-29a*, ambayo "Wanazarethi." "Wanazarethi na awaasi waliweza kutoweka kwa muda mfupi; walifutwa kutoka katika kitabu cha uzima na kutoandikwa kuwa walikuwa na imani."
5. Ilitumiwiwa na Justin Martyr, Dial. 126:1, ambaye alitumia *netzer* ya (Isa. 11:1) kumhusu Yesu.

C. Maoni ya Mwandishi

Nashangazwa sana na herufi za maneno, Ingawa nafahamu kwamba hili ni jambo geni kusikika katika Agano la Kale "Yoshua" ina herufi mbalimbali katika Kiebrania. Maelezo yafuatayo yananisababisha kubaki na mashaka kama maana yake dhahiri :

1. kama vile maana yake ya karibu na neno la Kimasihi "tawi" (*netzer*) au neno lililo sawa *nāzir* (aliyepakwa mafuta kwa maana ya nadhiri)
2. vidokezo hasi vya eneo la Galilaya kuyahusu mataifa
3. uchache au kutokuwepo kwa uthibitisho wa fasili za sasa kukusu mji wa Nazarethi katka Galilaya
4. inatoka katika kinywa cha pepo katika maana ya hukumu (yaani, "Umekuja kutuangamiza?").

Kwa wasifu kamili wa masomo ya kundi la neno hili, tazama Colin Brown (ed.), *New International Dictionary of New Testament Theology*, juzuu. 2, uk. 346 au Raymond E. Brown, *Birth of the Messiah*, kr. 209-213, 223-225.

◙ **"' Mwana wa Daudi'"** Hili lilikuwa jina la ki-Mashi (kama vile 2 Sam. 7), ambalo lilikuwa na maana za kitaifa. Jina hili lilikuwa adimu sana katika Marko (kama vile Marko 10:47,48; 12:35).

◙ **"' Mwana wa Daudi'"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati usio timilifu, yenye kudokeza mkazo. Hili lilikuwa ombi la kawaida katika Zaburi (kama vile Marko 51:1).

**10:48 "wengi wakamkemea ili anyamaze"** Hii ni kauli ya wakatai usio timilifu. Alilia tena na tena na wao katika mkutano walimdhihaki tena na tena (kama vile Luka 18:39).

**10:49 " Yesu akasimama akasema",** Yesu alikuwa na muda wa kumsikiliza mwombaji kipofu! Bado hii ni ishara ya kinabii toka kwa Isaya kwa wale ambao wangeliona hili kiroho!

◙ **"' Mwiteni. Wakamwita yule kipofu, wakamwambia, Jipe moyo; inuka, anakuita'"** Mara nyingi katika lugha ya Koine ya Kiyunani kila kifungu kinahusianishwa na kifungu cha awali kwa kutumia kiunganishi au kiwakilishi ambacho kinacholejelea jambo fulani katika muktadha wa awali. Kihusianishi kinapokosa (kama ilivyo hapa) hawa wanakuwa na umakini wa semi. Hii ni mikazo, semi zilizotenganishwa. Ya Kwanza nay a Pili ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo na ya mwisho ni kauli tendaji elekezi ya wakati uliopo.

**10:50 "Akatupa vazi lake"** Vazi hili lilitumika kwa ajili ya (1) kulalia na (2) kukusanyia chakula na misaada. Katika maana hii hii ilikuwa ishara ya imani yake ambayo ingemponya.

◙ **"akaruka"** Huu ni undani wa ushahidi wa macho uliokumbukwa na Petro.

**10:51** "'**Wataka nikufanyie nini?**'" Yesu alimlazimisha kutamka ombi lake la imani.

◙ **"'nataka nipate kuona'**" Kumponya kipofu na umuhimu wa ki- Masihi (kama vile Isa. 35:4-5; 42:7,16;
61:1). Hii ilikuwa moja ya hakikisho za ishara ambazo Mafarisayo walikuwa wakizitaka.

**10:52 "'imani yako imekuponya'"** Kiuhalisia ni "okolewa" (yaani., *sōzō*) katika muundo wa kauli tendaji elekezi ya wakatai timilifu. Neno hili linatumika kataika maana nyingine za Agano la Kale zihusuzo ukombozi wa mwili (kama vile Yakobo 5:15).

◙ "**akamfuata njiani**" Luka 18:45 anaongeza, "akimtukuza Mungu."

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe zaBiblia. Kila mmojaw etu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini wazazi walimtaka Yesu aweke mikono juu ya wagonjwa wao?
2. Kwa nini wanafaunzi walijaraibu kuwazuia?
3. Kwa nini Yesu alighadhabika sana kuwahusu?
4. Ni kwa namna gani watoto walihusiana na ufalme wa Mungu?
5. Ni viwango gani vya mtoto ambavyo Yesu anavitaka katika wanafunzi wake?
6. Kwa nini Yesu aliwaambia wanafunzi wake mara kwa kuhusu kukaribia kwa kifo chake?
7. Toa ufafanuzi wa ukuu wa kweli

# MARKO 11

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Kuingia kwa furaha Yerusalemu | Kuingia kwa furaha | Jumapili ya matawi | kuingia kwa furaha Yerusalemu | Masihi anaingia Yerusalemu |
| 11:1-11 | 11:1-11 | 11:1-10 | 11:1-3 | 11:1-11 |
| | | | 11:4-5 | |
| | | | 11:6-10 | |
| | | 11:11 | 11:11 | |
| Kulaaniwa kwa Mti wa mtini | mtini unanyauka | mtini unalaaniwa | Yesu anaulaani mtini | Mtini tasa |
| 11:12-14 | 11:12-14 | 11:12-14 | 11:12-14a | 11:12-14 |
| | | | 11:14b | |
| Kusafishwa kwa Hekalu | Yesu anasafisha Hekalu | Kusafisha Hekalu | Yesu anakwenda Hekaluni | kufukuzwa kwa wafanya biashara kutoka Hekaluni |
| 11:15-19 | 11:15-19 | 11:15-19 | 11:15-17 | 11:15-19 |
| | | | 11:18 | |
| | | | 11:19 | |
| Somo kutoka Mtini ulionyauka | Somo la Mtini Ulionyauka | Maana ya mtini Ulionyauka | Somo la Mtini Ulionyauka | Mtini ulionyauka Imani na Maombi |
| 11:20-25 | 11:20-24 | 11:20-24 | 11:20-21 | 11:20-25 |
| | Msamaha na Maombi | | 11:22-25 | |
| | 11:25-26 | 11:25 | | |
| Inaondoa Marko 11:26 | | Inaondoa Marko 11:26 | Inaondoa Marko 11:26 | Inaondoa Marko 11:26 |
| Mamlaka ya Yesu Yanahojiwa | Mamlaka ya Yesu yanahojiwa | Juu ya Mamlaka ya Yesu | Swali juu ya Mamlaka ya Yesu | Mamlaka ya Yesu Yanahojiwa |
| 11:27-33 | 11:27-33 | 11:27-33 | 11:27-28 | 11:27-33 |
| | | | 11:29-30 | |
| | | | 11:31-33a | |
| | | | 11:33b | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka"Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Kuingia kwa sherehe ilikuwa ishara muhimu ya kinabii; Yesu alitangazwa kama Masihi aliyehaidiwa. Inafanana na Mt. 21:1-11, Luka 19:29-44, na Yohana 12:12-19.

B. Kulikuwa na utata juu ya kipengele cha kuingia kwa shangwe. Yesu kiuwazi alikuwa anatimiliza unabii wa Zakaria 9:9 na shangwe za sauti (yaani liturjia kutoka Zaburi) ya makutano ilikuwa ukiri wa U-Masihi Wake. Hatahivyo lazima ikumbukwe kwamba Zaburi hizi zilitumika kukaribisha mahujaji kila mwaka wakati walipokuwa wakija kwa ajili ya Pasaka. Ile hali kwamba walikuwa wanafanyia kazi kwa mtu fulani ilikuwa ni nupekee wa tukio hili. Hii inaonekana katika hofu ya viongozi wa kidini.

C. Kusafishwa kwa hekalu kunakoandikwa katika Marko 11:15-19 kidhahiri kulikuwa ni kusafishwa kwa hekalu mara ya pili. Ya kwanza inaandikwa katika Yohana 2:15. Sikubaliani na nadharia za ukosoaji wa kifasihi ambazo zinavuta matukio yote haya mawili na kulifanya kuwa moja. Ingawa kuna tatizo katika kuunganisha mfuatano wa Vitabu vya Injili na Injili ya Yohana, bado inaonekana bora kwangu kwasababu ya tofauti kati ya hadithi hizi mbili, kushikilia kusafisha kuwili, moja mwanzoni mwa Huduma Yake na nyingine mwishoni.

    Hii pia inaweza kuelezea kuanza na kukua kwa uadui kati ya viongozi wa kidini wa Yerusalemu. Huku kusafisha kunafanana na Mt. 21:12-16 na Luka 19:45-47.

D. Kulaani kwa mtini ni rejea dhahiri kwa Uyahudi. Inafanana na Mt. 21:18-19 na Luka 19:45-48.

E. Mtini ulionyauka (Marko 11:20-25) kunafanana na Mt. 21:19-22 na Luka 21:37-38.

F. Mamlaka ya Yesu yanahojiwa (Marko 11:27-12:12). Mamlaka yake ni jambo la msingi la kithiolojia! Inafanana katika Mt. 21:23-46 na Luka 20:1-19**.**

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 11: 1-10**
**1 Hata walipokaribia Yerusalemu karibu na Bethfage na Bethania, kukabili mlima wa Mizeituni, aliwatuma wawili katika wanafunzi wake, 2akawaambia, Nendeni mpaka kile kijiji kinachowakabili; na katika kuingia ndani yake, mara mtaona mwana-punda amefungwa, asiyepandwa na mtu bado; mfungueni, kamleteni. 3Na mtu akiwaambia, Mbona mnafanya hivi? Semeni, Bwana anamhitaji na mara atamrudisha tena hapa. 4 Wakaenda zao, wakamwona mwana-punda amefungwa penye mlango, nje katika njia kuu, wakamfungua. 5Baadhi ya watu waliosimama huko wakawaambia, Mnafanya nini kumfungua mwana-punda? 6Wakawaambia kama Yesu alivyowaagiza, nao wakawaruhusu. 7Wakamletea Yesu yule mwana-punda, wakatandika mavazi yao juu yake; akaketi juu yake. 8Watu wengi wakatandaza mavazi yao njiani, na wengine matawi waliyoyakata mashambani. 9Nao watu waliotangulia na wale waliofuata wakapaza sauti, Hosana; ndiye mbarikiwa ajaye kwa jina la Bwana;10 umebarikiwa na ufalme ujao, wa baba yetu Daudi. Hosana juu mbinguni.**

**11:1 "Bethfage"** Jina linamaanisha "nyumba ya mitini" au "mahali pa mitini ambayo haijaiva." Ilikuwa pembezoni ikitazamama na Yerusalemu paitwapo Mlima wa Mizeituni. Katika Fasihi za ualimu wa Kiyahudi ni sehemu ya Yerusalemu. Ilikuwa karibu na barabara kuu kutoka Yeriko, ambayo mahujaji walitumia.

◙**"Bethania"** Jina linamaanisha "nyumba ya tende." Yohana 11:18 inasema ni maili mbili kusini mashariki mwa Yerusalemu katika barabara kuelekea Yeriko na ilikuwa nyumbani mwa Maria, Martha na Lazaro. Wakati wa siku za karamu kuu tatu za kila mwaka (kama vile Law. 23) kila mtu kuzunguka Yerusalemu alijitoa kushirikiana na mahujaji katika nyumba zao. Yesu alikaa mahali hapa wakati alipokuwa katika Yerusalemu (kama vile Marko 11:11; Mt. 21:17).

◙**"Mlima wa Mizeituni"** Hivi vijiji vidogo viwili vilikuwa katika eneo moja la pembezoni (kama urefu wa maili 2.5 hivi) ambapo panajulikana kama "Mlima wa Mizeituni."

◙**"Akawatuma wanafunzi wake wawili"** Yawezekana Petro alikuwa mmoja wao na walikumbuka tukio hili juu ya Yohana Marko.

**11:2 "mara"** Angalia dokezo katika Marko 1:10.

◙**"mavazi"** Tukio hili ni utimilizwaji wa unabii (kama vile Mwa. 49:11; Zek. 9:9). Punda walikuwa usafiri uliozoeleka wa wafalme wa Kiyahudi (Hii pia inatajwa katika Mbao za Mari na simulizi za Gilgamesh za Ki-Sumeri).Mwanapunda huyu angetimiliza unabii wa kifalme (ni mfalme tu ambaye angepanda punda wake mwenyewe, mwanapunda huyu hakuwahi kuwa amepandwa kabla), lakini pia ingekuwa ni kuzungumza kuwa amekuja kwa amani. Wakati wa Kuja kwa Mara ya Pili Bwana atatokea juu ya Farasi Mweupe kama Mfalme wa Wafalme na Hakimu wa ulimwengu wote (kama vile Ufu. 19:11-16). Walimu wa Kiyahudi walitambua nabii hizi za Kimasihi na kusema kuwa alikuwa anastahili, hata kwa siku moja kwamba Masihi angekuja katika mawingu ya utukufu lakini ikiwa haitakuwa hivyo bado angekuja siku moja katika punda.

◙**"'hakuna mtu amempanda bado'"** Punda wa Kifalme hakupandwa na yoyote isipokuwa mfalme. Mfano wa ishara hii yenye nguvu inaonekana pale Suleimani alipopanda punda wa Daudi (kama vile 1 Wafalme 1:33).

**11:3 "iwapo"** Hii ni sentensi yenye masharti ya daraja la tatu ambayo inazungumzia tukio linalotegemewa.

◙**"'Bwana anamuhitaji'"** Mara nyingi ni ngumu kuamua katika hadithi za Injili ikiwa Yesu anatumia maarifa ya kinabii au yeye mwenyewe ameandaa kabla matukio (kama vile Marko 14:12-16).

Haya ni matumizi nadra ya Marko juu ya *kurios* kama cheo kinachotumiwa na Yesu (kama vile Marko 7:28; 11:3). Kwakuwa neno linaweza kumaanisha "bwana" au "mmiliki," inaweza kumaanisha mmilikiwa farasi. Hatahivyo, muktadha unamaanisha kuwa inarejerea kwa Yesu. Umuhimu wa kithiolojia ungekuwa hii ni njia ya Agano la Kale kurejerea kwa YHWH (kama vile Marko 11:9) kwa jina la *Adon*, ambayo inamaanisha "mmiliki," "bwana," "mkuu," au "mume" katika Waebrania.

◙**"na mara atamrudisha kwako"** Haijulikani ikiwa haya ni maoni ya wanafunzi juu ya punda au sehemu ya ujumbe wa Yesu. Kuna tofauti ya maandiko kadhaa kwasababu ya utata.

**11:5 "baadhi ya watu wasimamao njiani"** Ufanano katika Luka 19:33 una "wamiliki."

**11:7 "wakatandika mavazi yao"** Koti lilifanya kazi kama kusheni au Blanketi la kukalia wa kati wa kuendesha punda. Rangi zao  zinaweza zikawa zilionesha mwonekano wa kisherehe au gwaride (yaani gwaride la kifalme).

**11:8 "wengi walitandika mavazi yao njiani"** Hii "wengi" inawarejerea wakina nani? Ikiwa ni wanafunzi basi hii ni ishara ya Ufalme wa Yesu (kama vile 2 Wafalme 9:13). Ikiwa ni watu wa mjini wa Yerusalemu mtu anaweza kushangaa kwamba walifanya hivi kwasababu ya uharibifu uliosababishwa na punda kutembea juu ya nguo katika barabara ngumu. Yawezekana walikuwa wamesikia juu ya Yesu na walitambua upekee wake.

◙**"wengine wakatandika majani"** Yohana 12:13 anasema kwamba yalikuwa ni majani ya mnazi yaliyoota juu ya Mlima Mizeituni (kama vile Josephus). Inavyoonekana yalikuwa ishara ya ushindi au ushindi (kama vile Ufu. 7:9). Ibada hii ilifanyika kila mwaka na wakazi wa Yerusalemu katika karamu ya Hema na Pasaka kwa ajili ya kikundi cha Mahujaji waliokuwa wakiusogelea mji. Mwaka huu umuhimu wa Mfalme ajaye ulikuwa unatimilizwa. Ingawakitendo cha ishara hii mara kwa mara kilikuwa kinafanyika wakati wa Karamu ya Mahema (kama vile Law. 23:13-20), matawi hayo yalikuwa makubwa kuliko haya. Matawi yalitumika hapa yalikuwa madogo na yanalinganishwa na desturi ya kisasa ya kumwaga petali za waridi kabla mbele ya maharusi wanapokuwa wakitembea kutoka madhabahuni. Matendo haya matatu—(1)

makuti ya wanyama, (2) makoti yalitandazwa katika barabara, na (3) matawi yalitandazwa katika barabara—inaonesha kwamba walikuwa wakimweshimu Yesu kama Mfalme ajaye (kama vile Zaburi 2), Daudi (kama vile 2 Samueli 7) Masihi.

**11:9 "wale. . .wakipiga kelele"** Inavyoonekana Liturujia ya Marko 11:9-10 ilikuwa sehemu ya sherehe ya mwisho wa Mwaka. Walikuwa na maana ya msingi ya kizalendo (yaani hii inweza kuwa nahau ya Kiaramu kwa "nguvu ya kifalme kwa"). Hatahivyo, kwakuwa walikuwa wakirudia kila mwaka, Warumi hawakutishwa na wao. Mwaka huu kipekee walikuwa na utimilizwaji katika Yesu wa Nazareti. Kile ambacho kilikuwa Lituryjia sasa kikawa Ufunuo!

◙**"'Hosanna'"** Nahau ya Kiebrania ilimaanisha "mwalikeni" Ilikuwa ni sehemu ya Zaburi 118:25, ambayo ilinukuliwa kila mwaka wakati mahujaji walipokuja Yerusalemu. Kibayana ilimaanisha "okoa sasa" (kama vile 2 Sam. 14:4; 2 Wafalme. 6:16), lakini ilikuwa imekwisha kuwa salamu ya kawaida.

◙**"'Amebarikiwa Yeye ajaye kwa jina la bwana"** Hii ni nukuu kutoka Zab. 118:26. Hii ni moja ya Zaburi (113-118) ikinukuliwa wakati wa karamu ya Pasaka. Zaburi 118 ilikuwa na maana yenye nguvu ya kimasihi (kama vile Marko 11:22). Ufanano katika Luka 19:38 ina "Amebarikiwa mfalme ajaye kwa jina la Bwana." Hii ibada ya lituruji ya mwisho wa mwaka imefanyika kutimilizwa kwa unabii!

**11:10 "'ufalme ujao wa baba yetu Daudi'"** Hii ina maana ya kiuzalendo (kama vile 2 Samweli 7; Hos. 3:5). Mtu anaweza kushangaa ikiwa hii ilikuwa desturi ya kila mwaka au iliongezwa haswa kumrejerea Yesu. Hii inaweza kuwa rejea kwa Zek. 9:9. Mathayo 21:5 inataja unabii huu moja kwa moja. Ufanano katika Luka 19:39 unaonesha hasira kali ya Mafarisayo wakati tungo hizi moja kwa moja zilihusianishwa na Yesu.

◙**"'Hosanna aliye juu'"** Hii nahau inaweza kumaanisha (1) sifa kwa Mungu wa Mbinguni au (2) Mungu wa mbinguni amwokoe (yaani Yesu).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 11:11**
**11Naye akaingia Yerusalemu hata ndani ya hekalu; na alipokwisha kutazama yote pande zote, kwa kuwa ni wakati wa jioni, akatoka, akaenda Bethania pamoja na wale Thenashara.**

**11:11 "hekalu"** Neno hilo (*hieron*) ilimaanisha eneo lote zima la hekalu, sio tu eneo la ibada (Mtakatifu wa Watakatifu na Mahali Patakatifu.)

◙**"muda ulikuwa umeenda tayari"** Tayari walikuwa wamekwisha tembea maili 18 kutokea Yeriko. Eneo la hekalu yawezekana tayari lilikuwa linakaribia kuwa tupu. Yesu alitaka wote kuona tendo lake la kiishara la kusafisha na kurejeshwa kwa hekalu kwa kusudi lake la asili lililopewa na Mungu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 11: 12-14**
**12Hata asubuhi yake walipotoka Bethania aliona njaa. 13Akaona kwa mbali mtini wenye majani, akaenda ili labda aone kitu juu yake; na alipoufikilia hakuona kitu ila majani; maana si wakati wa tini. 14Akajibu, akauambia, Tangu leo hata milele mtu asile matunda kwako. Wanafunzi wake wakasikia.**

**11:12** Yesu alitumia mahitaji yaliyozoeleka (yaani chakula) kama fursa kufundisha somo kubwa la nguvu la hukumu na kukataliwa.

**11:13 "mti wa mtini"** Kumbuka jina la jiji la Bethphage lina maana "nyumba ya mitini." Kwa uwazi kulikuwa na miti mingi ya matunda ya miti hii katika eneo.

◙**"majani"** Kumekuwa na mjadala mkubwa kati ya Wafasiri kuhusu mtini huu na kwanini Yesu alijongea kwake.

1. ilikuwa sehemu ya iliyojifisha walikuwa na majani mengi mapema, hivyo yawezekana pia ilikuwa na mitini kidogo

2. majani huonyesha ahadi, lakini pasipo utimilizwaji kama vile Israeli walivyofanya
3. Yesu hakuwa anatafuta mitini, bali ishara "kitasa" ambazo pia wakati mwingine huliwa (kama vile F.E. Bruce, *Answers to Questions*, kama vile 56 au *Hard Sayings of the Bible*, kurasa 441-442). Nafikiri ilikuwa ni tendo la uwakilishi wa hukumu (kama vile Luka 13:6-9), kama kusafisha hekalu la dini ya Uyahudi lililokuwa na makao makuu yake Yerusalemu. Ilitabiriwa uharibifu mnamo mwaka wa 70 B.K na kamanda wa Kirumi (Mfalme wa baadaye) Titus na hukumu ya siku za mwisho kwasababu ya hali yao ya kutoamini katika Yesu (kama vile Mstari wa 14).

◙**"si wakati wa mtini"** Ilikuwa majira ya Pasaska na mara kwea mara hata si majani kamili yalikuwa bado hayajatokea. Tungo hii inaonesha asili ya tukio hili la kiishara. Tazama pia Yesu alivyozungumza kwa sauti kwa wanafunzi ili wasikie. Israeli mara kwa mara iliwakilishwa na miti ya miti ya mitini (hatahivyo, siku zote zabibu, kama vile Yer. 29:17;Hos. 9:10; Yoeli 1:7; Mik. 7:1-6). Ukweli kwamba mti ulikuwa na majani mengi yalioneshwa kwamba ilitakiwa iwe imesha zaa matunda. Israeli haikuwa hivyo! Hadithi hii ya mtini imegawanyika katika sehemu kuu mbili pamoja na kusafishwa kwa hekalu kuwekwa kati kuashiria kwamba inarejerea hukumu ya Mungu katika karne ya kwanza ya mfumo wa Kiyahudi wa kidini na viongozi wa dini (kama ilivyofanyika katika kusafisha hekalu). Haijulikani ikiwa Israeli wote au ni viongozi wasiotambuliwa kisheria (yaani Masadukayo waliokuwa wamenunua ofisi kutoka kwa Warumi) walikuwa pia wamehukumiwa. Hukumu hii juu ya Israeli inasisitriza katika Luka 13:6-9 na Marko 12:1-12.

**11:14** Hii ni Hukumu kali na ya kudumu!

## MADA MAALUMU: MILELE (*'olam*)

Maelezo ya asili ya neno la Kiebrania 'olam, עולם (BDB 761, KB 798) hayajulikani (NIDOTTE, juzuu. 3, uk. 345). Yametumika katika maana mbali mbali (mara nyingi yanapimwa na maudhui). Ifuatayo ni mifano iliyochaguliwa tu.

1. vitu vya kale
   a. watu, Mwa. 6:4; 1 Sam. 27:8; Yer. 5:15; 28:8
   b. mahari, Isa. 58:12; 61:4
   c. Mungu, Zab. 93:2; Mith. 8:23; Isa. 63:16
   d. Vitu, Mwa. 49:26; Ayubu 22:15; Zab. 24:7,9; Isa. 46:9
   e. mda, Kumb. 32:7; Isa. 51:9; 63:9,11
2. muda/ wakati ujao
   a. maisha ya mtu, Kut. 21:6; Kumb. 15:17; 1 Sam. 1:22; 27:12
   b. heshima ya hali ya juu kwa mfalme, 1 Fal. 1:31; Zab. 61:7; Neh. 2:3
   c. uwepo endelevu
      1) dunia, Zab. 78:69; 104:5; Mhu. 1:4
      2) mbinguni, Zab. 148:5
   d. uwepo wa Mungu
      1) Mwa. 21:33
      2) Kut. 15:18
      3) Kumb. 32:40
      4) Zab. 93:2
      5) Isa. 40:28
      6) Yer. 10:10
      7) Dan. 12:7
   e. Agano
      1) Mwa. 9:12,16; 17:7,13,19
      2) Kut. 31:16
      3) Ufu. 24:8

4) Hes. 18:19
5) 2 Sam. 23:5
6) Zab. 105:10
7) Isa. 24:5; 55:3; 61:8
8) Yer. 32:40; 50:5

f. Agano maalumu na Daudi
1) 2 Sam. 7:13,16,25,29; 22:51; 23:5
2) 1 Fal. 2:33,45; 9:5
3) 2 Nya. 13:5
4) Zab. 18:50; 89:4,28,36,37
5) Isa. 9:7; 55:3

g. Masihi wa Mungu
1) Zab. 45:2; 72:17; 89:35-36; 110:4
2) Isa. 9:6

h. Sheria za Mungu
1) Kut. 29:28; 30:21
2) Ufu. 6:18,22; 7:34; 10:15; 24:9
3) Hes. 18:8,11,19
4) Zab. 119:89,160

i. Ahadi za Mungu
1) 2 Sam. 7:13,16,25; 22:51
2) 1 Fal. 9:5
3) Zab. 18:50
4) Isa. 40:8

j. Uzao wa Abrahamu na nchi ya ahadi
1) Mwa. 13:15; 17:19; 48:4
2) Kut. 32:13
3) 1 Nya. 16:17

k. Sikukuu za ahadi
1) Kut. 12:14,17,24
2) Ufu. 23:14,21,41
3) Hes. 10:8

l. umilele, kudumu milele
1) 1 Fal. 8:13
2) Zab. 61:7-8; 77:8; 90:2; 103:17; 145:13
3) Isa. 26:4; 45:17
4) Dan. 9:24

m. Zaburi inasema yapi yanayowapasa kufanya milele
1) kushukuru, Zab. 30:12; 79:13
2) kudumu katika uwepo Wake, Zab. 41:12; 61:4,7
3) amini katika huruma zake, Zab. 52:8
4) kumsifu Bwana, Zab. 52:9
5) imba nyimbo za sifa, Zab. 61:8; 89:1
6) tangaza haki zake, Zab. 75:7-9
7) tukuza jina lake,Zab. 86:12; 145:2
8) baliki jina lake, Zab. 145:1

n. linatumiwa na Isaya kueleza enzi mpya
1) agano la milele, Isa. 24:5; 55:3; 61:8
2) YHWH kama mwamba wa milele, Isa. 26:4
3) furaha ya milele,Isa. 35:10; 51:11; 61:7

4) Mungu wa Milele, Isa. 40:28
5) Wokovu wa milele, Isa. 45:17
6) Wema wa milele, Isa. 54:8
7) Ishara ya milele, Isa. 55:13
8) Jina la milele, Isa. 56:5; 63:12,16
9) Nuru ya milele, Isa. 60:19,20

Matumizi yenye hali ya ukanushi kuhusiana na adhabu ya milele kwa waharifu inapatikana katika Isa. 33:14, "moto wa milele." Isaya kila wakati anatumia "moto" kuelezea hasira ya Mungu (kama vile. Isa. 9:18,19; 10:16; 47:14), lakini katika Isa. 33:14 “ndipo anasema wa milele”

3. Wakati wa kurudi nyuma na kwenda mbele ("toka milele hadi milele")
   a. Zab. 41:13 (sifa kwa Mungu)
   b. Zab. 90:2 (Mungu pekee)
   c. Zab. 103:17 (huruma zake)

Kumbuka,mktadha huamua maudhui ya maana ya neno. Maagano ya ahadi za milele ni ya masharti (yaani , Yeremia 7, tazama Mada Maalumu: Agano). Kuwa mwangalifu unaposoma maoni ya kisasa kuhusu muda au Agano Jipya la theolojia iliyopangwa katika matumizi ya kila siku ya neno hili dhaifu katika Agano la Kale. Kumbuka pia, Agano Jipya linajumuisha ahadi zote za Agano la kale (tazama Mada Maalumu: utabiri wa mambo yajayo ya Agano la Kale dhidi ya utabiri wa mambo yajayo ya Agano Jipya.).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 11:15-18**

**15 Wakafika Yerusalemu, naye akaingia ndani ya hekalu, akaanza kuwafukuza wale waliokuwa wakiuza na kununua ndani ya hekalu, akazipindua meza za wabadili fedha, na viti vyao wauzao njiwa; 16 wala hakuacha mtu achukue chombo kati ya hekalu. 17 Akafundisha, akasema, Je! Haikuandikwa, Nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala kwa mataifa yote? Bali ninyi mmeifanya kuwa pango la wanyang'anyi. 18 Wakuu wa makuhani na waandishi wakapata habari wakatafuta jinsi ya kumwangamiza; maana walimwogopa, kwa sababu mkutano wote walishangaa kwa mafundisho yake.**

**11:15 "akaingia ndani ya hekalu"** Hii inarejerea haswa kwa mahakama ya Mataifa ambapo wafanyabiashara walikuwa na meza zao (meza hizo zilikuwa zikimilikiwa na familia ya Kuhani Mkuu). Injili ya Yohana inaandika juu ya kusafisha kwa mapema (kama vile Yohana 2:13 na kuendelea). Yesu hakuwa mtu mwenye tabia ya upole kila mara kama tunavyofikiria! Tendo hili liliwapa changamoto mamlaka ya Mafarisayo kama kitendo cha mahujaji na maneno juu ya kuingia kwa shangwe. Matendo haya yalipelekea kifo cha Yesu (kama vile Marko 11:18).

◙**"akaanza kuwafukuza wale waliokuwa wakiuza"** Haya yanaweza kuwa maelezo ya Zek. 14:21,"Hakutakuwa tena na Mkanaani (yaani mfanyabiashara) katika nyumba ya Bwana wa Majeshi siku ile."

◙**"waliokuwa wakiuza na kununua"** Wafanya biashara hawa waliwakilisha familia ya Kuhani Mkuu ambaye alikuwa amenunua vyote ukuhani na haki za kutambuliwa katika Rumi (yaani angalau mnamu mwaka 30 B.K na kuendelea. Nafikiria Yesu alisulubiwa mnamo mwaka 34 B.K).

◙**"wabadili fedha "** Kodi ya hekalu ilikuwa ½ shekeli (kama vile Kutoka. 30:13). Katika siku za Yesu Shekeli ilikuwa shejeli ya Tiro. Mahujaji walitozwa 1/24 kama tozo ya kubadilisha fedha zao.

◙**"wale wauzao njiwa"** Njiwa alikuwa sadaka kwa ajili ya masikini, walemavu na wanawake. Gharama ya kawaida ilitolzwa mara tatu kulipia meza hizi. Hata wakati mahujaji walipoleta wanayama wao wenyewe kama dhabihu kutoka kwao, kuhani angetafuta sababu ya kumfanya mtoa sadaka aone hawafai na anunue mnyama mwingine.

**11:16 "wala hakuacha mtu achukue chombo kati ya hekalu"** Tungo hii ina upekee katika Marko. Mahakama ya Mataifa ilifanyika njia ya mkato kati ya mji na Mlima wa Mizeituni. Ilikuwa imepoteza kusudi lake la kipekee la kidini kama sehemu kwa ajili ya mataifa kumwendea YHWH.

**11:17 "'nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala kwa mataifa yote'"** Hii ni nukuu kutoka Isa. 56:7. Inaonesha upendo wa Mungu kwa watu wote. Mathayo akiwaandikia Wayahudi anaaccha sehemu ya mwisho ya tungo hii.

◙**"'pango la wanyang'anyi'"** Hii ni nukuu kutoka katika mahubiri mashuhuri na yaliyopendwa sana na Yeremia ambayo yalishughulikia ibada zisizo za imani (kama vile Yer. 7:11). Kwa kutumia jina la kidini, faida kubwa zilitengenezwa kwa kuharibu utulivu na maombi yaliyokuwa yakifanywa na mataifa. Neno "wanyang'anyi" linaweza kumaanisha "wafitinishaji."

**11:18 "Wakuu wa makuhani na waandishi"** Familia tajiri ziliendesha ofisi ya Kuhani Mkuu. Hii haikuwa tena nafasi iliyokuwa ikifanana na ya Haruni lakini Ofisi inayouzwa na Warumi kwa mtu mwenye kutoa fedha kubwa.

◙**"waandishi"** Hiki kipengele kilianza na Ezra. Katika siku za Yesu wengi wao walikuwa Mafarisayo. Walifasiri sehemuza kutendea kazi za sheria kwa ajili ya watu wa kawaida, haswa kutoka katika Desturi za Mdomo (yaani Buku la sheria za Kiyahudi). Kundi hili ni sawasawa katika utendaji na mwalimu wa kisasa wa Kiyahudi. Angalia Mada Maalum katika Marko 2:6.

◙**"wakaanza kutafuta namna ya kumwangamiza"** Hii ni njeo ya wakati usio timilifu. Inaweza kumaanisha "alianza" (kama vile toleo la NASB,TEV), lakini inaweza pia kumaanisha walitafuta tena na tena wakati huu kumuua Yesu (kama vile NRSV). Vitenzi vyote katika Marko 11:18 are sio timilifu, vikimaanisha matendo yalioanza na kuendelea katika wiki hii ya mwisho ya maisha ya Yesu. Taratibu zinazojirudia zinaanza kuinuka. Kuingia kwa shangwe na kusafishwa kwa Hekalu kuliweka muhuiri wa mwisho wa Yesu, kama alijua kwamba ingetokea.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 11:19**
**[19]Na kulipokuwa jioni alitoka mjini.**

**11:19** Mstari huu yawezekana unaenda na aya ya Marko 11:15-18. Haya ni maelezo mengine ya ushuhuda wa Petro. Tungo hii ndogo inaandikwa tofauti katika maandiko kadhaa ya Kiyunani (baadhi yana wingi na mengine yana umoja).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 11:20-26**
**[20] Na asubuhi walipokuwa wakipita, waliuona ule mtini umenyauka toka shinani. [21]Petro akakumbuka habari yake, akamwambia, Rabi, tazama, mtini ulioulaani umenyauka. [22]Yesu akajibu, akamwambia, Mwaminini Mungu. [23]Amin, nawaambia, Ye yote atakayeuambia mlima huu, Ng'oka ukatupwe baharini, wala asione shaka moyoni mwake, ila aamini kwamba hayo asemayo yametukia, yatakuwa yake. [24]Kwa sababu hiyo nawaambia, Yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu. [25]Nanyi, kila msimamapo na kusali, sameheni, mkiwa na neno juu ya mtu; ili na Baba yenu aliye mbinguni awasamehe na ninyi makosa yenu. [26]Lakini kama ninyi hamsamehe, wala Baba yenu aliye mbinguni hatawasamehe ninyi makosa yenu.]**

**11:20 "walipokuwa wakipita"** Walimchukua njia ile ile ya kutokea Bethania kuelekea Yerusalemu.

◙**"umenyauka toka shinani"** Hii ilikuwa ishara ya kukataliwa kabisa kwa Israeli (kama vile Marko 12:1-12), au viongozi wake wa wakati huu.

**11:21 "akakumbuka habari yake, akamwambia"** Petro ana kumbukumbu vizuri!

**11:22 "Yesu akajibu akawaambia"** Petro tena akawa kama msemaji wa kile ambacho wanafunzi wote walikuwa wakikifikiria.

◙**"'Mwaminini Mungu'"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Hii ni mada iliyozoeleka katika Injili. Imani/kuamini/tumaini (yaani nomino, *pistis;* kitenzi*, pisteuō*; Angalia Mada maalumu katika Marko 1:15) katika YHWH (na Masihi Wake) ni tumaini pekee la mwanadamu aliyeanguka. Mfumo huu wa sasa wa Ulimwengu na nguvu muundo wa nguvu zake lazima zivute umakini wetu na kujali kwetu. Mungu yu pamoja nasi na kwa ajili yetu. Mwangalie yeye, Yeye tu!

Hili tendo la Kiuwakilishi na kukataliwa kuliathiri mfumo wote wa jadi wa imani. Tunaweza tu kufikiria namna gani mafundisho mapya ya Yesu na mitazamo ilivyokuwa yenye kushikilia msimamo kwa Wayahudi hawa wa jadi wa karne ya kwanza! Yesu kwa nguvu na kidhahiri alikataa hekalu (kama ilivyokuwa likifanya kazi) na uongozi wa Masadukayo na Mafarisayo (wote waliberali, wa-Hillel, na wenye msimamo, Shammai). Kulikuwa na utofauti wa maandiko ya Kiyunani ambayo yanaongeza kiamb ata cha Kiyunani chenye masharti *ei* (yaani "ikiwa") katika MSS א na D. Hii ingetengeneza sentensi ya daraja la kwanza lenye masharti. Hatahivyo uwepo wake unaweza kuwa nahau ya kiebrania kuashiria nukuu ya moja kwa moja. It is not included inHaiitimishwi katika MSS A, B, C, L, au W, wala katika fasiri yoyote ya Kingereza iliyotumika katika hii fasiri. Yawezekana lilitokea kwa waandishi waliotaka kulifanya liwe sawa na Luka 17:6 au hata Mt. 21:21 (ambalo lina *ean* badala ya lile la Luka la *ei*).

**11:23 "hakika"** Hii kibayana ni "amina." Angalia Mada Maalumu katika Marko 3:28.

◙**"'mlima huu'"** Hii ilikuwa (1) yawezekana rejea dhahiri kwa Mlima wa Mizeituni (kama vile Zek. 14:4) au (2) mbinu ya kimafumbo kama katika Zek. 4:7. Tungo hii ilikuwa sitiari ya kawaida ya kiualimu wa kiyahudi kwa ajili ya kuondoa magumu.

Katika Agano la Kale, aina hii ya lugha ya "usawazishaji" mara kwa mara ilitumika kuelezea ujio wa YHWH (kama vile Mika 1:3-4;Hab.3:6). Angepatikana kwa nchi yote kwasababu milima ingesawazishwa (kama vile Zek. 14:4) na mabonde yangejazwa na mito na bahari kukaushwa ili wote waweze kumkaribia katika Yerusalemu. Asili ya lugha hii ya kisitiari inarudishiwa katika Agano Jipya na watu wenye uhitaji wanaokuja kwa Yesu, sio Yerusalemu. Katika Agano Jipya "Yerusalemu" katika Palestina inakuwa "Yerusalemu mpya," mji mtakatifu ushukao kutoka mbinguni. Agano Jipya limeweka nabii za Agano la Kale kiulimwengu kuhusiana na Yerusalemu Kijiografia na Palestina.

◙**"'ukatupwe baharini"** Hii yawezekana ni rejea kwa Bahari ya Chumvi, ambayo inaonekana kutokea Mlima wa Mizeituni.

◙**"'asione shaka'"** Imani ni ufunguo wa kimsingi wa maombi (kama vile Yakobo 1:6-8).

◙**"moyoni"** Angalia Mada Maalumu katika Marko 2:6.

**11:23-24 "yatakuwa yenu"** Kauli hii lazima ifanyiwe uwiano na kauli zingine za kibiblia. Huu ni mfano mzuri wa kwanini hatutakiwi kuhakiki mstari mmoja na kusema "Biblia inasema, na hivyo ndivyo ilivyo." Biblia inazungumza zaidi sana juu ya maombi. Jambo baya kabisa Mungu angefanya kwa Wakristo wengi ni kujibu maombi yao! Mara nyingi tunaomba kwa vitu vyote visivyo sahihi. Tafadhali soma na utafakari Mada Maalum hapa chini "Maombi ya kumaanisha."

## MADA MAALUMU: MAOMBI YA KUSIHI

A. Kuhusiana na uhusiano wa mtu binafsi na nafsi za Mungu mmoja
   1. Inahusika kwenye mapenzi ya Baba
      a. Mathayo 6:10

b. 1 Yohana 3:22
c. 1 Yohana 5:14-15
2. Kukaa ndani ya Yesu Yohana 15:7
3. Kuomba kwa jina la Yesu
a. Yohana 14:13,14
b. Yohana 15:16
c. Yohana 16:23-24
4. Kuomba katika roho
a. Waefeso 6:18
b. Yuda 1:20
B. Inahusika na nia ya mtu binafsi
1. Kutokuyumba yumba
a. Yohana 21:22
b. Yakobo 1:6-7
2. Kuomba vibaya Yakobo 4:3
3. Kuomba kwa tama Yakobo 4:2-3
C. Inahusika na uchaguzi wa mtu binafsi
1. Ustahimilivu
a. Luka 18:1-8
b. Wakolosai 4:2
c. Yakobo
2. Ugomvi nyumbani 1 Petro 3:7
3. Dhambi
a. Zaburi 66:18
b. Isaya 59:1-2
c. Isaya 64:7

Maombi yote hujibiwa, lakini si maombi yote yanazaa matunda. Maombi ni uhusiano wa pande mbili. Jambo baya kuliko yote ambalo Mungu angalifanya ni kujibu maombi ya waaminio ambayo si sahihi.

**11:24 "'kwamba mmekwisha kuyapokea'"** Kuna aina ya maandiko yanayohusiana na njeo ya kitenzi *lambanō*. Wakati uliopita usio timilifu ambao unaaksi nahau ya Kiebrania juu ya utimilizwaji utarajiwao, unapatikana katika MSS ,א, B, C, L, na W. Inavyoonekana hii ilirekebishwa na waandishi (1) kwa njeo ya wakati ujao kushabihiana na Mt. 21:22 (kama vile MS D na Vulgate) au (2) kwa njeo ya wakati uliopo (kama vile MS A na fasiri ya ki-Armeni).

**11:25 "'msimamapo kuomba"** Mkao wa kawaida wa maombi ilikuwa ni kusimama wakati macho yakiwa yamefunguliwa na kichwa na mikono ikiwa imeinuliwa juu. Waliomba kana kwamba wako katika mazungumzo na Mungu.

◙**"'samehe, ikiwa watu wamewakosea'"** Msamaha wetu kwa wengine ni ushahidi, sio msingi wa sisi kusamehewa (kama vile Mt. 5:7; 6:14-15; 7:1-2; 18:21-35; Luka 6:36-37; Efe. 4:32; Kol. 3:13;Yakobo 2:13; 5:9). Mtu asiyesamehe hamjui Mungu!

◙**"ikiwa"** Hii ni sentensi ya daraja la kwanza lenye masharti. Waamini mara kwa mara huwa wanakaa na uchungu. Kumjua Mungu kupitia Kristo lazima kubadili mitazamo hii. Tunasamehewa sana, tunawezaje kuwatendea wengine walioumbwa kwa sura ya Mungu kwa uadui na chuki na tukiwa katika hali ya kuridhika tu?

◙**"'Baba yenu aliye mbinguni'"** Yesu alizungumza Kiaramu, ikimaanisha kwamba maeneo mengi ambayo "Baba" inatokea kama Kiyunani, *Pater,* inaweza kuaksi kiaramu *Abba* (kama vile Marko 14:36). Hili ni neno linalojulikana "Baba" au "Papa" linaloaksi ukaribu wa Yesu na Baba; Kufunua kwake hili kwa wafuasi Wake pia kunatutia moyo juu ya ukaribu

wetu wenyewe na Baba. Neno "Baba" lilikuwa likitumika katika Agano la Kale tu kwa ajili ya YHWH, lakini Yesu analitumia mara kwa mara na kuendelea. Ni ufunuo mkuu ya uhusiano wetu mpya na Mungu kupitia Kristo.

**11:26** Mstari huu haupo katika maandiko ya Kiyunani, א, B, L, na W. Unajumuishwa pamoja na aina kadhaa katika MSS A, D, K, X, na fasiri ya Peshitta na Diatessaron (yaani Injili nne zinazounganishwa kuwa moja). Inaonekana kwamba waandishi wa kale waliongeza tungo hii kutoka Mt. 6:15.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 11:27-33**
**27 Wakafika Yerusalemu tena; hata alipokuwa akitembea hekaluni, walimwendea wakuu wa makuhani, na waandishi, na wazee, 28 wakamwambia, Ni kwa mamlaka gani unatenda mambo haya? Naye ni nani aliyekupa mamlaka hii uyatende haya? 29 Yesu akawaambia, Nitawauliza neno moja, nanyi mnijibu, kisha nitawaambia ni kwa mamlaka gani nayatenda haya. 30 Ubatizo wa Yohana ulitoka mbinguni, au kwa wanadamu? Nijibuni. 31 Wakasemezana wao kwa wao, wakisema, Kama tukisema, Ulitoka mbinguni, atasema, Mbona, basi, hamkumwamini? 32 Ila tukisema, Ulitoka kwa wanadamu, -- waliogopa watu; maana watu wote walimwona Yohana kuwa nabii halisi. 33 Wakamjibu Yesu, wakasema, Hatujui. Yesu akawaambia, Wala mimi siwaambii ninyi ni kwa mamlaka gani nayatenda haya.**

**11:27 "Wakafika Yerusalemu"** Hii inaonekana kumaaanisha waliondoka Yerusalemu na kulala Bethania yawezekana pamoja na Lazaro, Maria na Martha.

◙**"akitembea hekaluni"** Unaweza kufikiria ni kwa namna gani wafanya biashara walikuwa wakimtazama! Yesu hakujificha au kuepuka makabiliano. Huu ulikuwa ni wakati Wake wa kuacha athari Yerusalemu.

◙**"wakuu wa makuhani, na waandishi, na wazee "** Haya ni maelezo kamili kwa ajili ya wakuu wa masinagogi. Hiki kilikuwa chombo rasmi cha wajumbe sabini katika Yerusalemu ambao walikuzwa kutoka katika Hekalu Kuu la enzi za Ezra. Lilijumuisha Kuhani Mkuu na familia, waandishi wa eneo moja na wazee wenye heshima na wenye mali nyingi. Angalia mada Maalum katika Marko 12:13.

**11:28 "'Ni kwa mamlaka gani unatenda mambo haya? '"** Hili limekuwa na ni swali muhimu juu ya Yesu. Alipata wapi mamlaka yake na nguvu ya kuzungumza na kutenda? Yesu hakuwa na sifa walizokuwa nazo kichwani juu ya Masihi wa YHWH ambavyo angetenda na kusema!

**11:29** Yesu mara kwa mara alitumia mbinu ya swali la pili wakati alipokuwa akikabiliana na wale waliojaribu kumtega na kumkamata (kama vile Marko 2:6-9,19,25-26; 3:23-24; 10:3,37-39; 12:14-16). Alikuwa muwazi kwao ikiwa walikuwa wazi kwake (kama vile Marko 11:33).

**11:30 "'Je ubatizo wa Yohana ulitoka mbinguni'"** Yesu alijibu swali lililohusiana na kumkataa Yohana Mbatizaji. Hawakuwa wakitafuta ukweli halisi (kama vile Marko 11:31-33). Walikuwa wakijalki hadhi zao na kushikilia madaraka (kama vile Marko 11:32).

**11:31 "ikiwa"** Hii ni sentensi ya daraja la tatu lenye masharti.

**11:33** Yesu anawajibu kwa mfano katika Marko 12:1-12, ni moja ya tuhuma kali ya Israeli na viongozi wake katika Agano Jipya lote.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Sura hii inafunua nini juu ya Yesu?
2. Kwanini Yesu alikubali jina la "Mwana wa Daudi?"
3. Je ni kwa namna gani Imani inahusiana na uponyaji?
4. Kwanini kuingia kwa Sherehe kulikuwa muhimu sana?
5. Je kelele na kupaza sauti kwa makutano kulimaanisha nini?
6. Kwanini Yesu aliulaani mtini?
7. Kwanini Yesu aliwafukuza na kuwatoa nje wafanyabiashara? Je ilikuwa mara ya kwanza?
8. Kwanini askari wa Hekalu hawakumkataza?
9. Je twaweza muomb a Mungu chochote? Je imani yetu inahusiana vipi na maombi kujibiwa?
10. Kwanini Marko 11:28 ni swali muhimu sana?

# MARKO 12

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| mfano wa shamba la mizabibu na watumwa | Mfano wa kikombe cha mvinyo ya uovu | Mfano wa shamba la mizabibu | Mfano wa watumwa katika shamba la mizabibu | Mfano wa watumwa waovu |
| 12:13-17 | 12:13-17 | 12:13-17 | 12:13-14<br>12:15<br>12:16a<br>12:16b<br>12:17a<br>12:17b | 12:13-17 |
| Swali kuhusu ufufuo | Masadukayo: unasemaje kuhusu ufufuo | Swali kuhusu ufufuo | Swali kuhusu kufufuliwa toka katika wafu | Ufufuo wa wafu |
| 12:18-27 | 12:18-27 | 12:18-23<br>12:24-27 | 12:18-23<br>12:24-27 | 12:18-23<br>12:24-27 |
| Amri iliyo kuu | Waandishi: ni ipi iliyo Amri kuu ya zote | Amri iliyo kuu | Amri iliyo kuu | Amri iliyo kuu kati ya zote |
| 12:28-34 | 12:28-34 | 12:28-34 | 12:28<br>12:29-31<br>12:32-33<br>12:34 | 12:28-34 |
| Swali kuhusu Mwana wa Daudi | Yesu: husemaje Daudi kumwita mwanae Bwana | Mwana wa Daudi | Swali kumhusu Masihi | Yesu sio tu ni mwana bali pia ni Bwana wa Daudi |
| 12:35-37 | 12:35-37 | 12:35-37 | 12:35-37a | 12:35-37 |
| Shutuma za Wandishi | Iweni makini na wandishi | Akisema juu ya kiburi na unyenyekevu | Yesu aonya juu ya walimu wa sheria | wandishi walaumiwa na Yesu |
| 12:38-40 | 12:38-40 | 12:38-40 | 12:37b-40 | 12:38-40 |
| Sadaka ya mjane | Senti mbili za mjane | Sadaka ya mjane | Sadaka ya mjane | Senti mbili ya mjane |
| 12:41-44 | 12:41-44 | 12:41-44 | 12:41-44 | 12:41-44 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka "Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza

2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## UFANANO WA VIDOKEZO VYA INJILI

A. Wawakilishi wa baraza la wakuu wa Sinagogi wakauliza maswali (kama vile Marko 11:27-12:12) na Yesu akajibu kwa mifano (Marko 12:1-12). Huu unafanana na ule ulioko Mt. 21:33-46 na Luka 20:1-19.

B. Mafarisayo na Maherodi wakauliza kuhusu kulipa kodi kwa Kaisari (Marko 12:13-17), ambapo kunafanana na kule kulioko Mt. 22:15-22 na Luka 20:20-26.

C. Masadukayo wakauliza swali kuhusu ufufuko (Marko 12:18-27), ambapo kunafanana na kule kulioko katika Mt.22:23-33 na Luka 20:27-40.

D. Mwandishi akauliza swali kuhusu amri iliyo kuu kupita zote (Marko 12:28-34), wenye kufanana na ule wa Mt.22:34-40.

E. Yesu akawauliza swali viongozi wa Kiyahudi kuhusu uhusiano wa Kimasihi na uzao wa Daudi (Marko 12:35-37), wenye kufanana na ule wa Mt. 22:41-46 na Luka 20:41-44.

F. Yesu akawakana haradhani waandishi (Marko 12:38-40) na unafanana na ule wa Mt. 23:1-39 na Luka 20:45-47.

G. Matoleo ya sadaka ya Yule mjane (Marko 12:41-44) unafanana na ule wa Luka 21:1-4.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 12:1-11**
**[1] Akaanza kusema nao kwa mifano; Mtu mmoja alipanda shamba la mizabibu, akazungusha ugo, akachimba shimo
la shinikizo, akajenga mnara, akapangisha wakulima, akasafiri. [2] Hata kwa wakati wake akatuma mtumwa kwa
wale wakulima, ili apokee kwa wakulima katika matunda ya mizabibu. [3] Wakamtwaa, wakampiga, wakamtoa nje,
hana kitu. [4] Akatuma tena kwao mtumwa mwingine, na huyo wakamtia jeraha za kichwa, wakamfanyia jeuri. [5]
Akamtuma mwingine, huyo wakamwua; na wengine wengi, hawa wakiwapiga na hawa wakiwaua. [6] Basi alikuwa
na mmoja bado, mwana mpendwa wake; huyu naye akamtuma kwao mwisho, akisema, Watamstahi mwanangu. [7]
Lakini wale wakulima wakasemezana, Huyu ni mrithi; haya, na tumwue, na urithi utakuwa wetu. [8] Wakamkamata,
wakamwua, wakamtupa nje ya shamba la mizabibu. [9] basi atafanyaje yule bwana wa shamba la mizabibu? Atakuja
na kuwaangamiza wale wakulima, na lile shamba la mizabibu atawapa wengine. [10] Hata andiko hili hamjalisoma,
Jiwe walilolikataa waashi, Hilo limekuwa jiwe kuu la pembeni. [11] Neno hili limetoka kwa Bwana, Nalo ni ajabu
machoni petu? [12] Nao wakatafuta kumkamata, wakaogopa mkutano; maana walitambua ya kwamba ule mfano
amewanenea wao. Wakamwacha wakaenda zao.**

**12:1 "Akaanza kusema nao kwa mifano"** Neno "nao" linarejelea moja kwa moja kwa wawakilishi wa baraza kuu la Sinagogi (kama vile Marko 11:27), lakini usio wa moja kwa moja kwenye umati mkubwa wa watu.
Sura hii nzima ni mlolongo wa maswali toka kwa viongozi wa dini:
1. Toka kwa wakuu wa Sinagogi (Marko 11:27-12:12)
2. Toka kwa Mafarisayo na Maherode (Marko 12:13-17)
3. Toka kwa Masadukayo (Marko 12:18-27)
4. Toka kwa waandishi (Marko 12:28-34)
5. Toka kwa Yesu (Marko 11:29-33; 12:9,35-37)

◙ **"'Mtu mmoja alipanda shamba la mizabibu, akazungusha ugo, akachimba shimo la shinikizo'"** Hili ni rejeo toka kwa tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania ya Isa. 5:1-2. Matunda ya mizabibu yalikuwa ni moja ya alama za taifa la Israeli (kama ulivyokuwa mti wa mtini katika Marko 11:12-14,20-25). Isaya 5 anatumia wimbo wa jadi kuhusu mizabibu kuielezea Israeli. Mathayo anajumuisha mifano mingine mbalimbali ambayo pia inayolielezea taifa la Israeli (kama vile Mt. 22:1-14). Ni vigumu kufanya maamuzi ikiwa Mungu aliikataa

1. Kuiharalisha Israeli, viongozi wasio uzao wa Haruni
2. Kujihesabia haki, kushikilia mno sheria za kimaamuzi
3. Kutokuamini kwao kwa taifa zima. Israeli, pamoja na fursa zote za kimaagano (kama vile Rum. 9:4-5), pia ilikuwa ikitegemewa na uwajibikaji wa agano la Musa (kama vile Kumbukumbu la Torati 27-28). inavutia kuona namna tofauti ya utaratibu wa Isaya 5 unavyouelezea upendo wa Mungu wa bure kwa wote watakao mwelekea ukilinganishwa na ukali na vurugu za hawa wapagazi wa kwenye mashamba katika mfano huu.

**12:2 "'kipindi cha mavuno'"** Mara nyingi ilichukua yapata miaka mitano kwa mizabibu kuanza kuzaa kwenye kiwango cha kibiashara. Mmiliki aliweka matarajio kwenye uwekezaji wake.

**12:2,4,5,6 "'akamtuma'"** Mungu alijaribu kuwasiliana kwa kuwatuma wawakilishi mbalimbali, hata mwanae pekee. Hili liliwakilisha maumivu ya Mungu na shauku yake ili kuimalisha ushirika wa kimaagano.

**12:2,4,5 "'mtumwa'"** Hawa watumwa wanawakilisha manabii wa Agano la Kale. Mathayo, kama ilivyo tabia yake, alikuwa na watumwa wawili (kama vile Mt. 21:34). Hili andiko kwa uwazi linaonyesha namna Mathayo alivyounganisha habari za Marko za watumwa mbalimbali kutokea mara moja.

**12:3 "'wakampiga'"** Hili linarejelea kipigo kikali. Kwa maana iliyo wazi inamaanisha "kukonda" (kama vile Marko 13:9).

**12:4 "'wakamtia jeraha za kichwa'"** Hili linarejelea kupigwa juu ya kichwa mara kadhaa. Inaonyesha matusi walioyapata wale waliomwakilisha Mungu na kunena kwa ajili yake (yaani., manabii wa Agano la Kale) kwa watu wake wa agano walioasi.

◙ **"'na wakamfanyia jeuri'"** Huu ni mwonekano wa usimuliaji wa jina Timotheo, lenye kumaanisha, "heshima" au "thamani" likiwa na kiambishi awali hasi. Linadokeza "kumfanya mtu kwa hila" au "kuonyesha utovu wa heshima" (kama vile Yakobo 2:6).

**12:5** Kwa nini Mungu alituma mtumishi mmoja baada ya mwingine? Mungu alimuumba mwanadamu kwa kusudi la—kuwa na ushirika na Yeye. Alitaka kuimalisha watu wawe kama Yeye, lakini hawataweza. Bado, Mungu anajaribu tena na tena kutufikia! Yeye ana "upendo usio na mwisho" kwa ajili ya uumbaji wake

**12:6 "' alikuwa na mmoja bado, mwana mpendwa wake'"** Dhahiri hili linarejelea kwa Yesu. Kifungu kile kile kinatumiwa na Baba kwenye ubatizo wa Yesu (Mt. 1:11; 3:17) na kipindi anabadilika sura (9:7; Mt. 17:5). Ukweli ule ule unaonekana kwenye Yohana 3:16 na Ebr. 1:1-2. Ni muunganiko wa wimbo wa Kifalme (yaani., 2:7) na kifungu cha Mtumishi Ateswaye (yaani., Isa. 42:1).

**12:7 "'na urithi utakuwa wetu'"** Hili kisheria linarejelea kwenye sheria za Kiyahudi za "kutokumiliki mali" inayoweza kudaiwa na mmiliki halali. Inaaksi tabia ya mwanadamu aliyeanguka ya "kujimilikisha vingi kwa gharama yeyote ile." Mwanadamu anataka kuwa kama Mungu (kama vile Mwanzo 3).

**12:8 "'wakamtupa nje ya shamba la mizabibu'"** Maziko yasiyofaa yanaonyesha moja kwa moja wapagazi kutokumuheshimu mmiliki na mwanae! Ufanano wa injili unaelezea utaratibu wa kumtupa mwana nje ya shamba na kumuuwa (kama vile Mt. 21:39; Luka 19:15). Hili yumkini lilikuwa ni kutambulisha zaidi kifo cha Yesu nje ya ukuta wa Yerusalemu.

**12:9** Huu mstari unaonyesha uwajibikaji wa Mungu dhidi ya wale waliomuuwa Mwana Wake. Katika injili ya Marko Yesu akawauliza mkutano swali. Hili linaaksi Isa. 5:3-4, ambapo manabii waliuliza swali. Wasikilizaji wanalaumiwa kutokana na midomo yao (yaani., Mt. 21:41). Mungu ataukumbatia uumbaji wote wenye utambuzi uwajibike kwenye zawadi ya uhai. Tutavuna kile tulichopanda (kama vile Marko 4:21-25; Mt. 13:12; 25:14-30; Gal. 6:7).

◙ **"shamba la mizabibu atawapa wengine**" Neno "wengine" linaonekana kulirejelea kanisa, lenye waamini wa Kiyahudi na watu wa mataifa (kama vile Efe. 2:11-3:13).

**12:10 "'Hata andiko hili hamjalisoma'"** Huu ni utangulizi wa Yesu ambao ulitumika kila mwaka kwenye makaribisho yao ya kimaonyesho ya kuwakaribisha mahojaji ndani ya Yerusalemu (yaani., Zab. 118:22-23). Swali hili ni dhana yenye kujirudia katika Agano Jipya (kama vile Mt.21:42; Luka 20:17; Mdo. 4:11; Rum. 9:32-33; 1 Pet. 2:7). Linaelezea tatizo namna jinsi Israeli itakavyomkosa Masihi (kama vile Rum. 9-11). Haya maelezo yalikuwa ni kofi la uso kwa Yule anayedai kuyajua maandiko!

◙ **"jiwe"** Hii ni rejea ya Zab. 118:22-23 kutoka kwenye tafsiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania. Katika maandiko ya sheria za Kiyahudi, haya mawe yanarejelea kwa Ibrahimu, Daudi, au Masihi (kama vile Dan. 2:34-35). Wimbo wa aina ile ile ulifanya rejeo kama sehemu ya wimbo wa Halleluyah, ulitumika kuwakaribisha mahojaji ndani ya Yerusalemu kwa ajili ya Pasaka.

◙ **"waashi"** Katika maandiko ya dini ya Kiyahudi neno hili lilirejelea waandishi. Hoja alizoziongeza Yesu zimeandikwa katika Mt. 21:43-44. Tambua hapa waashi wanalaumiwa kwa ajili ya kukosa ukweli muhimu: Yesu ni Masihi aliyeahidiwa.

◙ **"'jiwe kuu la pembeni'"** Stiari ya Masihi kama jiwe inatoka kwenye utumiaji mbalimbali wa Agano la Kake.
1. Nguvu na uimara wa YHWH (kama vile Zab. 18:1-2)
2. Maono ya Daniel katika sura ya 2 (kama vile Dan. 2:34-35,48)
3. Sehemu ya jengo ambayo
   a. hulianza jengo (yaani., jiwe kuu la pembeni)
   b. kushikilia uzito wa nyumba (yaani., jiwe kuu la katikati ya tao)
   c. jengo lililoisha (yaani., jiwe la juu ya msingi)

Jengo kiistiari linarejea kwa watu wa Mungu, hekalu halisi (kama vile 1 Kor. 3:16-17; 2 Kor. 6:16; Efe. 2:19-22).

## MADA MAALUM: JIWE KUU LA PEMBENI

I. Matumizi ya Agano la Kale
   A. Dhana ya jiwe kama kitu kigumu mkinachodumu ambacho kilitumika kutengeneza msingi kilitumika kuelezea YHWH (kama vile Ayubu 38:6; Zaburi 18:2 inatumia maneno mawili ya "mwamba," BDB 700, 849).
   B. Alafu baadae lilikuzwa kuwa cheo cha Kimasihi (kama vile Mwanzo 49:24; Mwanzo 118:22; Isaya 28:16).
   C. Neno "jiwe" au "mwamba" lilikuja kuwakilisha hukumu kutoka kwa YHWH Masihi (kama vile Isaya 8:16 [BDB 6 KUTENGENEZA BDB 103]; Danieli 2:34-35,44-45 [BDB 1078]).
   D. Hii ilikuzwa mpaka kuwa sitiari ya kiujenzi (hasa Isaya 28:16).
      1. linalowekwa la kwanza, ambalo lililuwa linahakikisha usalama na kuweka vipimo vya jengo lote linalosalia liliitwa" jiwe kuu la pembeni"
      2. Ingeweza pia kumaanisha jiwe la mwisho linalowekwa sehemu yake likishikilia kuta pamoja (kama vile Zekaria 4:7; Efe. 2:20, 21), liliitwa "jiwe kifuniko," kutoka katika Kiebrania *rosh* (yaani kichwa)
      3. Linaweza kumaanisha "jiwe la msingi," ambalo linakuwa katikati ya njia ya kuingilia na kushikilia uzito wa jengo la kuta nzima.

II. Matumizi ya Agano Jipya
   A. Yesu alinukuu Zaburi 118 mara kadhaa katika kujizungumzia mwenyewe (kama vile Mt. 21:41-46; Marko

12:10-11; Luka 20:17)

B. Paulo alitumia Zaburi 118 akiunganisha kukataliwa kwa YHWH na Waisraeli wasioamini na wenye kuasi (kama vile Rum. 9:33)

C. Paulo anatumia dhana ya "jiwe kuu la pembeni" katika Efe. 2:20-22 kama urejereo kwa Kristo

D. Petro anatumia dhana hii ya Yesu 1 Petro 2:1-10. Yesu ni jiwe kuu la pembeni na waamini ni mawe yaliyo hai (yaani waamini kama mahekalu, kama vile 1 Kor. 6:19), yakijengwa juu yake (yaani Yesu ni Hekelu jipya, kama vile Marko 14:58; Mt. 12:6; Yohana 2:19-20). Wayahudi walikataa msingi wa tumaini lao pale walipomkataa Yesu kama Masihi.

III. Kauli za Kithiolojia

A. YHWH alimruhusu Daudi/ Sulemani alijenge hekalu. Aliwaambia kwamba iwapo wangelitunza agano angeliwabariki na kuwa pamoja nao (kama vile 2 Samueli 7), lakini ikiwa wasingelishika agano, hekalu lingeliharibiwa (kama vile 1 Wafalme 9:1-9)!

B. Walimu wa kiyahudi waliweka mkazo katik muundo na ibada na kuachana na kipengele cha imani binafsi (kama vile Yeremia 31:31-34; Ezekieli 36:22-38). Mungu anatafuta uhusiano wa kila siku, wa binafsi na wa kiungu pamoja na wale walioumbwa kwa sura na mfano wake (kama vile Mwanzo 1:26-27). Luka 20:17-18 inajumuisha maneno ya kutisha ya hukumu kama ilivyo kwa Mathayo 5:20, kuelekezwa kwa uyahudi.

C. Yesu alitumia dhana ya hekalu kuwakilisha mwili wake mwenyewe (kama vile Yohana 2:19-22). Hii inaendelea na kupanuka kwa dhana ya imani binafsi katika Yesu kama masihi ni msingi wa mahusiano pamoja na YHWH (yaani Yohana 14:6; 1 Yohana 5:10-12).

D. Wokovu umemaanishwa kurejesha sura ya Mungu iliyoharibika katika wanadamu (Mwanzo 1:26-27 na Mwanzo 3) ili kwamba ushirika pamoja na Mungu uwezekane. Lengo la Ukristo ni kufanana na Kristo kwa sasa. Waamini wanatakiwa kuwa mawe yaliyohai (mahekalu madogo yaliyojengwa/kwa mfano wa Kristo).

E. Yesu ni msingi wa Imani yetu na jiwe letu la imani (yaani the Alfa na Omega). Bado, pia jiwe la kujikwaa na mwamba wa hatia (Isaya 28:16). Kumkosa Yeye ni kukosa kila kitu. Kunaweza kusiwe na ardhi nyingine ya kati hapa!

**12:11** Mstari huu unadokeza kuwa kila kitu kilichotokea kipindi cha kukataliwa na kifo cha Yesu kilikwisha kujulikana na kutabiriwa (kama vile Isa. 53:10; Luka 22:22; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 1 Pet. 1:20).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 12:12**
**12 Nao wakatafuta kumkamata, wakaogopa mkutano; maana walitambua ya kwamba ule mfano amewanenea wao. Wakamwacha wakaenda zao.**

**12:12 "wakatafuta kumkamata"** Viongozi wa Kiyahudi wakatambua kuwa mifano ilikuwa ikiwanena wao na wakatenda kwa namna ile ya utabiri (yaani., wakajaribu kumuuwa).

◙ **"wakaogopa mkutano"** Viongozi hawa walitizama kwenye hoja za wakati huo (kama vile Marko 11:18,32; Mt. 21:26,46; Luka 19:48) kuliko kuliangalia neno la Mungu ili kuyapima matendo yao.

◙ **"wakatambua kuwa ule mfano unawanenea wao"** Hiki kiwakilishi nomino "wao" chaweza kueleweka katika maana moja au mbili: (1) viongozi waliogopa kufaahamika sana kwa Yesu kwenye mkutano (kama vile Mt. 21:45) au (2) mkutano nao ukatambua mfano ulikuwa ukiwazungumzia viongozi wa dini.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 12:13-17**
**13 Wakatuma kwake baadhi ya Mafarisayo na Maherodi, ili wamnase kwa maneno. 14 Hata walipofika walimwambia, Mwalimu, twajua ya kuwa wewe u mtu wa kweli, wala hujali cheo cha mtu; kwa maana hutazami sura za watu; lakini katika kweli waifundisha njia ya Mungu. Je! Ni halali kumpa Kaisari kodi au siyo? 15 Tumpe, tusimpe? Naye, akijua unafiki wao, akawaambia, Mbona mmenijaribu? Nileteeni dinari niione. 16 Wakaileta. Akawaambia, Ni ya nani sanamu hii na anwani hii? Wakamwambia, Ni ya Kaisari. 17 Yesu akajibu, akawaambia,**

**Mpeni Kaisari yaliyo ya Kaisari, na yaliyo ya Mungu mpeni Mungu. Wakamstaajabia sana.**

**12:13 "wakatuma"** Hili linawarejelea wakuu wa Sinagogi, ambao walikuwa wenye mamlaka ya dini ya Kiyahudi (kama vile Marko 11:27).

## MADA MAALUM: BARAZA KUU LA WAZEE WA SINAGOGI

I. chanzo cha habari

A. Agano Jipya lenyewe

B. Flavian Yusufu wa mambo ya kale ya Kiyahudi

C. Sehemu ya Mishna juu ya sheria za kiibada za Kiyahudi (yaani., eneo la watu wa Sinagogi kuu).

Bahati mbaya Agano Jipya na Yusufu hawakubaliani na maandiko ya sheria za Kiyahudi, ambazo zinaonekana kuwathibitisha watu wawili wa Sinagogi kuu katika Yerusalemu, kuhani mmoja (yaani., Msadukayo), akidhibitiwa na kuhani mkuu na akishughulika na haki za jamii na uhalifu na wa pili ikidhibitiwa na mafarisayo na waandishi, waliohusiana na mambo ya kidini na kitamaduni. Hata hivyo, tarehe za maandiko ya sheria za Kiyahudi toka mwaka 200 B.K na kuangazia hali ya kitamaduni baada ya Yerusalemu kuangukia mikononi mwa kamanda Tito wa Rumi, mwaka wa 70 B.K. wayahudi (yaani., uongozi wa kifarisayo) waliimarisha tena makao makuu yao kwa minajili ya maisha ya kidini katika mji uitwao Jamnia na baadaye (yaani., mwaka wa 118 B.K) wakaondoka kwenda Galilaya.

II. Istilahi

Tatizo la kumtambua mtu wa kimahakama unahusisha majina tofauti yanayojulikana. Kuna maneno mengi yaliyotumika kuelezea watu wa kimahakama ndani ya jamii ya Kiyahudi ya Yerusalemu.

A. *Gerousia*-" seneti" au "baraza." Hili ni neno la zamani lililotumika kwenye kipindi cha mwisho cha Uajemi (kama vile vitu vya asili ya kale vya Yusufu 12.3.3 na II Wamakabayo 11:27). Linatumiwa na Luka katika Mdo 5:21 pamoja na "watu wa Sinagogi kuu." Yaweza kuwa ni njia ya kuelezea neno kwa viongozi wanaoongea Kiyunani (kama vile Wamakabayo 12:35)

B. *Synedrion*- "watu wa Sinagogi kuu." Huu ni muunganikano toka syn (pamoja na) na hedra (nafasi). Cha kushangaza neno hili linatumiaka katika lugha ya Kiarama, lakini likitazamisha neno la Kiyunani. mwishoni mwa kipindi cha Wamakabayo hili likajakuwa ni neno linalokubalika kuunda mahakama kuu ya Kiyahudi katika Yerusalemu (kama vile Mt. 26:59; Marko 15:1; Luk. 22:66; Yohana 11:47; Mdo 5:27). Tatizo hapa linakuja wakati maneno yale yale yanatumika katika mabaraza ya kimahakama ya mahali Fulani nje ya Yerusalem (kama vileMat. 5:22; 10:17)

C. *Presbyterion*- "baraza la wazee" (kama vile Luk 22:66). Huu ni mfumo wa Agano la Kale la viongozi wa kikabila. Hata hivyo, ilikuja kurejerea mahakama kuu katika Yerusalemu (cf. Mdo. 22:5)

D. *Boulē* –neno hili "baraza"lilitumiwa na Yusufu (yaani., vita 2.16.2; 5.4.2, lakini sio agano jipya) kuelezea watu mbali mbali wa kimahakama:

1. Senati kwenye mji wa Rumi
2. Mahakama za kawaida za Rumi
3. Mahakama kuu ya Kiyahudi katika Yerusalemu
4. Mahakama za kawaida za Kiyahudi

Yusufu wa Alimataya ameelezewa kama mwanajumuiya ya watu wa Sinagogi kuu kwa muundo wa neno hili (yaani., *bouleutē*, likimaanisha "mkuu wa baraza" kama vile Marko 15:43; Luka 23:50)

III. Maendeleo ya kihistoria

Mwanzoni kabisa Ezra alisema kulitengeneza Sinagogi kuu (kama vile Targum katika Wimbo ulio Bora 6:1)katika kipindi cha uhamisho, ambacho kilikuja onekana kuwa watu wa sinagogi kuu katika siku za Yesu.

A. Mishna (yaani., sheria za kiibada za Kiyahudi) zimeweka kumbu kumbu kwamba palikuwepo mahakama mbili kuu katika Yerusalem (kama vile Sanh. 7:1)

1. Moja iliyokuwa imeundwa na wanajumuiya 70 (au 71) (sand. 1:6 hata inaelezewa kuwa Musa alitengeneza hilo baraza la kwanza la watu wa Sinagogi kuu (Sanhedrin) la watu 11, kama vile Hes.11:16-25)
2. Lingine lililokuwa limeundwa na wanajumuiya 23 (lakini yawezekana inarejerea mabaraza ya Sinagogi ya kawaida).

3. Baadhi ya wasomi wa Kiyahudi waliamini kuwa palikuwepo na wanajumuiya 23 waliounda sinagogi kuu huko Yerusalemu. Wakati watatu wanaungana, pamoja na viongozi wawili, likiteua wanajumuiya 71 toka "watu wa sinagogi kuu."(yaani., Nasi na Av Bet Din).
    a. Kuhani mmoja (yaani., Sadukayo)
    b. Mwanasheria mmoja (pharisayo)
    c. Mtu wa ukoo bora mmoja (yaani., wazee)

B. Wakati wa ukimbizi toka mahali pao, kizazi cha Daudi kilichorudi ni Zurubabeli na kizazi cha Aroni alikuwa Yoshua. Baada ya kifo cha Zerubabeli, hapakuwepo na kizazi cha Daudi kilichoendeleza, kwa hiyo joho la kimahakama lilipitishwa pasipo kuwajumuisha makuhani (kama vile I Macc. 12:6) na wazee wa mahali (kama vile Neh. 2:16; 5:7).

C. Jukumu la kuhani katika mahakama lilithibitishwa na Diodorus 40:3:4-5 wakati wa

D. Jukumu hili la kuhani katika serikali liliendelea mpaka kipindi cha Selucid. Yusufu anamnukuu Antiokia "mkuu III" (223-187 K.K) katika mabo ya kale 12.138-142.

E. Mamlaka ya kuhani yaliendelea mpaka kipindi cha Wamakabayo kutokana na mambo ya kale ya Yusufu 13.10.5-6; 13.15.5

F. Wakati wa kipindi cha utawala wa Warumi gavana wa Syria (yaani., Gabinus toka 57-55 K.K) akaanzisha "sinsgogi kuu" za Kimikoa (kama vile mambo ya kale ya Yusufu 14.5.4; na Vita 1.8.5), lakini baadaye ilitenguliwa na Rumi (yaani., mwaka wa 47 K.K)

G. Watu wa Sinagogi kuu walikuwa na mkabiliano wa kisiasa na Herode (yaani., mambo ya kale 14.9.3-5) ambao, mwaka 37 K.K, wakalipiza kisasi na watu wengine wa baraza kuu wakauwawa (kama vile mambo ya kale ya Yusufu 14.9.4; 15.1.2)

H. Chini ya wakili wa Kirumi (yaani., 6-66 B.K) Yusufu anatuambia (kama vile mambo ya kale 20.200,251) kuwa watu wa Sinagogi kuu tena wakapata nguvu na umaarufu (kama vile Marko 14:55). Kuna majaribu matatu yalioandikwa katika Agano Jipya pale watu wa siangogi kuu, chini ya uongozi wa familia ya kuhani mkuu, walitenda haki.
    1. Jaribu la Yesu (kama vile Marko 14:53-15:1; Yohana 18:12-23,28-32)
    2. Petro na Yohana (kama vile Mdo. 4:3-6)
    3. Paulo (kama vile Mdo. 22:25-30)

I. Wakati Wayahudi walipoasi katika mwaka wa 66 K.K, Warumi baadaye wakaiharibu jamii yote ya Kiyahudi na Yerusalemu katika mwaka wa 70 K.K. watu wa sinagogi kuu moja kwa moja wakatenguliwa, ingawa Mfarisayo pale Jamnia wakajaribu kurudisha tena baraza kuu la kisheria (yaani., Beth Din) katika maisha ya dini ya Kiyahudi (lakini sio kwenye jamii au siasa)

IV. Uanachama

A. La kwanza Kibiblia kutajwa kwenye baraza kuu huku Yerusalemu ni lile la 2Nya. 19:8-11. Liliundwa na
    1. Walawi
    2. Makuhani
    3. Wakuu wa familia (yaani., wazee, kama vile I Wamak. 14:20; II Wamak.4:44)

B. Wakati wa kipindi cha Wamakabayo lilimilikiwa na (1) familia ya kikuhani ya Masadukayo na (2) familia ya ukoo bora wa mahali Fulani (kama vile I Wamak. 7:33; 11:23; 14:28). Baadaye katika kipindi hiki "waandishi" (wanasheria wa Musa, ambao mara nyingi walikuwa mafarisayo) waliongezwa, inaonekana na mke wa Alexanda Jannaeus, yaani Salome (76-67 B.K). Hata hivyo alisema kuwafanya mafarisayo kuwa kikundi cha maarufu (kama vile Yusufu, vita vya Wayahudi 1.5.2).

C. Wakati wa siku za Yesu baraza liliundwa na
    1. Familia ya kuhani mkuu
    2. Watu wa kawaida toka kwenye familia ya watu wenye uwezo
    3. Waandishi (kama vile Luk. 19:47)

V. Vyanzo vya maoni vikatafuta toka

A. Dictionary of Jesus and the Gospels, IVP, kur728-732

B. The Zondervan Pictorial Encyclopedia of the Bible, vol. 5, kur 268-273
C. The New Schaff-Herzog Encyclopedia of Religious Knowledge, vol. 10, kur. 203-204
D. The Interpreter's Dictionary of the Bible, vol. 4, kur. 214-218
E. Encyclopedia Judaica, vol. 14, kur. 836-839

◙ **"Mafarisayo"** Hiki kilikuwa ni kikundi cha kidini ambacho kilianzishwa kipindi cha Wamakabayo. Walikuwa wamejikita kwenye mapokeo ya fasihi simulizi (yaani., sheria za Kiyahudi). angalia MADA MAALUM: MAFARISAYO katika Marko 2:16.

◙ **"Maherodi"** Hiki kilikuwa ni kikundi cha kisiasa kilichounga mkono utawala wa Maherodi wa Edomu. Walikuwa wakipendelewa na hali ilivyokuwa ya Warumi. Kikawaida Mafarisayo na Maherodi walikuwa maadui. Ukweli kwamba walishirikiana inaonyesha namna walivyokuwa kinyume na mafundisho ya Yesu. Angalia MADA MAALUM: MAHERODI katika Marko 1:14.

◙ **"ili wamnase kwa maneno"** Kwa maana iliyo wazi ni "kukamata." Ilitumika kuwakamata wanyama wa mwitu. Ikajakuwa ni stiari kwa ajili ya kupata habari ili kwamba wampate na kosa (kama vile Luka 11:54). Walifikiri kuwa kwa kumuuliza maswali watamnasa kwenye makundi mawili haya kinzani. Mamlaka ya Kirumi na watu.

**12:14 "'Mwalimu, twajua ya kuwa wewe u mtu wa kweli, wala hujali cheo cha mtu; kwa maana hutazami sura za watu; lakini katika kweli waifundisha njia ya Mungu'"** Viongozi hawa walikuwa wakimfurahisha Yesu ili wampate na kosa, lakini kiukweli, walikuwa wakiongea sahihi kumhusu Yeye. Yesu aliushikiria ukweli sawa na YHWH alivyoushikiria. Hii ni kejeli ya hali ya juu! Maelezo yao ya kimtego yalikuwa katika kweli ya kumpa sifa kubwa.

◙ **"'hutazami sura ya watu'"** Nahau halisi ya Kiebrania ni"wewe hauangalii sura ya mtu." Kihistoria hili linarejelea kwa waamuzi wa Israeli. Walipolijaribu shitaka, watetezi wao waliinamisha vichwa vyao ili sura zao zisiweze kufahamika. Na pale hakimu anapowashika kidevu na kuinua nyuso zao ili kuona sura zao, nafasi kwa ajili ya kuwapendelea huongezeka. Kwa hiyo, haki hupindishwa!

◙ **"'ni halali kulipa'"** Hili ni swali la kisheria lenye kuhusiana na usajili wa sheria za Musa, lakini pia likihusiana na kumilikiwa kwa Israeli na Rumi. Hii ni aina ya maswali waandishi hushughulika nao kila siku. Kulikuwa na njia mbili za kujibu maswali, moja lilisimamia kwenye andiko la Musa na nyingine ilihusiana na ukweli wa sheria ya Kirumi na makazi. Hawa viongozi walitaka mazingira ya kisheria kuiingiza serikali ya Kirumi ndani ya tatizo la kidini (kama vile Luka 20:20). Kwa kujibu "ndiyo" atawakosea wafuasi wake; kwa kujibu "hapana" atakamatwa na serikali ya Kirumi.

◙ **"kodi"** Huu ulikuwa ni unukuzi wa neno la Kilatini "sensa." Ilikuwa ni kodi ya kichwa iliyowekwa na Rumi kwa watu wote waliokuwa mateka. Kwa wanaume waliopaswa kulipa kodi (yaani., 6-20 B.K) ni miaka kumi na mine hadi sitini na tano na wanawake waliopaswa kulipa ni kuanzia miaka kumi na miwili hadi sitini na mitano, walioishi ndani ya jimbo la kifalme walikwenda moja kwa moja kulipa kwa mfalme. Ndio ilikuwa sababu kwa nini Yusufu alipaswa kuondoka Nazareti na kwenda Bethelehemu akiwa na Mariam mjamzito (kama vile Luka 2:1-6).

**12:15 "akijua unafiki wao. . .mbona mnanijaribu"** Neno unafiki (*hupokrisis*) mwanzoni kabisa lilirejelea waigizaji wakicheza huku wakiwa wamejificha. Wakijifanya kuwa mtu Fulani lakini kumbe sivyo (kama vile Mt. 23:28; Luka 12:1; 20:20; 1 Tim. 4:2; 1 Pet. 2:1). Lilikuja kutumika kwa watu wajanja waliojaribu kuwatega wengine ili waweze kufikiri kuwa hakikuwa cha kweli. Kila kitu walichokisema hawa viongozi (kwa kumkejeli) kumhusu Yesu katika Marko 12:14 kilijikanganya na matendo yao yaliyoko Marko 12:15. Neno kujaribu (*peirazō*) lilikuwa na dokezo nyongezi la kumjaribu kwa kutazamia kushindwa. Angalia Mada Maalum: Maneno ya Kujaribu katika Marko 1:13.

◙ **"Dinari"** Hii sarafu ya shaba ilikuwa ndio njia pekee ya kuilipa kodi. Ulikuwa ni ujira wa siku wa mfanyakazi au mwanajeshi. Ilikuwa ni alama ya udhibiti wa Kirumi. Angalia Mada Maalum katika Marko 12:42.

**12:16 "'ni ya nani sanamu hii na anwani hii'"** Tiberius (mwaka wa 14-37 B.K) alikuwa ndiyo mfalme mkuu. Juu ya sarafu hii iliyodaiwa kuwa na sura ya mfalme. Mbele ya sarafu paliandikwa "Tiberi Kaisari Augusto, mwana wa Mungu Augusto." Upande wa nyuma wa sarafu palikuwa na picha ya Tiberi akiwa ameketi kwenye kiti cha enzi na maelezo "Kuhani Mkuu."

**12:17 "'mpeni Kaisari yaliyo ya Kaisari'"** Waamini wanapaswa kutii mamlaka ya kijamii kwa sababu Mungu amewawakfisha (kama vile Rum. 13:1-7; Tito 3:1; 1 Pet. 2:13-14). Neno la Kiyunani "mpeni" laweza kudokeza "kumrudishia mtu vitu vyake."

◙ **"'na yaliyo ya Mungu mpeni Mungu'"** Ingawa hali yenyewe ina ruhusu ya Kiungu, lakini haina hadhi ya Kiungu. Ikiwa hali yenyewe inadai kuwa na mamlaka ya ndani, hili linapaswa kukataliwa na wafuasi wa Mungu mmoja wa kweli. Wengi wamejaribu kuanzisha na kuunga mkono mafundisho ya kisiasa ya leo ya kujitenga na kanisa na serikali kutokana na mstari huu. kwa maana isio rasmi mstari huu unaelezea suala zima, lakini hakika sio wenye kuungwa mkono kimaandiko kwa ajili ya nadharia ya leo ya kisiasa. Hii nadharia kiukweli inaonekana kutoka kwenye historia, na wala kimsingi sio kutoka kwenye maandiko.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 12:18-27**
**18 Kisha Masadukayo, watu wasemao ya kwamba hakuna kiyama, wakamwendea, wakamwuliza na kusema, 19
Mwalimu, Musa alituandikia ya kwamba ndugu ya mtu akifa, akamwacha mkewe wala hana mtoto, ndugu yake amtwae yule mkewe akampatie ndugu yake mzao. 20 Basi kulikuwa na ndugu saba, wa kwanza akatwaa mke, akafa, asiache mzao. 21 Wa pili naye akamtwaa akafa, wala yeye hakuacha mzao. Na wa tatu kadhalika; 22 hata na wote saba, wasiache mzao. Mwisho wa wote yule mwanamke akafa naye. 23 Basi, katika kiyama atakuwa mke wa yupi katika hao? Maana wote saba walikuwa naye. 24 Yesu akajibu, akawaambia, Je! Hampotei kwa sababu hii, kwa kuwa hamyajui maandiko wala uweza wa Mungu? 25 Kwa maana watakapofufuka katika wafu, hawaoi wala hawaolewi, bali huwa kama malaika walioko mbinguni. 26 Na kwa habari ya wafu ya kwamba wafufuliwa, hamjasoma katika kitabu cha Musa, Sura ya Kijiti, jinsi Mungu alivyomwambia, akisema, Mimi ni Mungu wa Ibrahimu, na Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo? 27 Yeye si Mungu wa wafu, bali wa walio hai. Hivyo mwapotea sana.**

**12:18 "Masadukayo"** Hawa walikuwa ni jamii ya watu wakuu, makuhani wa dini ya Kiyahudi waliowasimamia Kuhani Mkuu na baraza la wazee wa Sinagogi. Walikuwa ni wenye mali, wenye makundi ya nguvu kisiasa. Walikuwa hawapendi mabadiliko na walikubaliana na maandiko ya Musa tu (yaani., Mwanzo mpaka Kumbukumbu la Torati) kwenye kutoa mamlaka (yaani., walikataa mapokeo ya fasihi simulizi).

## MADA MAALUM: MASADUKAYO

I. Chimbuko la Kundi
   A. Wasomi wengi wanaamini kuwa jina hili linatokana na Sadoki, mmoja wa makuhani wakuu wa Daudi (kama vile 2 Sam. 8:17; 15:24). Baadaye, Suleimani alimhamisha Abiathari kwa kuunga mkono uasi wa Adonia (kama vile 1 Flp. 2:26-27) na alimtambua Sadoki kama Kuhani Mkuu pekee (kama vile 1 Flp. 2:35). Baada ya uhamisho wa Babeli huu mpangilio wa kikuhani uliimarishwa tena katika Yoshua (kama vile Hag. 1:1). Hii familia ya Kilawi ilichaguliwa kwa ajili ya kusimamia hekalu. Baadaye wale waliokuwa miongoni mwa haya mapokeo ya kikuhani na wale wasaidizi wao waliitwa Wasadoki au Masadukayo.
   B. Ile karne ya tisa B. K. mapokeo ya Walimu wa Kisheria kwa Dini ya Kiyahudi neno (*Aboth* Mwalimu wa Sheria) anasema Sadoki alikuwa mwanafunzi wa Antigonus wa Sokho (karne ya pili K.K.). Sadoki hakuelewa usemi maarufu wa mshauri wake, "baada ya kifo thawabu,"na kuiendeleza thiolojia ambayo ilipingwa hapo nyuma na, ambapo pia ufufuo wa mwili ulipingwa.
   C. Baadaye ndani ya Dini ya Kiyahudi Masadukato walitambuliwa na wafuasi wa Boethus. Boethus pia alikuwa mwanafunzi wa Antigonus wa Sokho. Huyu aliikuza theolojia ile ile ya Sadoki, ambayo ilipingwa hapo nyuma.
   D. Hili jina Masadukayo halikuonekana hadi siku za Yohana Hyrcanus (135-104 B.K.), ambapo lilinukuliwana

Josephus (kama vile *Antiquities* 13.10.5-6). Katika *Antiquities* 13.5.9 Josephus anasema hawa wanaishi "shule tatu za," Mafarisayo, Masadukayo, na Wa-Essene.

E. Kuna nadharia za uamsho ambazo zilitokana na kile kipindi cha juhudi za utawala wa Selucid kuwafanya wawe wayunani ukuhani uliokuwa chini ya Antiokio IV Epiphanes (175-163 K.K.). Wamakabayo walipoasi ukuhani mpya ulianza katika Simoni Makabayo (142-135 K.K.) na uzao wake (kama vile I Mak. 14:41). Hawa makuhani wakuu wapya wa Hasmonia bila shaka walikuwa mwanzo wa makuhani wakuu yawezekana ulikuwa mwanzo wa utawala wa Masadukayo wa kimakabila. Mafarisayo walihimarika katika kipindi hiki hiki kutoka Hasidim (yaani, "waliotengwa," kama vile I Mak. 2:42; 7:5-23).

F. Kuna nadharia mpya (yaani, T. W. Manson) ambayo "Sadukayo" ni tafsri ya neno la Kiyunani *sundikoi.* Hili neno lilirejea juu ya mamlaka za mahali pale pale ambazo zilijitokeza pamoja mamlaka ya Kirumi. Hili linaweza kueleza kwanini baadhi ya Masadukayo hawakuwa makuhani wa utawala wa kimakabila, bali walikuwa mojawapo ya Wakuu wa baraza la Sinagogi.

II. Upekee wa Imani

A. Haya yalikuwa makundi madogo madogo ya kikuhani yasiyobadili msimamo (hawa walikubali kuwa Torati pekee kama iliyovuviwa) wa madhehebu ya maisha ya Kiyahudi wakati Hasmonean na vipindi vya Kirumi.

B. Hawa hasa walihusika na matukio ya hekalu, hitifaki, taratibu za dini, na liturujia.

C. Hawa walishikilia Torati iliyoandikwa yaani, Mwanzo – Kumbukumbu la Torati) kama utawala wa kikabila, lakini waliipinga desturi ya Orad (yaani, Buku la Sheria za Kiyahudi).

D. Hawa, kwa hiyo, walipinga mafundisho mengi yaliyotunzwa na kuendelezwa Mafarisayo

1. ufufuo wa mwili (kama vile Mt. 22:23; Marko. 12:18; Luka 20:27; Matendo ya Mitume 4:1-2; 23:8)
2. kufa kwa nafsi (kama vile *Antiquities* 18.1.3-4; *Wars* 2.8.14)
3. uwepo wa kueleza mpangilio wa malaika (kama vile Matendo ya Mitume 23:8)
4. hawa walichukulia "jino kwa jino" (yaani, *lex talionis)* kiuhalisi na waliunga mkono adhabu ya kimwili na adhabu za kifo (badala ya mapatano ya kifedha)

E. Eneo lingine la kithiolojia ilikuwa ni upinzani dhidi ya wazo la awali dhidi ya mapenzi huru. Ni makundi matatu yaliyotajwa na Josephus

1. Wa-Essene walikubali aina ya nadharia ya maamuzi
2. Masadukayo waliuondoa ule msisitizo juu ya mapenzi huru ya mwanadamu (kama vile *Antiquities* 13.5.9; *Wars* 2.8.14)
3. Mafarisayo walishikilia namna fulani ya usawa wa uelekeo kati ya haya mawili

F. Katika maana moja ya migogoro kati ya makundi mawili (yaani, Masadukayo – Mafarisayo) yaliyoangalia mvutano kati ya makuhani na manabii wa Kitabu cha Agano la Kale.Mvutano mwingine ulizuka kutokana na ukweli kwamba Masadukayo waliwakilisha daraja la kijamii na umiliki wa ardhi. Hawa walikuwa wenye mamlaka (kama vile Josephus' *Antiquities* 13.10.6; 18.1.4-5; 20.9.1), ambapo Mafarisayo na waandishi walikuwa wasomi na wacha Mungu miongoni mwa watu wa mahali pale. Mvutano huu ungeweza kubainishwa kama hekalu humo Yerusalemu dhidi masinagogi ya maeneo yote.

Mvutano mwingine unaweza kuwakilisha ule ukaidi wa Masadukayo wa ushawishi wa mafundisho ya Zorostra juu ya thiolojia ya kifarisayo. Mifano ya thiolojia yao ni (1) elimu ya juu ya kimalaika iliyokuzwa sana; (2) ule uwili kati ya HWH na Shetani; na (3) maelekezo mapendekezo ya maisha ya nyuma katika kukua kwa maneno ya wazi. Haya mazidi ya wa-Essene na Mafarisayo walisababisha mwitikio wa kithiolojia wa Masadukayo. Walirudi kwenye kushikiria nafasi yao ya thiolojia yao ya Musa tu katika kujaribu kuzuia mawazo mengine ya makundi mengine ya kiyahudi.

III. Chimbuko la Taarifa

A. Josephus ndiye chimbuko kuu la taarifa kuhusu Masadukayo. Alikuwa mbaguzi wa kujitoa kwake kwa Mafarisayo na nia katika kuweka wazi taswira chanya ya maisha ya kiyahudi ya Warumi.

B. vyanzo vingine vya taarifa ni fasihi ya kiualimu. Hatahivyo, hapa, pia, ubaguzi wa nguvu ni dhahiri. Masadukayo walikataa uhusiano na mamlaka ua desturi ya kinywa cha Wazee (yaani, Talmud). Maandiko haya ya Kifarisayo kwa uwazi yanafunua upinzani wao katika hali hasi, yawezekana ikiwa imetiwa chumvi (yaani mpinzani wa kubuni, mbinu) njia.

C. Hakuna maandiko yanayojulikana ya Kisadukayo yenyewe ambayo yamedumu. Pamoja na uharibifu wa

Yerusalemu na hekalu katika miaka ya 70 B.K nyaraka zote na ushawishi wa usomi wa kikuhani uliharibiwa. Walitaka kuendeleza amani ya kimkoa na njia pekee ya kufanya hivyo katika karne ya kwanza ilikuwa ni kushirikiana na Rumi (kama vile Yohana 11:48-50).

**12:19 "'Musa alituandikia '"** Hili linarejelea kwenye mazungumzo ya Musa ya ndoa ya Kurithishana wake iliyopo Kumb.25:5-10.

◙ **"'kwamba ndugu ya mtu akifa'"** Hizi sheria za Kiyahudi zilikuja kujulikana "ndoa za kurithishana wake." Ni neno la Kilatini lenye maana ya "mme wa nduguyo." Haki ya kurithi ilikuwa ni ya muhimu huko Israeli kwa sababu Mungu alikwisha wapa nchi ya ahadi kwa kabila la Lutu (kama vile Yoshua 12-19). Kwa hiyo, ikiwa mwanaume atakufa pasipo kijana mwingine wa kumrithi, hivyo nduguye alitarajia kumwoa mjane na kumzalia mtoto akiwa na mjane, baadaye mtoto atakuwa mrithi wa mali ya nduguye.

**12:23** Hapa kuna kusudio la swali, ili kubeza dhana ya ufufuo wa kimwili baada ya kufa.

**12:24** Swali la kufadhaisha la Yesu liliangazia juu ya Masadukayo kukosa ufahamu wa maandiko na Mungu. Muundo wake wa kisarufi unategemea jibu la "ndiyo".

**12:25 "'huwa kama malaika walioko mbinguni'"** Hili rejeo fupi limesababisha mitazamo mingi. Malaika katika Agano la Kale mara nyingi huwa jinsi ya kiume (isipokuwa kwa Zak. 5:9). Je hoja hii ya Yesu inarejelea kwenye ujinsia au kukutana kimwili? Ni kwa namna gani hili linaathiri uelewa wa mtu wa Mwa.6:1-2? Huenda tunajaribu kuwa na uelewa mwingi wa thiolojia kutokana na mkabiliano wa Masadukayo. Mbinguni kuna utofauti mkubwa wa uzoefu wa kimahusiano kuliko duniani. Namna kamili ya mahusiano yanayofanywa kati ya watu wawili, ulimwengu wa kiroho unavyotenda kazi haijulikani. Biblia imechagua kutodhihirisha habari nyingi kuhusu maisha baada ya kifo. Masadukayo walichukua huku kukosekana kwa taarifa kama sababu ya kukataa ukweli wa maisha baada ya kufa. Ni vizuri kuthibitisha ukweli uliosimamia juu ya ahadi ya Mungu na Kristo, lakini ukapenda kubaki pasipo kufahamu mpaka kifo. Biblia inatoa vyote mwamini anachohitaji kujua!
Yesu anadai kuwa hakuna dhana ya jinsia (yaani., kuzaliana) itakayokuwepo mbinguni. Kuna maswali mengi mtu angependa kuuliza kuhusiana na hili, lakini hapana maelezo kamili yaliyotolewa katika Agano Jipya. Laweza kidogo kurejea kwenye ukweli kwamba malaika wameumbwa na Mungu na sio kwa namna ya kuzaliana kimwili.

**12:25-26 "'malaika. . .lakini kwa habari ya wafu kufufuliwa'"** Masadukayo walikataa habari za malakia kuwepo na kufufuka. Mafarisayo walililidhithibitisha zote.

**12:26 "'lakini kwa habari ya wafu kufufuliwa'"** Kuna maandiko mbalimbali katika Agano la Kale yenye kuthibitisha ukweli huu (kama vile Ayubu 14:14-15; 19:25-27; Zab. 23:6; Isa. 25:6-9; 26:14-19; Dan. 12:2). Na bado maisha baada ya kifo katika Agano la Kale yanadokeza ukweli. Ufunuo endelevu wa Agano Jipya unaelezea ukweli, lakini bado katika dokezo la lugha ya kiistiari. Mbinguni ni ahadi ya kweli na uhakika, lakini asili yake kamili ni fumbo.

◙ **"'katika kitabu cha Musa'"** Yesu anadai kuwa Musa ndio chanzo cha Kumbukumbu la Torati. Hili swali pia linatarajia jibu la "ndiyo".

## MADA MAALUM: UANDISHI WA TORATI YA MUSA

A. Biblia yenyewe haisemi mwandishi ni nani (kama ilivyo kweli kwa vitabu vingi vya Agano la Kale). Kitabu cha Mwanzo hakina kipengere cha "Mimi" kama ilivyo kwa Ezra, Nehemia, au kipengere cha "sisi" kama ilivyo Matendo ya Mitume.

B. Desturi za Kiyahudi

1. waandishi wa kale wa Kiyahudi wanasema Musa ndiye aliandika
    a. kitabu cha Ben Sirah *Ecclesiasticus*, 24:23, kiliandikwa yapata mwaka wa 185 K.K.

b. *Baba Bathra* 14b, mbali na buku la sheria za Kiyahudi ambacho hutoa uandishi wa kimapokeo wa vitabu vya Agano la Kale
c. Filo wa Iskanderia, huko Misri, mwana falsafa wa Kiyahudi, aliyeishi yapata miaka ya 20 K.K. na 42 B.K
d. Flavius Josephus, mwana historia wa Kiyahudi, aliyeishi yapata miaka ya 37-70 B.K

2. YHWH anafunua ukweli kwa Musa
   a. Musa anasemekana kuyaandika kwa ajili ya watu
      1) Kutoka 17:14
      2) Kutoka 24:4, 7
      3) Kutoka 34:27, 28
      4) Hesabu 33:2
      5) Kumbukumbu la Torati 31:9, 22, 24-26
   b. Inasemekana Mungu aliongea na watu kupitia Musa
      1) Kumbukumbu la Torati 5:4-5, 22
      2) Kumbukumbu la Torati 6:1
      3) Kumbukumbu la Torati 10:1
   c. Inasemekana Musa aliyaongea maneno ya Torati kwa watu
      1) Kumbukumbu la Torati 1:1, 3
      2) Kumbukumbu la Torati 5:1
      3) Kumbukumbu la Torati 27:1
      4) Kumbukumbu la Torati 29:2
      5) Kumbukumbu la Torati 31:1, 30
      6) Kumbukumbu la Torati 32:44
      7) Kumbukumbu la Torati 33:1
3. wandishi wa Agano la Kale wanaliona kuwa la Musa
   a. Yoshua 8:31
   b. 2 Fal. 14:6
   c. Ezra 6:18
   d. Nehemia 8:1; 13:1-2
   e. 2 Nya. 25:4; 34:12; 35:12
   f. Danieli 9:11
   g. Malaki 4:4

C. Mapokeo ya Kikristo
1. Yesu anaziona nukuu zikitoka kwenye Torati kumwelekea Musa
   a. Mathayo 8:4; 19:8
   b. Marko 1:44; 7:10; 10:5; 12:26
   c. Luka 5:14; 16:31; 20:37; 24:27, 44
   d. Yohana 5:46-47; 7:19, 23
2. wandishi wengine wa Agano Jipya wanaziona nukuu zikitoka kwenye Torati kumwendea Musa
   a. Luka 2:22
   b. Mdo.3:22; 13:39; 15:1, 15-21; 26:22; 28:23
   c. Warumi 10:5, 19
   d. 1 Wakorintho 9:9
   e. 2 Wakorintho 3:15
   f. Waebrania 10:28
   g. Ufunuo 15:3
3. wengi wa wandishi na wanathiolojia wa kale walikubaliana na uandishi wa Musa. Hata hivy, Ireneaus, Clement wa Iskanderia, Origen, na Tertullian wote wana maswali kuhusu uhusiano wa Musa na muundo wa sasa wa sheria za kanisa za kitabu cha Mwanzo (kama vile D. 2. Kwenye ukurasa wa 3).

D. Wasomi wa kisasa
1. hakika pamekuwepo na baadhi ya maongezeko ya kihariri kwenye Torati (inavyoonekana kulifanya lile la

kale kueleweka vizuri kwa wasomaji wa leo, ambayo ilikuwa ni tabia ya wandishi wa Misri):

   a. Mwanzo 12:6; 13:7; 14:14; 21:34; 32:32; 36:31; 47:11
   b. Kutoka11:3; 16:36
   c. Hesabu 12:3; 13:22; 15:22-23; 21:14-15; 32:33 na kuendelea
   d. Kumbukumbu la Torati 3:14; 34:6

2. waandishi wa kale walikuwa wasomi na wenye weledi mkubwa. Mbinu zao, hata hivyo, zilitofautiana toka taifa moja hadi jingine:
   a. Huko Mesopotamia, walikuwa waangalifu kutobadilisha kitu chochote, hata kuweza kuangalia kazi yao kwa usahihi. Hapa kuna tanbihi ya mwandishi wa kale wa Kisumeri yapata toka mwaka wa 1400 K.K.: "kazi imekamilika toka mwanzo hadi mwisho, imekwisha kuchapishwa, kupitiwa, kulinganishwa, na kuthibitishwa kwa kusainiwa."
   b. Huko Misri pasipo kuzuiliwa waliweza kuyapitia tena upya maandiko ya kale ili kuyaboresha kwa ajili ya wasomi wa kisasa. Waandishi na wanathiolojia wa maeneo ya elimukale, Qumran (yaani., magombo ya Bahari ya Chumvi) walifuatisha huu mtazamo.
3. Wanazuoni wa karne ya 19 wanaongea kinadharia kuwa Torati ni mkusanyiko wa nyaraka toka vyanzo mbalimbali vya muda mrefu (Graff-Wellhausen). Hii nadharia ilikuwa imesimamia juu ya:
   a. Majina tofauti ya Mungu
   b. jozi ya kufanana ya wazi katika andiko
   c. Muundo wa fasihi wa habari yenyewe
   d. Thiolojia ya habari
4. vyanzo na tarehe za kudhaniwa
   a. chanzo J (kikitumika kwa YHWH toka Kusini mwa Israeli) – 950 K.K.
   b. chanzo E (kikitumia Elohim toka kaskazini mwa Israeli) – 850 K.K.
   c. JE vikiunganishwa pamoja – 750 K.K.
   d. chanzo D – 621 K.K. (kitabu cha sheria, 2 Fal. 22:8, kiligunduliwa wakati wa mageuzi ya Yoshua wakati wakilifanyia mabadiliko hekalu walidhani kitabu cha Kumbukumbu la Torati, kikiandikwa na kuhani asiyejulikana wa kipindi cha Yoshua kuyaunga mkono mageuzi yake).
   e. chanzo P (mwandishi wa kikuhani wa Agano la Kale, hasa ibada na taratibu) – 400 K.K.
5. dhahili pamekuwepo na ongezeko la kiuhariri kwenye Torati. Wayahudi wanadai kuwa alikuwa ni
   a. Kuhani Mkuu (au mwingine wa familia yake) kipindi cha uandishi
   b. Nabii Yermia
   c. mwandishi Ezra – IV Esdras anasema alikiandika teana kwa sababu kile cha mwanzo kiliharibiwa kipindi cha anguko la Yerusalem katika mwaka 586 K.K.
6. Hata hivyo, nadharia ya J. E. D. P. anasema zaidi kuhusu nadharia zetu za fasihi ya kisasa kuliko ushahidi wa Torati (R. K. Harrison, *Introduction to the Old Testament*, kur. 495-541 and *Tyndale's Commentaries*, "Leviticus," kur. 15-25).
7. Tabia za fasihi ya Kiebrania
   a. jozi za kufanana, kama ilivyo Mwanzo 1 & 2, ni la kawaida katika Kibrania. Mara nyingi maelezo ya pamoja hutolewa, yakifuatiwa na habari maalum.hili laweza kuwa namna ya kuutamka ukweli.
   b. walimu wa sheria ya Kiyahudi wa kale walisema majina mawili yaliyozoeleka kwa ajili ya Mungu yana umuhimu kithiolojia:
      1) YHWH – ni jina la agano la Kiungu kama linavyohusiana na Israeli kama mwokozi na mkombozi (kama vile Zab. 19:7-14; 103).
      2) Elohim – Mungu muumbaji, mtoaji, na mwezeshaji wa maisha yote ya duniani (kama vile Zab. 19:1-6; 104).
   c. ni kawaida kwa fasihi isiyo ya kibiblia ya Mashariki ya Karibu kuwa na aina mbalimbali za mitindo na misamiati kuonekana katika kazi ya fasihi iliyoko pamoja (kama vile R. K. Harrison, kur. 522-526).
8. kuna dharia zinazojitokeza kuwa palikuwepo na waandishi (katika sehemu mbalimbali za Israeli) wakitenda katika sehemu mbalimbali za torati na wakati huo huo chini ya maelekezo ya Samweli (kama vile 1 Sam. 10:25). Nadharia hii mara ya kwanza ilipendekezwa na E. Robertson's *The Old Testament*

*Problem*.

E. ushahidi toka fasihi ya kale ya Mashariki ya Karibu inadokeza kuwa Musa alitumia nyaraka zilizoandikwa kwenye kikabari au kwa mtindo wa Mesopotamia (wazee wa kaya) wa mapokeo ya fasihi simulizi kuandika kitabu cha Mwanzo. Pasipo namna ikimaanisha kudokeza kupunguza uvuvio, lakini ni jaribio la kuelezea tabia ya fasihi ya kitabu cha Mwanzo (kama vile P. J. Wiseman's *New Discoveries in Babylonia about Genesis*). Ukianzia katika Mwanzo 37, mamlaka ya wazi ya Kimisri ya mtindo, muundo, na msamiati inaonekana kuonyesha Musa huenda alitumia fasihi ilitengenezwa au mapokeo ya fasihi simulizi toka kwenye kipindi cha Waisraeli waliokuweko Misri na Mesopotamia. Elimu ya Musa ya awali hakika ilikuwa ni ya kutoka Misri! Mpangilio sahihi wa fasihi ya Torati haujulikani. Ninaamini kuwa Musa ndiye mtungaji na mwandishi wa sehemu kubwa ya Torati, ingawa akawa ametumia wandishi na/ mapokeo ya fasihi simulizi. Maandiko yake yamefanyiwa maboresho na waandishi wa baadaye. Tabia ya historia na uaminifu wa vitabu vichache vya kwanza vya Agano la Kale vimeelezewa kwa mifano na wanaakiolojia wa kisasa.

◙ **"'Mimi ni Mungu wa Ibrahimu'"** Hili rejeo toka Kut.3:2-6 ni mchezo juu ya njeo ya kitenzi cha Kiebrania "kuwa." Muundo wa kitenzi hiki (yaani., kisababishi) kikajakuwa ni jina la agano kwa ajili ya Mungu wa Israeli, YHWH (kama vile Kut. 3:14). Jina linadokeza kuwa ni Mungu pekee aishiye milele. Kwa vile anaishi, na watu wake wanaishi pia (kama vile Marko 12:27; Zab. 103:15-17; Isa. 40:6-8; 1 Pet. 1:24-25). Tambua kuwa Yesu anathibitisha kweli ya kuwepo kwa maisha baada ya kifo kutokana na maandiko ya Musa, ambacho kilikuwa kipengere cha sheria za Kiebrania kuwa hawa Masadukayo walikubaliana nayo kama mafundisho ya kimamlaka.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 12:28-34**

**28 Na mmojawapo wa waandishi akafika, akawasikia wakisemezana naye, akatambua ya kuwa amewajibu vema, akamwuliza, Katika amri zote ni ipi iliyo ya kwanza? 29 Yesu akamjibu, Ya kwanza ndiyo hii, Sikia, Israeli, Bwana Mungu wetu ni Bwana mmoja; 30 nawe mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote, na kwa nguvu zako zote. 31 Na ya pili ndiyo hii, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Hakuna amri nyingine iliyo kuu kuliko hizi. 32 Yule mwandishi akamwambia, Hakika, Mwalimu, umesema vema ya kwamba Mungu ni mmoja, wala hakuna mwingine ila yeye; 33 na kumpenda yeye kwa moyo wote, na kwa ufahamu wote, na kwa nguvu zote, na kumpenda jirani kama nafsi yako, kwafaa kuliko sadaka nzima za kuteketezwa na dhahibu zote pia. 34 Naye Yesu, alipoona kwamba amejibu kwa busara, alimwambia, Wewe hu mbali na ufalme wa Mungu. Wala hakuthubutu mtu kumsaili neno tena tokea hapo.**

**12:28 "waandishi"** Hawa mara nyingi hawakutokana na uzao wa kikuhani (yaani., hawakuwa Walawi), ambao walikuja kuwa wanazuoni katika mapokeo ya fasihi simulizi (yaani., sheria za Kiyahudi) za Wayahudi. Katika Agano la Kale Walawi wa maeneo ndio walitafasiri maandiko matakatifu kwa watu (kama vile Neh. 8). Kama Sinagogi la mahali lililoanzishwa huko uhamishoni Babeli, kazi ya walimu wa maeneo na watafasiri wakahitajika kwa wingi.katika siku za Yesu hawa waandishi walikuwa Wafarisayo. Kihistoria waliongezeka (yaani., baada ya kuliharibu hekalu) ndani ya walimu wa dini ya Kiyahudi. Angalia Mada Maalum katika Marko 2:6.

◙ **"akawasikia wakisemezana naye"** Ufanano ulioko katika Mt. 22:34-35 unaonekana kudokeza makusudi yaliyofichika, lakini injili ya Marko inadokeza kiukweli alifurahia maswali ya kithiolojia.

**12:29 "'sikia'"** Yesu anarejea toka Kumbu. 6:4-5, lakini sio kutoka katika Matoleo ya Kimasoreti au tafasiri za maandiko ya kale ya Kiebrania (ufanano katika Mt. 22:37 unakaribiana na ule wa toleo la MT, lakini haufanani kabisa). Rejeo la Yesu linaongeza kifungu kwenye matoleo ya Masoretic Hebrew text na Septuagint Greek text. Rejeo kamili halijulikani toka kwenye andiko la Agano la Kale. Toleo la LXX linabadili neno la Kiebrania "moyo" kwenda "sikia" au "elewa." Lakini rejeo hili linaongeza kifungu "kwa akili zenu zote"kwenye vifungu vitatu (yaani., moyo, nafsi, nguvu) katika toleo la MT na LXX. Toleo la NJB linalitambua hili kwa kuwekea alama kifungu kuwa sio moja ya sehemu ya rejeo la Agano Jipya (yaani., sio katika mwandiko wa mlazo). Inafurahisha kuwa maandishi ya herufi kubwa za Kiyunani D (yaani., Bezae) toka

karne ya tano yanaondoa kifungu chote "na kwa akili zako zote". Hili laweza kuaksi lile la asili kwa sababu kukosekana kwake kunaendana na wajibu wa waandishi katika Marko 12:33.
Katika ufanano wa Mathayo (yaani., 22:32) Mathayo ananukuu msemo wa Yesu, "kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote." Hapa kishazi cha Kiebrania "kwa nguvu zako zote" kimeondolewa. Inashangaza kuwa Marko na Mathayo hawakubaliana na kila mmoja kuhusiana na matoleo ya MT na LXX. Huu ni mfano kamili kutokujali mengi ya marejeo ya Agano la Kale ndani ya Agano Jipya (hata na yale yaliyotambuliwa na Yesu). Hapa ndipo kunatokea kukosekana kwa usahihi. Wote (yaani., toleo la LXX, Mathayo. na Marko) wanaaksi maana kamili ya rejea toka kwa Musa.

Hili andiko la Agano la Kale (yaani., Kumb. 6:4-5) linaitwa *Shema*, ambalo ni neno la Kiebrania "sikia." Inamaanisha kusikia ili kutenda. Limekuja kuwa thibitisho la Kiyahudi la imani ya Mungu mmoja. Linaombwa kila siku na Wayahudi waaminifu na kwa kila Sabato. Kuna maandiko mengine ya umoja na upekee wa Mungu katika manabii, lakini hili ni maandiko ya Musa (yaani., Mwanzo. — Kumb.) na kwa hiyo, yanawafunga wasikilizaji wote wa Yesu (yaani., Masadukayo na Mafarisayo).

**12:30** Majibu ya Yesu yanaonyesha kuwa kuna dhana mbili kwenye amri kuu za Mungu: (1) umoja na upekee wa Mungu na (2) kujitoa kwetu kikamilifu kwake na Yeye pekee!

◙ **"moyo"** Angalia Mada Maalum katika Marko 2:6.

**12:31 "'mpende jirani yako'"** Hii ni nukuu toka kwa Law. 19:18 kwenye tafasri ya maandiko ya kale ya Kiebrania. Yesu alihusianisha ukweli wa kithiolojia katika utendaji, hitaji la kimaadili (kama vile Zakaria 7-8). Haiwezekani kumpenda Mungu na kuwachukia wale wote walioumbwa kwa mfano wake (kama vile 1 Yohana 2:9-11; 3:15; 4:20).
Ni ngumu kumpenda jirani yako (yaani., ndugu wa agano) kama wewe mwenyewe unavyojipenda. Kuna upendo binafsi usiofaa ambao unasimamia juu ya upendo wa kwanza wa Mungu kwa ajili ya mwanadamu. Sisi tu uumbaji wake, tukitengenezwa kwa sura yake (kama vile Mwa. 1:26,27). Lazima tufurahi kwenye kutunukiwa kwetu na kukubali hulka zetu za mwili, akili, na saikolojia (kama vile Zab. 139). Kujibeza kwetu ni kumubeza Yeye aliyetuumba! Anaweza kubadili anguko letu kuwa mfanano wa utukufu Wake (yaani., kumfanana Kristo).
Ukristo unahusisha ahadi ya imani binafsi kwa Mungu kupitia Kristo. Inaanza na maamuzi binafsi ya hiari ya toba na imani. Hata hivyo, suala lake ni la tukio la kimahusiano. Tumekilimiwa kwa ajili ya vitu vizuri (kama vile 1 Kor. 12:7). Sisi tu sehemu ya mwili wa Kristo. Namna tuwatendeavyo wengine ndiko kunatuonyesha utii wetu kwa Kristo. Kufanyika kitu kimoja kwa Mungu na mwanadamu aliyefanywa kwa sura na mfano wa Mungu kunahitaji mwitikio sahihi dhidi ya Mungu na wanadamu wengine (yaani., hasa wale wa nyumbani mwa imani).

◙ **"'hapana amri zingine zillizo kuu kuliko hizi'"** Maelezo haya ni magumu kwa waamini wenye kushikilia sheria sana (yaani., wadhaifu; kama vile Rum. 14:1-15:13) kuweza kukubali. Tukiwa na upendo wa jumla kwa Mungu na ndugu wa agano (na hata waliopotea) hapana sheria juu ya hilo. Sheria lazima zibubujike toka kwenye moyo uliobadilika na fikra; haileti utukufu!

**12:32-33 "'Yeye. . .Yeye'"** Hivi viwakilishi nomino vinamrejelea YHWH. Kwa sababu ya Kut. 20:7, wengi wa Wayahudi wasingalijisikia vizuri kulitaja bure jina la Mungu wa agano.

◙ **"'hapana mwingine zaidi ya Yeye'"** Hiki kifungu hakipingi uwepo wa viumbe vingine vya kiroho kama vile malaika. Hii kwa maana iliyo wazi inamaanisha hapana mwingine aliyekuweko kabla au baada ya YHWH. Yeye ni aina ya kipekee (kama vile Kut. 8:10; 9:14; Kumb. 4:35,39). Huyu mwandishi anajaribu kuelezea upekee wa YHWH!

**12:33 "'kupenda. . .kwafaa zaidi kuliko sadaka ya kuteketeza'"** Huyu mwandishi alikuwa na uelewa mkubwa kuhusu uhusiano uliopo kati ya imani na ibada (kama vile 1 Sam. 15:22; Isa. 1:11-14; Hos. 6:6; Amos 5:21-24; Mika 6:6-8). Hii sio kupunguza ibada za hekaluni, bali ni kutetea kuwa makusudi sahihi na imani ndio vitu vya muhimu (yaani., kuungana na mitazamo ya kikuhani na kinabii).

**12:34 "'Wewe hu mbali na ufalme wa Mungu'"** Habari hii ilikuwa ni njia nyingine kuwa Yesu kama kitovu cha mwitikio chanya na imani. Ufalme unapatikana (yaani., kupitia imani katika Yesu), na sio mahali Fulani huko mbeleni. Ingawa huyu mtu akiitambua thiolojia ya agano la Kale, hakuwa sawa na Mungu pasipo kuweka imani yake katika Kristo. Thiolojia sahihi haitoi uhakika wa wokovu! Maarifa ya Biblia hayatoi uhakika wa wokovu! Utendaji wa ibada za kidini na liturujia hautoi uhakika wa wokovu! Lakini imani katika Kristo inatenda!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 12:35-37**
**[35] Hata Yesu alipokuwa akifundisha katika hekalu, alijibu, akasema, Husemaje waandishi ya kwamba Kristo ni Mwana wa Daudi? [36] Daudi mwenyewe alisema, kwa uweza wa Roho Mtakatifu, Bwana alimwambia Bwana wangu, Uketi mkono wangu wa kuume, Hata niwawekapo adui zako Kuwa chini ya miguu yako. [37] Daudi mwenyewe asema ni Bwana; basi amekuwaje mwanawe? Na mkutano mkubwa walikuwa wakimsikiliza kwa furaha.**

**12:35 "'Husemaje'"** Hii sura inaweka kumbukumbu ya mlolongo wa maswali

1. Toka kwa wakuu wa Sinagogi (Marko 11:27-12:12)
2. Toka kwa Mafarisayo na Maherodi (Marko 12:13-17)
3. Toka kwa Masadukayo (Marko 12:18-27)
4. Toka kwa waandishi (Marko 12:28-34)
5. toka kwa Yesu (Marko 11:29-33,35-37)

Yesu akawauliza swali kama alivyofanya kwa Marko 11:29-30. Hii njia ya swali na jibu ni tabia za waalimu wa dini ya Kiyahudi.

◙ **"'Kristo ni Mwana wa Daudi'"** Soma Mt. 12:23ff; 21:15; 2 Sam. 7:11-16 na ulinganishe na Zab. 110:1.
Yesu alikuwa akijaribu kuwafikia viongozi wa dini. Aliwatunza kwa hiyo alitumia aina yao ya kuyapima na kuyafasiri maandiko. Walikuwa na uelewa mkubwa, lakini walipofushwa na desturi.

**12:36 "Daudi mwenyewe alisema katika uweza wa Roho Mtakatifu"** Hili linatetea utiaji hamasa wa Zaburi 110 na Roho Mtakatifu. Biblia ni kweli ya Kiungu (yaani., toka kwa Roho), lakini likiandikwa katika lugha na tamaduni za waandishi wa mwanzo.

◙ **"'Bwana alimwambia bwana wangu'"** Hii ni nukuu toka Zab. 110:1 kutoka tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania. Katika Kiebrania lile neno la kwanza "Bwana" (yaani., lililotafasiriwa katika Kiingereza kwa herufi kubwa zote) ni namna zetu za tafasiri za Kiingereza za kumtafasiri YHWH. Hili lilitokea kwa sababu Waebrania walikuwa wanasita kutumia jina la agano kwa ajili ya Uungu. Kwa hiyo, mtu alipomwendea YHWH katika andiko ili liweze kusomwa kwa sauti, alilibadilishia kwenye neno la Kiebrania *Adon*, lenye kumaanisha "bwana," "mme," "mmiliki," au "bwana." Katika Kiyunani lilitafasiriwa *kurios*. Huu utofauti hauonyeshwi kwenye andiko la Kiyunani ambapo neno *kurios* linayatafasiri yote YHWH na *adon*.

## MADA MAALUM: MAJINA YA UUNGU

A. *El*
   1. Maana ya asili ya jina la jumla la kale kwa ajili ya Uungu haijulikani, ingawa wanataaluma wengi wanaamini linatoka katika mzizi wao wa lugha ya Akkadia, "kuwa shupavu" au "kuwa mwenye nguvu" (kama vile Mwanzo 17:1; Hesabu 23:19; Kumb 7:21; Zab. 50:1).
   2. Katika hekalu la miungu ya Wakanaani mungu mkuu ni *El* (maandiko ya Ras Shamra)
   3. Kalika Biblia *El* mara nyingi huwa haliambatani na maneno mengine. Miunganiko hii ilifanyika njia ya kuainisha tabia za Mungu.
      a. *El-Elyon* (Mungu aliye Mkuu sana), Mwanzo 14:18-22; Kumb. 32:8; Isa. 14:14
      b. *El-Roi* ("Mungu aonaye" au "Mungu ajifunuaye Mwenyewe"), Mwanzo 16:13
      c. *El-Shaddai* ("Mungu Mkuu" au "Mungu mwenye huruma zote" au "Mungu wa mlima"), Mwanzo 17:1; 35:11; 43:14; 49:25; Kutoka 6:3

d. *El-Olam* (Mungu wa milele yote), Mwanzo 21:33. Neno hili linaunganishwa na ahadi ya Mungu kwa Daudi, II Sam. 7:13,16
e. *El-Berit* (Mungu wa Agano"), Waamuzi 9:46

4. *El* inalinganishwa na
   a. YHWH katika Zaburi. 85:8; Isa. 42:5
   b. *Elohim* katika Mwanzo 46:3; Ayubu5:8, "Mimi ni *El*, *Elohim* wa baba yako
   c. *Shaddai* katika Mwanzo. 49:25
   d. "wivu" katika Kut. 34:14; Kumb. 4:24; 5:9; 6:15
   e. "rehema" katika Kumb. 4:31; Neh. 9:31; "mwaminifu" katika Kumb. 7:9; 32:4
   f. "mkuu na mzuri" katika Kumb. 7:21; 10:17; Neh. 1:5; 9:32; Dan. 9:4
   g. "maarifa" katika I Sam. 2:3
   h. "kimbilio langu" katika II Sam. 22:33
   i. "mlipa kisasi wangu" katika II Sam. 22:48
   j. "mtakatifu" katika Isa. 5:16
   k. "muweza" katika Isa. 10:21
   l. "wokovu wangu" katika Isa. 12:2
   m. "mkuu na mwenye nguvu" katika Yer. 32:18
   n. "anayepatiliza: katika Yer. 51:56
5. Muunganiko wa majina yote makubwa ya Agano la Kale yanapatikana katika Joshua 22:22 (*El, Elohim, YHWH,* kurudiwa)

B. *Elyon*
1. Maana yake ya msingi ni "juu," "aliyetukuzwa," au "kuinuliwa" (kama vile Mwanzo 40:17; I Wafalme. 9:8; II Wafalme.
   18:17; Neh. 3:25; Yer. 20:2; 36:10; Zab. 18:13).
2. Inatumika katika namna ya usambamba wa majina mengine/vyeo vya Mungu.
   a. *Elohim* – Zab. 47:1-2; 73:11; 107:11
   b. *YHWH* - Mwanzo 14:22; II am. 22:14
   c. *El-Shaddai* - Zab. 91:1,9
   d. *El* - Hes. 24:16
   e. *Elah* - iliyotumika mara kwa mara katika Danieli 2-6 na Ezra 4-7, inaunganishwa pamoja na *illair* (Kiaramaiki kwa ajili ya "Mungu aliye Juu") katika Dan. 3:26; 4:2; 5:18,21
3. Mara kwa mara inatumika kwa wasio waisraeli.
   a. Melkizedeki, Mwanzo 14:18-22
   b. Balaamu, Hes. 24:16
   c. Musa akizungumzia Mataifa katika Kumb. 32:8
   d. Injili ya Luka katika Agano Jipya, akiandika kwa Mataifa, pia akitumia maneno ya kufanana na Kiyunani *Hupsistos* (kama vile 1:32,35,76; 6:35; 8:28; Mdo 7:48; 16:17)

C. *Elohim* (wingi), *Eloah* (umoja), inatumika kimsingi katika ushairi
1. Neno hili halipatikani nje ya Agano la Kale.
2. Neno hili linaweza kumaanisha Mungu wa Israeli au miungu wa Mataifa (kama vile Kut. 12:12; 20:3). Familia ya Ibrahimu walikuwa Waabudu miungu wengi (kama vile Josh. 24:2).
3. Neno *elohim* pia linatumika juu ya viumbe vingine vya kiroho (malaika na mapepo) kama ilivyo katika Kumb. 32:8 (LXX); Zab. 8:5; Ayubu 1:6; 38:7. Inaweza kumaanisha waamuzi wa kibinadamu (kama vile Kut. 21:6; Zab. 82:6)
4. Katika Biblia cheo cha kwanza, jina kwa ajili ya Uungu (kama vile Mwanzo. 1:1). Linatumika bila mjumuisho mpaka Mwanzo. 2:4, ambapo linaunganishwa na YHWH. Kimsingi (kithiolojia) linamaanisha muumbaji, mtoshelevu na mpaji wa uhai wote juu ya sayari hii (kama vile Zab. 104). Ni sawa na kisawe *El* (kama vile Kumb. 32:15-19). Pia linaweza kuwa likifanana na YHWH kama Zab. 14 (*elohim*) ni sawasawa kabisa na Zab. 53 (YHWH), isipokuwa kwa mabadiliko katika majina ya kiungu.
5. Ingawa wingi unatumika juu ya miungu mingine, neno hili mara kwa mara linamaanisha Mungu wa

Israeli lakini siku zote lina kitenzi cha umoja kuelezea matumizi ya imani juu ya Mungu mmoja kama mtawala juu ya dunia nzima.

6. Neno hili linapatikana katika vinywa vya wasiokuwa Waisraeli kama jina la Uungu.
    a. Melkizedeki, Mwanzo. 14:18-22
    b. Balaamu, Hes. 24:2
    c. Musa anapozungumzia mataifa , Kumb. 32:8
7. Inashangaza kwamba jina lililozoeleka kwa imani juu ya Mungu mmoja wa Israeli liko katika Wingi! Ingawa hakuna uhakika, hapa zipo nadharia.
    a. Lugha ya Kiebrania ina maneno mengi yenye wingi, mara kwa mara hunatumika kuonesha msisitizo. Kwa ukaribu yanayohusiana na hili ni tabia ya kisarufi cha Kiebrania kinachoitwa "wingi wa ukuu," mahali ambapo wingi unatumika kukuza dhana.
    b. Hii inaweza kumaanisha baraza la kimalaika, ambalo Mungu hukutana nalo mbinguni na ambalo linafanya kazi za utekelezaji (kama vile I Wafalme. 22:19-23; Ayubu 1:6; Zab. 82:1; 89:5,7.
    c. Inawezekana hata inaaksi ufunuo wa Agano Jipya wa Mungu mmoja katika nafsi tatu. Katika Mwanzo. 1:1 Mungu anaumba; Mwanzo 1:2 Roho anachepusha na kutoka katika Agano Jipya Yesu ni wakala wa Baba katika Uumbaji (kama vile Yohana 1:3,10; Rum. 11:36; I Kor. 8:6; Kol. 1:15; Ebr. 1:2; 2:10).

D. YHWH

1. Hili ni jina ambalo linaaksi Uungu kama Mungu afanyaye maagano: Mungu kama mwokozi, mkombozi! Wanadamu wanavunja agano, lakini Mungu ni mwaminifu kwa neno lake, ahadi, agano (kama vile Zab. 103). Jina hili kwanza linatajwa katika munganiko pamoja na *Elohim* katika Mwanzo. 2:4. Hakuna masimulizi mawili ya uumbaji katika Mwanzo. 1-2, lakini msisitizo (1) Mungu kama muumbaji wa ulimwengu (wa kimwili) na (2) Mungu kama muumbaji maalum wa uanadamu. Mwanzo 2:4 inaanza na ufunuo maalum kuhusu nafasi ya upendeleo na kusudi la mwanadamu, pia tatizo la dhambi na uasi unaohusianishwa na nafasi ya upekee.

2. Katika Mwanzo 4:26 inasema"*wanadamu* wakaanza kuliiitia jina la BWANA" (YHWH). Hatahivyo Kutoka. 6:3 inamaanisha kwamba watu wa kwanza wa agano (wahudumu wa uzao wa kiume na familia zao) walimfahamu Mungu tu kama *El-Shaddai*. Jina YHWH linaelezewa kwa mara moja tu katika Kut. 3:13-16, hasa mstari wa 14. Hatahivyo, maandiko ya Musa mara kwa mara yanafasiri maneno kwa utani maarufu na sio kwa asili na chanzo chake (kama vile Mwanzo. 17:5; 27:36; 29:13-35). Kumekuwa na nadharia kadhaa juu ya maana ya jina hili (likichukuliwa kutoka IDB, vol. 2, kur. 409-11).
    a. kutoka katika mzizi wa kiarabu, "kuonesha upendo wa dhati"
    b. kutoka katika mzizi wa kiarabu "kupuliza" (YHWH kama Mungu wa dhoruba)
    c. kutoka katika mzizi wa lugha ya Ugariti (ya Wakanaani) "kuzungumza"
    d. kufuatia maandiko ya Ki-Foenike, KAULI SABABISHI ENDELEVU ikimaanisha "Yeye anayetosheleza," au "yeye anaye anzisha"
    e. kutoka katika muundo wa Kiebrania *Qal* "Yeye ambaye yupo," au "Yeye aliyepo sasa" (katika namna ya wakati ujao, "Yeye atakayekuwako")
    f. kutoka katika muundo wa kiebrania *Hiphil* "yeye asababishaye kuwa"
    g. kutoka katika mzizi wa Kiebrania "kuishi" (mfano Mwanzo. 3:20), maana "Mungu mmoja tu aishiye milele"
    h. kutoka katika muktadha wa Kut. 3:13-16 mbadilishano juu ya muundo wa KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU iliyotumika katika namna ya KAULI YA WAKATI ULIO TIMILIFU, "nitaendelea kuwa vile nilivyokuwa" au "nitaendelea kuwa vile ambavyo siku zote nimekuwa" (kama vile J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Old Testament*, ukurasa wa 67 Jina kamili la YHWH mara kwa mara linaelezewa katika vifupisho au yawezekana katika muundo wa asili
        (1) *Yah* (mfano Hallelu - *yah)*
        (2) *Yahu* (majina mfano Isaya)
        (3) *Yo* (majina mfano Joeli)

3. Katika Dini ya Kiyahudi ya baadaye jina la kiagano lilifanyika kuwa takatifu sana (Ni jina la kiebrania la Mungu lililofasiriwa kwa herufi nne) kwamba Wayahudi walikuwa na hofu kusema ili wasije wakavunja amri ya Kut. 20:7; Kum. 5:11; 6:13. Hivyo, alitafta mbadala wa neno la Kiebrania "mmiliki," "Mkuu," "mume," "bwana"—*adon* au *adonai* (bwana wangu). Walipofika kwa YHWH katika kusoma kwao maandiko ya Agano la Kale walitamka "bwana." Hii ndio maana YHWH inaandikwa BWANA katika fasiri za Kiingereza.
4. Kama ilivyo kwa *El*, mara kwa mara YHWH inaunganishwa na maneno mengine kusisitiza tabia fulani za Mungu wa Agano wa Israeli. Wakati kuna muunganiko mwingi wa maneno, hapa ni baadhi.
   a. *YHWH - Yireh* (YHWH atatoa ), Mwanzo. 22:14
   b. *YHWH - Rophekha* (YHWH ni mponyaji wako), Kutoka. 15:26
   c. *YHWH - Nissi* (YHWH ni bendera yangu), Kutoka. 17:15
   d. *YHWH - Meqaddishkem* (YHWH yeye awatakasaye), Kut. 31:13
   e. *YHWH - Shalom* (YHWH ni amani), Waamuzi. 6:24
   f. *YHWH - Sabbaoth* (YHWH wa majeshi), I Sam. 1:3,11; 4:4; 15:2; mara kwa mara katika manabii)
   g. *YHWH - Ro'I* (YHWH ni mchungaji wangu), Zab. 23:1
   h. *YHWH - Sidqenu* (YHWH ni haki yetu), Yer. 23:6
   i. *YHWH - Shammah* (YHWH yupo hapa), Ezek. 48:35

◙ **"'uketi mkono wangu wa kiume'"** Neno "wangu" linamrejea YHWH. Hiki kifungu chenye lugha ya kibinadamu kumrejelea Mungu (yaani., kumzungumzia Mungu kwa maneno ya kibinadamu) kilimaanisha kuonyesha nafasi ya Kimasihi ya nguvu, mamlaka, na ukuu wake. Hili lingaliaksi Mfalme wa ulimwengu akitumia kiti cha enzi na mwingine (yaani., Masihi Wake, kama vile Marko 14:62).

◙ **"'Hata niwawekapo adui zako chini ya miguu yako'"** Hili linaendeleza nukuu toka Zab. 110:1. Kifungu hiki kinatetea ushindi wa YHWH kwa niaba ya Masihi (kama vile Zaburi 2). Hii kweli inadhihirishwa zaidi katika1 Kor.15:24-27 na hata kuchukuliwa kiundani katika ufalme wa milele wa Baba katika 1 Kor. 15:28! Marko (na Mt. 22:44) inanukuu Zab. 110:1 imechepushwa toka kwenye toleo la Masoretic Hebrew text na tafasiri za maandiko ya kale ya Kiebrania (kama ilivyofanya nukuu ya Marko kwenye Kumb. 6:4-5 katika Mark 12:29-30). Matoleo la MT na LXX yana kifungu "hata nitakapowaweka adui zako chini ya miguu yako" (kama vile Luka 20:43; Mdo. 2:34-35). Waandishi (yaani., tafsiri za MSS ,א, A, L, na Vulgate na Peshitta) yalibadili nukuu ya Marko ili kuendana na nukuu za Agano la Kale.

**12:37** Hiki ndicho kilikuwa kiini cha swali. Inaonyesha kuwa (1) viongozi wa kidini hawakuweza kuelewa (yaani., kiroho walikuwa vipofu) kwenye maandiko, hata kumhusu Masihi au (2) Kristo, ingawa alikuwa mwana wa Daudi, lakini kiroho alikuwa zaidi ya Daudi na kiukweli, alikuwa Mungu tangia mwanzo. Walivyojaribu kumtega Yesu kwa maswali, hivyo akawauliza swali lililowanyamazisha. Nafikiri #2 ni jibu sahihi la kithiolojia. YHWH wa agano la Kale aliuchagua uzao wa Kimasihi tofauti na bidii za wanadamu au desturi za kitamaduni (yaani., wazee wote wa kaya walioa wanawake wasiozaa na kamwe hawakufanya wanawe wakubwa kuwa uzao uliochaguliwa)! Hili ni gumu, lakini lenye nguvu, likithibitisha kuwa Masihi atakuwa mkuu kuliko Daudi (yaani., "bwana" wa Daudi au "bwana"), ambalo kiuhakika linadokeza kitendo cha Kiungu, hata mtu wa Kiungu.

◙ **"na mkutano mkubwa walikuwa wakimsikiliza kwa furaha"** Umati mkubwa ni tabia ya injili inayojirudia ya Marko. Watu wa nchi, ambao mara nyingi walikuwa wakidhihakiwa na kudharauliwa na tabaka la wasomi wa kidini (kama vile Marko 12:38-40), walifurahia pale walipomwona Yesu akipindua meza juu ya wacha Mungu jeuri akitumia mbinu zao.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 12:38-40**
**38 Akawaambia katika mafundisho yake, Jihadharini na waandishi, wapendao kutembea wamevaa mavazi marefu, na kusalimiwa masokoni, 39 na kuketi mbele katika masinagogi, na viti vya mbele katika karamu; 40 ambao hula nyumba za wajane, na kwa unafiki husali sala ndefu; hawa watapata hukumu iliyo kubwa.**

**12:38 "'waandishi wapendao'"** Uhusiano wa kimpangilio wa matukio kati ya Marko 12:25-27 na Marko 12:38-40 haujulikani. Hakika anajaribu kuwaeleza aina ile ile ya viongozi (yaani., waandishi), lakini haijulikani kama waandishi wa 35-37 wamehutubiwa au waandishi wengine wapendao kuringishia dini zao. Amini, maneno ya Yesu pia yanahusiana na Masadukayo na Mafarisayo wavaao mavazi ya kidini kujionyesha mbele za watu ili watambilike.

◙ **"'wapendao kuvaa mavazi marefu'"** Haya yanarejelea mavazi meupe ya kipekee *tallith* yakiwa na mkanda mrefu wa bluu yakivaliwa na waandishi. Sheria ya Kiyahudi inafundisha kuwa mtu anapaswa kusimama mbele za walimu wa sheria za Kiyahudi. Watu hawa walipenda aina hii ya malezi (yaani., majoho yenye muonekano wa kipekee, salamu za heshima, wawekwe sehemu nzuru wakati wa ibada, na kuwekwa sehemu za heshima wakati wa maakuli). Walikuwa na kila kitu, lakini wakamkosa Kristo!

**12:40 "'ambao hula nyumba za wajane'"** Hii yawezakuwa ni lugha ya kiistiari ikirejelea kwenye (1) mzigo wa sadaka utolewao kwa maskini ambao hawa viongozi walihitaji kuubeba au (2) kitendo cha kuwashawishi wajane kutoa urithi wao (yaani., kipato) hekaluni. Hivyo hili linarejelea mbinu za uchangishaji fedha kwa ujanja za viongozi wa kidini.

◙ **"'na kwa unafiki husali sala ndefu'"** Huomba ili wapate kuonekana kwa wengine, na hawasikiwi na Mungu. Dini zao zilikuwa ndio mwonekano wao (kama vile Isa. 29:13; Mt. 7:21-23; Col. 2:16-23), lakini hawakupata kutambua kipawa kikuu cha Mungu!

◙ **"watapata hukumu iliyo kubwa"** Imani yao ya kidini ilikuwa ndio mwonekano wao wa nje, na sio imani tendaji ya ndani ya upendo na huduma (kama vile Marko 12:28-34). Kifungu hiki chaweza kuaksi (1) kiwango cha adhabu (kama vile Mt. 10:15; 11:22,24; 18:6; 25:21,23; Luka 12:47-48; 20:47; Yakobo 3:1) au (2) utiaji chumvi wa kiistiari uliozidi (yaani., utiaji chumvi).

## MADA MAALUM: VIWANGO VYA THAWABU NA ADHABU

A. Mwitikio unaofaa na usiofaa kwa Mungu umeegemea juu ya kiwango cha maarifa ya mtu. Kiwango kidogo cha maarifa alicho nacho mtu, ndio mwitikio mdogo alionao mtu. Pia kinyumechake ni kweli (yaani. Luka 12:45).
B. Maarifa ya Mungu huja katika njia mbili za msingi
   1. uumbaji (yaani Zaburi 19; Warumi 1-2)
   2. Andiko (yaani Zaburi 19; 119; Yesu, kama alivyofunuliwa katika Agano la Kale)
C. Ushahidi wa Agano la Kale
   1. thawabu
      a. Mwa. 15:1 (mara nyingi hii inahusiana na thawabu ya kidunia, pamoja na wana)
      b. Law. 26:1-13; Kumb. 28:1-14,58-68 (utii wa agano huleta baraka)
      c. Dan. 12:3
   2. adhabu – Law. 26:14-39; Kumb. 27:15-26; 28:15-37 (kutolitii agano huleta ulaanifu) Mpangilio wa Agano la Kale wa thawabu kwa mtu, haki ya kimaagano imerekebishwa kwa sababu ya dhambi ya mwanadamu. Marekebisho haya yanaonekana katika Yakobo na Zaburi 73 (yaani,"njia mbili," yaani Kumb. 30:15,19; Zaburi 1). Agano Jipya linachochea mitazamo katokana na tendo la fikra (kama vile ile Hotuba ya huko Mlimani, Mathayo 5-7).
D. Ushahidi wa Agano Jipya
   1. thawabu (nyuma ya wokovu)
      a. Marko 9:41
      b. Mt. 5:12,46; 6:1-4,5-6,6-18; 10:41-42; 16:27; 25:14-23
      c. Luka 6:23,35; 19:11-19,25-26
   2. adhabu
      a. Marko 12:38-40
      b. Luke 10:12; 12:47-48; 19:20-24; 20:47

c. Mathayo 5:22,29,30; 7:19; 10:15,28; 11:22-24; 13:49-50; 18:6; 25:14-30
d. Yakobo 3:1

E. Kwangu mimi ufanano huu wa kipekee ambao anaunda maana itokayo katika utungo wa wimbo. Mimi sishughulikii uwasilishaji wa utungo wa wimbo hivyo huo siuelewi. Kadri nilivyoufahamu ugumu huu na utata wa mtirirko huu, muziki, na dansi, ndivyo Kadri ambavyo ningeweza kuukubali utendaji. Naamini kuwa mbingu itavijaza vikombe vyetu, lakini naamini huduma zetu za kidunia zitabainisha saizi ya kikombe. Kwa hiyo, maarifa na mwitikio wa maarifa hayo huleta matokeo ya thawabu na adhabu (yaani Mt. 16:7; Luka 12:48; 1 Kor. 3:8,14; 9:17,18; Gal. 6:7; 2 Tim. 4:14). Kuna kanuni ya kiroho—tunavuna kile tulichokopanda! Wengine hupanda vingi na kuvuna vingi (kama vile Mt. 13:8,23).
F. "Lile taji la haki" ni letu katika kazi ya Kristo iliyomalizika (kama vile 2 Tim. 4:8), lakini tambua kwambat "taji la uzima" inahusiana na uvumilivu katika majaribu (yaani Yakobo 1:12; Ufu. 2:10; 3:10-11). Lile "taji la utukufu" kwa viongozi wa ki-Kristo linahusiana na namna walivyoyaishi maisha yao (kama vile 1 Pet. 5:1-4). Paulo alifahamu kuwa ana taji isiyoharibika, lina lakini zoezi la ziada la kujitawala mweyewe (kama vile 1 Kor. 9:24-27).

Siri ya maisha ya Mkristo ni kwamba ni ya huru kweli kweli katika kazi ya Kristo iliyomalizika, lakini yatupasa kuiitikia neema ya bure katika Kristo, pia yatupasa kuitikia nguvu ya Mungu kwa maisha ya Kristo. Maisha ya Mkristo ya kimiujiza kama ulivyo wokovu, bado yatupasa kuupokea na kuutunza. Ni wa bure lakini uliogharimikia fumbo la kila kitu na pia ni siri ya thawabu na upandaji/ uvunaji.

Hatuokolewi na kazi njema, bali kwa kazi njema (yaani Efe. 2:8-10). Kazi njema ni ushahidi wa kwama tumekutana naye (yani Mathayo 7). Manufaa ya mwanadamu katika eneo la wokovu huelekea katika uharibifu, bali maisha ya Uungu yana thawabu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 12:41-44**

**41 Naye akaketi kulielekea sanduku la hazina, akatazama jinsi mkutano watiavyo mapesa katika sanduku. Matajiri wengi wakatia mengi. 42 Akaja mwanamke mmoja, mjane, maskini, akatia senti mbili, kiasi cha nusu pesa. 43 Akawaita wanafunzi wake, akawaambia, Amin, nawaambia, Huyu mjane maskini ametia zaidi kuliko wote wanaotia katika sanduku la hazina; 44 maana hao wote walitia baadhi ya mali iliyowazidi; bali huyu katika umaskini wake ametia vyote alivyokuwa navyo, ndiyo riziki yake yote pia.**

**12:41 "sanduku la hazina"** Mishnah (mapokeo ya fasihi simulizi yaliyoandikwa pamoja) (and Alfred Edersheim's *Temple,* kur. 48-49) yanasema palikuwepo na tarumbeta zenye umbo la sanduku, kila moja liliwekwa alama kwa ajili ya makusudi maalumu ya hiari, yaliyoweka katika uwanda wa wanawake. Hapajawahi kupatikana ushahidi halisi wa haya wala uthibitisho mwingine wa fasihi mbali na ule wa Mishnah katika kuwepo kwao.

**12:42 "senti mbili"** Hii kwa maana iliyo halisi ni "sarafu " (nyembamba), ikiwa na thamani ya (1/24 au 1/96) ya dinari. Ilikuwa ni sarafu ya Kiyahudi yenye thamani ndogo.

◙ **"kiasi cha nusu pesa"** Hili ni neno la Kilatini *quadrans,* ambalo lilikuwa ni sawa na *lepton*, ni sarafu ndogo ya Kirumi (1/4 ya *assarion*, ilikuwa ni sawa na 1/16 ya dinari). Yumkini Marko ndiye aliandika kitabu cha Warumi.

## MADA MAALUM: SARAFU ZILIZOTUMIKA HUKO PALESTINA NYAKATI ZA YESU

I. Sarafu za shaba
   A. *cherma* – thamani ndogo (kama vile Yohana 2:15)
   B. *chalchos* – thamani ndogo (kama vile Mt. 10:9; Marko 12:41)
   C. *assarion* –sarafu ya shaba ya Kirumi yenye thamani ya senti 1/16 ya *a dēnarius* (kama vile Mat. 10:29)
   D. *kodrantes* – Sarafu ya shaba ya Kirumi yenye thamani 1/64 ya a dēnarius (kama vile Mt. 5:26)
   E. *lepton* – sarafu ya shaba ya Kiyunani yenye thamani ipatayo 1/128 ya dēnarius (kama vile Marko 12:42; Luka 21:2)

F. quadrans/farthing – Sarafu ya shaba ya Kirumi yenye thamani ndogo

II. Sarafu za fedha

A. *arguros* ("sarafu ya fedha") – yenye thamani kubwa zaidi kuliko shaba au sarafu za shaba nyeusi (kama vile Mt. 10:9; 26:15)

B. *dēnarius* – sarafu ya fedha ya Kirumi yenye thamani na ujira wa siku (kama vile Mt. 18:28; Marko 6:37)

C. *drachmē* –sarafu ya fedha ya Kiyunani iliyo na thamani sawa na a *dēnarius* (kama vile Luka 15:9)

D. *di-drachmon* –sarafu mbili za fedha ya kiyunani ilikuwa sawa na ½ shekel ya kiyahudi (kama vile Mt. 17:24)

E. *statēr* –sarafu ya fedha yenye thamani ipatayo *dēnarii* nne (kama vile Mat. 17:27)

III. Sarafu za dhahabu – *chrusos* ("sarafu za dhahabu") – zenye thamani zaidi (kama vile Mat. 10:9)

IV. Maneno ya jumla kwa uzito wa chuma

A. *mnaa* – Latini *mina*, uzito wa chuma uliosawa na 100 *dēnarii* (kama vile Luka 19:13)

B. *talanton* – Kizio cha Kiyunani cha uzito (kama vile Mt. 18:24; 25:15,16,20,24,25,28)

1. thamani ya fedha 6,000 *dēnarii*
2. thamani ya dhahabu 180,000 *dēnari*

A. *sheqel* – uzito wa fedha ya Kiyunani katika agano la kale(yaani,4 oz., kama ile Mwa. 23:15; 37:28; Kut. 21:32)

1. *pīm* – 2/3 *shekel*
2. *beka* – ½ *shekel*
3. gerah – 1/20 shekel

Vizio vikubwa

1. *maneh* – 50 *shekels*
2. *kikkar* – 3,000 *shekels*

**12:43 "'Amini'"** Kwa maana iliyo wazi ni "amina." Angalia Mada Maalum katika Marko 3:28.

**12:44** Hii imani kamili ya huyu mwanamke inakinzana na kiburi cha waaandishi wa dini na mambo yasiyo na mpango. Wakivuna mali za wajane. Huyu mjane hutoa mali yake yote aliyonayo kwa Mungu na kumtegemea Yeye kwa imani kupata mahitaji yake. Katika utoaji, Mungu huangalia moyo wake, na sio kiasi alichotoa (kama vile 2 Kor. 8-9). Lakini pia tambua kiasi alichokuwa nacho. Utoaji, kama yalivyo matendo na maneno, yanaufunua moyo ulivyo! Angalia MADA MAALUM: MALI katika Marko 10:23.

## MASWALI YA MJADALA.

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri inamaanisha kwamba unawajibika kwatafsiri zako mwenyeweza Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Mjadala huu wa maswali unawekwa ili kukusaidia wewe kufikiri maana ya chapisho kupitia sehemu ya kitabu. Wanamaanisha kuchochea sio kumalizia.

1. Orodhesha ni nini kila kipengere kifuatacho kinasimamia kwacho katika mfano wa (12:1-12)
   a. mmiliki wa shamba la mizabibu________________________________________
   b. Mizabibu______________________________________________________
   c. Wapagazi________________________________________________________
   d. Watumwa_________________________________________________________
   e. Mwana__________________________________________________________
2. Kwa nini sehemu ya nukuu ya Zaburi 118 inastahili hapa (yaani., Marko 12:10)?
3. Ni nini umuhimu wa mifano (yaani., Marko 12:1-12) kwa taifa la Israeli (kama vile Mt. 21:43-44)? Pia angalia Rum. 9-11 kwa ajili kulinganisha maelezo.
4. Andika kwa kifupi kiini cha ukweli wa maelezo ya Kristo.
   a. Katika mtazamo wa mamlaka ya kijamii (Marko 12:13-17)
   b. Katika mtizamo wa ufufuko (Marko 12:18-27)

   c. Katika mtizamo wa sheria (Marko 12:28-34)
   d. Katika mtizamo wa jina "Mwana wa Daudi" (Marko 12:35-40)
   e. Katika mtizamo wa kutoa na kujitoa (Marko 12:41-44)
5. Je kuna kiwango cha adhabu (kama vile Marko 12:40)?

# MARKO 13

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Maangamizi ya Hekalu yaliyotabiriwa | Yesu anatabiri juu ya Kuangamizwa Kwa hekalu | Kuangamizwa Kwa Yerusalemu Kunatabiriwa | Yesu Anazungumza juu ya Maangamizi ya Hekalu | Hotuba ya Matukio ya siku za mwisho: Utangulizi |
| 13:1-2 | 13:1-2 | 13:1-2 | 13:1-2 | 13:1-2 |
| Mwanzo wa Ole | Ishara za Nyakati na mwisho wa enzi | Juu ya mwisho wa enzi | Taabu na Mateso | |
| 13:3-13 | 13:3-13 | 13:3-13 | 13:3-8 | 13:3-4 |
| | | | | Mwanzo wa Utungu |
| | | | | 3:5-8 |
| | | | 13:9-13 | 13:9-10 |
| | | | | 13:11-13 |
| Dhiki Kuu | Dhiki Kuu | | Hofu ya Kutisha | Dhiki Kuu ya Yerusalemu |
| 13:14-23 | 13:14-23 | 13:14-23 | 13:14-20 | 13:14-20 |
| | | | 13:21-23 | 13:21-23 |
| Kuja kwa Mwana wa Adamu | Kuja kwa Mwana wa Adamu | | Kuja kwa Mwana wa Adamu | Kuja kwa Mwana wa Adamu |
| 13:24-27 | 13:24-27 | 13:24-27 | 13:24-27 | 13:24-27 |
| Somo la Mtini | Mfano wa Mtini | | Somo la Mtini Huu | Wakati wa Ujio |
| 13:28-31 | 13:28-31 | 13:28-31 | 13:28-31 | 13:28-31 |
| Siku na Saa Isiyojulikana | Hakuna Aijuaye Siku au Saa | | Hakuna Ajuaye Siku au Saa | |
| 13:32-37 | 13:32-37 | 13:32-37 | 13:32-37 | 13:32 |
| | | | | Angalieni |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka "Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo wa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Vifungu vya matukio ya siku za mwisho ya Agano Jipya vinaakisi utambuzi wa unabiii wa Agano la Kale ambao uliangalia juu ya nyakati za mwisho kupitia matukio ya sasa. Yesu anaufuata mfululizo huu. Manabiii wa Agano la Kale Mika na Yeremia wanatabiri maangamizi ya Yerusalemu na hekalu kama ishara ya hukumu ya Mungu juu ya Israeli isiyoamini. Mungu angeyaita mataifa kuwahukumu watu wake na kuichukua nchi yao. Na sasa kataika Agano Jipya watu wa Mungu bado wanaendelea kutenda mambo katika hali ya kutoakuamini. Wanamkataa Masihi wake. Wataangamizwa, kandokando na mji wao na hekalu lao (yaani .,70 b.k.na Titus). Nchi yao ya Ahadi sasa wanapewa wengine (kama vile Marko12:1-12, hasa Marko 13:9, yaani. huenda ni Mataifa ya waaminio. Maagizo ya Mataifa yanaelezwa katika Marko 13:9-13).

B. Mathayo 24, Marko 13, na Luka 21 pia ni vigumu kutafsiri injili zao kwa sababu wanashughulika na maswali kadhaa kwa namna ya mfululizo.
   1. hekalu litaharibiwa lini?
   2. ishara ya kurudi kwa Masihi ni ipi?
   3. nyakati hizi zitatimia lini?

C. Aina ya matukio ya siku za mwisho ya Agano Jipya mara nyingi ni muungano wa lugha ya unabii wa kipindi cha ukimya kati ya Agano la Kale na Agano Jipya, ambayo ina utata wa makusudi na yenye muundo mkubwa wa kiishara.

D. Vifungu kadhaa katika Agano Jipya (kama vile Mt. 24, Marko 13, Luka 17 na 21, 1 na 2 Thesolanike Na Ufu) vinashughulika na Kuja kwa mara ya Pili. Vifungu hivi vinasistiza
   1. kwamba wakati halisi wa matukio haya haujulikani, lakini tukio lina uhakika wa kutukia
   2. kwamba kizazi cha mwisho moja kwa moja kitaufahamu wakati, lakini wakati maalum, wa matukio haya
   3. kwamba hili litatukia ghafla na pasipo kutarajiwa
   4. kwamba kila kizazi cha waaminio lazima kiwe chenye tabia ya kuomba, kiwe tayari, na kiwe na uaminifu kwa kazi iliyoagizwa

E. Tazamio la awali la sura hii liko juu ya ushauri wa kivitendo ( kauli shurutishi 19), si kuuchanganua wakati halisi au mtiririko wa mfululizo wa matukio ya Kuja kwa mara ya Pili.

F. Vifungu viwili ya msingi ni (1) "Jihadharini" (Marko 13:5,9,23,33) na (2) "hayana budi" (Marko 13:7,10). Hii misistizo pacha ya "kaeni tayari" na "ngojeni kwa saburi" yamewekewa ulinganifu na mafumbo mengine ya "utayari na "hayana budi."

## MADA MAALUM: UTABIRI WA AGANO LA KALE JUU YA WAKATI UJAO DHIDI YA UTABIRI WA AGANO JIPYA – Kwa nini Wakristo wana Fasiri za Kiimani Kutokana na kitabu cha Ufunuo)

Wakati wote wa kujifunza kwangu matukio ya siku za mwisho nimejifunza kwamba Wakristo wengi hawana mfuatano wa matukio ya siku za mwisho au hawataki kuukuza. Kuna baadhi ya wakristo ambao wanaweka shabaha zao au wanaamua kujikita kwenye eneo la Ukristo kwa sababu za kithiolojia, kisaikolojia au kidini. Wakristo hawa wanaonekana kuchanganyikiwa na kwa namna gani itamalizika na kwa namna fulani kukosa umaana wa injili! Waaminio hawawezi kuathiri ajenda ya Mungu ya siku za mwisho, lakini wanaweza kushiriki katika upelekaji wa injili (kama vile Mt. 28:19-20; Luka 24:47; Mdo. 1:8). Waaminio wengi wanathibitisha kuja kwa mara ya pili kwa Kristo na kupelekea kwa siku za mwisho kwa ahadi za Mungu. Matatizo ya kiufasiri yanaibuka kutoka kwa namna gani kilele hiki cha muda kitakuja kutoka katika mitazamo kadhaa ya kibiblia (Angalia Mada Maalum:Ukinzani katika Maandiko)

1. mvutano katika ya nadharia za kinabii za agano la kale na nadharia za kitume za Agano Jipya
2. mvutano kati ya hali ya kuabudu Mungu mmoja (Mungu mmoja kwa ajili ya wote) na kuchaguliwa kwa Israeli (watu maalum)
3. mvutano katika ya hali ya kipengele chenye masharti cha maagano ya kibiblia na ahadi ("ikiwa. . .ndipo") na hali isiyo na masharti ya uaminifu wa Mungu kwa ukombozi wa mwanadamu aliyeanguka
4. mvutano kati ya aina za fasihi za Mashariki ya Karibu na nadharia za magharibi za kifasihi
5. mvutano kati ya ufalme wa Mungu kwa sasa na ule wa baadaye.
6. mvutano kati ya imani katika kurudi punde kwa Kristo na imani kwamba baadhi ya matukio lazima yatokee kwanza.

Ebu kwanza tujadili mivutano hii moja baada ya nyingine

**MVUTANO WA KWANZA** (vipengele vya kijiografia, kitaifa na kikabila vya Agano la Kale dhidi ya waaminio wote katika ulimwengu)

Manabii wa Agano la Kale walitabiri kurejeshwa kwa ufalme wa Kiyahudi katika Palestina ukiwekwa kitovu Yerusalemu ambapo mataifa yote ya nchi yatakusanyika kusifu na kutumikia mtawala wa Ki-Daudi, lakini Yesu au Mitume wa Agano Jipya hawajikiti katika agenda hii. Je kwani Agano la Kale halijavuviwa (kama vile Mt. 5:17-19)? Je waandishi wa Agano jipya wameondoa sehemu muhimu za matukio ya siku za mwisho?
Kuna vyanzo kadhaa vya taarifa kuhusu mwisho wa ulimwengu:

1. manabii wa Agano la Kale (Isaya, Mika, Malaki)
2. waandishi wa siku za mwisho (kama vile Ezek. 37-39; Dan. 7-12; Zek.)
3. Kipindi kati ya kuandikwa kwa Agano la Kale na Agano Jipya, waandishi wa siku za mwisho wa kiyahudi wasio wakanoni (kama I Enoch, ambaye anaelezewa katika Yuda)
4. Yesu mwenyewe (kama vile Mt. 24; Marko 13; Luka 21)
5. maandiko ya Paulo (kama vile I Kor. 15; II Kor. 5; I The. 4-5; II The. 2)
6. maandiko ya Yohana (I Yohana na Ufunuo).

Je haya yote kwa ufasaha yanafundisha ajenda ya siku za mwisho (matukio, mpangilio wa matukio, watu)? Ikiwa sio, kwanini? Je si kwamba wote wamevuviwa (isipokuwa maandiko ya kiyahudi ya kati ya kipindi cha ukimya kati ya Agano la Kale na Agano Jipya)?
Roho alifunua kweli kwa waandishi wa Agano la Kale kwa namna na vipengle ambavyo wangeweza kuelewa. Hatahivyo kupitia ufunuo endelevu Roho amepanua dhana hizi za matukio ya siku za mwisho kwa mtazamo wa kijumla ("siri za Kristo," kama vile Efe. 2:11-3:13. Angalia Mada Maalum katika 10:7). Hii hapa ni baadhi ya mifano inayoelekeana kwa umuhimu:

1. Jiji la Yerusalemu katika Agano la Kale linatumika kama sitiari ya watu wa Mungu (Sayuni), lakini inakadiriwa

katika Agano Jipya kama neno linaloelezea ukubalifu wa Mungu wa watubuo wote na wanadamu waaminio (Yerusalemu mpya ya Ufunuo 21- 22). Upanuzi wa kithiolojia wa jiji la kibayana la kimwili katika watu wapya wa Mungu (Wayahudi na Mataifa waaminio) inaakisiwa kwa kuoneshwa mbele katika ahadi za Mungu kukomboa mwanadamu aliyeanguka katika Mwanzo 3:15, kabla hata haijakuwako Myahudi yeyote au mji mkuu wa kiyahudi. Hata wito wa Ibrahimu (kama vile Mwanzo 12:1-3) ilijumuisha Mataifa (kama vile Mwanzo 12:3; Kutoka 19:5).

2. Katika Agano la Kale adui za watu wa Mungu ni mataifa yazungukayo mataifa ya Mashariki ya Karibu ya Kale, lakini katika Agano Jipya wamepanua kwa watu wasio amini, walio kinyume na Mungu na waliovuviwa kishetani. Vita vimehamisha kutoka kijiografia, kimgogoro wa kikanda kwenda ulimwenguni kote, mgogoro wa kiulimwengu (kamavile Wakolosai).
3. Ahadi ya nchi ya ambalo ni jambo kuu sana katika Aano la Kale (Ahadi kwa mababa wa imani katika Mwanzo, kama vile Mwanzo 12:7; 13:15; 15:7,15; 17:8) sasa imekuwa kwa dunia yote. Yerusalemu mpya inashuka chini kwa dunia iliyotengenezwa upya, sio Mashariki ya Karibu tu au kutojumuisha (kama vile Ufunuo 21-22).
4. Baadhi ya mifano mingine ni dhana za kinabii za Agano la Kale zilizopanuliwa ni
   a. uzao wa daudi saa umetahiriwa kiroho(kama vile Rum. 2:28-29)
   b. watu wa agano sasa wanajumuisha Mataifa (kama vile Hos. 1:10; 2:23, akinukuu katika Warumi 9:24-26; pia Mambo ya Walawi 26:12; Kutoka 29:45, ikinukuliwa katika II Kor. 6:16-18 na Kutoka 19:5; Kumb. 14:2, ikinukuliwa katika Tito 2:14)
   c. hekalu sasa ni Yesu (kama vile Mt. 26:61; 27:40; Yohana 2:19-21) na kupitia kanisa la mahali pamoja (kama vile I Kor. 3:16) au mwamini mmoja mmoja (kama vile I Kor. 6:19)
   d. Hata Israeli na tungo zinazofunua tabia za Agano la Kale sasa zinamaanisha watu wote wa Mungu (yaani "Israeli," kama vile Rum. 9:6; Gal. 6:16, yaani "ufalme wa makuhani," kama vile I Pet. 2:5, 9-10; Ufunuo 1:6)

Nadharia ya kinabii imetimilizwa, imepanuliwa na sasa imekuwa jumuishi. Yesu na waandishi wa kitume hawawasilishi nyakati za mwisho kwa namna ile ile ya Manabii wa Agano la Kale (kama vile Martin Wyngaarden, *The Future of The Kingdom in Prophecyand Fulfillment*). Wafasiri wa kisasa wanaojaribu kulifanya nadharia ya Agano la Kale kuwa ya maana ya wazi au ya tabia ya kawaida kugeuza ufunuo katika kitabu cha kiyahudi kabisa na kulazimisha maana! Waandishi wa Agano Jipya hawawakatai manabii wa Agano la Kale lakini wanaonesha ufanyaji wao kazi wa kilele wa kiulimwengu. Hakuna mpangilio au mfumo wa kimantiki kwa matukio ya siku za mwisho ya Yesu au Paulo. Makusudi yao kimsingi ni ukombozi na sio uchungaji.
Hatahivyo, hata ndani ya Agano Jipya kuna mvutano. Hakuna mfumo wa wazi wa matukio ya siku za mwisho. Katika njia nyingi Ufunuo kwa kushangaza unatumia Maelezo ya Agano la Kale katika kuelezea mwisho badala yamafundisho ya Yesu (kama vile Mt. 24; Marko 13)! Inafuata aina ya fasihi iliyoanzisha na Ezekieli, Daniel na Zekaria lakini ilikuzwa wakati wa kipindi kati ya uandishi wa Agano la Kale na Agano Jipya (fasihi ya kiyahudi ya siku za mwisho). Hii inaweza kuwa ilikuwa nji ya Yohana kuunganisha Maaagano ya Kale na Jipya. Inaonesha utaratibu wa zama-kuu ya uasi wa kibinadamu na kujizatiti kwa Mungu katika ukombozi! Lakini lazima itambuliwe kwamba ingawa Ufunuo unatumia lugha, watu na matukio ya Agano la Kale, inafasiri kwa ufahamu na namna ya karne ya kwanza ya Rumi (kama vile Ufunuo 1:7).

**MVUTANO WA PILI** (hali ya kuabudu Mungu mmoja dhidi ya wateule wa Mungu)

Msisitizo wa kibiblia upo juu ya Mungu binafsi, kiroho, muumbaji-mkombozi (kama vile 8:10; Isa. 44:24; 45:5-7,14,18,21- 22; 46:9; Yer. 10:6-7). Upekee wa Agano la Kale katika siku zake ilikuwa hali ya kuabudu Mungu mmoja (angalia Mada Maalum: Ibada kwa Mungu mmoja).Mataifa yote yanayozunguka yalikuwa ni waabudu miungu wengi. Kuwepo kwa Mungu mmoja ni moyo wa ufunuo wa Agano la Kale (kama vile Kumb. 6:4). Uumbaji ni jukwaa kwa kusudi la ushirika kati ya Mungu na mwanadamu, waliofanywa kwa sura yake na mfano (kama vile Mwanzo1:26-27). Hatahivyo, mwanadamu aliasi, akitenda dhambi dhidi ya upendo wa Mungu, uongozi na kusudi (kama vile Mwanzo 3). Upendo wa Mungu na kusudi lilikuwa kubwa na lenye nguvu sasa na hakika alihaidi kukomboa mwanadamu aliyeanguka (kama vile Mwanzo 3:15)!
Mvutano unainuka pale ambapo Mungu anachagua kumtumia mwanadamu mmoja, familia moja, taifa moja kufikia

wanadamu waliobakia. Wateule wa Mungu wa Ibrahimu na Wayahudi kama ukuhani wa kikuhani (kama vile Kutoka 19:4-6) kulisababisha kiburi badala ya huduma, kutengwa badala ya kujumuishwa. Wito wa Mungu kwa Ibrahimu ulijumuishwa Baraka za kimakusudi kwa wanadamu wote (kama vile Mwanzo 12:3). Lazima ikumbukwe na kusisitizwa kwamba uchaguzi wa Agano la Kale ulikuwa kwa ajili ya huduma, sio wokovu. Israeli yote haijawahi kuwa sawa na Mungu, haijawahi kukombolewa kimilele kwa msingi tu wa haki yake (kama vile Yohana 8:31-59; Mt. 3:9), lakini kwa imani binafsi na utii (kama vile Mwanzo 15:6, ikinukuliwa kutoka Warumi 4). Israeli ilipoteza lengo lake (kanisa sasa ni ufalme wa kikuhani, kama vile 1:6; II Pet.2:5,9), twakibadilisha majukumu kuwa upendeleo, huduma kuwa msimamo maalum! Mungu anachagua mmoja ili achague wote.

**MVUTANO WA TATU** (maagano yenye masharti dhidi ya maagano yasiyo na masharti)

Kuna mvutano wa kithiolojia au fumbo kati ya maagano yenye masharti na yale yasiyo na masharti. Ni hakika kweli kwamba kusudi/mpango wa Mungu na ukombozi sio wa kimasharti (kama vile Mwanzo 15:12-21). Hatahivyo, mwitikio wa kimajukumu wa kibiadamu siku zote huwa ni wa kimasharti!

Ile "ikiwa. . .basi" ya utaratibu huu unatokea kote katika Agano la Kale na Agano Jipya. Mungu ni mwaminifu; mwanadamu si mwaminifu. Mvutano huu umesababisha mkanganyiko mkubwa. Wafasiri wamejifanya kuweka shabaha juu ya moja tu "pembe ya mkanganyiko," Uaminifu wa Mungu au juhudi za mwanadamu, utawala wa Mungu au utashi huru wa mwanadamu. Vyote ni vya kibiblia na ni vya muhimu (Angalia Mada Maalumaaaa;Uchaguzi/Kuamriwa kabla na Hitaji la uwiano wa Kithiolojia)

Hii inahusiana na matukio ya siku za mwisho, kwa ahadi za Mungu za Agano la Kale kwa Israeli; Hadhi yake inajumuishwa (kama vile Ezek. 36:22-38). Maagano yenye masharti na yale yasiyo na masharti yanakutana katika Kristo (kama vile Isa. 53), sio Israeli! Kilele cha uaminifu wa Mungu kinategemea ukombozi wa wote watakaotubu na kuamini, sio nani alikuwa baba yako/mama yako, sio Israeli, ni msingi wa maagano yote ya Mungu na ahadi. Ikiwa kuna maelezo ya kithiolojia katika Biblia, sio kanisa bali Israeli (kama vile Mdo. 7 na Gal. 3).

Kusudio la ulimwengu la kutangaza injili limepita kwa kanisa (kama vile Mt. 28:19-20; Luka 24:47; Mdo. 1:8). Bado ni agano la kimasharti! Hii sio kumaanisha kwamba Mungu amekataa kabisa Wayahudi (kama vile Rum. 9-11). Kuna weza kuwa kuna mahali na kusudi la siku za mwisho, kuamini Israeli (kama vile Zek 12:10).

**MVUTANO WA NNE** (nadharia ya kifasihi ya Mashariki ya Karibu dhidi ya nadharia za kimagharibi).

Aina za fasihi ni kipengele muhimu katika usahihi wa kufasiri Biblia. Kanisa limeendelea katika mazingira ya kidesturi ya kimagharibi (kiyunani). Fasihi ya mashariki zaidi ni ya kimafumbo, ya kisitiari na kiishara kuliko kuwa ya kisasa,nadharia za desturi za kifasihi za kimagharibi (angalia Mada Maalum: Fasihi ya Mashariki (ukinzani wa kibiblia)). Imejikita kwa watu, matukio na mazingira kuliko kweli ziazopendekezwa. Wakristo wamekuwa na hatia ya kutumia historia na nadharia za kifasihi kufasiri nabii za Kibiblia (zote Agano la Kale na Agano Jipya). Kila kizazi na jambo la kijiografia limetumia desturi yake, historia na ubayana wake kufasiri Ufunuo. Kila mmoja wao amekuwa na makosa! Ni kiburi kufikiria kwamba desturi za kisasa za kimagharibi ni shabaha ya unabii wa kibiblia!

Aina ya fasihi ambayo kutoka kwake mwandishi wa asili na aliyevuviwa anachagua kuandika ni mkataba wa kifasihi na mwandishi. Kitabu cha Ufunuo sio masimulizi ya kihistoria. Ni muunganiko wa barua (sura za 1-3), unabii na zaidi fasihi ya nyakati za mwisho. Ni mbaya kuifanya Biblia kusema zaidi ya kilichokusudiwa na mwandishi wa asili kama ilivyo kuifanya iseme kidogo kuliko ilivyokusudiwa! Kiburi cha wafasiri na mafundisho hata zaidi isivyokuwa sawa katika kitabu kama ufunuo.

Kanisa halijawahi kukubaliana katika fasiri sahihi ya ufunuo. Shida yangu ni kusikia na kushughulikia Biblia nzima, sio baadhi ya sehemu zilizochaguliwa. Mtazamo wa mashariki wa Biblia inawasilisha ukweli katika jozi zilizojaa mvutano. Mwenendo wetu wa magharibi kuelekea ukweli unaopendekezwa usiokatalika lakini usio na uwiano! Nafikiri inawezekana kuondoa angalau baadhi ya vizuizi katika kufasiri Ufunuo kwa kutambua makusudi yake yanayobadilika kuelekea vizazi vinavyofuata vya waaminio. Ni dhahiri kwa wafasiri wengi kwamba Ufunuo lazima ufasiriwe katika ufahamu wa siku zake wenyewe na aina yake ya fasiri. Mkabiliano wa kihistoria kwa Ufunuo lazima ushughulikiwe na wasomaji wa kwanza wangefanya na wangeelewa. Kwa namna nyingi wafasiri wa kisasa wamepoteza maana za viwakilishi vya kitabu. Msukumo mkubwa wa kwanza wa Ufunuo. Ulikuwa ni kutia moyo waamini watesekao.

Ilionesha namna Mungu anavyoshughulikia historia (kama walivyofanya manabii wa Agano la Kale); Ilikiri kwamba historia inaenda kuelekea mwisho wa uteuzi, hukumu au baraka (kama walivyofanya manabii wa Agano la Kale). Ilikiri katika muktadha wa upendo wa Mungu, uwepo, nguvu na utawala wa siku za mwisho wa kiyahudi wa karne ya kwanza!

Inafanya kazi katika njia hizihizi za kithiolojia kwa kila kizazi cha waaminio. Inachukua mahangaiko ya kiulimwengu ya jumla ya mazuri na mabaya. Maelezo ya karne ya kwanza yanaweza yakawa yamepotea kwetu lakini yasiyo na nguvu wala ukweli wa kufariji. Wakati wafasiri wanajaribu kulazimisha maelezo ya ufunuo kwenye historia ya sasa, utaratibu wa fasiri za uongo!

Inawezekana kwamba maelezo ya kitabu yanaweza kufanyika fasihi isiyo ya kawaida tena (kama ilivyokuwa katika Agano la Kale kuhusiana na kuzaliwa, kuishi na kufa kwa Kristo) kwa kizazi cha mwisho cha Waaminio kama walivyokabiliana na kuchinjwa na kiongozi mpinga-Mungu (kama vile II The.2) na desturi. Hakuna mtu anayeweza kujua kutimilizwa huku kwa kibayana kwa Ufunuo mpaka maneno ya Yesu (kama vile Mt. 24; Marko13; na Luka 21) na Paulo (kama vile I Kor. 15; I The. 4-5; na II The. 2) pia inafanyika dhahiri kihistoria. Kudhania, kufikiria na mafundisho vyote hivi sio sahihi. Fasihi ya matukio ya siku za mwisho yanaruhusu mabadiliko. Mshukuru Mungu kwa taswira na viwakilishi ambavyo vinapita masimulizi ya kihistoria! Mungu anawawala na kushughulikia mabo yake; Anatawala; Anakuja!

Fasiri nyingi za kisasa zinakosa suala la uchaguzi wa aina ya fasihi ya uwasilishaji! Wafasiri wa kisasa wa Magharibi mara kwa mara wanatafuta mfumo sahihi uliowazi wenye mantiki wa kithiolojia kuliko kuchukuliana na aina ya fasihi yenye utata, wakilishi ya kitamthilia ya matukio ya siku za mwisho. Kweli hii inaelezewa vizuri na Ralph P. Martin katika makala yake,"Approaches to New Testament Exegesis," katika kitabu *New Testament Interpretation*, kilichohaririwa na I. Howard Marshall:

"Mpaka tutakapotambua ubora wa kitamthilia wa maandiko haya na kukumbuka njia ambayo lugha inatumika kama chombo cha kuelezea ukweli wa kidini, tutakuwa tumefanya kosa kubwa sana katika uelewa wetu wa matukio ya siku za mwisho na kimakosa kujaribu kufasiri maono yake kana kwamba ni kitabu cha riwaya ya kawaida na kinachojihusisha kuelezea matukio ya kihalisia na historia inayoandikika. Kujaribu njia ya pili ni kukimbia katika kila mtindo wa matatizo ya fasiri. Zaidi sana inapelekea kwenye uharibifu wa maana ya msingi katika lugha za hadithi za kufikirika za Mungu mtawala katika Kristo na fumbo la utawala wake ambao unaunganisha uweza na upendo (kama vile 5:5,6; Simba ndiye mwana kondoo)" (ukurasa wa 235).

W. Randolph Tate katika kitabu chake *Biblical Interpretations* alisema:

"Hakuna fasihi ingine ya Biblia ambayo imesomwa kwa dhati na shauku kubwa na kwa matokeo yenye kukatisha tama kama vitabu vya matukio ya siku za mwisho. Aina hii ya fasihi ilipata shida kutokana na historia ya kimajanga ya kufasiriwa vibaya kwasababu ya kukosekana kwa uelewa wa msingi wa muundo wake wa fasihi, mpangilio na kusudi. Kwasababu ya madai yake sana ya kufunua kile ambacho karibia kinatokea, vitabu vya mwisho wa ulimwengi vimekuwa vinatazamwa kama mwongozo kuelekea katika kuyajua jua mambo yajayo. Kosa kubwa zaidi katika mtazamo huu ni dhana kwamba muuundo wa vitabu vya rejea ni umri wa msomaji wa sasa kuliko kuwa wa mwandishi. Huu mkabiliano usio kuwa na mwongozo wa matukukio ya siku za mwisho (hasa Ufunuo) unaifanya kazi kama vile ni namba za siri ambazo matukio ya kisasa yanaweza kutumika kutafsiria viwakilishi vya andiko. . .Kwanza, mfasiri lazima atambue kwamba vitabu vya siku za mwisho vinazungumzia jumbe zake kupitia uwakilishi wa kiishara. Kufasiri ishara kibayana wakati inapokuwa kisitiari ni kupotosha fasiri. Tatizo sio kama matukio katika za mwisho ni ni ya kihistoria. Matukio yanaweza yakawa sio ya kihistoria; yanaweza kuwa kweli yalitokea, au yatatokea lakini mwandishi anayawasilisha na kuzungumza maana zake kupitia taswira na nadharia" (ukurasa wa 137).

Kutoka katika *Dictionary of Biblical Imagery*, iliyohaririwa na Ryken, Wilhost na Longman III:

"Wasomaji wa leo mara kwa mara wanashangazwa na kuchanganywa na aina hii ya fasihi. Taswira isiyotegemewa na ya nje ya uzoefu wa ulimwengu huu. Kuichukilia Fasihi hii kwa inavyoonekana inawaacha wasomaji wengi wakikwaruza kwaruza wakiwa wamejizatiti 'nini kitatokea wakati,' hivyo kukosa kusudio la ujumbe wa maandiko ya siku za mwisho" (ukurasa wa 35).

**MVUTANO WA TANO** (ufalme wa mungu uliopo sasa lakini wa baadaye)

Ufalme wa Mungu ni wa sasa na ni wa baadaye. Hili fumbo la kithiolojia linafanyika shabaha katika hatua ya matukio

ya siku ya mwisho. Ikiwa mtu atategemea kutimilizwa kwa kibayana kwa nabii zote za Agano la Kale kwa Israeli hivyo ufalme wa Mungu zaidi unafanyika urejesho wa Israeli kwenye eneo lao la kijiografia na utawala wa kabla wa kithiolojia! Hii ingepelekea kwamba Kanisa kwa siri linanyakuliwa katika sura ya 5 na sura zilizosalia zinahusiana na Israeli (lakini angalia dokezo katika Ufunuo 22:16).

Hatahivyo ikiwa shabaha ipo katika ufalme kuanzishwa na Masihi anayetabiriwa katika Agano la Kale, alafu lipo na kuja kwa mara ya kwanza kwa Kristo na alafu inaweka shabaha kwenye kufanyika mwili, maisha, mafundisho, kifo na kufufuka kwa Kristo. Msisitizo wa kithiolojia upo katika wokovu wa sasa.

Ufalme umekuja, Agano la Kale limetimilizwa katika kujitoa kwa wokovu kwa Kristo kwa wote na sio utawala wake wa Milenia na baadhi! Ni kwa kweli na hakika kwamba Biblia inazungumza juu ya ujio wote wa Kristo, lakini wapi ambapo msisitizo unawekwa? Inaonekana kwangu kwamba nabii nyingi za Agano la Kale zinalenga juu ya ujio wa kwanza, uanzishwaji wa ufalme wa Kimasihi (kama vile Danieli 2). Katika namna nyingi huu utawala wa Mungu unafananishwa na utawala wa milele wa Mungu (kama vile Danieli 7). Katika Agano la Kale shabaha ipo katika utawala wa Mungu wa milele, japo namna ya udhihirisho wa utawala huo ni huduma ya Masihi (kama vile I Kor. 15:26-27). Sio swali la nini ni kweli; vyote ni kweli lakini msisitizo upo wapi? Lazima isemwe kwamba baadhi ya wafasiri wanafanya kulenga kwenye utawala wa milenia wa Masihi (kama vile Ufunuo 20) kwamba wamekosa shabaha ya kibiblia juu ya utawala wa milele wa baba. Utawala wa Kristo ni tukio la kuanzia kama kiashiria. Kama kuja kwa mara mbili huku kwa Kristo hakukuwa dhahiri katika Agano la Kale, wala haitakuwa pia kutawala kwa muda kwa Masihi!

Msingi wa mahubiri na mafundisho ya Yesu ni ufalme wa Mungu. Ni vyote sasa (katika wokovu na huduma), na baadaye (katika utawala mkuu wa ulimwengu na nguvu). Ufunuo, ikiwa utalenga kwenye utawala wa kimasihi wa kimelenia (kama vile Ufunuo 20), itakuwa mwanzo tu na sio kilele (kama vile Ufunuo 21-22). Sio dhahiri kutoka katika Agano la Kale kwamba utawala wa muda ni mughimu; ukweli ni kwamba utawala wa Kimasihi wa Danieli 7, ni wa milele na wala sio wa ki-milenia.

**MVUTANO WA SITA** (kurudi kwa hakika kwa Kristo dhidi ya kuchelewa *Parousia*)

Waamini wengi wamefundishwa kwamba Yesu anakuja hivi karibuni, ghafla na bila taarifa (kama vile Mt. 10:23; 24:27,34,44; Marko 9:1; 13:30; Ufunuo 1:1,3; 2:16; 3:11; 22:7,10,12,20; angalia Mada Maalum:Kurudi Punde). Lakini katika kila kizazi kitarajiacho cha waamini hata hivyo kimekosea! Ukaribu (uharaka) wa kurudi kwa Yesu ni tumaini lenye nguvu lililohaidiwa kwa kila kizazi, lakini ukweli kwa mmoja tu (na yule aliyeteseka na huyo tu). Waaminio lazima waishi kama vile anarudi kesho, lakini apange na kufanyia kazi Agizo Kuu (kama vile Mt. 28:19-20) ikiwa atakawia.

Baadhi ya vifungu katika Injili na I na II Wathesalonike wamejikita katika kukawia katika Kuja kwa Mara ya Pili (*Parousia*). Kuna baadhi ya matukio ya kihistoria ambayo lazima yatokee kwanza:

1. kuhubiriwa kwa injili ulimwenguni kote (kama vile Mt. 24:14; Marko 13:10)
2. ufunuo "mwanadamu mdhambi" (kama vile Mt. 24:15; II The. 2; Ufunuo 13)
3. mateso makuu (kama vile Mt. 24:21,24; Ufunuo 13)

Kuna utata wa kimakusudi (kama vile Mt. 24:42-51; Marko 13:32-36)! Ishi kila siku kama vile ni siku yako ya mwisho lakini panga na jifunze kwa ajili ya huduma yako ya baadaye!

**MWENDELEZO NA UWIANO**

Lazima isemwe kwamba shule tofauti tofauti za fasiri za siku za mwisho zote zinajumuisha ukweli nusu. Wanaelezea na kufasiri vizuri baadhi ya maandiko. Tatizo linatokana na mwendelezo na uwiano. Mara kwa mara kuna mpangilio wa kauli za kupendekeza ambazo zinatumia maandiko ya kibiblia kujaza mafuvu yaliyowekwa kabla ya kithiolojia. Biblia haifunui mantiki, mtitiriko wa matukio na mfumo wa siku za mwisho. Iko kama albamu ya familia. Picha ni za kweli lakini siku zote hazipo katika mpangilio, katika muktadha katika mfuatano wa kimantiki. Baadhi ya picha zimeanguka kutoka kwenye albamu na vizazi vya baadaye vya ndugu wa familia hawajui hakika namna ya kuzirudisha. Msingi wa fasiri sahihi wa Ufunuo ni kusudio la mwandishi wa asili kama inavyofunuliwa katika uchaguzi wake wa ina ya fasihi anayoitumia. Wafasiri wengi wanajaribu kubeba vifaa vyao vya kutendea kazi na taratibu kutoka katika aina zingine za fasihi za Agano Jipya kwenda kwenye fasiri zao za Ufunuo. Wanaweka shabaha kwenye Agano la Kale badala ya kuruhusu mafundisho ya Yesu na Paulo kupangilia muundo wa kithiolojia na kuruhusu Ufunuo kufanya kazi kama

kielelezo.

Lazima nikiri kwamba naikabili fasiri hii juu ya Ufunuo nikiwa na baadhi ya uoga na wasiwasi si kwasababu ya laana ya Ufunuo 22:18-19, lakini ni kwasababu ya kiwango cha mkanganyiko ulioletwa na ufasiri wa kitabu hiki na kuendelea kusababisha kati ya watu wa Mungu. Napenda Ufunuo wa Mungu. Ni kweli wakati wanadamu wote wanakuwa waongo (kama vile Rum. 3:4)! Tafadhali tumia fasiri hii kama jaribio la kuamsha mawazo na sio kutoa maana ya mwisho kama kielekezi na sio mwongozo, kama "vipi ikiwa," na sio "hivyo Bwana asema." Nimekuja kugundua usio kwa uso mapungufu yangu mwenyewe, ubaguzi na ajenda ya kithiolojia. Lakini pia nimeona yale ya wafasiri wengine. Inakaribia kuonekana kwamba watu wanatafta Ufunuo kile wanachotegemea kukipata. Aina ya fasihi inajipelekea yenyewe katika matumizi mabaya!

Hata hivyo ipo katika Biblia kwa makusudi. Imewekwa katika kama hitimisho "neno" sio kwa ajali au bahati mbaya. Ina ujumbe kutoka kwa Mungu kwa watoto wake wa kila kizazi. Mungu anataka tuelewe! Tumuunge mkono, sio kutengeneza magenge; Ebu tukiri kile kilicho wazi na kilicho cha msingi na kikuu, sio yote yanaweza, yataweza au yangeweza kuwa kweli. Mungu atusaidie sisi sote!

## MADA MAALUM : FASIHI YA MATUKIO YA SIKU ZA MWISHO

Kitabu cha Ufunuo ni aina ya kipekee ya fasihi ya Kiyahudi, matukio ya siku za mwisho. Mara nyingi hii ilitumika katika nyakati zilizojaa mvutano uyakini kwamba Mungu alikuwa katika mamlaka ya historia na angeleta ukombozi kwa watu Wake. Hii aina ya fasihi inabainishwa na

1. maana nzito ya ukuu wa Mungu kiulimwengu (Mungu aliye mmoja na kuashiliwa)
2. mapambano kati ya wema na uovu, zama hizi na zama zijazo (dhana ya uwili)
3. matumizi ya mfumo wa maneno ya siri (mara nyingi kutoka Kitabu cha Agano la Kale au fasihi ya Kiyahudi ya matukio ya siku za mwisho katika Kipindi cha Agano la Kale na Agano Jipya)
4. matumizi ya rangi, namba, wanyama, wakati mwingine wanyama/wanadamu
5. matumizi ya upatanisho wa kimalaika kwa maana ya maonona ndoto, lakini mara nyingi kupitia upatanisho wa kimalaika
6. mitazamo ya mwanzo juu ya nyakati za mwisho (zama mpya)
7. matumizi ya muonekano wa ishara, si ukweli, ili kupasha habari ya nyakati za mwisho
8. Baadhi ya mifano ya hii aina hii ya fasihi ni
   a. Agano la Kale
      1) Isaya 24-27, 56-66
      2) Ezekieli 37-48
      3) Danieli 7-12
      4) Joeli 2:28-3:21
      5) Zekaria 1-6, 12-14
   b. Agano Jipya
      1) Mathayo 24, Maro 13, Luka 21, na 1 Wakorinhto 15 (katika njia nyingine)
      2) Ufunuo (sura 4-22)
   c. isiyo ya umbo- mwili (ilichukiliwa kutoka D. S. Russell, *The Method and Message of Jewish Apocalyptic,* kr. 37-38)
      1) I Enoch, II Enoch (the Secrets of Enoch)
      2) The Book of Jubilees
      3) The Sibylline Oracles III, IV, V
      4) The Testament of the Twelve Patriarchs
      5) The Psalms of Solomon
      6) The Assumption of Moses
      7) The Martyrdom of Isaiah
      8) The Apocalypse of Moses (Life of Adam and Eve)

9) The Apocalypse of Abraham
10) The Testament of Abraham
11) II Esdras (IV Esdras)
12) Baruch II, III

9. Kuna maana ya uwili katika fasifi hii. Hii inauangalia ukweli kama mtiririko wa uwili, tofauti, au mvutano (ni awaida sana katika maandiko ya Yohana) kati ya:
   a. mbingu – dunia
   b. zama za uovu (wanadamu wa uovu na malaika wa uovu) – zama mpya za wenye haki (watu wa Mungu na malaika wa Mungu)
   c. Kuwepo kwa sasa – kuwepo kwa baadaye

Hizi zote zinaelekea utimilifu ulioletwa na Mungu kumhusu Mungu. Huu si ulimwengu alioukusudia Mungu kuwa, bali Yeye azidi kutenda kazi na kuonyesha mapenzi yake kwa ajili ya urejesho wa uhusiano wa karibu ulionzia ndani ya Bustani ya Edeni. Tukio la Kristo ni mpango wa Mungu wa umwagaji maji, lakini ujio mbili unasababisha uwili wa sasa.

**MUHTASARI YAKINI UNAOHUSIANA NA MASWALI YA WANAFUNZI** (uliochukuliwa kutoka kwa E.F Bruce katika *Answers to Questions*, uk. 57)

A. Tahadhari dhidi ya kudanganywa (Marko 13:5-8)
B. Unabii wa Mateso (Marko 13:9-13)
C. Maangamizi ya Yerusalemu (Marko 13:14-23)
D. Kurudi kwa Kristo (Marko 13:24-27
E. Angalizo la kuwa macho katika hali yao ya sasa ambayo ilipelekea maangamizi ya Yerusalemu(Marko 13:28-31, yaani., kile kizazi cha Marko 13:34)
F. Angalizo la kuwa macho juu ya kurudi kwa Bwana (Marko 13:32-37; yaani., hakuna ajuaye isipokuwa Baba,Marko 13:36)
G. F. F. Bruce anaifanya Marko 13 kuwa na ufanano na muhuri sita ya kwanza ya Ufunuo 6 (kama vile uk. 57 na 138)

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 13:1-2**
[1]**Hata alipokuwa akitoka hekaluni, mmoja wa wanafunzi wake alimwambia, Mwalimu, tazama, yalivyo mawe na majengo haya!** [2] **Yesu akajibu, akamwambia, Wayaona majengo haya makubwa? Halitasalia hapa jiwe juu ya jiwe ambalo halitabomolewa.**

1**3:1"hekalu"** Hili lilikuwa neno (*hieron*) au kwa eneo zima la hekalu. Yesu alikuwa akifundisha tangu mataukio ya Marko 11 (kama vile Mt. 26:55). Haya majengo yamekuwa tumaini kuu la Wayahaudi, ishara ya pendo la pekee kwa Israeli (kama vile Yer. 7; Yohana 8:31-59).

◙**"mmoja wa wanafunzi wake"**Huyu anaweza kuwa Petro (kama vile Marko 13:3). Yohana aitwaye Marko anaweza kutupatia kumbukumbu ya Petro ya maneno ya Yesu.Huu ni mkusanyiko wa mafundisho katika Injili ya Marko.

◙**"'yalivyo mawe na majengo haya'"** Kiuhalisia hiki ni kifungu "mawe makubwa." Josephus anatwambia kuwa Herode Mkuu aliyatumia mawe makuu yenye kunakishishwa kwa chokaa au *mezzeh* ambayo yalipatikana katika eneo hili. Haya yalikuwa yenye dhiraa ya 25 x 8 x 12 (kama vile Antiquities 15.11.3). Mawe yenye maumbo ya kufanana na nyenzo zake bado zinapatikana katika ukuta humo Yerusalemu.

◙"**majengo haya**'" Kiuhalisia hiki ni kifungu "majengo makubwa." Haya yalikuwa yamenakishishwa kwa chokaa safi nyupe. Huu usanifu wa jengo hili kubwa na la thamani uliwapa Wayahaudi tumaini ambalo walikuwa wamekata juu ya

Idumean kuwa mfalme. Urejesho na upanuzi huu ulianza mnamo 20/19 b.k. na kuhitimishwa mnamo 63/64 b.k (kama vile Josephus' Antiquities15.11.1-7; *Wars* 5.5.1-6).

**13:2"'Halitasalia hapa jiwe juu ya jiwe'"**Kifungu hiki kina ukanushi mara mbili wenye dhamira tegemezi.Hakuna ukanushi yakini wa kisarufi katika lugha ya Kiyunani! Kifungu hiki kinazungumzia maangamizi ya jumla.Lazima hili liwe la kustaajabisha kwao! Josephus anatwambia kwamba mnamo 70 b.k Warumi waliliharibu eneo hili moja kwa moja na kulilima kama shamba (kama vile Mik. 3:12; Yer. 26:18). Kuna baadhi ya tofauti za machapisho yanayohusiana na kifungu hiki. Mtu anafuata upangaji wa maneno wa Mt. 24:2 unaopatikana katika herufi kubwa za machapisho ya kale ya Kiyunani א, B, L, na W. Upangaji wa pili wa maneno wa Luka 21:6 unapatikana katika MSA na Toleo la Kale la Kiyunani. Toleo la UBS[4] linaifuatisha Mt. 24:2, ambao unaongeza kielezi "hapa" au " katika hili sehemu hii."

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 13:3-8**
[3]**Hata alipokuwa ameketi katika mlima wa Mizeituni, kuelekea hekalu Petro, na Yakobo, na Yohana, na Andrea walimwuliza kwa faragha,** [4]**Tuambie, mambo hayo yatakuwa lini? Nayo ni nini dalili ya wakati, hayo yote yatakapokuwa karibu kutimia?** [5] **Yesu akaanza kuwaambia, Jihadharini, mtu asiwadanganye.** [6]**Wengi watakuja kwa jina langu, wakisema, Mimi ndiye, nao watadanganya wengi.** [7] **Nanyi mtakaposikia habari za vita na uvumi wa vita, msitishwe; hayo hayana budi kutukia, lakini ule mwisho bado.** [8]**Kwa maana taifa litaondoka kupigana na taifa, na ufalme kupigana na ufalme; kutakuwa na matetemeko ya nchi mahali mahali; kutakuwako na njaa; hayo ndiyo mwanzo wa utungu.**

**13:3"ameketi katika mlima wa Mizeituni"**Huu ukingo wa maili 2.5 ulio mashariki uliotazamwa (yaani.,yapata futi 300-400 kwa miguu) Yerusalemu na eneo la hekalu.

◙**"Petro, na Yakobo, na Yohana, na Andrea"** Ni injili ya Marko pekee yenye kutoa maelezo haya. Huenda huyu ni shahidi wa macho wa Petro aliyeandika kumbukumbu.

**13:4"'mambo hayo yatakuwa lini? Nayo ni nini dalili ya wakati, hayo yote yatakapokuwa karibu kutimia'"**Mathayo 24:3 ananukuu maswali yenye upanuzi. Kulikuwa na matukio kadhaa ambayo wanafunzi hawa walitaka kuyajua: (1) wakati wa maangamizi ya hekalu; (2) wakati wa Kuja mara ya Pili; na (3) wakati wa nyakati za mwisho. Huenda wanafunzi walifikiri kuwa matukio haya yote yangetukia kwa wakati mmoja. Tambua kuwa Yesu anayaunganisha kwa mtiririko na katika matukio ya siku za mwisho, kama manabii wa Agano la Kale walivyofanywa.

## MADA MAALUM: MAJIBU YA MASWALI MAWILI YA WANAFUNZI YAHUSIANAYO NA KURUDI KWA YESU KATIKA MATHAYO 24:3

(Na F. F. Bruce katika *Answers to Questions*, ukurasa wa 57).

Onyo dhidi ya kupotezwa na manabii wa uongo au majanga makuu kwa kufikiri kuwa huu ndiyo mwisho
1. Mt. 24:4-8
2. Marko 13:5-8
3. Luka 21:8-11

Utabiri wa mateso na ahadi kwa ajili ya msaada
1. Mt. 24:9-14
2. Marko 13:9-13
3. Luka 21:12-19

Majibu kwa swali la kwanza kuhusiana na uharibifu wa Yerusalemu na kutawanyika kwa wakazi wake
1. Mt. 24:15-28
2. Marko 13:14-23
3. Luka 21:20-24

Jibu la swali la pili ilikielezea kuja kwa Kristo
1. Mt. 24:29-31

2. Marko 13:24-27
3. Luka 21:20-24

Onyo juu ya kukesha katika hali inayoweza kupelekea kuanguka kwa Yerusalemu

1. Mt. 24:32-35
2. Marko 13:28-31
3. Luka 21:29-33

Onyo juu ya kukesha kwa ajili ya kuja kwa Kristo

1. Mt. 24:36-44
2. Marko 13:32-37
3. Luka 21:34-36

**13:5-13** "'**Jihadharini, mtu asiwadanganye**'""Jihadhari"ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Yesu anawaamuru kuzidi kuwa wavumilivu.Katika namna nyingine tamaduni za Wayahudi hawa kuhusu Masihi zilikuwa zimekwisha watenga naye.Mistari hii inataja ishara zisizo za kweli au ishara za mtesaji ambazo ziko katika kila zama. Usemi huu unarudiwa mara kwa mara (kama vile Marko 13:5,9,23,33). Kutakuwa na wengi watakaojaribu kuwadanganya kuhusiana na mambo haya.

Kila kizazi cha Wakristo kimejaribu kulazimisha historia yake ya sasa katika unabii wa kibiblia. Siku hizi wote wamekuwa waongo! Sehemu ya tatizo ni kwamba yawapasa waamini kuishi katika matarajio ya papo kwa papo ya Kuja kwa mara ya Pili, bado unabii wote ulioandikwa kuhusu matukio ya siku za mwisho yameandikwa kwa ajili ya kizazi cha waamini wateswao. Furahi kwamba haujui!

**13:6"'Wengi watakuja kwa jina langu'"**Kifungu hiki kinamrejelea Masihi (kama vile Mt. 24:11,23-24).Kumekuwa na rejea katika kitabu cha Josephus kinachojulikana kama *Wars of the Jews* 6.54 ambacho kinadai kwamba Warumi waliiharibu Yerusalemu kwa sababu ya utabiri wa manabii wa uongo, ambao uliwalaghai kwa ahadi za uongo za YHWH kuhusika katika kuiokoa Yerusalemu kwa mujibuwa nabii za Isaya (yaani , Isa. 37), lakini hawataji utabiri wa Yeremia uliojirudiarudia kuhusua kuanguka kwa Yerusalemu isiyo na imani.

◙**"'wakisema, Mimi ndiye"**' Kiuhalisia neno "Mimi" Hili ni jina la ki-Masihi lenye kutumia jina la Mungu wa agano la Agano la Kale, YHWH, kutokana na kitenzi cha Kiebrania"kuwa" (kama vile Kut. 3:12,14; Yohana 4:26; 8:24,58; 13:19; 18:5). Tazama Mada Maalum katika Marko 12:36.

◙**"'nao watadanganya wengi'"**Hizi aina za maangalizo na istilahi za kawaida katika kifasihi ya matukio ya siku za mwisho. Jambo hili linaonyesha nguvu ya ushawishi wa Masihi wa uongo na utupu wa kiroho wa mwanadamu aliyeanguka (kama vile Mt. 24:11,23-26). Pia linaonyesha unyoofu wa waamini wapya na /au Wakristo wa kimwili (kama vile 1 Kor. 3:1-3; Ebr. 5:11-14).

**13:7"'msitishwe'"** Hii ni kauli shurutishi ya wakati uliopo yenye kibainishi kanushi ambacho mara nyingi kinamaanisha kusitisha tendo ambalo liko katika mchakato.

◙**"hayo hayana budi kutukia, lakini ule mwisho bado'"**Vita na matetemeko ni ishara za nyakatai za mwisho, lakini watesaji/ishara za wakati katika kila zama (kila zama Marko 13:8,10; Mt. 24:6-8). Haya matukio ya asili ya kimachafuko si ishara ya Kuja mara ya Pili, bali maisha katika ulimwengu ulioanguka (kama vile John L. Bray, Mathayo 24 ilikamilishwa, uk. 25,28, ambayo ni uwasilishaji mzuri wa Fasiri za Matukio ya siku za mwisho za nabii za Biblia kama matukio yaliyokwisha tokea).

**13:8"'kutakuwako na njaa'"**Baadhi ya machapisho ya Kiyunani yanaongeza kifungu "na masumbufu" (kama vile MSS A,W, na NKJV). Kuna tofauti nyingine kadhaa, lakini tafsriri nyingik za Kiingereza zina kifungu "na njaa," ambacho kinapatikana katika Mt. 24:7 na MSS, א, B, na L (na MS D katika muundo fulani tofauti). Ufanano ulio katika Luka 21:11 una mambo mengine yaliyoorodheshwa. Toleo la $UBS^4$ linaupa usomaji mfupi sana daraja "B" (kuna uhakika kwa kiasi fulani).

◙**"'mwanzo wa utungu'"**Nahau kamili ni "utungu wa kuzaa" wa zama (kama vile Isa. 13:8; 26:17; Yer. 30:6-7; Mika4:9-10; Mt. 24:8; Marko 13:8; Matendo 2:24; 1 Thes. 5:3). Hiki kinaakisi imani ya Kiyahudi katika kuchochea uovu kabla ya zama mpya za haki (kama vile Marko na 13:19-20 na Book of Jubilees 23:18 sambamba na Apocalypse of Baruch 27-29). Wayahudi waliamini katika zama :zama za uovu wa sasa, zenye kubainishwa na dhambi na uasi dhidi ya Mungu, na "enzi zijazo." Enzi Mpya zingeweza kubainishwa na kuja kwa Masihi (kama vile Zaburi 2). Huu ungeweza kuwa wakati wa haki na uaminifu kwa Mungu. Japokuwa maoni ya Kiyahudi kwa namna fulani yalikuwa sawa, hayakuwa na ufafanuzi wa ujio wa mara mbili wa Masihi. Tunaishi katika zama mbili za ufalme wa Mungu ambazo zinapishana :zile "zilizokwisha kamilika" na zile ambazo "hazijakamilika".

## MADA MAALUMU: ENZI HII NA ENZI IJAYO

Manabii wa Agano la Kale waliutazama wakati ujao kama upanuzi wa wakati uliopo. Kwao wakati ujao utakuwa marejesho ya Israeli ya kijiografia. Hata hivyo, hata wao waliuona kama siku mpya (kama vile Isa. 65:17; 66:22). Kwa kwendelea kukataliwa YHWH kwa makusudi na uzao wa Abraham (hata baada ya uhamisho) ni kielelezo kiliicho dhihirika ndani ya hati ya Kiyahudi ya fasili ya mambo ya ufunuo wa matukio ya siku za mwisho (yaani, I Enoch, IV Ezra, II Baruch). Maandishi haya yanatengeneza utofauti kati ya zama hizi mbili: zama za uovu za sasa zinazomilikiwa na Shetani na zama zijazo za haki zinazomilikiwa na Roho na zilizozinduliwa na Masihi (apiganaye mwenyewe mara kwa mara).

Katika eneo hili la theolojia (hukumu, kifo na peponi) kuna maendeleo ya dhairi. Wanatheolojia wanalihita hili "ufunuo endelevu." Agano Jipya linakubaliana na ukweli huu mpya wa kiulimwengu wa zama hizi mbili (yaani, nyakati mbili

| **Yesu** | **Paulo** | **Webrania (Paulo)** |
|---|---|---|
| Mt. 12:32; 13:22,39 | Warumi 12:2 | Ebr.1:2; 6:5; 11:3 |
| Marko 10:30 | 1 Kor. 1:20; 2:6,8; 3:18 | |
| Luka 16:8; 18:30; 20:34-35 | 2 Kor. 4:4 | |
| | Wagalatia 1:4 | |
| | Efe. 1:21; 2:2,7; 6:12 | |
| | 1 Timotheo 6:17 | |
| | 2 Timotheo 4:10 | |
| | Tito 2:12 | |

Katika theolojia ya Agano Jipya zama hizi za Kiyahudi zimekuwa zikipishana kwa sababu ya tabiri zisizotarajiwa na ambazo hazikutiliwa maanani zilizohusu kuja kwa Masihi. Kuonekana kwa Yesu katika umbile la mwili kulitimiza unabii mwingi wa Agano la Kale uliohusu utambuzi wa zama mpya (Dan. 2:44-45). Hata hivyo, Agano la Kale pia liliutazama ujio Wake kama Hakimu na Mshindi, bado alikuja kwa mara ya kwanza kama Mtumishi Ateswaye (kama vile Isaya 53; Zek. 12:10), mnyenyekevu na mpole (kama vile Zekaria 9:9). Atarudi katika nguvu ile ile kama Agano la Kale liilivyotabiri (kama vile Ufunuo 19). Utimilifu wa zama hizi mbili ulisababisha Ufalme kuwepo (uliotambuliwa), lakini zile zijazo (hazijatimilika ipasavyo). Huu ni mvutano wa Agano Jipya wa uliopo tayari, lakini bado!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 13:9-13**
[9] **Nanyi jihadharini nafsi zenu; maana watawapeleka ninyi mabarazani; na katika masinagogi mtapigwa; nanyi mtachukuliwa mbele ya maliwali na wafalme kwa ajili yangu, kuwa ushuhuda kwao.** [10]**Na sharti Injili ihubiriwe kwanza katika mataifa yote.** [11]**Na watakapowachukua ninyi, na kuwasaliti, msitafakari kwanza mtakayosema, lakini lo lote mtakalopewa saa ile, lisemeni; kwa maana si ninyi msemao, bali ni Roho Mtakatifu.** [12] **Na ndugu atamsaliti ndugu yake ili auawe, na baba atamsaliti mtoto, na watoto watashambulia wazazi wao, na kuwafisha.** [13]**Nanyi mtakuwa mkichukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu; lakini mwenye kusaburi hata mwisho, ndiye atakayeokoka.**

**13:9-13** Nyenzo hii haifananishwi na Mathayo 24, bali inajitokeza katika Mt. 10:17-22. Hili linaonysha kwamba ilimpasa Yesu kurudia kweli hizi zinazofanana na juu ya matukio kadhaa au kwamba Mathayo na Marko wanaiunda nyenzo hii kwa muundo wa mada.

**13:9** "'**Nanyi jihadharini nafsi** '"Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakatai uliopo(sawa na muundo wa Marko 13:5 na 23).Kuna jambo la jukumu binafsi linalohusishwa katika maandalizi ya mateso ya matukio ya nyakati za mwisho.

◙"'**mabarazani**. . . **masinagogi**. . . **mbele ya maliwali na wafalme kwa ajili yangu**'" Kifungu "mabarazani na masinagogi," ni kifungu kinachopatikana katika Mt. 24:9, kinaonyesha mateso yatolewazo kwa Wakristo pande zote yaani ya kiserikali na kidini kwa Wakristo kwa pande zote Wayahudi na Mataifa (kama vile 1 Pet. 4:12-16).

◙**"'mabarazani'"**Huu ni muundo wa umoja wa Wakuu wa Sinagogi. Neno hili linayarejelea mabaraza ya masinagogi ya kienyeji (kama vile Kor. 11:24).

◙"'**mtapigwa**'"Kiuhalisia "mtachapwa" au "mtaumizwa" (kama vile 2 Kor. 11:24). Wayahudi waliwapiga mijeredi wahalifu mara therathini na nane—mara kumi na tatu mbele na nyuma na mara ishirini na sita mgongoni kwa mujibu wa Kut. 25:1-3.

**13:9,12** "' **kwa ajili yangu**'"Je! Waamini watateswa, si kwa madhaifu yao wenyewe au makosa ya kiraia, bali kwa sababu ni Wakristo (kama vile Mt. 5:10-16; 1 Pet. 4:12-16)?

**13:10 "'sharti Injili ihubiriwe kwanza katika mataifa yote**'"Hili neno "sharti" ni neno la Kiyunani *dei*,ambalo linamaanisha umuhimu. Yesu (au Petro au Marko, wote waliovuviwa) alikuwa akijaribu kuwaonyesha wanafunzi (1)maagizo yao kwa Mataifa (kama vile Mwa. 12:3; 1 Fal. 8:60; Isa. 42:6; 49:6; 51:4; 52:10; 60:1-3; Mt. 24:14; 28:19-20; Matendo 1:8; Rum. 11:25-27) na (2) kwamba kutakuwepo na kupanuka kwa kipindi cha wakati kati ya maangamizi ya Yerusalemu na Kuja mara ya Pili (kama vile 2 Wathesalonike 2; 2 Petro 2). Yatupasa kushikilia kwa mkazo huku kurudi kwa Bwana na ile kweli kwamba lazima mambo mengine yatokee kwanza. Kuna mkazo halisi katika Agano Jipya unaohusu wakati wa Kurudi mara ya Pili: ukaribu wa kutokea kwa matukio haya, kuchelewa, au kutojulikana.

**13:11** Roho atakuwa na waamini mara kwa mara! Roho atawawezesha waamini katikati ya mateso (kama vile Matendo 4)! Mara nyingi Roho anadhihirishwa na Yesu kama anavyofananishwa katika Luka 21:15 inavyoonyesha. Ahadi hii haiyaondoi maandalizi binafsi kwa ajili ya fursa za kila mara za mafundisho na mahubiri; hivyo, hii si ziada ya somo sahihi. Hii ni neema ya kipekee ambayo inawaruhusu waamini kutoa ushahidi wa imani katika Kristo katika kipindi cha mateso (kama vile Mt. 10:19-20; Luka 12:11-12; 21:14-15).

◙**"saa ile"**Tazama Mada Maalum: Saa katika Marko 14:35.

**13:12"'ndugu. . . ndugu'"**Familia ndiyo maisha ya Kiyahudi, lakini familia zitatengana katika Kristo (kama vile Mt. 10:21,35-37). Hii pia ni dhamira ya mara kwa mara katika maandiko ya matukio ya siku za mwisho (kama vile Jubilees 23:19 na II Baruch70:3).

**13:13"'lakini mwenye kusaburi hata mwisho, ndiye atakayeokoka'"**Hili ni fundisho la ustahimilivu (kama vile Mt. 10:22). Hili lazima lishikiliwe kataika mkazo wa mazungumzo pamoja na mafundsho yahusuyo usalama (kama vile Ufu.2:7,11,17,26; 3:5,12,21; 21:7). Tazama Mada Maalum :Hitaji la Ustahimilivu katika Marko 4:17.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 13:14-23**
**14Lakini mlionapo chukizo la uharibifu likisimama pasipolipasa, (asomaye na afahamu), ndipo walio katika Uyahudi**
**na wakimbilie milimani; 15na mtu aliye juu ya dari asishuke, wala asiingie kuchukua kitu nyumbani mwake; 16naye**
**aliye shambani asirudi nyuma kulichukua vazi lake. 17Lakini ole wao wenye mimba, nao wanyonyeshao siku hizo! 18**
**Ila ombeni yasitokee hayo wakati wa baridi. 19 Kwa maana siku hizo zitakuwa na dhiki, jinsi isivyokuwa tangu mwanzo wa kuumba alipoumba Mungu hata sasa, wala haitakuwa kamwe.**
**20Na kama Bwana asingalizikatiza siku hizo, asingeokoka mtu ye yote; lakini kwa ajili ya wateule aliowateua**
**amezikatiza siku hizo. 21Na wakati huo mtu akiwaambia, Tazama, Kristo yupo hapa, au yuko kule, msisadiki;**
**22kwa maana wataondoka Makristo wa uongo, na manabii wa uongo, watatoa ishara na maajabu, wapate**
**kuwadanganya, kama yamkini, hata hao wateule. 23Bali ninyi jihadharini; nimekwisha kuwaonya yote mbele.**
**24Lakini siku zile, baada ya dhiki hiyo, jua litatiwa giza, na mwezi hatautoa mwanga wake.**

**13:14**
**NASAB, NKJV "chukizo la uharibifu"**
**NRSV "chukizo la kimachafuko"**
**TEV "tishio lenye kuogofya"**
**JB "chikizo la kimajanga"**

## MADA MAALUM : CHUKIZO LA UHARIBIFU

M. R. Vincent anaelezea vizuri neno chukizo: "Hiki Kitenzi Mfanano, ßδελύσσμαι, kimaanisha kujihisi kichefuchefu au kupoteza hamu ya kula na hivyo kuchikizwa kwa ujumla. Katika namna ya kimaadili inaashiria jambo la kimaadili au kinyaa cha kidini (kama vile 2 Nyakati. 15:8; Yer. 13:27; Eze. 11:21; Dan. 9:27; 11:31). Inatumika sawa sawa na kuabudu sanamu katika 1 Wafalme 11:17; Kumb. 7:26; 2 Wafalme 23:13. Inaashiria chochote ambacho kutengwa na Mungu kunadhihirishwa kwenyewe, kama kula wanyawa najisi wasio safi. Law. 11:11; Kumb. 14:3; na miundo ya jumla ya kidunia. Hii namna ya kimaadili lazima isisitizwe katika matumizi ya Agano Jipya (yaani linganisha Luka 16:15; Ufunuo 17:4,5; 21:27). Haiashirii kinyaa tu cha kawaida cha kimwili cha hamu. Rejea hii hapa yawezekana inahusiana na kazi ya eneo la hekalu kutumika kwa ibada ya sanamu chini ya Warumi wakiongozwa na Titus pamoja na viwango vyao na kuweka viashiria.Josephus anasema kwamba baada ya kuchomwa kwa hekalu Warumi walizileta bendera zao na kuzisimika juy la lango la masharaiki, na walitoa dhabihu kwao, na kudai Tito, kwa vifijo, kuwa mfalme wao" (*Word Studies in the New Testament*,kr. 74-75).

Neno la Kibrania "uharibifu" (BDB 1055, KB 1640) lilimaanisha kufuru. Kifungu hiki kinatumika kataiaka Dan. 9:27, 11:31,na 12:11.

1. Kiuhalisia neno hili lilimrejelea Antiochus IV Epiphanes, ambaye alimjengea madhabahu Zeus Olympios katika hekalu lililokuwa Yerusalemu mnamo 167 k.k.na kutoa dhabihu ya nguruwe ndani ya hekalu hilo (kama vile Dan. 8:9-14; I Mak. 1:54, 59; II Mak. 6:1-2).
2. Katika Dan. 7:7-8 hili linahusiana na Wapinga Kristo wa nyakatai za mwisho (kama vile 2 The. 2:4).
3. Katika Mt. 24:15; Marko 13:14; Luka 21:20 hili linarejelea kuja kwa Generali wa Kirumi (Mfalme wa baadaye) Jeshi la Tito mnamo 70 b.k.aliyetoa dhabihu kwa majeshi yao ambayo iiapoza miungu ya kipagani, iliyoondolewa katika lango la mashariki karibia na hekalu. Hili haliwezi kurejelea kizuizi cha Yerusalemu yenyewe kwa sababu waamini wangekuwa wamechelewa sana kukiepuka.

Huu ni mfano wa kifungu kilichokuwa kikitumika katika maana kadhaa na mbalimbali, lakini che kuhusiana. Hiki kinaitwa "unabii uliotilika maradufu." Haiwezekani kukifasiri mpaka pale matukio yatakapotukia; kwa kurejea nyuma, uainishaji u dhahiri.

**NASAB "' likisimama pasipolipasa'"**
**NKJV "likisimama mahali pasipolipasa'"**

**NRSV, NJB "'likitenda pasipolipasa'"**
**TEV "'likisimama mahali lisipopasa kuwa'"**

Hii kauli endelevu ya neno likisimama ni kauli tendaji timilifu yenye kushutumu jinsi ya kiume katika *TheAnalytical Greek New Testament*naBarbara na Timothy Friberg, uk. 154 (kama vile TEV), lakini kauli tendaji isiyo na upande wo wote wakati uliopita katika*The AnalyticalLexicon to the Greek New Testament* naWilliam D. Mounce, uk.219 (kama vile NASB, NRSV, NJB). Ikiwa kauli isiyofungamana na upande wo wote, inarejelea juu ya (1) "chukizo" (*bdelugma*) au (2) juu ya jeshi la Tito (*strateuma*). Mathayo 24:15 inaongeza kifungu "likisimama Mahali Patakatifu" (yaani., Mahali Patakatifu pa hekalu), ambapo panamaanisha jinsi ya kiumena panamrejelea Generali wa Kirumi. Hii ni, hivyo, inaendana na Tito, ambaye alikuwa aliyeweka utaratibu wa Kirumi (ambao uliiwakilisha miungu yao) katika hekalu Yerusalemu.

◙"(**asomaye na afahamu**)"Hii inamaanisha "kufikiri kwa umakini " au "kufikiri vema" (kama vile 2 Tim. 2:7). Haya ni maoni yatokanayo na mwandishi wa Injli. Kwa namna iliyo dhahiri kifungu hiki kilimaanisha kuibuliwa mjadala mwingine (yaan.,Chukizo la Uharibifu kutoka Dan. 9:27; 11:31; 12:11) kuhusiana na somo hili toka kwa mtu anayesoma andiko tofauti na kundi la usomaji katika mpangilio wa kuabudu, kwa kiasi fulani ni kama madarasa yetu ya kila Jumapili.

◙**"'ndipo walio katika Uyahudi na wakimbilie milimani'"**Eusebius,historia ya kanisa toka karne ya nne, inanukuu kwamba Wakristo walikimbilia Yerusalemu hadi Pella, maili zipatazo ishirini upande wa kusini mwa Bahari ya Galilaya, kabla ya Rumi kuuzingira mji mnamo70 b.k (kama vile Hist. Muh.3:5:2-3).

**13:15 "'mtu aliye juu ya dari asishuke'"**Nyumba zilikuwa na paa za tambarare. Hizi zilitumikakama sehemu ya kusanyiko la kijamii katika majira ya miezi ya joto. Imekuwa ikisemekana kwamba mtu angetembea hadi Yerusalemu kupitia juu ya paa za nyumba.Kwa namna iliyo dhahiri nyumba nyingine zilizengwa nje ya ukuta wa mji. Majeshi yalipokuwa yakijitokeza, tendo la kuruka kwa haraka lilikuwa la muhimu.

**13:16** "'**vazi lake**'" hili lilirejelea joho la nje, ambalo pia lilitumika kama tandiko. Wanaume waliokuwa wakienda shambani wasingetembea huku wamelishikilia.

**13:17 "'ole'"**Hili neno linatumika katika Agano la Kale kutoa ainisho la unabii uhusuo hukumu. Hii ilikuwa namna ya kurejelea nyimbo za mazishi au maombolezo. Hukumu ya Mungu juu ya Yerusalemu ingewaathiri waamini pamoja na wale wasio amini (kama itakavyokuwa Dhiki Kuu).

◙**"'wenye mimba'"**Kwa usahihi kabisa kifungu hiki kinarejelea maangamizi ya Yerusalemu pekee. Kwa wanawake wenye mimba ingekuwa vigumu sana kuruka kwa haraka juu ya ukuta. Hakuna namna ya kufanya wakati wa Ujio wa mara ya Pili! Maswali ya wanafunzi hawa kwa Yesu yalihusiana na mambo matatu tofauti: maangamizi ya Yerusalemu, Kuja kwake kwa mara ya Pili, na zama za mwisho. Tatizo ni kwamba maswali haya yalihusika na mambo haya kwa wakati mmoja. Hakuna wepesi wa mgawanyo wa mstari kupitia mada tajwa.

**13:18"'wakati wa baridi'"**Safari ya haraka pia ingekuwa ngumu wakati wa baridi kwa wanawake wenye mimba na watoto wadogo.

**13:19** Hili linaweza kutazamwa kama (1) ukatili wa mateso ya zama za mwisho kwa waamini na hukumu ya Mungu juu ya wale walio amini au (2) uchochezi uliobobea. Ni vigumu kujua kama hizi rejea ndizo halisi au ni tamathari (linganisha Yoeli 2:28-32 na matumizi ya Petro katka Matendo 2, ambapo haielezwi kwa uhalisia). Agano Jipya ni kitabu cha kimashariki. Hawa walitamadunisha sana katika uchochezi na katika tamathali za semi kuliko tulivyo kama wanamashariki wa sasa. Kamwe hakuna swali liulizalo juu ya ufunuo. Hili ni swali la fasiri ya kibiblia ya kusudio asilia la mwandishi aliyevuviwa. Kulichukua Agano la Kale kwa uhalisia kila wakati na kila mahali si imani ya kibiblia, bali fasiri isiyo sahihi.Mstari huu unaweza kuwa dokezo la Dan. 12:1, lakini wenye kifungu kilichoongezwa. Walioteuliwa ni wale ambao majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima (yaani.,Wayahudi waaminio, mabaki ya kweli, na Mataifa ya waaminio, siri ya Mungu aliyefichwa, bali sasa inafunuliwa, kama vile Efe. 2:11-3:13)!

◙**"tangu mwanzo wa kuumba"**Tazama Mada Maalum katika Marko 10:6.

**13:20**Swali lenye kufasirika ni Je! matukio haya matatu (yaani, (1) kuangamizwa kwa Yerusalemu; (2)Kuja kwa Kristo; au (3) nyakati za mwisho) yanarejelea nini? Haya matukio matatu yanajadiliwa katika namna zinazopishana. Hakuna mgawanyo dhahiri na sahihi wa mstari. Kwangu mimi hili linaonekana kurejelea Kuja mara ya Pili na mwisho wa zama hizi na si maangamizi ya Yerusalemu, kwa sababu Wakristo waliuhama mji kabla ya maangamizi.

◙**"'Na kama'"**Hii ni sentensi yenye masharati daraja la pili iliyo adimu ambayo inaitwa "dhana kinzani."Hii inaeleza kigezo chenye mantiki kisicho sahihi ambacho kinatengeneza hitimisho lisilo sahihi. Kiuhalisia hii ingemaanisha "Kama Bwana hangelifupisha siku (alizoziumba) hakuna ambaye angeliokolewa (bali walikuwa hivyo)."

◙**"'Bwana'"**Lazima neno hili lilimrejelea YHWH si Yesu. YHWH ndiye ateuaye/achaguaye (kama vile Efe. 1:4).

◙**"'asingeokoka'"**Haya ni matumizi ya neno hili katika maana yake ya Agano la Kale la ukombozi wa kimwili (kama vile Yakobo 5:15), si wokovu wa kiroho.

◙**"'lakini kwa ajili ya wateule aliowateua'"**Tazama Mada Maalum hapa chini.

## MADA MAALUM : Uchaguzi/Maamuzi ya kabla na Hitaji la Usawa wa Kithiolojia

Uchaguzi ni fundisho la ajabu. Hata hivyo, si wito ulio na upendeleo, lakini ni wito kuwa njia, chombo, au njia za ukombozi kwa wengine! Katika Agano la Kale neno hilo lilitumiwa hasa kwa jili ya huduma; katika Agano Jipya linatumika hasa kwa ajili ya wokovu unaohusika katika huduma. Biblia hipatanishi kamwe kupingana kati ya Ufalme wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu, lakini inathibitisha zote mbili! Mfano mzuri wa mvutano wa kibiblia itakuwa Warumi 9 juu ya uchaguziwa Ufalme na Warumi 10 juu ya majibu muhimu ya wanadamu (kama vile.Warumi10:11,13).

Umuhimu wa huu muvatano wa kithiolojia unaweza kupatikana katika 1:4. Yesu ni mwandamu mchaguzi wa Mungu na wote ni uwezo wa kuchaguliwa ndani yake (Karl Barth). Yesu ni Mungu. Yesu "ndio" kwa mahitaji ya mwanadamu aliyeanguka (Karl Barth). Waefeso 1:4 pia husaidia kufafanua suala hilo kwa kuthibitisha kwamba lengo la majaaliwa si mbinguni tu, lakini utakatifu (mapenzi ya kristo). Mara nyingi sisi huvutiwa na faida za injili na kupuuza majukumu! Wito wa Mungu(uchaguzi) ni kwa wakati pamoja na milelel!
Mafundisho huja kuhusiana na ukweli mwingine, sio mmoja tu, ukweli usiohusiana. Hali au tabia nzuri inakuwa ni kundi dhidi ya nyota moja. Mugu hutoa ukweli katika mashariki na sio magharibi, mtindo. Hatupaswi kuondoa mvutano unaosababishwa na jozi za lahaja(fumbo la maneno) za kweli za mafundisho:

1. majaaaliwa/mchaguzi dhidi ya mapenzi huru ya mwanadamu
2. Usalama wa wanaoamini dhidi ya mahitaji ya uvumilivu
3. dhambi ya asili dhidi ya dhambi ya hiari
4. kutotenda dhambi dhidi ya kutenda dhambi kidogo
5. udhihilisho na utakaso wa papo kwa papo dhidi ya utakaso endelevu
6. Uhuru wa Kikristo dhidi ya wajibu wa Kikristo
7. Mungu anayeweza kupita uwezo wa binadamu dhidi ya Munngu wa asili
8. Mungu kama hatimaye isiyojulikana dhidi ya Mungu anayejulikana katika maandiko
9. Ufalme wa Mungu kama sasa dhidi ya kukamilishwa baadaye
10. Kutubu kama zawadi ya Mungu dhidi ya jibu muhumu la Agano la kibinadamu
11. Yesu kama Mungu dhidi ya Yesu kama mwanadamu
12. Yesu ni sawa na Mungu Baba dhidi ya Yesu wa kumtumikia Mungu Baba

Dhana ya kitheolojiaya “agano” inaunganisha Ufalme wa Mungu (ambaye daia huchukua hatua kwa kuweka mswada) pamoja na mamlaka ya mwanzo imani ya kuendelea kutubu kujibiwa kutoka kwa mwanadamu(k.v. Marko 1:15; Mdo. 3:16,19; 20:21). Kuwa mwangalifu wa maanddishi ya uthibitisho wa upande mmoja wa fumbo la

maneneo na punguza kwa mwingine! Kuwa mwangaliu wa kuthibitisha mafundisho yako ya mapenzi tu au mfumo wa thiolojia!

◙**"'asingalizikatiza siku hizo'"**Kifungu hiki kinamaanisha Mungu asiye badilika (kama vile Zab. 102:26-27; Mal. 3:6) anaweza kuibadili mipango yake!Tabia yake na makusudi yake ya ukombozi kamwe hayawezi kubadilika, bali maombi ya watu wake yanamgusa na mara kwa mara huibadili mipango yake. Hii ndiyo siri! Lakini ndiyo asili ya maombi ya kusihi.

## MADA MAALUMU: MAOMBI YA KUSIHI

I. Utangulizi
- A. Maombi ni ya muhimu kwa sababu ya mfano wa Yesu
  1. Maombi binafsi, Mk 1:35; Luka 3:21; 6:12; 9:29; 22:31-46
  2. Kulisafisha Hekalu, Mt. 21:13; Mk 11:17; Luka 19:46
  3. Maombi ya kuiga, Mt. 6:5-13; Luka 11:2-4
- B. Maombi yanaweka kuamini kwetu kwenye hali ya kugusika kwa mtu, Mungu anayejali ambaye yupo , anayependa na kutenda kwa niaba yetu na kwa ajili ya wengine, kupitia maombi yetu.
- C. Mungu binafsi amejizuia mwenyewe kutenda juu ya maombi ya watoto wake katika Nyanja nyingi (kama vile. Yakobo 4:2)
- D. Kusudi kuu la maombi ni ushirika na muda wetu kwa Mngu wa Utatu.
- E. Nafasi ya maombi ni mtu yeyote au kitu chochote kinachohusiana na waumini.Tunaweza kuomba,kuamini mara moja, au zaidi na zaidi tena kama fikra zinavyojirudia.
- F. Maombi yanaweza kuhusisha ishara/dalili mbali mbali
  1. Sifa na kuabudu kwa Mungu wa Utatu
  2. Shukrani kwa Mungu kwa ajili ya uwepo wake, ushirika, na upaji wake
  3. Ukiri wetu wa utendaji dhambi, kwa hali zote za siku zilizopita na wakati sasa
  4. Ombi la mahitaji yetu muhimu au hamu yetu
  5. Usihi wetu pale tunapoyawasilisha mahitaji ya wengine mbele za Baba
- G. Ombi la kusihi ni la ajabu. Mungu anawapenda wale tuwaombeao zaidi kuliko tufanyavyo, na bado maombi yetu yasifanye badiliko, uajibikaji, au hitaji lolote, sio tu kwetu binafsi, lakini hata kwao.

II. Taarifa za Kibiblia
- A. Agano la Kale
  1. Baadhi ya mifano ya maombi ya kusihi
     - a. Ibrahim aliomba maombi ya kuitetea Sodoma, Mwa. 18:22 na kuendelea
     - b. Maombi ya Musa kwa ajili ya Israeli
       - 1) Kutoka 5:22-23
       - 2) Kutoka 32:9-14,31-35
       - 3) Kutoka 33:12-16
       - 4) Kutoka 34:9
       - 5) Kumbu. 9:18,25-29
     - c. Samweli akiiombea Israel
       - 1) 1 Samweli 7:5-6,8-9
       - 2) 1 Samweli 12:16-23
       - 3) 1 Samweli 15:11
     - d. Maombi ya Daudi kwa ajili ya watoto wake, 2 Samweli 12:16-18
  2. Mungu anawatafuta waombeaji, Isaya 59:16
  3. Dhambi ijulikanayo, usio ikiri, tabia usizozitubia zinaathiri maombi yetu
     - a. Zaburi 66:18
     - b. Mithali 28:9
     - c. Isaya 59:1-2; 64:7

B. Agano Jipya
   1. Huduma ya kusihi/kuombea ya Mwana na Roho
      a. Yesu
         1) Warumi 8:34
         2) Waebrania 7:25
         3) 1 Yohana 2:1
      b. Roho Mtakatifu, Warumi 8:26-27
   2. Huduma ya Paulo ya kuombea kwa kusihi
      a. Akiomba kwa ajili ya Wayahudi
         1) Warumi 9:1ff
         2) Warumi 10:1
      b. Akiliombea kanisa
         1) Warumi 1:9
         2) Waefeso 1:16
         3) Wafilipi 1:3-4,9
         4) Wakolosai 1:3,9
         5) 1 Wathesolanike 1:2-3
         6) 2 Wathesolanike 1:11
         7) 2 Timotheo 1:3
         8) Filemon, uk. 4
      c. Paulo analiomba kanisa limwombee
         1) Warumi 15:30
         2) 2 Wakorinthp 1:11
         3) Waefeso 6:19
         4) Wakolosai 4:3
         5) 1 Wathesolanike 5:25
         6) 2 Wathesolanike 3:1
   3. Huduma ya kanisa ya maombi ya kusihi
      a. Kuombeana wao kwa wao
         1) Waefeso 6:18
         2) 1 Timotheo 2:1
         3) Yakobo 5:16
      b. Maombi yaliyohitajiwa na makundi maalumu
         1) Adui zetu, Mat. 5:44
         2) Wakristo watembeaji, Waebrania 13:18
         3) Watawala, 1 Timotheo 2:2
         4) wagonjwa, Yakobo 5:13-16
         5) waliorudi nyuma, 1 Yohana 5:16

III. masharti kwa ajili ya maombi yaliyotakiwa kujibiwa
   A. Mahusiano yetu kwa Yesu na Roho
      1. Kutii ndani yake, Yohana 15:7
      2. Katika jina lake , Yohana 14:13,14; 15:16; 16:23-24
      3. Katika Roho, Waefeso 6:18; Jude 20
      4. Kwa kadri ya mapenzi ya Mungu, Mathayo 6:10; 1 Yohana 3:22; 5:14-15

   B. Visababishi
      1. Kutotetereka, Mathayo 21:22; Yakobo 1:6-7
      2. Unyenyekevu na toba, Luka 18:9-14
      3. Kuomba vibaya, Yakobo 4:3
      4. Ubinafsi , Yakobo 4:2-3

C. Mitazamo mingine
   a. Usitahimilivu
   b. Luka 18:1-8
   c. Wakolosai 4:2
1. Endelea kuomba
   a. Mathayo 7:7-8
   b. Luka 11:5-13
   c. Yakobo 1:5
2. Kutoelewana nyumbani, 1 Petro 3:7
3. Kuwa huru kutoka katika dhambi zijulikanazo
   a. Zaburi 66:18
   b. Mithali 28:9
   c. Isaya 59:1-2
   d. Isaya 64:7

IV. Hitimisho la kithiolojia
   A. Ni faida ipi, fursa ipi, shughuli na uwajibikaji upi
   B. Yesu ni mfano wetu. Roho ni mwongozo wetu. Baba anasubiri kwa hamu.
   C. Inaweza kukubadilisha wewe, familia yako, rafiki zako na hata dunia

## MADA MAALUM : MIEZI AROBAINI NA MIWILI (kutoka DANIELI)

Hiki kifungu "miezi arobaini na mawili"kinabii ni sifa bainishi za kipindi cha mateso. Kutembea katika ua wa nje ni nahau izungumziayo watu wa Mungu chini ya utawala wa wale wasio amini katika vipindi tofautitofauti katika historia—Antiochus Epiphanes, Warumi wa 70 B.K, na Wapinga-Kristo wa nyakatai za mwisho.

Miezi arobaini na miwili, au usawa wake, inatajwa mara kadhaa katika Biblia. Chimbuko lake linaonekana kuwa kitabu cha Danieli.

1. Danieli 7:25; 12:7 inataja "wakati, nyakati, na nusu wakati" au siku 1277 (dhahanio "wakati" sawa na mwaka mmoja), kama vile Ufu. 12:14
2. Danieli 8:14 inataja 2300 asubuhi na jioni
3. Danieli 12:11 inataja siku 1290
4. Danieli 12:12 inataja siku 1335. Uwekaji wa kifungu cha maneno unaofanana unapatikana katika Ufu. 11:3; 12:6 (siku 1260 days) na 11:2; 13:5 (mienzi 42).

Njia nyingine ya kukiangalia kifungu hiki kilichifichika ni kukiangalia kama mfuatano : moja,mbili, lakini si tatu; hivyo, ni kiwango cha wakati kilichowekewa mipaka ki-Ungu chini ya falme za Mataifa ziwatesao watu wa Mungu. Mungu, katika kitabu cha Danieli, yu katika utawala kamili (kama vile Dan. 7:4,6,11,12,18,22,25,26,27)!

Matukio haya yanapotolewa ufafanuzi, tofauti zao zinaonekana katika kuzungumzia asili ya uwakilishi wa namba (tazama Mada Maalum: Uwakilishi wa Namba katika Maandiko), ambapo ukaribu wake wa miezi arobaini na miwili unaonekana kuonyesha kwamba ni uwakilishi wa namba wa kipindi cha mateso. Kwa kuwa tatu na nusu na nusu ya saba, inaonekana kuwa rejea ya kipindi kamili cha mateso ambayo yamekatishwa (kama vile Mt. 24:22; Marko 13:20; Luka 21:24). Mateso yamewekewa mipaka upendo wa Mungu kama hukumu.

**13:21"'akiwaambia'"**Hii ni sentensi daraja la tatu, yenye kumaanisha tendo lenye umuhimu.

**◙"'msisadiki'"**Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo yenye kibainishi hasi, ambacho mara nyingi kinamaanisha kustisha tendo lililo katika mchakato, lakini katika muktadha huu hii isingelikuwa na maana ya kawaida.

Wakristo wanahitaji kuwa wenye busara kama nyoka na kuwa wapole kama hua (kama vile Mt. 10:16). Wakristo wasiokuwa na hatia, Wakristo wanyenyekevu, Wakristo walio kama watoto wachanga wote ni wa kawaida pia. Yatupasa kuzijaribu roho (kama vile 1 Yohana 4:1) kuona kama ni watu wanaozungumza na Mungu kweli. Ni huzuni sana kwangu niwasikiapo waamini wanaabudu chini ya miti, runinga, au mahali patakatifu kwa ajili ya kumwona Yesu. Muktadha huu ni dhahiri sana! Atakapokuja wote watamwona na kumjua (kama vile Mt. 24:27). Muktadha wa papo kwa papo wa Marko 13:14-23 unawalejelea wale wanaokimbia toka Yerusalemu, si kukatishwa tamaa na mtu anayedai kuwa Kristo amejitokeza katika mji, katika eneo hili, au lile.

**13:22"'watatoa ishara na maajabu'"**Hawa wakristo wa uongo watafanya miujiza. Jihadhari juu ya utambuzi wa miujiza ya Mungu (kama vile Kut. 7:11-12,22; Kumb. 13:1 na kuendelea; Mt. 24:24; 2 The. 2:9-12; Ufu. 13:13-14). Waamini wa uongo nao wanaweza kufanya miujiza (kama vile Mt. 7:21-23).

**◙"'kama yamkini'"** Kwangu mimi inaonekana kwamba bahatisho la Marko 13:22 kimuktadha linaweza kuhusiana na tukio la Marko 13:20 (yaani.,ushurutishi wa daraja la tatu) kwa sababu wateule (kama vile Marko 13:20 and 22) hawawezi kuwekwa kando!

**13:23** Hii ilikuwa njia mojawapo za Yesu (ambayo iliaksi utabiri wa YHWH katika Agano la Kale) kuwachokonoa wafuasi wake katika kuitawala historia yake na ukombozi kwa kuyatabiri matukio yajayo. YHWH na Kristo wake huutawala wakati na historia! Hata wakati mgumu ni sehemu ya kuutekeleza mpango wake wa ukombozi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 13:24-27**
**[24] Lakini siku zile, baada ya dhiki hiyo, jua litatiwa giza, na mwezi hatautoa mwanga wake. [25]na nyota za mbinguni zitakuwa zikianguka, na nguvu zilizo mbinguni zitatikisika. [26]Hapo ndipo watakapomwona Mwana wa Adamu akija mawinguni kwa nguvu nyingi na utukufu. [27]Ndipo atakapowatuma malaika na kuwakusanya wateule wake toka pepo nne, toka upande wa mwisho wa nchi hata upande wa mwisho wa mbingu.**

**13:24 "'Lakini'"** Huu ni ukanushi wenye nguvu ambao unaonyesha kutoendelea kwenye muktadha. Mgawanyiko wa wakati umefunuliwa.

**13:24"'jua litatiwa giza'"**Hii ni lugha ya matukio ya siku za mwisho yaliyo katika Agano la Kale kuhusu nyakati za mwisho (kama vile Eze. 32:7- 8; Yoeli 2:10; 3:15; 28:3-4; Amosi 8:9; pia tazama II Esdras 5:5; Agano la Musa 10:5; na I Enoch 80:4-7). Huu ni mtiririko wa nukuu za Agano la Kale:

1. mst. wa 24 unatokana na Isa. 13:10
2. mst.wa 25 unatokana na Isa. 34:3
3. mst. wa 26 unatokana na Dan. 7:13

Bado kifungu hiki kinaweza kurejelea majanga ya asili kama mbinu za Muumbaji (kama vile 2 Pet. 3:7,10,11,12; Rum. 8:18- 22). Mara nyingi matukio ya siku za mwisho kiulimwengu yanatumika kutoa ufafanuzi wa kuanguka kwa utawala.

**13:25** Hii ni nukuu inayotokana na Isa. 34:4. Hii inaaksi imani kwamba nyota ni nguvu za kimbingu (kama vile Amu. 5:20; Ayubu 38:7).Katika fasihi ya matukio ya siku za mwisho kuanguka kwa nyota mara nyingi kunawarejelea malaika (kama vile Ufu. 8:10; 9:1; 12:4).Katika Biblia malaika ni watumishi wa Mungu, bali katika ibada za sanamu za ki-Mesopotamia hawa wanairejelea miungu ambayo huitawala hatima ya mwanadamu (yaani., ishara kumi na mbili za Zodiaki au kuzunguka kwa sayari).

**13:26 "'Mwana wa Adamu akija mawinguni'"**Utu wa Yesu na Uungu wake unasistizwa kwa neno "Mwana wa Adamu" kama linavyotumika katika Zab. 8:4; katika maana ya kawaida ya nahau ya Kiyahudi kama mwanadamu katika Eze. 2:1; na katika maana yake ya Uungu kwenye Dan. 7:13 (kama vile Marko 8:38; 13:26; 14:62 matumizi yote ya Dan. 7:13). Hii dhana kwamba huyu "Mwana wa Adamu" apaaye mawinguni inaonyesha Uungu wake (kama vile Zab. 68:4; 104:3). Mawingu ni usafiri na kifuniko cha YHWH (*Shekinah* Wingu la Utukufu wakati wa kipindi cha kutangatanga jangwani wakitoka Misri. Yesu aliondoka kupitia wingu [kama vile Matendo 1:9] na atarudi kupitia wingu [kama vile 1 The. 4:17]).

## MADA MAALUM:KUJA MAWINGUNI (maneno kadhaa ya Kiebrania , lakini zaidi *anan*, BDB 777, KB 857)

Huku kuja mawinguni ilikuwa ishara muhimu sana ya matukio ya siku za mwisho. Hii ilitumika katika Agano la Kale katika namna tatu tofauti.

1. kuonyesha uwepo wa Mungu unaoonekana, *Shekinah* wingu la Utukufu (kama vile Kut. 13:21; 14:19,20,24; 16:10; 19:9; Hes. 11:25; Neh. 9:19)
2. kuufunika utukufu wake ili mwanadamu asimwone na kufa (kama vile. Kut. 33:20; Isa. 6:5)
3. kuukuza Uungu(kama vile Zab. 18:9; 104:3; Isa. 19:1; Nah. 1:3; Matendo 1:9; 1 The. 4:17)

Katika Danieli 7:13 mawingu yalitumika kama usafiri wa ki-Ungu, Masihi mwandamu (tazama Mada Maalum: Masihi). Katika Dananieli unabii huu unadokezwa mara 30 katika Agano Jipya. Uhusiano huu na Masihi wenye kufanana na mawingu ya mbinguni unaweza kuonekana katika Mt. 24:30; 26:64; Marko 13:26; 14:62; Luka 21:27; Matendo 1:9,11; 1 The. 4:17; Ufu. 1:7.

◙ **"'nguvu nyingi na utukufu'"** Hili linaonyesha tofauti kati ya kuja mara ya kwanza (kama vile Zek. 9:9; Isa. 53) na Kuja mara ya Pili (kama vile Ufu. 19). Hili linafananishwa, lakini katika maneno tofauti, katika Mt. 24:30.

**13:27"'malaika'"**Katika 2 The. 1:7 malaika wanaitwa malaika wa Yesu. Mara nyingi wanaitwa malaika waYHWH (kama vile Yuda 14).

◙**"'kuwakusanya wateule wake'"** Hii ni lugha ya kinabii ya Agano la Kale (kama vile Kumb. 30:35; Isa. 43:6; na Zab. 50:5). Mpangilio maalum wa haya matukio halisi ya nyakati za mwisho haujulikani. Paulo anafundisha kwamba wakati wa kifo mwamini tayari anakuwa pamoja na Kristo (kama vile 2 Kor. 5:6,8). 1 The. 4:13-18 inafundisha kwamba kwa namna iliyo dhahiri kitu cho chote kinachohisiana na miili yetu, ambacho tulikiacha pale, kitaunganishwa na roho zetu kwenye ujio wa Bwana. Hii inamaanisha hali ya utengano kati ya kifo na siku ya ufufuo. Kuna mengi sana kuhusiana na matukio ya siku za mwisho na hali ya maisha baada ya kifo ambayo hayakunukuliwa katika Biblia.

◙**"'toka pepo nne, toka upande wa mwisho wa nchi hata upande wa mwisho wa mbingu'"**Kifungu hiki kinamaanisha ulimwengu wote kumfata Yesu! Pia kinamaanisha kipindi kirefu cha wakati cha kuenezwa injili. Namba nne katika Biblia ni ishara ya kiulimwengu. Hiki kinazirejelea pande nne za ulimwengu (Isa. 11:12), pepo manne za mbinguni (Dan. 7:2; Zek. 2:6), na miisho mine ya mbinguni (Yer. 49:36). Wateule watakusanywa popote pale walipotawanyikia.

## MADA MAALUM : UWAKILISHI WA NAMBA KATIKA MAANDIKO

A. Namba fulani zilitenda kazi maeneo yote kama tarakimu na ishara.

1. Moja – Mungu (yaani, Kumb. 6:4; Efe. 4:4-6)
2. Nne – dunia nzima (yaani, pembe nne, nchinne za dunia, yaani, Isa. 11:12; Yer. 49:36; Dan. 7:2; 11:4; Zek. 2:6; Mt. 24:31; Marko 13:27; Ufu. 7:1)
3. Sita – kutokamilika kwa mwanadamu (moja chini ya 7, m.f, Ufu. 13:18)
4. Saba – itimilifu wa Kiungu (siku saba za uumbaji). Tambua matumizi ya kiishara katika Ufunuo:
   a. vinara vya taa saba, Ufu. 1:12,20; 2:1
   b. nyota saba, Ufu. 1:16,20; 2:1
   c. makanisa saba, Ufu. 1:20
   d. Roho saba za Mungu, Ufu. 3:1; 4:5; 5:6
   e. taa saba, Ufu. 4:5
   f. Mihuri saba, Ufu. 5:1,5
   g. pembe saba na macho saba, Ufu. 5:6

h. malaika saba, Ufu. 8:2,6; 15:1,6,7,8; 16:1; 17:1
i. baragumu saba, Ufu. 8:2,6
j. nghurumo saba, Ufu. 10:3,4
k. elfu saba, Ufu. 11:13
l. vichwa saba, Ufu. 13:1; 17:3,7,9
m. mapigo saba, Ufu. 15:1,6,8; 21:9
n. vitasa saba, Ufu. 15:7; 21:9
o. wafalme saba, Ufu. 17:10

5. Kumi– ukamilifu
    a. matumizi katika Injili
        1) Mt. 20:24; 25:1,28
        2) Marko 10:41
        3) Luka 14:31; 15:8; 17:12,17; 19:13,16,17,24,25
    b. matumizi katika Ufunuo
        1) Ufu. 2:10, siku kumi dhiki
        2) Ufu. 12:3; 17:3,7,12,16, pembe kumi
        3) Ufu. 13:1, vilemba kumi
    c. Vigawe vya kumi katika Ufunuo
        1) 144,000 = 12x12x1000, kama vile Ufu. 7:4; 14:1,3
        2) 1,000 = 10x10x10, kama vile Ufu. 20:2,3,6
6. Kumi na Mbili – ushirika wa mwanadamu
    a. Wana kujmi na wawili wa Yakobo (yaani, makabila kumina mbili ya Israeli, Mwa. 35:22; 49:28)
    b. nguzo kumi na mbili, Kut. 24:4
    c. mawe kumi mawili katika juu ya kifua cha Kuhani Mkuu, Kut. 28:21; 39:14
    d. mikate kumina miwili, ju ya meza Mahali Patakatifu (ishara ya utoaji wa Mungu wa kwa makabila kumi na mawili), Law. 24:5; Kut. 25:30
    e. Watu kumina wawili, Kumb. 1:23;
    f. mawe kum na mawili, Yos. 4:2,3,4,8,9,20
    g. mitume kumi na wawili, Mt. 10:1
    matumizi katika UJfunuo
        1) makakabila kumi na mbili elfu waliotiwa mhuri, Ufu. 7:5-8
        2) nyotakumi na mbili, Ufu. 12:1
        3) milango kumi na mikwili, malaika kumi na wawili, makabila akumi na mawili, Ufu. 21:12
        4) misingi ya mawe kumi na mawili, majina ya Mitume kumi na mawili, Ufu. 21:14
        5) Yerusalemu mpya ilikuwa Yerusalemu ilikuwa vipimo vya mraba elfu kumi na mbili, Ufunuo 21:16
        6) milango kumi na miwili ilitotengenezwa kwa lulu kumi na mbili Ufu. 21:21
        7) mti wa uzima uzaao matunda, aima kumi na mbili, Ufu. 22:2
7. Arobaini –namba za nyakati
    a. wakati mwingine ni halisi (kuhamishwa na kutangatanga nyikani, m.f. Kut. 16:35); Kumb. 2:7; 8:2
    b. inaweza kuwa halisi au ya kiishara
        1) mafuriko, Mwa. 7:4,17; 8:6
        2) Musa juu ya Mlima Sinai, Kut. 24:18; 34:28; Kumb. 9:9,11,18,25
        3) mgawanyo wa maiksha ya Musa:
        4) miaka arobaini ndani ya Misri
        5) miaka arobaini jangwani
        6) miaka arobaini ya kuiongoza Israeli
        7) Yesu alifunga siku arobaini, Mt. 4:2; Marko 1:13; Luka 4:2
    c. Tambua (kwa maana ya Upatanisho) tarakimu za wakati hii tarakimu inajitokeza katika wakati wa

uteuzi ndani ya Bibia!

8. Sabini – namba ya jumla ya watu
    a. Israeli, Kut. 1:5
    b. wazee sabini, Kut. 24:1,9
    c. matukio ya siku za mwisho, Dan. 9:2,24
    d. kundi la huduma, Luka 10:1,17
    e. msamaha (70x7), Mt. 18:22

B. Marejeo mazuri
    1. John J. Davis, *Biblical Numerology*
    2. D. Brent Sandy, *Plowshares and Pruning Hooks*

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 13 : 28-32**
**28 Kwa mtini jifunzeni mfano; tawi lake liishapo kuwa laini, na kuchanua majani, mwatambua ya kuwa wakati wa mavuno ni karibu; 29 nanyi kadhalika, myaonapo mambo hayo yanaanza, tambueni ya kuwa yu karibu milangoni. 30 Amin, nawaambieni, Kizazi hiki hakitapita, hata hayo yote yatimie. 31 Mbingu na nchi zitapita; lakini maneno yangu hayatapita kamwe. 32 Walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata malaika walio mbinguni, wala Mwana, ila Baba.**

**3:28"'mtini'"**Katika mfano huu mtini si ishara dhahiri ya taifa la Israeli kama ilivyo katika Marko11:12-14, bali ni stiari ya waamini wayafahamuyo majira ya moja kwa moja, ikiwa si wakati maalum,wa kurudi kwa Bwana. Mtini ulikuwa umechelewa kutoa matunda. Hii iliashiria majira ya kiangazi yajayo, si ya baridi.

**13:29 "'myaonapo'"**Kwa vyo vyote vile hii ni kauli tendaji elekezi au shurutishi ya wakati uliopo. Kizazi cha mwisho kitavielewa vema vifungu hivi vya kinabii.Tatizo la kanisa ni kwamba kila kizazi cha waaminio kimekuwa kikijaribu kuzilazimisha nabii katika historia yake ya sasa na utamaduni wake. Vivyo hivyo kila kizazi kimekuwa kikikosea. Kanisa hupoteza sifa za hizi tabiri zote za uongo!

◙**"'yu'"**Hakuna nomino katika andiko la Kiyunani. Hiki kitenzi "unganishi" kinaweza kuwa jinsi ya kiume au isiyo na jinsi. Kwa sababu ya Marko 13:14, hii isio na jinsi inafaa zaidi. Ikiwa ni hivyo, hili linarejelea maangamizi ya Yerusalemu.

**13:30** Huu ni ukanushi maradufu wenye nguvu ambao ni utungaji wa kisaraufi.Hii inaweza kurejelea
1. maangamizi ya Yerusalemu
2. mabadiliko (kama vile Marko 9:1)
3. ishara za Kuja mara ya Pili

Tatizo ni kwamba Yesu aliyaunganisha maswali yote (kama vile Mt. 24:3) waliyomuuliza wanafunzi katika muktadha moja,pasipo mgawanyo dhahiri kati ya matukio.

**13:31"'Mbingu na nchi zitapita'"** Hii kweli iliyo kuu imeingizwa katika lugha ya matukio ya siku za mwisho katika Agano la Kale (kama vile 2 Pet. 3:7,10). Neno la Mungu haliwezi kupita, bali uumbaji uonekanao kwamba umeharibiwa kwa dhambi ya mwanadamu utatakaswa. Hii ndiyo dhana ya mara kwa mara ya Andiko (kama vile Yos. 21:45; 23:14-15; 1 Fal. 8:56;Isa. 40:6-8; 55:8-11; Mt. 5:17-20).

**13:32"'siku ile'"**Huu ni ufupisho wa kifungu cha Agano la Kale "Siku ya Bwana" (ni cha kawaida katika Amosi na Yoeli). Hiki kinaurejelea Ujio wa mara ya Pili au siku ya hukumu (yaani.,mfuatano wa matukio=maangamizi ya Yerusalemu au matukio ya siku za mwisho =hukumu ya mwisho).

◙**"au saa ile"**Tazama Mada Maalum : Saa katika Marko 14:35.

◙"'**hakuna aijuaye. . . ila Baba**'"Kifungi hiki kinalirejelea tendo la Kuja mara ya Pili na Enzi Mpya, si juu ya maangamizi ya Yerusalemu. Kwa namna ya kipekee Yesu anaeleza kizazi kilicho katika Marko 13:30. Huu ni mstari wenye nguvu wenye kuwaogofya Wakristo kutokana na kuweka mpangilio wa siku maalum ya Kuja mara ya Pili.

## MADA MAALUMU: BABA

Agano la Kale linaanzisha neno mbadala la ndani la Mungu kama Baba. (tazama Mada Maalum: Ubaba wa Mungu):

1. Taifa la Israel daima linaelezwa kama "mwana" wa YHWH (kama vile. Hos. 11:1; Mal. 3:17)
2. Hata mwanzoni kabisa mwa kitabu cha Kumbukumbu la torati mfanano wa Mungu kama Baba umetumika (1:31)
3. Katika kumbukumbu la torati 32 Israeli inaitwa "Mwana wake" na Mungu anaitwa "Baba yako"
4. Ufananisho huu unatajwa katika Zab. 103:13 na kuendelea katika Zab. 68:5 (baba wa yatima)
5. Lilikuwa la kawaida katika manabii (kama vile. Isa. 1:2; 63:8; Israeli kama mwana, Mungu kama Baba, 63:16; 64:8; Yer. 3:4, 19; 31:9).

Yesu alizungumza Kiaramu, ikimaanisha kuwa kuna sehemu nyingi ambapo "Baba" anaonekana, ni *Pater* yule wa Kiyunani, na linaweza kuwa linaakisi neno *Abba* la Kiaramu (kama vile. Marko 14:36). Neno hili la kawaida "Baba" au "Papa" linaonyesha ukaribu uliopo wa Yesu na Baba. Udhihilisho wake huu kwa wafuasi wake pia kunahamasisha ukaribu wetu na Baba. Neno "Baba" lilitumika kidogo sana katika Agano la Kale kwa YHWH, lakini Yesu analitumia daima na kwa kulieneza. Ni uthibitisho mkubwa wa uhusiano mpya wa Waamini na Mungu kupitia kwa Kristo (kama vile. Mathayo 6:9)

◙"'**hata malaika walio mbinguni**'"Malaika wanatazamwa kama waangalizi wa Mungu pale anaposhughulika na mwanadamu (kama vile 1 Kor. 4:9; Efa. 2:7; 3:10; 1 Pet. 3:12). Ijapokuwa wako pamoja na Mungu, hawailewi mipango yake moja kwa moja. Katika Kristo haya makusudi ya milele yanafanana kuwa ushahidi!

◙"'**wala Mwana**'"Huu uhaba wa taarifa kwa uwazi unaonyesha utu kamili wa Yesu. Yesu, ingawa ni mtu kamili na Mungu kamili, aliiacha sifa ya Uungu wake huko mbinguni pale alipotwaa umbo la mwili (kama vile Fil. 2:7). Hii mipaka iliendelea kuwepo hadi baada ya kupaa kwake.

Matumizi ya Yesu ya neno "Mwana" kujielezea mwenyewe kunadhihirisha uelewa wake mwenyewe (yaani ., YHWH ndiye Baba, Aliye teuliwa, Mwana wa Kimasihi). Haya ni matumizi adimu ya neno "Mwana "lenye kumaanisha "Mwana wa Baba" (yaani.,Mungu). Mara nyingi Yesu alijirejelea kama "Mwana wa Adamu," bali kifungu hiki kingekuwa kimeeleweka kwa wasikilizaji kama "nafsi ya mwanadamu" isipokuwa pale ambapo wangeyafahamu matumizi yake maalum katika Dan. 7:13. Bali, Dini ya Kiyahudi haikusistiza juu ya andiko na kichwa habari cha Agano la Kale.

Hiki kifungu "wala Mwana" hakikuhusishwa katika Mt. 24:36 wala katika herufi kubwa za machapisho ya Kiyunani א[a], K, L, W. Hiki kimejumuishwa katika tafsiri nyingi kwa sababu kinajitokeza katika machapisho א , B na D, Muungano wa Injili nne kama simulizi la aina moja, na maandiko ya Kiyunani yaliyojulikana kwa Irenaeus, Origen, Chrysostom, na machapisho ya Kilatini cha kale yaliyotumiwa na Jerome. Hii inaweza kuwa moja ya maandiko yaliyoboreshwa na maandishi ya imani nyingine ili kuweka msistizo juu ya Uungu wa Kristo dhidi ya walimu wa uongo (Tazama Bart D. Ehrman's *The Orthodox Corruption of Scripture,* Oxford University Press, 1993, uk. 91-92).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 13:33-37**

**[33]Angalieni, kesheni, [ombeni], kwa kuwa hamjui wakati ule utakapokuwapo. [34] Mfano wake ni kama mtu mwenye kusafiri, ameiacha nyumba yake, amewapa watumwa wake amri, na kila mtu kazi yake, naye amemwamuru bawabu akeshe. [35]Kesheni basi, kwa maana hamjui ajapo bwana wa nyumba, kwamba ni jioni, au kwamba ni usiku wa manane, au awikapo jimbi, au asubuhi; [36]asije akawasili ghafula akawakuta mmelala. [37]Na hilo niwaambialo ninyi, nawaambia wote, Kesheni.**

**13:33"'Angalieni, kesheni'"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo(kama vile Marko 13:5,9,23). Yawapasa waamini kuishi katika tumaini thabiti la Kuja mara ya Pili katika Marko 13:33-37 kuna maneno mawili tofauti ya Kiyunani yanayotafsiriwa kama "kesheni":

1. *Blepōk* (mstari wa 33, kama vile Gal. 6:1)

2. *grēgoreō* (mstari wa 34,35,37, kama vile Efe. 6:18)

Katika Louw na Nida's *Greek-English Lexicon of the New Testament Based on Semantic Domains* juzuu. 1, uk. 333, maneno haya yana mwingiliano wa kimantiki wa neno "kaeni tayari" au "kesheni" kwa #1 na "jihadhari" au "jihadharini" ya #2.

Ingawa ukweli kuhusu Kuja kwa mara ya Pili ndilo litakalokuwa tendo pekee la kizazi kimoja, kila kizazi kiishicho katika tumaini thabiti la kukaribia kurudi kwa Bwana. Hili linaeleza sababu iliyowafanaya Mitume na kanisa la mwanzo kufikiri kuwa kurudi huku kulikuwa karibu. Kuchelewa kwa miaka 2000 kunashangaza, lakini maunivu ya Mungu ya na mapenzi yake kwamba asipotee hata mmoja (kama vile 1 Tim. 2:4; 2 Pet. 3:9). Yeye atalijia kanisa ili liweze kutimiza Amri Kuu (kama vile Mt. 28:19-20; Luka 24:46-47; Matendo 1:8) na ya kwamba idadi kamili ya Waaminio na Mataifa ya waaminio watakusanyika katika (kama vile Rum. 11). Huku kurudi kunashangaza kwa waamini, lakini ni majanga ya matokeo ya milele kwa wale wasioamini.

[**"ombeni]"**] Maneno haya yapo katika herufi kubwa nyingi za machapisho ya kale ya Kiyunani, zikiwemo א, A, C, K,L, W, X, lakini hayamo katika matoleo ya B na D. Haya yanaweza kuwa halisi (kama vile toleo la NKJV). Toleo la UBS[4], hata hivyo, toleo hili linaupa usomaji huu mfupi daraja "B" (kwa kiasi fulani ni yakini).

◙**"'wakati ule utakapokuwapo'"**Hili ni neno lingine la mpangilio wa wakati wa neno *chromos*, ambalo halitumiki katika Marko, bali ni neno linalotumika kumaanisha wakati upasao (*kairos*, kama vile Marko 1:15). Hili linalirejelea tukio kuu la siku za mwisho. Swali ni nini : (1) maangamizi ya Yerusalemu; (2) kuja kwa Mwan wa Adamu; au (3) kuanza kwa Enzi Mpya? Namba moja ilijitokeza mnamo.70 b.k. Namba mbili, katika maana moja, imekwisha kutokea (yaani., kutwaa umbo la kimwili na maisha ya Yesu), lakini katika maana nyingine, ni wakati ujao (yaani., kakamilishwa kwa ufalme wa Mungu katika Ujio wa mara ya Pili). Namba tatu, kama ilivyo namba mbili, kwa kiasi fulani ina maana ambayo imekwisha kutokea. Waamini wanaishi katika Zama Mpya zilizokwisha kutokea – si zile ambazo bado, Ufalme wa Mungu (kama vile Fee na Stuart's *How to Read the Bible for All Its Worth*, kr. 131-134).

**13:34 "'ni kama mtu mwenye kusafiri**'" Hii ni istilahi ya kawaida ya mafundisho mengi ya kimafumbo ya (kama vile Marko 12:1; Mt. 21:33; 25:14; Luka 15:13; 19:12; 20:9). Suala ni wakati (kama vileMarko 13:35-37). Kwa kupewa wakati wa kutosha, asili halisi ya watu hujitokeza. Kuchelewa kwa kurudi huku kunasababisha uaminifu na vipaumbele vya watu kujidhihirisha kwao. Injili ya Mathayo inayapanua maneno haya katika Mt. 24:42-51.

◙**"'kila mtu kazi yake'"**Huenda hili linahusiana na karama za Roho, zilizoorodheshwa katika Rum. 12; 1Kor. 12; na Efe. 4. Wakristo watahukumiwa (kama vile 2 Kor. 5:10), lakini kwa ajili gani? Hakika si kwa ajili ya dhambi, kwa sababu ya damu ya Yesu kusamehe dhambi zote (kama vileEbr. 9). Bila shaka Wakristo watatoa hesabu kwa Mungu kwa ajili ya utumishi wao wa injili na matumizi ya karama za kiroho.

**13:35**
**NASB "' kwamba ni jioni, au kwamba ni usiku wa manane, au awikapo jimbi, au asubuhi'"**
**NKJV "'ya kwamba jioni, ya kwamba ni usiku wa manane, awikapo jimbi, au mapambazuko'"**
**NRSV "ya kwamba asubuhi, au usiku wa manane, au jogoo, au alfajiri'"**
**TEV "'ya kwamba asubuhi aua usiku wa manane au macheo'"**
**NJB "'asubuhi, usiku wa manane, awikapo jogoo au alfajiri'"**

Kifungu hiki kinaakisi mgawanyo wa vpindi vinne vya ulinzi wa Kirumi wenye masaa matatu kila moja:

1. jioni, 6 - 9
2. usiku wa manane, 9 usiku.
3. awikapo jogoo, 12:00 a.- 3.
4. alfajiri, 3 - 6 asubuhi.

**13:37** Tazama maelezo katikaMarko 13:33.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe zaBiblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni sababu ya msingi ya sura hii?
2. Je! Mstari wa4-7 unaeleza juu ya nyakatai za mwisho?
3. Ni kwa namna gani unabii wa Danieli wa sura za 7-12 ulihusiana na Kuja kwa mara ya Pili?
4. Kwa nini Yesu alitumia lugha ya matukio siku za mwisho kama mstarai wa 24?
5. Je! Waamini wanafahamu ni lini Bwana atakuja tena?
6. Je! Kuja kwa mara ya Pili :ukaribu wa tukio hili, kuchelewa, au wakatai haujulikani?
7. Ni kwa namna gani Yesu hafahamu wakatai wa kurudi kwake?
8. Je! unatarajia kurudi kwa Yesu wakati wa kuishi kwako

# MARKO 14

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NJKV | NRSV | TEV | NJB |
| Njama za Kumuua Yesu | Njama za kumuua Yesu | Kifo cha Yesu | Njama dhidi ya Yesu | Njama za chini kwa chini dhidi ya Yesu |
| | | (14:1-15:47) | | |
| 1 4:1-2 | 14:1-2 | 14:1-2 | 1 4:1-2 | 14:1-2 |
| Kutiwa mafuta Huko Bethania | Kutiwa mafuta huko Bethania | | Yesu anatiwa mafuta huko Bethania | Kutiwa mafuta huko Bethania |
| 14:3-9 | 14:3-9 | 14:3-9 | 14:3-5<br>14:6-9 | 14:3-9 |
| Makubaliano ya Yuda kumsaliti Yesu | Yuda anakubari Kumsaliti Yesu | | Yuda anakubali kumsaliti Yesu | Yuda anamsaliti Yesu |
| 14:10-11 | 14:10-11 | 14:10-11 | 14:10-11 | 14:10-11 |
| Pasaka akiwa na Wanafunzi | Yesu asherehekea Pasaka akiwa na Wanafunzi wake | Karamu ya mwisho | Yesu anakula Pasaka na wanafunzi wake | Maandalizi kwa ajili ya karamu ya Pasaka |
| 14:12-21 | 14:12-21 | 14:12-16 | 14:12<br>14:13-15 | 14:12-16 |
| 14:16 | Usaliti wa Yuda | | | |
| | | | | watabiriwa |
| | | 14:17-21 | 14:17-18<br>14:19<br>14:20-21 | 14:17-21 |
| Uanzishaji wa Karamu ya Bwana | Yesu aanzisha karamu ya Bwana | | Karamu ya Bwana | Uanzishaji wa Ekaristi |
| 14:22-26 | 14:22-26 | 14:22-25 | 14:22 | 14:22-25 |
| | | Gethsemani | 14:23-25 | Kukana kwa Petro kwatabiriwa |
| 14:26-31 | 14:26 | 14:26-31 | | |
| Kukana kwa Petro Kwatabiriwa | Yesu atabiri Petro atamkana | | Yesu atabiri Petro atamkana | |
| 1427-31 | 14:27-31 | | 14:27-28<br>14:29<br>14:30<br>14:31a<br>14:31b | |
| Maombi ya | Maombi ya | | Yesu aomba kule | Gethsemani |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Gethsemani | Gethsemani | | Gethsemani | |
| 14:32-42 | 14:32-42 | 14:32-42 | 14:32-34<br>14:35-36<br>14:37-38<br>14:39-40<br>14:41-42 | 14:32-42 |
| Kusalitiwa na Kukamatwa kwa Yesu | Kusalitiwa na kukamatwa kule Gethsemani | | Kukamatwa kwa Yesu | Kukamatwa |
| 14:43-50 | 14:43-50 | 14:43-50 | 14:43-52<br>14:45-49<br>14:50 | 14:43-44 |
| Kijana aliyewekwa Huru | kijana aliyekuwa uchi awekwa huru | | | |
| 14:51-52 | 14:51-52 | 14:51-52 | 14:51-52 | |
| Yesu mbele ya Baraza | Yesu akabiliana na wakuu wa Sinagogi | Yesu mbele ya Kayafa | Yesu mbele ya baraza | Yesu mbele ya wakuu wa Sinagogi |
| 14:53-65 | 14:53-65 | 14:53-65 | 14:53-56<br>14:55-64<br>14:57-59<br>14:60<br>14:61<br>14:62<br>14:63-64a<br>14:64b<br>14:65 14:65 | 14:53-54 |
| Petro kumkana Yesu | Petro amukana Yesu Na kulia | | Petro amukana Yesu | kukana kwa Petro |
| 14:66-72 | 14:66-72 | 14:66-72 | 14:66-67<br>14:68<br>14:69-70a<br>14:70b<br>14:71<br>14:72 | 14:66-72 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka ”Mwongozo wa usomaji  Mzuri wa Biblia”)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu

4. N.k

## UFANANO WA VIDOKEZO VYA INJILI

A. Njama za kumuuwa Yesu katika Marko 14:1-2 ni sawa na zile za Mt. 16:1-5 na Luka 22:1-2.
B. Utiwaji mafuta kule Bethania katika Marko 14:3-9 unafanana na ule katika Mt. 16:6-13 na Yohana 12:2-8 (yumkini utiwaji mafuta mwingine katika Galilaya katika Luka 7:36-39).
C. Makubaliano ya Yuda kumsaliti Yesu katika Marko 14:10-11 yanafanana na yale ya Mt. 26:14-16 na Luka 22:3-6.
D. Siku ya Pasaka akiwa na wanafunzi katika Marko 14:12-21 inafanana na ile ya Mt. 26:17-25, Luke 22:21-23, na Yohana 13:21-30.
E. Siku ya jumuiko kwenye chakula cha Bwana katika Marko 14:22-26 inafanana na ile ya Mt. 26:26-29 na Luka 22:17-20 (kama vile 1 Kor. 11:23-26).
F. Kukana kwa Petro kulikokwisha kunenwa katika Mark 14:27-31 kunafanana na kule kulioko katika Mt. 26:31-35.
G. Maombi ya Yesu kule Gethsemani katika Marko 14:32-42 yanafanana na Mt. 26:36-46, Luke 22:39-40, na Yohana 18:1.
H. Kusalitiwa na kukamatwa kwa Yesu katika Marko 14:43-50 kunafanana na kule kwa Mt. 26:47-56, Luka 22:47-53, na Yohana 18:2-12.
I. Yesu kabla ya kupelekwa mbele ya baraza la wakuu wa Sinagogi katika Marko 14:53-65 kunafanana na kule kwa Mt. 26:57-68 na Yohana 18:12,19-24.
J. Petro kumkana Yesu katika Marko 14:66-72 kunafanana na kule kwa Mt. 26:69-75, Luke 22:54-62, na Yohana 18:15-18,25-27.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 14:1-2**
**[1] Baada ya siku mbili ilikuwa sikukuu ya Pasaka, na mikate isiyochachwa; wakuu wa makuhani na waandishi wakatafuta njia ya kumkamata kwa hila na kumwua. [2]Kwa maana walisema, Isiwe kwa wakati wa sikukuu, isije ikatokea ghasia katika watu**

**14:1 "Sikukuu ya Pasaka na mikate isiyochachwa"** Mwanzoni kabisa hizi zilikuwa ni sikukuu mbili tofauti kabisa zenye kuweka kumbukumbu ya tukio linalofanana, pigo la mwisho lilimsababisha Farao awaruhusu Waebrania kuondoka Misri. Mahitaji kwa ajili ya chakula cha sikukuu ya Pasaka yanapatikana katika Kut. 12:1-14,21-28,43-51. Utaratibu kwa ajili ya sikukuu ya mikate isiotiwa chachu katika Kut. 12:8,15-20 (kama vile Hes. 28:16-25, Kumb.
16:1-8, na *nyakati za kale* za Yusufu 3.10.5).

◙**"baada ya siku mbili"** Kwa sababu palikuwepo na sikukuu mbili zilizowekwa pamoja, wakati mwingine Wayahudi walirejelea kwenye kipindi chote kama "Sikukuu ya Pasaka." Kwa hiyo, haijulikani ikiwa hizi "siku mbili" zinamaanisha (1) zile siku mbili kabla ya sikukuu ya siku ya nane au (2) siku mbili kabla ya sikukuu yenyewe ya Pasaka. Yohana 12:1-8 inasema hili lilitokea kwenye siku ya tofauti; mstari wa 3 na kuendelea. utaratibu wa kupanga matukio ya siku za mwisho za maisha ya Yesu yameandikwa tofauti na waandishi .katika maoni yangu kanisa la mwanzo lilitambua utofauti uliopo kati ya zile injili nne, lakini hawakujaribu kulirekebisha hili. Utofauti unasababishwa na (1) asili ya ushuhuda wa macho wa maandiko na (2) makusudi ya kithiolojia/kiinjilisti kwa kila mwandishi binafsi. Kila mmoja alikuwa na uhuru (chini ya uvuvio) kuchagua, kwendana, na kupanga matukio ya Yesu na matendo ili kwendana na kusudi la kundi (kama vile Gordon Fee na Doug Stuart, *How to Read the Bible for All Its Worth*, kur. 126-129).

◙**"makuhani na waandishi"** Mathayo anaongeza "wakuu," ambao ni usanifishaji mzima kwa ajili ya wazee wa baraza la Sinagogi. Angalia Mada Maalum katika Marko 12:13.

◙**"njia ya kumkamata kwa hila na kumwua"** Hili lilikuwa sio jambo geni (kama vile Marko 3:6; 11:18), lakini matendo ya Yesu yanakubaliana na uthibitisho wa uamati wa watu kipindi kile cha shangwe pindi akiingia Yerusalemu na kipindi kile cha kulisafisha hekalu toka kwenye baraza la watu wa mataifa akifunga mauti yake kwa
wote Mafarisayo na Masadukayo.

**14:2 "isije ikatokea ghasia kwa watu"** Yesu alikuwa ni mtu aliyefahamika huko Galilaya. Kipindi cha sikukuu ya Pasaka idadai ya watu Yerusalemu iliongezeka mara tatu kuliko kawaida ikiwa na mahojaji toka maeneo yote ya Mediterrania, wengi wao wakitokea Galilaya. Uwezekano wa kuwepo na "ghasia" umetajwa katika Mt. 26:5 na 27:24.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 14:3-9**
**[3]Naye alipokuwapo Bethania, nyumbani mwa Simoni mkoma, ameketi chakulani, alikuja mwanamke mwenye kibweta cha marhamu ya nardo safi ya thamani nyingi; akakivunja kibweta akaimimina kichwani pake. [4]Palikuwa na watu waliochukizwa katika nafsi zao wakisema, Kwani kupoteza marhamu namna hii? [5]Maana marhamu hii ingaliweza kuuzwa kwa dinari mia tatu na kuzidi, wakapewa maskini. Wakamnung'unikia sana yule mwanamke.**
**[6]Yesu akasema, Mwacheni; mbona mnamtaabisha? Amenitendea kazi njema; [7]maana sikuzote mnao maskini pamoja nanyi, na kila mpendapo mwaweza kuwatendea mema; lakini mimi hamnami sikuzote. [8]Ametenda alivyoweza; ametangulia kuupaka mwili wangu marhamu kwa ajili ya maziko. [9]Amin, nawaambia, Kila ihubiriwapo Injili katika ulimwengu wote, na hili alilotenda huyu litatajwa kwa kumbukumbu lake**

**14:3 "Bethania"** Ni mji uliokuwa kwenye mwinuko uliojulikana kama Mlima wa Mizeituni, ambao haukuwa mbali na Yerusalemu, ulikuwa ni mji unaojulikana kwa ajili ya mahojaji kulala hapo kipindi cha sikukuu muhimu tatu za mwaka. Kila familia ya Kiyahudi iliyoishi jirani na Yerusalemu ililazimika kitamaduni kuwakaribisha mahojaji.

◙**"Simoni mkoma"** Katika agano la kale ukoma ulionekana kama alama ya kukataliwa na Mungu. Ilikuwa na matokeo mabaya kijamii. Mtu huyu inavyoonekana aliponywa na Yesu. Ukoma katika ulimwengu wa kale ulitokana na magonjwa mbalimbali ya ngozi (kama vile Mambo ya Walawi 13-14), sio ukoma wetu wa sasa hivi. Ufanano katika Yohana 12:2-8 unadokeza kuwa hapa palikuwa nyumbani kwa Lazaro na yule Mariam, dadake, alikuwa mwanamke. Yawezekana kuwa ni yule Simoni ambaye alikuwa ni baba yao na wale Yesu aliowaponya
kipindi cha nyuma?

◙**"ameketi chakulani"** Hawakuwa wakitumia viti, lakini wakiwa wameketi safu tatu za meza wakitengeneza umbo la mpindo, wakiwa wamekalia miguu yao.

◙**"alikuja mwanamke"** Luka 7:36-50 anaandika kuhusika kwa aina ile ile , lakini na mwana mke mwenye dhambi. Yohana 12:3 inamtaji mwanamke huyu kuwa ni Mariam, dadake Lazaro, lakini Marko yeye hataji jina. Marko, alimwandika mapema, yumkini alikuwa akiogopa kutambulika kuwa ni mwanafunzi wa Yesu, wakati Yohana, akiandika baadaye, alijisikia huru kumtaja jina lake (kama vile Lenski's *St. Mark's Gospel*). Hakika hili ni tendo la
ajabu lenye kumaanisha maziko ya Yesu.

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"kibweta"** |
| **NKJV** | **"kibweta cha kiriba"** |
| **NRSV, TEV** | |
| **NJB** | **"kibweta cha mtungi"** |

Hiki ni chombo kilichotengenezwa kwa jiwe lisilopenyeza nuru kikiwa kimefungwa juu toka Alabastron, mji ulioko huko Misri, mara chombo hiki kilipofunguliwa hakikuweza tena kufungwa kwa urahisi. Yohana 12:3 inatuambia kilikuwa na uwezo wa ratili moja. Hii ingaliweza kuwa thamani ya mahari. Dhahili lilikuwa ni tendo la upendo

uliozidi na kujitoa.

**14:3**
**NASB** **"marhamu ya nardo safi"**
**NKJV** **"marhamu ya thamani ya nardo"**
**NRSV** **"mafuta ya thamani ya nardo"**
**TEV** **"marhamu aghali yakitengenezwa kwa nardo halisi"**
**NJB** **"mafuta ya thamani ya nardo halisi"**

Nardo ilitengenezwa kutokana na mizizi ya mimea iliyoota kwenye milima ya Himalaya. Ni yenye harufu kali.neno "safi" linatokana na *pistikos*, lenye kumaanisha thamani ya kuaminika (yaani., "halisi" au "isio changanywa na kitu," kama vile Yohana 12:3). Neno "nardo" yumkini ni la Kilatini (kama vile A. T. Robertson *Word Pictures in the NewTestament* juzuu. 1 uk. 380). Injili ya Marko ina maneno mengi ya Kilatini na vifungu kuliko injili yeyote.
Inavyoonekana ilikuwa imewalenga Warumi.

◙**"juu ya kichwa"** Injili ya Yohana inatuambia nardo ilimiminwa juu ya miguu yake (kama vile Yohana 12:3). Yumkini majibu yote ni sawa kwa sababu ratili moja ilikuwa nyingi kuweza kumiminwa yote kichwani, lakini ingaliweza kupaka mwili wote. Inawezekana kuwa kupakwa juu ya kichwa ingaliwakumbusha hawa Wayahudi juu ya kumpaka mfalme (kama vile 1 Sam. 10:1; 2 Fal. 9:3,6 na imedokezwa katika 1 Sam. 16:13). Hii yaweza kuwa ni alama ya kifalme ya Masihi vile vile pia ni utaratibu wa maziko/unabii (kama vile Marko 15:46; 16:1; Luka 23:56;
Yohana 19:39-40).

**14:4 "watu"** Yohana 12:4-5 anamtambua muuliza swali alikuwa ni Yuda Iskarioti. Inavyoonekana wanafunzi wa Yesu walikuwa wakirijadili hili kati yao (kama vile Marko 9:10; 10:26; 11:31; 12:7; 16:3).

◙**"waliokuwa wamechukizwa nafisini mwao"** Hii ni kauli isiotimilifu yenye mafumbo. Wanafunzi wakizungumza wao kwa wao wakilaumu uharibifu wa yule mwanamke aliokuwa akiufanya. Walichukizwa nafisini mwao. Hili neno linatumika juu ya mtizamo wa Yesu katika Marko 10:14 kuhusu wanafunzi kuwafukuza watoto nje.

◙**"'ingaliweza kuuzwa kwa Dinari mia tatu na zaidi'"** Ubadilishaji fedha wa leo sio wa kimsaada Zaidi kwa sababu ya kubadilika mara kwa mara kwa thamani ya fedha. Dinari moja ulikuwa ndio ujira wa askari au mfanyakazi;
hivyo, huu ulikuwa ni ujira wa mwaka mzima.

**14:5 "'wakapewa maskini'"** Kutoa pesa kuwapa maskini wakati wa sikukuu ya Pasaka ilikuwa ni sifa mojawapo muhimu ya kidini ya waalimu wa dini ya Kiyahudi.

## MADA MAALUM: MSAADA KWA WAHITAJI

I. Neno lenyewe
   A. Neno hili lilikuwa ndani ya Uyahudi.
   B. Ili linarejelea kuwapa wahitaji na/ama maskini.
   C. Neno la Kiyunani, kuwasaidia wahitaji, linatokana na ufupisho wa neno la Kiyunani *eleēmosunē*.
II. Dhana ya Agano la Kale
   A. Dhana ya kuwasaidia wahitaji iliidhinishwa katika torati ya kale
      1. muktadha unaofanana, Kumb. 15:7-11
      2. kusaza," kubakiza sehemu ya mavuno kwa wahitaji, Law. 19:9; 23:22; Kumb. 24:20
      3. "mwaka wa sabato,"kuwaruhusu maskini kula walichokizalisha mwaka wa saba ambao hawakuvuna,
   A. Dhana hii iliendelezwa katika Hekima ya Fasihi (mifano iliyoteuliwa)
      1. Ayubu 5:8-16; 29:12-17 (yule dhalimu anaelezwa katika 24:1-12)
      2. Zaburi, 11:7
      3. Mithali 11:4; 14:21,31; 16:6; 21:3,13

III. Uendelezwaji katika Uyhudi

A. Mgawanyo wa kwanza Mishnah unashughulika na kuwatunza wahitaji, maskini, na Walawi wa mahali palepale.

B. Nukuu zilizoteuliwa

1. Kitabu cha Mhubiri (pia kinajulikana kama Hekima ya Bin Sira) 3:30, "kama maji yazimishavyo ndimi za moto, ndivyo kuwasaidia wahitaji kulipiavyo dhambi" (NRSV)

2. Tobiti 4:6-11, **[6]"Maana ukitenda vitu kwa uaminifu utafanikiwa katika mambo yako yote. [7]Toa sehemu ya mali yako kuwapa maskini. Kamwe usimpe kisogo mtu maskini naye Mungu hatakupa kisogo. [8]Toa ulicho nacho. Ukiwa na zaidi, toa zaidi. Hata kama unacho kidogo tu, toa sehemu yake [9] Kwa kufanya hivyo utajiwekea hazina bara kwa wakati wa shida . [10] Kwa maana kusaidia maskini huokoa mtu kifoni na kumkinga asiingie katika makao ya giza. [11] Naam! Kusaidia maskini, kwa wale wanaofanya hivyo, ini sadaka bora mbele ya Mungu Mkuu."** (NRSV)

3. Tobiti 12:8-9, **"[8]Afadhali sala pamoja na ukweli na kusaidia maskini pamoja na kutenda haki kuliko kuwa tajiri na kukosa uaminifu. [9]Sadaka kwa maskinihumwokoa mtu na kifo na kumtakasa dhambi zake. Wale wanaowasaidia maskini watajaliwa uhai."** (NRSV)

A. Nukuu ya mwisho kutoka Tobiti 12:8-9 inaonyesha uendelevu wa tatizo. Matendo ya mwanadamu/ faida za mwanadamu zilionekana kama utaratibu kwa misamaha yote na utele.

B. Dhana hii iliendelea baadaye katika Maandiko ya Kale ya Kiyunani amababo nenola Kiyunani la "kuwasaidia wahitaji" (*eleēmosunē*) lilikuja kuwa kisawe cha "mwenye haki" (*dikaiosunē*). Haya yangeweza kubadili kila kitu katika kutafsiri Kiebrania "mwenye haki" (BDB 842, agano la upendo wa Mungu na uaminifu, kama vile Kumb. 6:25; 24:13; Isa. 1:27; 28:17; 59:16; Dan. 4:27).

C. Matendo ya mwanadamu ya huruma huwa kusudi ndani yake ili kufanikisha utele wa mtu binafsi hapa na wokovu wakati wa kifo. Tendo lenyewe, badala ya nia iliyo nyuma ya tendo, huwa sifa ya kitheolojia. Mungu huangalia mioyo, kisha hupima kazi ya mikono. Hili lilikuwa fundisho la Walimu wa sheria za Kiyahudi, lakini kwa kiasi fulani hii imepotezwa katika haki binafsi (kama vile Mika 6:8).

IV. Agano Jipya

A. Neno hili linapatikana katika

1. Mt. 6:1-4
2. Luka 11:41; 12:33
3. Matendo ya Mitume 3:2-3,10; 10:2,4,31; 24:17

B. Yesu anaelezea uelewa wa kitamaduni kuhusu haki kama (kama vile II Clement 16:4)

1. kuwasaidia wahitaji
2. kufunga
3. Maombi

Katika hotuba ya Yesu kule Mlimani (kama vile Mathayo 5-7), Kimsingi Yeye alieaelekeza upya mtazamo wa desturi iliyohusu haki (yaani, kusadiki katika matendoya mtu). Lile "agano jipya" la Yer. 31:31-34 lilkuja kuwa kipimo cha haki pamoja na Mungu (kama vile Rum. 3:19-31). Mungu hutoa moyo mpya, akili mpya, roho mpya. Tazamio haliko juu ya utendaji wa mwanadamu bali utendaji wa ki-Ungu (yaani, Eze. 36:26-27).

**14:6 "'Mwacheni'"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu. Yesu alitetea kitendo hiki cha upendo na huruma. Alikiona kuwa ni kitendo cha kinabii cha maandalio kwa ajili ya karibio la kifo chake na maziko (kama vile Marko 14:8).

**14:7 "'Maana siku zote mnao maskini pamoja nanyi'"** Hii haikuwa hoja yenye kuumiza kuwahusu maskini (kama vile Kumb. 15:4,11), lakini ni msisitizo juu ya upekee wa Yesu na muda wake maalumu akiwa duniani.

**14:8 "'ametangulia kuupaka mwili wangu marhamu kwa ajili ya maziko'"** Je huyu mama alielewa lipaswalo kufanyika ambalo wanafunzi hawakulijua? Aina ile ile ya marhamu ilitumika kwenye maandalio ya maziko (kama vile Yohana 19:40).

**14:9 "'Amini'"** Kwa maana iliyo halisi ni "amina."Angalia Mada Maalum katika Marko 3:28.

◙**"'kila ihubiriwapo injili'"** Injili inarejerea kwenye ujumbe alioufundisha kuhusu Mungu, kuhusu mwanadamu, kuhusu dhambi, kuhusu Yeye Mwenyewe, kuhusu wokovu, na kuhusu maisha baada ya kufa. Yesu aliidhihilisha hii kweli kwa waandishi waliovuviwa wa agano Jipya kupitia mpatanishi ambaye ni Roho. Ni ya kimafunuo, na sio ugunduzi wa kibinadamu. Kimsingi ni ufunuo wa mtu na uhusiano na mtu huyo, sio tu ni kanuni ya Imani au muundo wa mafundisho kumhusu mtu huyo. Inahusiana na mahusiano binafsi na Kristo kwa Imani na uelewa wa Yeye ni nani na kwa nini alikuja, ambao hutuongoza kuyafanana maisha yenye kumfanana Kristo katika mwanga wa mahusiano mapya na Mungu na moja kwa moja mtizamo mpya wa ulimwengu

◙**"'katika ulimwengu wote'"** Yesu alitegemea injili kuweza kupenya ulimwengu wote (kama vile Marko 13:27 na Mt. 28:19-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8).

◙**"'na hili alilotenda huyu linatajwa katika kumbukumbu zake'"** Yesu hakukisahau kitendo cha wema na kujioa cha huyu mama. Hili likaandikwa kwenye maandiko, lakini mengine yakabaki kwenye moyo wa Mungu na yatadhihilishwa kwenye siku ile kubwa ijayo (kama vile Gal. 6:7-9; 1 Tim. 5:25; Ufu. 14:13; pia 2:1,19; 3:8).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 14:10-11**
***10*Yuda Iskariote, yule mmoja katika wale Thenashara, akaenda zake kwa wakuu wa makuhani, apate kumsaliti kwao. *11*Nao waliposikia walifurahi, wakaahidi kumpa fedha. Akatafuta njia ya kumsaliti wakati wa kufaa.**

**14:10 "Yuda Iskarioti, mmoja wa wale Thenashara"** Kuna nadharia mbalimbali kuhusiana na Iskarioti (neno limeandikwa kwa namna tofauti katika maandiko mbalimbali ya Kiyunani). Laweza kurejelea kwa

1. Mtu wa Keriothi, mji wa Yuda
2. Mtu wa Kartamu, mji wa Galilaya
3. Mfuko uliotumika kuchukulia pesa
4. Neno la Kiebrania kwa ajili ya "kunyonga"
5. Neno la Kiyunani kwa ajili ya kisu kilichotumika kuulia

Ikiwa #1 ni wa kweli basi alikuwa ni Myuda pekee kati ya wale Thenashara. Ikiwa #4 au #5 ni wa kweli basi alikuwa ni mlokole kama Simoni. Hivi karibuni pamekuwepo na mawazo kinzani, lakini yenye unadharia mwingi (yenye kuikosoa injili ya Yohana), kitabu chenyekumtafasiri Yuda ni chenye msaada. Kitabu kilichoandikwa*Judas, Betrayer or Friend of Jesus?Na* William Klassen, Fortress Press, 1996.

◙**"ambaye alikuwa ni mmoja wa wale thenashara"** Alikuwa ni mmoja miongoni mwa wanafunzi aliowachagua Yesu. Alikuwa ni sehemu ya misafara ya kuipeleka injili na alikuwepo kwenye mafundisho ya Yesu, miujiza, na karamu ya mwisho. Kifungu hiki kina kibainishi cha wazi "mmoja wao." Pamekuwepo na maoni mbalimbali kama maana ya hili: (1) Yuda alikuwa ni kiongozi wa kundi la kitume. Alitunza pesa za kundi na alipata nafasi ya heshima kwenye karamu ya mwisho au (2) inarejerea kwenye manung'uniko ya Marko 14:4.

◙**"akaenda zake kwa wakuu wa makuhani"** Luka 22:4 inaongeza na "majemedari." Yuda akawauliza ni kiasi gani watampatia (kama vile Mt. 26:15). Ilikuwa ni bei ya mtumwa katili (kama vile Kut. 21:32; Zak. 11:12). Mathayo 26:16 inatuambia "vipande therathini vya fedha."Hili lilitimiliza unabii wa Zak. 11:12-13 (kama vile Mt. 27:9-10). Yesu alikuwa ni "mchungaji " aliyekataliwa.Waandishi wa injili wananukuu sura ya 9-14 ya Zakaria kama chanzo cha unabii au uainishi katika kuhusiana na huduma ya Yesu.

1. Mt. 21:4-5 inanukuu Zek. 9:9
2. Mt. 24:3 inanukuu Zek. 12:10
3. Mt. 26:15 inanukuu Zek. 11:12-13
4. Mt. 26:31 inanukuu Zek.13:7
5. Mt. 27:9-10 inanukuu Zek. 11:12-13

◙**"kumsaliti"** Hili ni neno la Kiyunani "kuacha" (*paradidōmi*). Biblia za Kiingereza mara nyingi hulitafasiri "kusaliti," lakini hii sio maana inayotambulika.Linaweza kuwa na maana chanya ya "kuaminisha" (kama vile Matt. 11:27) au "kurejesha" au "kuamuru" (kama vile Mdo. 14:26; 15:40), vile vile pia maana hasi ya "kukabidhi mamlaka kwa mtu" au "kumweka mtu mikononi mwa shatani" (kama vile 1 Kor. 5:5; 1 Tim. 1:20), au kwa ajili ya Mungu kujitenga na mtu kwenye habari ya ibada ya sanamu (kama vile Mdo. 7:42). Ni dhahili kuwa muktadha lazima uamue maana ya kitenzi hiki.Usaliti unafaa matendo ya Yuda.

**14:11 "waliposikia walifurahia"** Haisemi kuwa walishanganzwa.Mienendo ya Yuda mara nyingi imekuwa chanzo cha mitazamo. Hawa viongozi wa kidini wangaliona dosari yake toka kwenye kundi la kitume kama ushuhuda wa mipango yao ya mauaji!

◙**"wakati wa kufaa"** Luka 22:6 anaongeza "pasipokuwepo na umati."Wakahofu umaarufu wa Yesu pamoja na mahojaji toka Galilaya wakiwepo huko Yerusalemu kwa ajili ya karamu (kama vile Marko 11:18; 12:12; Mt. 26:5; 27:24).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 14:12-16**
**[12]Hata siku ya kwanza ya mikate isiyochachwa, walipoichinja pasaka, wanafunzi wake wakamwambia, Ni wapi utakapo tuende tukuandalie uile pasaka? [13]Akatuma wawili katika wanafunzi wake, akawaambia, Nendeni zenu mjini; atakutana nanyi mwanamume amechukua mtungi wa maji; mfuateni; [14]na po pote atakapoingia, mwambieni mwenye nyumba, Mwalimu asema, Ki wapi chumba changu cha wageni, niile pasaka humo, pamoja na wanafunzi wangu? [15]Naye mwenyewe atawaonyesha orofa kubwa, imeandikwa tayari; humo tuandalieni. [16]Wanafunzi wakatoka, wakaenda mjini, wakaona kama alivyowaambia, wakaiandaa pasaka.**

**14:12 "Hata siku ya kwanza ya mikate isiochachwa"** Pamekuwepo na tatizo kubwa kuhusu siku ambayo Bwana na wanafunzi wake walipokula karamu ya mwisho, tarehe 13 na 14 ya mwezi wa tatu au nne. Lakini Yohana anadokeza tarehe 13 (kama vile Marko 18:29; 19:14,31,32), wakati vidokezo vya injili vinaelezea siku ya 14. Yumkini tofauti inahusiana na

1. Utumiaji wa kalenda ya Kirumi dhidi ya kalenda ya Kiyahudi ya nyota
2. Njia tofauti za kuianza siku, yaani., wakati wa jioni kwa ajili ya Wayahudi dhidi ya wakati wa asubuhi kwa ajili ya Warumi
3. Ushahidi kuwa jamii ya watu waliokuweko maeneo ya bahari ya chumvi, wakifuatisha kalenda ya jua, walikuwa na siku ya pasaka mwanzoni kabisa kama ishara ya kuukataa uongozi wa kikuhani huko Yerusalemu.

Zile injili nne ni habari za ushahidi wa macho ulioandikwa kwa ajili ya makusudi ya kithiolojia na kiinjilisti. Waandishi walikuwa na haki, chini ya uvuvio, kuchagua, kupanga maisha na maneno ya Yesu. Habari hizi ni kwa ajili ya wengi waliotarajia kuwa na matatizo katika habari za injili (kama vile Fee and Stuart's *Howto Read the Bible forAll Its Worth*, kur. 126-129). Ukweli wenyewe ni kuwa pamekuwepo na maongenzi tofauti tofauti kuhusu uhalisia wao. Kanisa la mwanzo waliyakubali yale matoleo manne pasipo kuyaunganisha (isipokuwa simulizi za injili nne zilizounganishwa pamoja za Tatiani za karne ya pili). Kiufasiri injili inahitaji kutafasiriwa katika mtazamo wa muktadha wao wenyewe (kusudio la wandishi wenyewe) na sio kulinganisha na injili nyingine, ili tu kupata habari zaidi za kihistoria.

**14:13 "akatuma wawili kati ya wanafunzi wake"** Luka 22:8 inasema alikuwa ni Petro na Yohana. Kutokana na vyanzo vya Kibiblia tunatambua kwamba wawili tu kati ya kila familia ndio waliruhusiwa hekaluni kutoa mwanakondoo kwa msaada wa kuhani.

◙**"'atakutana nanyi mwanaume amechukua mtungi wa maji'"** Ilikuwa si kawaida kiutamaduni kumwona mwanaume amebeba maji na hasa akiwa amebeba ndani ya mtungi. Kama wanaume walihitajika kuteka maji mengi walitumia ngozi za kondoo au mbuzi, na sio vyungu. Huu nao ni ushuhuda wa macho wa Petro.

**14:14 "'mwambieni mwenye nyumba'"**Wengi waliamini kuwa hapa palikuwa ni nyumbani mwake Yohana aitwaye Marko (Yule mkusanya habari za Petro huko Rumi katika injili ya Marko), sehemu husika palipoandaliwa karamu ya mwisho na alipowatokea wanafunzi baada ya kufufuka. Yohana aitwaye Marko alikuwa ni binamu yake Barnaba na

mshirika mmojawapo wa wa safari ya kwanza ya umisheni wa Barnaba na Paulo (yaani., Paul). Pia alikuwa ni mwenza wa Petro na inavyoonekana mwandishi wa injili ya kwanza, akitumia kumbukumbu au hotuba za Petro. Hili linaonekana kuwa ni tukio lililopangwa kabla, na sio utabiri.

**14:15** Hii pia ilikuwa ni sehemu ile Yesu alipowatokea wanafunzi baada ya kufufuka (kama vile Mdo. 1:12). Hiki chumba kikawa ndio makao makuu huko Yerusalemu kwa ajili ya wanafunzi kukutanikia.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 14:17-21**
**17 Basi ilipokuwa jioni yuaja pamoja na wale Thenashara. 18 Nao walipokuwa wameketi chakulani, wakila, Yesu alisema, Amin, nawaambia, Mmoja wenu, naye anakula pamoja nami, atanisaliti. 19 Wakaanza kuhuzunika, wakamwambia mmoja mmoja, Je! Ni mimi? 20 Akawaambia, Ni mmoja wa hao Thenashara, ambaye achovya pamoja nami katika kombe. 21 Kwa maana Mwana wa Adamu aenda zake kama alivyoandikiwa; lakini ole wake mtu yule ambaye amsaliti Mwana wa Adamu; ingekuwa heri kwake mtu yule kama asingalizaliwa.**

**14:17 "Basi ilipokuwa jioni yuaja"** Kwa Wayahudi siku ilianza baaada ya kuzama kwa jua (kama vile Mwa. 1:5,8,13,19,23,31). Hiki kilikuwa ni chakula cha Pasaka kwa sababu mara nyingi kwa Wayahudi chakula chao cha jioni kililiwa majira ya mchana. Chakula cha Pasaka tu ndio kililiwa baada ya saa 12.00 jioni.

**14:18 "walipokuwa wameketi chakulani, wakila"** Mwanzoni Pasaka ilikuwa ikiliwa watu wakiwa wamesimama kwa sababu ya Kut. 12:11. Wayahudi wa karne ya kwanza hawakutumia viti, ni desturi waliojifunza toka Uajemi (kama vile Ester 1:6; 7:8). Walikuwa wakiwa wameketi kwenye mkeka, mara nyingi wakiwa watatu watatu, wakitengeneza umbo la nusu mduara (ili wahudumu waweze kuhudumia chakula kiurahisi), wakiketi miguuni pao wakitumia mito.

◙**"'Amini'"** Kwa maana iliyo ya wazi ni "amina." Angalia Mada Maalum katika Marko 3:28.

◙**"'mmoja wenu naye anakula pamoja nami—atanisaliti'"** Hili ni dokezo kwa Zab. 41:9. Kitamaduni hii ilikuwa ni namna ya kusisitiza kosa la Yuda (kama vileYohana 13:18). Ushirika wa kukaa pamoja ilikuwa ni alama muhimu ya kitamaduni ya urafiki na ahadi. Kumsariti mtu Yule mliyekula nae lilikuwa ni kosa kubwa lisilozungumzika kwa watu wa Mashariki.

**14:19 "wakamwambia mmoja mmoja, je ni mimi'"** Kila mmoja wa wale wanafunzi alidhani kuwa ni yeye. Hii inaonyesha kuwa kwa hoja hii kwa wakati ule, hakuna aliyemdhania kuwa ni Yuda. Kila mmoja hakuwa na uhakika kuhusu kusimama kwake.

**14:20 "'ambaye anachovya pamoja nami'"** Hili lilikuwa ni bakuri la rangi ya kijivu lenye maua, lenye kufanana na udongo wa tofari. Yuda alikuwa ameketi kuumeni kwa Yesu sehemu ya heshima! Yesu alikuwa bado, hata kwa wakati huu uliokuwa ameyoyoma sana, akijaribu kuwasiliana na Yuda kiroho.

**14:21 "'lakini ni ole wake Yule atakaye msaliti Mwana wa Adamu! Ingalikuwa ni nafuu kwake kama asingalizaliwa'"** Yohana 13:27 na kuendelea inadokeza kuwa Yuda alitoweka kwenye lile kusanyiko la karamu ya Bwana baada ya kumega tonge. Yuda alikuwa mtatanishi.Sababu zake za kumsaliti Yesu kamwe hazijawahi kuwekwa wazi. Baadhi wanamwona kama ni mzalendo wa Kiyahudi mwenye heshima (yaani., mlokole) akijaribu kumlazimisha Yesu kutenda kijeshi dhidi ya Rumi. Wengine wakimwona kuwa ni Myahudi mwenye kujitoa ambaye alikatishwa tamaa na kukataa kwa Yesu juu ya simulizi na kushiriki na wenye dhambi na waliotengwa kwenye jamii ya Kiyahudi. Injili ya Yohana inamwonyesha kama mwizi tokea mwanzo, mtu aliyekuwa akiendeshwa na tamaa ya fedha. Hata hivyo, matendo ya Yuda baada ya Yesu kukamatwa hayaendani na huu ubainishaji wa tabia. Hata iwe ni kwa sababu au mazingira, hata iwe ni kuhusika kwa shetani, hata iwe ni kujua kitu kabla kuliko tabiriwa, Yuda anawajibika kwa matendo yake kama tulivyo wote (kama vile Gal. 6:7).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 14:22-25**
**[22]Nao walipokuwa wakila, alitwaa mkate, akabariki, akaumega, akawapa, akasema, Twaeni; huu ndio mwili wangu. [23]Akatwaa kikombe, akashukuru, akawapa; wakakinywea wote. [24]Akawaambia, Hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi.[25]Amin, nawaambia ninyi, Sitakunywa tena kabisa uzao wa mzabibu, hata siku ile nitakapounywa mpya katika ufalme wa Mungu.**

**14:22 "alitwaa mkate"** Tambua haikuwa ni Pasaka ya Mwana Kondoo (wala mitishamba iliyo michungu), bali ni mikate isiochachwa (*azumos,* kama vile Marko 14:1). Neno la Kiyunani hapa ni *artos*, ambalo mara nyingi hutumika kumaanisha mkate wa kawaida (kama Marko 3:20; 6:8,16,36,37; 7:2,5,27; 8:4,14,16,17). Lakini pia hutumika kwa mikate isiochachwa katika ufanano wa Mt. 26:26; Luka 22:19. Yumkini mwana kondoo lilikuwa ni dokezo zaidi la kitaifa. Kwa ajili ya madokezo yote ya kihistoria kati ya Pasaka na Karamu ya mwisho, kuna tofauti ya kimakusudi ya kithiolojia.
IKiwa kuna mwendelezo wa uainishaji kati ya wana wa Israeli kwenda uhamishoni na Yesu, ambao unaonekana kuwakweli, hivyo mkate unaleta uhusiano maalum juu ya "manna" (kama vile Kutoka 16),chakula kilichotolewa na YHWH kipindi cha kutangatanga jangwani. Hiki kilileta mlo wenye kuleta nguvu kwa watu wa Mungu. Sasa YHWH hutoa mkate wa "kweli" wa mbinguni, hutoa maisha ya kweli "kweli" hutuma kiongozi "sahihi" , na huanzisha Pasaka mpya toka dhambini na mautini. Wandishi wa Agano Jipya mara nyingi hutumia uainishaji wa mpangilio wa matukio kwenye kumwasilisha Yesu kama ilivyoelezwa kabla katika Agano la Kale. Divai katika Agano la Kale ilijulikana kama damu ya matunda ya mzabibu na mara nyingi ilitumika katika maana ya kisheria (yaani.,hasira ya mizabibu). Sasa ni dhabihu ambayo huleta uzima wa milele. Taswira inaonekana wazi katika
Yohana 6.

◙**"baada ya kubariki"** Palikuwepo na utaratibu wa mkao kwa ajili ya mlo wa Pasaka. Kwa namna yeyote ile maana ya umegaji mkate na divai ilitokea kwenye hoja iliyoitwa "kikombe kile cha baraka" (kama vile 1 Kor.10:16).

## MADA MAALUM: PASAKA (UTARATIBU WA HUDUMA)

I. Maelezo ya ufunguzi
   A. Kitendo cha Kiungu cha hukumu ya Wamisri na ukombozi kwa ajili ya Israeli ni kipimo kwa ajili ya upendo wa YHWH na uanzishaji wa taifa la Israeli (yaani., hasa kwa ajili ya manabii).
   B. Safari ya kwenda uhamishoni kwa Waisraeli ni utimilifu maalum wa ahadi ya YHWH kwa Ibrahimu katika Mwa.15:12-21. Pasaka inaweka kama kumbukumbu kwa ajili ya safari ile ya kwenda uhamishoni.
   C. Hili ni la mwisho, lenye mwendelezo zaidi (kijiografia, yaani., Misri na Gosheni) na lenye kushangaza (wazaliwa wa kwanza wa binadamu na wanyama kuuwawa) kuhusu mapigo kumi yaliyotumwa na YHWH juu ya Misri kupitia Musa.

II. Neno lenyewe (BDB 820, KB 947)
   A. Maana ya NOMINO haijulikani
      1. kuhusiana na "pigo," hivyo "pigo moja" (yaani., Kut. 11:1); Malaika wa YHWH waliwapiga wazaliwa wa kwanza wa wanadamu na wanyama
   B. Maana ya KITENZI
      1. "kuchechemea" au "kuchopea" (kama vile 2 Sam. 4:4), likitumika kwa maana ya "kuruka juu ya nyumba zilizotiwa alama" (yaani., Kut. 12:13,23,27, BDB 619, asili ya neno la kawaida)
      2. "kucheza" (kama vile 1 Fal. 18:21)
      3. kwa lugha ya Akkadia – "kutuliza"
      4. kwa Wamisri – "kupiga"
      5. VITENZI mfanano katika Isa. 31:5, "kulinda juu ya" (kama vile toleo la REB la Kut. 12:13)
      6. Wakristo wa mwanzo waliokubalika walisikika wakitania toka kwenye neno la Kiebrania pasah kwenda neno la Kiyunani *paschō,* yaani "kuumia"
   C. Uwezekanao wa mifano ya kihistoria
      1. Dhabihu ya mchungaji kwa ajili ya mwaka mpya
      2. Dhabihu ya bedui na mlo wa kiushirika wakati wa kuyaondoa mahema kipindi cha kipupwe ili kutafuta malisho na kuepuka uovu

3. Dhabihu ya kuepusha uovu toka kwa wafugaji wanaohama hama

D. Sababu ni ngumu keleweka sio tu kuwa na uhakika wa maana ya neno lenyewe, bali pia asili yake kuwa pasaka za aina mbalimbali zilipatikana kwenye matambiko yao ya kale.
   1. tarehe za kipindi cha kipupwe
   2. Asli ya NOMINO haijulikani
   3. Lilihusiana na ulinzi wa usiku
   4. utumiaji wa damu
   5. Sanamu za malaika /mapepo
   6. chakula maalumu
   7. vitu muhimu vya mashambani (mikate isiyotiwa chachu)
   8. hakuna kuhani, hakuna madhabahu, wala kituo cha mahali

III. Tukio
   A. Tukio lenyewe limeandikwa katika kitabu cha Kutoka 11-12.
   B. Sherehe ya mwaka imeelezewa katika kitabu cha Kutoka 12 na kujumuishwa kwenye sherehe ya siku nane ikiwa na sikukuu ya mikate isiochachwa.
      1. Mwanzoni lilikuwa ni tukio la kawaida, kama vile Kut. 12:21-23; Kumb. 16:5 (kama vile Hesabu 9)
         a. hakuna kuhani
         b. hakuna madhabahu maalum
         c. wakijikita kwenye utumiaji wa damu
      2. ikajakuwa ni tukio kwenye madahahu ya ndani
      3. Huu ujumuishaji wa dhabihu ya eneo husika (yaani., damu ya mwana kondoo kukumbuka malaika wa mauti aliyekuwa akipita) na sikukuu ya mavuno kwenye madhabahu ya ndani ilikamilishwa kwa kupakana karibu kwa tarehe za 14 na 15-21 za mwezi wa tatu au nne
   C. uwakilishi wa kumiliki wazaliwa wote wa kwanza wa wanyama na wanadamu na ukombozi wao umeelezewa katika kitabu cha Kutoka 13

IV. Habari za kihistoria za utunzaji wake
   A. Pasaka ya kwanza ilisherehekewa huko Misri, Kutoka 12
   B. kwenye Mlima Horebu/Sinai, Hesabu 9
   C. Pasaka ya kwanza ilisherehekewa huko Kaani (Gilgali), Yos. 5:10-12
   D. kipindi cha Sulemani kuliweka wakfu Hekalu, 1 Fal. 9:25 na 2 Nya. 8:12 (ni yumkini,lakini haijaelezewa haswa)
   E. Kile kipindi cha utawala wa Hezekia, 2 Mambo ya Nyakati 30
   F. ile iliyofanyika kipindi cha mageuzi ya Yosia, 2 Fal. 23:21-23; 2 Nya. 35:1-18
   G. Tambua 2 Fal. 23:22 na 2 Nya. 35:18 inataja Israeli kuacha kuitunza hii sherehe ya mwaka

V. Umuhimu wake
   A. Hii ni moja kati ya zile tatu zilizohitajika kufanyika siku za sherehe ya mwaka (kama vile Kut. 23:14-17; 34:22-24; Kumb. 16:16):
      1. Pasaka/Mikate isiyochachwa
      2. Sherehe za wiki
      3. Sherehe ya vibanda
   B. Musa aliitabiri siku itafanyika kwenye madhabahu ya ndani (kama zilivyokuwa zile sherehe zingine mbili) katika Kumbukumbu la Torati
   C. Yesu alitumia matukio ya chakula cha Pasaka ya mwaka (au siku kabla) kudhihirisha Agano Jipya katika alama ya mkate na mvinyo, lakini hakutumia mwanakondoo:
      1. chakula cha ushirika
      2. dhabihu ya ukombozi
      3. umuhimu wa kuiendeleza kwa vizazi vijavyo

◙**"Twaeni, huu ndio mwili wangu"** Yohana 6:22 na kuendelea na 1 Kor. 10:16 inaonyesha taswira ya nguvu ya kithiolojia ya hii ibada. Maneno ya Yesu kuhusu mwili na damu yake yangaliwashangaza Wayahudi hawa. Ulaji nyama za watu na

kunywa damu ungalikuwa ni ukiukaji wa sheria za Law. 11. Haya maelezo dhahili ni kishirio, lakini bado yanashangaza. Yesu alikuwa akimaanisha kusulubishwa kwa kuumega mkate. Kama ilivyokuwa rangi ya mvinyo ikifanana na damu, ndivyo rangi ya mkate alifanana na mwili wa mwanadamu. Yesu alikuwa makate wa kweli (yaani., manna, kama vile Yohana 6:31-33,51), Pasaka ya kweli, uhamisho mpya!

## MADA MAALUM: KARAMU YA BWANA KATIKA YOHANA 6

A. Injili ya Yohana haijaandika kuhusu karamu ya Bwana, ingawa sura za 13-17 ziliandika mazungumzo na maombi yaliyofanyika chumba cha juu. Ondoleo hili linaweza kuwa la kimakusudi. Kanisa la karne ya kwanza lilianza kuitazama sheria katika maana ya ushirika mtakatifu. Wao waliona kama mlango wa neema. Yohana angaliweza kujibu hili kwenye mtazamo wa ushirika mtakatifu kwa kutokuandika ubatizo wa Yesu au karamu ya Bwana.

B. Yohana 6 ipo katika muktadha wa kuwalisha watu elfu tano. Hata hivyo, wengi wanaitumia kufundishia mtazamo wa ushirika mtakatifu wa Ekaristi. Hiki ndicho chanzo cha mafundisho ya kanisa la Romani kuhusu mkate na mvinyo kubadilika kuwa mwili wa Kristo (Yohana 6:53-56).

Swali juu ya namna sura ya 6 inavyohusiana kwenye Ekaristi Takatifu inaonyesha asili ya umiliki wa injili mbili. Dhahili, injili inhusiana na maneno ya Yesu na maisha, na bado iliandikwa miongo ya nyuma na kuelezea imani ya jamii ya wandishi binafsi. Kwa hiyo kuna hatua tatu za kusudi la uandishi:

1. Roho
2. Yesu na wasikiaji wa kwanza
3. wandishi wa injili na viongozi wao

Namna gani mtu anaweza kufasiri? Njia pekee iliyothibitishwa lazima iwe ya kimuktadha, kisarufi, mtazamo wa kimafumbo, kupata taarifa toka kwenye maeneo ya kihistoria.

C. lazima tukumbuke kuwa umati wa watu ulikuwa wa Wayahudi na mazingira ya kitamaduni yalikuwa ni matarajio ya walimu wa dini ya Kiyahudi wa Masihi kuwa zaidi ya Musa (kama vile Yohana 6:30-31), hasa katika mtazamo wa uelewa wa safari ya uhamishoni kama utoaji wa "manna." Walimu wa dini wangalitumia Zab. 72:16 kama uhakiki wa andiko. Maelezo ya Yesu yasiyo ya kawaida (kama vile Yohana 6:60-62, 66) yalimaanisha kutia wasiwasi matarajio ya uongo ya umati kuhusu Masihi (kama vile Yohana 6:14-15).

D. Makasisi wa kanisa la mwanzo wote hawakukubali kuwa hii sura inarejelea karamu ya Bwana. Clement wa Iskandria, Origen, and Eusebius kamwe hawakutaja karamu ya Bwana katika majadiliano yao kuhusu hii sura.

E. stiari ya hii sura yanafanana na maneno ya Yesu aliyotumia na yule "mwanamke kule kisimani" katika Yohana 4. Maji ya kidunia na mkate yanatumika kama stiari ya maisha ya milele na ukweli wa kiroho.

F. Huu uzidisho wa mikate ndiyo muujiza pekee ulioandikwa katika injili zote nne!

**14:23 "akashukuru"** Neno la Kiyunani kwa ajili ya "kushukuru" ni *eucharistē*, pale tunapopata jina la Kiingereza kwa ajili ya karamu ya Bwana, Ekaristi takatifu.

**14:24 "Hii ndiyo damu yangu ya agano"** Rangi ya divai ilifanana na rangi ya damu ya mwanadamu. Kifungu hiki kina mambo muhimu matatu kwenye mwanzo wa Agano la Kale.

1. Kut. 24:6-8, uanzishaji wa kitabu cha agano kwa damu ya agano
2. Yer. 31:31-34, ndiyo andiko pekee katika agano la kale lililotaja "agano jipya"
3. Zak. 9:11, ambayo ndiyo sehemu ya fasihi ya 9-14, chanzo cha nabii nyingi (yaani.,uainishi wa matukio ya Yesu) za maisha ya Yesu.

kuna tofauti mbili katika desturi za machapisho ya Kiyunani.

1. "agano" ikifuata Mt. 26:28, amalo hupatikana katika machapisho ya Kiyunani ,א, B, C, D2, na L (na pia D* na W kukiwa na mabadiliko kidogo). Toleo la UBS4 linaupa huu usomaji alama "A" (pasipo shaka).
2. "agano jipya" ikifuata Luka 22:20 na 1 Kor. 11:25, ambalo hupatikana katika toleo la MSS A na E na matoleo ya Vulgate, Kiashuru, Koptiki, na Armenia (kama vile toleo la NKJV). Yumkini hili lilikuwa ni nyongeza yenye kuhusiana na maneno ya Yesu kwenye agano "jipya" la Yer. 31:31-34.

Katika mazungumzo yote haya kitu kimoja ni cha ukweli. Kifo cha Yesu kilikuwa ni cha muhimu kwenye urejeshaji wa mwanadamu aliyeanguka kuwa na ushirika na Baba (kama vile Marko10:45). Yesu alikuja ili (1) kumdhihirisha Baba; (2)

kutupatia mfano wa namna ya kumfuata; na (3) kufa badala yetu kwa ajili ya dhambi. Hakuna njia nyingine kwa ajili ya ukombozi (kama vile Yohana 10,14). Hiki ndicho kilikuwa kiini cha sehemu ya mpango wa milele wa Mungu (kama vile Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29).

## MADA MAALUM: AGANO

Neno la Agano la Kale *berith* (BDB 136, KB 157), "Agano," sio rahisi kulielezea. Hakuna KITENZI kinachoshabihiana katika Kiebrania. Yote yanajaribu kupata ile asili ya neno au maana inayofanana inayodhihilisha kutoleta ushawishi. Yumkini ubashiri mzuri ni "kukata"ikimaanisha sadaka ya mnyama inayojumuishwa kwenye agano (kama vile Mwa. 156:10,17). Hata hivyo, kiini dhahili cha dhana yenyewe kimetizamishwa kwa wasomi kuchunguza matumizi ya kidunia katika jaribio la kupima maana yake ya kiutendaji. Agano ni namna ambayo Mungu wa kweli (angalia Mada Maalum: Uwepo wa Mungu Mmoja) anavyoshughulika na uumbaji wake wa Mwanadamu. Dhana ya Agano, mkataba, au makubaliano ni ya muhimu katika kuuelewa ufunuo wa Mungu. Mvutano kati ya Ukuu wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadmu kwa wazi unaonekana katika dhana ya Agano. Baadhi ya maagano yanaegamia moja kwa moja juu ya tabia ya Mungu na matendo.

1. Uumbaji wenyewe (kama vile Mwanzo 1-2)
2. Utunzaji na ahadi ya Nuhu (kama vile Mwanzo 6-9)
3. Wito wa Abrahamu (kama vile Mwanzo 12)
4. Agano pamoja na Abraham (kama vile Mwanzo 15)

Hata hivyo, ile asili ya Agano inahitaji mwitikio.

1. Kwa imani Adamu anapaswa kumtii Mungu na kutokula lile tunda la mti wa katikati ya Edeni
2. Kwa imani Nuhu anapaswa kutengeneza safina mbali na maji na kuwakusanya wanyama wote
3. Kwa imani Abraham anapaswa kuiacha familia yake, na kumfuata Mungu, na kuamini katika kizazi kijacho
4. Kwa imani Musa anawatoa wana wa Israeli toka Misri kwenda Mlima Sinai na kupokea maagizo maalum kwa ajili ya maisha ya kidini na kijamii yakiwa na ahadi ya Baraka na laana ( kama vile Walawi 26, Kumbu kumbu la Torati 27-28)

Mvutano ule ule unaohusiana na ushirika wa Mungu kwa mwanadamu unaelezewa katika "agano jipya" (kama vile. Yer. 31:31-34; Ebr. 7:22; 8:6,8,13; 9:15; 12:24). Mvutano kwa wazi unaweza kuonekana katika kulinganisha Ezek. 18:31 na Ezek. 36:27-38 (tendo la YHWH). Je agano linasimamia juu ya matendo ya neema ya Mungu au mamlaka ya mwitikio wa mwanadamu? Hili ni suala mtambuka kati ya Agano la Kale na Agano Jipya. Lengo la yote ni sawa:

1. Urejesho wa ushirika na YHWH uliopotea katika Mwanzo 3
2. Uimalishaji wa watu wa haki ambao wanaaksi tabia ya Mungu

Agano jipya la Yer. 31:31-34 linatatua mvutano kwa kuondoa utendaji wa kibinadamu kwa maana ya kupata ukubarifu. Sheria za Mungu zikaja kuwa shauku ya ndani badala ya sheria ya nje. Lengo la ki-Mungu, watu wenye haki linabaki vile vile, lakini njia zinabadilika. Wanadamu waliyoanguka wanathibitisha wao wenyewe pasipo utoshelevu kwa kuaksi taswira ya Mungu. Tatizo halikuwa agano la Mungu, bali ni udhaifu na dhambi za mwanadamu (kama vile Mwanzo 3; Warumi 7; Wagalatia 3).

Mvutano wa aina ile ile kati ya maagano ya Agano la Kale yasiyo na masharti na yenye masharti yanabaki katika Agano Jipya. Wokovu ni wa bure katika kazi aliyokwisha kuimaliza Yesu Kristo, lakini unahitaji toba na imani (mwanzoni na kuendelea, angalia Mada Maalum: Kuamini katika Agano Jipya). Yesu anaita ushirika wake mpya na waamini "agano jpya" (kama vile Mt. 26:28; Marko 14:24; Lk. 22:20; 1 Kor. 11:25). Yote ni matamko ya kisheria (ya kimahakama) na wito wa kumfanana na Kristo (kama vile Mt. 5:48; Rum. 8:29-30; 2 Kor. 3:18; 7:1; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 4:13; 1 The. 3:13; 4:3,7; 5:23; 1 Pet. 1:15), maelezo elekezi ya ukubalifu (Warumi 4) wito wa ushurutishi wa kuwa mtakatifu (kama vile Mt. 5:48)! Waamini hawaokolewi kwa utendaji kazi wao, lakini ni katika utii (kama vile (kama vile Efe. 2:8-10; 2 Kor. 3:5-6). Maisha ya ki-Mungu yamekuwa ni ushuhuda wa wokovu, na sio njia ya wokovu (yaani., Yakobo na 1Yohana). Hata hivyo, maisha ya milele yana tabia zinazochunguzika! Mvutano huu unaonekena kwa wazi katika maonyo yanayoonekana katika Agano Jipya (angalia Mada Maalum: Uasi)

◙"'**iliyomwagika kwa ajili ya wengi'"** Kifo cha Yesu, kikimaanishwa kwa damu yake kumwagika, kilikuwa ni dhabihu kwa ajili ya dhambi (kama vile Marko 10:45; Mt. 26:28; 1 Kor. 15:3; 2 Kor. 5:21; Ebr. 9:11-15). Neno "wengi" halirejelei kwa kundi fulani, bali ni stiari ya Kiebrania (au Kisemiti) kwa ajili ya "kwa wale wote watakao kubali." Hili linaweza kuonekana katika ufanano wa Rum. 5:18 na 5:19 vile vile pia angalia kwenye Isa. 53:6 neno "wote" ukilinganisha na 53:11-12, neno "wengi." Angalia kumbukumbu kwenye Marko 10:45.

## MADA MAALUM: ILIYOMWAGIKA

Neno la kitamaduni la Kiyunani *cheō* linamaanisha "kumwaga" (mara nyingi ni kwa maana iliyo wazi). Kwa maana ya iliyokuzwa neno, *ekcheō*, linachukua nafasi yake na kutengeneza madokezo mawili.

1. Damu ilimwagika isiyo na hatia, kama vile Mwa. 9:6; 37:22; Kumb. 19:10; Mt. 23:35; Mdo. 22:20; Rum. 3:15
2. Dhabihu iliyotolewa, kama vile Amu. 6:20; 1 Sam. 7:6; 2 Sam. 23:16; Mt. 26:28; Marko 14:24; Luka 22:20

Kwa Yesu maana hizi mbili zilikutana pale Kalvari (kama vile Colin Brown, ed., *The New International Dictionary of New Testament Theology* juzuu ya 2, kur. 853-855).

Biblia pia inatumia KITENZI hiki katika kuhusianisha na

1. Kumwaga kwa Roho Mtakatifu (kama vile Yoeli 2:28-29; Ezek. 39:29; Zak. 12:10; Mdo. 2:17-18,33; 10:45; Tito 3:6)
2. Upendo wa Mungu (kama vile Rum. 5:5; kumbuka ufanano wa kithiolojia katika Gal. 4:6)
3. Ghadhabu ya Mungu (kama vile Ufunuo 16, KITENZI kimetumika mara nane)

**14:25 "'Sintakunywa tena'"** Liturujia ya Pasaka ilihusiana na kikombe cha nne. Walimu wa sheria za Kiyahudi walianzisha utaratibu huu ulioegamia juu ya Kut. 6:6-7. Kikombe cha tatu kilimaanisha ukombozi. Hiki ni kile kinachounda msingi wa karamu ya Bwana. Yesu alikataa kunywa kikombe cha nne kwa sababu kilimaanisha ukamilisho. Yesu alihusianisha hili na siku ya mwisho ya karamu ya kimasihi (kama vile Isa. 25:6; 55; Mt. 8:11; Luka 13:29; 14:15,24; 22:30; Ufu. 19:9,17).

◙**"'mpaka siku hiyo'"** Hakika hili linarejelea ujio ujao wa Yesu katika utukufu wake na nguvu tofauti kutokana na hali yake ya sasa alipoikabili aibu, kukataliwa, na kifo! Ujio mara mbili wa Yesu unatofautisha kazi yake kama mkombozi (yaani.,lililotendwa kwa niaba yaw engine, upatanisho mbadala) na mshindi/mwamuzi. Huu ujio mara mbili uliwashangaza Wayahudi. Yumkini alikuwa ni Yesu Mwenyewe, huenda akiwa njiani kelekea Emmau, ambaye alionyesha umuhimu kamili wa sura muhimu za agano la kale (yaani., Mwa. 3:15; Zab. 22; Isa. 53 na Zak. 9-14).

◙**"'ufalme wa Mungu'"** Angalia Mada Maalum katika Marko 1:15c.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 14:26**
**26 Nao walipokwisha kuimba walitoka kwenda mlima wa Mizeituni.**

**14:26 "walipokwisha kuimba"** Hiki kitenzi cha Kiyunani ni chanzo cha neno la Kiingereza "wimbo." Hili yumkini sehemu ya wimbo wa Halleluh (yaani., Zab. 113-118, kama vile Mt. 26:30), ambayo ilikuwa ni sehemu ya mwisho ya ibada ya Pasaka.nyimbo hizi zilikuwa ni maneno ya furaha na shukrani kwa ajili ya ukombozi wa YHWH. Yameongelewa waziwazi au kuimbwa kwa sehemu kubwa, au kwa sehemu ndogo, kwenye siku zote za sherehe, isipokuwa siku ya upatanisho. Zaburi 113-114 huimbwa mapema katika chakula cha Pasaka na 115-118 mpaka mwisho wa chakula.

◙**"Mlima Mzeituni"** Yesu na wanafunzi lazima walikuwa wakitumia mara kwa mara hii sehemu kama kituo au mahali pa maombi wakati wa kipindi cha Pasaka (yaani., siku nane).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 14:27-31**
**[27]Yesu akawaambia, Mtakunguwazwa ninyi nyote kwa ajili yangu usiku huu; kwa kuwa imeandikwa, Nitampiga mchungaji, na kondoo watatawanyika. [28]Lakini baada ya kufufuka kwangu, nitawatangulia kwenda Galilaya. [29] Petro akamwambia, Hata wajapokunguwazwa wote, lakini siyo mimi. [30]Yesu akamwambia, Amin, nakuambia wewe, Leo, usiku huu, kabla ya kuwika jogoo mara mbili, utanikana mara tatu. [31]Naye akazidi sana kusema, Ijaponipasa kufa nawe, hata hivyo sitakukana kamwe. Na wote wakasema vile vile.**

**14:27**

| | |
|---|---|
| **NASB,NJB** | **"Mtakunguwazwa ninyi nyote"** |
| **NKJV** | **"ninyi nyote mtajikwaa"** |
| **NRSV** | **"ninyi nyote mtakuwa watoro"** |
| **TEV** | **"ninyi nyote mtakimbia"** |

Hii ni kauli tendwa elekezi ya wakati ujao. Huu ni ushahidi mwingine alioufahamu Yesu na kudhibiti matukio yajayo. Wazo tendwa lilivutia katika tafsiri ya ASV "wote mtaudhiwa" (yaani.,*skandalizō,* iliyotumika kuunganisha pamoja). Kuna kauli tendwa ya wakati ujao, "watatawaninyishwa,"toka Zak. 13:7. Istilahi ya aina ile ile ya kutokuamini (yaani., "kupotea") ilitumika kwa ajili ya wengine wakimkataa Kristo (kama vile Mt. 11:6; 13:21,57;24:10; 26:31). Imani ya wanafunzi itashindwa! Kukana kwa Petro ilikuwa ni utimilifu wa hofu zao.

◙**"'imeandikwa'"** Kwa maana iliyo wazi hii ni "imeandikwa," ambayo ni kauli tendwa timilifu ya hali ya kaurifu.kilikuwa ni kifungu cha uainishaji (yaani.,nahau ya Kiebrania) ikirejelea kwenye uvuvio wa Agano la Kale.

◙**"'nitawapiga'"** Hii ni nukuu tokaZak. 13:7. Ulikuwa ni mpango wa Baba kuwa Yesu ayatoe maisha yake kama dhabihu kwa ajili ya dhambi (kama vile Isa. 53:4,6,10; Marko 10:45; Luka 22:22; Matendo 2:23; 3:18; 4:28; 13:29; 2 Kor. 5:21).

**14:28** Yesu akawaambia wanafunzi mara kadhaa kuwa wataonana juu ya Mlima huko Galialaya (kama vile Mt.26:32; 28:7,10,16). Kutaniko hili maalumu lilikuwa ni tukio kwa ajili ya agizo kuu (kama vile Mt. 28:16-20), ambalo huenda ni lile alilotokea baada ya kufufuka kwake lililoandikwa katika 1 Kor. 15:6. Hili halirejelei kwenye kupalizwa, kulikotendeka kwenye Mlima Mzaituni siku ya Arobaini baada ya kufufuka (kama vile Mdo. 1:12). Huu ulikuwa ni utabiri wa ufufuo wake, lakini hawakuweza kutambua umuhimu wake. Kifungu hiki ni fursa nzuri kuonyesha kuwa Agano Jipya mara nyingi huainisha kazi ya ukombozi kwa watu wote watatu wa Uungu.

1. Mungu Baba akamwinua Yesu (kama vile Matendo 2:24; 3:15; 4:10; 5:30; 10:40; 13:30,33,34,37; 17:31; Rum.6:4,9; 10:9; 1 Kor. 6:14; 2 Kor. 4:14; Gal. 1:1;Efe. 1:20; Kol. 2:12; 1 The. 1:10)
2. Mungu Mwana akajiinua mwenyewe (kama vile Yohana 2:19-22; 10:17-18)
3. Mungu Roho akamwinua Yesu (kama vile Rum. 8:11). Msisitizo wa kuhusu watu wanaoamini juu ya Utatu katika Marko 14:9-10. Angalia MADA MAALUM: UTATU katika Marko 1:11.

**14:29 "'Hata'"** Kwa maana iliyo wazi ni "hata kama" (kama vile toleo la NKJV na NJB). Hii ni sentensi yenye masharti daraja la kwanza, ambayo inafikiriwa kuwa kwelie kutokana na mtizamo wa mwandishi au kusudio lake la kifasihi. Petro aliwafikilia wengine wangaliweza kukimbia, lakini sio yeye!

◙**"'lakini'"** Hii ni kauli nzito ya kiushindani ya neno *alla*. Petro alikuwa akitengeneza madai yenye msisitizo kuwa hatamwacha Yesu kamwe (kama vile Luka 22:33; Yohana 13:37-38). Petro alikuwa akisema wazi kwa utii asingaliweza kutimiza, shauku yake yenye kuzidi uwezo wake!

**14:30 "usiku huu, leo, nakuambia wewe, kabla jogoo hajawika mara mbili, wewe utanikana mara tatu"** "wewe,mwenyewe" ni kauli ya kimsisitizo! Hii ni kauli ya kati elekezi ya wakati ujao. Habari za Luka ni ndefu (kama vile Marko 22:31-34). Maelezo ya kuwa jogoo kabla ya kuwika mara mbili ni kumbukumbu ya ushauhuda wa macho wa Petro. Umeandikwa tu katika injili ya Marko.

**14:31**
**NASB "Naye akizidi sana kusema"**
**NKJV "akizidi kusema kwa bidii"**
**NRSV "akisema kwa bidii"**
**TEV "akisema hata kwa nguvu zaidi"**
**NJB "bado akirudia kusema zaidi "**

Neno hili (*perisseia*) kwa ajili ya kuzidi au kiwango kikubwa linatumika mara nyingi katika miundo mbalimbali katika Agano Jipya (kama vile Mt. 5:20; 27:23; Mdo. 26:11;Fil. 1:9; 1 The. 4:1). Muundo uliozidi ukiwa na kiambishi awali chenye kihusishi *ek* kinapatikana hapa tu katika Marko. Yumkini kinatoka kwa Petro mwenyewe!
Alikumbuka namna gani kukana kwake kwa nguvu kulivyokuwa!

◙**"'hata hivyo'"** Hii ni sentensi yenye masharti daraja la tatu yenye kumaanisha tendo muhimu.Kwa maana iliyo wazi ni"hata kama itanilazimu."

◙**"'sintakukana kamwe'"** Amini Petro alijisikia kusema namna hii.Kwa moyo wake wote na nguvu aliazimia kusimama na Yesu! Kama dhambi za Daudi na hatimaye msamaha kutenda kazi ili kuwatia moyo waamini wajao, sisi pia, tunamtetea Petro na kushindwa kwake. Mwanadamu mdhaifu, mwenye dhambi huhitaji kufanya vitu vya haki (kama vile Rum. 7), walijipata wenyewe hawawezi! Yesu anaweza kushughulika na wale wenye kushindwa, lakini sio wale wenye mashaka wasiopenda kutubu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 14:32-42**
**[32]Kisha wakaja mpaka bustani iitwayo Gethsemane; akawaambia wanafunzi wake, Ketini hapa muda niombapo.**
**[33]Akamtwaa Petro na Yakobo na Yohana pamoja naye, akaanza kufadhaika sana na kuhangaika. [34]Akawaambia,**
**Roho yangu ina huzuni nyingi kiasi cha kufa; kaeni hapa mkeshe. [35]Akaendelea mbele kidogo, akaanguka**
**kifudifudi, akiomba ya kuwa, ikiwezekana, saa hiyo imwepuke. [36]Akasema, Aba, Baba, yote yawezekana kwako;**
**uniondolee kikombe hiki; walakini, si kama nitakavyo mimi, bali utakavyo wewe. [37]Akaja akawakuta wamelala**
**usingizi, akamwambia Petro, Je! Simoni, umelala? Hukuweza kukesha saa moja? [38]Kesheni mwombe, msije**
**mkaingia majaribuni, roho i radhi ila mwili ni dhaifu. [39]Akaenda zake tena, akaomba, akisema neno lilo hilo.**
**[40]Akaja tena akawakuta wamelala, maana macho yao yamekuwa mazito, wala hawakujua la kumjibu. [41]Akaja**
**mara ya tatu, akawaambia, Laleni sasa, mpumzike; yatosha, saa imekuja; tazama, Mwana wa Adamu anatiwa**
**mikononi mwao wenye dhambi. [42]Ondokeni, twendeni zetu; tazama, yule anayenisaliti amekaribia.**

**14:32 "Gethsemane"** Neno "Gethsemani" linamaanisha "mgandamizo wa mafuta " katika Kiebrania. Inavyoonekana ilikuwa ni bustani ya faragha nje kidogo mwa mipaka ya mji wa Yerusalemu juu ya Mlima Mzeituni. Ilikuwa imekatazwa kuwa na bustani ndani ya mji kwa sababu ya mbolea iliyohitajika kwa ajili ya mimea iliufanya mji kuwa najisi. Inavyoonekana Yesu alikuwa akija katika bustani hii mara nyingi. Inawezekana kuwa wakati wa wiki ya mateso alipiga kambi ya muda akiwa na wanafunzi wake. Yuda anaifahamu sehemu hii vizuri.

◙**"'Ketini hapa muda niombapo'"** Katika ufanano wa Mt. 26:41 na Luka 22:40 Yesu aliwaambia kuomba ili wasije wakaingia majaribuni.

**14:33 "akamutwaa Petro na Yakobo na Yohana pamoja naye"** Huu ulikuwa ni uongozi wa jamii ya faragha iliyomzunguka Yesu kati ya wanafunzi wake. Walikuweko pamoja na Yesu kwenye matukio mbalimbali ya muhimu wakati wanafunzi wengine hawakuweko. Inavyoonekana hii iliwaongoza wote kwenye mafunzo maalum na kutamani kwa upande mwingine wa wanafunzi. Kwa uhakika ni kwa nini Yesu aliamua kuwa faragha na jamii ya watu waliomzunguka haijulikani. Orodha ya ya wale thenashara mara zote ilikuwa katika makundi manne yenye watu watatu watatu. Makundi kamwe hayakubadilika. Yawezekana kuwa makundi yalitengeneza ratiba ya mzunguko kwa ajili ya wanafunzi kwenda nyumbani kwa muda Fulani ili kuziangalia familia zao. Angalia Mada
Maalum katika Marko 3:16.

**NASB "akanza kufadhaika na kuhangaika"**
**NKJV "akaanza kuhangaika na kfadhaika sana"**
**NRSV "akaanza kufadhaika na kuhangaika"**
**TEV "kufadhaika na maumivu yakaanza kumwijilia"**
**NJB "akaanza kuwa na hofu na kuwa na maumivu"**

Yesu alikuwa katika hali nzito ya wasiwasi! Haya ni maneno mazito katika lugha ya Kiyunani. Kama ilivyo kwa wasomaji wa leo walivyo katika nchi takatifu hapa kwenye bustani kama tumwonavyo Mwana wa Mungu akiwa kwenye wakati hatari uliompasa mwanadamu kuwako. Yesu alipaswa kuihusianisha hili habari kwa wanafunzi wake baada ya kufufuka. Inavyoonekana ilimaanisha kuwa ya msaada kwa ajili ya wale wote wanaopata majaribu
na kwa ajili ya wale wanaotaka kujua mateso na gharama ya tukio la pale Kalvari.

◙**"'Roho yangu ina huzuni nyingi kiasi cha kufa'"** Haya ni maelezo yenye msisitizo ya kushangaza yakiwa na uhusika, hofu, na machungu kwa upande wa Yesu. Ingawa andiko lenyewe halitoi sababu, inaonekana kuwa kile Yesu alichokihofu ni usumbufu katika ushirika wa ndani aliojulikana siku zote akiwa na Baba. Hili linaainishwa na maneno ya Yesu katika Marko 15:34. Hii ni moja ya nyakati za mwanadamu tulizoruhusiwa kuzishuhudia ndani ya Yesu akiihangaikia imani.
Hii ilikuwa ni nahau ya Agano la Kale (kama vile Zab. 42:5) ambayo ilielezea nguvu kubwa iliyohusika kumkomboa mwanadamu mdhambi. Zaburi 42 inaaksi tukio zima la kukataliwa kwa Yesu na kifo kama ilivyofanya Zaburi 22. Kitu Fulani chenye kuhangaisha chaweza kuonekana katika ufanano wa Luka 22:43-44 (ingawa toleo la UBS4 linatathimini ondoleo lao kuipa alama "A" [pasipo mashaka]) ,ambapo linaweka kumbukumbu kuwa malaika akaja kumsaidia na akatoka jasho jingi la damu. Ushindi juu ya uovu ulishinda hapa katika bustani. Undani wa majaribu ya shetani katika Mathayo 4 na ya Petro yaliyodhaniwa kuwa ya kimsaada, lakini yenye uharibifu mkubwa, yenye
kuchangia hoja katika Mt. 16:22, yanadhihilishwa kikamilifu katika sura hii.

◙**"'kaeni hapa mkeshe'"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu ikifuatiwa na kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Walikuwa kwenye kazi ya ulinzi wakilinda kwa ajili ya Yuda na kundi lake, lakini wakasinzia!

**14:35 "akaanguka kifudifudi, akiomba"** Hizi ni kauli mbili zisizo timilifu. Mara nyingi hii njeo inamaanisha ni tendo endelevu kwenye wakati uliopita, lakini ni wazi hili haliwezikuwa kile kinachomaanishwa hapa. Utumiaji mwingine ya kawaida wa njeo ya kitenzi hiki cha Kiyunani ni mwanzo wa kitendo katika wakati uliopita.kuomba ukiwa umelala kifudifudi inaonyesha uzito wa jambo lenyewe au hisia kali ulizonazo juu ya jambo.

**14:35 "'ikiwezekana '"** Hii ni sentensi yenye masharti daraja la kwanza, ambayo inafikiriwa kuwa kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi. Yesu alijua YHWH anao uwezo wa kufanya kitu chochote (kama vile Marko 14:36,
"mambo yote yanawezekana kwake Yeye!").

◙**"saa"**

## MADA MAALUM: SAA

Neno "saa" limetumika kwa namna tofauti mbalimbali katika injili, kama

1. Rejea ya wakati (kama vile Mt. 8:13; 26:40; Luka 7:21; Yohana 11:9)
2. Stiari kwa ajili ya wakati wa kujaribiwa na majaribu (kama vile Mt. 10:19; Marko 13:11; Luka 12:12)
3. Stiari kwa ajili ya Yesu kuanza huduma Yake (kama vile Yohana 2:4; 4:23)
4. Stiari kwa ajili ya siku ya hukumu (yaani., ujio wa mara ya pili, kama vile Mt. 24:36,44; 25:13; Marko 13:32; Yohana 5:25,28)
5. Stiari kwa ajili ya wiki ya mateso ya Yesu (kama vile Mt. 26:45; Marko 14:35,41; Yohana 7:30; 8:20; 12:23,27; 13:1; 16:32; 17:1)

◙**"saa hiyo imwepuke"** Hii ni kauli tendaji tegemezi ya wakati uliopita usiotimilifu. Yesu anadai kuwa YHWH anaweza kufanya kitu chochote na Yesu anatarajia kuwa aweze kuepushwa na msalaba (kama vile Marko 14:36). Hili lilikuwa jaribu lenyewe la shetani akiwa nyikani, kama vile James Stewart's *The Life and Teaching of Jesus Christ*, kur.39-46). Toka Mt. 26:39,42 na 44 na Marko 14:39 na 41 tunajifunza kuwa Yesu aliomba maombi yale
yale mara tatu, ambayo ilikuwa ni njia ya Kiyahudi kuonyesha uzito wa jambo.

**14:36 "'Aba'"** Hiki ni Kiaramu kwa neno lililozoeleka ambalo watoto hutumia kumwita baba nyumbani, baba, papa, n.k. Yesu aliujua undani wa familia aliokuwanao na YHWH (kama vile Ebr. 1:2; 3:6; 5:8; 7:28). Kifo chake kingeleta ukaribu na sisi. Muktadha huu ndio wakati pekee neno la Kiarama *Abba* limetumika (kama vile katika andiko la Kiyunani) na Yesu. Yesu alidhihilisha mahangaiko mazito aliyokabiliana nayo kwa wakati huu wa majaribu ya mwili (kama vile.,alijaribu kuelezea hisia zake za ndani; akaanguka kifudifudi; akaomba mara tatu). Hapa anaomba akijaribu kutumia alichonacho ili kushinda hali ile, nafasi yake muafaka wa kubadili fikra za Baba kuhusu Kalvari. Alimwita YHWH kwa neno la ndani la kifamilia! Lakini bado kila ombi lake alimalizia na maneno "sio kwa mapenzi yangu, bali mapenzi yako yatimizwe." Mungu Baba aliuonyesha upendo wake kwa ajili ya mwanadamu aliyeanguka kwa kutojibu matakwa ya Yesu. Kulihitajika kuwepo na hatma ya dhabihu kwa ajili ya dhambi, lakini haikuwa rahisi au pasipo gharama kubwa, kihisia na kimwili, kwa ajili ya Yesu na kwa ajili ya Baba! Yesu anatujua kwa sababu anayajua majaribu yote ya mwanadamu (na bado hakuwa na dhambi). Hofu na
wasiwasi na kukatishwa tama sio dhambi! Ushindi ulipatika pale Gethsemani.

◙**"'Baba'"** Injili ya Marko mara nyingi hutumia maneno ya Kiarama na vifungu (kama vile Marko 3:17; 5:41; 7:34; 14:36;15:34). Kiarama kingalikuwa ni lugha itumiwayo na Yesu na wanafunzi wake. Marko anatafakari kila moja ya hili, pale inapoonyesha alikuwa haandikii wasomaji wa Kiyahudi, bali wale wasio Wayahudi, yumkini Warumi kwa sababu ya maneno ya Kilatini na vifungu vinavyopatikana katika kitabu cha Marko. Angalia Mada Maalum : Baba
katika Marko 13:32.

◙**"'kikombe hiki'"** Hii ilikuwa ni stiari kwa ajili ya hatma ya mtu (kama vile Zab. 16:5; 23:5; Yer. 51:2; Mt. 20:22).mara nyingi ilitumika kwa maana yakutoa maamuzi (yaani., kinyume) (kama vile Zab. 11:6; 75:8; Isa. 51:17,22; Yer. 25:15-16,27-28; 49:12; Omb. 4:21; Ezek. 23:31-33; Hab. 2:16). Nahau hii mara nyingi ilihusiana na ulevi , ambayo ni stiari nyingine ya Agano la Kale kwa ajili ya hukumu (kama vile Ayubu 21:20; Isa. 29:9; 63:6; Yer. 25:15-16,27-28). Yesu alihitaji kiondolewe!Hofu sio dhambi. Alijawa na hofu akiwa na imani; hivyo imetupasa na sisi!

◙**"'sio kwa mapenzi Yangu, bali kwa mapenzi Yako'"** Viwakilishi nomino "Mimi" na "Wewe" vipo katika nafasi ya msisitizo katika Kiyunani. Huu ulikuwa ni mwendelezo wa Yesu kujitoa kwenye mapenzi ya Baba. Katika muktadha huu ule ubinadamu wa kweli na imani ya Yesu ulionekana! Ingawa asili yake ya ubinadamu ililia kwa ajili ya kukombolewa, moyo wake ulikuwa tayari kuyatimiza mapenzi ya Baba kwa upatanisho mbadala (kama vile
Marko 10:45; Mt. 26:39).

**14:37,40 "akawakuta wakiwa wamelala"** Hawa wanafunzi pia walikutwa wamelala kipindi Yesu anabadilika sura (kama vile Mt. 26:43 na Luka 9:32). Halikuwa kosa au kutofikiri vizuri, lakini ni ubinadamu! Kabla hatujawa wepesi wa kuwalaumu wanafunzi, tutambue kuwa katika Luka 22:45 kifungu "walikuwa wamelala wakiwa na huzuni" kinaelezea kuwa hawakuweza kuchukuliana na maumivu ya unabii wa Yesu kuhusu kifo chake na hatimaye kutawanyika kwao. Ingawa Yesu alitamani kuwa na ushirika na mwanadamu na kuomba kwa kipindi hiki mahangaiko ya mwisho katika maisha yake, alipaswa kuukabili muda huu peke yake, na aliukabili kwa ajili ya
waamini wote!

**14:37 "'Simoni'"** Huu ndio muda pekee Yesu alipomwita "Simoni" tangu pale alipomwita katika Marko 3:16. Mwamba (yaani., Petro) alikuwa kila kitu lakini imara,mwenye uhakika, na mwaminifu. Petro alipaswa kukumbuka hili jina "lililogeuzwa" kwa maumivu makali. Nina uhakika kuwa aliupata ujumbe!

**14:38 "kesheni na kuomba'"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo na kauli ya kati (shahidi) shurutishi ya wakati uliopo. Muktadha ufuatao unamdhihilisha adui.

◙"'**kuwa msije mkaingia majaribuni'"** pamekuwepo na nadaharia mbalimbali kwa nini "majaribu" yanarejelewa katika muktadha huu:

1. Unabii wa Yesu wa papo kwa papo katika Marko 14:27
2. Wanafunzi kukutwa wakiwa wamelala badala ya kuomba, Marko 14:37,40
3. Wanafunzi kumwacha Yesu katika Marko 14:56
4. Kukana kwa Petro katika Marko 14:69-75
5. Majaribu ya kiserikali na kidini (kama vile Mt. 5:10-12; Yohana 9:22; 16:2)

Neno "majaribu" (*peirasmos*) lina kidokezo cha "kumjaribu au kujaribu kwa lengo la kuangamiza" (kama vile Mt. 6:13; Luka 11:4; Yakobo 1:13). Mara nyingi hukinzana na neno jingine la Kiyunani kwa ajili ya jaribu (*dokimazo*) ambalo lina kidokezo cha "kujaribu kukiwa na mtizamo wa kumtia mtu nguvu." Hata hivyo, haha madokezo mara zote hayako katika kila muktadha.Kithiolojia inaweza kusemekana kuwa Mungu hamjaribu mtu au watoto wake ili kuwaangamiza, bali hutoa fursa nyingine kwa ajili ya ukuwaji wa kiroho kupitia majaribu (kama vile Mwa. 22:1; Kut. 16:4; 20:20; Kumb. 8:2,16; Mt. 4; Luka 4; Ebr. 5:8). Hata hivyo, mara zote hutoa njia ya kutokea (kama vile 1 Kor. 10:13). Angalia Mada Maalum: Maneno ya Kiyunani Kwa ajili ya Kujaribu

◙"'**roho I radhi, lakini mwili u dhaifu'"** Hii yaweza kuwa ni hoja juu ya Petro na maneno mengine ya wanafunzi katika Marko 14:29,31. Yesu aliujua mvutano huu kikamilifu (kama vile Marko 14:36). Utumiaji wa neno "roho" likihusiana na roho ya mwanadamu huzungumzia maisha yetu ya ndani na fikra (kama vile Zab.51:10,12,17). Katika maandiko ya Paulo "roho" mara zote hukinzana na "mwili" (kama vile Rum. 8:1-11).

**14:40 "wala hawakujua la kumjibu"** Hawakuwa na sababu inayojielezea (kama vile Marko 9:6) isipokuwa udhaifu wa mwili (kama vile Luka 9:32).

**14:41 "'sasa laleni na mkapumzike'"** Ni ngumu kuitafasiri hii nahau ya Kiyunani. Je ni swali? Je ni kejeli? Je ni maelezo? Ingawa maana kamili haijulikani, ni dhahili kuwa Yesu amekwisha shinda na na sasa amesimama imara, tayari kuyakabiri majaribu ya usiku, mijeredi ya asubuhi na kusulubiwa.

◙**"yatosha"** Neno lilisababisha waandishi mbalimbali kubadilika katika desturi za machapisho ya Kiyunani. Je kifungu hiki kinarejelea kulala kwa wanafunzi? Chaweza kutafasiriwa (1) "yatosha"; (2) "yametimia"; au (3) "imekwisha" (kama vile toleo la NJB "yote yametimia"). Lilitumika katika mafunjo ya Kiyunani ya lugha ya kawaida ya Koine, huko Misri kwa ajili ya kitu fulani kilichokwisha lipiwa pasipo deni (kama vile Moulton and Milligan, *The Vocabulary of the Greek NewTestament*, kur. 57-58). Hii, hatimaye, ingalikuwa kitu Fulani chenye kufanana na kile kilichoko katika Yohana 19:30, "imekwisha" au "imekwisha lipiwa." Yumkini inarejelea kwa Yuda na usaliti wake, ambalo lilipaswa kupimwa kiuzito wake juu ya Yesu. Yesu alishinda ushindi wa kiroho pale Gethsemani!

**14:41c-42** Maelezo yasiyolandana yanasisitizwa kwa kuwa na viungo na viunganishi (*asyndeton*) kati yao. Matukio yalikuwa yakielezewa kama Yesu alivyokwisha tabiri. Muda umekwisha wadia

◙**"saa imewadia"** angalia Mada Maalum katikaMarko 14:35.

◙"'**anayenisaliti'"** Neno hili (*paradidōmi*) kwa kawaida linamaanisha "kukabidhiwa mikononi mwa" (kama vile Marko 9:31), lakini uhusiano wake na Yuda katika tafasiri nyingi za Kiingereza linaongeza uzito kwenye neno "kusaliti."angalia kumbukumbu kamili katika Marko 14:10d.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 14:43-50**
**[43]Basi alipokuwa katika kusema, mara Yuda alifika, mmoja wa wale Thenashara, na pamoja naye mkutano, wana panga na marungu, wametoka kwa wakuu wa makuhani, na waandishi, na wazee. [44]Na yule anayemsaliti alikuwa amewapa ishara, akisema, Nitakayembusu, huyo ndiye; mkamateni, mkamchukue salama. [45] Basi alipokuja, mara**

**akamwendea, akasema, Rabi, akambusu. 46Wakanyosha mikono yao wakamkamata. 47Na mmoja wao waliokuwapo akafuta upanga, akampiga mtumwa wa Kuhani Mkuu, akamkata sikio. 48Yesu akajibu, akawaambia, Je! Ni kama juu ya mnyang'anyi mmetoka wenye panga na marungu, kunitwaa mimi? 49Kila siku nalikuwa mbele yenu hekaluni nikifundisha, msinikamate; lakini haya yamekuwa ili maandiko yapate kutimia. 50Ndipo wakamwacha, wakakimbia wote.**

**14:43 "mara Yuda alipofika"** angalia kumbukumbu katika Marko 1:10.

◙**"mkutano"** Yohana 18:3,12 inasema askari wa Kirumi walikuwepo. Luka 22:52 inasema wawakilishi toka kwenye baraza kuu la Sinagogi walikuweko katika mkusanyiko ule, ambao walikuwa walinzi wa hekalu. Sababu ya kuwepo na walinzi wengi ilikuwa ni kwa sababu ilikuwa ni majira ya Pasaka na mamlaka ilikuwa ikihofu juu ya Maandamano (kama vile Marko 14:2; Mt. 26:5;27:24).

◙**"mapanga na marungu"** Neno "mapanga" yanarejelea panga fupi zilizovaliwa na askari wa Kirumi kwenye mishipi yao. "marungu" yanarejelea hasa kwenye silaha zilizotumiwa na askari wa hekaluni.

◙**"wakuu wa makuhani, na wandishi na wazee"** Hili linarejelea kwa wakuu wa Sinagogi. Angalia Mada Maalum katika Marko 12:13.

**14:44 "mkamateni"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu.

**NASB, NRSV**
**TEV "mkamchukue chini ya ulinzi"**
**NKJV "mkamchukue salama"**
**NJB "angalieni mnamlinda vizuri mtakapomchukua"**

Hili ni neno la Kiyunani *sphallomai* ( "kuanguka au kujikwaa") likiwa na kiambishi awali hasi, ambacho kinakanusha. Hili neno ni la kiistiari kwa ajili ya "kuwa salama, imara." Yuda aliogopa Yesu angalifanya kitu chochote cha kuweza kumzuia kukamatwa.Hii inadhihilisha hofu ya Yuda. Alikwishaona miujiza ya Yesu na uwezo wake.

**14:45 "akasema, 'Rabbi!' na akambusu"** Kumbusu mtu kwenye shavu au paji la uso ilikuwa ni salamu ya kawaida kwenye utamaduni huu (hasa kati ya walimu wa dini ya Kiyahudi). Soma hoja ya Yesu juu ya matendo ya Yuda katika Mt. 26:50; Luka 22:48.Hii ishara inaonyesha kuwa huenda walikuwa askari wa Kirumi kwa vile askari wa hekalu wangalimtambua Yesu.

**14:47 "Mmoja wao aliyekuwepo akafuta upanga"** Kutokana na ufanano wa Yohana 18:10 na Luka 22:50-51, tunatambua kuwa huyu alikuwa Petro na Yule mtumwa aliyejeruhiwa alikuwa Malkusi. Wanafunzi walikwisha onywa kununua mapanga (kama vile Luka 22:36-38), lakini inavyoonekana, hawakuelewa maana kamili ya Yesu kuhusu suala hili. Lilipaswa kusemwa kwa niaba ya Petro kuwa alikuwa tayari kufa kwa ajili ya Bwana. Kutokana na kuwepo uwezekano mkubwa, alichomoa moja ya zile panga mbili. Lakini, tena, kwa uharaka na matendo yasiyofaa yaliainisha tabia yake.

◙**"mtumwa wa kuhani mkuu"** Yohana 18:10 inamwita Malkusi.

◙**"akamkata sikio"** Katika Luka 22:51, Yesu akalirejesha!

**14:48**
**NASB, NKJV "mnyang’anyi"**
**NRSV, NJB "haramia"**
**TEV "mharifu"**

Walimtenda Yesu kama mharifu, na sio mwenye kukufuru. Walimtendea Yesu yale yaliyompasa Baraba kutendewa (kwake yeye maneno yale yale yalitumika, kama vile Yohana 18:40).

**14:49 "'Kila siku nalikuwa nanyi heakaluni nikifundisha'"** Hili lilisemwa kwa wakuu wa Sinagogi au askari wa hekalu. Yesu alifichua hoja yao ya siri.

◙**"'lakini haya yamekuwa ili maandiko yapate kutimia'"** Katika Marko 14:50 "wanafunzi wake wote wakamuacha" (kama vile Marko 14:27, inayonukuu Zak. 13:7 na Mt. 26:31). Mtu hushangaa ni namna gani Yohana 18:15-16 inafaa kwenye unabii huu. Inaonekana kuwa Yohana aliongozana na Yesu kwenye majaribu yote na alikuweko wakati akisulubiwa (kama vile Yohana 19:26-27).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 14:51-52**
**[51] Na kijana mmoja alimfuata, amejitanda mwili wake nguo ya kitani; wakamkamata; [52]naye akaiacha ile nguo ya kitani, akakimbia yu uchi.**

**14:51-52 "kijana mmoja. . .akivaa nguo ya kitani mwilini mwake"** Desturi za kanisa zinasema huyu alikuwa Yohana aitwaye Marko, mtungaji wa injili hii. Alikuwa ni Mmisionari mwenza wa mwanzo wa mjomba wake, Barnaba (kama vile Mdo. 12:25), na Sauli (Paulo) wa Tarso. Kidesturi kwa nguvu inadaiwa kuwa alikuwa ni mwandishi kwa ajili ya kumbukumbu ya Petro juu ya maisha ya Yesu (yaani.,injili ya Marko). Desturi pia zinasema palikuwa nyumbani kwake pale palipofanyika karamu ya mwisho (kama vile Mdo. 12:12). Haikujulikana kwa nini alivikwa hivi. Yumkini aliambiwa akiwa amelala kuwa Yesu alikuwa katika hatua ya kukamatwa au huenda alijaribu kuwa karibu na Yesu na wanafunzi na walikuwa wamelala karibu naye kule bustanini.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 14:53-65**
**[53]Nao wakamchukua Yesu kwa Kuhani Mkuu; wakamkusanyikia wote, wakuu wa makuhani na wazee na waandishi. [54]Naye Petro akamfuata kwa mbali, hata ndani katika behewa ya Kuhani Mkuu; akawa ameketi pamoja na watumishi, anakota moto mwangani. [55]Basi wakuu wa makuhani na baraza yote wakatafuta ushuhuda juu ya Yesu wapate kumwua; wasione. [56]Kwa maana wengi walimshuhudia uongo, walakini ushuhuda wao haukupatana. [57]Hata wengine wakasimama, wakamshuhudia uongo, wakisema, [58]Sisi tulimsikia akisema, Mimi nitalivunja hekalu hili lililofanyika kwa mikono, na katika siku tatu nitajenga jingine lisilofanyika kwa mikono. [59]Wala hata hivi ushuhuda wao haukupatana. [60] Kisha Kuhani Mkuu akasimama katikati, akamwuliza Yesu, akisema, Hujibu neno? Hawa wanakushuhudia nini? [61]Lakini akanyamaza, wala hakujibu neno. Kuhani Mkuu akamwuliza tena, akamwambia, Wewe ndiwe Kristo, Mwana wake Mtukufu? [62]Yesu akasema, Mimi ndiye, nanyi mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu, akija na mawingu ya mbinguni. [63]Kuhani Mkuu akararua nguo zake, akisema, Tuna haja gani tena ya mashahidi? [64]Mmesikia kufuru yake; mwaonaje ninyi? Wote wakamhukumu kuwa imempasa kuuawa. [65]Wengine wakaanza kumtemea mate, wakamfunika uso, na kumpiga makonde, na kumwambia, tabiri. Hata watumishi nao wakampiga makofi.**

**14:53 "Wakamchukua Yesu kwa Kuhani Mkuu"** Yohana 18:13a inamtaja Anasi, lakini Kayafa alikuwa ni Kuhani Mkuu toka 18-36 B.K (kama vile Mt. 26:57). Madokezo ya injili hayaandiki kuhusu mazungumzo yaliyofanywa na Anasi. Alikuwa ni Kuhani Mkuu aliyepita na aliyesimama kwa nguvu sehemu ya kazi (kama vile Yohana 18:13b).

◙**"wakuu wote wa makuhani na wazee na wandishi"** Hiki kifungu kilitumika kuonyesha baraza kuu, wakuu wa Sinagogi (kama vile Marko 14:55). Angalia Mada Maalum katika Marko 12:13.

**14:54** Huu mstari unaweka hoja kwa ajili ya kukana kwa Petro mbele ya baraza. Petro asingeweza kukaa mbali, lakini asingeweza kujitambua mwenyewe akiwa na Yesu. Ni kejeri namna gani!

**NASB "akiwa ameketi pamoja na maafisa"**
**NKJV "ameketi pamoja na watumishi"**

**NRSV "akiwa ameketi pamoja na walinzi"**
**TEV "akaketi chini pamoja na walinzi"**
**NJB "akiwa amekaa pamoja na watumishi"**

Hii ni kauli ya kati timilifu (shahidi) endelevu yenye mafumbo. Inaonekana kudokeza kuwa Petro alijaribu kutenda kama mmoja wa watumishi. Alitaka kupotea kwenye lile kundi, lakini mwonekano wake na rafudhi yake ni ya Kigalilaya. Petro anaukumbuka usiku ule vizuri!

**14:55** Hili halikuwa jaribu la kisheria; lilikuwa ni jaribu la kuiga (kama vile A. N. Sherwin-White, *Roman Society and RomanLawin The NewTestament*, kur. 24-47).

**14:56 "wengi walimshuhudia uongo"** Njeo ya wakati usiotimilifu (katika mstari huu imetokea mara mbili na katika Marko 14:57 na 59) inaonyesha jaribu lenye kujirudia la ushuhuda wa uongo. Hili lilikuwa ni gwaride la waongo wabaya!

◙**"ushuhuda wao haukupatana"** Katika agano la kale ulichukuliwa ushuhuda wa watu wawili ili kumweka mtu hatiani (kama vile Kumb. 17:6; 19:15). Pia katika Agano la Kale ikiwa mtu atashuhudia ushuhuda wa uongo iliruhusiwa kupewa adhabu ya mshitakiwa.

**14:58 "'nitalivunja hekalu hili '"** Mstari huu ni mfano mzuri kuhusu utumiaji wa Yesu wa stiari kuelezea matukio yajayo. neno "hekalu" linasimama kwa mambo mawili au vipindi viwili

1. Mwili wa Yesu (kama vile Yohana 2:19-22) ulisulubiwa, lakini ukafufuka ndani ya siku tatu (yaani., ishara ya Yona, kama vile Mt. 12:39-40; Luka 11:29-32). Hili lilitokea ndani ya masaa.
2. Hekalu la Herode huko Yerusalemu lilipelekea kuangamizwa na Warumi katika mwaka wa 70 B.K na halikujengwa tena.

Hii ilikuwa ni hukumu ya wakati ujao yapata miaka 40, lakini inaaksi hukumu ya siku za mwisho (yaani., 2 The. 2; na Ufunuo). Ni rahisi kuona namna maisha ya Yesu, bado ya kimatukio ya siku za mwisho na mfumo wake wa kimaadili waweza kueleka vibaya na wenye imani kali, washika sheria, watu wa dini, baadaye na sasa.

◙**"'katika siku tatu'"** Nukuu hii ya muda (kama vile Marko 8:31; 9:31; 10:34) inahusiana na unabii wa Agano la Kale katika 1 Kor.15:3-4. Muda wa"siku tatu" unahusiana na "hekalu jipya" na ufufuko mpya wa mwili. Yesu kwa makusudi aliyagawa haya mawili. Hekalu la enzi mpya ni waumini, kibinafsi na kwa wote (kama vile 1 Kor. 3:16; 6:19).

◙**"'nitajenga jingine lisilofanyika kwa mikono'"** Huu ni unabii wa kushangaza wa kifo cha Yesu na ufufuko.Kama hekalu lilivyokuwa muhimu katika ibada za Agano la Kale, sasa atakuwa Yesu mwenyewe. Yeye ni jiwe la pembeni lililokataliwa! Ni mtizamo mpya wa ibada! Ana nguvu za kuyatoa maisha yake na kuyachukua tena (kama vile Yohana 10:11,15,17,18). Yeye yuko katika uangalizi kamili wa maisha yake na kifo na ufufuko.

**14:60 "Kuhani Mkuu akasimama katikati, akamuuliza Yesu"** Kuhani Mkuu alikuwa akijaribu kumfanya Yesu aingie hatiani Mwenyewe. Hili lilikuwa ni kosa chini ya sheria za Kiyahudi, kwa vile lilikuwa jaribu la usiku na jaribu na adhabu kufanyika siku moja.

**14:61 "lakini akanyamaza"** Huu wawezakuwa ni utimilifu wa Isa. 53:7 (kama vile Mt. 26:63; 27:12-14; Marko 15:5; Luka 23:9; Yohana 19:9).

◙**"Kuhani Mkuu akamuuliza tena"** Mt. 26:63 inaongeza kuwa akamweka chini ya kiapo.

◙**"Kristo"** Hii ni tafasiri ya Kiyunani ya neno la Kiebrania Masihi lenye kumaanisha "mpakwa mafuta." Katika manabii wa Agano la Kale, makuhani, na wafalme walitiwa mafuta kama alama ya chaguo la Mungu na chombo kwa ajili ya kazi maalum. Neno likajakuwa likitumika kwa ajili ya ukuu maalum "mwana wa Daudi" (kama vile 2 Sam. 7) ambaye angaliiokoa na kuirejesha Israeli.

◙**"Mwana wake Mtukufu"** "Mbarikiwa" ni jina la kawaida la Kiyahudi (kama vile.,mwenye maneno mengi) kwa ajili ya Mungu. Wayahudi hawakutegemea Masihi kuwa Mungu mwenye kufanyika mwili, bali mwanadamu aliye kirimiwa/aliyetiwa nguvu, kama walivyo waamuzi. Lakini Yesu alitumia uhusiano wa kifamilia kutetea usawa wake kamili na Baba (kama vile Yohana 5:18;10:30,33; na pia 1:1).

**14:62 "'Mimi ndiye'"** Hili lingeweza kuwa dokezo kwenye Agano la Kale kwa jina la Mungu wa agano, YHWH, ambalo lilikuwa ni kutokana na kitenzi cha Kiebrania "kuwa" (kama vile Kut. 3:14; Kumb. 32:39; Isa. 41:4; 43:10; 46:4; Yohana 4:26; 8:24,28,58;13:19; 18:5). Angalia Mada Maalum: Majina ya Uungu katika Marko 12:36. Hili jibu la moja kwa moja linafanana na lile la Luka 22:70. Mathayo anaandika majibu mengi ya siri (kama vile Mt. 26:64). Ni injili ya Marko ambayo inaonyesha ufahamu binafsi wa Yesu tokea mwanzo kama mwana wa Mungu na Masihi (kama vile Marko 1:1). Mapepo pia yalimtambua na kwa maneno yakamthibitisha (kama vile Marko1:24,34; 3:11), lakini wanafunzi walikuwa wagumu kuweza kutambua (kama vile Marko 8:29) ubinadamu wa Yesu na kazi yake.

◙**"'mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu'"** Hili ni dokezo kwa Zab. 110:1. Ilikuwa ni stiari ya lugha ya binadamu kumueleza Mungu kwa ajili ya nafasi ya mamlaka. Neno "nguvu" ni rejeo la maneno ya kuzunguka kwa YHWH. Yesu (yaani.,mwana wa Adamu, kama vile Marko 14:21,41,62) inatetea katika maneno ya matukio ya siku ya mwisho ambayo yangalifahamika kuwa alikuwa Masihi wa YHWH. Hata kama Zab. 110:4 ina kidokezo cha kikuhani, mstari huu una kidokezo cha ufalme (kama vile Ebr. 1:3). lazima ifahamike kuwa ufahamu wa Kuhani Mkuu juu ya swali la Marko 14:61 ulikuwa tofauti na uelewa wa Yesu (ni ukweli unaofanana na swali la Pilato katika Marko 15). Kuhani mkuu alitambua ni tishio kwenye ukuu na mamlaka yake na mamlaka ya Kirumi.
Dhana ya Agano la Kale la Masihi kama mfalme ashindaye liligawanwa kwa usawa na Mitume (kama vile Marko 10:37). Yesu, hata hivyo, aliuona ufalme Wake kama wa kiroho na wa kutarajiwa (kama vile Yohana 18:36). Hii ndiyo sababu ananukuu hizi sura za matukio ya siku za mwisho toka Zaburi 110 na Danieli 7. Hakika kuna fumbo lilihusishwa kwenye ujio mara mbili, moja kama mwenye kunyenyekea, mtumishi ateswaye na nyingine kama mfalme aliyetukuka na mwamuzi. Agano la Kale linayawasilisha yote, lakini Wayahudi wanaliangazia lile la pili tu. Hii ni hofu ya kithiolojia ile ile kama ufalme wa Mungu—ulioanzishwa, lakini haukukamilishwa! Ni ngumu kwetu kuweza kufikiri ni namna gani ilivyokuwa vigumu kwa ajili ya Wayahudi wa siku za Yesu kuweza kuelewa ujumbe Wake.

◙**"'akija na mawingu ya mbinguni'"** Hii ni nukuu toka Dan. 7:13. Ni kifungu kilichotetea Uungu wa Yesu kwa maneno ya wazi ya Agano la Kale. Hakuna awezaye kuja juu ya mawingu isipokuwa YHWH, lakini sasa "mwana" Wake amefanya pia (kama vile Marko 13:26; Mdo. 1:9; Ufu. 1:7).

**14:63 "akiyararua mavazi yake"** Hii ilikuwa ishara ya ndani ya roho yenye hofu iliyosababishwa na makufuru yaliyodhaniwa. Adhabu kwa ajili ya kukufuru toka kitabu cha Law. 24:15 ilikuwa ni kifo kwa kupigwa mawe. Yesu alistahili kufa kwa msingi wa Kumb. 13:1-3 na 18:22 ikiwa hakuwa Yule ajaye, Masihi, mwana wa Mungu, mkombozi wa ulimwengu. Huenda ndiye aliyedai kuwa au ni Yule aliyekufuru akistahili kifo (kama vile Yosh McDowell's, *Evidence That Demands a Verdict*).

**14:64 "kufuru"** Aliyezungumza kinyume kuhusu YHWH alistahili adhabu ya kifo kwa kupigwa mawe (kama vile Law.24:14-16).

**14:65 "kumtemea mate"** Hii ilikuwa ni alama ya Agano la Kale ya kukataliwa (kama vile Heb. 12:14; Kumb. 25:9; Ayubu 17:6; 30:10; Isa. 50:6). Jamii ya wakuu wa Sinagogi na askari wa Kirumi (kama vile Marko 15:19) wakamtemea mate Yesu

◙**"wakamfunika uso, wakampiga makonde, na kumwambia, atabiri"** Wakamfunika uso, wakampiaga na kumuuliza, na kumuuliza, "tabiri?" walikuwa wakimdhihaki madai yake kuwa ni nabii wa Mungu. Walimu wa dini ya Kiyahudi wa siku za Yesu waliitafasiri Isa. 11:3 kuwa Masihi anaweza kutabiri kwa kunusa, na sio kuona. Hili laweza au halikurejelea hili tukio. Hakika linahusiana kwa Isa. 52:14. Walimu wa dini ya Kiyahudi waliutafasiri mstari huu kwa kusema Masihi angalikuwa na ukoma, lakini nafikiri hili lingerejea kwa haya mapigo mbalimbali toka kwa makundi ya askari tofauti. Maandiko mbalimbali ya Kiyunani yanaliongezea hili andiko la Marko kuliaksi

andiko la Mt. 26:68 na Luka 22:64.

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"wakampiga makonde"** |
| **NKJV** | **"wakampiga kwa makofi"** |
| **NRSV** | **"wakampiga"** |
| **TEV** | **"wakampiga"** |
| **NJB** | **"wakimpiga"** |

Habari hii ya kumtukana Yesu hutumia maneno ya Kiyunani *kolaphizō*, yenye kumaanisha kumpiga kwa makonde, na *hrapizō*,lenye kumaanisha kumpiga kwa kofi (kama vile Mt. 26:67). Kupiga kwa kofi ni alama ya awali ya kotofurahi (kama vile Mt. 5:39; Yohana 18:22; 19:3). Maneno yale yale yanarejelea "kupiga kwa fimbo" katika Mdo.16:27. Wote wakuu wa baraza la Sinagogi na askari wa Kirumi walimdhalilisha Yesu na kimwili kumtukana (kama vile Isa.52:14; 53:4).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 14:66-72**
**66 Na Petro alikuwa chini behewani; akaja mmoja wa vijakazi wa Kuhani Mkuu, 67akamwona Petro akikota moto;**
**akamkazia macho, akasema, Wewe nawe ulikuwapo pamoja na yule Mnazareti, Yesu. 68Akakana, akasema, Sijui**
**wala sisikii unayoyasema wewe. Akatoka nje hata ukumbini; jogoo akawika. 69Na yule kijakazi akamwona tena,**
**akaanza tena kuwaambia waliosimama pale, Huyu ni mmoja wao. 70Akakana tena. Kitambo kidogo tena wale**
**waliosimama pale wakamwambia Petro, Hakika u mmoja wao, kwa sababu u Mgalilaya wewe. 71Akaanza kulaani**
**na kuapiza, Simjui mtu huyu mnayemnena. 72Na mara jogoo akawika mara ya pili. Petro akalikumbuka lile neno**
**aliloambiwa na Yesu, Kabla ya kuwika jogoo mara mbili, utanikana mara tatu. Na alipolifikiri, akalia.**

**14:66 "akaja mmoja wa vijakazi wa Kuhani Mkuu"** Yohana 18:17 inasema kuwa alikuwa ni mlinzi wa mlangoni. Mathayo, kama kawaida, alikuwa na watu wawili, wakati Marko alikuwa na mtumwa mmoja tu (kama vile Mt. 26:69-71). Petro angalikwisha kumwambia Yohana aitwae Marko hii habari isiyofurahisha au aliitumia kwenye
moja ya jumbe zake huko Rumi na Yohana aitwae Marko aliusikia.

**14:67 "akamwona Petro"** Ulikuwa ni mwezi mkomavu (Pasaka) aliweze kumwona petro kwa mwanga wa moto Marko 14:54, 67; Yohana 18:18,25) na mwanga wa mbaramwezi.

◙**"' Yesu Mnazareti"** Wayahudi waliokulia Galilaya (kama vile Mt. 26:69) walikuwa na lafudhi tofauti.Hili linahusiana na Yesu kwa wanafunzi wake (kama vile Marko 14:70). Angalia Mada Maalum katika Marko 10:47.

**14:68 "'sijui wala sisikii unayoyasema wewe'"** Maelekezo kamili ya haya mashitaka matatu yanatofautina toka injili moja hadi nyingine.Ukweli kuwa Petro alimkana Yesu mara tatu mfululizo ni wa kawaida katika injili zote.

◙**"na akatoka nje hata ukumbuni"** Inavyoonekana Petro alijaribu kuondoka. Machapisho ya Kiyunani ya herufi kubwa yanagawa sawa juu ya kifungu ikiwa "na jogoo alipowika" kiweze kujumuishwa kwenye Marko 14:68 (maandiko ya herufi kubwa ya MSS A, C, D vile vile na tafasiri za Vulgate, Peshitta yanakijumusha, wakati, א, B, L, na W yanakiondoa). Kwa uwazi kinaelezewa "mara ya pili jogoo alipowika" kwenye Marko 14:72. Baadhi ya tafasiri za kisasa (kama vile NASB, NIV) zinakiondoa, lakini mengine mbalimbali yanakijumuisha kikiwa na tanbihi (kama vile NKJV, NRSV, TEV, NJB). Toleo la UBS[4] haliwezi kuamua ni lipi la mwanzo.

**14:70 "baada ya muda kitambo"** Luka 22:59 ina kifungu "yapata saa moja."

◙**"Wagalilaya"** Huenda kuzungumza kwa Petro au yumkini hata kuvaa kwake kulimsababisha aondoke.

**14:71 "akaanza kulaani na kuapiza"** Neo "kulaani" (*anathematizō*) mwanzoni lilirejelea kwa kitu Fulani kilichotolewa kwa Mungu (*anathēma*), lakini baadaye likaja kurejelea kwenye laana (kama vile Mdo. 23:12,14,21). Ilikuwa ni namna ya kutetea uaminifu wa maelezo kwa kushusha chini hukumu ya Mungu kwa mtu ambaye hakusema ukweli.Petro, kwa namna ya nguvu ya kimila (yaani.,kiapo na kuapiza) alisema uongo mbele za Mungu! Yuda hakufanya chochote kibaya

kuliko Petro! Petro alimkana Bwana kwa kujirudia, kwa msisitizo, na kwa maneno ya kukemea mbele ya watu (kama vile Mt. 26:34,74).

## MADA MAAALUM: LAANA (*ANATHEMA*)

I. AGANO LA KALE

Kuna maneno kadhaa katika Kiebarania yenye kuzungumzia neno"laana." Neno *Herem* (BDB 356, KB 353) lilitumika kumaanisha jambo fulani lilitolewa kwa Mungu (kama vile Agano la kale la Kiebrania - LXX linalitafsri neno hili kama *anathema,* BAGD 54, Lev. 27:28). Mara nyingi neno hili limehusishwa katika uharibifu wa vitu kwa sababu lilikuwa takatifu sana kwa matumizi ya mwanadamu (kama vile Kumb. 7:26; Yos. 6:17-18; 17:12). Hili lilikuwa neno lililotumika katika dhana ya "vita takatifu." Mungu alimwambia Yoshua kuwaaharibu Wakanaani. Yeriko ilikuwa nafasi ya kwanza, "matunda ya kwanza" ya uharibifu huu mtakatifu/ utakaso.

II. AGANO JIPYA

Katika Agano Jipya neno *anathema* na miundo yake inayohusiana ilitumika katika maana kadhaa na tofauti:

A. kama uzuri au sadaka kwa Mungu (kama vile Lukea21:5)
B. kama kiapo cha kifo (kama vile Matendo ya Mitume 23:14)
C. kulaani na kuapa (kama vile Marko 14:71)
D. Kanuni ya laana iliyohusiana na Yesu (kama vile 1 Kor. 12:3)
E. Mungu kumtia mtu au kitu fulani katika hukumu au uharibifu (kama vile Rum. 9:3; 1 Kor. 16:22; Gal. 1:8-9)

Namba D hapo juu inakanganya sana. Nimehusisha maelezo yangu kutoka 1 Kor. 12:3:

" Yesu amelaaniwa " ni usemi unaleta mshtuko. Kwa nini mtu ye yote (isipokuwa mapokeo ya Kiyahudi) adai azungumzie Mungu kuwa alinene hili? Hili neno (yaani, *anathema*) lenyewe lilikuwa na maelezo ya nyuma ya Agano la Kale (yaani, Kiebrania, herem). Hili lilihusiana na dhana ya Vita Takatifu, ambapo mji ulitengwa kwa ajili ya Mungu na, hivyo, ulikuwa mtakatifu. Hili lilimaanisha kwamba kila kitu kina pumzi ndani yake, mwanadamu au mnyama, yampasa kufa (kama vile Yos. 6:17; 7:12). Nadharia zinazohusu namana neno hili lilivyotumia katika Wakorintho ni:

1. kwamba hili lina muundo wa Kiyahudi uliohusu viapo vya sinagogi (kama vile Matendo ya Mitume 26:11,yaani, baadaye, kanuni za laana ya kisheria zilitumika kuwaondoa Wakristo katika sinagogi). Kubaki mmojawapo ilimpasa mtu kumkataa au kumlaani Yesu wa Nazarethi.
2. kwamba hili lina muundo wa Kirumi unaohusiana na kumwabudu Mfalme ambapo Kaizari pekee ndiye angeitwa "Bwana"
3. kwamba hili lina muundo wa ibada ya kipagani ambapo laana zilitamkwa juu ya watu kwa kuliitia jina la mungu. Hili pia linaweza kutafsiriwa, "Yesu Anaweza kulaani ——" (kama vile 1 Kor. 16:22).
4. kwamba alihusianisha kifungu hiki na dhana ya Yesu kithiolojia ya tabia za laana za Agano la Kale kwetu sisi (kama vile Kumb. 21:23; Gal. 3:13).
5. Mafunzo ya sasa kutoka Korintho (kama viletambihi #1 uk. 164 katika Bruce Winter's *After Paul Left Corinth*) inanukuu marekebisho neno laana linalopatikana katika makumbusho a zamani huko Korintho. Wasomi wa ki-Biblia wamekuwa wakidhani kwamba KITENZI unganishi "ni" lazima kiwekwe ndani ya kifungu, "Yesu anashtakiwa," lakini ushahidi huu wa elimu kale kwa usahihi kabisa unaonyesha kwamba laana hizi za kipindi cha karne ya kwanza ya Kirumi kutoka Korintho zinapungukiwa KITENZI (kama zilivyo baadhi ya laana katika Agano la Kale la Kiebrania- LXX la Kumb. 22:15-20), kama ifanyavyo 1 Kor. 12:3. Kuna ushahidi mwingine zaidi wa elimu kale kwamba Wakristo wa karne ya kwanza ya Korintho ya Kirumi walitumia kanuni za laana katika utaratibu wa mazishi (yaani, kipindi cha Byzantine, unaopatikana katika makaburi ya ki-Kristo (J. H. Kent, The Inscriptions,

1926-50. Princeton: American School of Classical Studies, 1966, juzuu. 8:3, na. 644).
Sehemu zingine za kanisa la huko Korintho zilikuwa zikirejea kwa laana za kipagani kwa jina la Yesu dhidi ya washirika wengine wa kanisa. Hii si njia pekee ya tatizo, bali pia sababu ya chukizo. Huu ni mfano mwingine wa mvutano ndani ya kanisa hili. Paulo aliwataka kujenga kanisa, kuliadilisha kanisa; hawa walitaka kuilaani sehemu ya kanisa!

◙**"'Simjui mtu huyu'"** Yawezekana kifungu "mtu huyu" ilikuwa ni nahau ya matusi ya lugha ya Kisemiti yenye kumrejelea Yesu.
**14:72 "na mara jogoo akawaika mara ya pili"** Petro akakumbuka maneno ya Yesu (kama vile Luka 22:31-32). Luka 22:61 inasema Yesu akamwangalia. Inavyoonekana Yesu akatolewa toka kwa Anasi hadi kwa Kayafa. Kifungu "mara ya pili" kimeondolewa kwenye baadhi ya machapisho ya Kiyunani. Tatizo walilolipata waandishi ni kuwa injili nyingine tatu (yaani., Mathayo, Luka na Yohana) zinataja tu jogoo alipowika mara ya kwanza, wakati Marko inaonyesha mara ya pili (kama vile maandiko ya MSS A, B, C2, D na W), kwa hiyo baadhi ya machapisho yanakiondoa kifungu hiki (kama vile MSS, א, C na L).

◙"**Na akaanza kulia"** Petro alikuwa akitimiliza unabii kwenye kukana kwake na kuwapa tumaini waamini wote waliomkana Yesu kwa ndimi zao, kwa maisha yao na kwa vipaumbele vyao. Pia kuna tumaini kwa kila mmoja amuijiaye Yeye kwa imani (kama vile Yohana 21).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni <u>mwongozo</u> wa kujifunza wa fasiri inamaanisha kwamba unawajibika kwatafsiri zako mwenyeweza Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Mjadala huu wa maswali unawekwa ili kukusaidia wewe kufikiri maana ya chapisho kupitia sehemu ya kitabu. Wanamaanisha kuchochea sio kumalizia.

1. Je kuna mkanganyiko kati ya Marko na Yohana kuhusiana na siku ile karamu ya Bwana ilipofanyika?
2. Kwa nini Mariamu alikuwa mbadhirifu?kwa nini Yesu aliliruhusu hili?
3. Je Marko 14:7 inafundisha kuhusu Yesu kutowajibika kwa ajili ya maskini?
4. Kwa nini viongozi wa dini walitaka kumuuwa Yesu?
5. Vipi kuhusu Yuda, tunaelezeaje matendo yake?
6. Ni kwa vipi Karamu ya Bwana inahusiana na Pasaka? Nini umuhimu wa Karamu ya Bwana?
7. Kwa nini Gethsemane imekaa kimafumbo (yaani.,Yesu alitaka kikombe kimuepuke, lakini tena akataka kwa mapenzi ya Baba)?
8. Kwa nini Kuhani Mkuu alikatishwa tamaana nukuu za Yesu za Zaburi 110 na Dan. 7:13?

# MARKO 15

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Yesu mbele ya Pilato | Yesu kumkabili Pilato | Yesu mbele ya Pilato | Yesu mbele ya Pilato | Yesu mbele ya Pilato |
| 15:1-5 | 15:1-5 | 15:1-5 | 15:1-2a | 15:1 |
| | | | 15:2b | 15:2-5 |
| | | | 15:3-4 | |
| | | | 15:5 | |
| Yesu anahukumiwa kifo | Kuchukua nafasi ya Baraba | | Yesu anahukumiwa Kifo | |
| 15:6-15 | 15:6-15 | 15:6-15 | 15:6-10 | 15:6-15 |
| | | | 15:11-12 | |
| | | | 15:13 | |
| | | | 15:14a | |
| | | | 15:14b | |
| | | | 15:15 | |
| Askari Wanamdhihaki Yesu | Askari wanamdhihaki Yesu | Usulubishwaji | Askari wanamkebehi Yesu | Yesu anavikwa taji ya miba |
| 15:16-20 | 15:16-20 | 15:16-20 | 15:16-20 | 15:16-20a |
| Usulubishwaji wa Yesu | Mfalme msalabani | | Yesu anasulubiwa | Njia kuelekea Msalabani |
| | | | | 15:20b-22 |
| 15:21-32 | 15:21-32 | 15:21-24 | 15:21-28 | Usulubishwaji |
| | | | | 15:23-28 |
| | | 15:25-32 | | |
| | | | 15:29-30 | Msulubishwaji Yesu Anadhihakiwa |
| | | | 15:31-32a | 15:29-32 |
| | | | 15:32b | |
| Kifo cha Yesu | Yesu anakufa Msalabani | | Kifo cha Yesu | Kifo cha Yesu |
| 15:33-41 | 15:33-41 | 15:33-41 | 15:33-34 | 15:33-39 |
| | | | 15:35-36 | |
| | | | 15:37 | |
| | | | 15:38-39 | Wanawake Kalvari |
| | | | 15:40-41 | 15:40-41 |
| Maziko ya Yesu | Yesu anazikwa Katika kaburi la Yusufu | | Maziko ya Yesu | Maziko |
| 15:42-47 | 15:42-47 | 15:42-47 | 15:42-47 | 15:42-47 |

**MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka ”Mwongozo wa usomaji  Mzuri wa Biblia”)**

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 15:1-5**
**1 Mara kulipokuwa asubuhi wakuu wa makuhani walifanya shauri pamoja na wazee na waandishi na baraza nzima, wakamfunga Yesu, wakamchukua, wakamleta mbele ya Pilato. 2 Pilato akamwuliza, Wewe ndiwe mfalme wa Wayahudi? Akajibu, akamwambia, Wewe wasema. 3 Nao wakuu wa makuhani walikuwa wakimshitaki mambo mengi. 4 Pilato akamwuliza tena akisema, Hujibu neno? Tazama ni mambo mangapi wanayokushitaki! 5 Wala Yesu hakujibu neno tena, hata Pilato akastaajabu.**

**15:1 "kulipokuwa asubuhi"** Marko kama maandiko mengine ya Kiyahudi hayalengi na kujikita katika nyakati fulani. Inawezekana kwamba Wayahudi wa siku za Yesu waligawa usiku na mchana katika masaa kumi na mbili kila moja (kama vile Yohana 11:9), ikiwa na vipengele vinne-vinne. Siku kuwa na masaa ishirini na nne inatoka Babeli. Wayunani na Wayahudi walichukua kutoka kwao. Siku iligawiwa katika vipengele kumi na mbili.

Katika Sura ya 15 Marko ina wekwa alama kadhaa za muda;

1. mapambazuko, Marko 15:1 (kuanzia saa 12 asubuhikulingana na majira ya mwaka)
2. saa ya tatu, Marko 15:25 (kuanzia saa 3 asubuhi)
3. saa ya sita, Marko 15:33 (wakati wa adhuhuri)
4. saa ya tisa, Marko 15:34 (mnamo saa 9 jioni)
5. wakati wa jioni, Marko 15:42 (machweo, mnamo saa 12 jioni)

Luka 22:66-71 inatoa maelezo ya mkutano huu. Mkutano huu wa mapema ulifanyika kama jaribio la kuyatetea mashitaka ya usiku yasiyofuata sheria yapate kuwa halali kisheria (kama vile A. N Sherwin-White, *Roman Society and Roman Lawin the NewTestament*, kurasa 24-47). Mfuatano wa mashitaka ya Yesu mbele ya Pilato na kusulubiwa kwake ni:

| | Mathayo | Marko | Luka | Yohana |
|---|---|---|---|---|
| Hukumu ya Pilato | | | | saa ya 6<br>19:14 |
| Usulubishwaji | | saa ya 3<br>15:25 | | |
| Giza kuanguka | saa 6 – ya 9<br>27:45 | saa 6 - ya 9<br>15:33 | saa 6- ya 9<br>23:44 | |
| Kupaza Sauti kwa Yesu | saa ya 9<br>27:46 | saa ya 9<br>15:34 | | |

Maelezo haya ya muda yanapolinganishwa, maoni mbadala mawili ya kifasiri yanaibuka: (1) Ni yale yale. Yohana alitumia muda wa Kirumi katika kuhesabu muda, akihesabu kuanzia saa 6 usiku (kama vile Gleason L. Archer, *Encyclopedia of Bible Difficulties*, ukurasa wa364), na vitabu vya Injili vilitumia muda wa Kiyahudi kwa kuhesabu kuanzia saa 6 (2) Yohana anaeleza baadaye juu ya muda wa kusulubiwa kwa Yesu ambao ungekuwa mfano mwingine wa utofauti kati ya Injili na

Yohana. Hatahivyo inaonekana Yohana 1:39 na 4:6 kwamba Yohana wakati mwingine inatumia muda wa Kiyahudi na wakati mwingine muda wa Kirumi (kama vile M. R. Vincent, *Word Studies*, Vol. 1, kurasa wa 403).
Maelezo ya muda yanaweza kuwa uwakilishi katika Injili zote nne kwamaana zina fana katika (1) muda wa dhabihu za kila siku (yaani mwendelezo) katika Hekalu (saa tatu na saa 9 jioni, kama vile Mdo. 2:15; 3:1) na (2) mara baada ya adhuhuri ya muda wa kuchinjwa Mwanakondoo wa Pasaka juu ya Nisan 14. Biblia ikiwa kitabu cha kale cha mashariki hakijikiti katika mfuatano mkali kama zilivyo hadithi za kihistoria za magharibi.

◙**"wakuu wa makuhani walifanya shauri pamoja na wazee na waandishi na baraza nzima"** Angalia Mada Maalum:Wakuu wa Sinagogi katika Marko 12:13.

◙**"mara"** Injili ya Marko in awekwa sifa ya matendo ("baadaye," "na," "mara").Yesu anafunuliwa kimsingi kupitia matendo Yake. Mtembeo wa hadithi na masimulizi unaenda mbele kupitia maneno haya ya matendo. Angalia dokezo katika Marko 1:10.

◙**"wakamfunga Yesu"**Hii inaweza kuwa utaratibu uliozoeleka kwa wakosaji au kiufahamu zaidi ilionesha hofu yao kwa Yesu. Wengi walikuwa na hofu kwamba alikuwa ni mwenye kufanya miujiza au mchawi na kwamba nguvu Zake zilikuwa katika mikono Yake.

◙**"wakamleta mbele ya Pilato"** Hakika kwanini hili lilifanyika haijulikani.Wengi wa Wanazuoni wanafikiri kwamba Pilato alikaa alikaa katika jumba la kifalme la Herode alipokuwa Yerusalemu. Makazi yake ya kawaida yalikuwa Kaisaria pembezoni mwa Bahari. Wengine walifikiri kwamba anakaa katika makao makuu ya jeshi ambapo palikuwa ni ngome ya Antionia, jirani na hekalu. Muda ungekuwa wakati wa mapumziko kufuatia desturi za Kirumi za mahakama ya mapema (yawezekana kwasababu ya joto). Pilato alitawala Palestina kama mwakilishi wa Mfalme kutoka 25/26-36/37 B.Kna alafu aliondolewa kwasababu ya mashitaka mfululizo yaliyoletwa na Vitellius, Mwanasheria wa Shamu.

## MADA MAALUMU: PONTIO PILATO

A. Mahali na wakati alipozaliwa havijulikani
B. Wa daraja au tabaka la Waendesha farasi (daraja la juu ngazi ya kati la jamii ya Warumi)
C. Alioa, lakini watoto hawajulikani
D. Teuzi za kiutawala wa awali (ambazo lazima zilikuwa nyingi) hazijulikani

I. Nafsi ya mtu
 A. Mitazamo miwili tofauti
  1. Philo (Legatio na Gaium, 299-305) na Josephus vitabu vya historia za kale 18.3.1 na vita vya kiyahudi 2.9.2-4) wanamwelezea mtawala wa ….. asiye na huruma na katili.
  2. Agano Jipya (Injili, Matendo) linamtoa kama wakili wa Kirumi dhaifu ambaye anaweza kuendeshwa kwa urahisi.
 B. Paul Barnett, Yesu na kuinuka kwa Ukristo wa kwanza, kur. 143-148, kinatoa maelezo yenye kukubalika kuhusu mitazamo hii miwili.
  1. Pilato aliteuliwa kuwa wakili mwaka 26 b.k chini ya Tiberia ambaye alikuwa anaunga mkono Wayahudi (kama vile Philo, Legatio and Gaium, 160-161).
  2. Tiberius alipata hasara ya kukosa nguvu za kisiasa L. Aelius Sejanus, kiranja wake mlinzi wa jumba la kifalme ambaye alikuwa nguvu halisi nyuma ya kiti chake cha kifalme na aliye wachukia Wayahudi (Philo, Legatio land Gaium, 159-160).
  3. Pilato alikuwa mfuasi wa Sejanus nana alijaribu kumvutia
   a. Kuleta viwango vya kirumi kwenye mji wa Yerusalemu (26 B.K), ambavyo mawakiri wengine hawakuwa wamefanya. Hizi alama za Miungu wa Kirumi iliwachochea Wayahudi (kama vile.

Josephus' Antiq. 18.3.1; Vita vya Kiyahudi 2.9.2-3).

b. Kuchapa sarafu (29-31 B.K) ambayo ilikuwa na picha za Warumi wakiabudu zimechongwa juu yake. Josephus anasema alikuwa kwa makusudi kabisa anajaribu kupindua sheria za kiyahudi na desturi (kama vile Josephus, Kitabu cha mabo na historia ya kale 18.4.1-2).
c. Kuchukua fedha kutoka hazina ya hekalu kujenga mfereji Yerusalemu (kama vile Josephus, Antiq. 18.3.2; Vita vya Kiyahudi 2.9.3).
d. kupata Wagalilaya baadhi na kuwaua wa kutoa dhabihu siku ya pasaka mjini Yerusalemu.
e. Kuleta ngao za Kirumi mjini Yerusalemu katika mwaka 31 b.k., mwana wa Herode mkuu aliyempelekea ombi kwake waondolewe. Lakini asingefanya hivyo walimwan dikia Tiberia ambaye aliwataka warejeshwe kaisaria kwa bahari (kama vile Philo, Legatio na Gaium, 299-305).
f. Kupata Wasamaria wengi wachinjwe juu ya mlima Gerizim (mwaka 36/37b.k) walipokuwa wanalifuta vifaa vyao vitakatifu vya dini yao, ambavyo vilikuwa vimekwisha potea. Jambo hili lilimsababisha mkuu wake Pilato wa mahali pale (Vitellius, kiranja wa Ashuru) amwondoe kutoka ofsini na kumtuma Roma (kama vile. Josephus, Antiq. 18.4.1-2).

4. Sejanus alihukumiwa katika mwaka 31 b.k na Tiberia alirejeshwa kwenye mamlaka ya kisiasa kwahiyo , #a, b, c, na d pengine zilifanywa na Pilato kupata imani kwa Sejanus' ; #e zingeweza kuwa ni majaribio ya kupata imani kwa Tiberia lakini yawezekana yakawa yamelipuka na kuharibika.
5. Ni dhahiri kwa amiri jeshi mfalme anayeunga mkono Wayahudi aliyerejeshwa pamoja na barua rasmi kwa mawakili kutoka Tiberia kuwa mwema kwa Wayahudi (kama vile Philo, Legatio na Gaium, 160-161), kwamba uongozi wa Kiyahudi katika Yerusalemu walichukua fursa ya udhaifu wa kisiasa wa Pilato na Tiberia na wakamrubuni ili amsababishe Yesu kusulubiwa. Nadharia ya Barnett inaleta pamoja mitazamo hiyo miwili ya Pilato katika njia inayoonekana kuwa yenye mantiki.

II. Hatma yake
A. Aliitwa tena na alifika Roma mara tu baada ya kifo cha Tiberia (mwaka 37 b.k).
B. Hakuteuliwa tena.
C. Mke wake hajulikani baada ya hili. Kuna nadharia nyingi za baadaye, lakini hakuna kweli zilizo salama.

**15:2 "Pilato akamwuliza"**Kwa kutumia lugha gani? Uwezekano wa Pilato kuzungumza Kiaramu ni mdogo sana kuliko wa Yesu kuweza kuzungumza Kiyunani cha Koine. Kwa ajili ya mjadala mzuri angalia

1. "Did Jesus Speak Greek" kilichoandikwa na Joseph A. Fitzmeyer, Sura ya 21, kurasa za 253-264 katika*Approaches to the Bible: the Best of Bible Review*
2. "The Languages of the New Testament" kilichoandikwa na J. Howard Greenlee katika*Expositor's Bible Commentary*, vol. 1, kurasa 410-411

**◙"'Wewe ndiwe mfalme wa Wayahudi?'"** "wewe" ni neno la kejeli na la huruma. Luka23:1-2 inaorodhesha mashitaka ya wakuu wa sinagogi. Yohana 19:8-19, anaongeza maelezo mengi kwenye mazungumzo kati ya Yesu na Pilato. Pilato hakuwa anaangalia kipengele cha mashitaka ya kidini bali kipengele cha siasa.

**NASB, NKJV** **"ni kama usemavyo"**
**NKJV, TEV** **"wewe wasema"**
**NJB** **"ni wewe usemaye"**

Hii ni sawa na kusema kwa uwazi "unasema kwamba Mimi ndiye," ambayo inaweza kuwa ukiri wa nahau ya Kiebrania (kama vile Mt. 26:25,64; Luka22:70; 23:3) au njia ya kimafumbo ya kujibu ikimaanisha, "wewe umesema hivyo lakini ninamaanisha aina tofauti ya mfalme." Hii inaonekana kuwa mazungumzo ya faragha (kama vile Yohana 18:33-38) ndani ya Pratori. Yesu lazima alikuwa amewaambia wanafunzi wake kuhusu hili au Yohana alikuwepo. Wayahudi wasingeweza kuingia kwasababu ingewafanya wao kuwa najisi katika kula Pasaka. Masimulizi ya mahojiano ya Herode Antipa yanaachwa katika Injili ya Marko, lakini inapatikana katika Luka 23:6-12.

**15:3**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **“Wakaanza kumshitaki kwa ukali”** |
| **NKJV, NRSV** | **“wamshitaki kwa mambo mengi”** |
| **TEV** | **“walikluwa wakimshtaki Yesu kwa mambo mengi”** |
| **NJB** | **“wakaleta mashtaka mengi dhidi yake”** |

Hii ni njeo ya wakati usio timilifu ikimaanisha kwamba walimshitaki tena na tena. Hii lazima ilitokea baada ya Pilato kuwa amezungumza na Yesu kwa faragha (kama vile Marko 15:4). Orodha ya baadhi ya mashitaka yanapatikana katika Luka 23:2.

**15:5 "Wala Yesu hakujibu neno tena"** Hii inaweza kuwa kutimilizwa kwa Isa. 53:7 (kama vile Marko 14:61; Mt. 26:63; 27:12; Yohana 19:9).

◙**"hata Pilato akastaajabu"** Kwanini Pilato alishangazwa?

1. Yesu alizungumza nae kwa faragha bali hakuzungumza mbele ya washitaki Wake.
2. Kuhani Mkuu alileta mashitaka mengi sana dhidi Yake na yalikuwa makubwa ya kutisha.
3. Yesu hakufanya kama ambavyo wafungwa wengi hufanya kwa kujitetea kwao kwingi sana.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 15:6-15**
**6Basi wakati wa sikukuu huwafungulia mfungwa mmoja, wamwombaye. 7Palikuwa na mtu aitwaye Baraba,**
**amefungwa pamoja na watu waliofanya fitina, na kufanya uuaji katika fitina ile. 8Makutano wakaja, wakaanza**
**kuomba awafanyie kama vile alivyozoea. 9Pilato akawajibu, akisema, Je! Mnataka niwafungulie mfalme wa**
**Wayahudi? 10Kwa maana alitambua ya kuwa wakuu wa makuhani wamemtoa kwa husuda. 11Lakini wakuu wa**
**makuhani wakawataharakisha makutano, kwamba afadhali awafungulie Baraba. 12Pilato akajibu tena**
**akawaambia, Basi nimtendeje huyu mnayemnena kuwa ni mfalme wa Wayahudi? 13Wakapiga kelele tena,**
**Msulibishe. 14Pilato akawaambia, Kwani, ni ubaya gani alioutenda? Wakazidi sana kupiga kelele, Msulibishe.**
**15Pilato akipenda kuwaridhisha makutano, akawafungulia Baraba; akamtoa Yesu, baada ya kumpiga mijeledi, ili asulibiwe.**

**15:6 "sikukuu"**Hii inaashiria Pasaka. Wanazuoni mara kwa mara wamebishana juu ya urefu wa huduma ya Yesu kwa watu. Sababu pekee ya kanisa kukiri huduma ya Yesu kwa watu kuwa ni miaka mitatu ni kwasababu ya Pasaka tatu zinazotajwa katika Injili ya Yohana. Hatahivyo, katika Yohana kunatajwa juu ya "karamu," hapa, ambayo inamaanisha Pasaka nyingine. Nafikiri Yesu anaweza kuwa alifanya huduma yake kwa watu kwa muda wa miaka mine au yawezekana mitano mpaka sita. Ni dhahiri kuwa waandishi wa Injili hawakutilia mkazo mfuatano hasa lakini thiolojia. Injili sio hadithi za magharibi bali masimulizi ya kithiolojia ya mashariki. Sio hadithi zilizoandikwa na watu wenyewe juu ya maisha yao au kuandika juu ya maisha ya watu wengine. Ni aina yake pekee ya uandishi. Waandishi wa Injili chini ya uvuvio walikuwa na uhuru wa kuchagua, kuasilisha na kupanga maneno na matendo ya Yesu ili kumuwasilisha kwa hadhira yao waliyoikusudia. Siamini kwamba walikuwa na uhuru wa kuweka maneno katika kinywa Chake; hatahivyo vitu vilivyoandikwa na kuwekewa kumbukumbu kwa muda wa baadaye pamoja na makusudi ya kithiolojia na kutofautiana kwa hadhira iliyokusudiwa, kunajibu maswali juu ya kwanini Injili nne zinatofautiana.

◙**"huwafungulia mfungwa mmoja, wamwombaye"** Hii inaonekana kufanyika desturi ya Kirumi ya mwisho wa mwaka katika Palestina wakati wa siku za Yesu. Hakuna uthibitisho wa kihistoria juu ya hili isipokuwa kwa Josephus katika *Antiquities of the Jews* 20:9:3. Pilato alikuwa natafuta kuwafanya umati wa makutano umuhurumie Yesu ili kwamba amwachie huru (kama vile Marko. 15:14; Luka 23:14-16; Yohana 18:38-39; 19:4).

**15:7 "Barabba"** Jina hili ni muunganiko wa Bar = "Mwana wa" na Abbas = "baba." Injili za Waebrania zisizo katika utakatifushwaji zina Bar Rabbas, "mwana wa Rabbi." Matoleo kadhaa ya Kiyunani ya MSS ya Mt. 27:16-17 yana "Yesu Barabba," ambalo ni jaribio la kebehi likijikita kote kuwili kuitwa "Yesu," ambaye alikuwa kweli "Mwana wa Baba."

◙**"waliofanya fitina"** Mtu ambaye makutano walitaka afunguliwe alikuwa ni aina ya mtu ambae walikuwa wakimshitaki Yesu kuwa na tabia kama zake. Kejeli iliyoje hii!

**15:8 "Makutano"** Baadhi wanafikiri marafiki wa Baraba walikuwa wakisubiri fursa hii ya mwisho wa mwaka. Wengine wanahisi makutano yalikuwa yanaundwa na mahujaji walio na ushuhuda wa uongo na wengine waliokuwa wakihusika na mashitaka ya usiku. Hawa hawakuwa na nia yoyote ya pamoja ila isipokuwa kwamba wote walitaka Barabba aachiliwe japo kwa sababu tofauti tofauti. Jiji lilikuwa limejaa mahujaji, wengi wao wakitoka Galilaya lakini isingekuwa mapema hivi na wala si katika mahakama ya Pilato.

| | |
|---|---|
| **NASB, NJB** | **"wakapanda juu"** |
| **NKJV** | **"wakapaza sauti"** |
| **NRSV** | **"wakaja"** |
| **TEV** | **"wakakusanyika"** |

Maneno ya Kiyunani "panda juu" (*anabainō*) na "kulia kwa sauti ya juu" (*anaboaō*) yana herufi zinazofanana na yanatamkwa sawasawa, ikiwa na maana kwamba walikuwa wamechanganywa kirahisi na mbinu ya kale au kutengeneza nakala za Agano Jipya kwa andiko lisomwalo na mwandishi mmoja kwa sauti ya juu na wengine kadhaa. Desturi ya maandiko ya Kiyunani inagawanyika:

1. "zikapanda juu" kauli tendaji endelevu ya wakati ukiopita usio timilifu MSS ,*א, B, na toleo la Vulgate.
2. "wakalia kwa sauti ya juu" kauli tendaji endelevu ya wakati uliopita usio timilifu MSS אi[2], A, C, W, na toleo la Peshitta.
3. "wakalia kwa sauti ya juu zaidi" haipatikani katika Marko katika maeneo mengine "zikapanda juu" inapatikana mara tisa kwa:
    1. vitu vinavyokuwa (4:7)
    2. kukodi meli (6:51)
    3. kuelekea juu (15:8)

Yawezekana matoleo ya NASB na NJB ni sahihi.

**15:9** Marko, kama Luka (yaani katika vyote Injili yake na Matendo ya Mitume), inaandika kuonesha kwamba Ukristo haukuwa tishio kwa mamlaka ya Kirumi.

**15:10 "kwasababu ya husuda"** Pilato alielewa nia za wakuu wa sinagogi (kama vile Mt. 27:18), lakini alikataa kutenda katika haki! Wivu hakika ni moja ya nia za uongozi wa Kiyahudi, japo sishangazwi kwamba nia zao za kithiolojia na kisiasa hazikuwa wazi sana kwa Pilato (yaani Luka 23:2). Inawezekana pia kwamba Pilato alikuwa amesikia juu ya Yesu kupitia washushushu au watoa taarifa (au hata mkewe, kama vile Mt. 27:19).

**15:12 "'ambaye mnamuita Mfalme wa Wayahudi'"** Yohana 19:15 inaandika kwamba makutano haya ya Wayahudi (yaaniwafitinishaji na viongozi wa Wayahudi) walisema "Hatuna mfalme ila Kaisari."Kebehi ya kiasi gani hii!

**15:13**

| | |
|---|---|
| **NASB, NRSV** | |
| **TEV, NJB** | **"wakajibu kwa sauti"** |
| **NKJV** | **"wakapaza sauti tena"** |

Neno la Kiyunani *palin* linafasiriwa kama "nyuma" na wafasiri wa kisasa. Zote mbili "tena" na "nyuma" ni mbadala wa fasiri pendekezwa na Bauer, Arndt, Gingrich na Danker, *A Greek-English Lexicon of the New Testament*, ukurasa wa 606. Muktadha hapa unaitaji "nyuma."

**15:14 "'ni ubaya gani ametenda'"** Injili ya Yohana inafanana na kauli hii ya Pilato mara tatu katika Marko18:38; 19:4,6. Pilato alijaribu kutafuta huruma kwa ajili ya Yesu na kumfungua (kama vileYohana 18:38; 19:6,12), lakini makutano haya yenye upendeleo hayakutaka!

**15:15**

| | |
|---|---|
| **NASB, NRSV** | **"akitaka kuwapendeza makutano"** |
| **NKJV** | **"akitaka kuwafurahisha makutano"** |
| **TEV** | **"alitaka kuwafurahisha makutano"** |
| **NJB** | **"akiwa na shauku kuwapendeza makutano"** |

Kwa Pilato amani ya watu ilikuwa jambo muhimu kuliko haki.Viongozi hawa wa Kiyahudi walikuwa wamefanikiwa katika kumuogopesha Pilato (kama Yohana 19:12). Pilato alikuwa ameshitakiwa kwa mambo mengi kwa mamlaka huko Shamu na Rumi. Hakuwa tayari kuendelea kushitakiwa tena.Walijua hili na walilitumia! Wataalamu wa lugha kadhaa wa kisasa wanakumbuka maneno haya ya Kiyunani*hikanon poiēsai*ni nahau za Kilatini (yaani, Bauer, Arndt na Gingrich, ukurasa wa 374; Moulton na Milligan, ukurasa wa 302; C. F. D. Moule, *An Idiom Book of the NewTestament Greek*, ukurasa wa 192). Hii ni muhimu sana kwasababu Marko ina maneno mengi sana ya Kilatini zikiwemo na tungo na nahau.

◙**"kumpiga mijeledi"** Hii ni kutimilizwa kwa Isa. 53:5. Kuchapwa viboko kulikuwa ni hatua za awali za taratibu za Kirumi kwa wale waliokuwa wakienda kusulubiwa. Huku kulikuwa ni kupigwa kusiko kwa kawaida. Mtu aliinamishwa na mikono yake ikiwa imefungwa chini katika gogo. Alafu askari wawili mmoja kila upande angempiga kwa mjeledi ulio na vichanuo tisa vya ngozi pamoja na vitu vigumu vilivyofungwa mwishoni mwa vichanuo hivyo. Mara kwa mara wafun gwa walikufa kutokana na kupigwa kwa namna hii.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 15:16-20**
**16 Nao askari wakamchukua ndani ya behewa, ndiyo Praitorio (yaani, nyumba ya uliwali), wakakusanya pamoja kikosi kizima. 17 Wakamvika vazi la rangi ya zambarau, wakasokota taji ya miiba, wakamtia kichwani; 18 wakaanza kumsalimu, Salamu, Mfalme wa Wayahudi! 19 Wakampiga mwanzi wa kichwa, wakamtemea mate, wakapiga magoti, wakamsujudia. 20 Hata wakiisha kumdhihaki, wakamvua lile vazi la rangi ya zambarau, wakamvika mavazi yake mwenyewe; wakamchukua nje ili wamsulibishe.**

**15:16 "Askari wakamchukua"** Hawa askari wa Kirumi (kama vile Mt. 27:27) walichukia Wayahudi kwasababu ya mtazamo wao wa kujitenga na hivyo wakamalizia uchungu wao na uadui wao kwa Yesu. Luka 23:11 inamaanisha kwamba askari wa Mtawala Herode pia walimkebehi yeye kama mfalme.

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"ndani ya jumba la kifalme (yaani Praitorio)** |
| **NKJV** | **"katika ukumbi uitwao Praitorio"** |
| **NRSV** | **"katika ukumbi ya jumba la kifalme (yaani makazi ya Gavana)** |
| **TEV** | **"ndani ya makazi ya jumba la kifalme la Gavana"** |
| **NJB** | **"katika sehemu ya ndani ya jumba la kifalme, yaani Praitorio"** |

Hii inarejerewa kama makazi ya Maafisa wa Kirumi pale ambapo walikuwa Yerusalemu. Hii inawezakuwa ngome ya Antonio, ambayo ilikuwa jirani na Hekaluau yawezekana zaidi jumba la kifalme la Herode Mkuu.

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"kikosi kizima cha Kirumi"** |
| **NKJV** | **"kikosi kizima"** |
| **NRSV, NJB** | **"kikosi kizima"** |
| **TEV** | **"kikosi kilichosalia"** |

Neno la Kiyunani *speiran* (yaani kikosi) kiasili ilirejerea kwa kitu kilichofunganishwa pamoja kama uzi au kamba. Ilikuja kutumika kifasihi kama kikundi cha watu wafanyao kazi kwa kusudi. Kikosi ni neno lingine la Kilatini. Lilitumika kama sehemu ya kumi ya jeshi, mara nyingi watu 600. Lakini ingeweza kurejerea chini zaidi (kama vile Yohana18:3). Jeshi la Kirumi lilikuwa lina muundo wa (1) majeshi, 6,000; (2) kikosi, 600; (3) kikundi, 200; na (4) maakida, 100.

**15:17 "Wakamvika vazi la rangi ya zambarau"** Mathayo 27:28 ina"vazi jekundu" la maafisa wa Kirumi. Zambarau ilikuwa ishara ya ufalme. Kwa asili vazi la afisa wa Kirumi lingekuwa jekundu. Walikuwa wakimkejeli Yesu kama aliyekuwa Mfalme wa Wayahudi (kama vile Marko 15:18,20; Yohana 19:2). Luka 23:1 inaandika kwamba askari wa Kiyahudi wa mtawala Herode au Herode Antipa pia alimdhihaki Yesu kama Mfalme/Masihi kwa kuweka vazi la kifalme juu yake.

◙**"taji la miba"** Kidesturi hii imekuwa ikifikiriwa kama mtindo wa utesaji ambapo miba iliwekwa katika fuvu la kichwa cha Jesu. Hatahivyo, inawezekana kabisa kwamba lilikuwa ni taji linalowaka lililotengenezwa kwa majani yamtende ambayo ilikuwa njia nyingine ya kumdhihaki Yesu kama mfalme (kama vile Mt. 27:27-31; Marko 15:15-20). Neno la Kiyunani"taji" (*stephanos*) lilitumika katika ushindi wa kimichezo lililovaliwa na Mfalme.

**15:19** Mstari huu unaelezea dhihaka za askari wa Kirumi.

1. "habari," salamu mahususi kwenda kwa viongozi (Marko 15:18)
2. "kupiga kichwa Chake na mwanzi," hii yawezekana kwanza ilikuwa imewekwa katika mkono wa Yesu kama fimbo ya kumdharaulia
3. "kumtemea mate," ishara ya kiutamaduni ya chuki na kutoridhishwa au kuigilizia busu (yaani aina ya salamu)
4. "kupiga magoti na kusujudu," ishara ingine ya dhihaka ya ufalme Wake
5. vazi la zambarau kuwekwa katika mabega Yake ikiwakilisha ufalme

Namba mbili mpaka nne ni njeo za wakati usiotimilifu, ambao unamaanisha matendo ya kujirudia rudia kwa wakati uliopita. Mengi wa askari wallifanya matendo haya tena na tena au yawezekana kila askari aliyekuwepo alifanya hivyo.

**15:20 "wakamtoa nje"** Yesu kama wafungwa wengine waliokwisha hukumiwa alitakiwa kubeba nguzo ya msalaba mpaka sehemu ya kusulubiwa nje ya kuta za jiji. Walichukua njia ndefu kupita mitaa ya Yerusalemu ili kwamba wote waweze kuona na kuogopa haki ya Kirumi.Huku kuongoza wakosaji nje ya kuta za Yerusalemu (kama vile Law. 24:14 na Hes. 15:35-36). Warumi hawakutaka ghasia na maandamano wakati wa siku hizi za karamu zilizojaa makutano ya watu.

◙**"ili kumsulubisha"** Wafoenike ndio waliobuni usulubishwaji. Iskanda Mkuu alisulubisha watu 2,000 baada ya kuanguka kwa Tiro. Warumi waliboresha mbinu ili kwamba wakosaji waliohukumiwa wateseke siku kadhaa kabla ya mauti kuwapata. Mateso haya yakikatili yalikusudiwakama kupunguza uhalifu. Hayakuweza kufanywa kwa raia wa Kirumi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 15:21**
**[21]Wakamshurutisha mtu aliyekuwa akipita, akitoka mashamba, Simoni Mkirene, baba yao Iskanda na Rufo, ili auchukue msalaba wake.**

**15:21 "Wakamshurutisha"** Hili ni neno lililokopwa la lugha ya Kiajemi lililotumika kufilisi mali rasmi au uorodheshwaji wa wafanyakazi kwa ajili ya matumizi ya kiserikali.

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"mtu aliyekuwa akipita"** |
| **NKJV** | **"alipokuwa akipita kutoka nje ya mji"** |
| **NRSV** | **"mtu aliyekuwa akipita"** |
| **TEV** | **"aliyekuwa akiingia ndani ya mji kutoka nje"** |
| **NJB** | **"mpitaji……aliyekuwa akitokea nje ya mji"** |

Je hii inamaanisha mtu aishiye Palestina au mgeni wa Pasaka? Nafikiri hii inarejerea hujaji aliyekuwa amepewa hifadhi katika mipaka ya Yerusalemu. Hatahivyo walikuwepo wengi waliotoka Kirenia (yaani Afrika Kaskazini) walioishi Yerusalemu. Kulikuwa na Sinagogi maalumu kwa ajili yao (kama vile Mdo. 6:9). Watoto wake wanatajwa ambao inavyoonekana walikuwa wakijulikana na kanisa la kwanza (sio katika Yerusalemu bali Rumi).

◙**"Simoni Mkirene"** Kirenia lilikuwa ni jimbo la Afrika Kaskazini. Kirene ulikuwa Mji wake Mkuu. Hatahivyo jina Simoni ni jina la Kiyahudi. Tunajifunza kutoka Matendo ya Mitume kwamba kulikuwa na Wayahudi wengi kutoka katika eneo hili (kama vile Mdo.2:10; 6:9; 11:20; 13:1). Kabila lake na utaifa wake haujulikani bado.Kulikuwa na Wayahudi weusi kutoka kwa Suleimani na siku za Malkia wa Kushi (yaani Ethiopia).

◙**"baba yao Iskanda na Rufo"** Ni dhahiri kwamba maelezo haya ya kibayana yanamaanisha kwamba Simoni na/au watoto wake walikuwa wakijulikana vyema katika kanisa la mwanzo. Kwa kuwa Marko anaandikwa kwa Warumi yawezekekana Rufo katika Rum. 16:13 ni jina lilelile.

◙**"msalaba"** Kuna maumbo kadhaa yawezekana yanayotumiwa na Warumi, T, X, t, au jukwaa linaloshikiliwa na nguzo zilizosimama kadhaa. Maumbo haya yote yamepatikana kwa tafiti za kiakolojia kama kutumiwa katika karne ya kwanza Palestina.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 15:22-26**
**22Wakamleta mpaka mahali paitwapo Golgotha, yaani, Fuvu la kichwa. 23Wakampa mvinyo iliyotiwa manemane, asiipokee. 24Wakamsulibisha, wakagawa mavazi yake, wakayapigia kura kila mtu atwae nini. 25 Basi ilikuwa saa tatu, nao wakamsulibisha. 26Palikuwa na anwani ya mashitaka yake iliyoandikwa juu, MFALME WA WAYAHUDI.**

**15:22 "Golgotha"** Hili ni neno la Kiaramu. Neno "Kalvari" la Kilatini likimaanisha"fuvu." Maneno hayamaanishi fuvu zima bali paji la uso. Eneo la mahali hapa haijulikani, lakini ilikuwa ni nje ya kuta za zamani za Yerusalemu yawezekana chini katika milima isiyokuwa na miti juu ya barabara kuu kuingia katika Jiji Takatifu (kama vileLaw. 24:14; Hes. 15:35-36; Yohana 19:20).

**15:23 "Wakampa mvinyo iliyotiwa manemane"** Hii ni njeo ya wakati usio timilifu ikimaanisha walijaribu mara kadhaa. Desturi ya Kiyahudi inasema kwamba wanawake wa Yerusalemu walifanya hili kama huduma kwa wafungwa waliohukumiwa. Ilikuwa ni dawa kali ya kupunguza maumivu na akili iliyozubaa.

◙**"asiipokee"** Sababu haijulikani.

**15:24 "wakamsulubisha"** Warumi hawakupigilia msumari katika viganja vya mikono lakini katika mikunjo ya mwili inayosaidiwa na vikamba vya mikono. Miguu ilikunjwa kidogo na makanyagio yalipigiliwa msumari kwenye boksi dogo la pembe tatu. Hii ilifanyika kumsababisha mtu aendelee mara kwa mara kujiinua mwenyewe juu ili kuweza kupumua. Kulikuwa pia kipande kidogo cha ubao kiitwacho shogi ambapo mtu angeweza kukaa na kidogo kupumzisha uzito wao.Watu wengi waliosulubiwa walikufa kutokana na kukosa hewa. Mtu aliinuliwa kidogo kutoka katika ardhi ili tu apate ahueni ya miguu yake kunyooka juu ya ardhi.

◙**"wakagawa mavazi yake"** Askari wa Kirumi waliosulubisha wahalifu walitafa namna ya kutunza mavazi yake kama sehemu ya malipo yao.

◙**"wakapiga kura"** Hii ilitabiriwa katika Zab. 22:18. Zaburi hii inaelezea usulubishwaji wa Yesu (Uainishaji wa maandiko kuhusu wa Kristo). Yesu ananukuu mstari wa kwanza wa Zaburi hii katika Marko 15:34. Pia Zab. 22:7-8 inatabiri maoni ya wale waliopita na kumdhihaki na kumkejeli Yesu (kama vile Marko 15:29).

**15:25 "saa ya tatu"** Katika Yohana 19:14 inasema "saa ya sita."Vitabu vya Injili kwa kuendelea vinatumia muda wa Kiyahudi wakati Yohana mara kwa mara japo bila kujitenga anatumia muda wa Kirumi.

◙**"wakamsulubisha"** Waandishi wa Injili hawachezei hisia zetu wakielezea hatua kwa hatua mateso ya kutisha ya kimwili yaliyokuwa yakimpata. Swala la kithiolojia sio namna gani (ingawa Kumb. 21:23ni muhimu, kama vile Gal. 3:13) Alikufa, lakini Yeye ni nani na kwanini alikufa!

**15:26**
**NASB, NRSV,**
**NJB** **"anwani …..iliyosomeka"**

**NKJV** **"anwani……..iliyosomeka juu"**
**TEV** **"hati ya mashitaka dhidi yake iliyosomeka"**

Taarifa kwamba bango hili lilikuwa kwa lugha tatu inatoka katika Yohana 19:20. Taarifa kwamba ilipigiliwa juu kidogo kilipokuwa kichwa cha Yesu inatoka katika Mt. 22:37. Matoleo ya KJV na NKJV yanafasiri Marko 15:26 kwa namna ya kumaanisha vizuri kueleweka"juu," lakini neno"bango la maelezo" linarudiwa katika kitenzi, mbalo linamaanisha kunakshiwa, kuchonga, kupigwa nakala, kuandika juu lakini sio "juu."

◙**"mashitaka yalisomeka"** Hii ilikuwa ishara ndogo iliyokuwa ikiitwa*Titulus* na Warumi. Siku zote ilikuwa yenye herufi nyeusi juu ya uso wa rangi nyeupe. Haya mashtaka aidha (1) yalibebwa mbele ya mtuhumiwa au (2) yalitundikwa katika shingo ya mtuhumiwa. Katika sehemu ya usulubiwaji ilitundikwa juu ya kichwa cha Yesu katika msalaba (kama vileMt. 27:37). Angalia*Manners and Customs of the Bible* na James M. Freeman, kurasa 395-6.

◙**"'MFALME WA WAYAHUDI'"** Inafurahisha kuona utofauti kati ya Injili juu ya maneno kabisa halisi ya mashitaka yaliyotundikwa katika kichwa cha Yesu msalabani.

1. Mt. 27:37 – "Huyu ni Yesu Mfalme wa Wayahudi"
2. Marko 15:26 – "Mfalme wa Wayahudi"
3. Luka 23:38 – "Huyu ni Mfalme wa Wayahudi"
4. Yohana 19:19 – "Yesu, Mnazareti, Mfalme wa Wayahudi"

Kila mmoja ni tofauti na mwingine lakini kimsingi ni yale yale. Hii ni kweli juu ya utofauti wa maelezo ya kihistoria kati ya Injili. Kila mwandishi aliandika kutokana na kumbukumbu yake (na vyanzo) katika namna inayotofautiana kidogo, lakini bado wao ni wale wale wenye hadithi ya ushuhuda wa macho. Pilato alitaka kuwakera viongozi wa Kiyahudi kwa kuweka cheo kile kile msalabani pa Yesu walichokiogopa (kama vile Marko15:21-22).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 15:27-32**
**27Na pamoja naye walisulibisha wanyang'anyi wawili, mmoja mkono wake wa kuume na mmoja mkono wake wa kushoto. [ 28Basi andiko likatimizwa linenalo, Alihesabiwa pamoja na waasi.] 29Nao waliokuwa wakipita njiani wakamtukana, wakitikisa-tikisa vichwa, wakisema, Ahaa! Wewe mwenye kulivunja hekalu na kulijenga katika siku tatu, 30jiponye nafsi yako, ushuke msalabani. 31Kadhalika na wakuu wa makuhani wakamdhihaki wao kwa wao, pamoja na waandishi, wakisema, Aliponya wengine; hawezi kujiponya mwenyewe. 32Kristo, mfalme wa Israeli, na ashuke sasa msalabani tupate kuona na kuamini. Hata wale waliosulibiwa pamoja naye wakamfyolea.**

**15:27 "pamoja naye walisulibisha wanyang'anyi wawili"** Neno hili "wanyang'anyi" au "wafitinishaji."Hii ni utimilizwaji wa Isa. 53:12. Zab. 22 na Isa. 52:13-53:12 ni bayana kwenye baadhi ya maelezo yao lakini si yote! Usomaji wa aina hizi za unabii wa ki-Masihi ni ngumu sana kwasababu ni baadhi tu ya maelezo yanayorandana na hali ya Yesu. Mengine yamkini yalikuwa (1) uwakilishi; (2) ushairi; au (3) kuhusiana na hali ya asili tu ya kihistoria. Ni kupitia tu uvuvio wa waandishi wa Agano Jipya kwamba aina hii ya uandishi wa ki-Kristo unakuwa sahihi. Waaminio wa kisasa wanaongozwa kwa Roho wakati wanaposoma Biblia (yaani kutiwa nuru), lakini hatukubaliani katika maelezo ambayo yanaonesha kwamba uvuvio yako juu kwa nuru. Aina ya uandishi imekosewa sana na waandishi waliofuata wa Agano Jipya kiasi kwamba nakataa kukubali aina hii ya ufasiri wa Kibiblia isipokuwa wakati inapoandikwa na waandishi wa Agano Jipya. Hatuwezi kuzalisha hatua za kifasiri za waandishi wa Kibiblia waliovuviwa. Lazima tutegemee uelewa wa kile kilichokuwa kinasemwa na waandishi wa asili waliovuviwa (Angalia makala ya utangulizi, "Usomaji mzuri wa Biblia"). Lazima sasa tuzifanyie kazi hizi kweli kwenye hali zetu za kidesturi.

**15:28** Mstari huu umeondolewa na maandiko ya kale ya Kiyunani, א, A, B, C, na D. Inaachwa na matoleo ya fasiri ya NRSV, TEV, NJB, na NIV. Inavyoonekana iliongezwa kama dokezo la pembezoni na waandishi wa kale kutoka Luka 22:37. Sio sehemu ya andiko la asili la Marko. Sio tabia ya kitabu cha Marko, kuandikia mataifa kujumuisha nukuu ya Agano la Kale (yaani Marko 15:28 ni maelezo ya Isa. 53:12). Toleo la UBS4 linatoa kuondolewa kwa alama ya "A" (hakika).

**15:29 "Nao waliokuwa wakipita njiani wakamtukana"** Yawezekana katika kuendeleza kusudi na taratibu za usulubishajiwa Kirumi, eneo la kusulubishia lilikuwa katika barabara kuu inayoingia Yerusalemu. Hawa wapiti njia walikuwa wanatimiliza unabii wa Zaburi 22:6-8,12-13,16-17.

◙**"'Ahaa! Wewe mwenye kulivunja hekalu na kulijenga'"** Hawa wafitinishaji wanaweza kuwa wale washitaki wa uongo waliokuwa katika mashitaka ya wakuu wa masinagogi (kama vile Marko 14:58).

**15:30** Fasiri hii ni mwendelezo wa dhihaka (kama vile Marko 15:31-32) ya nguvu za Yesu. Bado walikuwa wakitarajia miujiza hata siku ya mwisho. Walidai kuwa bado wangeendelea kumwamini (kama vile Marko 15:32).

**15:31 "aliokoa wengine"** Neno "kuokoa" linatumika katika namna ya ukombozi wa kimwili. Viongozi hawa hawakuweza kukataa miujiza ya Yesu lakini walihusianisha nguvu zake na shetani (kama vile Marko 3:22). Watu wa Yerusalemu walijua vizuri kwamba Yesu alikuwa amemfufua Lazaro (kama vile Yohana John 11).

**15:32 "Kristo, mfalme wa Israeli"** Hiki ni cheo kinachotolewa na wakuu wa makuhani kwa Pilato kama dhihaka kwa cheo cha Pilato, "Mfalme wa Wayahudi," Lililopigiliwa juu ya kichwa cha Yesu. Hii ni kebehi wala sio ukiri wala uthibitisho! Hii hakika inashabihiana na dhihaka inayotabiriwa katika Zaburi 22:6-8,12-13,16.

◙**"Hata wale waliosulibiwa pamoja naye wakamfyolea"** Inapatikana kipekee tu katika Luka 23:35-43 ambapo hadithi ya mhalifu anayetubu inaandikwa.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 15:33-39**
**[33]Na ilipokuwa saa sita, palikuwa na giza juu ya nchi yote, hata saa tisa. [34]Na saa tisa Yesu akapaza sauti yake kwa nguvu, Eloi, Eloi, lama sabakthani? Maana yake, Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha? [35]Na baadhi yao waliosimama pale, walisema, Tazama, anamwita Eliya. [36]Na mmoja akaenda mbio, akajaza sifongo siki, akaitia juu ya mwanzi, akamnywesha, akisema, Acheni, na tuone kwamba Eliya anakuja kumtelemsha. [37]Naye Yesu akatoa sauti kuu, akakata roho. [38]Pazia la hekalu likapasuka vipande viwili toka juu hata chini. [39]Basi yule akida, aliyesimama hapo akimwelekea, alipoona ya kuwa alikata roho jinsi hii, akasema, Hakika mtu huyu alikuwa Mwana wa Mungu.**

**15:33 "saa sita"** Ikiwa muda wa kiyahudi ulitumika hii ingekuwa saa sita kamili mchana. Angalia dokezo katika Marko 15:1.

◙**"palikuwa na giza juu ya nchi yote"** Hii ni moja ya ishara za hukumu ya Agano la Kale, aidha katika namna ya kiagano (yaani moja ya mapigo ya Kimisri, kama vile Kutoka 10:21; Kumb. 28:28-29) au namna ya matukio ya siku za mwisho (kama vile Yoeli2:2; Amosi 8:9-10; Zefania 1:15). Huu ulikuwa uwakilishi wa Mungu Baba kuuondoa uwepo wake mbali na mwanae ambaye alichukua dhambi za wanadamu wote. Hiki ndicho Yesu alikiogopa zaidi katika Gethsemane (ikiwakilishwa na "Mungu wangu! Mungu wangu! Kwa nini umeniacha?" katika Marko 15:34). Yesu alifanyika sadaka ya dhambina kuchukua dhambi kwa ajili ya ulimwengu wote (kama vile 2 Kor. 5:21). Alipitia utengano binafsi kutoka kwa Baba. Giza lilikuwa uwakilishi wa kimwili wa Mungu Baba kumuacha Mwanae.

**15:34 "saa tisa"** Ikiwa muda uliotumika ni wa Kiyahudi hii ilikuwa ni saa tisa mchana.

◙**"'Mungu wangu, Mungu wangu, kwanini umeniacha'"** Hii ni nukuu kutoka Zaburi 22:1. Kwa kuwa magombo ya Kiyahudi hayakuwa na sura na mgawanyo wa mstari (ambayo yote yaliongezwa kwenye maandiko ya Biblia katika zama za kale), inaonekana kwamba kwa kunukuu mstari wa kwanza, Yesu alitaka kuainisha Zaburi nzima.
Kuna tofauti ya maoni ya kisomi juu ya tungo hii inayotakiwa kufasiriwa

1. Tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani "Ee Mungu, Mungu wangu, niangalie haja zangu" (ambayo inatokea katika Zaburi)

2. Toleo la Peshitta (linalofasiriwa na George M. Lamsa) lina
    a. Zab 22:1, "Mungu wangu, Mungu wangu, kwanini umeniacha kuishi?"
    b. Marko 15:34, "Mungu wangu, Mungu wangu, kwa hili nalihifadhiwa!"
3. Chapisho la Kiyahudi la Society la America lina, Zab. 22:1 as "Mungu wangu, Mungu wangu, kwanini umeniacha?"
4. Codex Bezae (karne ya tano) ina "Mungu wangu, Mungu wangu, kwanini umenichukia?" Kwa ajili ya mjadala tofauti ya matatizo ya kiujuzi ikiunganishwa kwa mstari huu angalia, Bart D. Ehrman's *The Orthodox Corruption of Scripture: The Affect of Early Christological Controversies on the Text of the NewTestament*, ukurasa wa 143-145.

Yesu alikuwa akipitia kipimo kamili cha mwisho cha dhambi — utengano kutoka katika ushirika na Baba (kama vileIsa. 54:2). Wanadamu waliumbwa kwa ajili ya ushirika na Mungu; bilahili hatuwezi kuwa kamili!

**15:34,35 "tazama anamuita Eliya"** Yesu na Mitume (na Wayahudi wote katika Palestina wa karne ya kwanza) walizungumza Kiaramu. Marko akiwaandikia Warumi siku zote alifasiri tungo za Kiaramu ambazo Petro anazikumbuka vizuri. Katika Kiaramu Eliyani Elia. Tungo ya Kiaramu pia inaandikwa katika Mt. 27:46. Hii ni kati ya tungo za kushangaza za Yesu alipolia pale msalabani. Alijihisi mwenye kuachwa na Baba. Eliya kidesturi alikuwa nabii ambaye angekuja nyakati za taabu Kabla ya Masihi (kama vile Mal. 3:1-6; 4:4-6), hivyo wapitaji walifikiria Yesu alikuwa akimuomba aje ampatie msaada. Moja ya wandishi wangu niwapendao ni F. F. Bruce. Katika kitabu chake *Answers to Questions*, ukurasa wa 65, yanataja makala katika kuzunguka kwake Palestina kila robo ya mwaka, Jan. - Aprili, 1951, na Alfred Guillaume, ambayo inaweka dokezo kwamba kiambishi tamati "wangu" kinapatikana katika Magombo ya Bahari ya Chumvi *iya*. Pale Yesu aliposema, "Mungu wangu," muundo ungekuwa*Eliya*, ambalo linatamkwa karibu zaidi na jina la Eliya. Hii inaweza kuelezea kwanini wapitaji waliyaelewa vibaya maneno ya Yesu.

**15:36 "sifongo siki"** Huu ulikuwa mvinyo wa bei nafuu ambao ulinywewa na watu wengi na askari jeshi walikunywa. Hii inaweza kuhusiana na Zaburi 22:15. Yesu alikuwa na kiu sana kiasi kwamba alihitaji kinywaji ili kuweza kuzungungumza maneno machache ya mwisho kutokea msalabani (kama vile Yohana 19:28-30).

◙**"akaitia juu ya mwanzi"** Mwanzi ulitumika kufikia mdomo Wake. Kutoa kinywaji kwa mtu anayesulubiwa halikuwa tendo la huruma lakini njia ya kurefusha uhai na ombolezo.

◙**"'Acheni, na tuone kwamba Eliya anakuja kumtelemsha'"** Hii ilitokana na huruma, lakini shauku ya kuona muujiza (kama vile Mt. 27:47-48).

**15:37 "sauti kuu"** Yohana 19:30 anatwambia Alisema, "Imekwisha!" Neno hili limepatikana limeandikwa katika nyaraka za kibiashara za mafunjo ya Koine ya Kiyunani kutokea Misri. Inavyoonekana lilikuwa neno la kibiashara ambalo lilimaanisha "kulipwa kikamilifu" (yaani, Isaya 53).

**15:38 "Pazia la hekalu likapasuka vipande viwili toka juu hata chini"** Kulikuwa na mapazia mawili ndani ya madhabahu ya Hekalu, moja mahali Patakatifu nay a pili Patakatifu pa Patakatifu. Ikiwa ya pili ilichanwa hakuna mtu aliyeona isipokuwa makuhani, labda la kwanza mara kwa mara lilikuwa likivutwa nyuma na kufungwa upande upande. Mapazia haya yanaelezewa katika Kutoka. 26:31-37. Katika siku za Yesu, katika Hekalu la kimfano la Herode, pazia hii ilikuwa 60' kwa 30' na kama 4" unene. Ikiwa sehemu ya nje ilichanwa waabuduo wote katika makao mengine tofauti wangeyaona. Hii inaonekana kwamba njia ya kuweka karibu ushirika na Mungu umeanzishwa na Mungu upya wakati wa kifo cha Kristo (kama mvile Mwa. 3:15; Kut. 26:31-35). Katika Mt. 27:51-53 miujiza mingine inaandikwa kama uthibitisho wa kiishara.

**15:39 "akida"** Hiki kilikuwa cheo cha chini cha Afisa wa jeshi la Kirumi . Hii ilimaanisha kidhahiri "kiongozi mmoja wa mia." Hawa wanaume walikuwa uti wa mgongo wa jeshi la Kirumi. Kornelio katika Mdo. 10 pia ni akida. Marko imeandikwa kwa ajili ya kuwahubiria Warumi!

◙**"Hakika mtu huyu alikuwa Mwana wa Mungu"** Hii kibayana ni "mtu huyu alikuwa mwana wa Mungu." Hatahivyo kukosekana kwa kiambata haimaanishi kwamba haikuwa bainishi (kama vile Mt. 4:3,6; 14:33; 27:43; na Luka4:3,9). Huyu alikuwa ni askari wa nguvu wa Kirumi. Alikuwa ameona wengi wakifa (kama vile Mt. 27:54). Hii inaweza kuwa "kifungu cha habari chenye shabaha" ya Marko kwasababu hii injili iliandikwa hasa kwa ajili ya Warumi. Ina maneno mengi ya Kilatini na nukuu chache za Agano la Kale. Pia desturi za Kiyahudi na tungo za Kiaramu zinafasiriwa na kuelezewa. Huyu hapa ni akida wa Kirumi anayekiri imani kwa mfitinishaji wa kiyahudi aliyesulubiwa! Inawezekana ni kwa kusudi la kithiolojia kwamba wapitaji, wakuu wa makuhani na hata wasulubishwaji wenza wa Yesu wamdhihaki lakini akida wa Kitumi aitikie kwa ukiri chanya na mshangao!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 15:40-41**
**40 Palikuwako na wanawake wakitazama kwa mbali; miongoni mwao alikuwamo Mariamu Magdalene, na Mariamu mama yao Yakobo mdogo na Yose, na Salome; 41 hao ndio waliofuatana naye huko Galilaya, na kumtumikia; na wengine wengi waliopanda pamoja naye mpaka Yerusalemu.**

**15:40 "Palikuwako na wanawake wakitazama kwa mbali"** Kundi la Kitume lilihudumiwa vyote viwili kifedha na kimwili na wanawake kadhaa (yaani kupika, kuosha, n.k, kama vile Marko 15:41; Mt. 27:55; Luka 8:3).

## MADA MAALUMU: WANAWAKE KATIKA BIBLIA

I. Agano la Kale
   A. Katika mila na desturi wanawake walichukuliwa kama ni mali kwa aliyenaye
      1. Walijumuishwa katika orodha ya mali (Kutoka 20:17)
      2. Walivyotendewa wanawake watumwa (Kutoka 21:7-11)
      3. Nadhiri za wanawake kufutwa na waume wenye madaraka (Hesabu 30)
      4. Wanawake kama mateka wa vita (kumbukumbu 20:10-14; 21:10-14)
   B. Kiutendaji palikuwa na ushirikiano
      1. Mwanaume na mwanamke waliumbwa kwa mfano wa Mungu (Mwanzo 1:26-27)
      2. Heshima kwa baba na mama (Kutoka 20:12 [Kumb. 5:16])
      3. heshima kuu kwa baba na mama (Mambo ya Walawi 19:3; 20:9)
      4. mwanaume na mwanamke wangeweza kuwa Wanazareti (Hesabu 6:1-2)
      5. mabinti wana haki ya urithi (Hesabu 27:1-11)
      6. ni sehemu ya watu wa agano (Kumbu kumbu. 29:10-12)
      7. wanapata mafundisho ya baba na mama (Mithali 1:8; 6:20)
      8. wana wa kiume na mabinti wa Hemani (nyumba ya Kilawi) waliongoza muziki ndani ya Hekalu (1 Mambo ya Nyakati 25:5-6).
      9. Wana wa kiume na wa kike watatoa unabii katika enzi mpaya (Yoeli 2:28-29)
   C. Wanawake katika dhima ya uongozi
      1. Dada yake Musa, Miriamu, aliitwa nabii wa kike (Kutoka 15:20-21 vile vile nukuu Mika 6:4)
      2. Wanawake walikirimiwa toka kwa Mungu kusokota nguo za aina mbalimbali kwa ajili ya Vibanda(Kutoka 35:25-26)
      3. Mwanamke aliyeolewa, Debora, pia nabii (kama vileWaamuzi. 4:4), aliyaongoza makabila yote (Amu. 4:4-5; 5:7)
      4. Hulda alikuwa nabii ambaye mfalme Yosia alimsihi kusoma na kutafsiri kitabu kipya kilichotolewa "*Book of the Law*" (2 Falme 22:14; 2 Nya. 34:22-27)
      5. Malkia Esta, mwanamke aliyemcha Mungu, aliwaokoa Wayahudi katika Uajemi

II. Agano Jipya

A. Kwa utamaduni wa dini za Kiyahudi na ulmwengu wa kale wa Kiyunani na Rumi, wanawake walikuwa raia wa daraja la pili wenye haki na vipaumbele vichache (isipokuwa Makedonia).

B. Wanawake katika dhima ya uongozi

1. Elizabeti na Mariamu, wanawake waliomcha Mungu kwa kujihudhurisha mbele za Mungu (Luka 1-2)
2. Ana, nabii mwanamke akihudumu katika Hekalu (Luka 2:36)
3. Lidia, mwamini na kiongozi wa kanisa la nyumbani (Matendo 16:14,40)
4. Mabinti Filipo wanne waliokuwa mabikra na manabii (Matendo 21:8-9)
5. Fibii, shemasi wa kike wa kanisa katika Kenkrea (Rum. 16:1)
6. Priska (Prisila), mtendakazi pamoja na Paulo na mwalimu wa Apolo (Matendo 18:26; Rum. 16:3)
7. Maria, Trifaina, Trifosa, Persisi, Yulia, dada wa Nerea, wanawakae kadhaa watenda kazi amoja na Paulo (Rum. 16:6-16)
8. Yunia (KJV), bila shaka mwanamke mtume (Rum. 16:7)
9. Euodia na Sintike, watenda kazi pamoja na Paulo (Flp. 4:2-3)

III. Ni kwa namna gani mwamini wa sasa atailinganisha mifano hii tofauti ya kibiblia?

A. Ni kwa namna gani mtu ataupambanua kweli wa kihistoria na kiutamaduni, anaoutumia katika mazingire asilia pekee, kutoka katika ukweli wa milele ulio halali kwa makanisa yote, waamini wa rika zote?

1. Kwa umakini yatupasa kuchukuliana na kusudio la mwandishi asilia aliyevuviwa. Biblia ni neno la Mungu na njia na chanzo pekee cha imani na matendo.
2. Yatupasa kushughulika dhahiri na maandiko yenye masharti nay a kihistoria yaliyovuviwa.
   a. Utaratibu wa ibada (yaani, utaratibi na liturujia) wa Israeli (kama vile Matendo 15; Wagalatia 3)
   b. dini ya Kiyahudi ya karne ya kwanza
   c. semi dhahiri za Paulo zenye masharti kihistoria na katika 1 Wakorintho
      1) mfumo wa kisheria wa wapagani katika Rumi (1 Wakorintho 6)
      2) kubaki katika hali ya utumwa (1 Kor. 7:20-24)
      3) ujane/useja (1 Kor. 7:1-35)
      4) mabikra (1 Kor. 7:36-38)
      5) chakula kilichotolewa sadaka kwa sanamu (1 Kor. 8; 10:23-33)
      6) matendo yasiyofaa katika Karamu ya Bwana (1 Wakorintho 11)
3. Kwa uwazi na kwa ukamilifu Mungu alijifunuaa kwa utamaduni maalumu, siku maalumu. Yatupasa kuuchukua ufunuo kwa umakini mkubwa, sio kufanya marekebisho kwa kila kipengele. Neno la Mungu liliandikwa katika maneno ya mwanadamu, likaelezwa katika utamaduni maalumu kwa wakati maalumu .

B. Tafsiri za kibiblia inapaswa kutafuta kusudi la asilia la mwandishi, nini alichokuwa akikizungumzia katika sihu zake zile? Hili ndilo jambo la kimsingi na la muhimu sana la tafsiri sahihi. Lakini basi yatupasa tulitumie hili kwa wakati wetu huu tulio nao. Tatizo kubwa la kiutafsiri linanaweza kuelezea maana ya neno. Je! Ni wapi palikuwa na huduma nyingi kuliko wachungaji ambao walionekana kama viongozi? Je! Ni wapi wahudumu au mashemasi wa kike na manabii wa kike walionekana kama viongozi? Ni dhahiri sana kuwa Paulo, katika 1 Kor. 14:34-35 na 1 Tim. 2:9-15, anadai kuwa wanawake wasishike nafasi katika ibada ya hadharani! Lakini alitumie kwa namna gani katika siku kama hizi? Nisingetaka utamaduni wa Paulo au utamaduni wangu kunyamazisha neno la Mungu na mapenzi yake. Bila shaka katika siku zile za Paulo palikuwa na mipaka sana, lakini pia katika siku zangu hizi inaweza kuwa wazi mno. Najisikia kukosa amani sana kusema kwamba kuwa maneno na na mafundisho Paulo ni ya kimasharti, karne ya kwanza, ukweli unaoendana na mazingira ya wenyeji hao. Mimi ni nani hata niweze kusababisha akili yangu au utamaduni wangu kumpinga mwandishi aliyevuviwa?!

Hata hivyo, nitafanya nini ikiwa kuna mifano ya kibiblia ya wanawake waliokuwa viongozi (hata katika maandiko ya Paulo, kama vile Warumi 16)? Mfano mzuri wa hili ni mjadala wa Paulo kuhusu ibada ya hadharani katika 1

Wakorintho 11-14. Katika 1 Kor. 11:5 anaonekana kuyaruhusu mahubiri na maombi ya wanawake katika ibada za hadharani huku vichwa vyao vikiwa vimefunikwa, lakini bado katika 14:34-35 anawahitaji wawe kimya! Kulikuwa na watoa huduma wanawake (kama vile Rum. 16:1) na manabii wa kike (kama vile Matendo 21:9). Ni utofauti huu unaonipa uhuru wa kutambua maoni ya Paulo (kama inavyohusiana na maagizo kwa mwanamke) kama ilivyozuiliwa huko Korintho na Efeso katika karne ya kwanza. Katika makanisa yote mawili palikuwa na matatizo kwa wanawake katika kutumia uhuru wao mpya uliopatikana (kama vile. Bruce Winter, *After Paul Left Corinth*), ambapo ingeweza kusababisha ugumu kwa kanisa kuifikia jamii kwa ajili ya Kristo. Uhuru wao ulibidi kupunguzwa ili kwamba injili iweze kuleta matokeo mazuri.

Siku zangu ziko kinyume na siku za Paulo. Katika siku zangu injili inaweza kuwekewa mipaka ama ikiwa wanawake wenye uwezo wa kusema, waliofunzwa hawaruhusiwi kuchangia katika injili, hawaruhusiwi kuongoza! Ni nini hatima ya lengo la ibada ya hadharani? Si uinjilisti na nidhamu? Je! Mungu anaweza kuheshimiwa na kufurahishwa na viongozi wa kike? Biblia kwa ujumla wake inaonekana kusema "ndiyo"!

Nataka kukubaliana na Paulo; theolojia yangu kimsingi ni ya Kipauline. Sitaki kuathiriwa kwa kiwango kikubwa au kugeuzwa kifikra na sera za kisasa za kupigania haki za wanawake. Hata hivyo, nahisi kwamba kanisa limeenda pole pole katika kuitikia ukweli ulio wazi wa kibiblia, kama matendo yasiyo stahili kuhusu utumwa, ubaguzi, itikadi kali, na ubaguzi wa kijinsia. Hili pia limechelewa kwa kutoitikia vyema masuala ya uzalilishaji wa wanawake katika ulimwengu wa kisasa. Mungu katika Kristo amemweka huru mtumwa na mwanamke. Si thubutu kuruhusu maandiko yenye utamaduni unaopingana na haya.

Hoja moja zaidi: kama mtafsiri ninafahamu kuwa Korintho lilikuwa ni kanisa lililoharibiwa sana. Vipawa vilivyotolewa vilikuwa vya majivuno. Wanawake wangeweza kuwa wameshikwa katika hili. Pia ningeweza kuamini kuwa Efeso ilikuwa imeaathiliwa na walimu wa uongo waliofanikiwa kutumia wanawake kama wasemaji mbadala ndani ya makanisa ya Efeso.

C. Mapendekezo kwa usomaji zaidi
1. *How to Read the Bible For All Its Worth* by Gordon Fee and Doug Stuart (kur. 61-77)
2. *Gospel and Spirit: Issues in New Testament Hermeneutics* by Gordon Fee
3. *Hard Sayings of the Bible by* Walter C. Kaiser, Peter H. Davids, F. F. Bruce, na Manfred T. Branch (kur. 613-616; 665-667*)*

◙**"Maria Magdalena"** Magdala lilikuwa jiji dogo pembezoni mwa Bahari ya Galilaya, maili tatu kaskazini mwa Tiberia. Maria alimfuata Yesu baada ya kukombolewa kutoka katika mapepo kadhaa (kama vile Luka 8:2). Alikuwa anachukuliwa isivyo halali kama Malaya lakini hakuna ushahidi wa hili katika Agano Jipya. Angalia Mada Maalum katika Marko 16:1.

◙**"Mariamu mama yao Yakobo mdogo na Yose"** Katika Mt. 27:56 anaitwa "mama wa Yakobo na Yusufu." Katika Mt. 28:1 anaitwa "Yule Maria mwingine." Swali la muhimu ni alikuwa ameolewa na nani? Katika Yohana 19:25 yawezekana alikuwa ameolewa na Klopa, ila bado mwanawe Yakobo anasemekana kuwa "mwana wa Alfayo" (kama vile Mt. 10:3; Marko 3:18; Luka 6:15). Angalia Mada Maalum katika Marko 16:1.

◙**"Salome"** Huyu alikuwa mama wa Yakobo na Yohana, waliokuwa sehemu ya kikosi cha karibu cha wanafunzi wa Yesu na wana wa Zebedayo (kama vile Mt. 27:56; Marko 15:40; 16:1-2). Angalia Mada Mada maalum: Wanawake waliomfuata Yesu katika Marko 16:1.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 15:42-47**
**42Hata ikiisha kuwa jioni, kwa sababu ni Maandalio, ndiyo siku iliyo kabla ya sabato, 43akaenda Yusufu, mtu wa Arimathaya, mstahiki, mtu wa baraza ya mashauri, naye mwenyewe anautazamia ufalme wa Mungu; akafanya ujasiri, akaingia mbele ya Pilato akauomba mwili wake Yesu. 44Lakini Pilato akastaajabu, kwamba amekwisha kufa. Akamwita yule akida, akamwuliza kwamba amekufa kitambo. 45Hata alipokwisha kupata hakika kwa yule akida, alimpa Yusufu yule maiti. 46Naye akanunua sanda ya kitani, akamtelemsha, akamfungia ile sanda, akamweka katika kaburi lililochongwa mwambani; akavingirisha jiwe mbele ya mlango wa kaburi. 47Nao Mariamu Magdalene**

**na Mariamu mamaye Yose wakapatazama mahali alipowekwa.**

**15:42 "Hata ikiisha kuwa jioni"** Marko ni kitabu pekee kinachotaja hili. Kutoka 12:6 ina "jioni" kama vile zilikuwa mbili: (1) 9:00 mchana - 12:00 kamili na (2) 12:00 jioni na baadaye. Muktadha unamaanisha lazima ingekuwa baada ya 9:00 jioni (muda wa dhabihu za jioni), lakini kabla ya saa 12:00 jioni (mwanzo wa Pasaka ya Sabato).

◙**"Maandalio"** Hii inamaanisha kila siku ilitakiwa kufanywa tayari kwa Sabato ya Wiki ya Pasaka ya takatifu sana (yaani Pasaka na Mikate isiyotiwa chachu ilikuwa siku ya nane ya karamu hivyo ilikuwa na Sabato mbili), sio mlo wa Pasaka wenyewe.

**15:43 "Yusufu wa Armathaya"** Anaonekana kuwa mwanafunzi wa siri pamoja na Nikodemo (cf.kama vile Mt. 27:57; Yohana 12:42). Hatahivyo baada ya kifo cha Yesu alikwenda hadharani kumuomba Pilato mwili wa Yesu (kama vile Yohana19:38). Ilikuwa ni hatari kutambuliwa kama rafiki wa mfitinishaji aliyesulubiwa.
Kama Myahudi wa Orthodox wa siku za Yusufu angejifanya mwenyewe najisi kuangalia Pasaka ya Sabato kwa:

1. kwenda katika nyumba ya mataifa
2. kugusa mwili wa aliyekufa

Hatahivyo alikuwa akijaribu kuondoa laana ya Kumb. 21:22-23. Siku zote Warumi waliacha miili ya waliosulubiwa iiendelee kukaa bila kuzikwa katika eneo la kifo, Warumi waliwaruhusu kuzika wafu wao lakini siku zote sio kwa haraka. Neno Armathaya maana yake ni "urefu" na inavyoonekana ni jina lingine kwa jiji la Rama ambalo lilikuwa maili tano kaskazini mashariki mwa Yerusalemu.

◙**"mstahiki, mtu wa baraza ya mashauri"** Yusufu alikuwa mjumbe wa wakuu wa sinagogi kama ilivyokuwa kwa Nikodemo. Angalia Mada Maalum: Wakuu wa Sinagogi katika Marko 12:13.

◙**"anautazamia ufalme wa Mungu"** Yusufu alikuwa mtu wa dini (kama vile Mt. 27:58). Ufalme wa Mungu ulikuwa tarajio la Kiyahudi la kila siku lililozoeleka kati ya Mafarisayo na watu wa kawaida. Yesu mara kwa mara alihubiri juu ya mada hii. Ilikuwa ni mada yake ya kwanza na mahubiri yake ya mwisho na shabaha ya mafumbo Yake. Angalia Mada Maalumu katika Marko 1:15. Ni kwa namna gani Yusufu alikuwa kungojea kwa ufalme kulikuwa hakujulikana. Ni kwa namna gani alikuwa mwanafunzi wa Yesu na na bado asijue ufalme ulikuwa tayari ulikuwa umekwisha kuja? Yumkini alikuwa bado anatarajia ufalme wa duniani (kama wanafunzi, kama vile Mdo. 1:6).

◙**"akaingia mbele ya Pilato"** Hii ingemfanya kuwa najisi kushiriki katika sabato kuu ya Sabato ya wiki ya Pasaka. Hii pia ingemtambulisha yeye na Yesu, mfitinishaji aliyesulubiwa. Hili lilikuwa tendo la ujasiri na la ukakamavu.

◙**"akauomba mwili wake"** Kawaida Warumi waliacha miili katika msalaba ioze kama tendo la kuasi. Miili hii ilikuwa mali ya Rumi. Ilikuwa siku zote ikitolewa kwa familia kwa maziko sahihi ambayo hasa ilikuwa muhimu kwa Wayahudi. Hili lilikuwa ombi maalumu, ombi lisilo la kawaida. Lilitolewa kwasababu ya umakini wa Wayahudi juu ya miili ya wafu kuchafua nchi hasa wakati wa majira ya Pasaka.

**15:44 "Lakini Pilato akastaajabu, kwamba amekwisha kufa"** Usulubishaji ulikuwa ni wa taratibu na wa kifo cha maumivu. Mara kwa mara ilichukua siku kadhaa. Askari wa kirumi aliwapa wahanga maji au mvinyo kutoka muda mpaka muda sio kwa rehema lakini ni kwa ajili ya kurefusha mifo chao. Hatahivyo muda huu watuhumiwa walitakiwa kufa haraka kwasababu ya Pasaka ya Sabato ijayo (kama ville Yohana 19:31 na kuendelea). Hii ilikuwa hivyo ili kwamba wasiweze kurusha rusha miguu yao kupumua vizuri. Wangekufa mapema baada ya hili. Yesu hatahivyo alikuwa tayari amekwisha kufa hivyo miguu Yake haikuvunjwa.Hii inatimiliza unabii (kama vile Yohana 19:36, akinukuu kutokea Kutoka 12:46. Angalia maoni ya Tafsiri ya kimaandiko katika Marko 15:27)."ikiwa" sio alama kwa sentenzi zenye masharti lakini

maswali yasiyo ya moja kwa moja. Pilato alishangazwa kwamba Yesu alikuwa haraka sana, hivyo aliuliza wahudumu wake swali hili lisilo la moja kwa moja.

**15:45 "mwili"** Neno la Kiyunani sio*soma*, lakini *ptōma*, ambalo linamaanisha maiti. Yesu alikuwa amefariki!

**15:46 "Naye akanunua sanda ya kitani, akamtelemsha, akamfungia ile sanda"** Nikodemo pia alikuwepo (kama vile Yohana 19:39-40).Kwa haraka waliuhandaa mwili wa Yesu (yaani kwasababu ya mkabiliano wa haraka wa Sabato saa 12 jioni) kulingana na desturi za Kiyahudi. Wayahudi hawakufanyia kazi kama Wamisri walivyofanya lakini walikuwa wameweka hatua ikihusiaha kukunja kitambaa na manukato.

◙**"akamweka katika kaburi lililochongwa mwambani"** Hii inatimiliza unabii kibayana katika Isa. 53:9. Mt. 27:57-60 inatwambia sisi kwamba ilikuwa kaburi binafsi la Yusufu.

◙**"lililochongwa mwambani"** Yesu hakuzikwa katika ardhi lakini katika hifadhi ya kimalia ya Yusufu.Ilitengenezewa tundu kutoka katika genge la mwamba na ingejumuisha mabamba kadhaa ya maziko. Kulikuwa na mengi ya haya huko Yerusalemu.

◙**"mawe"** Hiki kipande kikubwa cha mviringo wa kibamba cha mwamba kilikuwa kimepewa umbo kama jiwe la kusagia. Makaburi haya mara kwa mara yalikuwa yakivamiwa kwa wizi kwa hiyo walikuwa wamefunga kwa mawe mazito. Kiwango cha mawe kilionesha kuwa ilikuwa nia jiwe la mtu tajiri.

**15:47 "wakapatazama mahali alipowekwa"** Neno hili lilimaanisha "kuangalia kwa shauku na umakini." Walitaka kuwa na uhakika kwamba Yesu alikuwa amefanyiwa maandalizi kwa ajili ya mazishi. Hatahivyo hii ilisaidia kupata mashuhuda wawili (yaani Kumb. 17:6; 19:15) kuthibitisha ushuhuda wa kisheria. Yesu alikufa na hawakwenda kwa kaburi lisilo sahihi!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni Nani aliyemkamata Yesu? (yaani aliyeongoza makutano)
2. Ni kwa namna gani mashitaka ya Yesu yalikuwa yamekosewa hata kwa taratibu za Kiyahudi?
3. Je kulikuwepoo wasaidizi watumishi wa kike mmoja au wawili katika mistari ya 66-69?
4. Kwanini Petro alikuwa mwenye mawazo mengi katika eneo la mahakama?
5. Soma habari za mashitaka katika Injili zote nne na tengeneza orodha yako mwenyewe iliyo na mtiririko.
6. Elezea panapowezekana msukumo wa Pilato katika haya yote?
7. Tunawezaje kuelezea tabia ya makutano ya watu?
8. Kwanini askari walimdhihaki Yesu? Ni makundi yapi tofauti tofauti yaliyomdhihaki?
9. Orodhesha njia mbali mbali zilizotumika kumdhihaki Yesu.
10. Yesu alisulubiwa wapi?
11. Kwanini Yesu alihisi kuachwa na Baba (kama vile Marko 15:34)?
12. Kwanini Marko 15:39 ni moja ya mistari ya msingi katika Injili ya Marko?
13. Kwanini Yusufu alitaka Yesu azikwe kwa haraka

# MARKO 16

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Ufufuo | Amefufuka | Pasaka ya Kwanza | Ufufuo | Kaburi Tupu<br>Ujumbe wa Malaika |
| 16:1-8 | 16:1-8 | 16:1-8 | 16:1-5 | 16:1-2 |
| | | | | 16:3-8 |
| | | | 16:6-7 | |
| | | | 16:8 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka "Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## UTAKATIFUSHAJI WA MISTARI YA 9-20

A. Siamini kama mistari ya 9-20 kuwa ilikuwepo toka mwanzo katika Injili ya Marko. Haina uvuvio na haipaswi kujumuishwa katika Agano Jipya.

B. Kila kitu kinachotangulia mstari wa 8 hakipo katika maandiko ya kale ya Kiyunani
   1. Sinaiticus, inajulikana kwa herusi yake ya kwanza ya Kiebrania א. Maandiko haya yanajumuisha Agano Jipya zima na inatoka katika karne ya nne. Ilipatikana katika jumba la watawa liitwalo Catherine katika Jebul Musa, eneo la kitamaduni la Mlima Sinai
   2. Vaticanus, lijulikanalo kwa harufi ya Kiyunani B. Maandiko haya yanajumuisha Agano Jipya lote isipokuwa Ufunuo na pia linatoka katika Karne ya nne. Lilipatikana katika nyakati ya kisasa katika Maktaba ya Vatikan katika Rumi.

C. Shahidi mwingine wa tatu wa kale kwa Agano Jipya la Kiyunani, Alexandrinus, anajulikana kwa herufi ya Kiyunani A. Maandiko haya yanajumuisha Agano Jipya lote na linatokea katika karne ya tano. Linatokea Alexandria, Misri. Haijumuishi hitimisho la Marko (lile linalopatikana katika Textus Receptus na KJV). Hili hitimisho refu la kwanza linaonekana katika toleo la Irenaeus (120-202 B.K) *Against Heresies* III:10:5; na tunzi za Titian (110-172 B.K) Injili nne ziitwazo Diatessaron. Hatahivyo Clement wa Alexandria wa Origen wa Alexandria hakuwahi kunukuu au kuelezea mistari hii hata mara moja. Hii inaniambia kwamba hitimisho halikuwa la asili hata katika Alexandrinus, ambayo ilikuwa ikitoka katika mji ule ule. Mistari hii inajumuishwa katika MS C, ambayo pia inatokea Alexandria wakati fulani wa karne ya tano.

D. Eusebius (275-340 B.K), Mwanahistoria wa kanisa la kwanza wa karne ya nne alihitimisha "nakala zilizo sahihi zaidi" katika Marko 16:8.

E. Jerome (347-420 B.K), mfasiri wa Vulgate ya Kilatini, alisema kwamba karibia maandiko yote ya Kiyunani yanakosa hitimisho baada ya mstari wa 8.

F. Mistari 9-20 inajumuisha maneno 14-17 ambayo hayatumiki kabla au yanatumika tofauti katika Injili ya Marko. Pia kuna mabadiliko yaliyo wazi ya staili na muundo na matumizi maneno. Ishara za dhahiri zisizokuwa za kibiblia za Marko 16:18 zianathibitisha asili isiyovuviwa ya mistari hii ya nyongeza.
G. Maandiko kutoka Misri (Koptiki) yana hitimisho nne tofauti tofauti baada ya mstari wa 8. Baadhi ya maandiko ya Kiyunani yanajumuisha hitimisho refu (yaani Marko 16:9-20) na alafu hitimisho fupi au hitimisho fupi zaidi na alafu hitimisho refu au moja ya mahitimisho mengine katika muunganiko.
   1. Hii hapa ni hitimisho fupi kutoka katika maandiko ya Koptiki: "Na mambo yote ambayo alimwamuru Petro na wale waliokuwa Wake, walipomaliza kuzungumza na baada ya hili Yesu alijidhihirisha Mwenyewe kwao;na toka mawio ya jua mpaka Magharibi, aliwatuma kuhubiri wokovu wa milele kwa Injili Takatifu isiyoharibika"
   2. Hii hapa hitimisho lingune fupi. "Lakini walimjulisha kwa ufupi Petro na wale aliokuwa pamoja nae yale yote waliyo kwisha kuambiwa. Na baada ya hili Yesu Mwenyewe akatuma wao, kuanzia mashariki mpaka Magharibi kutangaza wokovu wa milele mtakatifu usioharibika." Hii inaitwa "hitimisho fupi"na linapatikana katika maandiko ya zamani ya kilatini K.
H. Tatizo kubwa ni kwamba Injili ya Marko inaonekana kuhitimishwa ghafla katika mstari wa 8. Kuna nadharia nyingi lakini hakuna hata mmoja anayejua kwa hakika kwanini Marko anahitimisha ghafla kwa namna ya dokezo la hofu.
I. Kuna maelezo mazuri ya tatizo hili la kimuktadha katika kitabu cha Bruce M. Metzger kiitwacho *A TextualCommentary on the Greek NewTestament*,kilichochapishwa na the United Bible Societies, kurasa za 122-126,au Robert G. Bratcher ana kitabu cha Eugene Nida kiitwacho *A Translator's Handbook on the Gospel of Mark*,kilichochapishwa na United Bible Societies, kurasa za 517-522.
J. Kwa mjadala mfupi wa ukosoaji wa kimuktadha angalia Kiambatisho cha Pili mwishoni mwa fasiri hii.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MARKO 16:1-8**
**1 Hata sabato ilipokwisha kupita, Mariamu Magdalene na Mariamu mamaye Yakobo, na Salome walinunua manukato wapate kwenda kumpaka. 2 Hata alfajiri mapema, siku ya kwanza ya juma, wakaenda kaburini, jua lilipoanza kuchomoza; 3wakasemezana wao kwa wao, Ni nani atakayetuvingirishia lile jiwe mlangoni pa kaburi? 4**
**Hata walipotazama, waliona ya kuwa lile jiwe limekwisha kuvingirishwa; nalo lilikuwa kubwa mno. 5Wakaingia kaburini wakaona kijana ameketi upande wa kuume, amevaa vazi jeupe; wakastaajabu. 6Naye akawaambia, Msistaajabu; mnamtafuta Yesu Mnazareti, aliyesulibiwa; amefufuka; hayupo hapa; patazameni mahali walipomweka. 7Lakini enendeni zenu, mkawaambie wanafunzi wake, na Petro, ya kwamba awatangulia kwenda Galilaya; huko mtamwona, kama alivyowaambia. 8Wakatoka nje, wakakimbia kutoka kaburini; kwa maana wameingia tetemeko na ushangao; wala hawakumwambia mtu neno, maana waliogopa. [**

**16:1 "Sabato ilipokwisha kupita"** Waisraeli wa kale walianza siku zao wakati wa machweo (nyakati za jioni), kutokana na Mwanzo 1:5,8,13,19,23,31. Hata hivyo Warumi (na Wayunani) alikuwa ameasili mbinu za Wababeli za kugawa mchana na usiku katika mgawo wa kumi na mbili. Migawanyo hii haikuwa wa urefu uliosawa kwasababu ya mabadiliko ya kimajira ya urefu wa nyakati za usiku/giza. Marko 15 anatumia alama za vipimo vya nyakati (yaani saa la tatu, Marko 16:25; saa la sita, Marko 16:33; saa la tisa, Marko 16:34). Tungo hii inaonekana kumaanisha kwa mbinu ya kale ya Kiisraeli na ingeweza hatahivyo kuwa saa 12 jioni. Ijumaa mpaka saa 12 jumamosi kwa ajili ya Sabato.

◙**"Maria Magdalena, na Maria mama yake Yakobo, na Salome"** Angalia Mada Maalumu inayofuata.

## MADA MAALUM : WANAWAKE WALIOFUATANA NA YESU NA WANAFUNZI WAKE

Mathayo. 27:55-56 | Marko 15:40-41 | Luka 8:2-3; 23:49 | Yohana 19:25

| | | | |
|---|---|---|---|
| Maria Magdalene | Maria Magdalene | Maa Magdalene | Mariamu, mama wa Yesu |
| Mariamu, mama yao Yakobo na Yusufu | Mariamu, mama wa Yakobo Mdogo na, Yose | Yoana, mkewe Kuza (wakili wa Herode) | Umbu la mamaye |
| Mama wa wana wa Zebedayo (Yakobo na Yohana) | Salome | Susana na wengine wengi | Mariamu, wa Klopa |
| | | | Mariamu Magdalene |

Yafuatayo ni maelezo yahusuyo hawa wanawake kutokana na maoni yangu kuhusu Marko 15:40-41:

"**Palikuwepo na wanawake wakitazama kwa mbali."** Kundi la kimitume lilisaidiwa na wanawake kadhaa wanawake waliohudumia kwa vyote kiuchumi na kimwili (yaani, kupika, kusafisha, nk. Kama vile Marko 15:41; Mt. 27:55; Luka 8:3).

"**Mariamu Magdalene."** Magdala ulikuwa mji mdogo katika fukwe za Bahari ya Galilaya, umbali wa maili tatu kaskazini mwa Tiberia. Mariamu alimfuata Yesu kutoka Galilaya baada ya Yeye kumkomboa kutoka katika pepo kadhaa waliokuwa wachafu (kama vile Luka 8:2). Pasipokuwa na usawa huyu alitambuliwa kama kahaba lakini hakuna ushahidi wa Agano Jipya wa jambo hili.

"**Mariamu, mama yao Yakobo na Yusufu."** Katika Mt. 27:56 huyu anaitwa "mama yao Yakobo na Yusufu." Katika Mt. 28:1 huyu anaitwa "Mariamu yule wa pili." Swali la muhimu ni hili, huyu alikuwa mke wa nani? Katika Yohana 19:25 bila shaka huyu alikuwa mke wa Klopa, bado mwanaye Yakobo, aliyesemekana kuwa "mwana wa Alfayo" (kama vile Mt. 10:3; Marko 3:18; Luka 6:15).

**"Salome."** Huyu alikuwa mama wa Yakobo na Yohana, ambao walikuwa sehemu ya mzunguko wa ndani wa mwanafunzi wa Yesu, na mke wa Zebedayo (kama vile Mt. 27:56; Marko 15:40; 16:1-2).

Yafuatauyo ni maelezo yangu kuhusu wanawake hawa kutokana na maoni yangu ya Yohana 19:25:

"**Na penye msalaba wake Yesu walikua wamesimama mamaye, na umbu la mamaye, Mariamu wa Klopa, na Mariamu Magdalene"** Kuna mjadala mwingi kuhusu kwa vyovyote kuna majina mane hapa au majina matatu.

Inawezekana kwamba kuna majina matatu kwa sababu hapawezi kuwa na maumbu mawili wanaoitwa Mariamu. Umbu la Mariamu, Salome, limetajwa katika Marko 15:40 na Mt. 27:56. Ikiwa ndivyo ilivyo, hii ingemaanisha Yakobo, Yohana na Yesu walikuwa jamaa wa karibu. Karne ya pili ya desturi (Hegesippus) inasema kwamba Klopas alikuwa ndugu wa Yusufu. Mariamu wa Magdala alikuwa mmoja wa wale ambao Yesu aliwaondolea pepo saba, na wa kwanza aliyemchagua kujionyesha kwake baada ya ubatizo Wake (kama vile Yohana 20:1-2; 11-18; Marko 16:1; Luka 24:1-10).

◙**"wakaleta manukato. . .ili kumpaka"** Ingawa wanawake hawa walikuwa wamemwona Yusufu na Nikodemo wakiandaa na kuweka mwili wa Yesu katika kaburi, inavyoonekana kwasababu ya ufinyu wa muda (yaani kati ya 9 - 12 jioni) kitu fulani ambacho ni desturi ya Wayahudi katika mazishi lazima kilikuwa kimesahaulika (yawezekana mishumaa yenye kutoa harufu au baadhi ya aina fulani ya manukato), na wanawake hawa walikuwa wakienda kumalizia vizuri taratibu za kitamaduni za mazishi.

## MADA MAALUMU: MANUKATO YA MAZISHI

A. Mane mane, gundi yenye harufu nzuri kutoka kwenye miti ya Uarabuni (BDB 600, KB 629; see UBS, Fauna na Flora of the Bible, kurasa 147-148)
   1. Kiungo kimetajwa mara kumi na mbili katika Agano la Kale, hasa katika fasihi ya hekima (kama vile. Zab. 45:8; 1:13; 4:14; 5:1,5)

2. Ilikuwa mojawapo ya zawadi zilizoletwa na mamajusi kwa mtoto yesu (kama vile. Mt. 2:11)
3. Kuashiria kwake kunachoma
   a. Ilitumika kama "mafuta matakatifu ya kupaka" (Kut. 30:23-25)
   b. Ilitumika kama zawadi kwa mfalme (Mt. 2:11)
   c. Ilitumika kumpaka yesu kwenye maziko yake (kama vile. Yohana 19:39 kama ishara katika Yohana 11:2). Hii ilikuwa kwa mujibu wa desturi za Wayahudi zilivyoelezwa katika Buku la kanuni za Kiyahudi(Talmud) (yaani, Berakhoth 53a).
   d. Ilitumika na wanawake Yerusalemu katika kinywaji kilichotolewa kwa watu waliokuwa wameteswa wakielekea kwenda kusulubishwa (kama vile. Marko 15:23) kupoza mateso

B. Aloes, aina fulani ya mbao yenye harufu nzuri (BDB 14 III, KB 19)
   1. Imeunganishwa na manukato yenye harufu nzuri (kama vile. Hes. 24:6; Zab. 45:8; Mith. 7:17; wimbo ulio bora 4:14; see UBS, *Fauna and Flora of the Bible*, kurasa 90-91)
   2. Ilitumika, ikichanganywa, na marhamu, na Wamisri kama sehemu ya kuhifadhi mwili wa marehemu.
   3. Nicodemo alileta kiasi kikubwa cha hiyo kwenye maziko ya Yesu na kumpaka (kama vile. Yohana 19:39). Hii ilikuwa kwa mujibu wa desturiza Kiyahudi kama ilivyoelezwa katika buku la kanuni za Kiyahudi-Talmud (yaani, Betsah 6a). Tazama Mada Maalumu: Kanuni za Mazishi

**16:2 "alfajiri sana katika siku ya kwanza ya Juma. . .jua lilipokuwa limechomoza"** Injili zote zinaandika tofauti kidogo kati yao.

1. Mathayo 28:1 ina "wakati wa mawio"
2. Luka 24:1 ina "mapema wakati wa kupambazuka"
3. Yohana 20:1 "ikiwa bado mapambazuko"

Inavyoonekana wanawake hawa waliondoka nyumbani mwao wakati bado giza, lakini muda ule walifika (yawezekana walitakiwa kununua manukato) katika makaburi tayari kulikuwa na nuru.

**16:3 "walikuwa wakisemezana"** Hii ni njeo ya wakati usio timilifu. Waliendelea kuogopa na kuulizana tena na tena walipokuwa wakitembea makaburini.

◙**"'Nani atakayeliviringisha jiwe'"** Walikuwa tayari njiani pamoja na manukato yao kabla hawajafikiria juu ya jwe kubwa ambalo lilikuwa limetumika kufunga kaburi. Marko haikuandika chochote juu ya kuwepo walinzi na kuwepo kwa kufungwa kwa Mt.27:62-66. Jiwe hili lilikuwa la mviringo na limechongwa kutosha katika kishimo cha mlango lkilichochimbwa mbele ya mwamba sehemu ya kufungulia. Ilikuwa ni rahisi kusukuma katika mteremko kutosha kufunga lakini ngumu sana kulisukuma ili kuweka kufungua.

**16:4 "walipotazama"** Inavyoonekana walikuwa wamekata tama, wakiangalia ardhini kwa maombolezo.

◙**"jiwe limekwisha vilingishwa"** Kutoka Mt. 28:2 inaonekana kwamba jiwe lilikuwa limetolewa katika eneo lake la kufungia kwa tetemeko (lililosababishwa na malaika, kama vile Luka 24:4; Yohana 20:12) na lilikuwa limelala pembeni.

◙**"japo lilikuwa sana"** Wizi makaburini lilikuwa jambo lililokuwa likitokea mara kwa mara kwasababu ya thamani ya manukato na vitu vya kuzikia. Eneo na aina ya kifungio cha kaburi na pia kiasi cha jiwe kilikuwa kinaonesha kwamba kaburi hili lilikuwa la mtu tajiri (kama vile Isa. 53:9).

**16:5 "wakaingia kaburini"** Yohana 20:11 inamtaja Maria akiwa nje ya kaburi akichungulia ndani, lakini Luka 24:3 inathibitisha kwamba wakati fulani wanawake waliingia ndani.

◙**"wakamwona kijana ameketi upande wa kuume"** Mara kwa mara ni Mathayo ambayo ina wapagawa mapepo wawili—vipofu wawili wa Yeriko, nakadhalika.—lakini hapa ni Luka na Yohana ambayo ina malaika wawili wakati Marko na Mathayo tu ndiye ina mmoja. Katika Biblia malaika siku zote walioneshwa kwa jinsia ya kiume isipokuwa Zekaria 5:9-10.

◙**"amevaa mavazi meupe"** Masimulizi kamili ya kuvaa kwake yanapatikana katika Mt. 28:3 (kama vile Luka 24:4 iliyo na "mavazi yag'aayo ").

**16:6 "msistaajabu"** Hii ni kauli shurutishi ya wakati uliopo ikiwa na kiambata hasi ambayo mara kwa mara inamaanisha kusitisha kitendo ambacho kiko katika mchakato tayari. Wanadamu siku zote walishangazwa na kuogopa katika udhihirisho wa kimwili wa ulimwengu wa roho.

◙**"'Yesu Mnazareti'"** Angalia dokezo kamili katika Marko14:67.

◙**"aliyekuwa amesulubiwa"** Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati timilifu (kama vile Mt. 28:5). Hiki ni kiambata halisi na yawezekana jina, "Aliyesulubiwa" (kama vile 1 Kor. 1:23; 2:2; Gal. 3:1). Pale tutakapomwona Yesu atakuwa bado na alama za kusulubiwa ambayo imekuwa muhuri wa heshima na utukufu (kama vile 1 Kor. 15:4 na Ufunuo 5:12). Yesu ni Nafsi pekee yenye kuvaa mwili katika Utatu Mtakatifu wa Mungu.

◙**"Amefufuka"** Ufufuo ni nguzo kuu ya imani ya Mkristo (kama vile 1 Kor. 15). Hii inaonesha uthibitisho wa Mungu wa maisha ya Yesu na dhabihu. Haya ni maudhui yanayojirudia rudia (kama vile Mdo. 2:24-28,32, 3:15,26;4:10; 5:30; 10:40; 1 Pet. 1:13, 3:18,21, na Paulo, Mdo. 13:30,33,34,37; 17:31; Rum. 4:24, 8:11; 10:9; 2 Kor. 4:14). Huu ni uthibitisho wa ukubalifu wa Baba wa mbadala wa kifo wa Mwana (kama vile 1 Kor.15). Kithiolojia nafsi tatu za Utatu ulikuwa kazini katika ufufuo wa Kristo: Baba (Mdo. 2:24;3:15; 4:10; 5:30; 10:40; 13:30,33,34; 17:31); Roho (Rum. 8:11); na Mwana (Yohana 2:19-22; 10:17-18). Angalia MADA MAALUM: UFUFUO katika Marko 8:31.

◙**"tazameni mahali walipokuwa wamemweka"** Hii inarejerea moja ya jiwe kati ya mawe kadhaa yaliyo kama kitanda katika kaburi la Yusufu. Yohana 20:6-7 inaelezea sehemu hii ya mazishi na namna vitambaa vya maziko (sanda) vilikuwa viko tu.

**16:7 "lakini nendeni mkawaambie wanafunzi Wake na Petro"** Kwanini Petro anatajwa kwa upekee? Namna gani Bwana anavyotuwazia mema na kuturehemu (kupitia malaika), kwamba angeweza kumpa upekee Petro aliyerudi nyuma na mwenye kuumia! Petro anakumbuka!

◙**"Atawatangulia kwenda Galilaya"** Yesu alikuwa ameandaa kabla mkutano pamoja na wanafunzi Wake huko Galilaya. Wanafunzi hawakuelewa vizuri maan ya kithiolojia ya tukio hili (kama vile Marko 14:28; Mt. 28:32; 28:7,10; Yohana 21; 1 Kor. 15:6). Nafikiri huu ulikuwa muda na eneo la Agizo Kuu.

**16:8 "kutetemeka na mshangao vilikuwa vimewakamata"** Mathayo 28:8 inaongeza "kwa furaha kuu."

◙**"wala hawakumwambia mtu neon lolote"** Je hii ilikuwa ya muda tu au hawakutii ujumbe wa malaika wa Marko 16:7? Yohana 20:1-10 inatoa hadithi ya Maria Magdalena Magdala akitoa taarifa kwa wanafunzi juu ya kaburi kuwa wazi lakini sio ujumbe wa malaika!

◙**"kwa kuwa walikuwa na hofu"** Injili hii inahitimishwa ghafla na kwa namna ya dokezo hasi kwamba inavyoonekana waandishi wa kale walijaribu kuongeza baadhi ya aina za hitimisho la muhtasari kwenye hitimisho hili.

**16:9-20** Naapa kujizatiti kwa maandiko ya kitume yalkiyovuviwa kama neno la kweli la Mungu, chanzo pekee cha imani na shughuli zingine. Hatahivyo, mistari hii haina uvuvio, yawezekana hata ni ya uvumi na kusadikika (kunywa sumu, kushika nyoka). Nakataa kutoa maoni yangu juu yake! Kwa ajili ya mjadala kamili angalia Bruce M. Metzger, *A Textual Commentary On the Greek NewTestament*, kurasa za 122-126.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwanini kuna utofautiano mkubwa wa namna hiyo katika habari zilizo katika Injili nne?
2. Kwanini Injili ya Marko inahitimisha kwa namna hasi hivyo?
3. Kwanini Ufufuo ni nguzo kuu ya imani ya Mkristo?

# UTANGULIZI KWA 1 PETRO

## UANDISHI

A. Ushahidi wa ndani kwa uandishi wa Mtume Petro
   1. Kibayana inatajwa katika 1 Pet. 1:1
   2. maelezo ya maneno na matukio ya kimaisha ya Yesu na wale kumi na wawili
      a. mifano inatolewa kutoka E. G. Selwyn's *The First Epistle of St. Peter*, 1946
         (1) 1 Pet. 1:3 – Yohana 21:27
         (2) 1 Pet. 1:7-9 – Lk. 22:31; Marko 8:29
         (3) 1 Pet. 1:10-12 – Lk. 24:25; Mdo. 15:14 na kuendelea
         (4) 1 Pet. 3:15 – Marko 14:29,71
         (5) 1 Pet. 5:2 – Yn. 21:15ff
      b. mifano kutoka kwa Alan Stibbbs' *The First Epistle General of Peter*, 1971
         (1) 1 Pet. 1:16 – Mt. 5:48
         (2) 1 Pet. 1:17 – Mt. 22:16
         (3) 1 Pet. 1:18 – Marko 10:45
         (4) 1 Pet. 1:22 – Yohana 15:12
         (5) 1 Pet. 2:4 – Mt. 21:42 na kuendelea
         (6) 1 Pet. 2:19 – Lk. 6:32; Mt. 5:39
         (7) 1 Pet. 3:9 – Mt. 5:39
         (8) 1 Pet. 3:14 – Mt. 5:10
         (9) 1 Pet. 3:16 – Mt. 5:44; Luka 6:28
         (10)1 Pet. 3:20 – Mt. 24:37-38
         (11)1 Pet. 4:11 – Mt. 5:16
         (12)1 Pet. 4:13 – Mt. 5:10 na kuendelea
         (13)1 Pet. 4:18 – Mt. 24:22
         (14)1 Pet. 5:3 – Mt. 20:25
         (15)1 Pet. 5:7 – Mt. 6:25 na kuendelea
   3. maneno na tungo zinazofanana na mahubiri ya Petro katika Matendo ya Mitume
      a. 1 Pet. 1:20 – Mdo. 2:23
      b. 1 Pet. 2:7-8 – Mdo.4:10-11
      c. 1 Pet. 2:24 – Mdo. 5:30; 10:39 (haswa matumizi ya neno la Kiyunani *xylon* kwa ajili ya msalaba)
      d. 1 Pet. 4:5 – Mdo. 10:45
   4. ulinganifu wa kisasa wa umishionari wa karne ya kwanza
      a. Silvano (Sila) – 1 Pet. 5:12
      b. Marko (Yohana Marko) – 1 Pet. 5:13

B. Ushahidi wa nje kwa uandishi wa Mtume Petro
   1. unakubalika mapema na maeneo mengi ya kanisa la kwanza
      a. utungaji wa tungo ule ule, waweza kuwa nukuu ya Clement wa Rumi katika toleo lake la *Letter to Corinthians* (95 b.k)
      b. Tungo zinazofanana zaweza kuwa katika the *Epistle of Barnabas* (130 b.k)
      c. ilielezewa na Papias, Askofu wa Hieropolis (140 b.k) katika nukuu kutoka kwa Eusebius' *His. Eccl.*
      d. ikinukuliwa na Polycarp katika *Epistle to the Philippians* 8:1, lakini hataji 1 Petro kwa jina (Polycarp alikufa mnamo 155 b.k)
      e. ikinukuliwa na Irenaeus (140-203b.k)
      f. ikinukuliwa na Origen (185-253 b.k). Origen aliamini kwamba 1 Pet. 5:13, ambapo Petro anamwita Marko "mwanangu" ikimaanisha aliandika Injili ya Petro.
      g. ilinukuliwa na Tertullian (150-222 b.k)

C. sababu za kuhoji uandishi wa Mtume Petro

1. haiko katika orodha ya vitabu vya agano jipya, orodha ya vitabu vya kikanoni vilivyotungwa huko Rumi kati ya 180 na 200 b.k
2. Kiyunani ni kizuri, kikipendezeshwa na lugha ya Koine ya huko Uyunani, ambao ni mshangaao toka kwa "watu wasio na elimu" (*a grammatos)* kama vile Mdo. 4:13) Mvuvi wa Galilaya
3. Unasikika vizuri sana kama maandiko ya Paulo katika Warumi na Waefeso
4. maelezo ya kuteswa kwake yanayoelezwa katika 1 Petro yanashabihiana na tarehe za baadaye
    a. Ki-Domitian (81-96 b.k)
    b. Ki-Trajan (98-117 b.k)

D. Majibu yenye kuwezekana kwenye uhusika wa wanzuoni wa kisasa
1. Ile orodha ya vitabu vya agano jipya imeharibiwa na kukosa moja ya mstari wa andiko (kama vile B. F. Westcott's *A General Survey of the History of the Canon of the NewTestament*, 6th ed. Kur. 289).
2. Petro hakuwa na elimu (kama vile Mdo. 4:13), lakini hata kidogo hakuwahi kujifunza toka kwenye shule zilizotambulikana za dini ya Kiyahudi. Inavyoonekana wayahudi wengi wao katika Glilaya walikuwa wenye kuzungumza lugha mbili toka kuzaliwa kwao. Jambo kubwa jingine katika mjadala huu ni matumizi ya Petro ya uandishi. Uwekaji wa maneno ya 1 Pet. 5:12 yanabainisha kwamba anawezakuwa alimtumia Silvano (Sila).
3. wote Petro na Paulo mara kwa mara walinukuu liturujia au nyenzo zao za mafundisho (nyaraka za Katekisimu) zilizokuwa zimezoeleka katika kanisa la kwanza. Pia walikuwa na mawasiliano baina yao kwa mwaka mzima (yaani Mdo., Gal. na 2 Pet. 3:15-16). Kwangu mimi sababu kubwa hasa kwa ajili ya ufanano kati ya Petro na maandiko ya Paulo yanaweza kuelezewa kwa matumizi ya msaidizi wa kimishionari aitwaye Sila (Silvano) kama mwandishi.
4. 1 Petro haiaksi moja kwa moja mateso ya kipindi cha utawala wa Kifalme.. Ukiri wa Petro wa waamini akiwataka kutii serikali (kama vile 1 Pet. 2:13-17) ingekuwa si jambo la kawaida katika nyakati za mateso kipindi cha utawala wa kifalme.

    Kuumwa kwa Nero (54-68 b.k) kiakili (mfano madai ya grandiose) ilihamasisha ushirikina wa kifalme wa maeneo haswa Asia Ndogo kuchochea mateso kwenye maeneo husika. 1 Petro inashabihiana na siku njema za Nero kuliko za Domitia (81-96 b.k au siku za Trajan (98-117 b.k). Hata inawezekana pia kwamba baadhi ya mateso yalitoka katika vikundi vya Kiyahudi na pia vya kishirikina vya serikali rasmi au mfalme.

E. Hakuna chochote kile katika 1 Petro ambacho kinadai kipindi cha baadaye au mwandishi.

## TAREHE

A. Tarehe ni wazi kuwa inahusiana na uandishi.
B. Desturi inaunganisha vifo vya Petro na Paulo katika Rumi chini ya Nero yawezekana mnamo mwaka 65. Ikiwa ndivyo, basi 1 Petro lazima iliandikwa mnamo miaka ya 63-64.
C. Karne ya kwanza ya kati inawezekana ikiwa 1 Petro inaelezewa kwa Clement wa Rumi (mnamo 95 b.k).
D. A. T. Robertson anaamini kuwa Petro alikufa mnamo miaka ya 67-68 b.k na aliandika 1 Petro mnamo miaka ya 65-66 b.k. Mimi nafikiri alikufa mnamo miaka ya 64-65 na aliandika kabla ya hii.

## WAPOKEAJI

A. Aina za barua za karne ya kwanza, wapokeaji wanatambuliwa katika 1 Pet. 1:1 kama "wale waishio kama wageni waliotapakaa huko Pontus, Galatia, Cappadocia, Asia, na Bithynia."Haya majimbo ya Kirumi (ikikisiwa Galatia ni jimbo la kikabila la Galatia kaskazini) yako kaskazini mwa Uturuki ya sasa. Maeneo haya inavyoonekana kuwa sehemu ambazo Paulo hakuhubiri (kama vile Mdo. 16:6) wala Petro (kama vile 1 Pet. 1:12). Yawezekana makanisa haya yalikuwa na asili kutoka kwa waamini wa Kiyahudi ambao walirudi nyumbani baada ya Pentekoste (kama vile Mdo. 2:9-11).

B. Ingawa makanisa haya yanaweza kuwa na asilia ya kuanzishwa na waamini wa Kiyahudi wakati wa uandishi wa Petro, yalikuwa kwa sehemu kubwa ya mataifa
1. hapo kabla wasiomjua Mungu (1:14)
2. njia za uovu za maisha walizorithi kutoka kwa baba zao wa hapo kabla (1 Pet. 1:18)

3. sasa watu wa Mungu (1 Pet. 2:9-10, mzaha juu ya Hosea 1:9-10; 2:23)
4. kati ya mataifa (1 Pet. 2:12)
5. orodha ya wenza wa mataifa (1 Pet. 4:3-4)

C. kitabu kina viashiria vya Kiyahudi
   1. matumizi ya maneno "wageni" na "walio nje" inaaksi mazingira ya Kiyahudi (kama vile Yohana 7:35; Mdo. 7:6)
   2. matumizi ya maandiko ya Agano la Kale
      a. Kutoka 19 (kama vile 1 Pet. 2:5,9)
      b. Isaya 53 (kama vile 1 Pet. 1:19; 2:22,24,25)

   Hatahivyo mifano hii kimsingi haiaksi kanisa la kiyahudi
   1. kuhamisha majina ya Agano la Kale kutoka Israeli kwenda kwa kanisa (yaani "ufalme wa mkuhani")
      a. 1 Pet. 2:5
      b. 1 Pet. 2:9
   2. nyaraka za mafunzo ya kanisa (yaani nyenzo za Katekisimu kwa waamini wapya), ambayo yalijumuisha maandiko ya Kimasihi
      a. 1 Pet. 1:19 – Isaya 53:7 (yaani Mwana kondoo)
      b. 1 Pet. 2:22 – Isaya 53:5
      c. 1 Pet. 2:24 – Isaya 53:4,5,11,12
      d. 1 Pet. 2:25 – Isaya 53:6

D. Ingawa Petro aliitwa haswa kwa ajili ya kuwahudumia Wayahudi (kama vile Gal. 2:8), yeye kama Paulo alifanya kazi na wote Wayahudi na Mataifa (kama vile Mdo. 10). Kuongoka kwa Kornelio kulionesha kujumuishwa kulikoazimiwa na Injili! 1 Petro inaaksi uanzishwaji huu mpya.

## KUSUDI

A. 1 Petro ina vyote vipengele vya mafundisho na mambo mengine. Hatahivyo kama Paulo aligawa barua zake kwa sehemu yake ya mwanzo juu ya mafundisho na sehemu ya hitimisho juu ya utendeaji kazi, Petro anaunganisha vyote viwili. Kwa namna nyingi inaaksi mahubiri zaidi ya barua.

B. Jambo kubwa lililojadiliwa ni mateso na dhiki. Hii inafanywa kwa namna mbili.
   1. Yesu anawasilishwa kama kilele cha mfano wa kuteseka na kukataliwa (kama vile 1 Pet. 1:11; 2:21,23; 3:18; 4:1,13; 5:1).
   2. Wafuasi wa Yesu wanaitwa kumuiga mwenendo Wake na mtazamo (kama vile 1 Pet. 1:6-7; 2:19; 3:13-17; 4:1,12-19; 5:9-10).

C. Kwa ufahamu wa kuteseka na dhiki kuwa kawaida na kuzoeleka katika miaka ya mwanzo ya Ukristo, haishangazi namna mara kwa mara Kuja kwa Mara ya Pili kunatajwa. Kitabu hiki kama yalivyo maandiko mengi ya Agano Jipya, ni cha matukio ya siku za mwisho kweli kweli.

## AINA YA UANDISHI WA FASIHI

A. Kitabu hiki ni aina ya uandishi wa kipindi kuanza na kufungwa cha karne ya kwanza ya Wayunani-Warumi
   1. 1 Pet. 1:1-2
      a. Mwandishi
      b. wapokeaji
      c. maombi
   2. 1 Pet. 5:12-14
      a. salamu za ufungaji
         (1) kutoka kwa nani
         (2) kuelekea kwa nani
      b. maombi

B. Dhamira kuu ya barua inarandana na mahubiri kuliko barua. Baadhi wamedhania kwamba ilikuwa hivyo
   1. mahubiri ya kwanza
   2. liturujia ya ubatizo wa kwanza
   3. vipande vya katekisimu ya kanisa la kwanza

C. Barua ya kwanza inaaonekana kufungwa katika 1 Pet. 4:11 kwa sifa za Mungu, lakini hakuna maandiko ya Kiyunani yanayoishia hapa. Inawezekana kwamba 1 Pet. 4:12-5:11 ni muhtasari wa kimakusudi wa barua nzima.

D. Mimi binafsi ninaamini kwamba 1 Petro 1 inafanya kazi kama barua ya wazi kwa makanisa ambayo Petro yeye mwenyewe hakuyaanzisha, kama Paulo kwa Wakolosai (zikitumwa kwa Wakolosai, Walaodikia na Hierapoli, kama vile Kol. 4:13), lakini pia kutiwa moyo kwa ujumla kwa waamini kuwa makini na changamoto au matatizo yajayo.

   Hii aina ya fasihi ya jumla inaelezea kukosekana kwa ufunguzi binafsi na ufungaji wa barua. Pia inaelezea kukosekana kwa mifano halisia.

## UTAKATIFUSHAJI

A. Najumuisha katika kipengele che utakatifushaji katika 1 Petro kwa sababu ya suala ni tata pamoja na 2 Petro.

B. 1 Petro inatajwa katika Eusebius' *Eccl. His.* 3:3:25, kusemekana kuwa sehemu ya "vitabu visivyokuwa na mpinzani." Katika kanisa la kale haikutiliwa mashaka kama barua ya kweli kutoka kwa Mtume Petro.

C. Jambo la utakatifushaji linashikiliwa bango kwasababu ya maandiko kadhaa ya uongo yanayodaiwa kuwa ni ya Petro. Kanisa la kwanza halikuwahi kukubaliana na haya, likitambua tu 1 Petro na kutupitilia mbali 2 Petro kama hakika kutoka kwa Mtume.
   1. Matendo ya Petro
   2. Matendo ya Petro na Andrea
   3. Matendo ya Petro na Paulo
   4. Upendo wa Petro na Paulo
   5. Matendo ya Petro na Kumi na mbili
   6. Matukio ya mwisho ya Petro
   7. Injili ya Petro
   8. Upendo wa Petro
   9. Mahubiri ya Petro
   10. Matukio ya kitumwa ya Petro

(Kwa ajili ya mjadala wa maandiko haya yaayofanana kiungo na haya angalia *Zondervan Pictorial Encyclopedia of the Bible* Vol. 4; kur 721-723, 732-733, 740.) Hakuna hata moja ya maandiko haya yanayohusishwa ba Petro ambayo yalipewa umakini kuwa sehemu ya kanoni ya Agano Jipya. Hili lenyewe na katika yote inazungumza sana juu ya ujumuishi wa 1 Petro na 2 Petro.

## MZUNGUKO WA KWANZA WA USOMAJI (Kutoka"Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

3. Dhamira ya kitabu kizima
4. Aina ya fasihi iliyotumika (uwasilishaji)

## MZUNGUKO WA PILI WA USOMAJI **(Kutoka”Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia”)**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Mada ya sehemu ya kwanza ya fasihi
2. Mada ya sehemu ya pili ya fasihi
3. Mada ya sehemu ya tatu ya fasihi
4. Mada ya sehemu ya nne ya fasihi
5. N.k.

# 1 PETRO 1:1-2:3

| MIGAWANYO YA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Salamu | Salamu kwa mahujaji wateule | Salamu | Utangulizi | Mahubiri na salamu |
| 1:1-2 | 1:1-2 | 1:1-2 | 1:1a<br>1:b-2a<br>1:2b | 1:1-2 |
| Tumaini Hai | Urithi wa kimbingu | Kufurahi katika wokovu | Tumaini Hai | Utangulizi na Urithi wa Mkristo |
| 1:3-9 | 1:3-12 | 1:3-9 | 1:3-5 | 1:3-5 |
| | | | | Uaminifu kwa Kristo Na upendo kwa Kristo |
| | | | 1:6-9 | 1:6-9 |
| | | | | Tumaini la Manabii |
| 1:10-12 | | 1:10-12 | 1:10-12 | 1:10-12 |
| Wito wa Maisha Ya Utakatifu | Kuishi mbele za Mungu Baba | Wito wa Utakatifu<br>(1:13-2:10) | Wito wa Maisha ya Utakatifu | Hitaji la Maisha Mapya na Utakatifu wa Waliobatizwa Upya |
| 1:13-16 | 1:13-21 | 1:13-16 | 1:13-16 | 1:13-21 |
| 1:17-21 | | 1:17-21 | 1:17-21 | |
| | Neno lidumulo | | | Kuzalishwa kwa Neno |
| 1:22-25 | 1:22-2:3 | 1:22-2:3 | 1:22-25 | 1:22-2:3 |

* Ingawa hazijavuviwa, migawanyo ya aya ndiyo ufunguo wa kuelewa na kufuatilia kusudio la asili la mwandishi. Kila tafsiri ya kisasa imegawanya na kufanya muhtasari wa aya. Kila aya ina mada kuu, kweli au wazo. Kila toleo limebeba hiyo mada kwa namna yake ya pekee. Unaposoma maandiko ya mwandishi jiulize ni tafsiri ipi inawiana na uelewa wako wa somo na mgawanyo wa mistari.
Katika kila sura lazima tusome Biblia kwanza na kujaribu kutambua somo (aya), kisha tulinganishe na matoleo ya kisasa. Ni pale tunapoelewa kusudi la asili la mwandishi kwa kufuata mantiki yake na jinsi alivyojieleza tunaielewa kwa Biblia kiukweli. Ni mwandishi wa asili tu aliyevuviwa —wasomaji hawana haki ya kurekebisha ujumbe. Wasomaji wa biblia wana wajibu wa kutumia ukweli uliovuviwa kwenye siku na maisha yao.
Fahamu kwamba maneno yote ya kiufundi na vifupisho vimefafanuliwa kwa kirefu kwenye nyaraka zifuatazo: Maelezo Fasaha Ya Muundo Wa Sarufi Za Kiyunani(Brief Definitions of Greek Grammatical Structure),Uhakiki Wa Tofauti Za Kiandishi(Textual Criticism),Ufafanuzi na Maelezo ya Kimaandiko(Glossary).

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka"Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 PETRO 1:1-2**
**[1] Petro, mtume wa Yesu Kristo, kwa wateule wa Utawanyiko, wakaao hali ya ugeni katika Ponto, na Galatia, na Kapadokia, na Asia, na Bithinia; [2] kama vile Mungu Baba alivyotangulia kuwajua katika kutakaswa na Roho, hata mkapata kutii na kununyiziwa damu ya Yesu Kristo. Neema na amani na ziongezwe kwenu.**

**1:1 "Petro"** Petro likuwa msemaji wa dhahiri wa Mitume kumi na wawili. Alikuwa sehemu ya wanafunzi wa karibu zaidi (Petro, Yakobo na Yohana). Masimulizi ya ushuhuda wa Petro wa macho wa maisha na mafundisho ya Yesu (kama vile 1 Pet. 5:1) yanaandikwa katika Injili ya Marko (yawezekana injili ya kwanza kuandikwa: pia yawezekana iliandikwa na Marko kutoka katika mahubiri ya Petro katika Rumi).
Uhusiano maalumu wa Yesu kwa Petro unaandikwa katika vyote Mathayo 16 na Yohana 21. Hata hivyo uhusiano huu maalumu haukubaliwa kama ukuu. Petro kama kiongozi (Papa) wa Ukristo wa Magharibi ni ukuaji wa kihistoria (kama ilivyo mtazamo wa Kikatoliki juu ya Maria), sio mafundisho yaliyo wazi kibiblia. 1 Petro inatoa dirisha kuelekea katika moyo wa kichungaji na maisha ya furaha ya kiongozi huyu mzuri.
Neno *petros* katika Kiyunani inamaanisha "jiwe lililomeguka" kwa ulinganifu tofauti na (*petra*, yaani ya kike) "mwamba wa chini" (kama vile Mt. 16:18); Katika Kiaramu zote zingetafsiriwa *Cephas*; upekee wowote kati ya maneno ya Kiyunani yangekosekana katika maneno ya Yesu kwa Petro!

◙**"mtume"** Hii ilitumika katika Dini ya waalimu wa kiyahudi pamoja na kisawe cha "yeye aliyetumwa kwa mamlaka." Petro siku zote huwa anaorodheshwa kabla. Yesu aliwachagua wanafunzi kumi na mbili kuwa pamoja naye katika namna maalumu na kuwaita "Mitume" (kama vile Luka 6:13). Neno hili mara kwa mara linatumika juu ya Yesu kutumwa kutoka kwa Baba (kama vile Mt. 10:40; Marko 9:37; Luka 9:48; Yohana 4:34; 5:24,30,36,37,38; 6:29,38,39,40,57; 7:29; 8:42; 10:36; 11:42; 17:3,8,18,21,23,25; 20:21). Kumi na mbili wanaorodheshwa katika Mt. 10:1-4; Marko 3:13-19; Luka 6:12-16; Mdo. 1:12-13.

◙**"Yesu"** Neno la Kiebrania lilimaanisha "YHWH anaokoa" au "YHWH huleta wokovu." Jina hili lilifunuliwa kwa wazazi wake na malaika (kama vile Mt. 1:21). "Yesu" linatokana na neno la Kiebrania kwa ajili ya wokovu, *hosea*, iliwekewa ambishwa tamati kwa jina la Mungu la agano, YHWH. Ni sawaswa na neno la Kiebrania Yoshua.

◙**"Kristo"** Hili ni neno sawia la Kiyunani la neno la Kiebrania *messiah*, lililomaanisha "Yeye aliyepakwa mafuta." lilimaanisha "yeye aliyeitwa na kuwezeshwa na Mungu kwa ajili ya jukumu bayana fulani." Katika Agano la Kale makundi matatu ya viongozi walipakwa mafuta: makuhani, wafalme na manabii. Yesu alitimiliza nafasi za majukumu zote hizi tatu (kama vile Ebr. 1:2-3). Angalia MADA MAALUM: KUPAKWA MAFUTA KATIKA BIBLIA (BDB 603) katika Biblia katika Marko 6:13.

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"kwa wale wakaao katika hali ya ugeni"** |
| **NKJV** | **"kwa wateule wa utawanyiko"** |
| **NRSV** | **"kwa utawanyiko wa uhamishoni"** |
| **TEV** | **"watu wateule wa Mungu wakaao kama wakimbizi"** |
| **NJB** | **"kwa wale waishio kama wageni"** |

Barua hii ya mzunguko ilikuwa imetumwa kwa makusanyiko ya wengi wa waamini wa Mataifa (1 Pet. 1:14,18; 2:9-10,12; 4:3-4). Petro mara kwa mara anatumia maneno ya Agano la Kale kuelezea kanisa la Agano Jipya (kama vile 1 Pet. 2:5,9).

◙**"waliotawanyika"** Hii kinayana "walio uhamishoni," ambayo inamaanisha "kupanda." Neno hili lilikuwa siku zote likitumika na Wayahudi wa Palestina kurejerea Wayunani waishio nje ya Palestina (kama vile Yohana 7:35). Petro analitumia hili kurejerea makanisa ynayounda Mataifa na waamini wa Kiyahudi katika Asia Ndogo ya kaskazini. Waamini

hawa sasa ni raia wa mbinguni (kama vile Flp. 3:20; Ebr. 11:8-10,13-16), lakini kwa kuwakumbusha juu ya maisha yao ya hapa duniani wanaishi kama wageni na walioo uhamishoni.

◙**"Ponto, Galatia, Cappadocia, Asia, and Bithynia"** Ponto halikuwa jimbo la Kirumi. Orodha hii inarejerea zaidi makundi ya kikabila. Orodha inaonekana kuaksi njia ya mpelekaji wa barua hii, ikianzia mwanzo ni mwa Bahari Nyeusi na kuzunguka mpaka nyuma ya Birthynia. Makundi haya kadhaa yanatajwa kuwepo siku ya Pentekoste (kama vile Mdo. 2:9-11).

**1:2 "kama vile Mungu Baba alivyotangulia kuwajua"** Huu ni msisitizo wa nguvu juu ya Ukuu wa Mungu (ambalo unaipa sifa 1 Petro), mara kwa mara ilitumika katika Agano la Kale kutambua uchaguzi wa YHWH wa Israeli (kama vile Kumb. 4:37; 7:6-7; 14:2; Isa. 65:9). Katika uchaguzi wa Agano la Kale unahusiana na huduma: hatahivyo katika maneno ya Agano Jipya yanahusiana na wokovu wa kiroho.
Maarifa ya mbele (nomino [*prognōsis*] hapa tu na Mdo. 2:23; kitenzi [*proginōskō*] inatumika kithiolojia katika Rum. 8:29; 11:2) haihusiani na bidii za kibinadamu au vigezo (kama vile Efe. 2:8-9; 2 Tim. 1:9; Tito 3:5). Mungu ni mtawala na historia yote imeamjaa Yeye. Ni binadamu tu wanaopitia wakati uliopita, uliopo na ujao. Kumbuka kwamba Petro msemaji wa kundi la kitume na mkanaji wa Bwana ni yeye aliyeandika maneno haya. Petro alichaguliwa kwasababu ya Mungu alivyo sio kwa sababu Petro alivyokuwa! Neema ya Mungu haihusiani na maarifa ya mbele au isingekuwa hivyo wokovu ungekuwa umejikita katika matendo ya binadamu ya baadaye.
Utatu unaonekana katika utendaji hapa: Baba (1 Pet. 1:3-5); Mwana (1 Pet. 1:6-9); na Roho Mtakatifu (1 Pet. 1:10-12). Neno "Utatu" sio neno la kibiblia bali utatu wa Mungu mara kwa mara unatajwa katika umoja wa kimuktadha. Angalia Mada Maalum: Utatu katika Marko 1:11.

## MADA MAALUM: UCHAGUZI/MAJAALIWA NA UHITAJI WA USAWA KITHIOLOJIA

Uchaguzi ni fundisho la ajabu. Hata hiyo, si wito ulio na upendeleo, lakini ni wito kuwa njia, chombo, au njia za ukombozi kwa wengine! Katika Agano la Kale neno hilo lilitumiwa hasa kwa ajili ya huduma; katika Agano Jipya linatumika hasa kwa ajili ya wokovu unaohusika katika huduma. Biblia hipatanishi kamwe kupingana kati ya Ufalme wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu, lakini inathibitisha zote mbili! Mfano mzuri wa mvutano wa kibiblia itakuwa Warumi 9 juu ya uchaguziwa Ufalme na Warumi 10 juu ya majibu muhimu ya wanadamu (kama vile Warumi 10:11,13).
Umuhimu wa huu muvatano wa kitheolojia unaweza kupatikana katika 1:4. Yesu ni mwanadamu mchaguzi wa Mungu na wote ni uwezo wa kuchaguliwa ndani yake (Karl Barth). Yesu ni Mungu. Yesu "ndio" kwa mahitaji ya mwanadamu aliyeanguka (Karl Barth). Waefeso 1:4 pia husaidia kufafanua suala hilo kwa kuthibitisha kwamba lengo la majaaliwa si mbinguni tu, lakini utakatifu (mapenzi ya kristo). Mara nyingi sisi huvutiwa na faida za injili na kupuuza majukumu! Wito wa Mungu(uchaguzi) ni kwa wakati pamoja na milele!
Mafundisho huja kuhusiana na ukweli mwingine, sio mmoja tu, ukweli usiohusiana. Hali au tabia nzuri inakuwa ni kundi dhidi ya nyota moja. Mugu hutoa ukweli katika mashariki na sio magharibi, mtindo. Hatupaswi kuondoa mvutano unaosababishwa na jozi za lahaja(fumbo la maneno) za kweli za mafundisho:

1. majaaaliwa/mchaguzi dhidi ya mapenzi huru ya mwanadamu
2. Usalama wa wanaoamini dhidi ya mahitaji ya uvumilivu
3. dhambi ya asili dhidi ya dhambi ya hiari
4. kutotenda dhambi dhidi ya kutenda dhambi kidogo
5. udhihirisho na utakaso wa papo kwa papo dhidi ya utakaso endelevu
6. Uhuru wa Kikristo dhidi ya wajibu wa Kikristo
7. Mungu anayeweza kupita uwezo wa binadamu dhidi ya Mungu wa asili
8. Mungu kama hatimaye isiyojulikana dhidi ya Mungu anayejulikana katika maandiko
9. Ufalme wa Mungu kama sasa dhidi ya kukamilishwa baadaye
10. Kutubu kama zawadi ya Mungu dhidi ya jibu muhimu la Agano la kibinadamu
11. Yesu kama Mungu dhidi ya Yesu kama mwanadamu
12. Yesu ni sawa na Mungu Baba dhidi ya Yesu wa kumtumikia Mungu Baba
13. Dhana ya kithioloji aya “agano” inaunganisha Ufalme wa Mungu (ambaye daima huchukua hatua kwa

kuweka mswada) pamoja na mamlaka ya mwanzo imani ya kuendelea kutubu kujibiwa kutoka kwa mwanadamu(k.v. Marko 1:15; Mdo. 3:16,19; 20:21). Kuwa mwangalifu wa maandishi ya uthibitisho wa upande mmoja wa fumbo la maneno na punguza kwa mwingine! Kuwa mwangalifu wa kuthibitisha mafundisho yako ya mapenzi tu au mfumo wa thiolojia!

◙**"katika kutakaswa na Roho"** "takasa" linatoka katika mzizi wa Kiyunani kama "tukufu" au "takatifu"; katika Kiaramu mzizi huu unamaanisha "kutenga kwa ajili ya jukumu fulani maalum." Waamini wanaitwa "walioitwa, waliotengwa, na waliopewa jukumu" (kama vile 2 The. 2:13, ambacho pia ni kifungu cha utatu).

Ukiri huu wa ufunguzi wa kazi ya ukombozi wa nafsi tatu za Utatu kwa kushughulikia tatizo la dhambi ya mwanadamu aliyeanguka ni muhimu katika kuelewa injili ya Petro.

1. Baba – aliyechaguliwa
2. Roho – aliyetakaswa
3. Mwana – aliyetoa maisha Yake

Kwakuwa tungo hii inapatikana katika vyote 2 The. 2:13 na 1 Pet. 1:2, inashangaza kudhania ikiwa Silvano (kama vile 1 Pet. 5:12, pia anaitwa Sila) anaweza kuwa mwandishi wa Petro aliyetokea kuandika 1 Petro na pia kama mwandishi Paulo alivyoandika 1 na 2 Wathesalonike (kama vile 1 The. 1:1; 2 The. 1:1). Kuna madokezo kadhaa kama haya katika 1 Petro yote. Angalia Mada Maalum: Utu wa Roho katika Marko 3:29. Hii pia inaelezea uhuru a utunzi (yaani maneno na tungo) wanayopewa waandishi katika tungo za kiruturujia zilizozoeleka zilizotumika na jamii ya kanisa la kwanza.

◙**"kutii Yesu Kristo"** Biblia inawasilisha uhusiano wa mwanadamu na Mungu katika namna ya kimaagano. Mungu siku zote huchukua hatua na kuanzisha jambo, lakini mwanadamu lazima aitikie kwa toba, imani, utii, huduma na ustahimilivu. Tumeokolewa ili kutumikia! Utii ni muhimu (kama vile Luka 6:46; Efe. 2:10). Angalia MADA MAALUM: AGANO katika Marko 14:24.

◙**"kununyiziwa damu ya Yesu Kristo"** Hii ni sitiari ya Agano la Kale

1. kutakaswa na msamaha (kama vile Law. 14:1-7)
2. uanzishwaji wa kitabu cha Agano (kama vile Kut. 24:3-8)
3. kuwekwa katika nafasi mpya (kama vile Kut. 29:20-22)

Dhabihu ya Yesu (kama vile Isaya 53; Marko 10:45; 2 Kor. 5:21) inaruhusu wafuasi Wake kukubaliwa, kutakaswa, kusamehewa na kupata uhusiano mpya na Mungu (kama vile Ebr. 10:22; 12:24). Waamini wanaletwa kwa damu (kukombolewa) na watu kupakwa na damu (utakaso).

◙**"Neema na amani na ziongezwe kwenu"** Hii inafanana na 2 Pet. 2:1 na Yuda 2. Paulo pia alitumia ufunguzi wa namna hii katika barua zake. Petro yawezekana alikuwa nafahamu juu ya barua za Paulo haswa Warumi na Waefeso au wote walitoa katika desturi ya Katekisimu ya karne ya kwanza iliyokuwa imezoeleka (yaani kuandaa nyenzo za kufundishia kwa waamini wapya). Kumbuka kwamba Sila anaweza kuwa alitumika kama mwandishi wa wote Petro (kama vile 1 Pet. 5:12) na Paulo (kama vile 1 na 2 The. 1:1). Sila pia alichukua nafasi ya Yohana Marko ambaye yawezekana alifundisha waumini wapya. Ikiwa hivyo ndivo, Sila pia alijishughulisha katika mafunzo ya Katekisimu na hivyo kufahamu namna ya uandishi wa nyenzo za kufundishia waumini wapya.

"Neema na Amani" ni ufunguzi wa kipekee wa salamu ya Kikristo na pia ukiri wa kithiolojia wa kipaumbele cha tabia ya neema ya Mungu na matendo ya kiukombozi ambayo yanatengeneza jukwaa kwa amani ya mwanadamu, amani iletwayo na matendo ya Utatu wa Mungu (kama vile 1 Pet. 1:2). Amani yetu inawezekana tu kwasababu ya Mungu alivyo na kile alichofanya.

Ni utanuzi kidogo wa kuzungumzia ufunguzi wa barua za Kikristo uliozoeleka kama uthibitisho kwamba Petro aliandika kwa wote Mataifa waaminio (neema, ambayo ilikuwa katika mfumo wa salamu ya Kikristo ya Kiyunani, *charein*) na Wayahudi (amani, ambayo ilikuwa fasiri ya salamu halisi ya Kiyahudi *shalom*).

◙**"na ziongezwe kwenu"** Hii ni nahau ya Kiebrania katika maombi ya Wayahudi (kamavile 1 Pet. 1:2; Yuda 2)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 PETRO 1:3-9**
**[3] Ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa rehema zake nyingi alituzaa mara ya pili ili tupate tumaini lenye uzima kwa kufufuka kwake Yesu Kristo katika wafu; [4] tupate na urithi usioharibika, usio na uchafu, usionyauka, uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu. [5] Nanyi mnalindwa na nguvu za Mungu kwa njia ya imani hata mpate wokovu ulio tayari kufunuliwa wakati wa mwisho. [6] Mnafurahi sana wakati huo, ijapokuwa sasa kwa kitambo kidogo, ikiwa ni lazima, mmehuzunishwa kwa majaribu ya namna mbalimbali; [7] ili kwamba kujaribiwa kwa imani yenu, ambayo ina thamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo, ijapokuwa hiyo hujaribiwa kwa moto, kuonekane kuwa kwenye sifa na utukufu na heshima, katika kufunuliwa kwake Yesu Kristo.[8] Naye mwampenda, ijapokuwa hamkumwona; ambaye ijapokuwa hamwoni sasa, mnamwamini; na kufurahi sana, kwa furaha isiyoneneka, yenye utukufu, [9] katika kuupokea mwisho wa imani yenu, yaani, wokovu wa roho zenu.**

**1:3 "Ahimidiwe"** Neno hili (*eulogētos*) sio kama lile lililotumika katika Mathayo 5 (*makarios*). Linatuka isivyo jumuishi juu ya Mungu katika Agano Jipya. Tunapata neno la Kingereza "eulogy" kutoka katika neno hili. Hii ni sawasawa na sifa za Utatu inayopatikana katika Efe. 1:3-14: 1 Pet. 1:3-5 kuhusiana na Baba, 1 Pet. 1:6-9 kwa Mwana, na 1 Pet. 1:10-12 Roho.

◙**"Mungu Baba"** Thomas Aquinas anajaribu kuthibitisha Uwepo wa Mungu kwa kuweka shabaha juu ya

1. mpangilio
2. umuhimu wa kimantiki ya kisababishi cha kwanza au kianzilishi cha kwanza
3. kianzilishi na matokeo

Hatahivyo, hizi vinajishughulisha na umuhimu wa Kifalsafa na kimantiki. Biblia inamfunua Mungu katika kipengele cha kibinafsi asiyepatikana kwa mantiki ya kibinadamu au tafiti. Ufunuo tu unamfunua Mungu kama Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo. Angalia MADA MAALUM: BABA katika Marko 13:22.

◙**"Bwana"** Neno la Kiyunani "Bwana" *(kurios)* linaweza kutumika kwa namna ya kijumla au katika namna iliyokuzwa Kithiolojia. Inaweza kumaanisha "bwana," "mheshimiwa," "mkuu," "mmiliki," "mume" au "Mwanadamu-Mungu kamili" (kama vile Yohana 9:36, 38). Matumizi ya Agano la Kale ya neno hili (Kiebrania, *adon*) ilitokana na ukaidi/kusitasita kwa Wayahudi kutamka jina la kiagano la Mungu, YHWH, kutoka katika kitenzi Kiebrania "kisaidizi" (kama vile Kut. 3:14). Angalia Mada Maalum: Majina ya Uungu katika Marko 12:26. Walikuwa na hofu ya kuvunja Amri, "Hutalitaja bure jina la Mungu wako" (kama vile Kut. 20:7; Kut. 5:11). Hivyo walifikiri ikiwa wasingelitaja basi wasingetenda dhambi ya kulitaja bure. Hivyo wakati wanasoma maandiko waliweka mbadala ya neno la Kiebrania *adon,* ambalo lilikuwa na maana sawa na neno la Kiyunani *kurios* (Bwana). Waandishi wa Agano Jipya walitumia neno hili kuelezea Uungu kamili wa Kristo. Tungo "Yesu ni Bwana" inawezekana ukiri wa wazi wa imani na kanuni ya ubatizo wa kanisa la kwanza (kama vile Rum. 10:9-13; 1 Kor. 12:3; Flp. 2:11).

◙**"ambaye kwa rehema zake nyingi"** Kifungu hiki, kuabudu tabia ya Mungu Baba (1 Pet. 1:3-5), inaweza kuaksi tenzi, ushairi au liturujia ya Katekisimu ya kwanza. Tabia kuu ya Biblia ni Mungu! Ni kusudi lake, tabia na matendo ambayo ni tumaini tu la mwanadamu aliyeanguka kwa ukubalifu na ustahimilivu (kama vile Efe. 2:4; Tito 3:5).

◙**"ametufanya sisi"** Aina hii ya tungo inatumika kuelezea utawala wa Mungu kama kweli pekee ya Kibiblia inayohusiana na wokovu (kama vile Mdo. 11:18; Yakobo 1:18; Efe. 1:4), lakini hii ni nusu utu ya dhana ya agano. Angalia Mada Maalum katika Marko 14:24.

◙**"kuzaliwa upya"** Huu ni mzizi uleule (*anagennaō*, kama vile 1 Pet. 1:23) kama katika Yoaha 3:3 (*gennaō*). Ni kitendo cha wakati uliopita endelevu. Agano Jipya pia inatumia sitiari kuelezea wokovu wetu: (1) "kuharakisha" (kama vile Kol. 2:13; Efe. 2:4-5; (2) "uumbaji mpya" (kama vile 2 Kor. 5:17; Gal. 6:15); na (3) "Mshiriki wa uungu wa asili," (kama vile 2 Pet. 1:4). Paulo anatamani sitiari inayofahamika "uasilishaji" wakati Yohana na Petro wanapendelea sitiari inayofahamika "uzao mpya."Kuwa "kuzaliwa upya" au "kuzaliwa kutoka juu" ni msisitizo wa Kibiblia katika hitaji la mwanzo mpya kabisa, familia mpya (kama vile Rum. 5:12-21). Ukristo sio matengenezo au maadili mapya; ni mahusianao mapya na Mungu. Mahusiano haya mapya na Mungu ni kwasababu ya

1. Rehema na neema za Baba
2. dhabihu za Baba na ufufu kutoka katika wafu

3. kazi ya Roho (kama vile 1 Pet. 1:2)

Mapenzi ya kiungu na matendo yanawapa waamini maisha mapya, tumaini jipya na urithi wa uhakika.

◙**"tumaini lenye uzima"** Kivumishi "hai" ni msisitizo unaojirudia rudia 1 Petro (kama vile 1 Pet. 1:3,23; 2:4,5,24; 4:5,6). Yale yote ambayo Mungu hupenda na kuyafanya kuwa "hai" na hudumu (yaani mzaha juu ya YHWH).

◙**"kwa kufufuka kwake Yesu Kristo"** Yesu ni mwakilishi wa Baba na maana ya ukombozi (kama alivyo mwakilishi wa Baba katika uumbaji na pia hukumu). Ufufuowa Yesu ni kweli kuu ya Injili (kama vile Rum. 1:4; 1 Kor. 15). Ufufuo ni kipengele cha ujumbe wa Mkristo kwamba Wayunani wasingekubali (kama vile Mdo. 17:16-34).

**1:4 "tupate na urithi "** Katika Agano la Kale kila kabila isipokuwa Walawi walipokea urithi wa ardhi. Walawi kama kabila la makuhani, watumishi wa hekaluni na waalimu wa eneo la mahali walionekana kama wao ndio walikuwa na YHWH Himself Mwenyewe kama urithi wao (kama vile Zab. 16:5; 73:23-26; 119:57; 142:5; Omb. 3:24). Waandishi wa Agano Jipya mara kwa mara walichukua haki na nafasi ya Walawi na kuwapa waamini wote. Hii ilikuwa ni njia ya kueleza kwamba wafuasi wa Yesu walikuwa watu wa kweli wa Mungu na kwamba sasa waamini wote waliitwa kutumika kama makuhani wa Mungu (kama vile 1 Pet. 2:5,9; Ufu.1:6), kama Agano la Kale linavyoeleza juu ya Israeli wote (kama vile Kut. 19:4-6). Msisitizo wa Agano Jipya sio kwa mtu mmoja mmoja kama kuhani mwenye faida fulani fulani lakini juu ya ukweli kwamba waamini wote ni makuhani ambalo linahitaji mtazamo wa jamii moya wa utumishi (kama vile 1 Kor. 12:7). Watu wa Mungu wa Agano Jipya wamepewa jukumu katika Agano la Kale la muinjilishaji wa ulimwengu (kama vile Mwa. 12:3; Kut. 19:5b; Mt. 28:18-20; Mdo. 1:8).

Hii ni dhana ya Yesu kama mmiliki wa uumbaji kwasababu alikuwa Mwakilishi wa Baba wa uumbaji (kama vile Yohana 1:3,10; 1 Kor. 8:6; Kol. 1:16; Ebr. 1:2-3). Sisi ni warithi wasaidizi kwasababu Yeye ni mrithi (kama vile Rum. 8:17; Gal. 4:7; Kol. 3:24).

## MADA MAALUM: URITHI WA MWAMINI (toka 1 Petro 1)

Katika Agano la Kale kila kabila isipokuwa la Walawi lilipokea urithi wa ardhi (kama vile Yoshua 14-22). Walawi, kama kabila la kikuhani, wahudumu wa hekaluni, na waalimu wa kanisa la mahali, walionekana kuwa na YHWH Mwenyewe kama mrithi wao (kama vile. Zab. 16:5; 73:23-26; 119:57; 142:5; Wimb. 3:24). Waandishi wa Agano Jipya mara nyingi walichukua haki na upendeleo wa Walawi na kuitumia kwa waamini. Hii ilikuwa ni njia yao ya kudai kuwa wafuasi wa Yesu walikuwa watu wa Mungu na kwamba sasa waamini wote wameitwa kutumika kama makuhani mbele za Mungu (kama vile 1 Pet. 2:5,9; Uf. 1:6), kama Agano la Kale linavyo watetea Waisrael wote(kama vile Kut. 19:4-6). Msisitizo wa Agano Jipya sio juu ya mtu binafsi kama kuhani aliye na upendeleo Fulani, bali ni katika kweli kwamba waamini wote ni makuhani, wakihitaji ushirika wa mwenendo wa kitumishi (kama vile 1 Kor. 12:7). Watu wa Mungu wa Agano Jipya wamekwisha pewa majukumu ya Agano la Kale ya kueneza injili ulimwenguni (kama vile Mwa. 12:3; Kut. 19:5b; Mt. 28:18-20; Lk 24:46-47; Mdo 1:8; angalia Mada Maalum: Mpango wa YHWH wa ukombozi wa Milele).

Hii ni dhana ya Yesu kama mmiliki wa uumbaji kwa sababu alikuwa ni wakala wa Baba kipindi cha uumbaji (kama vile. Yn 1:3,10; 1 Kor. 8:6; Kol. 1:16; Ebr. 1:2-3). Sisi ni warithi wenza kwa vile Yeye ni mrithi (kama vile Rum. 8:17; Gal. 4:7; Kol. 3:24). Maandiko yanazungumza kuhusu kurithi kwa waamini (kama vile Mdo. 20:32; 26:18; Efe. 1:4; Kol. 1:12; 3:24) vitu vingi kwa sababu ya mahusiano yao ya kifamilia na Yesu ambaye ndiye mrithi wa vitu vyote (kama vile Ebr. 1:2). Kwa hiyo, wao pia ni warithi wenza (kama vile Rum. 8:17; Gal. 4:7) wa

1. Ufalme (kama vile Mt. 25:34, 1 Kor. 6:9-10; 15:50; Efe. 5:5)
2. Maisha ya milele (kama vile Mt. 19:29; Ebr. 9:15)
3. Ahadi za Mungu (kama vile Ebr. 6:12)
4. Ulinzi wa Mungu wa ahadi zake (kama vile 1 Pet. 1:4-5)

◙**"usioharibika, usio na uchafu, usionyauka"** Katika 1 Pet. 1:4 tungo tatu za maelezi zinatumika kuelezeaurithi wa waamini kwa kutumia maelezo ya kihistoria ya Agano la Kale kuelekea Nchi ya Ahadi. Palestina kijiografia lilikuwa eneo pekee la ardhi iliyo daraja kati ya Mesopotamia na Misri. Hii ilipelekea uvamizi. Urithi wa mwamini hauathiriwi na migogoro ya kidunia.

1. ni "isiyoharibika" au "salama mbali na uvamizi"

2. ni "isiyotiwa unajisi" au "isiyochakaa"
3. haita "chakaa"; hakuna muda wa ukomo wa muda juu ya umiliki wake

◙**"uliotunzwa mbinguni kwa ajili yenu"** Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati timilifu. Hili ni neno la kijeshi kwa ngome ilindwayo au ya kijeshi (kama vile Flp. 4:7).
Neno "mbingu" iko katika wingi. Hii inaaksi wingi wa Kiebrania. Kiebrania ya Kale ilikuwa na nomino ya wingi ambayo inaweza kuwa katika hali ya kuwasisitizia (mfano matumizi ya wingi wa Mungu wanaotumika kwa ajili ya Mungu ya walimuwa Kiyahudi baadaye). Walimu wa sheria za Kiyahudi walibishana ikiwa kulikuwa na viwango vitatu vya mbingu (kama vile Kumb. 10:14; 1 Wafalme. 8:27; Neh. 9:6; 2 Kor. 12:2) au mbingu saba kwasababu ya namba saba kuwa namba ya ukamilifu (kama vile Mwa. 2:1-3).

**1:5 "Nanyi mnalindwa na nguvu za Mungu"** Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati uliopo. Kama urithi wetu (maisha ya kiroho) yanalindwa, hivyo pia utu wetu (maisha ya kimwili). Utu wa Mungu na ahadi unazunguma maisha yetu katika kila kipengele. Hili lilikuwa neno la kutia moyo lenye msaada lililohitaji wakati wa dhiki, mateso na mafundisho ya uongo (kama vile 2 Petro). Hii haimaanishi kwamba waamini hawatauwawa na kuteswa; badala yake Mungu alikua pamoja nao na kwa ajili yao na hatimaye wawe washindi kupitia Yeye. Huku ni ufanano wa kithiolojia kwa ujumbe wa kitabu cha Ufunuo.

◙**"kwa njia ya imani"** Tambua kweli kinzani ya kiagano. Mungu anawalea na urithi wao lakini bado lazima waendelee katika imani. Ni uvutano kati ya jozi hizi za kilahaja za Kibiblia (yaani ukuu wa Mungu na utashi huru wa kibinadamu) mbayo imesababisha maendeleo ya mfumo wa kithiolojia yakisisitiza upande mmoja wa kinzani. Pande zote mbili ni za Kibiblia; pande zote mbili ni muhimu! Mungu hushughulikia wanadamu kwa namna isiyo na masharti (Mungu mpaji) na maagano yenye masharti (mwitikio wa mtu mmoja mmoja).

◙**"wokovu ulio tayari kufunuliwa "** Biblia inatumia maneno yote ya njeo za vitenzi vya Kiyunani. Hatutakuwa wakamilifu, kuokolewa kwa ukamilifu mpaka siku ya Ufufuo (kama vile 1 Yohana 3:2). Hii mara kwa mara inaitwa utukuzwaji (kama vile Rum. 8:29-30). Angalia Mada Maalum hapa chini.

## MADA MAALUM: WOKOVU (NJEO ZA VITENZI VYA KIYUNANI VILIVYOTUMIKA)

Wokovu siyo kitu, bali ni uhusiano. Haiishii hapo mtu anapomwamini Kristo; ndiyo safari imeanza! Siyo Sera ya bima ya moto, wala tiketi ya kwenda mbinguni, bali ni kukua kumfanana Kristo. Tunao usemi katika Amerikaunaosema, kadiri wawili katika ndoa wanavyoendelea kuishi, ndiyo wanaendelea kufanana. Hili ndilo lengo la wokovu!

**WOKOVU KAMA KITENDO KILICHO KAMILISHWA (WAKATI TIMILIFU)**

- Matendo 15:11
- Warumi 8:24
- 2 Timotheo 1:9
- Tito 3:5
- Warumi 13:11 (inajumuisha WAKATI TIMILIFU ukiwa na mazingira ya WAKATI UJAO )

**WOKOVU KAMA HALI YA KUWA (TIMILIFU)**

- Waefeso 2:5,8

**WOKOVU KAMA MCHAKATO UNAOENDELEA (WAKATI ULIOPO)**

- 1 Wakorintho 1:18; 15:2
- 2 Wakorintho 2:15
- 1 Petro 3:21

**WOKOVU KAMA UKAMILISHO UJAO (WAKATI UJAO katika NJEO YA KITENZI au MAZINGIRA)**

- Warumi 5:9, 10; 10:9,13
- 1 Wakoritho 3:15; 5:5
- Wafilipi 1:28;
- 1 Wathesalonike 5:8-9
- Waebrania 1:14; 9:28

- 1 Petro 1:5,9

Kwa hivyo, wokovu unaanza na uamuzi wa imani ya awali (kama vile Yohana 1:12; 3:16; Rum 10:9-13), lakini hili lazima liendane na mchakato wa imani katika mtindo ya maisha (kama vile Rum. 8:29; Gal. 3:19; Efe.1:4; 2:10), ambao siku moja utakuja kukamilishwa kwa kuonekana (kama vile 1Yoh. 3:2). Hatua hii ya mwisho inaitwa utukufu.Hili linaweza kuelezwa kama

4. Utukufu wa awali – udhihirisho (kukombolewa kutoka katika adhabu ya dhambi)
5. Wokovu endelevu–utakaso (kuokolewa toka katika nguvu ya dhambi)
6. Wokovu wa mwisho – utukufu (kuokolewa kutoka katika uwepo wa dhambi)

◙**"wakati wa mwisho"** Hili ni neno la baadaye la dhana ya Kiyahudi la zama mbili lakini kutoka Agano la Kale tunatambua kwamba zama mbili zinarandana. Siku za mwisho zilianza wakati wa kuvaa mwili katika Bethlehemu na atahitimisha wakati wa Ujio wa Pili. Tumekuwa katika siku za mwisho kwa takribani Milenia mbili. Angalia MADA MAALUM: ENZI HII NA ENZI IJAYO katika katika Marko 13:8.

**1:6**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **'katika hili muwe na furaha kuu"** |
| **NKJV** | **"katika hili mnafuraha"** |
| **NRSV** | |
| **(tanbihi)** | **"furahini katika hili"** |
| **TEV** | **"muwe na furaha katika hili"** |
| **NJB** | **"hii ni furaha kubwa juu yenu"** |

Hii ni kauli ya kati elekezi ya wakati uliopo (A. T. Robertson) au shurutishi (Barbara na Timothy Friberg). Waamini wanaendelea kusifu kwasababu ya uhusiano wao salama na Mungu (kama vile 1 Pet. 1:3-5) hata katikati ya ulimwengu ulioanguka (kama vile Yakobo 1:2-4; 1 The. 5:16; Rum. 5:3; 8:18).

◙**"ijapokuwa sasa kwa kitambo kidogo"** Majaribu na dhiki ya wakati huu hayawezi linganishwa na umilele wa Mungu wetu (kama vile Rum. 8:18).

◙**"ikiwa ni lazima, mmehuzunishwa kwa majaribu"** Hili ni neno la Kiyunani *dei*, ambalo linamaanisha uhitaji au kuunganishwa na sentensi yenye masharti. Kuna makisio ya kitenzi "kisaidizi" ambacho kingetengeneza iwe ya kwanza yenye masharti na yenye mafumbo inadhaniwa kuwa kweli. Petro anadhani kwamba maisha ya kiungu yatapelekea katika dhiki. Anarudia mada hii ya mateso mara kwa mara (kama vile 1 Pet. 1:6-7; 2:19; 3:14-17; 4:1,12-14,19; 5:9).

◙**"mmehuzunishwa"** Hii ni kauli tendwa ya wakati uliopita endelevu ya wakati timilifu. Mwakilishi asiyeelezewa wa irabu sauti ni ya uovu; Mungu anatumia hata uovu kwa makusudi yake mema. Hata Yesu Mwenyewe alikamilishwa kwa vitu vilivyomtesa zaidi (kama vile Ebr. 5:8-9). Mateso inatumikia lengo linalotiwa katika maisha ya imani!
Mtanziko wa kithiolojia ni kwamba kuteseka kuna vyanzo vitatu

1. yule aliye muovu
2. ulimwengu ulioanguka
3. Mungu
    a. kwa adhabu ya muda ya dhambi
    b. makuzi ya kufanana na Kristo

Tatizo ni sijawahi kujua kipi ni kipi! Hivyo Nachagua kuamini kwamba ikija, ndio itakuja, Mungu atalitumia kwa ajili ya makusudi Yake. Kitabu nikipendacho katika hili eneo ni Hannah Whithall Smith's *The Christian's Secret of a Happy Life*.

◙**"kwa majaribu ya namna mbalimbali"** Hiki kivumishi cha Kiyunani kinamaana ya rangi nyingi (kama vile Yakobo 1:2). Kuna aina nyingi za majaribu, mapito na mateso. Katika 1 Pet. 4:10 neno lilelile linatumika kueleza sehemu nyingi ya neema za Mungu. Hatujawahi kujaribu na kwenda zaidi ya upaji wake (kama vile 1 Kor. 10:13).

**1:7 "ili kwamba kujaribiwa kwa imani yenu"** Hii ni *hina* or au kishazi cha kusudi. Mateso yanafanya kazi ya kuimarisha imani. Katika Biblia yote, Mungu amejaribu watoto wake (kama vile Mwa. 22:1; Kut. 15:22-25; 16:4; Kumb. 8:2,16; 13:3; Amu. 2:22; 2Nyak. 32:31; Mt. 4:1; Luka 4:1-2; Rum. 5:2-4; Ebr. 5:8-9; Yakobo 1:2-4). Mstari huu una nomino *dikimon* na nomino endelevu ya *dikimazō*, vyote viwili vina visawe vya majaribu kwa mtazamo kuelekea kuimarisha na hivyo uthibitisho. Angalia Mada Maalum juu ya Maneno ya Kiyunani "Majaribu" na visawe vya Marko 1:13b.

◙**"ambayo ina thamani kuu kuliko dhahabu"** Katika maisha haya kipawa chetu kikuu (kama vile Yohana 20:27; 2 Kor. 4:17). Katika imani ya umilele imebadilishwa muono wa wazi. Mungu anaheshimiwa na kupendezwa wakati imani inaposhinda majaribu yasababishwayo na imani yetu katika Yeye (kama vile 1 Pet. 4:12-16). Ukuaji wa kiroho unakuja tu kupitia imani iliyojaribiwa (kama vile Rum. 5:2-5; Ebr. 12:11; Yakobo 1:2-4).

◙**"katika kufunuliwa kwake Yesu Kristo"** Neno hili lilelile (*apokalupsis*) inatumika kama cheo kwa kitabu cha Agano Jipya, Ufunuo. Inamaanisha "kufunua," "kuweka wazi," au "kufanya ijulikane." Hapa inarejerea kwa Ujio wa Mara ya Pili, maudhui yaliyozoeleka katika maandiko ya Petro (kama vile 1 Pet. 1:7,13; 2:12; 4:13; 5:4).

**1:8 "ijapokuwa hamkumwona"** Hata kati ya waaminio watesekao wanatakiwa kutumainia katika Yeye. Yesu aliwaombea wale walio muamini Yeye bila kumuona katika Yohana 17:20; 20:29.

◙**"sasa, mnamwamini"** Huu usuli wa kiasili wa neno hili unasaidia kuimarsha maana ya kisasa. Kumbuka wandishi wa Agano Jipya walikuwa wafikiriaji wa Kiebrania wakiandika katika Koine ya Uyunani. Katika Kiebrania kiasili ilirejerea kwa mtu mwenye msimamo thabiti, (miguu yake iliyowekwa ili isisukumwe). Ilikuja kutumika kisitiari kwa mtu ambaye alikuwa akitegemewa, mwaminifu au wa kutumainiwa. Neno sawa la Kiyunani (*pistis* au *pisteuō*) linafasiriwa katika neno la Kingereza kwa maneno "imani," "kuamini," na "tumaini." Imani ya Kibiblia au tumaini sio msingi tunachofanya, lakini mtu ambaye tunamtumaini. Ni Utumainifu wa Mungu sio wetu ambayo ni shabaha. Mwanadamu aliyeanguka anatimaini katika utumainifu wa Mungu, ana amini Uaminifu Wake, kuamini katika mpendwa Wake na katika upaji Wake. Shabaha sio katika wingi au kina cha imani ya mwanadamu bali kinachoangaliwa na hiyo aimani (kama vile 1 Pet. 1:8,21; 2:6-7). Angalia Mada Maalum katika Marko 1:15.

◙**"na kufurahi sana, kwa furaha isiyoneneka"** Neno "furaha kuu" ilitumika hapo mwanzo kabisa katika 1 Pet. 1:6. Inarejerea kwa furaha kuu mara nyingi ikiambatana na mwonekano wa nje kama vile kupaza sauti, kucheza, n.k (kama vile Luka 1:44,47; 10:21; Yohana 5:35; 8:56). Furaha hii amabayo Petro anaizungumzia inapatikana katikati ya mateso (kama vile 1 Pet. 4:13; Rum. 5:3; 1 The. 5:17). Furaha hii ni moja ya furaja isiyotegemewa ya Roho katika nyakati ya majaribu na taabu.

◙**"yenye utukufu"** Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati timilifu. Waaminio kwa imani (si kwa kuona) kulipuka kwa vyote furaha isiyoelezeka na utukufu kamili! Furaha hii na utukufu hauwezi kufichika. Ni chemi chemi inayotiririka inayozalishwa na Roho (kama vile Yohana 4:14; 7:38). Ni ushuhuda wa nguvu wa injili kwa wote waliokutana na injili ya watu chini ya shinikizo. Angalia MADA MAALUM: UTUKUFU *(DOXA)* katika Marko 10:37.

**1:9 "katika kuupokea mwisho wa imani yenu"** Hii ni kauli ya kauli ya kati endelevu ya wakati uliopo. Hii inamaanisha kwamba afuraha yetu sio ya utimilifu wa baadaye lakini pia uhalisia wa sasa hata katikati ta taabu kwasababu ya matendo ya Utatu wa Mungu kwa niaba yetu (kama vile 1 Pet. 1:2).

◙**"wokovu wa roho zenu"** Hii inarejerea utukuzwaji. Wokovu unachukuliwa katika Agano Jipya kama maamuzi yaliyofanywa (njeo ya wakati uliopita usio timilifu, kama vile Rum. 8:24), bali pia kama mchakato unaoendelea (kama vile 1 Kor. 1:18; 15:2; 1 The. 4:14) kutwaliwa kwa baadaye (yaani njeo ya wakati ujao, kama vile Rum. 5:9,10; 10:9). Angalia Mada Maalum katika 1 Petro 1:5. Hiki kipengele cha baadaye mara kwa mara kinajengwa na tabia kama "utukuzwaji" (kama vile Rum. 8:29-30). Waamini siku moja watamwona Yesu kama alivyo na kubadilishwa kufanana kama Yeye (kama vile 1 Yohana 3:2).
Neno la Kiyunani *psuchē* (nafsi) inatumika katika maandiko ya Petro (kama vile 1 Pet. 1:9,22; 2:11,25; 3:20; 4:19; 2 Pet. 2:8,14). Inatumika kama nahau ya Kiebrania kwa nafsi kamili. Wanadamu si wenye sehemu mbili wala viumbe vyenye

sehemu tatu bali umoja (kama vile Mwa. 2:7). Ni kweli kwamba sisi wanadamu tunahusiana na sayari hii kwasababu tumeumbwa kwa sura na mfano wa Mungu, tunahusiana na ulimwengu wa roho. Tu raia wa ulimwengu hizi mbili.
Si sawa kithiolojia kutengeneza mfumo wa kithiolojia juu ya 1 The. 5:23 na Ebr. 4:12 na hivyo kujaribu kulinganisha maandiko yote ya kibiblia kwenye sehemu hizi tatu (mwili, nafsi na roho). Yanarejerea tu mtu kamili na nguvu ipenyayo ya neno la Mungu. Kuwa makini na mtu anayedai kwamba msingi wa Biblia yote inapatikana katika maandiko mawili yaliyowazi, yaliyohakikiwa nje ya muktadha na kufanywa katika vipimo vya kithiolojia mabayo kupitia kwayo tunaangalia maandiko yote (Watchman Nee). Ikiwa huu ndio ulikuwa msingi Roho angekuwa ameweka wazi katika mafundisho ya wazi ya kimuktadha na angekuwa amerudia mara kwa mara. Biblia sio kitabu cha mafumbo au wachemsha bongo! Mungu anataka kuzungumza pamoja nasi na kweli kuu zinapatikana katika mafundisho yaliyowazi kimuktadha.

## UTAMBUZI WA MUKTADHA KWA MISTARI YA 1:10-21

A. 1 Pet. 1:10-12 inashughulikia na maarifa ya manabii wa Agano la Kale ya wokovu wa Agano Jipya katika Kristo.
B. "Roho" kupitia manabii anafunua mambo matatu kwa waaminio katika 1 Pet. 1:11-12.
   1. kuteseka kwa Masihi(Mwa. 3:15; Zab. 22; Isa. 52:13-53:12)
   2. Utukufu utakaofuata (Isaya 56-66)
   3. Manabii walikuwa wakizungumza zaidi ya siku zao (yaani Isaya, Ezekieli, Danieli, Mika, Zekaria)
C. Katika 1 Pet. 1:13-17, Petro anawaomba waaminio kufanya vitu sita ili kujilinda wenyewe
   1. kuandaa fahamu zao, 1 Pet. 1:13
   2. kuwa wapole wa roho, 1 Pet. 1:13
   3. kuweka matumaini yao kwenye neema ya wakati wa mwisho, 1 Pet. 1:13
   4. msiafuatishe namna ya ulimwengu wa sasa, 1 Pet. 1:14
   5. kuishi maisha matakatifu, 1 Pet. 1:15
   6. kuishi kwa kumuheshimu Mungu, 1 Pet. 1:17
   7. upendo udumuo wa kupendana (ya saba imeongezwa kutoka kwa 1 Pet. 1:22)

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 PETRO 1:10-12**
**[10] Katika habari ya wokovu huo manabii walitafuta-tafuta na kuchunguza-chunguza, ambao walitabiri habari za neema itakayowafikia ninyi. [11] Wakatafuta ni wakati upi, na wakati wa namna gani ulioonywa na Roho wa Kristo aliyekuwa ndani yao, ambaye alitangulia kuyashuhudia mateso yatakayompata Kristo, na utukufu utakaokuwako baada ya hayo. [12] Wakafunuliwa ya kuwa si kwa ajili yao wenyewe, bali kwa ajili yenu walihudumu katika mambo hayo, ambayo sasa yamehubiriwa kwenu na wale waliowahubiri ninyi Injili kwa Roho Mtakatifu aliyetumwa kutoka mbinguni. Mambo hayo malaika wanatamani kuyachungulia.**

**1:10 "Katika habari ya wokovu huo"** Hii imekuwa mada tangu (1) 1 Pet. 1:2, ambayo inaelezea kazi ya Mungu wa Utatu katika wokovu; (2) 1 Pet. 1:3-5, ambayo inaelezea mungu kuutunza na kuulinda huu wokovu; na (3) 1 Pet. 1:6-9, ambayo inaelezea mateso ya waaminio hawa kwasababu ya wokovu huu.

◙**"manabii"** Hii inarejerea manabii wa Agano la Kale (kama vile 1 Pet. 1:12). Katika mawazo ya walimu wa kiyahudi walifikiri waandishi wote waliovuviwa walichukuliwa kama manabii. Musa aliitwa nabii (kama vile Kumb. 18:18) na kile tunachokiita kwa Kingereza vitabu vya Kihistoria (yaani Yoshua mpaka Wafalme) waliitwa na Wayahudi "manabii wa kale."

◙**"za neema itakayowafikia ninyi"** Tungo hii inamaanisha kwamba manabii wa Agano la Kale walijua kitu fulani juu ya agano jipya. Hii pia inamaanisha kauli ya Yesu juu ya Ibrahimu katika Yohana 8:56 (kama vile II Esdras 3:14). Maana hii hii inatajwa katika Ebr. 11:13b. Ni ngumu kujua hakika kiasi gani manabii wa Agano la Kale walifahamu kuhusu injili. Maelezo ya Yeremia ya Agano Jipya katika Yer. 31:31-34 (pia Ezek. 36:22-38) inasonta kueleke ukubalifu uliojikita juu ya upendo na matendo, sio matendo ya kibinadamu. Mathayo 13:17 inasema kwamba wengi wa Manabii wa Agano la Kale wanaona na kusikia kile Yesu alichokuwa anakifanya na kusema.

Hata unabii wa Isaya juu ya kuzaa kwa Bikra (kama vile 1 Pet. 7:14), wakati invyotafsiriwa katika muktadha, inarejerea kuzaa kwa asili pamoja na ubaadaye (kama vile 1 Pet. 7:15-16), sio kuzaa kwa baadaye kwa kimasihi. Ni mathayo na Luka waonao maana kamili ya unabii wa Isaya. Hii inaweza kuwa kweli juu ya unabii bayana mwingine katika Hosea (kama vile Hos. 11:1) na Zekaria (kama vile Zek. 9:9; 11:13; 12:10). Ilikuwa ni Wayahudi wazungumzao Kiyunani wa Agano Jipya na Mitume (Uanishi wa elimu ya Kristo). Wanaweza kuwa wamejifunza hii kutoka kwa Yesu Mwenyewe kama alivyofundisha wale wawili njiani Emmau (kama vile Luka 24:13-35, especiallyhaswa 1 Pet. 1:27).

◙**"walitafuta-tafuta na kuchunguza-chunguza"** Hizi zinaonekana kuwa visawe (kama vile *Greek-English Lexicon of the NewTestament: based on Semantic Domains*, Vol. 1, kur. 331).

**1:11**
**NASB** **"wakitafta kujua wakina nani na muda gani"**
**NKJV** **"wakitafta kujua ni nini na muda gani"**
**NRSV** **"wakitafta kujua juu ya mtu na muda"**
**TEV (tanbihi)** **"wakijaribu kutafta ni lini ingekuwa na muda itakavyokuwa na namna gani itakuja kuwa"**
**NJB** **"wakitafta kujua muda na mazingira"**

Hii inamaanisha vyote mtu na muda. Walitegemea Masihi wa Kidaudi kuvunja historia wakati mahususi uliteuliwa na Mungu. Kama sisi, wao wali "walitazama kupitia kioo cha giza" (kama vile 1 Kor. 13:9-13).

◙**"Roho wa Kristo aliyekuwa ndani yao"** Roho na Masihi wanaunganishwa katika katika Agano la Kale (kama vile Isa. 11:1-2; 48:16; 61:1). Tambua kwamba Roho Mtakatifu ni "Roho ya Kristo" (kama vile Rum. 8:9; Gal.4:6). Tambua pia kipengele cha Roho akaaye ndani, hata katika Agano la Kale. Kazi za Yesu na Roho zinarandana. Angalia kweli ile ile inavyoelezewa katika 2 Pet. 1:21.

## MADA MAALUMU: YESU NA ROHO

Kuna bubujiko kati ya kazi ya Roho na Mwana. G. Campbell Morgan alisema jina zuri la Roho Mtakatifu ni "Yesu mwingine" (hata hivyo, tofauti yao, utu wa milele). Ufuatao ni mlinganisho wa mhutasari wa kazi na wadhifa wa Mwana na Roho.

1. Roho aitwaye "Roho wa Yesu" au maelezo yanayofanana (kama vile Rum. 8:9; 2 Kor. 3:17; Gal. 4:6; 1 Pet. 1:11).
2. Wote wanaitwa kwa maneno sawa
    a. "kweli"
        1) Yesu (Yohana 14:6)
        2) Roho (Yohana 14:17; 16:13)
    b. "mwombezi"
        1) Yesu (1 Yohana 2:1)
        2) Roho (Yohana 14:16,26; 15:26; 16:7)
    c. "Mtakatifu"
        1) Yesu (Marko 1:24; Luka 1:35; Matendo 3:14; 4:27,30)
        2) Roho (Luka 1:35)
3. Wote hukaa ndani ya waamini
    a. Yesu (Mt. 28:20; Yohana 14:20,23; 15:4-5; Rum. 8:10; 2 Kor. 13:5; Gal. 2:20; Efe. 3:17;Kol. 1:27)
    b. Roho (Yohana 14:16-17; Rum. 8:9,11; 1 Kor. 3:16; 6:19; 2 Tim. 1:14)
    c. Baba (Yohana 14:23; 2 Kor. 6:16)
4. Kazi ya Roho ni kutoa ushuhuda juu ya Yesu(kama vile Yohana 15:29; 16:13-15)

◙**"alitangulia kuyashuhudia mateso yatakayompata Kristo"** Hiki ndicho kilichowashangaza Wayahudi (kama vile 1 Kor. 1:23). Mtumishi atesekaye ilifanyika nguzo ya mahubiri ya mwanzo ya Petro na Paulo katika Matendo ya Mitume ambayo tunayaita *kerygma* (yaani kile ambacho kilitangazwa, kama vile Matendo ya Mitume 2:23,24; 3:18; 4:11; 10:39;

17:3; 26:23). Hiki ndicho haswa kile ambacho Yesu alikuwa amejaribu kuwaambia wale Kumi na Mbili wakati alipokuwa nao pamoja (kama vile Mt. 16:21; 20:17-19; Marko 8:31; Luka 9:22), lakini hawakuweza kupokea (kama vile Marko 9:31-32; 10:32-34; Luka 9:44-45; 18:31-34).

Kuna vidokezo vya mateso ya Masihi katika Agano la Kale (yaani Mwa. 3:15; Zaburi 22; Isaya 53), lakini Waisraeli wa Agano la Kale walikuwa wakitarajia Masihi kuja kama mtawala kuhukumu wanadamu wote na kurejesha Israeli kwenye nafasi ya utawala na nguvu. Walikosa ule ujio wa Masihi ambao ulikuwa umefunuliwa na maisha ya Yesu na mafundisho (yaani Mwokozi na Hakimu).

Chini ni jedwali la kuvutia la *kerygma* linalopatikana katika H. Wayne House's *Chronological and Background Charts of the NewTestament*, (kur. 120).

## MADA MAALUMU: MAFUNDISHO YA KANISA LA KWANZA

Kuna maoni mengi kuhusu Ukristo. Siku zetu hizi ni siku za wingi wa dini, kama ilivyokuwa karne ya kwanza. Binafsi, kwa pamoja nayajuisha na kuyakubali makundi yote yale yanayodai kumfahamu na kumwamini Yesu Kristo. Wote hatukubaliani kuhusu hili au lile lakini kimsingi ukristo ni kumhusu Yesu. hata hivyo, kuna makundi yanayodai kuwa wapo wakristo ambao wanaonekana “kufanana.” Ni kwa vipi naweza kuelezea tofauti ?

Sawa, kuna njia mbili:

A. Kitabu kinachoweza kusaidia kujua kile makundi ya madhehebu ya kisasa yanaamini (kutoka katika maandiko yao) *The Kingdom of the Cults* na Walter Martin.
B. Hotuba ya makanisa ya awali, hasa wale kupitia Mtume Petro na Paulo katika kitabu cha Matendo, wanatupatia maelezo ya msingi kwa vipi waandishi wa karne ya kwanza waliovuviwa waliuelezea Ukristo kwenye makundi. “matamko” haya ya awali au “mafundisho” (ambacho kitabu cha matendo ni mhutasari wake) yanaendana na neno la Kiyunani *Kerygma.* Ufuatao ni ukweli halisi wa injili kuhusu Yesu katika Matendo ya Mitume:
    1. Kutimiliza nabii nyingi za Agano la Kale- – Mdo. 2:17-21,30-31,34; 3:18-19,24; 10:43; 13:17-23,27; 33:33-37,40-41; 26: 6-7,22-23
    2. Alitumwa na YHWH kama alivyoahidi- Mdo. 2:23; 3:26
    3. Miujiza iliyotendeka kuthibitisha ujumbe wake na kudhihilisha huruma ya Mungu- – Mdo. 2:22; 3:16; 10:38
    4. Waliofunguliwa, wasiomilikiwa- Mdo. 3:13-14; 4:11
    5. Kusurubishwa – Mdo. 2:23; 3:14-15; 4:10; 10:39; 13:28; 26:23
    6. Alifufuliwa kuja uzimani- Mdo. 2:24,31-32; 3:15,26; 4:10; 10:40; 13:30; 17:31; 26;23
    7. Ameinuliwa mkono wa kulia wa Mungu Baba- Mdo. 2:33-36; 3:13,21
    8. Atakuja tena mara ya pili – Mdo. 3:20-21
    9. Alichaguliwa kuwa hakimu- Mdo. 10:42; 17:31
    10. Akamtuma Roho Mtakatifu- Mdo. 2:17-18,33,38-39; 10:44-47
    11. Mwokozi wa kila aaminiye- Mdo. 13:38-39
    12. Hakuna mwingine aliye mwokozi- Mdo. 4:12; 10:34-36

Hapa kuna baadhi ya njia za kukubali kwenye hizi nguzo za ukweli:

1. Tubu – Mdo. 2:38; 3:19; 17:30; 26:20
2. Amini – Mdo. 2:21; 10:43; 13:38-39
3. Ubatizwe – Mdo.2:38; 10:47-48
4. Mpokee Roho – Mdo. 2:38; 10:47
5. Yote yatakujilia- Mdo.2:39; 3:25; 26:23

Mpango huu ulitumika kama tamko la kanisa la mwanzo, ingawa waandishi tofauti wa Agano Jipya wanaweza kuacha sehemu au wakasisitiza wengine hasa katika maandiko yao. Injili yote ya Marko kwa karibu inafuata dhana ya mafundisho. Marko kiutamaduni anaonekana kama kuitengeneza hotuba ya Petro, iliyohubiriwa huko Roma, katika injili iliyoko kwenye maandishi. Injili zote za Mathayo na Luka zinafuata muundo wa Marko.

◙**"ana utukufu utakaokuwako baada ya hayo"** Hii imeelezewa kwenye Isa. 53:10-12.

**1:12 "si kwa ajili yao wenyewe, bali kwa ajili yenu"** Kuna mahali kadhaa katika maandiko ya Paulo ambapo anaelezea ukweli huu (kama vile Rum. 4:23-24; 15:4; 1 Kor. 9:9-10; 10:6,11). Hii kimsingi ni thiolojia ile ile inayofunuliwa katika 2 Tim. 3:15-17. Matendo ya Mungu (ufunuo) na kuandikwa kwake na fasiri yake (uvuvio) yalikuwa kwa waaminio wa baadaye (unurulishwaji).
Ikiwa Petro alikuwa akiandika zaidi kwa waaminio wa Mataifa, tungo hii ina nyongeza ya ukiri wa kithiolojia ya ujumuishi wa Mataifa jambo ambalo limekuwa mapango wa Mungu (kama vile Mwa. 3:15; Warumi 9-11; Efe. 2:11-3:13).

## MADA MAALUMU: MTAZAMO WA PAULO KUIHUSU SHERIA YA MUSA

Ni nzuri na inatoka kwa Mungu (kama vile Rum. 7:12,16).

A. Si njia ya kuielekea haki na ukubalifu wa Mungu (inaweza hata kuwa laana, kama vile Gal. 3). Tazama Mada Maalumu: Sheria ya Musa na Mkristo.
B. Bado ni mapenzi ya Mungu kwa waaminio kwa sababu ni ufunuo wa Mungu Mwenyewe (mara nyingi Paulo amelinukuu Agano la Kale kuwasadikisha na /au kuwatia moyo waaminio).
C. Waamini wanafahamishwa naAgano la Kale (kama vile Rum. 4:23-24; 15:4; 1 Kor. 10:6,11), lakini hawaokolewi na Agano la Kale (kama vile Matendo 15; Warumi 4; Wagalatia 3; Waebrania). Ina fanya kazi ndani ya utakaso lakini si uthibitisho.
D. Inafanya kazi ndani ya agano jipya ili:
    1. kuonyesha dhambi (kama vile Gal. 3:15-29)
    2. kuwaongoza wanadamu ndani ya jamii waliokombolewa
    3. kumfahamisha Mkristo maamuzi ya kimaadili

Ni mpangilio maalumu unaomulika kithiolojia uliohusiana na Sheria, kutoka katika hali ya kulaaniwa (kama vile Gal. 3:10-13) na badala yake kuwepo baraka za kudumu, jambo ambalo linasababisha tatizo katika kujaribu kuuelewa mtazamo wa Paulo kuihusu Sheria ya Musa. Mwanadamu aliye ndani ya Kristo, James Stewart analionyesha fumbo la fikra na maadiko ya Paulo:
"Kwa kawaida ungetarajia kuwepo kwa mwanadamu anayejiendesha mwenyewe ili kuunda mfumo wa fikra na mafundisho yaliyoimarishwa na kama kitu kisichobadilishwa kama alivyotumia maneno yenye manufaa. Ungetarajia yeye kuulenga usahihi katika kutumia maneno yalioziongoza fikra zake. Ungedai kwamba neno, linapotumiwa na mwandishi wetu katika maana mahususi, linapaswa kuibeba maana hiyo kotekote. Lakini kwa kuangalia muundo huu yakupasa kutomtia moyo Paulo. Matumizi mengi ya maneno yake ni marahisi, si magumu. . . anaandika 'Basi torati ni njema', 'Kwa maana naifurahia sheria ya Mungu kwa utu wa ndani' (kama vile Rum. 7:12,22) lakini ni dhahiri kwamba kipengele kingine cha *nomos* ndicho kinachomfanya kuzungumza hali hii pengine, 'Kristo alitukomboa katika laana ya torati' (kama vile Gal. 3:13)" (uk. 26).

◙**"wale waliowahubiri ninyi Injili"** Hii inaonekana kumaanisha kwamba Petro hakuanzisha makanisa haya yote. Yanaweza kuwa yalikuwa yamekwisha anzishwa na Wayahudi waaminio waliorudi kutoka kwenye Pentekoste (kama vile Mdo. 2), au kwa kuhubiri na Paulo au wainjilisti wengine.

◙**"kwa Roho Mtakatifu aliyetumwa kutoka mbinguni"** Roho Mtakatifu anatajwa katika sehemu kadhaa muhimu katika 1 Petro (kama vile 1 Pet. 1:2,11; 4:14). Tungo hii ilikuwa nahau ya Kiebrania kwa ajili ya kuelezea kwamba zama mpya za haki ambayo ilikuwa ikitoka kwa Mungu, ikiletwa na Roho ilikuwa imekuja kikamilifu (kama vile Mdo. 2).

◙**"Mambo hayo malaika wanatamani kuyachungulia"** Hii kinbayana "kuchungulia ili kuweza kuona" kama katika Yohana 20:5,11. Katika Yakobo 1:25 inafasiriwa "kukaza macho." Hii inarejerea kwa wote malaika waovu na wema (kama vile Efe. 3:10; 1 Kor. 4:9).
Katika Dini ya Kiyahudi malaika walionekana kama wapatanishi kati ya YHWH na Musa pale Mlima Mt. Sinai (kama vile Mdo. 7:53; Gal. 3:19; Ebr. 2:2). Walichukuliwa pia kama wenye wivu juu ya upendo wa Mungu na wenye kuwa makini na wanadamu. Katika Ebr. 1:14 malaika wanaelezewa kama watumishi wa "wale watakao rithi wokovu." Paulo hata anaelezea kwamba Waamini watawahukumu malaika (kama vile 1 Kor. 6:3).

Mungu kipekee alijifunua mwenyewe kwa malaika kupitia kushughulikia kwake ubinadamu ulioanguka (kama vile 1 Kor. 4:9; Efe. 2:7; 3:10).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 PETRO 1:13-16**
**[13] Kwa hiyo vifungeni viuno vya nia zenu, na kuwa na kiasi; mkiitumainia kwa utimilifu ile neema mtakayoletewa katika ufunuo wake Yesu Kristo. [14] Kama watoto wa kutii msijifananishe na tamaa zenu za kwanza za ujinga wenu; [15] bali kama yeye aliyewaita alivyo mtakatifu, ninyi nanyi iweni watakatifu katika mwenendo wenu wote; [16] kwa maana imeandikwa, Mtakuwa watakatifu kwa kuwa mimi ni mtakatifu.**

**1:13 "Kwa hiyo "** Hii (*dio*, kama vile 2 Pet. 1:10,12; 3:14) Inaonesha kwamba maonyo yanayofuata ni matokeo ya mjadala uliopita.

| | |
|---|---|
| **NASB** | **“andaeni nia zenu kwa ajili ya kutenda”** |
| **NKJV** | **“vifungeni viuno vya nia zenu”** |
| **NRSV** | **“andaeni nia zenu kwa ajili ya kutenda”** |
| **TEV** | **“andaeni akili zenu kwa ajili ya kutenda”** |
| **NJB** | **“nia zenu…….tayari kwa kutenda”** |

Hii ni kauli ya kati iliyopita endelevu ya wakati timilifu kama shurutishi. Muundo wake unaashiria kwamba tendo la ug’ag’anizi wa maamuzi binafsi linatakiwa. Hii ilitakiwa kuwa nahau ya Kiebrania, ikimaanisha kibayana" kujifunga na kukaza maarifa." Katika Mashariki ya Karibu ya Kale wote wanawake na wanaume walivaa makanzu. Kwa kufikia miguuni na kuvuta yale makanzu mbele na kuchomekea kwenye mkanda, kanzu lilikuwa kabutula jambao lililoruhusu matendo ya nguvu. Sawasawa na maonyo ya maandalizi kwa ajili ya shughuli za ufahamu inapatikana katika Rm. 12:2; Efe. 4:17,23.

◙**"vifungeni viuno vya nia zenu"** Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopita katika mfululizo wa shurutishi na endelevu iliyotumika pamoja na nguvu ya ushurutishi. Hii sio kuita upole/unyenyekevu bali sitiari kwa ajili ya umakini wa ufahamu na hali ya mkichwa kuwa sawa (kama vile 1 Pet. 4:7; 5:8; 1 The. 5:6,8; 2 Tim. 4:5).

◙**"mkiitumainia kwa utimilifu"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu ambayo inamaanisha kufanya maamuzi g’ag’anizi kutumaini kurudi kwa Kristo kikamilifu. "Tumaini" katika Agano Jipya kunarejerea katika Ujio wa Pili (kama vile Tito 2:13). Tumaini letu limejikita juu ya tabia thabiti na yenye uhakika na matendo ya Utatu wa Mungu (kama vile 1 Pet. 1:2,3-5).

◙**"ile neema mtakayoletewa katika ufunuo wake Yesu Kristo"** Hii ni neema ile ile ambayo kwayo manabii wa Agano la Kale walifanya tafiti makini (kama vile 1 Pet. 1:10). Hii kibayana inaonesha kwamba tumaini la waaminio iko katika tabia na matendo ya Mungu Utatu (kama mvile 1 Pet. 1:2,3-5) na kwamba Neema Yake itadhihirishwa wa kati wa kurudi kwa Yesu (kama vile 1 Yohana 3:2). Wokovu unaelezewa na njeo ya kitenzi cha Kiyunani. Angalia Mada Maalum katika 1 Petro 1:5.

**1:14 "watoto wa kutii"** Hii ni nahau ya Kiebrania juu ya mahusiano ya familia yetu na Mungu Baba na Yesu Mwana (maeklezo kanushi yanapatikana katika Efe. 2:2; 5:6). Waaminio ni warithi pamoja naye kupitia Yeye (kama vile Rum. 8:15-17). Cha kushangaza, watenda dhambi ni sehemu ya familia ya Mungu kwa mwaliko wake na dhabihu ya Yesu.

| | |
|---|---|
| **NASB, NRSV** | **“msienende”** |
| **NKJV** | **“ninyi msienende”** |
| **TEV** | **“msiruhusu maisha yenu yaongozwe”** |
| **NJB** | **“msijiruhusu wenyewe kuongozwa”** |

Hii ni kauli kati ya wakati uliopo au ni kauli tendwa enedelevu kama shurutishi. Kama ilivyo mara kwa mara katika Agano Jipya waamini wanaelezewa kama kuwezeshwa na Mungu au Roho Mtakatifu (sauti irabu tendwa), lakini kuna

uwezekano wa kisarufi kwamba waaminio wanaitwa ili waweze kuishi kabisa katika uhusiano wao mpya na Mungu kupitia nguvu ya Roho Mtakatifu (sauti irabu kati).
Kama wokovu ulivyo agano lenye masharti lililoanzishwa na Mungu lakini pamoja na muitikio wake ulioamriwa wenye majukumu, ndivyo pia maisha ya Mkristo (kama vile 1 Pet. 1:15). Zaidi juu ya misamiati ya Petro inatoka katika barua za Paulo, hapa Rum. 12:2.

◙**"tamaa zenu za kwanza za ujinga wenu"** Hii inarejerea hali ya waaminio wa Mataifa isiyo na maadili ya isiyo na Mungu ya kipagani (kama vile 1 Pet. 4:2-3; Efe. 4:17-19).

**1:15**
**NASB "lakini kama Yeye aliye Mtakatifu aliyewaita"**
**NKJV "lakini kama Yeye aliyewaita alivyo Mtakatifu"**
**NRSV "badala yake, aka yeye aliyewaita alivyo matakatifu"**
**TEV "badala yake,kama Mungu aliyewaita alivyo mtakatifu"**
**NJB "kama mfano wa Aliye Mtakatifu anayetuita"**

Huu ni msisitizo juu ya tabia ya Mungu na uamuzi wa kiutawala (kama vile 1 Pet. 2:9; 5:10). Hakuna awezaye kuja kwa Mungu isipokuwa Roho amemleta (kama vile Yohana 6:44,65). Hii ni njia nyingine ya kithiolojia ya kukataa ukubalifu wa uungu kwa matendo ya mwanadamu (Kama vile Efe. 2:8-9). Kichwa cha habari cha Mahubiri yangu juu ya andiko hili ni "Walio wa Mtakatifu wa watakatifu."

◙**"iweni watakatifu"** Hii ni kauli tendwa shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu (yenye ushahidi). Waamini wameitwa kuwa watakatifu. Mapenzi ya Mungu siku zote yamekuwa kwamba watoto Wake wachukue tabia Yake (kama vile Tito 2:14). Lengo la Ukristo sio tu mbinguni pale tutakapokufa lakini kufanana na Kristo sasa (kama vile Rum. 8:29-30; 2 Kor. 3:18; 7:1; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 2:10; 4:13; 1 The. 3:13; 4:3,7; 5:23). Jukumu la Yesu halikuwa tu juu ya kuondolewa kwa dhambi bali urejesho wa taswira ya Mungu kwa wanadamu walioanguka. Lazima siku zote tushukuru juu ya uhakika wa wokovu ambao unakosa kufanana na Kristo! Injili ni (1) kumualika mtu; (2) ukweli ambao mtu anatakiwa auamini; na (3) maisha ya kumfanya mtu atamani kuishi (kama vile Efe. 4:1; 5:1-2,15; 1 Yohana 1:7; 2:4-6). Kumbuka maneno ya kushangaza ya Yesu katika Mt. 5:20 na 48! Siku zote kuwa makini na ukristo "kuna faida gani kwa ajili yangu". Sisi tumeokolewa ili kutumikia.
Tumeitwa kuwa watakatifu kwa wakati masharti yasiyojulikana. Mungu rehemu kanisa la magharibi lililoshikiliwa na (1) mafanikio; (2) mali; na (3) mahubiri ya afya na mali!

## MADA MAALUMU: UTAKATIFU/ UTAKASO KATIKA AGANO JIPYA

Kitabu cha Agano jipya kinadai kwamba wenye dhambi wanapomgeukia Yesu kwa toba na imani (kama vile Marko 1:15; Matendo 3:16,19; 20:21), huthibitishwa na kutakaswa papo kwa papo. Hii ni nafasi mpya katika Kristo. Haki yake imewekwa ndani yao (kama vile Mwa. 15:6; Warumi 4). Wametangaziwa haki na utakatifu (tendo la ki-Mungu la kumtoa mtu hatiani).

Lakini Agano Jipya pia linawasistiza waamini kuwa katika utakatifu au utakaso. Hii ni nafasi ya kitheolojia katika kazi ya Yesu Kristo iliyomalizika na wito wa kufanana na Kristo katika mtazamo na matendo katika maisha ya kila siku. Kwa kuwa wokovu ni neema ya bure na gharama ya kila kitu cha mtindo wa maisha, hivyo hata hii, ni utakaso.

| Mwitikio wa Awali | Ufanano na Kristo Endelevu |
| --- | --- |
| Matendo 26:18 | Warumu 6:19 |
| Warumi 15:16 | 2 Kor. 7:1 |
| 1 Wakorintho 1:2-3; 6:11 | Waefeso 1:4; 2:10 |
| 2 Wathesalonike 2:13 | 1 Wathesalonike. 3:13; 4:3-4,7; 5:2 |
| Waebrania 2:11; 10:10,14; 13:12 | 1 Timotheo 2:15 |
| 2 Peter 1:2 | 2 Timotheo 2:21 |

1 Petro 1:15-16
Waebrania 12:14

◙**"katika mwenendo wenu wote"** Tazama msisitizo "yote." Changamoto haichaguliwi kwa haki, bali utakatifu unaoenea kote (kama vile 1 Yohana 3:3).

**1:16 "kwa maana imeandikwa, Mtakuwa watakatifu kwa kuwa mimi ni mtakatifu'"** "iliyoandikwa" ni kauli tendwa elekezi ya wakati timilifu, ambayo ni nahau kwa ajili ya maandiko yanayotumika mara kwa mara na Yesu, lakini hapa ni Petro. Hii ni nukuu kutoka Law. 11:44-45; 19:2; 20:7,26. Haya sio mahitaji mapya lakini mahitaji yanayorudiwa (kama vile Mt. 5:48). Utakatifu katika namna ya Agano la Kale waukuwa hali ya kutokuwa na dhambi bali kuendana na matakwa ya agano la Mungu (yaani Kut. 19:6; 22:31; Kumb. 14:2,21; 26:19). Agano Jipya pia lina matakwa ya agano ambayo katika kufanana na Kristo (kama vile Rum. 8:28-29; 2 Kor. 3:18; 7:1; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 4:13; 1 The. 3:13; 4:3,7; 5:23). Angalia Mada hapa chini.

## MADA MAALUMU: TAKATIFU

. Agano la Kale (likielezwa kwa zaidi kutoka Isaya)

A. Asili ya neno *kadosh* (BDB 872, KB 1072) halina uhakika, pengine ni Ki-kanaani (yaani, lugha Magharibi mwa Syria). Inawezekana kwamba sehemu ya mzizi wa neno (yaani, *kd*) unamaanisha "kugawanya."

Hiki ni chanzo cha ufafanuzi unaofahamika wa neno "tengwa (kutoka kwenye utamaduni wa ki- Kanaani, kama vile Kumb. 7:6; 14:2,21; 26:19) kwa matumizi ya Mungu."

B. Inahusiana na uwepo wa Mungu ndani ya vitu, mahali, wakati, na watu. Halitumiki katika kitabu cha Mwanzo, bali linakuwa la kawaida katika vitabu vya Kutoka, Mambo ya Walawi, na Hesabu.

C. Katika fasihi ya Kinabii (hasa Isaya na Hosea) hali ya kibinadamu ilikuwepo hapo awali, lakini haikuhimizwa kwa ajili ya kutenda kazi (tazama Mada Maalumu: Aliye Mtakatifu). Inakuwa njia ya kueleza asili ya Mungu.(kama vile Isa. 6:3). Mungu ni Mtakatifu. Jina Lake linalowakilisha sifa yake ni takatifu. Watu wake ndio wanaopaswa kuifunua sifa Yake kwa ulimwengu unaohitaji utakatifu (ikiwa watalitii agano katika imani).

1. KIVUMISHI, BDB 872 קדוש, "takatifu," "tukufu" linatumika juu ya
   a. Mungu, Isa. 5:16; 6:3 (mara tatu); tazama Mada Maalumu: Aliye Mtakatifu
   b. Jina Lake, Isa. 40:25; 49:7; 57:15
   c. kukaa Kwake ndani, Isa. 57:15
   d. Sabato, Isa. 58:13
2. KITENZI, BDB 872 קדשׁ, "kutengwa mbali," "wekwa wakfu"
   a. sifa ya Mungu, Isa. 5:16; 29:23
   b. Mungu, Isa. 8:13; 65:5
   c. malaika wa Mungu, Isa. 13:3
   d. jina la Mungu, Isa. 29:23
   e. sherehe za kidini, Isa. 30:29
   f. wanadamu walioweka wakfu, Isa. 66:17
3. NOMINO, BDB 871 קדשׁ, "utengwaji," "uwekwaji wakfu"
   a. uzao mtakatifu, Isa. 6:13
   b. mlima mtakatifu, Isa. 11:9; 27:13; 56:7; 57:13; 65:11,25; 66:20
   c. kutengwa, Isa. 23:18
   d. njia ya utakatifu, Isa. 35:8
   e. mahali patakatifu, Isa. 43:28; 62:9; 64:11
   f. mji mtakatifu, Isa. 48:2; 52:1
   g. aliye Mtakatifu, Isa. 49:7 (tazama Mada Maalumu: Aliye Mtakatifu)
   h. mkono mtakatifu, Isa. 52:10
   i. siku takatifu, Isa. 58:13

j. watu watakatifu, Isa. 62:12
k. Roha Mtakatifu, 63:10,11
l. Kiti cha enzi cha Mungu, Isa. 63:15
m. sehemu takatifu, Isa. 63:18
n. miji mitakatifu, Isa. 64:10

D. Huruma ya Mungu na upendo havitenganishwi kutoka katika dhana ya theojia ya maagano,haki, na sifa ya muhimu. Humu ndani pana mvutano wa Mungu dhidi ya utu ulioanguka, usio mtakatifu ,wenye kuasi. Kuna mada inayotia shauku sana kuhusiana na mahuhusiano kati ya Mungu kama "mwenye huruma" na Mungu kama "mtakatifu" katika kitabu cha Robert B. Girdlestone, *Synonyms of the Old Testament*, kr. 112-113.

. Agano Jipya

A. Waandishi wa Agano Jipya (isipokuwa Luka) walikuwa Waebrania wenye fikra pana, lakini waliandika katika lugha ya kawaida ya Koine. Kanisa la Agano Jipya lilitumia fasiri ya Kiyunani kufasiri kitabu cha Agano la Kale. Ilikuwa ni tafasili ya Kiyunani ya Agano la Kale, sio fasihi ya Kiyunani cha daraja la juu, fikra, au dini, iliyodhibiti misamiati yao.

B. Yesu ni mtakatifu kwa kuwa Yeye ni wa Mungu na ni sawa na Mungu (kama vile Luka 1:35; 4:34; Matendo 3:14; 4:27,30; Ufu. 3:7). Yeye ni Mtakatifu na Mwenye Haki (kama vile Matendo 3:14; 22:14). Yesu ni mtakatifu kwa sababu hana dhambi (kama vile Yohana 8:46; 2 Kor. 5:21; Ebr. 4:15; 7:26; 1 Pet. 1:19; 2:22; 1 Yohana 3:5).

C. Kwa kuwa Mungu ni mtakatifu (kama vile Yohana 17:11; 1 Pet. 1:156-16; Ufu. 4:8; 6:10), watoto Wake yawapasa kuwa watakatifu (kama vile Law. 11:44-45; 19:2; 20:7,26; Mt. 5:48; 1 Pet. 1:16). Kwa kuwa Yesu ni mtakatifu, wafuasi Wake yawapasa kuwa watakatifu (kama vile Rum. 8:28-29; 2 Kor. 3:18; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 1 The. 3:13; 4:3; 1 Pet. 1:15). Wakristo wameokolewa ili kutumika katika ufanano wa Kristo (wenye utakatifu).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 PETRO 1:17-21**

**17 Na ikiwa mnamwita Baba, yeye ahukumuye kila mtu pasipo upendeleo, kwa kadiri ya kazi yake, enendeni kwa hofu katika wakati wenu wa kukaa hapa kama wageni. 18 Nanyi mfahamu kwamba mlikombolewa si kwa vitu viharibikavyo, kwa fedha au dhahabu; mpate kutoka katika mwenendo wenu usiofaa mlioupokea kwa baba zenu; 19 bali kwa damu ya thamani, kama ya mwana-kondoo asiye na ila, asiye na waa, yaani, ya Kristo. 20 Naye amejulikana kweli tangu zamani, kabla haijawekwa misingi ya dunia; lakini alifunuliwa mwisho wa zamani kwa ajili yenu; 21 ambao kwa yeye mmekuwa wenye kumwamini Mungu, aliyemfufua katika wafu akampa utukufu; hata imani yenu na tumaini lenu liwe kwa Mungu.**

**1:17 "ikiwa"** Hii ni sentensi ya daraja la kwanza lenye masharti ambayo inadhaniwa kuwa kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au lkwa makusudi ya kifasihi.

◙**"mnamwita Baba"** Hii ni kauli ya kati elekezi ya wakati uliopo (kama vile Hos. 11:1-3; Yer. 3:19), ikimaanisha kwamba waaminio kumuitia YHWH katika masharti ya familia (kama vile Rum. 8:15; Gal. 4:6) kama Yesu alivyofundisha (kama vile Mt. 6:9). Angalia MADA MAALUM: BABA katika Marko 13:32.

◙**"yeye ahukumuye kila mtu pasipo upendeleo"** Mungu atatazama sio wale tu ambao hawajawi kumjua Yeye bali pia wale wanaodai kumjua Yeye (kama vile 1 Pet. 4:5,17-18; Rum. 14:12; 2 Kor. 5:10). Wale ambao wamepewa mengi, vingi vitatakwa kwao (kama vile Luka 12:48)!

Tutakapomuita Baba, basi tuoneshe tabia za kifamilia, kama afanyavyo Mwanawe mkubwa! Baba yetu, Yeye Aliye mtakatifu ni hakimu asiye na upendeleo (kama vile Kumb. 10:17; 2 Nyakati. 19:7; Mdo. 10:34; Rum. 2:11; Gal. 2:6; Efe. 6:9; Kol. 3:25; 1 Pet. 1:17).

Wanadamu wana maamuzi (kama vile Kumb. 30:15-20; Yos. 24:15; Ezek. 18:30-32) katika namna watakavyohusiana na Mungu. Anaweza kuwa baba mwenye upendo ikiwa watamtumaini Kristo (kama vile 1:12; Rum. 10:9-13) au anaweza hakimu mtakatifu ikiwa watategemea kwenye vigezo vyao wenyewe au matendo yao ya kidini, sheria na taratibu (kama vile Mt. 25:31-46; Kol. 2:20-23). Unahitaji Rehema au haki?

Neno "hana upendeleo" inaaksi nahau ya Agano la Kale, "kuinua uso." Hakimu hatakiwi kuathiriwa na anayeshitakiwa bali matendo yao.

◙**"kwa kadiri ya kazi yake"** Haya ni maadili ya kiulimwengu. Mungu ni hakimu. Wanadamu watatoa hesabu kwa Mungu kwa kipawa cha uhai (kama vile Mt. 25:31-46; 2 Kor. 5:10; Ufu. 20:11-15). Sisi ni mawakili na tunavuna kile tulichokipanda (kama vile Ayubu 34:11; Zab. 28:4; 62:12; Mith. 12:14; 24:12; Isa. 3:10-11; Yer. 17:10; Hos. 4:9; Mt. 16:27; 25:31-46; Rum. 2:6; 1 Kor. 3:8; Gal. 6:7; Kol. 3:25; Ufu. 2:23; 20:12-13; 22:12).

◙**"enendeni kwa hofu"** Kuna heshima inayopaswa kwasababu ya Mungu Mtakatifu (kama vile 2 Kor. 5:21). Heshima hiyo ni kwamba watoto Wake waishi maisha matakatifu, wakijua kwamba watatoa hesabu kwa Mungu kwa sababu ya kipawa cha uzima na Injili.

◙**"katika wakati wenu wa kukaa hapa kama wageni"** Hii inarejerea kwa waamini kusafiri katika nchi ya wageni (kama vile 1 Pet. 1:1; 2:11; Ebr. 11:9-10). Ulimwengu sio nyumbani kwetu!

**1:18 "mfahamu"** Maarifa yetu ya kazi ya Kristo aliyoifanya kwa niaba yetu inatusababisha sisi kuishi maisha ya kufanana na Kristo.
Kumekuwepo na madhanio kati ya wafasiri juu ya matumizi ya Petro ya matamko ya mafundisho ya kanisa la kwanza, tenzi au liturujia ya kuabudu. 1 Petro 1:18-21 na 2:21-25 inaonesha ishara ya utaratibu wa ushairi. Paulo pia alitumia matamko haya, tenzi na nyenzo za liturujia au yawezekana hata fasihi ya Katekisimu (kama vile Efe. 5:19; Flp. 2:6-11; Kol. 1:15-16; 3:15-20; 1 Tim. 3:16; 2 Tim. 2:11-13).

◙**"mlikombolewa"** Neno "waliokombolewa" inaaksi neno kila Agano la Kale "kumnunua mtu tena kwa kumrejesha" kutoka katika umasikini na utumwa. Kuna maneno mawili ya kiebrania (fidia, ukombozi). Moja ina nyongeza ya "kununuliwa tena na ndugu wa karibu" (*go'el*, mkombozi wa kiundugu, kama vile Ruthu 4:1,3,6,8,14). Yesu ni ndugu yetu wa karibu aliyenunua msamaha wetu kwa maisha yetu wenyewe (kama vile Isa. 53; Marko 10:45; 2 Kor. 5:21). Angalia MADA MAALUM:FIDIA/KOMBOA katika Marko 10:45.

| | |
|---|---|
| **NASB, NJB** | **"kutoka katika mwenendo wenu usio faa"** |
| **NKJV** | **"kutoka katika mwenendo wetu usiokuwa na lengo"** |
| **NRSV** | **"kutoka katika njia zisizofaa"** |
| **TEV** | **"kutoka katika mienendo ya maisha isiyofaa"** |

Kuna njia mbili za kufasiri tungo hii.

1. inarejerea desturi za Agano la Kale (kama vile Isa. 29:13; Mt. 15:1-20; Marko 7:1-23) na inaaksi neno la Kiebrania "tupu," "isiyokuwa na kitu" au "ukungu" (kama vile Yer. 2:5; Zek. 10:2). Tungo inayofuata inaelezea mfumo wa kidhabihu wa Agano la Kale. Ikiwa hivyo ndivyo, Petro anazungumza kwa Wayahudi waaminio.
2. Inarejerea 1 Pet. 1:14 na kwa kukosa maadili, kipagani, maarifa yaliyopita ya waaminio wa mataifa.

Kwa namna ya jumla ya neno hili angalia Mdo. 14:15; 1 Kor. 15:17; Tito 3:9 na Yakobo 1:26.

**1:19 "kwa damu ya thamani"** Tungo hii ni maelezo ya mfumo wa kutoa dhabihu ya Waisraeli (kama vile Law. 1-7). Mungu kwa neema aliruhusu mwanadamu mwenye dhambi kumkaribia kwa namna ya dhabihu. Dhambi inagharimu uhai. Uzima upo katika damu (kama vile Law. 18:11,14). Mungu aliruhusu mbadala wa maisha/uzima wa mnyama. Yohana mbatizaji alimuita Yesu "Mwana kondoo wa Mungu aondoaye dhambi ya ulimwengu" (kama vile Yohana 1:29). Yesu alitabiri kifo (kama vile Isa. 53:7-8) alishughulikia dhambi ya ulimwengu mzima (kama vile Yohana 3:16,17; 4:42; 1 Yohana 2:2; 4:14).

◙**"asiye na ila, asiye na waa"** Hizi ni sitiari za Agano la Kale kwa ajili dhabihu za wanyama wakubaliwao (kama vile Law. 22:19-20), lakini hapa zinarejerea hali ya Yesu kutokuwa na dhambi (kama vile Yohana 8:46; 14:30; Luka 23:41; 2 Kor. 5:21; Ebr. 4:15; 7:26-27: 1 Pet. 2:22, 3:18, 1 Yohana 3:5). Alikuwa dhabihu takatifu iliyokubalika.

**1:20 "Naye amejulikana"** Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati timilifu. Kazi ya Mungu ya Ukombozi inaelezewa kwa neno hili katika 1 Pet. 1:2. Kifo cha Yesu hakikuwa cha kuwaza na kujifikiria fikiria (kama vile Mwa Gen. 3:15; Zab. 22; Isa. 53; Marko 10:45; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29). Yesu alikuja ili kufa!

◙**"kabla haijawekwa misingi ya dunia"** Tungo hii inatumika mara kadhaa katika Agano Jipya. Inazungumzia shughuli za kuandaa uumbaji wa Mungu kwa ukombozi wa mwanadamu (kama vile Mt. 25:34; Yohana 17:24; Efe. 1:4; 1 Pet. 1:19-20; Ufu. 13:8). Hii pia inamaanisha kuwepo kabla kwanza kwa Yesu (kama vile Yohana 1:1-2, 8:57-58; 2 Kor. 8:9; Flp. 2:6-7; Kol. 1:17; Ufu. 13:8).

◙**"lakini alifunuliwa"** Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati uliopita usio timilifu "Mungu amemfanya Yeye kufunuliwa kwa uwazi" (kama vile Ebr. 9:26; 1 Yohana 1:2; 3:5,8).

◙**"mwisho wa zamani hizi"** Hii inarejerea kuvaa mwili kwa Yesu pale Bethlehemu. Alikuwepo kama Mungu milele yote lakini aliofunuliwa vizuri zaidi kiuwazi kwa muundo wa mwanadamu pale Bethlehemu (kama vile Mika. 5:2). Siku za mwisho zilianza na kuzaliwa kwa Yesu pale alipoingizwa rasmi katika ufalme. Watahitimishwa wakati wa Ujio wa pili. Angalia Mada maalum: Enzi hii na Enzi Ijayo katika 1 Petro 1:5.

◙**"ambao kwa yeye mmekuwa wenye kumwamini Mungu"** Hii kibayana ni "wale. . .waaminio." Kivumishi *pistos* kinatumika kama kiimarishi ("wale waaminio").
Usuli wa neno kuamini (Kiebrania *emeth,* Greek, *pistis*) inasaidia kutengeneza maana ya kisasa. Katika kiebrania kiasili ilirejerea mtu aliye na kusimama thabiti. Ilikuja kutumiwa kisitiari kwa mtu anayetegemewa, mwaminifu au mwenye kutumainika. Neno sawasawa la Kiyunani linafasiriwa katika Kingereza kwa maneno "imani," "kuamini," na "tumaini." Imani ya Kibiblia au tumaini kimsingi sio kitu tunachokifanya bali mtu ambaye tunamtumainia. Ni kule kutumainika kwa Mungu sio kwetu ambako kunakuwa shabaha. Tumaini la wanadamu walioanguka, anaamini Uaminifu Wake, wanaamini katika Mpendwa Wake. Shabaha sio juu ya utoshelevu au kina cha imani ya mwanadamu bali kile kinachokusudiwa katika hiyo imani.

**1:21 "aliyemfufua katika wafu"** Hii inaonesha uthibitisho wa maisha ya Yesu na kifo. Hii ni mada inayojirudia rudia ya Petro (kama vile 2:24-28,32, 3:15,26; 4:10; 5:30; 10:40; 1 Pet. 1:13, 3:18,21, na Paulo, Mdo. 13:30,,33,34,37; 17:31; Rum. 4:24, 8:11; 10:9; 2 Kor. 4:14). Huu ulikuwa uthibitisho wa ukubalifu wa Baba juu ya kifo cha mbadala wa Mwana (kama vile 1 Kor. 15). Kithiolojia nafsi zote tatu za Utatu walikuwa watendajii katika Ufufuo wa Kristo.

1. Baba (Mdo. 2:24; 3:15; 4:10; 5:30; 10:40; 13:30,33,34; 17:31)
2. Roho (Rum. 8:11)
3. Mwana (Yohana 2:19-22; 10:17-18)

◙**"akampa utukufu"** Katika Muktadha wa ukubalifu wa Baba na uthibitisho wa maneno ya mwana na kazi unaelezewa katika matukio makubwa mawili.

1. Ufufuo wa Yesu kutoka kwa Wafu
2. kupaa kwa Yesu kwenye mkono wa kuume wa Baba

Angalia MADA MAALUM: UTUKUFU *(DOXA)* katika Marko 10:37b.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 PETRO 1:22-25**
**[22] Mkiisha kujitakasa roho zenu kwa kuitii kweli, hata kuufikilia upendano wa ndugu usio na unafiki, basi jitahidini kupendana kwa moyo. [23] Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika; kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele. [24] Maana, Mwili wote ni kama majani, Na fahari yake yote ni kama ua la majani. Majani hukauka na ua lake huanguka; [25] Bali Neno la Bwana hudumu hata milele. Na neno hilo ni neno lile jema lililohubiriwa kwenu.**

**1:22 "kwa kuitii"**Utii ni mada ianyojirudia rudia katika sura ya kwanza (kama vile 1 Pet. 1:2,14,22). Inarejerea kupokea injili (yaani kweli, kama vile Yohana 17:17; 2 The. 2:12) na kutembea ndani yake. Kumbuka injili ni (1) a mtu; (2) ukweli

juu ya mtu huyo; na (3) maisha ya mtu huyo. Yesu anaelezea umuhimu wa utii kwa uwazi katika Luka 6:46. Utii ni ushahidi kwamba tumekutana Naye na kubadilishwa na Yeye. Uzima wa milele unatabia zinazoonekana.

◙**"kweli"** Kibayana "kwa kutii kweli," ambayo ni Shamirisho milikishi. Kweli ni tabia ya wote Mungu na watoto Wake. Angalia Mada Maalum: Kweli katika 2 Pet. 1:12.

◙**"kujitakasa roho zenu"** Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati timilifu. Utiifu kwa kweli unaondoa ubinafsi (kama vile Yakobo 4:8; 1 Yohana 3:3). Kujiondoa kiroho hakukufanyi upokee upendo wa Mungu na ukubalifu bali badala yake inauaksi. Huu mchakato wa utakasaji unaanzia na wokovu na kuendelea katika maisha yote (kauli tendaji endelevu ya wakati timilifu). Inapelekea katika upendo wa kweli ya ndugu (kama vile 1 Yohana 4:7-21). Ukristo ni vyote (1) mwitikio wa imani ya mtu mmoja mmoja kwa msaada wa Mungu wa wokovu kupitia Kristo na (2) maarifa ya kijamii ya huduma kwa mwili wa Kristo (kama vile 1 Kor. 12:7). Waaminio wanaelezea upendo wao kwa Mungu kwa kupenda watoto Wake (kama vile Rum. 14:1-15:13). Angalia dokezo kamili juu ya "nafsi" katika 1 Pet. 1:9.

◙**"upendano wa ndugu. . kupendana kwa moyo"** Matumizi ya kwanza ya "upendo" katika tungo hii ipo katika neno ambatani la Kiyunani *philadelphi* (upendano wa kindugu). Ya pili ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu ya kitenzi *agapaō*. Maneno haya (*phileō* na *agapaō*) yalitumika kwa mbadilishano wa maana sawa katika Agano Jipya (kama vile Yohana 5:20 dhidi 3:25 na 16:27 dhidi ya 17:23). Katika baadhi ya vifungu kama Yohana 21:15-17, wanaweza kuelezea vipengele mbali mbali tofauti vya upendo. Kanisa la kwanza walichukua nomino isiyotumika (*agapē*) na kuanza kuitumia kuelezea upendo wa kibinafsi wa kipekee wa Mungu katika Kristo.

**1:23 "Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili"** Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati uliopita usio timilifu. Hii inakuza wazo la kithiolojia kutoka 1 Pet. 1:3. Ni sitiari ya familia itumikayo kuelezea Wakristo kama wajumbe wapya wa familia ya Mungu kupitia imani yao katika Kristo (kama vile Yohana 1:12-13). Ni sawasawa katika maana na ile ya Yohana "kilichozaliwa kutoka juu" katika Yohana 3:3.
Tazama ukweli upendezao unaoelezwa katika kitenzi.

1. njeo ya wakati timilifu = wokovu wetu ulianza wakati uliopita na kuendelea katika hali yake ya sasa
2. sauti irabu = hatukujiokoa wenyewe, lilikuwa ni tendo la nje kwa Mungu wa Utatu
3. Muundo huu huu wa kitenzi (neno tofauti la Kiyunani) linapatikana katika Efe. 2:5,8, ambayo pia ni mstari wa kupendeza ya uhakika wa waamini na usalama.

◙**"si kwa mbegu iharibikayo"** Uzao ni sitiari ya Kibiblia kwa ajili ya (1) kuzaliana (yaani iliyotumiwa na walimu wa Kiyahudi kwa ajili ya mbegu za kiume za uzazi) au (2) kutokea katika mwili (yaani Mwa. 12:1-3 kwa uzao wa Ibrahimu). Ni kile kiletacho uzima.

◙**"kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo"** Kuhubiri injili kunapewa sifa ya kibinadamu kama namna ambayo Baba amewaleta waamini (kama vile Yakobo 1:18). Mahubiri haya ya Kitume ya kweli ya injili inaelezewa vyote kuwa hai na kuendelea kubaki (kama vile Ebr. 4:12), ambavyo vyote ni vipengele vya YHWH!

**1:24** Mistari ya 24-25 ni nukuu kutoka LXX of Isaiahya Isaya 40:6-8 (kama vile Ayubu 14:1-2; Zab. 90:5-6, 103:15-17) ambayo pia inasisitiza udhaifu wa maisha ya mwanadamu (kama vile Yakobo 1:10-11) dhidi ya umilele wa neno la Mungu (kama vile Yakobo 1:21). Katika muktadha wao wa asili mistari hii inarejerea Israeli lakini sasa wanarejerea kwa kanisa (kama vile 1 Pet. 2:5,9). Huu uhamisho ni tabia ya 1 Petro.

**1:25 "Neno la Bwana"** Kuna maneno mawili ya Kiyunani ambayo siku zote yanafasiriwa "neno" au "ujumbe." Katika Uyunani wa Koine *logos* (kama vile Yohana 1:1; 1 Pet. 1:23) na *rēma* (kama vile 1 Pet. 1:25 na kuelezewa katika 1 Pet. 1:25b) siku zote zinafanana. Muktadha sio msamiati unaoashiria ufanano. Mungu amejifunua mwenyewe (yaani ufunuo)!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 PETRO 2:1-3**
**[1] Basi, wekeni mbali uovu wote na hila yote, na unafiki na husuda na masingizio yote. [2] Kama watoto wachanga**

**waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu; [3] ikiwa mmeonja ya kwamba Bwana ni mwenye fadhili.**

**2:1 "Basi"** Hii inaonesha kwamba mjadala unaofuata umejadiliwa juu ya kile ambacho kimetajwa.

◙**"wekeni mbali"** Hii ni kauli kati endelevu ya wakati uliopita usio timilifu "kuvua." Kuvua nguo ni sitiari iliyozoeleka ya Kibiblia ikielezea maisha ya kiroho (kama vile Ayubu 29:14; Zab. 109; 29; Isa. 61:10; Rum. 13:12; Efe. 4:22,25,31; Kol. 3:8; Ebr. 12:1).
Tazama sauti irabu ya kati. Waaminio kwa mara ya kwanza na siku zote (njeo ya kitenzi klilichopita timilifu kama tendo lililotutimilika) kuvua vyote viovu. Hii inawezekana tu kwasababu ya uwasilishaji uliopita wa kithiolojia ya kazi ya Mungu Utatu (kama vile 1 Pet. 1:2). Mwanadamu aliyeanguka haiwezekani kusaidiwa kugeuza kutoka dhambini na uovu lakini Mungu katika Kristo kupitia nRoho amewawezesha waamini kugeuza kikamilifu kuelekea kwa Mungu (kama vile Rum. 6). Tatizo ni kwamba waaminio wanaendelea kuiacha nguvu hii itolewayo na Mungu na kuchagua kurudi katika uovu (kama vile Rum. 7).

◙**"uovu wote"** Hii inarejerea "kunia maovu kwa kutenda" (kama vile Rum. 1:29; 1 Kor. 5:8; 14:20; Efe. 4:31; Kol. 3:8; Tito 3:3; 1 Pet. 2:16). Orodha ya dhambi iliyokuwa imezoeleka katika ulimwengu wa Kirumi (mfano Wastoiki) na Agano Jipya (kama vile Marko 7:21-27; Rum. 1:29-31; 13:13; 1 Kor. 5:10; 6:9-10; 2 Kor. 12:2; Gal. 5:19-20; Efe. 4:31; Kol. 3:8; 1 Tim. 1:9-10; 2 Pet. 2:10-14; Ufu. 21:8, 22:15).

◙**"hila yote"** Neno hili lilitumika juu ya "chambo cha kuvulia." Inaelezea kujaribu kumtega mwingine kwa namna ya ujanjajanja (kama vile 1 Kor. 12:16; 1 The. 2:3; 1 Pet. 2:1,22; 3:10).

◙**"unafiki"** Hii kibayana ni "kuhukumu isivyotakiwa." Ni neno lililotiwa chumvi linalotumika juu ya waigizaji kuzungumza huku wamevaa barakoa.

◙**"husuda"** Huu ni wivu unaosababishwa na shauku ya kuwa na mali ambayo inamilikiwa na mtu mwingine (kama vile Mt. 27:18; Marko 15:10; Rum. 1:29; Flp. 1:15; 1 Tim. 6:4; Tito 3:3; Yakobo 4:5).

◙**"masingizio"** Hii inarejerea kuzungumza uovu juu ya mtu mwingine ili kuwapunguzia umaarufu walio nao (kama vile Rum. 1:30; 2 Kor. 12:20; 1 Pet. 2:1,12; 3:16). Hii ni shughuli inatumika katika vyote Agano la Kale na Agano Jipya kuelezea Shetani. Ni dhahiri kwa kutajwa kwake kwamba ilikuwa tatizo katika makanisa ya haya ya mwanzoni ambayo yalikuwa yanapitia mateso hayo.

**2:2 "kama watoto wachanga waliozaliwa"** Hii yawezekana inahusiana na maonyo ya Yesu kwa Wanafunzi wake kuwa na imani kama watoto (kama vile Mt. 18:3 na kuendelea). Pia inahusiana na sitiari inayojulikana ya kuzaliwa upya (kama vile 1 Pet. 1:3,23; Yohana 3:3).
Katika 1 Petro 2, Petro anatumia sitiari kadhaa kuelezea waaminio.

1. watoto waliozaliwa upya, 1 Pet. 2:1
2. mawe yaliyo hai yakitengeneza nyumba ya kiroho, 1 Pet. 2:5
3. ukuhani, 1 Pet. 2:5,9
4. watu, 1 Pet. 2:9-10
5. wageni na wapitaji, 1 Pet. 2:11
6. kondoo, 1 Pet. 2:25

◙**"yatamanini"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu. Hili ni neno la nguvu kwa ajili ya shauku (kama vile Flp. 1:8; 2:26). Ukuaji wa kiroho na ukomavu hauji moja kwa moja katika maisha ya Mkristo. Umuhimu wa amri hii unaweza kuonekana katika Zab. 42:1-4 na Mt. 5:6.

◙**"yasiyoghoshiwa"** Hili ni neno linalochukuliwa kutoka katika idara ya mvinyo ya karne ya kwanza. Ni neno *dolon* (danganyifu, kama vile 1 Pet. 1:1) ikiwa na kiambishi awali hasi. Mvinyo ulichanganywa na maji haswa mvinyo mku kuu.

Wafanyabiashara mara kwa mara walijaribu kuuza ule uliochanganywa na maji au uliochakachuliwa. Hivyo neno hili lilitumika kisitiari juu ya kile ambacho kilikuwa "hakijachanganywa" au "halisia."
Kwa kuendelea na sitiari ya Wakristo watoto waliozaliwa upya, hii inarejerea kirutubisho cha muhimu cha watoto waliozaliwa, maziwa. Watu hawa waliokolewa kwa neno la Mungu (kama vile 1 Pet. 1:23); sasa wanahitaji kukua katika neno la Mungu. Haya ni matokeo yanayotegemewa na matokeo yanayotarajiwa ya uzao mpya. Oh, tatizo la waamini wanaobakia kuwa Wakristo watoto.

◙**"maziwa"** Tertullian alitoa"waaminio wapya" maziwa na asali baada ya ubatizo wao na ishara ya maisha mapya katika Kristo yaliyojikita katika maandiko haya yenyewe. Tunahitaji kweli ya Mungu ambayo inafunuliwa katika Kristo na mahubiri ya Mitume kwa kuendelea (kama vile Ebr. 5:12).

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV** | **"ya neno"** |
| **NRSV, TEV** | |
| **NJB** | **"kiroho"** |

Hili ni neno la Kifalsafa *logikos* kama katika Rum. 12:1. Inarejerea kuwazua kwa akili (kama vile matoleo ya NASB, NKJV) au kiroho cha kisitiari (kama vile NRSV, TEV, NJB). Kibayana inahusiana na hitaji la waamini wapya la mahubiri ya kimitume na mafundisho (kama vile 1 Pet. 1:23-25). Waaminio wanahitajika kusoma na kuijua Biblia.

◙**"mpate kuukulia wokovu"** Hii ni kauli tendwa yenye dhamira tegemezi ya wakati uliopita tegemezi. Mahubiri ya kitume yanapewa sifa ya kibinadamu kama mwakilishi wa sauti irabu, ambayo inasababisha waaminio kukua.
Wokovu unachukuliwa katika Agano la Jipya kama
1. uamuzi uliopita (njeo ya wakati uliopita usio timilifu)
2. mchakato unaoendelea (njeo ya wakati uliopo)
3. tukio la wakati uliopita linalopelekea hali ya sasa (njeo ya wakati uliopo)
4. uhitimishwaji wa wakati ujao (njeo ya wakati ujao)

Muktadha huu unaelezea kwamba ukuaji wa kiroho kwa namna ya ukweli wa Mungu uliofunuliwa (kama vile 1 Pet. 1:23,25; 2:2) ni muhimu kwa ajili nya uhitimishwaji wa maisha ya Mkristo. Angalia Mada Maaluma katika 1 Pet. 1:5.

**2:3 "ikiwa mmeonja ya kwamba Bwana ni mwenye fadhili"** Hii kauli ya daraja la kwanza lenye masharti ambayo inadhaniwa kuwa kweli. Waaminio waliozoelea neema ya Mungu wanatarajia kutamani kweli ya Mungu katika wokovu kamili na uliokamilika. Mstari wa 3 ni maelezo ya Zab. 34:8. Zaburi inarejerea kwa YHWH, lakini hapa inamrejerea Yesu. Toleo la United Bible Societies *Handbook on the First Letter from Peter* inaelezea kwamba hii inaweza kurejerea kumunio ya kwanza ya mwamini (ukurasa wa 53).
1. mzaha kati ya wemas (*chrēstos*) na Kristo (*Christos*)
2. Zaburi 34 ilitumika na kanisa la kwanza wakati wa huduma za Komunio
3. "onja" (njeo ya wakati uliopita usio timilifu) inarejerea kumunio ya kwanza (yawezekana baada ya ubatizo)

## MASWALI YA MJADALA
Huu ni <u>mwongozo</u> wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uviteleze vitu hivi kwa mfasiri.
Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.
1. Je Petro anawaandikia Wayahudi au Mataifa, au wote wawili?
2. Upi ni ukweli mkuu juu ya maombi ya Petro katika 1 Pet. 1:3-9?
3. Kwanini Wakristo wanateseka?
4. Kwanini wokovu wetu unasemekana bado kuwa katika siku za baadaye?
5. Manabii wa Agano la Kale walitamani kujua nini katika 1 Pet. 1:10-12?
6. Orodhesha amri zinazopatikana katika 1 Pet. 1:13-22.
7. Waamini wanahitaji nini zaidi?

# 1 PETRO 2:4-25

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Jiwe lililohai na Taifa takatifu | Neno lidumulo | Hitaji la Utakatifu | Jiwe lililohai na Taifa Takatifu | kuzaliana kwa Neno |
| | (1:22-2:3) | (1:23-2:10) | | (1:22-2:3) |
| 2:1-8 | Jiwe Teule na Watu Wateule | | 2:1-8 | Ukuhani Mpya |
| | 2:4-10 | 2:4-8 | | 2:4-8 |
| 2:9-10 | | 2:9-10 | 2:9-10 | 2:9-10 |
| Kuishi kama Watumishi wa Mungu | Kuishi kwa kukabili ulimwengu | Jukumu la Wakristo | watumwa wa Mungu | Jukumu la Wakristo kuelekea kwa Wasioamini |
| | | (2:11-4:11) | | |
| 2:11-12 | 2:11-12 | 2:11-12 | 2:11-12 | 2:11-12 |
| | Kuitii serikali | | | Jukumu la Wakristo Kuelekea mamlaka Ya Jamii |
| 2:13-17 | 2:13-17 | 2:13-17 | 2:13-17 | 2:13-17 |
| Mfano wa mateso Ya Kristo | Kutii wenye mamlaka | | mfano wa mateso ya Kristo | Jukumu la Wakristo kwa Mabwana |
| 2:18-25 | 2:18-25 | 2:18-25 | 2:18-25 | 2:18-20<br>2:21-25 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka "Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 PETRO 2:4-8**

**4 Mmwendee yeye, jiwe lililo hai, lililokataliwa na wanadamu, bali kwa Mungu ni teule, lenye heshima. 5 Ninyi**
**nanyi, kama mawe yaliyo hai, mmejengwa mwe nyumba ya Roho, ukuhani mtakatifu, mtoe dhabihu za roho,**
**zinazokubaliwa na Mungu, kwa njia ya Yesu Kristo. 6 Kwa kuwa imeandikwa katika maandiko Tazama, naweka**
**katika Sayuni jiwe kuu la pembeni, teule, lenye heshima, Na kila amwaminiye hatatahayarika. 7 Basi, heshima hii ni**
**kwenu ninyi mnaoamini. Bali kwao wasioamini, Jiwe walilolikataa waashi, Limekuwa jiwe kuu la pembeni. 8 Tena,**
**Jiwe la kujikwaza mguu, na mwamba wa kuangusha, Kwa maana hujikwaza kwa neno lile,wasiliamini,nao waliwekwa kusudi wapate hayo.**

**2:4 "Mmwendee yeye"** Hii ni kauli ya kati ya wakati uliopo (yenye ushahidi) inayoendelea. Matoleo ya NKJV, NRSV na TEV yanafasiri hii kama kauli shurutishi. Tazama kwamba kuendelea kuja kwa kipengele cha kibinafsi, "kwa Yeye." Injili kimsingi ni mtu kualika, kutumaini na kuiga kufanana. Neno hili linaweza likawa na ufanano wa kumjongea Mungu kama kuhani au mwabudu (kama vile Ebr. 4:16; 7:25; 10:1, 22; 11:6). Petro anabadilisha sitiari yake kutoka maziwa katika 1 Pet. 2:2-3, kujenga sitiari katika 1 Pet. 2:4-8 (waamini kama mawe yaliyo hai na Yesu kama jiwe la pembeni). Hii yawezekana kuwa maelezo ya kuendelea kwa Zab. 34:4 kutoka katika Tafsiri ya agano la Kale la Kiyunani.

◙**"jiwe lililo hai"** Katika Agano la Kale, uhistahimilivu, uimara, nguvu mara kwa mara vinaelezewa kwa kutumia mifano ya mwamba kama jina (kama vile Kumb. 32:4,15,18,30; Zab. 18:2,31,46; 28:1; 31:3; 42:9; 71:3). Sitiari ya Yesu kama jiwe linapatikana katika

1. jiwe lililokataliwa (Zab. 118:22)
2. jiwe la kujengea (Zab. 118:22; Isa. 28:16)
3. jiwe la kujikwalia (Isa. 8:14-15)
4. jiwe la ushindi na kiutawala (ufalme), (Dan. 2:45)

Yesu alituma vifungu hivi kujielezea mwenyewe (kama vile Mt. 21:40; Marko 12:10; Luka 20:17).

◙**"lililokataliwa na wanadamu"** Hii ni kauli tendwa ya wakati timilifu endelevu. Hii inaweza kuwa maelezo kwa 1 Pet. 2:7, ambalo inatoka Tafsiri ya Agano la kale la Kiyunani la Zab. 118:22. Jiwe linadharauliwa na "wajenzi," ambayo inaweza kurejerea uongozi wa Kiyahudi lakini katika Petro inapanuliwa kwa wanadamu wasioamini. Neno hili kutoka *apo* na *dokimazō*, inamaanisha kumjaribu mtu au kitu ili kujua kama ni halisi. Wayahudi waliendelea kumkataa Yesu kama Masihi na kukataliwa huku kukawa hali ya upofu wa kiroho (kama vile Marko 8:31; Mt. 6:23).

◙**"bali kwa Mungu ni teule, lenye heshima"** Huu ni ulinganifu wa moja kwa moja na tungo iliyotangulia. Neno "kuchagua" kibayana imaaanisha "kufanya maamuzi kati ya vingi " kwa maana ya "kuwekwa wakfu kabla" (kama vile 1 Pet. 1:2,20). Masihi aliyekataliwa (aliyesulubiwa au ambaye hajapokelewa) amekuwa siku zote mpango pekee wa Mungu wa ukombozi (kama vile Luka 22:22; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29; Efe. 1:11).

**2:5 "kama mawe yaliyo hai"** Agano Jipya linatumia sitiari kadhaa za muunganiko za upamoja kuelezea kanisa.

1. mvinyo (Yohana 15:5)
2. mifugo (Yohana 10:16)
3. bibi harusi (yaani familia, kama vile Efe. 5:27; Ufu. 19:7, 21:9)
4. mwili (Efe. 1:22-23, 1 Kor. 12)
5. familia (Rum. 8:15-17; 1 Tim. 3:15)
6. mji (Ebr. 11:10,16; 12:22, 13:14; Ufu. 2:2,10)
7. hapa, hekalu (kama vile 1 Kor. 3:9,16; 6:19)

◙**"mmejengwa mwe nyumba ya Roho"** Hii yawezekana kuwa kauli tendwa elekezi ya wakati uliopo ingawa kwa namna kwamba iwe kauli tendwa shurutishi ya wakati uliopo. Hiki ni kitenzi kilekile kilichotumika katika Mt. 16:18 kuelezea kanisa kujengwa juu ya mwamba wa imani binafsi (yaani Petro kama mfano). Muktadha mzima unaendelea kukuza sitiari ya 1 Pet. 2:4. Yesu ni hekalu Jipya (kama vile Yohana 2:18-22). Waamini katika Kristo ni makuhani kamili. Wayahudi wasioamini wamejikwaa (kama vile 1 Pet. 2:7-8) mawe halisia ambayo YHWH amejenga juu yake hekalu lake la Kiroho—(1) Yesu na (2) kanisa (kama vile 1 Tim. 3:15). Ni wale tu wenye imani katika Kristo wanaoweza kufanya kazi katika hekalu la Mungu la kiroho, wanaojitoa dhabihu inayokubalika kiroho (yaani maisha matakatifu ya kujitoa, kama vile 1 Pet. 1:14-16; Rum. 12:1-2).

## MADA MAALUM: KUADILISHA

Neno hili *oikodomeō* na muundo wa maneno yake mengine yanatumiwa mara kwa mara na Paulo. Kidhahiri lilimaanisha "kujenga nyumba" (kama vile Mt. 7:24), lakini lilikuja kutumika kisitiari kwa:

1. Mwili wa Kristo, kanisa, 1 Kor. 3:9; Efe. 2:21; 4:16
2. Kujenga
   a. ndugu wadhaifu, Rum. 15:1
   b. majirani, Rum. 15:2
   c. ninyi kwa ninyi, Efe. 4:29; 1 Wathesalonike 5:11
   d. watakatifu kwa ajili ya huduma, Efe. 4:11
3. tunajenga au kuonya kwa
   a. upendo, 1 Kor. 8:1; Efe. 4:16
   b. kuweka mipaka juu ya uhuru binafsi, 1 Kor. 10:23-24
   c. kukwepa kudhaniwa, 1 Tim. 1:4
   d. kuweka mipaka ya wazungumzaji katika huduma za kuabudu (waimbaji, walimu, manabii, wanenaji kwa lugha, na wakalimani), 1 Kor. 14:3-4,12
4. vitu vyote sharti vionywe
   a. mamlaka ya Paulo, 2 Kor. 10:8; 12:19; 13:10
   b. kauli za kimutahsari katika Rum. 14:19 na 1 Kor. 14:26

◙**"kwa ajili ya ukuhani mtakatifu"** Petro anatumia majina ya watu wa Mungu wa Agano la Kale (kama vile Kutoka 19:5; 1 Pet. 2:9-10; Ufu. 1:6). Katika Agano la Kale YHWH aliahaidi kupitia uzao wa Hawa kuwakomboa wanadamu wote (kama vile Mwanzo 3:15). YHWH alimuita Abramu (kama vile Mwa. 12:1-3) kuita ufalme wa makuhani (kama vile Kutoka 19:5-6) kufikia ulimwengu wote (kama vile Mwa. 12:3 na Kutoka.19:5). Israeli alishindwa katika jukumu hili (kama vile Ezek. 36:27-38). Hivyo Mungu aliteua waumini wapya wa imani (kama vile Yer. 31:31-34; Ezek. 36:22-38) kufikia ulimwengu (kama vile Mt. 28:19-20; Luka 24:47 Mdo. 1:8; 1 Pet. 2:9).

Martin Luther alitumia mamlaka ya Biblia na ukweli wa Paulo wa kuhesabiwa haki kupitia imnai kukataa desturi za kanisa Katoliki. Alitengeneza tungo "ukuhani wa waamini" (umoja). Ubinafsi wa kimagharibi umechukua kauli mbiu hii na kibadili kuwa kibali kwa uhuru wa binafsi katika imani na mtindo wa maisha. Lakini dhana hii ni jumuishi ya umoja na sio ya kibinafsi (yaani tazama viwakilishi vya wingi katika 1 Pet. 2:5,7,9). Ni yenye mlengo na shabaha ya kutangaza injili, sio wenye shabaha ya uhuru binafsi. Waamini wamepwa jukumu la kiulimwengu la uinjilisti wa Israeli (kama vile Rum. 15:16; Ebr. 13:15-16). Kutazama ukuhani kama maana kwamba tuna kibali cha moja kwa moja kwa Mungu kupitia Kristo ni kweli, lakini hili si kusudi la sitiari. Kuhani anasimama kati ya watu wenye uhitaji na Mungu mtakatifu. Anakuwa wakili wa nafasi yake mwenyewe na mahitaji ya watu. Agano Jipya linakiri ukuhani wa waamini (wingi, jamii moja) wanapowaleta waliopotea kwa imani katika Kristo.

## MADA MAALUM: UKRISTO NI JAMII MOJA

A. Matumizi ya wingi wa sitiari ya Paulo na Petro kwa watu wa Mungu
   1. Mwili (kama vile. 1 Kor. 12:12-20)
   2. Shamba (kama vile. 1 Kor. 3:9)
   3. jengo (kama vile 1 Pet. 2:4-5)

B. Neno "mtakatifu" kila wakati ni WINGI (isipokuwa Flp. 4:21, lakini hata pale pia ni kundi)

C. Msisitizo wa matengezo wa Martin Luther kuhusu "ukuhani wa aaminiye" (yaani, uwezo wa nafsi) ni kuchukulia jambo kibiblia. Kiuhalisia Biblia husema juu ya "ukuhani wa waaminio" (kama vile Kut. 19:6; 1 Pet. 2:5,9; Ufu. 1:6).

D. Kila aaminiye amejaliwa kipawa kwa manufaa ya wote (kama vile 1 Kor. 12:7)

E. Ni katika kushirikiana tu ndipo watu wa Mungu wanaweza kupata matokeo. Huduma ni kushirikiana pamoja (kama vile. Efe. 4:11-12).

◙"**mtoe dhabihu za roho"** Baada ya uharibifu wa hekalu mnamo mwaka 70, Wayahudi waliweka msisitizo wa vifungu vya Agano la Kale ambalo linahamasisha dhabihu zisizokua za wanama (kama vile Zab 50:14, 51:27, 69:30-31, 107:22, 141:2; Hos. 14:2). Waebrania 13:5 inaaksi aina hii ya dhabihu za Kikristo. Katika Muktadha hii inarejerea kwa waamini kuishi maisha matakatifu na maisha ya kujititoa kutoka 1 Petro 1 (haswa 1 Pet. 2:14-16; Ebr. 13:15-16).

**2:6 "jiwe kuu la pembeni, teule, lenye heshima"** Hii ni nukuu kutoka Isa. 28:16. Dhana hii ya Masihi kama mwamba au jiwe inajirudia rudia katika Agano la Kale (kama vile Zab. 118:22; Dan. 2:34-35; Isa. 8:14, 28:16). Vifungu hivi vya agano la Kale mara kwa mara vinanukuliwa katika Agano Jipya (kama vile Mt. 21:42; Marko 12:10; Luka 20:17; 1 Kor. 10:4; Efe. 2:22; 1 Pet. 2:6-8) kurejerea Yesu kama Yule Aliyehaidiwa na Mungu. Petro pia aliitumia katika mahubiri Yake katika Mdo. 4:11. Angalia dokezo katika 1 Pet. 2:4b. Angalia Mada Maalum: Jiwe la Pembeni katika Marko 12:10.

**NASB** **"na wale waaminio katika Yeye hawatahayarika"**
**NKJV** **"na yeye aaminiye katika yeye kwa namna zote hataaibishwa"**
**NRSV** **"na yoyote aaminiye katika Yeye hataaibishwa"**
**TEV** **"yoyote aaminiye katika Yeye hatatahayarika"**
**NJB** **"hakuna amtegemeaye atakayeaibishwa"**

Tungo hii inatoka toleo la LXX la Isa. 28:16. Tazama mwaliko upo wazi kwa wote (kama vile Yohana 1:12; 3:16; Rum. 10:9-13; 1 Tim. 2:4; 2 Pet. 3:9). Huu ni ukanusi wa mara mbili, "kamwe, hapana kamwe, kukata tamaa" au "kuona haya." Kwa"waamini" angalia Mada Maalumu katika Marko 1:15.
F. F. Bruce, *answers to Questions* (ukurasa wa 158) inaelekeza tofauti kati Tafsiri ya Agano la Kale la Kiebrania na maandiko ya Masoteriki.

1. Toleo la LXX – "hatakatishwa tamaa" (NASB) au "kuabishwa" (NJB) ni kitenzi *yēbōsh*
2. Toleo la MT – "hatabughudhiwa" (NASB, pambizo), "kwa haraka" ni kitenzi *yahish*

Katika ukurasa wa 157 Bruce anatoa maoni kwamba waandishi wa Agano Jipya yawezekana walinukuu toleo katika matumizi ya kawaida katika kanisa la kwanza kama isingekuwa kwamba wana sababu maalumu ya kithiolojia kujitoa kwake na kutumia ingine. Msukumo wa jumla wa kifungu ni ufunguo kwa dhana ya uvuvio, sio mapigano juu ya mwingine na kwa maneno ya mtu binafsi. Wanadamu wamepewa ufunuo wa kuaminika!

**2:7 "waashi"** Toleo la Kiyahudi la Targums (fasiri ya kiaramu pamoja na tafsiri) inatumia neno hili kwa ajili ya walimu. Hii ni nukuu ya Zab. 118:22. Yesu anatumia nukuu ile ile ya Agano la Kale katika mifano Yake ya mpangaji mkulima katika Mt. 21:42. Mfano huu ulielezea uongozi wa Kiyahudi wa siku za Yesu. Haijulikani ikiwa maneno mazito ya Yesu ya hukumu yakihusiana na (1) Kukataa kwake dhana ya uongozi wa Kiyahudi usiokuwa wa Haruni (yaani Ana na Kayafa) walionunua nafasi zao kutoka Rumi au (2) Kukataa kwake watu wote wa Kiyahudi (yaani Israeli) ambaye alikataa kuamini katika Yeye (kama vile Rum. 9-11).

**2:8 "Tena, Jiwe la kujikwaza mguu, na mwamba wa kuangusha"** Hii ni nukuu kutoka Isa. 8:14. Pia inanukuliwa katika Rum. 9:32, ambapo inarejerea kwa Yesu. Jiwe maalumu lililokataliwa na kufanyika chombo cha uharibifu!

◙**"wao wasiotii"** Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo. Wao (wasioamini wa nyakati za Petro, wote Wayahudi na Mataifa) wanaendelea kuwa wasiotii kwasababu walimkataa Yesu kama Masihi Mtesekaji. Walikataa vyote mahubiri ya Yesu na yale ya Mitume Wake (kama vile 1 Pet. 1:24,25). Walikataa neno la milee yaani Injili, kama vile. 1 Pet. 1:22-2:2).

**NASB** **"na kwa mwisho huu waliteuliwa"**
**NKJV** **"kwa hayo pia waliteuliwa"**
**NRSV** **"nao waliwekwa kusudi wapate hayo"**
**TEV** **"hayo yalikuwa mapenzi ya Mungu kwao"**

Wafuasi wa Calvin walitumia mstari huu na Rum. 9:22; 1 The. 5:9 kuelezea kwamba Mungu alichagua baadhi kwa ajili ya wokovu na baadhi kwa ajili ya hukumu. Hata hivyo mistari kama Yohana 3:16; 1 Tim. 2:4; 2 Pet. 3:9 inaonesha kwamba hii haiwezi kuwa kweli. Uchaguzi wa Mungu kimsingi kwa ajili ya Utakatifu (kama vile Efe. 1:4; 2:10); kwa ajii ya kufanana na Kristo (kama vile Rum. 8:29).

Mstari huu unanikumbusha juu ya Isa. 6:9-13. Watu wa Mungu wa kiagano walikuwa na ufahamu wao waliouhitaji kuitikia sawasawa kwake lakini hawakufanya hivyo. Huku kukataa kunakoendelea kunakotolewa kwa mioyo migumu. Hukumu tu ndio iliyokuwa inawezekana. Mungu wa nyakati na Historia anajua kile kile wanadamu watakachokifanya lakini anawaruhusu wakifanye na alafu anakiri na kutambua matokeo ya maamuzi yao ya muda mfupi na ya milele. Lazima ilikuwa vigumu sana kwa waamini hawa wa Kiyahudi kushughulikia kumkataa kwao Yesu. Hii ingetokeaje? Hawa waamini wa kwanza walianza kusoma Maandiko kwa muhtasari kwa hali yao hii ya kutoamini.

1. Isaya 6:9-10; 8:14-15; 43:8
2. Yeremia 5:21; 7
3. Mt. 21:33-44; Marko 12:1-12
4. Luka 2:34; 20:9-18
5. Warumi 9-11
6. 1 Wakorintho 1:23

Nukuu ifuatayo ni kutoka F. F. Bruce, *Answers to Questions*, kur. 196-197, kuhusu "uchaguzi" dhidi ya "uteuzi." *"Are 'election to salvation' and 'election to damnation' correlative terms?*

"Katika mifumo fulan ya kithiolojia wana, lakini ni muhimu kujaribu mifumo yote ya kithiolojia kwa maandiko na kukumbuka kwamba wakati mafundisho ya maandiko yanaundiwa mfumo kitu fulani huwa kinaachwa nje ya mchakato. Neno 'uchaguzi' sasa umefanyika jumuishi sana katika utata wa kithiolojia kwamba namna ya mafundisho ya Kibiblia juu ya somo inaweza kueleweka vizuri ikiwa tutatumia neno linalotaka kutofanana na la kithiolojia 'uteuzi' katika nafasi yake. Kristo aliwateuwa wanaume kumi na mbili kuwa mitume (Luka 6:13); Aliteuwa Sauli wa Tarso kuwa 'chombo kiteule' (Mdo. 9:15); lakini uteuzi wake wa wanaume hawa kwa ajili ya kusudi maalumu inamaanisha hakukuwa na kutokufaaa kwa wale ambao hawakuchaguliwa. Mungu aliteuwa Israeli kati ya mataifa (Mdo. 13:17)—kwa ajili ya faida kuu ya mataifa mengine, sio kwa ajili ya hasara. Wakati uteuzi wa watu wa Mungu katika kizazi hiki uko katika maswali, sio sana juu ya 'uteuzi kwa ajili ya wokovu' kama ambavyo uteuzi wao wa utakatifu unavyotiliwa mkazo.

Hii iko hivyo kwa mfano, katika Efe. 1:4 na 1 Pet. 1:1f; na hivyo hivyo, katika Rum. 8:29, Kusudi ambalo Mungu aliwateuwa kabla wale ambao aliwajua tangu ilikuwa ni ili waje kuwa 'wafanane na sura ya Mwana wake.' Hakuna hata moja ya sehemu zote hizi kuna pendekezo la 'kuteuliwa ili kuhukumiwa' ina endana. Lazima tuwe makini kwa kuweka kiujumla kutoka kwa aina hizo za rejea katika Rum. 9:22 ('vyombo vya ghadhabu vilivyotengenezwa kwa ajili ya uharibifu') na 1 Pet. 2:8 'walijikwaa kwasababu hawakulitii neno, kama walivyokuwa wamekusudiwa kufanya'). Mfano wa jumla wa mafundisho ya kibiblia juu ya somo hili unaonesha kwamba baadhi wanachaguliwa au kuteuliwa na Mungu—sio kwa kusudi kwamba wengine, kuacha wao, waache katika adhabu ya jehanamu bali wengine kupitia wao waweze kubarikiwa."

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 PETRO 2:9-10**
**[9] Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu; [10] ninyi mliokuwa kwanza si taifa, bali sasa ni taifa la Mungu; mliokuwa hamkupata rehema, bali sasa mmepata rehema.**

**2:9 "But you bali ninyi"** Tazama wingi "ninyi" na ulinganifu wake. Mwandishi anatumia maelezo yaliyounganishwa kutoka Kutoka. 19:6 na alafu 19:5.

◙**"mzao mteule"** Maelezo haya haya yanapatikana katika Kumb. 7:6; 10:15; Isa. 43:20-21. Kuchaguliwa kwa ajili ya huduma! Hili ni jina la Agano la Kale kwa kuchagua watumishi.

◙**"ukuhani wa kifalme"** Jina hili linapatikana katika Kutoka. 19:6; Isa. 61:6; 66:21. Kama Israeli ilivyochaguliwa ili kuleta ufahamu wa YHWH kwa ulimwengu, sasa kanisa linaitwa kutoa taarifa na kuleta wahitaji, wenye dhambi kwa YHWH.

◙**"taifa takatifu"** Jina hili hili linapatikana katika.19:6; Kumb. 7:6; 14:2,21; 26:19. Israeli iliitwa kwa upekee kuwa takatifu na hivyo kumfunua Mungu Mtakatifu (kama vile Mt. 5:48; 1 Pet. 1:15-16) kwa ulimwengu ulioanguka.

◙**"watu wa milki ya Mungu"** Jina la maelezo haya haya linapatikana katika Kutoka.19:5; Kumb. 4:20; 7:6; 14:2; 26:18; Mal. 3:17. Kifungu hiki kinazungumzia kanisa kama Israeli ya kiroho (kama vile Gal. 6:16). Majina haya ya Agano la Kale kwa ajili ya watu wa Mungu sasa yanafanyiwa kazi na Mwili wa Kristo wa Agano Jipya (kama vile Rum. 2:28-29: Gal. 3;29, 6:16; Efe. 2:11-3:13; Ufu 1:6). Kwa namna fulani kanisa limechukua nafasi ya Israeli katika jukumu la kimisheni kwa ulimwengu (kama vile Mt. 28:19-20; Luka 24:47; Mdo. 1:8).

◙**"mpate kuzitangaza fadhili zake yeye"** Kusudi la Watu wa Mungu ni kushuhudia ukuu wa Mungu mmoja, muumbaji na Mkombozi! Wanachaguliwa na kuwezeshwa kuishi na kuzungumza Injili.

◙**"aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu"** Giza na nuru ni sitiari za kibiblia za dhambi, uasi, na maovu dhidi ya tumaini, uponyaji na wema (kama vile Yohana 1:4-5; 3:19-21; 8:12; 12:35-36,46; Mdo. 26:18; 2 Kor. 4:6; 1 Yohana 1:5; 2:8-9.11). Kama tungo iliyopita yaweza kuwa maelezo kwa Isa. 42:12, tungo hii inaweza kuelezewa na Isa. 42:16.

**2:10 "ninyi mliokuwa kwanza si taifa"** Hii inatambulisha nukuu kutoka Hos. 1:10 na 2:23. Neno la msingi ni *lo ammi* (jina la mmoja wa watoto wa Hosea), ambalo kwa asili linarejerea kwa Israeli kutokuwa watu wa Mungu kwasababu ya kuabudu kwao sanamu mna maisha yao ya kuvunja maangano. Walikuwa (1) wakitumainia muunganiko wa kisiasa na sio katika Mungu (2) waabudu Baali kwa kutumia jina la YHWH.

◙**"bali sasa ni taifa la Mungu"** Hii ni nukuu zaidi kutoka Hos. 2:23. Hiki kifungu katika muktadha wa Agano la Kale inathibitisha kwamba japo Israeli ilikuwa imetenda dhambi na kujitoa mbali na Mungu wao wa Agano, alikuwa tayari kulianzisha upya kwa kuwaweka katika nafasi ya agano (yaani sitiari ya ndoa). Mungu huyuhuyu mwenye upendo na mwenye kusamehe sasa anatoa mkono wake na kuunyoosha kufikia mataifa.
Huku kumtumia Hosea ambako kiasili kunazungumzia nji ya ufalme wa kaskazini ya Israeli katika karne ya nane K.K sasa kunatumiwa na Petro kuhusianisha na Mataifa ya Kipagani. Upanuzi huu wa maandiko ya Agano la Kale kutoka kwa muktadha wa Kiyahudi/Mataifa unatengeneza tabia ya Agano Jipya! Mataifa waaminio sasa wanajumuishwa katika watu wa agano wa Mungu (kama vile Efe. 2:11-3:13).

◙**"mliokuwa hamkupata rehema"** Nabii Hosea alikuwa na watoto watatu ambao aliwapa majina ya kinabii

1. mvulana aliyeitwa *Jezreel*, ikiwa na maana ya "Mungu hufanya faida"
2. binti aliyeitwa *Lo-Ruhamah*, ikiwa na maana ya "bila huruma"
3. kijana aliyeitwa *Lo-Ammi*, ikiwa na maana "sio watu wangu"

Kama sehemu ya kwanza ya 1 Pet. 2:10 anatumia jina la mtoto wa tatu, sehemu ya mwisho ya 1 Pet. 2:10 inatumia jina la mtoto wa pili (kama vile Hos. 1:6; 2:20,23). Mungu kikamilifu anapokea wenye dhambi kwasababu anayo huruma juu yao. Miundo ya kisarufi inapatikana katika 1 Pet. 2:10 ni ya msaada katika kuelezea jambo la kithiolojia. Kulikuwa na katazo lililotamkwa juu ya sehemu ya Mataifa ikiletwa na uwakala wa shetani (yaani kauli tendwa ya wakati timilifu endelevu), lakini Mungu wa Agano kwa kujizatiti ameingia katika historia kwa namna ya Masihi wake na kuleta siku mpya ya fursa kwa ujumuishi wa agano (yaani kauli tendwa ya wakati uliopita usio timilifu unaoendelea). Kweli hii ni sawasawa na siri ya mpango wa Mungu, iliyokuwa hapo mwanzo imefichwa bali sasa imefunguliwa (kama vile Efe. 2:11-3:13).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 PETRO 2:11-12**
**[11] Wapenzi, nawasihi kama wapitaji na wasafiri, ziepukeni tamaa za mwili zipiganazo na roho. [12] Mwe na mwenendo mzuri kati ya Mataifa, ili, iwapo huwasingizia kuwa watenda mabaya, wayatazamapo matendo yenu mazuri, wamtukuze Mungu siku ya kujiliwa.**

**2:11 "wapitaji"** Neno hili la Agano la Kale linazungumzia wasio wakazi wakiwa na haki zenye ukomo wakiishi katika mahali ambapo si nyumbani kwao (kama vile Mwanzo 23:4; Zab. 39:12; Ebr. 11:13; 1 Pet. 2:11). Hapa inatumika kisitiari kwa waamini waishio katika mfumo wa ulimwengu ulioanguka.

◙**"wasafiri"** Neno hili linamaanisha kukaa kwa muda mfupi (kama vile 1 Pet. 1:1,17). Hii inaelezea ukweli kwamba waamini ni raia wa ulimwengu wa roho, sio katika uhalisia wa mwili huu wa muda tu. Sisi ni viumbe wenye miili na nyama (kama vile Mwa. 1:26-27).

◙**"ziepukeni"** Hii kibayana "kuendelea kujizuia mwenyewe katika" (yaani tungo jina ya kati ya wakati uliopo). Waamini lazima waendelee kushughulikia dhambi majaribu (kama vile Warumi 7). Vita dhidi ya uovu haviishii katika wokovu (kama vile Efe 6:10-20). Kwa namna nyingi inaelezea kiundani. Mtu anapoamini na kumpokea Kristo, hukaliwa ndani na Roho (kama vile Rum. 8:9) na kupewa asili ya uungu (kama vile 2 Pet. 1:4). Hatahivyo hii haimaanishi asili ya dhambi ya kale inaondolewa. Inafanya kuzimwa na kazi iliyokwisha ya Kristo kwa niaba yetu (kama vile Warumi 6, angalia Mada Maalumu: Bila kitu na Tupu).
Walimu wanasema kwamba katika kila moyo wa mwanadamu kuna mbwa mweusi na mweupe. Yule unayemlisha zaidi ndiye anayezidi kua mkubwa. Waamini wanakabiliana na maamuzi yakuendelea ya kutafuta mazuri, kuka katika haki, kutembea katika nuru au kuamsha asili ya dhambi ya zamani (kuanguka kwa asili ya mwanadamu na Roho, kama vile Rum. 8:5-17); zama mbili (yaani kizazi cha sasa cha uovu na kizazi cha haki, kama vile Tito 2:11-14); Ipi inayoweka nguvu ya ushawishi zaidi?

◙**"tamaa za mwili"** Mwili wenyewe si muovu (fikra ya Kiyunani), bali ni uwanja wa majaribu ya ubinafsi na majaribu ya kishetani (kama vile Warumi 6-8; Gal. 5:16-24).

◙**"zipiganazo"** Hii ni kauli elekezi ya kati ya wakati uliopo. Vita hivi vinaelezewa katika Yakobo 4:1-4.

**2:12 "Mwe na mwenendo mzuri kati ya Mataifa"** Hii ni kauli tendaji endelevu ya wati uliopo iliyotumika kama shurutishi. Wasio amini wanatazama! Namna gani waamini wanaishi na kuitikia kwa shughuli za kawaida za maisha ni mashahidi wapigao sauti kwa wale wote wawajuao. Mara kwa mara maisha yetu huzungumza zaidi kuliko maneno yetu!

◙ **"huwasingizia kuwa watenda mabaya"** Wakristo wa kwanza walishutumia kwa

1. ulaji wa nyama (kwasababu ya maneno ya Karamu ya Bwana)
2. kujamiiana kwa maharimu (kwasababu walipendana sana)
3. upagani (kwasababu Mungu wao hakuwa anaonekana)
4. usaliti (kwasababu wasingeweza kutumika katika jeshi au kuwa waaminifu wapya kwa Kaisari )
5. mmomonyoko wa maadili (yawezekana kwa busu takatifu)

Huku kutoka katika Njia (kama vile 1 Pet. 24:14; Mdo. 28:22) kunaonekana kuwa kumeanzia na kukua katika majimbo ya mashariki mwa kabala ya Mfalme au Ufalme wa Rumi (Asia Ndogo).

◙**"wayatazamapo matendo yenu mazuri, wamtukuze Mungu"** Namna tunavyoishi kama Wakristo inaaksi Mungu tunayedai kumjua na kumtumikia (kama vile 1 Pet. 2:15; 3:16; Mt. 5:16; Flp. 2:15; Tito 2:7-8). Dhamira tegemezi inatambulisha tukio la uwezekano usiotajwa bado. Utukufu wa Mungu ni wito wetu wa hali ya juu sana na jukumu la kiuinjilisti (kama vile 1 Pet. 4:11,16).

◙**"siku ya kujiliwa"** Hii inamaansiaha kwa muda wowote ambao Mungu anatusogelea, aidha kwa Baraka au kwa ajili ya hukumu (kama vile Isa. 10:3; Yer. 8:12; 10:15; 11:23; 23:12; 46:21; 48:44; 50:27; 51:18; Hos. 9:7; Mik. 7:4). Inaweza kuwa ya muda au ya mtukio ya siku za mwisho (kama vile Luka 19:44). Baadhi wanaiona hii kama kuhusiana na waamini walio katika majaribio lakini katika muktadha inamaanisha fursa yoyote kwa ajili ya wasiookoka bado kusikia na kuitikia Yesu kama Mwokozi kabla hawajakutana naye kama Hakimu.

## AINISHO LA KIMUTAHSARI LA SEHEMU YA VITENDO YA 1 PETRO

A. kutii mamlaka na jamii (1 Pet. 2:13-17)

B. kutii mabwana wa duniani (1 Pet. 2:18-25)
C. kutii katika nyumba ya Mkristo (1 Pet. 3:1-7)
D. kutii katikati ya dhiki (1 Pet. 3:8-22)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 PETRO 2:13-17**
**13 Tiini kila kiamriwacho na watu, kwa ajili ya Bwana; ikiwa ni mfalme, kama mwenye cheo kikubwa; 14 ikiwa ni wakubwa, kama wanaotumwa naye ili kuwalipiza kisasi watenda mabaya na kuwasifu watenda mema. 15 Kwa sababu ndiyo mapenzi ya Mungu, kwamba kwa kutenda mema mzibe vinywa vya ujinga vya watu wapumbavu; 16 kama walio huru, ila wasioutumia uhuru huo kwa kusitiri ubaya, bali kama watumwa wa Mungu. 17 Waheshimuni watu wote. Wapendeni ndugu. Mcheni Mungu. Mpeni heshima mfalme.**

**2:13 "tiini"** Hii ni kauli tendwa shurutishi ya wakati uliopita usio timilivu, lakini toleo la NASB na NKJV linafasiri hii kama kati (kama vile 1 Pet. 2:18). "ninyi kwa ninyi" haitoki katika maandiko ya Kiyunani. Inamaanisha kwamba wanatakiwa kutengeneza uchaguzi wa kujizatiti kutii (kama vile 1 Pet. 2:18; 3:1). Hili ni neno la kijeshi linalotumika kwa ajili ya mnyororo wa amri. Kibayana inamaanisha "mtu kujipanga mwenyewe chini ya mamlaka." Haya ni maudhui yaliyozoeleka ya Petro (kama vile 1 Pet. 2:13,18; 3:1,5,22; 5:5). Kutii hakumaanishi kukosekana kwa usawa, kwakuwa Yesu anaelezewa na neno hili. Ni mtazamo wa huduma chini ya mamlaka. Katika Efe. 5:21 ni moja ya tabia tano za maisha ya mtu aliyejazwa na Roho (kunyenyekeana kwa utii katika Kristo).

## MADA MAALUM: KUJITOA *(HUPOTASSŌ)*

Tafasiri hii ya mandiko ya kale yanatumia neno hili kwa maneno 10 tofauti ya Kiebrania. Maana yake halisi kufuatana na Agano la kale ilikuwa “kuamuru” “ amri iliyo sawa” neno hili limechukuliwa kutoka katika tafasiri ya maandiko ya kale ya miaka ya 70.

1. Mungu anaamuru (kama vile Law. 10:1; Yn. 2:1; 4: 6-8)
2. Musa anaamuru (kama vile Kut. 36:6; Kumb. 27:1)
3. Amri za wafalme (kama vile 2 Nya. 31: 13)

Katika Agano jipya, maana hii inaendelea hadi katika Mdo. 10:48, ambapo Mtume anaamuru. Hata hivyo, mitazamo mipya imeibuka katika Agano Jipya.

1. Suala la hiari linaibuliwa (mara nyingi IRABU YA KATI)
2. Tendo la mtu pekee kujizuia linaweza kuonekana kwa Yesu kutii kwa Baba (Luk. 2: 51)
3. Waumini wanatii katika sura ya kijadi ili kwamba injili isiathiriwe sana.
    a. Waumini wengine (kama vile Efe.5:21)
    b. Wake za wanaoamini (kama vile Kol. 3:18; Efe. 5:22- 24; Tit.2:5; 1Petr.3:1.
    c. Waumini katika serikali za kipagani (kama vile Rum. 13:1-7; 1Pet. 2: 13).

Waumini wanatenda kutokana na msukumo wa upendo, kwa Mungu, kwa Kristo, na kwa Ufalme, kwa faida ya wengine. Kama *agapaō* (upendo), kanisaliliingiza neno hili kwa maana mpya iliyohusiana na mahitaji ya Ufalme na ya wengine. Neno hili tena linachukuliwa kama uzuri wa kutokuwa mbinafsi, usiohitaji amri, bali kwa ushirika mpya wa kujitoa kwa Mungu na Masihi Wake. Waumini wanatii na kukubali kwa manufaa ya wote na Baraka za familia ya Mungu.

◙**"kwa ajili ya Bwana"** Hii ni msukumo wa matendo yetu yote (kama vile 1 Pet. 4:11; 1 Kor. 10:31; Kol. 3:17; Efe. 6:5).

◙**"kama mwenye cheo kikubwa"** Kwa ajili ya "taasisi" angalia Mada maalumu katika Marko 10:6. Kutoka kwenye kile kinachofuata, haya ni maonyo kutii serikali au mamlaka ya umma zaidi kama Rum. 13:1-7 na Tito 3:1. Hii ni zaidi ya muhimu sana katika nuru ya dhiki ya kiserikali walioyopata waamini hawa. Haijulikani ikiwa dhiki ilikuwa ya Wayahudi, Wapagani, serikali ya maeneo au ufalme mzima sasa. Ushuhuda wetu wenye nguvu zaidi kwa nguvu ya Injili katika nyakati za dhiki. Mtazamo wetu, maneno na matendo yanapofanywa isivyo husababisha wasioamini kuyatazama.

# MADA MAALUMU: SERIKALI YA KIBINADAMU

I. UTANGULIZI

A. Ufafanuzi – serikali ni utaratibu wa kibinadamu wenyewe wa kutoa na kulinda kwa maana ya mahitaji (yaani, Mwanzo 4 na 11). Binadamu ni jamii ya viumbe hata kabla ya anguko (kama vile Mwa. 2:18).Familia, makabila, mataifa hutupatia jamii.

B. Kusudi – Mungu anapendelea kuwa utaratibu wafaaa kwenye utawala huria.

1. Sheria za Musa, hasa amri kumi za Mungu, ni mapenzi ya Mungu kwa wanadamu katika jamii. Inaleta ulinganifu wa ibada na Maisha.
2. Hakuna mfumo wa muundo wa serikari unatetewa katika maandiko, ingawa Serikali ya kale ya makasisi wa Israeli ni mfumo tarajiwa wa huko mbinguni. Sio demokrasia wala ubepari ni ukweli wa kibiblia. Wakristo wanapaswa kutenda ipasavyo kwenye mfumo wa serikali yeyote walioikuta. Kusudi la mkristo ni uinjilisti na huduma, sio mapinduzi. Serikali zote ni za mpito

C. Asili ya serikali ya mwandamu

1. Roman katoriki wanadai kwamba serikali ya mwanadamu ni hitaji la asili. Aristotle anaonekana kwanza kudai wazo hili. Anasema, “mwanadamu ni mnyama wa kisiasa” na kwa hili alimaanisha kwamba serikali “ipo kwa ajili ya msaada wa maisha mazuri.
2. Mprotestanti, hasa Martin Luther, anadai kuwa serikali ya mwanadamu ni ya asili toka kwenye anguko. Anaiita “ufalme wa Mungu wa mkono wa Kushoto.” Alisema kuwa “Njia ya Mungu ya kutawala wanadamu wabaya ni kuweka watu wabaya katika utawala.”
3. Karl Marx anadai kuwa Serikali ndiyo njia ambayo wasomi wachache wanawaweka watu wengi chini ya utawala. Kwa yeye, serikali na dini huwa na jukumu sawa

NYENZO ZA KIBIBLIA

A. Agano la Kale

1. Israeli ni mfumo ambao utatumika mbinguni. Katika Israeli ya kale YHWH alikuwa mfalme. Serikali ya makasisi ni neno linalotumika kuelezea utawala wa Mungu wa moja kwa moja (kama vile 1 Sam. 1. 8:4-9).
2. Utawala wa Mungu katika serikali ya mwanadamu unaweza kuonekana wazi katika kuteuwa kwake.
   a. wafalme wote, Dan. 2:21; 4:17,24-25
   b. Uongozi wa Musa, Dan. 2:44-45
   c. Nebuchadnezar (Babeli mpya), Yer. 27:6; Dan. 5:28
   d. Koreshi II (Uajemi), 2 Kor. 36:22; Ezra 1:1; Isa. 44:28; 45:1
3. Watu wa Mungu wanapaswa kuwa watiifu na wenye adabu hata kuvamia na kumiliki serikali…
   a. Danieli 1-4, Nebuchadnezar (Babeli mpya)
   b. Danieli 5, Belshazzar (Babeli mpya)
   c. Danieli 6, Dario (Uajemi)
   d. Ezra na Nehemia (Uajemi)
4. Kurudishwa kwa Yuda kulikuwa ni kuomba kwa Koreshi na kutawala na uzao wake..
   a. Ezra 6:10; 7:23
   b. Wayahudi walipaswa kuomba kwa mamlaka ya kiraia, Mihnah, Avot. 3:2

B. Agano Jipya

1. Yesu alionyesha heshima kwa serikali ya kibinadamuu.
   a. Mathayo 17:24-27, Yeye alilipa kodi ya hekalu (dini na utawala wa kiraia ulikuwa na maaana ya kuwa mmoja,kama ile Petro 2. 2:17)
   b. Mathayo 22:15-22; Marko 12:13-17; Luka 20:20-26, Alitetea nafasi ya kodi ya kirumi na hivyo mamlaka ya kiraia ya kirujmi.
   c. Yohana 19:11, Mungu aliruhusu utawala wa kiraia kufanya kazi.
2. Maneno ya Paulo yalihusiana na serikali ya kibinadamu.
   a. Warumi 13:1-5, waaminio lazima wawasilishe kwa utawala wa kiraia kwa kuwa walianzishwa na Mungu

b. Warumi 13:6-7, waaminio lazima kulipa kodi na kuheshimu utawala wa kiraia.
c. Timotheo 1. 2:1-3, waaminio lazima kuomba kwa utawala wa kiraia.
d. Tito 3:1, waaminio lazima kunyenyekea kwa utawala wa kiraia.

3. Maneno ya Petro yalihusiana na serikali ya kibinadamu.
   a. Matendo 4:1-31; 5:29, Petro na Yohana kabla ya wakuu wa sinagogi (hii inaonyesha kuendelea mbele kibiblia kwa kutokutii kwa raia)
   b. Petro 2. 2:13-17, waaaminio lazima wawasilishe kwa utawala wa kiraia kwa mazuri ya jamii na kwa uinjilisti.
4. Maneno ya Yohana yalihusiana na serikali ya kibinadamu.
   a. Ufunuo 17,uzinzi wa Babeli unawakilisha serikali ya wanadamu iliyoandaliwa na kufanya kazi mbali na Mungu.
   b. Ufunuo 18, uzinzi wa Babeli umeharibiwa.

. HITIMISHO

A. Serikali ya mwanadamu (katika ulimwengu ulioanguka) imewekwa na Mungu. Hii sio “haki ya kiungu ya wafalme,” bali kazi ya kiungu ya Serikali (yaani, amri sio machafuko). Hakuna mfumo wa mtu unaotetewa juu ya mwingine.
B. Ni wajibu wa dini kwa waaminio kutii na kuomba kwa mamlaka ya kiraia.
C. Ni sawa kwa waaminio kuunga mkono serikali ya wanadamu kwa kodo na mtazamo wa heshima.
D. Serikali ya mwanadamu ni kwa lengo la utaratibu wa kiraia. Wao ni watumishi wa Mungu kwa kazi hii.
E. Serikali ya mwanadamu sio mwisho. Ina kikomo katika mamlaka yake.Waaminio lazima kutenda kwa sababu ya dhamiri zao kwa kukataa mamlaka ya kiraia wakati inapita mipaka yake iliyowekwa na Mungu. Kama Augustino alionyesha katika *The City of God*, sisi ni raia wa falme mbili, moja ya muda na moja ya milele (kama vile. Wafil. 3:20). Tuna wajibu kwa wote, lakini ufalme wa Mungu ni mwisho! Kuna yote mwelekeo wa kibinafsi na ushirika katika wajibu wetu kwa Mungu.
F. Tunapaswa kuwatia moyo waminio katika mfumo wa kidemokrasia kushiriki kikamilifu katika mchakato wa serikali na kuutekeleza, wakati ikiwezekana, mafundisho ya maandiko.
G. Mabadiliko ya kijamii lazima kuendelezwa na ubadilishaji wa mtu binafsi. Hakuna tawi halisi la theolojia linalojishughulisha na kifo, hukumu, pepo na jehanamu la kudumu katika serikali. Serikali zote za mwanadamu, ingawa lazima na kutumiwa na Mungu, ni maonyesho ya dhambi ya shirika la mwanadamu mbali na Mungu. Dhana hii inaelezewa katika matumizi ya Johannine ya neno “ulimwengu (yaani, Yohana 1. 2:15-17).

◙**"kama mwenye mamlaka"** Neno hili katika Uyunani wa kati lilimaanisha "mwanzilishi mwanadamu wa mji"; hatahivyo katika Agano Jipya siku zote inatumika juu ya mamlaka ya Mungu (kama vile Mt. 22:21; Rum. 13:1-7; 1 Tim. 2:1-7; Tito 3:1-8), ambalo mara kwa mara inatolewa kwa ushirika wa kibinadamu. Mungu hupendelea utaratibu badala ya mivurugano.

**2:14 "ikiwa ni wakubwa, kama wanaotumwa naye"** Hii ni kauli tendewa endelevu ya wakati uliopo. Mungu anashughulikia mambo yote. Andiko hili halifundishi "haki za kiungu za Wafalme," lakini linakiri kwamba Mungu anakubaliana na sheria na utaratibu (yaani jamii iliyo imara) kuliko mivurugano.
Kiwakilishi "yeye" inaweza kumaanisha (1) Mungu au (2) mtawala.

◙**"ili kuwalipiza kisasi watenda mabaya"** Serikali ina mamlaka yaliyotokana na Mungu kuendelea kudumisha utaratibu na kupunguza na kuadhibu kukosekana kwa utaratibu. Adhabu ya mauti ni moja wapo ya aina ya mamlaka hizi (kama vile Rum. 13:4; Mdo. 25:11).

**2:15 "Kwa sababu ndiyo mapenzi ya Mungu"** Angalia Mada Maalum hapa chini.

## MADA MAALUMU: MAPENZI (*THELĒMA*) YA MUNGU

“Mapenzi” ya Mungu yamejikita katika namna mbalimbali.

INJILI YA YOHANA

- Yesu alikuja kuyatenda mapenzi ya Baba yake (kama vile Yohana 4:34; 5:30; 6:38)
- Kuwafufua siku ya mwisho wale wote Baba aliowampa Mwana (kama vile Yohana 6:39)
- Kwamba wote waamini katika Mwana (kama vile Yn. 6:29; 40)
- Maombi yaliyojibiwa kuhusiana na kuyatenda mapenzi ya Mungu (kama vile Yn 9:31 na Yn 5:14)

VODOKEZO VYA INJILI

- Kuyatenda mapenzi ya Mungu ni jambo la muhimu (kama vile Mt. 7:21)
- Kuyatenda mapenzi ya Mungu hutufanya kuwa kaka na dada pamoja na Yesu (kama vile Mt. 12:50; Marko 3:35)
- Sio mapenzi ya Mungu kwa yeyote kuangamia (kama vile Mt.18:14; 1 Tim. 2:4; 2 Pet. 3:9)
- Kalvari ilikuwa ni mapenzi ya Mungu kwa Yesu (kama vile Mt. 26:42; Luka 22:42)

NYARAKA ZA PAULO

- ukomavu na huduma ya waamini wote (kama vile Rum. 12:1-2)
- waamini waliondolewa kutoka katika enzi hii ya maovu (kama vile Gal. 1:4)
- mapenzi ya mungu ulikuwa ni mpango wake wa ukombozi (kama vile Efe.1:5, 9,15)
- waamini wanapitia na kuishi maisha yaliyojazwa na Roho (kama vile 5:17-18)
- waamini wamejazwa na maarifa ya Mungu (kama vile Kol. 1:9)
- waamini wanafanywa kuwa imara na wakamilifu (Kol. 4:12)
- waamini wanatakaswa (kama vile 1The. 4:3)
- waamini watoa shukrani katika vitu vyote (kama vile The.5:18)

NYARAKA ZA PETRO

- Waamini wanatenda haki (yaani, kunyenyekea kwenye mamlaka ya chini) na, kwa hiyo wanawanyamazisha watu wajinga, hivyo kuwapa fursa kwa kuijua injili/matendo mema (kama vile 1Pet. 2:15)
- Mateso ya waamini (kama vile 1 Pet. 3:17; 4:19)
- Waamini hawapaswi kuishi maisha ya ubinafsi (kama vile 1 Pet. 4:2)

NYARAKA ZA YOHANA

- waamini kuendelea kudumu milele (kama vile Yohana 2:17)
- waamini ni kielelezo kwa maombi yaliyojibiwa (kama vile 1 Yohana 5:14)

◙**"kimya"** Hii kibayana ni "ukimya" (kama vile Marko 1:25, 4:39).

◙**"ujinga"** Hii inamaanisha mtu anayekosa utambuzi wa kiroho (kama vile 1 Kor. 15:34).

◙**"vya watu wapumbavu"** Neno hili linaorodheshwa katika mfuatano wa dhambi katika Marko 7:22. Inaelezea walimu wa Kiyahudi wasioamini katika Rum. 3:20, lakini inatumika kuelezea waamini katika Efe. 5:17. Hivyo inamaanisha kuwa ina hali ya kivivu ya akili ambayo inaathiri wote waliookoka na wasiookoka. Hapa inarejerea wapagani wasio kuwa na taarifa ambao wanawashutumu waamini juu ya vitu visivyokuwa vya kweli (kama vile 1 Pet. 2:12).

**2:16 "kama walio huru"** Hii inamaanisha shurutishi (kama vile NASB, TEV, NIV). Ni ulinganifu kwa wapagani ambao wao ni watumwa kwa dhambi. Waamini ndio wenye maamuzi. Yesu amewafungua kutoka katika kutawaliwa na dhambi (kama vile Warumi 6), lakini mara kwa mara wanatumia uhuru wao kuchagua dhambi tena.

◙**"ila wasioutumia uhuru huo kwa kusitiri ubaya"** Hii kibayana "kuwa" (kauli tendwa endelevu ya wakati uliopo) iliyokanushwa, ikitumiwa kama shurutishi. Mara ngapi uhuru wetu umekuwa leseni (kama vile 1 Kor. 8:9; Gal. 5:13) badala ya kuwa shuhuda wa dhabihu inayoishi (kama vile Rum. 14:1-15:13). Uhuru siku zote unaleta uwajibikaji lakini kuwa makini juu ya uhalalishaji au ibada (kama vile 1 Kor. 8-10; Kol. 2:16-23). Waamini sasa wako huru mbali na dhambi ili kumtumikia Mungu (kama vile Warumi 6) na wenyewe kwa wenyewe (kama vile 1 Kor. 9:19-23).

◙**"bali kama watumwa wa Mungu"** Waamini wamewekwa huru kutoka katika dhambi na sasa wako huru kumtumikia Mungu (kama vile Rum. 6:22).

**2:17 "Waheshimuni watu wote"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu, muhtasari wa kwanza wa amri zisizokuwa na utata kati ya nne katika 1 Pet. 2:17. Hii inamaanisha kutambua uthamani wa wanadamu wote mbele za macho ya Mungu (kama vile Mwa. 1:26-27; Yohana 3:16) na kuishi ili kuwavuta kwenye imani katika Kristo (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:47; Mdo. 1:8).

◙**"Wapendeni ndugu"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Wakristo lazima waendelee kupendana (kama vile 1 Pet. 1:22; Yohana 13:34, 15:12,17; Rum. 12:10; 1 The. 4:9; Ebr. 13:1; 1 Yohana 2:7-8, 3:11, 23; 4:1,11; 2 Yohana 5). Upendo ni ushahidi wa kweli kwamba tunamjua Mungu, kwamba tumemtumainia Kristo, na kwamba tunaongozwa na Roho. Ni tabia ya kifamilia ya Mungu. Waamini wanatakiwa kuwapenda wanadamu wote kwa ajili ya Injili na kuwapenda Wakristo wengine kwasababu ni sehemu ya familia ya Mungu.

◙**"mcheni Mungu"** Hii ni kauli ya kati (yenye ushahidi) shurutishi (kama vile Ayubu 28:28; Zab. 111:10; Mith. 1:7;15:33). Tunapata neno la Kingereza "phobia" kutoka katika neno la Kiyunani. Linatumika katika namna ya heshima na adhama. Matendo ya waaminio lazima yatokane na mahusiano yao na heshima yao kwa Mungu!

◙**"mpeni heshima mfalme"** Kauli shurutishi hizi mbili za mwisho za wakati uliopo zaweza kuwa maelezo kwa Mith. 24:21. Kumbuka siku za Petro kwamba Mfalme alikuwa ni Nero (kama vile 1 Pet. 2:13)!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 PETRO 2:18-25**
**18 Enyi watumishi, watiini bwana zenu kwa hofu nyingi, sio wao walio wema na wenye upole tu, bali nao walio wakali. 19 Maana huu ndio wema hasa, mtu akivumilia huzuni kwa kumkumbuka Mungu, pale ateswapo isivyo haki. 20 Kwa maana ni sifa gani kustahimili, mtendapo dhambi na kupigwa makofi? Lakini kustahimili, mtendapo mema na kupata mateso, huu ndio wema hasa mbele za Mungu. 21 Kwa sababu ndio mlioitiwa; maana Kristo naye aliteswa kwa ajili yenu, akawaachia kielelezo, mfuate nyayo zake. 22 Yeye hakutenda dhambi, wala hila haikuonekana kinywani mwake. 23 Yeye alipotukanwa, hakurudisha matukano; alipoteswa, hakuogofya; bali alijikabidhi kwake yeye ahukumuye kwa haki. 24 Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu katika mwili wake juu ya mti, tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi, tuwe hai kwa mambo ya haki; na kwa kupigwa kwake mliponywa. 25 Kwa maana mlikuwa mnapotea kama kondoo; lakini sasa mmemrudia Mchungaji na Mwangalizi wa roho zenu.**

**2:18 "Enyi watumishi, watiini bwana zenu"** Hii ni kauli ya kati endelevu ya wakati uliopo iliyotumika kama shurutishi (angalia dokezo na mada maalumu katika 1 Pet. 2:13). Watumwa waaminio huheshimu mabwana zao wa duniani kwasababu ya heshima yao kwa Mungu! Hii hata inarejerea kwa wale mabwana waaminio wakati na wasio fanya haki au mabwana Wakristo walio na watumwa. Katika siku zetu kutendea kazi maonyo haya kungefana na waajili wa Kikristo na waajiliwa wa Kikristo. Hii ni sawasawa na mafundisho ya Paulo katika Efe. 6:5-9. Tazama #3 katika Mada maalum hapa chini.
Hii ni sehemu nzuri kujadili kipengele cha desturi ya ufasiri wa Kibiblia. Ikiwa Injili ilipewa changamoto (1) karne ya kwanza ya mababa wa imani ya kipindi kati ya desturi za Wayunani-Warumi (2) desturi ya kitumwa, ingekataliwa na kuharibiwa na jamii ya karne ya kwanza. Kwa kuhubiri Injili vikwazo hivi viwili vilianguka kwa muda! Biblia lazima ifasiriwe katika mazingira yake ya kihistoria na alafu kweli zenye uvuvio zifanyiwe kazi katika siku zetu na desturi pamoja na nguvu na matokeo. Haimaanishi kwamba tunajaribu kuzalisha desturi ya karne ya kwanza kama mapenzi ya Mungu kwa kila jamii katika kila kizazi. Lengo ni kuhubiri kweli ya milele ya injili ambayo inaleta atokeo kwa watu mmoja mmoja na hatimaye jamii yenyewe.

## MADA MAALUM: MAONYO YA PAULO KWA WATUMWA
1. utosheke, lakini kama patakuwepo na fursa kwa ajili ya kunufaika na uhuru wenyewe, chukua (1 Kor. 7:21-24).
2. Katika Kristo hapana mtumwa wala (Gal. 3:28; Kol. 3:11; kama vile 1 Kor. 12:13).
3. Tenda katika Bwana, naye atakulipa (Efe. 6:5-9; Kol. 3:22-25; kama vile 1 Pet. 2:18-20).
4. Katika Kristo watumwa huwa ndugu (1 Tim. 6:2; Filemoni 1:16-17).

5. Watumwa wa ki-Mungu huleta heshima kwa Mungu (1 Tim. 6:1; Tito 2:9).
Maonyo ya Paulo kwa wamiliki wa watumwa:

Watumwa wa Kikristo na mmiliki wa watumwa wana Bwana mmoja, kwa hiyo, kwa hiyo, wanapaswa kuwatenda wengine kwa heshima (Efe. 6:9; Kol. 4:1).

Utumwa ni moja ya iana ya kitamaduni (kama vile tamaduni za wazee wa kaya) ambao walikuwa ndio nguzo ya ulimwengu wa karne ya kwanza. Agano Jipya halileti changamoto wala mwelekeo. Hata hivyo, kweli ya injili, kwa muda iliathiri mabadiliko katika mwelekeo wa utamaduni.

**2:19**
**NASB “kwa maana huu ndio wema”**
**NKJV “kwa kuwa hii ndicho kinachopendekezwa”**
**NRSV “kwa kuwa hili ndilo mwesabiwalo haki”**
**TEV “Mungu awabariki ninyi kwa hili”**
**NJB “mnaona, kuna kigezo”**

Hii inarejerea ukubalifu wa Mungu wa utii hata kati kati ya dhiki, wakati mateso hayo yanahusianishwa na dhamiri zetu za Wakristo na tumaii katika Kristo (kama vile 1 Pet. 3:14,17; 4:13-14,16). "Kibali" ni neno la Kiyunani *charis* (neema) ikitumika katika namna yake isiyo ya kithiolojia.

◙**"kama"** Hii ni sentensi ya daraja la kwanza lenye masharti ambalo linakisiwa kuwa kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au kwa ajili ya makusudi yake ya kifasihi. Watumwa wakristo walikuwa wakiteseka chini ya ukatili wa mabwana wao kwa ajili ya Kristo.

◙**"dhamiri"** Angalia dokezo katika 1 Petro 3:16.

**2:20 "Kwa maana ni sifa gani"** Hili ni neno kwa ajili ya heshima lililounganishwa na hadhi ya mtu (kama vile Luka 6:32-34). Linatoka katika kitenzi cha Kiyunani *kaleō*, ambalo linamaanisha kuita. Hivyo linamaanisha kuita sifa, heshima au utukufu juu ya mtu.

◙**"ikiwa"** Kuna sentensi mbili za daraja la kwanza lenye masharti katika mstari huu ambalo lilikuwa linadhaniwa kuwa kweli. Sentensi ya kwanza yenye masharti inatumika katika namna ya ukanushi na ya pili katika namna chanya. Mungu anapendezwa pale waamini wanapoteseka isivyo halali lakini kwa uvumilivu kwakuwa ni waamini (kama vile 1 Pet. 1:29; 3:24,27; 4:12-16; Mt. 5:10-16).

**2:21 "Kwa sababu ndio mlioitiwa"** Hii ni kauli tendwa elekezi ya wakati uliopita usio timilifu. Katika muktadha tungo hii inamaanisha kwamba waamini waliitwa kuyaiga maisha ya Yesu ambayo yanaleta utukufu kwa Mungu na wokovu kwa wanadamu. Huu ni wito kuelekea unyenyekevu kwa niaba ya waamini wote ambayo inaleta makuzi ya kiroho na ushuhuda wenye nguvu wa injili.
Kwamba waaminio wameitwa na Mungu kuteseka ni kauli ya kushangaza, haswa kwa desturi za kimagharibi ambazo zinafikiria Ukristo kwa namna ya (1) "kuna faida gani kwa ajili yangu" au (2) injili ya mali, afya na mafanikio. Dhiki kwa waaminio ni uwezekano halisi kwa ulimwengu ulioanguka (kama vile Mdo. 14:22; Rum. 5:3-4; 8:17; Flp. 1:29; 1 The. 3:3-4; 2 Tim. 3:12; Yakobo 1:2-4; 1 Pet. 3:14; 4:12-19).

◙**"maana Kristo naye aliteswa"** Kuteseka kwa Masihi kulikuwa jambo la kushangaza kwa Wayahudi waliokuwa wakitegemea Masihi mpambanaji wa Kijeshi. Kuna madokezi kadhaa katika Agano la Kale (kama vile Mwa. 3:15; Zab. 22; Isa. 53). Yesu mwenyewe alionesha (1) Mitume Wake (kama vile Mt. 16:21; 17:12,22-23; 20:18-19) na (2) kanisa la kwanza vifungu hivi vya kinabii (kama vile Luka 24:25-27). Mateso yake na kifo vilikuwa sehemu ya mahubiri yake ya kitume ya kanisa la kwanza katika Mdo. na *Kerygma* (kama vile Mdo. 2:23; 3:13-14,18; 17:3; 26:23). Angalia Mada Maalum katika 1 Pet. 1:11.Kuna funguo kadhaa za kweli za kithiojia zilizounganishwa na mateso Yake.

1. Kristo ni mfano wetu (1 Pet. 2:21)

2. Kristo alichukua dhambi zetu msalabani (1 Pet. 2:24)
3. Kazi ya Kristo ilitusababishia sisi kufa kwa dhambi na kuishi kwa ajili ya Mungu (1 Pet. 2:24)
4. Kristo ni Mchungaji na Kiongozi wa nafsi zetu (1 Pet. 2:25)

Neno "kuteseka" (*epathen*) linapatikana katika MSS $P^{72}$, A, B, na C, lakini katika kale zingine MSS, $P^{81}$, א, zina "kufa" (*apethanen*). Toleo la UBS[4] linatoa usomaji wa kwanza alama ya "A" (hakika), ikidhaniwa kwamba "kufa" kumeondolewa na wanakili kutoka 3:18.

◙**"kielelezo"** Agano Jipya lina sababu tatu kwa nini Kristo alikuja:

1. Kufanyika mbadala, kuchukua nafasi ya upatanisho. Yeye, asiye na hatia, asiye na mawaa (kama vile 1 Pet. 2:22) Mwana kondoo wa Mungu (kama vile Yohana 1:29), akajitoa mwenyewe kwa niaba yetu (kama vile 1 Pet. 2:24).
2. Kufanyika ufunuo mkamilifu wa Baba (kama vile Yohana 1:1-14; 14:8-9).
3. Kuwa mfano kwa ajili ya waaminio (kama vile 1 Pet. 2:21) kuiga. Ni muisraeli kweli kweli, mtu mkamilifu, kile ambacho mwanadamu alitakiwa kuwa, angekuwa na siku moja atakuwa.

**2:22 "yeye hakutenda dhambi"** Hii ni nukuu kutoka Isa. 53:9. Dhana hii inaelezewa pia katika Yohana 8:46, 14:30; Luka 23:41; 2 Kor. 5:21; Ebr. 4:15, 7:26-27; 1 Pet. 1:19; 2:22; 3:18, 1 Yohana 3:5. Alikuwa kwa ajili ya dhambi zetu kwakuwa hakutakiwa kufa kw ajili ya dhambi Zake mwenyewe!

◙**"wala hila haikuonekana kinywani mwake"** Yesu alikuwa Mwisraeli mwenye sifa zote (kama vile Isa. 53:9 Zeph na Zef. 3:13).

**2:23 "Yeye alipotukanwa, hakurudisha matukano"** Kuna mfuatano wa kauli tendaji tatu elekezi za wakati usio timilifu linalomaanisha tendo linalojirudia rudia kwa wakati uliopita. Ya kwanza ni maelezo ya Isa. 53:7. Yesu alitimiliza unabii katika Majaribu Yake mbele ya Kayafa, Anna Kuhani Mkuu, Pilato na Herode.

◙**"alipoteswa, hakuogofya"** Alizungumza lakini kwa ajili ya msamaha kwa wale wote waliojihusisha katika kifo Chake (kama vile Luka 23:34).

◙**"bali alijikabidhi kwake yeye ahukumuye kwa haki"** Kujiaminisha huku kulikuwa mtazamo wa kawaida wa maisha ya Yesu. naonekana yenye nguvu katika Luka 22:42 na 23:46.

**2:24 “Yeye mwenyewe alizichukua dhambi zetu"** Hii kibayana ni Isa. 53:4,11,12. Neno "kuchukua" kunatumika juu ya dhabihu katika Law. 14:20 na Yakobo 2:21. Hii ni maana ya kufanyika mbada wa upatanisho wa dhambi (kama vile Marko 10:45; Rum. 5:6,8,10; 2 Kor. 5:21).

◙**"mwili wake juu ya mti"** Ingawa hakuna kiashiria halisia cha ujuzi uliounganishwa kwa 1 Petro (falsafa ya Kiyunani la Kikristo la kwanza ilielezea kwamba Yesu hakuwa mwanadamu wa kweli, kama vile Kol.; 1 Tim.; 1 Yohana). Andiko hili ni ukiri mwingine wenye nguvu wa ubinadam wa kweli na kifo cha mwili cha Yesu wa Nazareti (kama vile Kol. 1:22).
Tungo "msalabani" inaweza kuwa na muunganiko na Kumb. 21:23, ambapo yoyote aliyetungikwa nyama (yaani mtini) badala ya kuzikwa vizuri alikuwa amelaaniwa na Mungu. Katika siku za Yesu walimu walikuwa wamefasiri hii ikijumuisha usulubishwaji wa Warumi. Yesu alikuwa ameshitakiwa kwa kukufuru ambapo kulingana na sheria ya Musa ilidai kupigwa mawe. Kwanini sasa viongozi wa Kiyahudi walimtaka asulubishwe ambacho kilitaka ukubalifu wa Warumi na kunajisika karibia na Pasaka? Baadhi wamesema kwamba walifanya hivi kwasababu Wayahudi hawakuwa na mamlaka chini ya sheria ya Kirumi kumweka mtu katika adhabu ya kifo, lakini vipi kuhusu Stephano 7?
Nafikiria walitaka Yesu asulubiwe kuonesha kwamba huyu mnafiki ajifanyaje Masihi alikuwa amelaaniwa na Mungu. Lakini hii ni hasa kilichotokea. Yesu alifanyika laana kwa ajili yetu (kama vile Gal. 3:13). Agano la Kale lenyewe lilifanyika laana (kama vile Kol. 2:14). Ilidai kwamba nafsi itendayo dhambi sharti iuwawe (kama vile 2 Wafalme. 14:6; Ezek. 18:4,20). Lakini wanadamu wote wametenda dhambi (kama vile Rum. 3:9-18,23; Gal. 3:22). Hivyo wote wanastahili kufa na walikuwa chini ya adhabu ya kifo. Yesu mwanakondoo wa Mungu asiye na dhambi (Yohana 1:29) alichukua dhambi za ulimwengu wote ulioanguka (kama vile Rum. 5:12-21)

◙**"tukiwa wafu kwa mambo ya dhambi"** Hiki ni kishazi cha kusudi (*hina*). Hili ndilo lengo la Ukristo (kama vile Rum. 6:20; Gal. 2:20). Ni urejesho wa taswira ya Mungu ndani ya wanadamu ambayo inarejesha ushirika wa karibu pamoja na Mungu.

◙**"na kwa kupigwa kwake mliponywa"** Hii ni kauli tendwa elekezi ya wakati uliopita usio timilifu. Katika Isa. 53:4-6 hii inazungumzia uponyaji wetu wa kiroho, sio uponyaji wa mwilini. Sikatai uponyaji wa mwilini kama tukio la neema ya Mungu linaloendelea, lakini sikatai kwamba ni kiashiria kilichohaidiwa cha upatanisho wa Kristo. Katika Agano la Kale dhambi ilikuwa imejulikana kwa ugonjwa wa mwili (kama vile Isa. 1:5-6; Zab. 103:3). Hii ni sitiari kwa ajili ya msamaha wa dhambi na sio ahadi kwamba waamini wana imani ya kutosha Mungu atawaponya kila tatizo la mwili la kila mwamini. Kwa ajili ya mjadala mzuri wa Isa. 53:4 na matumizi yake kwa Mt. 8:17, F. F. Bruce's *Answers to Questions*, kur. 44- 45, kinaweza kusaidia.

**2:25 "Kwa maana mlikuwa mnapotea"** Haya ni maelezo kwa Isa. 53:6. Ni kauli tendwa isio timilifu yenye mafumbo, ambayo inarejerea kitendo cha kujirudia rudia kwa wakati uliopita au mwanzo wa kitendo. Je hii humaanisha kwa

1. Wayahudi wa Agano la Kale (kama vile Rum. 3:9-18, ambayo ni mfuatano wa nukuu za Agano la Kale)
2. Wanadamu wote
3. Waamini Mataifa waliojitoa kuteseka (yaani yawezekana kumkana Yesu wakati wa mashitaka)
4. waamini, Wayahudi na Mataifa waliokuwa wakipoteza vita vya kila siku kwa asili ya dhambi

◙**"lakini sasa mmemrudia"** Hii ni kauli tendwa elekezi ya wakati uliopita usio timilifu ambayo humaanisha kurudi kwa ug'ag'anizi kwa uwakala wa Mungu, Kristo au Roho (kama vile toleo la TEV "mmerejeshwa tena"). Fasiri nyingi zaidi za Kingereza zinafasiri hii kama kati (kama vile matoleo ya NASB, NRSV, NJB, NIV). Katika Agano la Kale "geuka" au "kurudi" (*shub*) mara kwa mara kunatumiwa kwa ajili ya watu wa Mungu kutubu na kumrudia Yeye.

◙**"Mchungaji"** Jina hili linatumiwa kwa ajili ya Mungu (kama vile Zab. 23:1, Ezek. 34) na hapa juu ya Yesu kama katika Yohana 10:1-18 na Ebr. 13:20. Inamaanisha pole, yenye karimu na kuendelea kujali. Cheo hiki kinaweza hata kuaksi majadiliano ya Petro pamoja na Yesu katika Yohana 21 (kama vile 1 Pet. 5:1-3).

**NASB, NRSV,**
**NJB** **"mlezi"**
**NKJV** **"mwangalizi"**
**TEV** **"mtunzaji"**

Hapa neno *episkopos* ilinatumika juu ya Yesu, lakini mara kwa mara viongozi wa makanisa ya nyumbani. Neno linafasiri "askofu" au "mwangalizi" na lina usuli wa mji wa Kiyunani, wakati neno linalofanana "mzee" (*presbuteros*) lina usuli wa kabila la Kiebrania. Maneno haya mara kwa mara yanatumia kwa ufanano sawa kurejerea jukumu la Mchungaji wa Agano Jipya (kama vile Mdo. 20:17,28; Tito 1:5,7).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je Wakristo wote wanaanza kama wakristo wachanga? Kwanini?
2. Kwanini Petro anatumia majina mengi ya Agano la Kale kuelezea waamini wa Agano Jipya?
3. Kuna sababu gani ya waamini kuitwa "mawe?"
4. Kwanini mitindo yetu ya maisha ni muhimu sana?
5. Kwa nini sisi kama Wakristo tutii mamlaka ya Kiserikali?
6. Kwanini Ukristo uliushambulia utumwa?
7. Upi ulikuwa ushauri wa Petro kwa wale waliokuwa hawatendi haki?
8. Nini umuhimu wa kifo cha Kristo?

# 1 PETRO 3

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Wake kwa waume | Utii kwa waume | Wajibu wa Mkristo (2:11-4:11) | Wake kwa waume | Wajibu wa wakristo: Katika ndoa |
| 3:1-6 | 3:1-6 | 3:1-6 | 3:1-6 | 3:1-6 |
| | Neno kwa wanaume | | | |
| 3:7 | 3:7 | 3:7 | 3:7 | 3:7 |
| Kuteseka kwa ajili Ya haki | Kuitiwa baraka | | Kuteseka kwa ajili ya mema | Wajibu wa Wakristo: kuwapenda nduguze |
| 3:8-12 | 3:8-12 | 3:8-12 | 3:8-12 | 3:8-12 |
| | Kuteseka kwa ajili ya mema na mabaya | | | Wajibu wa Wakristo wakati wa dhiki |
| 3:13-22 | 3:13-17 | 3:13-22 | 3:13-22 | 3:13-17 |
| | Mateso ya Kristo Na yakwetu | | | Kufufuka na kushuka kuzimu |
| | 3:18-4:6 | | | 3:18-22 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Kutoka "Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozokwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu. Kuandikaki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 PETRO 3:1-6**
**1 Kadhalika ninyi wake, watiini waume zenu; kusudi, ikiwa wako wasioliamini Neno, wavutwe kwa mwenendo wa**
**wake zao, pasipo lile Neno; 2 wakiutazama mwenendo wenu safi, na wa hofu. 3 Kujipamba kwenu, kusiwe**
**kujipamba kwa nje, yaani, kusuka nywele; na kujitia dhahabu, na kuvalia mavazi; 4 bali kuwe utu wa moyoni**
**usioonekana, katika mapambo yasiyoharibika; yaani, roho ya upole na utulivu, iliyo ya thamani kuu mbele za**
**Mungu. 5 Maana hivyo ndivyo walivyojipamba wanawake watakatifu wa zamani, waliomtumaini Mungu, na**
**kuwatii waume zao. 6 Kama vile Sara alivyomtii Ibrahimu, akamwita Bwana; nanyi ni watoto wake, mfanyapo**

| |
|---|
| **mema, wala hamkutishwa kwa hofu yo yote.** |

**3:1 "Kadhalika"** Hili linaturudisha nyuma kwenye maonyo yake kwa jamii ya Kikristo (kama vile 1 Pet. 2:13) na mateka wa Kikristo (kama vile 1 Pet. 2:18).

◙ **"ninyi wake, watiini"** Hii ni kauli ya kati ya hali ya kuendelea ya wakati uliopo kama ilivyo 2:18. Hili ni neno la kijeshi lenye kumaaanisha "kumweka mtu chini ya mamlaka" (kama vile Efe. 5:21-33; Kol. 3:18-19; Tito 2:4-5). Hii sura yote inahusiana na mazungumzo ya Petro juu ya "kutii" kwa waamini kwenye serikali (2:13-17) na watwana kuwaamini mabwana zao (2:18-20). Kutii sio neno lililo kinyume; linamwelezea Yesu mwenyewe. Alikuwa mtii kwa wazazi wake wa hapa duniani. Alikuwa mtii kwa Baba yake wa mbinguni.

◙ **"kusudi"** Hiki ni kishazinia (*hina*) , kinachoelezea kusudio la kithiolojia kwa ajili ya utii wa mwanamke. Mara nyingi ni kwa ajili ya uinjilisti! Waamini wanapaswa kila siku kutengeneza ufalme wa Mungu (kama vile hotuba ya Mlimani, Mathayo 5-7).

◙ **"ikiwa"** Hii ni sentensi yenye masharti daraja la kwanza ambayo inadhaniwa kuwa kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au kwa kusudio lake la kifasihi. Muktadha huu unazungumzia juu ya wanaume wasioamini. Katika karne ya kwanza nyingi za familia zilizochangamana zilikuwa maarufu kwa sababu mmoja wa mwenza wake alikuwa mwamini. Kibiblia huu sio uhakiki wa andiko kwa ajili ya kuoana na Yule asiyeamini!

◙ **"wako wasioamini"** Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati uliopo, yenye kudokeza tendo endelevu. Kama ilivyo Kibiblia imani ni tukio linaloendelea, hivyo pia, kwa asiyeamini!

◙ **"neno"** katika 1 Petro "neno" (yaani., *logos*) ni stiari kwa ajili ya kuihubiri injili Kitume. Waamini wamezaliwa mara ya pili kwa neno (kama vile 1 Pet. 1:23). Hutamani neno la kiroho au maziwa asili ya neno (yaani., *logikos*, kama vile 1 Pet. 2:2).

◙ **"wavutwe"** Hii ni kauli tendwa elekezi ya wakati ujao. Hili neno linamaanisha "kufaidika." Limetumika kwa ajili ya wokovu katika 1 Kor.9:19-22. Lengo la asili la mke anayeamini ni wokovu kwa ajili ya familia yake. Hili lapaswa kuwa lengo la waamini wote.

◙ **"pasipo neno"** Maisha yake ya imani yatazungumza zaidi na kwa uwazi kuliko maneno! Hata hivyo, kwa kiasi Fulani maneno huhitaji kupeleka ujumbe wa injili!

◙ **"kwa mwenendo"** Maisha yetu mara nyingi hupiga kelele zaidi kuliko maneno.

**3:2 "wakiutazama"** Hili neno lilitumiwa na wale walioshuhudia kwa macho. Petro amelitumia mara tatu katika nyaraka zake (kama vile 1 Pet. 2:12;3:2; 2 Pet. 1:16). Maisha ya waamini yanaonekana. Ingawa ni kanuni ni kweli kuwa maisha ya waamini ni Biblia pekee ambayo baadhi ya watu wataendelea kuisoma. Maisha ya waamini ni Yesu pekee ambayo baadhi ya watu wataendelea kuhitaji kuyajua. Ni wajibu wa kushangaza ulioje.

**NASB "mwenendo safi na wa kuheshimika"**
**NKJV "mwenendo wenu safi na wa hofu"**
**NRSV "maisha yenu safi na ya heshima"**
**TEV "mwenendo safi na wa heshima"**
**NJB "maisha safi na yenye heshima"**

Petro amelitumia neno "hofu,"likieleweka kama lenye heshima hapo mwanzo, katika 1 Pet. 1:17 na 2:18 (kama vile Mdo. 9:3; 10:2;Rum. 3:18; 13:7; Efe. 5:33; Ufu. 11:18).waamini huishi maisha yasiyo ya kibinafsi, kiungu, maisha yaliyokubalika kitamaduni kwa ajili ya kusudi la ufalme wa ushuhuda na uinjilisti.

Neno "safi" (*agnos*) linatafasiriwa katika namna mbalimbali (safi, pasipo doa, nyenyekevu, pasipo hatia, pasipo lawama). Limetumika kwa wanawake katika 2 Kor. 11:2; Tito 2:5; na hapa.

**3:3 "kujipamba kwenu, kusiwe kujipamba kwa nje"** Huu ni msisitizo juu ya thamani ya ndani ya mwamini, na sio zuio dhidi ya kujipamba kwa nje. Kujipamba kwa nje kulikotengenezwa na mwanadamu kwaweza kuwa tatizo kama kutakuwa kwa ndani na kiburi na kuuainisha moyo mwovu (kama vile Isa. 3:18-24). Namna mtu anavyovaa hufanya nafasi ndani ya moyo (kama vile 1 Pet. 3:4).
Neno "kujipamba" ni utumiaji wa kipekee wa neno, *kosmos* (muundo wa kitenzi katika 1 Pet. 3:5). Utumiaji huu ndipo tunapata neno la Kiingereza "kipodozi."

◙ **"kusuka nywele, kujitia dhahabu,au kuvalia mavazi"** Haya yote yanarejelea kwenye ughali na nywele zilizotengenezwa kwa gharama na mitindo ya mavazi ya wanawake kipindi cha Wagiriki-Warumi cha karne ya kwanza. Waamini hawapaswi kutamani au kuiga tama hii kwa ajili ya kukubalika kijamii na kukupima kijamii kuliko simamia kwenye mapambo ya nje. Hii haimaanishi tuvae vibaya, lakini kuwa mwamini anapaswa avae kwa namna ambayo atakubalika kijamii hasa kutokana na utamaduni wake na wakati, lakini usisababishe kuvuta usikivu toka kwao.

**3:4 "utu wa moyoni"** Hili linarejelea kwa Yule mtu mpya baada ya wokovu. Agano Jipya limekwisha toa moyo mpya na roho mpya (kama vile Ezek. 36:22-38). Kwa ajili ya "moyo" angalia Mada Maalum katika Marko 2:6.

◙ **"mapambo yasiyoharibika"** Petro ametumia neno hili kwa ajili ya (1) urithi wa Mungu wa milele, ambao huulinda kwa ajili ya waamini huko mbinguni (yaani., 1:4) na (2) kwa waamini kuzaliwa upya kwa mbegu isioharibika (yaani.,1:23).Paulo anatumia neno lile lile kwenye ufufuo wetu wa miili mipya katika 1 Kor. 15. Na taji ya waamini isioharibika katika 1 Kor. 9:25.

◙ **"roho ya upole na utulivu"** Neno la kwanza *praus* (unyenyekevu, upole) unamwelezea Yesu katika Mt. 11:29 na 21:5 na kuwatofautisha waamini katika ibada ya kumbariki Kristo (kama vile Mt. 5:5). Pia limetumika katika 1 Pet. 3:15 kuuelezea ushahidi wa mwamini.
Neno la pili , *hēsuchios* au *hēsuchia*, limetumika mra nyingi katika maandiko ya Paulo kuelezea pumziko, amani , na utulivu wa mwamini (kama vile 1 The. 4:11; 2 The. 3:12; 1 Tim. 2:2,11,12).
Kuna utofauti uliotumika kwenye mtindo wa ubadilishaji wa neno (kama vile 1 Pet. 3:3) na tabia tulivu za maisha yaliyokombolewa (kama vile 1 Pet. 3:4).

**3:5 "kuwatii"** Hii ni dhamira ya ujumla ya muktadha huu wote (waamini hutii kwenye mamlaka ya kijamii,1 Pet. 2:13-17; waamini walio watumwa hutii kwa bwana wao, 1 Pet. 2:18-20; Kristo hutii mpango wa Baba, 1 Pet. 2:21-25; wake wanaoamini hutii waume zao, 1 Pet. 3:1-6). Ni maelekezo ya tena ya kuchunguzika toka kwenye anguko la Mwanzo 3. Waamini hawaishi kwa ajili yao wenyewe, bali kwa ajili ya Mungu.

**3:6 "Sara. . .akamwita Bwana"** Huu ni mfano wa Agano la Kale (yaaani., Mwa. 18:12) wa mwanamke mwenye kuishi maisha ya kutii Kiungu.

◙ **"nanyi ni watoto wake"** Watakatifu wa Agano la Kale mara nyingi huwatia moyo waamini (kama vile Ebr. 11). Pia hutumika kuonyesha kuwa waamini hukubaliwa moja kwa moja na Mungu kwa imani kupitia Kristo (kama vile Rum. 2:28-29;4:11; Gal. 3:7,9). Sisi ni wa familia ya imani ya Ibrahimu na Sara. Sisi ni watu wapya wa Mungu.
Waisraeli wapya wa imani (kama vile Gal. 6:16; 1 Pet. 2:5,9).

◙ **"mfanyapo mema"** Angalia kumbukumbu katika 1 Pet. 2:14. Kipengere cha kimasharti ("ikiwa") kilichoelezewa katika tafasiri ya Kiingereza (NASB, NKJV, TEV) hakiko katika andiko la Kiyunani, lakini kimedokezwa. Maisha ya imani yana tabia zenye kuchunguzika.

◙ **"wala hamkutishwa kwa hofu yeyote"** Hii ni tabia nyingine ya maisha ya imani (kama vile 1 Pet.3:6,14). Hili laweza kuwa dokezo kwenye Mith. 3:25 na ukweli wa Zab. 23:4; 27:1; na 91:5.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 PETRO 3:7**
**[7] Kadhalika ninyi waume, kaeni na wake zenu kwa akili; na kumpa mke heshima, kama chombo kisicho na nguvu; na kama warithi pamoja wa neema ya uzima, kusudi kuomba kwenu kusizuiliwe.**

**3:7 "Ninyi waume"** Sehemu hii kwa waume wanao amini ni fupi zaidi kuliko kile kilichoelezewa kwa wake wanaoamini; hata hivyo, unaaksi mlinganyo chanya wa moja kwa moja kwa ajil;I ya siku ya Petro, zaidi kama Paulo
(kama vile Efe. 5:21-31).

◙ **"kwa akili"** Hili lingaliweza kurejelea kwenye (1) ukweli wa maandiko (yaani., Mwa. 1:26-27; 2:18-25; Gal. 3:28) au (2) tukiwazia maumbo ya kike yenye muonekano wa kipekee (angalia kumbukumbu hapo chini).

◙ **"chombo dhaifu"** Hii inamaanisha kimwili (kama vile Ayubu 4:19; 10:9; 33:6; 2 Kor. 4:7), na sio kiroho au kisomi (kama vile Gal. 3:28). Baadhi ya watoa maoni wanalihusianisha na masuala ya kijamii. Neno "chombo" cha aina ile ile chaweza kutumika katika 1 The. 4:4 kama rejea kwa mke wa mtu (au nahau yenye kuelezea roho ya ndani
kwenye mwili ulitengenezwa kwa udongo , kama vile Mwa. 2:7; 3:19).

◙ **"kama warithi pamoja na neema ya uzima"** Hili linaaksi thamani ya kiroho (yaani., warithi wenza, kama vile 1 Pet. 1:4-5) wa mwanamke na mwanaume (kama vile Mwa. 1:27; 2:18; Gal. 3:28). Kwa namna nyingine hata sasa wokovu unaondoa madhara ya anguko (kama vile Mwa. 3:16) na kurejesha ukomavu kati ya mwanaume na
mwanamke wa Mwanzo 1-2.

◙ **"kusudi kuomba kwenu kusizuiliwe"** Ni namna gani wenza wanaoamini hutendea mwenzake ndicho kinachoathiri uhusiano na Mungu (kama vile 1 Kor. 7:5).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 PETRO 3:8-12**
**[8] Neno la mwisho ni hili; mwe na nia moja, wenye kuhurumiana, wenye kupendana kama ndugu, wasikitikivu, wanyenyekevu; [9] watu wasiolipa baya kwa baya, au laumu kwa laumu; bali wenye kubariki; kwa sababu hayo ndiyo mliyoitiwa ili mrithi baraka. [10] Kwa maana, Atakaye kupenda maisha, Na kuona siku njema, Auzuie ulimi wake usinene mabaya, Na midomo yake isiseme hila. [11] Na aache mabaya, atende mema; Atafute amani, aifuate sana. [12] Kwa kuwa macho ya Bwana huwaelekea wenye haki, Na masikio yake husikiliza maombi yao; Bali uso wa Bwana ni juu ya watenda mabaya.**

**3:8**

| | |
|---|---|
| **NSB** | **"kwa kuhitimisha"** |
| **NKJB, NRSV** | |
| **TEV** | **"Hatimaye"** |
| **NJB** | **"Kuhitimsha hili"** |

Hii ni nahau ya Kiyunani (“mwisho") lenye kumaanisha "kuhitimisha," sio waraka wote, lakini kwenye muktadha huu juu ya kutii (kama vile 1 Pet. 2:13-17,18-25; 3:1-7,8-22).

◙ **"mueni"** Hili linaambiwa kwa jamii nzima yenye imani. Hapana kitenzi kwenye orodha hii ya dhana ya kutiwa moyo.

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"kupendana"** |
| **NKJV** | **"nia moja"** |
| **NRSV** | **"kuhurumiana"** |
| **TEV** | **"wenye mwelekeo mmoja"** |
| **NJB** | **"wenye kusikilizana"** |

Hili kwa maana iliyo wazi ni ambani ya neno *homos* (moja au la aina ile ile) na *phrēn* (fikra au tafakuri). Dhana ya aina ile ile ni ya kutia moyo katika Yohana 17:20-23; Rum. 12:16; Fil. 1:27 na 2:2.

**NASB, NJB "wenye kuhurumiana"**
**NKJV "mkihurumiana ninyi kwa ninyi"**
**NRSV "huruma"**
**TEV "mkiwa na nia moja"**

Hii kwa maana iliyo wazi ni ambatani ya neno *sun* (ikiwa) na *paschō* (kuteseka). Tunapata neno la Kiingereza "huruma" toka kwenye neno ambani la Kiyunani. Kipindi cha mateso na majaribu hili ni la muhimu, kama tabia zingine zilizokwisha tajwa katika 1 Pet. 3:8.

**NASB "mkipendana kidugu"**
**NKJV "mkipendana kama ndugu"**
**NRSV "mkipendana ninyi kwa ninyi"**
**TEV "mkipendana ninyi kwa ninyi"**
**NJB "mkipendana kama ndugu"**

Hii kwa maana iliyo wazi ni ambani ya neno *philos* (upendo) na *adelphos* (ndugu). Haya ni, matumizi mapana ya neno ndugu. Yumkini namna nzuri ya kulielezea hili ni "kuonyesha upendo wa kidugu kwa ajili ya waamini wote"(kama vile Rum. 12:10; 1The. 4:9). Hili linaaksi amri ya Yesu katika Yohana 13:34; 1 Yohana 3:23; 4:7-8,11-12,19-21. Katika lugha ya Koine,huko Uyunani *philos* na *agapē* mara nyingi yalikuwa ni maneno yenye kuendana
(linganisha Yohana 3:35 na 5:20).

**NASB "mwenye huruma"**
**NKJV "mpole"**
**NRSV "moyo wa upole"**
**TEV "uwe mweme"**
**NJB "kuwa na huruma"**

Hii ni ambatani ya neno *eu* (zuri) na *splagchnon* (viungo vya ndani, matumbo). Watu wa kale waliamini kuwa utumbo wa chini (kama vile Mdo. 1:18) ilikuwa sehemu ya hisia (kama vile Luka 1:28; 2 Kor. 6:12; Fil. 1:8). Huu mwito ambatani juu ya waamini kuwa na "fikra nzuri" dhidi ya mwingine (kama vile Efe. 4:32).

**NASB "moyo wa unyenyekevu"**
**NKJV "heshima"**
**NRSV "mawazo ya unyenyekevu"**
**TEV "wanyenyekevu"**
**NJB "mwenye staha"**

Hii ni ambatani ya neno *tapeinos* (unyenyekevu) na *phrēn* (kumbukumbu). Limetumika katika Mdo.20:19; Efe. 4:2 na Fil. 2:3. Hii kipekee ni maadili ya Kikristo. Inamaanisha kinyume cha madai binafsi na kiburi binafsi.

**3:9 "wasiolipa baya kwa baya"** Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo iliyotumika kama shurutishi. Hili linarejelea kwenye msamaha wa kweli (kama vile Mith. 17:13, 20:22; Rum. 12:17, 1 The. 5:15). Kumbuka kuwa 1 Petro imeandikwa kwa waamini wenye dhiki na mateso, lakini lazima tuitikie kama Kristo alivyoitika kama tendo lisilofaa.

◙ **"laumu kwa laumu"** Hili linaaksi maisha ya Yesu (kama vile 1 Pet. 2:23).

◙ **"bali wenye kubariki"** Hii ni kauli nyingine tendaji endelevu ya wakati uliopo iliyotumika kama kauli shurutishi. Kwa maana iliyo wazi inamaanisha "kubariki" au "kusifu" in English (kama vile Mt. 5:10,12,44, 6:14-15; Luka 6:28;

Rum. 12:143; 1 Kor. 4:12).

**3:9 "kwa sababu hayo ndiyo mlioitiwa"** Hakika huu ni ukweli ule ule ulioelezewa katika 1 Pet. 2:21. Mateso, kama ulivyo mfano wa Yesu, ni namna ya ukomavu wa mwamini (kama vile Ebr. 5:8)na ushuhuda (kama vile 1 Pet.3:15).

◙ **"ili mrithi baraka"** Hili linaaksi maneno ya Yesu katika Mt. 5:44 na Luka 6:28. Urithi wa mwamini umekuwa ni dhamira ya mwamini inayojirudia (kama vile 1 Pet. 1:4-5; 3:7,9). Sisi tu wanafamilia tukiwa na Mungu na warithi wenza wakiwa na Yesu (kama vile Rum. 8:17).

**3:10-12** Hii ni nukuu toka Zaburi 34, toka toleo la MT na sio kutoka kwenye tafasiri za maandiko ya kale ya Kiebrania. Zaburi pia inadokeza kwenye

1. 1 Pet. 2:3 – Zab. 34:8 (kama vile Ebr. 6:5)
2. 1 Pet. 2:22 – Zab. 34:13
3. 1 Pet. 3:10 – Zab. 34:12-13
4. 1 Pet. 3:11 – Zab. 34:14 (kama vile Rum. 14:19; Ebr. 12:14)
5. 1 Pet. 3:12 – Zab. 34:15-16

◙ Tambua maonyo matatu.

1. Ulinde ulimi wako kunena maovu (1 Pet. 3:10, angalia MADA MAALUM: LUGHA YA KIBINADAMU katika Marko 7:20)
2. Lazima tuuache uovu (1 Pet. 3:11)
3. Lazima tuitafute amani na kuitenda (1 Pet. 3:11) take

Hii inaonyesha mwitikio wa dhana ya binadamu ya agano la mwamini. Sababu kwa ajili ya matendo ya waamini zimetolewa katika 1 Pet. 3:12:

1. Bwana kupata uchunguzi binafsi dhidi ya wenye haki
2. Bwana huwasikia wenye haki
3. Bwana yu kinyume na walio waovu

Kwenye kitabu cha Zaburi chote neno "Bwana" mwanzoni lilirejelea kwa YHWH, Mungu wa agano la Israeli, mpaka sasa katika muktadha huu linarejelea kwa Yesu, mletaji wa agano jipya (kama ifanyavyo 1:25 na 2:3). Hii ni mbinu ya kawaida la wandishi wa Agano Jipya ili kuuthibitisha Uungu wa Yesu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 PETRO 3:13-22**
**[13] Naye ni nani atakayewadhuru, mkiwa wenye juhudi katika mema? [14] Lakini mjapoteswa kwa sababu ya haki mna heri. Msiogope kutisha kwao, wala msifadhaike; bali mtakaseni Kristo Bwana mioyoni mwenu. [15] Mwe tayari siku zote kumjibu kila mtu awaulizaye habari za tumaini lililo ndani yenu; lakini kwa upole na kwa hofu. [16] Nanyi mwe na dhamiri njema, ili katika neno lile mnalosingiziwa, watahayarishwe wale wautukanao mwenendo wenu mwema katika Kristo. [17] Maana ni afadhali kuteswa kwa kutenda mema, ikiwa ndiyo mapenzi ya Mungu, kuliko kwa kutenda mabaya. [18] Kwa maana Kristo naye aliteswa mara moja kwa ajili ya dhambi, mwenye haki kwa ajili yao wasio haki, ili atulete kwa Mungu; mwili wake akauawa, bali roho yake akahuishwa, [19] ambayo kwa hiyo aliwaendea roho waliokaa kifungoni, akawahubiri; [20] watu wasiotii hapo zamani, uvumilivu wa Mungu ulipokuwa ukingoja, siku za Nuhu, safina ilipokuwa ikitengenezwa; ambamo ndani yake wachache, yaani, watu wanane, waliokoka kwa maji. [21] Mfano wa mambo hayo ni ubatizo, unaowaokoa ninyi pia siku hizi; (siyo kuwekea mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu), kwa kufufuka kwake Yesu Kristo. [22] Naye yupo mkono wa kuume wa Mungu, amekwenda zake mbinguni, malaika na enzi na nguvu zikiisha kutiishwa chini yake.**

**3:13 "Ni nani atakaye wadhuru"** Hili laweza kuwa ni dokezo kwa Zab. 118:6 kwa sababu Zaburi hii imenukuliwa katika1 Pet. 2:7 na 9. Ukweli wa aina ile ile unaelezewa katika Rum. 8:31-34.

Waamini lazima waendelee kukumbushwa kuwa ulimwengu huu sio mahali pao na vitu vilivyomo sio hatma ya kweli! Sisi tu wageni hapa, tunapita hapa tu. Hatupaswi kuogopa (yaani., 1 Pet. 3:14).

Kuna kejeli kuwa wale wote wanaolindwa na Bwana mara nyingi ndio wale wanaoteswa. Kwa kulifahamu hili, kupenda na kumtumikia Mungu hakumlindi mtu toka kwenye tabia zisizofaa, maumivu, hata kifo. Yaweza kuonekana kama

mwovu ameshinda, lakini husubiri, hata katikati ya mateso, mwamini hubarikiwa (kama vile Mt. 5:10-12; Mdo. 5:41).

◙ **"mkiwa wenye juhudi katika mema?"** Hii ni sentensi yenye masharti daraja la tatu yenye kumaanisha tendo muhimu. Waliteseka hasa kwa sababu walikuwa Wakristo (kama vile 1 Pet. 3:14; 2:19; 3:16;4:16). Hata hivyo, tambua tukio lenyewe (yaani., dhamira tegemezi), "moyo kwa ajili ya kutenda yaliyo mema"!

**3:14 "Lakini mjapoteswa"** Hii ni sentensi adimu yenye masharti daraja la nne (hali ya mbali na ukweli), ambao unamaanisha kuwepo na uwezekano, na wala sio kitendo fulani (kama vile 2 Tim. 3:12). Sio kila mwamini kila mahali alikuwa akiteseka. Kamwe mateso na kamwe halijawahi kuwa suluhisho kwa kila Mkristo, lakini kila Mkristo anapaswa kuwa tayari (kama vile 1 Pet. 4:12-16; Yohana 15:20; Mdo. 14:22; Ufu. 8:17)!

◙ **"haki"** Katika muktadha huu waweza kurejelea maisha ya Kiungu au ushuhuda wetu wa maneno kuihusu injili. Angalia Mada Maalum ifuatayo.

## MADA MAALUM: HAKI

"Haki"ni mada muhimu ambayo mwannafunzi wa Biblia yampasa kufanya ni upanuzi binafsi wa kusoma juu ya dhana yenyewe.

Katika Agano la Kale sifa za Mungu zinaelezwa kama "halali" au "haki" (kitenzi, BDB 842, KB 1003; nomino jinsi ya kiume, BDB 841, KB 1004; nomino jinsi ya kike, BDB 842, KB 1006). Neno la Mesopotamia lenyewe linatokana na "mafunjo ya mto" ambayo yalitumika kama chombo cha matengenezo ya utaalamu wa mlalo ulionyooka na uelekeo wa ukuta na ua. Mungu alilichagua neno lililotakiwa kutumika kistiari juu ya asili Yake mwenyewe. Yeye ni ukingo ulionyooka (kiongozi) ambapo vitu vyote vinatathiminiwa toka kwake. Dhana hii inatetea haki ya Mungu pamoja na Haki Yake ya kuhukumu.

Mwanadamu aliumbwa katika mfano wa Mungu (kama vile Mwa. 1:26-27; 5:1,3; 9:6). Mwanadamu aliumbwa kwa ushirika wa Mungu (yaani, Mwa. 3:8). Uumbaji wote ni hatua au mrejesho kwa Mungu na mwingiliano wa wanadamu. Mungu aliutaka uumbaji Wake mkuu, mwanadamu, kumjua Yeye, kumpenda Yeye, kumtumikia Yeye, na kuwa kama Yeye! Uaminifu wa mwanadamu ulipimwa (kama vile Mwanzo 3) na watu hawa wanadoa wa mwanzo walishindwa jaribio. Hii ilileta matokeo ya kuvunjika kwa uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu (kama vile Rum. 5:12-21).

Mungu aliahidi kufanya marekebisho na kurejesha ushirika (kama vile Mwa. 3:15; tazama Mada Maalumu: Mpango wa Wokovu wa Milele wa YHWH). Alifanya hivi kupitia mapenzi Yake mwenyewe na Mwanae. Wanadamu hawawezi kurejesha ahadi iliyovunjwa (kama vile Rum. 1:18-3:20; Ufunuo 5).

Baada ya Anguko,hatua ya kwanza ya Mungu kuuelekea urejesho ilikuwa dhana ya agano lililojikita katika mwaliko Wake na toba ya mwanadamu, imani, mwitikio wa utii (kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:22-38). Kwa sababu ya Maanguko yote, wanadamu huwakuweza kujitenga na tendo (kama vile Rum. 3:21-31; Wagalatia 3). Mungu Pekee ilimbidi kuanzisha upya agano lililokuwa limevunjwa na wanadamu. Alifanya hivi kwa

A. kutangaza haki ya mwanadamu kupitia kazi ya Kristo (yaani, haki ya mahakama)
B. kwa kutoa haki huru kwa mwanadamu kupitia kazi ya Kristo (yaani, haki ya kuzuliwa)
C. kumtoa Roho akaaye ndani ambaye huleta haki (yaani, Ufanano na Kristo, urejeshaji wa mfano wa Mungu) ndani ya mwanadamu
D. kurejesha ushirika wa Bustani ya Edeni (linganisha Mwanzo 1-2 na Ufunuo 21-22)

Hata hivyo, Mungu anahitaji mwitikio wa kimaagano. Mungu hutoa maagizo (yaani, hutoa kwa uhuru, Warumi 5:8; 6:23) lakini yawapasa wanadamu kuitikia na kuendelea kuitika katika

A. Toba
B. Imani
C. Utii kwenye stadi ya maisha
D. Ustahimilivu

Haki, kwa hiyo, ni agano, ni makubaliano kati ya Mungu na uumbaji Wake wa juu, uliyojikita juu ya sifa za Mungu, kazi ya Kristo, na Roho mwezeshaji, ambapo kila mtu kibinafsi anapaswa kuitikia kwa namna ifaavyo.Dhana inaitwa "haki kwa neema kupitia imani" (yaani, Efe. 2:8-9). Dhana inafunuliwa katika Injili, lakini si katika maneno haya. Kimsingi ilielezwa na Paulo, ambaye anatumia neno la Kiyunani "mwenye haki" katika miundo yake mbalimbali zaidi ya mara

100.
Paulo, akiwa mwalimu wa sheria aliyefundishwa, anatumia neno *dikaiosunē* katika maana yake ya Kiebrania ya neno *tsaddiq* lililotumika katika Tafsiri za Maandiko ya Kale ya Kiebrania, na si kutoka katika fasiri ya Kiyunani. Katika maandishi ya Kiyunani neno linamhusu yule ambaye amethibitisha matarajio ya Mungu na jamii (yaani, Nuhu, Ayubu). Katika maana ya Kiebrania mara nyingi limendwa katika maneno ya kimaagano (tazama Mada Maalumu: Agano). YHWH ni haki, maadili, Mungu mwema. Anawataka watu Wake kuwa viumbe vipya ili kwendana na sifa zake. Mwanadamu aliyekombolewa anakuwa kiumbe kipya (kama vile 2 Kor. 5:17; Gal. 6:15). Upya huu unaleta matokeo katika mtindo mpya wa maisha ya Kimungu (kama vile Mathayo 5-7; Gal. 5:22-24; Yakobo; 1 Yohana).Tangu Israeli ilipokuwa katika mfumo wa utawala wa kidini hapakuwepo na maelezo sahihi na ya kinagaubaga kati ya ulimwengu (kanuni za kijamii) na Mungu (mapenzi ya Mungu). Utofauti huu unaelezwa katika maneno ya Kiebrania na Kiyunani kuwa ya kutafsirika katika Kiingereza kama "haki" (yakihusiana na jamii)na "mwenye haki" (ikihusiana na dini).
Injili (habari njema) juu ya Yesu ni kwamba wanadamu walioanguka wamerejesha ushirika na Mungu. Hii limetimizwa kupitia pendo la Baba, huruma, na neema; maisha ya Mwana, kifo, na ufufuo; na kuugua kwa Roho na kielelezo cha injili. Haki ni tendo huru la Mungu, lakini linapaswa kuwa jambo la kimungu (Mtazamo wa Augustine, ambao unaakisi vyote msistizo wa Mabadiliko mapya juu ya uhuru wa injili na msisitizo wa Kanisa Katoriki juu ya maisha yaliyobadilishwa ya upendo na uaminifu). Kwa waleta mabadiliko neno "haki ya Mungu" ni shamilisho milikishi (yaani, tendo la mwanadamu aliyetenda dhambi kukubaliwa na Mungud [utakaso wa mahali], ambapo kwa Wakathoriki ni kiima milikishi, ambapo ni tendo la kuimarika zaidi kama Mungu [utakaso endelevu na uliozoeleka].
Katika mtazamo wangu, Biblia nzima kutoka Mwanzo 4 – Ufunuo 20 ni maandiko yenye kuonyesha urejesho wa ushirika wa Mungu pale Edeni. Biblia inaanza kati ya Mungu na mwanadamu kuleta ushirika na mpangilio wa dunia (kama vile Mwanzo 1-2) na Biblia inaridhia mpangilio huo huo (kama vile Ufunuo 21-22). Mfano wa Mungu na kusudi lake vitarejeshwa!
Ili kuthibitisha mjadala wa hapo juu andika vifungu vilivyochguliwa vya Agano Jipya vyenye vielelezo vya kundi la neno la Kiyunani.

A. Mungu ni haki (mara kwa mara imeunganishwa kwa Mungu kama Hakimu)
   1. Warumi 3:26
   2. 2 Wathesalonike 1:5-6
   3. 2 Timotheo 4:8
   4. Ufunuo 16:5
B. Yesu ni haki
   1. Matendo 3:14; 7:52; 22:14 (jina la Masihi)
   2. Mathayo 27:19
   3. 1 Yohana 2:1,29; 3:7
C. Mapenzi ya Mungu kwa uumbaji Wakeni ya haki.
   1. Mambo ya Walawi 19:2
   2. Mathayo 5:48 (kama vile 5:17-20)
D. Kusudi la Mungu kutoa na kutoa haki
   1. Warumi 3:21-31
   2. Warumi 4
   3. Warumi 5:6-11
   4. Wagalatia 3:6-14
   5. Iliyotolewa na Mungu
      a. Warumi 3:24; 6:23
      b. 1 Wakorintho 1:30
      c. Waefeso 2:8-9
   6. Iliyopokelewa kwa imani
      a. Warumi 1:17; 3:22,26; 4:3,5,13; 9:30; 10:4,6,10
      b. 2 Wakorintho 5:7,21
   7. kupitia matendo ya Mwana
      a. Warumi 5:21

b. 2 Wakorintho 5:21
c. Wafilipi 2:6-11

E. Mapenzi ya Mungu ni kwamba wafuasi Wake wawe wenye haki
1. Mathayo 5:3-48; 7:24-27
2. Warumi 2:13; 5:1-5; 6:1-23
3. Waefeso 1:4; 2:10
4. 1 Timotheo 6:11
5. 2 Timotheo 2:22; 3:16
6. 1 Yohana3:7
7. 1 Petro 2:24

F. Mungu ataihukumu dunia kwa haki
1. Matendo 17:31
2. 2 Timotheo 4:8

Haki ni atabia ya Mungu, iliyotolewa huru kwa wanadamu wenye dhambi kupitia Kristo. Hilo ni

A. agizo la Mungu
B. zawadi ya Mungu
C. tendo la Kristo

Lakini pia ni tendo la kuwa mwenye haki ambapo ni lazima kuwa na juhudi, uaminifu na kuishikilia, kwamba siku moja itatimizwa katika Ujio wa Pili. Ushirika na Mungu unarejeshwa katika wokovu lakini unaendelea katika maisha mazima ili kukutana naye ana kwa ana (kama vile 1 Yohana 3:2) katika kifo au ujio wa pili!

Hapa kuna dondoo nzuri ya kuhitimisha mjadala huu. Imechukuliwa kutoka Kamusi ya Paulo na barua zake kutoka IVP "Calvin, zaidi sana kuliko Luther, inasistiza kipengele cha uhusiano wa haki ya Mungu. Mtazamo wa Luther juu ya haki ya Mungu unaonekana kuwa dhana ya kuwa huru. Calvin anasisitiza asili ya ajabu ya mawasiliano au kutuarifu juu ya haki ya Mungu" (uk. 834).

Kwangu mimi uhusiano wa waumini na Mungu una vipengele vitatu.

A. injili ni mtu (msistizo wa Kanisa la Mashariki na Calvin)
B. injili ni ukweli (msisitizo wa Augustine na Luther)
C. injili ni maisha yaliobadilishwa (msistizo wa Katoliki)

Yote ni sawa na yanapaswa kuungamanishwa kwa pamoja kwa ajili ya afya, sauti, Ukristo wa kibiblia. Ikiwa ye yote anasisitizwa sana au anapunguza thamani, matatizo yanatokea.

Yatupasa kumkaribisha Yesu!

Yatupasa kuiamini injili!

Yatupasa kuwa na ushawishi juu ya ufanano wa Kristo!

◙ **"mna heri"** Hili ni neno tofauti toka 1 Pet. 3:9. Hili ni neno lililotumika katika ibada ya kubarikiwa kwa Kristo juu ya Mlima (kama vile Mt. 5:10-12). Waamini wanahusianishwa na manabii wa agano la kale kama nuru ya Mungu na ufunuo kwenye ulimwengu uliopotea. Kwa ushuhuda wetu hata katikati ya mateso, asiyeamini aweza kugeuka na kumsifu Mungu (kama vile 1 Pet. 3:1,8-9).

◙ **"msiogope kutisha kwao"** Hili ni dokezo kwa Isa. 8:12-13 (angalia dhana ya ufanano katika Isa. 50:9;54:17; Rum. 8:31-38). Kwa maana iliyo wazi ina maana ya"usiogope hofu zao." Kifungu hiki chaweza kueleweka katika namna mbili: (1) hofu ya Mungu ambayo wenye kuteseka huipata au (2) ile hofu ambayo huiweka kwa wengine. Kukosekana kwa hofu ni tabia ya wana wa Mungu (kama vile 1 Pet. 3:6).

**3:15 "bali mtakaseni"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu, ambayo hudokeza kitendo cha maamuzi kilichopita cha kumtenga mtu kwa ajili ya matumizi ya Mungu (hili pia laweza kuaksi Isa. 8:14, ambayo ina neno "madhabahu"). Waamini wanapaswa kumtakasa Kristo ndani ya mioyo yao kama Kristo alivyojitakasa Mwenyewe kwa ajili yao (kama vile Yohana 17:19).

Tambua kuwa katika 1 The. 5:23 ni Mungu ambaye huwatakasa waamini. Sasa waamini wanalazimika kujitakasa wenyewe. Hili ni agano lenye fumbo la imani ya kibiblia (linganisha Ezek. 18:31 with 36:26-27). Mungu ni Mkuu, na bado wanadamu pia wako huru na wanapaswa kuutenda huo uhuru katika mapenzi ya Mungu. Ni namna gani tunaweza kumtakasa Kristo?

1. Kwa upendo wetu kwa wengine (kama vile 1 Pet. 3:8-9)
2. Kwa maisha yetu (kama vile 1 Pet. 3:13-14)
3. Kwa ushuhuda wa maneno yetu (kama vile 1 Pet. 3:15)

◙ **"Kristo Bwana"** Toleo la King James lina "Bwana Mungu," ambalo linaaksi Isa. 8:12-13, ambayo ina "Bwana wa vita," wakati 1 Pet. 3:14 ni andiko la Kimasihi. Hata hivyo, machapisho ya kale ya Kiyunani $P^{72}$, א, A, B, na C yana "Kristo kama Bwana," ambalo linaufaa huu muktadha vizuri.

◙ **"mioyoni mwenu"** Neno"Moyo" ni lahaja ya Agano la Kale yenye kurejelea mtu kamili. Angalia MADA MAALUM: MOYO katika Marko 2:6.

◙ **"muwe tayari siku zote kumjibu"** Hili ni neno la Kiyunani *apologia*, ambalo ni neno ambani la *apo* (kutoka) na *logos* (neno). Linarejelea kwenye utetezi wa kisheria kwenye chumba cha mahakama (kama vile Mdo. 19:33; 22:1; 25:16;26:1,2,24). Hili andiko mara nyingi hutumika kuwatia moyo waamini kuwa mashuhuda wa uinjilisti, ambacho ndiyo kitu kinachohitajika, lakini katika muktadha huu hili linarejelea majaribu binafsi au mahojiano. Tambua kuwa ni muhimu kwa ajili ya waamini wote ili wajiandae, kuiwakilisha imani yao katika Kristo kimantiki, ikiwa kwa ajili ya baraza au kwa ajili ya mtu wa karibu.kila mwamini anapaswa kuwa tayari kwa ajili ya ushahidi wa maneno!

◙ **"kwa ajili ya tumaini lililomo ndani yenu"** Neno tumaini hapa ni neno la ujumla kwa ajili ya injili na utimilifu ujao. Waamini sasa wanaishi kwa namna ya maisha ya Kiungu kwa sababu ya uhakika wao katika ahadi za Kristo na kurudi kwake.

## MADA MAALUM: TUMAINI

Paulo alilitumia neno hili mara nyingi kwa namna tofauti lakini katika maana zinazoshabihiana. Mara nyingi lilihusiana na utimilifu wa imani ya waamini (mfano., 1 Tim. 1:1). Hili laweza kuellezewa kama utukufu, maisha ya milele, hatma ya wokovu, ujio wa mara ya pili, n.k. Utimilifu huu unajulikana, bali sula la muda ni mbeleni na halijulikani. Tumaini mara nyingi lilihusiana na "imani" na "upendo" (kama vile 1 Kor. 13:13; 1 The. 1:3; 2 The. 2:16). Orodha ya muda ya baadhi ya matumizi ya Paulo ni:

1. Ujio wa mara ya pili, Gal. 5:5; Efe. 1:18; 4:4; Tit. 2:13
2. Yesu ni tumaini letu, 1 Tim. 1:1 (Mungu ni tumaini letu, 1 Tim. 5:5; 1 Pet. 3:5)
3. Waamini kuwasilishwa mbele ya Mungu, Kol. 1:22-23; 1 The. 2:19
4. Tumaini likewekwa mbinguni, Kol. 1:5
5. Imani katika injili, Kol. 1:23; 1 The. 2:19
6. Hatma ya wokovu, Kol. 1:5; 1 The. 4:13; 5:8
7. Utukufu wa Mungu, Rum. 5:2, 2 Kor. 3:12; Kol. 1:27
8. Wokovu wa watu wa mataifakupitia Kristo, Kol. 1:27
9. Uhakika wa wokovu, 1 The. 5:8
10. Maisha ya milele, Tit. 1:2; 3:7
11. matokeo ya ukomavu wa Mkristo, Rum. 5:2-5
12. ukombozi wa uumbaji wote, Rum. 8:20-22
13. kukubali utimilifu, Rum. 8:23-25
14. wadhifa wa Mungu, Rum. 15:13
15. shauku ya Paulo kwa waamini, 2 Kor. 1:7
16. agano la Kale kama mwongozo wa waamini wa Agano Jipya, Rum. 15:4

◙ **"kwa upole na kwa hofu"** Neno la kwanza limetumika kwa wanawake katika 1 Pet. 3:4, ambapo linaelezea mwenendo unaompendeza Mungu. Hii ni kweli, sio tu kwa mahusiano ya nyumbani, lakini pia mahusiano ya mwamini kwa wengine, hata kwa wale wanaochochea adhabu (kama vile 2 Tim. 2:25).
Neno la pili linatumika mara nyingi katika 1 Petro na pia huaksi siku ya dhiki na utisho (kama vile 1 Pet. 1:17; 2:17,18; 3:2,15). Tunapaswa kumheshimu Mungu na kwa sababu ya hili, hesshima hata kwa mabwana wasio amini, waume, na watesaji, kama tushuhudiavyo nguvu Zake na ufalme.

**3:16** Kuna baadhi ya mkanganyiko pale 1 Pet. 3:16 inapoanzia. Tolea la NASB na NKJV linaanzia hapa na toleo la UBS4, NRSV, TEV, na NJB linaanza na kifungu mwanzoni.

◙ **"mueni na dhamira njema"** Hii ni kauli tendaji yenye hali ya kuendelea ya wakati uliopo iliyotumika kama kauli shurutishi. Hapana mlandano wa neno la Kiyunani la Agano la Kale la neno "dhamiri" isipokuwa neno la Kiebrania "ungama" lidokeze maarifa binafsi na mienendo yake. Mwanzoni kabisa neno la Kiyunani lilirejelea kwenye ufahamu unaohusiana na milango mitano ya fahamu. Lilikuja kutumika kwenye fahamu za ndani (kama vile Rum. 2:15). Paulo anatumia hili neno mara mbili katika majaribu yake katika kitabu cha Matendo (kama vile Mdo. 23:1 na 24:16). Linarejelea kwenye ufahamu wake kuwa kwa ufahamu wake hajawahi kukiuka shughuli yeyote
iliyotarajiwa dhidi ya Mungu (kama vile 1 Kor. 4:4).
Dhamiri ni uelewa endelevu wa mienendo ya mwamini na matendo yaliyoegama juu ya

1. Mtizamo wa ulimwengu Kibiblia
2. Roho aishie ndani mwetu
3. Maarifa ya neno la Mungu
4. Mapokezi binafsi ya injili

Petro ameyatumia maelezo haya mara tatu, 1 Pet. 2:19; 3:16 na 21. Hiki ndicho kile wale walioshika sana mambo ya dini hawezi kukifanya, lakini injili inaweza.

◙ **"ili katika neno lile mnalosingiziwa, watahayarishwe wale wautukanao mwenendo wenu mwema katika Kristo"** Angalia maelezo katika 1 Pet. 2:12 na 2:15.

**3:17 "ikiwa ndiyo mapenzi ya Mungu"** Hii ni sentensi adimu yenye masharti daraja la nne kama ilivyo katika 1 Pet. 3:14. Petro ameendlea kulielezea tukio, lakini sio kwa uhakika, la mateso na dhiki (kama vile 1 Pet. 1:6; 2:15;3:17; 4:14).

**3:18-22** Richard N. Longenecker, *Biblical Exegesis In the Apostolic Period*, kur. 69, 172, anadai kuwa mistari hii ni kutoka kwenye nyimbo za ubatizo. Grant Osborne, *The Hermeneutical Spiral*, anaifikiria 1 Pet. 3:18 kuwa ni ya kiushairi (hakuna tafasiri zilizotumika katika fasihi hii iliyotolewa kama ushairi). Kama ni wimbo wa dini au ushairi,
hivyo haipaswi "kuhimizwa" kwa ajili ya mafundisho!

**3:18 "Kristo naye alikufa"** Hiki kifungu kinatumika katika tafasiri ya maandiko ya agano la kale la Kiebrania kwa ajili ya "ondoleo la dhambi" (kama vile Law.5:7, 6:30; Isaya 53; 2 Kor. 5:21). Kifungu hiki kinazungumza juu ya kifo mbadala cha Yesu, kama ilivyofanyika katika 2:22-24. Kuna sehemu mbili za kifungu hiki ambazo zinatofautiana na Kiyunani.

1. "Yesu alikufa" (kama vile toleo la NASB, TEV, NJB). Hili linapatikana katika machapisho ya Kiyunani $P^{72}$, א, A, B, na C. maandishi mengine ya herufi kubwa ya Kiyunani yana neno "aliteseka" (NKJV, NRSV, yaani., MSS B, K na P). Neno"aliteseka" linafaa kote kwenye muktadha na misamiati ya Petro (anatumia neno "kuteseka" mara kumi na moja), lakini kama lilikuwa ni la asili kwa nini mwandishi alibadilishe na kuandika "alikufa"?
2. "kwa ajili ya dhambi." Kuna tofauti zaidi ya saba ya hiki kipengele cha huu mstari. Mengi yao yameshirikisha neno "kwa ajili yetu" au "kwa niaba yetu." Tatizo ni kwamba kihusishi cha Kiyunani *peri* kimetumika katika uhusiano wa dhambi badala ya matarajio zaidi ya neno *huper*.

◙**"mara moja kwa ajili ya wote"** Hii ni dhamira ya kitabu cha Kiebrania (kama vile Rum. 6:10; Ebr. 7:17; 9:12,18,26,28;10:10). Kristo ni dhabihu kamili, ya thamani, iliyotolewa mara moja kwa ajili ya dhambi!

◙ **"wenye haki kwa ajili ya wasio na haki"** Hili lawezakuwa ni dokezo kwa Isa. 53:11-12 na laweza kutafasiriwa "mwenye haki kwa ajili ya wasio na haki" (kama vile NRSV). Neno "mwenye haki" lingeweza kuwa ni jina la Yesu kwenye kanisa la mwanzo (kama vile Mdo.3:14; 7:52; 1 Yohana 2:1,29; 3:7). Husisitiza maisha yake yasio na dhambi (kama vile 1 Pet. 1:19; 2:22) aliyoyatoa kwa ajili ya wenye dhambi (kama vile 1 Pet. 2:24).

◙ **"ili kwamba"** Hiki ni kitenzijina (*hina*).

◙ **"ili atulete kwa Mungu"** Hili linarejelea kwenye "ufikikaji" au "utangulizi" kwenye Uungu (kama vile Rum. 5:2; Efe. 2:18;3:12). Kifo cha Yesu kilirejesha uhusiano na Mungu uliopotea kwenye anguko. Taswira ya Mungu kwa mwanadamu imerejeshwa kupitia Kristo. Waamini wana nafasi ya mahasiano ya ndani na Mungu kama alivyokuwa Adamu na Hawa walivyokuwa bustanini kabla ya anguko katika Mwanzo 3.

◙ **"mwili wake ukauwawa, bali roho yake ikahuishwa"** kuna utofauti (dhana ya ufanano) kati ya maisha ya kimwili ya Yesu (kama vile 1 Pet. 4:1) na maisha ya Yake ya kiroho (kama vile 1 Pet. 4:6; 1 Kor.15:45). Ukweli huu unaaksiwa kwenye mafundisho ya mwanzo au nyimbo zilizoandikwa katika 1 Tim. 3:16.
Vifungu hivi vyote ni kauli tendwa zenye hali ya kuendelea ya wakati uliopita usiotimilifu, ambavyo vinadokeza matukio ya kihistoria (kusulubiwa na kufufuka, kama vile Rum. 1:3-4) yaliyotendeka na jamii iliyoko nje (yaani., Baba au Roho Mtakatifu). Ni vigumu kuamua katika kifungu hiki ikiwa neno "roho" liwe katika herufi kubwa (yaani., Roho Mtakatifu) au la (yaani., roho ya Yesu ya kibinadamu). Napendelea linalofuata (kama afanyavyo A. T. Robertson), lakini F. F. Bruce anapendelea la mwanzo.

◙ **"akawahubiri"** Hili ni neno la Kiyunani *kērussō*, ambalo linamaanisha kutangaza au kuzungumza kwa uwazi. Katika kifungu kinachofanana, 4:6, kitenzi ni *euangelizō*, ambacho kinarejelea kwa pamoja kuihubiri injili. Haijulikani ikiwa utofauti lazima utolewe kwenye muktadha kati ya yale maneno mawili (kama vile Marko 5:20; Luka 9:60, ambapo neno *kērussō* limetumika kwenye kutangaza injili). Nafikiri ni yenye ufanano.

◙ **"roho"** Kuna nadharia mbili kuhusiana na hili: (1) waliokufa (4:6; Ebr. 12:23) au (2) malaika waovu (Mwa. 6; 2 Pet. 2:4-5; Yuda 6: I Enoch). Wanadamu hawarejelewi katika kwenye Agano Jipya kama "roho" pasipo wengine waliofuzu (kama vile F. F. Bruce, *answers to Questions*, uk. 128).

◙ **"waliokaa kifungoni"** Kuna vipengele mbalimbali katika muktadha huu ambavyo vinapaswa kuhusiana pamoja kwa namna Fulani Tkuweza kuamua ni kipi Petro alikuwa akikirejelea:

1. Yesu alikuwa "katika roho" (1 Pet. 3:18)
2. Yesu alizihubiri zile roho zilizokuwa katika kifungo (1 Pet. 3:19)
3. Roho zilikuwa zenye ukaidi siku zile za Nuhu (1 Pet. 3:20)

Pale haya yote yanapolinganishwa, ujumbe kwa malaika walioanguka wa Mwanzo 6 au binadamu wa siku za Nuhu waliozama majini zinaonekana kuwa za kiuchaguzi katika muktadha huu. Siku za Nuhu pia zimetajwa katika 2 Pet. 2:4-5, zikiendana na Sodoma na Gomora (kama vile 2 Pet. 2:6). Katika Yuda, malaika waasi (kama vile Yuda 6) na Sodoma na Gomora (kama vile Yuda 7) pia zimehusianishwa pamoja.
Haifahamiki toka kwenye muktadha mpana kwa nini Petro hata kulitaja somo hili ikiwa atatumia mafuriko kama mfanano wa ubatizo (yaani., kuokolewa kwa maji, kama vile 1 Pet. 3:20).
Hoja kuu mbili za mabishano juu ya utafasiri wa kifungu hiki ni (1) lini na (2) maudhui ya Yesu kulifundisha hili ni?

1. Uwepo wa Kristo kabla uliohubiriwa na Nuhu (kama vile 1 Pet. 1:11 ambapo Roho wa Kristo alihubiri kupitia wandishi wa Agano la Kale) kwa watu wa kipindi chake, sasa wako kifungoni (Augustine)
2. Kristo, kati ya kifo na ufufuko, akalihubiri kwa watu waliofungwa wa siku za Nuhu
    a. laana i juu yao
    b. wokovu u kwao (Clement of Alexandria)
    c. mambo mzuri yako kwa Nuhu na familia yake (Paradiso) mbele yao (in *Tartarus*)
3. Kristo, kati ya mauti na ufufuo, alihubiri kwa
    a. malaika walioenda na binti za wanadamu na kuzaa nao (kama vile Mwa. 6:1-2)

b. wana wa Mungu, wana wa wanadamu wa Mwa. 6:4 (angalia Mada Maalum katika Mwanzo 6 kwenye mtandao www.freebiblecommentary.org). Maudhui ya ujumbe yalikuwa ni hukumu yao na ushindi wake. I Enoch anasema wana wa Mungu/binti za wanadamu ni mapepo ya Agano Jipya.

4. Kristo kama Masihi mshindi alikuja toka mbinguni (yaani, viwango vya kimalaika vya wenye ujuzi au mbingu saba za walimu wa dini ya Kiyahudi, kama vile 1 Pet. 3:22; Efe. 4:9). II Enoch 7:1-5 inasema kuwa malaika walioanguka wamefungwa kwenye mbingu ya pili. Yeye, kwa tendo hili, alitangaza ushindi Wake juu ya ulimwengu wa kimalaika (yaani., upinzani wote wa kiroho, the *Jerome Bible Commentary*, uk. 367). Naupenda uchaguzi huu katika muktadha huu.

## MADA MAALUM: WAFU WAKO WAPI?

I. Agano la Kale
   A. Watu wote wanakwenda shimoni (*sheol)* (hakuna mizizi yenye chanzo kimoja cha neno na asili ya neno lenyewe haijulikani, BDB 982, KB 1368), ambayo ndiyo ilikuwa njia ya kurejerea mahali pale wafu wanaishi au kaburi, hasa hasa katika kitabu cha Ayubu na Isaya. Katika Agano la Kale ilikuwa ni kivuri, utambuzi, lakini maisha yasiyo na furaha (kama vile Ayubu 10:21-22; 38:17)
   B. Tabia za shimoni (*sheol*)
      1. Inahusiana na hukumu ya Mungu (moto), kumb.32:22
      2. Gereza lenye vizuizi, Ayubu 38:17; Zab. 9:13; 107:18
      3. eneo ambalo huwezi rudi tena, Ayu. 7:9 (sifa ya mkazi wa Akkad kwa ajili ya umauti)
      4. Eneo/ulimwengu wa giza, Ayu. 10:21-22; 17:13; 18:18
      5. Mahali penye utulivu, Zab.. 28:1; 31:17; 94:17; 115:17; Isa. 47:5
      6. panahusiana na mateso hata kabla ya siku ya hukumu, Zab. 18:4-5
      7. panahusiana na *utelekezaj*i (maangamizo; angalia Mada Maalumu: *Kutelekezwa*. . .*Apollyon*), ambapo pia Mungu yupo, Ayu. 26:6; Zab.. 139:8; Amo. 9:2
      8. panahusiana na "shimo lefu" (kaburi), Zab.16:10; 88:3-4; Isa. 14:15; Ezek. 31:15-17
      9. waovu hushuka ndani ya shimo la *sheol*,Hes. 16:30,33; Ayu. 7:9; Zab.. 55:15
      10. mara nyingi hujibadilisha kama mnyama mwenye mdomo mkubwa, Hes. 16:30; Mith. 1:12; Isa. 5:14; Hab. 2:5
      11. kule watu huitwa *Repha'im* (yaani., "roho za mauti"), Ayu. 26:5; Mith. 2:18; 21:16; 26:14 Isa. 14:9-11)
      12. Hata hivyo, YHWH yupo hata hapa, Ayu. 26:6; Zab.. 139:8; Mithali. 15:11

II. Agano Jipya
   A. Kwa Kiebrania *Sheol* limetafasiliwa kwa Kiyunani kama Kuzimu (ulimwengu usio onekana)
   B. Tabia za kuzimu (nyingi zinafanana kama za *Sheo*l)
      1. Anarejerea mauti, Mt. 16:18
      2. Imehusianishwa na mauti, Ufu. 1:18; 6:8; 20:13-14
      3. mara nyingi panafanana na mahali pa mateso ya milele (Gehenna), Mt. 11:23 (nukuu toka agano la kale); Luk 10:15; 16:23-24
      4. mara nyingi inafanana na kuwekwa kaburini, Lk. 16:23
   C. Yumkini imegawanywa na (walimu wa dini ya Kiyahudi)
      1. Sehemu ya watakatifu iitwayo Paradiso (ki-ukweli ni jina lingine la Mbinguni, kama vile. 2 Kor. 12:4; Ufu. 2:7), Lk. 23:43
      2. Sehemu ya waovu iitwayo "kwenye vifungo vya giza",iliyoko chini kabisa ya kuzimu, 2 Petr 2:4, mahali palipowekwa kwa ajili ya malaika waovu (k.v Mwanzo 6; I Enoch). Inahusiana na kutupwa "shimoni" Luk. 8:31; Rum. 10:7; Ufu. 9:1-2,11; 11:7; 17:18; 20:1,3
   *D. Gehenna*
      1. inaangazia kwenye kifungu cha agano la kale, "bonde la wana wa Hinnom (kusini mwa Yerusalem). Palikuwa ni mahali Wafoenike walipoichoma miungu ya , Molech (BDB 574, KB 591), ilikuwa inaabudiwa wakati wa kuwadhabihu watoto (kama vile 2 Fal. 16:3; 21:6; 2 Nya. 28:3; 33:6), ambavyo ilikuwa imekataliwa katika Law. 18:21; 20:2-5.
      2. Yeremia alibadili toka sehemu ya ibada ya wapagani kuwa mahali pa hukumu ya YWHW (Kama vile

Yer. 7:32; 19:6-7). Ikajakuwa mahali pa hukumu kali, ya milele katika I Enoch 90:26-27 na Sib. 1:103.

3. Wayahudi wa enzi ya Yesu waliogopeshwa na ushiriki wa wazee wao katika ibada ya kipagani kwa kuwadhabihu watoto, kwamba waliigeuza sehemu hii kuwa sehemu ya kutupa takataka kwa ajili ya Jerusalemu. Mingi ya misemo ya Yesu kwa ajili ya hukumu ya milele ilitokana na sehemu hii iliyojaza (moto, moshi, minyoo, funza,kama vile Mk 9:44,46). Neno Gehenna limetumiwa na Yesu tu (hasa katika Yakobo 3:6).
4. Matumizi ya Yesu juu ya neno Gehenna
   a. Moto, Mt. 5:22; 18:9; Mk 9:43
   b. Mahali pa milele, Mk 9:48 (Mt. 25:46)
   c. mahali pa maangamizo (kwa mwili na roho), Mt. 10:28
   d. panafanana na *Sheol,* Mt. 5:29-30; 18:9
   e. Panaainisha waovu kama "wana wa Jehanamu" Mt. 23:15
   f. Ni matokeo ya hukumu ya kimahakama, Mt. 23:33; Luk 12:5
   g. Dhana ya Gehenna inafanana na mauti ya pili (kama vile Ufu. 2:11; 20:6,14) au ziwa la moto (k.v. Mt. 13:42,50; Ufu. 19:20; 20:10,14-15; 21:8).Yawezekana ziwa la moto pakawa ndo mahali pa watu kuishi milele (wanaotoka kuzimu) na malaika waovu (waliotoka shimoni, 2 Petr. 2:4; Yuda 1:6 au shimoni, kama vile Luk 8:31; Ufu. 9:1-11; 20:1,3).
   h. ilikuwa haikusanifiwa kwa ajili ya binadamu, lakini ilikuwa ni kwa ajili ya shetani na malaika wake, Mt. 25:41

E. yawezekana, kwa sababu ya kupishana kwa maneno shimoni (*sheol),* kuzimu(*hades)* na Jehanamu(*Gehenna*) kuwa
   1. kiasili watu wote walikwenda shimoni/kuzimu
   2. uzoefu wao wa (mema/mabaya) utazidishwa kwenye siku ya hukumu ya mwisho, lakini sehemu ya watenda maovu itabaki kuwa ile ile (hi indo kwa sababu toleo la KJV linaitafasili kama kuzimu (kaburi) kama Jehanamu .
   3. Andiko katika agano jipya linalotaja kuhusu mateso kabla ya hukumu ni pale penye mfano katika Luka 16:19-31(Lazaro na mtu tajiri). Sheol pia pameelezewa kama mahali pa mateso (kama vile Kumb. 32:22; Zab. 18:1-5). Hata hivyo, mtu hawezi kutengeneza andiko juu ya mfano.

III. Hali ya mwingiliano kati ya mauti na ufufuo

A. Agano jipya halifundishi juu ya "zinaa ya nafsi," ambacho ni moja ya kitu kati ya mitazamo mingi ya kale juu ya maisha baada ya kufa , ambapo panadaiwa kuwa
   1. nafsi ya mwanadamu huwepo hata kabla ya maisha haya ya kimwili
   2. nafsi ya mwanadamu ni ya milele kabla na baada ya kifo cha kimwili
   3. mara nyingi mwili unaonekana kuwa gereza na mauti inaurudisha kwenye hali uliokuwanayo kabla

B. Agano Jipya linadokeza juu ya hali ya kutoungana kati ya mauti na ufufuo
   1. Yesu anaongelea juu ya utengano wa mwili na roho, Mt. 10:28
   2. Ibrahamu angeweza tayari kuwa na mwili, Mk. 12:26-27; Luka 16:23
   3. Musa na Eliya walikuwa na mwili wa nyama kipindi Yesu anageuka sura, Mathayo 17
   4. Paulo anadai kuwa kipindi cha Yesu kurudi mara ya pili, waamini watakuwa na mwili mpya, 1 The. 4:13-18
   5. Paulo anadai kuwa waamini watapata mili mipya ya kiroho siku ya kufufuka, 1 Kor. 15:23,52
   6. Paulo anadai kuwa waumini hawaendi kuzimu, lakini huwa wamekufa huwa na Yesu, 2 Kor. 5:6,8; Fil. 1:23. Yesu aliyashinda mauti na kuwachukuwa watakatifu akaenda nao mbinguni, 1 Pet. 3:18-22.

IV. Mbinguni

A. Neno hili limetumika kwa maana tatu katika Biblia.
   1. kwa maana ya anga juu ya dunia, Mwa. 1:1,8; Isa. 42:5; 45:18
   2. Mbingu yenye nyota, Mwa. 1:14; Kumb. 10:14; Zab. 148:4; Heb. 4:14; 7:26
   3. Mahali pa kiti cha Enzi cha Mungu, Kumb. 10:14; 1 Fal. 8:27; Zab. 148:4; Efe. 4:10; Heb. 9:24 (Mbingu ya tatu, 2 Kor. 12:2)

B. Biblia haifunui mengi kuhusu maisha baada ya kifo, yumkini kwa sababu ya mwanadamu aliyeanguka

hana njia au uwezo wa kuelewa (kama vile 1 Kor. 2:9).

C. Mbinguni kumesimama kwa yote ni mahali (kama vile Yn. 14:2-3) na mtu kamili (kama vile 2 Kor. 5:6,8). Mbinguni paweza kuwa ni bustani ya Edeni iliyorejeshwa (Mwanzo 1-2; Ufunuo 21-22). Dunia itatakaswa na kurejeshwa (k.v. Mdo.3:21; Rum. 8:21; 2 Pet. 3:10). Taswira ya Mungu (Mwa. 1:26-27) imerejeshwa katika Kristo. Sasa ushirika ule wa ndani kwenye bustani ya Edeni yawezekana ukarejea tena. Hata hivyo, huu wawezakuwa ni msemo (mbinguni kama mji mkubwa Ufu. 21:9-27) na sio halisi. 1 Korintho 15 inaelezea tofauti kati ya mwili halisi na mwili wa kiroho kama mbegu ya mti uliokomaa. Tena, 1 Kor. 2:9 (nukuu toka Isaya 64:4 na 65:17) ni ahadi kubwa na tumaini! Nafahamu kuwa tutakapomwona Yeye tutafanana naye (kama vile 1 Yoh.3:2).

V. Vyanzo vya kusaidia
   A. William Hendriksen, *The Bible On the Life Hereafter*
   B. Maurice Rawlings, *Beyond Death's Door*

**3:20 "uvumulivu wa Mungu uliokuwa ukingoja"** Hii ni ambatani ya neno *mēkos* (hali ya kitu kuwa mbali) na *thumos* (hasira). Hii ni kauli ya kati (shahidi) elekezi ya wakati usiotimilifu, ikidokeza Mungu Mwenyewe akisubiri tena na tena. Mungu mwenye kusamehe, asiye mwepesi kulipa kisasi, mvumilivu huainisha mambo yake na mwanadamu aliyeasi (kama vile 1 Pet. 3:20; Kut. 34:6; Nah. 9:16-23; Zab. 103:8-14; Yoeli 2:13; Mika 6:18-20; 2 Pet. 3:15; Rum. 2:4; 9:22). Hii tabia ya Kiungu pia inastahili kudhihilishwa kwa watoto Wake (kama vile 2 Kor. 6:6; Gal.5:22; Efe. 4:2; Kol. 1:11; 3:12; 1 Tim. 1:16; 2 Tim. 3:10; 4:2).
Katika maandiko ya Petro Mungu anaelezewa kama mwenye uvumilivu na akiisubilisha hukumu yake ili watu wapate kuokolewa.

1. Alisubiri kwenye siku za Nuhu, 1 Pet. 3:20
2. Aliusubirisha ujio wa mara ya pili, 2 Pet. 3:9

Mungu anahitaji watu waote wapate kuokolewa (kama vile 2 Pet. 3:9,15)!

◙ **"watu wasiotii hapo zaman.....siku za Nuhu"** Hili linaonekana kurejelea kwa malaika wa Mwanzo 6 (kama vile 2 Pet. 2:4-5; Yuda 6) au wale ambao hawakuamini katika siku za Nuhu.

◙ **"waliokoka kwa maji"** Kimuktadha inaonekana kuwa Petro alileta habari za Nuhu na gharika kama njia ya kuzungumza kuhusu "kuokolewa" (kuokolewa kimwili kwenye Agano la Kale dhidi ya wokovu wa kiroho wa Agano Jipya) kwa maji (yaani., gharika la Agano la Kale la Mwanzo 6-9 dhidi ya ubatizo wa Kikristo). Ikiwa I Enoch ni historia ya nyuma, hivyo Nuhu na familia yake (yaani., wanadamu wote) waliokolewa kwa maji ya gharika toka kwenye uovu, kizazi kilichochangamana cha watu na malaika.

**3:21**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"mfano wa mambo hayo"** |
| **NKJV** | **"pia hapana mfanoe"** |
| **NRSV** | **"ambacho ni kivuli"** |
| **TEV** | **"ilikuwa ni alama ya kuelekeza hayo"** |
| **NJB** | **"mfano wa hayo"** |

Hili ni neno la Kiyunani *antitupon*, ambalo ni ambani ya neno *anti* (yaani., lenye kufanana na) na neno *tupos* (kama taswira au mfano). Huu ni mfano pekee wa kivumishi katika Agano Jipya, lakini nomino ipo katika Ebr.9:24. Kifungu kinaonyesha alama, asili ya kiuainishi wa nukuu za Petro.

◙ **"ubatizo"** Ubatizo ilikuwa ni nafsi ya kanisa la mwanzo kwa ajili ya tamko la mtu hadharani (au ukiri). Haukuwa ni mbinu kwa ajili ya wokovu, lakini ni tukio la uthibitisho wa maneno ya imani. Kumbuka makanisa ya mwanzo yalikuwa hayana majengo na walikutana nyumbani au mara nyingi katika sehemu za siri kwa sababu ya kuhofia mateso.

Wengi wa watoa maoni wamedai kuwa 1 Petro ni mahubiri ya kiubatizo. Ingawa hili linawezekana, lakini linaweza lisiwe chaguo sahihi. Ni kweli kwamba Petro mara nyingi alitumia ubatizo kama tendo muhimu la imani (kama vile Mdo.2:38,41; 10:47). Ingawa, halikuwa ni tukio la kisakramenti, bali ni tukio la imani, likiashiria kifo, kuzikwa, na kufufuka kama mwamini anavyotambuliwa na tukio lake Kristo (kama vile Rum. 6:7-9; Kol. 2:12). Tendo lenyewe ni la kiishara, na sio la kisakramenti, tendo ni tukio la ukiri, wala sio mbinu za wokovu.

◙ **"anawaokoa ninyi"** Hili neno mara nyingi linatumika katika Agano la Kale kwa ajili ya ukombozi wa kimwili, lakini mara nyingi limetumika katika Agano Jipya kwa ajili ya ukombozi wa kiroho. Katika muktadha huu kuhusu mateso dhahili lina madokezo yote.

◙ **"bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu"** Hili linaonyesha kuwa sio ibada ya ubatizo inayookoa, bali ni mwenendo wa mwamini dhidi ya Mungu (kama vile 1 Pet. 3:16). Hata hivyo, naongezea kuwa ubatizo sio suala la uchaguzi bali (1) ni mfano uliotolewa na Yesu (kama vile Mt. 3:13-17; Marko 1:9-11; Luka 3:21-22; Yohana 1:31-34 na (2) ni amri toka kwa Yesu (kama vile Mt. 28:19) kwa ajili ya waamini wote. Agano Jipya halielewi kitu chochote kuhusu waamini ambao hawajabatizwa. Katika Agano Jipya ubatizo haukutenganishwa kuhusiana na ukiri wa imani ya mtu. Angalia maelezo juu ya "dhamiri" katika 1 Pet. 3:16.

◙ **"kwa kufufuka kwake Yesu Kristo"** Hii inaonyesha kwamba asili ya wokovu iko ndani ya ufufuko wa Yesu (kama vile Rum. 1:4-5), na sio ubatizo. Hii safu ya fikra kwa wazi inaonekana katika Rum. 6:3-4. Ubatizo kwa mfanano, kuzamishwa, kunamaanisha kifo, kuzikwa, na kufufuka. Kiukweli maana halisi sio muhimu kama moyo wa mshirika.

**3:22 "Naye yupo mkono wa kuume"** Hii ni stiari ya lugha ya binadamu kumwelezea Mungu juu ya mamlaka, nguvu, na heshima (kama vile 1 Yohana 2:1). Taswira hii ni kivutio toka Zab. 110:1.
Biblia inatumia lugha ya kibinadamu kelezea nguvu zisizo za kawaida za watu, mahali, na matukio. Ni dhahili kimfanano, kiishara, na kiistiari. Inawezekana kuuzungumza ukweli, lakini ndani ya mipaka (mipaka ya (1) mitazamo yetu ya kibinadamu iliyoanguka na (2) maumbile yake, ukomo wa muda, utofauti wa tamaduni). Inatosheleza, lakini sio yenye kuhitimisha.

◙ **"malaika na enzi na nguvu zikiisha kutiishwa chini Yake"** Hili linarejelea viwango vya kimalaika (kama vile Rum. 8:38-39; 1 Kor. 15:24; Efe. 1:20-21, 6:12; Kol. 2:15; I Enoch). Inaonyesha mamlaka kamili ya Kristo na nguvu juu ya ulimwengu wa kiroho.
Ingawa 1 Petro haizungumzii moja kwa moja dhana ya ujuzi, ni wazi toka kwenye maandiko ya Agano Jipya (Kol., Efe,. 1 Tim., Tito, na 1 Yohana) kuwa muktadha wa kitamaduni wa karne ya kwanza ya ulimwengu wa Wagiriki na Warumi ulipambanishwa na fikra za kifalsafa/kithiolojia.
Katika karne ya pili dhana ya wenye ujuzi (na maandiko ya Nag Hammadi) wa neno la Kiyunani *pleroma* (utimilifu), likitumiwa mara nyingi na Paulo, linarejelea "ukamilifu wa Mungu," viwango vya kimalaika (*aeons* yaani., yumkini mbingu saba za Kiyahudi) kati ya mungu mkuu aliye juu na miungu wadogo. Yesu ndiye suluhisho la mbinguni, sio namba za siri au maarifa yahusianayo na wale malaika/mapepo waingiliayo kati.
Hata kama dahari ya wenye ujuzi sio mtizamo wa kifungu hiki inaonekana kuwa malaika ndio walengwao! Hili laweza kurejelea kuwa "roho zilizoko kifungoni" zinarejelea malaika waasi waliowachukua binti za wanadamu na kuzaa nao wana (kama vile Mwa. 6:1-4).

## MADA MAALUM: WENYE UJUZI

I. Muundo wa karne ya kwanza

Ulimwengu wa Kirumi wa karne ya kwanza ulikuwa ni wakati wa nadharia kati ya dini za Mashariki na Magharibi. Miungu yote ya dini ya Kiyunani na Kirumi ilikuwa katika uovu uliojulika sana. Dini ya siri ilikuwa maarufu sana kwa sababu ya msisitizo wao juu ya uhusiano binafsi pamoja na Uungu na maarifa ya siri. Falsafa ya ulimwengu wa Kiyunani ilikuwa maarufu na ilikuwa kiunganishi cha maoni mengine ya ulimwengu. Katika Ulimwengu huu wa dini isiyokuwa na msimamo mmoja ilikuja ili kusiwepo kujichanganya na imani ya ki-Kristo (Yesu ndiye njia pekee kwa Mungu, kama vile. Yohana 14:6). Vyo vyote ulivyo usuli halisi wa uasi,

ilikuwa jaribio la kutochanganya na Ukristo (yaani, Yohana 14:6; Yohana 1.5:12) wenye kuelekea na wenye kukubaliwa na kiakili na kwa mapana na halaiki ya Wayunani wa Kirumi. Inawezekana kwamba mawazo ya kimafunuo yalianzia miongoni mwa madhehebu ya Kiyahudi (yaani, mfano mmoja: Dhehebu la DSS). Hii inaweza kuelezea baadhi ya vipengele vya Kiyahudi vya vitabu vya Agano Jipya vinavyohusiana na Mafunuo.

II. Baadhi ya mafundisho ya kimsingi ya uasi kwa ushahidi wa ndani kutoka Yohana 1.
   A. kukataa umbo mwili laYesu
   B. kukataa ukuu wa Yesu Kristo katika wokovu
   C. ukosefu wa maisha sahihi ya Kikristo
   D. mkazo juu ya marifa (siri ya mara kwa mara)
   E. uelekeo wa kutochanganyikana na tabaka la wasomi

III. Mafunuo ya kwanza ya karne ya kwanza
   A. Mafundisho ya kimsingi ya Mafunuo ya karne ya kwanza yanaonekana kuwa ni msisitizo juu ya nadharia ya maisha (milele) ya uwili kati ya roho na vitu. Roho (Mungu mkuu) alifikiriwa kuwa mwema, ambapo vitu vilikuwa viovu vya kurithika. Mkinzano huu unafanana
      1. Wazo bora la falsafa ya Plato ya umwili
      2. mbinguni dhidi ya dunia
      3. Isiyooonekana dhidi ya inayoonekana. Pia kulikuwa na msisitizo mkubwa juu ya umuhimu wa maarifa ya siri (neno la siri au alama za siri ambazo zinaruhusu nafsi kuingiliana katika eneo/uwanja wa malaika [aeons] hadi mungu mkuu) muhimu kwa wakovu.
      4. inawezekana ukawa ushawishi kutoka kwa wafuasi wa Zoroaster
   B. Kuna aina mbili za Mafunuo ya Kwanza ambazo kama inavyoonekana zingeweza kuwa usuli wa Yohana 1
      1. Mafunuo ya mafundisho ya awali kuwa yanayopinga mateso ya Yesu, na kifo cha msalaba, ambayo yanakataa ubinadamu wa kweli wa Yesu kwa sababu vitu ni viovu
      2. Mafunuo ya Cerinthia, ambayo hufafanua Kristo kuwa mmoja wa muda mrefu *aeons* au mwenye viwango vya utakatifu kati ya mungu mkuu na vitu viovu. Huyu "Roho wa Kristo" mwenye kukaa ndani ya utu wa Yesu wakati wa ubatizo wake na kumwacha kabla ya kusulubiwa kwake.
      3. kati ya haya makundi mawili baadhi walifanya mazoezi ya kujilinda na uovu wa mwili (ikiwa mwili unataka, huo ni uovu), wengine waliokuwa kinyume na sheria (ikiwa mwili unataka, fanya)
   C. Hakuna ushahidi wo wote wa mfumo wa Mafunuo ulioboreshwa katika karne ya kwanza. Si kufikia katikati ya karne ya pili kwamba ushahidi ulioandikwa ulikuwepo. (tazama Maandishi ya Nag Hammadi). Kwa habari zaidi kuhusu "Mafunuo" tazama
      1. *The Gnostic Religion* kupitia Hans Jonas, iliyochapishwa na Beacon Press
      2. *The Gnostic Gospels kupitia Elaine Pagels*, iliyochapishwa na Random House
      3. *The Nag Hammadi Gnostic Texts na the Bible* kupitia Andrew Helmbold

IV. Uasi wa Leo
   A. Roho ya huu uasi iko pamoja nasi leo wakati watu wanapojaribu kuchanganya ukweli wa ki-Kristo na mifumo mingine ya mawazo.
   B. Roho ya huu uasi iko pamoja nasi leo wakati watu wanaposisitiza "usahihi" mafundisho ya kuepuka uhusiano binafsi na imani ya mtindo wa maisha.
   C. Roho ya huu uas iko pamoja nasi leo wakati watu wapougeuza Ukristo kuwa katika hali ya kujitenga na watu wenye werevu na tabaka la wasomi.
   D. Roho ya huu uasi uko pamoja nasi leo wakati watu a Kidini wanapogeuka kwa kujilinda na uovu wa mwili au kuwa kinyume na sheria kama njia ya kupata upendeleo kwa Mungu.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni <u>mwongozo</u> wa kujifunza wa fasiri inamaanisha kwamba unawajibika kwatafsiri zako mwenyeweza Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Mjadala huu wa maswali unawekwa ili kukusaidia wewe kufikiri maana ya chapisho kupitia sehemu ya kitabu. Wanamaanisha kuchochea sio kutoa maana ya mwisho.

1. Ni wapi waandishi wa jinsia ya kiume wa Agano Jipya?
2. Ni kwa vipi wanawake wanapaswa kuvaa? (Send for my tape #1337 iliyoandikwa "Thiolojia ya mavazi ya mwanamke")
3. Ni kwa namna gani uhusiano wetu wa kifamilia unaweza kuayaathiri maombi?
4. Orodhesha tabia ambazo zinaweza kuuongoza uhusiano wetu wa kijamii.
5. Ni kwa nini Wakristo wanateseka?
6. Ni lazima kila Mkristo awe mwenye kushuhudia kwa maneno?
7. Ni wapi roho walioko kifungoni?
8. Je wokovu umeweza kutuokoa? (Send for my tape #1962 kilichoandikwa "Baptismal Regeneration")

# 1 PETRO 4

| MGAWANYO WA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Wakili mwema wa neema ya Mungu | Mateso ya Kristo na Yetu<br><br>(3:18-4:6) | Majukumu ya Wakristo<br><br>(2:11-4:11) | Maisha yaliyo Badilishwa | Kustisha Dhambi |
| 4:1-6 | | 4:1-6 | 4:1-6 | 4:1-6 |
| | Kutumika kwa Ajili ya Utukufu Wa Mungu | | Watawala wema Wa Karama za Mungu | Ufunuo wa Kristo U karibu |
| 4:7-11 | 4:7-11 | 4:7-11 | 4:7-11 | 4:7-11 |
| Kuteseka kama Mkristo<br><br>Kuteseka kwa Ajili ya Kristo | Kuteseka kwa Ajili ya utkufu wa Mugu | Muhutasari | Kuteseka kama Mkristo | |
| 4:12-19 | 4:12-19 | 4:12-19 | 4:12-19 | 4:12-19 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka "Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 PETRO 4:1-6**

**1 Basi kwa kuwa Kristo aliteswa katika mwili wake, ninyi nanyi jivikeni silaha ya nia ile ile; kwa maana yeye**
**aliyeteswa katika mwili ameachana na dhambi. 2 Tangu sasa msiendelee kuishi katika tamaa za wanadamu, bali**
**katika mapenzi ya Mungu, wakati wenu uliobaki wa kukaa hapa duniani. 3 Maana wakati wa maisha yetu uliopita**
**watosha kwa kutenda mapenzi ya Mataifa; kuenenda katika ufisadi, na tamaa, na ulevi, na karamu za ulafi, na**
**vileo, na ibada ya sanamu isiyo halali; 4 mambo ambayo wao huona kuwa ni ajabu ya ninyi kutokwenda mbio**
**pamoja nao katika ufisadi ule ule usio na kiasi, wakiwatukana. 5 Nao watatoa hesabu kwake yeye aliye tayari**
**kuwahukumu walio hai na waliokufa. 6 Maana kwa ajili hiyo hata hao waliokufa walihubiriwa Injili, ili kwamba**
**wahukumiwe katika mwili kama wahukumiwavyo wanadamu; bali wawe hai katika roho kama Mungu alivyo hai.**

**4:1 "Basi"** Neno hili linaunganisha mjadala uliopita katika kile kinachofuatia.

◙ **"Kristo aliteswa katika mwili"** Kifungu hiki kinahusiana na 3:18. Mwili unarejelea masha ya mwili ya Yesu. Hakika alikuwa mmoja wetu (yaani., mwanadamu). Yeye alikufa badala yetu (kama vile 1 Pet. 4:18; Isaya 53; Marko 10:45; 2 Kor. 5:21). 1 Petro anaweka msistizo wa mateso ya Kristo (kama vile 1 Pet. 2:21,23; 3:18; 4:1) na ukweli wa mateso ya wafuasi wake kwa sababu wanamfuata yeye (kama vile 1 Pet. 2:19-20; 3:14,17; 4:15,19; 5:10).
Asili ya ubadala wa mateso ya Kristo uliotajwa katika 1 Pet. 3:18 na 2:21 unawekewa msistizo na machapisho kadhaa ya Kiyunani yennye kuongeza kifungu "alitseka kwa ajili yako" (yaani., א) au "kwa ajili yetu" (yaani., א c, A, K, na P).
Aina ile ile ya Kiwakilishi kinachobainisha ongezeko pia inaweza kuonekana katika 1Pet. 4:3. Waandishi wa kanisa la mwanzo walijaribu kuyaweka wazi maandishi yao.

◙ **"ninyi nanyi jivikeni silaha"** Hii ni kauli ya kati shurutishi ya wakatai uliopita usio timilifu. "Kujivika silaha" ni neno la kijeshi lenye maana ya kuvaa kiti kizito na kwa ajili ya kujiandaa kwa ajili ya mapambano. Kuna migogoro ya kiroho katika maisha yetu ya kila siku (kama vile Efe. 6:10-20; Rum. 13:12; 1 The. 5:8).

◙ **"nia ile ile"** Mtazamo wa Yesu kuhusu mateso, ikiwemo kuteseka pasipo hatia, ni hali ya kawaida kwa wacha-Mungu katika ulimwengu ulioanguka kiroho (kama vile Yohana 15:20; Rum. 8:17; Flp. 1:29; 2 Tim. 3:12; 1 Pet.4:12-19).

◙ **"kwa maana yeye aliyeteswa katika mwili ameachana na dhambi"** Kifungu hiki kinaweza kufasiriwa katika namna mbalimbali kwa kuingia kwa undani katika mundo wa kisarufi. Kristo ni mfano wetu katika mateso ya kutokuwa na hatia, hata kwa kuwakifishwa kwake (kauli tendaji endelevu ya wakati uliopita usio timilifu). Waamini wanahusishwa katika mateso kwa sababu ya kutambuliwa katika yeye.
Kitenzi kikuu chaweza kuwa cha kati (A. T. Robertson's *Word Pictures of the New Testament* , uk. 121) au tendwa (Moulton's *Analytical Greek Lexicon* na Barbara and Tim Friberg's *Analytical Greek New Testament*). Ikiwa ni cha kati kinawasistiza waamini kutojihusisha ipasavyo katika makubaliano ya wao kuwa kama wafuasi wa mfano wa Kristo. Ikiwa ni tendwa basi inasistiza juu ya ukweli wa kiroho wa ukombozi wa waamini kutoka katika nguvu ya dhambi.
Kifo huitimisha uhusiano wa ntu na dhambi. Suala hili linaweza kuhusianishwa na dhana ya kithioloja ya Rum. 6. Kwa maisha ya kale kifo huleta uwezekano wa huduma kwa Mungu (kama vile Rum. 6:2,6,7) au ubatizo huashiria upya wa maisha (kama vile Rum. 6:4; Kol. 2:12).
Hoja nzima ni kuwa kadri waamini wanvyoufuatisha mfano wa mateso ya Kristo, ndivyo, Ndivyo ulivyo mfano wake katika kuishinda dhambi. Sisi tu viumbe vipya katika Kristo! Yatupasa kuisha kama ilivyo. Kufanana na Kristo ni mapenzi ya Mungu (kama vile Rum. 8:28-29; 2 Kor. 3:18; 7:1; Gal. 4:19; Efeh. 1:4; 4:13; 1 The. 3:13; 4:3,7; 5:23; 1 Pet. 1:15). Hii inaakisi ukweli kwamba sura ya Mungu iliyopotea katika Anguko (kama vile Mwanzo 3) inarejeshwa kwa ukamilfu kupitia Kristo. Wakristo wanao uchaguzi mwingine kuhusu kuhusu namna ya watakavyoishi. Si watumwa tena wa dhambi! Tenbea katika yeye!

**4:2 "Tangu sasa msiendelee kuishi katika tamaa za wanadamu"** Kifungu hiki kinaiakisi kweli ile ile ya kithiolojia kama ilivyo Warumi 6. Waamini wameifia dhambi na sasa wako hai kwa ajili ya utumishi wa Mungu (kama vile Rm. 6:20). Wokovu ni maisha mapya ya uumbaji.Una sifa zilizo wazi.

◙ **"bali katika mapenzi ya Mungu "** Tazama Mada Maalum: Mapenzi ya Mungu katika1 Petro 2:15.

**4:3** Kifungu hiki ni dai la maisha ya viongozi yaliyopita katika upagani. Hii ni moja ya mistari inayowasababisha watoa maoni kudai kwamba makanisa anayoyaandikia Petro ya mikusanyiko ya ki–Mataifa. Jamii ya kipagani ilikuw imepotoka sana, hata katika taratibu zake za kiibada. Ukristo lazima utengeneze tofauti isiyo ya kawaida na mabadiliko katika mienendo ya maisha. Badiliko hili mara nyingi ni mwanzo wa mateso ya wapagani wengine. Dhambi huitaji ushirikiano.
Baada ya ufunguzi wa "ya," maandiko mengine ya Kiyunani yanaongeza neno "ninyi" na mengine "sisi." Hizi ni nyongeza ya kiuandishi zenye kujaribu kuweka wazi maneno ya mwandishi.

## MADA MAALUM:UOVU NA WEMA KATIKA AGANO JIPYA

Orodha zote za mabaya na mema ni ya kawaida katika Agano Jipya. Mara nyingi yanaaksi orodha za sheria za Kiyahudi na kitamaduni. Orodha ya tabia kinzani ya Agano Jipya zinaweza onekana katika:

| | Maovu | Mema |
|---|---|---|
| 1. Paulo | Rum. 1:28-32 | --- |
| | Rum. 13:13 | Rum. 12:9-21 |
| | 1 Kor. 5:9-11 | --- |
| | 1 Kor. 6:10 | 1 Kor. 6:6-9 |
| | 2 Kor. 12:20 | 2 Kor. 6:4-10 |
| | Gal. 5:19-21 | Gal. 5:22-23 |
| | Efe. 4:25-32 | --- |
| | Efe. 5:3-5 | --- |
| | --- | Flp. 4:8-9 |
| | Kol. 3:5,8 | Kol. 3:12-14 |
| | 1 Tim. 1:9-10 | --- |
| | 1 Tim. 6:4-5 | --- |
| | 2 Tim. 2:22a, 23 | 2 Tim. 2:22b,24 |
| | Tito 1:7, 3:3 | Tito 1:8-9; 3:1-2 |
| 2. Yakobo | Yak. 3:15-16 | Yak. 3:17-18 |
| 3. Petro | 1 Pet. 4:3 | 1 Pet. 4:7-11 |
| | 2 Pet. 1:9 | 2 Pet. 1:5-8 |
| 4. Yohana | Ufu. 21:8; 22:15 | …….. |

◙ **"wakati wa maisha yetu uliopita watosha**"Hii ni kauli ya kati endelevu ya wakati timilifu. Wasioamini kimakusudi na kwa kudumu wameamua kuwa wabinafsi na watenda dhambi.

**NASB** **"tamaa"**
**NKJV, NRSV** **"anasa"**
**TEV** **"kukosa ustaarabu"**
**NJB** **"kuenenda kusiko faa"**

Neno hili linamaanisha ukosefu wa kiasi, uvunjifu wa taratibu za kijamii, haswa eneo la kingono (kama vile Marko 7:22; Rum. 13:13; 2 Kor. 12:21; Gal. 5:19; Efe. 4:19; 1 Pet. 4:3; 2 Pet. 2:7,18; Yuda 6).

◙ **"tamaa"** Hili neno linamaanisha shauku ya nguvu ya kitu au mtu. Shauku hii kubwa inaweza kuwa chanya (kama vile. Luka 22:15; 1 Tim. 2:1; 1 Pet. 1:12), lakini huwa ni hasi mara nyingi (kama vile. 1 Pet. 1:14; 2:11; 4:2,3; 2 Pet. 1:4; 2:10,18; 3:3; Marko 4:19).

◙ **"ulevi"** Hili ni neno ambatani linalopatikana hapa tu katika Agano Jipya juu ya "divai" (*oinos*) na "kuweka vipovu"(*phluō*). Ulimwengu wa Kale ulikunywa divai mara kwa mara kama Yesu alivyofanya (kama Mt. 11:18-19) na kanisa la kale. Ni ziada inayoshutumiwa (kama vile Mithali. 23:29-35; Rum. 13:13; Gal. 5:21).

## MADA MAALUM: MTAZAMO WA BIBLIA DHIDI YA ULEVI NA KILEO

Maneno ya Kibiblia

A. Agano la Kale

1. *Yayin* – Hili ni neno la jumla la divai (BDB 406, KB 409), ambalo limetumika mara 141. Asili ya neno hili si yumkini kwa sababu haitokani na mzizi wa Kiebrania. Hiii mara nyingi inamaanisha juisi ya matunda iliyochacha, mara nyingi tunda aina ya balungi. Baadhi ya vifungu bainishi ni Mwa. 9:21; Kut. 29:40; Hes. 15:5,10.
2. *Tirosh* – Hiii ni "divai mpya" (BDB 440, KB 1727). Kwa sababu ya tabia ya nchi ya Mashariki ya Karibu, uchachu unaanza ndani ya masaa sita baada ya kutengeneza juisi. Neno hili hurejerea juu ya divai katika hatua ya kuchachusha. Kwa vifungu vibainishi tazama Kut. 12:17; 18:4; Isa. 62:8-9; Hos. 4:11.
3. *Asis* – Kwa uhalisia hiki ni kinywaji aina ya kileo ("divai mpya" BDB 779, KB 860, m.f. Yoeli 1:5; Isa. 49:26).
4. *Sekar* – Hili ni neno "kinywaji kikali" (BDB 1016, KB 1500). Mzizi wa Kiebrania unatumika ndani ya neno "kulewa" au "mlevi." Mara nyingi hiki huongezwa ndani yake ili kukifanya kileweshe zaidi. Hiki ni sawa na *yayin* (kama vile Mit. 20:1; 31:6; Isa. 28:7).

B. Agano Jipya
   1. *Oinos* – neno lililo sawa kimaana na *yayin*
   2. *Neos oinos* (divai mpya) – ni neno linalofanana la Kiyunani sawa na tirosh (kama vile Marko 2:22).
   3. *Gleuchos vinos* (divai mpya, asis) – ni ile divai inayotengenezwa katika hatua za mwanzo kabla ya kuchachushwa (kama vile Matendo ya Mitume 2:13).

I. Matumizi ya Kibiblia

A. Agano la Kale
1. Mvinyo ni zawadi ya Mungu (Mwa. 27:28; Zab 104:14-15; Mhu. 9:7; Hos. 2:8-9; Yoeli 2:19,24; Amosi 9:13; Zek. 10:7).
2. Divai ni sehemu ya sadaka ya kuteketeza (Kut. 29:40; Law. 23:13; Hes. 15:7,10; 28:14; Kumb. 14:26; Amu. 9:13).
3. Mvinyo ilitumika katika sherehe za Israeli (kama vile Kumb. 14:26)
4. Divai inatumika kama tiba (2 Sam. 16:2;Mit. 31:6-7).
5. Divai inaweza kuwa chanzo cha tatizo (Nuhu –Mwa. 9:21; Lutu – Mwa. 19:33,35; Samsoni – Waamuzi 16; Nabali – 1 Sam. 25:36; Uria– 2 Sam. 11:13; Amnoni– 2 Sam. 13:28; Ela– 1 Fal. 16:9; Ben-hadad i– 1 Fal. 20:12; Watawala – Amosi 6:6; na Wanawake – Amosi 4).
6. Divai inaweza kutumika vibaya (Mit. 20:1; 23:29-35; 31:4-5; Isa. 5:11,22; 19:14; 28:7-8; Hosea 4:11).
7. Divai ilizuiliwa kwa makundi fulani (makuhani waliokuwa katika zamu, Law. 10:9; Eze. 44:21; Wanazareti, Hesabu 6; na watawala, Mit. 31:4-5; Isa. 56:11-12; Hosea 7:5).
8. Divai ilitumika katika mpangilio wa matukio ya siku za mwisho (Amosi 9:13; Yoeli 3:18; Zek. 9:17).

B. Kipindi cha utulivu kati ya Agano la Kale na Agano Jipya
   1. Divai katika upatanisho ina msaada (Mhubiri 31:27-33).
   2. Walimu wa Sheria za Kiyahudi wanasema, "Divai ni kuu kuliko tiba zote, mahali palipo na uhaba wa divai, madawa ya kulevya yanahitajika." (BB 58b).

C. Agano Jipya
   1. Yesu alikibadili kiwango kikubwa cha maji kuwa divai (Yohana 2:1-11).
   2. Yesu alikunywa divai (Mt. 11:18-19; Luka 7:33-34; 22:17 na kuendelea)
   3. Petro alidhihakiwa kwa ulevi "mvinyo mpya" siku ya Pentekoste (Mdo. 2:13).
   4. Divai inaweza kutumika kama matibabu (Marko 15:23; Luka 10:34; 1 Tim. 5:23).
   5. Watawala hawatakiwi kuwa watumiaji wabaya. Hii haimaanishi kujinyima moja kwa moja (1 Tim. 3:3,8; Tito 1:7; 2:3; 1 Pet. 4:3).
   6. Divai ilitumika katika kupangili matukio ya siku za mwisho (Mathayo 22:1na kuendelea; Ufu. 19:9).
   7. Ulevi huleta majuto (Mt. 24:49; Luka 12:45; 21:34; 1 Kor. 5:11-13; 6:10; Gal. 5:21; 1 Pet. 4:3; Rum. 13:13-14).

II. Utambuzi wa ndani wa Kithiolojia

A. Mkazo wa Kiupembuzi
1. Divai ni zawadi kutoka kwa Mungu.
2. Ulevi ni tatizo kubwa.

3. Waamini katika baadhi ya tamaduni yawapasa kuweka uhuru wa mipaka yao kwa ajili ya injili (Mt. 15:1-20; Marko 7:1- 23; 1 Wakorintho 8-10; Warumi 14).

B. Mwelekeo wa kwenda nje ya mipaka iliyokusudiwa
   1. Mungu ndiye mwanzilishi wa mambo yote mazuri.
      a. chakula – Marko 7:19; Luka 11:44; 1 Kor. 10:25-26
      b. vitu vyote visivyo najisi – Rum. 14:14,20; 1 Tim. 4:4
      c. Vitu vyote vilivyo vya kisheria– 1 Kor. 6:12; 10:23
      d. Vitu vyote vilivyo safi – Tito 1:15
   2. Mwanadamu aliyeanguka amezitumia vibaya karama za Mungu kwa kuzifanyia kazi nje ya mipaka ya Mungu aliyoikusudia.

C. Matumizi mabaya yako ndani yetu, si ndani ya vitu. Hakuna kilicho kiovu ndani ya uumbaji wa vitu vinanyoonekana (kama vile Rum. 14:14,20).

III. maelezo ya kufungia
   A. kuwe na uhakika na uzoefu wako, thiolojia, na utafasiri wa kibilia havimshushi thamani Yesu na tamaduni za Kikristo/ Kiyahudi za karne ya kwanza! Kiuhakika hawakuwa wenye kujizuiya kunywa mvinyo.
   B. Mimi sitetei jamiii ya watumia pombe. Hata hivyo, wengi wamekwenda mbali juu ya nafasi ya Biblia kuhusu somo hili na sasa kudai kuwa wenye haki sana wakisimamia juu ya upendeleo wa kimadhehebu/ kitamaduni.
   C. Kwangu mimi, Warumi 14 na 1 Wakorintho 8-10 vimetoa mwanga na mwongozo uliosimamia juu ya upendo na heshima kwa wapendwa wengine na uenezaji wa injili katika tamaduni zetu, na sio uhuru binafsi au ukosoaji wa kimaamuzi. Kama Biblia ndio chanzo pekee cha imani na utendaji, kwa hiyo yawezekana wote tulifikirie jambo hili.

Tukijizuiya kabisa kunywa mvinyo kama yalivyo mapenzi ya Mungu, tunadokeza nini kuhusu Yesu, pia tamaduni za sasa za wale wanaotumia kileo mara kwa mara (mf. Ulaya, Israeli, Argentina)

**NASB "karamu za ulevi"**
**NKJV "karamu za ulevi"**
**NRSV "ulevi"**
**TEV "karamu ya ulafi"**

Neno hili *kōmos*is linauhusiano na neno la Kiyunani kwa ajili ya kijiji, *kōmē*. Inamaanisha jamii kubwa na pana ya karamu zinazojumisha ulaji na unywaji wa ziada na matendo ya kujamiiana yasiyowekewa utaratibu (kama vile Rum. 13:13; Gal. 5:21).

◙ **"na vileo"**Hili ni neno linalohusiana na neno lililotangulia. Toleo la linaziunganisha zote katika "kufanya sherehe za nguvu zenye kuambatana na ulevi."

**NASB, NKJV "ibada za sanamu zichukizajo"**
**NRSV "ibada za sanamu zisizofuata sheria"**
**TEV "ibada mbaya zinazochukiza"**
**NJB "kiuzushi wakiabudu miungu ya uongo"**

Hii ni orodha ya dhambi ya tabia za ibada za kipagani ambazo mara kwa mara zinajumuisha kunywa kwa ziada, kula na kujamiiana kusiko na maadili kuliko pitiliza. Ilikuwa sawasawa na ibada za ustawi wa Wakanaani zilizoshutumiwa katika Agano la Kale.

**4:4** Mstari huu unahusiana na 2:12,15; 3:16. Wakristo walieleweka vibaya na kushambuliwa (1) maisha yao na vipaumbele vilibadilishwa kibayana na kiukamilifu kwamba Familia, urafiki na jirani walitambua na (2) baadhi ya masharti ya Mkristo na matendo yalitafsiriwa vibaya (yaani karamu za upendo kati ya marihamu, Karamu ya Bwana kama ya wanyama walao wengine, n.k.).

**4:5"watatoa hesabu kwake yeye aliye tayari kuwahukumu"**Hukumu ni hakika (kama vile Mt. 12:36; Ebr.9:27; 10:27; 2 Pet. 2:4,9; 3:7). Yeye ahukumuye

1. Mungu (kama vile Rum. 2:2-3; 14:10,12; 1 Pet. 1:17; 2:23; Ufu. 20:11-15)
2. Kristo (kama vile Yohana 9:39; Mt. 16:27; 25:31-46; Mdo. 10:42; 17:31; 2 Kor. 5:10; 2 Tim. 4:1)
3. Baba kupitia Mwana (kama vile Yohana 5:22-27; Mdo. 17:31; Rum. 2:16)

Hukumu ni mada isiyovutia lakini ni mada inayojirudia rudia katika Biblia. Imejikita katika kweli kadhaa za msingi wa Kibiblia.

1. Haya ni maadili ya kiujumla yanatengenezwa na Mungu wa maadili (tunavuna kile tunachopanda, kama vile. Gal. 6:7).
2. Ubinadamu umeanguka; tumeasi.
3. Huu si ulimwengu ambao Mungu aliukusudia kuwa.
4. Ulimwengu wote unaojitambua (malaika na wanadamu) watatoa hesabu yao kwa Muumbaji kwa kipawa cha uzima. Tu mawakili.
5. Umilele utadumu ukiamriwa na matendo yetu na maamuzi yaliyofanywa katika haya maisha.

◙ **"walio hai na waliokufa"**Hii inamaanisha wanadamu, wote wale walio hai na wale ambaowamekufa tayari (kama vile Flp. 2:10; Ufu. 2:13).

**4:6"kwa ajili hiyo hata hao waliokufa walihubiriwa Injili"**Kuna nadharia kadhaa juu ya tungo hii:

1. Inafanana na 3:18-20 (yaani "roho zilizomo vifungoni")
2. Inarejerea kwa wanadamu wote kwasababu wanadamu wote, waamini na wasioamini wanakufa kimwili kwasababu ya dhambi (inafanana na 1 Pet. 4:5)
3. Inarejerea kwa wale wote walioitikia Injili lakini sasa wamekufa (kauli tendwa ya wakati uliopita usio timilifu)
4. inarejerea kifo cha kiroho (yaani waliopotea) kulingana na Augustine, Bede, Erasmus, na Luther (kama vile Luka 15:24,32; Efe. 2:1,5; 5:14; Kol. 2:13)

Hii nadharia ya mwisho inaweka makisio kwamba baadhi (yaani ambao hawajawahi kusikia injili) watapokea nafasi ya kumpokea Kristo baada ya kifo. Nadharia hii inavutia kwa mantiki ya kibinadamu (yaani Ebr. 9:27). Inakanusha uharaka na umuhimu wa uinjilisti na misheni za sasa! Nafikiria uchaguzi wa 1 au 3 unafaa zaidi kaika muktadha huu.

◙ **"wahukumiwe katika mwili kama wahukumiwavyo wanadamu; bali wawe hai katika roho"**Tungo hii inafanana na maelezo ya Yesu katika 1 Pet. 3:18. Inathibitisha ukweli wa maisha ya baadaye (kama vile. Dan. 12:2; Mt. 25:46; Yohana 5:28-2

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 PETRO 4:7-11**
**[7]Lakini mwisho wa mambo yote umekaribia; basi, iweni na akili, mkeshe katika sala. [8]Zaidi ya yote iweni na juhudi nyingi katika kupendana; kwa sababu upendano husitiri wingi wa dhambi. [9] Mkaribishane ninyi kwa ninyi, pasipo kunung'unika; [10]kila mmoja kwa kadiri alivyoipokea karama, itumieni kwa kuhudumiana; kama mawakili wema wa neema mbalimbali za Mungu. [11]Mtu akisema, na aseme kama mausia ya Mungu; mtu akihudumu, na ahudumu kwa nguvu anazojaliwa na Mungu; ili Mungu atukuzwe katika mambo yote kwa Yesu Kristo. Utukufu na uweza una yeye hata milele na milele. Amina**

**4:7 "mwisho wa mambo yote umekaribia"** Hii ni kauli tendaji elekezi yawakati timilifu. Ujio wa mara ya Pili ndiyo dhima ya mara kwa mara katika 1 Petro (kama vile 1 Pet. 1:5,6; 4:13,17; 5:1,10). Dunia inayoonekana itaharibiwa /kusafishwa kwa moto utakasao (kama vile 2 Pet. 3:10). Lile oni la kukaribia kwa tukio hili la Parousia pia linaonekana katika Yesu (kama vile Marko1:15; Luka 21:32); Paulo (kama vile Rum. 13:11); Yakobo (kama vile Yakobo 5:8); na Yohana (kama vile Ufu. 1:1,3; 3:11;22:6,7,10,12,20).

Kukaribia kwa kurudi kwa Yesu limekuwa fundisho la hotuba nyingi kwa maelefu ya miaka na bado Hajaraudi. Je! hii linamaanisha (1) kwamba hatakuja au (2) kwamba Agano Jipya limekosea kuzngumzia kuhusu kakaribia kwa kuja kwake (kama vile Mt. 24:36) Hili linatushangaza na ni sehemu ya siri ya kutwaa umbo-mwili.

Kukaribia kwa kurudi huku kunaonekana kuwa mtazamo wa waandisi wa Agano Jipya.Nini kimetokea? Kwanza, hebu kumbuka kwamba muda ni muhimu kwa wale tu waliojikita ndani yake. Mungu hakawii, bali pia Mungu yu juu ya wakati.

Ukaribu wa kurudi kwa Yesu limekuwa tendo la kutia moyo na motisha kwa wacha- Mungu wanaoishi kwa kila kizazi cha waamiio. Bado, kithiolojia 2 Wathesalonike inatabiri juu ya kukawia kwa ujio huu (yaani., si hadi "kufunuiwa kwa mtu asiye wa torati"). Kuja kwa mara ya Pili ni dhima ya mara kwa mara, lakini ukweli kwa kizazi kimoja pekee cha waaminio (kama vle. 2 Pet. 3).

**NASB "iweni na akili, mkeshe katika sala"**
**NKJV "iweni makini na mkeshe"**
**NRSV "iweni akini na mfunzane ninyi kwa ninyi"**
**TEV "yawapasa kujilinda na kuwa tayari"**
**NJB "hivyo jiadharaini kwa amanaia na kwa bidii"**

Huu ni mwanzo wa mlolongo wa kauishurutishi au kauli endelevu zinazotumika kama kauli shurutishi, zenye kusistiza juu ya maisha ya ucha- Mungu (kama vile 1 Pet. 4:6c). Haya maneno mawili yanaurejelea utayari wa kifikra, hasa katika eneo la maombi. Neno la kwanza ni *sōphroneō*. Hili (na miundo yake inayohusiana) linarejelea utulivu, utimamu, uhimara, na kufikiri kwa namna ya juu (hili linatumika maranyingi katika Nyaraka za Paulo za Kichungaji, kama vile f. 1 Tim. 2:9,15; 3:2; 2 Tim. 1:7; Tito 1:8; 2:2,4,5,6,12). Neno la pili ni *nēphō* (na miundo yake inyohusiana), ambalo kifasihi lilihusiana na ulevi, lakini linatumika kiishara kumaanisha mantiki, kujitawala, kufikiri kwa utimamu, kujitawala wenyewe (kama vile 1 The. 5:6,8; 1 Tim. 3:11;Tito 2:2; na 1 Pet. 1:13; 5:8).
Hata hivyo, tambua kwamba Petro anasema kuwa hakuna mwisho wa matukio yenye kuhusianishwa na kurudimkwa Kristo. Yeye anaitumia kweli kama msukumo wake wa kuishi maisha ya ucha -Mungu. Hizi ni zote ni kauli shurutishi za wakati usio timiifu. Huenda jambo hili linahusiana na uzoefu wa Petro ndani ya bustani ya Gethsemani (kama vile Mt. 26:40-41). Mtazamo wa haraka wa Parousia ni utiaji moyo wa kuishi kwa kumfanana Kristo katika kila zama, hasa katikati ya mateso makali.

◙ **"iweni na akili, mkeshe katika sala"** Maombi ni siraha yenye nguvu katika nyakatai za mateso na majaribu (kama vie Efe. 6:18-19), si kwa mtu pekee, bali kwa wengine (kama vile 1 The. 5:17,25; Yakobo 5:16). Kama 1 Pet. 4:3 inavyoeleza juu ya tabia zisizofaa za wapagani wasio amni, 1 Pet. 4:7-11 inaeleza juu ya tabia zinazotarajiwa kwa waamini.

**4:8**
**NASAB, NRSV**
**NJB "juu ya vyote"**
**NKJV "juu ya mambo yote"**
**TEV "juu ya kila kitu"**

Hii ni nahaua ya Kuyunani yeye kuzungumzia kutangulia (kama vile Yakobo 5:12). Upendo ni kumtangulizana (kama vile 1 Pet. 1:22; 3:8; John 13:34;15:12,17; 1 Kor. 13; 1 Yohana 2:7-8; 3:11,23; 4:7-21).

◙ **"juhudi nyingi katika kupendana"** Hii ni kauli tendaji endelevu yenye kutumika kama kali shurutishi. Hii ni mamlaka ya upendo endelevu kwa waamini wengine, ambayo ndiyo dhima ya 1 Petro aliyoitanguliza hapo awali (kama vile 1 Pet. 1:22; 3:8).

◙ **"ninyi kwa ninyii"** Yatambue matumizifungamano ya kifugu "ninyi kwa ninyi" (kama vile 1 Pet. 4:8, 9, na 10). Ukristo ni ushirika. Tumepewa ili tuwape wengine (kama vile 1 Kor. 12:7).

◙ **"upendano husitiri wingi wa dhambi"** Kuna nadharia kadhaa zinazohusiananana kifungu hiki.

1. hii ni nukuu ya Agano la Kale inayotoka katika Mit. 10:12 (kutokana na toleo la MT na si LXX) ambapo upendo hauhesabu mabaya
2. hii inahusiana na Yakobo 5:20 wambapo upendo humsaidia kumrejesha mwenye dhambi atoke dhambini kwa kuiokoa roho na mauti na kufunika wingi wadhambi.
3. Hii inahusiana na Mt. 6:14-15 na Marko 11:25 ambapo msamaha wetu kwa wengine ni uthibitisho wa kusamehewa kwetu (yaani, Origen na Tertullian)

4. Inahusiana na 1 Kor. 13:7, Wakristo wenzetu chini ya mateso

**4:9 "Mkaribishane ninyi kwa ninyi"** Hili ni neno ambatani la neno *phileō* (upendo) na neno *xenos* (mgeni). Hii tendo la kuwapenda wageni lilihitajika hasa kwa Wakristo waliokuwa wakiwatembelea kwa siku ambapo mji wa Insi ukuwa maarufu kwa ouvu (kama vile Mt. 25:35 na kuendelea; Rum. 12:13; 1 Tim. 3:2; Tito 1:8; Ebr. 13:2; 2 Yohana 5-8). Hakuna kitenzi katika kifungu hiki katika andiko la Kiyunani. Kwa sababu ya idadi ya kauli shurutishi, huenda hli ni agizo endelevu.

◙ **"kunung'unika"** Mtazamo wa waamini nimuhimu. Waamini hutambua kuwa hawamiliki cho chote na wao ni mawakili wa kila kitu. Hii sera iliyo wazi haikuwa ya muhimu kwa wahudumu wa kanisa watembeleo watu pekee, bali pia kwa waamini wenyeji waliopoteza kazi zao kwa sababu ya mateso. Hii ni amri, kama wengine wanavyoonyesha msingi wa ushirika wa imani ya Kikristo.

**4:10 "kwa kadiri alivyoipokea karama"** Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakatai uliopita usio timlifue, yenye kumaanisha tendo kamili lililo katika wakati uliopita. Hili neno karama (charisma) linatokana na asili ya neno "neema" (*charis*). Karama hizi hazilazimishwi, ni karama za upendo kwa ajili ya huduma. Kila mwamini anayo karama ya kiroho, aliyopewa na Mungu kupitia wokovu, kwa ajili ya makusudi ya huduma na kwa ajili ya Kanisa (kama vile Rum. 12:6-8; 1 Kor. 12:7,11,18; Efe. 4:7). Hizi karama zaweza kuwa vipaji asilia, ikiwa ni hivyo, kwa nguvu isiyo ya kawaida zinachochewa kwa ajili ya utukufu wa Kristo!
Mtazamo wa kimatendo wa kweli hii ya Agano Jipya ni kwamba kila mwamini anazo kwa wakatgi wote, amehitwa, amekirimiwa kuwa mhudumu wa Kristo (kama vile Efe. 4:12). Kila mwamini ni muhimu kwa ajili ya utendaji imara wa kanisa la mahali. Haya masahihisho ya kibiblia kwa makasi/ waleini kawaida sana katika kanisa la leo, lakini hatyafanyi kazi. Kamwe ulimwengu hautashinda kwa kufunzwa kwa kulipwa au kupewa vitu mbalimbali!

◙ **"itumieni kwa kuhudumiana"** Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo yenye kutumika kama kauli shurutishi. Hii inatokana na neno la Kiyunani la wakii (*diakonos*). Baadaye lilibadilika na kuwa majina ya mashemasi (kama vile Flp. 1:1). Katika Ukristo viongozi ni watumishi, si wakuu. Karama za kiroho ni kwa ajili ya wengine , si kwa ajili yetu (kama vile 1 Kor. 12:7). Karama za kiroho si kwa ajili ya manufaa "kufaidika" bali" kwa kufaidisha huduma."

◙ **"kama mawakili wema"** Kiuhalisia hiki ni kifungu "wakuu wa majumbani." Kanisa ni nyumba ya Mungu (kama vile 1 Pet. 4:17). Waamini watatoa hesabu kwa Mungu kupita Kristo kwa ajili ya uwakii wao wa karama za kiroho (kama vile 1 Kor. 3:10-17; 2 Kor. 5:10).

◙ **"neema mbalimbali za Mungu"** Hili neno "mbalimbali" limejitokeza mara mbili katika 1 Petro, lenye maana ya "tofautitofauti" kama nuru endelevu kupitia mmea. Huu muhtasari unaweka uwiano wa 1 Pet. 1:6. Kwa kila jaribu (kama vile Yakobo 1:2) kuna neena sahihi ya Mungu na Mungu iliyochaguliwa kwa ajili ya upatikanaji kupitia waamni wengine. Hakuna mwamini aliye pekee.

**4:11 "akisema . . . aseme"** Hizi ni kauli mbili shurutishi dalaja la kwanza. Watumishi wakilimiwa na Mungu wanatarajiwa kuzungumza na kuhudumu kupitia nguvu zake. Tukiyazungumzia maneno yake. Ikiwa tunatumika ni kwa nguvu zake.

◙ **"anazojaliwa na Mungu"** Hii ni kauli tendaji elekezi ya wakati uliopo ya neno lililotumika kumaanisha yule anaye fadhiliwa kifedha "kibwagizo" (*chorēgēo*, ambalo mi neno ambatani *choros* na *hēgeomai*). Mungu ana endelea kuzigawa karama zake (kama vile 2 Kor. 9:10, lile lile panoja na neno *epi* lililoambishwa awali, linaojitokeza katika 2 Pet. 1:5,11). Inatia shauku kwamba Paulo anaonekana kumpa Roho karama hizi (kama vile Rum. 12) au kwa Kristo (kama vile Efe. 4:11), lakini Petro anampa Mungu Baba karama hizi. Mfano mwingine ambao nafsi zote za Uungu zimewekwa ndani yao kwa ajili ya kazi ufalme (kama vile 1 Kor. 12:4-6).

◙ **"ili Mungu atukuzwe katika mambo yote kwa Yesu Kristo"** Hiki ni kishazi cha kusudi (*hina*). Karama za kiroho lazima zimtukuze Mungu, si kwa ajili uhusiano wa kibinadamu. Karama zetu ziwe kwa ajili ya Mungu (kama vile Mt. 5:16; 1 Kor.10:31; 1 Pet. 2:12).

◙ **"Utukufu na uweza una yeye hata milele na milele"** Kipengele hiki kinamrejelea Yesu katika muktadha huu (kama vile 2 Tim. 4:18; 2 Pet. 3:18; Ufu. 1:6). Katika Ufu. 5:13 kipengele hiki kinatumika kwa wote Baba na Mwana. Mara nyingine kifungu hiki kinamrejelea Baba (kama vile 1 Pet. 5:11; Rum. 11:36; 16:27; Efe. 3:21; Flp. 4:20; 1 Tim. 1:17; 1 Pet. 5:11; Yuda 25; Ufu. 7:12). Kwa maelezo yanayohsu neno "utukufu" tazama 1:21.

◙ Nyimbo za kumsifu Mungu ni kawaida katika Agano Jipya. Waandishi wa Agano Jipya mara nyingi The NT zilitokea ghafla katika kumsifu Mungu (kama vile Rum. 11:33-36;Efe. 3:20-21; 1 Pet. 5:11).

◙ **"Amina"** Tazama MADA MAALUM: AMINA katika Marko 3 : 28

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 PETRO 4:12-19**
**[12] Wapenzi, msione kuwa ni ajabu ule msiba ulio kati yenu, unaowapata kama moto ili kuwajaribu, kana kwamba ni kitu kigeni kiwapatacho. [13] Lakini kama mnavyoyashiriki mateso ya Kristo, furahini; ili na katika ufunuo wa utukufu wake mfurahi kwa shangwe. [14] Mkilaumiwa kwa ajili ya jina la Kristo ni heri yenu; kwa kuwa Roho wa utukufu na wa Mungu anawakalia. [15] Maana mtu wa kwenu asiteswe kama mwuaji, au mwivi, au mtenda mabaya, au kama mtu ajishughulishaye na mambo ya watu wengine. [16] Lakini ikiwa kwa sababu ni Mkristo asione haya, bali amtukuze Mungu katika jina hilo. [17] Kwa maana wakati umefika wa hukumu kuanza katika nyumba ya Mungu; na ikianza kwetu sisi, mwisho wao wasioitii injili ya Mungu utakuwaje? [18] Na mwenye haki akiokoka kwa shida, yule asiyemcha Mungu na mwenye dhambi ataonekana wapi? [19] Basi wao wateswao kwa mapenzi ya Mungu na wamwekee amana roho zao, katika kutenda mema, kama kwa Muumba mwaminifu.**

**4:12 "Wapenzi"** Hii ni njia ya Baba ya kumrejelea Mwanae (katika ubatizo wa Yesu, kama vile Mt. 3:17; nukuu toka Isa. 42:1,12:18; katika kubadilika kwa Yesu, 17:5). Baadaye hili linaamia kwa wafuasi wake (kama vile 1 Pet. 2:11; 4:12; 2 Pet. 1:17; 3:1,8,15,15,17; na linatumika kwa kurudiwa rudiwa katika maandiko ya Paulo).

◙ **"msione kuwa ni ajabu"** Hii ni kauli tendwa shurutishi yenye kibainishi hasi ambacho mara nyingi hurejelea kustisha tendo ambalo tayarai liko katika mchakato. Waamini hawa walistaajabishwa na mateso haya.

◙ **"ule msiba"** Hii ni stiari ya majaribu na mateso (si matatizo ya maisha ya kawaida ya kila siku, kama vile 1 Pet. 4:14,18; lakini ni kwa namna gani tunaushikilia utamaduni wa maisha yetu ni kwa ushahidi) . Kuna maandiko mengi sana ya kibiblia yenye kudai kuwa mateso na taabu ni hali ya kawaida kwa wale wanaonfuata Kristo kama vile Mt. 5:10-12; Yohana 15:18-21; 16:1-3; 17:14; Matendo ya Mitume 14:22; Rum. 5:3-4; 8:17; 2 Kor. 4:16-18; 6:3-10; 11:23-30; Flp. 1:29; 1 The. 3:3;2 Tim. 3:12; Yakobo 1:2-4; 1 Pet. 4:12-16). Hawa ni wa Baba kwa ajili ya yeye kuuzalisha ufanano na Kristo (kama vile Ebr. 5:8).

◙ **"ulio kati yenu"** Hii si kauli ya wakati ujao, bali kauli endelevu ya wakati uliopo. Hii ilikuwa kweli isiyotarajiwa ya wakati uliopo!

◙ **"ili kuwajaribu"** Hiki ni kitenzi cha Kiyunani *periazō*, tazama Mada Maalum katika Marko 1:13, #2, c.

◙ **"kana kwamba ni kitu kigeni kiwapatacho"** Kifungu hiki kinaweza kuwa na kitenzi ambatani (kauli tendaji endelevu ya wakataia uliopo) yenye kihusishi jua, chenye kumaanisha "shirikiana pamoja na." Waamini hawa walikuwa wanapitia mateso. Walihitaji kujua

1. haikuwa hali ya kawaida kwa waamini
2. hayakuwa matokeo ya dhambi (yaani., Kumb. 27-28)
3. ilikuwa na makusdi katika mapenzi ya Mungu

## MADA MAALUM: KWANINI WAKRISTO WANATESEKA?

1. Kwasababu ya dhambi binafsi (hukumu ya muda). Hii haimaanishi kwamba matatizo yote na mazingira magumu ni matokeo ya dhambi (kama vile Ayubu; Zaburi 73; Luka 14:1-5; Nehemia 9; Yohana 9; Mdo. 5:1-11; 1 Kor. 11:29-30; Gal. 6:7).
2. Kukuza hali ya kufanana na Kristo (Ebr. 5:8). Hata Yesu, ukizungumza kibinadamu alitakiwa akomae na ndivyo inavyowapasa wafuasi wake (kama vile Rum. 5:3-4, 8:28-29; 2 Kor. 12:7-10; Flp. 3:10; Ebr. 12:5-12; Yakobo 1:2-4; 1 Pet. 1:7).
3. Kukuza ushuhuda wenye nguvu na wenye uhalisia (kama vile Mt. 5:10-12; Yohana 15:18-22; 1 Pet. 2:18-21, 3:13-17).
4. Kama ishara ya kuzaa kwa uchungu kwa Zama mpya (kama vile Mt. 24:6; Marko 13:8).

Vitabu viwili ambavyo vimenisaidia mimi kushughulikia kutokuwepo na usawa na uovu wa ulimwengu ulioanguka ni Hannah Whithall Smith, The Christian's Secret of a Happy Life na John W. Wenham, The Goodness of God.
Mwamini lazima akumbuke kwamba matatizo na mateso sio kwamba ni ishara ya hasira ya Mungu au kukataliwa. Vitu vibaya hutokea kwa wafuasi waamiifu katika ulimwengu ulioanguka (kama vile. 1 Pet. 4:12-19). Ahadi za Mungu na kujitoa kwa Kristo ni ishara za upendo wa Mungu (kama vile Rum. 5:8). Maandiko lazima yachukue nafasi juu ya hali za muda!

**4:13"mnavyoyashiriki"** Tazama Mada Maalum hapa chini.

## MADA MAALUM : KOINŌNIA

Neno "ushirika" (*koinōnia*) unamaanisha

1. Ushirika wa karibu na mtu
   a. na Mwana (kama vile 1 Kor 1:9; 1 Yohana 1:6)
   b. na Roho (kama vile. 2 Kor. 13:14; Flp. 2:1)
   c. na Baba na Mwana (kama vile. 1 Yohana 1:3)
   d. na ndugu wa agano wa kiume/kike (kama vile. Matendo 2:42; 2 Kor. 8:23; Gal. 2:9; Filimoni aya. 17; 1 Yohana 1:3,7)
   e. usionauovu (kama vile. 2 Kor. 6:14)
2. ushirika wa karibu na vitu ama makundi
   a. na injili (kama vile Flp. 1:5; Filimoni aya. 6)
   b. na damu ya Kristo (kama vile 1 Kor. 10:16)
   c. usio na giza (kama vile 2 Kor. 6:14)
   d. na mateso (kama vile. 2 Kor. 1:7; Flp. 3:10; 4:14; 1 Pet. 4:13)
3. Zawadi amac hangizo zilizotolewa kwa mtindo wa ukarimu (kama vile Rum. 12:13; 15:26; 2 Kor. 8:4; 9:13; Flp. 4:15; Ebr. 13:16)
4. Kipawa cha Mungu cha neema, kupitia Kristo kinachorejesha ushirika wa mwanadamu na yeye na ndugu zake wa kiume na kike.

Hii inatangaza uhusiano unaofanana (mwanadamu kwa mwanadamu) ambao unaletwa kwa uhusiano wa kweli (mwanadamu na muumbaji). Pia unasisitiza hitaji na furaha ya jumuiya ya Kikristo (yaani, Ebr. 10:25).

◙ **"furahini"** Hii ni kauli tendji shurutishi ya wakatai uliopo. Inashangaza kwamba kuteseka kwa ajili ya Kristo kumeunganishwa na furaha. Hili linaonyesha umuhimu wa mtazamo wa ulimwengu mpya ambao waamini wanaupokea kwa imani pale waiwekapo hatima ya tumaini lao katika Kristo. Yesu mwenyewe aliitaja kweli hii kwa mara ya kwanza katika Mt. 5:10-12. Paulo anaieleza kweli ile ile katika Rum. 5:2,3.

◙ **"ili na katika ufunuo wa utukufu wake"** Kipengele hiki kinakurejelea kurudi kwa Kristo kwa namna ya utukufu kwa ajili ya kuwapokea walio wake (kama vile Yohana 14:1-3).

**4:14 "Mkilaumiwa"** Hii ni sentensi shurutishi daraja la tatu, yenye kudhaaniwa kuwa ya kweli na yenye kukamilika kulingana na mtazamo wa mwandishi au makusudi yake ya kiuandishi.

◙ **"anawakalia"** Hili neno "anawakalia" linatoka katika Mt. 5:11. Ilimpasa Petro kuukumbuka uponyaji aliyouzungunzia Yesu katika kila jambo.

◙ **"ya jina la Kristo"** Kwa jina la . . ."ni nahau ya Agano la Kale yenye kumrejelea mtu. Kuliitia jina la Bwana (yaani., Yoeli 2:32; Matendo 2:21, kama vile Rum. 10:9-13) inamaanisha kumwanini Yesu kama Mwokozi. Kuomba kwa jina la Bwana (kama vile Yohana 14:13; 15:16; 16:23-24) kunamaanisha kuomba kataika nafsi yake na kwa sifa yake.

◙ **"heri yenu"** Hili ni neno la kiyunani *makarios*, llililotumiwa na Yesu katika heri za baraka (kama vile Mt. 5:3-9). Mstari huu unaaikisi Mt. 5:10-12. Kweli ile ile (na neon lie lile) pia iko katika 1 Pet. 3:14. Jambo hili linawashangaza wanauyakinifu wa magharibi kuona hii ile taabu na mateso inaleta furaha na baraka.

◙ **"Roho wa utukufu na wa Mungu anawakalia"** Kwa vyo vyote vile hili ni dokezo la (1) uzoefu wenye kufanana na ubatizo wa Kristo (kama vile Mt. 3:16; Yohana 1:32) au (2) namna Roho alivyomwezesha Masihi (kama vile Isa. 11:2,42:2, 59:21, 61:1). Uzoefu wa Yesu kwa ajili ya mateso sasa ndio tulio nao (kama vile Rum. 8:17). Uwepo wa Roho hauleti wingi wa mali, na mafanikio, bali mateso (kama vile Yohana 15:18; 17:14). Yesu aliahidi kumtuma Roho na atakayetusaidia nyakati za mateso (kama vile Mt. 10:16-23, hasa. 1 Pet. 4:20). Kuna tofauti kadhaa (4) za kifungu hiki katika machapisho ya Kiyunani. Toleo la UBS[4] linaipa moja wapo iliyonukuliwa katika toleo la NASB daraja "A" (yakini).
Toleo la Textus Receptus linakiongeza kifungu katika hoja hii ambacho kinaakisiwa katika toleo la KJV na NKJV: "Kwa upande wao kufedheheshwa, bali kwa upande wetu yeye anatukuzwa." Kifungu hiki kinaonekana katika miundo tofautitofauti katika machapisho ya herufi kubwa tu yaliyofuatia (yaani, Kutoka karne ya 9th; L kutoka karne ya 8; na kutoka karne ya 6 ) na huenda si halisi. Toleo la UBS[4] linaubainisha uondoaji wake kama "yakini."

**4:15 "mtu wa kwenu asiteswe kama"** Hii ni kauli tendaji shurutishi yenye kibainishi hasi anbacho mara nyingi kinamaanisha kustisha tendo ambalo tayari liko katika mchakato.

◙ "**mtenda mabaya"** Neno hili linatumika hapa tu katika maandishi yote ya Kiyunani. Hili ni neon ambatani linalotokana na maneno mawili ya Kiyunani, "kumilikiwa na mwingine" (yaani., *allotrios*) na "kuangalia kwa niaba ya" au "kukagua" (yaani., *episkopos*). Hili pia linamwaakisi mtu mwenye kujishughulisha na mambo ya watu wengine, mwili wenye kushughulika.

**4:16 "ikiwa"** Hii ni sentensi nyingine shurutishi daraja la kwanza, yenye kudhaaniwa kuwa ya kweli. Wakristo walikuwa wakiteseka kwa sababu tu walikuwa Wakristo.

◙ **"Mkristo"** Kiuhalisia hili lilikuwa kundi lenye kudharauliwa (kama vile Matendo 11:26; 26:28). Neno hili limetumika mara tatu katika Agano Jipya. Hili linamaanisha "wakristo wachanga" (yaani, *Christianos*). Huu ulikuwa utambulisho wa kawaida kwa waamini katikati ya karne ya kwanza (yaani, Tacitus, Ann. 15:44).

◙ **"asione haya"** Hii ni kauli tendewa shurutishi ya wakati uliopo yenye kibainishi hasi ambacho mara nyingi kinamaanisha kustisha tendo ambalo tayari liko katika mchakato. Hii inaweza kwa rejea ya Petro juu ya majaribu liyoyapata Yesu usiku pale alipokuwa akifedheheshwa (kama vile Mat. 26:69-75; Marko 14:66-72; Luka 22:56-62; Yohana 18:16-18,25-27).

**4:17 "Kwa maana wakati umefika wa hukumu kuanza"** Hili linaweza kuwa dokezo la Mal. 3:1-6 ambapo hukumu inaanza kwa ujio wa Masihi wa ghafua na kwa namana ya kushangaza kwa watu wake mwenyewe (inatoewa kwa nani, engi yanahitajika, kama vile Yer. 25:29). Ikiwa kuna watenda dhambi wenye kuirudia dhambi kwa makusudi na kwa hiari

miongoniwa watu wa Mungu (na hapa wapo) watahukumiwa kwanza. Tumaini lao pekee ni sifa ya YHWH ya kutobadilika (kama vile Mal. 1:6).

Kifungu hiki pia kinaweza kuwa nahau ya Kiyahudi ya kukaribia kwa Ujio wa Kristo kama Hakimu. Wayahudi wa Agano la Kale (na Mitume wa Agano Jipya) walihitimisha kwa namna ya kutsha ambapo ni historia ya mwanadamu, mara nyingi tendo hili liiitwa "utungu wa kuzaa wa enzi mpya," ambapapolinaelezwa vema na Yesu mwenyewe katika Marko 13:8.

◙ **"katika nyumba ya Mungu"** Kuna sitiari mbili za kiujenzi katika 1 Petro zenye kuhusiana na kanisa : (1) kanisa kama hekalu lililojengwa kwa mawe yaliyo hai (kama vile 1 Pet. 2:4-10) na (2) kanisa kama nyumba ya Mungu (stiari ya ushirika wa watu au nyumba yenye famiia kubwa, kama vile 1 Pet. 4:17; 1 Tim. 3:15; Ebr. 3:6).

◙ "**ikianza"** Hii ni sentensi nyingine shurutishi dalaja la kwanza kama iivyo 1 Pet. 4:16 na 18.

**4:18 "mwenye haki akiokoka kwa shida**" Hililni dokezo la Mit. 11:31katika Agano la Kale la Kibrania ("ikiwa kuna mwenye haki anaokolewa kwa nguvu zote, je! wadhaifu na wenye dhambi watapatikana wapi?").

**4:19 "wateswao kwa mapenzi ya Mungu" Ikiwa katika limwengu huu ni yule** "mwnye haki" ateswaye (Hii sentensi shurutishi daraja la kwanza ya 1 Pet. 4:18), je! kwa wale wasio na haki watatokewa nini katika siku za hukumu ya Mungu? Bwana yuko na walewaliookoewa (kama vile 1 Pet. 3:12,14), lakini yu kinyume na wale walioasi na wasioamini na watesaji (kama vile. 1 Pet. 3:12).

◙ "**wamwekee amana roho zao"** Hii ni kauli ya kati shurutishi ya wakati uliopo yenye kumaanisha kuwa wao wenyewe wanahitaji kuendelea kujitoa kwa Mungu. Paulo aliikabidhi injii kwa Timotheo (kama vile 1 Tim. 1:18). Paulo aliikabidhi injili kwa waamini ili waendelee nayo (kama vile 2 Tim. 2:2). Hili ni neno la kibenki la neno "uhifadhi." Yesu alilitumia neno hii hili wakatai wa kifo chake alipokuwa msalabani. Yeye aliikabidhi roho yake kwa Babaye (kama vile Luka 23:46).

◙ **"Muumba mwaminifu"** Mungu ni mwaminifu! Huu ndiyo ukiri wa kimsingi wa Biblia (kama vile Hes. 23:19; Kumb. 7:9;Isa. 40:8; 49:7; 55:11; 1 Kor. 1:9; 10:23; 2 kor. 1:18; 1 Thes. 5:24; 2 Thes. 3:3; 2 Tim. 2:13 na 1 Pet.1:19). Hii ni tabia ya Mungu isiyobadilika (kama vile Mal. 3:6) ambayo ni tumaini la akika kwa kila mwamini. Mungu atalifanya lile aliliosema kulifanya!

◙ **"katika kutenda mema"** Hili neno la Kiyunanani linamaanisha "kutenda wema" au "kufanya yaliyomazuri." Hii ni dhima yenye kurudiwarudiwa katika Petro (kama vile 1 Pet. 2:14,15,20; 3:6,17; 4:19). Waraka huu unaawaliwa na maonyo yenye kuhitaji maisha ya haki na kujiandaa kwa ajili ya mateso. Tazama MADA MAALUM: KWA NINI WAKRISTO WANATESEKA? katika 1 Pet. 4:14.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki.

1. Orodhesha mambo yanayopaswa kufanywa na waamini kwa sababu ya kukaribia kwa Ujio wa mara ya Pili.
2. Je! Agano Jipya linatarajia kuja kwa Bwana kuwai au kuchelewa sana?
3. Ni kwa namna gani upendo hustiri wingi wa dhambi? Dhambi zipi?
4. Je! Lazima kila Mkristo awe na karama za kiroho? Ikiwa ni hivyo, kwa nini?
5. Je! Mateso ni ya kawaida kwa waamini au si kawaida kwa waamini?
6. Nini makusudi ya kuteseke bila hati na najaribu katika maisha ya waamini?
7. Ni kwa namna gani Wakristo wanapaswa kuyapokea mateso yasiyo na hatia?
8. Je! Wakristo watahukumiwa? Kwa namna gani? Kwa nini?

# 1 PETRO 5

| MIGAWANYO YA AYA KATIKA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **UBS[4]** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Mafundisho ya Kundi la Mungu | Kulichunga Kundi la Mungu | Kuhitimisha Nasaha na Salamu | Kundi la Mungu | Maangizo:Kwa Wazee |
| 5:1-4 | 5:1-4 | 5:1-5 | 5:1-4 | 5:1-4 |
| | Kumtii Mugu, Mapambano ya Kumpinga Ibilisi | | | Maagizo: kwa Waaminifu |
| 5:5 | 5:5-11 | | 5:5-7 | 5:5-11 |
| 5:6-7 | | 5:6-11 | | |
| 5:8-11 | | 5:8-11 | | |
| Salamau za Mwisho | Maagano na Amani | | Salamu za Mwisho | Maneno ya salamu za Mwisho |
| 5:12-14 | 5:12-14 | 5:12-14a | 5:12 | 5:12 |
| | | | 5:13-14a | 5:13 |
| | | 5:14b | 5:14b | 5:14 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka "Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 PETRO 5:1-5**
**1 Nawasihi wazee walio kwenu, mimi niliye mzee, mwenzi wao, na shahidi wa mateso ya Kristo, na mshirika wa**
**utukufu utakaofunuliwa baadaye; 2 lichungeni kundi la Mungu lililo kwenu, na kulisimamia, si kwa kulazimishwa,**
**bali kwa hiari kama Mungu atakavyo; si kwa kutaka fedha ya aibu, bali kwa moyo. 3 Wala si kama wajifanyao**
**mabwana juu ya mitaa yao, bali kwa kujifanya vielelezo kwa lile kundi. 4 Na Mchungaji mkuu atakapodhihirishwa,**

**mtaipokea taji ya utukufu, ile isiyokauka. [5] Vivyo hivyo ninyi vijana, watiini wazee. Naam, ninyi nyote jifungeni unyenyekevu, mpate kuhudumiana; kwa sababu Mungu huwapinga wenye kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema.**

**5:1 "wazee. . . mimi niliye mzee" Hii ni minu ya kucheza na maneno ya neno mzee** (*presbuteros*) katika 1 Pet. 5:1 na 5. Hili neno kwa uwazi linatumika kama cheo cha uongozi (kama vile 1 Pet. 5:1) na kutoa wasifu wa umri (kama vile1 Pet. 5:5). Matumizi ya neno hili yanashangaza kwa kuzingatia kwamba kimsingi huu ni wasifu wa uongozi wa kikabila kwa Wayahudi, ambapo neno "askofu" au "msimamizi" (*episcopos*) alikuwa na wasifu wa uongozi wa kuongoza serikali ya Kiyunani. 1 analitumia maneno ya Kiyunani kuwaasa waamini wa Mataifa .Petro anajiita "niliye mzee,"hili neno *presbuteros* kuongeza kihusishi *syn*, ambacho kinamaanisha "ushiriki unganifu." Petro haelezei juu ya Mamlaka yake ya ki-Utume (kama vile 2 Yohana 1 ambapo Mtume mwingine anajiita "mzee"), anawaonya (yaani., "Nawasihi," kauli tendaji elekezi ya wakati uliopo) viongozi wenyeji kutenda na kuishi sawa na nuru ilivyo katika

1. Mfano wa Kristo
2. Kukaribia kwa kurudi kwake

Makanisa ya mwanzo hayakuwa na nafasi za uongozi, bali yalizitambua karama za uongozi zilizotolewa na Mungu na uongozi ulio katika kila kanisa la wenyeji. Huu uthibitisho wa tunu hii ulitakiwa kuwekewa ulinganifu pamoja na ule wa kitamaduni wa "hekima ya watu wazima," hasa miongoni mwa jamii ya Wayahudi waaminio. Hivyo, Petro anatoa nasaha kwa aina zote za uongozi.

Pia tambua kuwa neno "wazee" ni wingi. Hili linaweza kurejelea juu ya (1) adadi ya viongozi wa makanisa ya nyumbani (kama vile Matendo 20:17) au (2) karama tofautitofauti za kiroho miongoni mwa kundi la wazee (kama vile Efe. 4:11), ambazo kwa uwazi zinaelezea kwamba huduma ni kwa ajili ya waamini wote. Hili linafanana na dhana ya "ufalme wa makuhani" (kama vile1 Pet. 2:5,9).

◙" **shahidi wa mateso ya Kristo**" Huu ni uthibitisho wa ukusanyaji wa ushahidi wa macho wa Petro kuhuisu maisha ya Yesu (kama vile Matendo 3:15; 10:39). Pia unaweza kuaksi kumbukumbu ya Petro kuhusiana na maneno ya Yesu katika Matendo 1:8. Hili neno "mateso" linaurejelea usulibishaji. Petrlitumia neno mateso mara kwa mara (kama vile1 Pet. 1:11; 2:19,20,21,23; 3:14,17,18; 4:1[mara mbili],13,15,19; 5:1,10). Mjadala unaohusu Yesu kuteseka kama mkombozi wa vyote na kama mfano kwa waamini wanaopaswa kuufuata, uaunda wazo kuu katika 1 Petro.

◙ "**mshirika wa utukufu utakaofunuliwa**" Hii si rejea pekee ijayo kuhusu Kuja kwa mara ya Pili (kama vile 1 Pet. 1:5,7; 4:13; 5:4), bali huenda ni rejea ya ushahidi wa macho uliorudiwa (ukumbusho) wa Mabadiliko (kama vile Mt. 17; Marko 9:2-8; 2 Pet. 1:16-18). Tazama Mada Maalum: Utukufu katika Marko 10:37. 5:2 "mchungaji wa kundi la Mungu"
Hii ni kauli tendaji shurutishi za wakati usio timilifu. Neno"Mchungaji" ni stiari ya Agano la Kale yenye kummaanisha Mungu (kkama vile Zab. 23:1; 100:3). Baadaye ilibadilika kuwa cheo cha wazee (kama vile Eze. 34:7-10). Kondi linahitaji uangalizi,ulinzi, na umakini. Yesu anaitwa "Mchungaji Mwema" katikaYohana 10 na anamwambia Petro kuwa mchungaji wa kondoo wake katika Yohana 21. Katika Agano Jipya kuna majina kadhaa ya majina ya viongozi wa makanisa ya wenyeji.

1. Wazee
2. Wasimamizi au maaskofu
3. Wachungaji au mashemasi

Haya yote yanaonekana kutumika namna ya mbadilishano (kama vile Matendo 20:17,28 na Tito 1:5,7).

**NASB " kulisimamia"**
**NKJV "mkilitumikia kama wasimamizi"**
**NRSV "kulisimamia"**
**TEV -linaondoa**
**TEV -linaondoa**

Machapisho kadhaa ya Kiyunani (yaani., $P^{72}$, $\aleph^{2}$, A, P, na Toleo la Kiyunani) yajumuisha muundo wa kivitenzi (kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo) wa neno "msimamizi" linalotumika katika viunganishi pamojana kazi ya wazee.

Baadhi ya machapisho ya kale yanaiondoa hali ya uendelevu (yaani., א* na B). Haijulikani kama ondoleo hili ni makusudi ya waandishi ambaoa hawakuwa na uhakika wa maneo ya kufanyia kazi au kazi ya wazee na wasimamizi.

**5:2-3** Hii inaanza na mlolongo mlolongo (kama vile1 Pet. 5:2-3) wa kuzitofautisha sifa za wazee wa kanisa.

| | Yakinifu | Kanusho |
|---|---|---|
| 1. | hiari | si chini ya amri |
| 2. | kwa shauku | si kwa huzuni nyingine |
| 3. | kama mfano | milki |

Mtu anashangaa ni kwa namna gani hizi kanushi zinaakisi hali halisi za uongozi wa baadhi ya makanisa za nyumbani unaohusiana na walimu wa uongo (kama vile 2 Petro).

◙ **"kama Mungu atakavyo"** Kifungu hiki ni kimo katika machapisho mengi ya kale ya Kiyunani (yaani., $P^{72}$,$א^{2}$, A, na P), lakini kimeondolewa katika MSS B, K,na L. Hiki kimo katika tafsiri nyingi za Kiingereza, kinakosekana katika KJV. Petro anakitumia kifungu hiki mara kwa mara katika 1 Petro (kama vile 1 Pet. 2:15; 3:17; 4:2,3,19). Hivyo, huenda kilikuwa kifungu halisi.

◙**" vielelezo"** Tazama Mada Maalum ifuatayo.

**5:4** "**Mchungaji mkuu**" Istilahi ya Petro ya Kristo kama Mchungaji (kama vile 1 Pet. 2:25) inaweza kuwa imetokana na ufmazungumzo kati yake na Bwana aliyefufuka ambayo yamenukiliwa yanaelezwa katika Yohana 21:15-17. Hapa Petro anamwita Kristo kwa ku neno ambatani *archi* pamoja na *poimen*, lenye kumaanisha kuu au mchungaji wa kwanza (kama vile Yohana. 10:1-18). Katika Ebr. 13:20 Kristo anaelezwa kama "Mchungaji mkuu." Viongozi wengine wote ("wazee" au "wasimamizi") wako chini ya wachungaji.
Inawezekana kwamba Petro anadokeza juu ya Isa. 63:11, ambapo Musa anaitwa "mchungaji."

◙ **"atakapodhihirishwa"** Hili ni rejea nyingine ya Kuja mara ya Pili (kama vile 1 Pet. 5:1; 1:5,7; 4:13).

◙ **"ile isiyokauka"**Katika muktadha huu (yaani., 1 Pet. 5:1-5) kifungu hiki kinarejelea juu ya kifungu "chini ya wachungaji." Petro anachanganya stiari ya kiriadha (kama vile 1 Kor. 9:23) pamoja na stiari ya mimea. Hili tajj ya utukufu isiyoharibika inaweza kuurejelea urithi wa waamini iliyotunzwa na Mung katika 1 Pet. 1:4. Hii ni sawa na
1. Paulo "taji ya haki" katika 2 Tim. 4:8
2. Yakobo '"taji ya uzima" katika Yakobo 1:12
3. Yesu' "taji ya uzima" katika Ufu. 2:10; 3:11

Hii ni ishara ya ushindi wa mwamini katika mapambano dhid ya dhambi, wenyewe, pamija na eir uvumilivu wao, fuaminifu wa kuteseka kwa ajili ya Kristo.

**5:5 "ninyi vijana"** Katika jamii ya Kiyahudi mtoto wa kiume alifikiriwa kuwa kijana hadi kufikia umri wa miaka arobaini. Kulitakiwa kuwepo uwazi kati ya kizazi ndani ya jamii ya waaminio, lakini yenye maafikiano ya kuheshimiana (yaani., "vivyo hivyo" ya 1 Pet. 5:5).

◙ **"watiini wazee"** Hii ni kauli tendwa shurutishi ya wakati usio timilifu enye kueleza maisha yenye utaratibu thabiti. Muktadha huu unamaanisha kwamba neno "wazee" la1 Pet. 5:1 ni sawa na "wazee" la 1 Pet. 5:5. Hata hivyo, neno "vijana" lazima liakisi tofauti (kama vile 1 Tim. 5:1, inayomrejelea mtu mzee, ambapo 1 Tim. 5:17 inamarejelea mzee wa kanisa). Tazama Mada Maalum: Utii Pet. 2:13.

◙ **"ninyi nyote"** Petro anazidi kuwaasa wazee wa kanisa na watu wengine wa kusanyiko la watu wote wa kanisa (kama vile Efe. 5:21). Ni muhimu kwamba waamini wayaelewe majukumu yaoa binafsi kwa amani na umoja katika ushirika (kama vile Efe. 4:2-3).

◙ **"jifungeni "**Hii ni kauli ya kati shurutishi ya wakati usio timilifu. Kujivika na kujivua ni nahau ya kibiblia kwa mwenendo wa maisha ya waamini (kama vile Ayubu 29:14; Zab. 109:29; Isa. 61:10; Efe. 4:22,24,25,31). Yawapasa kuzivaa tabia za Mungu na kujivika roho ya unyenyekevu. Neno la Kiyunani la "kuvaa"kiuhalisia ni "funga." Inawezekana kwamba Petro anayaaksi matendo ya Yesu aliyoyafanya ghorofani, yaliyoandikwa katika Yohana 13:2-11 (Yesu alijifunga kwa kitambaa cha watumwa na kuwaosha wanafaunzi miguu). Petro aliuona unyenyekevu wa kweli na sasa anawahitaji waamini kumfuatisha Kristo (kama vile Flp. 2:8; Yakobo 4:10).

◙ **"unyenyekevu"** Hili ni neno ambatani la "unyenyekevun" na "fahamu." Tazama maelezo katika 1 Pet. 3:8.

◙ **"kuhudumiana"** Huu ni msistizo unaotolewa kwa jamii (kama vile 1 Pet. 3:9; Efe. 5:21). Waamini wamepewa (na kukirimiwa, kama vile 1 Kor. 12:7) kwa kila mmoja. Tunasimama au kuanguka kwa pamoja!

◙ **"kwa sababu Mungu huwapinga wenye kiburi, lakini huwapa wanyenyekevu neema"** Hii ni nukuu toka Mit. 3:34 (kama vile Yakobo 4:6). Hili neno "neema" katika Agano la Kale linatumika kwa maana ya "upendeleo."

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 PETRO 5:6-11**
**[6] Basi nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio hodari, ili awakweze kwa wakati wake; [7] huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu. [8] Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama simba angurumaye, huzunguka-zunguka, akitafuta mtu ammeze. [9] Nanyi mpingeni huyo, mkiwa thabiti katika imani, mkijua ya kuwa mateso yale yale yanatimizwa kwa ndugu zenu walioko duniani.**
**[10] Na Mungu wa neema yote, aliyewaita kuingia katika utukufu wake wa milele katika Kristo, mkiisha kuteswa kwa muda kidogo, yeye mwenyewe atawatengeneza, na kuwathibitisha, na kuwatia nguvu. [11] Uweza una yeye hata milele na milele. Amina.**

**5:6 "nyenyekeeni"** Hii ni kauli tendwaji shurutishi ya wakati usio timilifu. Hii ndio sifa bainishi ya Yesu (kama vile Mt. 11:29) ambayo ilikuja kuwa kipimo cha wafuasi wake (kama vile Yakobo 4:10).

◙ **"mkono wa Mungu ulio hodari"** Hiki ni kifungu cha kumweleza Mungu kama mwanadamu (kama vile Yakobo 4:6,10) chenye kuzungumzia juu ya uangalizi, utoaji, na uaminifu wa pendo la Mungu, hata katikati ya mateso. Yeye ni "mkono usioonekana," kama ilivyo katika Estha!

◙ **"ili awakweze"** Kipengele hiki kinaakisiwa na maneno ya Yesu iliyo katika Mt. 23:12 na onyo la Yakobo katika Yakobo 4:6. YHWH anachorwa mara kwa mara kama mwenye kupinga majivuno na mwenye kuwanyenyekeza wanaojishusha (kama vile Ayubu 5:11; Ps. 138:6; Mit. 3:34; Eze. 17:24; 21:26).

**NASAB** **"kwa wakati wake"**
**NKJV, NRSV,**
**NJB** **"wakati wake mwenyewe"**
**TEV** **"katika wakati wake"**

Katika muktadha huu hili jambo hili linatenda kazi katika makusudi mawili ya kithiolojia: (1) kwa sasa wasomaji wanayapitia mateso, si furaha na (2) wakatai wa kufurahia ni ule wa Ujio wa mara ya Pili. Utayari, unyenyekevu, na kutokuwa fadhaa ni mambo muhimu mbelekatikakati ya mateso yaliyovuviwa na Shetani.

**5:7 "mkimtwika yeye fadhaa zenu"** Hii ni kauli tendji endelevu ya wakati usio timilifu yenye kutumika kama kauli shurutishi na inaweza kuwa dokezo lenye kuidokeza Zab. 55:22 katika Agano la Kale la Kiebrania. Hii ni nahau ya kuyaondoa masumbufu ya mtu kifikra na kumtwika Kristo (kama vile Mt. 6:25). Yeye huyabeba kwa ajili yetu hata katikati ya mateso na maumivu. Yeye anachoshwa nadhambi zetu na sasa anazibeba fadhaa zetu na hofu zetu!
Waamini wanaweza kulifanya hili kwa kuwa twajua ya kuwa anatutunza. Tunajua hili kutokana na :

1. Kifo chake (kama 1 Pet. 2:22-24; 3:18)

2. Upatanisho wake (kama vile1 Yohana 2:1-2)
3. Uchungaji wake (kama vile 1 Pet. 2:25; 5:4)

**5:8 "Mwe na kiasi, na kukesha"** Hizi ni kauli tendaji shurutishi za wati usio timilifu. Yawapasa waamini kufanya hatima ya uchuguzi wa kuwa tayari kifikra (kama vile Mt. 24:42; 25:13; 26:41; Marko 13:35,37; 14:38; Matendo 20:31; 1 Kor. 16:13; Kol. 4:2; 1 The. 5:6,10; Ufu. 3:2-3; 16:15). Petro ameyasistiza haya (yaani., kiasi na kukesha) kabla (kama 1 Pet. 1:13; 4:7). Ukeshaji na kufikiri vema vinaweza kuishinda hofu na majaribu.

◙ **"mshitaki wenu Ibilisi"** Hili neno "mshataki" linaliakisi jina la Kiebrania Shetani (limetumika mara 36 katika Agano Jipya), lenye kumaanisha mshtaki. Hili jina "Ibilisil" (limetumika 37 mara katika Agano Jipya) ni neno ambatani la Kiyunani "kutupa kando" lenye maana ya tupilia mbali. Tazama Mada Maalum hapa chini.

## MADA MAALUM :UOVU BINAFSI

Hili ni somo gumu kutokana na sababu mbali mbali:

1. Agano la Kale halibainishi adui mkubwa wa (Mungu), bali mtumishi wa YHWH ambaye anawapa wanadamu mbadala na kutuhumu huyu mwanadamu kwa kutokuwa na haki (A. B. Davidson,

*A Theology of the OT,* kur. 300-306).

2. Dhana ya adui mkubwa wa Mungu ulianza wakati wa fasili kati ya Biblia (zisizo na taratibu za kikanisa) katika kipindi cha dini ya kiislamu iliyoanzishwa na Zoroaster huko Uajemi. Hii kwa namna nyingine, kwa kiwango kikubwa ilisababisha sheria ya dini ya Kiyahudi (yaani, waliokuwa wametengwa na kuishi nje ya Israel yaani Babiloni, na Persia).
3. Agano Jipya linaunda dharura ya Agano la Kale katika ugumu wa ajabu lakini makundi yaliyochaguliwa

kama mtu anaanza kusoma habari za uovu katika mtizamo wa thiolojia ya biblia (kila kitabu au mwandishi au michoro alisoma na kuandika kwa kifupi kwa kutenganisha) basi mawazo mbalimbali kuhusu uovu yangeibuliwa. hata hivyo, mtu ataanza kusoma kuhusu uovu lakini kwa njia isiyo ya kibiblia au nje zaidi ya biblia mfano dini za kiulimwengu au dini za mashariki, basi sehemu kubwa ya mambo mengi ya maendeleo ya agano jipya yalionyeshwa katika pande mbili za uajemi na tabia za uyunani na kiroma.

Kama mtu alidhaniwa kujitoa kwa uwezo wa kiungu neno la Mungu (kama nilivyo!),kwa hiyo mambo ya Agano Jipya lazima yaonekane kama ufunuo endelevu. Wakristo yawapasa wajilinde dhidi ya kuruhusu simulizi za Kiyahudi au fasihi za Kiingereza (yaani, Dante, Milton) kufafanua zaidi dhana hiyo bila shaka miujiza na maana tofauti tofauti katika eneo hili la wokovu. Mungu amechagua kutobainisha mambo yote ya uovu, asili yake,kusudi lake,lakini amebainisha kushindwa kwake!

Katika Agano la kale neno Shetani au mshitaki linaonekana kuhusiana na makundi matatu tofauti.

1. Washtaki wa wanadamu (1 Sam. 29:4; 2 Sam. 19:22; 1 Fal. 5:4, 11:14,23,25; Zab. 109:6,20,29
2. Washtaki wa kimalaika (Hes. 22:22-23; Zak. 3:1)
3. Washtaki wa kimapepo (bila shaka shetani) (1 Fal. 22:21; Zak. 13:2)

Baadaye katika kipindi cha kuingia agano jipya ibilisi wa Mwanzo 3 alijulikana ni shetani (kama vile Kitabu cha Hekima 2:23-24; II Enoch 31:3), na hata baadaye ambapo anakuja kuwa chaguo la viongozi wa kidini wa Uyahudi (kama vile. *Sot* 9b na *Sanh*. 29a). "wana wa Mungu" wa Mwanzo 6 wanakuwa malaika wa uovu katika I Enoch 54:6. Wanakuwa waanzilishi wa uovu katika thiolojia ya viongozi wa kidini wa Kiyahudi. Nalitaja hili sio kwa kuonyesha usahihi wake wa kithiolojia, bali kuonyesha maendeleo yake katika Agano Jipya, shuguli hizi za Agano la Kale zinachangia katika uovu wa malaika wa nuru (yaani shetani) katika 2 Kor. 11:3; Ufu. 12:9.

Asili ya uovu wa yule aliyejigeuza kuwa malaika wa nuru ni mgumu au haiwezekani (kutegemea maoni yako) kuupima toka katika Agano la Kale. Sababu moja wapo ni ile imani ya nguvu juu ya uwepo wa Mungu mmoja tu. (kama vile. Kumb. 6:4-6; 1 Fal. 22:20-22; Mhu. 7:14; Isa. 45:7; Amos 3:6). Majeruhi wote walipelekea YHWH kuonyesha kwa vitendo alivyo wa pekee na mkuu (kama vile. Isa. 43:11; 44:6,8,24; 45:5-6,14,18,21,22).

Uwezekano wa vyanzo vya habari ni (1) Ayubu 1-2, ambapo shetani ni mojawapo wa wana wa Mungu "mwana wa Mungu" (yaani, malaika) au (2) Isaya 14; Ezekieli 28, ambapo ujivuni karibu na wafalme wa mashariki (Babeli na Uturuki) wamekuwa wakielezea sifa au ujivuni wa shetani (kama vile 1 Tim. 3:6). Nimechanganya mihemko kuhusu

kuliendea suala hili. Ezekieli anatumia bustani ya Edeni kama neno mbadala sio tu kwa mfalme wa Uturuki kama shetani (kama vile. Eze. 28:12-16), lakini pia kwa ufalme wa Misri kama mti wa maarifa wa mema na mabaya (Ezekieli 31). Hata hivyo, Isaya 14, hasa kurasa 12-14, anaonekana kuelezea uasi wa malaika kupitia majivuno kama Mungu alivyotaka kubainisha kwetu jinsi alivyo hasa na asili ya shetani hii ni njia isiyo elezea moja kwa moja na mahali pa kuifanya (tazama Mada Mada Maalumu: Lusifa). Lazima tujilinde dhidi ya mwenendo wa Theolojia wa kuchukua sehemu ndogo ndogo, tata toka kwenye maeneo yenye maana mbalimbali ya waandishi, vitabu, na kuviunganisha kama vipande vipande vya fumbo la Kiungu.

Alfred Edersheim (*The Life and Times of Jesus the Messiah*, juzuu. 2, kiambatisho XIII [kur.. 748-763] na XVI [kur. 770-776]) anasema mafundisho ya sheria za Kiyahudi yameathiriwa wazi kabisa na umiliki wa pande mbili za Uajemi na mtizamo wa kimapepo. Viongozi hawa wa kidini sio vyanzo vizuri vya ukweli katika eneo. Yesu kimsingi anakwepa kutoka kwenye mafundisho ya sinagogi. Nafikiri kuwa dhana ya viongozi wa dini ya kiyahudi ya upatanisho wa kimalaika (kama vile Matendo 7:53) na upinzani katika kutoa sheria za Musa kwenye mlima Sinai ilifungua mlango kwa dhana ya adui mkuu wa YHWH kadhalika na mwanadamu. Palikuwa na Mungu wawili wa pande mbili za Iran (ufuasi wa Zoroastra).

1. *Ahura Mazda,* baadaye akaitwa *Ohrmazd*, aliyekuwa mungu muumbaji, mungu mwema
2. *Angra Mainyu,*baadaye aliitwa *Ahriman*,roho aangamizaye, mungu mwovu,

Vita juu ya ukuu na dunia ikawa kama uwanja wa vita. Umiliki wa pande mbili ukajengeka ndani ya pande mbili za Kiyahudi zenye ukomo kati ya YHWH na shetani.

Hakika kuna mafunuo endelevu katika agano Jipya kama ilivyo kwenye uovu, lakini sio kama ilivyoelezewa kama walimu wa dini ya Kiyahudi wanavyodai. mfano mzuri wa utofauti huu ni "vita vya mbinguni." Kuanguka kwa shetani (Mwovu) ni mantiki yenye umuhimu, lakini sehemu husika haikutolewa (Tazama Mada Maalumu: Kuanguka kwa shetani na malaika wake). Hata hivyo kile kilichotolewa kimefichika kwenye mafunuo tanzu (k.v. Ufu. 12:4,7,12-13). Ingawa shetani ameshindwa na kutupwa duniani, bado anatenda kazi kama mtumishi wa YHWH (kama vile. Mt. 4:1; Luka 22:31-32; 1 Kor. 5:5; 1 Tim. 1:20).

Lazima tuthibiti kiu yetu katika eneo hili. Kuna nguvu binafsi ya majaribu na uovu lakini bado kuna Mungu mmoja tu na mwanadamu bado anawajibika kwa uchaguzi wake. kuna vita ya kiroho kabla na baada ya wokovu. Ushindi waweza kuja tu na kubakia ndani na kupitia Mungu wa Utatu. Uovu umekwisha shindwa na utaondolewa.

◙ **"angurumaye, huzunguka-zunguka"** Hii stiari ya mnyama yemye kumaanisha Shetani huenda inatoka kataika Agao la Kale.

1. ishara ya adaui mwenye nguvu (kama vile Zab. 7:2; 10:2; 17:12; 22:13,21; 2 Tim. 4:17)
2. moja ya njia za Mungu kuwahukumu watu wake (kama vile 2 Fal. 17:25; Isa. 15:9; Yer. 50:17)

◙ **"akitafuta mtu ammeze"** Hatima ya kusudi la shetani inawekwa wazi—uharibifu na kifo. Ni adui yale yaliyo mema, ya ki- Mungu, na ya kweli.

**5:9 "mpingeni huyo"** Hii ni kauli nyingine tendaji shurutishi ya wakati usio timilifu. Katika Yesu waamini wanayo nguvu ya kumpinga ibilisi na yule mwovu! Katika Yakobo 4:7 onyo kama hili linahusianishwa na Shetani, lakini hapa linaunganishwa na mateso na taabu endelevu. Ushindi dhidi ya Ibilisi si kutokuwepo kwa mateso!

◙ "**mkiwa thabiti katika imani"** Yawapasa waamini kuendelea katika imani yao (kama vile Kol. 2:5). Mafanikio na afya si ishara za Baraka za Mungu za mara kwa mara (kama vile Ayubu, Zab. 73). Yawapasa waamini kuitendea kazi imani yao katika mambo yote. Kuendelea huku ni muhimu (kama vile Matendo 14:22; Rum. 8:17).

## MADA MAALUM : USTAHIMILIVU

Mafundisho ya kibiblia yaliyohusiana na maisha ya Mkristo ni vigumu kuyaelezea kwa sababu yanawasilishwa katika namna ile ile ya mashariki, milinganyo ya kirahaja (tazama Mada Maalumu: Fasihi ya Mashariki [mafumbo ya kibiblia]). Milinganyo hii inaonekana kuwa na mkanganyiko, bado mihimili yote ni ya kibiblia. Wakristo wa Mashariki walielekea

kuchagua ukweli ulio mmoja na kuachana au kukashifu kweli iliyo kinyume. Baadhi ya Mifano ni:

1. Je! Wokovu ni maamuzi asilia ya kumwamini Kristo au ni maisha yenye wajibu ya kiuwanafunzi?
2. Je! Wokovu ni uchaguzi kwa maana ya neema kutoka katika mamlaka ya Mungu au imani na mwitikio wa toba kwa sehemu ya mwanadamu kwa majitoleo ya Mungu?
3. Je! wokovu, unapopokelewa, haiwezekani kuupoteza, au kuna uhitaji wa jitihada endelevu

Jambo hili la ustahimilivu limekuwa la kibishi katika historia nzima ya kanisa. Tatizo linaanza na muonekano wa mgogoro wa vifungu vya Agano Jipya:

1. maandiko yahusuyo uhakika
    a. semi za Yesu katika Injili ya Yohana (Yohana 6:37; 10:28-29)
    b. semi za Paulo (Rum. 8:35-39; Efe. 1:13; 2:5,8-9; Flp. 1:6; 2:13; 2 The. 3:3; 2 Tim. 1:12; 4:18)
    c. semi za Petro (1 Pet. 1:4-5)
2. maandiko yahusuyo umuhimu wa ustahimilivu
    a. semi za Yesu katika Injili za Kimhutasari (Mt. 10:22; 13:1-9,24-30; 24:13; Marko 13:13)
    b. semi za Yesu katika Injili ya Yohana (Yohana 8:31; 15:4-10)
    c. semi za Paulo (Rum. 11:22; 1 Kor. 15:2; 2 Kor. 13:5; Gal. 1:6; 3:4; 5:4; 6:9; Flp. 2:12; 3:18-20; Kol. 1:23; 2 Tim. 3:2)
    d. semi za mwandishi wa Kiebrania (2:1; 3:6,14; 4:14; 6:11)
    e. semi za Yohana (1 Yohana 2:6; 2 Yohana 9; Ufu. 2:7,17,26; 3:5,12,21; 21:7)

Mambo ya wokovu ndani ya biblia hutoka katika pendo, huruma, na neema ya mamlaka ya Mungu wa Utatu. Hakuna mwanadamu awezaye kuokolewa pasipo kuingiliwa na Roho (kama vile Yohana 6:44,65). Mungu alikuja na kupangilia mambo muhimu, lakini alidai kwamba wanadamu wanapaswa kuitikia katika imani na toba, katika namna zote kwa uanzilishi na kwa uendelevu. Mungu hutenda kazi na wanadamu katika uhusiano wa agano. Kuna upendeleo na majukumu!

Wokovu umetolewa kwa wanadamu wote. Kifo cha Yesu kilihusika na tatizo la dhambi ya uumbaji ulioanguka! Mungu ameleta njia na anahitaji wale wote walioumbwa kwa mfano Wake kuliitikia pendo Lake na utoaji katika Yesu. Kama ungependa kusoma zaidi juu ya somo hili tazama

1. Dale Moody, *The Word of Truth*, Eerdmans, 1981 (kur. 348-365)
2. Howard Marshall, *Kept by the Power of God*, Bethany Fellowship, 1969
3. Robert Shank, *Life in the Son*, Westcott, 1961

Biblia inashughulikia matatizo mawili tofauti katika eneo hili: (1) kuchukulia imani kama msimamo wa kuishi bila kuzaa matunda, maisha ya ubinafsi au (2) kuwatia moyo wale wanaopambana na huduma na dhambi binafsi. Tatizo ni kwamba makundi yasiyo sahihi yana uchukuwa ujumbe usio sahihi na kutengeneza mifumo ya kitheolojia yenye vifungu vya kibiblia vyenye kuwekewa mipaka. Baadhi ya Wakristo wakiwa katika hali ya kukata tamaa wanahitaji ujumbe wa kuwatia moyo, wakati wengine wanahitaji kuonywa kwa ukali kuhusiana na uvumilivu! Wewe uko ndani ya kundi lipi?

Kuna mabishano ya historia ya kitheolojia iliyomuhusisha Augustine dhidi ya Pelagius na Calvin dhidi ya Arminius (semi-Pelagian). Jambo hili lilihusisha swali la wokovu : kama mtu akiokolewa kiukweli, yampasa kustahimili katika imani na uamiifu?

Wafuasi wa Calvin wamesimama nyuma ya maandiko yale ya kibiblia ambayo yanadai kwamba mamlaka ya Mungu na nguvu idumuyo (Yohana 10:27-30; Rum. 8:31-39; 1 Yohana 5:13,18; 1 Pet. 1:3-5) na vitenzi vya nyakati kama kauli tendewa timilifu endelevu ya Efe. 2:5,8.

Wafuasi wa Arminius wamesimamia maandiko yale ya kibiblia ambayo yanamuonya yule aaminiye "kusimama imara," "kudumu," au "kuendelea" (Mt. 10:22; 24:9-13; Marko 13:13; Yohana 15:4-6; 1 Kor. 15:2; Gal. 6:9; Ufu. 2:7,11,17,26; 3:5,12,21; 21:7). Mimi binafsi siamini kwamba Waebrania 6 na 10 zinatumika, lakini wafuasi wengi wa Arminius wanazitumia kama onyo dhidi ya uasi. Mfano wa Mpanzi katika Mathayo 13 na Marko 4 inashughulikia suala la imani, kama inavyofanya Yohana 8:31-59. Kama wafuasi wa Calvin wanavyo nukuu vitenzi vya kauli ya wakati uliopo timilifu vilivyotumika kueleza wokovu, Wafuasi wa Arminius wana nukuu vifungu vya kauli ya wakati uliopo kama 1 Kor. 1:18; 15:2; 2 Kor. 2:15.

- Huu ni mfano kamili wa namna mfumo wa kitheolijia unayotumia vibaya njia ya uhakiki wa fasiri za maandiko. Mara nyingi kanuni inayoongoza au andiko kuu linatumika kutengeneza ufito wa kitheolojia

ambapo maandiko mengine yote yanatazamiwa. Kuwa makini na mfumo kutoka vyanzo vyo vyote vile. Vitokana na ufafanuzi wa mantiki ya mashariki, si ufunuo. Biblia ni kitabu cha mashariki. Inawakilisha kweli katika mvutano uliokamilishwa, ulinganifu wa mafumbo yaonekanayo. Wakristo wanamaanisha kukubaliana na yote na kuishi ndani ya mvutano huo. Agano Jipya linawasilisha vyote yaani ulinzi wa mwaamini na dai la imani endelevu na uovu. Ukristo ni mwitikio wa mwanzo wa toba na imani inayofatiwa na mwitikio endelevu wa toba na imani. Wokovu si kama matokeo (tiketia ya kwenda mbinguni au sera ya bima ya moto), bali uhusiano. Ni maamuzi na uwanafunzi. Inaelezwa katika Agano Jipya 3:5

- utimilifu (tendo lililokamilishwa na matokeo endelevu), Efe. 2:5,8
- inawasilisha (tendo endelevu), 1 Kor. 1:18; 15:2; 2 Kor. 2:15
- wakati ujao (matukio yajayo au matukio fulani), Rum. 5:8,10; 10:9; 1 Kor. 3:15; Flp. 1:28; 1 The. 5:8-9; Ebr. 1:14; 9:28

katika vitenzi vyote ni vya nyakati:

- kauli (tendo timilifu), Matendo 15:11; Rum. 8:24; 2 Tim. 1:9; Tito

◙ **"mkijua ya kuwa mateso yale yale yanatimizwa kwa ndugu zenu walioko duniani."** Matumizi ya Petro ya uzoefu wa kawaida wa waamini yalitapakaa katika himaya nzima ya Kirumi kama sehemu ya kuwatia moyo hawa waamini wenye mateso. Uzoefu wao haukuwa wa kawaida, bali wa kedesturi.

**5:10 "mkiisha kuteswa kwa muda kidogo"** Hiki kinayalejelea maisha haya (kama vile 1 Pet. 1:6).

◙ **"Mungu wa neema yote"** Tumaini la waamini linahimarishwa, tabia yake ya kupenda, neema, huruma ya Mungu isiyobadilika. Ijapokuwa tunaishi katika ulimwengu wa uovu na uasi, tunapomwamini hakuna awezaye kututenganisha naye (kama vile Rum. 8:31-39).Toleo la NIDOTTE, juzuu ya 2, kr. 78-79, lina orodha yenye kushangaza ambayao ina kishazi kimilikishi kinachotumika kumwelezea Mungu.

1. Mungu wa amani – Rum. 15:33; 16:20; 1 Kor. 14:33; 1 The. 5:23; Flp. 4:9; Ebr. 13:20
2. Mungu wa huruma – Luka 1:78
3. Mungu wa faraja – Rum. 12:1; 2 Kor. 1:3
4. Mungu wa neema yote – 1 Pet. 5:10,12
5. Mungu wa upendo – 2 Kor. 13:11
6. Hakuna Mungu wa machafuko – 1 Kor. 14:33

◙ **"aliyewaita kuingia katika utukufu wake wa milele katika Kristo"** Huu ni msistizo mwingine wa utambulisho wetu pamoja na Kristo. Sasa tunatambulishwa pamoja naye katika kifo chake(kama vile Rum. 6:4) na mateso (kama vile Rum. 8:17), lakini pia kwa ufufuko na utukufu wake (kama vile 2 Kor. 4:17; 2 Tim. 2:10). Huu utukufu wa milele unakuja tu kwa uzoefu wa kifo cha mwili au Kuja mara ya Pili!

**5:11 "yeye mwenyewe atawatengeneza, na kuwathibitisha, na kuwatia nguvu"** shabaha ya Mungu kwa waamini wote ni kumfanana Kristo kupitia mateso na mapambano (kama vile 1 Pet. 4:13; Rum. 8:17; 2 Kor. 1:5,7; Flp. 3:19; 2 Tim. 2:12; Eb.r 2:10; 5:8). Bado ni yeye atoaye mahitaji yote. Hapa pia ni dhana ya fumbo la kiagano. Mungu anaifanya sehemu yake nasi yatupasa kuifanya sehemu yetu!

◙ **"Uweza una yeye hata milele na milele"** Kwa mara nyingine kipengele hiki kinatoa melezo ya s 4:11, isipokuwa hapa hakuna kitenzi. Hivyo mawazo mengi ya 1 Petro (kama 1 Yohana) ni kama mikondoya utaratibu wa urembo au rahani katika muziki wenye kurudiwarudiwa kwa namna tofautitofauti. Mungu anayatawala mambo yote (kama vile Rum. 11:36).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 PETRO 5:12-14a**

**12 Kwa mkono wa Silwano, ndugu mwaminifu kama nionavyo, nimewaandikia kwa maneno machache, kuonya na kushuhudia ya kuwa hii ndiyo neema ya kweli ya Mungu. Simameni imara katika hiyo.**
**13 Mwenzenu mteule hapa Babeli awasalimu, na Marko mwanangu. 14 Salimianeni kwa busu la upendo**

**5:12 " Kwa mkono wa Silwano"** Huyu ni Sila wa Matendo 15:40. Mttu huyu ndiye msingi wa Petero, aliyepatana na Yohana Marko, ya thiolojia na maandiko ya Paulo. Maandiko ya Petero yanafanana sana nay ale ya Paulo katika namna nyingi. Kumekuwa na madhaanio mengi kuhusiana na uhusiano na uandishi wa 1 Petro. Nafikiri hakuna shaka kuhusiana na Petro kutumika kama mwandishi, bali alikuwa Silwano? Kibainishi chenye kuvutia katika Makala ya *Journal of the Evangelical Theological Society* , Juzuu. 43 No. 3, kr. 417-432, inayoitwa "Silvanus Was Not Peter's Secretary" na E. Randolph Richards, kimeniridhisha kwamba kifungu hiki huenda kinamrejelea Siliwano mwenye mtazamo wa barua hii kwa wasomaji wake, si muhimu kulishikilia kwa ajili ya Petro.

## MADA MAALUM : SILA/SILVANO

Sila, au Silvanus, ni mtu ambaye Paulo alimchagua kwenda nae katika safari yake ya pili ya umisiaonari (yaani., Mdo. 15:40-18:5) baada ya Barnaba na Yohana kurudi Kipro (yaani., baada ya kubishana na Marko, kama vile Mdo. 15:36-39).

A. ni wa kwanza kutajwa katika Biblia kwenye Mdo.15:22 ambapo anaitwa kiongozi kati ya wapendwa walioko katika kanisa la huko Yerusalem.
B. Pia yeye alikuwa nabii (kama vile Mdo. 15:32).
C. Alikuwa raia wa Kirumi kama alivyokuwa Paulo (kama vile Mdo. 16:37).
D. Yeye na Yuda Barsaba walipelekwa Antiokia na kanisa la Yerusalem kwa ajili ya kuchunguza eneo (kama vile Mdo. 15:22,30-35).
E. Paulo anamtaja yeye katika 2 Kor. 1:19 kama mfuasi wa kuihubiri injili.
F. Baadaye anatambuliwa na Petro katika maandiko 1 Petro. (kama vile 1 Pet. 5:12; huenda ndo maana Petro anasikika sana kama Paulo).

Wote Paulo na Petro wanamwita Silvanus, wakati Luka anamwita Sila (muundo wa Sauli wa lugha ya Kiaramu). Yawezekana Sila lilikuwa jina lake la Kiyahudi na Silvanus lilikuwa la Kilatini (kama vile F. F. Bruce, Paul: Apostle of the Heart Set Free, uk. 213).

◙ **"ndiyo neema ya kweli ya Mungu"** Katika kipindi cha uandishi wa Petro, mawazo mengine ya Yesu yameboreshwa. Petro anadai kuwa ipo lakini ni neema moja tu—injil. Petro inasistiza juu ya neema ya Mungu mara nyingi katika 1 Petro (kama vile 1 Pet. 1:10,13; 2:3; 3:7; 4:10; 5:5,10,12). Injili ya Yesu Kristo kwa ukweli inaaksi moyo wa YHWH. Hii inaitwa "ya kweli" hapa ni kwa sababu imekuwa ikihimarishwa katika maisha ya waamini hawa wateswao!

◙ **"Simameni imara katika hiyo"** Hii ni kauli tendaji shurutishi isiyo timilifu. Hii ni muhimu katika siku za mateso. Kifungu "Simameni" kinahusiana na kifungu "kirini katika imani yenu" katika 1 Pet. 5:9.Huu ni mtazamo unaomuhusu Mungu, kumhusu Kristo na kuwa mbali na dhambi, mtu mwenyewena Shetani.Hili ni neno la kijeshi katika Efe. 6:11,13,14. Paulo analitumia katika namna kadhaa na mbalimbli.

1. muhtasari wa injili katika 1 Kor. 15:1
2. maelezo ya " tumepata kwa njia ya imani" katika Rum. 5:2
3. maonyo kwa Mataifa kuitunza imani katika Rum. 11:20
4. onyo kuhusu kiburi cha kiroho katika 1 Kor. 10:12

Waamini wanalo jukumu la kiagano la kusimama imara! Tazama Mada Maalum: Ustahimilivu katika 1 Pet. 5:9.

**5:13 " mteule"** Mara nyingi makaisa yalivulishwa uhusika kama mwanamke (kama vile 2 Yohana) huenda ni kwa sababu ya dhana ya Agano la Kale kumhusu YHWH kama mwaname na kama mke wa Israeli (kama vile Hos. 1-3). Kanisa ni bibi-arusi wa Kristo (kama vile Efe. 5:21-31).

◙ **"Babeli"** Huenda hii ni rejea ya fumbo la Rume (kama vile Ufu. 14:8; 17:5; 18:2,10; Sibylline Oracles 5:143,152; Baruch 9:1). Rumi, katika siku za Petro, ilikuwa kieleezo cha nguvu ya ulimwengu wa Agano la Kale (yaani., Ashuru, Babeli, Uajemi). Huu ulikuwa ubainishaji wa mfumo wa nguvu ya ulimwengu, majivuno, na ibada ya sanamu kinyume na Mungu (kama vile E ph. 2:2a). Petro aliandika akiwa katika pango la wanyama. Kanisa la Mungu lilisimikwa katika eneo la maadui.

◙**"Marko"** Jina hili linamrejelea Yohana Marko. Kanisa la mwanzo lilikutana nyummbani mwake kumo Yerusalemu (kama vile Matendo 12:12). Pia ndilo eneo alilionekana Bwana baada ya siku tatu za ufufuo na kuja kwa yule Roho. Yohana Marko aliambatana na Paulo na mjomba wake a Barnaba (kama vile Kol. 4:10) katika safari ya kwanza ya kimisheni (kama vile Matendo12:25-13:13).Kutokana na sababu fulani aliachana na kundi na kurudi nyumbani (kama vile Matendo 15:38). Barnaba alitaka kumweka katika safari ya pili ya umisheni, lakini Pauo alikataa (kama vile Matendo 15:36-41). Hili lilileteleza utengano kati ya Paulo na Barnaba. Barnaba alimchukua Yohana Marko huko Kipro (kama vile Matendo15:39). Baadaye, Paulo akiwa gerezani, alimtaja Yohana Marko katika namna iliyo njema (kama vile Kol. 4:10) na bado katika kufungwa kwa Paulo kwa mara pili huko Rumi, kabla ya kifo chake, anamtaja Yohana Marko kwa mara nyingine (kama vile 2 Tim. 4:11).

Kwa uwazi Yohaan Marko alikuwa sehemu ya kuduma ya kundi la Petro (kama vile 1 Pet. 5:13). Eusebius' Eccl. His. 3:39:12 inatupa maelezo yenye kusisimua kuhusu uhusianao wa Yohana na Petro.

"Katika kitabu chake Papias auatupa maelezo ya semi za Bwana zinazopatikana katika Aristion au zilizofundishwa moja kwa moja kutoka kwa mzee wa kanisa Yohana. Kwa kuyaingiza haya katika fikra za wasomi, yanipasa kufuatilia kauli ambazo zimekwisha kunukuliwa kutoka kwake nikitumia baadhi ya uthibitisho aliouanza kwa kumfuatisha Marko, mwandishi wa injili: Hii, pia, mzee huyu wa kanisa. 'Marko, alikuwa mkalimani wa Petro, aliandika kwa umakini, lakini si kwa mpangilio, yale yote aliyoyakumbuka yalikuwa matamko na matendo ya Mungu. Yeye hakumsikia Bwana au wala kuwa mmoja wa wafuasi wake, bali baadaye, kama nilivyokwisha kusema, alikuwa mmoja wa wale wafuasi wa Petro. Petro aliyazoelea mafaundisho yake katika kila tukio lililotukia, pasipo kufanya mpangilio maalum wa wa matamko ya Bwana, ili kwamba Marko aweze kuthibitishwa katika kuandika baadhi ya mambo kwa namna alivyokuwa akiyakumbuka. Kwke alikuwa na kusudi moja pekee—kutokuacha kitu chochote ambacho alikisikia, na kutoandika usemi touti na jambo hilo'" (uk.152).

Katika nukuu hii ya Papias jambo hili linamrejelea "Yohana mzee wa kanisa," katika namna tofauti na Heresies 5:33:4, Irenaeus inayosema "na mambo haya ni ushahidi unaokubalika katika katika maandishi ya Papias, msikilizaji wa Yohana, na wenza wa Polycarp."Hili linamaanisha kuwa Papias alilisikia hili toka kwa Yohana Mtume. Yohana Marko aliziandika kumbukumbu na hotuba za Petro kumhusu Yesu katika injili.

**5:14 "busu la upendo"** Huu ni uanishaji wa utamaduni wa salamu miongoni mwa wanafamilia. Kwa mara ya kwanza ilikubaliwa na wana wa nyumba ya Mungu (kama vile Rum. 16:16; 1 Kor. 16:20; 2 Kor. 13:12; 1 The. 5:6). Katika karne ya nne b.k. busu hili liliruhusiwa kwa watu wa jinsia moja kwa sababu ya matumizi mabaya ndani ya kanisa na mtazamo kutokuielewa vema kutoka nje ya kanisa. Huu utaratibu wa tendo la ushirika ilikuwa sehemu ya kawaida ya Karamu ya Bwana au Siku Kuu ya Upendo.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1 PETRO 5:14b**
**14b Amani na iwe kwenu nyote, mlio katika Kristo. Amina.**

**5:14b** Ni wale tu walio katika Kristo wawezao kuwa na amani (kama vile Luka 2:14). Wale walio na amani ya Kristo mara nyingi huwa na amani ya ulimwengu (kama vile Mt. 10:34; Luka 12:49-53; Yohana 14:27).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe zaBiblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Orodhesha na elezea maneno ya Agano Jipya yaliyotumika kwa ajili ya kiongozi wa makanisa ya nyumbani ya maeneo.
2. Orodhesha maonyo manne kwa wachungaji katika1 Pet. 5:2-3.
3. Orodhesha maelezo yamawasiliano binafsi ya Petro pamoja na Yesu ambayo yanatajwa katika sura hii.
4. Ni kwa namna gani mateso yanahusianishwa na ukomavu wa Mkristo? Kwa shetani?

# UTANGULIZI WA 2 PETRO

## MAELEZO YA UFUNGUZI

A. Kusudi au upeo wa utangulizi huu sio kujadili kwa undani matatizo yanayohusiana na uandishi wa 2 Petro. Mimi mwenyewe nimekamilisha kuwa hakuna sababu ya kulazimisha kukataa uandishi wa Petro. Vyanzo vitatu vilikuwa vya kusaidia katika kufikiri kupitia suala hili.
   1. Makala ya Bruce M. Metzger "Upasuaji wa Vitabu na Pseudepigrapha ya Kikristo" katika *Jarida la Jamii ya Fasihi ya Kibiblia*, 1972, pp. 3-24.
   2. Makala ya Michael J. Kruger ya "Ukweli wa 2 Petro" katika *Jarida ya Kiinjilisti ya Jamii ya kithiolojia*, Vol. 42, No. 4, uk. 645-671.
   3. E. M. B. Green's book *2 Peter Reconsidered*, Tyndale Press, 1961.

B. Kama nadhani kuhusu uwezekano wa kuwa 2 Petro haukuandikwa na Petro, mambo mengi yanatumia mawazo yangu.
   1. Yule aliyeandika 2 Petro hakubadili mtazamo wangu kwamba umefunuliwa na kuaminika. Uandishi huathiri ufafanuzi wa fasiri, sio msukumo, ambao ni imani ya kuaminika na mchakato wa kihistoria wa kumbukumbu.
   2. Kwa nini ninasumbuliwa na udanganyifu? Inavyoonekana karne ya kwanza ya ulimwengu wa Wagirki na Warumi ilikuwa umezoea (makala ya Metzger).
   3. Je, sikubali kuruhusu kwa sababu ya mapendekezo yangu mwenyewe au ninaweza kutathmini uaminifu wa kihistoria na waandishi? Je, mila imepata hitimisho fulani?
   4. Kanisa la kale liliuliza uandishi wa Petro, lakini siyo ujumbe wa kitabu (isipokuwa kanisa la Shamu). Ni ujumbe wa kidini katika umoja wa kitheolojia na vitabu vingine vya Agano Jipya na ushirika mwingi kwa mahubiri ya Petro katika Matendo.

C. Eusebius alitumia makundi matatu kuelezea maandiko ya Kikristo:
   1. alikubaliwa
   2. kupingana
   3. hasira

Alihitimisha 2 Petro pamoja na Yakobo, Yuda, 2 Yohana, na 3 Yohana katika jamii ya 2 (yaani, kupingana). Eusebius alikubali 1 Petro; alikuwa na wasiwasi juu ya 2 Petro, na kukataliwa kama maandishi mengine yaliyotakiwa ya Petro (1) Matendo ya Petro; (2) Injili ya Petro; (3) Kuhubiri kwa Petro; na (4) usemi wa Petro kuhusu matukio ya siku za mwisho.

## UANDISHI

A. Hiki ndicho kitabu cha Agano Jipya cha mgogoro zaidi kuhusu uandishi wa jadi.

B. Sababu za mashaka haya ni ya ndani (mtindo wake na maudhui yake) na ya nje (kukubalika kwa muda mrefu).

## WAHUSIKA WA NDANI

1. Mtindo
   a. Mtindo ni tofauti sana kutoka 1 Petro. Hii ilitambuliwa na Origen na Jerome.
      (1) Origen alikiri kuwa baadhi ya uandishi wa Petro aliukataa, lakini alinukuu kutoka 2 Petro mara sita katika maandiko yake.
      (2) Jerome alihusisha hii kwa matumizi ya Petro ya mwandishi tofauti. Pia anakiri kwamba baadhi ya siku zake walikataa uandishi wa Petro.

(3) Eusebius anazungumzia jambo hili katika *Mhu. His*. 3: 3: 1: "lakini kinachoitwa pili Waraka hatukupokea kama kanisa, lakini hata hivyo imeonekana kuwa ya manufaa kwa wengi, na imesoma na Maandiko mengine. "

b. Mtindo wa 2 Petro ni tofauti sana. Katika *Barua ya Yakobo*, *Petro na Yuda* katika Biblia salama, pp. 146-147, B. Reicke anaiita "Uasia."

"Uliitwa " mtindo wa Ki-Asia kwa sababu wawakilishi wake wa kwanza walikuja kutoka Asia ndogo, na ulikuwa na sifa ya kubeba, maneno mengi ya sauti ya juu kujieleza kuelekea kwenye riwaya ya ajabu, na bila kujali kuhusu kukiuka maadili ya kawaida ya unyenyekevu. Hatimaye barua yetu ilikuwa imeandikwa kulingana na sheria za shule ya Asia ambayo ilikuwa bado muhimu wakati wa karne ya kwanza ya Kikristo. "

c. Inawezekana kwamba Petro alijaribu kuandika kwa lugha (yaani, Koine huko Uyunani) ambayo haikuwa na kazi kamili. Lugha yake mama ilikuwa Kiaramu.

2. Aina
   a. Je! Hii ni mfano wa barua ya karne ya kwanza?
      (1) ina ufunguzi wa kawaida na wa karibu
      (2) hata hivyo, inaonekana kuwa barua ya makanisa kwa makanisa kadhaa, kama Wagalatia,Waefeso, Yakobo, na 1 Yohana
   b. Inaweza kuwa aina ya Kiyahudi maalumu inayoitwa "agano," ambayo inajulikana na
      (1) hotuba ya kuacha
         a) Kumbukumbu la Torati 31-33
         b) Yoshua 24
         c) Agano la Wazee kumi na wawili
         d) Yohana 13-17
         e) Matendo 20:17-28
      (2) utabiri wa kifo cha karibu (tazama 2 Timotheo)
      (3) ushauri wa wasikilizaji wake kuendelea na mila yake
3. Uhusiano kati ya 2 Petro 2 na Yuda
   a. Kuna uwazi kuwa kuna kukopa kwa fasihi.
   b. Kusema kwa vyanzo visivyo vya kisheria kumesababisha wengi kukataa Yuda na 2 Petro, hata hivyo 1 Petro anasema kwa mimi Enoki na Paulo hata akitoa mashairi ya washairi wa Kiyunani.
4. Kitabu chenyewe kinasema kuwa ni kutoka kwa Petro yule Mtume
   a. Jina lake katika 2 Pet. 1:1. Anaitwa Simoni Petro. Petro ni jina alilopewa na Yesu (tazama Mathayo 16). Simoni (si Simoni) ni wa kawaida na isiyo ya kawaida. Ikiwa mtu alikuwa akijaribu kuandika kwa jina la Petro uchaguzi wa herufi hii ya Kiislamu ni ya kushangaza sana na haizuii kwa udanganyifu.
   b. Anasema kuwa ni ushuhuda wa jicho juu ya kubadilika kwa sura (tazama Mathayo 17: 1-8; Marko 9: 2-8; Luka 9: 28-36) katika 2 Pet. 1: 16-18..
   c. Anadai kuwa ameandika barua ya kwanza (tazama 2 Pet 3: 1), ambayo ina maana 1 Petro.

5. Imani halisi
   a. Hakuna kitu katika barua hii ambacho kinapinga mafundisho ya Kitume.
   b. Kuna vitu vichache vya kipekee (yaani, dunia iliyoharibiwa na moto na maandiko ya Paulo yameonekana kama Maandiko), lakini hakuna mwenye ujuzi au kibinadamu au dhahiri kimwili.

## WAHUSIKA WA NJE

1. Eusebius anataja maandiko ya Kikristo ya karne ya kwanza na ya pili katika makundi matatu
   a. kukubalika
   b. kupingana
   c. hasira

   2 Petro, pamoja na Waebrania, Yakobo, 2 na 3 Yohana wameorodheshwa katika kikundi kinachokabiliana.
2. 2 Petro hajitokei kwenye gazeti la Marcion (154 B.K), lakini Marcion pia alikataa vitabu vingi vya Agano Jipya.

3. Petro haijatokea katika vitabu vya agano jipya (180-200 B.K), lakini orodha hiyo inaonekana imeharibiwa na pia haijasingizia Waebrania, Yakobo, au 1 Petro.
4. Ilikataliwa na Kanisa la Mashariki (Shamu)
   a. si katika Peshitta (nusu ya kwanza ya karne ya tano)
   b. lilijumuishwa katika waraka mdogo wa Philoxeniana (507 B.K) kutoka Iraq na toleo la Harclean (616 B.K) kutoka kaskazini mwa Afrika
   c. Chrysostom na Theodore wa Mopsuestia (yaani, viongozi wa shule ya Antiokia ya tafsiri) walikataa barua zote za Katoliki.
5. 2 Petro anaonekana kuwa alinukuliwa katika "Injili ya Kweli" na "mandiko yasiyokubalika ya Yohana" yaliyopatikana katika maandiko ya Nag Hammadi aliyesadikiwa kuwa na ujuzi wa pekee (tazama Maandiko ya *Nag Hammati Gnostic na Biblia* na Andrew K. Helmbold, uk. 91) . Maandishi haya ya watu wa asili ya Misri ni tafsiri za maandishi ya awali ya Kiyunani. Ikiwa 2 Petro inaelezewa kuwa haiwezekani kuwa imeandikwa katika karne ya pili.
6. Ni pamoja na $P^{72}$, iliyoandikwa na $UBS^4$ (uk. 8) kama karne ya tatu au ya nne.6.
7. Inaelezea au kunukuliwa na Clement wa Roma (aya 95)
   a. Mimi Clement (9: 2 - 2 Petro 1:17)
   b. Mimi Clement (23: 3 - 2 Petro 3: 4)
   c. Mimi Clement (35: 5 - 2 Petro 2: 2)
8. Inaweza kutajwa katika Justin Martyr (Mnamo miaka ya 115-165 B.K) *Majadiliano na Trypho* 82: 1 - 2 Pet. 2: 1. Hizi ni sehemu mbili tu katika maandiko ya kale ya Kikristo ambako neno la Kigiriki *pseudoppophetai* hutumiwa.
9. Irenaeus (manamo mwaka 130-200 B.K) labda linaelezea 2 Petro (yeye alinukuliwa na Eusebius *'His Mhubiri* 5: 32: 2 - 2 Pet 3: 8 na 3: 1: 1 - 2 Pet 1:15 ).
10. Clement wa Alexandria (150-215 B.K) aliandika ufafanuzi wa kwanza (ingawa sasa umepotea) juu ya 2 Petro.
11. Inaonekana katika barua ya Pasaka (367 B.K), ambayo ilikuwa orodha ya sasa ya vitabu vya kanisa.
12. Ilikubaliwa kama kanisa la makanisa ya awali la Laodikia (uk. 372) na Carthage (uk. 397).
13. Ni jambo la kushangaza kwamba maandiko mengine yaliyotakiwa ya Petro (yaani, Matendo ya Petro, Matendo ya Andrea na Petro, Matendo ya Petro na Paulo, Pasaka ya Petro na Paulo, Matendo ya Petro na Mitume kumi na wawili, Usemi wa Petro kuhusu matukio ya siku za mwisho, na Kuhubiri kwa Petro) wote walikataliwa na makanisa ya mapema kama ya uongo (yaani, yasiyo ya kuongozwa).

C. Richard N. Longenecker, *Ushauri wa Kibiblia katika Kipindi cha Mitume* (ukurasa wa p 174) hufanya maoni kwamba 2 Petro anaweza kuwa ameandika mwenyewe bila kutumia mwandishi (yaani, Sila katika 1 Petro 5:12 na Yohana Marko kwa Injili). Kwa ushahidi anasema kuwa 1 Petro anatumia Fasiri ya Kiyunani ya Agano la Kale peke yake katika vyuo vya Agano la Kale, lakini 2 Petro (tazama 2 Petro 2:22) anatumia MT ya Pro. 26:11, ambayo inaashiria asili ya Kiebrania.

## TAREHE

A. Hii inategemea uandishi.
B. Ikiwa mtu anaamini uandishi wa Petro basi wakati mwingine kabla ya kifo chake (kama vile 2 Pet 1:14).
C. Hadithi za kanisa zinasema kwamba Mtume Petro alikufa Roma wakati Nero alikuwa Kaisari. Nero alianzisha mateso kwa Wakristo mnamo mwaka 64 B.K. Alijiua mnamo mwaka 68 B.K.
D. Kama mfuasi wa Petro aliandika kwa jina lake, basi tarehe imechelewa kama 130-150 B.K inawezekana kwa sababu 2 Petro ametajwa katika *Apocalypse ya Petro* pamoja na *Injili ya Kweli* na *Apocryphon ya Yohana*.
E. Mchezaji wa kale wa Marekani, W. F. Albright, anasema kwamba imeandikwa kabla ya 80 B.K kwa sababu ya kufanana kwake na Maandiko ya Bahari ya Mauti.

## WAPOKEAJI

A. Ikiwa 1 Petro anatumiwa katika 2 Petro 3:1 basi wapokeaji watakuwa sawa (yaani kaskazini mwa Uturuki).
B. 2 Petro anaweza kuwa ushuhuda wa kuwatia moyo waumini wote kushikamanika wakati wa majaribio, kupinga walimu wa uongo, na kuishi kwa uaminifu katika utamaduni wa injili kwa kutarajia kuja kwa pili.

## WAKATI

A. Kama 1 Petro anataja mateso na masumbufu, 2 Petro huwaambia walimu wa uongo.

B. Asili halisi ya mafundisho ya uwongo haijulikani, lakini inaweza kuwa na uhusiano na wenye kupinga sheria na kuataka mambo yaende kwa neema (tazama. 2 Pet 2: 1-22, 3: 15-18). Kitabu hiki hutumia msamiati wa kiufundi ambao unatumiwa na wale wenye ujuzi walioko hatua ya mwanzo na dini za siri. Hii inaweza kuwa mbinu ya kuomba msamaha ya kushambulia theolojia yao.

C. Kitabu hiki, kama 2 Wathesalonike, kinasema jambo la kuchelewa, lakini la pili, Kuja kwa Pili,ambapo watoto wa Mungu watatukuzwa na wasioamini watahukumiwa (tazama 2 Pet 3: 3-4). Inavutia kwamba1 Petro hutumia neno hili *apocalupsis* kutaja kurudi kwa Yesu, wakati 2 Petro anatumia *parousia*. Hii inaweza kuonyesha matumizi ya waandishi tofauti (yaani, Jerome).

## MZUNGUKO WA KWANZA WA USOMAJI **(Kutoka "Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Dhamira ya kitabu kizima
2. Aina ya fasihi iliyotumika (uwasilishaji)

## MZUNGUKO WA PILI WA USOMAJI **(Kutoka "Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")**

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Mada ya sehemu ya kwanza ya fasihi
2. Mada ya sehemu ya pili ya fasihi
3. Mada ya sehemu ya tatu ya fasihi
4. Mada ya sehemu ya nne ya fasihi
5. N.k.

# 2 PETRO 1

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Salamu<br>1:1-2 | kusalimu Waaminifu<br>1:1-4 | salamu<br>1:1-2 | utangulizi<br>1:1<br>1:2 | salamu<br>1:1-2 |
| Wito wa Mkristo<br>Na uchaguzi<br>1:3-11 | | maonyo ya utakatifu<br>1:3-11 | Wito wa Mungu na<br>Uchaguzi<br>1:3-9 | Wema wa Mungu<br>1:3-11 |
| | Kukua kwa kuzaa<br>Matunda katika<br>Imani<br>1:5-11 | | | |
| | Mkabiliano wa Petro<br>Na kifo | | | Ushuda wa Kitume |
| 1:12-15 | 1:12-15 | 1:12-15 | 1:12-15 | 1:12-15 |
| Utukufu wa Kristo<br>Na Neno la Kinabii<br>1:16-21 | Kutumainika<br>Neno la Kinabii<br>1:16-21 | 1:16-18 | Ushuhuda wa Utukufu<br>wa Kristo<br>1:16-18 | 1:16-18 |
| | | | | Thamani ya Unabii |
| | | 1:19-21 | 1:19-21 | 1:19-21 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka "Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu shartiatembe katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu.
Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishiwa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

* Ingawa hazijavuviwa, migawanyo ya aya ndiyo ufunguo wa kuelewa na kufuatilia kusudio la asili la mwandishi. Kila tafsiri ya kisasa imegawanya na kufanya muhtasari wa aya. Kila aya ina mada kuu, kweli au wazo. Kila toleo limebeba hiyo mada kwa namna yake ya pekee. Unaposoma maandiko ya mwandishi jiulize ni tafsiri ipi inawiana na uelewa wako wa somo na mgawanyo wa mistari.
Katika kila sura lazima tusome Biblia kwanza na kujaribu kutambua somo (aya), kisha tulinganishe na matoleo ya kisasa. Ni pale tunapoelewa kusudi la asili la mwandishi kwa kufuata mantiki yake na jinsi alivyojieleza tunaielewa kwa Biblia kiukweli. Ni mwandishi wa asili tu aliyevuviwa —wasomaji hawana haki ya kurekebisha ujumbe. Wasomaji wa biblia wana wajibu wa kutumia ukweli uliovuviwa kwenye siku na maisha yao.
Fahamu kwamba maneno yote ya kiufundi na vifupisho vimefafanuliwa kwa kirefu kwenye nyaraka zifuatazo: Maelezo Fasaha Ya Muundo Wa Sarufi Za Kiyunani(Brief Definitions of Greek Grammatical Structure),Uhakiki Wa Tofauti Za Kiandishi(Textual Criticism),Ufafanuzi na Maelezo ya Kimaandiko(Glossary).

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA KWA MISTARI YA 1-11

A. Mistari ya 1-11 ni sentensi moja ya Kiyunani ikiunganisha vipengele vyote vya agano:neema huru itawalayo na maisha ya mamlaka ya ufanano na Kristo.
B. Ainisho linaonekna kuwa

1. Utangulizi wa asili (2 Pet. 1:1-2)
    a. kutoka kwa nani
    b. kuelekea kwa nani
    c. salamu
2. mistari 3-4 — sehemu ya Mungu
3. mistari 5-7 — sehemu ya waaminio
4. mistari 8-9 — vipengele chanya na hasi vya uaminifu
5. mistari 10-11 — uhakika kupitia mtindo wa maisha ya utauwa

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 PETRO 1:1-11**
**1 Simoni Petro, mtumwa na mtume wa Yesu Kristo, kwa wale waliopata imani moja na sisi, yenye thamani, katika hali ya Mungu wetu, na Mwokozi Yesu Kristo. 2 Neema na iwe kwenu na amani iongezwe katika kumjua Mungu na Yesu Bwana wetu. 3 Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe. 4 Tena kwa hayo ametukirimia ahadi kubwa mno, za thamani, ili kwamba kwa hizo mpate kuwa washirika wa tabia ya Uungu, mkiokolewa na uharibifu uliomo duniani kwa sababu ya tamaa. 5 Naam, na kwa sababu iyo hiyo mkijitahidi sana kwa upande wenu, katika imani yenu tieni na wema, na katika wema wenu maarifa, 6 na katika maarifa yenu kiasi, na katika kiasi chenu saburi, na katika saburi yenu utauwa, 7 na katika utauwa wenu upendano wa ndugu, na katika upendano wa ndugu, upendo. 8 Maana mambo hayo yakiwa kwenu na kujaa tele, yawafanya ninyi kuwa si wavivu wala si watu wasio na matunda, kwa kumjua Bwana wetu Yesu Kristo. 9 Maana yeye asiyekuwa na hayo ni kipofu, hawezi kuona vitu vilivyo mbali, amesahau kule kutakaswa dhambi zake za zamani. 10 Kwa hiyo ndugu, jitahidini zaidi kufanya imara kuitwa kwenu na uteule wenu; maana mkitenda hayo hamtajikwaa kamwe. 11 Maana hivi mtaruzukiwa kwa ukarimu kuingia katika ufalme wa milele wa Bwana wetu, Mwokozi wetu Yesu Kristo.**

**1:1 "Simoni"** Hii kwa maana iliyo wazi ni "Simoni " (angalia Bruce Metzger, *A Textual Commentary On the Greek New Testament*, uk. 699). Hili ni jina la Petro la Kiebrania, na moja ya yale makabila kumi na mawili. Aina ile ile inaonekana katika Mdo. 15:14. Ikiwa waraka huu ulikuwa sio wenyewe, hakika mwandishi angalitumia matamushi ya kawaida "Simoni."

◙ **"Petro"** Hii kwa maana iliyo wazi ni *Petros*, ambalo ni neno la Kiyunani lenye kumaanisha mwamba au jiwe kubwa. Lilikuwa ni jina la utani alilopewa Simoni na Yesu katika Mt. 16:18 na pia Yohana 1:42. Katika kifungu hiki kwenye Yohana neno la Kiaramu *Cephas* linatajwa. Kwenye mazungumzo ya kila siku Yesu aliongea kwa Kiarama, sio Kiebrania, wala Kiyunani. Paulo mara nyingi alitumia *Cephas* (kama vile 1 Kor. 1:12; 3:22; 9:5; 15:5; Gal. 1:18; 2:9,11,14).
Pamekuwepo na mijadala mbali mbali kati ya wanazuoni wa Kikatoliki na Kiprostanti kuhusu umuhimu wa badiliko la jina hili (ambalo lilikuwa la muhimu kwa Abram, Yakobo, n.k. katika Agano la Kale). Katika Mt. 16:18 Petro aliye mwamba anasemekana kuwa ndiye msingi wa kanisa. Waprostanti wamelifanya kuwa hoja ya kithiolojia kuelezea kuwa "Petro" ni jinsi ya kiume (yaani., *Petros*), lakini "mwamba" ni jinsi ya kike (yaani., *Petra*), kwa hiyo ukiri wa imani wa Petro, na sio Petro mwenyewe, ni msingi wa kanisa. Hata hivyo, utofauti huu katika sarufi za Kiyunani usingalikuwepo katika lugha ya Kiarama, ambapo *Cephas* lingalitumika pande zote.
Kama mwana thiolojia sihitaji kuutilia shaka uongozi wa Petro, lakini pia nitambue kuwa Mitume wengine hawakuitambua nafasi yake (kama vile Marko 9:34; Luka 9:46; 22:24-27; Mt. 20:20-24). Ingawa Yesu kimazungumzo hakuliongea Kiyunani, andiko lililovuviwa limeandikwa katika Kiyunani, kwa hiyo, utofauti wa kisarufi unaonekana kuvuviwa.

◙ **"mtumwa"** Hili ni neno la Kiyunani *doulos*, ambalo linarejelea kwa mtumishi au mtumwa. Haya huenda ni mazingira ya Agano la Kale ya kuheshimisha "mtumishi wa Bwana" (yaani., Musa, Yoshua, Daudi, and Isaya) au mtizamo wa Agano Jipya juu ya unyenyekevu wenye kuhusiana na Yesu kama Bwana (kama vile Mt. 10:24-25).

◙ **"mtume"** Dhahili hii ni namna ya fasihi kwa ajili ya mwandishi wa 2 Petro kutetea ubinafsi wake kama shuhuda wa macho, wafuasi, na wanafunzi pendwa wa Yesu.

Neno "mtume" linatokana na kitenzi cha Kiyunani "nawatuma" (*apostellō*). Yesu aliwachagua kumi na wawili wa wanafunzi wake kuambatana naye kwa madhumuni maalum na kuwaita "Mitume" (kama vile Luka 6:13). Neno hili mara nyingi lilitumiwa na Yesu akiwa ametumwa na Baba (kama vile Mt. 10:40; 15:24; Marko 9:37; Luka 9:48; Yohana 4:34; 5:24, 30, 36, 37,38,40,57; 7:29; 8:42; 10:36; 11:42; 17:3,8,18,21, 23,25; 20:21). Katika vyanzo vya Kiyahudi lilitumika kuwa mtu aliyetumwa kama mwakilishi rasmi wa mwingine, lenye kufanana na "balozi" (kama vile 2 Kor. 5:20). Petro anatetea mamlaka yake aliyopewa na Yesu!

Lilikuja kuwa na matumizi mapana zaidi ya lile "kumi na wawili" (kama vile Mdo. 14:4, 14, Barnaba; Rum. 16:7, Andronia and Yunia; 1 Kor. 4:6, 9; 12:28-29; 15:7, Apolo; Fil. 2:25, Epafrodito; 1 The. 2:6,Silvano na Timotheo). Kazi zao haswa hazijulikani, lakini linajumuisha kuitangaza injili na uongozi wa kitumishi wa kanisa. Yawezekana kuwa Rum. 16:7 (KJV "Junia") linarejelea mitume wa kike!

◙ **"Yesu Kristo"** Angalia maelezo katika 1 Peter 1:1.

**NASB, NRSV**
**NJB** **"kwa wale walioipata imani"**
**NKJV** **"kwa wale walioipata kama imani ya thamani"**
**TEV** **"kwa wale. . .walikwishapewa imani"**

Hii ni kauli tendaji yenye hali ya kuendelea ya wakati uliopita usiotimilifu toka neno (*lagchanō*), ambayo inarejelea kuenea kwa makundi

1. Kama kwenye kamari (kama vile Yohana 19:24)
2. Kwa maana ya shughuli au uwajibikaji (kama vile Luka 1:9)
3. Kwa namna ya kuonyesha uchaguzi wa Kiungu (kama vile Mdo. 1:17)

Kwa kawaida laweza kumaanisha "kupata" au "kupokea," lakini laweza kuwa na dokezo la nyongeza katika utumiaji wa tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania "kwa mapenzi yake Mungu." Somo lile lile lipo katika 2 Pet. 1:3 na 4 "limeridhiwa" (mara mbili) na "kuitwa" ; pia angalia 2 Pet.1:10 "wito wako na kuchaguli kwako."

Utata huu kwa karibu unafanana kama fumbo la wokovu. Wokovu ni uchaguzi wa Mungu au ni uchaguzi wa Yule aliyeupokea? Kwa uhakika jawabu ni ndiyo! Biblia iko wazi kuwa huu ni ulimwengu wake Mungu. Anahusika kwa namna zote. Amechagua kushughulika na utambuzi wa uumbaji wa agano. Huanzisha mawasiliano. Huweka hoja, lakini hutuhitaji tuitikie (yaani., mwanzoni na kuendelea).

Wasomaji hawa hupokea imani ambayo ilikuwa ni mapenzi ya Mungu kwa ajili yao (na kwa ajili ya wote). Neno "imani" linatoka kwenye neno la Kiyunani *pistis*, ambalo hutafasiriwa katika Kiingereza kama "imani," "kuamini," au"kusadiki." Mwanzoni katika Kiebrania dhana hii ilirejelea kwenye mkao ulio imara, lakini likajakuwa likimaanisha kwa mtu Yule aliyemwaminifu, mtiifu, wa kuaminika, au kutumainika. Katika Biblia sio imani ya mwamini, bali ni uaminifu wa Mungu; na sio imani ya mwamini, bali ni kutumainika kwa Mungu. Angalia Mada Maalum katika Marko 1:15.

**NASB** **"moja na sisi"**
**NKJV** **"kama ya thamani"**
**NRSV, TEV,**
**NJB** **"ya thamani kama"**

Hili ni neno ambani la Kiyunani *isotimos*, neno ambatani la *isos* (yaani., sawasawa, kama, au kuendana na) na *timē* (yaani., bei, thamani, au yenye thamani inayoendana na ughali). Imani itolewayo na Mungu ilikuwa ya thamani kubwa (kama vile 1 Pet. 1:7) na waamini wote wanashiriki katika aina ya imani ile ile. Hakuna imani ya mtu kwa ajili ya Mitume na nyingine kwa ajili ya Wayahudi na watu wa mataifa au kwa ajili ya waamini wengine (kama vile 1 Kor. 12:13; Gal. 3:28; Kol.3:11). Kuna karama tofauti, lakini imani moja (kama vile Efe. 4:5).

◙ **"haki"** Hili linarejelea sio kwa haki yetu tuliyopewa (kama vile Warumi 4), lakini kwa Kristo (kama vile Mdo.3:14; 7:52; 22:14; 1 Yohana 2:1,29; 3:7). Angalia MADA MAALUM: HAKI katika 1 Pet. 3:14. Hili ni eneo lililosafi katika Agano Jipya pale neno *Theos* linatumika kwa Yesu.
Huu mzizi wa Kiyunani (ambao unaaksi mziziz wa Kiebrania, צרק BDB 841) umetumika mara nyingi katika 2 Petro.

1. Haki, mwenye haki (*dikaios*) – 2:8, mtu mwenye haki
2. Haki, kuhesabiwa haki (*dikniosunē*)
   1:1 – haki ya Yesu
   2:5 – haki ya Nuhu (kama vile Mwa. 7:1)
   2:21 – njia ya haki
   3:13 –mbingu mpya na nchi mpya ambayo haki huishi
3. kweli (*dikaion*)
   1:13 – kweli, sawa
   2:7 –Lutu mwenye haki
   2:8 – mtu mwenye haki

Yesu ni mwenye haki, waamini huhesabiwa haki katika Yeye; kwa hiyo, wanapaswa kuishi katika maisha yenye haki, ambayo yanaaksi enzi mpya!

◙ **"Mungu wetu na mwokozi, Yesu Kristo"** Hiki kifungu kinamrejelea Yesu mwanyewe.

1. Kibainishi cha wazi huwa kabla ya nomino iliyotangulia (Granville Sharp's rule)
2. Aina ya visarufi vya maneno yote muhimu, "Mungu," "Mwokozi," "Yesu," na "Kristo" (kimilikishi jinsi ya kiume umoja)
3. Aina ya kujirudia kisarufi (isipokuwa "Bwana" badala ya "Mungu") katika 2 Pet. 1:11; 2:20; na 3:18
4. A. T. Robertson's *Word Pictures in the NewTestament*, Vol. 6, p. 148, anatukumbusha kuwa katika 2 Petro neno *gnōsis* na *epignōsis* mara zote linatumika kumhusu Yesu
5. Kuna sehemu zingine katika Agano Jipya ambapo Uungu wa Yesu unathibitishwa (kama vile Yohana 1:1; 8:57-58; 20:28; Rum.9:5; Fil. 2:6-11; 2 The. 1:12; Tito 2:13; Ebr. 1:8; na 1 Yohana 5:20), ambazo zinashangaza machoni pa wenye imani ya Mungu mmoja.

Katika Agano la Kale neno "Mwokozi" mara zote hutumika kwa YHWH, lakini mara kadhaa kuhusu Masihi. katika Agano Jipya mara nyingi linarejelea kwa Mungu Baba. Katika kitabu cha Tito kifungu kimetumuika mara tatu kwa ajili ya Baba (kama vile Tito 1:3; 2:10; 3:4), hata hivyo katika baadhi ya muktadha pia linatumika kumhusu Yesu (kama vile Tito 1:4; 2:13; 3:6). katika 2 Petro linatumika kiujumla na mara nyingi kwa Yesu (kama vile 2 Pet. 1:1,11; 2:20; 3:2,18).

**1:2 "Neema na amani iwe kwenu"** Hili linafanana na 1 Pet. 1:2. Paulo mara nyingi hutumia "neema na amani," lakini ikifuatiwa na maneno "toka kwa Mungu Baba Yetu" na mara nyingi huongezea "na Bwana wetu Yesu Kristo." Neema huaksi ukweli wokovu wa mwanadamu aliyetenda dhambi na matokeo ya ushirika kutokana na tabia na utoaji wa Mungu. Huu uhusiano mpya (yaani., uliorejeshwa) pamoja na Mungu matokeo yake huishia kwenye amani. Wanadamu waliumbwa kwa ajili ya kuwa na ushirika na Mungu, katika taswira hiyo ndio maana tuliumbwa, na tukiwa na wengine. Neema mara nyingi huleta amani! Kitenzi ni kauli tendwa yenye dhamira ya uchaguzi ya wakati uliopita usiotimilifu. Hili ndilo ombi ambalo Petro humhitaji Mungu atoe vyote neema na amani.

◙ **"katika kumjua Mungu"** Neema na amani hutolewa na Mungu (yaani., sauti irabu tendewa) kupitia maarifa ya kiutendaji ya neno (*epignōsis*) kwa wote Yeye Mwenyewe na Mwana Wake. Maarifa ni somo linalojirudia katika 2 Petro, yumkini ni kwa sababu ya walimu wa uongo (yaani., waliodhaniwa kuwa wenye ujuzi), kama kitabu cha Wakolosai na 1 Yohana.

1. *epignosis* (maarifa kamili); *epignōskō* (kuwa na ufahamu kamili)
   2 Pet 2:21

   2 Pet. 1:2
   2 Pet. 1:3
   2 Pet. 1:8
   2 Pet. 2:20

2. *gnosis* (maarifa) — *ginōskō* (kufahamu)

| | |
|---|---|
| 2. *gnosis* (maarifa) | *ginōskō* (kufahamu) |
| 2 Pet. 1:5 | 2 Pet 1:20 |
| 2 Pet. 1:6 | 2 Pet 3:3 |
| 2 Pet. 2:21 (mara mbili) | *gnōrizō* (kulifanya lifahamike) |
| | 2 Pet. 1:16 |

Walimu wa uongo wa sura ya pili wanaonekana kuwa na tabia ambayo ilikuja kujulikana kama waumini wa nadharia kwamba neema inatosha na haiitajiki kuifuata sheria na nadharia ya wenye ujuzi wa pekee. Mtindo ulioanzishwa wa falsafa/kuwa na maoni tofauti kithiolojia ulianza katika karne ya pili, lakini ulikuwa na mizizi yake katika karne ya kwanza. Uliainishwa kwa dhana ya kutojumuishwa kuliko egamia juu ya maarifa ya siri. Wokovu ulihusianishwa na maarifa haya, na sio maadili. Angalia Mada Maalum katika 1 Pet. 3:22.

◙ **"Mungu na Bwana wetu"** Nilifanya hoja zifuatazo za kisarufi katika 2 Pet. 1:1 zilizohusiana na kifungu chenye kurejelea hasa kwa Yesu.

1. Kibainishi kimoja
2. Miundo yote ya vimilikishi

Hizi sura za visarufi za aina ya kufanana zinapatikana katika kifungu hiki pia ambazo lazima ziongeze baadhi ya viwango vya dhana ya mashaka kuhusu ikiwa 2 Pet. 1:1 inarejelea kwa Yesu pekee au kwa Baba na Mwana. Hata hivyo, tofauti iliyopo hujumuisha kutofautiana kwa machapisho magumu ya Kiyunani. Sarufi za 2 Pet. 1:1 haina utofauti na machapisho ya Kiyunani. Kwa ajili ya tofauti kamili zilizopo angalia tanbihi ya United Bible Society's fourth edition Greek New Testament, uk. 799 and Bart Ehrman, *The Orthodox Corruption of Scripture*, p. 85).

**1:3-7** Hii ni moja ya sentensi ndefu ya Kiyunani.

**1:3 "kwa kuwa"** Toleo la NASB (LILILOBORESHWA) kwa kiasi fulani ni la kinahau. Kiambata cha neno "kwa kuwa" hakiko katika andiko la Kiyunani.

◙ **"Wake"** Hiki kiwakilishi nomino kinarejelea huenda kwa Mungu Baba au Mungu Mwana. Viwakilishi vyote kwenye mistari hizi za ufunguzi kimfanano ni tata. Hii ni tabia ya Petro. Yawezekana kuwa huu ni utata wa kimakusudi (yaani., ingizo mara mbili, kama ilivyo katika maandiko ya Yohana). Yesu anajulikana kama "Mungu" katika 2 Pet. 1:1; wote Baba na Mwana wanahusiana kisarufi katika 2 Pet. 1:2; na kivumishi cha "uungu" katika 2 Pet. 1:3 kinarejelea kwa wote.

◙ **"ametukirimia"** Hii ni kauli ya kati timilifu (shahidi) ya hali ya kuendelea. Huu muundo wa neno la Kiyunani (*dōreomai* toka *didōmi*) umetumika tu katika Marko (kama vile Marko 15:45) na Petro (kama vile 1 Pet. 1:3,4), ambao waweza kuelezea ushirika wa kifasihi wa injili ya Marko na 1 Petro.

◙ **"vitu vyote vipasavyo uzima"** Mstari wa tatu kimsingi ni kanusho la utengano wa kithiolojia wa wokovu wa walimu wa uongo wenye kuwa na ujuzi kupitia maarifa ya siri na maisha ya kiungu ya kila siku. Uungu hutolewa kwa ajili ya maisha ya milele (yaani., *zoe*) na ufanano wa kila siku na Kristo (i.e., *eusebeia*). Maarifa ya kweli ni imani katika Kristo yenye kuleta maisha ya kila siku. Waamini wanachohitaji kiroho ni kuwa katika Kristo! Hatuhitaji kutafuta maarifa ya ukweli wa ndani!

◙ **"na utauwa"** Hili neno ambatani (yaani., *eusebia*) linatokana na neno "vizuri" na "kuabudu." Lina kidokezo cha maisha ya kila siku yanayokubalika na Mungu. Petro alisisitiza kwa kurudia hitaji kwa ajili kuishi maisha ya kiungu kwa sababu ya kutotunza maadili na uadilifu binafsi wa walimu wa uongo (kama vile 2 Pet. 1:3,6,7; 2:9; 3:11). Angalia maelezo kamili katika 2 Pet. 1:6.

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"kwa kumjua yeye"** |
| **NKJV, NRSV,** | |
| **NJB** | **"kwa kumjua"** |
| **TEV** | **"kujua kwetu"** |

Hili ni pigo lingine la msisistizo wa walimu wa uongo juu ya maarifa ya siri (kama vile 2 Pet. 2:20-21). Injili, kama ilivyohubiriwa na Mitume, ni maarifa ya kweli na Yesu ndiye kweli yenyewe (kama vile Yohana 14:6). Huu ni muundo uliopanuliwa, *epignōsis*, ambao una kidokezo cha maarifa ya kiutendaji (kama vile 2 Pet. 1:2,3,8; 2:20). Injili ni nafsi na ni lazima itendewe kazi, na sio kuelezewa kithiolojia.

◙ **"yeye aliyetuita"** Hiki ni kitenzi kinachotumiwa mara kadhaa katika Petro (1 Pet. 1:15; 2:9,21; 3:9; 5:10; 2 Pet.1:3). Mara zote hurejelea wito toka kwa Mungu. Hakuna mtu ajae kwa Mungu asipovutwa na Roho (kama vile Yohana 6:44.65; Efe. 1:4-5).

◙ **"kwa utukufu wake na wema wake"** Kuna utofauti wa machapisho ya Kiyunani katika hoja hii.

1. Machapisho ya P[72], B, K, L, na mengi yenye herufi ndogo yana *dia* (kote) utukufu na wema (kama vile NKJV).
2. Machapisho, א, A, C, P, na hasa tafasiri za kale zina *idia* (Wake) utukufu na wema (kama vile toleo la NASB, NRSV, TEV, NJB).

Swali la kifafanuzi ni, "Waamini wameitwa (1) kwa maana tabia ya uungu (yaani., Baba au Mwana) au (2) kushiriki hizi tabia?" Kamati ya utafasiri ya toleo la UBS[4] hutoa alama "B" (kiwastani kuna mashaka) kwenye uchaguzi namba 1.

**1:4 "Kwa hayo ametukirimia"** Hii ni kauli ya kati timilifu (yenye ushahidi) elekezi inayoendana na ile ya hali ya kuendelea katika 2 Pet. 1:3. Nguvu za uungu wa Mungu zimeisha tolewa na zinaendelea kuwapa waamini yote waliyoyahitaji pale mwanzoni (kuhesabiwa haki) na (utakaso endelevu kwa maana ya ahadi zake.

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"ahadi za thamani na kubwa"** |
| **NKJV** | **"ahadi kubwa mno na za thamani"** |
| **NRSV** | **"ahadi za thamani na kubwa mno"** |
| **TEV** | **"ahadi kubwa mno na zawadi za thamani"** |
| **NJB** | **"ahadi kubwa mno na za thamani"** |

Haya maneno ya kimaelezo lazima yarejelee kwenye injili, ambapo waamini huwa washiriki wenza wa asili ya uungu (yaani., Roho Mtakatifu aishie ndani). Tumaini la mwanadamu aliyeanguka ni tabia thabiti na fadhili zake Mungu, zilizoelezewa kupitia ahadi Zake (yaani., kote kwenye Agano la Kale, lakini hasa katika Kristo, kama vile Ebr. 6:17-18). Utaratibu wa haya maneno mawili unabadilika katika maandiko ya Kiyunani.
Neno "thamani" lilikuwa likitumika katika 1 Pet. 1:19 kwa ajili ya dhabihu ya Kristo ya umwagaji damu. Neno hutengeneza mzizi wa jina "Timotheo."

◙ **"washirika wa tabia za Uungu"** Hili hurejelea kwa (1) Yule Roho Mtakatifu aishie ndani yetu (kama vile 2 Pet. 1:3), ambaye hutokana na wokovu au (2) namna nyingine ya kurejelea kuzaliwa upya (kama vile 1 Pet. 1:3,23). Hili linakuwa la tofauti toka dhana ya kifalsafa ya Kiyunani (ingawa msamiati unatokana na Wastoiki) la mng'ao wa uungu katika wanadamu wote waliotokana na uumbaji. Hili halimaanishi kuwa sisi ni miungu au itatokea tuwe, lakini tunamaanisha kuwa kama Yesu (kama vile Rum. 8:29; Efe. 1:4; Yohana 3:2). Waamini wanapaswa kuziwakilisha tabia za familia ya Mungu (yaani., taswira ya Mungu). Neno "uungu" limetumika kote 2 Pet. 1:3 na 4 ni *theios*, lenye kumaanisha "kiungu" au "mfano wa mungu."

◙ **"mkiokolewa"** Hili neno linajitokeza hapa tu katika 2 Petro kwenye Agano Jipya (kama vile 2 Pet. 1:4; 2:18,20). Hii ni kauli tendaji yenye hali ya kuendelea ya wakati uliopita usiotimilifu, ikidokeza utimilifu wa kitendo (kama vile., wokovu, muda wa kuipokea injili, kama vile 2 Pet. 1:1).

◙ **"uharibifu uliomo duniani na tama za dunia"** Suala katika 2 Petro ni walimu wa uongo waliokuwa wakitetea maarifa ya siri (yaani., dhana ya kuwa na ujuzi), lakini ikipunguza maisha ya uungu ya kila siku (kama vile 1 Pet.1:14; 2:11; 4:3; 2 Pet. 2:10,18). Sura ya kwanza inakubaliana na kosa hili la 2 Pet. 1:3-11!
Maisha ya waamini ni ushuhuda wa (na sio msingi wa) mazungumzo yao ya kweli (kama vile Yakobo na 1 Yohana). Pasipo tunda, hakuna mzizi (kama vile Marko 4:1-20).

**1:5 "na kwa sababu iyo hiyo"** Hili linarejelea mwitikio wa waamini kwenye ahadi na karama za Mungu katika 2 Pet.1:3-4 (kama vile Fil. 2:12-13). Angalia MADA MAALUM: UOVU NA WEMA katika 1 Pet. 4:3.

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"mkijitahidi kwa upande wenu. . .tieni"** |
| **NKJV** | **"mkijitoa kwa upande wen, tieni"** |
| **NRSV** | **"jitahidini upande wenu"** |
| **TEV** | **"jitahidini kuongeza"** |
| **NJB** | **"jitahidini kusaidia"** |

Kwa maana iliyo wazi hiki kifungu cha maneno ni "jitahidini kwa upande wenu, tieni. . ." Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopita usiotimilifu iliyotumika kama kauli shurutishi na kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu. Mungu kwa ajabu kabisa akautoa wokovu (kama vile 2 Pet. 1:3-4); sasa waamini wanapaswa kutembea katika huo (kama vile 2 Pet. 1:5-7). Injili moja kwa moja ni ya bure kutokana na (1) mapenzi ya Mungu; (2) kazi iliyokwisha fanywa na Kristo; na (3) Roho auguaye ndani yetu, lakini tunapompokea mara moja, huwa ni uanafunzi wenye kugharimu kila kitu maishani. Hili ni fumbo la injili. Ni zawadi (kama vile Yohana 4:10; Rum. 3:24; 6:23; Efe. 2:8; Ebr. 6:4), lakini pia ni agano lenye faida na uwajibikaji. Injili ya kweli huathiri fikra, moyo, na utoaji!

◙ **"Imani"** Hili neno lina vidokezo tofauti mbalimbali.

1. mazingira ya nyuma ya Agano la Kale "uaminifu" au "kutumainiwa"
2. ukubalifu wetu au upokeaji wa msamaha wa Mungu wa bure katika Kristo
3. Uaminifu, maisha ya utauwa
4. Maana ya pamoja ya imani ya Kikristo au ukweli kumhusu Kristo (kama vile Mdo. 6:7 na Yuda 3,20).

Katika muktadha huu (yaani., 2 Pet. 1:1) inarejelea kumpokea Kristo kama Mwokozi. Sasa waamini wanapaswa kukua na kuendelea.
Matarajio ya kukua kwa Mkristo pia yameelezewa katika Rum. 5:3-4; Yakobo 1:3-4.

## MADA MAALUM: UKUAJI WA MKRISTO (tabia)

| Warumi 5:3-4 | Wagalatia 5:22-23 | Yakobo 1:3-4 | 2 Petro 1:5-7 |
|---|---|---|---|
| Dhiki inasababisha<br>* ustahimilivu<br>* tabia iliyothibitishwa<br>* tumaini (kama vile Mstari wa 2) | Tunda la Roho<br>* upendo<br>* furaha<br>* amani<br>* uvumilivu<br>* wema<br>* ukarimu<br>* uaminifu<br>* upole<br>* kiasi | Majaribu huzaa<br>* uvumilivu<br>* ukomavu<br>1. bidii<br>2.ukamilifu | Kufanyia kazi kwa bidii<br>* tabia njema<br>* maarifa<br>* kiasi<br>* ustahimilvu<br>* utauwa<br>* ukarimu wa kindugu (*philadelphia*)<br>* upendo wa kikristo (*agapē*) |

◙ **"wema"** Hii sifa ilitumika kwa Yesu (au Mungu Baba) katika 2 Pet. 1:3. Hili ni moja ya tunda la roho (kama vile Gal. 5:22-23). Ni kinyume cha neno "wingi" (kama vile 2 Pet. 2:3,14). Angalia MADA MAALUM: UOVU NA WEMA katika Agano Jipya kwenye 1 Peter. 4:2.

◙ **"maarifa"** Maarifa (*gnōsis*) ya injili ambayo hutuongoza kwenye mfanano wa Kristo ni kitu cha ajabu. Walimu wa uongo walikuwa wakitetea maarifa ya uongo ambayo yalituongoza kwenye kutenda uovu.

◙ **"kiasi"** Huu wema unamwelezea mtu mwenye uwezo wa kuzuia ubinafsi wa asili ya anguko la dhambi (kama vile Mdo. 24:25; Gal. 5:23; Tito 1:8). Katika baadhi ya muktadha (yaani., 1 Kor. 7:9) hudokeza kwenye mambo ya kujamiiana yasiyo sawa na kwa sababu ya tabia ya kwenda kinyume na sheria kwa walimu wa uongo, laweza kujumuisha hicho kidokezo hapa.

◙ **"saburi"** Hili neno linarejelea uvumilivu wa kiutendaji, wa hiari. Ni kama tabia za uvumilivu wa Mungu kwa watu na matukio (kama vile Rum. 5:3-4; Yakobo 1:3).

◙ **"utauwa"** Hili ni neno muhimu katika nyaraka za Kiuchungaji, vile vile 2 Petro (angalia maelezo katika 2 Pet.1:3), ambalo nataka kulinukuu toka kwenye fasiri yangu, juzuu ya 9, 1 Timothea 4:7:
"Hili ni neno muhimu kwenye nyaraka za kichungaji. Linarejelea kwenye kimafundisho na matumizi ya kila siku ya maisha ya injili (kama vile 1 Tim. 3:16). Halielezei upekee, bali kinachotarajiwa. Ni neno ambatani toka 'wema' (*eu*) na 'ibada' (*sebomai*). Ibada ya kweli ni maisha ya kila siku kwa namna ya fikra sahihi (kama vile 1 Tim. 4:16a). Tambua ni mara ngapi hili neno limetumika katika nyaraka za Kichungaji:

1. nomino (*eusebeia*), 1 Tim. 2:2; 3:16; 4:7,8; 6:3,5,6,11; 2 Tim. 3:5; Tito 1:1
2. kielezi (*eusebēs*), 2 Tim. 3:12; Titus 2:12
3. kitenzi (*eusebeō*), 1 Tim. 5:4
4. neno linalohusiana na *theosebeia*, 1 Tim. 2:10
5. neno kanushi (kiambishi awali hasi, yaani., *asebeia*), 2 Tim. 2:16; Tito 2:12" (p. 53).

**1:7**

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV** | **"upendo wa ndugu, upendo"** |
| **NRSV** | **"upendo wa kidugu ukiwa na upendo"** |
| **TEV** | **"upendo wa Kikristo na upendo"** |
| **NJB** | **"huruma ya kidugu ikiwa na upendo"** |

Hili ni neno ambatani la Kiyunani *phileō* (yaani., upendo) na *adephos* (yaani., ndugu). Pia linajitokeza katika 1 Pet.1:22.katika muktadha huu linarejelea kwa ndugu wa agano na dada.
Mara nyingi inasemekana kuwa neno *phileō* linarejelea upendo mdogo kuliko neno *agapeō* (kama vile 2 Pet. 1:7), lakini katika lugha ya Koine, haya maneno ni visawe (kama vile Yohana 5:20, ambayo hutumia neno *phileō* kwa ajili ya upendo wa Baba kwa ajili ya Yesu). Hata hivyo, hapa na katika Yohana 21 panaweza kuwepo na utofauti uliokusudiwa.

**1:8 "maana"** Huu sio muundo wa kawaida wa sentensi yenye masharti katika Kiyunani (kama vile NJB, hata hivyo, katika *Word Pictures in the NewTestament* A. T. Robertson inakitambua hiki kifungu kama kauli tendaji mbili endelevu za wakati uliopo zenye kueleza habari zote
[yenye masharti], kama vile juzuu ya 6, uk. 151), lakini umuhimu wa ushahidi ulitamkwa kwa ajili ya kuwa na uhakika ambao umesimamia juu ya maisha yaliyobadilika na yanayoendelea kubadilika ya toba, imani, utii, huduma, na saburi.maisha ya milele (yaani., asili ya uungu) yana tabia zinazochunguzika.

1. Waamini kuonyesha tabia za Kikristo, 2 Pet. 1:5-7
2. Waamini wana thamani na wanaongezeka (zote ni kauli tendaji za hali ya kuendelea za wakati uliopo), 2 Pet. 1:8
3. Waamini ni watendaji na wenye kuzaa matunda kwa Mungu, 2 Pet. 1:8
4. Waamini huyaishi maarifa ya kweli ya Mungu (yaani., maisha yenye kumfanana na Kristo, kama vile 2 Pet. 1:8)

◙ **"si wavivu wala watu wasio na matunda"** Kwa huzuni kubwa hili mara nyingi hujitokeza katika hali ya kiroho ya waamini.

1. Wavivu au wasio na matunda – Yakobo 2:20
2. Wasiozaa matunda – Mt. 7:16-19; 13:22; Marko 4:19; Kol. 1:10; Tito 3:14
3. Paulo analitumia neno kwenye maonyo "msishiriki katika matendo ya giza yasiozaa matunda"

Iweni waangalifu – hapana tunda, lililobaya! Maisha ya milele yana tabia zinazochunguzika. Pasipo tunda – hakuna mzizi!

**1:9** Kama ilivyo 2 Pet. 1:8 inavyoelezea Mkristo wa kweli, 2 Pet. 1:9 inaelezea waamini ambao wanashawishiwa na walimu wa uongo wenye mwainisho wa uwili kati ya maarifa–uhai, thiolojia–maadili, imani halisi–tabia njema

◙ **"kipofu"** Hii kwa maana iliyo wazi ni "kupepesa," "kukonyeza," au "makengeza." Lilitumika kiistiari kwa mtu anayejaribu kuangalia vizuri, lakini anashindwa, yumkini akiigeukia nuru (kama vile *The Vocabulary of the Greek Testament: Illustrated from the Papyri and Other Non-literary Sources* na James Hope Moulton na George Milligan, uk. 420).

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"amesahau kule kutakaswa dhambi zake za zamani"** |
| **NKJV** | **"amesahau kuwa alikwisha takaswa dhambi zake"** |
| **NRSV** | **"amesahau kutakaswa dhambi zake za zamani"** |
| **TEV** | **"amesahau kuwa amekwisha takaswa toka dhambi zake za zamani"** |
| **NJB** | **"amesahau namna dhambi zake za zamani zilivyotakaswa"** |

Hili linamaanisha kuwa hawa ni waamini, lakini wamerudi nyuma kwenye maisha ya kipagani na walimu wa uongo (kama vile 2 Petro 2). Ni huzuni iliyoje.

1. Maisha haya hayaleti furaha, amani, na uhakika
2. Maisha haya yanazuia uinjilisti
3. Maisha haya yanaangamiza huduma iliyosimama
4. -Maisha yaletayo haraka mauti

Katika kifungu hiki Petro anarejelea utakaso toka dhambini ambao hutokea kupitia kifo mbadala cha Yesu kwa ajili yetu (kama vile 1 Pet. 1:18; 2:24; 3:18).

**1:10 "fanyeni bidii zaidi"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usiotimilifu. Neno hili (kama vile 2 Pet. 1:15; 3:14) laweza kumaanisha

1. Kufanya kitu Fulani haraka (kama vile Tito 3:12)
2. Kufanya moja lililo bora (kama vile Efe. 4:3)
3. Kuwa na shauku (kama vile Mdo. 20:16; Gal. 2:10)

Uchaguzi #3 unaonekana kuwa mzuri (kama vile toleo la NRSV).

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"kufanya imara"** |
| **NKJV** | **"kufanya. . .hakika"** |
| **NRSV** | **"kuthibitisha"** |
| **TEV** | **"kufanya. . .imara"** |
| **NJB** | **"kutoruhusu. . .kutetereka"** |

Hili neno limetumika katika namna tatu.

1. Uhakika wa kuwa vizuri umetambulika (kama vile Rum. 4:16)
2. kutegemewa (kama vile 2 Pet. 2:19 na Ebr. 3:14; 6:19)
3. Kuweza kuthibitika (likitumika katika mafunjo ya lugha ya koine huko Egypt kwa ajili ya uhakika wa mambo ya sheria kama kuthibitisha utashi)

Wakristo wanaweza kuwa na uhakika (kama vile Fil. 2:12-13; 1 Yohana 5:13). Angalia Mada Maalum hapa chini.

## MADA MAALUM: DHAMANA YA MKRISTO

Dhamana ni (1) kweli ya kibiblia, (2) uzoefu wa imani ya mwamini, na (3) uthibitisho wa mtindo wa maisha.

A. Misingi ya kibiblia ya dhamana ni

1. Tabia za Mungu Baba na kusudi
    a. Kutoka 34:6-7 (tazama Mada Maalum: Tabia za Mungu wa Israeli)
    b. Nehemia 9:17
    c. Yohana 3:16; 10:28-29 (tazama Mada Maalum: Mpango wa YHWH wa Ukombozi wa Milele)
    d. Warumi 8:38-39
    e. Waefeso 1:3-14; 2:5,8-9
    f. Wafilipi 1:6
    g. 2 Timotheo 1:12
    h. 1 Petro 1:3-5

2. Kazi ya Mungu Mwana
    a. Maombi yake ya kikuhani, Yohana 17:9-24, hasa mst. wa 12; Waebrania 7-9
    b. Kujitoa kwake kama dhabihu (kama vile. Isa. 52:13-53:12)
        1) Marko 10:45
        2) 2 Wakorintho 5:21
        3) 1 Yohana 2:2; 4:9-10
    c. Kusihi kwake katika hali endelevu
        1) Warumi 8:34
        2) Waebrenia 7:25
        3) 1 Yohana 2:1

3. Uwezesho wa Mungu Roho Mtakatifu
    a. Wito wake, Yohana 6:44,65
    b. Hatima yake
        1) 2 Wakorintho 1:22; 5:5
        2) Waefeso 1:13-14; 4:30
    c. Dhamana yake binafsi
        1) Warumi 8:16-17
        2) 1 Yohana 5:7-13

B. Umuhimu wa mwitikio wa kimaagano wa mwamini ni (angalia Mada Maalum: Agano)
1. Toba na imani ya mwanzo na endelevu (tazama Mada Maalum: Je! "Pokea," "Amini," "Kiri/Ungama," na "Kusihi" kunamaanisha nini?)
    a. Marko 1:15
    b. Yohana 1:12
    c. Matendo 3:16; 20:21
    d. Warumi 10:9-13
    e.
2. Kumbuka kwamba lengo la wakovu ni kumfanana Kristo
    a. Warumi 8:28-29
    b. 2 Wakorintho 3:18
    c. Wagalatia 4:19
    d. Waefeso 1:4; 2:10; 4:13
    e. 1 Wathesalonike
    f. 2 Wathesalonike 3:13; 4:3; 5:23
    g. Tito 2:14
    h. 1 Petro 1:15
3. kwa kukumbuka kwamba dhamana inakamilishwa na mtindo wa maisha
    a. Yokobo
    b. 1 Yohana
4. kwa kukumbuka kwamba dhamana inakamilishwa kwa imani thabiti na ustahimilivu (tazama Mada

Maalum: Ustahimilivu)

a. Marko 13:13
b. 1 Wakorintho 15:2
c. Waebrania 3:14; 4:14
d. 2 Petro 1:10
e. Yuda 1:20-21

◙ **"kuitwa kwenu"**Neno "kwenu" haliko katika andiko la Kiyunani, lakini linadokeza toka 2 Pet. 1:3. Tumaini la mwisho la mwamini liko katika tabia ya Mungu, kazi ya Mwana, Roho auguaye ndani mwetu. Hata hivyo, haya yanathibitishwa ndani mwamini pekee kwa maisha ya imani walionayo, utauwa. (kama vile 2 Pet. 1:5-7; Fil. 2:12-13). Mungu hushughulika na mwanadamu katika uhusiano wa kiagano. Huweka mkakati, huanzisha mpambano, hutuvuta kwenda kwake, lakini lazima tuitike mwanzoni na kuendelea katika toba, imani, huduma, utii, na saburi. Injili ni nafsi inayotakiwa kukaribishwa, ukweli wa kuaminiwa, na maisha ya kuishi kwayo! Ikiwa mtu ataondoka, kukua, wokovu wa Kibiblia hauwezekani.

## MADA MAALUMU: KUITWA

Siku zote Mungu anachukua uwezo wa kuanzisha jambo katika mwito, uchaguzi, na akiwatafuta waumini waje kwake (kama vile. Yohana 6:44,65; 15:16; 1 Kor. 1:1-2; Efe. 1:4-5,11). Neno “kuitwa” limetumika kwa maana nyingi za kithiolojia.

A. Katika Agano la Kale “uitaji wa jina” mara nyingi ulikuwa katika mazingira ya kuabudu (kama vile. Mwa. 4:26; 12:8; 21:33; 26:25; Kut. 34:5).
B. Wenye dhambi wanaitwa kwenye wokovu kwa neema ya Mungu (yaani., Kut. 34:6-7) kupitia katika kazi aliyoimaliza Kristo na kwa kusadikishwa na Roho ((yaani., *klētos*, kama vile. Rum. 1:6-7; 9:24, ambayo kithiolojia inafanana na 1 Kor. 1:1-2 na 2 Tim. 1:9; 2 Petr. 1:10).
C. Wenye dhambi wanaliitia jina la Bwana ili waokolewe (yaani., *epikaleō*, kama vile. Mdo. 2:21; 22:16; Rum. 10:9-13). Maelezo haya ni nahahu ya Kiyahudi katika taratibu za kuabudu.
D. Waumini huliita jina lake nyakati za migogora na msongo wa mawazo (yaani., Mdo.7:59).
E. Waumini wameitwa kuishi maisha yanayomfanana Yesu i.e., *klēsis*, kama vile. 1 Kor. 1:26; 7:20; Efe. 4:1; Fil. 3:14; 2 The. 1:11; 2 Tim. 1:9).

Waumini wameitwa kwenye kazi ya huduma (kama vile. Mdo. 13:2; 1 Kor. 12:4-7; Efe. 4:1).

◙ **"na uteule wenu"** Nomino *eklogē* mara nyingi hutumika kwenye uchaguzi wa Mungu.

1. Yakobo/Israeli – Rum. 9:11
2. Mabaki waliochaguliwa – Rum. 11:5,28
3. Waamini wa Agano Jipya – Rum. 11:7
4. Kanisa – 1 The. 1:4; 2 Pet. 1:10

Angalia Mada Maalum katika Marko 13:20 na 1 Petro 1:2.

◙ **"maana mkienenda katika hayo, hamtajikwaa kamwe"** Neno "mambo haya" linarejelea kwa 2 Pet.1:3-7. Maisha ya milele yana tabia zinazochunguzika.
Kisarufi (yaani., kanusho mara mbili) na neno *pote* (yaani., "wakati wowote" au "milele") huleta uhakika mkubwa kwa mwamini anyehangaika katikati ya mateso na dhiki (yaani., 1 Petro) na mafundisho ya uongo (yaani., 2 Petro).
Katika *Word Pictures in the NewTestament*, vol. 6, p. 153, A. T. Robertson anatambua kitenzi "enendeni" (yaani., *pioeō*) kama kauli tendaji yenye masharti endelevu ya wakati uliopo, kama 2 Pet. 1:8. Toleo la NASB, NKJV, NRSV, na TEV hujumuisha neno la kiingereza lenye masharti "ikiwa" katika utafasiri wao (kama 2 Pet. 1:8).

◙ **"hamtajikwaa kamwe"** Huu ni muundo wa kisarufi (kanushi mara mbili na dhamira tegemezi),ambayo ni namna ya nguvu ya kukanusha jambo. Ukweli wa namna ile ile umeelezewa katika Yuda 24.

Hata hivyo, kama ilivyo Waebrania (kama vile Ebr. 2:1-4; 3:7-4:11; 5:11-6:12; 10:9-39; 12:14-29), 2 Petro ina baadhi ya maonyo ya kusikitisha (kama vile 2 Pet. 2:1,20-22; 3:17). Wokovu ni ulinzi (kama vile 1 Pet. 1:4-6), lakini ni lazima utunzwe.

## MADA MAALUMU: UASI (*APHISTĒMI*)

Neno la Kiyunani *aphistēmi* lina uwanja mpana wa elimu-maana. Hata hivyo, Neno la Kiingereza "uasi" limetokana na neno hili na athari za matumizi yake kwa wasomaji wa sasa. Muktadha, kama iliyo kawaida, ndio ufunguo, sio maelezo ya wakati uliopo.

Hili ni neno lililounganishwa kutokana na KIHUSISHI *apo*, ambacho kinamaanisha "kutokana na" au "mbali na" and *histēmi*, "kukaa," "kusimama," au "kupachika." Angalia matumizi yafuatayo (yasiyo ya kithiolojia):

1. kuondoa kimwili
    1. kutoka Hekaluni, Luka 2:37
    2. kutoka katika nyumba, Marko 13:34
    3. kutoka kwa mtu, Marko12:12; 14:50; Matendo 5:38
    4. kutoka katika vitu vyote, Mt. 19:27,29
2. kuondoa kisiasa, Matendo 5:37
3. kuondoa kimahusiano, Matendo 5:38; 15:38; 19:9; 22:29
4. kuondoa kisheria (tarakisha), Kumb. 24:1,3 (LXX ) na Agano Jipya, Mat. 5:31; 19:7; Marko 10:4; 1 Cor. 7:11
5. kuondao deni, Mt. 18:7
6. kuonyesha kutokuhusika kwa kuondoka, Mt. 4:20; Yohana 4:28; 16:32
7. kuonyesha kutokuhusika kwa kutoondoka, Yohana 8:29; 14:18
8. kuruhsu au kutoa kibali, Mt. 13:30; 19:14; Marko 14:6; Luka 13:8

Katika maana ya kitheolojia KITENZI pia kina matumizi mapana:

1. kufuta, kusamehe, kuifuta hatia ya dhambi, Kut.32:32 (70) (LXX); Hes. 14:19; Yak. 42:10 na Agano Jipya, Mt. 6:12,14-15; Marko 11:25-26
2. kujiondoa toka dhambini, 2 Tim. 2:1
3. kukataa kwa kujiondoa toka kwenye
    a. Sheria, Mat. 23:23; Matendo 21:21
    b. imani, Ezek. 20:8 (LXX ); Luka 8:13; 2 The. 2:3; 1 Tim. 4:1; Ebr. 3:12

Waamini wa sasa wanauliza maswali mengi ya kitheolojia ambayo waandishi wengi wa Agano Jipya wasingalifikiri kuyahusu. Moja ya haya yangeliweza kuhusiana na uelekeo wa sasa wa kuitenga imani (uthibitisho) kutoka kwenye imani (utakaso).

Kuna watu katika Biblia walihusishwa miongoni mwa watu wa Mungu na jambo lililotokea na kusababisha wao kuondoka.

I. Agano la Kale
    A. Wale walioisikia taarifa ya wale wapelelezi kumi na wawili (kumi), Namba 14 (kama vile Heb. 3:16-19)
    B. Kora, Namba 16
    C. Wana wa Eli, 1 Samueli 2, 4
    D. Sauli, 1 Samueli 11-31
    E. Manabii wa uongo (mifano)
        1. Kumb. 13:1-5 18:19-22 (nji za kumtambau nabii wa uongo)
        2. Yeremia 28
        3. Ezekieli 13:1-7
    F. Manabii wa uongo
        1. Ezekieli 13:17
        2. Nehemia 6:14
    G. Uovu wa viongozi wa Israeli (mifano)
        1. Yeremia 5:30-31; 8:1-2; 23:1-4
        2. Ezekieli 22:23-31

3. Mika 3:5-12

II. Agano Jipya

A. Hili neno la Kiyunani kifasihi linamaanisha "kuasi."Vitabu vyote vya Agano la Kale na Agano Jipya vinathibitisha uchochezi wa uovu na mafundisho ya uongo kabla ya Ujio wa Pili (kama vile Mt. 24:24; Marko 13:22;

Matendo 20:29,30; 2 The. 2:9-12; 2 Tim. 4:4). Neno hili la Kiyunani linaweza kuyaaakisi maneno ya Yesu katika Mfano wa Udongo unaopatikana katika Mathayo 13; Marko 4; na Luka 8. Kwa kudhaniwa walimu hawa wa uongo si Wakristo, bali waamini wachanga (kama vile Ebr. 3:12).

Swali la kitheolojia ni hili walimu wa uongo wanawapeleka wapi waamini? Hili ni vigumu kulijibu kwa kuwa kulikuwa na walimu wa uongo katika makanisa anzilishi (kama vile 1 Yohana 2:18-19). Mara nyingi tamaduni au madhehebu yetu yanajibu swali hili pasipokuwa na marejeo ya maandiko ya Biblia mahususi (isipokuwa njia ya kuhakiki kwa nukuu mstari ulio nje ya muktadha ili kwa uangalifu kuhakiki madhara yaliyomo).

B. Imani Thabiti

1. Yuda, Yohana 17:1
2. Simoni mchawi, Matendo 8
3. Wale waliozungumziwa katika Mat. 7:13-2
4. Wale waliozungumziwa katika Mathayo 13; Marko 4; Luka
5. Wayahudi wa Yohana 8:31-59
6. Alexanda na Himenayo, 1 Tim. 1:19-20
7. Wale wa 1 Tim. 6:21
8. Himanayo na Fileto, 2 Tim. 2:16-18
9. Dema, 2 Tim. 4:10
10. Walimu wa uongo, 2 Petro 2:19-22; Yuda 1:12-19
11. wapinga Kristo, 1 Yohana 2:18-19

C. mani isiyo kuwa na matunda

1. 1 Wakorintho 3:10-15
2. 2 Petro 1:8-11

Mara chache tunafikiri juu ya haya maandiko kwa kuwa mfumo wa injlili yetu (Ufuatao mtazamo wa Calvn, Arminian, n.k.) unaamuru mwitikio wa kimamlaka. Tafadhari usinihukumu kabla kwa kuwa nafundisha somo langu. Shauku yangu ni hatua ya kiufasiri. Tunapaswa kuipa nafasi Biblia ili izungumze nasi na si kuiumba katika mpangilio wa thiolojia iliyopita. Mara nyingi hii inaumiza na kushtua kwa kuwa thiolojia zetu zilizo nyingi ni za kimadhehebu, kitamaduni, kimahusiano (mzazi, rafiki,mchungaji), si za kibiblia (tazama Mada Maalumu: Nini maana ya neno "Kupokea," "Kuamini," "Kiri/Ungama,"na "Itisha"?). Wengine walio miongoni mwa watu wa Mungu wanarudi nyuma na kutokuwa miongoni mwa watu wa Mungu (m.f. Rum. 9:6).

**1:11 "ufalme wa milele"** Hili linarejelea kwenye utawala wa YHWH na Masihi (kama vile Isa. 9:7; Dan.7:14,27; Luke 1:33; 1 Tim. 6:16; Ufu. 11:15, 22:5). Hili halirejelei kwenye utawala wa miaka elfu moja wala kutenda andiko lolote la Agano Jipya, isipokuwa Ufunuo 20, ingawa baadhi wanaliona kama nukuu ya moja kwa moja katika 1 Kor. 15:25-28.

◙ **"Bwana na Mwokozi"** Kifungu cha aina ile ile kimetumika kwa mfalme mkuu. Ni jina adimu lililotumika mara nyingi katika kitabu hiki (kama vile 2 Pet. 1:11; 2:20; 3:2,18).

◙ **"maana mtaruzukiwa"** Hii ni kauli tendwa elekezi ya wakati ujao. Muundo shurutishi ulitumika katika 2 Pet. 1:5. Mungu atatoa mahitaji ya waamini wote (kama vile 2 Pet. 1:3). Waamini wanaamrishwa kuitikia vizuri katika nuru ya utoaji wa Mungu (kama vile 2 Pet. 1:4). Mwitikio wao haukuwa namna ya kukubaliwa na Mungu, lakini ushuhuda ya kuwa wamekubaliwa na Mungu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 PETRO 1:12-15**

**[12] Kwa hiyo nitakuwa tayari kuwakumbusha hayo siku zote, ijapokuwa mnayajua na kuthibitishwa katika kweli mliyo nayo. [13] Nami naona ni haki, maadamu nipo mimi katika maskani hii, kuwaamsha kwa kuwakumbusha. [14] Nikijua kwamba kule kuwekea mbali maskani yangu kwaja upesi, kama Bwana wetu Yesu Kristo alivyonionyesha. [15]**

**Walakini nitajitahidi, kwamba kila wakati baada ya kufariki kwangu mpate kuyakumbuka mambo hayo.**

**1:12 "kwa hiyo"** ikipatikana juu ya kweli ya injili ya 2 Peter 1.

◙ **"nitakuwa tayari kuwakumbusha hayo"** Hili ni somo linalojirudia (kama vile 2 Pet. 1:12-13,15; 3:1-2; Fil.3:1; Yuda 5,17). Huu ukweli wa injili unahitaji kurudiwa tena na tena kwa ajili ya kuwataarifu waamini wapya na kutunza uaminifu kwa waamini waliokomaa. Mistari ya 12-15 mara nyingi inatambulika kama uwasilisho wa "shuhuda." Mara nyingi inahusiana na maneno ya mwisho ya mtu kabla ya kufa (kama vile Yos. 23-24; 1 Sam. 12; 2 Tim. 4:6-8; 2 Pet. 1:12-15).

◙ **"mkithibitishwa"** Hii ni kauli tendwa timilifu ya hali ya kuendele. Hii yaweza kurejelea (1) kuihubiri injili au (2) kuidhihirisha miujiza. Tambua ni nguvu ya Mungu (sauti irabu tendwa) ziletazo nguvu za mwamini (kama vile 1 Pet. 5:10). Lakini mwamini anapaswa kuzilinda (kama vile 2 Pet. 3:17; 1 Pet. 5:9).

◙ **"katika kweli"** Maneno "ukweli/kweli/kutumainika" ni dhana za kibiblia ambazo ni muhimu ambazo ningepaswa kushirikishana na wewe kwenye maada maalum zilizochukuliwa toka kitabu cha Yohana (Vol. 4).

## MADA MAALUM: "UKWELI" (DHANA) KATIKA MAANDIKO YA YOHANA

Kwa namna fulani Yohana anaunganisha historia ya Waebrania na historia ya nyuma ya Wayunani ya alētheia "ukweli" kama alivyofanya logos (kama vile 1:1-14). Waebrania (angalia Mada maalum: Amini, Tumaini, Imani na Uaminifu) inaashiria kile ambacho ni kweli, au kinachotumainika (mara kwa mara inahusianishwa katika tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani pisteuō). Katika Kiyunani ilihusianishwa uhalisia wa Plato dhidi ya kukosekana kwa uhalisia; kimbingu dhidi ya kidunia. Hii inashabihiana na nadharia ya U-pili wa Yohana. Mungu amefunua kwa uwazi (asili ya alētheia ni kufunua, kuweka wazi, kudhihirisha wazi) Yeye mwenyewe ndani ya Mwana. Hii inaelezewa katika njia kadhaa.

1. nomino, alētheia, kweli
   a. Yesu amejaa neema na kweli (kama vile Yohana 1:14,17 – masharti ya Agano la Kale)
   b. Yesu ndiye lengo la ushuhuda wa Yohana Mbatizaji (kama vile Yohana 1:32-34; 18:37 – nabii wa mwisho wa Agano la Kale)
   c. Yesu anazungumza kweli (kama vile Yohana 8:40,44,45,46 – Ufunuo ni wa binafsi na unashawishi)
   d. Yesu ni njia kweli na uzima (kama vile Yohana 14:6)
   e. Yesu anawatakasa katika kweli (kama vile Yohana 17:17)
   f. Yesu (Logos, 1:1-3) ni kweli (kama vile Yohana 17:17)
2. kivumishi, alēthēs, kweli, enye kutumainiwa
   a. ushuhuda wa Yesu (kama vile Yohana 5:31-32; 7:18; 8:13-14)
   b. hukumu ya Yesu (kama vile Yohana 8:16)
3. kivumishi, alēthinus, hakika
   a. Yesu ni nuru ya kweli (kama vile Yohana 1:9)
   b. Yesu ni mkate wa kweli (kama vile Yohana 6:32)
   c. Yesu ni divai ya kweli (kama vile Yohana 15:1)
   d. Yesu ni shuhuda wa kweli (kama vile Yohana 19:35)
4. adverbkielezi, alēthōs, trulycha kweli
   a. Msamaria anamshuhudia Yesu kama mwokozi wa ulimwengu(kama vile Yohana 4:42)
   b. Yesu ni chakula cha kweli ukitofautisha na manna ya siku za Musa (kama vile Yohana 6:55)
5. Neno kweli na vielezi vyake pia linaelezea ushuhuda wa wengine kwa Yesu, alēthēs
   a. Ushuhuda wa Yohana Mbatizaji ni kweli (kama vile Yohana 10:41)
   b. Ushuhuda wa Yohana (mwandishi wa injili) ni kweli (kama vile Yohana 19:35; 21:24)
   c. Yesu anaonekana kama nabii wa kweli (kama vile Yohana 6:14; 7:40)

Kwa mjadala mzuri wa kweli katika Agano Jipya na Agano la Kale angalia George E. Ladd's A Theology of the New Testament, kur. 263-269.

## MADA MAALUM: "KWELI" (NENO) KATIKA MAANDIKO YA YOHANA

1. Mungu Baba
   a. Mungu ndiye wa kutumainiwa kweli (kama vile Yohana 3:33; 7:18,28; 8:26; 17:3; Rum. 3:4; 1 The. 1:9; 1 Yohana 5:20; Ufu. 6:10)
   b. Njia za Mungu ni kweli (kama vile Ufu. 15:3)
   c. Hukumu za Mungu ni kweli (kama vile Ufu. 16:7; 19:2)
   d. Misemo ya Mungu ni kweli (kama vile Ufu. 19:11)
2. Mungu Mwana
   a. Mwana ni kweli
      1) mwanga wa kweli (kama vile Yohana 1:9; 1 Yohana 2:8)
      2) divai ya kweli  (kama vile Yohana 15:1)
      3) amejaa neema na kweli (kama vile Yohana 1:14,17)
      4) Yeye ni ukweli (kama vile Yohana 14:6; 8:32)
      5) Yeye ni kweli (kama vile Ufu. 3:7,14; 19:11)
   b. Ushuhuda wa Mwana ni kweli (kama vile Yohana 18:37)
3. Linaweza kuwa na aina ya ulinganifu
   a. sheria ya Musa dhidi ya neema na kweli (kama vile Yohana 1:17)
   b. hema jangwani dhidi ya hema la kimbingu (kama vile Ebr. 8:2; 9:1)
4. Kama ilivyo katika maandiko ya Yohana neno hili lilikuwa na visawe kadhaa (vya kiebrania na Kiyunani). Yohana anavitumia vyote kuelezea Baba na Mwana kama nafsi, wazungumzaji na kama jumbe zao ambazo zinatakiwa kufikishwa kwa wafuasi wao (kama vile Yohana 4:23; 19:35; Ebr. 10:22; Ufu. 22:6).
5. Kwa Yohana vivumishi hivi viwili kumuelezea Baba kama Mungu pekee tu mwenye kutumainika (kama vile 5:44; 1 Yohana 5:20) na Yesu na Ufunuo Wake mkamilifu na pekee kwa makusudi ya ukombozi na sio tu kueleza kweli za kiakili!

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"mliyo nayo"** |
| **NKJV** | **"iliyo katika kweli"** |
| **NRSV** | **"iliyo waajilia"** |
| **TEV** | **"mliyo ipokea"** |
| **NJB** | **(kifungu kimeondolewa)** |

Kwa maana iliyo wazi ni "iliyo katika kweli." Ni kwa namna gani"ukweli" unakuwepo? Ukweli ni (1) ni tabia na maneno ya Mungu ya kuaminika na (2) ni maelezzo ya Yesu na namna yanavyorejelewa katika ujumbe wa injili (yaani., neno liishilo na neno lililoandikwa).
Neno "iliyopo" ni neno *parousē*, lililotumika kuelezea ujio wa mara ya pili wa Kristo kama "alivyokuwepo" (kama vile 2 Pet. 1:16; 3:4,12).

**1:13 "maadamu nipo"** Paulo pia anatumia kifungu hiki 2 Kor. 5:1-10 kurejelea kwenye uwepo wake kimwili. Mistari ya 14 na 15 kwa wazi inaonyesha kuwa Petro alitarajiwa kuuwawa hivi karibuni.

**1:14 "Bwana wetu Yesu Kristo"** Hili jina lingaliweza kumaanisha kweli mbalimbali za kithiolojia kwenye karne ya kwanza ya uongozi wa Kiyahudi/Kikristo.

◙ **"Bwana"** Neno la Kiyunani Bwana (*kurios*) laweza kutumika katika maana ya pamoja au maana ya thiolojia endelevu. Laweza kumaanisha "bwana," "bwana" (kama vile Yohana 4:11), "bwana," "mmiliki," "bwana," au "Mungu mwanadamu kamili" (kama vile Yohana 9:36,38). Matumizi ya Agano la Kale (Kiebrania, *adon*)ya neno hili lilitokana na Wayahudi

kushindwa kutamka jina la agano la YHWH, toka kwenye kitenzi cha Kiebrania "kuwa" (kama vile Kut. 3:14). Angalia Mada Maalum: Majina ya Uungu katika Marko 12:36. Waliogopa kuivunja amri, ambayo inasema, "usilitaje bure jina la Mungu wako" (kama vile Kut. 20:7; Kumb. 5:11). Kwa hiyo, walifikiri kama hawatalitamka, hawawezi kulitaja bure. Kwa hiyo, walitumia jina mbadala *adon*, lenye kuwa na maana inayofanana na ile ya Kiyunani *kurios* (Bwana). Waandishi wa Agano Jipyawalitumia neno hili kuelezea uungu kamili wa Kristo. kifungu "Yesu ni Bwana" ulikuwa ni ukiri wa wazi wa imani na njia ya kiubatizo ya kanisa la mwanzo (kama vile Rum. 10:9-13; 1 Kor. 12:3; Fil. 2:11).

◙ **"Yesu"** Hili jina la Kiebrania lilimaanisha "YHWH anaokoa" au "YHWH huleta wokovu." Lilifunuliwa kwa wazazi wake na malaika (kama vile Mt. 1:21). Neno "Yesu" lilitolewa toka neno la Kiebrania kwa ajili ya wokovu, *hosea*, kiambishi tamati kwenye jina la agano la Mungu, YHWH. Linafanana na jina la Kiebrania Yoshua.

◙ **"Kristo"** Hili ni neno la Kiyunani linalofanana na neno la Kiebrania, *messiah*, lenye kumaanisha "aliyepakwa mafuta." linamaanisha "mmoja aliyeitwa na kuwezeshwa na Mungu kwa ajili ya kazi maalum." Katika Agano la Kale makundi matatu ya viongozi: kuhani,wafalme, na manabii ndio walitiwa mafuta. Yesu alitimiza vigezo vya hizi ofisi tatu (kama vile Ebr. 1:2-3).

◙ **"alivyonionyesha"** hili laweza kurejelea kifo cha Petro (kama vile Yohana 13:36) au namna ya kifo cha Petro ambacho kilifunuliwa na Bwana kwa Petro katika Yohana 21:18-19.

**1:15 "baada ya kufa kwangu"** Hili ni neno "kuondoka" (kama vile Luk 9:31) likitumika kwa maana ya kifo (yaani., a tasifida) au kurudi mbinguni.

◙ **"mpate kuyakumbuka mambo haya"** Hili lingaliweza kurejelea kwenye kitabu cha 1 Petro, 2 Petro, au injili ya Marko (kama vile Irenaeus). Petro anatambua kuwa Roho angelitumia maandiko yake baada ya kufariki. Alikuwa akimaanisha kuwa Roho alikuwa akiongea kupitia yeye kwa ajili ya Wakristo kusoma na kuyatumia baada ya kifo!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 PETRO 1:16-18**
**[16] Maana hatukufuata hadithi zilizotungwa kwa werevu, tulipowajulisha ninyi nguvu zake Bwana wetu Yesu Kristo na kuja kwake; bali tulikuwa tumeuona wenyewe ukuu wake. [17] Maana alipata kwa Mungu Baba heshima na utukufu, hapo alipoletewa sauti iliyotoka katika utukufu mkuu, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye. [18] Na sauti hiyo sisi tuliisikia ikitoka mbinguni tulipokuwa pamoja naye katika mlima ule mtakatifu.**

**1:16**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"hadithi zilizotungwa kwa werevu"** |
| **NKJV** | **"hadithi za kitapeli zidanganyazo"** |
| **NRSV** | **"Hadithi zilizotungwa kwa werevu"** |
| **TEV** | **"hadithi zilizotungwa tungwa"** |
| **NJB** | **"hadithi za kubuniwa kwa werevu"** |

Hii ni kauli tendwa timilifu ya hali ya kuendelea, yenye kudokeza hali ya kudumu ya kudanganya (njeo ya wakati uliotimilifu) iletwayo na wawakilishi wa nje wasiojulikana (sauti irabu tendwa) ambao wangewezakuwa walimu wa uongo wao wenyewe au Yule mwovu. Tunapata neno la Kiingereza "hadithi za kutungwa" toka neno hili la Kiyunani, ambalo hupatikana hapa tu katika

1. 1 Tim. 1:4; 4:7
2. 2 Tim. 4:4
3. Tito 3:9,14
4. 2 Pet. 1:16

Tangu pale hawa walimu wa uongo (kutokana na maelezo ya 2 Petro 2) walikuwa ni wenye ujuzi wa mwanzo wakiwa na baadhi ya tabia za Kiyahudi (yaani., #2), hizi hadithi za kutunga zingalirejea kwa

1. viwango vya malaika kati ya mungu mtakatifu na viumbe wengine wadogo (aeons) na majina yao ya siri
2. Vizazi vinavyohusiana na Masihi kama mtu wa mbinguni tofauti toka Kristo aliyekuwa mwanadamu kamili
3. Utengano wa kimakusudi wa kithiolojia kwenye wokovu na maadili/uadilifu

Kwa ajili ya mjadala mzuri wa namna mbalimbali za "hadithi za kubuniwa" zilizotumika, angalia G. B. Caird, *The Language and Imagery of the Bible*, sura za 12-13, kur. 201-243.

◙ **"kuja kwake Bwana"** Hiki ni kiini kingine cha somo cha kitabu hiki. *Parousia*, kikielezewa kama "kuja" au "kuwepo" (mzizi wa aina ile ile katika 2 Pet. 1:12), unatumika katika lugha ya Koine kwa ajili ya ujio wa kifalme wa mfalme. Neno *parousia* mara nyingi linarejelea ujio wa mara ya pili (kama vile 2 Pet. 3:4,12), lakini laweza kurejelea kwenye kufanyika mwili. Laweza kurejelea hivyo hapa kwa sababu ya dokezo la kimuktadha kwenye kubadilika sura kifungu kinachofuata.

## MADA MAALUM: MANENO KWA UJIO WA MARA YA PILI

Kuna maneno na vifungu kadhaa ambavyo vinarejea juu ya kurudi kwa Yesu.

1. *parousia*" yaani, Yakobo 5:7), ambalo linamaanisha "kuwepo," lililotumika kifalme(kama vile Mt. 24:3,27,37,39; 1 Kor. 15:23; 1 The. 2:19; 3:13; 4:15; 5:23; 2 The. 2:1,8; 2 Pet. 1:16; 3:4,12; 1 Yohana 2:28)
2. *epiphaneia*, "mwonekano wa ana kwa ana" (yaani, 1 Tim. 6:14; 2 Tim. 1:10; 4:1,8; Tito 2:13)
3. *apokalupis*, "kufunua" au "konyesha" (yaani, 1 Kor. 1:7; 2 The.1:7; 1 Pet. 1:5,13; 4:13; 5:1)
4. "siku ya Bwana" na mabadiliko ya kifungu hiki (angalia Mada Maalum: Siku ya Bwana)

Kitabu cha Agano Jipya kama kilivyo kizima kimeandikwandani ya mtazamo wa ulimwengu wa Agano la Kale, ambao unadai kwamba

1. uovu wa sasa, zama za uasi
2. zama mpya za haki zijazo
3. hii ingeletwa na ushirika wa Roho kupitia kazi ya Masihi (Mpakwa Mafuta; tazama Mada Maalum: Masihi)

Dhanio la kithiolojia la uhusiano endelevu linahitajika kwa sababu waandishi wa Agano Jipya kwa uchache wanabadilisha matarajio ya Israeli. Badala ya jeshi, ilitazamiwa kitaifa (Israeli) ujio wa Masihi, kuna ujio wa mara ya pili. Ujio wa mara ya kwanza ulikuwa wa umbo-mwili la Uungu katika kutungungwa mimba na kuzaliwa kwa Yesu Mnazarethi. Yeye alikuja kama mtu asiye na majeshi, si mtu wa sheria "mtumwa ateswaye" wa Isaya 53; pia aliyejifanya mdogo juu ya juu ya mngongo wa punda (si farasi wa vita au nyumbu wa vita), wa Zek. 9:9. Ujio wa kwanza ulizitambulisha Zama Mpya za Kimasihi, ufalme wa Mungu hapa duniani (tazama Mada Maalum: Ufalme wa Mungu). Katika maana moja ufalme wa Mungu uko hapa, lakini kwa jinsi hiyo, katika maana nyingine huu bado u mbali. Huu ni mvutano kati ya ujio wa aina mbili wa Masihi ambao, katika maana, huku ni kupishana kwa zama za Kiyahudi ambazo zilikuwa hazikuonekana, au hata kutokuwa sawa, kutoka Agano la Kale (tazama Mada Maalum: Zama hizi na Zama Zijazo). Katika ukweli, ujio ulio katika uwili unasistiza juu ya ahadi za YHWH za kuwakomboa watu wote (kama vile Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5 na kuhubiri kwa manabii, hasa Isaya na Yona; tazama Mada Maalum: Mpango wa YHWH wa Ukumbozi wa Milele).

Kanisa halisubirii ule utimilifu wa Agano la Kale kwa sababu unabii ulio mwingi unarejea juu ya ujio wa kwanza (kama vile *How to Read the Bible For All Its Worth,* uk. 165-166). Nini waamini wanakitarajia ndani ya ujio wa utukufu wa Mfalme wa Wafalme na Bwana wa Mabwana, historia ya utimilifu wa zama mpya za haki zilizotarajiwa hapa duniani bado iko mbinguni (kama vile Mt. 6:10). Uwasilishaji wa Agano la Kale haukuwa sahihi, bali haukukamilika. Yeye atakuja tena kama manabii walivyotabiri, katika uweza na mamlaka ya YHWH (tazama Mada Maalum: Kwa nini Ahadi za Kiagano Zinaonekana Tofauti Sana Ahadi za Agano Jipyana Agano Jipya?).

Ujio wa Mara ya Pili si neno la kibiblia, bali ni muundo wa dhana ya matazamo wa ulimwengu na sura ya Agano Jipya lote. Mungu atayaweka mambo yote sawa. Ushirika na kati ya Mungu na mwanadamu aliyeumbwa kwa sura na mfano Wake utajejeshwa (kama vile Ufuunuo 21-22). Waovu watahukumiwa na kuondoshwa (kama vile Ufu. 20:11-15). Makusudi ya Mungu ataweza, hawezi, atashindwa!

◙ **"tumeuona wenyewe ukuu wake"** Hili linadai kuwa uandishi wa Petro ni wa kushuhudia kwa macho maisha ya Yesu

akiwa hapa duniani. Hili haswa linarejelea kipindi alipogeuka sura (kama vile 2 Pet. 1:18 na Marko 9:2-8). Kifungu hiki pia kilitumika kwenye uanzishaji wa mambo ya dini kisiri wakipitia hali ya kuwa pamoja na mungu. Petro, kama Paulo, mara nyingi alitumia vifungu vya wapinzani wake kama namna ya kuwapinga au kuwapatia maana iliyo sahihi.
Yesu anaelezewa kwa neno "mkuu." Katika mstari unaofuata (2 Pet. 1:17) Mungu Baba anatambuliwa kwa neno lilelile "Ukuu wa Utukufu." Umuhimu wa Uungu ndani ya Yesu haukuwekwa wazi kwenye kundi la wanafunzi (yaani., Petro, Yakobo, na Yohana) pale walipokuwa mlimani.

◙ **1:17 "heshima na utukufu"** Yawezekana hii ni nukuu kwenye "wingu la utukufu *Shekinah*" (vile walimu wa sheria za Kiyahudi wanavyoliita wingu katika kitabu cha Kutoka na Hesabu),wingu ambalo Mungu alizungumza kupitia kwalo (kama vile Marko 9:2-8). Angalia MADA MAALUM: UTUKUFU *(DOXA)* katika 1 Peter 1:21.

◙ **"Baba"** Angalia Mada Maalum katika Marko 13:32.

◙ **"sauti"** Walimu wa sheria za Kiyahudi waliita hili neno *Bath Kol* (yaani., sauti itokayo mbinguni), ambalo lilikuwa ni uthibitisho wa mapenzi ya Mungu toka Malaki hadi Yohana Mbatizaji ambapo hapakuwepo na sauti ya nabii. Baba anamthibitisha Yesu kote kwenye ubatizo wake na kipindi cha kubadilika sura (kama vile Marko 1:11; Mt. 17:5-6).

◙ **"Mwanangu Mpendwa"** Hili ni jina la Kimasihi toka Zab. 2:7.

◙ **"ninayependezwa naye"** Hili ni dokezo kwa Isa. 42:1 (kama vile Mt. 3:17; 17:5). Kwa kuhusianisha Zaburi 2 na Isaya 42, Petro anasisitiza dhana zote za kifalme na mtumishi atesekaye za Masihi. hizi dhana mbili pia zinaelezea ujio wake mara mbili: kufanyika mwili = Mtumishi atesekaye; ujio wa mara ya pili = Mfalme na mwamuzi!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 PETRO 1:19-21**
**19 Nasi tuna lile neno la unabii lililo imara zaidi, ambalo, mkiliangalia, kama taa ing'aayo mahali penye giza, mwafanya vyema, mpaka kutakapopambazuka, na nyota ya asubuhi kuzuka mioyoni mwenu.**
**20 Mkijua neno hili kwanza, ya kwamba hakuna unabii katika maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu. 21 Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu.**

**1:19 "Neno la kinabii"** Hili linarejelea (1) maandiko ya Agano la Kale (yaani., 2 Pet. 1:17) au (2) mashuhuda wa Kitume wa Agano Jipya (kama vile 2 Pet. 1:12; 1 Yohana 1:1-5).

◙ **"lililo imara zaidi"** Ufunuo wa Mungu wa Agano la Kale umethibitishwa katika ufunuo wa Agano Jipya. Hakika Agano la Kale ni muhimu kulielewa agano Jipya (kama vile Marko 1:1-3). Aya hii nzima inahusiana na kuchelewa kwa ujio wa mara ya pili, ambao baadhi wameanza kuutilia mashaka. Petro anataka kuwahakikishia wasomaji kwa

1. Tukio lake la enzi mpya (yaani., kugeuka sura kwa Yesu)
2. Kuutimiza unabii katika maisha, mafundisho, kifo, na ufufuo wa Yesu

Siku mpya imekwisha wadia na itatimilizwa (yaani., kama taa ing’aavyo, kama nyota ya asubuhi izukavyo). Angalia F. F. Bruce, *answers to Questions*, p. 130.

◙ **"kama taa ing’aavyo mahali pa giza"** Hili ni dokezo kwa Zab. 119:105 na yumkini Mith. 6:23. Mungu amekwisha toa kwa mwanadamu aliyeanguka habari nzima wanazozihitaji ili kujongea kwake kwa imani (yaani., ufunuo, uvuvio, na nuru). Ufunuo binafsi wa Mungu kupitia Agano la Kale na moja kwa moja kupitia kwa Kristo, ambao umeandikwa na kuelezewa na wandishi wa Agano Jipya, limetoshereza kikamilifu (ingawa sio kwa ukamilifu). Ufunuo huu (Agano la Kale na Agano Jipya) ni kama taa ing’aayo gizani mwa mwanadamu na dhambi za kimalaika na uasi. Lakini siku moja kwa uzuri

zaidi nuru ing'aayo (yaani., uso kwa uso tukikabiliana na Yesu) itaangazia kila moyo na fikra za mwamini. Lengo la ufunuo sio habari, bali ni wokovu (yaani., uliorejeshwa, ushirika wa ndani).
Walimu wa uongo walidai kuwa na mafuno maalum toka kwa mungu toka kwa Mungu, lakini Petro anathibitisha kuwa Yesu ni Mungu kamili na ufunuo kamili binafsi.

◙ **"nyota ya asubuhi"** Kwa maana iliyo wazi ni "mtoa nuru" au "nyota ya adhuhuri" (kama vile Ufu. 2:28; 22:16). Kutokana na neno hili la Kiyunani tunapata neno la Kiingereza "fosforasi." Dhana hii ya kung'aa kwa nuru ina madokezo mbalimbali ya Agano la Kale.

1. Inahusiana na neno la Kiebrania *helel*, lenye kutafasiriwa "nyota ya asubuhi" (Ibilisi katika Kilatini, kama vile Isa. 14:12), mara nyingi likirejelea sayari ya zuhura.
2. Inahusiana na ujio wa Masihi katika Hes. 24:17 (yaani., "nyota itatokea katika Yakobo") na Mal.4:2 (yaani., "jua la haki litawazukia").
3. Inahusiana na kufufuka tena kwa watakatifu katika Dan. 12:3 (yaani., "watang'aa kama mwangaza wa anga").
4. Inahusiana na kufanyika mwili kwa Masihi katika Ufu. 22:16 (yaani., "uzao wa Daudi ile nyota ing'aayo asubuhi").

◙ **"kuzuka mioyoni mwenu"** Katika muktadha hili linarejelea kwenye mkabiliano wenye kuhusu maisha na Mungu ulioletwa kwa maono yake binafsi katika maandiko (Agano la Kale), Yesu (kufanyika mwili), na maandiko ya Kitume (Agano Jipya). Kwa kiasi Fulani mwanadamu aliyeanguka ana muda wa kuelewa. Ukweli wa Mungu hugawanyika ndani ya akili zetu. Mchakato huu wa uelewa na imani huongozwa na Roho Mtakatifu (kama vile Yohana 6:44,65).
Ukristo huanza kama mpambano binafsi na mwitikio wa imani kwa Mungu kupitia Kristo. Hutoka katika tukio la pamoja la upendo wa family na huduma ya familia (kama vile 1 Kor. 12:7). Angalia MADA MAALUM: MOYO katika marko 2:6.

**1:20 "maandiko"** Hii ni moja ya aya mbalimbali katika Agano Jipya ambayo huzungumza kuhusu ufunuo binafsi wa Mungu katika mafundisho ya Agano la Kale na Agano Jipya (yaani., maandiko).

1. Mathayo 5:17-19
2. 1 Wagalatia 2:9-13
3. 1 Wathesalonike 2:13
4. 2 Timotheo 3:16
5. 1 Petro 1:23-25
6. 2 Petro 1:20-21
7. 2 Petro 3:15-16

Kiini cha haya yote ni kuwa maandiko yanatoka kwa Mungu na ni ya Mungu, na sio binadamu kiuasilia. Mungu aliwavuvia waandishi (kama vile 2 Pet. 1:20-21) na maandiko yao (kama vile 2 Tim. 3:16).

◙ **"upatao kutafasiliwa kama mtu apendavyo"** Kifungu hiki hakika kinaelezea mvutano uliopo uliosababishwa na walimu wa uongo katika kanisa. Yawezekana kuwa walikuwa wakinukuu maandiko na baadaye kuweka mambo yao wenyewe (ambapo ni kitu cha kawaida siku hizi).
Katika muktadha ni vigumu kuelewa ikiwa kifungu hiki kinarejelea (1) wandishi wa Agano la Kale au (2) walimu wa uongo wa sasa. Ikiwa uchaguzi wa kwanza, unazungumza uvuvio wa dhana ya kithiolojia (kama vile 2 Tim. 3:16). Mstari unaofuata unathibitisha huu utafasiri. Kama chaguo la pili, unazungumzo nuru ya dhana ya thiolojia (yaani., kuwa Roho humwongoza mwamini katika utafasiri wa Biblia).
Lazima ifahamike kuwa dhana ya kiunjilisti ya "ukuhani wa mwamini" mara nyingi inafahamika kama uwezo wa Roho uliopewa kuitafasiri Biblia kwa ajili ya mtu binafsi. Hata hivyo, Kibiblia, kifungu kinarejelea kwenye kanisa kama mwakilishi wa kulikamilisha agizo kuu, kama vile 1 Pet. 2:5,9; Ufu. 1:6. Angalia katika Agano la Kale (kama vile. 19:6) na kifungu cha Agano Jipya "ukuhani wa mwamini" ni wingi (yaani., ya wote), sio mtu binafsi.

**1:21 "wakiongozwa na Roho Mtakatifu"** Hili kwa maana iliyo wazi ni "wakiongozwa," ambalo ni kauli tendwa ya hali ya kuendelea ya wakati uliopo. Hili linaongeza msisitizo kwenye ukweli kuwa Biblia ni ujumbe wa Mungu, na sio ujumbe wa mwanadamu! Ni kweli kwamba Biblia iko katika maneno ya mwanadamu,lakini mwanadamu alikuwa akiongozwa na roho. Biblia sio ukweli mpana kwa vile hakuna mwanadamu aweze kuelewa kwenye kiwango cha ukweli, bali ni kuaminika kwake, ukweli tosherevu kuhusu Mungu, kuhusu dhambi, kuhusu wokovu, kuhusu maisha ya kiungu, na kuhusu maisha ya milele..

Usahihi wa namna ya uvuvio unatofautiana.

1. udhihirisho wa Mungu katika mwili
2. Urxdim na Thummin/lots
3. Ndoto
4. Maono
5. Kuzimia
6. Malaika
7. Matendo ya kiishara
8. Matukio maalum na utafasiri

Swali linabaki kuwa (1) je Mungu hutoa dhima na mwanadamu hutunga muundo au (2) je Mungu huyafanya hayo yote?

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyeweza Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Mjadala huu wa maswali unawekwa ili kukusaidia wewe kufikiri maana ya chapisho kupitia sehemu ya kitabu. Wanamaanisha kuchochea sio kumalizia.

1. Je maisha ya Mkristo kimsingi ni wajibu wa Mungu au wetu?
2. Ni sehemu ipi wanadamu tulio nayo kwenye mahusiano na Mungu?
3. Je maisha ya Mkristo yanaweza kutenganishwa toka kwenye wokovu?
4. Je wokovu ni lazima?
5. Ni wapi walimu wa uongo ambao Petro alikuwa akikabiliana nao katika waraka huu?
6. Ni upi umuhimu wa maneno ya Baba katika 2 Pet. 1:19?
7. Ni kipi mistari ya 20-21 inakizungumzia kuhusu Biblia?

# 2 PETRO 2

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Walimu na Manabii Wa Uongo | Mafundisho ya Uharibifu | Mashambulizi juu ya walimu wa Uongo | Walimu wa Uongo | Walimu wa Uongo |
| 2:1-3 | 2:1-3 | 2:1-3 | 2:1-3 | 2:1-3 |
| | Hatima ya walimu Wa Uongo | | | Mafundisho ya nyuma |
| 2:4-10a | 2:4-11 | 2:4-10 | 2:4-10 | 2:4-10a |
| | | | | Adhabu Ijayo |
| 2:10b-16 | Mapotofu ya walimu Wa Uongo 2:12-17 | 2:10b-16 | 2:10b-16 | 2:10b-12 |
| | | | | 2:13-16 |
| 2:17-22 | Udanganyifu wa walimu Wa Uongo 2:18-22 | 2:17-22 | 2:17-22 | 2:17-22 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka "Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano ha pojuu.
Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA NDANI YA 2 PETRO 2:1-22

A. Kipengere hiki kinafanana na kitabu cha Yuda. Pamekuwepo na uazimaji maneno kifasihi, lakini haijulikani nani kaazima toka kwa nani. Yawezekana Yuda anadokeza kwenye unabii wa Petro kwa sababu baada ya kifo chake, imekuja kuwa kweli (NET Bible).

B. Hawa walimu wa uongo wameonekana kuwa na mtazamo kwamba Wakristo wanafunikwa na neema badala ya kufuata sheria, wenye ujuzi wa mwanzo wakiwa na elimu endelevu juu ya Malaika (ambao waweza kuaksi ushawishi wa Uajemi; kama vile 1 Tim. 6:3-5). Habari zote za Agano la Kale zilizotajwa zinahusiana na malaika kwa namna fulani.

C. Petro alivutwa toka kwenye maarifa ya kawaida katika siku zake (habari za Agano la Kale; I Enoch; vyanzo vya kipagani).

D. Biblia ni yenye utata kama ilivyo ya mwanzo, anguko na shughuli za ulimwengu wa kimalaika. Biblia imejaa utata tokea mwanzo wake, anguko na shughuli za ulimwengu wa kimalaika. Usiruhusu udadisi wako kwenda mbali zaidi ya habari uliopewa na Mungu (kama vile., tamthilia za kisasa).

E. Kuna orodha ya tabia za walimu wa uongo
   1. Kuingiza werevu wa kupoteza kwa siri (2 Pet. 2:1)
   2. Kumkana Bwana (2 Pet. 2:1)
   3. Kufuata ufisadi (2 Pet. 2:2)
   4. Wenye tamaa (2 Pet. 2:3)
   5. Wanaodharau mamlaka (2 Pet. 2:10)
   6. Waenendao kama wanyama (2 Pet. 2:12)
   7. Wapendao starehe (2 Pet. 2:13)
   8. wapotoshao karamu za upendo za Wakristo (2 Pet. 2:13)
   9. wawasababishao waaminio dhaifu kutenda dhambi (2 Pet. 2:14)
   10. Uhuru upao tumainilakini ni watumwa (2 Pet. 2:19).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 PETRO 2:1-3**
**[1] Lakini kuliondokea manabii wa uongo katika wale watu, kama vile kwenu kutakavyokuwako waalimu wa uongo, watakaoingiza kwa werevu uzushi wa kupoteza, wakimkana hata Bwana aliyewanunua, wakijiletea uharibifu usiokawia. [2] Na wengi watafuata ufisadi wao; na kwa hao njia ya kweli itatukanwa. [3] Na katika kutamani watajipatia faida kwenu kwa maneno yaliyotungwa; ambao hukumu yao tangu zamani haikawii, wala uvunjifu wao hausinzii.**

**2:1 "manabii wa uongo"** manabii wa kweli wanaongelewa katika 2 Pet. 1:19-21. Agano la Kale linawataja manabii wa uongo mara nyingi (kama vile Kumb. 13:1-5, 18:19-22; 1 Fal. 18:19, 22:6ff; Yer. 5:3, 23:9-18), kama lifanyavyo Agano Jipya (kama vile Mt. 7:15; 24:11,24; Marko 13:22; Luka 6:26; Mdo. 13:6; 2 Pet. 2:1; 1 Yohana 4:1; Ufu. 16:13; 19:20; 20:10). Angalia MADA MAALUM: UASI *(APHISTĒMI)* katika 2 Peter 1:10.

◙ **"katika wale watu"** Hili linarejelea watu wa Mungu wa Agano la Kale. Tambua ufanano kati ya vishazi viwili vya mwanzo ("miongoni mwa"). Tambua manabii hutokana na watu wa Mungu, na sio kutokana na watu wa nje.

◙ **"walimu wa uongo"** Ushahidi katika 2 Petro 2 inaonyesha kuwa hawa walikuwa ni wale wenye ujuzi wa mwanzo. Angalia Mada Maalum: Wenye Ujuzi katika 1 Pet. 3:22.

◙ **"watakaoingiza kwa werevu"** Neno ambatani la *para* na *eisagō* lina kidokezo cha "walioingizwa kwa siri" (kama vile Gal. 2:4 na Yuda mstari wa 4).

◙ **"uzushi wa kupoteza"** Neno "uzushi" (magawanyiko) linatumika katika namna tatu kwenye Agano Jipya.
   1. Kama kundi la kidini (kama vile Mdo. 24:14; 26:5)
   2. Kama migawanyiko ndani ya Wakristo (kama vile 1 Kor. 11:19)
   3. Kama mafundisho ambayo ni tofauti imani halisi

Mara nyingi ni mchanganyiko wa ukweli na uongo. Mara kadhaa, wanakuza baadhi ya kweli ili kuondoa kweli zingine za Biblia au upotoshaji unaohusiana na maisha ya Yesu. Uzushi mara nyingi hutoka ndani ya jamii ya Kikristo (kama vile Mt. 7:15-23, 24:24; 1 Tim. 4:1-5; 1 Yohana 2:18-25). Maelezo juu ya matendo yao yaweza kuonekana katika (1) Tambuzi za Muktadha E. na (2) Gal. 5:19.

◙ **"hata Bwana waliyemnunua"** Hii ni kauli ya kati (shahidi) yenye hali ya kuendelea, ambayo inazungumzia mwendelezo binafsi wa walimu wa uongo kumkataa Kristo. Hili linarejelea huenda kumkana Kristo (1) kwa thiolojia au (2) mfumo wa maisha (kama vile Yuda 4). Hiki ni kifungu cha kwanza kati ya vile vinne venye maelezo (2 Pet. 2:1-3) kuhusu waalimu wa uongo kumkana Bwana kwa
   1. Kwa matendo na imani zao
   2. Kwa njia zao zisizosawa
   3. Ulafi wao
   4. Uongo wao

Jina "bwana" ni neno *despotēs*, lenye kumaanisha "bwana" au "bwana." Linatumika kwenye wamiliki wa watumwa (kama vile 1Tim. 6:1,2; Tito 2:9; 1 Pet. 2:18).
Inafurahisha kutambua kuwa neno "bwana" mara nyingi hutumika kwa ajili ya Mungu Baba (kama vilke Luka 2:29; Mdo.4:24 [wakinukuu tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania ya Kut. 20:11 au Zab. 146:6]). Hata hivyo, pia linatumika kumhusu Kristo (kama vile 2 Tim. 2:21; Yuda 4; Ufu. 6:10). Hili ni jina jingine la Baba kuuhamisha Uungu wake kwa Mwana.

◙ **"wakajiletea"** Hii ni kauli tendaji ya hali ya kuendelea ya wakati uliopita usiotimilifu. Hili linaonekana, kama 2 Pet. 2:20-22, kumaanisha kuwa, walikwisha okolewa, lakini sio sasa! Hili ni rejeo kwa (1) YHWH akiwaokoa watu wake katika Agano la Kale au (2) kazi ya ukombozi ya Kristo katika Agano Jipya (kama vile Marko 10:45; Mdo. 20:28; 1 Kor. 6:20; Efe. 1:7; 1 Tim. 2:6; Ebr. 2:9;1 Pet. 1:19; 1 Yohana 2:2; Ufu. 5:9). Katika Agano la Kale kumrejesha mtu toka utumwani (yaani., kumkomboa au kulipa fidia) kunarejelea ukombozi wa kimwili. Mara nyingi katika Agano Jipya linarejea kwenye wokovu. Katika Agano la Kale kumuuza mtu mwingine mkononi mwa adui kunarejelea hukumu.
Toleo la NJB lina tafasiri ya kufurahisha. "Aliyewaletea uhuru." Inavyoonekana wanauangalia muktadha (2 Pet. 2:2-3) kama wenye kuhusiana na waamini wenye kuishi maisha ya kiungu na kuleta aibu juu ya Kristo na Ukristo. Baadaye lingelirejelea kwa waamini waliokufa mapema kwa sababu ya maisha yao ya kiungu na ushawishi wenye uharibifu.

◙ **"wakijiletea uharibifu juu yao"** Hakuna mwamini wa karne ya kwanza angaliweza kuuliza swali hili, lakini waamini wa sasa wanalifikiri sana, hasa namna wanavyohakikishiwa na mitazamo ya makundi yao! Baadhi wanakioanisha kifungu kwa “YHWH" au "watu," ambao baadaye ungalirejea kwenda uhamishoni (yaani., kipindi cha kutangatanga jangwani).
Swali la msingi ni kuwa, "kweli wazushi wataokolewa?" naamini kuwa mafundisho ya Biblia hutolewa kilahaja au kimafumbo, ambao ni uainishaji wa fasihi za Kimashariki. Wasomaji wa sasa wa Magharibi na watafasiri wanajaribu kuwiainisha na kuondoa kwenye muktadha mistari. Inatuhakikishia ulinzi wa mwamini, lakini najisikia kutokuwa sawa na kifungu "ukiokolewa, unaokolewa jumla" kwa sababu kifungu kama hiki.
Ulinzi unathibitishiwa kwa (hauegamii juu) maisha ya kiungu (kama vile Yakobo na 1 Yohana). Waamini wanajitahidi na wanatenda dhambi, lakini wanaendelea kuamini katika Kristo na kuitika (wakati mwingine taratibu) kwenye marejeo ya Roho Mtakatifu.
Hata hivyo, mfano wa udongo (kama vile Mathayo 13) na wanadai ni watendaji, lakini waliopotea, wa Mt. 7:15-27, wananithibitishia kuwa zipo kazi za uongo za imani (kama vile 2 Pet. 2:20-22; 1 Yohana 2:18-19).
Waalimu wa uongo wamesababisha na wanaendelea kusababisha machafuko makubwa kanisani. Katika kitabu cha 1 Yohana kuna majaribu mengi kwa ajili ya mwamini wa kweli

1. Utayari wa kuzikiri dhambi (1 Yohana 1:5; 2:22)
2. Kutii namna ya kuenenda (1 Yohana 2:3-6)
3. Upendo kwenye mfumo wa maisha (1 Yohana 2:7-11)
4. Ushindi dhidi ya maovu (1 Yohana 2:12-14)
5. Kuusamehe ulimwengu (1Yohana 2:15-17)
6. saburi (1 Yoahana 2:19)
7. mafundisho (1 Yohana 2:20-24)

Petro pia aliorodhesha matendo ya hovyo ya hawa waalimu wa uongo (angalia Tambuzi za Kimuktadha, E). kama ni kweli kuwa injili ni (1) nafsi; (2) ujumbe kumhusu mtu; na (3) mfumo wa maisha uelezao mtu huyo, hivyo hawa waalimu wa uongo wamezivunja zote tatu. Mtu awezakuwa “amenunuliwa" na Yesu na kumkana Yesu? Hili ndilo tatizo. Wakovu ni bure na kwa ajili ya wale wote watakaokubari toba, imani, utii, na saburi. Lakini, ukomavu ni ushirika wenye kugharimu. Lazima tushikamane kwenye kweli zote za Kibiblia. Mafundisho hutokana na jozi ya misukosuko kwa sababu Ukristo sio tu thiolojia ya Kibiblia (kama vile Rum.6), bali ni mapambano ya kila siku (kama vile Warumi 7) kwa ajili ya uchaji wa mungu. Wokovu ni ushirika, na sio maamuzi yenye kujitenga!

**2:2 "Wengi watafuata"** Hatari ya kuwapotosha wengine (kama vile Mt. 18:6-7). Petro anatumia hili neno ambatani mara kadhaa (kama vile 2 Pet. 1:16; 2:2,15,21; Mt. 18:6).

**NASB** **"ufisadi wao"**
**NKJV** **"njia zao za uharibifu"**

**NRSV "njia zao za uovu"**
**TEV "njia zao mbaya"**
**NJB "tabia zao mbaya**

Neno *aselgeia* laweza kutafasiriwa kama "uharibifu," "potofu," au "fisadi," ikimaanisha kutokuwa na kiasi kwenye tamaa za mwili (kama vile 2 Pet. 2:2,7,18; 1 Pet. 4:3; Yuda 4). Mara kadhaa limejumuishwa kwenye orodha ya dhambi za jamii za wapagani (kama vile Rum. 13:13; 1 Kor. 12:21; Gal. 5:19).

◙ **"kwa hao njia ya kweli itatukanwa"** Ni muhimu kujua namna waamini waishivyo. Wanapaswa kuaksi tabia ya familia ya Mungu (yaani., imani katika Kristo inarejesha taswira ya Mungu ndani ya mwanadamu, kama vile 1 Tim.6:1; Tito 2:5).

◙ **"njia ya kweli"** Neno "njia" lilikuwa jina la mwanzo lililotumiwa kwa ajili ya Wakristo (kama vile Mdo. 9:2; 18:25-26; 19:9,23;22:4; 24:14,22). Linaaksi dhana ya imani ya Kibiblia ya Agano la Kale kama njia safi itupasayo kuifuata (kama vile Zab. 119:105; Mith. 6:23). Kifungu hiki kinarejelea kwenye ujumbe wa injili. Dhahili maisha ya kiungu ni dhana muhimu ya wokovu (Eph. 1:4; 2:10).

◙ **"itatukanwa"** Wapagani waliwapotosha waamini na kuwashutumu kwa matendo yao yasiyo ya kiadilifu. Maisha ya walimu wa uongo yaliongeza huu upotoshaji.

**2:3 "katika kutamani kwao"** Neno hili lina dokezo lililo kinyume kote katika tafasiri ya maandiko ya Kiebrania na Agano la Kale. Walimu wa uongo wanaainishwa kwa kuwa na tamaa nyingi kwa gharama yoyote ile (kama vile 2 Pet. 2:14; Mika 3:11; 1 Tim. 6:5; Tito 1:11; Yuda 16). Hili neno mara kadhaa limetumika katika Agano Jipya (kama vile Marko 7:22; Luka 12:15; Rum. 1:29; 2 Kor. 9:5; Efe. 5:3; Kol. 3:5; 1 The. 2:5; 2 Pet. 2:3,14) kwa sababu inaainisha asili ya ubinafsi wa mwanadamu aliyeanguka. Hili laweza kurejea kwenye tamaa ya fedha, tamaa ya mapenzi, au mahali pa heshima (yaani., walimu) ndani ya makanisa.

◙ **"watajipatia faida"** Toleo la King James lina "kujipatia faida." Tunapata neno la Kiingereza "gulio" toka kwenye neno la Kiyunani.

**NASB "kwa maneno ya uongo"**
**NKJV, NRSV "maneno ya udanganyifu"**
**NJB "hadithi zisizo za kweli"**

Kivumishi kinaonyesha kile kilichofinyangwa au kutengenezwa (kama vile Rum. 9:20). Tunapata neno la Kiingereza "plastiki" toka kwenye neno la Kiyunani. Waalimu wa uongo wamesababisha matatizo ndani ya watu waaminio na katika jamii.maisha yao yameleta aibu kwenye injili na kuupindisha ujumbe wa injili.

◙ **"hukumu yao"** Mara zote pamekuwepo na waalimu wa uongo kati ya watu wa Mungu. Wamelaumiwa katika Agano la Kale (kama vile Kumb. 13:1-5,6-11,12-18). Hukumu yao ya duniani, siku ya mwisho ipo na wala haichelewi (kama vile Gal. 6:7). Katika andiko hili vyote "hukumu" na "maangamizi" ipo. Hii ni kanuni ya kiroho. Mungu ni mwadilifu na vile vile uumbaji wake. Wanadamu hujiondoa wenyewe juu ya viwango vya Mungu. Tunavuna kile tulichopanda. Hili ni kweli kwa waamini (lakini haliathiri wokovu) na wasio amini (kama vile Ayubu 34:11; Zab. 28:4; 62:12; Mith. 24:12; Wimb. 12:14; Yer. 17:10; 32:19; Mt. 16:27; 25:31-46; Rum. 2:6; 14:12; 1 Kor. 3:8; Gal. 6:7-10; 2 Tim. 4:14; 1 Pet. 1:17; Ufu. 2:23; 20:12; 22:12).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 PETRO 2:4-10a**
**4 Kwa maana ikiwa Mungu hakuwaachilia malaika waliokosa, bali aliwatupa shimoni, akawatia katika vifungo vya giza, walindwe hata ije hukumu; 5 wala hakuuachilia ulimwengu wa kale, bali alimhifadhi Nuhu, mjumbe wa haki, na watu wengine saba, hapo alipoleta Gharika juu ya ulimwengu wa wasiomcha Mungu; 6 tena akaihukumu miji ya Sodoma na Gomora, akiipindua na kuifanya majivu, akaifanya iwe ishara kwa watu watakaokuwa hawamchi Mungu baada ya haya; 7 akamwokoa Lutu, yule mwenye haki aliyehuzunishwa sana na mwenendo wa ufisadi wa**

**hao wahalifu; [8] maana mtu huyu mwenye haki akikaa kati yao, kwa kuona na kusikia, alijitesa roho yake yenye haki, siku baada ya siku, kwa matendo yao yasiyo na sheria; [9] basi, Bwana ajua kuwaokoa watauwa na majaribu, na kuwaweka wasio haki katika hali ya adhabu hata siku ya hukumu; [10] na hasa wale waufuatao mwili katika tamaa ya mambo machafu. na kudharau mamlaka.**

**2:4 "ikiwa"** Hii ni sentensi yenye masharti daraja la kwanza ambayo mara nyingi inafikiriwa kuwa kweli kutokana na matazamo wa mwandishi au kwa ajili ya kusudi lake kifasihi. Hili hurefusha sentensi hata kwenda mpaka 10a. inawezekana kuwa hiki kiengere chenye masharti kinapaswa kurudiwa kwenye hii sentensi ndefu ya Kiyunani. Toleo la NRSV lina neno "ikiwa" katika 2 Pet. 2:4,5,6,7; toleo la NIV lina neno "ikiwa" katika 2 Pet. 2:4,5,6,7,9, lakini linajitokeza tu katika andiko la Kiyunani kwenye 2 Pet.2:4. Huu muktadha huelezea mfuatano wa hukumu za Agano la Kale wakijumuishwa na malaika.

◙ **"malaika waliokosa"** Hili linafanana na lile la Yuda 6. Zifuatazo ni hoja toka kwenye fasiri yangu kwenye Yuda na Yakobo (Vol. 11).

---

**Hoja Zangu Toka Fasiri Ya Yuda**

**Yuda 6 "Na malaika wasioilinda enzi yao wenyewe, lakini wakayaacha makao yao yaliyowahusu, amewaweka katika vifungo vya milele chini ya giza kwa hukumu ya siku ile kuu"** Sodoma na Gomora, kwa namna ile ile kama walivyo hawa malaika, hujiingiza kwenye uchafu usiofaa na kuwaendea walio wageni. Yote huonyeshwa kama mfano kuiendea ile hukumu ya moto wa milele.

**Yuda 6 "na malaika"** Mstari huu unaongeza malaika kwenye orodha yake kwa wale wote mwanzoni walimwabudu na baadaye wakaasi dhidi ya YHWH na hivyo wakaangamiza au kuhukumiwa. Lakini malaika wapi? Baadhi ya taarifa hutolewa kuelezea kundi hili la malaika:

1. Hawakutunza enzi yao
2. Wakayaacha makao yao
3. Watawekwa katika vifungo vya milele chini ya giza kwa ajili ya hukumu ile iliyo kuu
4. "wametenda dhambi" (2 Pet. 2:4)
5. "wamejiingiza kwa siri *Tartarus*" (2 Pet. 2:4)
6. "wameingizwa kwenye shimo la giza lililotunzwa kwa ajili ya hukumu" (2 Pet. 2:4)

Ni malaika wapi walioasi na kutenda dhambi?

1. Malaika ni nguvu nyuma ya ibada za kipagani
2. viumbe vya malaika wadogo, wakiitwa haswa kwa majina ya kihayawani katika Agano la Kale. Mfano: Lilith (kama vile Isa.34:14), Azazel (kama vile Law. 16:8), na majini (kama vile Law. 17:7)
3. "wana wa Mungu" katika Mwa. 6 (mara nyingi likijadiliwa katika maandiko ya siku za mwisho kipindi cha utulivu, I Enoch 86-88; 106; II Enoch 7,18; II Baruch 56; Jubilees 5)
4. Malaika waliotajwa ni wa kimfano toka maandiko ya Kiyahudi ya siku za mwisho kipindi cha utulivu (kwa sababu ya utumiaji wa Yuda wa vitabu vingine vya aina hii katika Yuda 9, 14)

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"ambao hawakuitunza enzi yao"** |
| **NKJV** | **"ambao hawakuitunza enzi yao vizuri"** |
| **NRSV** | **"ambao hawakuitunza nafasi yao"** |
| **TEV** | **"ambao hawakubaki ndani ya mipaka yao ya mamlaka sahihi"** |
| **NJB** | **"ambao hawakutunza mamlaka waliokuwa nayo"** |

Kuna mchezo wa maneno kwenye njeo ya kitenzi "kutunza" katika 2 Pet. 2:6. Malaika hawakuzitunza nafasi zao (ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopita usiotimilifu) kwa hiyo Mungu amewatunza kifungoni mpaka ije ile siku ya mwisho (kauli tendaji timilifu elekezi). Wale malaika waliokwenda kinyume na mapenzi ya Mungu wamekwisha pata hukumu yao

ya duniani na siku ile ya mwisho, kama walivyoasi Waisraeli kipindi cha kutangatanga jangwani na kuharibiwa kwa Sodoma na Gomora.
Neno "enzi" ni neno la Kiyunani *arch*ē, lenye kumaanisha "mwanzo" au "asili" ya kitu.

1. Mwanzo wa utaratibu wa uumbaji (kama vile Yohana 1:1; 1 Yohana 1:1)
2. Mwanzo wa injili (kama vile Marko 1:1; Fil. 4:15)
3. Shuhuda wa macho wa mwanzo (kama vile Luka 1:2)
4. Mwanzo wa ishara (miujiza, kama vile Yohana 2:11)
5. Kuanzisha kanuni (kama vile Ebr. 5:12)
6. Mwanzo wa uhakika (kama vile Ebr. 3:14)

lilikuja kutumika kwenye "utawala" au "mamlaka"

1. Kwa maafisa wa serikali
   a. Luka 12:11
   b. Luka 20:20
   c. Warumi13:3; Tito 3:1
2. Mamlaka ya kimalaika
   a. Warumi 8:38
   b. 1 Kor. 15:24
   c. Efe. 1:21; 3:10; 6:10
   d. Kol. 1:16; 2:10,15

Hawa waalimu wa uongo walidharau mamlaka yote, ya kidunia na ya kimbingu. Walikuwa ni watu huru wa kidini wanaoamini juu ya neema na kutofuata sheria. Walijitanguliza na kuziweka shauku zao mbele kuliko Mungu, malaika, mamlaka ya kijamii, na viongozi wa kanisa.

**NASB** **"bali waliacha majukumu yao yaliyowahusu"**
**NKJV** **"bali waliacha makazi yao"**
**NRSV** **"bali waliacha makazi yao sahihi"**
**TEV** **"bali waliacha makazi waishiyo"**
**NJB** **"bali walitelekeza maeneo waliyopewa"**

Malaika hawa waliacha maeneo yao wakaenda pengine (duniani). Hii inashabiana na tafsiri ya Mwanzo 6:1-4 kisawia kabisa. Hiki kilikuwa ni kitendo cha kukataa mapenzi ya Mungu na mamlaka yake kwa hiari.

◙**"katika vifungo vya milele"** Minyororo inatumika juu ya malaika I Enoch na shetani amefungwa "kwa mnyororo mkubwa" katika Ufu. 20:1-2. Neno"milele" inaweza kumaanisha "kwa nguvu," "vya kutosheleza," "uhakika," sio ubayana wa milelel, kwasababu malaika hawa wanashikiliwa tu wakingoja siku ya hukumu, wakati namna zingine za matezo zitakapotumika (kama vile Ufu. 20:10,14-15). Suala ni baadhi ya malaika wako gerezani sasa ili kuweza kuthibiti shughuli zao.

◙**"chini gizani"** Neno *Tartarus* (halitumiki katika Yuda bali lipo katika 2 Pet. 2:4 na I Enoch 20:2) lilitumika katika hadithi za kishujaa za Kiyahudi kwa ajili ya kushikilia majitu ya vita ambayo yalikuwa nusu binadamu na nusu yenye nguvu mithili ya nguvu ya Mungu. Hii inashabihiana na fasiri ya kimalaika ya Mwanzo 6. I Enoch inaelezea makazi mapya ya malaika hawa waasi (kama vile. I Enoch 10:5,12) kama giza la milele. Namna ilivyo tofauti na mg'ao wa kimbingu (utukufu). Walimu wa Uyahudi waligawa *Sheol* katika"Paradiso" (kwa ajili ya wenye haki) na *Tartarus* (kwa wabaya). Neno "kuzimu" (kama vile Luka 8:3, Rev. 9:1; 11:7; 20:3) ni sawasawa na sitiari za giza zitumikazo katika mstari 13b.

◙**"Siku kuu"** Hii ni namna nyingine ya kurejerea Siku ya Hukumu, siku ambayo Mungu atahoji uwajibikaji na hesabu ya kipawa cha uzima juu ya uumbaji wote (kama vile Flp. 2:10-11; Isa. 45:23; Rum. 14:10-12).

## MADA MAALUM: "wana wa Mungu" katika Mwanzo 6

A. Kuna mkanganyiko mkubwa juu ya utambuzi wa kifungu "wana wa Mungu." Pamekuwepo na tafasiri tatu kuu
   1. Kifungu kinarejea juu ya uzao wa ki-Mungu wa Sethi (kama vile Mwanzo 5, soma maelezo kwenye 4:14

2. Kifungu kinarejea juu ya kikundi cha viumbe wa kimalaika
3. Kifungu kinarejea juu ya wafalme, wadhalimu au uzao wa Kaini (kama vile Mwanzo 4)

B. Ushahidi kwa ajili ya kifungu hiki unarejea juu ya uzao wa Sethi
1. Muktadha wa haraka wa fasihi wa Mwanzo 4 na 5 unaonyesha maendeleo ya uzao wa uasi wa Kaini na uzao wa Sethi uliochaguliwa. Kwa hiyo, ushahidi wa kimuktadha unaonekana kuupendelea uzao wa ki-Mungu wa Sethi
2. Walimu wa dini ya Kiyahudi wamekuwa wakitofautiana juu ya uelewa wa kifungu hiki. Baadhi wanadai kuwa kinamrejelea Sethi (lakini wengi wanadai malaika)
3. Kifungu cha umoja "wana wa Mungu," ingawa mara nyingi kinatumika kwa viumbe vya kimalaika, mara chache kinarejelea wanadamu.
   a. Kumb. 14:1 – "wana wa YHWH Mungu wako"
   b. Kumb. 32:5 – "Wana wake"
   c. Kut. 22:8-9; 21:6 (yumkini mwamuzi wa Kilawi)
   d. Zaburi 73:15 – "wana wenu"
   e. Hosea 1:10 – "wana wa Mungu aliye hai"

C. Ushahidi wa kifungu unaorejelea viumbe vya kimalaika
1. Huu umekuwa ni uelewa wa kawaida wa kimapokeao wa kifungu hiki. Muktadha mpana wa kitabu cha Mwanzo ungaliunga mkono huu mtizamo kama mfano mwingine wa uovu wa kimiujiza wa kuyazuia mapenzi ya Mungu kwa mwanadamu (walimu wa dini waliyasema haya kwa kinyongo)
2. Wingi wa kifungu(wana wa Mungu) unatumika kwa wingi kabisa katika Agano la Kale kwa ajili ya malaika
   a. Ayubu 1:6
   b. Ayubu 2:1
   c. Ayubu 38:7
   d. Zaburi 29:1
   e. Zaburi 89:6,7
   f. Danieli 89:6
3. Kitabu cha 1 Henoko kipindi kati ya Agano la Kale na Agano Jipya (kama vile I Enoch 6:1-8:4; 12:4-6; 19:1-3; 21:1-10) na Yubileyi (kama vile Ayub 5:1), ambacho kilikuwa kikifahamika kati ya waamini kipindi cha Agano Jipya , kikiwa na *Genesis Apocryphon* toka kwenye magombo ya Bahari ya Chumvi, vinayafasiri haya kama malaika wale walioasi
4. Muktadha wa haraka wa sura ya 6 unaonekana kudokeza kuwa "watu wale wenye nguvu ambao walikuwa ni watu wa kale waliojulikana" walitokana na mchanganyiko huu usio sawa wa utaratibu wa uumbaji.
5. Maandiko ya kale ya Kiyunani yanalitafasiri hili "wana wa Mungu" kama "malaika wa Mungu"
6. 1 Henoko hata anadai kuwa gharika ya Nuhu ilikuwa kuangamiza huu muunganikano wa malaika/mwanadamu ambao haukuwa wa kirafiki dhidi yake na YHWH na mpango wake wa uumbaji (kama vile I Enoch 7:1na kuendelea; 15:1na kuendelea; 86:1na kuendelea)
7. Katika fasihi ya Ugaritic "wana wa Mungu" inarejele kwa washirika wa hekalu la miungu wengi (yaani., wale viumbe wa chini wa kiroho)

D. Ushahidi wa kifungu unarejelea kwa wafalme au wadhalimu wa uzao wa Kaini
1. Kuna tafasiri mbali mbali za kale ambazo zinaunga mkono huu mtizamo
   a. Targum wa Onkelo (karne ya pili B.K) inatafasiri "wana wa Mungu" kama "wana wa watu wenye uwezo"
   b. Symmachus (karne ya pili B.K) tafasiri ya Kiyunani, inaritafasiri "wana wa Mungu" kama "wana wa wafalme"
   c. Neno *"elohim"* linatumika kwa viongozi wa Israel (kama vile Kut. 21:6; 22:8; Zab. 82:1,6), kumbuka Biblia ya NIV na NET
   d. *Nephilim* lililounganishwa na *Gibborim* katika Mwa. 6:4, *Gibborim* ni kutoka *Gibbor* likimaanisha "mwanaume mwenye nguvu jasiri; utajiri au nguvu
   e. Ufasiri huu na ushahidi umechukuliwa toka maneno magumu ya Biblia kur. 106-108.

E. Ushahidi wa kihistoria wa watetezi wa matumizi yote

1. Kifungu kinarejelea kwa Sethi
    a. Cyril of Alexander
    b. Theodoret
    c. Augustine
    d. Jerome
    e. Calvin
    f. Kyle
    g. Gleason Archer
    h. Watts
2. Kifungu kinarejelea kwa viumbe wa kimalaika
    a. Waandishi wa tafasiri ya maandiko ya kale
    b. b. Philo
    c. Josephus (*Antiquities* 1:3:1)
    d. Justin Martyr
    e. Irenaeus
    f. Clement wa Isakanderia
    g. Tertullian
    h. Origen
    i. Luther
    j. Ewald
    k. Delitzsch
    l. Hengstenberg
    m. Olford
    n. Westermann
    o. Wenham
    p. NET Bible

F. Ni kwa namna gani "Manefili" wa Mwanzo 6:4 wanahusiana na "wana wa Mungu" na "binti za wanadamu" wa Mwanzo 6:1-2? Kumbuka hizi nadharia:
1. Wao ni matokeo ya majitu makubwa (kama vile Hesabu 13:33) wa muunganikano kati ya malaika na binadamu wa kike.
2. Havihusiani kabisa. Vimetajwa tu kama viliwahi kuwepo kwenye uso wa dunia kwenye nyakati za matukio ya Mwanzo 6:1-2 na pia baadaye
3. R. K. Harrison in *Introduction to the Old Testament*, uk. 557, ana nukuu yenye kutatiza, "kukoswa moja kwa moja thamani ya utambuzi wa ndani juu ya elimu ya binadamu na maendeleo yake kuelekea kwenye mwingiliano wa mahusiano ya *homo sapiens* na viumbe wa mwanzo waliotokana na Adamu ambamo sura nzima imehusika, na ambayo imekubalika kwa wale wasomi ambao wameweza kuwafatilia." Hili linanijulisha kuwa aliyaona haya makundi mawili kama yenye kuwakilisha makundi tofauti ya tabia za kibinadamu. Hili lingalidokeza uumbaji maalum wa baadae wa Adamu na Hawa, lakini pia maendeleo ya kimabadiliko ya viumbe *Homo erectus*

G. Ni haki kuweka wazi uelewa wangu wa mkanganyiko wa andiko hili. Kwanza, ngoja tukumbushane sisi sote kuwa andiko kwenye Mwanzo ni fupi na ni gumu. Msikiaji wa mwanzo ambaye ni Musa alikuwa amekwisha kuwa na utambuzi wa ndani zaidi wa kihistoria au Musa alitumia utaribu wa simulizi au kuandikwa toka kipindi cha utawala wa kiume kwamba yeye mwenyewe hakuelewa kwa ukamilifu. Hili suala sio mada muhimu ya kithiolojia. Mara nyingi tunakuwa wadadisi kuhusu vitu ambavyo maandiko yanavigusia lakini ni vigumu kueleweka. Itakuwa bahati mbaya kufanya thiolojia kiundani nje ya hili na sehemu zenye kufanana za habari ya kibiblia. Kama tungetaka habari hizi Mungu angaliweza kuzitoa kwa uwazi na ukamilifu. Mimi pekee naamini walikuwa malaika na wanadamu kwa sababu:
1. Ni mwendelezo, ingawa haikukatazwa, kukitumia kifungu "wana wa Mungu" kwa ajili ya malaika katika Agano la Kale
2. Mtafasiri wa maandiko ya kale ya Kiebrania (Iskanderia) analitafasiri (karne ya kwanza K.K) "wana wa Mungu" kama "malaika wa Mungu"
3. Kitabu cha maandiko ya uongo chenye matukio ya mwisho cha 1Henoko (yumkini yaliandikwa miaka ya 200 K.K) ni halisia kuwa yanarejelea kwa malaika (kama vile sura ya 6-7)
4. Kithiolojia inaunganisha na 2 Petro 2 na Yuda juu ya malaika waliotenda dhambi na hawakutunza mazingira yao vizuri, ninajua kuwa kwa kiasi Fulani hili linaleta mkanganyiko kwa Mathayo 22:30, lakini hawa malaika maalum hawako mbinguni wala duniani bali wako katika gereza maalum(Tartarus)
5. Nafikiria kuwa sababu mojawapo ya matukio mengi ya Mwanzo 1-11 yanapatikana katika tamaduni (yaani., habari za uumbaji wenye kufanana , habari za kufanana za gharika, habari mfanano za malaika kuwachukua malaika) ni kwa sababu wanadamu wote walikuwa pamoja na walikuwa na maarifa juu ya YHWH wakati wa kipindi hiki, lakini baada ya kutawanyika kwenye mnara wa Babel maarifa haya yakapotoshwa na kubadilishwa kwenye imani ya miungu wengi.

Mfano mzuri wa hadithi za kubuniwa zilikuwa ni watu wenye maumbo makubwa nusu wanadamu wenye uwezo mkubwa wa kufikiri yaliyoitwa majitu (titans) yaliyokuwa yamewekwa gerezani kwenye *Tartarus*, hili ni jina lililotumika mara moja kwenye Biblia (kama vile 2 Petro 2) kwa ajili ya sehemu ya kuwaweka malaika wasiotunza vizuri

ukazi wao. Katika thiolojia ya sheria za dini ya Kiyahudi kuzimu kuligawanywa katika sehemu mbili kwa ajili ya watakatifu paliitwa Paradiso na kwa ajili ya waovu paliitwa (*Tartarus*).

NASB, NKJV
**NRSV, TEV**
**NIV** **"kuzimu"**
**NJB** **"shimoni"**
**Weymouth** **"shimoni"**

Angalia dokezo juu katika "chini ya giza" katika dokezo juu ya Yuda 6

---

◙ **"vifungo vya giza"** Hili neno *sirois* linapatikana katika machapisho ya herufi kubwa za Kiyunani ,א ,A, B, na C. Toleo la King James Versionlina neno "vifungo" (*seirais*), ambalo linafanana na maana ya neno "bonds" (*demois*) katika Yuda 6, linapatikana katika machapisho ya mafunjo ya kala P[72], pia linganisha I Enoch 10:12, ).

**2:5 "wala hakuuachilia ulimwengu wa kale"** Kipengele kinairejelea hukumu ya Mungu juu ya udhaifu wa mwanadamu (kama vile Mwa. 6:5,11-12,13; 8:21b). Hii iliyoshuka kwa kutumia maji inaelezwa katika Mwa. 6-9. Tukio kama hili linatajwa katika1 Pet. 3:18-22.

◙ **"Nuhu"** Ni mtu na nyumba yake **"**akapata neema machoni pa Bwana" (yaani, Nuhu, kama vile Mwa. 6:8-9,18). Tukio pia linaelezwa katika Josephus' *Antiquities of the Jews* 1.3.1; I Clement 7.6, 9.4; na Sibylline Oracles 1.128).

◙ **"mjumbe wa haki"** Kitabu cha Agano la Kale hakikuyataja mafundisho yamhusuyo Nuhu, bali utamaduni wa walimu wa Kiyahudi hivyo kwa hakika (kama vile Yubilee 7:20-29; Sibylline Oracles 1.128-129).

◙ **"Gharika"** Hili neno la Kiyunani linatokana na neno la Kiingereza "maafa makubwa." Kulingana na I Enoch, hii hukumu ya Mungu katika kwa wanadamu wa rangi mchanganyiko/mahusiano ya kujamiiana ya kimalaika ya Mwa. 6:1-4.

**2:6 "Sodoma na Gomora"** Maangamizi ya hii miji dharimu yanaelezwa katika Mwa. 19:24-28. Malaika yalikuwa kwa minajiri ya kumwepusha Lutu na nyumba yake na, kwa namna fulani, hawa walihusishwa katika maangamizi ya miji hii kwa uwazi.
Hii ni sawa na Yuda 7. Inaonekana kwamba Nuhu ni nfano wa hukumu kupitia maji na Sodoma na Gomora kama nfano wa hukumu kupitia moto.
Nimejumuisha maelezo yafuatayo toka katika fasiri yangu juu ya Yuda 7

---

**Muhtasari toka Fasiri ya Yuda**

**Yuda 7 "Sodoma na Gomora"** Huu ni mfano wa tatu wa uasi uliohusisha matendo ya kujamiiana kwa jinsia moja nje ya mpango wa Mungu uliokusudiwa kuhusu ndoa:
1. ibada ya ustawi ya Kikanaani huko Shitimu (kam vile Hes. 25)
2. jaribio ala malaika kuuvuruga mpangilio wa uumbaji (kama vile Mwa. 6:1-4; 2 Pet. 2:4)
3. tendo la Sodoma na Gomora kuwa na shauku ya kujamiiana malaika kwa namna ya jinsia moja (kama vile Mwa. 19; 2 Pet. 2:6)

◙ **"na miji iliyokuwa kando-kando,"** Hii miji imeorodheshwa kwa majina yake katika Kumb. 29:23.

◙ **"kwa jinsi moja"** Hiki ni kitenzi chebnye kushtumu ambacho kisarufi kinahusiana na malaika (kama vile Yuda 6), si "niji jirani." Inekuwa ikidhahaniwa kwamba Yuda aliyatumia maelezo haya ya Agano la Kale kwa sababu malaika walijitwalia wanawake katika Mwanzo, vivyo hivyo na hapa watu wanajaribu kujitwalia malaika (kama vile Mwa. 18:22; 19:1). Ikiwa

ni hivyo, huu unaweza kuwa mfano mwingine wa jaribio la kuuvuruga mtiririko wa uuumbaji. Hata hivyo, kwangu mimi inaonekana kwamba wakazi wa Sodoma hawakuwatambua vizuri malaiaka hawa na walifikiri kuwa hawa wangekuwa malaiaka (kama vile Mwa. 18:22).

◙ **"wakaenda kufuata mambo ya mwili yasiyo ya asili,"** Kifungu hiki kiko katika rejea ya kifungu "wakaenda kufuata mambo ya mwili yasiyo ya asili (*heteros*) ." Hiki kinaonekana kuhusiana na wote (1) malaika na wana wake kwa mujibu wa Josephus katika *Antiquities of the Jews* 1:3:1 na (2) kujamiiana kwa jinsia moja (kama vile Rum. 1:26-27) temdo lililokuwa limeenea sana katika eneo la Sodoma.

◙ **"imewekwa kuwa dalili, wakiadhibiwa katika moto wa milele"** Yuda anatumia mifano ya Agano la Kale kama onyo dhahiri kwa wasomaji wake. Jihadharini na unyanyasaji wa kingono na mtu ye yote. Agano Jipya linazungunza wazi juu ya adhabu ya milele (kama vile Mt. 25:41,46; 2 The. 2:8-9;Ufu. 19:20; 20:11,14- 15; 21:28; na pia I Enoch 54:1). Suala hili ni vigumu kulijadili kwa sababu Biblia haitoa ufafanuzi zidi kuhusu mbinguni au jehanamu. Inakubaliana na ukweli wao, lakini haifunui maelezo kwa uyakinikifu, mara nyingi hufunua katika lugha ya kistiari. Yesu anakitumia kifungu "bonde la wana wa Hinomu," eneo ambalo liko kusini mwa Yerusalemu na lilitumiwa na Waisraeli chini ya Manase kwa ajili ya kumwabudu Moleki, mungu wa moto mwenye asili ya Kikanaani aliyehitaji dhabihu za watoto. Wayahudi, mbali na kutubia ushiriki wao katika tambiko hizi za ustawi, walilibadilisha eneo hili na kuwa jalala kwa ajili ya Yerusalemu. Stiari ya Yesu yenye kuzungumzia moto, moshi, na minyoo ilitokana na eneo hili, Gehena.
Hili eneo lenye kuchukiza halikuumbwa kwa ajili ya mwanadamu, bali kwa ajili ya malaika walio asi (kama vile Mt. 25:41). Waovu wa namna zote wataondolewa na kutengwa na uumbaji wa Mungu. Jehanamu ni ni eneo linalotumiwa na Biblia kuelezea mgawanyo wa kudumu.

Kabla siachana na mada hii hebu nieleze maunivu ninayoyasikia kuhusiana na suala hili. Haya ndiyo mateso pekee katika Biblia ambayo si ya kiukombozi. Haya si mapenzi ya Mungu kwa mtu ye yote. Haya ni matokeo ya kuwa wennye hiari, uasi endelevu, kwa namna zote kimalaika na kibinadamu, maumivu yenye kuusababisha moyo wa Mungu kuvuja damu ambapo hkamwe hataweza kuutibu! Mapenzi ya Mungu kuyaruhusu mapenzi huru miongoni mwa viumbe vyake huwa ma matokeo ya maunivu fulani, upotevu wa milele.

Kitabu cha *The Jerome Biblical Commentary*, juzuu l. II, uk. 379 kinataja kwamba maelezo ya Yuda juu ya adhabu za malaiaka hawa zina fanana sana na zile zilizo katika Enoch 10:4-6,11,13; 12:4; 15:3; 19:1. Suala hili linaonekana kuyakinisha ufahamu wa Yuda kuhusiana na kazi hii ya Yuda yenye kuzungumzia kipindi cha utulivu kati ya Agano la Kale na Agano Jipya chenye kuzungumzia matukio ya mwisho

**2:7-8 "Lutu, yule mwenye haki"** Hili linaweza kuwa dokezo la (1) kitabu cha ziada cha sheria za dini ya Kiyahudi ambacho ni Hekima ya Suleimani 10:6 au (2) mapokeo ya sheria za Kiyahudi. Lutu alikuwa akiugua kiroho kutokana na matendo ya watu waovu waliokuwepo wakati huo (baadhi ya mapokeo ya sheria za Kiyahudi yanaaksiwa katika 2 Pet. 2:8 na I Clem. 11:1) kama ilivyo kwa wasomaji wa 2 Petro walikuwa walimu wa uongo wenye mwenendo mbaya.

Hiki kipengele chote ni mfumo wa uanishaji wa Agano la Kale. Mambo yaliyotukia katika historia ya Israeli yalirudiwa katika nyakati za Petro.

**2:9** Hili ni hitimisho la maelezo niliyoyafanyia upanuzi yaliyoanzia katika 2 Pet. 2:4. Mungu atawasalimisha walio wake (yaani, Nuhu, 2 Pet. 2:5 na Lutu, 2 Pet. 2:7) na kuwaachili wasio haki kuwajibika kwa ajili ya matendo yao (yaani., malaika na wanadamu).

**2:10 " wale waufuatao mwili katika tamaa ya mambo machafu"** Maelezo haya yanairejelea silka ya mwanadamu aliyopewa na Mungu lakini kwa maagizo fulani (yaani., kujamiiana kwa mwanadamu, lakini ndani ya ndoa). Mwanadamu aliyeanguka huzichukulia kinyume zawadi za Mungu na nje ya mipaka ya Mungu iliyowekwa kwa ajili ya mwili, kwa sababu za tamaa (zaidi na zaidi kwangu mimi kwa gharama yo yote).

◙ **"kudharau mamlaka**" Hii ni sawa na Yuda 8 katika namna kadhaa.

| **2 Petro 2:10** | **Yuda 8** |
|---|---|

1. waufuatao mwili
2. kudharau mamlaka
3. wakiyatukana matukufu

1. huutia mwili uchafu
2. hukataa kutawaliwa
3. kuyatukana matukufu

Kwa usahihi Yuda anawarejelea malaika kupitia kifungu hiki, bali 2 Petro anaweza kuiunganisha vema 2 Pet. 2:4 na kingine kinachofuatia kinalirejelea tendo la kumkana Kristo. Nimeweka maelezo yangu ya Yuda 8.

---

**Muhtasari kutoka Fasiri ya Yuda**

**Yuda 8 "Kadhalika"**Walimu wa uongo wa nyakati za Yuda walikuwa na ufanano na uasi wa zamani. Asili halisi ya ufanano si yakini.

◙ **"hawa"** Hii ni mbinu ya Yuda kuwarejelea walimu wa uomgo waliokuwa wamelivamia kanisa (kama vile Yuda 8,10,12,14,16,19).

◙ **"katika kuota kwao"** Hili neno linatumika kumaanisha manabii wa Agano la Kale (kama vile Kumb. 13:1-5; Yer. 3:25-32), wale waliodai kuwa na mafunuo ya kipekee toka kwa Mungu (kama vile Kol. 2:18).

◙ **"huutia mwili uchafu"** Haya ni matumizi ya kistiari ya neno "chafua." Kwa namna iliyo dhahiri kulikuwa na kipengele cha maadili katika mafaundisho yao na /au maisha. Hii mifano yote ya Agano la Kale ilihusisha baadhi ya aina fulani ya dhambi za uzinzi (kama vile 2 Tim. 3:1 na kuendelea; 2 Pet. 2).

◙ **"hukataa kutawaliwa, na kuyatukana matukufu"** Kuna sifa tatu za neno "hawa."

1. "kuutia mwili uchafu"
2. "kakataa kutawaliwa" (NASB, NKJV, NRSV)
   "kuidharau mamlaka ya Mungu" (TEV)
   "kukataa kutawaliwa" (NJB)
3. "kuyatukana matukufu" (NASB)
   "kunena uovu juu ya wakuu" (NKJV)
   "kuwakashifu wenye utukufu" (NRSV)
   "kuwafedhehesha viumbe walio juu" (TEV)
   "kuzinenea vibaya Tukufu" (NJB

Ni dhahiri kuwa ya kwanza inazungumzia dhambi za uzinzi, lakini Je! ya pili na ya tatu ni nini? Udhihirisho wa pili, "kukataa kutawaliwa," kimekuwa kikifasiriwa katika namna mbili.

1. neno la Kiyunani "mamlaka" ni *kuriotēa*, ambalo linahusiana na neno "Bwana" (*kurios)*; hivyo wengine wanaliunganisha tendo hili la ukanaji (japokuwa lugha za kivitendo ni tofauti) na lile tendo la kumkana Yesu katika Yuda 4 ( " peke yake Mola, na Bwana wetu Yesu Kristo.")
2. neno la Kiyunani "mamlaka" ni *kuriotēta*, lenye kuhusiana na neno *kuriotēs*, lilitumika katika 2 Pet. 2:10 (kama vile Efe. 1:21; Kol. 1:16) kumrejelea malaika

Muktadha huu unaonekana kuwarejelea malaika, hivyo #2 inafaa zaidi.

Uthibitisho wa tatu unalitumianeo la Agano la Kale "utukufu" (*kabod*), ambalao lilitumiwa na Mungu (kama vile Yuda 24,25; 2 Pet. 1:3,17; 3:18) na mambo yote yaliyohusiana na Mungu, hasa yale ya mbinguni au maisha yajayo. Katika mfano huu Yuda anachambua maelezo ya kipindi cha uwazi kati ya Agano la Kale na Agano Jipya ya dhana hii kuvirejelea viumbe vya kimalaika, viumbe vyenye nguvu na mamlaka.

Hili pia linaweza kurejelea ukanaji wa Torati ya Agano la Kale kwa sababu Wayahnudi waliamini kwamba malaika walitumika kama wapatanishi wa YHWH kwa kumpa Musa Amri juu ya Mlima. Sinai (kama vile Matendo 7:35).

Hii hoja ya muktadha huu iko nje ya maisha ya "hawa" walimu wa uongo katika eneo la maadili na mamlaka. Orodha ya tabia za hawa walimu wa uongo yenye uwezekano wa kuanza katika Yuda 1-4 inaendelezwa : (1) kuidharau mamlaka, 2 Pet. 2:10; (2) kama wanyama 2 Pet. 2:12; (3) wakifuata anasa , 2 Pet. 2:13; (4) upendo wenye mateso wakatai wa

karamu zao Y uda 13; (5) huwasababisha waaminio kutenda dhambi Yuda 14; vna (6) huahidi uhuru huku wao ni watumwa, Yuda 19.

---

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 PETRO 2:10b-16**
**10b na hasa wale waufuataao mwili katika tamaa ya mambo machafu na kudharau mamlaka. 11 Wenye ushupavu, wenye kujikinai, hawatetemeki wakiyatukana matukufu; ijapokuwa malaika ambao ni wakuu zaidi kwa uwezo na nguvu, hawaleti mashitaka mabaya juu yao mbele za Bwana. 12 Lakini hao kama wanyama wasio na akili, ambao walizaliwa kama wanyama tu wa kukamatwa na kupotezwa, wakikufuru katika mambo wasiyoyajua, wataangamizwa katika maangamizo yao; 13 Wakipatikana na madhara, ambayo ni ujira wa udhalimu wao, wakidhania kuwa ulevi wakati wa mchana ni anasa; wamekuwa ni mawaa na aibu wakifuata anasa zisizo kiasi katika karamu zao za upendo, wafanyapo karamu pamoja nanyi; 14 wenye macho yajaayo uzinzi, watu wasiokoma kutenda dhambi, wenye kuhadaa roho zisizo imara, wenye mioyo iliyozoezwa kutamani, wana wa laana; 15 wakiiacha njia iliyonyoka, wakapotea, wakiifuata njia ya Balaamu, mwana wa Beori, aliyependa ujira wa udhalimu;**
**16 lakini alikaripiwa kwa uhalifu wake mwenyewe; punda, asiyeweza kusema, akinena kwa sauti ya kibinadamu, aliuzuia wazimu wa nabii yule.**

**2:10b "waufuatao"** (kama vile Marko 12:34; 15:43)

◙ **"tamaa ya mambo machafu"** (kama vile Tito 1:7)

◙ **"hawatetemeki"** (kama vile Mt. 28:4; Luka 8:47; Matendo 7:32; 1 Kor. 2:3).

Haya maneno matatu ya awali yanawaelezea walimu wa uongo kukosa heshima kwa nguvu na mamlaka ua kiroho. Huenda hawa wanahusianishwa na ile thiolojia yenye mapana ya Mafunuo ya Uongo kuhusiana na viwango vya kimalaika (*aeons*) na na majina ya siri ya malaika hawa hasa katika umuhimu wa kupitia ufalme wao katika namna ya ushirika wao pamoja na ngazi ya juu, mungu mzuri.

**NASB** " **wakiyatukana matukufu"**
**NKJV** **"wakinena matukufu"**
**NRSV** **"wakiwabeza wenye utukufu"**
**TEV** **"hakuna hayaheshimuye matukufu yaliyo juu"**
**NJB** **"wakimkashifu mwenye utukufu"**

Angalia dokezo katia sehemu iliyotangulia kutoka Yuda juu ya "utukufu" (*doxai*).

**2:11 "hawaleti mashitaka mabaya juu yao mbele za Bwana"** Kifungu hiki ni sawa na Yuda 9, ambacho kinaweza kuwa nukuu inayotokana na *The Assumption of Moses.* Hiki kinahusianisha matukio kati ya Mikaeli (yaani.,Malika mkuu na mlinzi wa Israeli) na Shetani dhidi ya mwili wa Mosa (kama vile Kumb. 34:6).
Kuna tofauti ya machapisho katika kifungu hiki.

1. machoni Bwana (*para* pamoja na kielekezi, א B, C, K, P, kama vile NASB, NKJV, TEV, NJB)
2. toka kwa Bwana (*para* pamoja na kielezi cha kuondoa, $P^{72}$, kama vile NRSV)

**2:12** Mstari huu unafana na Yuda 10. Yuda 9 inamwelezea Mikaeli akikabiliana na Shetani. Mstari huu katika 2 Petro na Yuda 10 unaeleza namna walimu wa uongo alivyopambana na mamlaka na nguvu za kimalaika

1. kama wanyama wasio na akili
2. wayatambuayo kwa asili

Kile wanachokijua (na wanatenda kwa namna gani) kitawaangamiza

◙ **"wataangamizwa. . . maangamizo "** Tazama Mada Maalum ifuatayo.

## MADA MAALUM: ANGAMIZA, HARIBU, CHAFUKA (*phtheirō*))

Maana ya msingi ya neno hili phtheirō ni kuangamiza, kuharibu, kuchafua, au kuvuruga. Linaweza tumika kwa:

1. maangamizi ya kifedha (yawezekana 2 Kor. 7:2)
2. uharibifu wa kimwili (kama vile 1 Kor. 3:17a)
3. upotoshaji wa kimaadili (kama vile Rum. 1:23; 8:21; 1 Kor. 15:33,42,50; Gal. 6:8; Ufu. 19:2)
4. Utongozaji wa kingono (kama vile 2 Kor. 11:3)
5. uharibifu wa milele (kama vile 2 Pet. 2:12,19)
6. tamaduni za wanadamu zipoteazo (kama vile Kol. 2:22)

Mara nyingi neno hili limetumika katika muktadha uleule kama unavyokanusha pinzani yake (kama vile Rum. 1:23; 1 Kor. 9:25; 15:50,53). Angalia mvutano wa usambamba kati ya miili yetu ya duniani na miili yetu ya kimbingu isiyoharibika.

1. iharibikayo dhidi ya isiyoharibika, 1 Kor. 15:42,50
2. kukosa heshima dhidi ya utukufu, 1 Kor. 15:43
3. udhaifu dhidi ya nguvu, 1 Kor. 15:43
4. mwili wa asili dhidi ya mwili wa kiroho, 1 Kor. 15:44
5. adamu wa kwanza dhidi ya Adamu wa mwisho, 1 Kor. 15:45
6. taswira ya duniani dhidi ya taswira ya kimbingu, 1 Kor. 15:49

**2:13 "Wakipatikana na madhara, ambayo ni ujira wa udhalimu wao"** Huu ni utunzi usio wa kawaida ambao kwa vyo vyote (1) ni nahaua au (2) mbinu ya uchezaji wa naneno (yaani., *adikoumenoi*, lenye kumaanisha "wakipatikana na madhara" na *adikias*, li natafsriwa "wenye makosa").

◙ **"wakidhania kuwa ulevi wakati wa mchana"** Hawa walitamba kwa matendo yao ili waonekane na wote. Kifungu hiki na kifungu cha mwisho cha 2 Pet. 2:12 vinazungunzia kitu kile kile.

**NASB "wakikufuru katika mambo wasiyoyajua "**
**NKJV "tia doa na kukufuru"**
**NRSV "chafua na kukufuru"**
**TEV "aibu na kutoheshimu"**
**NJB "fedhedhehesha kwa kuchafua"**

Hili neno *spilas* (na miundo yake) lina maana mbili zenye kutofautiana (1) kiasilia lile neno linazirejelea hatari zisizoonekana, kiuhalisia, zile zilizofichika au miamba myembamba (kama vile Yuda 12) na (2) mawaa au madoa (kama vile Efe. 5:27; Yakobo 3:6; 2 Pet. 2:13; Yuda 23).

Neno la pili kwa kiasi fulani ni visawe. Hili linatumika kistiari kumaamisha "makufuru" au "mawa." Yote haya yanarejelea mwenendo mbaya wa walimu wa uongo na ukatili katika kujamiiana kwa waamini katika sikukuu za upendo wa Kikristo (mlo wa karamu ya Bwana).

**NASB "wafanyapo karamu pamoja nanyi"**
**NKJV, NRSV "washerehekeapo panoja nanyi"**
**TEV "waonganao nanyi karamuni"**
**NJB "hata walipo shiriki nanyi chakulani"**

Kipengele hiki kinafanana na Yuda 12. Karamu iliyorejelewa iliitwa "Karamu ya Sikukuu ya Upendo" (kama vile 1 Kor. 11:17-22), ambayo ilikuwa ushirika wa Ekaristi wa jamii iaminiyo.

**2:14 "wenye macho yajaayo uzinzi"** Hawa walikuwa wakimtazama kila mwanamke wakati wa meza ya Kristo kama vifaa kama chombo cha starehe. Hwa walimu wa uongo walikuwa wanyanyasaji wa kingono (kama vile 2 Pet. 2:2,10,14,18). Walimu wa sheria za Kiyahudi walisema kwamba macho ni madairisha ya nafsi. Dhambi huanzia katika maisha ya fikra. Macho ya walimu wa uongo hayahutulia kamwe!

◙**"wenye mioyo iliyozoezwa kutamani"** Hawa waliwatega na kuwanasa waanini wadhaifu au wapya (kama vile Mt. 18:6; 2 Tim. 3:6).

◙**"aliyependa ujira wa udhalimu"** Hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati timilifu. Hapa tunalipata neno la Kiingereza "ukumbi wa michezo" kutokana na neno hili. Kwa namna ya kawaida walifundisha ili wapate vingi zaidi kwa ajili yao kwa gharama yo yote! Tazama MADA MAALUM: MOYO katika Marko 2:6.

**NASB "kuhadaa roho zisizo imara"**
**NKJV "na wanaziadaa roho szisizo imara"**
**NRSV "Wakiziadaa roho zisizo imara"**
**TEV "Wako chini ya laana ya Mungu"**
**NJB "Wako chini ya laana"**

Hii nahau ya Kiebrania (kama vile Efe. 2:3). Hawa wanadadavua tabia na sifa ya baba yao iliyoinarishwa, Ibilisi. Kinyume yakini cha nahau hii ni "watoto wa kutii" wa 1 Pet. 1:14!

**2:15 wakiiacha njia iliyonyoka"** Kipengele hiki kinaiakisi nahaua ya Kiebrania lenye maana ya "dhambi" (kama vile NRSV, TEV, NJB). Haki ilielezwa kama njia au barabara. Yawapasa wacha- Mungu kuifuata njia (kama vile Zab. 119:105; Mit. 6:23). Kwenda nje njia kwa namna yo yote ile ilikuwa dhambi.

◙ **"wakapotea"** Hili neno "wakapotea" ni neno letu la Kiingereza "ilimwengu," ambalo linamaanisha "mtangatangaji" Hii ni sawa na Yuda 13.

◙ **"njia ya Balaamu"** Hili tukio la Agano Jipya lenye kufanana linatajwa katika Yuda 11. Hili linanukuliwa katika Hes. 22-25; 31:8,16. Kama Balaamu alivyopenda ujira, vivyo hivyo, hawa walimu wa uongo (yaani., udhalimu, 2 Pet. 2:14).

**NASB, NKJV**
**TEV "Beori"**
**NRSV, NJB "Bosori"**

Usomaji wa kwanza unatokana na Agano la Kale la Kiebrania lenye kuzungumzia Hesabu 22 na ni usomaji ulio katika MS B. Usonaji wa pili unapatikana katika $P^{72}$, $א^{2}$, $A^{c}$, C, na toleo la $UBS^{4}$ linaupa usomaji huu daraja "A" (yakini). Hata hivyo, hakua mfano wa jina hii mahali po pote pale.

**2:16 "punda, asiyeweza kusema, akinena kwa sauti ya kibinadamu"** Kipengele hiki kinairejelea Hes. 22:24 na 31, tukio lingine la Agano la Kale lenye kumuhusisha malaika.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 PETRO 2: 17-22**

**[17] Hawa ni visima visivyo na maji, na mawingu yachukuliwayo na tufani, ambao weusi wa giza ni akiba waliyowekewa. [18] Maana wakinena maneno makuu mno ya kiburi, kwa tamaa za mwili na kwa ufisadi huwahadaa watu walioanza kuwakimbia wale wanaoenenda katika udanganyifu; [19] wakiwaahidia uhuru, nao wenyewe ni watumwa wa uharibifu, maana mtu akishindwa na mtu huwa mtumwa wa mtu yule. [20] Kwa maana wale waliokwisha kuyakimbia machafu ya dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo, kama wakinaswa tena na kushindwa, hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya kwanza. [21] Maana ingekuwa heri kwao kama wasingaliijua njia ya haki, kuliko kuijua, kisha kuiacha ile amri takatifu waliyopewa. [22] Lakini imetukia kwao sawasawa na ile mithali ya kweli, Mbwa ameyarudia matapiko yake mwenyewe, na nguruwe aliyeoshwa amerudi**

**kugaa-gaa matopeni.**

**2:17 "visima visivyo na maji"** Kifungu hiki kinafananishwa na Yuda 12. Hawa walikuwa wamehaidiwa baraka, lakini waliambuia kifo tu

.

◙**" ambao weusi wa giza ni akiba waliyowekewa "**Kiuhalisia hili ni neno "kiza kinene cha giza" (kama vile 2 Pet. 2:4; Yuda 6,13). Kitenzi hiki ni kauli tendwa elekezi ya wakati timilifu yenye kumaanisha hukumu ya kudumu na kifungo cha Mungu. Pia hiki kinafananishwa na Yuda 13.

Hii ni stiari ya adhabu ya milele kwa kutumia giza (kama vile Mt. 8:12; 22:13; 25:30 na I Enoch 10:4-5; 63:6).

**2:18**
**NASB " wakinena maneno makuu mno ya kiburi "**
**NJKV "wakinena maneno machafu ya utopu"**
**NRSV "wakinena kwa nakeke yasiyo na maana"**
**TEV "wazungumza majivuno na ujinga"**
**NJB "wakipasa sauti lakini wakizungunza utupu"**

Kipengele hiki kinafanana na 2 Pet. 2:17 na Yuda 12-13,16. Wanaonekana kuwa wa kiroho na waaminifu, lakini wanaiga, ni udanganyifu.

**NASB " kwa tamaa za mwili na kwa ufisadi huwahadaa"**
**NKJV "wnavutia kupitia tama za mwili, kupita uharibifu"**
**NRSV "kwa uharibifu wanatamani yaliyo ya mwili"**
**TEV "wanautumia uharibifu wa mwaili kwa ajili ya kunasa"**
**NJB "wanajaribu. . .kwa tama mbaya a asili ya kibinadamu"**

Kwa mara nyingine hivi ni vipengele vya kujamiiana vya walimu wa uongo. Hawa hawakuwa wakoseshaji kithiolojia pekee, bali hata kimaadili.

**NASB "walioanza kuwakimbia"**
**NKJV "waliokwepa mara nyingi"**
**NRSV "walioondoka"**
**TEV "wale waliokuwa wameanza kuondoka"**
**NJB "watu walio tawanyika mbali sana"**

Kuna tofauti za kimachapisho ya Kiyunani katika kifungu

1. *oligōs*, lenye kumaanisha "karibia" (kama vile MSS $P^{72}$, $א^{2}$, A, B, na Vulgate; ki- Shamu, na tafsiri za Koptiki)
2. *ontō*s, lenye maana " kwa ukweli" au "kiuhalisia" (kama vile MSS , א* ,C, na tafsiri za ki Marekani na ki Slavoni).Suala la kithiolojia ni kwamba waamini hawa wa kthiolojia wanapotelea wapi (kama NKJV, NRSV, NIV) au takribani waamini (kama vile NASB, NRSV [tambihi], TEV)? Huu muktadha wa 2 Pet. 2:20-21 kwa hakika unamaanisha hawa walikuwa waamini (yaani., sentensi shurutishi daraja la kwanza).

**2:19 " wakiwaahidia uhuru"**Hawa walimu wa uongo walikuwa wakihaidi uhuru katika maana mbili: (1) uhuru wa kithiolojia uliojikita katika maarifa ya siri ya utawala wa kimalaika na (2) uhuru toka mipaka ilijikita katika wokovu pekee ikihusisha utitmilif wa ufahamu (yaani., apotoe ya ukware au upinzani wa anasa).

Paulo anadai kuwa haiwapasi waamini kuutumia uhuru wao kama kibali cha kuingia dhabini (kama vile Gal. 2:16), kama alivyofanya Petro (kama vile 1 Pet. 2:16). Mara nyingi uhuru umekuwa tunda lili lozuiiwa. Kujitawala ni alama ya ukomavu wa kiroho (kama vile Gal. 5:23). Hii si kwaa maana ya nadharia ya uvumilivu izungunziaa kujitawala , bali katika maana ya Kikristo kwa waamini wampokeao Rogo akaaye ndani na kujitolea katika mafunuo ya Mungu (Agano Jipya). Swali halisi ni hili ni nani au ni kijitolea kwa namna gani na/ au kunakoleta sifa bainishi katika maisha yetu?

◙ **"uharibifu"** Tazama Mada Maalum katika 2 Pet. 2:12.

**2:20 "kama"** Hii ni sentensi shurutishi daraja la kwanza yenye kudhaaniwa kuwa ya kweli kutokana na mtazamo wa mwandishi au sababu zake za kiuandishi. Neno hili linamaanisha kwamba waathirka wa 2 Pet. 2:18 walikuwa waamini.

◙**" wale waliokwisha kuyakimbia machafu ya dunia"** Hii ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopita usio timilifu, yenye kamaanisha tendo lililokamillika (utaalamu wao katika Kristo). Injili imewatenga na nguvu ya asili ya anguko (kama vile Rum. 6).

◙ **"kwa kumjua Bwana"** Hili ni neno *epignōskō*, lenye maana nyingine zilizo jaa maarifa yatokanayo na uzoefu (kama vile 2 Pet. 1:2). Maana ya wokovu wao ilikuwa injili ambayo ni mtu, ukweli wenye kumhusu mtu, na maisha kama mtu. Walimu wa uongo waliyakiuka haya m ambo yote matatu!

◙**"kama wakinaswa tena na kushindwa"** Kitenzi cha kwanza ni kauli tendwa endelevu ya wakati uliopita usio timilifu, ambapo cha pili ni kaulik tendwa elekezi ya wakati uliopo. Itambue irabu tendwa, yenye kumaanisha uhusika wa nje (yaani., walimu wa uongo au mwovu). Muktadha wa papo kwa papo unafafanua mtego kama hisia na tama za kimwili. Kwa mjadala ulio nzuri wa mstari huu tazama *Hard Sayings of the Bible*, kr. 729-730. Nakubaliana kabisa na usemi wao.

◙ **"hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya kwanza"** Hiki kipengele kingeweza kuhusiana na (1) waamini wapya (2 Pet. 2:14b, 18b, 21) au (2) walimu wa uomgo (2 Pet. 2:17, 18a). Huu utata wenye kufanana una uhusiano na 2 Pet. 2:19.

**2:21** Ni kwa namna gani sharti lao lingeweza kuwa la kimakosa? (1) Hawa waliwekewa kinga dhidi ya imani ya kweli. Hawa ni sawa na Ebr. 2:1-4; 6:4-6 na10:26-31 (yaani., wasioamini katika uwepo wa nuru kuu); (2) Hili lingeweza kuurejelea ushahidi wa maisha ya waamini wapya au walio wadhaifu wenye kupoteza zaidi ya wokovu wao binafsi. Kuna mapambano yenye nguvu kati ya asili za kale na zile mpya (kama vile Rumi 7), zilizokuwepo kabla ya vokovu na baada ya wokovu.

◙ **"njia ya haki"** Kifunguu hiki kinairejelea injili, kama kilivyo kifungu "amri takatifu" pia katika 2 Pet. 2:21 na "maarifa ya Bwana" katika 2 Pet. 2:20 (kama vile 2 Pet. 3:2).

**2:22 "mithali ya kweli"** Hii mithali yenye kuzungunzia mbwa inatoka katika toleo la MT, na si LXX la Mit. 26:11. Hii mithali yeye kumzungumzia nguruwe inatokana na kitabu cha hekina ya Kiaramu cha Ahika (yaani., 8:18), ambacho kilijulikana vema kwa Wayahudi kipindi cha uhamisho wa Ashuru. Ahika anatajwa katika kitabu cha Kiyahudi *Tobit* kama mtu mwenye hekima toka makabila ya kaskazini yaliyopelekwa uhamishoni. Mapokeo ya Kiyahudi yanasema kuwa huyu aliinuka sana na kuwa kiongozi wa utawala huo yaani., kama Danieli) wakati wa utawala wa Senakaribu na Esarhadoni. Hawa walimu wa uongo walionekana kama waanimi (yaani., wenye hekima), lakini matendo yao yalioonyesha kuwa ilikuwa sura ya nje tu haikuwa toba ya kweli (kama vile Mathayo 7 na13).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni <u>mwongozo</u> wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je! Walimu wa uongo walikuwa Wakristo wa kweli? (2 Pet. 2:1)
2. Je! Wafuasi wao walikuwa Wakristo?
3. Orodhesha tabia za hawa walimu wa uongo.
4. Kwa nini kjuna maziungumzo mengi yahusuyo malaika katika sura hii?
5. Nini maana ya mistari ya 20-22?

# 2 PETRO 3

| MIGAWANYO YA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| UBS[4] | NKJV | NRSV | TEV | NJB |
| Ahadi ya ujio wa Bwana 3:1-7 | Ahadi ya Mungu sio ya uvivu 3:1-9 | Siku ya Bwana 3:1-7 | Ahadi ya ujio wa Bwana 3:1-7 | Siku ya Bwana: Manabii na mitume 3:1-2 |
| | | | | Siku ya Bwana: Walimu wa uongo 3:3-7 |
| 3:8-13 | Siku ya Bwana | 3:8-10 | 3:8-9 | 3:8-10 |
| | 3:10-13 | | 3:10-13 | Wito kuelekea Utakatifu. Wimbo wa kumsifu Mungu |
| | Kuwa imara | 3:11-13 | | 3:11-18 |
| 3:14-18 | 3:14-18 | 3:14-18 | 3:14-16 | |
| | | | 3:17-18 | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (kutoka "Mwongozo wa usomaji Mzuri wa Biblia")

*KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu. Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuatilia kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 PETRO 3:1-7**

[1] **Wapenzi, waraka huu ndio wa pili niwaandikiao ninyi; katika zote mbili naziamsha nia zenu safi kwa kuwakumbusha, [2] mpate kuyakumbuka yale maneno yaliyonenwa zamani na manabii watakatifu, na ile amri ya Bwana na Mwokozi iliyoletwa na mitume wenu. [3]Mkijua kwanza neno hili ya kwamba katika siku za mwisho watakuja na dhihaka zao watu wenye kudhihaki, wafuatao tamaa zao wenyewe, [4]na kusema, Iko wapi ahadi ile ya kuja kwake? Kwa maana, tangu hapo babu zetu walipolala, vitu vyote vinakaa hali iyo hiyo, tangu mwanzo wa kuumbwa. [5]Maana hufumba macho yao wasione neno hili ya kuwa zilikuwako mbingu tangu zamani, na nchi pia, imefanyizwa kutoka katika maji, na ndani ya maji, kwa neno la Mungu; [6]kwa hayo dunia ile ya wakati ule iligharikishwa na maji, ikaangamia. [7]Lakini mbingu za sasa na nchi zimewekwa akiba kwa moto, kwa neno lilo hilo, zikilindwa hata siku ya hukumu, na ya kuangamia kwao wanadamu wasiomcha Mungu.**

**3:1 "Wapenzi"** neno hili ni la asili lililotumiwa na Mungu Baba kwa ajili ya mwana kwenye ubatizo wake (kama vile. Mt. 3:17) na kubadilika kwake (kama vile Mt. 17:5 na 2 Pet. 1:17). Lilikuja kuwa jina kwa ajili ya watu wa Mungu (kama vile.

Rum. 1:7).limetumika mara moja tu kwenye 1 Petro (kama vile. 1 Pet. 2:11; 4:12),lakini limetumika kwa mapana zaidi kwenye 2 Petro 3 (kama vile. 2 Pet. 3:1,8,14,15-17).pia ni la kawaida sana kwenye 1 na 3 Yohana.

◙**"waraka huu ndio wa pili"** hii ni wazi anarejelea katika 1 Petro,kama wewe unaamini Petro ndiye msingi wa waraka wa 1 na 2 Petro,kitu ambacho hata mimi naamini.

**NASB ”nia aminifu"**
**NKJV "nia zenu safi"**
**NRSV "dhamira yenu aminifu"**
**TEV "fikra zenu safi"**
**NJB "ufahamu angavu"**

Neno hili linaweza kuwa na maana ya safi maadili bora (kama vile Flp. 1:10). Walimu wa uongo hawakuwa safi kwa maana yeyote ile. Walikuwa waovu na waliendesha mambo yao kwa kujipendekeza.

◙**"kwa kuwakumbusha"** haya ni maneno ya wazi ya 2 Pet. 1:13-14 (kama vile Yuda 17). Ndani ya Biblia mwanadamu mara nyingi ameitwa ili kumkumbuka Mungu, neno lake, na matendo yake. Mungu, hata hivyo, anajiimarisha ili kuzisahau dhambi zao (yaani, Yer. 31:34; Isa. 43:25; sitiari iliyo kwenye Zab. 103:3; Isa. 1:18; 38:17; 44:22; Mik. 7:18).

**3:2 "mpate kuyakumbuka yale maneno"** hii ni kauli tendwa shurutishi ya kitenzi jina hakisi. Huu ni ufahamu unaotiliwa mkazo (1) Agano la kale (kama vile. 2 Pet. 1:21); (2) maneno ya Yesu (kama vile. 2 Pet. 2:21); na (3) na utumishi wao wa kitume (kama vile.2 Pet. 1:1). Hii inafanana na kwenye Yuda 17. Kufahamu/kukumbuka ilimaanisha kuwatia nguvu waamini katika kuishi kama Kristo na kurudi kwake mara ya pili!

◙**"yaliyonenwa zamani na manabii watakatifu"** Hii ni kauli timilifu tendwa ya hali ya kuendelea, ambayo inadokeza ufunuo wa milele (njeo timilifu, kama vile Mt. 5:17-19; 1 Pet. 1:25) unaotolewa na Roho (kauli ya kutendwa, kama vile 2 Pet. 1:20-21).Hii inarejelea kwa Agano la Kale lote. Wayahudi waliamini kwamba maandiko yote yaliandikwa na manabii. Hii ndio sababu Musa aliitwa nabii kwenye Kumb. 18:15 na kwamba Yoshua kupitia kwa wafalme aliitwa"manabii wa kale."

◙**"amri ya Bwana na Mwokozi “**Hii ni nahau inayorejelea injili ( "amri takatifu," kama vile. 2 Pet. 2:21; "amri" 1 Tim. 6:14).Ni nahau inayosimuliwa "sheria ya Kristo" (kama vile. Gal. 6:2).

◙**"mitume wenu"** kama nabii alipewa Agano la kwanza, mitume wanapewa la pili!

**3:3 "mkijua kwanza neno hili"** tungo hii ni sawa na iliyotumika kwenye 2 Pet. 1:20. Petro alitumia nahau ya fasihi kuyawekea alama malengo yake makuu.

◙**"katika siku za mwisho"**tungo hii ya Agano la kale inadokeza kipindi cha wakati kabla ya historia ya mwanadamu kufikia kilele.Petro ana mashaka kidogo kipindi hiki kinarejelea wakati gani. Kwenye 2 Petro 2, anaongelea “kuja”kwa waalimu waongo, na tayari wameshaonekana siku zake. Hii ni thiolojia inayofanana na “mpinga kristo wa Yohana.. .wapinga kristo" wa 1 Yohana 2:18. Waalimu hawa wa uongo na wenye kudhihaki wataonyesha tabia zao kwa kila kipindi kijacho cha historia ya kanisa, wakianza na karne ya kwanza. Tazama mada maalumu katika Marko 13:8.

◙**" watakuja na dhihaka zao watu wenye kudhihaki"** hii inafanana na Yuda 18. Pendekezo na miundo iliyosaidia ya jina sawa yametumika kwa ajili ya kukazia. Hawa waalimu wa uongo wanafanya na wataendelea kutimiza ahadi kubwa za kibiblia juu ya ujio wa kristo (kama vile 2 Pet. 3:4)

◙ " **wafuatao tamaa zao wenyewe**” waalimu wa uongo wako dhahili kwa sababu ya maneno na matendo yao (kama vile Mt. 7:15-20 na 2 Tim. 3:2-5). Hili linafanana na Yuda 18.

**3:4** "**Iko wapi ahadi ile ya kuja kwake**" hii inarejelea katika (1) Agano la kale siku ya kuja YHWH au (2) Agano jipya kristo kuja mara ya pili.

**NASB, NKJV "mababa"**
**NRSV, TEV "ukoo wetu"**
**NJB "baba zetu"**

Kipindi cha Agano la kale kimetajwa kwenye 2 Pet. 3:2, hivyo "mababa" lazima itarejelea kwenye mababa wa imani katika Agano la kale au viongozi wa kabila. Hili linathibitishwa na 2 Pet. 3:4-6, ambalo linazungumzia uumbaji.
Ni dhahili muktadha unarejelea ujio wa Mungu kwenye hukumu (kama vile. 2 Petro 2). Agano la kale linadai kwamba wanadamu siku moja watasamehewa na Mungu kwa ajili ya utumishi kama zawadi ya maisha (yaani Mt. 25:31-46; 20:11-15). Wenye dhihaka hawa sio tu kwamba wanakataa udhihilisho wa Yesu katika mwili, wanakejeli kurudi kwake kama hakimu.

◙ "**walipolala**" hiki ni kisawe cha Agano la kale kwa ajili ya kifo, ambacho kimeendelea hadi kwenye Agano jipya (kama vile. Mat. 27:53; Marko 5:39; Yohana 11:11; 1 Kor. 11:30; 15:51; Efe. 5:14; 1 The. 4:14).

◙ **"vitu vyote vinakaa hali iyo hiyo, tangu mwanzo wa kuumbwa"** historia ya mwanadamu, bado ndogo sana kulinganisha na muda wa historia ya kijiografia, inampatia mwanadamu maana ya kawaida. Hili ni dhanio la sayansi ya kisasa (yaani, mfanano mmoja) kwamba utaratibu wa kiasili na sheria za kawaida za asili zinaweza kuonyeshwa zote kwenye muda uliopita na ujao. Biblia inadai kwamba kuna mwanzo wa uumbaji na kutakuwa na mwisho. Mungu aliumba kwa kusudi. Kwamba kusudi ni ushirika na viumbe alivyoviumba kwa mfano wake kuaksi tabia yake. Ulimwengu unawajibika katika haki, Mungu mwenye maadili. Hata hivyo, taswira ya nyakati za mwisho na kawaida za asili zinasababisha waalimu wa uongo kukataa ufunuo wa maandiko, maneno ya Yesu, na bainisho la kitume. Historia ya mwanadamu na kudumu kwa kila mmoja mmoja kuwa kimya kwa muda mrefu huwapeleka wanadamu kwenye utambuzi mwovu wa kujiamini kwenye “kesho kama leo"!

**3:5**
**NASB "watakimbia ishara zao"**
**NKJV "watasahau kabisa"**
**NRSV, NJB "kwa makusudi wakikana"**
**TEV "kwa makusudi wakikataa"**

Neno hili lina kidokezo cha kusahau kitu au kuficha kitu, hivyo basi,shauku yenye nia iko ndani ya neno (kama vile. 2 Pet. 1:9; 3:5,8)waalimu hawa wa uongo "wasahaurifu wafaao" au"chagua kukana" kuhisika kwa Mungu kwenye uumbaji wake na shauku yake ya kipekee ya uwajibikaji kwa uumbaji wote (yaani,hukumu).

◙ "**kwa neno la Mungu**"huu ni uumbaji kwa maneno yaliyosemwa (kama vile Mwa. 1:3,6,8,14,20,24). Unaitwa kwenye thiolojia kwa neno la kilatini "ruhusa," lenye maana "kwa maana ya neno lililosemwa," tazama John L. Walter, *The Lost World of Genesis One*, ambapo anadai kwamba katika kitabu cha Mwanzo 1 sio jambo la uumbaji, lakini ulimwengu utendao kazi. Walimu waongo wanakataa kwamba Mungu mtakatifu anaweza kuwa umbo, asiye na utele, kuumba asiye na dhambi, kuwa pamoja.

**NASB "dunia imefanyizwa kutoka katika maji, na ndani ya maji"**
**NKJV "dunia imesimama kutoka katika maji na ndani ya maji"**
**NRSV "dunia imefanyizwa kutoka katika maji na kwa maana ya maji"**
**NJB "dunia imefanyizwa kwa neno la Mungu kutoka katika maji na kati ya maji"**

Maji ni sehemu ya muhimu sana kwenye Mwa. 1:2 (“kilindi" na"maji"). Hayazungumzwi kwa maana ya kutajwa kama yalikuwepo. Kihusishi cha kiyunani "kupitia" (dia) maji yanaweza pia kumaanisha "kati ya,"toleo la NASB " mzunguko,"

"katikati," "matendo ya," au "kwa kuhimili" (kama vile Zab. 24:2; 136:6). Tungo hii inaweza kurejelea katika Mwa. 1:2;1:6; au 1:9.

**3:6 "dunia ile ya wakati ule iligharikishwa"** hii inarejelea gharika ya nyakati za Nuhu (kama vile. Mwa. 6-8). Nimehusisha na muhtasari kidogo kutoka kwenye fasihi yangu iliyoko katika Mwa. 1-11.

---

**MWANZO**

"Kuna baadhi ya kisio kwamba neno "gharika"yumkini likasimulia neno la Kiashuru "kuharibu."

Je gharika nyakati za Nuhu ilienea ulimwengu mzima au mashariki ya karibu ya kale pekee? Neno hili "dunia"mara nyingi linatafsiriwa kama "nchi" kwa maana ya mahali. Ikiwa wanadamu hawakuenea katika sehemu zote za dunia, ambapo ni uhakika wa dokezo la mnara wa Babeli linaloerezewa katika 2 Petro 10-11, hivyo gharika la mahali lilifanya kazi. Kitabu bora zaidi nilichosoma chenye uwiano wa ushahidi kwa ajili ya gharika hilo ni kitabu cha Bernard Ramm's *The Christian View of Science and Scripture*" (uk. 62).

---

**3:7**

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"kwa neno lake"** |
| **NKJV, NRSV** | **"kwa neno hilo hilo"** |
| **TEV** | **"kwa amri hiyo hiyo"** |
| **NJB** | **"ni neno hilo hilo"** |

Kama Mungu aliumba kwa neno la kutamka na kutawala kwa neno (yaani, Kristo, kama vile. Yohana 1:1), tumezaliwa mara pili kwa neno la Mungu lililo hai na linalotawala (1 Pet. 1:23). Pia atasafisha kwa neno la kutamka (yaani., hukumu ya gharika, hukumu ya moto). Sitiari ya Yesu kwenye Ufu. 19:15 kama kuja na upanga ukatao kuwili utokao kinywani mwake ni njia nyingine ya kuelezea ukweli huu mmoja.

◙**"mbingu za sasa na nchi zimewekwa akiba kwa moto"** Kauli tendwa timilifu endelevu yenye mafumbo, ambayo inaongelea jambo ambalo tayari limetendeka. Hapa imetumika maana ya kinabii kwa hakika ya tukio lijalo ambalo msingi wake ni uaminifu wa neno la Mungu. Muktadha huu mzima unakazia nguvu na waliokuwepo kabla ya neno la Mungu (kama vile. 2 Pet. 1:19; 3:5,7; 1 Pet. 1:23; 2:8; 3:1).

Hukumu hii ya moto huenda inakuja kwa maana mbili kutoka Agano la kale: (1) zaburi inaongelea moto utokeao mbele za Bwana (kama vile Zab. 18:8; 50:3; 97:3) au (2) hukumu za YHWH kwenye jangwa walilotangatanga (kama vile Law.10:2; Hes. 11:1-3; 16:35; 26:10) au matukio ya siku za mwisho (kama vile Dan. 7:10; Isa.30:27,30,33).

Moto mara nyingi uliambatana na uwepo wa YHWH kwenye Agano la kale. Hii yumkini ilihusiana na (1) Mungu kama mwakilishi wa maarifa na ufunuo(nuru); (2) Mungu kama mwakilishi safi; au (3) Mungu kama hakimu (yaani., mwakilishi mharibifu).

## MADA MAALUM: MOTO (BDB 77, KB 92)

Moto unavyo vidokezo chanya na hasi katika maandiko.

A. Chanya
   1. Husisimua (kama vile Isaya 44:15; Yohana 18:18)
   2. Huwasha nuru (kama vile Isaya 50:11; Mt. 25:1-13)
   3. Hupikia (kama vile. Kutok 12:8; Isaya 44:15:16; Yohana 21:9)
   4. Husafisha (kama vile. Hes 31:22-23; Mith. 17:3; Isaya 1:25; 6:6-8; Yer. 6:29; Malaki 3:2-3)
   5. Utakatifu wa Mungu (kama vile Mwa. 15:17; Kutoka 3:2; 19:18; Ezek 1:27; Waebrania 12:29)
   6. Uongozi wa Mungu (kama vile Kutoka 13:21; Hes. 14:14; Wafalme 1. 18:24)
   7. Uwezeshaji wa Mungu (kama vile. Matendo 2:3)
   8. Ulinzi wa Mungu (kama vile Zekaria 2:5)

B. Hasi
   1. Huunguza (kama vile Yos 6:24; 8:8; 11:11; Mt. 22:7

2. Huangamiza (kama vile Mwa 19:24; Walawi 10:1-2)
3. Hasira (kama vile. Hes 21:28; Isaya 10:16; Zek 123:6)
4. Adhabu (kama vile Mwa. 38:24; Walawi 20:14; 21:9; Yoshua 7:17
5. Ishara ya mbaya ya siku ya mwisho (kama vile.Ufunuo 13:13)

C. Hasira ya Mungu dhidi ya dhambi mara nyingi hudhihirishwa kwa tanuru ya moto.
   1. Hasira yake huunguza (Kama vile Hos. 8:5; Sefania 3:8)
   2. Humimina moto (kama vile Nah 1:6)
   3. Moto wa milele (kama vile Yer. 15:14; 17:4; Mt 25:41; Yuda aya ya 7)
   4. Hukumu ya siku ya mwisho (kama vile Mt.3:10; 5:22; 13:40; Yohana 15:5; The. 2. 1:7; Petro 2. 3:7-10; Ufu. 8:7; 16:8; 20:14-15)
D. Moto mara nyingi huonekana katika tanuru
   1. Mwa. 15:17
   2. Kutoka 3:2
   3. Kutoka 19:18
   4. Zaburi 18:7-15; 29:7
   5. Ezek. 1:4, 27; 10:2
   6. Ebr. 1:7; 12:29
E. Kama sitiari yingi katika Biblia (yaan., chachu, simba) moto unaweza kuwa Baraka au kufuatana na mazingira au muktadha.

◙**"zikilindwa hata siku ya hukumu. . .wasiomcha Mungu"** hii ni kauli tendewa endelevu ya wakati uliopo. Zote nyaraka za 2 Petro 2 na Yuda zinatilia mkazo kwamba malaika waovu na wanadamu waovu wametunzwa kwa ajili ya siku ya hukumu.viumbe wote wenye ufahamu (kama vile Fil. 2:9-11) watalazimika siku moja kushikiliwa kama kipawa cha uzima kwa utumishi (kama vile Gal. 6:7).Matukio haya ya siku za mwisho ni wakati kwa ajili ya hukumu ya wasio mcha Mungu, lakini ni wakati wa dhawabu kuu kwa ajili ya waaminio. kanisa linaloteswa linahitaji kujua kwamba siku moja Mungu atafanya mambo yote kuwa sawa!

◙**"kuangamia"** Tunapata neno la kiingereza Apollyon kutokana na neno hili (kama vile. Ufu. 9:11).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 PETRO 3:8-10**
**8Lakini, wapenzi, msilisahau neno hili, kwamba kwa Bwana siku moja ni kama miaka elfu, na miaka elfu ni kama siku moja. 9Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba. 10Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwivi; katika siku hiyo mbingu zitatoweka kwa mshindo mkuu, na viumbe vya asili vitaunguzwa, na kufumuliwa, na nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea.**

**3:8**
**NASB "usiache jambo hili likapita fahamu zako"**
**NKJV "msilisahau neno hili moja"**
**NRSV "usilikatae jambo hili"**
**TEV "usisahau jambo moja"**
**NJB "kuna jambo moja . . .usilisahau kamwe"**

Hii ni kauli shurutishi ya wakati uliopo ikiwa na chembe za kukana, ambayo kwa kawaida inadokeza “kuacha utaratibu wa tendos."kwa sababu ya mateso (kama vile. 1 Pet.) na walimu wa uongo (kama vile 2 Pet.) waaminio wataanza kuuliza uaminifu wa matukio ya siku za mwisho kibiblia.

◙**"siku moja ni kama miaka elfu"** Hii ni taswira ya Zab. 90:4. Imani inadai kwamba muda sio kipengerele cha Mungu wa milele. Viumbe wake pekee ndio unaojua nyakati za sasa, zilizopita, na zijazo. Sisi ni mwisho wa muda, tunafahamu muda. Waaminio ni lazima washike ukweli kwamba ni nini ahadi za Mungu, Mungu atatenda (kama vile. 1

Fal.8:24,26,56). Tunaamini katika tabia yake, ahadi zake, neno lake,na mwana wake! Muda usiopaswa ingawa Mungu anatumia muda kwa ajili makusudi yake tajwa.
Kizazi cha kwanza cha waaminio walitarajia Yesu atarudi haraka (kama vile. Marko 13:30). Hii ndio sababu kwa nini hawakuandika maneno ya Yesu na matendo (injili) kwa miaka mingi. Lakini wakiendelea kukawia

1. Mashahidi walianza kufa
2. Walimu wa uongo walianza kujiimarisha
3. Baadhi walianza kuwa na mashaka kwa nini

Wote Paulo (kama vile 2 Thesalonike 2) na Petro (kama vile 2 Petro 3) wanaelezea jambo hili la kukawia ujio wa mara ya pili. Hata katika mafundisho ya Yesu kuna wasiwasi kati ya kurudi upesi (kama vile Mt.10:23;24:27,34,44; Marko 9:1; 13:30) na "baadhi ya matukio ni lazima yatokee kwanza"

1. Injili ya Urejesho kwa ulimwengu, kama vile Mt. 24:15; Marko 13:10
2. Ufunuo wa “dhambi ya mwanadamu”, kama vile Mt. 24:15; 2 Thesalonike 2; ufunuo 13
3. Dhiki kuu, kama vile Mt. 24:21,24; Ufunuo 13

Petro kwa upekee anaunganisha kukawia na huruma za Mungu kwa ajili ya walio potea! Mungu amekawiza kurudi kwa kristo kwa maana kwamba wengi watubu na kurejea kwake kupitia kwa kristo. Maisha ya wacha Mungu yanalenga kuwaelekeza wasio amini kwa Mungu!

**3:9 "Bwana hakawii"**neno hili “Bwana” lazima linarejelea kwa YHWH. Mipango ya Mungu iliyopangwa (kama vile. Hab. 2:3) ya uumbaji na ukombozi inaonekana kwenda pole pole kwa wanadamu. Sehemu ya muda inaturuhusu kuendelea kuwa na imani ndani ya muda. Nyakati hizi za maisha yetu ni muda pekee wa waamini kuishi kwa imani, ambao unampendeza Mungu.Uvumilivu wetu na maisha ya u-chaji Mungu unaelezewa na ushahidi wa imani yetu/kumwamini yeye.

**◙"**, **bali huvumilia kwenu"** mojawapo ya tabia ya Mungu ni uvumilivu kwa ajili ya watenda dhambi na watakatifu. Hata hivyo, uvumilivu wake una faida kwa makundi yote mawili. Uvumilivu wake una kusudi, kurejesha sura iliyopotea kwenye maangamizi.

**◙"maana hapendi mtu yeyote apotee"** hii ni kauli ya kati (yenye ushahidi) endelevu ya wakati uliopo. Mungu anapenda wanadamu wote waokolewe (kama vile. Ezek. 18:23,32; 33:11; Yn. 3:16; 4:42; Mdo. 17:30; Rum. 11:32; 1 Tim. 2:4,6; 4:10; Tito 2:11; Ebr. 2:9; 1 Yn 2:2).kwa sababu wanadumu wote wameumbwa kwa sura yake kwa ajili ya ushirika binafsi, akamtuma mwanae afe ili kwamba wote wampokee yeye (kama vile Rum. 5:12-21). Huu ni uwiano wa muhimu kwa utaratibu wa thiolojia ambao msingi wake ni sehemu ya Mungu katika wokovu, lakini kupunguzwa maisha ya mwanadamu kunahitaji kutekeleza maagano. Nimehusisha muhtasari wangu kutoka kwenye kitabu cha 1 Tim. 2:4 (juzuu. 9, uk. 25) tazama hii mada.

---

**Muhtasari kutoka fasiri yangu kwenye 1 Timotheo 2:4**

**2:4 "ambaye hutaka watu wote waokolewe"** waaminio waombe kwa ajili ya watu wote kwa sababu Mungu anapenda watu wote waokolewe. Hii ni kauli ya kushangaza kwa walimu wa uongo, wawe wenye ujuzi au myahudi au, inawezekana zaidi kwenye barua za kichungaji, kwa pamoja.Huu ni ukweli mkuu juu ya upendo wa Mungu kwa ajili ya wanadamu (kama vile. 1 Tim. 4:10; Ezek. 18:23,32; 33:11; Yn 3:16; Mdo 17:30; Rum. 11:22; 1 Tim. 2:4,6; 4:10;Tito 2:11; Ebr. 2:9; 2 Pet. 3:9; 1 Yn 2:2). Mistari hii inaonyesha tofauti ya imani ya kanisa, super-lapsarian, hatima ya upanga ukatao kuwili ambao unakazia utawala wa Mungu mbali na kuhitajika kwa kwa mwitikio wowote wa mwanadamu. Inadhibitisha kweli ya “alama tano” mafundisho ya Calvin, hasa hasa “rehema za msukumo”na "upatanisho usio kamili”wavunja maagano sehemu ya imani kibiblia.ni kukoswa nidhamu kwa kupunguza wigo wa Mungu kuwaweka wanadamu huru, kama vile pia ni kutokuwa na nidhamu kwa kupunguza wigo wa wanadamu juu ya mapenzi ya kiroho.Mungu kwenye utawala wake alichagua kuhusika na mwanadamu aliyeanguka kwa maana ya maagano. Mara zote alianzisha muundo wa maagano (kama vile. Yn 6:44,65), lakini alikuwa na mamlaka kwamba mwanadamu ni lazima akubalie na aendelee kukubali katika kutubu na imani (kama vile. Marko 1:15; Mdo 3:16,19; 20:21), kama vile utiifu na kuvumilia!

---

Mara nyingi mjadala wa kitheolojia wa utawala wa Mungu (majaaliwa) na kuwekwa huru mwanadamu utapunguza hoja ya ushahidi wa andiko. Biblia kwa wazi inafunua utawala wa YHWH. Hata hivyo, pia inafunua uumbaji wake mkuu,mwanadamu, aliyemuumba kwa sura yake, nakupewa maamuzi ya kushangaza kwa kuchagua maadili sahihi. Mwanadamu ni lazima ashirikiane na Mungu katika kila eneo la maisha.

Neno "wengi" limetumika kutetea kwamba Mungu alichagua baadhi (waliochaguliwa) lakini sio wote; kwamba Yesu alikufa kwa ajili ya baadhi,sio wote. Usomaji makini wa maandiko yanayofuatia unaonyesha kwamba haya yametumika kwa maana inayofanana!

| **Isaya 53** | **Warumi 5** |
|---|---|
| 1. "wote" (Isa. 53:6) | 1. "wote" (Rum. 5:18) |
| 2. “wengi”(Isa.53:11-12) | 2. "wengi" (Rum. 5:19) |

**MADA MAALUM: MPANGO WA UKOMBOZI WA MILELE WA YHWH**

Nalazimika kukubali kwako kiongozi kuwa ninao upendeleo juu ya hoja hii. Mpangilio wangu wa kithiolojia sio wa ufuasi wa Calvin au mfumo wa kidini, bali ni agizo kuu la kiunjilisti (kama vile Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8). Naamini Mungu ana mpango wa milele kwa ajili ya ukombozi wa mwanadamu (mf., Mwa. 3:15; 12:3; Kut. 19:5-6; Yer. 31:31-34; Eze. 18; 36:22-39; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29; Rum. 3:9-18,19-20,21-31),wale wote walio umbwa kwa sura na ufanano wake (kama vile Mwa. 1:26-27). Maagano yote yameunganishwa katika Kristo (kama vile Gal. 3:28-29; Kol. 3:11). Yesu ni fumbo la Mungu, lilijificha ambalo halijafunuliwa (kama vile Efe. 2:11-3:13)! Injili ya Agano Jipya, sio Israel, ni ufunguo wa maandiko.

Huu uelewa wangu wa kabla unanakshi tafasiri zangu zote za maandiko. Nasoma maandiko kwa kuyapitia yote! Hakika ni upendeleo (walionao watafsiri wote), lakini ni dhahanio za utaarifishwaji wa kimaandiko.
Mtizamo wa Mwanzo 1-2 ni YHWH akiandaa mahali ambapo Yeye na Uumbaji wake ulio juu, mwanadamu, waweza kuwa na ushirika (kama vile Mwanzo. 1:26,27; 3:8). Uumbaji wake wa vitu ni hatua kwa ajili ya ajenda ya ki-Ungu kati ya watu wawili.

1. St. Augustine anauanisha kama tundu lenye muonekano wa ki-Ungu katika kila mtu ambaye anaweza kujazwa tu na Mungu mwenyewe.
2. C.S. Lewis aliita sayari hii "sayari inayoshikika," (yaani., iliyoandaliwa na Mungu kwa ajili ya wanadamu).

Agano la Kale lina vidokezo vingi vya ajenda hii ya ki-Ungu.

1. Mwanzo 3:15 ni ahadi ya kwanza kuwa YHWH hatamwacha mwanadamu katika hali tete ya dhambi na uasi. Hii hairejelei kwa Israel kwa sababu hapakuwepo na Israel, wala watu wa agano, mpaka pale Ibrahimu alipoitwa katika Mwanzo 12
2. Mwanzo 12:1-3 ni wito wa awali wa YHWH na ufunuo kwa Abraham ambao ndio ulikuja kuwa watu wa agano, Israel. Lakini hata katika huu wito wa awali, Mungu alikuwa anaangalia ulimwengu wote. Angalia Mwanzo 12:3!
3. Katika Kutoka 20 (Kumbu kumbu la Torati 5) YHWH alimpa Musa sheria ili kuwaongoza watu wake maalum. Tambua kuwa katika Kutoka 19:5-6, YHWH alidhihirisha kwa Musa uhusiano wa kipekee ambao Israel itakuwa nao. Lakini pia tambua kuwa wao walichaguliwa, kama Ibrahim, kuubariki ulimwengu (kama vile Kut. 19:5, “kwa vile vitu vyote vya Dunia ni mali yangu”). Israel ilipaswa kuwa chombo kwa mataifa kumjua YHWH na kuvutwa kwake. Kwa masikitiko makubwa wakashindwa (kama vile Eze. 36:22-38)
4. Katika 1 Wafalme 8 Sulemani aliliwakilisha hekalu ili wote waje kwa YHWH (kama vile 1 Fal. 8:43,60).
5. Katika Zaburi– 22:27-28; 66:4; 86:9 (Ufu. 15:4)
6. Kupitia kwa manabii wa YHWH kuendelea kudhihilisha mpango wake wa ukombozi kwa watu wote.
   a. Isaya – 2:2-4; 12:4-5; 25:6-9; 42:6,10-12; 45:22; 49:5-6; 51:4-5; 56:6-8; 60:1-3; 66:18,23
   b. Yeremia – 3:17; 4:2; 16:19
   c. Mika 4:1-3

d. Malaki 1:11

Msisitizo huu wa wote umerahisishwa na uwepo wa “agano jipya” (kama vile Yer.31:31-34; Ezek. 36:22-38), ambao unaangazia juu ya huruma ya YHWH, na sio utendaji wa mwanadamu aliyeanguka. Kuna “moyo mpya,” “mawazo mapya,” na “roho mpya.” Utii ni kitu cha muhimu lakini ni cha ndani, na sio mfumo wa nje tu (kama vile Rum. 3:21-31).

Agano Jipya linaimalisha mpango wa ukombozi wa wote kwa njia mbali mbali.

1. Agizo kuu – Mt. 28:18-20; Luka 24:46-47; Mdo. 1:8
2. Mpango wa Mungu wa milele (yaani ulio amuliwa kabla) – Luka 22:22; Mdo. 2:23; 3:18; 4:28; 13:29
3. Mungu anawataka wanadamu wote waokolewe – Yohana 3:16; 4:42; Mdo. 10:34-35; 1 Tim. 2:4-6; Tit. 2:11; 2 Pet. 3:9; 1 Yohana 2:2; 4:14
4. Kristo anaunganisha Agano la Kale na Agano Jipya – Gal. 3:28-29; Efe. 2:11-3:13; Kol. 3:11. Mipaka yote na tofauti zote za mwanadamu zimeondolewa katika Kristo. Yesu ni “fumbo la Mungu,” lililofichika lakini sasa limedhihirishwa (Efe. 2:11-3:13).

Agano Jipya linaangazia juu ya Yesu, na sio Israel. Injili, sio utaifa wala eneo la kijiografia, ni kitu cha muhimu. Israeli ilikuwa ndio ufunuo wa mwanzo lakini Yesu ni hatma ya ufunuo huo (kama vile Mt. 5:17-48).

Natumai utapata wasaa wa kusoma Mada Maalum: kwa nini ahadi za Agano la Kale zinaonekana kuwa tofauti toka ahadi za Agano Jipya. Waweza kupata katika mtandao wa www.freebiblecommentary.org.

◙**"baliwote wafikilie toba"**Tambuwa mkazo kwenye “wote," sio "baadhi" (yaani., waliochaguliwa). Kila mmoja ana kipawa cha kuchaguliwa na kristo. Tazama MADA MAALUM: TOBA KATIKA AGANO LA KALE katika Marko 1:4.

**3:10 "Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwivi"** tungo hii "siku ya Bwana" ni tungo ya Agano la kale kwa ajili ya nyakati za mwisho. Wezi mara nyingi wametumiwa kama sitiari kwa ajili ya kuijiliwa kusikotarajiwa (kama vile. Mt. 24:43-44;Luka 12:39; 1 The. 5:2; Ufu. 3:3; 16:15) na Mungu (yaani.,siku ya hukumu/kuja mara ya pili/siku ya ufufuo).

◙**"katika siku hiyo mbingu zitatoweka kwa mshindo mkuu"**hii ni dhana ya kurudia (yaani., uumbaji halisi utakoma, lakini sio neno la Mungu, kama vile. Marko 13:31; Mat. 5:18; 24:35) maelezo ya muda kitambo na uumbaji wa uhalisia (kama vile Ufu. 21:1).

**NASB** **"na mungurumo"**
**NKJV** **"na sauti kuu"**
**NRSV** **"na sauti kubwa"**
**TEV** **"na mshindo mkuu"**

Neno hili lina kidokezo cha sauti ya mvumo wa kitu kinachoenda kwa haraka angani. Ukamilisho na kusafisha enzi mpya kunakuja na sauti na nuru kama ilivyotokea enzi mpya siku ya Pentekoste (kama vile. Mdo 2:2-3).

◙**"asili"** maneno mengi yametokana na halisi, maana ya uhalisia ya upana wa sitiari.Neno hili (*stoicheia*) kiasilia linarejelea kitu kilicho kwenye mstari,mfuatano. Linatokana na vidokezo kadhaa:

1. Msingi halisi wa ujenzi wa matofari ulimwengu (hewa, maji, dunia, na moto, kama vile. 2 Pet. 3:10, 12).
2. Msingi wa somo la mafundisho (kama vile. Ebr. 5:12; 6:1 kwa ajili ya uyahudi).
3. Nguvu za injili nyuma ya mbingu (kama vile I Henoko 52:8-9; mababa wa kanisa wa mwanzo; Kol. 2:8, 20; 1 Kor. 15:24) au cheo cha malaika (a*eons*) ya walimu wa uongo wenye ujuzi (kama vile Kol. 2:10, 15 Efe. 3:10).
4. Uadui wa malaika kwa wanadamu waliojaribu kuwazuia wasifuate sheria za Musa walizopewa (kama vile. Mdo 7:38; Ebr. 2:2).
5. Inawezekana umbo la dunia iliyoanguka liliruhusu anguko la mwanadamu kuonekana wazi kutoka kwa Mungu (elimu, utawala, madawa, dini, nk., kama vile. Gal. 4:3, 8-9 na Hendrik Berkhof's *Christ and the Powers* by Herald Press,uk. 32).

◙**"vitaunguzwa,"** hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati uliopoinayomdokeza Mungu kama mwakilishi asiye na jina. Hili ni neno la kitabibu kuelezea homa kali.

**NASB "nchi na kazi zilizomo ndani yake zitateketea."**
**NKJV "nchi na kazi zilizomo kwamba zitaangamizwa"**
**NRSV "nchi na kila kilichofanywa kitaharibiwa"**
**TEV "nchi na vyote vilivyomo vitaharibiwa"**
**NJB "nchi na vyote vilivyomo vitateketea"**

Kuna machapisho mbalimbali ya kigiriki yaliyomo kwenye tungo hii.
1. "itafunuliwa" (kama vile MSS א, B, K, P)
2. "itaharibiwa" (kama vile MS $P^{72}$)
3. "itachomwa" (kama vile MS A)
4. "itafichwa" (kama vile MS C)

Hakuna andiko la asili la kigiriki la uhakika, au hata linalowezekana, kwenye tungo hii iliyotafsiriwa.

**ANDIKO NASB (LILILOBORESHWA) 2 PETRO 3:11-13**
**11 Basi, kwa kuwa vitu hivi vyote vitafumuliwa hivyo, imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenendo mtakatifu na utauwa, 12 mkitazamia hata ije siku ile ya Mungu, na kuihimiza; ambayo katika hiyo mbingu zitafumuliwa zikiungua, na viumbe vya asili vitateketea na kuyeyuka? 13 Lakini, kama ilivyo ahadi yake, mnatazamia mbingu mpya na nchi mpya, ambayo haki yakaa ndani yake.**

**3:11 " imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani "**walimu wa uongo walitilia mkazo maadili na mtindo wa maisha ya utauwa ,hivyo Petro anaendelea kusisitizia mambo haya.

◙**" mwenendo mtakatifu na utauwa"** neno "utauwa"ni dhana ya muhimu sana kwenye 2 Petro kama vile nyaraka ya kichungaji. Nimenakili muhtasari wangu kutoka 1 Tim. 4:7 (kama vile. juzuul. 9, uk. 53). 2 Petro ametumia nomino kwenye 2 Pet. 1:3,6,7 na 3:11 na kielezi kwenye 2 Pet. 2:9.

---

**Dokezo kutoka katika fasiri yangu juu ya 1 Timotheo**

◙**"utauwa"** hili ni neno la msingi kwenye nyaraka za kichungaji. Inarejelea mafundisho na maisha ya kila siku yanayohusisha injili (kama vile. 1 Tim. 3:16). Linaelezewa sio maudhui, lakini linalotarajiwa. Ni neno lililochanganywa kutoka "nzuri" (*eu*) na "kuabudu" (*sebomai*). Ibada ya kweli ni kuishi kila siku kwa maana ya kufikiri kikamilifu (kama vile. 1 Tim. 4:16a). tambuwa namba za muda dunia hii imetumia kwenye nyaraka za kichungaji:
1. nomino (*eusebeia*), 1 Tim. 2:2; 3:16; 4:7,8; 6:3,5,6,11; 2 Tim. 3:5; Tito 1:1
2. kielezi (*eusebēs*), 2 Tim. 3:12; Tito 2:12
3. kitenzi (*eusebeō*), 1 Tim. 5:4
4. neno la kusimulia*theosebeia*, 1 Tim. 2:10
5. Neno la kukanusha (mwanzo binafsi, yaani., *asebeia*), 2 Tim. 2:16; Tito 2:12

---

**3:12**
**NASB, NKJV "mkitazamia hata ije siku ile ya Mungu, na kuihimiza "**
**NRSV "mkisubiria hata ije ile siku ya Mungu na kuihimiza"**
**TEV "kama unavyosubiria siku ya Mungu inayokuja upesi tenda mema"**
**NJB "unapoendelea kuisubilia hata ije siku ya Mungu, jaribu kuihimiza kuja kwake"**

Hizi zote ni kauli tendaji endelevu ya wakati uliopo, ambazo zinaelezea muunganiko wa vipengele viwili vya ujio wa mara ya pili, hapa kwa upekee inaitwa "siku ya Mungu." Neno la kwanza kimsingi linamaanisha "kuangalia matumaini"

(kama vile. Mdo 3:5; 10:24) au "kusubilia ukiwa na hofu" (kama vile. Luka 21:26; Mdo 27:33; 28:6). Imetumika mara tatu kwenye 2 Petro 3:12,13, na 14. Waaminio wanasubilia matumaini, lakini wasio amini wanaiogopa siku hii ya kuhesabiwa.

Neno la pili lina namna mbili zinazohusiana na muundo wa kisarufi ambao unapatikana:

1. Kama ni kitenzi elekezi (yaani., tendo kupita kwenye kusudi lengwa) inamaanisha "kuhimiza," "kuwa na shauku ya" (kama vile. Tanbihi ya toleo la NRSV, ASV, NEB, NIV, Peshitta,na New Century Version, ina maana sawa na *maranatha* kanisa la mwanzo).
2. Kama ni tungo ya muundo wa kisarufi wa kitenzi kisicho elekezi (yaani, inaelezea hali au kulenga tendo la mwakilishi) inamaanisha "kuhimiza" (kama vile Luka 19:5; Mdo. 22:18). Theolojia ya matendo ya waamini inaweza kuhimiza kurudi kwa Bwana unaopatikana kwenye Mt. 6:10 (maombi) na Mdo. 3:19-20 (uamusho); Rum. 9-11 (makutano makubwa ya mataifa na wayahudi waokolewa). Katika muktadha huu maisha ya wacha Mungu waaminio wanatiwa moyo na matumaini ya karibu ya matukio ya siku za mwisho.

Haya ni maelezo magumu kwa sababu ya ufahamu wetu wa kisasa ambao umeshusha thamani kweli kinzani. Mungu ni mtawala na amepangilia tarehe ya kurudi kristo, lakini matendo ya waaminio (yaani ., maombi, mashahidi, utauwa) yumkini yakabadilisha tarehe (yaani., mapema au kuchelewa). Hiki ni kipengele cha maagano ya ukweli kibiblia ambacho huwachanganya watu wa sasa wa magharibi. Mungu anaathiriwa na watoto wake (hasi na chanya wote)! Hata hivyo, ukweli huu ni kazi ya maombi ya kusihi.

◙**"ambayo katika hiyo mbingu zitafumuliwa zikiungua, na viumbe vya asili vitateketea na kuyeyuka"** swali la kujiuliza ni, "je hizi ni dokezo za kuaminika au ni ufunuo wa siku za mwisho?" aina hii ya maelezo ya Agano la kale inafanana sawa na Isa. 10:10-13; 34:4; 51:6; Yoeli 2:28-32; Mik. 1:4. Muktadha huu unarejelea mara kadhaa muda wa huu ufalme halisi na mwisho wa dunia kuunganishwa na moto. Utaratibu huu wa kusafisha unaandaa hatua ya kiroho kwa ajili mbingu mpya na nchi mpya.itakuwa halisia (Edeni itarejeshwa) au kiroho (kama vile. 1 Kor. 15:35-58)? Ni vigumu kuelezea mwisho na uhalisia wa kiroho duniani kwa maneno ya wanadamu. Uhalisia hauwezi kuathiriwa kwa jinsi hii!

**3:13 "Lakini, kama ilivyo ahadi yake"** (kama vile. Isa. 65:17-25; 66:22-24)

◙ **"mbingu mpya na nchi mpya "(**kama vile. Isa. 11:6-9; 65:17; 66:22; Ufu.21:1-27)

◙ **"ambayo haki yakaa ndani yake "** Mungu anatamani utaratibu na watu wamfanane tabia yake (kama vile. Isa. 45:24-25). Mungu mtakatifu anataka watu watakatifu (kama vile Isa. 60:12; Mt. 5:48). Ni uumbaji mpya kwa sababu ni kinyume cha uumbaji ulioanguka (kama vile Mwa. 3).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2 PETRO 3:14-18**
**[14] Kwa hiyo, wapenzi, kwa kuwa mnatazamia mambo hayo, fanyeni bidii ili mwonekane katika amani kuwa hamna mawaa wala aibu mbele yake. [15] Nanyi uhesabuni uvumilivu wa Bwana wetu kuwa ni wokovu, kama vile na ndugu yetu mpenzi Paulo alivyowaandikia kwa hekima aliyopewa; [16] vile vile kama katika nyaraka zake zote pia, akitoa humo habari za mambo hayo; katika nyaraka hizo yamo mambo ambayo ni vigumu kuelewa nayo; na mambo hayo watu wasio na elimu, wasio imara, huyapotoa, kama vile wayapotoavyo na maandiko mengine, kwa uvunjifu wao wenyewe. [17] Basi, wapenzi mkitangulia kujua hayo, jilindeni nafsi zenu, msije mkachukuliwa na kosa la hao wahalifu mkaanguka na kuuacha uthibitifu wenu. [18] Lakini, kueni katika neema, na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo. Utukufu una yeye sasa na hata milele.Amina**

**3:14 "fanyeni bidii ili mwonekane katika amani"** Hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopita usio timilifu, ambayo inatilia mkazo haraka. Waaminio wanalazimika kuishi maisha ya uchaji Mungu. Lazima kuwe na Agano lifaalo linaloitikia upendo wa Mungu.

Kitenzi cha pili ni kauli tendwa ya kitenzi jina ya wakati uliopita usio timilifu. Ni dhahili inarejelea "siku ya Mungu" kwenye 2 Pet. 3:12. Yesu mara nyingi alitumia picha ya waaminio kama watumishi waliowekwa katika nchi na Bwana wao. Ni lazima wawe tayali muda wowote kwa ajili ya ujio wake na kwamba muda waliopewa ni kwa ajili ya utumishi wao (kama vile Marko 13:33- 37; Luka 18:8).

Amani pekee inawezekana ikiwa (1) mtu ataitikia na kuipokea injili ; (2) mtu ataufahamu ujumbe wa injili; na (3) mtu kila siku ataishi nje ya injili. Waalimu wa uongo na wafuasi wao wameshindwa kwenye hayo maeneo matatu na hawana amani!

◙ **"hamna mawaa wala aibu "** tungo hii imetumika kwenye 1 Petro 1:19 kumrejelea Kristo (kama vile. Yn 8:46; 14:30; Luka 23:41; 2 Kor. 5:21; Ebr. 4:15; 7:26-27; 1 Pet. 2:22; 3:18; 1 Yn 2:2; 4:14). Ni sitiari ya Agano la kale iliyoelezea wanyama safi wa sadaka ya kuteketezwa (kama vile. Law. 22:19-20). Tunaishi kwenye nuru ya (1) mfano wa Kristo, (2) amri za Kristo, na (3) ujio wa Kristo!

**3:15**

| | |
|---|---|
| **NASB, NRSV** | **"angalia uvumilivu wa Bwana wetu ni wokovu"** |
| **NKJV** | **"na hesabuni kwamba uvumilivu wa Bwana wetu ni wokovu"** |
| **TEV** | **"angalia uvumilivu wa Bwana wetu kama nafasi aliyokupa uokolewe"** |
| **NJB** | **"fikilia uvumilivu wa Bwana wetu kama nafasi yako ya kuokolewa"** |

Hii inamrejelea nani (1) wakristo wote ambao tayari wameokolewa au (2) wasiomcha Mungu na waalimu wa uongo waasi na wafuasi wao? Ni dhahiri inatazama nyuma uvumilivu wa Mungu kwenye 2 Pet. 3:9. Wengine wamechukulia rehema za Mungu kwa manufaa ya kutenda dhambi na kuishi maisha ya ubinafsi. Wengine wameshikilia msamaha wa Mungu na kufuatisha tabia yake.

◙ **"kama vile na ndugu yetu mpenzi Paulo "**tungo hii kwa dhahili inaonyesha kwamba hakuna mashaka kati ya Paulo na Petro. Kila mmoja alimtambua mwenzake kwa kumuita na kumpa zawadi mwingine (kama vile. Gal. 2: 7-10). Jambo hili limeandikwa kwenye Gal. 2:11-21 halikusababisha nafasi ya kudumu kwao.

◙ **"alivyowaandikia"**haina mashaka kwamba nyaraka za Paulo zilimrejelea nani.kama wapokeaji (Asia ndogo) ni sawa na kama 1 Petro na Paulo aliandika kitabu cha Wagalatia kwa kundi la kaskazini mwa makanisa ya Asia ndogo, hivyo kitabu cha wagalatia kiliandikwa mapema sawa na mahali ambapo 2 Petro iliandikwa, na inawezekana chaguo bora ni Wagalatia. Lakini kwa uhakika hatufahamu.

Chaguo namba mbili ni kwamba tangu mada nzima ya sura hii ni ujio wa pili, hivyo inawezekana nyaraka ya mwanzo ya Paulo kwa Wathesalonike ilikuwa inarejelea hilo. Chaguo la tatu ni kwamba baadhi ya sehemu ya Warumi inakisia inafaa kwa asili kama nyaraka inayojirudia. Kwangu mimi Wagalatia au Warumi,ambavyo ni vitabu vya kitheolojia vya Paulo vilivyobobea kwenye wokovu zaidi, inawezekana ni vya kusifiwa zaidi.

**3:16 "vile vile kama katika nyaraka zake zote pia"** uhakiki zaidi wa 2 Petro ulioandikwa na mtume Petro unasimulia hii rejea ya nyaraka za Paulo. Ni kweli kwamba nyaraka zote za Paulo zilikusanywa pamoja kwa jina "mtume", lakini hili lilifanyika baadae baada ya kifo cha Petro chini ya utawala wa Nero (64-68 B.K).
Hata hivyo, andiko hili halitetei kwamba ni nyaraka ngapi za Paulo zinaongelea hilo, wala rejea hii haidokezi mzunguko wa maandishi yote mwandishi.

◙ **"akitoa humo habari za mambo hayo; katika nyaraka hizo yamo mambo ambayo ni vigumu kuelewa nayo"** mambo gani?(1) Ufunuo (kama vile. 2 Pet. 3:2); (2) siku za mwisho (2 Pet. 3:3-4a); (3) uumbaji (2 Pet. 3:4b-5); (4) gharika ya Nuhu (2 Pet. 3:6); (5) siku ya hukumu (2 Pet. 3:7,10); (6) wakati wa Mungu (2 Pet. 3:9); (7) ujio mara ya pili (2 Pet. 3:12); (8) enzi mpya ya haki (2 Pet. 3:12-13); (9) wokovu binafsi (2 Pet. 3:14a, 15a); (10) maisha ya uchaji Mungu (2 Pet. 3:11,14b); au (11) mambo ya sura ya kwanza au ya pili?

Kwa vyovyote ni walimu wa uongo wasioelewa na kuyapopotoa kwa ajili ya maangamizi yao. Kwa maana hii inawezekana mkazo wa Paulo kwenye wokovu kama kipawa toka kwa Mungu kwa mwanadamu atendae haki (yaani.,haki kwa imani). Inawezekana kwamba Yakobo (kama vile. Yakobo 2:14-26) inakusanya baadhi ya mahubiri ya Paulo ambayo ni magumu kueleweka.

◙ **“wasio na elimu, wasio imara, huyapotoa, kama vile wayapotoavyo na maandiko mengine "**Inanisaidia mimi kutambua kwamba mitume ambao walitembea na Yesu kwa ukaribu zaidi kwa miaka kadhaa mara zote hawakumfahamu (kama vile. Marko 9:32; Luka 2:50; 9:45; 18:34; Yn 2:22; 10:6; 12:16; 16:18). Si mitume wote waliyaelewa maandiko ya mitume wengine. Tumeitwa tuwe mashahidi wa imani na wacha Mungu ndugu wa maagano! Hakuna hata mmoja wetu anaefahamu mambo yote.

Kwenye Agano la kale neno “maandiko” mara zote linarejelea kwenye Agano la kale. Agano jipya halikukamiliki na kukusanywa hadi mwisho wa karne ya kwanza. Maandiko mengi yanayofanana yenye uvuvio na kutumainika yanarejelea katika Agano la kale(kama vile. Mt. 5:17-19; 1 Kor. 2:9-13; 1 The. 2:13; 2 Tim. 3:16; 1 Pet. 1:23-25; 2 Pet. 1:20-21).

Hii ni sehemu mojawapo chache kwenye Agano jipya ambapo maandishi yapo sawa na maandiko ya Agano la kale. Petro anathibitisha uvuvio wa Paulo na mamlaka ya maandishi yake kwa tungo hii.

◙ **"kwa uvunjifu wao wenyewe "** biblia ni ufunuo pekee wa Mungu kwa ulimwengu wa waliopotea na wahitaji. Wanadamu watenda maouvu (yaani .,walimu wa uongo) wakijilaghai kwa kuangamizwa kwao. Hukumu inakuja; Yesu pekee ndiye tumaini; kila mmoja atasimama mbele za Mungu siku moja!

**3:17 "mkitangulia kujua hayo "** walimu wa uongo mara zote wapo! Viongozi wanakua na mashaka juu ya walimu wa uongo kutuyatumia maandiko (yaani.,Agano la kale) na maandishi ya mitume (kama vile. 2 Pet. 3:2). Kuna njia kadhaa za kibiblia za kumtofautisha mwalimu wa uongo.

1. Ishara au maajabu, lakini kwa jina miungu wengine (Kumb. 13:1-5)
2. Unabii wa kweli wa siku zijazo,lakini kwa jina la miungu wengine (Kumb. 18:18-22)
3. Mtindo wa maisha (Mt. 7; Yakobo, 1 Yn, na 2 Petro)
4. Miujiza sio ishara ya moja kwa moja ya Mungu (Mt. 24:24)
5. ujumbe lazima umlenge kristo (1 Yn 4:1-6)
6. Kutafsiri vibaya ufunuo wa Mungu (2 Pet. 3:2)

◙ **“jilindeni nafsi zenu”** hii ni kauli ya kati shurutishi ya wakati uliopo. Hili ni neno la kijeshi kama 1 Petro 1:4.
Waaminio wanawajibika binafsi kuendelea kuangalia na kutathimini juu ya kile wengine wanaongea kumhusu Mungu/Kristo. Kuna wadanganyifu ndani yake na wasiokuwa na ushirika (kama vile Efe. 4:14; 6:11-12).usiwe mchanga kiroho!

◙ **“msije mkachukuliwa”** hii ni kauli tendwa endelevu ya wakati uliopita usio timilifu. Ni kinyume cha neno la kwenye Agano la kale kwa ajili ya imani lenye maana ya miguu imara (yaani., kutumanika au thabiti). Hili ni sawa na neno lililoerezewa kwenye matendo ya Petro mwenyewe katika Gal. 2:13.

**3:18 " Lakini, kueni katika neema, na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo "** hii ni kauli tendaji shurutishi ya wakati uliopo. Ni dhamira ya kati ya kitabu. Waaminio wawe tahadhari dhidi ya makosa kwa kukua katika maarifa ya injili na kuishi kinyume na injili. Hii inafanana na Yuda 20.

◙ **“Utukufu una yeye "** tungo hii imetumika kwa Mungu Baba mwenye nguvu (tazama muhtasari katika 1 Pet. 4:11,
kama vile. Yuda; 2 Pet. 3:24-25), lakini mara chache kwa Yesu (kama vile. 2 Tim. 4:18; 2 Pet. 3:18; Ufu. 1:6).

Kwenye Agano la kale neno kuu la Kiebrania “utukufu” (*kbd*) asili yake ni neno la manufaa ambalo linarejelea mizani miwili na linamaanisha “kuwa nzito”. Kwamba uzito ulikuwa na thamani au thamani asilia. Mara nyingi dhana ya uchangamfu inaongezwa ili kuelezea utukufu wa Mungu (kama vile. Kut. 19:16-18; 24:17; Isa. 60:12). Yeye pekee ni wa thamani na mtukufu. Yeye pia ni mng’ao kwa ajili kumshikilia mwanadamu aliyeanguka dhambini (kama vile. Kut. 33:17-23; Isa. 6:5). Mungu anaweza kuwa ukweli pekee uliojulikana kupitia kwa Kristo (kama vile. Yer. 1:14; Mt. 17:2; Ebr. 1:3; Yak 2:1).

Neno utukufu lina utata kidogo.

1. Yumkini likafanana na “haki ya Mungu”
2. Yumkini likarejelea utakatifu au ukamilifu wa Mungu

3. Linaweza kurejelea sura ya Mungu ambayo kwayo mwanadamu aliumbwa (kama vile Mwa. 1:26-27; 5:1; 9:6), lakini ambayo baadae ilitiwa dosari kupitia uasi (kama vile. Mwa. 3:1-22)

Limetumika kwa mara ya kwanza kama uwepo wa YHWH na watu wake kwenye Kut. 16:7,10; Law. 9:23; Hes. 14:10.

**NASB, NRSV "yeye sasa na hata milele "**
**NKJV "yeye na hata milele"**
**TEV "sasa na hata milele"**
**NJB "kwa wakati na milele"**

Hii ni kawaida "yeye sasa na milele." Ni muundo wa kipekee wa mwisho, unaofanana na Yuda 1:25. Wayahudi aliangalia historia katika enzi mbili, enzi ya mwovu na ujio wa enzi ya haki. Ujio wa enzi hii ni kisawe chenye ufalme wa milele. Tazama mada maalumu katika Marko 13:8.

◙ **"Amina"** neno hili halionekani kwenye machapisho ya kale ya Kigiriki B (yaani, Vaticanus),lakini linaonekana kwenye matoleo ya $P^{72}$, א, A, na C. tazama mada maalumu katika Marko 3:28.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa fasiri, inamaanisha kwamba una wajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Kwa nini wenye ujuzi wanakataa ujio wa pili?
2. Ni nini msingi mkuu wa ujumbe wa Agano jipya unaohusisha ujio wa pili?
3. Kwa nini Petro ametaja maandiko ya Paulo?

# TAFASIRI SAHIHI ZA ISTILAHI ZA VISARUFI VYA KIYUNANI

Lugha ya kawaida ya Koine mara nyingi inafahamika kama Kiyunani kilichobobea, ilikuwa ni lugha ya kawaida ya ulimwengu wa Meditarania ilianzishwa na Alexanda mkuu (336-323 B.K) na ikadumu mpaka miaka ya (300 K.K-B.K 500). Haikuwa rahisi, Kiyunani kuwa cha daraja la juu, lakini kwa njia nyingi ni dhana ya Kiyunani ambayo ilikuja kuwa lugha ya pili karibu na mashariki ya kale na ulimwengu wa Mediterania.

Kiyunani cha Agano Jipya kilikuwa ni cha kipekee kwa njia kadhaa kwa watumiaji wake, isipokuwa Luka mwandishi wa kitabu cha Waebrania, yamkini alitumia lugha ya Kiarama kama lugha ya msingi. Kwa hiyo, uandishi wao uliathiliwa na dhana ya muundo wa Kiarama. Pia, walisoma na kunukuu wandishi wa maandiko ya kale (tafasiri ya Kiyunani ya maandiko ya kale) ambayo pia yaliandikwa kwa lugha ya Koine. Lakini maandiko ya kale pia yaliandikwa kwa wasomi wa Kiyahudi ambao lugha yao ya asili ilikuwa sio ya Kiyunani.

Hii ilisaidia kuwa kama kumbukumbu ambayo haiwezi kulipeleka Agano Jipya kwenye muundo mgumu wa kisarufi. Ni wa kipekee na bado una mambo mengi yaliyo pamoja na (1) maandiko ya kale (2) maandiko ya kale kama yale ya Yusufu na (3) mafunjo yaliyopatikana Misri. Kwa hiyo tunakabilianaje na uchambuzi wa visarufi vya Agano Jipya.

Muundo wa kisarufi wa lugha ya Koine na Agano Jipya la lugha ya Koine ulibadilika. Kwa njia tofauti ulikuwa ni urahisishaji wa sarufi. Mazingira ndio yatakuwa mwongozo wetu mkuu. Maneno pekee yana maana katika upanuzi wa mazingira, kwa hiyo, muundo wa kisarufi unaweza tu kueleweka katika mwanga wa (1) aina mahsusi ya mwandishi, na (2) mazingira mahsusi

Hapana hitimisho la fasiri ya dhana na muundo wa Kiyunani unaowezekana. Kimsingi lugha ya Koine ilikuwa ni lugha ya maneno tu. Mara nyingi msingi wa utafasiri ni aina na dhana ya maneno. Mara nyingi vishazi vikuu hutokea kwanza, vikionyesha kushinda vingine vyote. Katika kueleza kitenzi cha Kiyunani, vipande vitatu vya habari lazima vizingatiwe (1) kiini cha msisitizo wa njeo, sauti na dhamira (tukio au umbo); (2) kiini cha maana husika ya kitenzi (usawidi kamusi); na (3) mtiririko wa mazingira yenyewe (isimu ya mpangilio wa maneno)

I. NJEO

A. NJEO au sura inajumuisha uhusiano wa VITENZI ili kukamilisha kitendo au kutokamilisha kitendo. Mara nyingi huitwa "utimilifu" au "utoutimilifu"
   1. Njeo timilifu zinaangazia juu ya utoaji wa kitendo. Hakuna taarifa nyingine zilizotolewa isipokuwa ya kile kilichotokea! Kuanza kwake, mwendelezo au ukomo wake haukueiezwa.
   2. Njeo zisizo timilifu zinaangazia juu ya mchakato endelevu wa kitendo. Zinaweza kuelezewa dhidi ya unasaba wa kitendo, kudumu kwa kitendo, mwendelezo wa kitendo, n.k.

B. Njeo zaweza kugawanywa kwa jinsi mwandishi anavyoona kitendo kinavyoendelea.
   1. Kimetokea-KITENZI TIMILIFU
   2. Kilivyotokea au matokeo yake-KITENZI CHA WAKATI ULIOPITA
   3. Kilivyokuwa kikitokea nyuma na matokeo yake yakastahimili, lakini sio sasa-KITENZI CHA WAKATI ULIOPITA TIMILIFU
   4. Kinatokea –WAKATI ULIOPO
   5. Kilikuwa kikitokea- WAKATI USIOTIMILIFU
   6. Kitatokea –WAKATI UJAO

Mfano thabiti wa jinsi njeo hizi zinasaidia katika utafasiri ungalikuwa wa neno "okoa." Lilitumika katika NJEO nyingi tofauti kuonyesha kwa pamoja mchakato na ukomo.

1. KITENZI CHA WAKATI TIMILIFU- "okolewa" (Rum 8:24)
2. KITENZI CHA WAKATI ULIOPITA- "ameokolewa na matokeo yake yanaendelea" (Efe 2:5,8)

3. KITENZI CHA WAKATI ULIOPO- “anaokolewa” (kama vile 1Kor 1:18; 15:2)
4. KITENZI CHA WAKATI UJAO- “ataokolewa” (kama vile Rum 5:9,10; 10:9)

C. Katika kuzingatia juu ya VITENZI VYA NJEO, mfasiri huangalia sababu za mwandishi wa kwanza alichagua kuelezea yeye binafsi NJEO fulani. Tarajio la NJEO “hakuna madoido” lilikuwa ni la KITENZI CHA WAKATI TIMILIFU. Kilikuwa ni muundo wa KITENZI cha kawaida “kisichoainishwa” “kisichotambulika” “kisichochoka.” Chaweza tumika katika Nyanja pana ambamo mazingira lazima yaelezee. Kwa kawaida kilikuwa kinaelezea kuwa kitu fulani kimetendeka. Sura ya muda uliopita ulikusudia tu katika DHAMIRA ELEKEZI. Kama pana NJEO nyingine zilizotumika, uainishaji wa kitu fulani ulikuwa unasisitizwa. Lakini ni nini?
   1. NJEO YA WAKATI ULIOPITA. Hii inaongelea juu ya tendo lililokwisha tendeka na matokeo yakiendelea kuwepo. Katika namna fulani ilikuwa ni muunganikano wa NJEO ZA WAKATI TIMILIFU na ZA WAKATI ULIOPITA. Mara kwa mara mlengo ulikuwa juu ya matokeo yalioendelea kuwepo au kumalizika kwa kitendo. Mfano: Efe 2:5 & 8, “umekuwa na unaendelea kuokolewa.”
   2. NJEO YA WAKATI ULIOPITA AINISHI. Hii ilikuwa kama njeo ya WAKATI ULIOPITA isipokuwa matokeo yalishakoma. Mfano: “Petro alikuwa akisimama nje mlangoni” (Yoh 18:16)
   3. NJEO YA WAKATI ULIOPO. Hii inazungumzia juu ya kitendo kisichokiwisha au kisichotimilifu. Mtizamo mara nyingi ni juu ya uendelezaji wa tukio. Mfano: “kila mmoja ashikamanae ndani yake haendelei kutenda dhambi”, “kila mmoja aliyesamehewa na Mungu haendelei kutenda dhambi” (1Yoh 3:6 & 9).
   4. NJEO YA WAKATI USIOTIMILIFU. Katika njeo hii uhusiano na NJEO YA WAKATI ULIOPO ni mwendelezo wa uhusiano kati ya WAKATI ULIOPITA na WAKATI ULIOPITA AINISHI. WAKATI USIOTIMILIFU unaongea juu ya kitendo ambacho hakijaisha kutendeka ambacho kilikuwa kinatokea lakini sasa kimekoma au mwanzo wa kitendo awali. Mfano: “kwa hiyo Yerusalemu yote waliendelea kumwacha” au “ Yerusalemu yote wakaanza kumwacha”(Mt3:5)
   5. NJEO YA WAKATI UJAO. Hii inaongelea juu ya kitendo ambacho kawaida kilijitokeza ndani ya muda mwafaka. Inaangazia juu ya umuhimu wa jambo kutokea kuliko utokeaji wa uhalisia. Mara nyingi unazungumzia juu ya ualakini wa tukio. Mfano: “Heri wale….wata...”(Mt 5:4-9).

II IRABU

A. Irabu inaelezea mahusiano kati ya kitendo cha KITENZI na KIIMA
B. IRABU TENDAJI ilikuwa ni njia ya kawaida, tarajiwa, isiosisitiza utetezi wa kwamba kiima kilikuwa kikitenda kitendo cha KITENZI.
C. IRABU TENDEWA ina maana kuwa KIIMA kilikuwa kikipokea kitendo cha KITENZI kilichotolewa na mtu wan je. Mtu wa nje anayetoa kitendo alionyeshwa katika Agano Jipya la Kiyunani kwa mambo na VIHUSISHI vifuatavyo:
   1. Mtu binafsi wa moja kwa moja wa *hupo* kukiwa na UHUSIKA WA KUONDOA (cf. Mt 1:22; Mdo 22:30)
   2. Mtu binafsi wa kati na *dia* kukiwa na UHUSIKA WA KUONDOA (cf. Mt 1:22)
   3. Mtu wa kawaida asiyehusika na *en* kukiwa na UHUSIKA WA JAMBO
   4. Wakati mwingine ni mtu binafsi au asiyehusika kukiwa na UHUSIKA WA JAMBO pekee.
D. IRABU YA KATI inamaanisha kuwa KIIMA kinatoa tendo la KITENZI na pia moja kwa moja kinahusishwa katika kitendo cha KITENZI. Mara nyingi huitwa irabu ya kurefusha matakwa binafsi. Muundo huu unasisitizia KIIMA cha kishazi au sentesi kwa namna nyingine. Muunganikano huu haupatikani katika Kiingereza. Una uwezekano mpana wa maana na ufasiri katika Kiyunani. Baadhi ya mifano ya dhana hizi ni;
   1. YENYE KUJIREJEA – kitendo cha moja kwa moja cha kiima chenyewe. Mfano: “kajiangika mwenyewe” (Mt 27:5)
   2. YENYE KUTIA MKAZO- kiima kinazaa kitendo chake chenyewe. Mfano: “shetani mwenyewe anajifanya kama malaika wa nuru” ( 2Kor 11:14)
   3. Kukubaliana – mwingiliano wa viima viwili. Mfano: “walishauliana wao kwa wao” (Mt 26:4)

III. DHAMIRA (au "NAMNA")

A. Kuna namna nne za DHAMIRA katika lugha ya Koine. Zinaashiria uhusiano wa KITENZI kuwa kweli, haswa ndani ya wazo la mwandishi mwenyewe. DHAMIRA hizi zinagawanyika katika namna pana mbili: ile inayoonyesha ukweli (ELEKEZI) na ile inayoonyesha umuhimu (UTEGEMEZI, KUAMURU/KUSHURUTISHA na HALI Y A UCHAGUZI).
B. DHAMIRA ELEKEZI ilikuwa ni NAMNA ya kawaida ya kuelekeza kitendo ambacho kimekwisha tokea au kilikuwa kinatokea, haswa kwenye wazo la mwandishi. Ilikuwa namna pekee ya Kiyunani ya kueleza ukomo wa muda na hata hapa sura hii ilikuwa daraja la pili.
C. DHAMIRA TEGEMEZI kinaelekeza yumkini kitendo kitakachotokea mbeleni. Kitu fulani ambacho hakijawahi tokea lakini nafasi ya kutokea ingaliwezekana. Ina vitu vingi vinavyofanana na KITENZI CHA WAKATI UJAO ELEKEZI. Utofauti ni kuwa UTEGEMEZI unaelezea kiwango fulani cha mashaka. Katika Kiingereza hii mara nyingi inaelezewa na neno "ingalikuwa", "ingaliweza", "yawezekana" au "yenye uwezo".
D. DHAMIRA YA UCHAGUZI inaelezea utashi ambao kinadharia unawezekana. Ilifikiliwa ni hatua moja mbele kutoka katika ukweli kuliko HALI YA UTEGEMEZI. HALI YA UCHAGUZI inaelezea uwezekano chini ya hali fulani. HALI YA UCHAGUZI ilikuwa ni nadra katika Agano Jipya. Utumikaji wake mara nyingi kilikuwa ni kifungu maarufu cha Paulo. "yawezekana isiwe" (KJV, Mungu anakataza), kimetumika mara kumi na tano (kama vile Rum 3:4,6,31; 6:2,15; 7:7,13; 9:14; 11:1,11; 1Kor 6:15; Gal 2:17; 3:21; 6:14) mfano mwingine unapatikana katika Thes 1:38, 20:16, Mdo. 8:20 na 1Thes 3:11
E. DHAMIRA SHURUTISHI inasisitizia juu ya amri ambayo iliwezekana, lakini msisitizo ulikuwa juu ya dhamira ya mnenaji. Inatetea juu ya uwezekano wa hiari na ilishurutishwa juu ya chaguzi za wengine. Kulikuwa na matumizi ya kipekee ya HALI YA KUSHURUTISHA katika maombi na hitaji la mtu wa tatu. Amri hizi zinapatikana tu katika WAKATI ULIOPO na njeo ya WAKATI TIMILIFU katika Agano Jipya.
F. Baadhi ya visarufi vinabainisha VIAMBATA kama moja aina ya NAMNA. Ni vya kawaida katika Agano Jipya la Kiyunani, mara nyingi vikielezewa kama KIVUMISHI CHA TENDO. Vinatafasiriwa kama muunganiko wa VITENZI vikuu ambavyo vinafanana. Tofauti pana iliwezekana katika utafasiri wa viambata. Ni vizuri kuzirejea tafasiri nyingi za Kiingereza. *The Bible in Twenty Six Translation* kilichochapishwa na Baker ni msaada mkubwa hapa.
G. KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI kilikuwa ni njia ya kawaida au "kisichotambulika" cha Kuingiza matokeo. Njeo nyingine, irabu au zilikuwa na ufasiri mahususi ambao mwandishi wa kwanza alihitaji kuwasilisha.

IV. Kwa mtu ambaye hayuko na uzoefu na lugha ya kiyunani, msaada wa usomaji unaofuata utatoa taarifa inayohitajika;

A. Friberg, Barbara na Timothy. Analytical Greek New Testament. Grand Rapids: Baker 1988
B. Marshall, Alfred. Interlinear Greek-English New Testament. Grand Rapids: Zondervan 1976
C. Mounce, William D. The Analytical Lexicon to the Greek New Testament. Grand Rapids: Zondervan 1993
D. Summer Ray. Essential of the New Testament Greek Nashville: Broadman 1950
E. Kitaaluma mtangamano wa kozi ya lugha ya Koine unapatikana kupitia taasisi ya Moody Bible iliyoko Chikago II

V. NOMINO

A. Ki-isimu, NOMINO zinaainishwa kwa jambo. Jambo ni lile lililoshurutisha dhana ya NOMINO ambayo ilionyesha kuwa na uhusiano na KITENZI na sehemu nyingine ya sentesi. Katika lugha ya Koine kazi nyingi za uhusika zilionyeshwa na VIHUSISHI. Tangu dhana ya uhusika iliweza kutambua tofauti ya mahusiano mbali mbali, VIHUSISHI vilitokea kutoa utengano mzuri wa kazi hizo.
B. Uhusika wa Kiyunani uliainishwa kwa njia nane zifuatazo;
   1. UHUSIKA WA KIIMA ulitumika kwa ajili ya kutaja na kawaida kilikuwa ni kiima cha sentesi au kishazi. Pia ilitumika kwa NOMINO ARIFU na VIVUMISHI vikiunganishwa na VITENZI "kuwa" au "kufaa"

2. UHUSIKA MILIKISHI ulitumika kwa ajili ya kuelezea na kawaida ulitoa kivumishi au thamani ya nenolililofanana nalo. Ulijibu swali, “aina gani?” mara nyingi ulielezewa na utumiaji wa KIHUSISHI cha Kiingereza “ya/za”
3. UHUSIKA WA KUONDOA ulitumia dhana ile ile ya kushurutisha kama ya UMILIKISHI, lakini ulitumika kuelezea utenganifu. Kawaida ulidokeza utengano wa alama kwenye muda, nafasi, kiini, chanzo au degrii. Mara nyingi ulielezewa na matumizi ya KIHUSISHI cha Kiingereza “kutoka”.
4. UHUSIKA WA WAKATI ulitumika kuelezea matwaka ya mtu binafsi. Hii ingalidokeza mtizamo chanya au hasi. Mara nyingi hiki kilikuwa si kitu cha moja kwa moja. Mara nyingi ulielezewa na KIHUSISHI cha Kiingereza “ya”.
5. UHUSIKA WA MAHALI ilikuwa dhana shurutishi ya WAKATI, lakini ilielezea mahali au eneo kwenye nafasi, muda au ukomo. Mara nyingi ulielezewa na KIHUSISHI cha Kiingereza “ndani, juu, ni, kati, kwa, juu ya na mbali na”
6. UHUSIKA WA KUTUMIKA ilikuwa ni dhana shurutishi kama uhusika wa WAKATI na MAHALI. Unaelezea namna au uhusiano. Mara nyingi ulielezewa na KIHUSISHI cha Kiingereza cha neno “kwa” au “enye”
7. UHUSIKA WA KUSHUTUMU ulihusika kuelezea hitimisho la kitendo. Unaelwzea ukomo. Haswa utumikaji wake ulikuwa kwenye dhana ya moja kwa moja. Ulijibu maswali “kwa umbali gani” au “kwa namna gani”
8. UHUSIKA WA KAULI ulitumika kuelezea moja kwa moja.

VI. VIUNGO NA VIUNGANISHO

A. Kiyunani ni lugha sahihi kwa sababu ina viunganishi vingi. Viunganisho fikra ( vishazi, sentesi na aya). Ni vya kawaida kwamba utouwepo wao mara nyingi unakuzwa. Kama jambo la uhakika, viunganisho na viungo hivi vinaonyesha muelekeo wa fikra za mwandishi. Mara nyingi ni vya maana kupima ni kipi haswa anajaribu kukiwakilisha.

B. Hapa pan orodha ya baadhi ya viunganishi na viungo na maana zake (taarifa hizi zimekusanywa haswa toka kwa H.E Dana na Julius K. Mantery. A Manual Grammar of the Greek New Testament

1. Viunganishi vya wakati
   (a) *epei, epedē,hopote, hōs, hote, hotan (*TEGEMEZI)- “lini”
   (b) *heōs- “*wakati”
   (c) *hotan, epan (*TEGEMEZI)- “kila, wakati wowote”
   (d) *heōs, achri, mechri (*Tegemezi)- “mpaka”
      a. *priv (*kitenzijina)- “kabla”
      b. *hōs-* “tangu”, “lini”, “kama”.
2. Viunganishi venye mantiki
   a. Kusudi/dhumuni
      1) *hina* (TEGEMEZI) *hopōs (*TEGEMEZI) *hōs-* “ya kwamba”, “kuwa”
      2) *hōste(*KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO)- “kuwa”
      3) *pros(*KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO) au *eis* (KIUNGO SHUTUMU KISICHO NA UKOMO)- “kuwa”
   b. Tokeo (kuna uhusiano wa karibu kati ya kusudio la dhana ya kisarufi na tokeo)
      (1) *hōste(*ISIYO NA KIKOMO, hasa hiki ni cha kawaida)- “ili kwamba”, “hivyo”
      (2) *hiva(*TEGEMEZI)- “ya kwamba”
      (3) *ara-* “kwa kiasi hicho”
   c. Chanzo au sababu
      1) *gar(*chanzo/athari au sababu/hitimisho)- “kwa”, “kwa sababu ya”
      2) *dioti, hotiy- “*kwa sababu ya”

3) *epei, epeidē, hōs*- "tangu"
4) *dia(*ikiwa na SHUTUMA) na (ikiwa na KIUNGO KISICHO NA UKOMO)- "kwa sababu ya"

d. Maamuzi
   (1) *ara, poinun, hōste*- "kwa hiyo"
   (2) *dio(*KIUNGO HITIMISHO chenye nguvu)- "kwa sababu ipi", "kwa nini", "kwa hiyo basi"
   (3) *oun- "*kwa hiyo basi", "kwa kiasi hicho", "hatimaye", "hivyo basi"
   (4) *tinoun*- "kufuatana na"

e. –a kinyume au tofauti
   (1) *alla(* yenye KINYUME thabiti)-"lakini", "isipokuwa"
   (2) *de- "*lakini", "ingawa", "bado", "kwa upande mwingine"
   (3) *kai- "lakini"*
   (4) *mentoi, oun- "ingawa"*
   (5) *plēn*- "hata hivyo" (haswa katika Luka)
   (6) *oun- "ingawa"*

f. Ulinganifu
   (1) *hōs,kathōs (*ingiza vishazi linganifu)
   (2) *kata(*kwa muunganiko, *katho, kathoti, kathōsper, kathaper)*
   (3) *hasos(*katika Kiebrania)
   (4) *ē- "kuliko"*

g. Enye mlolongo au mtiririko
   (1) *de- "*na", "sasa"
   (2) *kai- "*na"
   (3) *tei*- "na"
   (4) *hina, oun- "*kile"
   (5) *oun- "*kasha"(katika Yohana)

3. Matumizi yenye mkazo
   a. *alla- "*kwa hakika", "naam", "kwa kweli"
   b. *ara- "*hakika", agharabu", "kweli"
   c. *gar- "*lakini kweli", "agharabu", "hakika"
   d. *de- "*hakika"
   e. *ean- "*hata"
   f. *kai*- "hata", "hakika", "kweli"
   g. *mentoi- "*hakika"
   h. *oun*- "kweli", "kwa hali zote"

VII.

A. SENTESI SHURUTISHI ni ile iliyo na kishazi kimoja au zaidi. Muundo huu wa kisarufi unaongeza utafasiri kwa sababu unatoa amri, sababu au chanzo kwa nini kitendo cha KITENZI kikuu kimetokea au hakikutokea. Palikuwa na aina nne za sentesi shurutishi. Zilitoka kwa zile zilizofikiriwa kuwa kweli toka kwa mtizamo wa mwandishi au kwa kusudio lake kwa lile alilokuwa na utashi nalo.

B. SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA KWANZA ilielezea kitendo au kile kilichofikiliwa kuwa kweli toka kwa mtimamo wa mwandishi au kusudio lake. Ingawa ilielezewa kwa neno "kama." Katika mazingira tofauti lingeweza kutafasiriwa "tangu"(cf. Mt 4:3, Rum 8:31). Ingawa hii haimaanishi kudokeza kuwa MADARAJA YA KWANZA yote ni ya kweli. Mara nyingi yalitumika kuweka alama kwenye hoja au kuangazia kosa(cf. Mt 12:27)

C. SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA PILI mara nyingi huitwa “inayopingana na ukweli”. Inaelezea kitu ambacho kilikuwa ni cha uongo kwenye ukweli wa kufanya jambo. Mfano:
   1. “kama kweli alikuwa nabii, ambapo sio, alikuwa sasa nani na mwanamke wa tabia gani anaye mng’ang’ania yeye, lakini hawezi (Thess 7:39)
   2. Kama kweli Musa, lakini hamkumwamini, mngaliniamini na mimi lakini hamkuniamini (Yoh 5:46)
   3. Kama ningalitaka kuwapendezesha wanadamu lakini sivyo, nisingalikuwa mtumwa wa Christo hata sasa(Gal 1:10)

D. DARAJA LA TATU linaongelea juu ya tukio lijalo ambalo laweza kutokea. Mara nyingi unafikirika uwezekanao wa kitendo kutokea. Kawaida inaashiria tahadhari. Kitendo cha KITENZI kikuu ni tahadhari juu ya tendo la kishazi “hiki”. Mfano toka 1Yoh 1:6-10; 2:4,6,9,15,20,21,24,29; 4:20; 5:14,16

E. DARAJA LA NNE ni daraja la mbali lililoondolewa kwenye uhakika. Ni adimu katika Agano Jipya. Kama jambo la kweli, hakuna SENTESI SHURUTISHI DARAJA LA NNE lililokamilika ambamo pande zote za jambo zinastahili maelezo. Mfano wa DARAJA LA NNE ni ufunguzi wa kishazi katika 1Pet 3:14. Mfano wa sehemu DARAJA LA NNE ni katika kuhitimisha kishazi katika Mdo 8:31.

VIII. VIZUIZI

A. KITENZI CHA KUAMURU CHA WAKATI ULIOPO kikiwa na KIAMBATA MĒ mara nyingi (lakini hakitengwi) kina msisitizo wa kusimamisha tendo ambalo liko kwenye mchakato. Baadhi ya mifano: “msijiwekee hazina yenu duniani………….”(Mt 6:19); “msisumbukie maisha yenu……….” ( Mt 6:25); “wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi…….”(Rum 6:13); “wala msimhuzunishe Yule Roho Mtakatifu wa Mungu (Efe 4:30) na “tena msilewe kwa mvinyo…………………”(Ef 5:18)

B. KITENZI TEGEMEZI TIMILIFU kina mkazo wa “udhahanifu au mwanzo wa kutenda kitendo” baadhi ya mifano: “msidhani ya kuwa……..”(Mt 5:17); “msisumbuke………”(Mt 6:31); “msiuonee haya………..”(2Tim 1:8)

C. KITENZI HASI CHENYE JOZI kikiwa na DHAMIRA TEGEMEZI ni chenye msisitizo hasi. “kamwe, katu” au “kwa hali yeyote ile”. Baadhi ya mifano: “kamwe, hataonja mauti………”(Yoh 8:51); “hakika, kamwe………..”(1Kor 8:13)

XI

A. Katika lugha ya Koine, KIBAINISHI CHA WAZI cha neno “wale, Yule,ile” kina matumizi mfanano na kwenye Kiingereza. Kazi yake kuu ilikuwa ni ya “muonyeshwaji”, ni njia ya kukamata hisia ya neno, jina au kirai. Utumiaji unatofautiana kati ya mwandishi na mwandishi kwenye Agano Jipya. KIBAINISHI CHA WAZI pia chaweza kutenda
   1. Kama chombo cha kutofautisha mfano cha kuonyesha
   2. Kama alama ya kurejea KIIMA kilichowekwa awali au mtu
   3. Kama njia ya kutambua kiima kwenye sentesi kikiwa na KITENZI kinchounganisha. Mfano: “Mungu ni Roho” Yoh 4:24, “Mungu ni nuru” 1Yoh 1:5; “Mungu ni upendo” 4:8,16

B. Lugha ya Koine haina KIBAINISHI KISICHO CHA WAZI kama ilivyo kwenye Kiingereza cha neno “a” herufi ya kwanza ya alfabeti au “an” mbadala wa “a” kwenye irabu zinazoanza na herufi kama “e”, “h”. Kutokuwepo na KIBAINISHI CHA WAZI chaweza kumaanisha;
   1. Mlengo juu ya tabia au thamani ya kitu
   2. Mlengo juu ya aina ya kitu

C. Waandishi wa Agano Jipya walitofautiana sana kwa jinsi KIBAINISHI kilivyotumiwa.

X NJIA ZA KUONYESHA MKAZO KWENYE AGANO JIPYA LA KIYUNANI

A. Mbinu za kuonyesha msisitizo zinatofautiana toka kwa mwandishi mmoja hadi mwingine kwenye Agano Jipya. Waandishi waendelezaji na warasimishaji walikuwa ni Luka na mwandishi wa Waebrania.

B. Mwanzo kabisa tumesema ya kuwa KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI kilikuwa ni kipimo na kisichoangaliwa kwenye msisitizo, lakini njeo nyingine, irabu au dhamira zina umuhimu wa ufasiri. Hii sio kumaanisha kuwa

KITENZI TENDAJI TIMILIFU ELEKEZI mara nyingi hakikutumika kwenye umakinishaji wa kisarufi. Mfano: Rum 6:10 (mara mbili)

C. Upangiliaji wa neno kwenye lugha ya Koine.
   1. Lugha ya Koine ilikuwa ni lugha ngumu isiyo tegemezi, kama vile Kiingereza, kwenye mpangilio wa maneno. Kwa hiyo mwandishi angaliweza kutofautiana kwenye mpangilio wa kawaida aliotegemea kuonyesha.
      a. Kile mwandishi alihitaji kusisitiza kwa viongozi
      b. Kile mwandishi angalikishangaza kwa viongozi
      c. Kile mwandishi alichosikia toka ndani
   2. Mpangilio wa kawaida wa neno kwenye Kiyunani bado ni jambo ambalo halijatulia ingawa mpangilio wa kawaida unaokusudiwa ni
      a. Kiunganishi cha VITENZI/Vitenzi unganishi
         (1) KITENZI
         (2) KIIMA
         (3) SIFA
      b. VITENZI elekezi
         (1) KITENZI
         (2) KIIMA
         (3) KISHAMILISHI
         (4) KISHAMILISHI KISICHO DHAHIRI
         (5) KIRAI HUSISHI
      c. Virai vya NOMINO
         (1) NOMINO
         (2) KIVUMISHI
         (3) KIRAI HUSISHI
   3. Mpanglio wa neno waweza kuwa muhimu mno kwenye upangiliaji wake. Mfano:
      a. “walinipa mimi na Barnaba mkono wa kuume wa shirika” (Gal 2:9) kirai “mkono wa kuume wa shirika” imegawanyika na kuwekwa mbele kuonyesha umuhimu wake.
      b. Pamoja na Kristo (Gal 2:20), iliwekwa kwanza kifo chake kilikuwa kiini.
      c. “ni sehemu nyingi na kwa njia nyingi” (Ebr 1:1), iliwekwa kwanza. Ilikuwa ni kwa namna Mungu alivyojidhihilisha mwenyewe kwa tofauti na sio ukweli wa mafunuo.

D. Kawaida kwa kiasi fulani cha degrii ya msisitizo ulionyeshwa na
   1. Urudiaji wa KIWAKILISHI ambacho tayari kilikuwepo katika KITENZI kilichonyambulika. Mfano: “mimi mwenyewe, hakika nitakuwa nawe…….”(Mt 28:20)
   2. Ukosekanaji wa KIUNGO tarajiwa, au kitu kingine cha kuunganisha maneno, virai, vishazi au sentesi. Hii inaitwa (isiofungamana). Kitu unganishi kilikuwa ni
      a. Ibada ya kubarikiwa kwa Kristo, Mt 5:3 ff(ikisisitizia orodha)
      b. Yohana 14:1 (maada mpya)
      c. Rumi 9:1 (kifungu kipya)
      d. 2Kor 12:20 ( inasisitizia orodha)
   3. Urudiaji wa maneno au virai vilivyomo katika mazingira tajwa. Mfano: “usifiwe utukufu wa neema yake” (Efe 1:6, 12 & 14). Kirai hiki kilitumika kuonyesha kazi ya kila mtu wa utatu.
   4. Utumiaji wa nahau au neno (sauti) unakaa kati ya istilahi.
      a. Tasifida- maneno mbadala kwa viima vyenye miiko kama “lala” kwa kifo (Yoh 11:11-14) au “nyayo” kwa viungo vya uzazi vya kiume (Ruth 3:7-8; 1Sam 24:3)

b. Maneno ya kuzunguka- mbadala wa maneno kwa jina la Mungu, kama “ufalme wa mbingu” (Mt 3:21) au “sauti toka mbinguni” (Mt 3:17)

c. Maumbo ya hotuba

(1) Kutowezekana kuyakuza (Mt 3:9; 5:29-30; 19:24)

(2) Upole wa maelezo (Mt 3:5; Mdo 2:36)

(3) Mfano halisi wa (1Kor 15:55)

(4) Kejeli (Gal 5:12)

(5) Dondoo za kishairi (Flp 2:6-11)

(6) Mvumo unaokaa kati ya maneno

(a) “kanisa”

i. “kanisa” (Efe 3:21)

ii. “Kuitwa” (Efe 4:1,4)

iii. “Kuitwa” (Efe 4:1,4)

(b) “huru “

i. “Mwanamke huru” (Gal 4:31)

ii. “uhuru” (Gal 5:1)

iii. “huru” (Gal 5:1)

d. Lugha ya kinahau- ni lugha ambayo mara nyingi ni ya kitamaduni na lugha bayana

(1) Hii ilikuwa ni matumizi ya kistiari ya neno “chakula” (Yoh 4:31-34)

(2) Hii ilikuwa ni matumizi ya kiistiari ya neno “hekalu” (Yoh 2:19; Mt 26:61)

(3) Hii ilikuwa ni nahau ya Kiebrania ya kuonyesha huruma, ya neno “chukia” (Mwa. 29:31; Kumb.21:15; Thess 14:36; Yoh 12:25; Rum 9:13)

(4) “wote” dhidi ya “wengi”. Linganisha Isa. 53:6 (“wote”) na 53:11 & 12 (“wengi”). Istilahi hizi zina maneno sawa kama Rum 5:18 na 19 kama inavyoonyesha.

5. Utumiaji wa kifungu cha isimu moja kwa moja badala ya neno moja. Mfano: “Bwana Yesu Kristo”.

6. Utumiaji maalumu wa neno *autos*

a. Wakati likiwa na KIFUNGU (nafasi ya kivumishi angama) kilichofasiliwa “sawa”

b. Wakati bila KIFUNGU (nafasi ya kuarifu) kilitafasiliwa kama KIWAKILISHI CHENYE MKAZO CHA KUJIREJEA- “mwenyewe jinsia ya ME” “mwenyewe jinsia ya KE” au “yenyewe/chenyewe”

E. Wanafunzi wa Biblia wasio weza soma Kiyunani waweza kutambua mkazo katika Nyanja tofauti:

1. Utumiaji wa misamiati ya kichambuzi na andiko nasaba la Kiyunani/ Kiingereza.

2. Mlinganyo wa fasili za Kiingereza, hasa toka kwa nadharia za fasiri zinazotofautiana. Mfano: ufasiri mlinganyo wa “neno kwa neno” (KJV, NKJV, ASV, NASB, RSV, NRSV) na “mfanano wa karibu” (William, NIV, NEB, REB, JB, NJB, TEV)

Msaada mzuri hapa ungalikuwa ni ule toka *The Bible in Twenty-Six Translation* kilichochapishwa na Baker.

3. Utumiaji wa *The Ephasized Bible* cha Joseph Bryant Rotherham (Kregel, 1994).

4. Utumiaji wa tafasiri yenyewe.

a. *The American Standard Version* ya mwaka 1901

b. Young’s Lateral Translation of the Bible cha Robert Young (Guardian Press, 1976)

Usomaji wa kisarufi unachosha lakini unafaa kwa ufasiri mzuri. Maelezo hasa sahihi, maoni na mifano inahamasisha na kuwaamusha watu wasiojua Kiyunani kutumia mihitasari ya kisarufi iliyotumiwa kwenye juzuu hii. Hakika maana hizi zimerahisishwa zaidi. Zisingaliweza kutumika katika hali madhubuti nay a kulazimisha, lakini kama ngazi ya kupandia kwenda kwenye uelewa mkubwa wa isimu za Agano Jipya. Kimatumaini maana hizi zitawawezesha wasomaji kuelewa maoni ya msaada mwingine wa usomaji kama vile maoni ya kiufundi juu ya Agano Jipya.

Ni lazima tuweze kuthibitisha ufasiri wetu uliolenga kwenye habari iliyopatikana kwenye maandishi ya Biblia. Sarufi ni moja ya msaada mkubwa wa vipengere hivi, vipengere vingine vingalijumuisha muundo wa kihistoria, maandishi ya kifasihi, utumiaji wa neno la wakati ule ule na dondoo zinazorandana.

# Uhakiki wa Tofauti za Kiuandishi

Somo hili litajikita kwa namna moja kutoa maelezo yanayopatikana katika maoni haya.
Mhutasari ufuatao utahusika

I. Vyanzo vya maelezo ya Biblia zetu za Kiingereza
   A. Agano la Kale
   B. Agano Jipya
II. Maelezo mafupi ya matatizo na nadharia ya "maoni dhaifu" pia yanaitwa "uhakiki wa maandiko"
III. Vyanzo vilivyopendekezwa kwa ajili ya usomaji wa badaye

I. Vyanzo vya maandiko ya Biblia yetu ya Kiingereza

A. Agano la Kale
   1. Machapisho ya kale ya Kiebrania ya karne ya kumi na tisa (MT)-maandiko ya konsonanti za Kiebrania yalipangwa na Rabbi Aquiba miaka 100 Baada ya Kristo. Nukta za irabu na lafudhinukuu za pembeni, vituo vya uandishi na alama za nukta zilizoongezwa katika karne ya sita Baada ya Kristo na vilihitimishwa katika karne ya tisa Baada ya Kristo. Yalifanywa na familia ya wasomi wa Kiyahudi wajulikanao kama Wana-maandiko ya Kale ya Kiebrania. Muundo wa maandiko walioutumia ulikuwa sawa na ule katika Mishnah, Talmud, Targums, Peshitta, na Vulgate.
   2. Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale la Kiebrania (LXX) –Utamaduni unasema Tafsiri ya Kiyunani ya Agano la Kale la Kiebrania ilitengenezwa na wasomi wa Kiyahudi 70 katika siku 70 katika maktaba ya Alexandria chini ya ufadhili wa Mfalme Ptolemy wa II (285-246 K.K). Tafsiri ilidhaniwa kuwa matakwa ya kiongozi wa Kiyahudi aliyeishi katika Alexandria. Utamaduni huu unatokana na "Herufi Aristeas." Mara kwa mara Tafsiri ya Agano Kale(LXX) ilijikita katika kutofautiana kwa utamaduni wa maandishi ya Kiebrania kutoka katika maandishi ya Rabbi Aquiba (MT).
   3. Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (MBC)-Michoro ya Bahari ya Chumvi -iliandikwa huko Ruma kipindi cha K.K(200 Kabla ya Kristo hadi Baada ya Kristo 70) na madhehebu ya Kiyahudi waliojitenga waitwao " Esene". Machapisho ya Kiebrania, yalikutwa katika sehemu nyingi kandokando ya Bahari ya Chumvi yakionyesha baadhi ya zile tofauti za machapisho ya familia za Kiebrania nyuma ya Machapisho ya Kale ya Kiebrania (MKK)na Tafsiri za Kale za Kiebrania (70).
   4. Baadhi ya mifano ya mahususi ni kwa namna gani ulinganifu wa maandishi haya imewasaidia wakalimani kulielewa Agano la Kale.
      a. Tafsiri za Kale za Kiebrania zimewasaidia watafsiri na wasomi kuyaelewa maandishi ya Kale ya Kiebrania.
         (1) Tafsiri za Kale za Kiebrania za Isa. 52:14, "Kama vile wengi watakavyo shangazwa <u>Naye</u>."
         (2) Maandishi ya Kale ya Kiebrania ya Isa. 52:14, "Bado kama vile wengi walivyo staajabishwa <u>Nawe</u>."
         (3) Katika Isa. 52:15 tofauti ya kiwakilishi cha Tafsiri za Kale za Kiebrania imehakikishwa
            (a) Tafsiri za Kale za Kiebrania, "hivyo mataifa mengi yatashangazwa naye"
            (b) Maandishi ya Kale ya Kiebrania, "hivyo yeye ameyatapakaza mataifa mengi"
      b. Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (DSS) yamewasaidia watafsiri na wasomi kuyaelewa Maandishi ya Kale ya Kiebrania
         (1) Mafunjo ya Bahari ya Chumvi ya Isa. 21:8, "ndipo akalia Karibu na mlinzi wa mnara nilipo simama."
         (2) Maandishi ya Kale ya Kiebrania (MT) ya Isa. 21:8, "ndipo akalia kama simba, Ee Bwana, mimi nasimama daima juu ya mnara wakati wa mchana……"
      c. Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na Mafunjo ya Bahari ya Chumvi (DSS) zote zilisaidia kuichuja Isa. 53:11
         (1) Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na Mafunjo ya Bahari Chumvi (DSS), "Baada ya kutaabika sana, mtumishi wangu atafurahi. Kwa kuwajibika kwake kikimilifu, atatosheka na matokeo hayo.''
         (2) Maandishi ya Kale ya Kale ya Kiebrania (MT), "Ataona …… ya taabu ya nafsi yake, na kuridhika. Kwa maarifa yake mtumishi wangu mwenye haki Atawafanya wengi kuwa wenye haki."

B. Agano Jipya

1. Maandishi yapatayo 5,300 yote au sehemu za Agano Jipya la Kiyunani yapo hadi leo. Yapatayo 85 yameandikwa katika karatasi za mafunjo na 268 ni maandishi yaliyoandikwa yote kwa herufi kubwa (maandiko adimu) Baadaye, mnamo karne ya tisa B.K., maandishi yaliyo somwa (madogo sana) yalikuzwa. Maandishi ya Kiyunani yaliandikwa kutoka namba zipatazo 2,700. Pia tunazo nakala zipatazo 2,100 za orodha ya Machapisho ya maandiko Matakatifu yalitumika katika kuabudu ambayo tunaiita misale ya waumini.
2. Machapisho ya Kiyunani yapatayo 85 yaliyokuwa na sehemu za Agano Jipya zilizoandikwa katika karatasi za mafunjo yamejengewa katika makumbusho. Baadhi yao yamewekwa katika kipindi maalumu kutoka karne ya pili B.K., yaliyo mengi ni kuanzia karne za tatu na nne A.D. Hakuna kati ya machapisho ya kale. Hizi zilizo na Agano Jipya Kamili. Hii ni kwa sababu hizi ni nakala za kale za Agano Jipya hazimaanishi kuwa sio ya kujiendesha yenyewe zina tofauti chache. Zilizo nyingizilinukuliwa kwa kasi kwa matumizi ya kawaida. Utunzaji haukuzingatiwa katika utendaji. Hivyo, zina utofauti mwingi.
3. Kitabu cha miswada ya kale chenye maandishi ya Kale ya Kiyunani ya karne ya nne B.K. kinachojulikana kwa herufi ya Kiebrania א (*aleph*) au (01), iliyokutwa katika nyumba ya Mt. Katarina juu ya Mlima Sinai na Tischendorf. Tarehe yake imeandikwa kuanzia karne ya nne B.K. iliyokuwa na zote Tafsiri za Kale za Kiebrania (LXX) na za Agano Jipya la Kiyunani. Ni aina ya"Maandishi ya Kialekzandria."
4. Kitabu cha miswada ya Kale cha Alekzandrianus, kijulikanacho kama "A" au (02), machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano ambayo ilipatikana katika Alekzandria, Misri.
5. Kitabu cha miswada ya Kale cha Machapisho ya Kiyunani cha karne ya nne, kijulikanacho kama "B" au (03), iliyopatika katika maktaba ya Vatikani katika Roma na imeandikiwa tarehe kuanzia katikati ya karne ya nne B.K. Ina zote Tafsiri za Kale za Kiebrania za Agano la Kale na Agano Jipya la Kiyunani. Yalikuwa aina ya "Maandishi ya Kialekzandria."
6. Kitabu cha miswada ya kale cha Ephraemi, kijulikanacho kama "C" au (02), machapisho ya Kiyunani ya karne ya tano ambayokwa makusudi yaliaribiwa.
7. Kitabu cha miswada ya Kale cha Bazae, kijulikanacho kama "D" au (05), machapisho ya Kiyunani ya karne ya karnre ya tano au sita. Ni mwakilishi mkuu wa kile kinachojulikana kama "Maandishi ya Magharibi." Ina maongezeko mengi ulikuwa ushahidi mkuu wa tafsiri ya Mfalme James.
8. Agano Jipya la machapisho ya kale yanaweza kuwekwa katika makundi matatu, kadria nne, familia ambazo zimeshiriki sifa fulani.
   a. Maandishi ya Kialekzandria kutoka Misri
      (1) $P^{75}$,$P^{76}$ ( yapata 200 B. K.), ambayo inachukua kumbukumbu ya Injili.
      (2) $P^{46}$ (yapata 225 B. K.), ambayo ilichukua kumbukumbu ya barua za Paulo
      (3) $P^{72}$(yapata 225-250 B. K.), ambayo ilichukua kumbukumbu ya Petro na Yuda
      (4) Kitabu cha miswada ya Kale B, kiitwacho Viticanus (mnamo 325 B. K), ambacho kimebeba Agano la Kale zima na Agano Jipya
      (5) Origen alinukuu kutoka aina hii ya maandiko
      (6) Machapisho ya kale mengine ambayo yanaonyesha aina hii ya maandishi ni א,C, L, W, 33
   b. Maandishi ya Magharibi kutoka Afrika ya Kaskazini
      (1) alinukuu kutoka wakuu wa kanisa wa Afrika ya Kaskazini, Tertullian, Cyprian, na tafsiri za Kale za Kilatini
      (2) yalinukuliwa kutoka Irenaeus
      (3) ilinukuliwa kutoka Kilatini na tafsri za kale za Kisiria
      (4) Andiko D la Machapisho ya kale "Bezae" ilifuata aina ya maandishi haya
   c. Byzantine Mashariki kutoka Constantinople
      (1) aina ya maandishi inaakisiwa katika 80% ya 5,300 MSS
      (2) ilinukuliwa na kanisa la mapadre wa Antiokia ya Silia, Cappadoceans, Chrisostom, natherodoret
      (3) Andiko A la machapisho ya kale, katika Injili tu
      (4) Andiko E la machapisho ya kale, (karne ya nane) ya Agano Jipya
   d. aina ya nne iwezekanayo ni ya "Kikaizari" kutoka Palestina
      (1) kwanza inaonekana katika Mrko tu

(2) baadhi ya shuhuda zake ni $P^{45}$ na W

II. Matatizo na nadharia ya "ukosoaji dhaifu."

A. Ni kwa namna gani tofauti zilitokea
  1. isio angalifu au bila kukusudia (matukio mengi mno)
     a. makosa madogo madogo ya macho katika kunakili kwa mkono ambapo ulisomwa mfano wa pili wa maneno yanayofanana na pale ambapo yanaondoa maneno yote katikati (mfanano wa maneno)
        (1) makosa madogo madogo ya macho katika kuondoa maneno ya herufi jozi au vifungu (urudiaji wa maneno)
        (2) makosa madogo madogo ya kumbukumbu katika kurudia kifungu au msitari wa maandishi ya Kiyunani (mshabaha ule ule)
     b. makosa madogo madogo ya masikio katika kunakili maneno ya imla ambapo makosa ya kiuandishi hutokea (itacism). Mara nyingi makosa ya kiuandishi hudokeza au kutaja herufizenye mfananowa sauti za maneno ya Kiyunani.
     c. maandishi ya Kiyunani ya kale hayakuwa na sura au mgawanyo wa mistari, chache au alama za uandishi na hakuna mgawanyo kati ya maneno. Inawezekana kuzigawa herufi katika nafasi kuunda maneno tofauti.
  2. makusudi
     a. mabadiliko yalifanywa ili kufanikisha muundo wa kisarufi wa maandishi yaliyo nakiliwa
     b. mabadiliko yalifanywa ili kuyaleta maandiko katika ulinganifu na maandiko mengine ya kibiblia (mlinganyosambamba)
     c. mabadiliko yalifanywa kwa kuuunganisha masomo mawili au zaidi yaliyokuwa tofauti katika muungano mmoja wa maandishi marefu (conflation)
     d. mabadiliko yalifanywa kusahihisha makosa yaliyotambuliwa katika maandishi ( cf. I Kor. 11-27 na I Yohana 5:7-8)
     e. baadhi ya taarifa za nyongeza kama mpangilio wa kihistoria au ufafanuzi sahihi wa maandishi uliwekwa pembezoni kwa nakala moja lakini zilihamishiwa katika maandishi kwa kuzinakili mara ya pili ( Yohana 5:4)

B. Mafundisho muhumu ya ukosoaji wa maandiko (mwongozo wa kimantiki ili kubainisha usomaji halisi wa maandishi wakati tofauti inapojitokeza)
  1. maandishi ambayo hayakuwa na ustadi zaidi au ambayo hayakuwa muhimu kisarufi yamkini ni halisi
  2. maandishi mafupi zaidi yamkini ni halisi
  3. maandishi ya kale yamepewa uzito zaidi kwa sababu ya ukaribu wake kihistoria katika uhalisia, kila kitu kuwa sawa zaidi
  4. Machapisho ya kale ni namna mbali mbali ya kijiografia mara nyingi yana usomaji halisi
  5. Kimafundisho maandishi ya wanyonge, hasa yale yanayohusiana na majadiliano makuu ya kitheolojia ya kipindi cha mabadiliko ya machapisho kama Utatu katika Yohana 5:7-8, yanapaswa kupendelewa.
  6. maandishi ambayo yanaweza kuelezea zaidiasili ya tofauti zingine
  7. nukuu mbili ambazozinzsaidia kuonyesha usawa katika tofauti zinazotaabisha
     *a.* kitabu cha J. Harold Greenless, *Inroduction to New Testament Textual Criticism*, "Hakuna mafundisho ya Kikristo yanayoning'inia juu ya maandishi yenye kujadiliwa; na mwanafunzi wa Agano wa Jipya anapaswa kuyatambua maandiko yake anayoyataka kuwa mwenye imani zaidi au kuwa mwenye nguvu kimafundisho kuliko msukumo asilia" (uk. 68).
     *b.* W. A. Criswell alimwambia Greg Garrison ya *The Birmingham News ambayo yeye* ( Criswell) haamini kila neno katika Biblia ni la kutia moyo "angalau si kila neno ambalo limekwisha kutolewa kwa alaiki ya kisasa kwa karne za watafsiri." Criswell alisema "Mimi ni mwamini sana katika ukosoaji wa maandishi. Kama vile, Nafikiri, nusu ya sura ya 16 ya Marko ni uasi: haitii moyo, imebuniwa…Unapolinganisha machapisho hayo kwa kurudi huko nyuma, hakukuwa na kitu kama hicho kama lilehitimisho la Kitabu cha Marko. Mtu fulani alikiongeza…" Mababa wa uzao wa SBC wasio wakosaji walidai kuwa "kutia maneno yasiokuwepo katika kitabu" pia ni dhahiri katika Yohana, uwajibikaji wa Yesu katika bwawa la Bethesda. Na alijadili tofauti mbili za uwajibikaji wa kujinyonga kwa Yuda (Mt. 27 na Matendo 1): "Ni maoni tofauti ya kujinyonga," Criswell alisema "Kama iko katika

Biblia, kuna maelezo yake. Na hatia mbili za kujinyonga kwa Yuda ziko katika Biblia."Criswell aliongeza, "Ukosoaji wa Maandishi nisayansi ya ajabu ndani yake yenyewe. Si ya muda mfupi kupita, si isiyo husiana.Ni yenye nguvu na kuu…"

III. Matatizo ya machapisho (ukosoaji wa maandishi)

A. Vyanzo vilivyopendekezwa kwa ajili ya kusoma zaidi

1. *Biblical Critcism, Historical, Literary and Textual*, na R. H. Harrison
2. *The Textual of the New Testmemt: Its Transmission, Corruption and Restoration*, na Bruce M. Metzger
3. *Introduction to New Testament Txtual Critism*, na J. H Greenlee

# KAULI YA KIMAFUNDISHO

Mimi siangalii hasa habari za imani au kanuni za imani. Napendelea kuthibitisha Biblia yenyewe. Ingawa, natambua kuwa habari ya imani itawaleta wale tusiojuana ili kupima mtizamo wa mafundisho yangu. Katika siku zetu za leo zenye makosa mengi ya kithiolojia na upotofu, natoa muhtsari mfupi wa thiolojia yangu kama ifuatavyo.

1. Biblia, yote katika Agano la Kale na Agano Jipya, ni neno la Mungu lililovuviwa, lenye uhakika, lenye uzima na lenye mamlaka. Ni ufunuo pekee wa Mungu ulioandikwa na watu chini ya uongozi wa nguvu za ajabu. Ni kiini pekee cha ukweli sahihi kuhusu Mungu na Kusudi Lake. Pia ni kiini pekee cha imani na utendaji wa kanisa lake.
2. Kuna Mungu mmoja tu wa uzima, muumbaji na mkombozi. Yeye ndiye muumbaji wa vitu vyote, vionekanavyo na visivyo onekana. Amejidhihilisha mwenyewe kama Mungu wa upendo na anayejali ingawa pia ni Mungu asiye na upendeleo. Amejidhihilisha mwenyewe katika nafsi tatu tofauti: Baba, Mwana na Roho; haswa wanatengana lakini wanafanya kazi moja.
3. Muda wote Mungu yuko hai kuangalia ulimwengu huu. Kuna mpango wa milelekwa uumbaji wake usiobadilika na mtazamo wa kipekee unaomfanya binadamu kutenda mapenzi huru. Hakuna kinachoweza kutokea pasipo ruhusa na maarifa ya Mungu, bado anaruhusu uchaguzi kwa wote malaika na wanadamu. Yesu ni chaguo la Baba na wote kimanufaa wamechaguliwa katika Yeye. Ufahamu wa mbele wa Mungu kuhusu matukio hayampunguzii binadamu kubainisha maandiko yaliyoandikwa kabla. Wote tunahusika kwa mawazo yetu na matendo.
4. Binadamu, japo aliumbwa kwa sura ya Mungu na mbali na dhambi, aliamua kumwasi Mungu. Ingawa alijaribiwa na kitu chenye nguvu ya ziada. Adamu na Hawa waliwajibika kwa utashi wao wenyewe kuamua. Uasi wao umeathiri utu wa uumbaji. Watu wote tunahitaji rehema na huruma ya Mungu yote kwa hali ya ushirika katika Adamu na uasi binafsi wa hiari.
5. Mungu anatoa aina ya msamaha na urejesho kwa binadamu aliyeanguka. Yesu Kristo, Mwana pekee wa Mungu Baba, akawa mwanadamu, akaishi maisha yasio na dhambi, na kwa kifo chake mbadala, akalipa malipo ya dhambi ya mwanadamu. Ndiyo njia pekee ya kurejesha ushirika wetu na Mungu. Hakuna njia nyingine ya wokovu isipokuwa kupitia imani ya kazi yake aliyoimaliza.
6. Kila mmoja wetu binafsi yampasa kupokea ahadi ya msamaha na urejesho katika Kristo. Hilo linatimizwa kwa njia ya imani ya hiari katika ahadi za Mungu kupitia Kristo Yesu na kugeuka kwa mapenzi huru kwa dhambi inayojulikana.
7. Sisi sote tumesamehewa jumla na urejesho umelenga juu ya kuamini katika Kristo na toba toka dhambini. Ingawa, ushahidi wa mahusiano mapya unaonekana katika mabadiliko na badiliko endelevu. Dhumuni la Mungu kwa wanadamu sio tu kwenda mbinguni siku moja, lakini kufanana na Kristo kwa sasa. Wale wote ambao wanakombolewa kweli ingawa wakati mwingine wanatenda dhambi, wataendelea katika imani na toba siku zao zote za maisha.
8. Roho Mtakatifu ni “Yesu mwingine”. Yuko duniani kuwaongoza wale wote waliopotea katika Kristo na kujenga ufanano wa Kristo katika kuokolewa. Karama za rohoni zinapewa toka kwenye wokovu. Ni maisha na huduma ya Yesu yaliyogawiwa katika mwili wake, yaani kanisa. Vipawa 358 ambavyo kimsingi ndio mwelekeo na msukumo wa hitaji la Yesu likihamasishwa na tunda la Roho. Roho yu hai katika siku zetu kama alivyokuwa katika enzi za Biblia.
9. Baba amemfanya Yesu Kristo aliyefufuka kama mwamuzi w vitu vyote. Atarudi duniani kuhukumu wanadamu wote. Wale wote walioamini Yesu na majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima cha mwanakondoo watapata mwili na utukufu ataporudi. Wataishi nae milele. Ingawa, wale wote walioikataa

kweli ya Mungu watatengwa milele toka katika furaha ya ushirika wa Mungu wa Utatu. Watahukumiwa pamoja na shetani na malaika zake.

Hii hakika haijaisha au kukamilika lakini natarajia itakupa ladha ya kithiolojia ya moyo wangu, nafurahia maelezo:

"Katika mambo ya msingi-umoja, mambo yaliyo ukingoni-uhuru, katika mambo yote-upendo."